

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Saba

An-Nuur mpaka Al-Ahzab

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Yaliyomo:

Tafsiri ya Surat An-Nuur	1
Umuhimu wa <i>Surat An-Nnuur</i>	2
Ufafanuzi wa <i>Hadd</i> Adhabu ya Zinaa.....	2
Isiwepo kwenu Huruma katika Kusimamisha Adhabu (<i>Haddi</i>).....	4
Simamisheni Adhabu Hadharani.....	5
Ubainifu wa Adhabu ya <i>Qadhf</i> (Kusingizia).....	8
Ubainifu wa Toba ya Msingizaji.....	8
Ubainifu wa Kiapo cha Kulaaniana (<i>Liaan</i>).....	11
Sababu ya Kuteremshwa Ayah za Kiapo cha Kulaaniana (<i>liaan</i>).....	13
Simulizi za Uongo na Uzushi.....	17
Kuwaadabisha Waumini kwa Kueneza Tuhuma.....	26
Fadhila ya Allah تعالى kwa Kuwapa Wazushi (<i>Ahlu-ifk</i>) Fursa ya Kutubu.....	28
Mafunzo ya Adabu kwa Mara Nyingine.....	31
Kuwatia Adabu wale wanaopenda Kuwatangazia Machafu Waumini.....	34
Kukumbushwa Fadhila za Allah تعالى na Kuonywa	35
Kuhimiza Kutoa na Kusamehe kwa Waliojaaliwa Fadhila ya Mali.....	37
Onyo kwa wenye Kuwasingizia Wanawake Wenye Staha	39
Ubora wa Aishah رضي الله عنها ni kwa Sababu ya Kuolewa.....	43
Kupiga hodi na adabu za kuingia majumbani.....	45
Amri ya kuinamisha macho.....	52
Hukumu za Hijabu.....	57
Adabu za wanawake kutembea barabarani.....	63
Amri ya kuoia.....	66
Amri ya kujizuilia (na machafu) ikiwa hana uwezo wa kuoia.....	68
Amri ya kuandikiana mkataba na watumwa ili wapate uhuru wao.....	69
Kukataza kuwalazimisha vijakazi kuzini.....	71
Mfano wa Nuru ya Allah تعالى	77
Ubora wa Misikiti na adabu zake	84
Mifano miwili ya aina mbili za makafiri.....	94
Kila kitu kinamtakasa Allah تعالى na Ufalme ni Wake.....	97
Tanabahisho juu ya Uweza wa Allah تعالى katika Kuumba	99
Uweza wa Allah تعالى katika Uumbaji wa wanyama.....	102
Hila za Wanafiki na hali ya Waumini.....	105
Ahadi ya Allah تعالى kwa Waumini kuwa Atawapa Ukhalifa.....	112
Agizo la Kusali, Kutoa Zakah na Kutii na Ubainifu.....	120
Nyakati za kutaka idhini kwa watumwa na watoto wadogo.....	122
Hapana tatizo kwa Ajuza ikiwa hatavaa Hijabu.....	124
Kula katika nyumba za ndugu zenu.....	128

Kutaka Idhini ya Wanapokuwa katika Mnasaba wa Jambo Moja.....	133
Ubainifu wa Kuzungumza na Mtume ﷺ.....	135
Kukatazwa Kukhalifu Amri ya Mtume ﷺ.....	136
Allah تعالی Anajua mliyo nayo.....	138
Tafsiri ya Suratul Furqaan.....	143
Utukufu wa Allah تعالی.....	144
Ubainifu katika Upumbavu wa Washirikina.....	147
Kauli za makafiri kuhusu Qur'ani.....	149
Kauli za Makafiri Kumhusu Mtume ﷺ na Majibu Yao.....	154
Je, Moto ndio Kheri au Pepo?.....	159
Miungu ya Washirikina itawakataa Siku ya Kiyama.....	161
Mitume Wote Waliotangulia Walikuwa Binadamu.....	165
Ubainifu wa Inadi na Ukaidi wa Makafiri.....	168
Makazi ya Watu wa Peponi.....	174
Vitisho vya Siku ya Kiyama na Kutamani Dhalimu Kufuata Njia.....	176
Mtume ﷺ Anashitakia Wanaompinga.....	176
Hekima ya Kuteremshwa Qur'ani kwa Awamu.....	183
Kuwahofisha Washirikina wa Kiquraysh.....	185
Makafiri Kumfanyia Mtume ﷺ Mzaha.....	190
Kuchukua Matamanio yao kuwa mungu.....	191
Dalili za Kuwepo kwa Mtengenezaji na Uweza Wake.....	192
Ujumbe wa Muhammad ﷺ ni kwa Watu Wote.....	198
Ujinga wa Washirikina.....	204
Mtume ni Mbashiri na Mwonyaji.....	205
Amri kwa Mtume Kumtegemea Allah تعالی na Kutaja Baadhi ya Sifa.....	206
Shutuma kwa Mushirikina.....	209
Ubainifu wa Utukufu na Uweza wa Allah تعالی.....	210
Ubainifu wa Sifa za Waja wa Mwingi wa Rehema.....	213
Miongoni mwa Sifa za Waja wa <i>Ar-Rahmaan</i>	219
Baadhi ya Sifa za Waja wa <i>Ar-Rahmaan</i> (Sifa za Ziada).....	224
Jazaa kwa Waja wa <i>Ar-Rahmaan</i> na Onyo kwa Watu wa Makkah.....	229
Tafsiri ya Suratu Shu'araa.....	233
Makafiri Kuichukia kwao Qur'an.....	234
Baina ya Musa عليه السلام na Firauni.....	240
Iliposimama Hoja, Firauni Alitumia Nguvu.....	249
Baina ya Musa عليه السلام na Wachawi.....	252
Baina ya Firauni na Wachawi.....	257
Kutoka kwa Wana wa Israeli Misri.....	259
Firauni Kuwaandama Wana wa Israeli na Kuangamia yeye na Watu Wake.....	262
Waadhi wa Kipenzi cha Allah تعالی, Ibraahim عليه السلام.....	266

Ibraahim عليه السلام Anataja Ukariimu wa Allah تعالى Kwake.....	269
Dua ya Nabii Ibraahim عليه السلام Kwake Yeye Mwenyewe.....	271
Wachamungu na Wapotovu Siku ya Kiyama.....	277
Waadhi wa Nuuh عليه السلام kwa Watu Wake na Majibu Yao.....	281
Matakwa ya Watu wa Nuhu عليه السلام na Majibu Yake.....	282
Vitisho vya Kaumu Yake, Dua ya Nuuh عليه السلام Dhidi Yao na Kuangamizwa.....	285
Ulinganiaji wa Huud عليه السلام kwa Kaumu Yake.....	287
Jawabu ya Kaumu ya Huud عليه السلام na Adhabu Yao.....	290
Nabii Swaleh عليه السلام na Kaumu ya Thamud.....	295
Kuwakumbusha Hali zao na Neema Walizopata.....	296
Jawabu la Thamudi Kutaka Kwao Ishara	299
Lutw عليه السلام na Da'wah Yake.....	301
Katazo la Lutw عليه السلام kwa Matendo ya Kaumu yake.....	303
Mawaidha ya Shu'ayb عليه السلام kwa Watu wa Aykah.....	305
Amri ya Kukamilisha Kipimo na Mizani.....	307
Jawabu ya Kaumu ya Shu'ayb عليه السلام katika Kumkanusha Yeye.....	310
Qur'ani Imeteremshwa na Allah تعالى.....	314
Qur'ani Imetajwa katika Vitabu vya Kale.....	316
Ukanushaji Mkali wa Maquraysh.....	317
Wanaokadhibisha Hawataamini Mpaka Waione Adhabu.....	319
Qur'ani Iliteremshwa na Jibril عليه السلام wala sio Shetani.....	324
Amri ya Kuwaonya Jamaa wa Karibu.....	327
Kukanusha Uwongo wa Washirikina.....	333
Kukanusha Dai kuwa Mtume ﷺ Alikuwa Mshairi.....	336
Tafsiri ya Surat An-Naml	343
Qur'ani ni Uwongofu na Bishara Njema kwa Waumini.....	344
Kisa cha Musa عليه السلام na Mwisho wa Firauni.....	348
Kutajwa Dawud عليه السلام na Sulaymaan عليه السلام na Nidhamu ya Jeshi Lake.....	355
Kutoonekana kwa Hud-hud.....	359
Hud-hud Kaja Mbele ya Sulayman عليه السلام Kumpasha Habari ya Sabai.....	362
Barua ya Sulaymaan عليه السلام kwa Bilqis.....	366
Balqis Ashauriana na Viongozi Wake Wakuu.....	368
Hadiya na Jawabu ya Sulaymaan عليه السلام.....	370
Kuletwa Kiti cha Bilqis kwa Haraka.....	373
Mtihani wa Bilqis.....	377
Jumba Kubwa la Vioo la Sulayman عليه السلام.....	389
Swaleh عليه السلام na Thamuud.....	383
Vitimbi vya Kikundi cha Mafisadi na Khatima ya Kaumu ya Thamuud.....	386
Lutw عليه السلام na Kaumu Yake.....	387
Amri ya Kumhimidi Allah تعالى na Kuwatakia Amani Mitume Yake.....	393

Dalili Kadhaa za <i>Tawhid</i> (Kumpwekesha Allah <small>تعالى</small>).....	394
Kisa cha Mujaahid Aliyepigana katika Njia ya Allah <small>تعالى</small>	399
Warithi wa Dunia.....	400
Mwenye Elimu ya Ghaibu ni Allah <small>تعالى</small>	405
Kuwa na Shaka na Kubainisha Hoja Hiyo.....	409
Qur'ani Inahadithia Tofauti baina ya Wana wa Israeli.....	414
Amri ya Kumtegemea Allah <small>تعالى</small> katika Kufikisha Ujumbe.....	415
Kutoka Mnyama katika Ardhi.....	416
Kukusanywa Madhalimu Siku ya Kiyama.....	421
Vitisho vya Siku ya Kiyama, Jazaa kwa Mema na Maovu.....	424
Amri ya Kumuabudu Allah <small>تعالى</small> tu na Kuwaita Watu.....	431
Tafsiri ya <i>Suratul Qasas</i>.....	435
Habari za Musa <small>عليه السلام</small> na Firauni, na Alichotaka Allah <small>تعالى</small>	437
Ufunuo kwa Mamake Musa <small>عليه السلام</small> Kuoneshwa mikakati.....	440
Musa <small>عليه السلام</small> katika Nyumba ya Firauni.....	441
Huzuni Kubwa Ilimpata Mama Yake Musa <small>عليه السلام</small>	445
Huzuni kubwa Ilimpata Mamake Kisha na Musa <small>عليه السلام</small>	446
Musa <small>عليه السلام</small> Kumuuu Mkibiti.....	449
Kufichuka Siri ya Musa <small>عليه السلام</small> kuua.....	453
Musa <small>عليه السلام</small> Akiwa Madyan na Kuwanyweshea wanyama.....	456
Musa <small>عليه السلام</small> Akakutana na Mzazi wa Wanawake Wawili.....	459
Musa <small>عليه السلام</small> Anarudi Misri na Kukirimiwa Utume na Miujiza Njjiani.....	464
Musa <small>عليه السلام</small> Anaomba Usaidizi wa Nduguye Haaruun.....	471
Musa <small>عليه السلام</small> Mbele ya Firauni na Kaumu yake.....	475
Matokeo ya Kiburi cha Firauni.....	477
Kubainisha Neema za Allah <small>تعالى</small> kwa Musa <small>عليه السلام</small>	481
Tanbihi ya Ushahidi wa Unabii wa Muhammad <small>ﷺ</small>	483
Ukaidi wa Makafiri na Kujibiwa Kwao.....	488
Wakaidi hawaamini Miujiza.....	489
Kuwazulia Uwongo Musa <small>عليه السلام</small> na Haaruun <small>عليه السلام</small>	489
Jawabu Dhidi ya Uzushi.....	491
Upotevu wa Wenye Kufuata Matamanio.....	492
Waumini Miongoni mwa Watu wa Kitabu.....	495
Allah <small>تعالى</small> Humuongoa Amtakaye.....	499
Kuangamizwa Miji Baada ya Kusimamishiwa Hoja.....	503
Dunia Haidumu na Wenye Kuishughulikia Hawawi Sawa.....	506
Kujitenga Washirikina na Washirika Wao Siku ya Akhera.....	510
Msimamo wao kwa Mtume Siku ya Kiyama.....	513
Allah <small>تعالى</small> Peke Yake Ndiye Muumbaji, Mwenye Elimu na Uchaguzi.....	514
Usiku na Mchana ni katika Neema za Allah <small>تعالى</small>	517

Kuwakemea Washirikina.....	519
Kisa cha Qaaruni na Kupatiwa Waadhi na Kaumu Yake.....	521
Qaaruni Alivyotoka na Mapambo yake,	525
Kudidimizwa Qaaruni na Nyumba Yake Ardhini.....	528
Watu Kuwaidhika kwa Kudidimizwa Kwake.....	529
Neema za Akhera ni za Waumini Wanyenyekevu.....	531
Amri ya Kufikisha Ujumbe wa Tawhiidi.....	533
Tafsiri ya <i>Suratul 'Ankabut</i>.....	539
Waumini Hujaribiwa Mpaka Ajulikane Mkweli na Mwongo.....	540
Waovu Hawataweza Kumtoroka Allah تعالی.....	542
Allah تعالی Atayatimiza Matarajio ya Waja Wema.....	543
Amri ya Kuwafanyia Ihsani Wazazi.....	545
Tabia za Wanafiki na Mwenendo wa Allah تعالی katika Kuwajaribu.....	548
Ujasiri wa Makafiri kwamba Watabeba Madhambi ya Wengine.....	551
Nuh عليه السلام na Kaumu Yake.....	555
Ibrahim عليه السلام Awahutubia Watu Wake.....	558
Ushahidi wa Kuwepo Maisha Mengine baada ya Kifo.....	562
Majibu ya Watu wa Ibrahim عليه السلام na Namna Allah تعالی Alivyoudhibiti.....	565
Waadhi wa Ibrahim عليه السلام kwa Watu Wake.....	566
Imani ya Lut عليه السلام na Kuhama Kwake Pamoja na Ibrahim عليه السلام.....	568
Allah تعالی Ampatia Ibrahim عليه السلام Watoto	569
Khotuba za Lut عليه السلام na Kilichotokea Baina Yake na Watu Wake.....	573
Lut عليه السلام Aomba Nusura kwa Mola Wake na Ujio wa Malaika.....	575
Kisa cha Shu'ayb عليه السلام na Kaumu Yake.....	577
Kutajwa Kuangamizwa Umma Uliowakataa Mitume Wao.....	580
Kumithilishwa kwa Miungu ya Washirikina na Nyumba ya Buibui.....	582
Amri ya Kufikisha Ujumbe, Kusoma Qur'an na Kuswali.....	584
Kujadiliana na Watu wa Kitabu.....	586
Ushahidi kwamba Qur'an Iliteremshwa kutoka kwa Allah تعالی.....	590
Washirikina Wanataka Ishara, na jawabu kwao.....	594
Washirikina Waomba Waharakishiwe Adhabu.....	598
Amri ya Kuhama na Ahadi ya Kuruzukiwa na Kulipwa Malipo Mema.....	602
Ushahidi wa <i>Tawhiid</i>	605
Ukafiri wa Makuraishi Pamoja na Neema Walizopewa.....	609
Tafsiri ya <i>Suratu Ar-Rum</i>.....	613
Kuubashiri Ushindi wa Warumi.....	614
Warumi ni Akina Nani.....	617
Namna Kaisari Alivyomshinda Kisra.....	618
Alama za Upekee wa Allah تعالی (<i>Tauhid</i>).....	624
Amri ya Swala Tano.....	629

Miongoni mwa Ishara za Allah تعالى	632
Kurudia Kuumba ni Rahisi Mno.....	640
Mfano Unaojulisha Upekee wa Allah تعالى (Tauhid)	643
Amri ya Kushikamana na Itikadi ya Upekee wa Allah تعالى (Tauhid)	645
Kugawanyika katika Madhehebu.....	649
Kuyumba kwa Mwanadamu baina ya Kumpwekesha Allah تعالى	651
Amri ya Kushikamana na Udugu na Kuharamishwa kwa Riba.....	655
Kuumba, Kuruzuku, Kufisha na Kuhuisha Vipo.....	656
Madhara ya Madhambi Humu Duniani.....	658
Amri ya Kuifuata Njia Iliyonyooka Kabla ya Siku ya Kiyama.....	661
Miongoni mwa Ishara za Allah تعالى ni Pepo Zinzovuma.....	662
Kuhuishwa kwa Ardhi ni Dalili ya Kufufuliwa.....	665
Makafiri ni Sawa na Maiti, Viziwi na Vipofu.....	669
Kutaja Hali Mbalimbali za Mwanaadamu.....	671
Ujahili wa Makafiri Duniani na Akhera.....	672
Kufundisha kwa kutumia Mifano Ndani ya Qur'an.....	674
Fadhila za Usomaji Sura Hii Wakati wa Sala ya Alfajiri.....	675
Tafsiri ya Suratu Luqman	677
Waovu Hujishughulisha na Mazungumzo ya Kipuuzi.....	679
Kutajwa Makazi Mema kwa Waumini	680
Ushahidi wa Upekee wa Allah تعالى (Tawhid)	684
Kutajwa kwa Luqman.....	686
Wasia wa Luqman kwa Mwanaye.....	688
Amri ya Kutembea kwa Wastani.....	696
Nasaha za Luqman.....	697
Kukumbushwa Neema.....	699
Washirikina Wanakiri Kwamba Allah تعالى Ndiye Muumbaji.....	702
Maneno ya Allah تعالى Hayawezi Kuhesabiwa au Kumalizwa.....	703
Kutajwa Uweza wa Allah تعالى na Ukubwa Wake.....	708
Amri ya Kumcha Allah تعالى na Kuikumbuka Siku ya Kufufuliwa.....	712
Allah تعالى Ndiye Ajuaye Ghaibu.....	714
Hadithi ya Ibn 'Umar رضي الله عنهما	715
Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه	716
Tafsiri ya Suratu As Sajda	721
Qur'an ni Kitabu cha Allah تعالى Ambacho Hakina Shaka Ndani Yake.....	722
Allah تعالى Ndiye Muumbaji na Mwenye Kuuendesha Ulimwengu.....	724
Uumbwaji wa Mwanaadamu Hatua kwa Hatua.....	726
Jibu kwa Wale Wanaokanusha Kufufuliwa.....	727
Hali ya Washirikina Siku ya Kufufuliwa.....	730
Hali ya Watu wa Imani na Malipo yao.....	733

Muumini na Fasiki Hawako Sawa.....	739
Kitabu cha Musa عليه السلام na Uongozi wa Wana wa Israel.....	742
Jifunzeni Kutokana na Yaliyopita.....	745
Kuhuishwa Ardhi kwa Maji ni Ushahidi wa Kufufuliwa.....	747
Makafiri Walivyoomba Kuharakishiwa Adhabu na Kujibiwa Kwao.....	748
Tafsiri ya Surat Al-Ahzaab.....	753
Amri ya Kutowatii Makafiri na Wanafiki, na Kufuata Wahyi.....	754
Kubatilishwa Ubini wa Mtoto wa Hiari.....	756
Mtoto wa Hiari Aitwe kwa Jina la Baba Yake Halisi.....	759
Utiifu kwa Mtume ﷺ na Wakeze ni Mama wa Waumini.....	765
Ahadi na Agano la Mitume.....	769
Kusambaratishwa Maadui katika vita vya Ahzab (Khandaq).....	772
Kujaribiwa kwa Waumini, na Msimamo wa Wanafiki Katika Tukio.....	778
Amri ya Kumfuata Mtume ﷺ.....	786
Msimamo wa Waumini kwa Al-Ahzaab (Makundi).....	786
Kusifiwa kwa Msimamo wa Waumini na Kukataliwa Jambo la Wanafiki.....	788
Allah تعالى Alirudisha Nyuma Makundi ya Makafiri.....	793
Kampeni Dhidi ya Banu Quraydhwah.....	796
Kuharishwa kwa Wake wa Mtume.....	801
Wake wa Mtume ﷺ si kama Wanawake Wengine.....	804
Amri ya Kuwa na Adabu kwa Mama wa Waumini Ili wawe kigezo.....	806
Wake wa Mtume ﷺ ni katika Familia yake (Ahlul - Bayt).....	809
Amri ya Kufuata Qur'an na Sunna.....	811
Maelezo Kuhusu Sababu za Kuteremshwa.....	815
Sababu za Kuteremshwa.....	822
Allah تعالى Anamlaumu Mtume Wake Katika Kisa cha Zayd رضي الله عنه.....	826
Kuwasifu Wanaofikisha Ujumbe wa Allah تعالى.....	831
Mtume ﷺ si Baba wa Yeyote.....	832
Yeye ni Mtume wa Mwisho.....	832
Fadhila za Kumkumbuka Sana Allah تعالى.....	839
Ufafanuzi wa Rehema ya Allah تعالى.....	842
Sifa za Mtume ﷺ.....	845
Kitoka Nyumba na Hukumu ya Eda ya Mwanamke Aliyeachwa.....	849
Wanawake Waliohalalishwa kwa Mtume ﷺ.....	852

Tafsiri ya Suratu An-Nuur

Sura ya 24

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Kurehemu

سُورَةُ النُّورِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سُورَةٌ أَنْزَلْنَاهَا وَفَرَضْنَاهَا وَأَنْزَلْنَا فِيهَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿١﴾

الزَّائِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيَشْهَدَ عِدَاهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢﴾

الزَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ وَحُرِّمَ ذَلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣﴾

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤﴾

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِن بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥﴾

سُورَةٌ أَنْزَلْنَاهَا وَفَرَضْنَاهَا وَأَنْزَلْنَا فِيهَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿١﴾

الزَّائِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيَشْهَدَ عِدَاهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢﴾

1. Hii ni sura Tuliyoitere msha na Tukailazimisha; Na Tukateremsha ndani yake Aya zilizo wazi ili wapate kukumbuka

2. Mzinifu mwanamke [ambae hajaolewa] na mzinifu mwanaume, [ambae hajaoa] mtandikeni kila mmoja wao [miongoni

mwao] mijeledi mia moja wala isikushikeni kwao huruma katika Dini ya Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini.

Umuhimu wa Suratu Nnuur.

سُورَةٌ أَنْزَلْنَاهَا

“Hii ni Sura Tuliyoiteremsha”.

Hapa Allah تعالى Anatanabahisha juu ya kuzingatia mno surah hii; Na hii haikanushi utukufu wa sura nyingine.

وَفَرَضْنَاهَا

“Na Tukailazimisha”.

Mujaahid na Qataadah wamesema, “Anakusudia; Tumbainisha Halali na Haramu, Maagizo na Makatazo na Hududi (Adhabu zilizowekwa)”¹. Bukhari amesema, “Wale wanaoisoma: *Faradhwanaahaa*, Tumeifaradhisha juu yenu, na juu ya wale wanaokuja baada yenu”²

وَأَنْزَلْنَا فِيهَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ

“Na Tumeteremsha ndani yake Aya zilizo wazi”.

Inamaanisha, zilizotafsiriwa kwa uwazi kabisa.

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“Ili mpate kukumbuka”.

Ufafanuzi wa Hadd (Adhabu ya) Zinaa

Baada ya hapo Allah تعالى Anasema:

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ

“Mzinifu mwanamke [ambae hajaolewa] na mzinifu mwanaume [ambae hajaoa] mtandikeni kila mmoja wao mijeledi mia moja.”

Aya hii tukufu ndani yake kuna hukumu ya sheria ya *Haddi* kwa mzinifu, na adhabu imeelezwa kwa kina. Mtu huyo anaweza kuwa ni *Bikra* naye ni ambaye hajaoa au hajaolewa kabisa, au *Muhswan* naye ni ambaye atakuwa

¹ Atw-Twabariy 19:89, Ad-Durr al - Manthur 6:124.

² Fath al-Baari 8:301.

ameoa au ameolewa, kumaanisha kuwa tayari amejamiiana akiwa ndani ya ndoa sahihi na ilhali yeye akiwa ni muungwana [huru], baleghe na mwenye akili timamu. Ama kwa ambaye [hajaolewa], adhabu iliyowekwa ni mijeledi mia moja kama ilivyoenezwa katika Aya. Zaidi ya hayo ni kuwa anahamishiwa ugenini kutoka kwenye mji wake kwa muda wa mwaka mmoja, kama ilivyothibiti katika Sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurayrah na Zayd ibn Khaalid al-Juhaniy رضي الله عنهم katika Hadithi ya Mabedui wawili waliokuja kwa Mtume ﷺ. Mmoja wao alisema: “Ewe Mtume wa Allah, mtoto wangu huyu alikuwa ni muajiriwa wa mtu huyu na amezini na mke wake. Nimemlipa fidia kwa niaba ya mtoto wangu kondoo mia moja na kijakazi, nimewauliza watu wenye elimu, wameniambia kuwa mtoto wangu apigwe mijeledi mia moja na atolewe mjini kwa muda wa mwaka mmoja, na mke wa huyu mtu apoplewe mpaka afe”. Mtume ﷺ akasema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَأُنْفِصِرَنَّ بَيْنَكُمَا بِكِتَابِ اللَّهِ تَعَالَى، الْوَالِدَةُ وَالْعَنَمُ رَدُّ عَلَيْكَ، وَعَلَى ابْنِكَ جَلْدٌ مِائَةٌ وَتَغْرِيْبٌ عَامٌ، وَاعْدُ يَا أُتَيْسُ! - لِرَجُلٍ مِنْ أَسْلَمَ - إِلَى امْرَأَةٍ هَذَا، فَإِنْ اعْتَرَفَتْ فَارْجُمَهَا»

“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Nitahukumu baina yenu kulingana na Kitabu cha Allah Aliyetukuka. Chukua kijakazi chako na kondoo wako, na mtoto wako anafaa kupigwa viboko mia moja na kupelekwa ugenini kwa mwaka mmoja. Na ewe Unays, alimwambia mtu mmoja kutoka katika kabila la Aslam, nenda kwa mke wa mtu huyu, ikiwa atakiri (kosa hilo), mpige mawe mpaka afe.”

Unays رضي الله عنه alikwenda kwake, naye alikiri kosa lake, hivyo alipigwa mawe mpaka akafa.¹ Katika hili kuna dalili ya kumhamisha mjini mzinifu pamoja na kumchapa fimbo mia kama hajaolewa au hajaoa. Lakini ikiwa ameo na amewahi kujamiiana katika ndoa sahihi naye ni mtu huru (muungwana), mtu mzima (aliye baleghe) na mwenye akili timamu, hakika huyo [anarujumiwa] anapigwa mawe mpaka afe.

Kama alivyopokea Imamu Maalik رحمه الله تعالى; kuwa ‘Umar Ibn Al-Khatwaab رضي الله عنه, alisimama na akamhimidi pamoja na kumsifu Allah تعالى, kisha akasema: “Enyi watu! Allah تعالى amemtuma Muhammad kwa haki na

¹ Fat - hal-Baari 5: 355 na Muslim 3:1324.

Akamteremshia Kitabu. Na ikawa katika alivyomteremshia ni Aya ya *Rajm* (kupiga mawe), ambayo tuliisoma na kuifahamu. Mtume ﷺ alitekeleza adhabu hiyo ya kuwapiga mawe (wazinifu) na baada yake tuliendelea kufanya hivyo, lakini nahofia kuwa siku zinapopita kwa watu asije kusema mwenye kusema kuwa hawakuiona Aya ya *Rajm* katika kitabu cha Allah, na watapotea kwa kuacha faradhi alioiteremsha Allah تعالى. *Rajm* katika kitabu cha Allah ni haki juu ya mzinifu mwenye kuonja ndoa- mume au mke ikiwa ushahidi wa wazi utatolewa, au ikiwa mimba itatokana na hicho (kitendo), au ikiwa watakiri kosa lao¹. Pia imeripotiwa katika sahihi mbili katika Hadithi ndefu ya Maalik, ambayo tumeinukuu kwa muhtasari ile sehemu tu ambayo inahusiana na mazungumzo yetu haya.²

Isiwepo kwenu Huruma katika Kusimamisha Adhabu (Haddi)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ

“Wala isikushikeni huruma kwa ajili yao katika Hukumu ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: “Msiwaonee huruma katika kutekeleza sheria ya Allah تعالى”. Hakika si jingine linalokatazwa ni huruma inayofanya hakimu kuacha kusimamisha adhabu (*haddi*) katika kutekeleza linalokatazwa sio ile huruma ya kimaumbile juu ya kutekeleza adhabu (*haddi*). Basi, halijuzu kwake hakimu jambo hilo. Mujaahid amesema,

وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ

“Wala isikushikeni huruma kwa ajili yao katika Hukumu ya Mwenyezi Mungu.”

Ikiwa kosa lenye kustahiki kusimamisha adhabu (*haddi*) limepelekwa mbele ya Hakimu; adhabu ni lazima itekelezwa na haiwezi kusitishwa. Na kama hivi imepokewa kutoka kwa Sa'id ibn Jubayr na 'Atwaa' ibn Rabaah.³ Na hakika imekuja katika Hadithi,

¹ Muwatwtwaa ' 2:823.

² *Fat-h al-Baari* 13:148 na *Muslim* 3: 1317

³ *Al-Baghawiy* 3:321.

«تَعَاَفُوا الْحُدُودَ يَمَّا يَتَّبِعُكُمْ، فَمَا بَلَغَنِي مِنْ حَدٍّ فَقَدْ وَجِبَ»

“Sameheaneni adhabu (haddi) baina yenu, lakini kesi ikiletwa kwangu, kutoa adhabu inakuwa ni wajibu (lazima).”¹

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Ikiwa nyinyi mnamwamini Allah na Siku ya Mwisho”.

Basi fanyeni hivyo na simamisheni adhabu kwa aliyezini na mcharazeni barabara bila ya kumjeruhi ili arudi nyuma kwalo yeye na anayefanya mfano wa hilo. Imepokewa katika *Musnad* kutoka kwa baadhi ya Maswahaba kuwa waliuliza: “Ewe Mtume wa Allah! Hakika mimi huchinja kondoo na huku namhurumia”. Akasema:

«وَلَكَ فِي ذَلِكَ أُجْرٌ»

“Na wewe una ujira katika kufanya hivyo.”²

Simamisheni Adhabu Hadharani

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلْيَشْهَدْ عَذَابَهُمَا طَائِفَةٌ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

“Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini.”

Hii ni katika kuwatesa wazindi, wanapopigwa hadharani (mbele ya watu). Hakika hilo linakuwa ni lenye kufikisha zaidi ujumbe katika kuwakemea na kuchukua uovu huo na ufanisi katika kuwarudisha (katika njia ya sawa). Na katika hilo kunapatikana kukemea, kukaripia, kulaumu na kusuta na pia kufedhehesha, ikiwa watu wamehudhuria. Amesema Al-Hasan Al-Basriy رحمه الله تعالى katika Kauli ya Allah تعالى:

وَلْيَشْهَدْ عَذَابَهُمَا طَائِفَةٌ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

“Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini”. “Hadharani”.

الرَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ ۖ وَحَرِّمَ ذَلِكَ

عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

¹ Abu Dawwud 4:540.

² Ahmad 5:34.

3. “Mwanamume mzinifu hamuoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharamishwa kwa Waumini.”

Hii ni habari kutoka kwa Allah Aliyetukuka kuwa mzinifu mwanaume hajamiiani isipokuwa na mzinifu mwanamke au *Mshirikina* mwanamke, yaani hakubaliani kwa malengo ya zinaa isipokuwa na mzinifu aliyeasi mwanamke au *Mshirikina* mwanamke ambaye haoni uharamu wowote wa hilo. Na hivyo hivyo,

وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ

“Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu.”Maana yake: aliyeasi kwa kufanya kitendo cha zinaa au

أَوْ مُشْرِكٌ

“Au Mshirikina” Ambaye haitakidi wala haamini kuwa zinaa ni haramu. Na Kauli yake Allah Aliyetukuka:

وَحُرْمَ ذَلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥﴾

“Na ndoa kama hizo zimeharamishwa kwa Waumini wa kweli.”

Maana yake: Kujamiiana na kuwaoa malaya au kuwaoza wanawake watiifu kwa wanaume waovu. Na Qataadah na Muqaatil ibn Hayyaan wamesema: “Allah تعالی Ameharamisha kwa Waumini kuoja malaya”¹. Na Aya hii ni kama Kauli ya Allah تعالی:

مُحْصَنَاتٍ غَيْرِ مُسْفِحَاتٍ وَلَا مُتَّخِذَاتِ أَحْدَانٍ

“Waoeni na hali ya kuwa ni wanawake wema wasiokuwa wenye kuzini na kila mtu wala si wenye kuzini na wanaume mahsusi (wa kinyumba).” (4:25).

Na Kauli Yake:

مُحْصِنِينَ غَيْرِ مُسْفِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَحْدَانٍ

“Mkafunga nao ndoa, bila kufanya uzinzi (kwa mwanamke huyu na huyu), wala kuwaweka kinyumba.” (5:5).

¹Ad - Dur Al - Manthuur 6:127.

Na amepokea Imam Ahmad kutoka kwa 'Abdullah ibn 'Amr رضي الله عنه kuwa mwanamume mmoja katika Waumini alitaka idhini kwa Mtume ﷺ ili aweze kumuoa mwanamke aliyekuwa akiitwa Umm Mahzuul ambaye alikuwa mzinifu na akaahidi ya kuwa matumizi atajigharamia mwenyewe. Akasema: "Nikamuomba ruhusa Mtume ﷺ au alimtajia jambo lake hili". Akasema: "Mtume ﷺ alimsomea Aya hii:

الرَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَلَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ وَحُرْمَ ذَلِكَ

عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٠﴾

"Mwanamume mzinifu hamuoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharamishwa kwa Waumini."¹

Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَنْكِحُ الرَّانِي الْمَجْلُودُ إِلَّا مِنْهُ»

"Haoi mwanamume mzinifu aliyepigwa mijeledi isipokuwa wa mfano wake." Na ndivyo alivyopokea Abu Daawuud katika Sunan yake².

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدَةً وَلَا

تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥١﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ

وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٢﴾

4. "Na wanaowasingizia wanawake mahashumu, kisha wasilete mashahidi wanne, basi watandikeni bakora thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena. Na hao ndio wapotovu.

5. Isipokuwa wale waliotubu baada ya hayo na wakategemea; kwani bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye Kurehemu."

¹ Ahmad 2:158 na an-Nasaa'iy katika *al-Kubraa* 6:415.

² Abu Daawuud 2: 543.

Ubainifu wa Adhabu ya Qadhf (Kusingizia)

Katika Ayah hii tukufu kunabainishwa hukumu ya kupigwa mijeledi anayemsingizia mwanamke muungwana, aliye baleghe, mwenye kujihifadhi na machafu. Kadhalika itatekelezwa ikiwa aliyesingiziwa ni mwanamume. Msingizaji akitoa ushahidi wa kweli wa aliyoyasema adhabu itamwondokea. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا
وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٠﴾

“Kisha hawaleti mashahidi wanne, wapigeni mijeledi thamanini na kamwe msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki”.

Hivyo imewajibika kwa msingizaji ikiwa hakisimamisha ushahidi wa kubaini ukweli wa aliyoyasema (ambao unaweza kumwondoshea adhabu) – anapata hukumu tatu: Mosi: Kupigwa mijeledi thamanini. Pili: Kuwa ushahidi wake hautakubaliwa daima. Tatu: Kuwa atakuwa fasiki sio muadilifu si mbele ya Allah تعالى tu bali hata mbele ya watu.

Ubainifu wa Toba ya Msingizaji

Kisha Akasema Allah تعالى:

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥١﴾

“Isipokuwa wale wenye kutubu baada ya hayo na kujirekebisha; bila shaka Allah ni Msamehevu na Mrehevu.” (24:5).

Hii ‘Istithnaa’ (yaani kukivua kitu kutoka katika vitu vingine) inarudi katika hukumu ya pili na ya tatu. Ama kutandikwa mijeledi tayari huwa imepita katika hukumu na imeisha awe ametubia au ameazimia kuendelea wala hapana hukumu kwake baada ya hilo bila tofauti yoyote ya wanazuoni. Pindi akitubia, ushahidi wake utakubaliwa na itaondoka kwake hukumu ya ufasiki. Ameerza hayo Sa’iid ibn al-Musayyab رحمه الله تعالى, Mkubwa wa Taabi’iin na pia pote kubwa la salaf (watangulizi) wema¹. Na amesema Ash-Sha’biy na Adh-Dhahhaak:

¹ Atw-Twabariy 19:105.

“Ushahidi wake haukubaliwi hata akitubu isipokuwa tu anapokiri juu ya nafsi yake kuwa yeye kwa hakika amesema uzushi (uwongo). Wakati huo ndio ushahidi wake utakubaliwa”¹. Na Allah تعالیٰ Anajua zaidi.



¹ Atw-Twabariy 19:103, 108.

وَالَّذِينَ يَزْمُونَ أَرْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ شُهَدَاءُ إِلَّا أَنْفُسُهُمْ فَشَهَدُوا أَحَدِهِمْ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٦﴾ وَالْخَمِيسَةَ أَنْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كَانَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٧﴾ وَيَذَرُوا عَنْهَا الْعَذَابَ أَنْ تَشْهَدَ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٨﴾ وَالْخَمِيسَةَ أَنْ غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهَا إِنْ كَانَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٩﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِنكُمْ لَا نَحْسَبُهُمْ شُرَكَاءَ لَكُمْ بَلْ هُمْ خَيْرٌ لَكُمْ لِكُلِّ أَمْرٍ مِّنْهُمْ مَا أَكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١١﴾ لَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بِأَنْفُسِهِمْ خَيْرًا وَقَالُوا هَذَا إِفْكٌ مُّبِينٌ ﴿١٢﴾ لَوْلَا جَاءُوا عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا بِالشُّهَدَاءِ فَأُولَئِكَ عِنْدَ اللَّهِ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿١٣﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِي مَا أَفَضْتُمْ فِيهِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٤﴾ إِذْ تَلَقَّوْنَهُ بِأَلْسِنَتِكُمْ وَتَقُولُونَ بِأَفْوَاهِكُمْ مَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّئًا وَهُوَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾

وَالَّذِينَ يَزْمُونَ أَرْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ شُهَدَاءُ إِلَّا أَنْفُسُهُمْ فَشَهَدُوا أَحَدِهِمْ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٦﴾ وَالْخَمِيسَةَ أَنْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كَانَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٧﴾ وَيَذَرُوا عَنْهَا الْعَذَابَ أَنْ تَشْهَدَ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٨﴾ وَالْخَمِيسَةَ أَنْ غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهَا إِنْ كَانَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٩﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾

6. "Na wale wanaowasingizia wake zao (kuwa wamezini) na hawakuwa nao mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa ni kuapia mara nne kwa Jina la Allah: ya kwamba hakika yeye ni mkweli (katika madai yake).

7. "Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Allah iwe juu yake ikiwa yeye ni miongoni mwa waongo.

8. ***“Na (mke) itamwondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Allah kuwa huyu (mume) ni miongoni mwa waongo,***

9. ***“Na mara ya tano (aape) kwamba Ghabu ya Allah iwe juu yake, kama (mumewe) yu miongoni mwa wakweli (katika madai yake).***

10. ***“Na kama Allah Asingewaonesheni Fadhila na Rehema Zake. na hakika Allah ni Msamehevu Mwingi wa Hekima.”***

Ubainifu wa Kiapo cha Kulaaniana (Liaan)

Aya hizi tukufu zina faraja kwa waume na utatuzi wa ziada pindi mume anapomtuhumu mkewe na ikawa kwake vigumu kusimamisha ushahidi basi atalaaniana naye kama alivyoamrisha Allah تعالى. Nako ni kumpeleka mbele ya Imamu na kueleza tuhuma zake dhidi ya mkewe.

Imamu atamwapisha kiapo mara nne kwa Jina la Allah تعالى mbele ya mashahidi wanne kuwa yeye ni miongoni mwa wa kweli katika kumtuhumu mkewe kwa zinaa.

إِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٦٠﴾

“Ya kwamba yeye ni mkweli (katika madai yake)”.

Kisha atakula kiapo cha tano, kwa kusema,

وَالْخَمِيسَةَ أَنْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كَانَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٦١﴾

“Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Allah iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo”.

Pindi akisema hilo, mwanamke ataachika kwa mujibu wa hii - Li'aan na ataharamishwa kwake milele na atampa mahari yake na adhabu ya zinaa itamwelekea yeye mwanamke.

Na adhabu ya zinaa haitamwondokea mpaka naye aape mara nne kwa Jina la Allah تعالى kuwa mumewe ni miongoni mwa waongo, yaani kwa yale anayomtuhumu nayo:

وَالْخَمِيْسَةُ اَنْ لَعْنَتَ اللّٰهِ عَلَيْهِ اِنْ كَانَ مِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿١٥﴾

“Na mara ya tano (aape) kwamba Ghadhabu ya Allah iwe juu yake, kama (mumewe) yu miongoni mwa wakweli (katika madai yake).”

Na kwa hili Amesema Allah تعالى:

وَيَذْرُوْا عَنْهَا الْعَذٰبَ

“Na (mke) itamwondokea adhabu.”

Maana yake: *Hadd* (adhabu hiyo maalumu),

اَنْ تَشْهَدَ اَرْبَعَ شَهَدَاتٍ بِاللّٰهِ اِنَّهُ لَمِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿١٦﴾ وَالْخَمِيْسَةَ اَنْ غَضَبَ اللّٰهُ عَلَيْهَا
اِنْ كَانَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿١٧﴾

“Kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Allah kuwa huyu (mume) ni miongoni mwa waongo. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Allah iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa wa kweli.”

Akamhusisha mwanamke na ghadhabu, kama ambavyo mara nyingi mume hawezi kufichua fedheha ya mke wake na kumshutumu kwa uzinzi isipokuwa ni kweli na ana sababu ya kufanya hivyo. Na mke anajua ukweli wa mumewe kwa anayomshutumu nayo. Na hivyo kiapo cha tano kikawa katika haki yake kuwa ghadhabu ya Allah juu yake, na kawaida anayeghadhibikiwa ni yule anayejua haki kisha anapotoka na kukengeuka. Kisha ametaja Aliyetukuka Huruma Yake kwa waja Wake na Ulaini na Upole Wake kwao katika sheria Yake kwao kwa kupatikana faraja na utatuzi wa shida na dhiki waliyonayo. Hivyo Akasema Aliyetukuka:

وَلَوْلَا فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ

“Na kama Allah Asingewaonesheni Fadhila na Rehema Zake.”

Maana yake: Mungekuwa na dhiki na mambo yenu mengi yangukuwa magumu. Lakini jueni kuwa,

وَأَنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ حَكِيمٌ ﴿١٥﴾

“Na hakika Allah ni Msamehevu mno.”

حَكِيمٌ ﴿١٥﴾

“Mwingi wa Hikima.”

Katika sheria Anazotuwekea na Anayotuamrisha na Anayotukataza. Hakika zimekuja Hadithi nyingi kwa muktadha wa kutumia Ayah hii na kutaja sababu ya kuteremshwa kwake, na juu ya nani imeshuka miongoni mwa sahaba.

Sababu ya Kuteremshwa Ayah za Kiapo cha Kulaniana (Liaan)

Imamu Ahmad amepokea toka kwa Ibnu 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Pindi ilipoteremka Aya,

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا

‘Na wale wanaowasingizia wanawake watahirifu kwa masingizio ya uongo (kuwa wamezini) kisha hawaleti mashahidi wane, wapigeni mijeledi thamanini na kamwe msiwakubalie ushahidi wao tena’ (24: 4).

Sa’d ibn ‘Ubadah رضي الله عنه aliuliza, ‘Je hivi ndivyo ilivyoteremshwa, ewe Mtume wa Allah?’ Mtume ﷺ alisema:

«يَا مَعْشَرَ الْأَنْصَارِ أَلَا تَسْمَعُونَ مَا يَقُولُ سَيِّدُكُمْ؟»

“Enyi kongamano la Answaar, je hamsikii anavyosema kiongozi wenu?”

Wakasema, ‘Ewe Mtume wa Allah, usimlaumu, kwani yeye ni mtu mwenye wivu sana. Naapa kwa Allah! Hajaoa mwanamke asiye bikra, na hajamtaliki mwanamke katu, Kisha akawa jasiri mmoja wetu kumuoia kwa sababu ana wivu mno’. Sa’d رضي الله عنه akasema, ‘Wallaahi, ewe Mtume wa Allah! Najua

kwamba Aya hii ni kweli na inatoka kwa Allah تعالى, lakini mimi nimestaajabu. Nitakapomuona mtu muovu amelala na mke wangu, hainifalii mimi kumkaripia au kumsukasuka mpaka nitakapoleta mashahidi wane? Naapa kwa Allah تعالى siwezi kuwaleta wakati huo atakuwa amemaliza haja yake kabla ya mimi kuja nao'. Hawakukaa isipokuwa kwa muda mchache akaja Hilaal ibn Umayyah عنه رضي الله عنه mmoja kati ya wale watatu ambao toba yao ilikubaliwa.¹ Alikuwa usiku kutoka kondeni kwake na kumkuta mkewe akiwa na mwanaume. Aliona kwa macho yake na kusikia kwa masikio yake, lakini hakumgombeza hadi kulipokucha asubuhi. Asubuhi ilipofika alikwenda kwa Mtume عليه السلام na kumwambia, "Ewe Mtume wa Allah! Nilifika kwa mke wangu jana usiku na kumkuta mwanaume akiwa pamoja naye, na niliona kwa macho yangu na kusikia kwa masikio yangu". Mtume عليه السلام alichukizwa na aliyokuja nayo na alichukia sana. Answaar walimzunguka na kusema, "Hakika tumejaribiwa kwa aliyoyasema Sa'd ibn 'Ubadah عنه رضي الله عنه sasa hivi Mtume wa Allah atampiga Hilaal ibn Umayyah عنه رضي الله عنه na kubatilisha ushahidi wake mbele ya watu kuwa haukubaliki." Hilaal عنه رضي الله عنه alisema, "Naapa kwa Allah تعالى! Hakika mimi natarajia Allah تعالى Atanijaalia hukumu itakayonitoe katika tatizo hili." Hilaal akasema tena, "Ewe Mtume wa Allah! Naona umefadhaika sana kwa yale niliyoyasema lakini Allah تعالى Anajua kuwa mimi hakika ni mkweli." Naapa kwa Allah تعالى, Mtume عليه السلام alikuwa anataka kumuadhibu, Tahamaki Allah تعالى Aliteremsha wahyi kwa Mtume Wake عليه السلام. Alipoteremshiwa wahyi, walijua hilo kwa kusawijika uso wake, hivyo walimuacha peke yake mpaka wahyi ulipomalizika.

Allah تعالى Aliteremsha Aya ifuatayo:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ أَزْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ شُهَدَاءُ إِلَّا أَنْفُسُهُمْ فَشَهَدَتْ أَعْيُنُهُمْ
شَهَادَاتٍ بِاللَّهِ

"Na wale wanaowasingizia wake zao kuwa wamezini na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa ni kuapia mara nne kwa Jina la Allah." (24:6).

Baadae wahyi ulipomalizika, Mtume عليه السلام alisema,

¹ Tizama maelekezo ya Suratut Tawbah (9:118).

«أَبَشِرْ يَا هِلَالٌ فَقَدْ جَعَلَ اللهُ لَكَ فَرْجًا وَمَخْرَجًا»

"Furahia ewe Hilaal, kwani hakika Allah Amekuletea faraja na matokeo katika tatizo hilo".

Hilaal رضي الله عنه akasema, "Hakika natarajia hili kutoka kwa Mola wangu Mlezi عزوجل. Mtume ﷺ alisema,

«أَرْسَلُوا إِلَيْهَا»

"Kamwiteni mkewe".

Hivyo aliitwa naye akaja. Mtume ﷺ aliwasomea Ayah hii wote wawili, na kuwakumbusha kuwa adhabu ya Akhera ni kali na kubwa kuliko adhabu ya dunia hii. Hilaal رضي الله عنه alisema, "Naapa kwa Allah, ewe Mtume wa Allah! Mimi nimesema kweli kumhusu yeye." Mkewe akasema: "Amedanganya". Mtume ﷺ akasema,

«لَا عُنَا بَيْنَهُمَا»

"Waapizeni baina yao".

Hivyo Hilaal رضي الله عنه aliambiwa aape, Hilaal رضي الله عنه akaapa mara nne kwa Jina la Allah تعالى kuwa yeye ni mkweli. Alipokuwa katika mara ya tano, aliambiwa:

"Ewe Hilaal, mche Mwenyezi Mungu; adhabu ya dunia ni sahali zaidi kuliko adhabu ya Akhera. Hiki kiapo cha tano kimewajibisha adhabu ya Akhera juu yako."

Lakini Hilaal رضي الله عنه akasema: "Naapa kwa Allah, hakika Allah Hataniadhibu juu yake (mwanamke) akhera kama ambavyo hakunitandika mijeledi juu yake (mwanamke). Baada ya hayo akaapia kiapo cha tano kuwa laana ya Allah iwe juu yake ikiwa ni katika waongo. Kisha mwanamke akaambiwa, "Aape mara nne kwa Jina la Allah تعالى kuwa yeye (mwanaume) ni miongoni mwa waongo". Mkewe akaapa mara nne. Akaambiwa kabla ya kiapo chake cha tano, alishauriwa, "Mche Allah, adhabu ya dunia ni sahali zaidi kuliko ya Akhera. Hiki kiapo cha tano kimewajibisha adhabu ya akhera lazima iwe juu yako. Aliposikia hayo alisita kidogo, akatamani kukiri makosa yake, kisha akasema: "Naapa kwa Allah, sitaki kufedhehesha watu wangu", naye akaapa kiapo cha

tano pia kuwa ghadhabu ya Allah iwe juu yake ikiwa mumewe anasema ukweli. Hapo Mtume ﷺ aliwatenganisha baina yao, na kuwa mtoto atakayemzaa asimwite nasaba ya baba wa yeyote yule na asisingiziwe mtoto wala mama na yeyote. Atakayemshutumu mama yule au mtoto wake baada ya kula kiapo cha *Li'aan*, atapewa adhabu ya *Qadhf* na kwamba mke yule hana haki ya makazi wala chakula kwa sababu ya kutengana bila talaka na wala kufiwa na mume. Kisha Mtume ﷺ alisema:

«إِنْ جَاءَتْ بِهِ أَصْنِيبَ [أَرْبَيْحَ] حَمْسَ السَّاقِينِ، فَهُوَ لِهَلَالٍ، وَإِنْ جَاءَتْ بِهِ أَوْزَقِ
جَعْدًا جُمَالًا خَدَلَجَ السَّاقِينَ سَابِعَ الْأَيْتِينَ، فَهُوَ لِلذِّي رُمِيَتْ بِهِ»

"Ikiwa atazaa mtoto mwenye nywele nyekundu (na mapaja kondofu) na miguu membamba, huyo atakuwa mtoto wa Hilaal, lakini akizaa mtoto mwenye nywele za mapindi na miguu mipana na matako manene, huyo ni wa yule aliyetuhumiwa naye."

Baadae alizaa mtoto ambaye nywele zake zilikuwa za mapindi pamoja na miguu mipana na matako manene, hapo Mtume ﷺ alisema,

«لَوْلَا الْإِنْسَانُ لَكَانَ لِي وَلَهَا شَأْنٌ»

"Kama isingekuwa vile viapo kati yangu ingekuwa mimi na yeye (mwanamke) tuna jambo kubwa (akimaanisha angemwadhibu adhabu kali)."

Ikrimah amesema, "Mtoto baadae alikua mkubwa na kuwa liwali wa Misri, na alikuwa akiitwa kwa jina la mama na hakunasibishwa na baba yeyote"¹. Abu Daawud amepokea Hadithi kama hii kwa ufupi. Na Hadithi hii ina ushahidi wa Hadithi nyengine nyingi katika Vitabu Sahihi na nyenginezo kwa njia nyingi.

Allah تعالیٰ Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنكُمْ لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُم بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ لِكُلِّ آخِرٍ مِّنْهُمْ مَا أَكْتَسَبَ مِنَ الْإِنْتِمَارِ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٠٠﴾

"Hakika wale walioleta masingizio hayo, ni kundi miongoni mwenu. Msifikiri ni shari kwenu, bali hiyo ni kheri kwenu. Yeyote

¹ Abu Daawud 2:688.

aliyeshiriki, ameshapata nasibu yake ya dhambi kama anavyostahiki, na yule aliyebeba jukumu kubwa zaidi (katika masingizio) atapata adhabu kali zaidi.”

Simulizi za Uongo na Uzushi

Aya hizi kumi Ziliteremka katika shani ya Mama wa Waumini, Aishah رضي الله عنها pale watu wa Ifk (uzushi na uongo) walipomsingizia miongoni mwa wanafiki, kwa waliyosema katika ni halisi na uzushi ambao Allah تعالى Alimlinda (‘Aishah رضي الله عنها) na Mtume Wake ﷺ. Allah تعالى Aliteremsha Aya kumtakasa na uzushi huo na kuhifadhi heshima ya Mtume ﷺ. Akasema Aliyetukuka:

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنكُمْ

“Hakika wale walioleta masingizio hayo, ni kundi miongoni mwenu.”

Maana yake: Kundi miongoni mwenu ikimaanisha si mmoja wala wawili bali kundi. Na yule aliyekuwa kiongozi katika hili ni ‘Abdallah ibn Ubayy ibn Saluul, kiongozi wa wanafiki. Hakika yeye alikuwa akiwakusanya watu na kuwashawishi mpaka yakaingia hayo katika akili za baadhi ya Waislamu, nao wakaanza kuyazungumza. Na wakayajuzisha hayo wengine miongoni mwao na jambo hili likabaki hivyo kwa takriban mwezi mmoja mpaka ikateremka Qur’an na mtiririko wake unapatikana katika Hadithi Sahihi.

Ampokea Imamu Ahmad kutoka kwa Az-Zuhriy ambaye amesema: Amenieleza mimi Said ibn Al-Musayyab na ‘Urwah ibn Az-Zubayr na Alqamah Ibn Waqqaasw na Ubaydullah Ibn Abdullah Ibn Utbah Ibn Mas’uud kutoka kwa Aishah رضي الله عنها mke wa Mtume pale waliposema watu wazushi (Ifk) waliyosema. Allah تعالى Akamtakasa mama Aishah رضي الله عنها na kila mmoja alikuwa amenihadithia sehemu ya Hadithi yake na baadhi yao walikuwa na ufahamu mzuri zaidi wa Hadithi yake kuliko wengine na wenye kuthubutu zaidi kuielezea. Hakika nimezingatia kutoka kwa kila mmoja miongoni mwao Hadithi aliyonihadithia kutoka kwa Aishah رضي الله عنها. Na baadhi ya hadithi zao zinasadikisha nyingine, wametaja kuwa Aishah رضي الله عنها mke wa Mtume ﷺ amesema: “Alikuwa Mtume kila alipotaka kwenda safari alipiga kura kati ya wake zake. Yeyote ambaye mshale wake ndio umetokea, anatoka pamoja naye Mtume ﷺ”. Akasema Aishah رضي الله عنها, “Basi akapiga kura baina yetu wakati

wa vita fulani alivyopigana na ukatoka ndani yake mshale wangu na hivyo nikatoka pamoja na Mtume wa Allah na wakati huo ilikuwa ni baada ya kuteremshwa Aya za hijabu. Nami nikawa ninabebwa katika *Hawdaj* yangu (kibanda kilichofungwa juu ya mnyama) na niliteremshwa ndani yake. Tuliendelea na safari mpaka Mtume wa Allah alipokwishamaliza vita vyake hivyo, na kurejea, na tukakaribia Madinah. Ilikuwa ni usiku walipokuwa wameanza kujitayarisha na safari. Nami nikatoka nje ya kambi ili nikajisaidie. Niliporudi na kufika karibu na pahala pangu nilishika kifua changu, niligundua kuwa kidani changu kimepotea. Nikarudi nyuma kukitafuta, walikuja wale wanaonibeba wakanyanyua *Hawdaj* na kuiweka juu ya ngamia niliyekuwa nikimpanda, wao walidhaniana nimo ndani". Akasema: "Na walikuwa wanawake wakati huo hafifu (wepesi) na walikuwa hawana nyama, (kwani kulikuwa na uhaba wa chakula siku hizo).

Hivyo watu hawakutambua uhafifu (wepesi) wa *Hawdaj* pale walipoinyanyua na kuibeba, nami nilikuwa msichana mdogo wa umri. Walimswaga ngamia na wakaenda, nami nikakipata kidani changu baada ya jeshi kwenda mbele na msafara. Nikaja katika nyumba zao na hapakuwa na mwenye kuita wala mwenye kujibu, nikakusudia ile nyumba niliyokuwa ndani yake. Nikadhania kuwa wangenikosa na kunirudia na wakati nimeketi pahali hapo macho yangu yalishindwa na usingizi nami nikalala. Na alikuwa Swafwaan Ibnu Al-Mu'atwtwal As Sulamiy kisha Adh-Dhakwaani¹ amebaki nyuma ya jeshi, alipita karibu yangu na akaona weusi wa mwanadamu aliyelala, akaja, naye akanitambua pindi aliponiona, kwani alishaniona mara kadhaa kabla ya kuteremshwa amri ya hijabu. Nami niliamka kutokana na sauti yake pale aliponitambua nami nikaufunika uso wangu kwa *baibui. Wallahi!* Hakuzungumza nami hata neno moja wala sikusikia kutoka kwake neno lolote isipokuwa lile neno *istirjaa*: 'Huzuni ilioje' mpaka alipomkalisha ngamia wake na akauweka mkono wake chini nami nikapanda akaondoka. Akimwongoza ngamia wangu hadi tukalikuta jeshi letu wakati wa Adhuhuri, (ulipokuwa umetua na) akaangamia mwenye kuangamia kwa jambo langu hilo. Na yule aliyeueneza uzushi huu alikuwa ni 'Abdullah ibn Ubayy ibn Saluul. Tulipofika Madina nikashitakia ugonjwa (ambao

¹ Sa'd ibn 'Ubaadah alikuwa Muisilamu mwema na mwaminifu na mfuasi bora wa Mtume ﷺ pia alikuwa mmoja kati ya watu maarufu, na alifanya mengi katika kueneza Uislamu Madinah. Lakini juu ya yote hayo alikuwa ameelekea sana upande wa uhusiano wa ukoo wake. Ndio maana alimtetea 'Abdullah ibn 'Ubayy - *Tafhiimul - Qur'an*.

ulinifanya nilale kitandani) mwezi mzima na watu walikuwa wanaeneza kauli za watu wazushi (*Ifk*) na wala sikujua chochote katika hilo. Lililonisumbua katika ugonjwa wangu ni kuwa mie siuoni upole wa Mtume ﷺ nilipougua. Hakika si jingine Mtume ﷺ alikuwa akiingia na kutoa salamu kisha akiuliza:

«كَيْفَ نَيْكُم؟»

'Vipi hali yenu?'

Hili lilisumbua fikra zangu lakini sikuhi shari yoyote mpaka nilipotoka baada ya kuwa nimepata nafuu, na nilitoka na Ummu Mistwah (mamake Mistwah) tukielekea al-Manaswi, sehemu ambayo tulikuwa tunakwenda kutekeleza haja zetu (ndogo au kubwa/ mfano wa vyoo) na tulikuwa hatutoki isipokuwa usiku, na hiyo ilikuwa kabla ya kujengwa kwa vyoo karibu na nyumba zetu. Na desturi yetu ilikuwa ni desturi ya Waarabu wa mwanzo kwenda haja jangwani na tulikuwa tunaadhiwa na vyoo kuwa majumbani mwetu. Tuliondoka mimi na Ummu Mistwah, naye ni binti wa Abi Ruhm Ibn Al-Mutwallib Ibn Abd Manaaf na mamake alikuwa ni binti wa Swakhr Ibn Amir, (Khaalati) ni mama mdogo au mkubwa wa Abu Bakr – Swiddiq na mtoto wake alikuwa Mistwah ibn Uthaathah ibn 'Abbaad Ibn Al-Mutwallib. Tukawa tunarudi mimi na Ummu Mistwah nyumbani kwetu baada ya kumaliza shughuli zetu, Ummu Mistwah akajikwaa alipokuwa anatembea, naye akasema: 'Aangamie Mistwah'. Nami nikamwambia: 'Ni jambo ovu ulilosema. Je, unamtukana mtu aliyeshuhudia vita vya Badr?' Akanambia: 'Binti yangu mpendwa, hukusikia aliyoyasema?' Nikamuuliza: 'Na ni nini alichosema?' Akasema: 'Alinihadithia yote ya watu wazushi (*Ifk*) na hapo nikazidi maradhi juu ya maradhi yangu.' Niliporejea nyumbani kwangu alikuja Mtume ﷺ na akatoa salamu, kisha akasema:

«كَيْفَ نَيْكُم؟»

'Unajisikiaje?'

Nikamwambia: 'Je, utaniruhusu kwenda kwa wazazi wangu?' Akasema: Aishah رضي الله عنه, 'Nami wakati huo nilikuwa nataka kuyakinisha habari hiyo kutoka kwako.' Mtume ﷺ alinipa idhini, hivyo nikaenda kwa wazazi wangu. Nilimwambia mama yangu: 'Ewe mama yangu kwanini watu wanazungumza kuhusu hili?' Akasema: 'Tulia, naapa kwa Allah, hapana mwanamke ambaye anapendwa na mumewe na ana wake wenza isipokuwa wale wake wenza

watazidisha kusema vibaya'. Nilisema: 'Subhaanallah (Ametakasika Allah na upungufu wa aina yoyote)! Hakika watu wanazungumza kweli habari hii?' Nililia usiku kucha mpaka asubuhi. Machozi yangu hayakusimama kabisa usiku na nikapambazukiwa asubuhi nikiwa ninalia. Mtume ﷺ alimuita 'Ally ibn Abi Twaalib na Usaamah ibn Zayd رضي الله عنهما Akawataka ushauri katika kumuacha mke wake wakati Wahyi uliposimama. Ama Usaamah رضي الله عنه alinitaja kwa uzuri wa kadri alivyokuwa akijua kusalimika kwa mke wa Mtume na jinsi mapenzi ya Mtume yalivyo kwake. Hivyo Usaamah رضي الله عنه alimwambia: 'Ewe Mtume ﷺ, huyo ni mkeo, nasi hatujaona kwa mkeo isipokuwa kheri. Yote haya yasemwayo ni uongo na masingizio'. Ama Ally رضي الله عنه alisema: 'Ewe Mtume wa Allah, Allah تعالى Hajakudhiki na wanawake, unaweza ukipenda kuo mwengine. Hata hivyo kama ukipenda unaweza kulichunguza jambo lenyewe, unaweza kumwita kijakazi wake ukamwuliza kuhusu jambo hilo naye akakwambia ukweli'. Hivyo, Mtume ﷺ akamuita Barirah رضي الله عنها na kumwuliza:

«أَيُّ بَرِيرَةٍ هَلْ رَأَيْتِ مِنْ شَيْءٍ يَرِيْبُكَ مِنْ عَائِشَةَ؟»

'Ewe Barirah, umeona kitu chochote ambacho kitakutia shaka kuhusu Aishah'.

Naye akajibu: 'Naapa kwa Jina la Allah تعالى, Aliyekutuma kwa ukweli ni kwamba sijaona ubaya wowote kwake ila tu, analala ninapomwambia aangalie unga uliokandwa na kuumuka wakati sipo, na mbuzi huja na kuula.' Siku hiyo Mtume ﷺ alisimama na akaomba utetezi wa kitendo alichokifanya Abdillah bin Ubayy bin Salul. Mtume ﷺ aliwahutubia watu juu ya mimbari, akasema:

«يَا مَعْشَرَ الْمُسْلِمِينَ! مَنْ يَعْدِرُنِي مِنْ رَجُلٍ قَدْ بَلَغَنِي أَذَاهُ فِي أَهْلِ بَيْتِي، فَوَاللَّهِ مَا عَلِمْتُ عَلَى أَهْلِي إِلَّا خَيْرًا، وَلَقَدْ ذَكَرُوا رَجُلًا مَا عَلِمْتُ عَلَيْهِ إِلَّا خَيْرًا، وَمَا كَانَ يَدْخُلُ عَلَى أَهْلِي إِلَّا مَعِي»

"Enyi kongamano la Waislamu, ni nani atanitetea kwa mtu ambaye yamenifikia maudhi yake katika kumsingizia mke wangu, Naapa kwa Allah sijapatapo kujua chochote kwake yeye (Aisha) isipokuwa kheri tupu. Na hakika wamemtaja mtu, sijui kutoka kwake isipokuwa kheri tupu. Na hakuwa akiingia kwa wake zangu isipokuwa akiwa pamoja nami".

Hapo Sa'd ibn Mu'aadh Al - Answaariy رضي الله عنه alisimama na kusema: 'Ewe Mtume wa Allah! Naapa kwa Allah, mimi nitakuletea. Kama mtu huyo ni wa kabila letu la (Aus) basi tutamuua kwa kukata kichwa chake, na kama ni wa kabila la Khazraj utatuamrisha nasi tutekeleze amri yako. Aliposikia hayo Sa'd ibn 'Ubaadah رضي الله عنه¹, kiongozi wa kabila la Khazraj na alikuwa ni mtu Mwema, lakini mwenye ukabila. Alisimama na kumwambia Sa'd ibn Mu'aadh رضي الله عنه: 'Naapa kwa Allah تعالى, hutamuua na kamwe huwezi kumuua'. Hapo Usayd ibn Hudhayr رضي الله عنه ambaye alikuwa binamu yake Sa'd ibn Mu'aadh رضي الله عنه alisimama na kumwambia Sa'd ibn 'Ubaadah رضي الله عنه: 'Wewe unaongopa! Naapa kwa Allah تعالى, tutamuua, na wewe ni mnafiki ndio maana unamtetea mnafiki'. Hapo makabila mawili ya Aws na Khazraj yakagombana hadi yakataka kupigana. Mtume ﷺ akiwa amesimama juu ya mimbari, aliwatuliza ghadhabu zao mpaka wakatulia, kisha akateremka toka kwenye mimbari.

Siku hiyo niliendelea kulia sana, na machozi yangu hayakuacha kububujika na sikulala kabisa. Wazazi wangu walifikiria kilio kitapasua maini yangu. Pale wazazi wangu walipokuwa wamekaa nami ninalia, mwanamke wa Ki-answaar aliomba ruhusa ya kuingia kuniona. Nilimruhusu, naye alikaa na kulia pamoja nami. Baina ya kuwa tumekaa katika hali hiyo, Mtume ﷺ tahamaki akatuingilia, akatutolea salamu na kukaa karibu nami, kitu ambacho hakuwa amekifanya toka yaliposemwa yaliyosemwa, na mwezi ulikuwa umepita bila kuteremshiwa wahyi kuhusu kadhia yangu. Mtume ﷺ alitoa shahada alipokaa, baadae akasema:

'Baada ya hayo, Ewe 'Aishah hakika imenifikia kuhusu wewe kadha wa kadha, kama wewe uko mbali nalo nataraji Allah Atanidhihirishia kusalimika kwako, na kama umetenda dhambi mtake istighfar Allah na kisha tubia kwake. Kwani mja akikosa na akiomba msamaha, na kutubu, Allah humkubalia toba yake.'

Mtume ﷺ alipomaliza maneno yake, machozi yangu yalisimama kabisa na si kuhisi hata tone moja. Hapo nilimwambia babangu: 'Nijibie kwa Mtume ﷺ kwa niaba yangu'. Naye akasema: 'Mwanangu, Wallahi sijui nini nimwambie Mtume ﷺ kwa hiyo nikamuomba mama yangu 'Mjibu Mtume ﷺ kwa niaba

¹ Ahmad 1:194.

yangu'. Naye alisema: 'Mwanangu, sijui la kumwambia Mtume ﷺ'. Japokuwa nilikuwa msichana mdogo wa miaka sijahifadhi sana Qur'ani, nikasema: 'Naapa kwa Allah! Najua nyinyi mmesikia jambo kuhusu mimi na mmeamini. Na ikiwa nitakuambieni – hamtaamini, na kama nitakiri kosa ambalo sikufanya – na Allah تعالى Anajua kuwa sikufanya nyinyi mtaamini'. Hakika mimi naapa kwa Allah تعالى sioni mfano kati yangu na nyinyi ila ni kama alivyosema babake Yusufu:

فَصَبِّرْ حَمِيلًا ۖ وَاللَّهُ أَلْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١٨﴾

"Lakini subira ni njema; na Mwenyezi Mungu Ndiye wa Kuombwa msaada kwa haya mnayoeleza." (12:18)

Baada ya kusema hayo nikajilaza kitandani kwangu na kugeukia upande mwengine. Hali ya kuwa mimi Wallahi, Allah تعالى Anajua kuwa sina hatia, na bila shaka ni Yeye Pekee Anayejua kusalimika kwangu, sikufikiria kuwa itateremshwa sehemu ya Qur'ani katika kunitetea na ambayo itasomwa na watu hadi Siku ya Mwisho. Nilichofikiria ni kuwa labda Mtume ﷺ ataoneshwa ndoto ambayo Allah تعالى Atamjua kuwa sina hatia. Lakini hapo hapo ghafla dalili za kupokea Wahyi zilijidhihirisha kwa Mtume ﷺ, ambapo matone ya jasho kama lulu yalijikusanya juu ya uso wake: hali ambayo ilijitokeza hata msimu wa baridi, hii ni kwa sababu ya uzito wa maneno aliyokuwa akiteremshiwa. Tukajizuiya kimya. Alipokwisha pokea Wahyi, Mtume ﷺ alionesha kuwa amefurahi sana. Huku amezidiwa na furaha huku anacheka, maneno ya kwanza aliyosema yalikuwa:

«أُبَشِّرِي يَا عَائِشَةُ، أَمَا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ فَقَدْ بَرَّأَكَ»

"Hongera eeh 'Aishah, Allah Amekutakasa (na hatia)."

Hapo mama akaniambia: 'Simama uende kwake na umshukuru.' Nikasema: 'Naapa kwa Allah تعالى! Sitamshukuru yeye wala nyinyi wawili bali namshukuru Allah تعالى Aliyenidhihirishia kutokuwa kwangu na hatia'. Hivyo Allah تعالى Aliteremsha:

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِآلِفِكَ غَضَبًا مِنْكَ ۖ

"Hakika wale walioleta uzushi ni kundi miongoni mwenu..."

Mpaka Aya ya kumi. Allah تعالى Aliteremsha Aya hizi kumi kunitoa mimi hatiani. Abubakr رضي الله عنه, ambaye alikuwa akimsaidia Mistwah kwa sababu ya ujamaa

na kwa kuwa alikuwa maskini, alisema: 'Naapa kwa Allah تعالى! Sitamsaidia tena baada ya haya aliyoyasema kuhusu 'Aa'ishah رضي الله عنها'. Hapo Allah تعالى Aliteremsha:

وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَىٰ

“Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao...”

Mpaka,

أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٢﴾

“Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu Akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”
(24:22)

Abubakr رضي الله عنه aliposikia tu Aya hii alisema: 'Wallahi! Bila shaka ninapenda Allah تعالى Anisamehe'. Naye akaanza tena kumsaidia Mistwah na kwa ukunjufu zaidi kuliko awali, na akasema: 'Naapa kwa Allah تعالى, sitaacha kumsaidia'. Mtume ﷺ alimuuliza Zaynab bint Jahshi رضي الله عنها kuhusu mimi,

«يَا زَيْنَبُ مَاذَا عَلِمْتِ أَوْ رَأَيْتِ؟»

'Ewe Zaynab, unajua nini na umeona nini?'

Akamjibu: “Ewe Mtume wa Allah! Namuomba Allah تعالى Aulinde usikizi wangu na uoni wangu. Naapa kwa Allah تعالى, sijagundua chochote kumhusu ('Aishah رضي الله عنها) isipokuwa kheri na ucha-Mungu'. Na yeye (Zaynab) ndiye aliyekuwa akishinda nami kati ya wake za Mtume ﷺ, Allah تعالى Akamuhifadhi kwa ucha-Mungu wake. Lakini dadake Hamnah bint Jahshi alijiingiza katika uvumi kwa kumpinga dada yake, hivyo akajiletea maangamivu pamoja na wale walioangamia.” Amesema Ibn Shihaab: “Hivi ndivyo tunavyojua kuhusu kikundi hicho cha watu”¹. Pia Bukhari na Muslim wameinukuu Hadithi katika Sahihi zao kutoka kwa Hadithi ya Az-Zuhriy² na kwa Ibn Ishaq pia kutoka kwa Az-Zuhriy³. Pia kama hivyo alisema: “Yahya Ibn Abbaad ibn 'Abdullah ibn Az-Zubayr aliniambia mimi kutoka kwa babake kuwa 'Aishah رضي الله عنها na

¹ Ahmad 1:194.

² 306 Muslim 4:2129.

³ Fat-h al-Baariy 8:340.

'Abdullahi ibn Abu Bakr ibn Muhammad ibn 'Amr ibn Hazm Al-Answaariy ameniambia kutoka kwa 'Amrah, kutoka kwa 'Aa'ishah رضي الله عنها (ripoti) sawa na simulizi zilizotangulia. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Na Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِآلِفِكَ

"Hakika wale walioleta uzushi huo."

Inamaanisha, uongo, tuhuma na uzushi.

عُصْبَةٌ مِّنكُمْ

"Ni kundi miongoni mwao."

Inamaanisha ni kipote kati yenu Waislamu.

لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُمْ

"Msifikiri ni shari kwenu."

Enyi familia ya Abubakr رضي الله عنه.

بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ

"Bali hiyo ni kheri kwenu."

Inamaanisha, hapa ulimwenguni na kesho Akhera, utajo mtukufu na wa heshima hapa duniani na hadhi ya hali ya juu Kesho Akhera. Allah تعالى Ameonesha ile hadhi ambayo Ameipa familia ya Abubakr pale Alipomtetea Mama wa Waumini, Aishah رضي الله عنها, kwa Kuteremsha Qur'ani ambayo ilimtakasa na tuhuma aliyozushiwa. Qur'an ambayo,

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ

"Hautafikia upotovu mbele yake wala nyuma yake." (41:42).

Na kutokana na Mukdadha huu, wakati Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما alipoingia kwa Aishah رضي الله عنها huku akiwa katika machungu ya kifo, akamwambia: "Furahi, kwani wewe ni mke wa Mtume ﷺ na alikuwa anakupenda sana; hakuoa bikira isipokuwa wewe na uthibitisho wa kuwa hauna hatia uliteremshwa kutoka mbinguni."¹

¹ Fat'h Al-Bari 8:340.

Na Kauli yake Allah تعالى،

لِكُلِّ أَمْرٍ مِّنْهُم مَّا آكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ

“Yeyote aliyeshiriki, ameshapata nasibu yake ya dhambi kama anavyostahiki.”

“Yeyote aliyeshiriki, ameshapata nasibu yake ya dhambi kama anavyostahiki”, inamaanisha kuwa kila aliyezungumza kuhusu mas-ala haya na kumtuhumu Mama wa Waumini, ‘Aishah رضي الله عنها, kwa uasherati wa aina yoyote, atakuwa na fungu kubwa la adhabu.

وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ

“Na yule aliyebeba jukumu kubwa zaidi (katika masingizio).”

Inasemekana kuwa hii inamhusu yule aliyeanzisha uvumi na umbeya huu, au pia husemwa: Kwa Yule aliyekusanya uvumi na kuueneza kwa watu.

لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Atapata adhabu kali zaidi.”

Maana yake: Huyu alikuwa ‘Abdullah ibn Ubayy ibn Saluul, Allah تعالى Amfedheheshe pamoja na Kumlaani.

لَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بِأَنْفُسِهِمْ خَيْرًا وَقَالُوا هَذَا إِفْكٌ مُّبِينٌ ﴿١٢﴾

لَوْلَا جَاءُوا عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ ۚ فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا بِالشُّهَدَاءِ فَأُولَئِكَ عِنْدَ اللَّهِ هُمُ

الْكَاذِبُونَ ﴿١٣﴾

12. “Mbona mliposikia habari hii, wanaume Waumini na wanawake Waumini hawangewadhania wenzao wema, na kusema: Huu ni uzushi dhahiri?”

13. Kwa nini hawakuleta mashahidi wane? Na ilivyokuwa hawakuleta mashahidi wanne basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo”.

Kuwaadabisha Waumini Kwa Kueneza Tuhuma

Hapa Allah تعالى Anawakanya Waumini kuhusu mas-ala ya Aishah رضي الله عنها, kwani baadhi yao walihusika katika kueneza habari hizi ovu na uzushi uliotajwa. Hivyo Allah تعالى Anasema:

لَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ

“Mbona mliposikia habari hii”.

Maana yake: Habari zilizomsingizia Mama wa Waumini, Aishah رضي الله عنها.

ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَأَنْفُسِهِمْ خَيْرًا

“Wanaume Waumini na wanawake Waumini hawangewadhania wenzao mema”.

Inamaanisha, kwanini hawakulinganisha, yale waliyoyasikia na wao wenyewe ikiwa jambo kama hilo, haliwezi kulingana na hadhi yao, basi ni muhali kutukia kwa Mama wa Waumini, na hivyo hayamkiniki kuwa na hatia. Inasemwa ya kuwa Aya hii imeteremshwa kuhusu Abu Ayyub Khaalid ibn Zayd al-Answaariy pamoja na mkewe. Imamu Muhammad Ibn Ishaq Ibn Yasaar رحمه الله تعالى anasimulia kuwa: “Mke wake Abu Ayyub, Ummu Ayyub alimwambia mumewe, ‘Ewe Abu Ayyub, umesikia uvumi unaosemwa na watu dhidi ya mama Aa’ishah?’ Naye alisema: ‘Ndio na yote hayo ni uongo. Ewe Umm Ayyub kama ungekuwa mahala pa mama Aishah رضي الله عنها, ungeweza kufanya hivyo?’ Akajibu: ‘Wallahi nisingeweza kufanya hivyo’. Abu Ayyub رضي الله عنه akasema: ‘Na mama Aishah ni mbora kuliko wewe. Qur’ani ilipoteremshwa, Allah تعالى Aliwataja wale waliozungumza tendo hilo ovu miongoni mwa watu wazushi (Ifk) kwa masingizio,

إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنكُمْ

“Hakika wale walio leta uongo ni kundi miongoni mwenu.” (24:11)

Hii inamuhusu Hassaan ibn Thaabit na washirika wake ambao walisema waliyosema. Kisha Allah تعالى Akasema:

لَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ

“Mbona mliposikia habari hii, wanaume Waumini hawakuwadhania.”

Maana yake: Kama alivyofanya Abu Ayyub na mkewe رضي الله عنهما¹. Kauli ya Allah تعالى:

ظَنَّ الْمُؤْمِنُونَ

“Wakawadhania Waumini wanaume”.

Maana yake: Kwanini hawakuwadhanika mema, kwa sababu Mama wa Waumini ni mkewe Mtume ﷺ na yuko karibu sana naye. Hii inahusiana na hisia za ndani kabisa. Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَقَالُوا

“Na wakasema.”

Maana yake: Kwa ndimi zao, kwa maneno,

هَذَا إِفْكٌ مُّبِينٌ

“Huu ni uzushi dhahiri?”

Maana yake: Uongo wa Dhahiri kabisa unaomuelezea Mama wa Waumini. Lililotokea lilikuwa halifai kuwa ni sababu ya kutia shaka. Kwa hakika kitendo cha Mama wa Waumini kujitokeza wazi, akiwa amepanda ngamia wa Swafwaan ibn al-Mu’atwtwal wakati wa adhuhuri, huku jeshi zima likiwa linaangalia na Mtume ﷺ mwenyewe akiwa miongoni mwao, ilikuwa ni dhahiri kuwa hapana sababu ya kutilia shaka. Kama kungelikuwa na kitu chochote cha kutilia shaka kuhusu jambo hilo, hawangekuwa ni wenye kuja kwa njia hiyo mbele ya mashahidi wengi; wangekuja kwa siri. Kwa msingi huu, yale waliokuwa wakiyasema wenye kumtuhumu Mama wa Waumini yalikuwa ni uongo mtupu, uzushi na mazungumzo maovu ya kipuuzi, ambayo watu waliojishughulisha nayo walipotea. Allah تعالى Anasema:

لَوْلَا جَاءُوا عَلَيْهِ بِأَرْبَعَةٍ شُهَدَاءَ

“Kwanini hawakuleta mashahidi wanne?”

Kumaanisha kuwa hiyo ni dalili tosha dhidi ya wanayoyasema.

¹ Atw-Twabariy 19: 129 Isnadi yake ni dhaifu.

فَإِذْ لَمْ يَأْتُوا بِالشَّهَادَةِ فَأَوَّلْتِكِ عِنْدَ اللَّهِ هُمْ الْكَذِبُونَ ﴿١٤﴾

“Na ilivyokuwa hawakuleta mashahidi wanne basi hao mbele ya Mwenyezi Mungu ni waongo.”

Allah تعالی Amehukumu kuwa hawa walikuwa watu waongo walio waovu.

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِي مَا أَفَضْتُمْ فِيهِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾ إِذْ تَلَقَّوْنَهُ بِالسِّنِّتِمْ وَتَقُولُونَ بِلُغْوِكُمْ مَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّنًا وَهُوَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾

14. “Na lau kuwa si Fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na Rehema Yake katika dunia na Akhera, bila ya shaka ingekupatani adhabu kubwa kwa sababu ya yule mliyojiingiza.

15. Mlipoyapokea kwa ndimi zenu na mkasema kwa vinywa vyenu msiyoyajua, na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa”.

Fadhila ya Allah تعالی kwa Kuwapa Wazushi (Ahlu-ifk) Fursa ya Kutubu

Allah تعالی Anasema:

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Na lau kuwa si Fadhila ya Allah juu yenu na Rehema Yake katika dunia na Akhera”

Aya hii inawasemesha wale waliomzulia Aishah رضي الله عنها; Enyi mliolingia katika mjadala na kumtuhumu Aishah رضي الله عنها, Allah تعالی Amekubali toba yenu na kunyenyekea kwenu Kwake hapa duniani, na Amekusameheni kwa sababu ya Imani yenu kuhusu kesho Akhera.

لَمَسَّكُمْ فِي مَا أَفَضْتُمْ فِيهِ

“Bila ya shaka ingekupatani kwa sababu ya yale mliyojiingiza.”

Kwa ajili ya kadhiya ya uzushi (ifk.)

عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Adhabu kali”.

Hii inawahusu wale waliokuwa na Imani kwa Allah تعالى kwa sababu ya kutubu kwao, kwa mfano Mistwah, Hassan ibn Thaabit na Hamnah bint Jahshi, dada yake Zaynab bint Jahshi رضي الله عنهم. Ama kuhusu wanafiki walioshiriki katika uzushi (ifk) kama 'Abdullah ibn Ubayy ibn Saluul na wenzake, sio waliokusudiwa katika Ayah hii, kwa sababu hawakuwa na Imani thabiti na amali njema inayolingana na hili katika mizani yao au kufuta yale waliyoyafanya. Kwa jinsi hiyo, lilokemewa lilokuja kwa tendo maalumu ni lazima lilitokelezwa kwa sharti zake, ikiwa hakuna toba au matendo mazuri ya kutosha katika mizani au kuyazidi. Baadae Allah تعالى Anasema:

إِذْ تَلَقَّوْنَهُ بِأَلْسِنَتِكُمْ

“Mliyoyapokea kwa ndimi zenu.”

Mujaahid na Sa'iid ibn Jubayr wamesema: “Baadhi yenu mlikuwa mkiwasimulia wengine”¹, pale mmoja aliposema: “Nimesikia haya kutoka kwa Fulani, na Fulani amesema kadhaa wa kadhaa, na watu wamehadithia hivi na hivi”. Na wengine wanaisoma Aya hii:

“Idh Taliqunahu Bialsinatikum - Mlipozua uongo kwa ndimi zenu”

(Na ile ya mwanzo inasomwa – *Idh Talaqqawnahu Bialsinatikum*).

Katika Sahiih Bukhari, imepokewa kuwa Aishah رضي الله عنها alikuwa anaisoma hivyo.² Kisomo cha mwanzo ni mashuhuri sana na ndio kilichopendekezwa na jopo la wanazuoni (Jamhuri), na wengi wanasoma hivyo, ila kisomo cha pili kimenukuliwa kutoka kwa Mama wa Waumini, 'Aa'ishah رضي الله عنها.

وَتَقُولُونَ بِأَفْوَاهِكُمْ مَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ

“Na mkasema kwa vinywa vyenu msiyokuwa na elimu nayo.”

Maana yake: Mlikuwa mkizungumza kuhusu jambo msilolijua. kisha Allah تعالى Akasema:

¹ Atw-Twabariy 19:132.

² Fat-h al-Baariy 8: 340.

وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّئًا وَهُوَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمٌ ﴿٦﴾

“Na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Allah ni kubwa”.

Hii inamaanisha, ‘Mliyosema kuhusu Mama wa Waumini na kulichukulia kuwa jepesi na sahali, hata asingekuwa mke wa Mtume halingekuwa dogo. Itakuwaje kwa mke wa Mtume ﷺ asiyesoma kilichoandikwa, Nabii wa mwisho na Bwana wa Mitume? Ni kubwa mno mbele ya Allah kuhusu mke wa Mtume Wake ﷺ. Hakika Allah Aliyetukuka Anakasirika kutoheshimiwa mke wa Mtume ﷺ yeyote katika Mitume wake. Na kama hili hatolikubali litokee. Na kwa kuwa halikuwa kwa waliotangulia. Vipi litakuwa hili kwa mama bora kabisa wa wake wa Mitume wote, mke wa Mtukufu wa mwana wa Adam Duniani na Akhera? Allah تعالی Anasema:

وَتَحْسَبُونَهُ هَيِّئًا وَهُوَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمٌ ﴿٦﴾

“Na mlifikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Allah ni kubwa”.

Na katika Sahihi mbili imenukuliwa:

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ سَحَطِ اللَّهِ، لَا يَذَرِي مَا تَبْلُغُ، يَهْرِي بِهَا فِي النَّارِ
أَبْعَدَ مَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ»

“Hakika mtu huenda akasema neno katika yanayomkasirisha Allah bila kutambua litafika umbali gani, anaingia nalo katika moto (wa Jahanamu) mbali zaidi kuliko baina ya mbingu na ardhi”.

Kulingana na riwaya nyengine imekuja:

«لَا يُلْفِي لَهَا بَأَلَا»

“Huenda akawa hata hakulifikiria”¹

* * *

¹ Fat-h al-Baariy 11:314 na Muslim 4:2290.

وَلَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُمْ مَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَتَّكِلَ بِهَذَا
 سُبْحَانَكَ هَذَا بُهْتَانٌ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾ يَعِظُكُمُ اللَّهُ أَنْ تَعُودُوا
 لِمِثْلِهِ أَبَدًا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٧﴾ وَيُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ
 الْآيَاتِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ
 تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ ءَامَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي
 الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾ وَلَوْلَا
 فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ زَعُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٢٠﴾
 * يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّبِعُوا خُطُوبَ الشَّيْطَانِ وَمَنْ
 يَتَّبِعْ خُطُوبَ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ
 وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ
 أَبَدًا وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢١﴾ وَلَا
 يَأْتِلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ أَنْ يُؤْتُوا أُولَى الْقُرْبَى
 وَالْمَسْكِينِ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلْيَعْفُوا
 وَلْيَصْفَحُوا أَلَا يُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ
 رَحِيمٌ ﴿٢٢﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ
 الْمُؤْمِنَاتِ لَعُنُوا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ
 ﴿٢٣﴾ يَوْمَ نَشْهَدُ عَلَيْهِمْ أَلْسِنَتُهُمْ وَأَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا
 كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٤﴾ يَوْمَئِذٍ يُوفِّيهِمُ اللَّهُ دِينَهُمُ الْحَقَّ
 وَيَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ الْمُبِينُ ﴿٢٥﴾

وَلَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُمْ مَا يَكُونُ
 لَنَا أَنْ نَتَّكِلَ بِهَذَا سُبْحَانَكَ هَذَا
 بُهْتَانٌ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾ يَعِظُكُمُ اللَّهُ أَنْ
 تَعُودُوا لِمِثْلِهِ أَبَدًا إِنْ كُنْتُمْ
 مُؤْمِنِينَ ﴿١٧﴾ وَيُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ
 الْآيَاتِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٨﴾

16. "Na mbona mliposikia hamkusema: 'Haitupasii kuzungumza haya: Utukufu ni wa Allah! Haya ni masingizio makubwa'.

17. Allah Anakunasihini kwamba (siku zijazo) msirudie kabisa kufanya mfano wa haya, ikiwa nyinyi ni Waumini kweli.

18. Na Allah Anakubainishieni Aya Zake, na Allah Ndiye Ajuaye, Mwenye Hikima zaidi".

Mafunzo ya Adabu kwa Mara Nyingine

Hili ni funzo jingine la adabu baada ya ile amri ya agizo la kwanza la kuwadhania watu kheri, yaani jambo lisilo sawa iwapo limetajwa

kuhusu watu wema, basi bora zaidi mtu anatakiwa kuwadhania wao kheri, na asihisi katika nafsi kitu chochote kuhusu wao mbali na hilo. Baada ya hapo ikiwa mtu nafsi yake inaingia kitu katika dhana potofu kama wasiwasi wa Shetani au mawazo mabaya basi haifai kwake kuzungumza chochote kuhusu hilo. Kwani Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى تَجَاوَزَ لِأُمَّتِي عَمَّا حَدَّثَتْ بِهِ أَنْفُسَهَا مَا لَمْ تَقُلْ أَوْ تَعْمَلْ»

“Hakika Allah Aliyetukuka Ameusamehe Ummah wangu, kilichowaza nafsi zao maadamu hawatakizungumza au kufanya (kimatendo).”

Hii imenukuliwa kutoka katika Sahihi mbili¹.

Na Allah تعالى Amesema:

وَلَوْلَا إِذْ سَمِعْتُمُوهُ قُلْتُمْ مَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَتَكَلَّمَ بِهَذَا

“Na mbona mliposikia hamkusema: ‘Haitupasii kuzungumza haya”.

Maana yake: Haifai kwetu sisi kuzungumza maneno haya kwa midomo yetu wala kuyataja kwa yeyote yule.

سُبْحَانَكَ هَذَا بُهْتَنٌ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾

“Utukufu ni wako Allah! Huu ni uzushi mkubwa.”

Maana yake: Ametakasika Allah تعالى (na Ameepukana na kila aina ya upungufu) kwa kusemwa maneno haya juu ya mke wa Mtume Wake na Kipenzi cha kipenzi Chake.

Kisha Allah تعالى Anasema:

يَعْظُمُ اللَّهُ أَنْ تَعُودُوا لِمِثْلِهِ أَبَدًا

“Allah Anakunasihini kwamba (siku zijazo) msirudie kabisa kufanya mambo kama haya.”

¹ Fat-h al-Baariy 11:557 na Muslim 1:116-117.

Maana yake: Allah Anakukatazeni na kukuonyeni jambo linalofanana na hili mara nyingine tena katika siku zijazo na msirudie tena jambo hilo daima.

Kwa hii Akasema:

﴿١٦﴾ إِنَّ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Ikiwa nyinyi ni Waumini wa ukweli.”

Maana yake: Mkiwa kweli nyinyi mnamuamini Allah تعالى na Sheria Zake na mnaheshimu na kumtukuza Mtume Wake. Ama kwa wale waliosifiwa na kuelezwa kuwa ni makafiri, basi wao hukumu yao ni nyengine.

Kisha Akasema Aliyetukuka:

﴿١٧﴾ وَيُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَاتِ

“Allah Anakubainishieni Ayah Zake”.

Maana yake: Amezibainisha na Kuziweka wazi kwenu Hukumu Zake za kisheria na hikima za Qadari. Na jueni kuwa:

﴿١٨﴾ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

“Na Allah Ndiye Ajuaye zaidi Mwingi wa Hikima.”

Maana yake: Allah تعالى ni Mjuzi zaidi kwa mambo yanayowafaa waja Wake na Mwingi wa Hikima kwa (kutunga) Sheria Zake na Kuweka Qadari Yake.

﴿١٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ ءَامَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا

﴿٢٠﴾ وَالْآخِرَةِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٠﴾

19. Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini, watapata adhabu iumizayo mno, katika dunia na akhera. Na Allah Anaijua nanyi hamjui (athari yake)

Kuwatia Adabu wale wanaopenda kuwatangazia machafu waumini.

Hii ni adabu ya tatu kwa mwenye kusikia jambo lolote miongoni mwa maneno maovu, kikaingia akilini mwake kitu, (alichokiamini) katika maneno hayo, basi asizidishe mazungumzo kutokana nayo, wala asiyaeneze na kuyatangaza kwa wengine.

Hakika Allah تعالى Amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ آمَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini, watapata adhabu iumizayo mno.”

لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا

“Wao wana adhabu iumizayo mno katika dunia.”

Maana yake: Adhabu ya Kiboko (*Haddi*) na katika Akhera Adhabu (ya moto).

وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٥﴾

“Na Allah Anajua nanyi hamjui (athari yake).”

Maana yake: Yarudisheni mambo yote Kwake na mtaongoka. Na amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Thawbaan رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا تُؤْذِرُوا عِبَادَ اللَّهِ وَلَا تُعَيِّرُوهُمْ، وَلَا تَطْلُبُوا عَوْرَاتِهِمْ، فَإِنَّهُ مَنْ طَلَبَ عَوْرَةَ أَخِيهِ الْمُسْلِمِ طَلَبَ اللَّهُ عَوْرَتَهُ، حَتَّى يَفْضَحَهُ فِي بَيْتِهِ»

“Musiwaudhi waja wa Allah wala msiwaaibishe na wala musitafute aibu zao. Yeyote mwenye kutafuta aibu za nduguye Muislamu, Allah Atafichua aibu zake, mpaka amfedheheshe hata akiwa ndani ya nyumba yake.”¹

¹ Ahmad 5:279.

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ رءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٠﴾ * يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
تَتَّبِعُوا خُطُوتِ الشَّيْطَانِ ۚ وَمَنْ يَتَّبِعْ خُطُوتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ
وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَنْ يَشَاءُ
وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢١﴾

20. "Kama Allah Asinge waonesheni Fadhila na Rehema Zake juu yenu, (kashfa hii ingeleta matokeo mabaya sana): Kwa hakika Allah ni Mpole mno, Mwingi wa Huruma."

21. "Enyi mlioamini! Msizifuata nyayo za Shetani basi yeye huamrisha machafu na maovu. Na lau kuwa si Fadhila ya Mwenyezi Mungu na Rehema Yake juu yenu, asingelitakasika miongoni mwenu kabisa hata mmoja. Lakini Mwenyezi Mungu Humtakasa Amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua."

Kukumbushwa Fadhila za Allah تعالی na Kuonywa Dhidi ya Kufuata Nyayo za Shetani

Allah تعالی Amesema:

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ رءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٠﴾

"Kama Allah Asingewaonesheni Fadhila na Rehema Zake juu yenu, (kashfa hii ingeleta matokeo mabaya sana): Kwa hakika Allah ni Mpole, Mwingi wa huruma."

Maana yake: Lau isingelikuwa jambo hili lingetokea jambo jingine, lakini Allah تعالی ni Mpole kwa waja Wake na Mwenye Huruma sana kwao. Hivyo, Allah تعالی Akawasamehe wale wenye kuomba toba kutoka Kwake kwa dhambi ya kadhiya hii, na pia kuwasafisha miongoni mwa wale waliosafishwa kwa adhabu ya kiboko (Hadd).

Kisha Allah Aliyetukuka Anasema:

﴿ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ﴾

“Enyi Mlioamini! Msifuate nyayo za shetani.”

Maana yake: Njia zake na mapitio yake na yale anayoyaamrisha.

﴿ وَمَنْ يَتَّبِعْ خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ﴾

“Na atayefuata nyayo za shetani (atapotea), kwani yeye huamrisha mambo machafu na maovu.”

Huku ni kukemea na kuhadharisha kutokana na hilo, kwa ibara fasaha zaidi yenu kufikisha ujumbe na kwa muhtasari mzuri mno wenye kunasihi na kuufikisha ujumbe. Amesema ‘Aliy ibn Abi Twalha ambaye kapokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa,

﴿ خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ﴾

“Nyayo za shetani”.

Inamaanisha amali zake.¹ Na amesema Ikrimah inamaanisha: “Wasiwasi wake mbaya”. Na amesema Qataadah ina maana ya kuwa: “Kila maasi (mambo ya madhambi, maovu) yametokana na nyayo za shetani.”² Amesema Abu Mijlaz: “Nadhiri katika kufanya maasi ni katika nyayo za shetani.”³ Kisha Allah تعالى Akasema,

﴿ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ أَبَدًا ﴾

“Na lau kuwa si Fadhila za Allah na Rehema Zake hangetakasika kabisa miongoni mwenu yoyote.”

Maana yake: Lau kuwa si Yeye kuwa Anamruzuku Amtakaye kutubia na kurudi Kwake na Kuzitakasa nafsi kutokana na ushirikina wake, uovu wake na uchafu wake, na yaliyomo ndani yake (nafsi) katika tabia chafu kila mtu kulingana na kiwango chake, hakuna hata mmoja ambaye angetakasika wala kuwa mwema.

¹ Atw-Twabariry 3:301.

² Ad-Durr al-Manthuur 1:404.

³ Atw-Twabariry 3:301.

وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَن يَشَاءُ

“Lakini Allah Peke Yake Ndiye Anayemtakasa Amtakaye.”

Inamaanisha, miongoni mwa viumbe Vyake na Humpoteza Amtakaye, kwa Kumuacha na madhambi.

وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

Maana yake: Ni msikivu wa waja Wake. Na pia Yeye “Anajua zaidi” anayestahiki kuongozwa miongoni mwao, na anayestahiki kupotoka.

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ ۚ وَمَن يَتَّبِعْ خُطُوَاتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ۚ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنكُمْ مِّنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَن يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴾

21. Na wale katika nyinyi wenye Fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na waliohama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu Akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.

Kuhimiza Kutoa na Kusamehe kwa Waliojaaliwa Fadhila ya Mali

Anasema Aliyetukuka:

وَلَا يَأْتَلِ

“Na wala wasiape.” Maana yake: Kula kiapo.

أُولُوا الْفَضْلِ مِنكُمْ

“Wale miongoni mwenu, ambao wamepatiwa fadhila.”

Maana yake: Wale wenye uwezo wa kutoa sadaka na kufanya wema.

وَالسَّعَةِ

“Na (wenye) wasaa.” Maana yake: Wale wenye mali (na bahati nzuri).

أَنْ يُؤْتُوا أَوْلِيَ الْقُرْبَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْمُهَاجِرِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

“Wawe ni wenye kuwapa na kuwasaidia jamaa zao, masikini na Muhaajirina katika njia ya Allah.”

Maana yake: Msiape kuwa hamtawathamini jamaa zenu masikini na waliohama kwa ajili ya Allah تعالى, na huu ndio upeo wa ukarimu na huruma katika kuenzi undugu. Na kwa ajili hii Allah تعالى Anasema:

وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا

“Na wasamehe na wastahamili.”

Maana yake: Matusi yaliyopita na kutendewa maudhi. Hii ni sehemu ya Upole, Ukarimu na Huruma Yake Allah تعالى kwa viumbe Vyake, pamoja na kuwa wanajidhulumu nafsi zao. Ayah hii iliteremshwa kuhusu Abubakr Asw-swiddiq رضي الله عنه, pale alipoapa kuwa hatamsaidia tena Mistwah ibn Uthaathah baada ya kusema aliyoyasema kumhusu Aishah رضي الله عنها kama tulivyoona katika Hadithi iliyotangulia awali kueleza.

Baada ya Allah تعالى Kuteremsha utakaso wa Mama wa Waumini. Na nafsi za waumini kupata utulivu na kuridhika na matokeo ya tukio hilo, na wale Waumini walioeneza habari hiyo kutubia, na adhabu ya viboko (*Hadd*) ikatekelezwa kwa baadhi ya wale waliohusika. Hapo Allah تعالى Aliulainisha moyo wa As-Swiddiq kwa jamaa yake Mistwah, ambaye alikuwa ni mtoto wa mama yake mdogo au mkubwa, kwani yeye alikuwa masikini sana hana mali yoyote isipokuwa kile alichokuwa akipewa na Abubakr رضي الله عنه. Alikuwa ni miongoni mwa wale waliohama kwa ajili ya Allah تعالى. Alizua uongo na hayo masingizio, lakini Allah تعالى Alikubali toba yake na adhabu ya kiboko (*Hadd*) iliyowekwa ilitekelezwa kwake. Asw-Swiddiq alikuwa akijulikana kwa ukarimu wake na alikuwa akiwafadhili jamaa zake na wageni sawa sawa. Pindi Aya hii ilipoteremshwa: Hadi katika Kauli yake.

أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ

“Je, hampendi Allah Akusameheni?”

Ambayo inaonesha thawabu inakwenda sanjari na amali, na ukiwasamehe wengine Tutakusamehe, na ukipatana na mgomvi wako, nasi pia Tutaswafiana

nawe, hapo Asw-Swiddiq رضي الله عنه akasema, "Bila shaka, naapa kwa Allah تعالى, tunapenda, Mola wetu Mlezi Utusamehe makosa yetu". Baada ya hapo alirudia tena kumsaidia Mistwah, na kusema, "Naapa kwa Allah تعالى! Sitaacha kumsaidia daima". Hii ilikuwa ni kuyarudi yale maneno aliyoyasema awali, "Wallaah, sitamsaidia tena milele". Hii ni dalili ya kuonesha kuwa anastahiki kuitwa Asw-Swiddiq [mwenye kusadikisha]. Allah تعالى Amridhie Yeye na pia Amridhie binti yake.

إِنَّ الَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ لَعُنُوا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَهُمْ
عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٦﴾ يَوْمَ تَشْهَدُ عَلَيْهِمْ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾
يَوْمَ يُؤْفِكُ اللَّهُ دِينَهُمُ الْحَقَّ وَيَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ الْمُبِينُ ﴿١٨﴾

23. Hakika wale wanaowasingizia wanawake, wanaojihishimu (wastahivu), walioghafilika, Waumini, wamelaaniwa duniani na Akhera, nao watapata adhabu kubwa.

24. Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa waliyokuwa wakiyatenda.

25. Siku hiyo Mwenyezi Mungu Atawalipa sawa sawa malipo yao ya haki, na watajua kwamba Allah Ndiye Haki na Ndiye Mwenye Kuidhihirisha Haki".

Onyo kwa wenye kuwasingizia wanawake wenye staha wasiojua maovu na waumini wa kweli.

Hili ni onyo kubwa kutoka kwa Allah تعالى kwa wale wenye kuwasingizia wanawake wenye staha, ambao hawajawahi hata kufikiria kitu chochote kitakachoathiri heshima yao kwani wao ni Waumini wa kweli. Mama wa Waumini ni awla na bora zaidi kuingia katika kundi hili kuliko mwanamke mwengine yeyote mwenye staha, hasa yule ambaye Aya hii iliteremshwa kwa ajili yake: Aishah bint Asw-Swiddiq رضي الله عنها. Wanazuoni wote wameafikiana kuwa yeyote mwenye kumsingizia yeye (رضي الله عنها 'Aa'ishah) au kumshutumu dhidi yake baada ya yale yaliyosemwa katika Aya hii, ni kafiri, kwa sababu ya ukaidi na inadi yake dhidi ya Qur'ani. Hukumu hii inawajumlisha wake wote wa Waumini.

لُعِنُوا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Wamelaaniwa duniani na Akhera.”

Hii ni kama Aya ifuatayo:

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Hakika wanaomuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake...” (33: 57).

‘Abdur-Rahman ibn Zayd ibn Aslam amesema: “Hii ni kuhusu Aishah رضي الله عنها, na yeyote mwenye kufanya mfano wa hayo kwa leo kwa Waislamu wanawake, atapata hayo hayo Aliyoyasema Allah تعالى. Lakini Aishah رضي الله عنها ndiye muhusika halisi wa Aya hii.”¹

Ampokea ibn Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«اجْتَنِبُوا السَّبْعَ الْمُفْبِقَاتِ»

“Jiepusheni na madhambi saba yanayoangamiza.”

Watu wakauliza: “Ewe Mtume wa Allah ni yapi hayo?” Akasema:

«الشُّرْكَ بِاللَّهِ، وَالسَّخِرُ، وَقَتْلُ النَّفْسِ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ، وَأَكْلُ الرِّبَا، وَأَكْلُ مَالِ الْيَتِيمِ، وَالتَّوَلَّى يَوْمَ الرَّحْبِ، وَقَذْفُ الْمُحْصَنَاتِ الْغَافِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ»

“Kumshirikisha Allah; uchawi; kuua nafsi ambayo Allah Ameiharamisha isipokuwa kwa haki; kula riba; kula mali ya yatima; kukimbia siku ya vita na kuwatuhumu kwa zinaa wanawake waliohifadhiwa na Allah, Waumini wasiyo na habari za zinaa.”

Imenukuliwa Hadithi kutoka katika Sahihi mbili.²

يَوْمَ تَشْهَدُ عَلَيْهِمْ أَلْسِنُهُمْ وَأَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢٤﴾

“Wasiisahau ile Siku ambayo ndimi zao wenyewe na mikono yao itatoa ushahidi kwa waliyoyatenda”.

¹ At-Twabary 19:139.

² Fat'h al-Baariy 5:462 na Muslim 1:92.

ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: "Hakika washirikina pindi watakapoona kuwa hawaingii Peponi isipokuwa watu wema wanaosali, watasema: "Njoooni, tupinge." Na Watakataa kila kitu, hivyo watafungwa midomo yao. Baada ya hapo mikono yao pamoja na miguu yao itashuhudia na wala haitaweza kumficha Allah تعالى chochote."¹ Na amepokea tena Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Anas ibn Maalik رضي الله عنه aliyesema: "Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ akacheka mpaka magego yake yakaonekana. Kisha akasema:

«أَتَذَرُونَ مِمَّ أَضْحَكُ؟»

'Je, mnajua kwa nini ninacheka?'

Tukasema: 'Allah تعالى na Mtume Wake wanajua zaidi'. Akasema:

«مِنْ مُجَادَلَةِ الْعَبْدِ لِرَبِّهِ يَقُولُ: يَا رَبِّ أَلَمْ تُجْرِنِي مِنَ الظُّلْمِ؟ فَيَقُولُ: بَلَى، فَيَقُولُ: لَا أَجِيزُ عَلَيَّ شَاهِدًا إِلَّا مِنْ نَفْسِي، فَيَقُولُ: كَفَى بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ شَهِيدًا وَبِالْكَرَامِ عَلَيْكَ شُهُودًا، فَيُخْتَمُ عَلَى فِيهِ وَيُقَالُ لِأَرْكَانِيهِ: انْطِقِي فَتَنْطِقِ بِعَمَلِيهِ، ثُمَّ يُخَلِّي بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْكَلَامِ فَيَقُولُ: بَعْدًا لَكُنَّ وَسُخْرًا فَعَتَكُنَّ كُنْتُ أَنَا ضِلُّ»

'Kwa sababu ya mjadala wa mja na Mola Wake': atasema: 'Ewe Mola wangu! Je, Hukunikinga kufanya dhulma?' Atasema: 'La'. Atasema: 'Sitakubali shahidi isipokuwa nafsi yangu'. Allah Atasema: 'Inatoshia nafsi yako leo kuwa shahidi dhidi yako, nawe unao mashahidi watukufu. Mdomo wake utafungwa, viungo vyake vitaambiwa; Zungumzeni!. Navyo vitazungumzia amali yake (aliyokuwa akiitenda)'. Baada ya hapo ataruhusiwa kuzungumza, naye atasema: 'Ondokeni muwe mbali nami na muangamie! Mimi nilikuwa nikiwatetea nyinyi.'² Amenukuu Muslim na Annassai.

Na kwa Kauli Yake تعالى:

يَوْمَ يَدْعُ يَوْمَئِذٍ يُؤْفِكِهِمْ اللَّهُ دِينَهُمُ الْحَقَّ

"Siku hiyo Mwenyezi Mungu Atawapa sawa sawa malipo yao ya haki."

¹ Ad-Durr ul-Manthuur 6:167 na At-Twabaray 19:142.

² Muslim 2969.

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما:

دِينَهُمْ

“Diinahumu.”

Maana yake: “Ni hesabu yao. Na kila mahali ambapo neno hili linapatikana ndani ya Qur’ani basi linamaanisha hesabu zao”. Na hivyo ndivyo walivyosema wanazuoni zaidi ya mmoja”.¹ Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَيَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ الْمُبِينُ ﴿١٦﴾

“Na watajua kwamba Allah Ndiye Haki dhahiri.”

Maana yake: Ahadi Yake na Maonyo Yake na Hesabu Yake - yote ni ya Uadilifu hamna dhulma ndani yake.

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:141.

الْحَيِّثُ لِلْحَيِّثِ وَالْحَيِّثُ لِلْحَيِّثِ وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ
 وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا
 يَقُولُونَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٢٦﴾ يَتَأْتِيَ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّى تَسْتَأْذِنُوا
 وَتُسَلِّمُوا عَلَى أَهْلِهَا ؕ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ
 ﴿٢٧﴾ فَإِنْ لَمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّى
 يُؤْذَنَ لَكُمْ ؕ وَإِنْ قِيلَ لَكُمْ آرْجِعُوا فَآرْجِعُوا ۗ هُوَ أَزْكَى
 لَكُمْ ؕ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ
 أَنْ تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ فِيهَا مَتَعٌ لَّكُمْ ؕ وَاللَّهُ يَعْلَمُ
 مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٢٩﴾ قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ
 يَغْضُؤْنَ مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ؕ ذَٰلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ
 إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٣٠﴾

الْحَيِّثُ لِلْحَيِّثِ وَالْحَيِّثُ لِلْحَيِّثِ وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ
 وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا
 يَقُولُونَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٢٦﴾

26. "Wanawake waovu ni wa wanaume waovu, na wanaume waovu ni wa wanawake waovu. Na wanawake wema ni wa wanaume wema, na wanaume wema ni wa wanawake wema. Hao wameepushwa na hayo wanayoyasema; wao watapata msamaha na riziki ya ukarimu iliyo nzuri."

Ubora wa Aishah رضي الله عنها ni kwa Sababu ya Kuolewa na Mbora wa Wanadamu

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Maneno mabaya ni kwa wanaume wabaya, na wanaume waovu ni kwa kauli mbaya. Na maneno mazuri ni kwa wanaume wazuri, na wanaume wazuri ni kwa kauli zilizo nzuri." Akasema: 'Hii imeteremshwa kumhusu Aishah رضي الله عنها na watu wazushi (Ifk).'¹ Na hivi ndivyo ilivyopokewa kutoka kwa Mujaahid, 'Atwaa', Sa'iid ibn Jubayr, Ash-Sha'biy, Adh-Dhahhaak, na hii pia ndiyo rai iliyochaguliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى.² Alifasiri kumaanisha kuwa maneno maovu yanastahiki zaidi kwa

¹ Atw-Twabariy 19:142. Ad-Durr al-Manthuur 6:167.

² At-Tabari 19:143-144.

walio waovu miongoni mwa watu na maneno mazuri yanastahiki zaidi kwa walio wazuri miongoni mwa walio wazuri mwa watu. Hivyo waliyoyanasibisha wanafiki kwa 'Aa'ishah رضي الله عنها wao ndio yanawafaa zaidi, naye alikuwa anastahiki zaidi kuwa mbali na hatia na kutakasika nao. Na kuzingatia hilo, Anasema Aliyetukuka:

أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَ

"Hao wameepushwa na hayo wanayo yasema."

'Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibnu Aslam amesema: "Wanawake waovu ni wa wanaume waovu na wanaume waovu ni wa wanawake waovu. Na wanaume wema ni wa wanawake wema na wanawake wema ni wa wanaume wema."¹

Na hii pia kwa lazima inarudi kwa yale waliyoyasema, hiyo ni kusema Allah تعالى Hangemfanya Aishah رضي الله عنها kuwa mke wa Mtume ﷺ isipokuwa yeye ni mzuri kwa sababu (Mtume ﷺ) alikuwa ni mbora na mzuri kuliko wanadamu wote. Lau kama angekuwa muovu hangefaa kuwa mke wa Mtume ﷺ si katika sheria wala katika Qadari.' Na kwa kuzingatia hilo ndio Allah تعالى Anasema:

أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَ

"Hao wameepushwa na hayo wanayoyasema."

Maana yake: Wao wako mbali na wanayoyasema watu wazushi (*lffk*) na uadui.

لَهُمْ مَغْفِرَةٌ

"Wao watapata msamaha."

Maana yake: Kwa sababu ya uongo uliyosemwa dhidi yao (na kuwahuu wao).

وَرِزْقٌ كَرِيمٌ

"Na riziki ya ukarimu iliyo nzuri."

Maana yake: Mbele ya Allah تعالى katika Pepo ya Neema. Hii inamaanisha ahadi ya kuwa yeye atakuwa mke wa Mtume ﷺ Peponi.

¹ At-Tabari 19:143-144.

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْذِنُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا
 ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾ فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ
 يُؤْذَنَ لَكُمْ وَإِن قِيلَ لَكُمْ فَارْجِعُوا فَارْجِعُوا ۗ هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ
 ﴿٢٨﴾ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ فِيهَا مَتَعٌ لَّكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا
 تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ ﴿٢٩﴾

27. Enyi mlioamini! Msiingie nyumba zisizo nyumba zenu mpaka muombe ruhusa, na muatolee salamu wenyewe. Hayo ni bora kwenu mpate kukumbuka.

28. Na msipomkuta mtu humo basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa Rudini! Basi rudini. Hii ni takaso zaidi kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi mno wa mnayoyatenda.

29. Hata hivyo, si vibaya kwenu kuingia nyumba ambazo si maskani, lakini zina mahitaji yenu. Na Allah Anajua mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha.”

Kupiga hodi na adabu za kuingia majumbani

Hizi ni adabu za Kisheria ambazo Allah تعالیٰ Amewafundisha waja Wake Waumini na hiyo ni katika kutaka idhini. Amewaamrisha wasiwe ni wenye kuingia nyumba zisizokuwa zao mpaka kwanza waombe ruhusa, yaani watake idhini, kabla ya kuingia na baada yake watoe salamu.

Na inatakiwa mtu apige hodi mara tatu. Ikiwa ruhusa imetolewa ya kuingia, basi aingie, kinyume cha hivyo aende zake. Imethubutu katika Hadithi Sahihi kuwa Abu Musa Al - Ash'ariy رضي الله عنه alipiga hodi mara tatu kuingia nyumba ya 'Umar رضي الله عنه, hakuruhusiwa, hivyo akaondoka zake. Kisha 'Umar رضي الله عنه akasema: "Nilisikia sauti ya Abdullah ibn Qays رضي الله عنه akiomba kuingia? Mruhusuni aingie." Wakamfuata, lakini hawakumuona alikuwa ameshaondoka. Aliporudi baadae, 'Umar alisema: "Kwa nini uliondoka?" Akasema: "Mimi niliomba ruhusa mara tatu lakini sikupewa ruhusa, nami nimemsikia Mtume ﷺ anasema,

«إِذَا اسْتَأْذَنَ أَحَدُكُمْ ثَلَاثًا فَلَمْ يُؤْذَنَ لَهُ فَلْيَنْصِرْهُ»

“Mmoja wenu anapoomba ruhusa mara tatu na hakupewa idhini, basi aende zake.”

Akasema ‘Umar رضي الله عنه: “Utaniletea ushahidi juu ya haya au nitakuumiza kwa kipigo.” Aliondoka na kuendea kikundi cha Answaar kuwaeleza alivyosema ‘Umar رضي الله عنه. Wakamwambia: “Hatakutolea ushahidi isipokuwa aliye mdogo kabisa miongoni mwetu.” Hivyo, Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه alikwenda naye, naye akamweleza Umar رضي الله عنه kuhusu jambo hilo. ‘Umar رضي الله عنه akasema: “Sikupata kujifunza jambo hilo kutokana na kushughulika kwangu katika masoko.”¹ Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Anas رضي الله عنه au mwengine (ghairi yake) kuwa Mtume ﷺ aliomba ruhusa kuingia katika nyumba ya Said ibn Ubaadah رضي الله عنه naye akasema:

«السَّلَامُ عَلَيْكَ وَرَحْمَةُ اللَّهِ»

“As-Salaamu ‘Alayka wa Rahmatullaahi - Amani na Rehema ya Allah iwe juu yako.”

Sa’d رضي الله عنه naye akajibu: “Wa ‘Alaykas Salaam wa Rahmatullaahi – Na juu yako pia iwe amani na rehema”, Na Mtume ﷺ hakusikia jawabu hilo mpaka alipotoa salamu mara tatu na Sa’d رضي الله عنه naye ameijibu salamu hiyo mara tatu, lakini hakumsikilizisha Mtume (yaani Sa’d رضي الله عنه alikuwa akijibu kwa sauti ndogo). Hivyo, Mtume ﷺ akarudi, na Sa’d رضي الله عنه naye akamfuata na kusema: “Ewe Mtume wa Allah, babangu na mamangu wawe fidia kwako. Hakika salamu ulizotoa nimezijibu, lakini sikuwa nimekusikilizisha. Nilikuwa nataka kupata salamu zako nyingi zaidi na Baraka.” Baada ya hapo alimpa idhini kuingia na kumpa zabibu, Mtume ﷺ akala. Alipomaliza akasema:

«أَكَلْ طَعَامَكُمْ الْأَبْرَارُ، وَصَلَّتْ عَلَيْكُمْ الْمَلَائِكَةُ، وَأَنْظَرَ عَنْدَكُمْ الصَّائِمُونَ»

“Wamekula chakula chenu watu wema, na Malaika wamekutakieni rehema na wamefuturu kwenu waliofunga.”²

¹ Fat’hu-Albari 13:332.

² Ahmad 3:138.

Kisha ieleweke kuwa yule mwenye kutaka idhini asimame mbele ya mlango; anafaa asimame ama upande wa kulia au wa kushoto wa mlango, kwa sababu ya Hadithi iliyonukuliwa na Abu Daawuud kutoka kwa 'Abdullah ibnu Busr رضي الله عنه ambaye amesema: "Mtume ﷺ pindi alipokuwa akienda mlango kwa watu hauelekei mlango kwa uso wake, bali alikuwa akisimama ama kwa upande wake wa kulia au kushoto, na husema,

«السَّلَامُ عَلَيْكُمْ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ»

"As-Salaamu 'Alaykum, As-Salaamu 'Alaykum."

Hii ni kwa sababu ya kuwa wakati huo hakukuwa na mapazia. Hadithi hii imepokewa na Abu Dawuud peke yake.¹ Katika Sahihi mbili, imeripotiwa kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَوْ أَنَّ امْرَأًا اطَّلَعَ عَلَيْكَ بِغَيْرِ إِذْنٍ فَخَذَفْتَهُ بِحَصَاةٍ فَقَمَّاتٍ عَيْنَهُ، مَا كَانَ عَلَيْكَ مِنْ جُنَاحٍ»

*"Kama mtu akichungulia nyumbani mwako bila ya idhini, ukimrushia jiwe ukalipofua jicho lake haitakuwa dhambi juu yako."*²

Jama'ah wameripoti toka kwa Jaabir رضي الله عنه, amesema: "Nilikwenda nyumbani kwa Mtume ﷺ kuhusu deni la baba yangu (analodaiwa) na nikagonga mlango." Mtume ﷺ akauliza:

«مَنْ ذَا؟»

"Nani"

Nikajibu: "Mimi" Mtume ﷺ akasema:

«أَنَا أَنَا»

"Mimi, mimi"

Kana kwamba alichukizwa na jibu langu.³ Hakupendelea jambo hilo kwa sababu neno hili 'mimi' halimaanishi mhusika hadi ataje jina lake kwa uwazi kabisa

¹ Abu Dawuud 5:374.

² Fat'hu-Al- Bari 12:253 na Muslim 3:1699.

³ Fat'hu-Al- Bari 11:37 na Muslim 3:1697.

au jina la utani (*kuni-a*) ambalo ni maarufu kwake. Kila mmoja atajiita “mimi”, kwa hiyo hayatapatikana makusudio katika kutaka idhini ya kuingia, kama ilivyoamrisha katika Ayah. Al-Awf amepokea kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما, “*‘al- Istiinas’*- Kuondosha Woga ni kubisha hodi.” Hii pia ndiyo iliyokuwa rai ya wanazuoni wengine.¹ Imamu Ahmad ameripoti kutoka kwa Kaladah ibn Hanbal kuwa wakati wa kutekwa Makkah, Safwaan ibn Umayyah alimtuma kupeleka maziwa, ndama wa paa na matango, pale Mtume ﷺ alipokuwa mlimani. Alisema: “Niliingia kwa Mtume ﷺ bila ya kutoa salamu wala kuomba ruhusa ya kuingia. Mtume ﷺ aliniambia:

«ارْجِعْ نَفْسُكَ: السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَدْخُلْ؟»

“Rudi nje kisha uingie baada ya kusema As-Salaamu ‘Alaykum, je niingie?”

Hii ilikuwa baada ya Safwaan kusilimu.²

Hii pia imenukuliwa na Abu Dawuud, at-Tirmidhiy na an-Nasaa’iy, na at-Tirmidhiy amesema ni Hadithi *Hasan Ghariib*.³ Ibn Jurayj رحمه الله تعالى amesema kuwa alimsikia ‘Atwaa’ ibnu Rabaah akihadithia kuwa Ibnu ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Zipo Aya tatu ambazo wamezipinga (hukumu zake watu wanazipuuzza). Allah تعالى Anasema:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْوَكُمْ

“Hakika Mtukufu wenu zaidi ya mbele ya Allah ni Yule mcha Mungu wenu.” (49:13).

Lakini kwa sasa wanasema mtukufu wenu zaidi miongoni mwenu mbele ya Allah تعالى ni yule mkubwa zaidi wa nyumba. Ama kuhusu kubisha hodi, watu wameipinga kabisa. Nikamuuliza: “Je, niombe ruhusa kuingia kwa dada zangu mayatima ambao wanaishi nami nyumba moja?” Akasema: “Ndio”. Nikamtaka anipatie ruhusa akakataa katakata na kusema: “Je, unataka kuwaona wakiwa

¹ Abu Dawuud 5:374, *Tuhfat al-Ahwadhi* 7:491, an-Nasaa’iy katika *al-Kubraa* 6:90 na Ibn Majah 2:1222.

² Atw-Twabariy 19:146.

³ *Ad-Durr al-Manthuur* 6:176.

uchi?" Nikasema: "La". Akasema: "Basi omba idhini kuingia nyumbani (kwako)." Nikamuuliza tena, naye akasema: "Je, unataka kumtii Allah?" Nikasema: "Ndio". Akasema: "Hivyo, omba ruhusa".

Amesema Ibn Jurayj رحمه الله تعالى: "Ibnu Twaawuus alinipa khabari kuwa baba yake alimwambia: "Hapana mwanamke ambaye nachukia kumuona uchi wake kuliko maharimu yangu." Alishadidia sana katika jambo hili. Ibn Jurayj amehadithia kuwa az-Zuhriy amesema: "Nimemsikia Huzayl ibn Shurahbil al-Awdi Al-A'maa (akisema kuwa) amemsikia Ibn Mas'ud رضي الله عنه akisema: "Ni lazima muombe ruhusa kuingia katika nyumba za mama zenu". Ibn Jurayj amesema: "Nilimuuliza 'Atwaa': "Je, ni lazima mtu kuomba ruhusa anapotaka kuingia kwa mke wake?" Akasema: "La, na hili ifahamike kuwa si wajibu, lakini ni bora kwake kumjulisha kuwa anakuja ili asimshitue kwa sababu anaweza kuwa katika hali ambayo mke hataki mumewe amuone."

Abu Ja'far ibnu Jaarir رحمه الله تعالى amehadithia kutoka kwa mpwa wa kiume wa Zaynab, mke wa 'Abdullah ibn Mas'uud رضي الله عنه, kuwa Zaynab رضي الله عنها amesema: "Alipokuwa 'Abdullah akirudi kutoka kwenye shughuli zake, akiashiria kufika kwake nyumbani kwa kukohoa na kutema mate, kwa sababu hakupenda kuingia nyumbani mwake kwa ghafla na kutukuta sisi katika hali inayomchukiza." Isnadi yake ni sahihi.¹ Na amesema Muqatil ibn Hayyaan katika Kauli ya Allah تعالى:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْذِنُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا

"Enyi Mliamini! Msiingie nyumba zisizo nyumba zenu mpaka mwombe ruhusa, na muatolee salamu wenyewe."

Wakati wa ujahiliya, mtu alipokutana na rafiki yake, alikuwa hamsalimii kwa kumtolea salamu; bali alikuwa akisema: "Hiyyiita Swabaahan au Hiyyiita Masaa'an (sawa na habari za asubuhi na habari za jioni). Hii ndiyo salamu iliyokuwa ikitumika kati ya watu wakati huo. Hawakuomba ruhusa kuingia nyumba za wenziwao; mtu alikuwa akiingia ndani moja kwa moja na kusema: "Nimeingia ndani", na mfano wake. Hii lilikuwa ni jambo gumu kwa mtu kuvumilia, kwani anaweza kuwa na mkewe. Hivyo, Allah تعالى Alibadilisha yote hayo kwa kuamrisha kujifunika (kujisitiri) na ustahifu, na kuleta maamkizi

¹ Atw-Twabariy 19: 148.

mazuri yasiyokuwa na dosari au uchafu na dhambi yoyote. Akasema Aliyetukuka:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْذِنُوا وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا

“Enyi Mlioamini! Msiingie nyumba zisizo nyumba zenu mpaka muombe ruhusa, na muatolee salamu wenyewe.”¹

Haya aliyosema Muqatil ni Hasan. Na kwa hilo Akasema Aliyetukuka:

ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ

“Hilo ni kheri kwenu.”

Maana yake: Ya kutaka ruhusa ni bora kwenu kwa kuwa ni nzuri kwa pande zote mbili, kwa mwenye kutaka idhini na mwenye nyumba.

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾

“ili mpate kukumbuka.”

Na kwa Kauli Yake تعالى:

فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ

“Na msipomkuta yeyote basi msiingie mpaka mruhusiwe.”

Na hilo ni kwa vile ndani yake kuna kutumia uhuru na mipaka ya watu wengine bila ya idhini. Hivyo, akitaka, ataruhusu, na asipotaka hataruhusu.

وَإِن قِيلَ لَكُمْ آرْجِعُوا فَآرْجِعُوا ۗ هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ

“Na kama mkiambiwa ‘rudini’ basi hamna budi mrudi. Hii ni njia ya utakaso kwenu.”

Maana yake: Ikiwa mtarudishwa mlangoni, kabla ya kupatikana idhini, basi

¹Ad-Durr al-Manthuur 6:176.

فَارْجِعُوا^ط هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ

“Rudini’ basi hamna budi mrudi. Hii ni njia ya utakaso kwenu”.

Maana yake: Kurudi kwenu ni utakaso zaidi kwenu na usafi zaidi.

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٦﴾

“Na Allah Anajua mnayoyatenda”.

Amesema Qataadah: “Walisema baadhi ya Muhajirina: Hakika nimejaribu maisha yangu yote kuifuata Ayah hii, sijawahi kuomba ruhusa kuingia moja ya nyumba ya ndugu zangu akanitaka mimi nirudi, nikarudi hali ya kuwa nimechukia. Kwa sababu ya Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِنْ قِيلَ لَكُمْ آرْجِعُوا فَارْجِعُوا^ط هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ^ع وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٦﴾

“Na kama mkiambiwa ‘rudini’ basi hamna budi mrudi. Hii ni njia ya utakaso kwenu, Na Allah Anajua mnayoyatenda.”¹

Na amesema Said ibn Jubayr: Hii ina maana, msisimame kwenye milango ya watu. Na Kauli Yake تعالى:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ

“Hata hivyo, si vibaya kama mkiingia nyumba ambazo zisizokaliwa”.

Aya hii tukufu ni mahsusi zaidi kuliko ile iliyotangulia, kwa sababu inapelekea kujuzisha kuingia katika nyumba ambazo hazina ndani yake mtu yeyote. Kama kuna ndani yake mzigo wake, kama vile nyumba zinazotayarishwa kwa wageni, ikiwa atakuwa amepatiwa idhini mara ya kwanza, hivyo hiyo ruhusa inatosha. Amesema Ibn Jurayj, Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ

“Msiingie nyumba zisizo nyumba zenu”.

¹ Atw-Twabariy 19:150.

Kisha hukumu hii ilifutwa na ikaondoshwa na hukumu nyingine kwa kuzingatia hali fulani. Allah تعالى Amesema,

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ مَسْكُونَةٍ فِيهَا مَتَعٌ لَكُمْ

“Hata hivyo, si vibaya kama mkiingia nyumba ambazo zisizokaliwa, lakini zina mahitaji yenu”.

Hivyo ndivyo ilivyopokewa kutoka kwa ‘Ikrimah¹ na Hasan Al-Basriy.

قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ

بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٣٠﴾

30. “Ewe Mtume, waambie Waumini wanaume wainamisha macho yao (wadhibiti mitazamo yao), na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtambuzi zaidi wa wanayofanya”.

Amri ya kuinamisha macho

Hii ni Amri ya Allah تعالى kwa waja Wake Waumini kuinamisha macho yao kwa yaliyoharamishwa kwao. Hivyo wasitazame ila Aliyowahalalishia na wainamisha macho yao kwa yaliyoharamishwa. Lakini ikiangalia yaliyo haramishwa bila kukusudia, anatakiwa haraka ageuze uso wake. Hii ni kama alivyopokea Muslim katika Sahihi yake kutoka kwa Jariir ibn Abdullah Al-Bajaliy عنه رضي الله عنه ambaye anasema kuwa alimuuliza Mtume ﷺ: “Je, vipi nikitazama kwa ghafla?’ Mtume ﷺ aliniamuru kugeuza uso wangu au kuteremsha macho yangu.² Na katika Hadithi Sahihi kutoka kwa Abi Sa’iid عنه رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِيَّاكُمْ وَالْجُلُوسَ عَلَى الطَّرَقَاتِ»

“Jiepusheni kukaa barabarani”

Wakasema: “Ewe Mtume wa Allah, hatuna budi kukaa kwani huwa tunazungumza humo”. Mtume ﷺ akasema :

¹ Atw-Twabariy 19:153.

² Muslim 3:1699. Hii pia amepokea Ahmad, Abu Dawuud, at-Tirmidhiy na an-Nasaai.

«إِنَّ أَبِيئْتُمْ فَأَغَطُوا الطَّرِيقَ حَقَّهُ»

“Ikiwa hamuna budi kukaa basi ipeni barabara haki yake.”

Wakasema: “Na haki ya barabara ni ipi, ewe Mtume wa Allah?” Akasema:

«غَضُّ الْبُصْرِ، وَكَفُّ الْأَدَى، وَرَدُّ السَّلَامِ، وَالْأَمْرُ بِالْمَعْرُوفِ، وَالنَّهْيُ عَنِ الْمُنْكَرِ»

“Kuinamisha macho, na kuondosha uchafu, na kujibu salamu, na kuamrisha mema na kukataza maovu.”¹

Na imepokewa na Abul Qasim Al-Baghawiy kutoka kwa Abi Umamah رضي الله عنه ambaye amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«اَكْفُلُوا لِي سَيِّئًا أَكْفَلُ لَكُمْ بِالْجَنَّةِ: إِذَا حَدَّثَ أَحَدُكُمْ فَلَا يَكْذِبْ، وَإِذَا ائْتَمَنَ فَلَا يَخُنْ، وَإِذَا وَعَدَ فَلَا يُخْلِفْ، وَغَضُّوا أَبْصَارَكُمْ، وَكَفُّوا أَيْدِيَكُمْ، وَاحْفَظُوا فُرُوجَكُمْ»

“Nidhaminieni mambo sita, nami nitawadhaminia Pepo; Anapozungumza mmoja wenu asiongope; anapoaminiwa asikhini; anapoahidi asikhalifu; na inamisheni macho yenu; na izuilieni mikono yenu na zilindeni tupu zenu.”²

Na kwa kuwa kutazama kunaukurubisha moyo na maovu, Allah تعالی Aliamrisha kuhifadhi tupu kama Alivyoamrisha kuinamisha macho ambayo ni yenye kushawishi jambo hilo. Akasema Aliyetukuka:

«وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٥﴾»

“Na ambao tupu zao wanazilinda.” (23:5)

Wakati mwengine inakuwa ni kuihifadhi (tupu), kwa kutokuangalia, kama ilivyokuja katika Hadithi ya *Musnad Ahmad* na *Sunan*:

¹ Fat-h al-Baariy 5:134.

² *Taarikh al-Khatwiib* 7:392, at-Twabaraaniy katika *al-Mu'jam al-Kabiir*8: 314 na Ibn Hibaan katika *al-Majruuhim* 2:204. Isnadi yake ni dhaifu.

«اخْفِظْ عَوْرَتَكَ إِلَّا مِنْ زَوْجِكَ أَوْ مَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ»

“Hifadhi tupu yako isipokuwa kwa mkeo au kwa (wanawake) iliyowamiliki mikono yako ya kuume”.¹

ذَلِكَ أَرْكَىٰ هُمْ

“Hili ni takaso bora kwako.”

Maana yake: Ni takaso zaidi kwa nyoyo zao na ni safisho bora kwa Dini yao, kama ilivyosemwa: “Yeyote mwenye kuhifadhi macho yake, Allah Atamrithisha nuru katika uoni na fahamu yake”. Na pia imepokewa ‘katika moyo wake.’ Na kwa Kauli Yake تعالى:

إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٢٦﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtambuzi zaidi kamili wa yote wanayoyafanya.”

Kama pia Alivyosema تعالى:

يَعْلَمُ خَائِبَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ ﴿١٩﴾

“(Allah) Anajua khiyana ya macho na yanayoficha vifua.” (40:19)

Na katika Hadithi Sahihi kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كُتِبَ عَلَى ابْنِ آدَمَ حِفْظُهُ مِنَ الزَّوْنِ أَدْرَكَ ذَلِكَ لَا مَحَالَةَ، فَرْنَا الْعَيْنَيْنِ النَّظْرُ، وَرْنَا اللِّسَانَ النَّطْقُ، وَرْنَا الْأَذُنَيْنِ الْأَسْتِمَاعُ، وَرْنَا الْيَدَيْنِ الْبَطْشُ، وَرْنَا الرُّجْلَيْنِ الْخُطَى، وَالتَّقْسُ تَمَّتْ وَتَشْتَبِي، وَالْفَرْجُ يُصَدَّقُ ذَلِكَ أَوْ يُكَذَّبُهُ»

“Mwanadamu ameandikiwa hisa yake katika zinaa, na atalipata hilo bila pingamizi lolote. Zinaa ya macho mawili ni kutazama, zinaa ya ulimi ni mazungumzo, na zinaa ya masikio ni kusikiliza, na zinaa

¹ Ahmad 5:3, Abu Dawuud 4:303, at-Tirmidhiy 8:53, an-Nasaa’iy katika *al-Kubraa* 5:313 na Ibn Maajah 1:618.

ya mikono miwili ni kushika, na zinaa ya miguu miwili ni kutembea, na nafsi inatamani na inataka. Na tupu aidha inaliswadikisha hilo au inalikanusha”.

Imepokewa na Bukhaari kwa Isnadi isiyokamilika.¹ Na Muslim pia amenukuu Hadithi kama hii kwa Isnadi tofauti.² Na hakika *Salaf* wengi wamesema: “Walikuwa wakiwakataza wanaume kuwatizama kwa kuwakazia macho na kwa matamano, vijana wazuri wasiokuwa na ndevu.” Ibn Abi Dunia رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Abuu Huraira عنه رضي الله امesema, Mtume ﷺ amesema:

«كُلُّ عَيْنٍ بَاكِئَةٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِلَّا عَيْنًا غَضَّتْ عَنْ مَحَارِمِ اللَّهِ، وَعَيْنًا سَهَرَتْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَعَيْنًا يَخْرُجُ مِنْهَا مِثْلُ رَأْسِ الذَّبَابِ مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Kila jicho la Mtu litalia siku ya Kiyama, isipokuwa jicho lilojizua kutazama yaliyoharamishwa na Allah تعالى. Au jicho lililokeshwa katika Dini ya Allah na jicho linalotoka machozi mithili ya kichwa cha nzi kutokana na kumuogopa Allah تعالى.”³

* * *

¹ Fath al-Baariy 11:28.

² Muslim 4:2047.

³ Al-Firdausi cha Addailimi 3:256 na Adduru Al-Manthuru 6:187 Isnadi yake ni dhaifu.

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ
 وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۗ وَلْيَضْرِبْنَ خُمُرِهِنَّ
 عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ ۗ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ
 آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاؤِ
 بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي أَخَوَاتِهِنَّ
 أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوِ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولِي
 الْإِرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا عَلَىٰ
 عَوْرَتِ النِّسَاءِ ۗ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِنَ
 زِينَتِهِنَّ ۗ وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ
 تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾ وَأَنْكِحُوا الْأَيْمَىٰ مِنْكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ
 عِبَادِكُمْ وَإِمَائِكُمْ ۚ إِنْ يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ
 ۗ وَاللَّهُ وَسِعَ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾ وَلَيْسَتَعَفِيفِ الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا
 حَتَّىٰ يُغْنِيَهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَالَّذِينَ يَبْتِغُونَ الْكِتَابَ بِمَا
 مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا ۗ وَءَاتُوهُمْ
 مِنْ مَالِ اللَّهِ الَّذِي ءَاتَاكُمْ ۗ وَلَا تَكْرِهُوا فَتِيهَتِكُمْ عَلَىٰ الْبِغَاءِ
 إِنْ أَرَدْنَ تَحَصُّنًا لِيَبْتِغُوا عَرَضَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَمَنْ يَكْرِهُنَّ
 فَإِنَّ اللَّهَ مِنْ بَعْدِ إِكْرَاهِهِنَّ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٣﴾ وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا
 إِلَيْكُمْ ءَايَاتٍ مُبَيِّنَاتٍ وَمَثَلًا لِمَنِ الَّذِينَ حَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ
 وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٣٤﴾

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ
 أَبْصَرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا
 يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۗ
 وَلْيَضْرِبْنَ خُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ ۗ وَلَا
 يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ
 آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ
 أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاؤِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ
 إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي
 أَخَوَاتِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ
 أَيْمَانُهُنَّ أَوِ التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولِي
 الْإِرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ
 الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا عَلَىٰ عَوْرَتِ
 النِّسَاءِ ۗ وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ
 مَا يُخْفِينَ مِنَ زِينَتِهِنَّ ۗ وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ
 جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ
 تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾

31. "Na ewe Mtume,
 waambie Waumini wana-
 wake wainamishe macho
 yao, na wazilinde tupu zao,
 wala wasioneshe mapambo
 yao isipokuwa yale yanayo-

dhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasioneshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao wa kiume, au watoto wa waume zao wa kiume, au kaka zao, au wana wa kiume wa kaka zao, au wana wa kiume wa dada zao, au wanawake wenzao, au wale inayomiliki mikono yao ya kuume, au watumishi wanaume wasio na matamano, au watoto ambao bado hawajajua mambo yanayohusu uke. Wala wasipige chini miguu yao ili yajulikane wanayoyaficha. Na tubuni nyote kwa Allah, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa.”

Hukumu za Hijabu

Hii ni Amri kutoka kwa Allah تعالى kwa Waumini wanawake, na kwa Ghera yake (ule wivu) kwa waja Wake Waumini. Hii pia ni kuwatofautisha wanawake Waumini na zile sifa za wanawake wa zama za Ujahiliya na matendo ya wanawake washirikina. Na ilikuwa sababu ya kuteremshwa Aya hii ni maelezo aliyotaja Muqatil ibn Hayyan, pale aliposema: “Imetufikia sisi – na Allah تعالى Anajua zaidi – kuwa Jaabir ibn ‘Abdullah Ibn Al-Answaariy alihadithia kuwa Asmaa’ bint Murshidah رضي الله عنها alikuwa ndani ya nyumba yake katika mtaa wa Bani Haarithah. Na wanawake wakawa wanakwenda kwake bila ya izari (nguo ya chini kama kikoi), kukadhihiri yaliyo miguuni mwao, pamoja na vifua vyao na shungi za nywele zao za mbele. Akasema Asmaa’: “Ni uovu ulioje huu”. Baada ya hapo Allah تعالى Akateremsha:

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ

“Na ewe Mtume, waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao.”¹

Na Kauli Yake تعالى:

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ

“Na ewe Mtume, waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao.”

¹ Bukhari 4:454 na At-Tabari 19:154.

Maana yake: Kwa yale ambayo Allah تعالى Amewaharamisha kutizama, mbali na waume zao. Baadhi ya wanazuoni wanasema kuwa inaruhusiwa kwa wanawake kuwatizama wanaume *ajnabi* (wasio maharimu zao) bila ya matamano yoyote, kama ilivyonukuliwa katika Hadithi Sahihi. Mtume wa Allah alitizama michezo ya kutumia mikuki ya Wahabeshi ndani ya Msikiti siku ya Idi, na Mama wa Waumini, Aishah رضي الله عنها alikuwa akiwatizama nyuma ya mgongo wake, naye alikuwa akimsitiri asionekane nao mpaka akachoka na kwenda zake.¹ Na Kauli Yake تعالى:

وَمَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ

“Na wazilinde tupu zao”.

Amesema Sa’iid ibn Jubayr: “Kutokana na matendo machafu.” Na amesema Abul ‘Aliyah: “Kila Aya iliyoteremka katika Qur’ani ambayo inatajwa kuzilinda tupu inamaanisha zinaa isipokuwa Aya hii,

وَمَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ

“Na wazilinde tupu zao”.

“Kuilinda isionekane na yeyote”.² Na Kauli Yake تعالى:

وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا

“Wala wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa ambayo yamedhihirika katika hayo”.

Maana yake: Wasidhihirishe chochote katika mapambo kwa wanaume wasiokuwa maharimu zao ila kwa yasiyowezekana kufichika. Ibn Mas’ud رضي الله عنه amesema: “Kama mtandio (vazi la nje) na nguo”,³ akimaanisha mavazi yaliyokuwa yakitumiwa na wanawake wa Kiarabu ikichanganya ile nguo (ya nje) iliyokuwa ikifunika nguo zao na chochote kinachoonekana chini ya nguo hiyo ya nje. Hapana kosa kwa hili, kwa sababu hiki ni kitu ambacho hakiwezi kufichika. Na mfano wake katika mapambo ya wanawake ni kile

¹ Al-Bukhari 454 n.k.

² At-Twabariy 19:154.

³ At-Twabariy 19:156.

kinachodhihirika chini ya kikoi chake na hakifichiki. Na wale waliosema kama alivyosema Ibn Mas'ud رضي الله عنه ni Al-Hasan, Ibn Siirin, Abu Al-Jawzaa', Ibn An-Nakha'iy na wengineo.¹ Na Kauli Yake تعالى:

وَلْيَضْرِبَنَّ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ

“Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao.”

Maana yake: Wanatakiwa wavae majuba yenye kufunika vifua na mbavu ili watofautiane na wanawake wa Kijahiliya, ambao hawakufanya hivyo. Bali walikuwa wakipita mbele ya wanaume vifua vyao na shingo zao vikiwa wazi kabisa havifunikwi na chochote, na hali pia shungi za mbele za nywele, nywele na vipuli vikiwa wazi kabisa. Hivyo, Allah تعالى Aliwaamrisha Waumini wanawake kujifunika (kujistiri), kama Alivyosema:

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلٌّ لِّأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْرِكُنَّ عَلَىٰ مِّنْ جَلْبَيْبِهِنَّ^٤ ذَٰلِكَ
أَدَّتْ أَنْ يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذِنَنَّ^٥

“Ewe Mtume! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake Waumini (wengine), wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo ni kwenye kupelekea zaidi wajulikane (kuwa ni watu wa hishima ili) wasiudhiwe”. (33: 59).

Na Amesema katika Aya hii tukufu:

وَلْيَضْرِبَنَّ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ

“Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao.”

Na *Khumur* ni wingi wa *Khimaar*, nacho ni kitu kinachofunika, yaani kinachotumika kufunika kichwa. Nacho ni kile kinachofunikiwa kichwa, na hii ndio watu wanayoita shungi. Amesema Said ibn Jabayr:

وَلْيَضْرِبَنَّ

‘Na waangushe’. Inamaanisha kukivuta pande zote na kukikaza barabara.

¹ At-Twabariy 19:156.

يُخْمَرِينَ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ

“Shungi zao juu ya vifua vyao.”

Inamaanisha juu ya shingo zao na vifua vyao ili kisionekane kitu chake chochote.¹ Amepokea Bukhaari kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kwamba amesema: “Allah Awarehemu wanawake wa Muhajirina wa mwanzo pale Allah Alipowateremshia Aya hii:

وَلْيَضْرِبْنَ يُخْمَرِينَ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ

“Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao.”

Walichana nguo zao na wakajifunika nazo². Na pia imepokewa kwa Swafiyah bint Shaybah kuwa ‘Aa’ishah رضي الله عنها alikuwa akisema: “Ilipoteremka aya hii,

وَلْيَضْرِبْنَ يُخْمَرِينَ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ

“Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao.”

Walichukua - vikoi vyao na kuvikata pembezoni mwake na wakajifunika nazo³. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ
أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ

“Wala wasioneshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao wa kiume, au watoto wa waume zao wa kiume, au kaka zao, au wana wa kiume wa kaka zao, au wana wa kiume wa dada zao.”

Wote hao ni jamaa wa karibu mwanamke wasioweza kumuoa (yaani, maharimu zake) na hivyo anaruhusiwa kuonesha mapambo yake kwao, bila ya kuvuka na kujifunua ovyo ovyo. Ibn al-Mundhir amehadithia kuwa ‘Ikrimah alielezea yafuatayo kuhusu Aya hii,

¹ Ad-Durr al-Manthuur 6:182.

² Fat-h al-Baariy 8: 347.

³ Fat-h al-Baariy 8: 347.

وَلَا يُعْدِلُونَ إِلَّا لِبُعُولَتِهِمْ أَوْ لِأَبَائِهِمْ أَوْ لِأُمَّهَاتِهِمْ

“Wala wasioneshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba za waume zao...”

Hadi akamaliza Aya hii. Hapa hakutajwa ami (ndugu wa baba) wala mjomba, kwa sababu wanaweza kuwasifia watoto wao wa kiume, hivyo mwanamke hafai kuvua shungi yake (*Khimaar*) yake mbele yao (ami na mjomba).¹ Ama kuhusu mume wake, yote haya ni kwa ajili yake, hivyo anatakiwa ajitahidi upeo wa uwezo wake kujipamba, tofauti na anavyotakiwa mbele ya wengine. Na Kauli Yake Allah تعالى:

أَوْ نِسَائِهِمْ

“Au wanawake wenzao.”

Maana yake: Pia anaweza kuvaa mapambo yake mbele ya wanawake wenzake Waislamu na wasio Waislamu - wanawake wa *Ahli Dhimmah* (wasiokuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu) japokuwa hili la kuwasifia wanaume zao uzuri wa wanawake wa Kiislamu limekatazwa kwa wanawake wote wasio Waislamu, lakini hasa hasa zaidi kwa wanawake wa *Ahl adh-Dhimmah*, kwa sababu hakuna kinachowazuia kufanya hivyo, ama wanawake Waislamu wanafahamu ya kuwa jambo hilo ni haramu na hivyo litawaepusha wao kutenda hilo. Na hakika Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَبَايِرِ الْمَرْأَةَ الْمَرْأَةَ فَتَنْتَعِبَهَا لِرُؤُوسِهَا كَأَنَّهُ يَنْظُرُ إِلَيْهَا»

“Mke asitoe wasifu wa mwanamke mwengine kwa mumewe kana kwamba mume wake anamwalia.”

Hadithi hii wameinukuu katika Sahihi mbili kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه².

أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ

“Au wale iliowamiliki mikono yao ya kuume.”

¹ Ibn Abii Shaiba 4:338.

² Fat-hul Al-bari 9:250.

Ibnu Jariir رحمه الله تعالى amesema: “Hii inamaanisha miongoni mwa wanawake washirikina, hivyo inajuzu kudhihirisha mapambo yake hata akiwa mbele ya mjakazi wake mshirikina mwanamke kwani huyo ni kijakazi chake”.¹ Hii ndiyo iliokuwa rai ya Sa’iid ibn Al-Musayyab.² Na Kauli Yake Allah تعالى:

أَوِ الشَّعْبِ غَيْرِ أُولَى الْأَرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ

“Au watumishi wanaume wasio na matamano.”

Hawa ni kama watumishi walioajiriwa na wategemizi wengine ambao hawapo daraja moja katika hadhi na mwanamke, pamoja na hayo wana akili zao na hawana matamano ya wanawake. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Huyu ni aina ya mtu punguani ambaye hana matamano (ya wanawake)”.³ Na amesema ‘Ikrimah: “Huyu ni *hanithi* ambaye uume wake hausimami”. Na hivyo hivyo wamesema zaidi ya mmoja miongoni mwa *Salaf*. Katika Hadithi Sahihi kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa *hanithi* mmoja alikuwa akiingia nyumba za wakeze Mtume ﷺ. Walikuwa wakimhesabu asiye na matamano, Mtume ﷺ akaingia alipokuwa akimsifia mwanamke fulani akisema: “Kwa mbele ana mikunjo mine na kwa nyuma ana mikunjo nane”. Mtume ﷺ akasema,

«أَلَا أَرَى هَذَا يَنْعَلُ مَا هَهُنَا لَا يَدْخُلَنَّ عَلَيْكُمْ»

“Huyu anayajua yanayojiri humu ndani, na asiingie kwenu.”

Alimtoa, hivyo akakaa Majangwani Baydaa’ na alikuwa akiingia siku ya Ijumaa kuchukua chakula.⁴ Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا عَلَى عَوْرَتِ النِّسَاءِ

“Au wale wavulana wadogo ambao bado hawajajua mambo yanayohusu uke.”

¹ Atw-Twabariy 19:160.

² Ad-Durr al-Manthuur 6:183.

³ Atw-Twabariy 19:161.

⁴ Muslim 4: 1715, 1716, Ahmad 6:152, An-Nasaa’iy katika *al-Kubraa* 5:395 na Abu Daudi 6:152.

Maana yake: Wao ni wadogo kwa udogo wao hawafahamu hali za wanawake, uchi wao au mazungumzo yao laini au uzuri wa ulegevu wao katika kutembea na harakati zao na utulivu wao. Ikiwa mtoto ni mdogo hajui hayo, hakuna ubaya kwake, lakini akiwa amebaleghe au karibu na kubaleghe, hufahamu hayo, na anaweza kutofautisha baina ya mrembo huyo anakuwa hafai kuingia kwa wanawake (*haso Aj-nabi.*) Imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِيَّاكُمْ وَالذُّخُولَ عَلَى النِّسَاءِ»

“Jiepusheni na kuingia kwa wanawake”.

Pakasemwa: “Ewe Mtume wa Allah! Unamuonaje shemeji?” Akasema:

«الْحَمْرُ: التَّمَوْتُ»

“Shemeji (wa kiume) ni mauti”¹

Adabu za wanawake kutembea barabarani

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ

“Wala wasipige chini miguu yao”.

Wanawake katika zama za jahiliya walikuwa wanapotembea barabarani huku wamevaa vikuku ambavyo sauti zake hazisikiki, walikuwa wakipiga miguu yao chini ili sauti za vikuku hivyo zisikike na wanaume vikilia. Allah تعالى Akawakataza Waumini wanawake kufanya hivyo. Hivyo hivyo, wanawake wamekatazwa kutembea kwa jinsi itakayoonesha yaliyofinikwa. Kwa hivyo sababu Allah تعالى Anasema:

وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ

“Wala wasipige chini miguu yao.”

Mpaka mwisho wa Aya.

¹ Atw-Twabariy 19:161.

² Muslim 4:1715, 1716, Ahmad 6:152, An-Nasaa'iy katika *al-Kubraa* 5:395 na Abu Daudi 6:152.

Kutokana na hayo, mwanamke amekatazwa kutia manukato na uturi atokapo nyumbani kwake, hivyo wanaume kupata harufu ya manukato yao. Abu 'Isaa At-Tirmidhi amenukuu kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كُلُّ عَيْنٍ زَانِيَةٌ، وَالْمَرْأَةُ إِذَا اسْتَعْطَرَتْ فَمَرَّتْ بِالْمَجْلِسِ فَيَبِي كَذَا وَكَذَا»

“Kila jicho ni lenye kuzini, na mwanamke anapojipaka manukato na akapita kikao cha watu, basi yeye ni kadha wa kadha”.

Akasema: “Na ipo Hadithi kama hii kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه”. Na hii iliyopokewa katika mlango huu ni Hasan Sahih.² Pia imepokewa na Abu Dawud na An-Nasa'iy.³ Na katika hilo pia, wanawake wanakatazwa kutembea kati kati ya barabara, kwa sababu hii inahusisha kujifunua ovyo.

Abu Dawud amepokea kutoka kwa Abi Ubayd Al-Answaariy رضي الله عنه kuwa amemsikia Mtume ﷺ akisema pale alipokuwa nje ya Msikiti na kuwakuta wanaume na wanawake wamechanganyika. Aliwaambia wanawake:

«اسْتَأْخِرْنَ فَإِنَّهُ لَيْسَ لَكُنَّ أَنْ تَحْفُقْنَ الطَّرِيقَ، عَلَيْكُنَّ بِحَافَاتِ الطَّرِيقِ»

‘Kaeni nyuma, kwani nyinyi hamna haki ya kutembea katikati ya barabara. Ni juu yenu kutembea pembezoni mwa barabara.’

Kwa mnasaba wa amri hii mwanamke alikuwa akijiambatanisha na ukuta kwa kiasi ambacho nguo zilikuwa zikishika kwenye ukuta.⁴

﴿وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُتُوبُونَ لَمَّا كَرُفُلِحْتُمْ﴾

“Na tubuni nyote kwa Allah, enyi Waumini, ili mpate kufaulu.”

Hii maana yake, fanyeni sifa hizi nzuri na tabia tukufu alizokuamrisheni, na acheni waliyokuwa nayo majahili katika tabia na sifa chafu. Kwani kufaulu

¹ Fat-h al-Baariy 5:242 na Muslim 4: 1711.

² Tuhfat al-Ahwadhi 8:70.

³ Abu Daawuud 4:400 na An-Nasaa'iy 8:153.

⁴ Abu Daawuud 5:422. Hii ni Hadithi dhaifu, lakini zipo Hadithi nyengine kuunga mkono maana ya Hadithi ambayo inaiainisha kuwa *Hasan*.

kote ni katika kufanya Aliyoamrisha Allah رضي الله عنه na Mtume Wake ﷺ na kuacha aliyokataza, na Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuombwa msaada.

وَأَنْكِحُوا الْأَيْمَىٰ مِنْكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَإِمَائِكُمْ ۚ إِنْ يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٣١﴾ وَلَيْسَتَعَفِيفِ الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا حَتَّىٰ يُغْنِيَهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَالَّذِينَ يَبْتِغُونَ الْكِتَابَ مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا ۗ وَآتُوهُمْ مِّنْ مَّالِ اللَّهِ الَّذِي آتَاكُمْ ۚ وَلَا تَكْرَهُوا فَتَيِّبْتِكُمْ عَلَىٰ الْبِغَاءِ إِنْ أَرَدْنَ تَحَصُّنًا لِّتَبْتَغُوا عَرَضَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَمَنْ يُكْرِهِنَّ فَإِنَّ اللَّهَ مِنْ بَعْدِ إِكْرَاهِهِنَّ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣٢﴾ وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ آيَاتٍ مُّبَيِّنَاتٍ وَمَثَلًا لِّمَنِ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٣٣﴾

32. Na waozeni wajane miongoni mwenu na wema katika watumwa wenu na wajakazi wenu. Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu Atawatajirisha kwa Fadhila Yake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa Mwenye Kujua.

33. Na wajizuilie na machafu wale wasiopata cha kuolea, mpaka Mwenyezi Mungu Awatajirisha kwa Fadhila Yake. Na wanaotaka kuandikiwa uhuru katika wale amabo mikono yenu ya kulia imewamiliki, basi waandikieni kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu Aliyokupeni. Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya zinaa kwa ajili ya kutafuta pato la maisha ya dunia, ilhali wao wanataka kujihishimu. Na atakayewalazimisha basi Mwenyezi Mungu baada ya kulazimishwa kwao huko, Atawasamehe, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

34. Na kwa yakini Tumekuteremshieni Ishara zilizo wazi na mifano kutokana na waliotangulia kabla yenu na mawaidha kwa wachamungu.

Amri ya kuoa

Ayah hizi tukufu zilizo wazi kabisa zimekusanya jumla ya hukumu madhubuti na amri imara kabisa. Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَنكِحُوا الْأَيْمَىٰ مِنكُمْ

“Na waozeni wajane miongoni mwenu (waungwana)....”

Hii ni Amri ya kuoa. Na amesema Mtume ﷺ:

يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ، مَنِ اسْتَطَاعَ مِنكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ، فَإِنَّهُ أَغْضَىٰ لِلْبَصْرِ وَأَحْصَنُ
لِلْفَرْجِ، وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالصُّومِ فَإِنَّهُ لَهُ وَجَاءٌ،

“Enyi kongamano la vijana! Mwenye kuweza miongoni mwenu kuoa, na aoe, kwani hii ni yenye kufumbisha zaidi jicho na kuhifadhi zaidi tupu. Na asiyeweza ni juu yake kufunga, kwani hiyo ni kinga kwake (katika kuidhibiti nafsi yake)”.

Imenukuliwa katika Sahihi Mbili kutoka kwa Hadithi ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه.¹ Na imekuja katika Sunah kwa njia zaidi ya moja kuwa Mtume ﷺ amesema:

تَزَوَّجُوا تَوَالِدُوا تَتَأَمَّلُوا فَإِنِّي مَبَاهٍ بِكُمْ الْأَمَمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

*“Oeni muzaane (kwa wingi) na mulete dhuria, kwani mimi nitajifakhiri nanyi juu ya Ummah mwingine Siku ya Kiyama”.*²

Neno “Al-Ayaamaa” ni wingi wa Ayyim, na husemwa hivyo kwa maana ya mwanamke mjane ambaye hana mume na mume mjane ambaye hana mke, sawa alikuwa ameoa kisha akaachana au hajaoa. Amezungumza haya Al-Jawhariy kutoka kwa wanazuoni wa lugha (ya kiarabu). Hutamkwa mwanamume Ayyim na mwanamke Ayyim (sifa hii inatumika kwa mwanamume na mwanamke).

¹ Fat-h al-Baariy 9:14 na Muslim 2:1019.

² Hatujapata lafudhi hii ya Hadithi, na hakika imepokewa na Abu Dawud na An-Nasa'iy kwa lafudhi iliyo karibu na hii.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنْ يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu Atawatajirisha kwa Fadhila Zake”.

Amesema ‘Aliy ibn Twalhah kuwa kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Allah تعالى Amewahimiza kuo na Akawaamuru waungwana na watumwa na Akawaahidi kuwatajirisha”¹. Akasema:

إِنْ يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu Atawatajirisha kwa Fadhila Zake”.

Na imepokewa na Ibn Mas‘ud رضي الله عنهما alisema: ‘Tafuteni utajiri kwa kuo, kwani Allah تعالى Amesema:

إِنْ يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Wakiwa mafakiri Mwenyezi Mungu Atawatajirisha kwa Fadhila Zake”.

Imepokewa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى.² Na ametaja Al-Baghawiy mfano wa maneno haya kutoka kwa ‘Umar رضي الله عنه.³ Na amenukuu Al - Layth kutoka kwa Muhammad ibn ‘Ajlaan kutoka kwa Said Al-Maqburiy kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«ثَلَاثَةٌ حَقَّ عَلَى اللَّهِ عَزْوُهُمْ: التَّائِبُ يُرِيدُ الْعَفَاةَ، وَالْمُكَاتِبُ يُرِيدُ الْأَدَاءَ، وَالنَّازِي فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Watu watatu ni haki kwa Allah Kuwasaidia: Mwenye kuo ili ajihifadhi: mtumwa anayetaka mkataba na bwana wake kwa lengo la kununua uhuru wake; na mwenye kupigana katika njia ya Allah”.

¹ Atw-Twabariy 19:166.

² Atw-Twabariy 19:166.

³ Al-Baghawiy 3:342.

Hii Hadithi ameipokea Imamu Ahmad, At-Tirmidhiy, An-Nasa'iy na Ibn Maajah.¹

Mtume ﷺ alimwozesha mtu ambaye hakuwa na chochote isipokuwa shuka (izari) yake na hakuweza hata kununua pete ya chuma.

Pamoja na hayo alimwozesha mwanamke, na akajaalia mahari yake kumfundisha mkewe alichohifadhi katika Qur'ani. Na inajulikana kuwa kwa ukarimu wa Allah تعالى na Huruma Yake Aliwaruzuku wao wawili kwa kile kilichowatosheleza mahitaji yao.

Amri ya kujizuilia (na machafu) ikiwa hana uwezo wa kuoa

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَيْسَتَعْفِيفِ الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا حَتَّى يُغْنِيَهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Na wajizuilie na machafu wale wasiokuwa na cha kuolea, mpaka Mwenyezi Mungu Awatajirishe kwa Fadhila Zake”.

Hii ni Amri kutoka kwa Allah تعالى kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kuoa kwa kujichunga na haramu, kama alivyosema Mtume ﷺ:

يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ مَنِ اسْتَطَاعَ مِنْكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ فَإِنَّهُ أَغْضُ لِلْبَصْرِ وَأَخْصَنُ لِلْفَرْجِ، وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالْصَّوْمِ فَإِنَّهُ لَهُ وَجَاءٌ

*“Enyi kongamano la vijana! Mwenye kuweza miongoni mwenu kuoa, basi na aoe, kwani hii ni yenye kufumbisha zaidi jicho na kuhifadhi zaidi tupu. Na asiyeweza basi ni juu yeke kufunga, kwani hiyo ni kinga kwake (katika kuidhibiti nafsi yake)”.*²

Aya hii ina maana ya kiujumla, na Aya katika Suratun Nisaa' ni mahususi, kwa Kauli ya Aliyetukuka:

¹ Ahmad 2:251, Tufhat Al-Ahwadh 5:296, An-Nasaa'iy 6:61 na Ibn Maajah 2:841.

² Fat'h al-Baariy 9: 14.

وَمَنْ لَّمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ طَوْلًا أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ

“Na asiyeweza katika nyie kupata mali ya kuo a wanawake waungwana Waumini...”

Mpaka Kauli Yake,

وَأَنْ تَصْبِرُوا خَيْرٌ لَكُمْ

“... Na mkisubiri (msiwaoe mpaka mpate fedha za kuo a muungwana) ndio bora kwenu...” (4:25).

Hii inamaanisha ni bora kwenu kusubiri na kuacha kuo a kijakazi, kwa sababu mtoto atakayezaliwa atakuwa pia ni mtumwa. Na jueni kuwa,

وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Na Allah ni Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Kurehemu”.

Amesema ‘Ikrimah kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَلَيْسَتَعَفِيفِ الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا

“Na wajizuilie na machafu wale wasiokuwa na cha kuolea”.

Kuwa ni mtu aliyemuona mwanamke na akawa anahisi matamanio (anamtaka yule mwanamke); ikiwa ana mke basi aende kwa mkewe ili kukidhi haja yake na ikiwa hana mke, basi atafakari juu ya ule Ufalme wa mbingu na ardhi mpaka Allah تعالى Ampe njia ya maisha yake (Amtajirishhe).

Amri ya kuandikiana mkataba na watumwa ili wapate uhuru wao

Kauli Yake Aliyetukuka:

وَالَّذِينَ يَبْتِغُونَ الْكِتَابَ مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا

“Na wanaotaka kuandikiwa uhuru katika wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki, basi andikianeni kama mkiona wema kwao”.

¹ Fat’h al-Baariy 9: 14.

Hii ni Amri kutoka kwa Allah Aliyetukuka kwa mabwana (wenye kumiliki watumwa) ikiwa watumwa wametaka kutoka kwao kuandikiana ili wanunue uhuru wao, hivyo waandikiane ikiwa mtumwa ana ujuzi na pato ambalo kwalo atampatia bwana wake mali ambayo ameandikiana nae kuyalipa. Amesema Bukhari: Amehadithia Rawh kutoka kwa Ibn Jurayj: “Nilimuuliza ‘Atwaa’, “Je, nikijua kuwa mtumwa wangu ana mali inakuwa wajibu kwangu kuandika mkataba naye ili anunue uhuru wake?” Akasema: “Sifikirii kuwa kitu chengine chochote isipokuwa ni wajibu”. ‘Amr ibn Dinaar alisema: “Nilimwambia ‘Atwaa’, “Je, umehadithia haya kutoka kwa yeyote?” Akasema: “Hapana”. Kisha akaniambia kuwa Musa ibn Anas alimwambia kuwa Siiriin, ambaye alikuwa tajiri, alimuomba Anas waandikiane (ili apate uhuru wake), naye akakataa. Hivyo, alikwenda kwa ‘Umar ibn al-Khatwtwaab رضي الله عنه’ ambaye alisema: “Mwandikie”. Na hata hivyo Anas رضي الله عنه Alikataa, hapo ‘Umar رضي الله عنه alimpiga mjeledi wake na akasoma,

فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا

“Basi andikianeni kama mkiona wema kwao.”

Hapo akaandikiana naye mkataba. Hii imetajwa na Bukhari kwa Isnadi isiyokamilika (*Muallaq*).¹ Pia imenukuliwa na ‘Abdur-Razzaaq ambaye amesema Ibn Jurayj aliwaambia: Nilimuuliza ‘Atwaa’, “Je, nikijua kuwa mtumwa wangu ana mali inakuwa wajibu kwangu kuandika mkataba naye ili anunue uhuru wake?” Akasema: “Sifikirii kuwa ni kitu chengine chochote isipokuwa ni wajibu”² Na amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Anas ibn Maalik رضي الله عنه kuwa Siiriin alitaka kununua uhuru wake, naye akachelewa katika hilo, baadae ‘Umar رضي الله عنه alimwambia: “Ni lazima kwako umwandikie mkataba wa uhuru wake”. Isnadi yake ni Sahihi.³

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا

“Kama mkiona wema kwao.”

¹ Fat-h al-Baariy 5:219.

² Abdur-Razzaaq 8:371.

³ Atw-Twabariy 19:167.

Wamesema baadhi yao (wanazuoni) kuwa hii inamaanisha uaminifu. Na wengine wakasema kuwa ni ukweli. Na wengine wakasema huo ni uwezo wa mali. Na wengine wakasema ni werevu na uwezo wa kuchuma pato. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَتَوْهُمْ مِّن مَّالِ اللَّهِ الَّذِي آتَاكُمْ

“Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu Aliyokupeni.”

Hii ni ile sehemu ya Zakah ambayo Allah تعالى Amefaradhisha kuwa haki yao. Hii ni rai ya Al-Hasan, Abdur-Rahmaan Ibn Zayd ibn Aslam na baba yake na Muqaatil ibn Hayyaan. Na hii pia ni rai aliyoichagua Ibnu Jariir رحمه الله تعالى¹. Na amesema Ibrahim An-Nakha'iy katika Kauli ya Allah تعالى:

وَأَتَوْهُمْ مِّن مَّالِ اللَّهِ الَّذِي آتَاكُمْ

“Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu Aliyokupeni.”

“Amewahimiza watu juu yao, bwana wake na watu wengine”. Na rai hiyo ndiyo ya Buraydah Ibn Al-Huswayb Al-Aslamiy na Qataadah. Na amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: “Allah تعالى Amewaamuru Waumini kusaidia katika kuacha huru watumwa.”

Kukataza kuwalizimisha vijakazi kuzini

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَا تُكْرَهُوا فَتَيَاتِكُمْ عَلَى الْبِغَاءِ

“Wala msiwashurutisha vijakazi vyenu kufanya zinaa.”

Walikuwa watu katika enzi za Ujahiliya ikiwa mmoja wao ana kijakazi alikuwa akimpeleka kuzini na anaweka kiwango cha fedha anachokichukua kila wakati. Ulipokuja Uislamu, Allah تعالى Aliwakataza Waumini kufanya hivyo na ilikuwa sababu ya kuteremka Aya hii tukufu, kulingana na yaliyotajwa na wafasiri wa Qur'an zaidi ya mmoja miongoni mwa Salafi (Waliotangulia) na pia wa sasa, ni kutokana na vitendo vya Abdullah ibn Ubayy ibn Saluul. Yeye alikuwa na vijakazi ambao aliwashurutisha kufanya umalaya ili achukue mapato yao, na alitamani pia wazae watoto ambao wataikuza hadhi yake kama alivyokuwa akidai.

¹ At-Tabari 19:173 na Al-Baghawiy 3:343.

Kutaja Maneno ya Maswahaba na Tabiin (Athar) katika mada hii

Amepokea Al- Haafidh Abu Bakr Ahmad ibn 'Amr ibn 'Abdul-Khaaliq Al-Bazzar katika Musnad wake kuwa Az-Zuhriy amesema: "Abdullah ibn Ubayy Ibn Saluul alikuwa na kijakazi aliyekuwa akiitwa Mu'adhah, ambaye alimlazimisha kuingia katika umalaya. Ulipokuja Uislamu, iliteremshwa Aya hii,

وَلَا تُكْرَهُوا فَتَيَاتِكُمْ عَلَى الْبِغَاءِ

"Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya umalaya".¹

Na amepokea Al-A'mash kutoka kwa Abu Sufyaan kuwa Jaabir amesema yafuatayo kuhusu Ayah hii: "Hii Aya iliteremshwa kuhusiana na kijakazi wa 'Abdullah ibn Ubayy ibn Saluul, ambaye jina lake lilikuwa Musaykah. Alikuwa akimlazimisha kufanya uasherati, lakini yeye hakuwa na makosa yoyote, hivyo alikataa. Hapo Allah تعالى Aliteremsha Aya hii:

وَلَا تُكْرَهُوا فَتَيَاتِكُمْ عَلَى الْبِغَاءِ

"Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya umalaya."

Mpaka Kauli Yake:

وَمَنْ يُكْرِهُهُنَّ فَإِنَّ اللَّهَ مِنْ بَعْدِ إِكْرَاهِهِنَّ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣١﴾

"Na atakayewalazimisha basi Mwenyezi Mungu baada ya kulazimishwa kwao huko, Atawasamehe, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu".²

Na amepokea an-Nasaa'iy mfano wake.³

Muqaatil Ibn Hayyaan amesema: "Nimesikia – na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi – kuwa Aya hii imeteremshwa kuhusiana na watu wawili waliokuwa wakiwashurutisha vijakazi wao katika umalaya. Mmoja wao alikuwa akiitwa Musaykah, ambaye alikuwa ni wa Answaari, na Umaymah, mama wa

¹ Kashf Al-Astaar 3:61. Ni ya kubuni: Taz "Majmau Azawaid" 7:83 "Majmau Azawaid" 3:509

² Atw-Twabariy 19:174.

³ An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:419, Muslim 26:3059.

Musaykah aliyemilikiwa na 'Abdullah ibn Ubayy. Mu'adhah na Arwah walikuwa katika hali hiyo hiyo. Baadae Musaykah na mama yake walikuja kwa Mtume na kumweleza kuhusu hilo.

Hapo Allah تعالى Akateremsha:

وَلَا تُكْرَهُوا فَتَيَاتِكُمْ عَلَى الْبِغَاءِ

“Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya umalaya.”

Maana yake: Zinaa.¹

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنَّ أَرْدَنَ مَحْصُنًا

“Ihali wao wanataka kujihifadhi.”

Maana yake: Ikiwa wanataka kubaki katika staha ambayo ndiyo hali ya wengi miongoni mwa vijakazi.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لَتَبْتَغُوا عَرَضَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Kwa ajili ya kutafuta pato la maisha ya dunia.”

Maana yake: Kwa pesa wanazochuma wao na watoto wao. Mtume ﷺ amekataza pesa za mwumikaji, na malaya na mpiga ramli.²

Na katika riwaya nyengine:

«مَهْرُ الْبَيْعِ خَيْثُ وَكَسْبُ الْحَجَّامِ خَيْثُ، وَتَمَنُّ الْكَلْبِ خَيْثُ»

“Pato la malaya ni fedha chafu, na pato la mwumikaji ni fedha chafu na thamani ya mbwa ni fedha chafu.”³

¹ Ad-Durr Al-Manthuur 6:193.

² Muslim 3:1198.

³ Muslim 3: 1199.

Na Kauli ya Allah تعالى:

وَمَنْ يُكْرِهْنَهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ مِنْ بَعْدِ إِكْرَاهِهِمْ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٦﴾

“Na atakayewalazimisha basi Mwenyezi Mungu baada ya kulazimishwa kwao huko, Atawasamehe, kwani Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.”

Maana yake: Kwao wao kama ilivyotangulia katika Hadithi ya Jaabir.¹

Na amesema Ibnu Abi Tualhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Ikiwa mtafanya hivyo, hakika Allah تعالى kwao wao ni Msamehevu mno na Mrehevu mno na madhambi yao yatakuwa kwa wale waliowashurutisha”.²

Na hivyo ndivyo alivyosema Mujahid, ‘Atwa’, al-Khurasaniy, al-A’mash na Qatadah.³

Baada ya Allah تعالى Kuelezea hukumu hizi kwa kina na kuzibainisha, Amesema:

وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ آيَاتٍ مُبَيِّنَاتٍ

“Na kwa yakini Tumekuteremshieni Ishara (ayah) zilizo wazi.”

Maana yake: Qur’ani. Ndani yake zipo Ayah zilizo wazi na zenye kueleza mambo kwa Uwazi. Na pia,

وَمَثَلًا مِّنَ الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلِكُمْ

“Na mifano kutokana na waliotangulia kabla yenu.”

Maana yake: Habari za kaumu zilizotangulia na yaliyowafikia pale walipokwenda dhidi ya maagizo ya Allah تعالى kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَجَعَلْنَاهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِّلْآخِرِينَ ﴿٥٦﴾

“Kisha Tukawafanya kuwa mfano (kumbukumbu) na hadithi kwa watu wanaokuja baada yao.” (43:56).

¹ An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:419.

² Atw-Twabariy 19:175.

³ Atw-Twabariy 19:175, 176 na Ad-Durr Al-Manthuur 6:195.

Na pia:

﴿٢٤﴾ وَمَوْعِظَةٌ لِّلْمُتَّقِينَ

“Na kwa wachamungu.”

Maana yake: Tuliwafanya wao kuwa ni funzo (kwa wengine) na Kuwakaripia kwa kufanya madhambi na kuyaendea ya haramu kwa wale wenye kumtaja na kumkumbuka Allah تعالى na kumcha Yeye.

* * *

* اللَّهُ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^ع
 مِثْلُ نُورِهِ كَمِشْكُوهٍ فِيهَا مِصْبَاحٌ^ط
 الْمِصْبَاحُ فِي زُجَاجَةٍ^ط الزُّجَاجَةُ كَأَنَّهَا
 كَوْكَبٌ دُرِّيٌّ يُوقَدُ مِنْ شَجَرَةٍ
 مُبْرَكَةٍ زَيْتُونَةٍ لَا شَرْقِيَّةٍ وَلَا
 غَرْبِيَّةٍ يَكَادُ زَيْتُهَا يُضِيءُ وَلَوْ لَمْ
 تَمْسَسْهُ نَارٌ نُورٌ عَلَى نُورٍ يَهْدِي
 اللَّهُ لِنُورِهِ مَن يَشَاءُ^ع وَيَضْرِبُ اللَّهُ
 الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ^ط وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ
 عَلِيمٌ ﴿٣٥﴾

* اللَّهُ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^ع مِثْلُ نُورِهِ كَمِشْكُوهٍ فِيهَا
 مِصْبَاحٌ^ط الْمِصْبَاحُ فِي زُجَاجَةٍ^ط الزُّجَاجَةُ كَأَنَّهَا كَوْكَبٌ
 دُرِّيٌّ يُوقَدُ مِنْ شَجَرَةٍ مُبْرَكَةٍ زَيْتُونَةٍ لَا شَرْقِيَّةٍ وَلَا
 غَرْبِيَّةٍ يَكَادُ زَيْتُهَا يُضِيءُ وَلَوْ لَمْ تَمْسَسْهُ نَارٌ نُورٌ عَلَى نُورٍ
 يَهْدِي اللَّهُ لِنُورِهِ مَن يَشَاءُ^ع وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ
 وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣٥﴾ فِي بَيوتِ أذنِ اللَّهِ أَنْ تَرْفَعُ
 وَيُذَكِّرَ فِيهَا أَسْمُهُ يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿٣٦﴾
 رِجَالٌ لَا تُلْهِيهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ
 وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخَافُونَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ
 ﴿٣٧﴾ لِيَجْزِيََهُمُ اللَّهُ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَيَزِيدَهُم مِّن فَضْلِهِ^ط
 وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَن يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا
 أَعْمَلُوهُمْ كَسْرَابٍ بِقَيْعَةٍ يَخْسَبُهُ الظَّمْآنُ مَاءً حَتَّى إِذَا
 جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ شَيْئًا وَوَجَدَ اللَّهَ عِنْدَهُ فَوَفَّاهُ حِسَابَهُ^ط
 وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٣٩﴾ أَوْ كَظُلُمْتِ فِي بَحْرٍ لُجِّيٍّ يَغْشَاهُ
 مَوْجٌ مِّن فَوْقِهِ مَوْجٌ مِّن فَوْقِهِ سَحَابٌ^ع ظَلَمْتُمْ بَعْضُهَا
 فَوْقَ بَعْضٍ إِذَا أَخْرَجَ يَدَهُ لَمْ يَكَدْ يَرْلَاهَا^ط وَمَنْ لَمْ يَجْعَلِ
 اللَّهُ لَهُ نُورًا فَمَا لَهُ مِن نُّورٍ ﴿٤٠﴾

35. Mwenyezi Mungu ni
 Nuru ya Mbingu na Ardhi.
 Mfano wa Nuru yake ni
 kama shubaka lenye
 kuwekwa ndani yake taa.
 Taa ile imo katika tungi.
 Tungi lile ni kama nyota
 inayomeremeta, inayo-
 washwa kwa mafuta yana-
 yotoka katika mti ulio-
 barikiwa, mzaituni. Si wa
 Mashariki wala Magharibi.
 Yanakaribia mafuta yake

kung'aa wenyewe ingawa moto haujayagusa – Nuru juu ya Nuru. Mwenyezi
 Mungu Humwongoa kwenye Nuru Yake Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu
 Huwapigia watu mifano. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua kila kitu".

Mfano wa Nuru ya Allah تعالى

Amesema 'Aliy ibn Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

﴿ اللَّهُ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ﴾

“Allah ni Nuru ya Mbingu na Ardhi.”

Yaani, “Anawaongoza walio mbinguni na walio ardhini”.¹ Amesema Ibn Jurayj: “Wamesema Mujaahid na Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kwa Kauli ya Aliyetukuka:

﴿ اللَّهُ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ﴾

“Allah ni Nuru ya Mbingu na Ardhi.”

Ni kuwa Anaongoza mambo yake na kudhibiti nyota zake, jua na mwezi”.² As-Suddiy amesema haya kuhusiana na Aya hii:

﴿ اللَّهُ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ﴾

“Allah ni Nuru ya Mbingu na Ardhi.”

Kwa Nuru Yake mbingu na ardhi zinapata mwangaza. Katika Sahihi mbili, imehadithiwa kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: ‘Alikuwa Mtume ﷺ anapoinuka usiku kwa ajili ya Sala anaomba:

«اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ، أَنْتَ قَيِّمُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ، وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ»

“Ewe Mola wangu! Wewe Unastahiki Sifa zote njema. Wewe Ndiwe Mwenye Kuzisimamia mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake. Sifa zote Unastahiki Wewe, Nawe ni Nuru ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani Yake.”³

Na imepokewa kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuwa amesema: “Hakika Mola wenu Mlezi Kwake hakuna usiku wala mchana, Nuru ya Arshi Yake inatokana na Nuru ya Uso Wake”. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

¹ At-Tabari 19: 177.

² Fat-hul al-Baariy 3: 5 na Muslim 1: 532.

مَثَلُ نُورِهِ

“Mfano wa Nuru Yake”.

Zipo kauli mbili katika dhamiri (ya uwakilishi nomino) ‘Yake.’ Ya kwanza ni kuwa inarudi kwa Allah تعالى, yaani mfano wa Uwongofu Wake katika moyo wa Muumini.

كَمِشْكُورَةٍ

“Ni kama shubaka”.

Amesema hivyo Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa ni kama shubaka.¹ Na ya pili ni kuwa dhamiri (kiwakilishi) inarudi kwa Muumini, ambayo inaashiriwa na matini ya maneno, na makadirio yake ni kuwa, mfano wa nuru ya Muumini ilio moyoni mwake ni kama shubaka, kwa hiyo akafananisha moyo wa muumini na uongofu wake wa kimaumbile na kwa yale anayojifunza katika Qur’ani yanaafikiana na uongofu wake wa kimaumbile. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَفَمَنْ كَانَ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّهِ وَيَتْلُوهُ شَاهِدٌ مِّنْهُ

“Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola wake na anaifuata (dalili hiyo) shahidi atokaye kwake Mwenyezi Mungu.”
(11:17).

Hivyo, ukafananishwa moyo wa Muumini kwa sababu ya usafi wake katika nafsi yake kama kandili iliyo ndani ya kioo angavu kinachofanana na mafuta mazuri, safi, yanayong’aa ambayo hayana takataka wala upotovu.

Hivyo Kauli Yake,

كَمِشْكُورَةٍ

“Ni kama shubaka”.

Amesema Ibn ‘Abbaas, Mujahid, Muhammad ibn Ka’b na wengineo kuwa, “Hii ni ile sehemu ya utambi katika kandili”.²

Hii ndiyo rai iliyo mashuhuri na kwa hivyo Akasema baada yake:

¹ Atw-Twabariy 19:179.

² Atw-Twabariy 19:181, 182.

فِيهَا مِصْبَاحٌ

“Lenye kuwekwa ndani kwenye taa”.

Na huo ni mwako unaowaka kwa mng’ao. Na panasemwa: “Hii *al-Mishkaat* (shubaka) ni shubaka ndani ya nyumba”. Huu ndio mfano uliotolewa na Allah تعالى kwa kule kumtii Yeye.

Na Allah تعالى Anauita utii huu kuwa ni Nuru, pia baadaye Anauita kwa majina mengine mengi. Ubayy ibn Ka’b رضي الله عنه amesema: “Kandili ndio nuru, na hii inamaanisha Qur’ani na Imani iliyo kifuani mwake”.¹

Na amesema As-suddiy: “Hiyo ni kandili”.

الْمِصْبَاحُ فِي زُجَاجَةٍ

“Taa ile imo katika tungi (kioo).”

Hii ina maana kuwa mwangaza huo unang’aa katika kioo cheupe angavu. Na amesema Ubayy ibn Ka’b na wengineo رضي الله عنهم: “Huu ni mfano wa moyo wa Muumini.”²

Anaendelea Aliyetukuka:

الزُّجَاجَةُ كَأَنَّهَا كَوْكَبٌ دُرِّيٌّ

“Tungi lile ni kama nyota inayomeremeta.”

Wameisoma baadhi ya wanazuoni wataalamu neno hilo *Durriyyum* - lulu ikiwa na *Dhammah Daal* bila ya *Hamzah* ambayo inatokana na *ad-Durr*, yaani kama nyota iliyotengenezwa na lulu.

Wengine wanaisoma *Durri’un* au pia *Dirri’yyun* kwa *Daal* yenye *Kasrah* au *Dhammah* na *Hamzah* mwisho, ambayo ina maana ya kurudisha (nuru), kuakisi, (*Dirriyyu*), kwa sababu nyota zinaporushwa zinang’aa zaidi kuliko wakati mwengine, Waarabu nyota wasizozijua *wanaziita Daraariy*. Amesema Ubayy ibn Ka’b رضي الله عنه: “Nyota zinazong’aa”. Na amesema Qatadah: “Mng’ao wa wazi mkubwa sana”.

¹ Atw-Twabariy 19:181.

² Atw-Twabariy 19:178.

يُوقَدُ مِنْ شَجَرَةٍ مُبْرَكَةٍ

“Inayowashwa kwa mafuta yanayotoka katika mti uliobarikiwa.”

Maana yake: Yanatumia mafuta ya Zaituni, yanayopatikana kutokana na mti uliobarikiwa.

زَيْتُونَةٍ

“Mzaituni.”

Hii ni *badali*, au *atfu bayaan*, inayobainisha ule mti uliobarikiwa uliotangulia kutajwa hapa juu.

لَا شَرْقِيَّةٍ وَلَا غَرْبِيَّةٍ

“Si wa Mashariki wala Magharibi.”

Hii ina maana ya kuwa haupo katika sehemu ya Mashariki ya ardhi hivyo kutopata jua kabisa wakati wa mwanzo wa siku, na wala pia si katika sehemu ya Magharibi ya ardhi, hivyo kuwa imefunikwa isimulikwe na jua kabla ya machweo. Lakini upo kati kati ya ardhi, hivyo kupata jua la kutosha kuanzia mwanzo wa siku mpaka mwisho wake. Hivyo, mafuta yake ni safi, mazuri yanayong’aa.

Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake:

زَيْتُونَةٍ لَا شَرْقِيَّةٍ وَلَا غَرْبِيَّةٍ

“Mzaituni, ambao si wa Mashariki wala Magharibi”.

Huu ni mti ambao unamea jangwani, hivyo haufunikwi na miti mingine wala mlima (na jabali) wala pango wala haufunikwi na chochote kile, na hii ni bora kwa mafuta yake”¹ Na amesema Mujahid kuhusu Kauli ya Aliyetukuka:

لَا شَرْقِيَّةٍ وَلَا غَرْبِيَّةٍ

“Si wa Mashariki wala Magharibi”.

¹ Ibn Abi Haatim 8:2600. Sanadi yake ni dhaifu.

Akasema: “Haupo Mashariki ambapo utapata jua wakati wa machweo wala Magharibi ambapo utapata jua wakati wa kuchomoza kwake. Lakini upo katika sehemu ambayo unapata jua linapochomoza na linapozama”.¹

Amesema Said Ibn Jubayr kwa Kauli Yake:

زَيْتُونَةٌ لَّا شَرْقِيَّةٍ وَلَا غَرْبِيَّةٍ يَكَادُ زَيْتُهَا يُضِيءُ

“Mzaituni, si wa Mashariki wala Magharibi. Yanakaribia mafuta yake kung’aa yenyewe.”

Amesema: “Haya ni aina bora zaidi ya mafuta. Jua linapochomoza linaufikia mti kutoka Mashariki na linapokuchwa linaufikia kutoka Magharibi, hivyo jua linaufikia asubuhi na jioni. Kwa sababu hiyo unahesabiwa kuwa upo Mashariki na Magharibi”. Amesema Aliyetukuka:

يَكَادُ زَيْتُهَا يُضِيءُ وَلَوْ لَمْ تَمْسَسْهُ نَارٌ

“Yanakaribia mafuta yake kung’aa yenyewe ingawa moto haujayagusa.”

‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam amesema: “Hii ni kwa sababu ya kuwa mafuta yenyewe yanang’aa”.²

Na kwa Kauli Yake Aliyetukuka:

نُورٌ عَلَى نُورٍ

“Ni Nuru juu ya Nuru”.

Al-‘Awfiy amepokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa hii inamaanisha Imani na amali za mtu.³ Na amesema As-Suddiy kuielezea Kauli ya Aliyetukuka:

نُورٌ عَلَى نُورٍ

“Ni Nuru juu ya Nuru”.

¹ Atw-Twabariy 19:186.

² Atw-Twabariy 19:183.

³ Atw-Twabariy 19:182.

Amesema: “Nuru ya moto na nuru ya mafuta; zinapojumlishwa zinatoa mng’aro, na hapana hata moja ambayo inatoa mng’aro bila ya mwenziwe. Hivyo nuru ya Qur’ani na nuru ya Imani zinapokuja pamoja, haiwezi kuwa moja peke yake bila mwenzake”.¹ Na Kauli Yake Aliyetukuka:

يَهْدِي اللَّهُ لِنُورِهِ مَن يَشَاءُ

“Allah Humwongoa kwenye Nuru Yake Amtakaye”.

Hii ina maana ya kuwa Allah تعالى Humuongoza Aliyemchagua kwa kuwa (anastahiki kuongozwa), kama ilivyokuwa katika Hadithi aliyonukuu Imamu Ahmad kutoka kwa ‘Abdullah ibn ‘Amr رضي الله عنه ambaye amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى خَلَقَ خَلْقَهُ فِي ظُلْمَةٍ ثُمَّ أَلْقَى عَلَيْهِمْ مِنْ نُورِهِ يَوْمَئِذٍ، فَمَنْ أَصَابَ مِنْ نُورِهِ يَوْمَئِذٍ اهْتَدَى وَمَنْ أَخْطَأَ ضَلَّ فَلِذَلِكَ أَقُولُ: جَفَّ الْقَلَمُ عَلَى عِلْمِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Hakika Allah Aliyetukuka Ameumba viumbe Wake katika giza, kisha siku hiyo hiyo Akawatumia Nuru Yake. Yeyote aliyeguswa na Nuru Yake siku hiyo ataongozwa, na yeyote aliyeikosa atapotea. Hivyo nasema: Kalamu imeshaandika kulingana na Elimu ya Allah Aliyetukuka”.²

Na Kauli ya Allah تعالى،

وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَلَ لِلنَّاسِ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣٥﴾

“Na Allah Huwapigia watu mifano. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kujua kila kitu”.

Baada ya Kutaja Aliyetukuka mfano huu wa Nuru ya uwongofu Wake kwa moyo wa Muumini, Allah تعالى Anamalizia Aya kwa maneno haya:

وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَلَ لِلنَّاسِ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣٥﴾

“Na Allah Huwapigia watu mifano. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kujua kila kitu.”

¹ Ad-Durr al-Manthuur 6: 202.

² Ahmad 2:176.

Hii ina maana kuwa Yeye Anajua zaidi yule anayestahiki uwongofu na yule anayefaa kuachwa katika upotevu.

«الْقُلُوبُ أَرْبَعَةٌ: قَلْبٌ أَجْرَدٌ فِيهِ مِثْلُ السَّرَاجِ يُزْهِرُ، وَقَلْبٌ أَغْلَفٌ مَرْبُوطٌ عَلَى غِلَافِهِ، وَقَلْبٌ مَنكُوسٌ، وَقَلْبٌ مُضْفَعٌ. فَأَمَّا الْقَلْبُ الْأَجْرَدُ: فَقَلْبُ الْمُؤْمِنِ سِرَاجُهُ فِيهِ نُورُهُ، وَأَمَّا الْقَلْبُ الْأَغْلَفُ فَقَلْبُ الْكَافِرِ، وَأَمَّا الْقَلْبُ الْمَنكُوسُ فَقَلْبُ الْمُنَافِقِ، عَرَفَ ثُمَّ أَنْكَرَ، وَأَمَّا الْقَلْبُ الْمُضْفَعُ فَقَلْبٌ فِيهِ إِيْمَانٌ وَنِفَاقٌ، وَمِثْلُ الْإِيْمَانِ فِيهِ كَمَثَلِ الْبَقْلَةِ يُمِدُّهَا الْمَاءُ الطَّيِّبُ، وَمِثْلُ النِّفَاقِ فِيهِ كَمَثَلِ الْقَرْحَةِ يُمِدُّهَا الدَّمُ وَالْفَيْحُ، فَأَيُّ الْمَدَّتَيْنِ غَلَبَتْ عَلَى الْأُخْرَى غَلَبَتْ عَلَيْهِ»

“Nyoyo zipo za aina nne: moyo safi mfano wa taa inayoangaza; na moyo uliofunikwa na ukafungwa kwa kifuniko; na moyo ulioinamishwa; na moyo ulio na utando wa chuma. Ama moyo msafi ni moyo wa Muumini, taa yake ni nuru yake; ama moyo uliofunikwa ni moyo wa kafiri; ama moyo ulioinamishwa ni moyo wa mnafiki amejua kisha akakanusha; na ama moyo ulio na utando wa chuma ni moyo ndani yake kuna imani na unafiki, mfano wa Imani ndani yake ni kama mfano wa tikiti maji linavuta maji mazuri, na mfano wa unafiki ndani yake ni mfano wa jeraha linavuta damu na usaha, chochote katika hivi viwili kitakachoshinda kingine kitashinda moyo”.

فِي بُيُوتٍ أَدْنَى اللَّهِ أَنْ تُرْفَعَ وَيُذْكَرَ فِيهَا أَسْمُهُ يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿٣٦﴾
 رِجَالٌ لَا تُلْهِيهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخَافُونَ يَوْمًا
 تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ ﴿٣٧﴾ لِيَجْزِيَ اللَّهُ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَيَزِيدَهُمْ مِنْ فَضْلِهِ
 وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٨﴾

36. Katika Nyumba ambazo Mwenyezi Mungu Ameamrisha zitukuzwe, na humo litajwe Jina Lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni.

37. Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Swala, na kutoa Zaka. Wanaikhofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka.

38. Ili Mwenyezi Mungu Awalipe bora ya waliyoyatenda, na Awa zidishie katika Fadhila zake. Na Mwenyezi Mungu Humruzuku amtakaye bila hisabu.

Ubora wa Misikiti na adabu zake na ubora wa wale wenye kuishughulikia.

Baada ya Allah تعالى kupiga mfano wa moyo wa Muumini na yaliyomo ndani yake katika uongofu na elimu kwa taa iliyowashwa na mafuta mazuri yanayong'aa ndani ya kioo angavu, nayo ni kama kandili. Allah تعالى Ametaja baada ya hayo, mahali ambamo inatakiwa taa hiyo iwe, napo ni Misikitini, sehemu katika ardhi ambayo inapendwa sana na Allah تعالى. Misikiti ni nyumba Zake ambazo Yeye Peke Yake Ndiye Mwenye Kuabudiwa na Kupwekeshwa. Hivyo Anasema Aliyetukuka:

فِي بُيُوتٍ أُذِنَ لِلَّهِ أَنْ تَرْفَعَ

“Katika nyumba ambazo Allah Aameamrisha zitukuzwe”.

Hii ina maana ya kwamba Allah تعالى Aameamrisha ianzishwe na isafishwe kutokana na uchafu, na upuuzi, na maneno, na vitendo ambavyo havifai ndani yake, kama alivyosema ‘Aliy ibn abi Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Aya hii tukufu:

فِي بُيُوتٍ أُذِنَ لِلَّهِ أَنْ تَرْفَعَ

“Katika nyumba ambazo Allah Aameamrisha zitukuzwe”.

Akasema: “Allah تعالى Amekataza mambo ya upuuzi ndani yake”.¹ Na ndivyo alivyosema ‘Ikrimah, Abu Swalih, adh-Dhahhaak, Naafi’ ibn Jubayr, Abu Bakr ibn Sulayman ibn Abi Hathamah, Sufyaan ibn Husayn na wengineo miongoni mwa wanazuoni wa tafsiri.

Hakika zimekuja Hadithi nyingi kuhusu ujenzi wa Misikiti, kuitukuza kwake, kuiheshimu kwake na kuitia manukato na kuifukiza. Masiala haya yamezungumzwa kwa kina zaidi sehemu maalumu, nami nimeandika kitabu kuhusu mada hii peke yake, na wa kushukuriwa ni Allah kwa Ukarimu Wake.

¹ Atw-Twabariy 19:191.

Nasi kwa usaidizi wa Allah تعالى tutataja sehemu ya Hadithi hizi, Apendapo Allah. Na Kwake kuna matarajio yetu.

Imepokewa kwa Amiri wa Waumini, 'Uthmaan ibn 'Affaan رضي الله عنه kwamba: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَنْ بَنَى مَسْجِدًا يَتَّبِعِي بِهِ وَجْهَ اللَّهِ بَنَى اللَّهُ لَهُ مِثْلَهُ فِي الْجَنَّةِ»

*"Aliyejenga Msikiti, kwa ajili ya kupata ridhaa ya Allah, basi Allah Atamjengea mfano wake (nyumba) Peponi."*¹

Imenukuliwa katika Sahihi mbili.

Na amepokea Ibn Maajah kutoka kwa 'Umar ibn Al-Khatwatwaab رضي الله عنه kwamba, Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ بَنَى مَسْجِدًا يُذَكِّرُ فِيهِ اسْمُ اللَّهِ بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ»

*"Aliyejenga Msikiti ambao linatajwa humo Jina la Allah, basi Allah Atamjengea nyumba Peponi"*².

Na An-Nasa'iy amenukuu mfano wake.³ Na Hadithi katika Masiala haya ni nyingi sana. Na imepokewa kwa Aishah رضي الله عنها kuwa, "Mtume ﷺ ametuamuru kutengeneza 'Muswalla' sehemu ya kusalia nyumbani, kuisafisha na kuitia manukato". Hii imenukuliwa na Ahmad na watu wa Sunan isipokuwa Nasa'iy.⁴ Pia imenukuliwa mfano wake na Ahmad na Abu Dawud kutoka kwa Samurah ibn Jundub رضي الله عنه.⁵ Na amesema Bukhari: 'Umar رضي الله عنه amesema: "Wajengeeni watu sehemu ya kumuabudu Allah, na tahadharini sana kupaka rangi nyekundu au manjano kwa ajili ya mapambo, hivyo kuvuta mawazo na kuwashughulisha watu kwayo."⁶

¹ Fat - h al-Baariy 1:648 na Muslim 1:378.

² Ibn Maajah 1:243.

³ An-Nasaa'iy 2:31.

⁴ Ahmad 6: 279, Tufhat al-Awadhiy 3:206 na Ibn Maajah1:250.

⁵ Ahmad 5: 17 na Abu Daawud 1:315.

⁶ Fat-h al-Baariy 1:642.

Na amepokea Abu Dawud kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا أَمَرْتُ بِتَشْيِيدِ الْمَسَاجِدِ»

“Sijaamriwa kuinakishi kwa mapambo misikiti.”

Amesema ibn 'Abbaas رضي الله عنه: “Kuyarembesha na kuipamba kama wanavyopamba Mayahudi na Manaswara”.¹ Na imepokewa kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَقْرُومُ السَّاعَةَ حَتَّى يَبَاهِيَ النَّاسُ فِي الْمَسَاجِدِ»

“Kiyama hakitosimama (hakitafika) mpaka watu washindande katika kujenga Misikiti kwa kujifaharisha”.

Hadithi hii imenukuliwa na Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan*, isipokuwa at-Tirmidhiy.² Imepokewa kwa Buraydah kuwa mtu alikuja Msikitini kisha akasimama na kutangaza kwa kusema: “Kuna yeyote Mwenye kunionea ngamia mwekundu?” Mtume ﷺ akasema:

«لَا، وَجَدْتُ، إِنَّمَا بُنِيَ الْمَسَاجِدُ لِمَا بُنِيَ لَهُ»

“Usimpate kamwe! Hakika si jingine Misikiti imejengwa kwa yaliyojengwa kwayo”. (Imepokewa na Muslim)³

Imepokewa kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا رَأَيْتُمْ مَنْ يَبِيعُ أَوْ يَبْتَاعُ فِي الْمَسْجِدِ، فَقُولُوا: لَا أَرْبَحَ اللهُ بِنَجَارَتِكَ، وَإِذَا رَأَيْتُمْ مَنْ يَنْشُدُ ضَالَّةً فِي الْمَسْجِدِ فَقُولُوا: لَا رَدَّهَا اللهُ عَلَيْكَ»

“Ukimuona mtu anauza na kununua ndani ya Msikiti mwambie: “Allah Asikupe faida katika biashara yako”. Na ukimuona mtu anatangaza kuhusu kitu kilichopotea, mwambie, “Allah Asikurudishie kabisa kitu hicho”. Imenukuliwa na At-Tirmidhiy na akasema ni *Hasan Ghaarib* (ngeni).¹

¹ Abu-Daawud 1:310.

² Ahmad 3:134, Abu Daawud 1:311, An-Nasaa'iy 2:32 na Ibn Maajah 1:244.

³ Musilm 1:397.

⁴ Tuhfatul Al-Awadhiy 4:550.

Na amepokea Bukhaari kutoka kwa As-Saa'ib ibnu Yazid Al-Kindiy ambaye amesema: "Nilikuwa nimekaa Msikitini mara mtu akanipiga kijiwe, nilipoangalia nikamkuta kuwa ni 'Umar Ibnu Al-Khatwtwaab ambaye aliniambia: "Nenda ukaniletee wale watu wawili". Nami nilikuja nao kwake, akawauliza: "Nyinyi ni nani? Au nyinyi mumetoka wapi?" Wakasema: "Sisi tunatoka Twaif". 'Umar رضي الله عنه akasema: "Lau mungekuwa ni watu wa mji huu basi ningewapiga, mnanyanyua sauti zenu katika Msikiti wa Mtume wa Allah?"¹ Na amepokea An-Nasa'iy kutoka kwa Ibrahim ibn 'Abdur-Rahmaan ibn 'Awf ambaye amesema: "'Umar رضي الله عنه alisikia sauti ya mtu Msikitini". Akamuuliza: "Je, wewe unafikiria uko wapi?" Na Hadithi hii pia ni Sahihi.²

Al-Haafidh abu Ya'laa Al-Muuswiliy amenukuu kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa 'Umar رضي الله عنه alikuwa akifukiza kwa kuwashia udi Msikiti wa Mtume ﷺ kila siku ya Ijumaa. Isnadi yake ni *Hasan* na haina ubaya, na Allah ni Mjuzi zaidi.³ Na hakika imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

«صَلَاةُ الرَّجُلِ فِي الْجَمَاعَةِ تَضَعُ عَلَى صَلَاتِهِ فِي بَيْتِهِ وَفِي سُوقِهِ خُمُسًا وَعِشْرِينَ ضِعْفًا وَذَلِكَ أَنَّهُ إِذَا تَوَضَّأَ فَأَحْسَنَ رُضُوءَهُ ثُمَّ خَرَجَ إِلَى الْمَسْجِدِ لَا يُخْرِجُهُ إِلَّا الصَّلَاةُ لَمْ يَخْطُ خَطْوَةً إِلَّا رُفِعَ لَهُ بِهَا دَرَجَةٌ وَحُطَّ عَنْهُ بِهَا خَطِيئَةٌ. فَإِذَا صَلَّى لَمْ تَزَلِ الْمَلَائِكَةُ تُصَلِّي عَلَيْهِ مَا دَامَ فِي مُصَلَّاهُ: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَيْهِ، اللَّهُمَّ ارْحَمْهُ. وَلَا يَزَالُ فِي صَلَاةٍ مَا أَنْتَظِرَ الصَّلَاةَ»

"Swala ya mtu katika jamaa inazidi Swala yake nyumbani kwake na sokoni kwake kwa daraja ishirini na tano. Na hiyo ni kuwa anapotawadha mmoja wenu akaufanya vizuri udhu wake na kisha akaingia Msikitini hakuna kilichomtoa ila Swala basi hatoinua hatua yoyote isipokuwa Allah kwa hatua hiyo Atamuinua daraja na Atamuondoshea kosa. Anaposwali, Malaika wanaendelea kumtakia rahmah maadamu anabaki katika sehemu anayoswali, wanasema: "Ewe Allah Mrehemu (Mbariki), ewe Allah, Msamehe". Na huzingatiwa kuwa yuko katika Sala kwa muda ambao anaingoja Sala nyingine".⁴

¹ Fat-h Al-Baariy 1:667.

² Tuhfatul Al-Awadhiy 8:4.

³ Musnad wa Abu Ya'laa 1:170.

⁴ Al-Bukhariy 647 na Muslim 649.

Na katika Sunan nyingine, tuna Hadithi ifuatayo:

«بَشِّرِ الْمَشَّائِينَ إِلَى الْمَسَاجِدِ فِي الظُّلَمِ بِالنُّورِ النَّامِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*“Wabashirie wale wenye kutembea gizani kuelekea Misikitini kwa Nuru timilifu Siku ya Kiyama”.*¹

Na inapendeza kwa mwenye kuingia Msikitini aingie na mguu wa kulia, na aseme kama ilivyothibiti katika Hadithi Sahihi ya Mtume ﷺ alikuwa anapoingia Msikitini akisema:

«أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ وَبِرَّجْوِهِ الْكَرِيمِ، وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ، مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ»

“Najilinda kwa Allah Aliye Mkubwa na kwa Dhati Yake Tukufu na Utawala Wake wa Kale kutokana na Shetani aliyelaaniwa”.

Akasema: *“Anaposema hivyo, Shetani husema: “Atakingwa kutokana nami kwa siku nzima.”*² Na amepokea Muslim kwa Isnadi yake kutoka kwa Abi Humayd au Abi Usayd رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا دَخَلَ أَحَدُكُمْ الْمَسْجِدَ فَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ. وَإِذَا خَرَجَ فَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ»

*“Anapoingia mmoja wenu Msikitini na aseme: “Ewe Allah, nifungulie milango ya Rehema Zako”. Na anapotoka aseme: “Ewe Allah, hakika mimi nakuomba Fadhila Zako”.*³

Na amepokea An-Nasa’iy kutoka kwao kutoka kwa Mtume ﷺ. Na imepokewa na Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا دَخَلَ أَحَدُكُمْ الْمَسْجِدَ فَلْيَسَلِّمْ عَلَى النَّبِيِّ . وَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ، وَإِذَا خَرَجَ فَلْيَسَلِّمْ عَلَى النَّبِيِّ وَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ اغْصِنِي مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ»

¹Abu Dawud 561 na At-Tirmidhiy 223.

²Abu Dawud 2:318.

³Muslim 1:494.

*“Anapoingia mmoja wenu Msikitini, na amsalimie Mtume, kisha aseme: “Ewe Allah, nifungulie milango ya Rehema Zako”. Na anapotoka amtakie amani Mtume, kisha aseme: “Ewe Allah, niepushe na Unilinde kutokana na Shetani aliyelaaniwa”.*¹

Imepokewa na Ibn Maajah, Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan katika Sahihi zao.²

Na Kauli Yake تعالی:

وَيُذَكِّرُ فِيهَا أَسْمُهُ

“Na humo litajwe Jina Lake.”

Maana yake: Jina la Allah تعالی. Hii ni kama ile Aya inayosema:

﴿ يَبْقَىٰ آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ ﴾

“Enyi wanadamu! Chukueni mapambo yenu kwenye kila wakati wa Swala”. (7:31).

Na Kauli Yake تعالی:

وَأَقِيمُوا وُجُوهَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

“na elekezeni nyuso zenu (Kwake) kwenye wakati wa kila Swala na mwabuduni Yeye hali ya kumtakasia Yeye Dini.” (7:29).

Na Kauli Yake تعالی:

وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ

“Na kwa hakika Misikiti yote ni ya Allah.” (72:18).

Na Kauli Yake تعالی:

وَيُذَكِّرُ فِيهَا أَسْمُهُ

“Na humo linatajwa Jina Lake.”

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Hii inamaanisha kuwa humo Kitabu Chake kinasomwa”.³

¹ An-Nasa’iy 2:53.

² Ibn Majah 1:254, Ibn Khuzaymah 1:231 na Ibn Hibbaan 3:246 na 247.

³ Atw-Twabariry 19: 191.

يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿٣٥﴾

“Wanamtakasa humo asubuhi na jioni.”

Maana yake: Asubuhi na mapema na jioni. Na, “Na jioni”, hili neno ni wingi wa Aswiil nayo ni mwisho wa mchana. Na Kauli Yake تعالى:

رَجَالٌ لَا تُلْهِيمُ تِجَارَةً وَلَا بَيْعًا عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ

“Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Allah”.

Hii ni kama ile Kauli Yake تعالى:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ ءَمْوَالُكُمْ وَلَا ءَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ

“Enyi Mlioamini! Yasikupumbazeni mali yenu wala watoto wenu kumkumbuka Allah.” (63: 9).

Na Kauli Yake تعالى:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ

“Enyi Mlioamini! Kukinadiwa kwa ajili ya Swalah siku ya Ijumaa, nendeni upesi kumtaja Allah na acheni biashara”. (62: 9)

Amesema Aliyetukuka kuwa dunia, na mapambo yake wala vivutio vyake na ladha ya kuuza na faida isiwashughulisha wala kuwatoa katika kumkumbuka Mola Wao Mlezi Ambaye ni Muumba Wao Mwenye Kuwaruzuku. Na ambao wanajua ya kwamba yaliyo kwa Allah تعالى ni bora kwao kuliko waliyonayo wao, kwa sababu waliyonayo yatakwisha lakini yaliyo kwa Allah تعالى ni yenye kubakia daima dawamu. Na kwa hili Akasema Aliyetukuka:

لَا تُلْهِيمُ تِجَارَةً وَلَا بَيْعًا عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ

“Biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Allah na kusimamisha Swala, na kutoa Zakah”.

Hii ina maana ya kuwa wanatanguliza kumtii Allah تعالى na Matakwa Yake na Mapenzi Yake kuliko wanachotaka wao na vinavyowaridhisha wao wenyewe.

Amepokea Salim kutoka kwa 'Abdullah Ibn Umar رضى الله عنه alikuwa sokoni na mara Swala ikakimiwa, wote walifunga maduka yao na kuingia Msikitini. Ibn 'Umar رضى الله عنه akasema: "Kwa sababu yao ndio hii Aya imeteremshwa:

رَجَالٌ لَا تُلْهِهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَن ذِكْرِ اللَّهِ

"Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Allah" (63:9)

Hii ameipokea Ibn Abi Haatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى na Ibn Jariir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى.¹ Na amesema 'Aliy ibn Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضى الله عنهما amesema:

رَجَالٌ لَا تُلْهِهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَن ذِكْرِ اللَّهِ

"Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Allah." (63:9)

Akasema: "Hii ina maana ya Swala za Faradhi".² Na hivyo ndivyo alivyosema Muqaatil ibn Hayyaan na Ar-Rabbi' ibn Anas. Na akasema As-Suddiy: "Kutokana na Swala ya jamaa". Na amesema Muqaatil ibn Hayyaan: "Haliwashughulishi na hilo kuhudhuria Swala na kuisimamisha kama alivyowaamrisha Allah na kuhifadhi nyakati zake zilizowekwa na kufanya yote waliyoagizwa kufanywa na Allah". Na Kauli Yake تَعَالَى:

خَافُونَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ ﴿٣٧﴾

"Wanaikhofu siku ambayo moyo na macho yatatahayari".

Hii inamaanisha Siku ya Kiyama ambayo nyoyo na macho vitataharuki, kwa shida ya kufazaika na ukubwa wa vitisho kama Kauli Yake تَعَالَى:

وَأَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْآزِفَةِ

"Na waonye Siku ya Kiyama ambayo iko karibu mno (na kufika)..." (40:18).

¹ Ibn Abi Haatim 8:2607. Isnadi yake ni dhaifu

² At-Twabariy 19:193.

Na Kauli Yake تعالی:

إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ ﴿٤٢﴾

“Hakika Yeye Anawaakhirisha tu mpaka siku ambayo macho yao yatakodoka (yatoke nje kwa hofu).” (14:42).

Na Allah تعالی Amesema:

وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٤٣﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكْرًا ﴿٤٤﴾ إِنَّا نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿٤٥﴾ فَوَقَّهْمُ اللَّهُ سِرَّ ذَلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَّهْمُ نَصْرَةً وَسُرُورًا ﴿٤٦﴾ وَحَرِيرًا ﴿٤٧﴾

“Na kuwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajahi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaigopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu. Basi Mwenyezi Mungu Atawalinda na shari ya siku hiyo, na Atawakutanisha na raha na furaha. Na Atawajazia Bustani za Peponi na maguo ya Hariri kwa vile walivyo subiri”. (76:8-12).

Na hapa Allah تعالی Anasema:

لِيَجْزِيَهُمُ اللَّهُ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا

“Ili Allah Awalipe mema kwa yale mazuri waliyoyatenda.”

Hawa ni wale ambao Allah تعالی Atakubali matendo yao mazuri na Kuwasamehe makosa yao. Na Kauli Yake تعالی :

وَيَزِيدَهُم مِّن فَضْلِهِ

“Na Awazidishie katika Fadhila Zake”.

Maana yake: Atazikubali amali zao njema na Atawaongezea thawabu maradufu, kama Alivyosema Aliyetukuka:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ

“Hakika Allah Hadhulumu (viumbe Vyake hata kitu kilicho sawa na) uzito wa atomu;...” (4:40).

Na Allah تعالى Amesema,

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا

“Mwenye kuleta Jema (moja) ana malipo mara kumi mfano wake.” (6:160).

Na Akasema:

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا

“Ni nani atakayemkatia Allah sehemu bora (ya mali yake kwa kuwapa masikini na kutoa katika mambo mengine ya kheri)...” (2:245).

Na Allah تعالى Amesema,

﴿وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ﴾

“Na Allah Humruzuku Amtakaye bila ya hisabu.”

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُوهُم كَسَرَابٍ بِقِيَعَةٍ نَحْسَبُهُ الظَّمْثَانَ مَاءً حَتَّى إِذَا جَاءَهُمْ لَمْ يَجِدْهُ شَيْئًا وَوَجَدَ اللَّهُ عِنْدَهُمْ فَوْقَهُمْ حِسَابَهُ^١ وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٣٩﴾ أَوْ كَظُلُمْتُمْ فِي تَحْرِيرِ لُجِيِّ يَغْشَاهُ مَوْجٌ مِّن فَوْقِهِ مَوْجٌ مِّن فَوْقِهِ سَحَابٌ^٢ ظَلُمْتُمْ بَعْضُهَا فَوْقَ بَعْضٍ إِذَا أَخْرَجَ يَدَهُ لَمْ يَكَدْ يَرِنُهَا^٣ وَمَنْ لَّمْ يَجْعَلِ اللَّهُ لَهُ نُورًا فَمَا لَهُ مِن نُّورٍ ﴿٤٠﴾

39. “Na waliokufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote. Na Atamkuta Mwenyezi Mungu hapo Naye Amlipe hisabu yake sawa sawa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.

40. Au ni kama giza katika bahari kuu, iliyofunikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake anakaribia asiuone. Na ambaye Mwenyezi Mungu Hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru”.

Mifano miwili ya aina mbili za makafiri.

Hii ni Mifano miwili ambayo Allah تعالى Ameitoa kwa aina mbili za makafiri. Kama Alivyotoa mifano miwili ya wanafiki mwanzoni mwa *Suratil Baqarah*: mfano moto na maji. Hivyo ndivyo, kama alivyotolea mfano jinsi Anavyotuliza nyoyo kwa uongofu na elimu katika *Suratur Ra'd* akapiga mifano miwili: Moto na maji. Tumeleeza yote hiyo katika sehemu zake mahsusi na hapana haja kurudia tena hapa, na Sifa zote njema Anastahiki Allah تعالى na Ndiye Mwenye kutegemewa. Ama mfano wa kwanza katika miwili hii ni wa makafiri ambao wanalingania katika ukafiri wao, wakidhania kuwa wako juu ya jambo lenye maana (wana matendo mazuri na imani), lakini kwa hakika si hivyo. Mfano wao ni kama mazigazi ambayo yanaonekana katika mbuga yenye jangwa, ukiangalia kutoka mbali ni kama bahari yenye kina kirefu. Neno *Qi'ah* inamaanisha ardhi pana tambarare ambayo mazigazi yanaweza tokea na kuonekana. Zipo aina tofauti za mazigazi, moja ni ile inayoonekana baada ya Adhuhuri na nyengine inapatikana Asubuhi, ambayo inaonekana kama maji baina ya mbingu na ardhi. Mtu ambaye anahitaji maji anapoonza mazigazi, anadhania kuwa ni maji, hivyo anayaenda ili kupata ya kunywa kutoka hapo, lakini anapofika,

لَمْ يَجِدْهُ شَيْئًا

“Hapati chochote”.

Na hivyo hivyo, kafiri anadhani kuwa amefanya amali na kuwa amepata kitu. Hivyo, amkutapo Allah تعالى Siku ya Kiyama na Kumhesabu kwayo na Kumjadili kwa matendo yake, anajikuta hana chochote kabisa ambacho kimekubaliwa. Hii ni kwa kuwa ama kwa ukosefu wa ikhlasi au kukosekana kufuata njia ya kisheria, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنثُورًا ﴿٢٣﴾

“Na Tutayaenda yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, Tuvifanye kama mavumbi yaliyotawanyika”. (25: 23).

Na Anasema hapa:

وَوَجَدَ اللَّهُ عِنْدَهُ فَوْقَهُ حِسَابَهُ ۗ وَاللَّهُ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٣٥﴾

“Na atamkuta Allah hapo Naye Atampa hisabu yake sawa sawa. Na Allah ni Mwepesi wa Kuhisabu”.

Na hivi ndivyo ilivyopokelewa kutoka kwa Ubayy ibn Ka’b, ibn ‘Abbaas, Mujahid, Qatadah na wengineo.¹

Katika Sahihi mbili, imeripotwiwa kuwa Siku ya Kiyama Mayahudi wataambiwa, “Mlikuwa mnaabudu nini?” Nao watajibu: “Tulikuwa tukimuabudia Uzayr, mtoto wa Allah”. Wataambiwa: “Mumesema uongo kwani Allah تعالی Hakuzaa mtoto”. Wataulizwa: “Munahitaji nini?” Watasema: “Ewe Mola wetu, tunasikia kiu, tupatie kitu cha kunywa”. Wataambiwa: “Je, hamuoni?” Hapo atawaonesha moto wa Jahanamu ukiwa kama mazigazi, baadhi ya sehemu zake zikimeza sehemu nyengine, na watakwenda na kuangukiana ndani yake.² Huu ni mfano wa wajinga (waliopetuka kwa ujinga wao). Ama kwa wale ambao

ujinga wao ni wa wastani, wale ambao ni mambumbumbu wanawafuata kimbumbumbu viongozi wao wa ukafiri, ni viziwi, vipofu ambao hawafahamu chochote, mfano wao ni kama Alivyosema Allah تعالی:

أَوْ كَظَلَمْتَ فِي نَحْرِ لُجِّي يَغْشَاهُ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهِ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهِ سَحَابٌ ۗ ظَلَمْتَ بَعْضَهَا
فَوْقَ بَعْضٍ إِذَا أَخْرَجَ يَدَهُ لَمْ يَكْذِبْ يَرْنَهَا ۗ

“Au ni kama giza katika bahari kuu, inaifunika mawimbi juu ya mawimbi kwa mawimbi mengine, na juu yake yapo mawingu. Ni giza juu ya baadhi yake juu ya vingine mno kiasi pindi akiutoa mtu mkono wake hawezi kuuona.”

Hii ina maana kuwa hawezi kuuona kwa sababu ya kiza totoro. Huu ni mfano wa moyo wa kafiri, ambaye ujinga wake ni wa wastani, ambaye anafuata tu na hajui maumbile halisi ya anayemfuata au anakokwenda. Yeye ni kama mfano

¹ Atw-Twabariy 19:196.

² Fat-h al-Baariy13:431 na Muslim 1:168

wa mtu mjinga katika lile fumbo alipoulizwa, “Unakwenda wapi?” Alijibu: “Pamoja nao” Aliulizwa: “Wao wanakwenda wapi?” Akajibu: “Sijui”. Na Kauli Yake Allah تعالى:

ظَلَمْتُ بَعْضَهَا فَوْقَ بَعْضٍ

“Giza juu ya giza.”

Amesema Ubayy ibn Ka’b: “Amefunikwa na giza aina Tano: mazungumzo yake ni kiza, kuingia kwake ndani ni kiza, kutoka kwake nje ni kiza, na Qadari yake Siku ya Kiyama itakuwa ni kiza katika moto wa Jahanamu.”¹ As-Suddiy na ar-Rabii’ ibn Anas pia alisema kauli sawa na hiyo.

وَمَنْ لَمْ يَجْعَلِ اللَّهُ لَهُ نُورًا فَمَا لَهُ مِنْ نُورٍ ﴿١٨٦﴾

“Na Ambaye Allah hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru.”

Yule ambaye hakuongozwa na Allah تعالى ni mjinga na ameangamia, amefeli kabisa na ni kafiri. Hii ni kama ile Aya:

مَنْ يُضَلِّلِ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ^٤

“Aliyemwacha Mwenyezi Mungu kapotea hana wa kumwongoa.”
(7:186).

Hii ni kinyume na Aliyoyasema Allah تعالى kuhusu Waumini.

يَهْدِي اللَّهُ لِنُورِهِ مَن يَشَاءُ

“Allah Humuongoza kwa nuru Yake Amtakaye.” (24:35).

Tunamuomba Allah تعالى Atie nuru katika nyoyo zetu na Atupatie nuru kuumeni kwetu na kushotoni kwetu na Atuzidishie sisi nuru.

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:198.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُسَبِّحُ لَهُ مِنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالطَّيْرِ
 صَفَّتْ كُلُّ قَدِّ عِلْمِ صَلَاتِهِ وَتَسْبِيحِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِمَا
 يَفْعَلُونَ ﴿٤١﴾ وَاللَّهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَى اللَّهِ
 الْمَصِيرُ ﴿٤٢﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُزِيحُ سَحَابًا ثُمَّ يُؤَلِّفُ بَيْنَهُ
 ثُمَّ يَجْعَلُهُ رُكَامًا فَتَرَى الْوَدْقَ يَخْرُجُ مِنْ خِلَالِهِ وَيُنزِلُ
 مِنَ السَّمَاءِ مِنْ جِبَالٍ فِيهَا مِنْ بَرَدٍ فَيُصِيبُ بِهِ مَنْ يَشَاءُ
 وَيَصْرِفُهُ عَنْ مَنْ يَشَاءُ ۗ يَكَادُ سَنَا بَرْقِهِ يَذْهَبَ بِالْأَبْصَرِ
 ﴿٤٣﴾ يُقَلِّبُ اللَّهُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لَأُولِي
 الْأَبْصَارِ ﴿٤٤﴾ وَاللَّهُ خَلَقَ كُلَّ دَابَّةٍ مِنْ مَاءٍ ۗ فَمِنْهُمْ مَنْ
 يَمْشِي عَلَى بَطْنِهِ وَمِنْهُمْ مَنْ يَمْشِي عَلَى رِجْلَيْنِ وَمِنْهُمْ مَنْ
 يَمْشِي عَلَى أَرْبَعٍ ۗ يَخْلُقُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ
 شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٥﴾ لَقَدْ أَنْزَلْنَا آيَاتٍ مُبِينَاتٍ ۗ وَاللَّهُ يَهْدِي
 مَنْ يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٤٦﴾

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُسَبِّحُ لَهُ مِنْ فِي
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالطَّيْرِ صَفَّتْ
 كُلُّ قَدِّ عِلْمِ صَلَاتِهِ وَتَسْبِيحِهِ ۗ
 وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٤١﴾
 وَاللَّهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَى اللَّهِ
 الْمَصِيرُ ﴿٤٢﴾

41. Je, huoni kwamba Allah vinamtakasa vilivyomo mbinguni na ardhini, na ndege wakikunjua mbawa zao? Kila mmoja amekwisha jua Swala yake na namna ya kumtukuza (Allah). Na Allah ni Mjuzi mno wa yote wayatendayo.

42. Na ni wa Allah Ufalme wa mbingu na ardhi, na kwa Allah ndio marejeo ya wote”.

Kila kitu kinamtakasa Allah تعالی na Ufalme ni Wake

Allah تعالی Anatueleza kuwa vyote vilivyoko mbinguni na ardhini, yaani Malaika, Wanadamu, Majini, Wanyama na hata vitu visivyokuwa na uhai, vinamtakasa na kumtukuza Yeye. Hii ni kama ile Aya:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ

“Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake..” (17:44).

وَالطَّيْرُ صَوَّفَتْ^ط

“Na ndege wakikunjua mbawa zao”.

Maana yake: Wanaporuka kupaa angani huwa wanamtukuza Mola wao na kumuabudu Yeye kwa kumtakasa kwa ilhamu waliopewa na kwa njia ambayo wanaongozwa. Allah تعالى Anajua wanayoyafanya, na hivyo Akasema:

كُلُّ قَدِّ عَلِمَ صَلَاتَهُ وَتَسْبِيحَهُ

“Kila mmoja amekwisha jua Swala yake na namna ya kumtukuza (Allah)”.

Maana yake: Allah تعالى Ameongoza kila kiumbe kwa namna yake ya kumuabudu Yeye. Kisha Anatuambia kuwa Yeye Anajua yote hayo na hakuna chochote kilichojificha Kwake, (hakuna asilojua), Allah تعالى Anasema:

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٤١﴾

“Na Allah ni Mjuzi mno wa yote wayatendayo”.

Kisha Allah تعالى Anatueleza kuwa Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake, na Yeye ni Hakim Mwendeshaji mambo, Mola Mwenye Kuabudiwa, Ambaye haipasi ibada (kwa yeyote) isipokuwa kwa ajili Yake tu.

Hivyo hivyo, hakuna awezaye kuirudisha Hukumu Yake.

وَالِلَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٤٢﴾

“Na kwa Allah ndio marejeo ya wote”.

Maana yake: Siku ya Malipo, Allah تعالى Atakapohukumu Atakavyo.

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَفُؤْا بِمَا عَمِلُوا

“Ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda.” (53:31).

Yeye Ndiye Mola Mlezi, Muumbaji, Mfalme, na kwa hakika ni Yake Mamlaka yaliyo makubwa hapa duniani na kesho Akhera. Yeye Ndiye Anayestahiki sifa zote njema duniani.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُزْجِي سَحَابًا ثُمَّ يُؤَلِّفُ بَيْنَهُ ثُمَّ يَجْعَلُهُ رُكَّامًا فَتَرَى الْوَدْقَ سَوْحًا مِّنْ خِلَالِهِ وَيُنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ مِزَّابًا فِيهَا مِنْ بَرَدٍ فَيَقْبِضُ بِهِ مَنْ يَشَاءُ وَيَصْرِفُهُ عَنِ مَنْ يَشَاءُ يَكَادُ سَنَا بَرْقِهِ يَذْهَبُ بِالْأَبْصَرِ ﴿٤١﴾ يُقَلِّبُ اللَّهُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّأُولِي الْأَبْصَارِ ﴿٤٢﴾

43. "Je! Huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu Huyasukuma mawingu, kisha Huyaambatisha, kisha Huyafanya mirundi? Basi utaona mvua ikitoka kati yake. Na Huteremsha kutoka juu kwenye milima ya mawingu mvua ya mawe, Akamsibu nayo Amtakaye na Akamuepusha nayo Amtakaye. Hukurubia mmetuko wa umeme wake kupofua macho".

44. Mwenyezi Mungu Hubadilisha usiku na mchana. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye kuona".

Tanabahisho juu ya Uweza wa Allah تعالى katika Kuumba mawingu na viambata vyake

Allah تعالى Anataueleza kuwa Anayaendesha mawingu kuanzia mwanzo, pale Anapoyakusanya yakiwa bado ni mepesi na dhaifu. Hii ni ile hali ya "kuendeshwa pole pole".

ثُمَّ يُؤَلِّفُ بَيْنَهُ

"Kisha Huyaambatanisha pamoja".

Hii ina maana Anayakusanya pamoja baada ya kuwa yametawanyika.

ثُمَّ يَجْعَلُهُ رُكَّامًا

"Kisha Huyakusanya pamoja katika mawingu mazito".

Maana yake: Huyakusanya pamoja moja juu ya jengine.

فَتَرَى الْوَدْقَ

"Kisha utaona Wadq". Maana yake: Mvua.

مَخْرُجٌ مِّنْ خِلَالِهِ

“Ikitoka katikati yake”.

Yenye kumaanisha kutoka katika penyo zake. Hivyi ndivyo ilivyosomoka kwa Ibn Abbaas na Adh-Dhahaak.¹ Ubayd Ibn Umar Al-Laythiy amesema: “Allah تعالی Anautuma upepo wenye kutawanyisha, ambao unanyanyua vile vilivyoko juu ya ardhi. Baadaye Anatuma kizalishi (upepo), ambacho kinaunda mawingu. Baadaye Anatuma kiambatanishi (upepo), ambao unayaleta mawingu pamoja. Kisha Anatuma mbolea (upepo), ambao unaipatia rutuba, mbolea na mbegu, mawingu”. Hii ameinukuu Ibnu Abi Haatim na Ibn Jariir (Mwenyezi Mungu Awarehemu).²

Na Kauli Yake Allah تعالی,

وَيُنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ مِثْرًا مِّمَّنْ جِبَالٍ فِيهَا مِنْ بَرَدٍ

“Na Huteremsha toka juu ya milima ya mbinguni: mvua ya barafu”.

Wamesema baadhi ya wanazuoni wa nahau (wanasarufi) kuwa *Min* ya kwanza inaelezea mwanzo wa mwelekeo (*Ibtidail-ghaya*), na *Min* ya pili inahusisha baadhi au sehemu ya mbingu (*littab-iidh*) kubaadhisha, na *Min* ya tatu inatoa maelezo ya aina na anuwai (*Bayanul-Jins*). Huu ni mtazamo wa wanazuoni wa Tafsir wanaosema ya kwamba:

مِن جِبَالٍ فِيهَا مِنْ بَرَدٍ

“Toka juu kwenye milima ndani yake ipo barafu”.

Maana yake: Ni kuwa katika mbingu ipo milima ya barafu kutokana nayo Allah تعالی Huteremsha barafu. Na ama wale ambao wamejaalia milima kuwa *Istia-rra* neno liloazimwa kwa maana ya mawingu, wanadhania kuwa *Min* ya pili katika Aya hii inaelezea sehemu ambayo barafu inatoka, yaani ina kuwa kama ya kwanza na hivyo kuwa ni badala ya ile ya kwanza. Na Allah تعالی ni Mjuzi zaidi. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

¹ Atw-Twabariy 19: 202.

² Atw-Twabariy 19: 201.

فَيَصِيبُ بِمَن يَشَاءُ وَيَصْرِفُهُ عَن مَّن يَشَاءُ

“Kisha Humsibisha nayo Amtakaye na kumuepusha nayo Amtakaye.”

Inawezekana kuwa muradi wa Kauli Yake:

فَيَصِيبُ بِمَن

“Kisha Humsibisha nayo...”

Maana yake: Kwa yale Anayoteremsha kutoka mbinguni kwa aina mbalimbali ya mvua na barafu. Hivyo, Kauli Yake itakuwa:

فَيَصِيبُ بِمَن يَشَاءُ

“Kisha Humpata nayo Amtakaye.”

Maana yake: Rehema kwao.

وَيَصْرِفُهُ عَن مَّن يَشَاءُ

“Na kumwepusha nayo Amtakaye.”

Maana yake: Anawacheleweshea mvua. Na pia huenda ikawa muradi wa Kauli Yake: Yaani kwa hiyo barafu inakuwa ni adhabu kwa yule Amtakaye, kwa kugonga matunda yao na kuharibu mazao na miti yao na Humuepusha Amtakaye kuwa ni rehema kwao. Na Kauli Yake:

يَكَادُ سَنَا بَرْقِمْ يَذْهَبُ بِالْأَبْصَرِ ﴿٤١﴾

“Kisha mwanga wa umeme wake hukaribia kupofua macho.”

Maana yake: Ule mwanga wa radi unakaribia kuondoa nuru ya macho yao ikiwa ataifuata na kuiangalia. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

يُقَلِّبُ اللَّهُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ

“Anabadilisha Allah usiku na mchana”.

Anavidhibiti, hivyo Anachukua kutoka kwa kimoja wapo urefu wake na Kuuweka kwenye ufupi wa kingine hadi vinalingana. Kisha Anachukua toka kwa kimoja

na huongezea kwa kingine, hivyo hurefuka uliokuwa mfupi, na huwa mfupi uliokuwa mrefu. Allah تعالى Ndio Mdhhibiti wa hilo kwa Amri Yake na Nguvu Zake na Utukufu Wake na Elimu Yake. Kwa hakika ni dalili ya Ukubwa Wake Aliyetukuka. Kama Alivyosema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّأُولِي الْأَبْصَارِ ﴿٤٤﴾

“Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye macho ya kuchunguza.”

Kwa hakika hii ni dalili ya Ukubwa Wake Aliyetukuka, kama Alivyosema:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾

“Katika Kuumba mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko dalili kuonesha kuwepo kwa Allah Aliye Mmoja, kwa wenye akili”. (3:190).

Na Aya tukufu zinazokuja baada yake.

وَاللَّهُ خَلَقَ كُلَّ دَابَّةٍ مِّن مَّاءٍ فَمِنْهُمْ مَّن يَمْشِي عَلَىٰ بَطْنِهِ وَمِنْهُمْ مَّن يَمْشِي عَلَىٰ رِجْلَيْنِ
وَمِنْهُمْ مَّن يَمْشِي عَلَىٰ أَرْبَعٍ ۗ يَخْلُقُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٥﴾

45. “Na Allah Ameumba kila mnyama kutokana na maji. Wengine katika wao hutembea kwa matumbo yao, na wengine hutembea kwa miguu miwili, na wengine hutembea kwa miguu minne. Allah Huumba Atakavyo. Hakika Allah ni Muweza mno wa kila kitu”.

Uweza wa Allah تعالى katika Uumbaji wa wanyama

Allah تعالى Anataja Uweza Wake uliokamilika na Ufalme Wake Mtukufu kwa Kuumba Kwake aina tofauti ya wanyama wakiwa na umbile, rangi tofauti pamoja na tofauti katika harakati zao na kutulia kwao, japokuwa wameumbwa kutokana na maji aina moja.

فَمِنْهُمْ مَّن يَمْشِي عَلَىٰ بَطْنِهِ

“Wengine katika wao hutembea kwa matumbo yao.”

Kama nyoka na wengine wanaofanana nao.

وَمِنْهُمْ مَّن يَمْشِي عَلَى رِجْلَيْنِ

“Na wengine huenda kwa miguu miwili.”

Kama binadamu na ndege.

وَمِنْهُمْ مَّن يَمْشِي عَلَى أَرْبَعٍ

“Na wengine huenda kwa miguu minne.”

Kama nyama howa (mifugo) na hayawani wote wengine. Na kwa hili Amesema:

سَخَّلْتُ لِلَّهِ مَا يَشَاءُ

“Allah Huumba Atakavyo.”

Maana yake: Kwa Uweza Wake, kwani Alitakalo huwa na Asilolitaka basi haliwi. Na Akasema:

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٦﴾

“Hakika Allah ni Muweza wa kila kitu.”

لَقَدْ أَنْزَلْنَا آيَاتٍ مُّبِينَاتٍ وَاللَّهُ يَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٤٧﴾

46. “Kwa yakini Tumeteremsha Ayah zenye kubainisha. Na Allah Humwongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.”

Allah تعالى Anaamua kuwa Yeye Ameteremsha katika hii Qur’ani hukumu za wazi, maneno ya hekima pamoja na mifano iliyo wazi madhubuti mingi sana. Na kuwa Yeye Huwaongoza watu wenye ufahamu, uoni, wenye akili ya kuzingatia na kufahamu. Na kwa hili Akasema:

وَاللَّهُ يَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٤٧﴾

“Na Allah Humwongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka”.

* * *

وَيَقُولُونَ ءَأَمْنَا بِاللَّهِ وَبِالرَّسُولِ وَأَطَعْنَا ثُمَّ يَتَوَلَّى فَرِيقٌ مِّنْهُم مِّنْ بَعْدِ ذَلِكَ ۖ وَمَا أُولَٰئِكَ بِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾
 وَإِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٤٨﴾ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ

47. "Na wanasema: Tume-muamini Allah na Mtume, na tumetii. Kisha kikundi katika hao hugeuka baada ya hayo. Watu kama hao si Waumini.

48. Na wanapoitwa kwa Allah na Mtume Wake ili-

وَيَقُولُونَ ءَأَمْنَا بِاللَّهِ وَبِالرَّسُولِ وَأَطَعْنَا ثُمَّ يَتَوَلَّى فَرِيقٌ مِّنْهُمْ مِّنْ بَعْدِ ذَلِكَ ۖ وَمَا أُولَٰئِكَ بِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾
 وَإِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٤٨﴾ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ وَإِن يَكُنْ هُمْ أَحَقُّ بِأَنْتَوَا إِلَيْهِ مُذْعَبِينَ ۖ أَمَّا قُلُوبُهُمْ مُّرَّضَةٌ بِمَنَافِقَةٍ ۖ

الْفٰسِقُونَ ﴿٤٩﴾

ahukumu baina yao, kipo kikundi katika wao kinakataa.

49. Na ikiwa haki ni yao, wanamjia kwa kutii.

50. Je, wana maradhi katika nyoyo zao, au wanaona shaka? Au wanaogopa ya kuwa Allah na Mtume Wake watawadhulumu? Kwa hakika wao wenyewe ndio madhalimu.

51. Haiwi kauli ya Waumini wanapoitwa kwa Allah na Mtume Wake ahukumu baina yao husema: “Tumesikia na tumetii”. Na hao ndio wenye kufaulu.

52. Na wenye kumtii Allah na Mtume Wake, na kumwogopa Allah na kujiepusha kumwasi, basi hao ndio wenye kufuzu”

Hila za Wanafiki na hali ya Waumini

Allah Aliyetukuka Anatupa khabari ya sifa za wanafiki ambao wanadhihirisha kinyume cha wanayoficha. Kawaida wanasema maneno kwa ndimi zao:

ءَامَنَّا بِاللّٰهِ وَبِالرَّسُوْلِ وَاَطَعْنَا ثُمَّ يَتَوَلٰى فَرِيقٌ مِّنْهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ

“Tumemuamini Allah na Mtume, na tumetii. Kisha kikundi katika hao hugeuka baada ya hayo”.

Wanakhalifu kauli zao kwa matendo yao, hivyo wanayasema wasiyotenda. Anasema Aliyetukuka:

وَمَا اُولٰٓئِكَ بِالْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٧٧﴾

“Watu kama hao si Waumini”.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِذَا دُعُوْا إِلَى اللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ لِيَحْكُمْ بَيْنَهُمْ

“Na wanapoitwa kwa Allah na Mtume Wake ili ahukumu baina yao”.

Hii ni kuwa wanapotakiwa kufuata uongofu aliouteremsha Allah تعالى kwa Mtume Wake hugeukageuka na kufanya kiburi katika nafsi zao katika kumfuata. Na hii Kauli ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ ءَامَنُوا بِمَا نُزِّلَ إِلَيْكَ وَمَا نُزِّلَ مِنْ قَبْلِكَ

“Hawakuona wale wanaodai kwamba wameyaamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako?...”

Mpaka Kauli Yake Aliyetukuka:

رَأَيْتَ الْمُتَنَفِقِينَ يَصُدُّونَ عَنْكَ صُدُودًا

“...utawaona wanafiki wanakukwepa kwa upinzani”. (4:60-61).

وَإِنْ يَكُنْ هُمْ الْآحَقُّ يَأْتُوا إِلَيْهِ مُذْعِنِينَ

“Na ikiwa haki ni yao, wanamjia kwa kutii”.

Maana yake: Ikiwa hukumu iliyotolewa ni kuwapa haki wao na sio dhidi yao wanakuja hali ya kuwa wanakusikiliza hali ya kutii. Na hiyo ndio maana ya kauli Yake:

مُذْعِنِينَ

“Kwa kutii”.

Lakini ikiwa hukumu ni dhidi yake anakegeuka, na kuipa nyongo na kudai lisilo la haki kinyume na haki na ukweli, na wakati huo hupendelea kuipeleka kadhia yake kwa mtu mwingine asiyekuwa Mtume ili apate kuupamba uongo wake. Kunyenyeka kwake mwanzoni si kwa sababu ya (Imani) kuwa huo ni ukweli, lakini ni kwa sababu iliafiki utashi wake. Hivyo, pale haki ilipokuwa imekhalifu utashi wake aliyokuwa akiutazamia alikengeuka kuelekea upande mwingine.

أَفِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ

“Je, wana maradhi katika nyoyo zao?...”

Hii ina maana kuwa hali yao haiwezi kuwa ni nyengine, zaidi ya kuwa ni lazima kuwa wao wana maradhi nyoyoni mwao, au wana baadhi ya shaka juu ya Dini, au wanaogopa kuwa Allah تعالی na Mtume Wake watawadhulumu katika hukumu zao dhidi yao. Hali yoyote itakayo kuwa, inaonesha ukafiri ulio wazi, na Allah تعالی Anajua ni zipi katika hizi sifa bainifu kila mmoja wao anazo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

بَلْ أَوْلِيَّكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٥٥﴾

“Kwa hakika wao wenyewe ndio madhalimu”.

Bali wao ndio madhalimu mafisadi, na Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wapo mbali na hawana hatima ya dhulma wala kutotenda haki kama wanavyodhania wao. Ametukuka Allah تعالى na Mtume Wake kwa hayo wanayowasingizia nayo. Kisha Allah تعالى Anatupasha habari ya sifa za Waumini wanaomwitikia Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ, ambao hawatafuti njia ya maisha mbali na ile iliyoelezwa katika Kitabu cha Allah na Sunna ya Mtume Wake ﷺ. Akasema:

إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَنْ يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا

“Haiwi kauli ya Waumini wanapoitwa kwa Allah na Mtume Wake ili Mtume ahukumu baina yao, ila husema “Tumesikia, na tumetii”.

Maana yake: Kusikiliza na kutii. Hivyo, Allah تعالى Amewasifu wao kuwa wamefaulu, ambayo ni kupata kile mtu anachotaka na kuepushwa na kile anachoogopa. Hivyo Allah تعالى Akasema:

وَأَوْلِيَّكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥٦﴾

“Na hao ndio wenye kufaulu”.

Na amesema Qataadah kuhusu aya hii:

أَنْ يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا

“Ila husema, “Tumesikia, na tumetii”.

Ametutajia kuwa ‘Ubadah ibn Asw-Swaamit رضي الله عنه ambaye alishiriki katika Bay’ah ya Aqabah na Vita vya Badr, na alikuwa ni mmoja wa viongozi wa Answaar, alipokuwa anaaga dunia. Alimwambia mpwa wake wa kiume, Junaadah ibn Abi Umayyah: “Je, sikuambii yale unayopasa kufanya na yale ya kwako?” Akasema: “Kwa nini (yaani niambie).” Akasema: “Ni juu yako kusikia na kutii wakati wa dhiki na faraja, na unapohisi kuwa una nguvu na unapokuwa

hutaki, na unapojihisi ubinafsi na choyo. Ni juu yako kuuzoesha ulimi wako kuzungumza ukweli. Usipingane na viongozi, isipokuwa tu wanapokuamuru kwa dhahiri kumuasi Allah تعالى. Na pia unapoamriwa kufanya kitu kinachokwenda kinyume na Kitabu cha Allah تعالى, basi fuata Kitabu cha Allah تعالى.¹

Na amesema Qataadah: “Tumeelezwa kuwa Abu Ad-Dardaa’ رضي الله عنه alisema: “Hapana Uislamu isipokuwa kutii, na hapana kheri isipokuwa kwa *Jama’ah*. Na nasaha ni kwa Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na Khalifa wa Waumini wa kawaida”. Amesema Qataadah: “Na tumetajiwa kuwa “Umar ibn Al-Khatwtwaab رضي الله عنه alikuwa akisema: “Mafungamano ya Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana muabudiwa wa kweli isipokuwa Allah تعالى, na kusimamisha Swala, na kutoa Zaka na kumtii aliyechaguliwa na Allah تعالى kusimamia mambo ya Waislamu”. Imepokewa na Ibn Hatiim² رحمه الله تعالى.

Na Hadithi pamoja na Athaar kuhusu wajibu wa kutii Kitabu cha Allah تعالى, na Sunnah za Mtume Wake ﷺ, Makhaliifa Waongofu, viongozi, na Maimamu wanapoamuru kumtii Allah تعالى ni nyingi sana, haiwezekani kuwekwa katika sehemu hii ndogo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Na mweye kumtii Allah na Mtume Wake.”

Kwa yale waliyoamrisha na kuacha waliyoyakataza, na pia:

وَيَحْشَ اللَّهَ

“Na kumwogopa Allah.”

Katika dhambi zilizopita,

وَيَتَّقِهِ

“Na kujiepusha kumwasi.”

Kwa madhambi ambayo hutenda katika siku zijazo.

¹ Ibn Abi Haatim 8:2623. Isnadi yake ni dhaifu.

² Ibn Hatiim 8:2623 na 2624.

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥٤﴾

“Basi hao ndio wenye kufuzu”.

Hao ndio waliofuzu katika kheri zote na kusalimika na shari zote hapa duniani na Akhera.

* وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن أُمِرُوا لَيُخْرِجَنَّ قُلَّ لَا تُقْسِمُوا طَاعَةً مَّعْرُوفَةً إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٥٥﴾ قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلْتُمْ مَّا حُمِّلْتُمْ وَإِن تُطِيعُوهُ تَهْتَدُوا وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلْغُ الْمُبِينُ ﴿٥٦﴾

53. “Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa kiapo chao ya kwamba ukiwaamrisha kwa yakini watatoka. Sema: “Msiape, Ut’iifu unajulikana. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda”.

54. Sema: “Mt’iini Mwenyezi Mungu, na mt’iini Mtume. Na mkigeuka, basi yaliyo juu yake ni aliyobebeshwa, na yaliyo juu yenu ni mliyobebeshwa nyinyi. Ni mkimt’ii Yeye mtaongoka. Na hapana juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe wazi wazi”.

Allah تعالیٰ Anasema Akitoa khabari za wanafiki wakimuapia Mtume kuwa lau utatuamrisha twende vitani basi tutatoka bila ya wasiwasi. Allah تعالیٰ Anasema:

قُلْ لَا تُقْسِمُوا

“Waambie: Msiape”,

Maana yake: Musile kiapo.

Na Kauli Yake:

طَاعَةً مَّعْرُوفَةً

“Kwani utiifu unajulikana vema”.

Inasemekana maana ya ibara hii ni kuwa, utiifu wenu umejulikana ni kwamba ni wa maneno matupu bila ya vitendo aina yoyote. Na kila mara munapoapa munaongopa. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

تَحْلِفُونَ لَكُمْ لَتَرْضَوْا عَنْهُمْ

“Wanakuapieni ili muwe radhi nao”. (9:96).

Na Amesema Aliyetukuka:

أَتَّخِذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً

“Wamefanya viapo vyao vya uongo kuwa ngao yao”. (58:16).

Na wao katika tabia zao ni kuongopa hata katika masiala na mambo wanayo chagua wenyewe kwa khiari. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

* أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١١﴾ لَئِنْ أُخْرِجُوا لَا يَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِنْ قُوتِلُوا لَا يَنْصُرُوهُمْ وَلَئِنْ نَصَرُوهُمْ لَيُوَلُّنَّ الْأَدْبَرَ ثُمَّ لَا يُصَرُّونَ ﴿١٢﴾

“Huwaoni wanaofanya unafiki wanawaambia nduguzo waliokufuru katika Watu wa Kitabu: “Mkitolewa na sisi lazima tutatoka pamoja nanyi, wala hatutamt’ii yeyote kabisa dhidi yenu. Na mkipigwa vita lazima tutakusaidieni. Na Mwenyezi Mungu Anashuhudia kuwa hakika bila shaka ni waongo. Pindi wakitolewa hawatatoka pamoja nao, na wikipigwa vita hawatawasaidia. Na kama wakiwasaidia basi watageuza migongo; kisha hawatanusuriwa”. (59:11-12).

Kisha Amesema Aliyetukuka:

قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ

“Sema: Mtiini Allah, na mtiini Mtume.”

Maana yake: Kifuateni Kitabu cha Allah تعالى na Sunnah za Mtume Wake ﷺ. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَلْيَنْتَوَلَّوْا

“Na mkikengeuka.” Maana yake: Mkigeuka na kupuuza Aliyokuleteeni,

فَإِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلَ

“Basi yaliyo juu yake ni aliyobebeshwa.”

Nayo ni kufikisha ujumbe na kutekeleza amana.

وَعَلَيْكُمْ مَا حُمِّلْتُمْ

“Na yaliyo juu yenu ni mliyobebeshwa nyinyi.”

Kwa kukubali hilo ni kutukuza na kuitekeleza kama ilivyoamriwa.

وَإِن تَطِيعُوهُ تَهْتَدُوا

“Na mkimtii yeye mtaongoka.”

Kwa kuwa yeye anaita katika njia nyoofu (iliyonyooka).

صِرَاطَ اللَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“Njia ya Allah Ambaye ni Vyake (Peke Yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi.” (42: 53).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا أَلْبَلَّغُ الْمُبِينِ ﴿٥٤﴾

“Na sio jukumu la Mtume ni kufikisha tu Ujumbe wazi wazi?”

Hii ni kama ile Kauli ya Aliyetukuka:

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَّغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٥٥﴾

“Basi! Hakika si jingine juu yako ni kufikisha tu (uliyoamrishwa), na juu Yetu ni hesabu (Siku ya Kiyama).” (13:40).

Na Kauli Yake:

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿٨٨﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿٨٩﴾

“Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia.” (88:21-22).

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا
 اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ
 خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

55. "Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya Makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya Makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinshirikishe na chochote. Na wataokufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu".

Ahadi ya Allah تعالیٰ kwa waumini kuwa Atawapa Ukhalifa

Hii ni ahadi ya Allah تعالیٰ kwa Mtume Wake ﷺ kuwa Ataufanya Ummah wake uwe ni makhalifa wa ardhi, yaani viongozi wa watu na watawala juu yao, kupitia kwao Miji itatengamaa na waja nao watasalimu amri kwa kunyenyekea. Hivyo, Atawabadilishia mbadala wa khofu waliokuwa nayo kwa watu kuwa ni amani na utulivu. Na hakika Allah تعالیٰ Alitekeleza hilo, na Yeye Ndiye Mwenye kushukuriwa na kusifiwa. Kwani hakika Mtume ﷺ hakuaga dunia hadi Allah تعالیٰ Amempa nusra na ushindi kwa kuikomboa Makkah na Khaybar na Bahrayn na sehemu nyengine zote za Bara Arabu na ardhi ya Yemen yote. Na pia akawa ni mwenye kuchukua kodi (*Jizyah*) kutoka kwa Majusi wa Hajar na sehemu za pembezoni mwa Shaam. Na akabadilishana zawadi na Hiraql (*Heraclius*) mfalme wa Roma na mtemi wa Misri na Iskandariyah (*Alexandria*), naye ni Mqawqis (*Almgoks*), na pia wafalme wa Uman (*Oman*) na Najjaashiy (*Negus*) mfalme wa Uhabeshi (*Ethiopia*) ambaye alitawala baada ya As-himah, Allah تعالیٰ Amrehemu na Amkirimu.

Kisha alipokufa Mtume ﷺ na Allah تعالیٰ Akamchagulia hadhi Aliyonayo na karamah na cheo, akasimamia uongozi baada yake khalifa wake, Abubakr Asw-Swiddiq رضي الله عنه ambaye aliunganisha Ummah na kuuzuia usivunjike. Alichukua hatamu za uongozi za Rasi ya Uarabuni, naye alipeleka majeshi ya

Kiislamu katika ardhi ya Miji ya Fursi, chini ya uongozi wake Khaalid ibn al-Walid رضي الله عنه ambaye alifungua baadhi ya sehemu akapigana na baadhi ya watu wake. Alituma jeshi lengine chini ya uongozi wa Abu 'Ubaydah 'Aamir Ibn Al-Jarraah رضي الله عنه, na majemedari wengine waliokuja baada yake katika ardhi ya Shaam (Syria na Palestina). Alituma jeshi la tatu chini ya uongozi wa Amr Ibn Al-Aasw رضي الله عنه, Misri. Allah تعالى Aliliwezesha lile jeshi lililotumwa Shaam kuifatihi Basra na Damascus na mikoja yake katika ardhi ya Hawraan na vitongoji vyake. Waislamu walibarikiwa ya kuwa Abubakr رضي الله عنه alipata ilhamu ya kumchagua Umar Al-Faaruu رضي الله عنه kama mrithi wake wa ukhalifa, na hivyo alichukua hatamu za uongozi baada yake na akafanya kazi nzuri sana. Baada ya Mitume, ulimwengu haujapata kumuona yeyote kwa ubora na maadili na uadilifu wa hali ya juu na kamili kama 'Umar رضي الله عنه. Katika utawala wake, sehemu iliyobaki ya Syria na Misri, na sehemu kubwa ya Uajemi, zilitekwa. Kisra alishindwa, na hivyo kumfanya akimbie kwenda sehemu ya mbali zaidi katika dola yake hiyo. Nguvu za Kaisari zilipunguzwa, utawala wake Syria ulipinduliwa, na hivyo kumfanya akimbie na kukaa Istanbul, Uturuki. Mali zao zilitumiwa katika njia ya Allah تعالى kama alivyotabiri na kuahidi Mtume ﷺ

Katika enzi za 'Uthmaan رضي الله عنه, dola ya Kiislamu ilipanuka sana na kufika sehemu za mbali kabisa katika ardhi, mashariki na magharibi yake. Ardhi za sehemu ya magharibi zilitekwa zikijumlisha Kuprus na Andalusi (Spain), Qayrawan¹ na Sebta ambayo inapakana na Bahari ya Atlantic. Upande wa Mashariki, mpaka ulifika mbali zaidi karibu na China. Kisra aliuliwa, na dola yake ikaharibika kabisa na miji ya Iraq, Khurasan na al-Ahwaaz ilitekwa. Waislamu waliwaua Waturuki wengi na Allah تعالى Alimtweza mfalme wao mkubwa ajulikanaye kama Khaqaan. *Jiyzah*¹ ilikusanywa kutoka sehemu za mashariki na magharibi, na kuletwa kwa Amiri wa Waumini, 'Uthmaan ibn 'Affaan رضي الله عنه. Hii ilikuwa ni baraka iliyoletwa na kusoma kwake na kujifunza kwake Qur'ani, na kwa kuuleta Ummah pamoja katika kuuhifadhi na kuikusanya Qur'an. Katika Sahihi imepokewa kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ اللَّهَ زَوَى لِي الْأَرْضَ فَرَأَيْتُ مَشَارِقَهَا وَمَغَارِبَهَا، وَسَيَلُّعُ مُلْكِ أُمَّتِي مَا زُوِيَ لِي مِنْهَا»

¹ Ushuru ambao unalipwa na wasiokuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu.

“Allah Alinionesha ardhi yote, basi nami nikaenda Mashariki yake na Magharibi yake. Utafika ufalme wa Ummah wangu kote nilikooneshwa”.¹

Na sisi sasa tunastarehe kwa yale ambayo Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wametuahidi, kwani Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wamesema ukweli. Tunamuomba Allah تعالى Atupe Imani ya kumuamini Yeye na Mtume Wake ﷺ, na Atusaidie kumshukuru kwa njia ambayo tutapata Radhi Zake.

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا
 اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ
 خَوْفِهِمْ أَمْنًا

“Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao”.

Ar-Rabi’ ibn Anas amesema kuwa Abul Aliyah amesema: “Mtume ﷺ na Maswahaba wake walikuwa Makkah kwa takriban miaka kumi, wakiwaita watu kwa siri kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya kumshirikisha Yeye na chochote. Walikuwa katika hali ya khofu na hawakuamriwa wakati huo kupigana mpaka baada ya wao kuhamia Madinah ndipo walipoamrisha kupigana. Walipokuja Madina bado walikuwa wanaogopa, hivyo walikuwa wanabeba silaha zao asubuhi na jioni. Hivyo ndivyo walivyokuwa kwa muda ambao Allah تعالى Alitaka...” Baadaye Allah تعالى Aliteremsha ayah hii.²

Siku moja swahaba mmoja akamwambia Mtume ﷺ: “Ee! Mtume wa Allah, hadi lini tutakuwa waoga? Hakuna siku tutakuwa na amani tukaacha kubeba silaha?” Mtume ﷺ akasema: “Hamtasubiri isipokuwa muda mchache tu atakuja kukaa mtu miongoni mwenu katika kundi la watu akiwa hana silaha yoyote.” hivyo Allah تعالى Akateremsha Aya hii.¹ Allah تعالى Alimuezesha Mtume

¹ Muslim 4:2215.

² At-Twabari 19:209.

Wake ﷺ kuwashinda wote waliosimama dhidi yake katika Rasi ya Bara Arabu, na baada ya hapo wakawa katika amani na usalama na wakaweka chini silaha zao. Kisha Allah ﷻ Alimchukua Mtume Wake ﷺ, nao wakabaki katika hali hiyo ya amani na usalama katika enzi za Abubakr, 'Umar na 'Uthmaan رضي الله عنهم, mpaka yale yaliyotokea yakatokea. Wakati huo ndio hofu ilirudi tena, hadi waliweka walinzi na jeshi la usalama. Walibadilika, hivyo kufanya hali nayo ibadilike. Mmoja kati ya *Salaf* alisema: “Ukhalifa wa Abubakr na 'Umar رضي الله عنهما ulikuwa wa kweli na walishikilia barabara Kitabu cha Allah ﷻ. Kisha akasoma Aya hii.” Al-Baraa' ibn Aazib رضي الله عنه amesema: “Aya hii iliteremshwa tulipokuwa katika hali ya khofu kubwa.” Hii ni kama ile aya:

وَأَذْكُرُوا إِذْ أَنْتُمْ قَلِيلٌ مُسْتَضْعَفُونَ فِي الْأَرْضِ

“Na kumbukeni mlipokuwa wachache, mkifanywa wanyonge katika ardhi,...” (8:26). Mpaka Kauli Yake:

لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٢٦﴾

“...ili mpate kushukuru.” (8:26)

Na Kauli Yake Allah ﷻ,

كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Kama Alivyowafanya makhalifa amba waliokuwa kabla yao.”

Hii ni kama ile Aya ambapo Allah ﷻ Anatuambia kuwa Musa عليه السلام alipowaambia watu wake:

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْأَرْضِ

“Huenda Mola wenu Mlezi Akamhulikisha adui wenu na Akakufanyeni nyinyi ndio makhalifa katika ardhi.” (7:129).

Na Allah ﷻ Anasema:

وَتُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضِعُوا فِي الْأَرْضِ

“Na Tukataka kuwafadhili waliodhoofishwa katika ardhi hiyo...” Mpaka Aya mbili baada yake. (28:5-6).

¹Ad-Durr al-Manthuur 6:215..

وَلَيْمَكِّنَنَّ هُمْ دِيَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ

“Na kwa yakini Atawamakinishia Dini yao aliyoiridhia kwao.”

Kama Mtume ﷺ alivyomwambia ‘Adiyy ibn Haatim alipokuja kwake pamoja na wawakilishi:

«أَتَعْرِفُ الْحِيرَةَ؟»

“Je, unaujua mji wa Hirah?”

Nikajibu: “Siujui, lakini nimesikia khabari zake.” Mtume ﷺ akasema:

«فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَيُيَمِّنَنَّ اللَّهُ هَذَا الْأَمْرَ حَتَّىٰ تَخْرُجَ الطَّيِّبَةُ مِنَ الْحِيرَةِ حَتَّىٰ تَطُوفَ بِالنَّبِيِّ فِي غَيْرِ جَوَارٍ أَحَدٍ، وَلَتَمْتَحُنَنَّ كُنُوزَ كِسْرَىٰ بْنِ هُرْمُزٍ»

“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, Allah Atilitimiza jambo hili (yaani Uislamu) mpaka mwanamke mpanda ngamia atatoka Hirah na kutufu kwenye Nyumba (Al-Ka’bah) bila kuhitaji ulinzi wa yeyote, naapa kwa Allah kuwa hazina za Kisra ibn Hurmuz mtazifungua”.

Nikauliza: “Kisra mtoto wa Hurmuz?” Akasema:

«نَعَمْ، كِسْرَىٰ بْنُ هُرْمُزٍ، وَلَيُيَذَلَّنَّ الْمَالُ حَتَّىٰ لَا يَقْبَلَهُ أَحَدٌ»

“Ndio, Kisra ibn Hurmuz na mali itagawiwa hadi mpaka kusipatikane mtu wa kuipokea”.

‘Adiyy ibn Haatim amesema: “Basi hivi sasa inatokea mwanamke msafiri kutoka Hirah juu ya ngamia huja kutufu kwenye Nyumba ya Allah bila ya kuhitaji ulinzi wa yeyote. Nami nilikuwa miongoni mwa wale waliofungua hazina za Kisra ibn Hurmuz. Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, jambo la tatu pia litatokea, kwa sababu Mtume ﷺ amesema hivyo.”¹

يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا

“Waniabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote”.

¹ Ahmad 4:257.

Imamu Ahmad amepokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Mu'aadh ibn Jabal رضي الله عنه alimwambia: "Baina ya kuwa mimi nimepanda punda nikiwa nyuma ya Mtume ﷺ na hakuna baina yangu na yeye isipokuwa tandiko akaniita:

«يَا مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ!»

"Ewe Mu'aadh!"

Nikamjibu: "Labbayka wa Sa'adayka (na niko katika huduma yako). Ewe Mtume wa Allah" Kisha akaenda kwa muda kisha akaniita:

«يَا مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ!»

"Ewe Mu'aadh ibn Jabal!"

Nikaitika: "Labbayka wa Sa'adayka. Ewe Mtume wa Allah". Kisha akaenda kwa muda kisha akaniita:

«يَا مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ!»

"Ee Mu'aadh ibn Jabal!"

Nikamjibu: "Labbayka wa Sa'adayka. Ewe Mtume wa Allah". Akaniuliza:

«هَلْ تَدْرِي مَا حَقُّ اللَّهِ عَلَى الْعِبَادِ؟»

"Je, wajua haki ya Allah iliyo juu ya waja Wake?"

Nikamjibu: "Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ ni Wajuzi zaidi". Akaniambia:

«فَإِنَّ حَقَّ اللَّهِ عَلَى الْعِبَادِ أَنْ يَعْبُدُوهُ وَلَا يُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا»

"Hakika Haki ya Allah iliyo juu ya waja Wake ni kumuabudu Yeye Pekee bila ya kumshirikisha na chochote".

Kisha akaenda, baada ya muda akaniuliza:

«يَا مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ!»

"Ee Mu'aadh ibn Jabal!"

Nikaitika: "Labbayka wa Sa'adayka. Ewe Mtume wa Allah". Akaniuliza:

«فَهَلْ تَدْرِي مَا حَقَّ الْعِبَادِ عَلَى اللَّهِ إِذَا فَعَلُوا ذَلِكَ؟»

“Je, wajua haki ya waja kwa Allah, kama wakitekeleza (haki ya Allah)?”

Nikamjibu: “Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wanajua zaidi”. Akaniambia:

«فَإِنَّ حَقَّ الْعِبَادِ عَلَى اللَّهِ أَنْ لَا يُعَذِّبَهُمْ»

“Haki ya waja juu ya Allah ni Kutowaadhibu”.¹

Hii Hadithi wameitoa katika Sahihi mbili.² Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

“Na watakaokufuru baada ya hayo, basi hao ndio mafasiki (mafasiki)”.

Maana yake: Yeyote atakayetoka katika utii wangu moja kwa moja ametoka katika kumtii Mola Wake Mlezi. Na hilo linatosha kuwa ni dhambi kubwa. Basi maswahaba walivyokuwa ni wenye msimamo zaidi ya watu wengine baada ya Mtume katika kutekeleza Amri za Allah تعالى na utiifu wao mkubwa kwa Allah تعالى. Ikawa nusura iko upande wao wakadhihirisha kalima ya Allah تعالى. Walifanya mpaka Neno la Allah تعالى likae Mashariki ya ardhi na Magharibi, na Allah تعالى Aliwasaidia sana, hivyo wakaweza kutawala watu na ardhi zote. Pale watu walipolegea katika misimamo yao kwa baadhi ya maagizo na amri, nguvu zao zilipungua sana kulingana na msimamo wao. Lakini imethibiti katika Sahihi mbili kwa njia (Isnadi) zaidi ya moja kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَزَالُ طَائِفَةٌ مِنْ أُمَّتِي ظَاهِرِينَ عَلَى الْحَقِّ، لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَذَلَهُمْ وَلَا مَنْ خَالَفَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Hakika hakitaacha kuwepo kikundi katika umma wangu chenye kuipigania Haki, hawatawadhuru wao wenye kuwatelekeza wala wenye kukhalifiana nao mpaka siku ya Kiyama”³

¹ Ahmad 5:242.

² Fat-h al-Baariy 10:412 na Muslim 1:58.

³ Muslim 1:137.

Na katika riwaya nyingine:

«حَتَّىٰ يَأْتِيَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَذٰلِكَ»

“Mpaka itakapokuja Amri ya Allah na wao wapo kama walivyo (bila ya kubadilika katika msimamo).”¹

Na katika riwaya nyingine:

«حَتَّىٰ يُقَاتِلُوا الدَّجَالَ»

“Mpaka wapigane na Dajjaal”¹

Na katika riwaya nyingine:

«حَتَّىٰ يَنْزِلَ عِيسَىٰ ابْنُ مَرْيَمَ وَهُمْ ظَاهِرُونَ»

“Mpaka ateremke ‘Isaa ibn Maryam na wao ni wenye kushinda.”²

Na riwaya zote hizi ni Sahihi wala hakuna mgongano baina yake.

* * *

¹ Muslim 3:1523.

² Ahmad 4:437.

³ Fat-h Al-Baariy 13:306.

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٥٦﴾ لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ مِنَ النَّارِ وَلَيْسَ الْمَصِيرُ ﴿٥٧﴾ يَتَأَيَّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِيَسْتَفْذِنُكُمُ الَّذِينَ ءَمَلَتْ ءَايْمَنُكُمْ وَالَّذِينَ لَمْ يَبْلُغُوا الْحُلُمَ مِنْكُمْ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ مِّن قَبْلِ صَلَاةِ الْفَجْرِ وَحِينَ تَضَعُونَ ثِيَابَكُمْ مِّنَ الظُّهْرِ وَمِنَ بَعْدِ صَلَاةِ الْعِشَاءِ ۚ ثَلَاثُ عَوْرَاتٍ لَّكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ وَلَا عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ بَعْدَهُنَّ طَوَافُونَ ۗ عَلَيْكُمْ بَعْضُكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ ءَايَاتِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٨﴾ وَإِذَا بَلَغَ الْأَطْفَالُ مِنكُمُ الْحُلُمَ فَلْيَسْتَفْذِنُوا كَمَا ءَسْتَفْذِنُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ ءَايَاتِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٩﴾ وَالْقَوَاعِدُ مِنَ النِّسَاءِ الَّتِي لَا يَرْجُونَ نِكَاحًا فَلَيْسَ عَلَيْهِنَّ جُنَاحٌ أَن يَضَعْنَ ثِيَابَهُنَّ غَيْرَ مُتَبَرِّجَاتٍ بِزِينَةٍ ۗ وَأَن يَسْتَعْفِفْنَ خَيْرٌ لَهُنَّ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٦٠﴾

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ
وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ
﴿٥٦﴾ لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا
مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ
النَّارِ وَلَيْسَ الْمَصِيرُ ﴿٥٧﴾

56. "Na shikeni Swala, na toeni Zakah, na mtiini Mtume, ili mpate kurehemewa."

57. Msiwadhanie walio-kufuru kwamba watashinda katika nchi. Na makazi yao ni Motoni, na hakika ni maovu kweli marejeo yao."

Agizo la Kuswali, Kutoa Zakah na Kutii na Ubainifu wa Kushindwa Makafiri Kuepuka Hatima Yao.

Anasema Aliyetukuka katika Kuwaamuru waja Wake Waumini kusimamisha

Swala, na hiyo ni kumuabudu Allah تعالى Peke Yake Ambaye Hana mshirika yeyote. Na pia kutoa Zakah, nayo ni Kuwafanyia ihsani viumbe walio dhaifu na mafukara miongoni mwao. Na wawe katika hali ya kutekeleza hayo ni wenye kumtii Mtume ﷺ. Hiyo ni kufuata mwenendo wake kama Alivyowaamuru na kuacha Aliyokataza, huenda Allah تعالى Akawarehemu kwa hilo. Na wala hakuna chembe ya shaka kuwa mwenye hayo, Allah تعالى Atamrehemu, kama Alivyosema katika Aya nyengine:

أُولَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ

“Hao ndio ambao Allah Atawarehemu.”

Na Kauli yake Allah تعالى،

لَا تَحْسَبَنَّ

“Msiwadhanie.”

Maana yake: Usidhanie, Ewe Muhammad kuwa,

الَّذِينَ كَفَرُوا

“Wale waliokufuru.”

Maana yake: Waliokukhalifu wewe na kukukadhibisha.

مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ

“Kwamba ni wenye kushinda katika nchi.”

Hii maana yake, wao hawawezi kumshinda Allah تعالى، bali Allah تعالى Anawaweza na Atawaadhibu kwa hilo adhabu kali sana. Na kwa hili Akasema:

وَمَا أُولَئِكَ

“Na makazi yao.”

Maana yake: Katika Nyumba ya Akhera.

النَّارِ وَلَيْسَ الْمَصِيرُ ﴿٥٧﴾

“Ni Motoni, na hakika ni ubaya ulioje wa marejeo yao.”

Maana yake: Marejeo mabaya sana ni marejeo ya makafiri, na ni sehemu ovu ya makazi na sehemu mbaya sana ya mapumziko.

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِيَسْتَعِذَّ بِكُمْ الَّذِينَ مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ وَالَّذِينَ لَمْ يَبْلُغُوا الْحُلُمَ مِنْكُمْ
ثَلَاثَ مَرَّاتٍ ۚ مِنْ قَبْلِ صَلَاةِ الْفَجْرِ وَحِينَ تَضَعُونَ ثِيَابَكُمْ مِنَ الظَّهِيرَةِ وَمِنْ بَعْدِ صَلَاةِ
الْعِشَاءِ ۚ ثَلَاثُ عَوْرَاتٍ لَكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ وَلَا عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ بَعْدَهُنَّ طَوَّافُونَ عَلَيْكُمْ

بَعْضُكُمْ عَلَى بَعْضٍ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٨﴾ وَإِذَا بَلَغَ الْأَطْفَالُ مِنْكُمُ الْحُلُمَ فَلْيَسْتَعِذُوا كَمَا أَسْتَعِذَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٩﴾ وَالْقَوَاعِدُ مِنَ النِّسَاءِ الَّتِي لَا يَرْجُونَ نِكَاحًا فَلَيْسَ عَلَيْهِنَّ جُنَاحٌ أَنْ يَضَعْنَ ثِيَابَهُنَّ غَيْرَ مُتَبَرِّجَاتٍ بِزِينَةٍ ۗ وَأَنْ يَسْتَغْفِرْنَ خَيْرٌ لَهُنَّ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٦٠﴾

58. "Enyi Mliomini! Na wakutakeni idhini wale mliowamiliki kwa mikono yenu ya kuume na walio bado kufikia baleghe miongoni mwenu mara tatu; kabla ya Swala ya Alfajiri, na wakati mnapovua nguo zenu mchana, na baada ya Swala ya 'Ishaa. Hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si vibaya kwenu wala kwao baada ya nyakati hizi, kuzungukiana nyinyi kwa nyinyi. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Ayah Zake, na Allah ni Mjuzi mno wa yote Mwingi wa Hikima.

59. Na watoto wanapobaleghe, basi na watake ruhusa, kama walivyotaka ruhusa wa kabla yao. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Ayah Zake, na Allah ni Mjuzi wa yote Mwenye Hikima.

60. Na wanawake wazee wasiotaraji kuolewa, si vibaya kwao kupunguza nguo zao za nje, maadamu kufanya kwao hivyo hakupelekei kudhihirisha mapambo yao. Hata hivyo, wakijistahi ni bora kwao. Na Allah ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua kila kitu".

Nyakati za kutaka idhini kwa watumwa na watoto wadogo

Hizi Ayah zimekusanya kuomba ruhusa ndugu wa karibu wao kwa wao, Aya zilizotangulia mwanzo wa sura ni kwa ajili ya kuomba idhini ya *Ajnabiy* (wasio maharimu). Akawaamuru Waumini kuona kwamba watumwa wao na watoto ambao hawajabaleghe watake idhini katika nyakati tatu; wakati wa kwanza ni kabla ya Swala ya Alfajiri, kwani wakati huo watu wanakuwa wamelala vitandani mwao.

وَحِينَ تَضَعُونَ ثِيَابَكُمْ مِنَ الظَّهِيرَةِ

“Na wakati mnapovua nguo zenu mchana.”

Maana yake: Katika wakati wa mapumziko (*Qaylulah*), kwani wakati huo huenda mtu akawa mtu amevua nguo zake pamoja na mkewe.

وَمِنْ بَعْدِ صَلَاةِ الْعِشَاءِ

“Na baada ya Swala ya ‘Ishaa.”

Kwani huu ni wakati wa kulala. Hivyo, watumishi na watoto wameamuriwa wasiingie kwa ghafla kwa watu wa nyumbani kwa wakati huu, kwani inaogopewa kuwa mume anaweza kuwa na mkewe katika hali ya kimapenzi au katika shughuli mfano wa hiyo. Na hivyo Akasema

ثَلَاثُ عَوْرَاتٍ لَكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ وَلَا عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ بَعْدَهُنَّ

“Hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si vibaya kwenu wala kwao baada ya nyakati hizi”.

Ikiwa wataingia katika wakati mbali na hizi, hakuna dhambi wala kosa lolote kwenu kwa kuwaachilia kuingia, na pia hapana makosa kwao lau wataona kitu chochote kwa wakati mbali na zile nyakati tatu. Hakika wao wamepewa ruhusa kuingia kwa ghafla, kwani wao ni watu wanaozunguka nyumbani ili kuwahudumikia nyinyi na kufanya mambo mengine. Na hivyo wanasamehewa kwa vitu ambavyo wengine hawatasamehewa. Na muda wa kuwa Ayah hii iko wazi na hukumu yake haijafutwa. Utekelezaji wa watu katika Ayah hizi ni mdogo mno, na hivyo ‘Abdullah ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما aliwakanya na kuwashutumu watu kwa hilo.

Abu Daawud amepokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما akisema: “Watu wengi hawakuiamini Ayah inayozungumzia kutaka idhini, lakini namwambia kijakazi wangu aombe ruhusa kuingia”. Abu Dawud amesema: “Na ‘Atwaa’ pia amehadithia kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما aliamuru hilo.”¹ Na amesema Ath-Thawriy kuwa Musa ibn Abi Aishah amesema: “Nilimuuliza Ash-Sha’biy kuhusu Aya hii:

¹ Abu Daawud 5:377.

﴿لِيَسْتَفْزِمَكُمُ الَّذِينَ مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ﴾

“Na wakubishieni hodi wale iliowamiliki mikono yenu ya kuume”.

Akasema: “Ayah hii haijafutwa”.¹ Nikasema: “Lakini watu hawaitekelezi.”

Akasema: “Allah تعالى Ndio Mwenye kuombwa msaada”. Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَإِذَا بَلَغَ الْأَطْفَالُ مِنْكُمُ الْحُلُمَ فَلْيَسْتَعِذُوا كَمَا أَسْتَعِذْنَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Na watoto wanapobaleghe, basi na watake ruhusa, kama walivyotaka ruhusa wa kabla yao.”

Hii ina maana kuwa wale watoto ambao walikuwa wakiomba ruhusa katika zile nyakati tatu za faragha, pindi wanapobaleghe wanawajibika kubisha hodi katika nyakati zote, kulingana na wale ambao sio maharimu zao na katika ule wakati ambao huenda mume akawa na mkewe, hata ikiwa si katika zile nyakati tatu.

Hapana tatizo kwa Ajuza ikiwa hatavaa Hijabu

Na Kauli Yake:

وَالْقَوَاعِدُ مِنَ النِّسَاءِ

“Na wanawake wazee.”

Amesema Sa’iid ibnu Jubayr, Muqaatil ibn Hayyaan, Adh-Dhahhaak na Qataadah: “Hawa ni wale wanawake ambao hawapati hedhi (hedhi yao imekatika) na ambao hawawezi kuzaa tena”. Na wale ambao hawana matarajio tena ya kuolewa.

الَّتِي لَا يَرْجُونَ نِكَاحًا

“...wasiotaraji kuolewa...”

Maana yake: Wasiokuwa na matarajio yoyote ya kuolewa,

¹ Atw-Twabariy 19:213.

فَلَيْسَ عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ أَنْ يَضَعُوا يَدَيْهِمْ عَنْ مَتَّبِعَتِ بِرَبِّنَا

“Si vibaya kwao kupunguza nguo zao za nje, kama majuba na mitandio na nguo nyingine za kujifunika maadamu kufanya kwao hivyo hakupelekei kudhihirisha mapambo yao.”

Maana yake: Si lazima kwao kujistiri kama wanavyojifunika na kujistiri wanawake wengine.¹

Ampokea Abu Dawud kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa:

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ

“Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho.” (24:31),

Hukumu ya Aya hii haiwahusu,

الَّتِي لَا يَرْجُونَ نِكَاحًا

“Wanawake wazee wasiotaraji kuolewa.”²

Amesema Ibn Mas‘uud رضي الله عنه katika kuelezea Kauli ya Aliyetukuka:

فَلَيْسَ عَلَيْهِمْ جُنَاحٌ أَنْ يَضَعُوا يَدَيْهِمْ

“Si vibaya kwao kupunguza nguo zao za nje.”

Akasema: “Hayo ni majuba na mitandio.³ Rai sawa na hii imepokewa kutoka kwa Ibn ‘Abbaas, Ibn ‘Umar, Mujaahid, Sa’iid ibn Jubayr, Abi Ahs-Sha’thaa, Ibrahim An-Nakha’iy, Al-Hasan, Qataadah, Az-Zuhriy, Al-Awzaa’iy na wengineo رضي الله عنهم.⁴

Na amesema Sa’iid Ibn Jubayr kuhusu Ayah:

¹ Ad-Durr Al-Manthuur 6:222 na Atw-Twabariy 19:216.

² Abu Daawuud 4: 361.

³ Atw-Twabariy 19: 217. Na hapa *Jilbaab* na *Ridaa’* zimetumika kumaanisha kitu kimoja, ambayo ni nguo ndefu inayofunika *Khiimaar* (sehemu ya kifua, shingo na utosi).

⁴ Atw-Twabariy 19: 217,218.

غَيْرَ مُتَّبِعَاتٍ بِزِينَةٍ

“Maadamu kufanya kwao hivyo hakupelekei kudhihirisha mapambo yao.”

Wasijifunue kiasi cha kuonekana mapambo yao nje (*Jilbaab*), hivyo mapambo yao kuonekana. Na Kauli Yake:

وَأَنْ يَسْتَعْفِفَ. خَيْرٌ لَهُمْ.

“Na kujichunga ni bora kwao.”

Maana yake: Na kutoacha kwao kuvaa nguo za nje japokuwa wameruhusiwa (kutovaa) ni bora na afadhali sana kwao.

وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

“Na Allah ni Mwingi wa Kusikia, Mwingi wa Kujua.”

* * *

¹ Abu Daawuud 4:361.

² Atw-Twabariy 19:217. Na hapa *Jilbaab* na *Ridaa'* zimetumika kumaanisha kitu kimoja, ambayo ni nguo ndefu inayofunika *Khiimaar* (sehemu ya kifua, shingo na utosi).

³ Atw-Twabariy 19:217,218.

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَى حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْأَعْرَجِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى أَنْفُسِكُمْ أَنْ تَأْكُلُوا مِنْ بُيُوتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ آبَائِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ بُيُوتِ عَمَّاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَخَوَاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَعْمَمِكُمْ أَوْ بُيُوتِ عَمَّاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ مِمَّا مَلَكَتُمْ مَفَاحِجَهُمْ أَوْ صَدِيقِكُمْ ۗ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعًا أَوْ أَشْتَاتًا ۚ فَإِذَا دَخَلْتُمْ بُيُوتًا فَسَلِّمُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ تَحِيَّةً مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُبْرَكَةً طَيِّبَةً ۚ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦١﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَإِذَا كَانُوا مَعَهُ عَلَى أَمْرٍ جَامِعٍ لَّمْ يَذْهَبُوا حَتَّى يَسْتَأْذِنُوهُ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ فَإِذَا أَسْتَأْذِنُوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأُذِنَ لِمَنْ شِئْتَ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ اللَّهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٢﴾ لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا ۚ قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنْكُمْ لِوَاذًا ۚ فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ ۚ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾ أَلَا إِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ قَدْ يَعْلَمُ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ وَيَوْمَ يُرْجَعُونَ إِلَيْهِ فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٦٤﴾

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَى حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْأَعْرَجِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرْجٌ وَلَا عَلَى أَنْفُسِكُمْ أَنْ تَأْكُلُوا مِنْ بُيُوتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ آبَائِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ بُيُوتِ عَمَّاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَخَوَاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَعْمَمِكُمْ أَوْ بُيُوتِ عَمَّاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ مِمَّا مَلَكَتُمْ مَفَاحِجَهُمْ أَوْ صَدِيقِكُمْ ۗ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعًا أَوْ أَشْتَاتًا ۚ فَإِذَا دَخَلْتُمْ بُيُوتًا فَسَلِّمُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ تَحِيَّةً مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُبْرَكَةً طَيِّبَةً ۚ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦١﴾

61. "Si vibaya kwa kipofu, wala si vibaya kwa mlemavu, wala si vibaya kwa mgonjwa, wala kwenu nyinyi, mkila kutoka katika nyumba zenu, au nyumba za baba zenu, au nyumba za mama zenu, au nyumba za kaka zenu, au nyumba za

shangazi zenu, au nyumba za wajomba zenu, au nyumba za khalati (dada wa mama) zenu, au za mliowashikia funguo zao, au rafiki zenu. Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali. Na mkiingia katika nyumba, jisalimieni wenyewe, kuwa ni maamkuzi yatokayo kwa Allah, yenye Baraka nzuri. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Aya Zake mpate kufahamu.”

Kula katika nyumba za ndugu zenu

Makusudio hapo ni kwamba wao walikuwa wakijisikia vibaya kula na kipofu, kwa sababu hakioni chakula au sehemu ya chakula na matonge mazuri yalipo, hivyo wengine wangeweza kuchukua kile kizuri dhidi yake. Pia walihisi vibaya kula na kiguru, kwa sababu hawezi kukaa vizuri kwa starehe, na hivyo rafiki zake waweza kuchukua fursa dhidi yake. Na pia walihisi vibaya kula na mgonjwa kwa sababu hawezi kula kama wengineo. Hivyo, waliogopa na kuwa na khofu kula nao ili wasiwe ni wenye kuwadhulumu kwa njia moja au nyengine. Kisha Allah تعالی Aliteremsha Aya hii, kuwapa wao uamuzi katika masiala haya. Hii ni rai ya Sa’iid ibn Jubayr na Miqsam.¹

Adh-Dhahhaak amesema: “Kabla ya risala ya Mtume ﷺ, watu walikuwa wakiona vibaya kula na watu hawa kwa sababu ya kuona kinyaa na kujiona bora, hivyo hawakuwa ni wenye kula na watu hawa, ili isiwapelekee kuwasaidia. Hivyo Allah تعالی Aliteremsha Aya hii.”²

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَىٰ حَرَجٌ

“Si vibaya kwa kipofu.”

‘Abdur-Razzaaq رحمه الله تعالی amenukuu kutoka kwa Mujaahid aliyesema: “Mtu alikuwa akimchukua kiguru, kilema au mgonjwa nyumbani kwa ndugu yake au dada yake au shangazi yake, na wakati huo hawa watu walemavu walikuwa wakiona vibaya kwa jambo hilo. Hivyo, walisema: “Wanatuchukua katika nyumba za watu wengine.” Hivyo, Aya hii ndipo iliposhuka kuwapa wao ruhusa kufanya hilo.”³

¹ Ad-Durr al-Manthuur 6:223 na Atw-Twabariy 19:221.

² Atw-Twabariy 19:219.

³ Abdur-Razzaaq 3:64.

As-Suddiy amesema: “Mtu alikuwa akiingia katika nyumba ya baba yake au ndugu yake au ya mtoto wake, na mke wa nyumba hiyo anamwandalia chakula, lakini mtu huyo (mgeni) alikuwa anakataa kula chakula hicho kwa sababu mwenye nyumba hayupo. Hivyo, Allah تعالی Akateremsha:

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَىٰ حَرَجٌ

“Si vibaya kwa vipofu.” Na pia,

وَلَا عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ أَنْ تَأْكُلُوا مِنْ بُيُوتِكُمْ

“Wala kwenu nyinyi, mkila katika nyumba zenu.”

Hakika si jingine hii (nyumba zenu) imetajwa hapa japokuwa inafahamika kwa hakika, ili kuanzia hapa nyumba za wengine ziweze kutajwa na kuwekwa wazi kuwa hukumu yake ni sawasawa na iliyotangulia kutajwa. Na hukumu hii kadhalika inahusu nyumba za watoto japokuwa hazikutajwa, na kuzingatia hilo, wametolea hoja wale wenye kuona mali ya mtoto ni sehemu ya mali ya baba. Imekuja katika Musnad na Sunan, kutoka kwa njia zaidi ya moja kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَنْتَ وَمَالُكَ لِأَبِيكَ»

“Wewe na mali yako ni ya babako.”²

أَوْ بُيُوتِ آبَائِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أُمَّهَاتِكُمْ

“Au nyumba za baba zenu, au nyumba za mama zenu.”

Mpaka Kauli Yake:

أَوْ مَا مَلَكَتْهُم مَّفَاحِيهُ

“Au za mliowashikilia funguo zao.”

Hii iko wazi kabisa, na inatumika kama dalili kwa wale wanaodhanika kuwa ni lazima kwa jamaa kutoa kwa kuwapa jamaa wenziwao. Na Kauli ya Aliyetukuka:

¹ Ahmad 2:279, 204, 214 na Ibn Maajah 2:769.

أَوْ مَا مَلَكَتُمْ مَفَاتِحَهُۥ

“Au za mliowashikilia funguo zao.”

Said ibnu Jubayr na As-Suddiy wamesema: “Hii inahusu mtumishi wa mtu akiwemo mtumwa na msimamizi wa nyumba, hapana kosa kula chakula alichomhifadhia katika vyakula kwa wema”. Na Az-Zuhriy amepokea kutoka kwa ‘Urwah kuwa Aishah رضي الله عنها amesema: “Walikuwa Waislamu wakienda katika msafara pamoja na Mtume ﷺ, hivyo wakiacha funguo zao kwa wadhamini wao (watunzaji) wao na kuwaambia: “Hakika tumewaruhusu nyinyi kula munachohitajia”. Nao wakasema: “Hakika wao hawakuturuhusu sisi kula, bila shaka wao wameturuhusu bila ya nafsi zao kuwa radhi. Kwa hakika sisi ni wasimamizi tu.” Allah تعالى Akateremsha:

أَوْ مَا مَلَكَتُمْ مَفَاتِحَهُۥ

“Au za mliowashikilia funguo zao.”

Na Kauli Yake Allah تعالى:

أَوْ صَدِيقِكُمْ

“Au rafiki zenu.”

Maana yake: Nyumba ya rafiki zenu au sahibu zenu, hapana kosa juu yenu kula kwao unapojua kuwa hilo halitawaletea matatizo wala hawatachukia hilo. Na Kauli Yake:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعًا أَوْ أَشْتَاتًا

“Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali.”

Amepokea ‘Aliy ibn Abi Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Aya hii: Na hiyo ni baada ya Allah تعالى Kuteremsha:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالِكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

“Enyi Mlioamini! Msile mali zenu baina yenu kwa batili.” (4:29).

¹ Kashaf Al-Astaar 3:61, 62.

Hapo Waislamu walisema: “Hakika Allah تعالى Ametukataza kula mali zetu baina yetu kwa batili na dhulma, na chakula ni bora kuliko mali. Kwa hiyo haifai kwa yeyote miongoni mwetu kula kwa mwengine, hivyo watu wakaacha hilo. Allah تعالى Akateremsha:

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَى حَرَجٌ

“Si vibaya kwa vipofu.”

Mpaka kwa Kauli Yake:

أَوْ صَدِيقِكُمْ

“Au rafiki zenu.”

Na pia walikuwa hawajihisi kuwa na nguvu ya kula mmoja wao akila chakula peke yake mpaka awe na wenzake. Allah تعالى Aliwasahilishia hilo kwa kuwaambia:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعًا أَوْ أَشْتَاتًا

“Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali.”¹

Na amesema Qataadah: “Huu ulikuwa ni mji wa Banu Kinaanah ambao wakati wa Ujahiliya walidhania kuwa ni aibu kwa mmoja wao kula chakula peke yake kwa kiasi ambacho mtu alikuwa akiendelea na safari yake kwa kumuendesha ngamia aliyebeba mzigo japokuwa ana njaa mpaka apate mtu wa kula na kunywa naye. Allah تعالى Akateremsha:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعًا أَوْ أَشْتَاتًا

“Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali.”²

Hii ni ruhusa kutoka kwa Allah تعالى Aliyompa mtu ama kula peke yake au pamoja na jamaa (kikundi), japokuwa kula pamoja na jamaa kuna baraka na ni bora zaidi.

Imamu Ahmad amepokea Hadithi kutoka kwa Wahshiy ibn Harb kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake kuwa mtu mmoja alimwambia Mtume ﷺ: “Hakika sisi tunakula lakini hatushibi”. Akasema:

¹ Atw-Twabariy 19:224.

² Atw-Twabariy 19:224.

«لَعَلَّكُمْ تَأْكُلُونَ مُتَّفَرِّقِينَ، اجْتَمِعُوا عَلَى طَعَامِكُمْ، وَادْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ، يُبَارِكْ لَكُمْ فِيهِ»

“Huenda kuwa nyinyi mnakula mbalimbali, kusanyikeni kwenye chakula chenu, Mtabarikiwa ndani yake”.

Imepokewa na Abu Dawud na Ibn Maajah.¹ Na pia imepokewa na Ibn Maajah kutoka kwa Saalim kutoka kwa baba yake kutoka kwa ‘Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كُلُوا جَمِيعًا، وَلَا تَفَرَّقُوا، فَإِنَّ الْبِرْكَهَ مَعَ الْجَمَاعَةِ»

*“Kuleni pamoja wala msile mbalimbali, hakika Baraka iko pamoja na wanaokula kwa jamaa”.*²

Na Kauli Yake:

فَإِذَا دَخَلْتُمْ بُيُوتًا فَسَلِّمُوا عَلَىٰ أَنفُسِكُمْ

“Na mkiingia katika nyumba, zisalimieni nafsi zenu”.

Sa’iid ibn Jubayr, Al-Hasan, Al-Baswriy, Qataadah na Az-Zuhriy wamesema: “Hii inamaanisha kwamba salimianeni”.³ Abu Az - Zubayr amesema; “Nimemsikia Jaabir ibn ‘Abdullah akisema: “Ukiingia nyumbani kwa familia yako, basi watolee salamu kwa maamkio yanayotoka kwa Allah تعالى, yenye baraka na yaliyo mazuri”. Akasema: “Silioni hilo isipokuwa ameliwajibisha”. Amesema Ibn Jurayj: Na Ziyaad kuwa Ibn Twawuus alikuwa akisema: “Yeyote kati yenu anapoingia katika nyumba yake, basi atoe salamu”.⁴

Mujaahid amesema: “Na unapoingia Msikitini, sema: “Salamu kwa Mtume ﷺ. Na unapoingia kwa familia yako, watolee salamu, na unapoingia nyumba ambayo haina mtu, sema: “Assalaamu ‘Alayna wa’Alaa ‘Ibaadillahi s-Swalihiin (Amani iwe juu yetu na pia iwe juu waja wema wa Allah تعالى).”⁵

¹ Ahmad 3:501, Abu Daawuud 3764 na Ibn Maajah 3286.

² Ibn Maajah 3287.

³ Al-Baghawiy 3:358 na Atw-Twabariy 19: 226.

⁴ Atw-Twabariy 19:225.

⁵ Abdur-Razzaq 3:228.

Kwani lilikuwa likiamriwa hilo, na ametusimulia kuwa malaika wanajibu salamu yake hiyo.¹ Na Kauli Yake Allah تعالى،

كَذَلِكَ يَبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦٦﴾

“Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Ayah Zake mpate kufahamu”.

Pindi alipotaja yaliyokuwa ndani ya sura hii tukufu, hukumu madhubuti na sheria zilizotatiwa zenye Baraka, hivyo Allah تعالى Anawatanabahisha waja Wake na Kuwaelezea Aya Zake kwa wazi kabisa ili waweze kuzingatia na kufahamu maana zake.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَإِذَا كَانُوا مَعَهُ عَلَىٰ أَمْرٍ جَامِعٍ لَّمْ يَذْهَبُوا حَتَّىٰ يَسْتَأْذِنُوهُ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ فَإِذَا أَسْتَأْذِنُوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأَذَنَ لِمَن شِئْتَ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ اللَّهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ

رَّحِيمٌ ﴿٦٦﴾

62. “Hakika Waumini wa kweli ni waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na wanapokuwa pamoja naye kwa jambo la kuwahusu wote hawaondoki mpaka wamtake ruhusa. Kwa hakika wale wanaokuomba ruhusa, hao ndio wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na wakikuomba ruhusa kwa baadhi ya kazi zao, mruhusu umtakaye miongoni mwao, uwaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.

Kutaka Idhini ya Wanapokuwa Katika Mnasaba wa Jambo Moja

Na hii pia ni adabu ambayo Allah تعالى Amewaongoza kwayo waja Wake Waumini. Kama vile Alivyowaamuru watake idhini wanapotaka kuingia nyumbani, hivyo hivyo Aliwaamuru kutaka ruhusa wanapoondoka hasa wanapokuwa wanafanya shughuli pamoja na Mtume, kama vile Swala ya

¹ Ad-Durr al-Manthuur 6:228.

Ijumaa, Idi au Swala za *Jamaa'ah*, au mkutano kwa ajili ya kushauriana na mfano wake. Allah تعالى Aliwaamuru wasiondoke katika hali hizi mpaka wapate idhini. Ikiwa watafanya hilo (la kutaka ruhusa), basi watakuwa Waumini kamili. Baada ya hapo Allah تعالى Alimuamuru Mtume Wake ﷺ kutoa ruhusa pale anapombwa, ikiwa atataka. Akasema:

فَأَذِنَ لِمَن شِئْتِ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ اللَّهُ

“Mruhusu umtakaye miongoni mwao, uwaombe msamaha kwa Allah”.

Abu Dawud amepokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema:

«إِذَا انْتَهَى أَحَدُكُمْ إِلَى الْمَجْلِسِ فَلْيَسَلِّمْ، فَإِذَا أَرَادَ أَنْ يَقُومَ فَلْيَسَلِّمْ، فَلْيَسَلِّمِ الْأُولَى بِأَحَقِّ مِنَ الْآخِرَةِ»

*“Pindi yeyote miongoni mwenu anapofika kwenye kikao, basi atoe salamu, na anapotaka kuondoka, pia atoe salamu. Hakika salamu ya kwanza si muhimu zaidi kuliko ile ya pili”.*¹

Hii pia ameipokea at-Tirmidhiy na An-Nasaa'iy. At-Tirmidhiy amesema: “Hii ni Hadithi Hasan”.²

لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا ۗ قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنْكُمْ لِوَاذًا ۗ فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾

63. “Msifanye wito wa Mtume baina yenu ni kama wito wa nyinyi kwa nyinyi. Hakika Allah Anawajua miongoni mwenu wanaondoka kwa uficho. Basi na watahadhari wanaokhalifu Amri Yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu”.

¹ Abu Daawuud 5:386.

² *Tuhfat ul-Awadhyy* 7:485 na An-Nass 'iy katika *Al-Kubraa* 6:100.

Ubainifu wa Kuzungumza na Mtume ﷺ

Amepokea Ad-Dhahhaak kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Walikuwa wakiita ewe Muhammad au ewe Abul Qaasim, Allah تعالى Akawakataza hilo kwa kumtukuza Mtume Wake na Akawaambia waite, “Ewe Nabii wa Allah! Ewe Mtume wa Allah”¹ Na hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid na Said ibn Jubayr.² Na amesema Qataadah: “Allah تعالى Aliamuru kuwa Mtume Wake ﷺ lazima astahiwe, atukuzwe, aadhimishwe na aheshimiwe”³ Na amesema Muqaatil kuhusu Kauli Yake:

لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا

“Msifanye wito wa Mtume baina yenu ni kama wito wa nyinyi kwa nyinyi”.

Mnapomuita, Msiseme: “Ewe Muhammad” wala musimuite “Ewe mtoto wa ‘Abdullah’ lakini mheshimuni na semeni: “Ewe Nabii wa Allah! Ewe Mtume wa Allah!” Na mtazamo wa pili katika hilo, ni kuwa maana yake, ‘Msiitakidi ya kwamba dua yake dhidi ya mtu mwingine ni kama dua ya mtu mwingine anapoomba dhidi ya mwenziwe, kwani dua yake inajibiwa. Hivyo, tahadharini sana kulaaniwa naye mukaangamia. Ameitaja Hadithi hii Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn 'Abbaas, Al-Hasan, Al-Basriy na 'Atwiyyah Al-'Awfi رضي الله عنهم. Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.³ Na Kauli Yake:

قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنْكُمْ

“Hakika Allah Anawajua vyema wale miongoni mwenu wanaoondoka kwa uficho”

Amesema Muqaatil ibn Hayyaan: “Hao ni wanafiki ambao walikuwa wanaona uzito mkubwa kusikiliza Khutba ya Ijumaa, hivyo wakawa wanajificha nyuma ya baadhi ya Maswahaba wa Muhammad ﷺ hadi wanapotoka Msikitini. Na ilikuwa mtu haruhusiwi kutoka Msikitini ila kwa idhini ya Mtume ﷺ. Na ilikuwa anapotaka mmoja wao kutoka huashiria kwa kidole chake kwa Mtume ﷺ, na

¹ Ad-Durr al-Manthuur 6:230. Sanadi yake ni dhaifu.

² Atw-Twabariy 19:230.

³ Atw-Twabariy 19:230.

Mtume ﷺ alikuwa akiwapa idhini bila ya mtu kuzungumza. Hiyo ni kwa kuwa lau atazungumza mmoja wao na hali ya kuwa Mtume ﷺ anahutubu basi Ijumaa yake itabilika.”¹ Na amesema As-Suddiy: “Walikuwa wanapokuwa naye katika Swala ya Jamaa’ah, walijificha nyuma baadhi yao kwa wengine mpaka anakuwa hawaoni”.

Kukatazwa kukhalifu Amri ya Mtume ﷺ

Na Kauli Yake:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ

“Basi na watahadhari wale wanaokhalifu Amri yake.”

Maana yake: Amri ya Mtume ﷺ, na ni njia yake, Sunnah na Sheria yake. Maneno yote na kauli zote zitapimwa kwa maneno yake na amali zake; yanayoafikiana naye yatakubaliwa, na yanayokhalifiana naye yanarudishwa kwa msemaji wake na mtendaji wake. Kama ilivyothibiti katika Sahihi mbili na wengineo kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا فَهُوَ رَدٌّ»

“Mwenye kufanya amali isiyokuwa nje ya Sharia ya Uislamu, itakataliwa amali hiyo.”²

Hii ina maana kuwa atahadhari sana pamoja na kuogopa yule anayekwenda kinyume na Sheria ya Mtume ﷺ kwa siri na kwa dhahiri.

أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ

“Kupatwa na msiba.”

Maana yake: Katika nyoyo zao kwa kuingiwa na ukafiri au unafiki au *bida’h* (uzushi).

¹ Aduru Al-Manthur 6:231.

² Fat-h Al-Baariy 4: 416 na Muslim 3: 1343.

أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٤﴾

“Au ikawapata adhabu chungu”,

Maana yake: Hapa duniani kwa kuuawa au kukabiliwa na *Hadd* (adhabu maalumu iliyowekwa na Sheria) au kifungo au mfano wake. Imepokewa na Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَثَلِي وَمَثَلُكُمْ كَمَثَلِ رَجُلٍ اسْتَوْقَدَ نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهَا جَعَلَ الْفَرَاشُ وَهَذِهِ الدَّوَابُّ اللَّائِي يَقَعْنَ فِي النَّارِ يَقَعْنَ فِيهَا، وَجَعَلَ يَحْجِرُهُنَّ وَيَغْلِبُهُ فَيَقْتَحِمْنَ فِيهَا - قَالَ: - فَذَلِكَ مَثَلِي وَمَثَلُكُمْ، أَنَا أَخِذُ بِحُجْرِكُمْ عَنِ النَّارِ هَلُمَّ عَنِ النَّارِ، فَتَغْلِبُونِي وَتَقْتَحِمُونَ فِيهَا»

“Mfano wangu na wenu ni mfano wa mtu aliyeoka moto, na ulipoangazia pembezoni mwake, nondo na hawa wanyama wengine wanaoangukia ndani ya moto, wanaanguka ndani yake. Naye akiwazuilia wanamshinda, na wanaanguka ndani yake”. Akasema: “Huu ndio mfano wangu na nyinyi. Hakika mimi najaribu kuwazuilia na kuwaweka mbali na moto, lakini mukanishinda na mukawa munaingia ndani”.

Hii pia ameipokea Al-Bukhari na Muslim¹

أَلَا إِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ قَدْ يَعْلَمُ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ وَيَوْمَ يُرْجَعُونَ إِلَيْهِ
فَيَنْتَبِهُهُمْ بِمَا عَمِلُوا ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٦٤﴾

64. “Jueni kuwa hakika ni vya Allah vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Hakika Yeye Anajua mliyo nayo. Na siku watakaporudishwa Kwake, Atawaeleza waliyoyafanya. Na Allah ni Mjuzi mno wa kila kitu”.

¹ Ahmad 2:312 na Muslim 2284.

Allah تعالی Anajua mliyo nayo

Allah تعالی Anatuambia kuwa, Yeye ni Mfalme wa mbingu na ardhi, na kuwa Yeye ni Mjuzi wa yasiyoonekana na yenye kuonekana. Naye pia ni Mjuzi kwa wanayoyafanya waja Wake kwa siri zao au dhahiri zao. Akasema:

قَدْ يَعْلَمُ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ

“Hakika Yeye Anajua mliyonayo.”

Na neno Qad ni la kuhakikisha, hivyo kutokuwa na shaka ya aina yoyote, Hii ni kama Alivyosema kabla yake,

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٦٧﴾

“Na umtegemee Mtukufu Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu.”

Na Allah تعالی Amesema,

إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٨﴾

“Hakika Yeye Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.” (26:17-20).

Na Kauli yake Allah تعالی:

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا

إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا

أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦٩﴾

“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi. (10:61)

Aidha Allah تعالی Amesema,

أَفَمَنْ هُوَ قَائِمٌ عَلَىٰ كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ

**“Je! ni nani Anayeisimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma...?”
(13:33)**

Anaona yote ya waja wake wanayofanya, mazuri na mabaya. Na Allah تعالى Amesema:

أَلَا حِينَ يَسْتَعْشُونَ يُبَاهِئُهُمْ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٥﴾

**“Juani kuwa wanapojigubika nguo zao Yeye Anajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.”
(11:5).**

Na Amesema:

سَوَاءٌ مِّنْكُمْ مَّنْ أَسْرَأَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ

**“Ni sawa anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhihirisha.”
(13:10)**

Aidha Allah تعالى Amesema,

* وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَىٰ اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۗ كُلٌّ فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٧﴾

“Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:7).

Aidha Amesema;

* وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۗ وَمَا تَسْقُطُ مِنَ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٧٠﴾

“Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye Anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila

Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha.” (6:59).

Na zipo Aya na Hadithi nyingi sana katika maudhui hii. Na Kauli Yake:

وَيَوْمَ يُرْجَعُونَ إِلَيْهِ

“Na siku mtakaporudishwa Kwake.”

Maana yake: Siku ambayo viumbe watarejeshwa Kwake Allah تعالى, nayo ni Siku ya Kiyama.

فَيُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا

“Naye Atawaeleza mliyoyafanya.”

Maana yake: Allah تعالى Atawaeleza waja Wake yale waliyoyafanya duniani, matukufu, duni na makubwa na madogo.

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

يُنَبِّئُوا إِلَّا نَسْنُ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمُوا وَأَخْرَجَ

“Siku hiyo ataambiwa mwanadamu aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha.” (75: 13).

Na Akasema:

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَا لِ هَذَا
الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا وَلَا يَظْلُمُ
رَبُّكَ أَحَدًا

“Na kitawekwa kitabu. Basi utawaona wakosefu ni wenye kuogopa yaliyomo humo. Na watasema: “Ole wetu! Kinani kitabu hiki?! Hakiachi dogo wala kubwa ila kimelehibiti?” Na watayakuta waliyoyatenda yamehudhuria hapo. Na Mola wako Mlezi Hamdhulumu yeyote.” (18:49).

Na kwa hilo pia Amesema:

وَيَوْمَ يُرْجَعُونَ إِلَيْهِ فَيُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوا ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٦٤﴾

***“Na siku watakaporudishwa Kwake, Atawaeleza waliyoyafanya.
Na Allah ni Mjuzi mno wa kila kitu.”***

Na Shukrani pamoja na Sifa zote njema Anastahiki Allah تعالی, Mola Mlezi wa walimwengu wote, na tunamuomba atusaidie kufikia utimilifu.

Mwisho wa Tafsiri ya Suratun Nuur, Allah تعالی Ndiye Mwenye Kustahiki Shukrani, Sifa na Ihsani.

* * *

Tafsiri ya Suratul Furqaan

Sura ya 25

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الْفُرْقَانِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿١﴾ الَّذِي لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمَلِكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٢﴾ وَأَخَذُوا مِنْ دُونِهِ ءِالِهَةً لَا يَخْلُقُونَ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ وَلَا يَمْلِكُونَ لِأَنفُسِهِمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا وَلَا يَمْلِكُونَ مَوْتًا وَلَا حَيَاةً وَلَا نُشُورًا ﴿٣﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَذَا إِلَّا إِفْكٌ افْتَرَاهُ وَأَعَانَهُ عَلَيْهِ قَوْمٌ ءِآخَرُونَ فَقَدْ جَاءُوا ظُلْمًا وَزُورًا ﴿٤﴾ وَقَالُوا أَسْطِطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٥﴾ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٦﴾ قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٧﴾

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿١﴾ الَّذِي لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمَلِكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٢﴾

1. Ametukuka Aliyete-remsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.

2. Ambaye ni Wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala Hakuwa na mwana, wala Hakuwa na mshirika katika Ufalme, na Akaumba kila kitu na Akakikadiria kwa kipimo.

Utukufu wa Allah تعالى

Allah تعالى hapa Anajisifu Mwenyewe kwa Aliyoteremsha kwa Mtume Wake Mtukufu, Qur'ani Tukufu. Hii ni kama ile Aya inayosema:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجًا ۖ قَيِّمًا لِّيُنذِرَ بَأْسًا شَدِيدًا مِّنْ لَّدُنْهُ وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا حَسَنًا ۖ

“Kuhimidiwa ni kwa Allah, Ambaye Amemteremshia mja Wake Kitabu, wala Hakukifanya kina upogo. Kimenyooka sawa, ili kitoe onyo kali kutoka Kwake, na kiwabashirie Waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri”. (18:1-2)

Na hapa Anasema:

تَبَارَكَ

“Ametukuka.”

Kitenzi hiki kimetumika hapa kuwa Baraka Zake ni za kuendelea, thabiti na za kudumu milele.

الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ

“Ambaye Aliyeteremsha Furqani.”

Nazzala ni kitenzi kinachomaanisha kurudia mara kwa mara na kwa wingi. Hii ni kama Kauli Yake:

وَالْكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي أَنْزَلَ مِنْ قَبْلُ

“Na Kitabu Alichoteremsha juu ya Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha kabla yake.” (4:136).

Hivyo ni kwa vitabu vilivyotangulia vilikuwa vikiteremshwa mara moja, lakini Qur'ani imeteremshwa polepole, kidogo kidogo, Aya moja baada ya nyengine, hukumu baada ya hukumu, Sura baada ya Sura.

Na kuteremshwa namna hii ni ufasaha na umbuji na ni ishara ya uangalifu mkubwa kwa Aliyeteremshiwa, kama Alivyosema Allah تعالى baadaye katika Surah hii hii:

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْآنُ جُمْلَةً وَاحِدَةً ۖ كَذَلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ ۗ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلًا ﴿٣٣﴾ وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا ﴿٣٤﴾

“Na wakasema waliokufuru: Kwa nini hakuteremshiwa Qur’ani kwa jumla moja? Hayo ni hivyo ili Tuuthibitisha moyo wako, na ndio Tumeisoma kwa mafungu. Wala hawatakuletea mfano wowote, ila na Sisi Tutakuletea (jawabu) kwa haki, na tafsiri iliyo bora.” (25:32-33).

Kwa hiyo Surah hii iliitwa hapa *Al-Furqaan* kwa kuwa inapambanua baina ya haki na batili, uongofu na upotevu, sawa na makosa, na halali na haramu.

عَلَىٰ عِبْدِهِ

“Kwa mja Wake.” Huu wasifu ni wa kusifu na kutukuza kwani Mtume ﷺ amehusishwa na Allah تعالى, kwa kutambulishwa kwa wasifu wa kuwa ni mja Wake. Allah تعالى pia Alimtambulisha kwa njia hii pale Alipotaja tukio tukufu miongoni mwa matukio matukufu, usiku wa *Israa’*, kama Alivyosema:

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلًا

“Ametakasika Aliyemchukua mja Wake usiku mmoja.” (17:1).

Na kama Alivyomtambulisha kwa njia hii pale Alipoeleza wasifu wake jinsi alivyosimama na kumuita Yeye:

وَأَنَّهُ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾

“Na hakika Mja wa Mwenyezi Mungu aliposimama kumwomba, wao walikuwa karibu kumzonga!” (72: 19)

Wasifu huu pia unatumiwa hapa, pale Allah تعالى Alipoelezea jinsi Kitabu kilipoteremshwa kwake pamoja na kushuka Malaika.

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِ

“Ametukuka Aliyeteremsha Furqani kwa mja Wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.”

لِيَكُونَ لِلْعَلَمِينَ نَذِيرًا ﴿١٤﴾

“Ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.”

Maana yake: Amemchagua yeye kumpa Kitabu hiki kinachoelezea kwa kina (tafsiri), kinaweka mambo wazi wazi na bila ya kuwa na utata, ambacho,

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿١٥﴾

“Haitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Ahimidiwaye.” (41:42).

Yule Aliyekileta Amekifanya kuwa kipambanuzi kikuu, hakika Amemchagua yeye kufikisha risala kwa wenye kutaka kukaa chini ya vivuli vya miti na wale wanaoishi ardhini, kama alivyosema Mtume ﷺ:

«بُعِثْتُ إِلَى الْأَخْمَرِ وَالْأَسْوَدِ»

“Nimetumwa kwa wekundu na weusi.”¹

Na amesema:

«إِنِّي أُعْطِيتُ حَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ قَبْلِي»

“Hakika mimi nimepewa mambo matano ambayo hakupewa Nabii yeyote kabla yangu”.

Na akataja miongoni mwayo:

«كَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

“Alikuwa Nabii akitumwa kwa watu wake hasa, na mimi nimetumwa kwa wanadamu wote kwa ujumla”.²

Na Allah تعالی Anasema:

قُلْ يَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote”.
(7:158).

¹ Ahmad 5:145.

² Fat’hul Al-Bari 1/634.

Hii inamaanisha kuwa Yeye Aliyenituma Ndiye Mfalme wa mbingu na ardhi Ambaye Anakiambia kitu chochote kuwa na kikawa, Naye Ndiye Mwenye Kuhuisha na Kufisha. Na hapa ndivyo Alivyosema:

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ

“Ambaye ni Wake Ufalme wa mbingu na ardhi, wala Hakuwa na mwana, wala Hakuwa na mshirika katika Ufalme.”

Ameivua Nafsi Yake kwa kuwa na mtoto (kuzaa) na pia kuwa na mshirika. Kisha Akatupa habari kuwa Yeye:

وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا

“Na Akaumba kila kitu na Akakikadiria kwa kipimo.”

Hii ina maana kuwa kila kitu mbali na Yeye kimeumbwa na ni chenye kuwa chini Yake. Yeye Ndiye Muumbaji wa kila kitu na Ndiye Mola Mlezi na Mwenye Kumiliki na Muabudiwa na kila kitu kipo chini ya Mamlaka Yake, na Upelekeshaji Wake, na vinyenyenyekea Kwake na Ndiye Mwenye Kuvikadiria.

وَأَتَّخِذُوا مِن دُونِي ءَالِهَةً لَا مَخْلُوقَاتٍ شَيْئًا وَهُمْ مَخْلُوقَاتٌ وَلَا يَمْلِكُونَ لِأَنفُسِهِمْ

ضَرًّا وَلَا نَفْعًا وَلَا يَمْلِكُونَ مَوْتًا وَلَا حَيَاةً وَلَا نُشُورًا

3. “Na wamechukua badala Yake miungu ambayo haiumbi chochote, bali hiyo inaumbwa, haijamilikii nafsi zao madhara wala manufaa, wala haimiliki mauti, wala uhai, wala kufufuka”.

Ubainifu Upumbavu wa Washirikina

Allah تعالی Anatueleza kuhusu ujinga wa washirikina kwa kuabudu kwao miungu badala ya Allah تعالی, ambaye ni Muumbaji wa kila kitu, Ambaye Ndiye Mwenye Kumiliki mambo ya vitu vyote; Ambaye Anachotaka kinakuwa na Asichotaka basi hakiwi. Na pamoja na hayo, bado waliabudu masanamu ambayo hayana uwezo wa kuumba hata bawa la mbu, bali yenyewe yameumbwa. Wao hawamiliki uwezo wa kudhuru wala kuleta manufaa kwa wao wenyewe, vipi tena wataweza kufanya jambo lolote kwa wanaoabaabudu? Na wao:

وَلَا يَمْلِكُونَ مَوْتًا وَلَا حَيَاةً وَلَا نُشُورًا ﴿٢٨﴾

“Wala hawamiliki mauti, wala uhai, wala kufufuka.”

Maana yake: Hawawezi wao kufanya chochote kati ya mambo hayo; uwezo huo unamilikiwa na Allah تعالى Peke Yake Ambaye Anahuisha na Kufisha, na Yeye Ndiye Atakayerudishia uhai viumbe Wake wa mwanzo na mwisho siku ya Kiyama.

مَا خَلَقْنَاكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ ۚ

“Hakukuwa Kuumbwa kwenu wala Kufufuliwa kwenu ila kama kitu kimoja ...” (31: 28).

Hii ni kama Kauli Yake:

وَمَا أَمَرْنَا إِلَّا وَاحِدَةً كَلِمَةً بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾

“Na hakukuwa (kupitisha) Amri Yetu ila ni mara moja (tu hivi) kama kupepesa jicho kufumba na kufumbua.” (54: 50).

Na Kauli Yake:

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٤﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٣﴾

“Kwa hakika hicho (Kiyama) kitakuwa kwa kupigwa ukelele mmoja tu. Mara wao (viumbe wote) watakuwa katika ardhi mpya.” (79:13-14). Na pia:

إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٥٣﴾

“Haitakuwa ila ukelele mmoja tu, tahamaki wote wamehudhurishwa mbele Yetu.” (37:53). Na pia:

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ فَإِذَا هُمْ يَنْظُرُونَ ﴿١٩﴾

“Huko kufufuliwa utakuwa ni ukelele mmoja tu, mara wanaona Kiyama kimefika.” (36:19).

Yeye Ndiye Allah تعالى Ambaye hakuna Mungu mwengine wa kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Yeye. Na wala hakuna Mola mwengine isipokuwa Yeye wa Pekee. Na ibada haifai kutekelezwa kwa mwengine isipokuwa Kwake Yeye. Kwa kuwa Analolitaka huwa, na Asilolitaka haliwi. Yeye Hana Mwana wala mzazi. Hamna Mshirika mwenza wala wa kulingana Naye. Hana msaidizi wala waziri. Bali Yeye ni wa Pekee Anayekusudiwa kwa shida zote, Ambaye Hakuzaa wala Hakuzaliwa, na wala Hakufanana na kiumbe chochote.

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ هَذَا إِلَّا إِفْكٌ وَإِفْكٌ أَفْتَرْتَهُ وَأَعَانَهُ عَلَيْهِ قَوْمٌ آخَرُونَ فَقَدْ جَاءُوا ظُلْمًا
وَزُورًا ﴿١٠﴾ وَقَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿١١﴾ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿١٢﴾ قُلْ
أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٣﴾

4. “Na wamesema waliokufuru: Haya si chochote ila ni uzushi alio uzua, na wamemsaidia kwa haya watu wengine! Hakika hawa wamekuja na dhulma na uwongo.

5. Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni. Sema: Ameyateremsha haya Ajuaye siri za katika mbingu na ardhi.

6. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”

Kauli za makafiri kuhusu Qur’ani

Allah تعالى Anatujulisha ule upumbavu wa akili za kijinga za makafiri kwa kauli yao kuhusu:

إِنَّ هَذَا إِلَّا إِفْكٌ

“Haya si chochote ila ni uzushi.”

Kumaanisha uwongo.

أَفْتَرْتَهُ

“Aliouzua.”

Hii ni kumaanisha kuwa Mtume ﷺ ndiye aliyezua uwongo huo.

وَأَعَانَهُ عَلَيْهِ قَوْمٌ آخَرُونَ

“Na wamemsaidia kwa haya watu wengine!”

Hii inamaanisha alitaka msaada kwa watu wengine katika kuikusanya. Allah تعالی Akasema:

فَقَدَّ جَاءُوا ظُلْمًا وَزُورًا ﴿١٠﴾

“Hakika hawa wamekuja na dhulma na uwongo.”

Ukweli ni kuwa wao ndio waliozua maneno ya uwongo, na hali wanajua kuwa huo wao ndio uwongo na wanautambia kuwa huo ni uwongo kwa nafsi zao wenyewe kwa wanaodai. Hapo wakasema:

وَقَالُوا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ أَكْتَبَهَا

“Na wakasema, Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha.”

Wakimaanisha kuwa watu wa awali ndio walioandika, naye Mtume ﷺ amenakili kutoka kwao.

فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ

“Nazo anasomewa (na kutolewa imla kwake).”

Maana yake: Anazosomewa (na huku anasikiliza). Na anasomewa,

بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿١١﴾

“Asubuhi na jioni.”

Maana yake: Mwanzo na mwisho wa mchana. Na maneno haya ni kwa sababu ya upumbavu wao na uwongo pamoja na kuzua kwao, jambo ambalo kila mmoja anaelewa na kujua uwongo wao. Hakika inaeleweka kwa mapokezi mengi kuwa Muhammad, Mtume ﷺ alikuwa hajui kusoma wala kuandika, mwanzo na mwisho wa uhai wa maisha yake. Alikuwa miongoni mwao kwa muda wa miaka arobaini, toka kuzaliwa mpaka wakati alipopewa Utume. Walijua yote yanayomhusu, kuingia na kutoka kwake na ukweli na uadilifu wake, wema na uaminifu wake na kujitenga kwake na uwongo, uasherati na mengine yote maovu. Hata wao walikuwa wakimuita katika utoto wake, mpaka alipopewa Utume, *Al-amiin* (Muaminifu) kwa kuwa walikuwa wakijua ukweli

na wema wake. Pale Allah تعالى Alipomkirimu kwa yale Aliyomkirimu nayo walianza kumfanyia uadui na kumzulia madai haya yote ambayo kila mwenye akili anajua kuwa yeye hana hatia yoyote. Hawakuwa na hakika wamtuhumu kwa lipi. Wakati mwengine walikuwa wanasema kuwa yeye ni mchawi, na mara nyengine wakisema kuwa ni mshairi. Na mara nyengine tena kuwa yeye ni mwendawazimu na mara nyengine tena kuwa ni muongo. Allah تعالى Akasema:

﴿أَنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا﴾

“Tazama vipi wanavyokupigia mifano. Basi wamepotea. Kwa hivyo hawawezi kuipata njia.” (17:48).

Na Akasema Aliyetukuka kwa Kuwajibu kwa ukaidi wao hapa kwa kule kuzua kwao:

﴿قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ﴾

“Sema: Ameyateremsha haya Ajuaye siri za katika mbingu na ardhi.”

Hii inamaanisha kuwa Ameteremsha Qur’ani ambayo imekusanya habari za watu wa mwanzo na waliokuja baadaye, habari ya uhakika, juu ya yaliyopita na yale yajayo.

﴿الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ﴾

“Ambaye kwamba Anajua siri.”

Maana yake: Allah تعالى Ndiye Mwenye Elimu ya ghaibu za mbingu na ardhi na Anajua siri zote kama vile Anavyojua yale ya dhahiri. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

﴿إِنَّهُمْ كَانُوا غُفُورًا رَحِيمًا﴾

“Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”

Huku ni kuwalingania ili warudi kwa Allah تعالى na kutubia kutokana wa makosa yao, na pia kuwapasha habari kuwa Yeye Allah ni Mwenye Rehema nyingi na Subira Yake ni kubwa na kuwa yeyote anayetaka msamaha Kwake basi Yeye Humsamehe. Hivyo, hawa watu mbali na uwongo wao, kuzua kwao, uovu wao na ukafiri wao na inadi na kauli zao kuhusu Mtume na Qur’ani, bado Allah تعالى Anawalingania warudi na kutubia na kuacha madhambi yao, na waje kwenye Uislamu na uongofu wa kweli. Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى:

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهُ وَاحِدٌ وَإِنْ لَمْ يَنْتَهُوا
عَمَّا يَقُولُونَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٦﴾ أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى
اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونَهُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٧٧﴾

“Kwa hakika wamekufuru waliosema: Allah ni wa tatu wa utatu. Hali hakuna muabudiwa ila Mwenyezi Mungu Mmoja tu. Na ikiwa hawaachi hayo wanayoyasema, kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanaokufuru. Je, hawatubu kwa Allah na waka muomba msamaha? Na Allah ni Mwenye Maghufira na Mwenye Kurehemu.” (5:73-74).

Na Amesema Aliyetukuka:

إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَتُوبُوا فَلَهُمْ عَذَابٌ جَهَنَّمَ وَهُمْ عَذَابٌ
الْحَرِيقِ ﴿٨٥﴾

“Hakika wale walio waadhibu Waumini wanaume na Waumini wanawake, kisha wasitubie basi watapata adhabu ya Jahanamu na watapata adhabu ya kuungua barabara.” (85:10).

Amesema Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى: “Tizama huruma na ukarimu huu, wameua Marafiki Zake, Naye Anawaita watubie na kwa Rehema (itokayo Kwake).”

* * *

وَقَالُوا مَالِ هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ
 الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ لَوْلَا
 أَنْزَلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُونُ مَعَهُ
 نَذِيرًا ﴿٧﴾ أَوْ يُلْقَىٰ إِلَيْهِ كِتَابٌ
 تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا وَقَالَ
 الظَّالِمُونَ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا
 رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿٨﴾ أَنْظِرْ
 كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَلِ فَضَلُّوا
 فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٩﴾ تَبَارَكَ
 الَّذِي إِنْ شَاءَ جَعَلَ لَكَ خَيْرًا مِنْ
 ذَلِكَ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا
 الْأَنْهَارُ وَيَجْعَلُ لَكَ فُصُورًا ﴿١٠﴾
 بَلْ كَذَّبُوا بِالسَّاعَةِ وَأَعْتَدْنَا
 لِمَنْ كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا ﴿١١﴾
 إِذَا رَأَتْهُمْ مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ
 سَمِعُوا لَهَا تَغِيظًا وَزَفِيرًا ﴿١٢﴾
 وَإِذَا أَلْقَا مِنْهَا مَكَانًا
 صَبِيحًا مَفْرِينَ ﴿١٣﴾ دَعَوْا
 هُنَالِكَ ثُبُورًا ﴿١٤﴾ لَا تَدْعُوا
 الْيَوْمَ ثُبُورًا وَاحِدًا وَادْعُوا
 ثُبُورًا كَثِيرًا ﴿١٥﴾ قُلْ أَدْرِيكَ
 خَيْرٌ أَمْ جَنَّةُ الْخُلْدِ
 الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ ؕ كَانَتْ لَهُمْ
 جَزَاءً وَمَصِيرًا ﴿١٦﴾ هُمْ
 فِيهَا مَا يَشَاءُونَ خَالِدِينَ ؕ كَاتَبَ
 عَلَىٰ رَبِّكَ وَعَدَا مَسْئُولًا ﴿١٧﴾
 وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ
 مِنْ دُونِ اللَّهِ فَيَقُولُ هَٰ أَنتُمْ
 أَضَلَلْتُمْ عِبَادِي هَٰتُولَٰئِكَ أَمْ
 هُمْ ضَلُّوا السَّبِيلَ ﴿١٨﴾ قَالُوا
 سُبْحٰنَكَ مَا كَانَ يُدْبِعِي لَنَا
 أَنْ نَتَّخِذَ مِنْ دُونِكَ مِنْ أَوْلِيَاءَ
 وَلَكِنْ مَتَّعْتَهُمْ وَعَٰبَاءَهُمْ
 حَتَّىٰ نَسُوا الذِّكْرَ وَكَانُوا
 قَوْمًا بُورًا ﴿١٩﴾ فَقَدْ كَذَّبْتُمْ
 بِمَا تَقُولُونَ فَمَا تَسْتَطِيعُونَ
 صَرْفًا وَلَا نَصْرًا ؕ وَمَنْ يَظْلِمِ
 مِنْكُمْ نُذِقْهُ عَذَابًا كَثِيرًا ﴿٢٠﴾

وَقَالُوا مَالِ هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ
 الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ لَوْلَا
 أَنْزَلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُونُ مَعَهُ
 نَذِيرًا ﴿٧﴾ أَوْ يُلْقَىٰ إِلَيْهِ كِتَابٌ
 تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا وَقَالَ
 الظَّالِمُونَ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا
 رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿٨﴾ أَنْظِرْ
 كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَلِ فَضَلُّوا
 فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٩﴾ تَبَارَكَ
 الَّذِي إِنْ شَاءَ جَعَلَ لَكَ خَيْرًا مِنْ ذَلِكَ
 جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ
 وَيَجْعَلُ لَكَ فُصُورًا ﴿١٠﴾ بَلْ كَذَّبُوا
 بِالسَّاعَةِ وَأَعْتَدْنَا لِمَنْ كَذَّبَ
 بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا ﴿١١﴾ إِذَا رَأَتْهُمْ
 مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ سَمِعُوا لَهَا
 تَغِيظًا وَزَفِيرًا ﴿١٢﴾ وَإِذَا أَلْقَا
 مِنْهَا مَكَانًا صَبِيحًا
 مَفْرِينَ ﴿١٣﴾ دَعَوْا هُنَالِكَ
 ثُبُورًا ﴿١٤﴾ لَا تَدْعُوا الْيَوْمَ
 ثُبُورًا وَاحِدًا وَادْعُوا
 ثُبُورًا كَثِيرًا ﴿١٥﴾

7. "Na wakasema: Ana nini Mtume huyu? Anakula

chakula, na anatembea masokoni! Mbona hakuteremshiwa Malaika akawa mwonyaji pamoja naye?

8. Au akaangushiwa hazina juu yake, au akawa na bustani ale katika hiyo? Wakasema madhalimu: Nyinyi hamumfuati ila mtu aliyerogwa.

9. Tazama jinsi wanavyokupigia mfano. Basi wamepotea, wala hawataiweza njia.

10. Ametukuka ambaye akitaka Atakujaaliya yaliyo bora kuliko hayo, nazo ni bustani zipitazo mito kati yake, na Atakujaalia majumba ya fahari.

11. Bali wanaikanusha Saa (Siku ya Kiyama). Na Sisi Tumemuandalia Moto mkali kabisa huyo mwenye kuikanusha Saa.

12. Ule moto ukiwaona tangu mahali mbali wao watasikia hasira yake na ngurumo yake.

13. Na watakapotupwa humo mahali dhiki, hali wamefungwa, wataomba wafe.

14. Msiombe kufa mara moja tu, bali mfe mara nyingi!"

Kauli za Makafiri Kumhusu Mtume na Majibu Yao na Kubainisha Khatima Yao

Anatupasha habari Aliyetukuka kuhusu ukaidi wa makafiri na kukadhibisha kwao haki bila ya hoja wala dalili kutoka kwao. Na hakika udhuru wao ni:

مَا لِي هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَامَ

"Ana nini Mtume huyu? Anakula chakula."

Hapa wanamaanisha kama tunavyokula sisi, naye anahitaji chakula kama tunavyokihitaji sisi. Na pia,

وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ

"Na anatembea masokoni!" Maana yake: Anazunguka ndani yake na kufanya biashara na kutafuta riziki.

لَوْلَا أَنْزَلَ إِلَيْنَا مَلَكٌ فَيَكُونُ مَعَهُ نَذِيرًا ﴿٧﴾

“Mbona hakuteremshiwa Malaika akawa mwonyaji pamoja naye?”

Hawa watu wanasema, kwa nini hateremshwi Malaika akaja kwake kutoka kwa Allah تعالى, ili awe ni shahidi kuwa lile dai lake ni la kweli? Hivi ni kama alivyosema Firauni:

لَوْلَا أُلْقِيَ عَلَيْهِ أَسْوِرَةٌ مِّنْ ذَهَبٍ أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَأِكَةُ مُقْتَرِبِينَ ﴿٥٣﴾

“Basi mbona hakuvishwa vikuku vya dhahabu, au kuja Malaika pamoja naye wakimfuata?” (43:53)

Na hivyo kauli za hawa zipo sawa, mioyo imefanana. Hivyo wakasema: “Au akaangushiwa hazina juu yake.” Yaani hazina ambayo anaweza kuitumia kwa mahitaji yake.

أَوْ تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا

“Au akawa na bustani ale katika hiyo?”

Hii inamaanisha bustani ambayo itamfuata anapokwenda. Na haya yote ni sahali sana kwa Allah تعالى, lakini Yeye Ana Hikima Yake kwa Kuacha Kufanya hayo yote, Naye Ana hoja kamili na nzito.

وَقَالَ الظَّالِمُونَ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿٦١﴾

“Wakasema madhalimu: Nyinyi hamumfuati ila mtu aliyerogwa.”

Allah تعالى Anasema:

أَنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَلَ فَضَلُّوا

“Tazama jinsi wanavyokupigia mfano. Basi wamepotea.”

Hii ina maana kuwa wamekuja na wanayokutuhumu nayo na wanaku kadhibisha pale waliposema wewe ni mchawi au umerogwa au mwendawazimu au muongo au mshairi. Na zote hizo ni kauli ambazo ni batili na ni za uwongo, kwani kila mwenye ufahamu mchache na akili anafahamu kuwa uwongo wao na kuzua kwao katika hilo. Hivyo Akasema:

فَضَّلُوا

“Basi wamepotea.”

Kutokana na njia ya uwongofu.

فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا

“Wala hawataiweza njia.”

Na hiyo ni kuwa kila anayetoka katika haki na njia ya uwongofu, hakika yeye amepotea kila atakapoelekea, kwani haki ni moja na mfumo wake ni mmoja, baadhi ya sehemu zake zikiyakinisha nyengine.

Kisha Aliyetukuka Akasema Kumwambia Mtume Wake kuwa ikiwa anataka Atamletea yeye kheri kwa yale wanayoyasema hapa duniani ziizo bora na nzuri zaidi kuliko wanazosema. Akasema:

تَبَارَكَ الَّذِي إِنْ شَاءَ جَعَلَ لَكَ خَيْرًا مِّنْ ذَلِكَ

“Ametukuka Ambaye Akitaka Atakujaalia yaliyo bora kuliko hayo.”

Mujaahid Amesema: “Hii ina maana ya hapa duniani.” Na akasema: “Maquraysh walikuwa wakiita kila nyumba iliyojengwa na mawe kuwa ni ‘Kasri’, ikiwa ni kubwa au ndogo”.¹ Na Kauli Yake:

بَلْ كَذَّبُوا بِالسَّاعَةِ

“Bali wanaikanusha Saa (Siku ya Kiyama).”

Hakika wao wanasema hivyo kwa kukanusha na inadi, sio kuwa wao wanataka kujua kwa yakini na uwongofu, lakini kukadhibisha kwao kwa Siku ya Kiyama ambayo inawafanya wao waseme waliyosema katika kauli zao hizi. Na pia:

وَأَعْتَدْنَا

“Na Sisi Tumemuandalia.”

Maana yake: Tumemuwekea tayari kabisa.

¹ Atw-Twabariy 19:243.

لِمَنْ كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا ﴿١٧﴾

“Moto mkali kabisa huyo mwenye kuikanusha Saa.”

Hiyo ni adhabu ya moto mkali sana, ambayo haiwezi kuvumilika. Na kauli Yake:

إِذَا رَأَتْهُمْ

“Unapowaona.”

Maana yake: Pindi moto utakapowaona.

مِنْ مَّكَانٍ بَعِيدٍ

“Tangu mahali mbali.”

Maana yake: Kutoka sehemu ya makutano katika Siku hiyo ya Kiyama.

سَمِعُوا هَا تَغِيظًا وَزَفِيرًا ﴿١٨﴾

“Wao watasikia hasira yake na mngurumo wake.”

Maana yake: Kwa kuwaghadhibikia wao.

Kama Allah تعالى Alivyosema,

إِذَا أَلْقُوا فِيهَا سَمِعُوا لَهَا شَهيقًا وَهِيَ تَفُورُ ﴿١٩﴾ تَكَادُ تَمَيِّزُ مِنَ الْغَيْظِ

“Watakapo tupwa humo watausikia mngurumo wake na huku inafoka. Inakaribia kupasuka kwa hasira.” (67:7-8)

Moto wa Jahannam unakaribia kukatika kutokana na hasira kali juu ya waliomkufuru Allah تعالى. Imamu Abu Jafar bin Jariri رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنهما amesema: “Hakika Mtu Atakotwa kupelekwa Motoni, Moto utajikusanya na kujiweka vizuri, Arrahman Atauambia: “Umepatwa na jambo gani?” Utasema: “Hakika Yeye anataka uwokovu kwangu mimi.” Allah تعالى atasema: Mwacheni Mja wangu. Na hakika atakotwa kupelekwa Motoni, Atasema: “Ewe Mola wangu! Sikudhania kwako wewe yote haya.” Allah تعالى atasema, “Dhana yako ilikuwa ni ipi?” Mja atasema: “Kupata huruma yako, Allah تعالى atasema: “Mwachieni mja wangu.”

Na hakika mtu atabebwa mzobemzobe kwenda Motoni. Moto utamuungurumia kama muungurumo wa nyumbu anapona Shayiri. Na utatoa sauti kali kiasi ambachp hakuna yeyote atakayekuwepo isipokuwa ataogopa.¹

Na 'Abdur-Razzaq amepokea kutoka kwa 'Ubayd ibn 'Umayr ambaye amesema kuhusu Kauli Yake:

سَمِعُوا لَهَا تَغِيظًا وَزَفِيرًا ﴿٧﴾

“Wao watasikia hasira yake na mngurumo wake.”

Amesema: “Hakika Jahannamu itatoa sauti, hakuna Malaika aliyekurubishwa kwa Allah, au Mtume aliyetumwa, isipokuwa ataangukia chini na kutetemeka. Hata Nabii Ibrahim atapiga magoti na kusema “Ewe Mola wangu leo hii si kuombi isipokuwa nafsi yangu tu.”² Kauli Yake Allah تعالى،

وَإِذَا أَلْفُؤا مِنْهَا مَكَانًا صَبِيحًا مُّفْرَيْنِ

“Na watakapotupwa humo mahali dhiki, hali wamefungwa.”

Qataadah amepokea kutoka kwa Abu Ayyub alimsikia 'Abdullah ibn 'Amr akisema: “Mfano wa ncha ya mkuki (yaani, wembamba wake).”³ Na Kauli Yake:

مُفْرَيْنِ

“Hali wamefungwa pamoja.”

Abu Swalih amesema: “Hiyo ni kuwa wamefungwa katika mabega yao.” Na hapo,

دَعَوْا هُنَالِكَ ثُبُورًا ﴿٨﴾

“Wataomba wafe.”

Maana yake: Watalia vilio vya maangamivu, majuto, hasara na kufadhaishwa. Hivyo,

لَا تَدْعُوا الْيَوْمَ ثُبُورًا وَاحِدًا وَادْعُوا ثُبُورًا كَثِيرًا ﴿٩﴾

“Msiombe kufa mara moja tu, bali mfe mara nyingi!.”

¹ Abdurrazaq 3:67.

² Addur Al-Manthur 6:240.

³ At-Twabari 19:247.

قُلْ أَذَلِكَ خَيْرٌ أَمْ جَنَّةُ الْخَالِدِينَ أَلَيْسَ وَعْدَ الْمُتَّقُونَ^٤ كَانَتْ لَهُمْ جَزَاءً وَاصِرًا ﴿٥﴾ هُمْ
فِيهَا مَا يَشَاءُونَ خَالِدِينَ كَانَتْ عَلَى رَبِّكَ وَعْدًا مَسْئُولًا ﴿٦﴾

“Sema: “Je! Haya ni bora au Pepo ya milele, ambayo wameahidiwa wachamungu, iwe kwao malipo na marejeo? Watayapata humo wayatakayo daima dawamu. Hii ni ahadi juu ya Mola wako Mlezi, inayoombwa”.

Je, Moto ndio Kheri au Pepo?

Anasema Aliyetukuka: “Ewe Muhammad hii ni hali ya wale waovu Tuliokuelezea, ambao watakokotwa kwa nyuso zao mpaka katika Moto wa Jahanamu, ambao utawapokea kwa kuwakunjia uso, kwa hasira na mingurumo. Huko watatupwa na kufungwa katika sehemu zao finyu, ambamo hawataweza kunyanyua hatua wala kuomba usaidizi na hawatakuwa na fursa ya kukimbia. Je, hii ndio kheri au Pepo ya milele ambayo Allah Amewaahidi waja Wake wema. Hiyo Amewaandalia wao kama tunu na zawadi, na malipo na marejeo kwa kumtii Yeye hapa duniani.” *“Watayapata humo wayatakayo daima dawamu”*. Miongoni mwa ladha mbalimbali kama vyakula, vinywaji, nguo, makazi, vipando na njia ya usafiri na mandhari na vyenginevyo ambavyo hakuna jicho lililoona, wala sikio lililosikia wala hisia kwenye moyo wa yeyote. Watakaa humo milele; daima na haitamalizika wala kukatika na hawatatoka humo wala kupitiwa na miaka. Na haya ni yale Aliyoyaahidi Allah تعالیٰ kwa wale Aliowabariki na wale Aliowaneemesha. Na kwa hiyo Akasema:

كَانَتْ عَلَى رَبِّكَ وَعْدًا مَسْئُولًا ﴿٦﴾

“Hii ni ahadi juu ya Mola wako Mlezi, inayoombwa”.

Yaani, ni lazima hilo litokee na iwe kama Alivyolizungumzia. Abu Ja’far ibn Jariir رحمه الله تعالیٰ kutoka kwa baadhi ya wanazuoni wa Kiarabu kuhusu maana ya Kauli Yake:

وَعْدًا مَسْئُولًا ﴿٦﴾

“Ahadi inayoombwa.”¹ Maana yake: Ahadi iliyo wajibu kutekelezwa.

¹ At-Twabari 19:247.

Na katika sehemu ya Surah hii, Allah تعالى Anataja Moto, kisha kututanabaishia hali za watu wa Peponi. Kuhusu wao Allah تعالى Ametaja katika Suratis-Swaafaat hali za watu wa Peponi, uzuri na furaha iliyomo. Kisha Akasema:

أَذَلِكْ حَيْرٌ نُّزُلًا أَمْ شَجَرَةُ الزُّقُومِ ﴿٧﴾ إِنَّا جَعَلْنَاهَا فِتْنَةً لِلظَّالِمِينَ ﴿٨﴾ إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ
فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٩﴾ طَلْعُهَا كَأَنَّهُ زُرُّوسُ الشَّيْطَانِ ﴿١٠﴾ فَلَيْسَ لَكُمْ مِنْهَا فَمَا لَعُونُ
مِنْهَا أَبْطُونَ ﴿١١﴾ ثُمَّ إِنَّ لَهُمْ عَلَيْهَا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيمٍ ﴿١٢﴾ ثُمَّ إِنَّ مَرْجِعَهُمْ لَإِلَى الْجَحِيمِ
﴿١٣﴾ إِنَّهُمْ أَلْفَوْا آبَاءَهُمْ ضَالِّينَ ﴿١٤﴾ فَهُمْ عَلَىٰ آثَرِهِمْ يُرْعُونَ ﴿١٥﴾

“Je, karibisho la namna hii silo bora au kupata mti wa zakkum (mti mchungu watakaolishwa watu wa Motoni)? Kwa yakini Sisi Tumeufanya ni adhabu ya hao madhalimu. Hakika huo ni mti unaotoka katikati ya Jahanamu. Panda za matunda yake zinatisha kana kwamba ni vichwa vya mashetani. Bila shaka wao watakula katika mti huo, na kwa huo wajaze matumbo yao. Kisha bila shaka utawathubutukia, juu ya uchungu wa mti huo, mchanganyiko wa maji ya moto. Halafu, kwa yakini, marejeo yao yatakuwa huko huko katika Jahanamu. Hakika wao waliwakuta baba zao wamepotea. Na wao pia wakaendeshwa kufuata nyayo zao (hivyo wakakataa kusikiliza maneno ya Mtume).” (37:62-70).

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ فَيَقُولُ ءَأَنْتُمْ أَضَلُّتُمْ عِبَادِيَ هَتُّوْلَاءِ أَمْ
هُمْ ضَلُّوا السَّبِيلَ ﴿١٦﴾ قَالُوا سُبْحٰنَكَ مَا كَانَ يُدْبِغِي لَنَا أَن نَّتَّخِذَ مِن دُونِكَ مِن
أَوْلِيَاءَ وَلٰكِن مَّتَّعْتَهُمْ وءَابَاءَهُمْ حَتَّىٰ نَسُوا الذِّكْرَ وَكَانُوا قَوْمًا بُورًا ﴿١٧﴾ فَقَدْ
كَذَّبْتُمْ بِمَا تَقُولُونَ فَمَا تَسْتَطِيعُونَ صِرْفًا وَلَا نَصْرًا وَمَنْ يَظْلِم مِّنكُمْ
نُذِقْهُ عَذَابًا كَبِيرًا ﴿١٨﴾

17. “Na siku Atakapowakusanya wao na hao wanaowaabudu, na Akasema: Je! Ni nyinyi mliowapoteza waja Wangu hawa, au wao wenyewe walipotea njia.”

18. Watasema: Umetakasika na upungufu! Haikutupasia sisi kuchukulia walinzi badala yako, lakini Wewe Uliwastarehesha wao na baba zao hata wakasahau kukumbuka, na wakawa watu walioangamia.

19. Basi walikukanusheni kwa mliyoyasema. Kwa hivyo hamwezi kujiondolea wala kujisaidia. Na atakayedhulumu miongoni mwenu Tutamwonjesha adhabu kubwa."

Miungu ya Washirikina itawakataa Siku ya Kiyama

Allah Aliyetukuka Anatueleza yatakayotokea Siku ya Kiyama, wakati ambapo wale makafiri waliokuwa wakiabudu vitu vingine mbali na Allah kama Malaika na wengineo watawakana vikali. Na Allah تعالى Akasema:

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ

"Na siku Atakapowakusanya wao na hao wanaowaabudu."

Mujaahid amesema: "Hawa ni "Isaa, 'Uzayr na Malaika"¹

فَيَقُولُ أَأَنْتُمْ أَضَلَلْتُمْ عِبَادِي هُنَّوَلَا

"Na atasema: Je! Ni nyinyi mliowapoteza waja wangu hawa."

Maana yake: Allah تعالى Atawaambia wale walioabudiwa: "Je, nyinyi ndio mliwalingania hawa kuwaabuduni nyinyi badala Yangu Mimi, au ilikuwa rai yao kuwaabuduni, bila ya nyinyi kuwalingania katika hilo?" Kama Allah تعالى: Alivyosema

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ ۗ أَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُوتِي إِلَهَيْنِ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ قَالَ
 سُبْحٰنَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقِّ ۗ إِن كُنْتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ ۗ تَعَلَّمَ مَا
 فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۗ إِنَّكَ أَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ ﴿١١٠﴾ مَا قُلْتُ هُمْ إِلَّا مَا
 أَمَرْتَنِي بِهِ ۗ

¹ Atw-Twabariy 19:247.

“Na pale Allah Atakaposema: Ewe ‘Isaa mtoto wa Maryam! Ati wewe uliwaambia watu: “Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Allah? Na ‘Isaa atasema: “Subhaanaka, Wewe Umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila ya shaka Umekwisha yajua. Wewe Unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yao. Hakika Wewe Ndiye Mjuzi mkubwa kwa yaliyofichikana. Sikuwaambia ila yale Uliyoni amrisha.” (5:116-117).

Na kwa hili Amesema Aliyetukuka Akitupasha habari kwa watakatoyajibu Siku ya Kiyama.

قَالُوا سُبْحَانَكَ مَا كَانَ يَنْبَغِي لَنَا أَنْ نَتَّخِذَ مِنْ دُونِكَ مِنْ أَوْلِيَاءَ

“Watasema: Umetakasika na upungufu! Haikutupasia sisi kuchukulia walinzi badala yako”.

Wanazuoni wengi wamesoma kwa kuweka irabu ya *Fat-hah* katika Nuun ya neno *Nattakhidh* katika Kauli Yake:

أَنْ نَتَّخِذَ مِنْ دُونِكَ مِنْ أَوْلِيَاءَ

“Sisi kuchukulia walinzi badala yako”.

Hii ina maana kuwa haifai kwa viumbe wote, sio sisi wala wao kumuabudu yeyote yule asiyekuwa Wewe. Hakika ni kuwa sisi hatukuwalingania kufanya hayo, bali wao walifanya hayo kwa hiyari ya nafsi zao, bila ya sisi kuwaambia kutekeleza hilo au kukubali. Nasi tuko mbali na ‘lbada zao wala sisi hatuna hatia.

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَيَقُولُ أَأَنْتُمْ أَضَلَلْتُمْ عِبَادِي هَؤُلَاءِ أَمْ هُمْ

ضَلُّوا السَّبِيلَ ﴿١٧﴾ قَالُوا سُبْحَانَكَ

“Na wakumbushe siku Atakayowakusanya wote, kisha Atawaambia Malaika: “Je! Hawa walikuwa wakiwaabuduni?” Watasema: “Subhaanaka (Umeepukana na kila upungufu)”.

Na wanazuoni wengine wamesoma: Kwa kuweka Irabu ya *Dhumma* katika neno *Nuttakhadh* Yenye kumaanisha, “Haimpasi yeyote kutuabudu sisi, kwani sisi ni waja Wako na tunakuhitaji Wewe”. Maana hii iko karibu sana na ile ya kwanza. Neno *Nattakhidh* katika kisomo cha hawa wanazuoni wengine kinabadilika na kuwa *Nuttakhadh*.

وَلٰكِنْ مَّتَّعْتَهُمْ وَاٰبَاءَهُمْ

“Lakini Wewe uliwastarehesha wao na baba zao”.

Maana yake: Uliacha muda mwingi upite mpaka wakasahau ukumbusho. Hii ina maana ya kuwa walisahau yaliyoteremshwa kwao kupitia kwa Mitume waliowaita katika kukuabudu Wewe Peke Yako bila ya kukushirikisha.

وَكَانُوا قَوْمًا بُورًا

“Na wakawa watu walioangamia”.

Ibn ‘Abbaas amesema: “Hii ina maana; walihilikishwa”.¹ Na Al-Hasan Al-Baswriy na Maalik wamemnuku Az-Zuhriy: “Hawakuwa na kheri miongoni mwao”.² Na Allah Aliyetukuka Amesema:

فَقَدْ كَذَّبْتُمْ بِمَا تَقُولُونَ

“Basi walikukanusheni kwa mliyoyasema”.

Hii inamaanisha kuwa wale wanaomuabudu asiyekuwa Allah تعالى wanawakadhinisheni kwa madai yenu kuwa wao ni wasaidizi wenu na kuwa wao wanawafikisheni karibu sana na Allah تعالى. Hii ni kama Aya:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ

دُعَائِهِمْ غٰفِلُونَ ﴿٥٦﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كٰفِرِينَ ﴿٥٧﴾

“Na wapotofu wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Allah ambao hawatawajibu mpaka Siku ya Kiyama, na hawatambui dua zao. Na ambao watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ‘Ibadah yao.” (46:5-6).

¹ Atw-Twabariy 19:248.

² Atw-Twabariy 19:248.

فَمَا تَسْتَطِيعُونَ صَرْفًا وَلَا نَصْرًا

“Kwa hivyo hamwezi kujiondolea wala kujisaidia.”

Maana yake: Hawana uwezo wa kujiondolea adhabu wala kuziokoa nafsi zao.

وَمَنْ يَظْلِمِ مِنْكُمْ

“Na atakayedhulumu miongoni mwenu.”

Kwa kumshirikisha Allah تعالى. Hao ndio:

تَذِقُهُ عَذَابًا كَبِيرًا ﴿١٩﴾

“Tutamwonjesha adhabu kubwa.”

* * *

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ
 الطَّعَامَ وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ ۗ وَجَعَلْنَا بَعْضَكُمْ
 لِبَعْضٍ فِتْنَةً أَنْتَصِرُونَ ۗ وَكَانَ رَبُّكَ بَصِيرًا ﴿٢٠﴾ *
 وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْنَا
 الْآيَاتُ الْكُبْرَىٰ أَوْ نَرَىٰ رَبَّنَا لَقَدِ اسْتَكْبَرُوا فِي أَنْفُسِهِمْ وَعَتَوْا
 عُتُوًّا كَبِيرًا ﴿٢١﴾ يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلَائِكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ
 لِلْمُجْرِمِينَ وَيَقُولُونَ حَجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٢٢﴾ وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا
 عَمِلُوا مِنْ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَنْثُورًا ﴿٢٣﴾ أَصْحَابُ
 الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا ﴿٢٤﴾ وَيَوْمَ
 نَشْفُقُ السَّمَاءَ بِالْغَمِيمِ وَنُزِّلُ الْمَلَائِكَةَ تَنْزِيلًا ﴿٢٥﴾
 الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ ۗ وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكَافِرِينَ
 عَسِيرًا ﴿٢٦﴾ وَيَوْمَ يَعْضُ الظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيْهِ يَقُولُ يَلَيْتَنِي
 اتَّخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَبِيلًا ﴿٢٧﴾ يَتَوَلَّىٰ لِيَتَنِي لَمَّا اتَّخَذَ
 فُلَانًا خَلِيلًا ﴿٢٨﴾ لَقَدْ أَضَلَّنِي عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ إِذٍ
 جَاءَنِي ۗ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِلْإِنْسَانِ خَذُولًا ﴿٢٩﴾
 وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ
 مَهْجُورًا ﴿٣٠﴾ وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِنَ
 الْمُجْرِمِينَ ۗ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ هَادِيًا وَنَصِيرًا ﴿٣١﴾

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ
 إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ
 وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ ۗ وَجَعَلْنَا
 بَعْضَكُمْ لِبَعْضٍ فِتْنَةً أَنْتَصِرُونَ ۗ
 وَكَانَ رَبُّكَ بَصِيرًا ﴿٢٠﴾

20. "Na hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakienda masokoni. Na Tumewajaalia baadhi yenu wawe ni majaribio kwa wengine; Je! Mtasubiri? Na Mola wako Mlezi ni Mwenye Kuona".

Mitume Wote Waliotangulia Walikuwa Binadamu

Allah تعالى Anatumjulisha kuhusu Mitume wote walio-tangulia ambao Yeye aliwa-tuma kuwa walikuwa wakila chakula na kutaka lishe. Na walikuwa wakienda maso-koni ili kupata pato na wali-kuwa wakifanya biashara. Na hilo halikuwa ni lenye kuteremsha cheo na hadhi zao kama Mitume. Hakika Allah تعالى Aliwajaalia wao

kuwa na tabia nzuri na sifa njema na maneno mazuri na amali zilizokamilika na Akawapa miujiza na dalili za dhahiri kabisa, ambazo mtu yeyote mwenye uoni thabiti na akili nzuri ataona ukweli wa yale waliyokuja nayo kutoka kwa Allah تعالى. Na inayofanana na hii Aya tukufu ni Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ

“Na Hatukuwatumia Mitume kabla yako isipokuwa wanaume Tuliowafanulia wahyi miongoni mwa watu wa mijini.” (12:109).

وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ

“Wala hatukuwafanya miili isiyokula chakula.” (21:8).

Aidha Kauli yake,

وَجَعَلْنَا بَعْضَكُمْ لِبَعْضٍ فِتْنَةً أَتَصْبِرُونَ^٥

“Na Tumewajaalia baadhi yenu wawe ni majaribio kwa wengine.”

Hii inamaanisha kuwa Tunawajaribu baadhi yenu kwa wengine na Tunawapatia maafa na mikasa baadhi yenu kwa wengine ili Tupate Kuwajua wenye kutii na wenye kuasi. Na hivyo Akasema:

أَتَصْبِرُونَ^٥ وَكَانَ رَبُّكَ بَصِيرًا ﴿٥﴾

“Je! Mtasubiri? Na Mola wako Mlezi ni Mwenye Kuona.”

Maana yake: Allah تعالى Anamjua Anaye stahiki kupata wahyi, kama Alivyosema Aliyetukuka:

اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ

“Allah Ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi Anaweka ujumbe Wake.” (6:124).

Naye Anajua pia anayestahiki uongofu kwa ujumbe Aliowatumia nao, na yule asiyestahiki kupata huo uongofu. Na Muhammad ibn Ishaq رحمه الله تعالى amesema kuhusu Kauli Yake:

وَجَعَلْنَا بَعْضَكُمْ لِبَعْضٍ فِتْنَةً أَتَصْبِرُونَ¹

“Na Tumewajaalia baadhi yenu wawe ni majaribio kwa wengine”.

Amesema: “Anasema Allah تعالى: Lau Ninataka Kuifanya hii dunia iwe hakuna yeyote wa Kuwapinga Mitume Yangu, Ningefanya hivyo. Lakini Mimi Ninataka Kuwapa mtihani waja Wangu na Niwajaribuni kwayo.”¹ Na katika Sahihi Muslim kutoka kwa ‘Iyaadh ibn Himaar kwamba Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللهُ تَعَالَى: إِنِّي مُبْتَلِيكَ وَمُتَبَّلِيكَ»

*“Allah Aliyetukuka Anasema: Nitakujaribuni na Kuwajaribu wengine kupitia wewe”.*²

Na katika Hadithi Sahihi imenukuliwa kuwa Mtume ﷺ alipatiwa uchaguzi wa kuwa Nabii au Mfalme au awe mja na Mtume ﷺ, naye alichagua kuwa mja na Mtume ﷺ.³

• وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْآمْتِلِيكَةُ أَوْ نَرَىٰ رَبَّنَا لَقَدِ اسْتَكْبَرُوا فِي أَنفُسِهِمْ وَعَتَوْا عُتُوًا كَبِيرًا ﴿١١﴾ يَوْمَ يَرَوْنَ الْآمْتِلِيكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ لِلْمُجْرِمِينَ وَيَقُولُونَ حَجْرًا مَّحْجُورًا ﴿١٢﴾ وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنْثُورًا ﴿١٣﴾ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقْرَرًا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا ﴿١٤﴾

21. “Na walisema wale wasiotaraji kukutana nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika au hatumuoni Mola wetu Mlezi? Kwa yakini hawa wamejiona bora nafsi zao, na wamepanda kichwa vikubwa mno!

22. Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wakosefu. Na watasema : Mungu apishe mbali!

¹ Atw-Twabariy 19:377.

² Muslim 2865.

³ Ahmad 2:231.

23. Na Tutayaendea yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, tuvifanye kama mavumbi yaliyotawanyika.

24. Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mahali penye starehe nzuri”.

Ubainifu wa Inadi na Ukaidi wa Makafiri

Anasema Aliyetukuka kwa Kutupasha habari kuhusu ukaidi wa makafiri katika kufuru yao na inadi yao kwa Kauli yao:

لَوْلَا أَنْزَلَ عَلَيْنَا الْمَلَائِكَةَ ﴿١٧٩﴾

“Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika.”

Hii ni kama ile kauli waliyosema:

أَوْ تَأْتِي بِاللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا ﴿١٨٠﴾

“Au utuletee Allah na Malaika uso kwa uso’. (17:92).

Ili tuwaone kwa macho yetu nao watuambie kwamba Muhammad ﷺ ni Mtume. Na hii nayo ni mfano wa kauli yao:

أَوْ نَرَى رَبَّنَا

“Au ni kwa nini hatumwoni Mola wetu Mlezi?.”

Allah تعالیٰ Anawajibu kwa Kusema:

لَقَدْ اسْتَكْبَرُوا فِي أَنْفُسِهِمْ وَعَتَوْا عُتُوًا كَبِيرًا ﴿١٨١﴾

“Kwa yakini hawa wamejiona bora nafsi zao, na wamepanda kichwa vikubwa mno!”

Na Allah تعالیٰ Anasema:

﴿ وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ ﴾

“Na lau kuwa Tungewateremshia Malaika, na maiti wakazungumza nao...”(6: 111).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلَائِكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ لِلْمُجْرِمِينَ وَيَقُولُونَ حِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٢٧﴾

“Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wakosefu. Na watasema: Mungu apishe mbali!”

Hii ina maana kuwa wao hawatawaona Malaika siku ya kheri kwao, bali siku watakayowaona kutakuwa hakuna bishara njema kwao, siku hiyo (yaani itakuwa siku mbaya kwao siku watayokutana na Malaika). Na huo ni ule wakati wa kukata roho pale Malaika watakapowabashiria Moto wa Jahanamu na Ghadhabu ya kutoka kwa *Al-Jabbar* (Mwenye kulazimisha viumbe wafanye Analolitaka Yeye). Hapo Malaika atamwambia kafiri wakati wa kutoa roho yake: “Toka, ee nafsi mbovu katika mwili muovu. Toka uelekee kwenye muwako mkali wa upepo na maji yenye kuchemka, na vivuli vya moshi mweusi.” Roho yake itakataa kutoka na itaanza kusambaa katika mwili wake na hapo watampiga, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ يَتَوَقَّى الَّذِينَ كَفَرُوا الْمَلَائِكَةَ يَصْرُبُونَ وُجُوهُهُمْ وَأَدْبُرَهُمْ

“Na laiti ungeliona Malaika wanapowafisha wale waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao.” (8: 50).

Na Anasema Aliyetukuka:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ الظَّالِمُونَ فِي غَمْرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُوا أَيْدِيهِمْ

“Na lau ungeliliwaona madhalimu wanavyokuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyoshea mikono.” (6:93).

Na hiyo inatekelezwa kwa kuwapiga. Na Malaika watakuwa wanawaambia,

أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمْ الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ

وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٢٧﴾

“Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyasema juu ya Allah yasiyo ya haki, na mliyokuwa mkizifanyia kiburi na kuzikataa Ayah na Ishara Zake.” (6:93).

Na hivyo Akasema katika Aya hii Tukufu:

يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلَائِكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ لِلْمُجْرِمِينَ

“Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wakosefu”.

Na matukio haya ni kinyume na hali ya Waumini wakati wa kukata roho kwao, kwani wao watapewa bishara njema ya kheri nyingi na kupata yenye kufurahisha. Allah تعالى Anasema :

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَفْتَمُوا تَنْزِيلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا
وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾ نَحْنُ أَوْلِيَاؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ
وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهُنَّ أَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ﴿٣١﴾ نُزُلًا مِنْ غَفُورٍ رَحِيمٍ ﴿٣٢﴾

“Wale waliosema: “Mola wetu Mlezi ni Allah”, kisha wakenda mwendo mzuri, hao huwateremkia Malaika (wakati wa kutoka roho wakawaambia): “Msiogope wala msihuzunike, na furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa”. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na huku katika Akhera, na humo mtapata mnavyovitaka. Ni karamu itokayo kwa Allah, Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Kurehemu” (41:30-32).

Kulingana na Hadithi Sahihi kutoka kwa Al-Baraa’ ibn ‘Aazib رضي الله عنه anasema: “Hakika Malaika wanaiambia roho ya Muumini: “Toka, ee roho nzuri kwenye mwili mzuri, kama ulivyokuwa ukiishi ndani yake. Toka uelekee kwenye mapumziko na mirehani (mimea yenye harufu nzuri) na kwa Mola Mlezi Asiye na Ghadhabu”.¹ Na wakasema wengine kuwa muradi wa Ayah hii:

يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلَائِكَةَ لَا بُشْرَىٰ

“Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha.”

¹ Muslim 4:2202.

Inamaanisha Siku ya Kiyama. Hii ni rai ya Mujaahid, Adh-Dhahhaak na wengineo. Na rai hizi mbili hazina ukinzani wowote, kwa sababu katika siku zote hizo mbili – siku ya kifo na Siku ya Kiyama – Malaika watawatokea Waumini na makafiri, na watatoa bishara njema ya rehema kutoka kwa Allah تعالى, starehe na furaha kwa Waumini. Ilhali watawapa makafiri habari ambazo zitawaletea majuto na huzuni, hivyo hakutakuwa na bishara njema kwa madhalimu watenda maovu wahalifu Siku hiyo. Na Malaika watasema:

﴿وَيَقُولُونَ حَبْرًا مَّجْنُونًا﴾

“Hijran Mahjuura (Mungu apishe mbali!).”

Maana yake: Malaika atamwambia kafiri: “Ufanisi umeharamishwa kwenu leo”. Na asili ya *Hijr* ni kukatazwa au kuharamishwa, hivyo neno hilo hutumika katika ibara: “*Hajara al-Qaadhi ‘ala Fulaan*” “Qadhi [hakimu] alimkataza mtu fulani’, pale anapomkataza kutumia mali yake kwa sababu ya - ama kufilisika, au upumbavu, au utoto na kadhalika. Na neno hili *al-Hijr* (ukuta wa chini ulio nusu duara karibu na Al-Ka’bah) pia limetokana na chimbuko hili, kwa sababu inawazuilia wenye kutufu kufanya *Tawaaf* ndani yake. Hivyo inafaa waizunguke nyuma yake na lengo ni kuwa kiwakilishi katika ibara ya Kauli Yake:

﴿وَيَقُولُونَ

“*Na watasema.*”

Ibara hii inarudi kwa Malaika. Na hii ni rai ya Mujaahid, ‘Ikrimah, Adh-Dhahhaak, Al-Hasan, Qataadah, Atwiyyah, Al-Awfiy, Atwaa, Al-Khurasaniiy, Khusayf na wengineo; na hii ndio rai aliyoichagua Ibn Jariir رحمه الله تعالى.¹

Na Ibn Jariir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Ibn Jurayj amesema: “Hayo ni katika maneno ya washrikina”.²

﴿يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلَائِكَةَ

“*Siku watakayo waona Malaika.*”

Hii ina maana kuwa watataka ulinzi kutoka kwa Malaika. Na hiyo ni kuwa Waarabu walikuwa anapopata mmoja wao maafa au shida alikuwa akisema:

¹ Atw-Twabariy 19:256 na *al-Muharrar al-Wajiiz* 4:206.

² Atw-Twabariy 19:254.

“Hijran Mahjuura”. Na kauli hii japokuwa kuna hoja ndani yake, lakini muktadha uko mbali sana na maana hii, na pia wanazuoni wengi wamefasiri kinyume na maana hayo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ

“Na Tutayaendea yale waliyoyatenda katika vitendo vyao.”

Hii inahusu Siku ya Kiyama wakati ambapo Allah تعالی Atawafanyia hesabu waja Wake kwa waliyoyafanya katika mambo ya kheri na shari. Allah تعالی Anatupasha habari kuwa hawa washrikina hawatapata chochote kwa vitendo vyao ambavyo walidhania vitawaokoa wao. Hii ni kwa sababu amali hizo hazikutimiza masharti ya kisheria, ama ikhlasi au kufuata sheria ya Allah تعالی. Hivyo, kila amali ambayo haina ikhlasi ndani yake au kutofanywa kulingana na sheria ya Allah تعالی itakuwa batili. Na amali za makafiri hazikosi kutokuwa na mojawapo ya sharti hizi au nyengine na huenda zikakosa sharti zote mbili, na ikiwa hivyo basi inakuwa haiwezi kabisa kukubaliwa. Na hivyo Allah تعالی Anasema:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنْثُورًا ﴿٢٣﴾

“Na Tutayaendea yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, Tuvifanye mavumbi yaliyotawanyika.” (25:23)

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنْثُورًا ﴿٢٣﴾

“Tuvifanye mavumbi yaliyotawanyika.”

Sufyaan Ath-Thawriy رحمه الله تعالی amepokea kutoka kwa Abi Ishaah kutoka kwa Al-Hariith naye kwa ‘Aliy kuhusu Kauli Yake:

فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنْثُورًا ﴿٢٣﴾

“Tuvifanye mavumbi yaliyotawanyika.”

Akasema: “Hiyo ni miale ya jua inapopita kwenye kipenyo kidogo.”¹ Rai inayofanana na hiyo imenukuliwa kwa Isnadi tofauti kutoka kwa ‘Aliy na mfano

¹ Isnadi yake ina udhaifu.

wake. Pia imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas, Mujaahid, 'Ikrimah, Said ibn Jubayr, As-Suddiy, Adh-Dhahhaak na wengineo.¹ Na hivyo amesema Al-Hasan Al-Baswriy: "Hiyo miale inapita katika kidirisha kidogo, na mtu anapojaribu kuishika, anashindwa".² Na amepokea Abu Al-Ahwasw kutoka kwa Abi Ishaq kutoka kwa Al-Haarith kutoka kwa 'Aliy ambaye amesema:

هَبَاءٌ مَّنْثُورًا ﴿٢٥﴾

"Mavumbi yaliyotawanyika."

Amesema: "*Habaa*" ni 'vumbi linalonyanyuliwa na wanyama."³ Na imepokewa mfano wake kwa Ibn 'Abbaas na Adh-Dhahhaak, na hii pia ilisemwa na 'Abdur-Rahman ibn Zayd ibn Aslam. Na amesema Qataadah katika Kauli Yake Aliyetukuka:

هَبَاءٌ مَّنْثُورًا ﴿٢٥﴾

"Mavumbi yaliyo tawanyika".

Akasema: "Je, hujaona miti mikavu inapopeperushwa na upepo? Hii inahusu majani hayo."⁴ Na amesema Ya'laa ibn 'Ubayd: "Hakika hii *Habaa* ni majivu na mavumbi yanapopigwa na upepo". Kuhitimisha ni kuwa kauli zote hizi ni kututanabahisha sisi kuwa amali za makafiri zitakuwa kama kitu ambacho hakitawasaidia kwa chochote. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

مَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۖ أَعْمَلُهُمْ كَرَمًا ۖ أَشْتَدَّتْ بِهِ الرِّيحُ

"Mfano wa walio mkufuru Mola wao Mlezi – vitendo vyao ni kama jivu linalopeperushwa kwa nguvu za upepo." (14:18).

Na Amesema Aliyetukuka:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُبْطِلُوا صَدَقَتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَى

"Enyi Mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi", Mpaka Kauli Yake:

¹ At-Tabari 19:257 na 258.

² At-Tabari 19:257.

³ At-tabari 19:258.

⁴ Rejaa pitio la nyuma.

لَا يَقْدِرُونَ عَلَى شَيْءٍ مِّمَّا كَسَبُوا

“Basi hawatakuwa na uwezo wowote kwa walivyochuma.” (2:264).

Na Amesema Aliyetukuka:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُوهُمْ كَسْرَابٍ بِقَيْعَةٍ يَحْسَبُهُ الظَّمْثَانُ مَاءً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ
شَيْئًا

“Na wale waliokufuru, vitendo vyao (wanavyoviona vizuri) ni kama mazigazi jangwani, mwenye kiu huyadhani ni maji, akiyaendea haoni chochote.” (24: 39).

Makazi ya Watu wa Peponi

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقْرَأًا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا ﴿٢٠﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mahali penye starehe nzuri.”

Hii inamaanisha Siku ya Kiyama, Allah تعالى Anasema:

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi; watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.” (59: 20).

Hivyo ni kuwa watu wa Peponi wataelekea kwenye daraja na vyeo vya juu na vikubwa, na maghorofa yenye utulivu, nao watakuwa katika sehemu za usalama zenye mandhari nzuri na makao mazuri.

Allah تعالى Anasema:

خَالِدِينَ فِيهَا حَسَنَتْ مُسْتَقْرَأًا وَمُقَامًا ﴿٧٦﴾

“Wadumu humo – kituo na makao mazuri kabisa.” (25:76).

Na watu wa Motoni wataelekea katika tabaka za chini kabisa, zenye hasara zinazofuatana, na sampuli tofauti za mateso yenye kuumiza na adhabu kali. Allah تعالى Anasema:

﴿إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا﴾

“Hakika hicho ni kituo na makao mabaya.” (25:66).

Hii inamaanisha kuwa hicho ni kituo kibaya kimandhari na makao mabaya. Na kwa hilo Akasema Aliyetukuka:

﴿أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mahali penye starehe nzuri”.

Maana yake: Kwa zile amali walizofanya zilizokubaliwa wamepata waliyopata, na wakafika walipofika. Kinyume na watu wa Motoni ambao hawana amali hata moja ambayo itawafanya wao kuingia Peponi na kuepushwa na Moto. Allah تعالى Akatanabahisha hali ya walio wazuri kwa habari za hali za waovu, na kuwa wao hawatakuwa na kheri yoyote.

Na amesema Said ibn Jubayr: “Allah تعالى Atamaliza hesabu (za waja) nusu ya mchana, watu wa Peponi na watu wa Motoni wataelekezwa Motoni. Anasema Allah تعالى:

﴿أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mahali penye starehe nzuri”

Na amesema ‘Ikrimah: “Hakika mimi najua wakati watakaolingia watu wa Peponi, Peponi, na watu wa Motoni, Motoni. Na huo ni wakati ambao duniani inakuwa baada ya adhuhuri, watu wanaporudi kwa wake zao kupumzika (Qayluulah). Wakati huo watu wa Motoni wataelekea Motoni, na ama watu wa Peponi watapelekwa Peponi, na Qayluulah yao itakuwa peponi na hapo watakula ini la nyangumi na wote watashiba”. Na hiyo ni kwa Kauli Yake:

﴿أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mahali penye starehe nzuri”.

وَيَوْمَ تَشْقُقُ السَّمَاءُ بِالْغَمِّمْ وَتُزَلُّ الْمَلَائِكَةُ تَزِيلًا ﴿٢٥﴾ الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ
 وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكَافِرِينَ عَسِيرًا ﴿٢٦﴾ وَيَوْمَ يَعْصُ الْأَطْلَامُ عَلَى يَدَيْهِ يَقُولُ يَلَيْتَنِي
 اتَّخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَبِيلًا ﴿٢٧﴾ يَدْوِلْتُنِي لَيْتَنِي لَمْ أُتَّخَذْ فُلَانًا خَلِيلًا ﴿٢٨﴾ لَقَدْ أَصَلَّنِي
 عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ إِذْ جَاءَنِي ۗ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِلْإِنْسَانِ خَذُولًا ﴿٢٩﴾

25. "Na siku zitakapopasuka mbingu, zilete chungu ya mawingu, na wateremshwe Malaika kwa wingi.

26. Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Ar-Rahmaan, Mwingi wa Rehema, na itakuwa siku ngumu kwa makafiri.

27. Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku anasema: Laiti ningelishika njia pamoja na Mtume!

28. Ee Mola wangu! Laiti nisingelimfanya fulani kuwa rafiki!

29. Amenipoteza, nikaacha Ukumbusho, baada ya kwisha njia, na kweli Shetani ni khaini kwa mwanadamu".

Vitisho vya Siku ya Kiyama na Kutamani Dhalimu Kufuata Njia ya Mtume

Anatupasha habari Aliyetukuka kuhusu vitisho vya siku ya Kiyama na yatakayotukia katika mambo makubwa, miongoni mwayo ni kupasuka kwa mbingu na kufunguka kwa kuleta mawingu mengi, nayo ni vivuli vya nuru kubwa ambayo inapofua macho. Na kuteremka kwa Malaika wa mbinguni siku hiyo na kutangamana na viumbe katika uwanja wa ufufuo, kisha ndio atakapokuja Mola Mlezi Aliyetukuka Atoe hukumu. Amesema Mujaahid: Na hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ ﴿٢٥﴾

"Je wanangoja mpaka Allah Awajie katika vivuli vya mawingu pamoja na Malaika." (2: 210).¹

Na hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

¹ Atw-Twabariy 19:260.

الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ

“Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Ar-Rahmaan, Mwingi wa Rehema.”

Hii Aya ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

لَمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ ۖ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿١٦﴾

“Leo Ufalme ni wa nani? Ni wa Allah Mmoja, Mwenye Nguvu (ya Kufanya Atakalo).” (40: 16).

Na katika Hadithi Sahihi:

«أَنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَطْوِي السَّمَوَاتِ بِيَمِينِهِ، وَيَأْخُذُ الْأَرْضِينَ بِيَدِهِ الْأُخْرَى، ثُمَّ يَقُولُ: أَنَا الْمَلِكُ أَنَا الدَّيَّانُ، أَيْنَ مُلْكُ الْأَرْضِ؟ أَيْنَ الْجَبَّارُونَ؟ أَيْنَ الْمُتَكَبِّرُونَ؟»

“Hakika Allah Aliyetukuka Ataikunja mbingu kwa Mkono Wake wa Kuume na Atazikamata ardhi kwa Mkono Wake Mwengine, kisha Atasema: “Mimi Ndiye Mfalme, Mimi Ndiye Ad-Dayyaan (Hakimu). Wapo wapi wafalme wa ardhi? Wako wapi wale majabari? Wako wapi wenye kiburi?”¹

وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكَافِرِينَ عَسِيرًا ﴿٩﴾

“Na itakuwa siku ngumu kwa makafiri.” Maana yake: Itakuwa siku ngumu, kwa sababu siku hiyo itakuwa siku ya uadilifu na kupata hukumu. Kama Allah تعالى Alivyosema:

فَذَلِكَ يَوْمًا يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿٩﴾ عَلَى الْكَافِرِينَ غَيْرُ يَسِيرٍ ﴿١٠﴾

“Siku hiyo, basi, itakuwa siku ngumu. Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.” (74:9-10)

Hii ndio itakuwa hali ya Makafiri katika siku hii. Ama upande wa waumini Allah تعالى Amewaelezea kwa Kusema:

لَا تَحْزَنُهُمُ الْفَرَعُ الْأَكْبَرُ

“Hawatahuzunishwa na huzuni kubwa.” (21:103).

¹ Fat-h al-Baariy 11:379 na Muslim 4:2148.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَيَوْمَ يَعْصُ الظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيْهِ يَقُولُ يَلِيَّتِي أَخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَيْبًا ﴿٢٧﴾

“Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku akisema: Laiti ningelishika njia pamoja na Mtume.”

Anatupasha habari Aliyetukuka kwa majuto ya dhalimu aliyetengana na njia ya Mtume na yale aliyokuja nayo kutoka kwa Allah تعالى katika haki iliyo wazi ambayo haina shaka ndani yake. Badala yake akafuata njia nyengine isiyokuwa ya Mtume ﴿٢٧﴾. Siku hiyo ya Kiyama atajuta kwa hayo lakini hayo majuto hayatakuwa ni yenye kumfalia kitu chochote. Atajiuma mikono yake kwa hasara aliyoipata na kuwa na masikitiko. Hata kama sababu ya kuteremshwa Aya hii ni kwa ajili ya ‘Uqbah ibn Abi Mu’itw au mwengine asiyekuwa yeye kati ya wale waovu. Kwa hakika Aya hii ni ya kijumla inamuhusu kila dhalimu. Hii ni sawa na yale Aliyosema Allah تعالى:

يَوْمَ تَقَلَّبُ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ

“Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa Motoni.” (33:66-67).

Hivyo kila dhalimu atajuta Siku ya Kiyama upeo wa kujuta, na watajiuma mikono yao, wakisema:

وَيَوْمَ يَعْصُ الظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيْهِ يَقُولُ يَلِيَّتِي أَخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَيْبًا ﴿٢٧﴾ يَوَيْلَاتِي لِيَّتِي

لَمْ أَخَذْ فَلَانًا خَلِيلًا ﴿٢٨﴾

“Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku akisema: Laiti ningelishika pamoja na Mtume. Ee Mola wangu! Laiti nisingelimfanya fulani kuwa rafiki!”

Hii ni kuwa walimtoa katika uongofu na kumpeleka katika njia ya upotovu kupitia walinganiaji wa upotevu. Na sawa katika hilo linamlenga Umayyah ibn Khalaf au nduguye Ubayy ibn Khalaf au wengineo. Anasema Aliyetukuka:

لَقَدْ أَضَلَّنِي عَنِ الذِّكْرِ

“Amenipoteza nikaacha Ukumbusho.”

Nayo ni Qur'ani.

بَعْدَ إِذْ جَاءَنِي

“Baada ya kwisha njia”.

Maana yake: Baada ya kunifikia mimi.

Amesema Allah Aliyetukuka:

وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِلْإِنْسَانِ خَذُولًا ﴿٢٥﴾

“Na kweli Shetani ni khaini kwa mwanadamu”.

Hii ina maana kuwa Shetani anamtoa mtu katika haki na anamtenganisha nayo na anamtumia yeye katika batili na anamuita kwayo.

وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُورًا ﴿٣٠﴾ وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ

نَجِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ ﴿٣١﴾ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ هَادِيًّا وَنَصِيرًا ﴿٣٢﴾

30. “Na Mtume alikuwa akisema: Ee Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya Qur’ani ni kihame.”

31. Na vivi hivi Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu, na Mola wako Mlezi Anatosha kuwa Mwenye Kuongoa na Mwenye Kunusuru”.

Mtume ﷺ Anashitakia Wanaompinga

Anasema Aliyetukuka Kutupatia habari sisi kuhusu Mtume ﷺ na Nabii Wake, rehma na amani zimfikie daima mpaka Siku ya Malipo, kuwa alisema:

يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُورًا ﴿٣٠﴾

“Ee Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya hii Qur’ani ni kihame”.

Na hilo ni kuwa washirikina walikuwa hawataki kusikiliza Qur’ani kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا هَذَا الْقُرْآنَ وَالْغَوْا فِيهِ

***“Na walisema waliokufuru (kuambizana wenyewe kwa wenyewe):
“Msisikilize Qur’ani na ipigieni makelele isomwapo.” (41:26).***

Na walikuwa wanaposomewa Qur’ani wakizidisha makelele na mazungumzo mengine hata wasiwe ni wenye kuisikiliza huku ndiko kuihama. Na kuacha elimu yake na kuihifadhi, pia ni kuihama. Na kuacha kuiamini na kuisadiki. Pia ni katika kuihama. Na kuacha kuizingatia na kuifahamu ni katika kuihama. Na kuacha amali kwayo na kufuata amri zake na kujiepusha na yanayokatazwa nayo pia ni kuihama. Na kujitenga nayo kwa kuvipa umuhimu vitu vyenginevyo katika mashairi au kauli au nyimbo au mambo ya upuuzi au maneno au njia iliyochukuliwa kwengineko, ni katika kuihama. Tunamuomba Allah تعالی, Mwenye Ukarimu na Muweza wa Kufanya Anachotaka, Atuondolee yale yanayomkasirisha na Atutumie kwa yale yanayomridhisha. Miongoni mwayo ni kuhifadhi Kitabu Chake na kukifahamu na kusimama imara kulingana na Anayotaka usiku kucha na katika ncha za mchana (asubuhi na jioni) na kwa njia ambayo Anaipenda na Kumridhisha, hakika Yeye ni Mtukufu Mwenye Ukarimu na Mpaji Mkuu.

Na kauli Yake Aliyetukuka:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ

“Na vivi hivi Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu.”

Hii inamaanisha kuwa kama ulivyopatikana wewe, ee Muhammad na kaumu yako miongoni mwa wale wenye kuihama Qur’ani, hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa kaumu iliopita. Kwani Allah تعالی Amejaalia kwa kila Nabii adui miongoni mwa wahalifu, ambao wanawaita watu katika upotevu wao na kufuru zao. Hii ni kama ile Kauli Yake:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَاطِئِينَ الْإِنْسِ وَالْجِنَّ

“Na kadhalika Tumemfanyia kila Nabii maadui mashetani wa kiwatu.” (6:112-113).

Na kwa hilo Amesema hapa Aliyetukuka:

وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ هَادِيًا وَنَصِيرًا ﴿٢٠﴾

“Na Mola wako Mlezi Anatosha kuwa Mwenye Kuongoa na Mwenye Kunusuru.”

Hii ina maana kwa wale waliomfuata Mtume Wake na wakaamini Kitabu Chake, na kumsadiki na kumfuata, hakika Allah تعالیٰ Ndiye Mwenye Kumuongoa na Kumnusuru hapa duniani na Akhera. Na hakika Amesema:

هَادِيًا وَنَصِيرًا ﴿٢١﴾

“Mwenye Kuongoa na Mwenye Kunusuru.”

Kwani washrikina walikuwa wakiwaekea watu vikwazo katika kuifuata Qur’ani ili asiwe ni mwenye kuongoka mmoja wao na njia yao isishindwe na ile njia ya Qur’ani. Kwa hiyo Allah تعالیٰ Akasema:

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ

“Na vivi hivi Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu”.

* * *

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْآنُ جُمْلَةً وَاحِدَةً ۚ كَذَلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ ۗ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلًا ۗ وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا ﴿٣٢﴾
 الَّذِينَ يُحْشَرُونَ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ إِلَىٰ جَهَنَّمَ أُولَٰئِكَ شَرٌّ مَكَانًا وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٣٣﴾
 وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ وَجَعَلْنَا مَعَهُ رَاحَةَ هَارُونَ وَزِيْرًا ﴿٣٤﴾ فَقُلْنَا أَذْهَبَا إِلَىٰ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَبُوا بِآيَاتِنَا فَدَمْزَلْنَهُمْ تَدْمِيرًا ﴿٣٥﴾ وَقَوْمَ نُوحٍ لَمَّا كَذَبُوا الرُّسُلَ أَغْرَقْنَاهُمْ وَجَعَلْنَاهُمْ لِلنَّاسِ آيَةً ۗ وَأَعْتَدْنَا لِلظَّالِمِينَ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٣٦﴾ وَعَادًا وَثَمُودًا وَأَصْحَابَ الرَّسِّ وَقُرُونًا بَيْنَ ذَلِكَ كَثِيرًا ﴿٣٧﴾ وَكُلًّا صَبَرْنَا لَهُ الْأَمَثَل ۗ وَكُلًّا تَبَرْنَا تَنْبِيْرًا ﴿٣٨﴾
 وَلَقَدْ أَتَوْا عَلَى الْقَرْيَةِ الَّتِي أَمْطَرْنَا مَطَرًا سَوْءًا ۚ أَفَلَمْ يَكُونُوا يَرْتَوْنَهَا ۚ بَلْ كَانُوا لَا يَرْجُونَ نُشُورًا ﴿٣٩﴾ وَإِذَا رَأَوْكَ إِذْ يَتَخَذُونَكَ إِلَّا هُزُوًا أِهْدِنَا الَّذِي بَعَثَ اللَّهُ رُسُلًا ﴿٤٠﴾ إِنْ كَادَ لَيُضِلَّنَا عَنْ ءَالِهَتِنَا لَوْلَا أَنْ صَبَرْنَا عَلَيْهَا ۚ وَسَوْفَ يَعْلَمُونَ حَيْثُ يَرَوْنَ الْعَذَابَ مِنَ أَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٤١﴾ أَرَأَيْتَ مَنْ أَخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكِيلًا ﴿٤٢﴾ أَمْ تَحْسَبُ أَنَّ أَكْثَرَهُمْ يَسْمَعُونَ أَوْ يَعْقِلُونَ ۚ إِنْ هُمْ إِلَّا كَالْأَنْعَامِ ۗ بَلْ هُمْ أَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٤٣﴾

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْآنُ جُمْلَةً وَاحِدَةً ۚ كَذَلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِ فُؤَادَكَ ۗ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلًا ۗ وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا ﴿٣٢﴾
 الَّذِينَ يُحْشَرُونَ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ إِلَىٰ جَهَنَّمَ أُولَٰئِكَ شَرٌّ مَكَانًا وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٣٣﴾

32. "Na wakasema walio-kufuru: Kwa nini haku-teremshiwa Qur'ani kwa jumla moja? Hayo ni hivyo ili Tuuthibitisha moyo wako, na ndio Tumeisoma kwa mafungu.

33. Wala hawatakuletea mfano wowote, ila Sisi Tutakuletea (jawabu) kwa haki, na tafsiri iliyo bora.

34. Wale ambao watakokuwanywa na kubururwa kifudufudi mpaka kwenye Jahanamu, hao watakuwa na mahali pabaya, ndio wenye kuipotea sana njia".

Hekima ya Kuteremshwa Qur’ani kwa Awamu na Kuwajibu Makafiri na Kubainisha Mashukio yao

Anasema Aliyetukuka Kutupasha habari sisi kuhusu kukithiri kupinga kwa makafiri na inadi zao na maneno yao yasiyowahusu, kwani wao walisema:

لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْآنُ جُمْلَةً وَاحِدَةً

“Kwa nini hakuteremshiwa Qur’ani kwa jumla moja?”

Maana: Angeteremshiwa yeye hiki Kitabu mara moja kama vilivyoteremshwa Vitabu kabla yake kwa mpigo mmoja, kwa mfano Taurati, Injili, Zaburi na vitabu vingine vya Allah تعالى. Allah تعالى Akawajibu kuwa kuteremshwa huko polepole katika kipindi cha miaka ishirini na tatu (23) kulingana na matukio na pale panapohitajika kwa hukumu, ni kwa ajili ya kuithibitisha mioyo ya Waumini. Hii ni kama Kauli Yake:

وَقُرْآنًا فَرَقْنَاهُ

“Na Qur’ani Tumeigawanya sehemu mbali mbali.” (17:106).

Na hivyo Akasema:

لِنُنزِّلَنَّ بِهِ فُؤَادَكَ ط وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلًا

“ ili Tuuthibitisha moyo wako, na ndio Tumeisoma kwa mafungu.”

Amesema Qataadah: “Amebainisha wazi wazi”. Na amesema ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam: “Na Tumeielezea na Kuifasiri wazi wazi kabisa”.¹

وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ

“Wala hawatakuletea mfano wowote.”

Maana yake: Kwa hoja zenye kulinganishwa. Anasema Aliyetukuka:

إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا ﴿٣٦﴾

“Ila Sisi Tutakuletea (jawabu) kwa haki, na tafsiri iliyo bora.”

Hii ina maana kuwa wala hawatasema kauli yoyote inayopinga haki isipokwa Tutawajibu kwa yaliyo na haki na ukweli kwa wakati ule ule na kwa uwazi na ufasaha kabisa kuliko kauli zao na maneno yao.

¹ Atw-Twabariy 19:266.

Abu 'Abdur-Rahmaan An-Nasaa'iy amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: "Qur'ani iliteremshwa kwa mkupuo mmoja mpaka wingu wa dunia katika usiku wa hishima (*Laylatul Qadr*). Kisha ikateremshwa baada ya hapo kwa miaka ishirini".¹ Allah تعالى Amesema:

وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا ﴿٣٦﴾

"Wala hawatakuletea mfano wowote, ila Sisi Tutakuletea (jawabu) kwa haki, na tafsiri iliyo bora".

Na Amesema Aliyetukuka:

وَقُرْءَانًا فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى النَّاسِ عَلَى مُكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنْزِيلًا ﴿١٧﴾

"Na Qur'ani Tumeigawanya sehemu mbali mbali ili uwasomee watu kwa kituo, na Tumeiteremsha asteaste (kidogo kidogo)." (17: 106).

Kisha akasema Aliyetukuka Kutueleza kuhusu hali mbaya ya makafiri katika makazi yao Siku ya Kiyama na kukusanywa kwao Jahanamu katika hali mbovu sana na kwa sifa za kutwezwa na kutahayarisha. Na Allah تعالى Anasema:

الَّذِينَ تَحْمُرُونَ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ إِلَىٰ جَهَنَّمَ أُولَٰئِكَ سَرُّ مَكَانًا وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٣٧﴾

"Wale ambao watakaokusanywa na kubururwa kifudifudi mpaka kwenye Jahanamu, hao watakuwa na mahali pabaya, ndio wenye kuipotea sana njia."

Na katika Hadithi Sahihi kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa mtu mmoja aliuliza: "Ewe Mtume! Vipi watakusanywa makafiri na kuburuzwa kifudifudi (kwa nyuso zao) Siku ya Kiyama?" Akasema:

«إِنَّ الَّذِي أَمْسَاهُ عَلَىٰ رِجْلَيْهِ قَادِرٌ أَنْ يُمْشِيَهُ عَلَىٰ وَجْهِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

"Hakika Yule Aliyewafanya kutembea kwa miguu yao miwili, Ana Uwezo Kuwafanya watembee kifudifudi Siku ya Kiyama".²

¹ An-Nasaa'iy katika *Al-Kubraa* 6:421.

² Ahmad 3:229.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَجَعَلْنَا مَعَهُ أَخَاهُ هَارُونَ وَزِيْرًا ﴿٣٥﴾ فَقُلْنَا أَذْهَبَا إِلَى
 الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَبُوا بِآيَاتِنَا فَدَمْزَلْنَهُمْ نَدْمِيرًا ﴿٣٦﴾ وَقَوْمَ نُوحٍ لَمَّا كَذَبُوا الرُّسُلَ
 أَغْرَقْنَاهُمْ وَجَعَلْنَاهُمْ لِلنَّاسِ آيَةً وَأَعْتَدْنَا لِلظَّالِمِينَ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٣٧﴾ وَعَادًا وَثَمُودًا
 وَأَصْحَابَ الرِّسِّ وَقُرُونًا بَيْنَ ذَلِكَ كَثِيرًا ﴿٣٨﴾ وَكُلًّا ضَرَبْنَا لَهُ الْأَمْثَالَ ط وَكُلًّا تَبَّرْنَا
 تَتْبِيرًا ﴿٣٩﴾ وَلَقَدْ أَتَوْا عَلَى الْقَرْيَةِ الَّتِي أَمْطَرْنَا مَطَرَ السَّوْءِ ء أَفَلَمْ يَكُونُوا يَرَوْنَهَا بَلْ
 كَانُوا لَا يَرْجُونَ نُشُورًا ﴿٤٠﴾

35. "Na hakika Tulimpa Musa Kitabu na Tukamweka pamoja naye nduguye, Haaruna kuwa waziri.

36. Tukawaambia: Nendeni kwa watu waliokanusha Ishara zetu. Basi Tukawateketeza kabisa.

37. Na watu wa Nuhu, walipowakanusha Mitume, Tuliwazamisha, na Tukawafanya ni Ishara kwa watu. Na Tumewaandalia wenye kudhulumu adhabu chungu.

38. Na Tuliwaangamiza kina 'Aadi na Thamuud na watu wa Rass na vizazi vingi vilivyokuwa kati yao.

39. Na wote Tuliwapigia mifano, na wote Tuliwaangamiza kabisa.

40. Na kwa yakini wao wanafika kwenye nchi ilioteremshwa mvua mbaya. Basi, je, hawakuwa wakiiona? Bali walikuwa hawataraji kufufuliwa".

Kuwahofisha Washirikina wa Kiquraysh

Allah تعالیٰ Anasema huku Akiwaahidi wale wanaomkadhibisha Mtume Wake Muhammad ﷺ miongoni mwa washirikina wa kaumu yake na kila anayempinga yeye, na kuwaonya na ikabu na ukali wa adhabu Yake kama Alivyowateremshia Ummah uliopita uliokadhibisha Mitume Yake. Allah تعالیٰ Anaanza kwa Kumtaja Nabii Musa عليه السلام na kuwa Alimtuma yeye pamoja na nduguye Haarun عليه السلام, kama msaidizi na waziri wake, yaani Nabii aliye waziri mwenye kumsaidia na kumnusuru. Firauni na jeshi lake waliwakadhibisha kwa hivyo,

دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ط وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَلُهَا ﴿٤٧﴾

“Allah Aliwaangamiza na kwa makafiri hawa itakuwa adhabu kama hiyo.” (47:10).

Na vivyo hivyo, Allah تعالى Alifanya kwa kaumu ya Nuuh عليه السلام pale ilipomkadhibisha Mtume Wake Nuuh عليه السلام. Kwa mtu yeyote kumkadhibisha Mtume mmoja basi ni sawa na kuwakadhibisha Mitume wote, kwani hapana tofauti baina ya Mtume mmoja na mwingine. Ikichukuliwa lau kuwa Allah تعالى Angewatuma Mitume wote, hakika wao wangewakadhibisha. Na kwa hilo Allah تعالى Anasema:

وَقَوْمَ نُوحٍ لَمَّا كَذَبُوا الرُّسُلَ

“Na watu wa Nuhu, walipowakanusha Mitume.”

Hakika ni kuwa wao hawakupelekewa Mtume isipokuwa Nuuh عليه السلام ambaye alikaa pamoja nao miaka elfu moja kupungua hamsini (yaani miaka mia tisa na hamsini – 950) akiwaita warudi kwa Allah Aliyetukuka. Na hapo Nuuh عليه السلام akawa anawaonya kwa maangamivu yatakawafikia, lakini:

وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٤٨﴾

“Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.” (11:40).

Na kwa hilo Allah تعالى Aliwagharikisha wote na hakubakia yeyote miongoni mwao na hakuachwa binadamu katika ulimwengu isipokuwa wale watu wa safina tu.

وَجَعَلْنَاهُمْ لِلنَّاسِ ءَايَةً

“Na Tukawafanya ni ishara kwa watu.”

Yaani, mafunzo ambayo watazingatia kwayo. Hii ni sawa na Alivyosema تعالى:

إِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ ﴿٦٩﴾ لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذِكْرًا وَتَعْيَبَ أُذُنٌ وَعَيْبَةً ﴿٧٠﴾

“Maji yalipofurika (katika zama za Nuuh) Sisi Tulikupandisheni katika hicho kinachokwenda (baharini). Ili Tuifanye ukumbusho kwenu; na sikio lisikialo lisikie.” (69:11-12).

Hii ina maana, Tuliwabakisha katika safina ambayo mtaweza kuipanda kwenye kina kirefu cha bahari ili muweze kukumbuka neema ya Allah تعالى juu yenu

kwa kuokolewa katika gharika hiyo. Na Akawajaalia kizazi chenye kumuamini na kusadiki Amri Zake. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَعَادًا وَثَمُودًا وَأَصْحَابَ الرَّسِّ

“Na Tuliwaangamiza kina ‘Aadi na Thamuud na watu wa Rass.”

Hakika tayari tushazungumzia visa katika Surah zilizotangulia kama Suratul A'raaf, hivyo hapana haja ya kurudia. Ama watu wa *Rass*, amepokea Ibn Jurayj kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hao walikuwa ni watu wa kijiji katika vijiji vya Thamuud”.¹ Na amepokea Ath-Thawriy kutoka kwa Abi Bukair naye kutoka kwa ‘Ikrimah ambaye amesema: “*Rass* ni kisima cha *Rassuu* ambamo alizikwa Nabii wao”.² Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقُرُونًا بَيْنَ ذَلِكَ كَثِيرًا ﴿٣٦﴾

“Na vizazi vingi vilivyokuwa kati yao.” Yaani na Ummah nyingi sana kuliko zile Tulizotaja Tuliwaangamiza. Na hivyo Akasema:

وَكُلًّا صَبَرْنَا لَهُ الْأَمْثَلُ

“Na wote Tuliwapiga mifano.” Hii ina maana, Tuliwabainishia hoja na Tukawawekea wazi kabisa dalili Zetu, kama alivyosema Qataadah: “Na Tukawaondolea udhuru kwao”.³ Allah تعالى Anasema:

وَكُلًّا تَبَرْنَا تَتَبِيرًا ﴿٣٧﴾

“Na wote Tuliwaangamiza kabisa.”

Hii inamaanisha kuhilikishwa kabisa bila kubakishwa chochote chao. Hii ni sawa na ile Kauli ya Aliyetukuka:

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُونِ مِنْ بَعْدِ نُوحٍ

“Na kaumu ngapi Tumeziangamiza baada ya Nuuh.” (17:17).

Na *Qarn* ni Ummah wa watu. Kama Kauli Yake:

¹ Atw-Twabariy 19:269.

² Al-Baghawiy 3:369 na Al-Qurtwubiy 13:32.

³ Atw-Twabariy 19:272.

ثُمَّ أَدْنَيْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قُرُونًا آخَرِينَ ﴿٤٢﴾

“Kisha Tukaleta baada yao vizazi vingine.” (23:42).

Wamesema baadhi ya wanazuoni kuwa *Qarn* ni miaka mia na ishirini, na wengine wanasema ni mia moja, na wengine tena wanasema ni themanini na panasemwa kuwa ni arobaini na kauli nyenginezo. Na iliyo dhahiri ni kuwa *Qarn* ni Ummah unaoishi katika zama na wakati mmoja, hivyo wanapoondoka na kuacha kizazi chengine hiyo itakuwa ni *Qarn* nyengine. Maana hii imethibiti katika Hadithi Sahihi:

«خَيْرُ الْقُرُونِ ثَرْنِي، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ»

“Bora ya karne (*Qarn*) ni hii yangu, kisha ni ile inayofuata, kisha ni ile inayofuata”.¹

Na kwa Kauli Yake:

﴿وَلَقَدْ أَنزَلْنَا عَلَى الْقَرْيَةِ الَّتِي أَنطَرْت مَطَرَ السَّوَاءِ﴾

“Na kwa yakini wao wanafika kwenye nchi ilioteremshwa mvua mbaya.”

Maana yake: Kijiji cha kaumu ya Luutw عليه السلام, nayo ni Sodom na muamala wao ambao uliwafanya waangamizwe na Allah تعالى kwa kugeuzwa juu chini na kuteremshiwa mvua ya mawe ya udongo wa kuokwa. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَسَاءَ مَطَرُ الْمُنذَرِينَ﴾

“Na Tukawanyeshelezea mvua (ya mawe), basi ni mbaya mno, mvua ya hao walioonywa wasionyeke.” (26:173).

Na Allah تعالى Amesema,

﴿وَأَنكُرْ لَتَمُرُونَ عَلَيْهِمْ مُصْبِحِينَ﴾ ﴿١٣٧﴾ ﴿وَبِالْآيِلِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ﴾ ﴿١٣٨﴾

“Na kwa yakini mnawapita asubuhi na usiku pia. Basi je, hamfahamu?” (37:13 -138).

¹ Fat-hul-Bari 5:306 na Muslim 4:1963.

Na Allah تعالى Amesema,

وَأِنَّا لَبَسِيلٌ مُّقِيمٌ ﴿٦٦﴾

“Na miji hiyo ipo katika njia inayopitiwa.” (15:76).

Na Allah تعالى Amesema,

وَأَيْتُمَا لِبِإِمَامٍ مُّبِينٍ ﴿٦٧﴾

“Na nchi hizo mbii ziko katika njia zilizo dhahiri.” (15:79).

Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Akasema:

أَفَلَمْ يَكُونُوا يَرَوْنَهَا

“...Basi, je, hawakuwa wakiona?”

Ili waweze kuzingatia kwa wale watu waliofikiwa na mateso na adhabu ya kupigiwa mfano kwa sababu ya kumkadhibisha Mtume ﷺ na kwenda kinyume na Amri za Allah تعالى.

بَلْ كَانُوا لَا يَرْجُونَ نُشُورًا ﴿٦٨﴾

“Bali walikuwa hawataraji kufufuliwa.”

Hii ina maana kuwa wale wanaopita njia hizo miongoni mwa makafiri hawapati mafundisho wala mazingatio kwani wao hawataraji kufufuliwa, yaani kurudi Siku ya Kiyama.

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوعًا أَوْ هُزُوعًا أَهْدَا الَّذِي بَعَثَ اللَّهُ رَسُولًا ﴿٦٩﴾ إِن كَادَ لَيُضِلَّنَا
عَنْ ءَالِهَتِنَا لَوْلَا أَن صَبَرْنَا عَلَيْهَا ۗ وَسَوْفَ يَعْلَمُونَ حَيْثُ يَرَوْنَ الْعَذَابَ مَنْ أَضَلُّ
سَبِيلًا ﴿٧٠﴾ أَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ ۗ أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكِيلًا ﴿٧١﴾ أَمْ تَحْسَبُ
أَن أَكْثَرَهُمْ يَسْمَعُونَ ۖ أَوْ يَعْقِلُونَ ۗ إِن هُمْ إِلَّا كَالْأَنْعَامِ ۗ بَلْ هُمْ أَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾

41. “Na wanapokuona hawakuchukulii ila ni mzaha tu, na (wanasema): Ati ndiye huyu aliyetumwa na Allah kuwa Mtume?”

42. Kwa hakika alikuwa karibu kutupoteza tuiache miungu yetu, ingelikuwa hatukushikamana nayo kwa kuvumilia. Bado watakuja jua, watakapoiona adhabu, ni nani aliyepotea njia.

43. Je! Umemwona aliyeyafanya matamania yake kuwa ndio miungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?

44. Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa? Hao hawakuwa ila ni kama nyama hoa tu, bali wao wamepotea zaidi njia.

Makafiri Kumfanyia Mtume ﷺ Mzaha

Allah تعالى Anatupa sisi habari kuhusiana na washirikina kumfanyia mzaha Mtume ﷺ pindi wanapomuona tu, kama Alivyosema:

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوًا

“Na wanapokuona hawakuchukulii ila ni mzaha tu.”

Wakimaanisha kuwa ana aibu na upungufu. Hivyo wanasema hapa:

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوًا أَهْدَا الَّذِي بَعَثَ اللَّهُ رَسُولًا ﷺ

**“Na wanapokuona hawakuchukulii ila ni mzaha tu, na (wanasema):
Ati ndiye huyu aliyetumwa na Allah kuwa Mtume?”**

Hii ilikuwa ni kwa njia ya kuonesha upungufu na kumbeza, hivyo Allah تعالى Akasema, kama Alivyosema:

وَلَقَدْ اسْتَهْزَيْتُمْ بِرُسُلِي مِن قَبْلِكَ

“Na hakika Mitume waliokuja kabla yako walifanyiwa kejeli.” (6: 10).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِن كَادَ لَيُضِلَّنَا عَنْ ءِالِهَتِنَا

“Kwa hakika alikuwa karibu kutupoteza tuiache miungu yetu.”

Hii ina maana walikuwa karibu kuacha kuabudu masanamu yao lau hawangekuwa ni wenye kusubiri, kuwa imara na kuendelea kwayo. Allah تعالى Anawaahidi na kutoa changamoto:

وَسَوْفَ يَعْلَمُونَ حِينَ يَرَوْنَ الْعَذَابَ

“Bado watakuja jua, watakapoiona adhabu, ni nani aliyepotea njia”.

Kuchukua Matamanio yao kuwa Mungu na kuwa wao Wamepotea kuliko Nyama hoa

Kisha Allah تعالى Akasema Kumtanabahisha Nabii Wake kuwa aliyeandikiwa na Allah تعالى kuwa muovu na kupotea hakuna yeyote anayeweza kumuongoa ila Yeye:

أَرَأَيْتَ مَنْ أَخَذَ إِلَيْنَهُدْ هَوْنَهُ

“Je! Umemuona aliyeyafanya matamanio yake kuwa ndio miungu wake?”

Hii ina maana japokuwa atajaribu kufanya kitu kwa uzuri na akakiona ni kizuri katika matamanio ya nafsi yake, hiyo ndiyo itakuwa dini na madhehebu yake. Hii ni kama vile Alivyosema Aliyetukuka:

أَفَمَنْ زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ فَرَآهُ حَسَنًا فَإِنَّ اللَّهَ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ

“Je! Yule aliyepambiwa amali zake mbaya na akazona njema? Bila shaka Allah Humuacha kupotea Amtakaye (kwa kuwa hataki mwenyewe kuongoka).” (35:8).

Na hivyo hapa Akasema:

أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكَيْلًا

“Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?”

Ibn ‘Abbaas amesema: “Alikuwa mtu katika zama za ujahiliya akiabudu jiwe jeupe kwa kipindi, lakini pindi alipoliona jiwe jingine lililo bora alikuwa akiabudu hili la pili na kuliacha la kwanza.”¹ Kisha Akasema Aliyetukuka: “Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa?” Hakika ni kuwa wao ni wabaya zaidi hata kuliko nyama hoa (wanyama wa kufugwa), kwani hao wanafanya kwa yale walioumbiwa kwayo. Na hawa (makafiri) wameumbwa ili wamwabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya kumshirikisha na chochote lakini wao hawafanyi hivyo. Badala yake wanawaabudu wengine na wanamshirikisha na Allah تعالى pamoja na kuletewa hoja na kutumiwa Mitume.

¹ Ad-Durra-Manthuur 6: 260.

أَلَمْ تَرَ إِلَىٰ رَبِّكَ كَيْفَ مَدَّ الظِّلَّ وَلَوْ
 شَاءَ لَجَعَلَهُ سَاكِنًا ثُمَّ جَعَلْنَا
 الشَّمْسَ عَلَيْهِ دَلِيلًا ﴿٤٥﴾ ثُمَّ قَبَضْنَاهُ إِلَيْنَا
 قَبْضًا يَسِيرًا ﴿٤٦﴾ وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ لِبَاسًا
 وَالنَّوْمَ سُبَاتًا وَجَعَلَ النَّهَارَ نُشُورًا ﴿٤٧﴾ وَهُوَ الَّذِي أَرْسَلَ
 الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۗ وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ
 مَاءً طَهُورًا ﴿٤٨﴾ لِنُحْيِيَ بِهِ بَلْدَةً مَيْتًا وَنُسْقِيَهُ مِمَّا
 خَلَقْنَا أَنْعَمًا وَأُنَاسِيًّا كَثِيرًا ﴿٤٩﴾ وَلَقَدْ صَرَّفْنَاهُ بَيْنَهُمْ
 لِيَذَّكَّرُوا فَأَبَىٰ أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٥٠﴾ وَلَوْ شِئْنَا
 لَبَعَثْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ نَذِيرًا ﴿٥١﴾ فَلَا تَطِعِ الْكَافِرِينَ
 وَجَاهِدْهُمْ بِهِ جِهَادًا كَبِيرًا ﴿٥٢﴾ * وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ
 الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ وَجَعَلَ
 بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا وَحِجْرًا مَحْجُورًا ﴿٥٣﴾ وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ مِنَ
 الْمَاءِ بَشَرًا فَجَعَلَهُ نَسَبًا وَصِهْرًا ۗ وَكَانَ رَبُّكَ قَدِيرًا ﴿٥٤﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَىٰ رَبِّكَ كَيْفَ مَدَّ الظِّلَّ وَلَوْ
 شَاءَ لَجَعَلَهُ سَاكِنًا ثُمَّ جَعَلْنَا
 الشَّمْسَ عَلَيْهِ دَلِيلًا ﴿٤٥﴾ ثُمَّ
 قَبَضْنَاهُ إِلَيْنَا قَبْضًا يَسِيرًا ﴿٤٦﴾ وَهُوَ
 الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ لِبَاسًا وَالنَّوْمَ
 سُبَاتًا وَجَعَلَ النَّهَارَ نُشُورًا ﴿٤٧﴾

45. "Je! Huoni jinsi Mola wako Mlezi Anavyokitandaza kivuli. Na Angelitaka angelikifanya kikatulia tu. Kisha Tumelifanya jua kuwa ni kiongozi wake.

46. Kisha Tunakivutia kwetu kidogo kidogo.

47. Naye Ndiye Aliyekufanyieni usiku kuwa ni vazi, na usingizi kuwa mapumziko, na Akakufanyieni mchana ni kufufuka".

Dalili za Kuwepo kwa Mtengenezaji na Uweza Wake

Kuanzia hapa Mtukufu Aliyetakasika Ameanza Kubainisha dalili zinazoonesha Kuwepo Kwake na Ukamilifu na Uweza Wake katika Kuumba vitu tofauti na kinyume chake. Amesema Aliyetukuka:

أَلَمْ تَرَ إِلَىٰ رَبِّكَ كَيْفَ مَدَّ الظِّلَّ

"Je! Huoni jinsi Mola wako Mlezi Anavyokitandaza kivuli".

Ibn 'Abbaas, Ibn 'Umar, Abul Aliyah, Abu Maaliki, Masruuq, Mujaahid, Said ibn Jubayr, An-Nakha'iy, Adh-Dhahhaak, Al-Hasan, Qataadah na As-Suddiy na wengineo wamesema: "Hiyo (inapatikana) baina ya kuingia Alfajiri mpaka kuzama jua".¹ Anaendelea Kusema:

وَلَوْ شَاءَ لَجَعَلَهُ سَاكِنًا

"Na angelitaka Angelikifanya kikatulia tu."

Maana yake: Daima na milele na halizami. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ اللَّيْلَ سَرْمَدًا

**"Sema: Niambieni kama Allah Akiufanya usiku ukukalieni milele."
(28:71).**

ثُمَّ جَعَلْنَا الشَّمْسَ عَلَيْهِ دَلِيلًا ﴿٧١﴾

"Kisha Tumelifanya jua kuwa ni kiongozi wake."

Hii inamaanisha kuwa lau jua lisingechomoza juu yake usingejulikana, kwani kilicho kinyume hakitambulikani isipokuwa kwa kinyume chake. Na amesema Qataadah na As-Suddiy: "Dalili ya kuwa linatoka na linauandama usiku na kuufuata linakuja lote juu yake".² Na Kauli Yake Aliyetukuka:

ثُمَّ قَبَضْنَاهُ إِلَيْنَا قَبْضًا يَسِيرًا ﴿٧٢﴾

"Kisha Tunakivutia kwetu kidogo kidogo."

Maana yake: Hicho kivuli.

يَسِيرًا ﴿٧٢﴾

"Yasiira."

Maana yake: Kwa wepesi na usahali. Na As-Suddiy amesema: "Kushikwa kusikojulikana hadi kusibakie kivuli katika ardhi ila chini ya sakafu au mti, na jua limefunika vya juu yake". Na Ayyub ibn Musaa amesema kuhusu Aya hii:

¹ Atw-Twabariy 19:275 na Al-Qurtwubiy 13:37.

² Ad-Durr al-Manthuur 6:262.

قَبْضًا يَسِيرًا ﴿٢٥﴾

“Tunakivutia kwetu Yasiiraa.”

Maana yake: Kidogo kidogo.¹ Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ اللَّيْلَ لِبَاسًا

“Naye Ndiye Aliyekufanyieni usiku kuwa ni vazi.”

Maana yake: Inaficha na kufunika vitu vyote kabisa. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿٢٦﴾

“Naapa kwa usiku ufunikapo kila kitu.” (92:1).

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَالنَّوْمَ سُبَاتًا

“Na usingizi kuwa mapumziko.”

Maana yake” Inakata harakati na mizunguko na hivyo kuwa starehe mwilini, kwani viungo vinapata uzito mwingi wa mihangaiko wakati wa mchana ili kutafuta riziki na maisha. Hivyo, ukija usiku na utulivu wake, harakati zinapungua, hivyo kupumzika. Mtu akawa anapata usingizi wenye raha tele kwa mwili na roho pamoja. Kisha Anasema Allah تعالى:

وَجَعَلَ النَّهَارَ ذُشُورًا ﴿٢٧﴾

“Na Akakufanyieni mchana ni kufufuka.”

Maana yake: Wanatawanyika watu kutafuta riziki ndani yake na mapato yao na sababu zao. Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

وَمِن رَّحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

“Na kwa Rehema Zake Amekufanyieni usiku na mchana ili mpumue hapo usiku na mtafute Fadhila Zake (hapo mchana).” (28:73).

¹ Rejea pitio la nyuma.

وَهُوَ الَّذِي أَرْسَلَ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۗ وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً طَهُورًا ﴿٤٨﴾
 لِنُحْيِيَ بِهِ بَلَدَةً مَيِّتًا وَنُسْقِيَهُ مِمَّا خَلَقْنَا أَنْعَمًا وَأُنَاسٍ كَثِيرًا ﴿٤٩﴾ وَلَقَدْ صَرَّفْنَاهُ
 بَيْنَهُمْ لِيَذَّكَّرُوا فَأَبَى أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٥٠﴾

48. Naye Ndiye Anayezituma pepo kuwa bishara njema kabla ya Rehema Yake, na Tunayateremsha kutoka mbinguni maji safi.

49. Ili kwa hayo Tuihuishe nchi iliyokufa, na Tuwanyweshe wanyama na watu wengi Tuliowaumba.

50. Na kwa yakini Tumeisarifu kati yao wapate kukumbuka. Lakini watu wengi wanakataa ila kukufuru”.

Na hii pia ni katika Uweza Wake uliokamilika na Ufalme Wake Mtukufu. Na Yeye Ndiye Mwenye Kutuma upepo kuwa ni bishara njema, yaani kwa kuja mawingu baada yake. Na pepo ni aina kadhaa katika sifa nyingi, kutegemea na malengo ya kutumwa kwake. Baadhi yake zinatengeneza mawingu, na nyengine zinayabeba, na nyengine zinayasafirisha, na nyengine zinazokuja kabla ya hapo hushitua ardhi na nyengine zinayabandikiza mawingu ili kunyeshe mvua. Na kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً طَهُورًا ﴿٤٨﴾

“Na Tunayateremsha kutoka mbinguni maji safi.”

Yaani, kama zana ya kujisafishia kutokana na chakula, mafuta na unavyofanana na hivyo. Na imepokewa kwa Abi Said kuwa aliulizwa Mtume wa Allah: “Je, tunaweza tawadha maji ya kisima cha *Budhaa’ah*? Nacho ni kisima kinachonuka kwa taka na nyama ya mbwa inayotupwa ndani yake?” Akasema:

«إِنَّ الْمَاءَ طَهُورٌ لَا يُتَجَسَّهُ شَيْءٌ»

“Hakika maji ni safi na tohara, hivyo hayanajisiki na chochote”.

Hii Hadithi imenukuliwa na Ash-Shaafi’iy na Ahmad ambaye ameisahihisha, Abu Dawud, At-Tirmidhiy amesema kuwa ni Hasan na An-Nasa’iy.¹

¹ *Musnad* Ash-Shafi’iy 1:21, Ahmad 3:31, Abu Dawud 1:53, *Tuhfat ul-Ahwadh* 1:203 na Annasai 1:174.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لِنُخِىَ بِهِ بَلَدَةً مَّيْتًا

“Ili kwa hayo Tuihishe nchi iliyokufa.”

Maana yake: Ardhi ambayo imengojea sana mvua, hivyo kuifanya yabisi, na iliyokufa haina mimea, miti wala kitu chochote. Lakini pindi unapokuja uhai inaishi na kupata kuongezeka kwa aina na rangi tofauti za maua, kama Alivyosema Allah تعالى:

فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ

“Lakini Tunapoyateremsha maji juu yake husisimka na kututumka.” (22:5).

Na hapa Amesema Aliyetukuka:

وَدُشِقِيهِمْ مِمَّا خَلَقْنَا أَنْعَمًا وَنَاسِيًّا كَثِيرًا

“Na Tuwanyweshe wanyama na watu wengi Tuliowaumba.”

Hii inamaanisha wanakunywa hayawani miongoni mwa nyama hoa na watu wanaohitaji upeo wa haja kwa kunywa na kwa ukulima na matunda pia. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَأَنْظُرْ إِلَىٰ آثَارِ رَحْمَتِ اللَّهِ كَيْفَ يُخَيِّ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا

“Basi ziangalie alama za Rehema za Allah. Jinsi Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake” (30:50).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَقَدْ صَرَّفْنَاهُ بَيْنَهُمْ لِيَذَّكَّرُوا

“Na kwa yakini Tumeisarifu kati yao wapate kukumbuka”.

Maana yake: Tunateremsha mvua sehemu ya ardhi na kuinyima nyengine, na pia Tunalibebesha mzigo wingu linalopita juu ya sehemu ya ardhi moja na kwenda katika ardhi nyengine na kunyesha hapo mvua ambayo inawatosha au kujaalia kuwa nyingi sana. Na ilhali ile ardhi iliyo nyuma yake haijanyesha hata tone moja la maji, kuna sababu na hekima kubwa mno nyuma ya hili.

Ibn 'Abbaas na Ibn Mas'uud رضي الله عنهما wamesema: "Sio mwaka mmoja una mvua nyingi zaidi kuliko mwaka mwengine, lakini Allah تعالى Anaisarifu Anavyotaka." Kisha wakasoma Aya hii:

وَلَقَدْ صَرَّفْنَاهُ بَيْنَهُمْ لِيَذَّكَّرُوا فَأَبَى أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٥٤﴾

"Na kwa yakini Tumeisarifu kati yao wapate kukumbuka. Lakini watu wengi wanakataa ila kukufuru".¹

Ili waweze kukumbuka vile Allah تعالى Alivyoihisha ardhi iliyokufa kuwa Yeye Anaweza Kuwahuisha maiti na pia mabaki ya mifupa. Au wakumbuke kuwa aliyewanyima mvua ni kwa sababu ya madhambi wanayoyafanya, Kwa hivyo wajivue kwenye yale waliyonayo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَأَبَى أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٥٤﴾

"Lakini watu wengi wanakataa ila kukufuru".

Amesema 'Ikrimah: "Hii inamaanisha wale wanaosema kuwa mvua imenyeshwa kwa sababu ya kadhaa na kadhaa".² Haya ndiyo aliyosema 'Ikrimah kama ilivyokuja katika Hadithi Sahihi iliyonukuliwa katika Sahih Muslim kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa aliwaambia Maswahaba wake siku moja - kwa ile athari ya mawingu iliyoonekana usiku wake:

«أَتَذَرُونَ مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ؟»

"Je, munajua aliyosema Mola wenu Mlezi?"

Wakasema: "Allah na Mtume wake wanajua zaidi". Akasema:

«قَالَ: أَصْبَحَ مِنْ عِبَادِي مُؤْمِنٌ بِي وَكَافِرٌ، فَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِفَضْلِ اللَّهِ وَرَحْمَتِهِ فَذَلِكَ مُؤْمِنٌ بِي، كَافِرٌ بِالْكَوْكِبِ، وَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِتَوَّءٍ كَذَا وَكَذَا، فَذَلِكَ كَافِرٌ بِي، مُؤْمِنٌ بِالْكَوْكِبِ»

"Amepambazukiwa mja Wangu Muumini na Kafiri. Ama kwa yule aliyesema: Mvua imenyeshwa kwa Fadhila ya Allah na Rehema Yake, basi huyo ndiye aliyeniamini na kukufuru nyota. Na ama yule aliyesema: Kumenyeshwa kwa sababu ya kadhaa na kadhaa, basi huyo amenikanusha Mimi na kuamini nyota".³

¹ Atw-Twabariy 19:280.

² Atw-Twabariy 19:280.

³ Muslim 1:83.

وَلَوْ شِئْنَا لَبَعَثْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ نَذِيرًا ﴿٥١﴾ فَلَا تَطِعِ الْكَافِرِينَ وَجَاهِدْهُمْ بِهِ جِهَادًا
كَبِيرًا ﴿٥٢﴾ * وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ وَجَعَلَ
بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا وَحِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٥٣﴾ وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ مِنَ الْمَاءِ بَشَرًا فَجَعَلَهُ نَسَبًا وَصِهْرًا
وَكَانَ رَبُّكَ قَدِيرًا ﴿٥٤﴾

51. "Na Tungelitaka Tungelipeleka katika kila mji Mwonyaji.

52. Basi usiwatii makafiri. Na pambana nao kwayo kwa Jihadi kubwa.

53. Naye Ndiye Aliyezipeleka bahari mbili, hii tamu mno, na hii ya chumvi chungu. Na Akaweka baina yao kinga na kizuizi kizuiacho.

54. Naye Ndiye Aliyeumba mwanadamu kutokana na maji, Akamjaalia kuwa na nasaba na ushemeji. Na Mola wako Mlezi ni Muweza".

Ujumbe wa Muhammad ﷺ ni kwa Watu Wote, na Ukumbusho wa Neema za Allah تعالیٰ kwa Wanadamu.

Ili hawa waonyaji waweze kuwalingania kwa Allah Aliyetukuka, lakini Tumekuteua wewe ee Muhammad uwe ni mjumbe kwa wanadamu wote katika ardhi. Na hivyo hivyo Tumekuamuru kuifikisha hii Qur'ani (kwa kila mtu). Allah تعالیٰ Anasema:

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

"Ili kwayo Nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia." (6:19).

Aidha Kauli Yake

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَأَلْنَاوْهُ مَوْعِدَهُ

"Na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao." (11: 17). Kadhalika

لَتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا

"Na ili uwaonye Mama wa Miji na walio pembezoni mwake." (6: 92). Na pia:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote.”
(7:158).

Na katika Sahihi mbili:

«بُعِثْتُ إِلَى الْأَحْمَرِ وَالْأَسْوَدِ»

“Nimetumwa kwa wekundu na weusi”.

Na ndani ya sahihi hizo:

«وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

“Na kila Mtume alikuwa akitumwa hasa kwa kaumu yake, lakini mimi nimetumwa kwa watu wote kwa ujumla”.¹

Na kwa hiyo, Allah تعالى Amesema:

فَلَا تُطِعِ الْكَافِرِينَ وَجَاهِدْهُمْ بِهِ

“Basi usiwatii makafiri. Na pambana nao kwayo kwa Jihadi kubwa”.

Maana yake: Kwa kutumia Qurani. Amesema hayo Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما.²

Kisha Akasema:

جِهَادًا كَبِيرًا

“Jihadi kubwa”.

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ جَاهِدِ الْكُفَّارَ وَالْمُنَافِقِينَ

“Ewe Nabii! Shindana na makafiri na wanafiki.” (66: 9).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

* وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ

“Naye Ndiye Aliyezipeleka bahari mbili, hii tamu mno, na hii ya chumvi chungu.”

¹ Fat’h al-Baariy 1:634 na Muslim 1:370.

² Atw-Twabariy 19:281.

Hii ina maana kuwa Allah تعالی Ameumba maji aina mbili: ya tamu na ya chumvi. Maji hayo yaliyo tamu ni kama yale ya mito, na chemichemi, vijito na visima, na hii ndio bahari tamu mno. Amesema haya Ibn Jurayj na Ibn Jariir. Na hii ina maana ambayo haina shaka ndani yake, kwani hakuna bahari tulivu ila hii yenye maji ya tamu. Na hakika Allah تعالی Amehabarisha uhalisia wa jambo hili, ili Awazindue waja kwa Neema Yake juu yao wapate kumshukuru. Hakika ni kuwa bahari hii ya tamu ni inayopita baina ya watu, Ameitenga Allah تعالی baina ya waja Wake kwa mahitaji yao, mito na chemichemi kila sehemu ya ardhi kutegemea mahitaji yao na kuwatosheleza nayo kwa ajili ya nafsi na ardhi zao. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ

“Na hii ya chumvi chungu.”

Maana yake: yenye chumvi chungu isiyopendeza. Ambayo ni Mjumuiiko wa bahari zinazojulikana Mashariki na Magharibi ya ardhi: Bahari ya Atlantiki mpaka kufikia ile mikono yake membamba, na Bahari nyekundu, na Bahari ya Yemen, na Bahari ya Basrah, Bahari ya Uajemi. Na pia Bahari ya China na Hindi, na Bahari ya Mediterania, Bahari ya Khazar na zingine na bahari zilizotulia ambazo hazitembei. Lakini zenye mawimbi na kufura na kugongana wakati wa kusi (baridi) na ukali wa upepo. Na kuna bahari ambazo Maji yake hujaa na kupwa katika kila mwanzo wa mwezi maji hujaa na kufurika. Na mwezi kila unapopungua siku zake maji nayo hupungua na kurudi katika sura yake ya mwanzo. Na mwezi mwandamo unapochomoza tarehe ya mwezi mwengine nayo huanza kujaa na kuzidi hadi tarehe ya mwezi kumi na nne, kisha huanza tena kupungua. Hivyo Anayapeleka Allah تعالی, Naye ni Mwenye Uweza uliotimia, Ameweka kanuni katika hizo. Bahari zote hizi zimetulia, Amezifanya kuwa chumvi ili kuzuia uvundo kwa sababu ya hayawani wanaokufa ndani yake, hivyo ardhi yote ikaharibika. Na kwa kuwa maji yake ni ya chumvi, hewa yake ni sahihi na maiti wake ni wazuri. Na kwa ajili hiyo Mtume ﷺ alisema baada ya kuulizwa kuhusu maji ya bahari: “Je, tunaweza kuyatawadhia?” Akasema:

¹ Al-Muwatwtwa' 1:22, Musnad Ash-Shaafi'iy 1:23, Ahmad 2:361, Abu Daawuud 1:64, Tuhfat al-Ahwadhiy 1: 224, An-Nasaa'iy 1:50 na Ibn Maajah 1:136.

«هُوَ الطَّهُورُ مَاؤُهُ، الْحِلُّ مَيْتُهُ»

“Maji yake ni safi na tohara na maiti zake ni halali.”

Imepokewa na Maimamu - Malik, Ash-Shaafi’iy, Ahmad na watu wa Sunan kwa Isnadi nzuri.¹ Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا وَحِجْرًا

“Na akaweka baina yao kinga na kizuizi.”

Maana yake: Baina ya yale maji matamu na ya chumvi.

بَرْزَخًا

“Kingo.” Maana yake: Nchi kavu katika ardhi.

وَحِجْرًا مَحْجُورًا

“Na kizuizi kizuicho.”

Maana yake: Yenye kuzuilia ili isifike moja wapo kwa ile nyingine. Hii ni sawa na Kauli ya Aliyetukuka:

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ﴿٥٥﴾ بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَّا يَبْغِيَانِ ﴿٥٦﴾ فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٧﴾

“Anazikutanisha bahari mbili (ya maji ya chumvi na yale ya tamu). Baina yao kuna kizuizi, haziingiliani kabla. Basi ipi katika neema za Mola wenu Mlezi mnayoikanusha.” (55:19-21).

Na Kauli Yake:

أَمَّنْ جَعَلَ الْأَرْضَ قَرَارًا وَجَعَلَ خِلَالَهَا أَنْهَارًا وَجَعَلَ لَهَا رَوَاسِيَ وَجَعَلَ بَيْنَ الْبَحْرَيْنِ حَاجِزًا ۗ أَلَيْسَ مَعَ اللَّهِ بِلَا أَكْثَرُ لَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦١﴾

“Au Yule Aliyefanya ardhi kuwa mahali pa matulio, na Akaweka ndani yake mito na Akaiweka milima, na Akaweka kizuizi baina ya bahari mbili, Je, yuko mungu pamoja na Allah? Bali wengi katika wao hawajui.” (27: 61).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ مِنَ الْمَاءِ بَشَرًا

“Naye Ndiye Aliyeumba mwanadamu kutokana na maji.”

Hii ina maana kuwa mwanadamu ameumbwa kwa mchanganyiko wa mbegu za uzazi (ya mwanaume na mwanamke) dhaifu, Akamtengeneza na kumlinganisha sawa sawa na Akamjaalia kuwa kamili katika umbo la mwanaume au mwanamke kama Anavyopenda. Kisha Akasema:

فَجَعَلَهُ نَسَبًا وَصِهْرًا

“Akamjaalia kuwa na nasaba na ushemeji.”

Mwanzoni mwa kuzaliwa kwake anakuwa na nasaba inayojulikana, kisha anaoa, hivyo kuwa na ukwe. Kisha anakuwa na mashemeji na jamaa. Na yote hayo yanapatikana kwa maji yaliyo dhaifu. Na hivyo Akasema Aliyetukuka:

وَكَانَ رَبُّكَ قَدِيرًا

“Na Mola wako Mlezi ni Muweza.”

* * *

وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُهُمْ وَلَا يَضُرُّهُمْ ۗ وَكَانَ
 الْكَافِرُ عَلَىٰ رَبِّهِ ظَهِيرًا ﴿٥٥﴾ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا مُبَشِّرًا
 وَنَذِيرًا ﴿٥٦﴾ قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِلَّا مَنْ شَاءَ
 أَنْ يَتَّخِذَ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿٥٧﴾ وَتَوَكَّلْ عَلَىٰ آلِهِنَا
 الَّتِي لَا يَمُوتُ وَسَبِّحْ بِحَمْدِهِ ۗ وَكَفَىٰ بِهِ بِذُنُوبِ
 عِبَادِهِ خَبِيرًا ﴿٥٨﴾ الَّتِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا
 بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۗ الرَّحْمَنُ
 فَسْتَلِّ بِهِ خَبِيرًا ﴿٥٩﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اسْجُدُوا لِلرَّحْمَنِ
 قَالُوا وَمَا الرَّحْمَنُ أَنَسْجُدُ لِمَا تَأْمُرُنَا وَزَادَهُمْ نُفُورًا ﴿٦٠﴾
 تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَجَعَلَ فِيهَا سِرَاجًا
 وَقَمَرًا مُنِيرًا ﴿٦١﴾ وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ خِلْفَةً
 لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يَذَّكَّرَ أَوْ أَرَادَ شُكُورًا ﴿٦٢﴾ وَعِبَادُ
 الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ
 الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٦٣﴾ وَالَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ
 سُجَّدًا وَقِيَامًا ﴿٦٤﴾ وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا
 عَذَابَ جَهَنَّمَ ۗ إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٥﴾ وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ
 يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا ﴿٦٦﴾

وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُهُمْ وَلَا يَضُرُّهُمْ ۗ وَكَانَ الْكَافِرُ
 عَلَىٰ رَبِّهِ ظَهِيرًا ﴿٥٥﴾ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ
 إِلَّا مُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٥٦﴾ قُلْ مَا
 أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِلَّا مَنْ شَاءَ
 أَنْ يَتَّخِذَ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿٥٧﴾
 وَتَوَكَّلْ عَلَىٰ آلِهِنَا الَّتِي لَا
 يَمُوتُ وَسَبِّحْ بِحَمْدِهِ ۗ وَكَفَىٰ
 بِهِ بِذُنُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا ﴿٥٨﴾
 الَّتِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا
 بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى
 الْعَرْشِ ۗ الرَّحْمَنُ فَسْتَلِّ بِهِ خَبِيرًا
 ﴿٥٩﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اسْجُدُوا
 لِلرَّحْمَنِ قَالُوا وَمَا الرَّحْمَنُ أَنَسْجُدُ
 لِمَا تَأْمُرُنَا وَزَادَهُمْ نُفُورًا ﴿٦٠﴾

55. "Na wanayaabudu badala ya Allah yasiyo-wafaa wala yasiyowadhuru. Na kafiri daima ni msaidizi wa kumpinga Mola wake Mlezi.

56. Nasi Hatukukutuma ila kuwa ni Mbashiri na Mwonyaji.

57. Sema: Sikukuombeni ujira juu yake; ila atakaye na ashike njia iendayo kwa Mola wake Mlezi.

58. Na mtegemee Aliye Hai, Ambaye Hafi. Na umtukuze kwa Sifa Zake. Na yatosha Kwake kuwa Yeye ni Mwenye habari za dhambi za waja Wake.

59. Ambaye Ameziumba mbingu na ardhi, na vilivyomo ndani yake kwa siku sita. Kisha Akakaa juu ya Arshi, Ar-Rahmaan, Mwingi wa Rehema! Uliza habari Zake kwa wamjuaye.

60. Na wanapoambiwa: Msujudieni Ar-Rahmaan! Wao husema: Ni nani Ar-Rahmaan? Je! Tumsujudie unayetumrisha wewe tu? Na huwazidishia chuki”.

Ujinga wa Washirikina

Allah تعالی Anatupasha habari kuhusu ujinga wa washirikina ambao wanaabudu asiyekuwa Allah تعالی kama masanamu ambayo hayawezi kuwadhuru wala kuwanufaisha. Wanafanya haya bila dalili wala hoja iliyowapelekea katika hilo bali ni rai tu na hawaa na matamano yao. Hivyo, wanawachukua kama wasaidizi na wanapigana kwa ajili yao, na wanakuwa na uadui dhidi ya Allah تعالی, na Mtume Wake na Waumini kwa ajili yao. Na kwa hivyo Akasema Aliyetukuka:

وَكَانَ الْكَافِرُ عَلَىٰ رَبِّهِ ظَهِيرًا ﴿٥٦﴾

“Na kafiri daima ni msaidizi wa kumpinga Mola wake Mlezi.”

Hii ina maana kuwa yeye ni msaidizi katika njia ya Shetani dhidi ya kipote cha Allah تعالی, na kipote cha Allah تعالی ndicho chenye kushinda. Hayo ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَاتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّهِ ءَالِهَةً لَّعَلَّهُمْ يُنصَرُونَ ﴿٥٧﴾ لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَهُمْ وَهُمْ لَهُم جُنْدٌ

مُحْضَرُونَ ﴿٥٨﴾

“Na wameishika miungu mingine badala ya Allah ili wapate kusaidiwa nao! Lakini hawawezi kuwasaidia kabisa. Wao hao wanaowaabudu ndio wanaokuwa maaskari wanaohudhurishwa.” (36:74-75).

Hii inamaanisha wale miungu yao ambao wamewachukua mbali na Allah تعالى, wao hawamiliki usaidizi na nusra. Na hawa wajinga ndio wanakuwa ni maaskari wa masanamu hayo nao wanapigana kwa ajili yao na wanalinda madhabahu yao, lakini mwisho wake ushindi utakuwa ni wa Allah تعالى, Mtume Wake na Waumini hapa duniani na kesho Akhera. Amesema Mujaahid:

وَكَانَ الْكَافِرُ عَلَىٰ رَبِّهِ ظَهِيرًا ﴿٥٨﴾

“Na kafiri daima ni msaidizi wa kumpinga Mola wake Mlezi”.

Akasema: “Anamsaidia Shetani katika kumuasi Allah تعالى.”

Mtume ﷺ ni Mbashiri na Mwonyaji

Kisha Aliyetukuka Anamwambia Mtume Wake:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا مُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٥٩﴾

“Nasi Hatukukutuma ila kuwa ni Mbashiri na Mwonyaji”.

Hii ina maana kuwa unawapa bishara njema Waumini na kuwaonya makafiri. Unatoa bishara kwa mwenye kumtii Allah تعالى kuwa mashukio yake yatakuwa Peponi na kuonya adhabu kali kwa wale wenye kwenda kinyume na Amri ya Allah تعالى. Anasema Aliyetukuka:

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ

“Sema: Sikukuombeni ujira juu yake”,

Maana yake: Sitaki ujira wa malipo katika mali yenu kwa kufikisha ujumbe huo na onyo hili. Kwa hakika mimi nafanya hayo ili kupata Radhi za Allah تعالى. Naye Anasema:

لِمَنْ شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَسْتَقِيمَ ﴿٦٠﴾

“Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kushika njia.” (81:28).

Na Anaendelea:

إِلَّا مَنْ شَاءَ أَنْ يَتَّخِذَ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿٦١﴾

“Ila atakaye na ashike njia iendayo kwa Mola wake Mlezi.”

Maana yake: Njia na mfumo wa kufuatwa kwa niliyokuja nayo.

Amri kwa Mtume Kumtegemea Allah تعالى na Kutaja Baadhi ya Sifa Zake

Kisha Anasema Aliyetukuka:

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْحَيِّ الَّذِي لَا يَمُوتُ

“Na mtegemee Aliye Hai, Ambaye Hafi”.

Maana yake: Katika mambo yako yote kuwa ni mwenye kumtegemea Allah تعالى Aliye Hai ambaye hafi daima (Atabaki Hai milele). Ambaye:

الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣﴾

“Yeye Ndiye wa Mwanzo na Ndiye wa Mwisho, Naye Ndiye wa Dhahiri na wa Siri, Naye Ndiye Mjuzi wa kila kitu” (57:3).

Yeye Ndiye wa Milele, Mwenye Kubaki, Mwenye Kuishi wakati wote na daima, Aliye Hai, Mwendeshaji wa mambo yote na Mola Mlezi wa kila kitu na Mwenye vyote hivyo. Na ni Yeye Ambaye unatakiwa urudi Kwake kila wakati. Naye Ndiye Ambaye Anategemewa na Ambaye unatakiwa urudi Kwake kupata ulinzi, kwani Yeye Atakutosha na Atakusaidia na Atakufanya ushinde. Kwa hilo Aliyetukuka Amesema:

﴿ يَتَأْتِيهَا الرُّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَغْتَ رِسَالَتَهُ ۗ وَاللَّهُ

يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe Wake. Na Allah Atakulinda na watu.” (5:67)

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَسَبِّحْ بِحَمْدِهِ

“Na umtukuze kwa Sifa Zake”, Maana yake: Changanya baina ya Kumhimidi (kwa kusema *Alhamdulillah*) na Kumtakasa. Na kutekeleza hilo Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ»

“Umetakasika, ewe Allah, Mola wetu Mlezi na Sifa zote njema ni Zako”.¹

¹Fat-h al-Baariy 2:328.

Hii ina maana, Ninamtakasia 'Ibada Yake na Kumtegemea, kama Alivyosema:

رَبِّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾

“Yeye Ndiye Mola Mlezi wa mashariki na magharibi - hakuna muabudiwa ila Yeye, basi mfanye kuwa Mlinzi wako.” (73:9).

Na Amesema Aliyetukuka:

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ

“Basi muabudu Yeye na umtegemee Yeye.” (11:123).

Na Amesema Aliyetukuka:

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ ءَامَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا

“Sema: Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema, tunamuamini Yeye, na tunamtegemea Yeye.” (67:28).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَكَفَىٰ بِهِ بَدَأُتُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا ﴿٢٨﴾

“Na yatasha Kwake kuwa Yeye ni Mwenye habari za dhambi za waja Wake.”

Hii ina maana, kwa Elimu Yake iliyotimu, ambayo hapana linalojificha Kwake. Wala hakifichikani Kwake kitu chochote, hata kile chenye uzito wa chembe ndogo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

“Ambaye Ameziumba mbingu na ardhi.” Maana: Yeye Ndiye Aliye Hai daima na Hafi. Naye Ndiye Muumbaji wa kila kitu na ni Mola Mlezi na Mwenye Kumiliki. Yeye Ndiye Aliyeumba kwa Uweza wa Ufalme Wake, mbingu saba kwa urefu wake mkubwa na upana wake na ardhi saba zenye kina kirefu na uzito mkubwa. Anasema Allah تعالیٰ:

فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

“Kwa siku sita. Kisha Akakaa juu ya Arshi.”

Maana yake: Anapelekesha mambo yote, na Anahukumu kwa haki na Yeye ni Mbora wa wenye kuhukumu. Na Kauli Yake:

ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۗ الرَّحْمَنُ فَسَلَّ بِهِ خَيْرًا ﴿٥٥﴾

**“Kisha Akakaa juu ya Arshi, Ar-Rahmaan, Mwingi wa Rehema!
Uliza habari Zake kwa wamjuaye.”**

Hii ina maana, kuwa mjue Yeye kwa yule mwenye kumjua vyema kabisa na hivyo mchukue Yeye kama kielelezo chako. Inajulikana kuwa hakuna anayemjua zaidi Allah تعالیٰ, kuliko Muhammad ﷺ mja Wake na Mtume Wake, mtukufu wa kizazi cha Nabii Adam عليه السلام duniani na Akhera. Hakika yeye hazungumzi kwa matamania ya nafsi yake bali anayozungumza ni Wahyi anaoteremshiwa. Lolote analosema ni sawa na kweli, naye ni kiongozi (Imamu) mwenye kuhukumu. Pindi wazozanapo watu katika jambo lolote ni wajibu kuurudisha mzozo wao kwake na lolote linalokwenda sambamba na kauli na vitendo vyake ni haki, na linalokwenda kinyume navyo linakataliwa kwa huyo msemaji au mtendaji yeyote awaye. Allah تعالیٰ Anasema:

فَإِن تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ

**“Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi
Mungu na Mtume.” (4:59).**

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِنْ شَيْءٍ فَحُكِّمُوهُ إِلَى اللَّهِ

**“Na mkihitilafiana katika jambo lolote hukumu yake iko kwa
Allah.” (42:10).**

Na Allah تعالیٰ Amesema,

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

**“Na yametimia Maneno ya Mola wako Mlezi kwa kweli na uadilifu.”
(6:115).**

Hii inamaanisha kuwa, ni Mkweli katika Kutoa Habari na ni Muadilifu katika Kutoa Amri na Makatazo. Na hivyo hapa Anasema:

فَسَلَّ بِهِ خَيْرًا ﴿٥٥﴾

“Uliza habari Zake kwa wamjuaye.”

Shutuma kwa Mushirikina

Kisha Allah تعالى Anasema - Kuwakaripia washirikina ambao wanasujudia masanamu na wapinzani wengine badala ya Allah تعالى:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اسْجُدُوا لِلرَّحْمَنِ قَالُوا وَمَا الرَّحْمَنُ

“Na wanapoambiwa: Msujudieni Ar-Rahmaan! Wao husema: Ni nani Ar-Rahmaan?”

Hii ina maana kuwa sisi hatumjui Ar-Rahmaan. Hakika wao hawakupendelea kabisa Allah تعالى kuitwa kwa jina la Ar-Rahmaan kama walivyokataa hilo Siku ya Hodaybiyah pale Mtume ﷺ alipomuambia mwandishi:

«اتَّخَبَ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ»

“Andika kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu (Bismillahir Rahmaanir Rahiim).”

Wakasema: “Sisi hatumjui Ar-Rahmaan wala Ar-Rahiim, lakini kama tulivyokuwa tukiandika: Bismika Allahumma (Kwa jina Lako ewe Allah)”¹ Kwa ajili hiyo Allah تعالى Aliteremsha:

قُلْ أَدْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيًّا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ

“Sema: Muombeni Allah, au muombeni Ar-Rahmaan, kwa jina lolote mnalomuita. Kwani Yeye Ana Majina mazuri mazuri” (17: 110).

Hii ina maana kuwa Yeye ni Allah تعالى na pia Yeye ni Ar-Rahmaan. Na katika Ayah hii Allah تعالى Anasema:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اسْجُدُوا لِلرَّحْمَنِ قَالُوا وَمَا الرَّحْمَنُ

“Na wanapoambiwa: Msujudieni Ar-Rahmaan! Wao husema: Ni nani Ar-Rahmaan?”

Maana yake: Hatumjui wala hatulikubali Jina hilo.

¹ Ahmad 3:268.

أَسْجُدْ لِمَا تَأْمُرُنَا ﴿٦٦﴾

“Je Tumsujudie unayetuarisha wewe tu?”

Hii ina maana kuwa kwa ajili tu ya kauli yako kwetu sisi. Na hivyo:

وَزَادَهُمْ ثُفُورًا ﴿٦٧﴾

“Na huwazidishia chuki”.

Ama Waumini, hakika wao wanamuabudu Allah تعالى, Ambaye Ndiye Ar-Rahmaan na Ar-Rahiim, na wanampwekesha Yeye katika 'Ibadah na Uungu na wanamsujudia Yeye tu. Na hakika wameafikiana wanazuoni, Allah Awarehemu, ya kuwa sijda hii ambayo iko katika *Suratul Furqaan* kwa mwenye kusoma au kuisikia ni sharia mtu asujudu anapofika sehemu hiyo. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَجَعَلَ فِيهَا سِرَاجًا وَقَمَرًا مُنِيرًا ﴿٦٨﴾ وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ

الَّيْلَ وَالنَّهَارَ خَلْفَةً لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يَذَّكَّرَ أَوْ أَرَادَ شُكُورًا ﴿٦٩﴾

61. “Ametukuka Aliyeziijaalia nyota mbinguni, na Akajaalia humo taa na mwezi unaong’ara.

62. Naye Ndiye Aliyefanya usiku na mchana kufuatana kwa nafuu ya anayetaka kukumbuka, au anayetaka kushukuru”.

Ubainifu wa Utukufu na Uweza wa Allah تعالى

Anasema Aliyetukuka kwa Kujisifu Yeye Mwenyewe na Kujitukuza kutokana na uzuri wa Alivyoviumba mbinguni kama *Al-Buruj*, nazo ni sayari kubwa, kama walivyosema Mujaahid na Sa’iid ibn Jubayr, na Abi Swalih, na Al-Hasan na Qataadah.¹ Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحَ

“Na hakika Tumeipamba mbingu hii ya karibu kwa mataa.” (67:5).

¹ Atw-Twabariy 19:289 na Al-Baghawaiy 3:374.

Na hivyo Akasema Aliyetukuka:

تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا

“Ametukuka Aliyezijaalia nyota mbinguni, na Akajaalia humo taa.”

Na hilo ni jua ambalo linawaka na kung'aa kama taa kwa kuwepo kwake. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَجَعَلْنَا سِرَاجًا وَهَاجًا ﴿١٣﴾

“Na Tukaifanya taa ing'arayo na yenye joto kubwa.” (78:13).

وَقَمَرًا مُنِيرًا ﴿١٤﴾

“Na mwezi unaong'ara.”

Maana yake: Ing'arayo na kumulikwa na mwangaza wa kitu chengine, tofauti na mwangaza wa jua, kama Alivyosema Aliyetukuka:

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا

“Yeye Ndiye Aliyejaalia jua kuwa na mwangaza, na mwezi ukawa na nuru.” (10:5).

Na Allah تعالى Anatuelezea kuhusu Nuuh عليه السلام alipowaambia kaumu zake:

أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا ﴿٥١﴾ وَجَعَلَ الْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسَ

سِرَاجًا ﴿٥٢﴾

“Je, hamuoni jinsi Allah Alivyoziumba mbingu saba tabaka tabaka. Na Akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru na Akalifanya jua kuwa taa.” (71:15-16).

Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ خِلْفَةً

“Naye Ndiye Aliyefanya usiku na mchana kufuatana.”

Hii ina maana kuwa kila moja kinakuja baada ya chengine, zinabadilishana bila ya kikomo. Kinapotoweka hiki kinakuja hiki, na kinapokuja hiki kinakwenda kile, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَسَخَّرَ لَكُمْ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبِينَ^١

“Na Akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu.”
(14: 33).

Na Akasema:

يُغْشَى اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا

“Huufunika usiku na mchana, ufuatao upesi upesi.” (7:54).

Na Akasema:

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ

“Haliwi jua kuufikia mwezi.” (36:40).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يَذْكَرَ أَوْ أَرَادَ شُكُورًا

“Kwa nafuu ya anayetaka kukumbuka, au anayetaka kushukuru.”

Hii inamaanisha kuwa Allah تعالى Amezijaalia kufuatana moja baada ya nyingine ili kutuonesha nyakati za waja Wake kumuabudia Yeye. Hivyo, yeyote atakayekosa kufanya amali wakati wa usiku, anaweza kuzifanya wakati wa mchana. Na yeyote atakayekosa kufanya amali wakati wa mchana anaweza kuzifanya wakati wa usiku. Hakika imenukuliwa Hadithi Sahihi:

«إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يَسْطُرُ يَدَهُ بِاللَّيْلِ لِيَتُوبَ مُسِيءَ النَّهَارِ، وَيَسْطُرُ يَدَهُ بِالنَّهَارِ لِيَتُوبَ مُسِيءَ اللَّيْلِ»

“Hakika Allah Aliyetukuka Hunyoosha Mkono Wake usiku kwa yule aliyefanya dhambi mchana kutubia. Na pia Hunyoosha Mkono Wake mchana kwa yule aliyefanya madhambi usiku kutubia.”¹

¹ Muslim 4:2113.

Na wamesema Mujaahid na Qataadah: “*Khilfatan*”, Ina maana ya tofauti, yaani moja kiza na nyingine ni ya mwangaza.¹

وَعِبَادُ الرَّحْمَنِ الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٥٧﴾ وَالَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقِيَامًا ﴿٥٨﴾ وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٥٩﴾ إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٠﴾ وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا ﴿٦١﴾

63. “Na waja wa Ar-Rahmaan (Mwingi wa Rehema) ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza husema: Salama!

64. Na wale wanaokesha kwa ajili ya Mola wao Mlezi kwa kusujudu na kusimama.

65. Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu ya Jahanamu. Hakika adhabu yake ikimpata mtu haimwachi.

66. Hakika hicho ni kituo na makao mabaya.

67. Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo”.

Ubainifu wa Sifa za Waja wa Mwingi wa Rehema

Hizi ni sifa za Waja Waumini wa Allah تعالى. Allah تعالى Anasema:

الَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى الْأَرْضِ هَوْنًا

“Ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha.”

Maana yake: Kwa utulivu, staha na unyenyekevu bila ya kujigamba wala kiburi. Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

¹ At-Tabari 19:290–291.

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا

“Wala usitembee katika ardhi kwa maringo.” (17:37).

Ama watu hawa, wanatembea bila ya kiburi wala maringo wala mzaha wala kwa majivuno na majisifu. Hii haimaanishi kuwa watembea kama wagonjwa, kwa kujifanyiza na kuwaonesha watu, kwani hakika Mtukufu wa watoto wa Adam عليه السلام, Mtume ﷺ alikuwa akitembea kama kwamba anashuka mlima na kama kwamba ardhi ilikuwa ikivunjwa chini yake. Na hakika maana halisi ya *Hawn* hapa ni utulivu, staha na unyenyekevu, kwani Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا أَتَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَلَا تَأْتَوْهَا وَآتَيْتُمْ تَسْمَعُونَ، وَأَتَوْهَا وَعَلَيْكُمْ السَّكِينَةُ فَمَا أَدْرَكْتُمْ مِنْهَا فَصَلُّوا، وَمَا فَاتَكُمْ فَأْتُوا»

“Mnapokuja kwa ajili ya Swala, msije na ilhali mnakimbia kwa haraka. ijieni hali ya kuwa katika utulivu, mtakachopataswalini, na kilichowapita, timizeni (kamilisheni).”¹

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِذَا حَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا

“Na wajinga wakiwasemeza husema: Salama!”

Pale wanapotukanwa na watu wajinga kwa maneno mabaya, hawawakabili kwa maneno mfano wake, bali wao wanasamehe na kupuuzza, na hawasemi lolote ila maneno mazuri. Hivi ndivyo alivyofanya Mtume ﷺ, kila watu wanapokuwa wajinga ndiyo alivyokuwa akivumilia zaidi. Hivyo, ndivyo Alivyosema Aliyetukuka:

وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ

“Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao.” (28:55).

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Annu’aman bin Muqarrim Al-Muzani amesema: Mtume ﷺ amesema, “Mtu mmoja alimtukana mwenzake mbele

¹ *Fat-h al-Baariy* 2:453.

yake. Amesema: "Ikawa yule aliyetukanwa anasema: Amani iwe juu yake, Akasema Mtume ﷺ, "Hakika si vinginevyo Malaika anakutetea wewe kila huyu mwenzako anapokutusi Malaika humuambia yeye: Bali wewe mwenyewe, wewe ndio unastahiki zaidi tusi hilo. Na wewe unapomwambia yeye: Amani iwe juu yako." Malaika husema: Hapana, bali iwe juu yako (wewe uliyeitamka) na wewe ndiye unayestahiki zaidi amani hiyo." Isnadi ya Hadithi hii ni Hasani. Wala waandishi wa vitabu vya Sunnan hawakuinukuu.¹

Kisha Allah ﷻ Anataja kuwa siku yao ni bora zaidi ya siku nyingine. Kama Alivyosema:

وَالَّذِينَ يَبِيتُونَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَقِيَمًا ﴿٥٥﴾

"Na wale wanaokeshwa kwa ajili ya Mola wao Mlezi kwa kusujudu na kusimama."

Maana yake: Katika kumtii na kumuabudu Yeye. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ﴿٥٦﴾ وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٥٧﴾

"Walikuwa wakilala kidogo tu usiku. Na wakiomba maghufira, nyakati za kabla ya alfajir." (51:17-18).

Na Kauli Yake:

تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ

"Huinuka mbavu zao kutoka vitandani." (32: 16)

Na Amesema Aliyetukuka:

أَمَّنْ هُوَ قَنِيتٌ ءَأَنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُو رَحْمَةَ رَبِّهِ

"Je, afanyae 'Ibadah nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake Mlezi?'" (39:9).

Na hivyo Akasema Aliye tukuka:

¹ Ahmad 5:445.

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَصْرِفَ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّا عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٥٥﴾

“Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu ya Jahanamu. Hakika adhabu yake ikimpata mtu haimuachi.”

Maana yake: Itakuwepo nyakati zote na daima dawamu.

Na kwa hilo alisema Al-Hasan katika Kauli Yake:

﴿٥٦﴾ إِنَّا عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٥٦﴾

“Hakika adhabu yake ikimpata mtu haimuachi.”

“Hii ni kuwa kila jambo humsibu binadamu na kisha kuondoka, na wala halidumu, Na hakika jambo hudumu maadamu mbingu na ardhi bado zingalipo.”¹

Na vivyo hivyo ndivyo alivyo sema Sulaymaan At-Taymiy.² Allah تعالى Anasema:

﴿٥٧﴾ إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٥٧﴾

“Hakika hicho ni kituo na makao mabaya.”

Hii maana yake, ni kituo kibaya kimandhari na sehemu mbaya ya kupumzika. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا

“Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili.”

Maana yake: Wao si wabadhirifu katika matumizi yao kwa kuwa hawatumii zaidi ya mahitaji yao. Wala si mabakhili kwa familia zao kwa kuwanyima haki zao. Bali wao wanaifuata njia bora ya uadilifu. Na mambo yaliyo bora ni ya kati na kati, kwa maana si njia ya ubadhirifu wala si njia ya ubakhili.

¹ Atw-Twabariy 19:297.

² Abdur-Razzaaq 3:72.

Katika hilo kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ

“Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa.” (17:29).

* * *

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا ءآخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ
 أَنفُسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ ۗ وَمَنْ
 يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٦٨﴾ يُضْعَفُ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدُ فِيهِ مُهَانًا ﴿٦٩﴾ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ
 وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ
 حَسَنَاتٍ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٧٠﴾ وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ
 صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللَّهِ مَتَابًا ﴿٧١﴾ وَالَّذِينَ لَا
 يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٧٢﴾
 وَالَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا
 وَعُمَمَانًا ﴿٧٣﴾ وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ
 أَرْوَاحِنَا وَذُرِّيَّتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ ۖ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا
 ﴿٧٤﴾ أُولَئِكَ يُجْزَوْنَ الْغُرْفَةَ بِمَا صَبَرُوا وَيُلَقَّوْنَ
 فِيهَا نَحِيَّةً وَسَلَامًا ﴿٧٥﴾ خَلَائِدِينَ فِيهَا حَسُنَتْ مُسْتَقَرًّا
 وَمُقَامًا ﴿٧٦﴾ قُلْ مَا يَعْبُؤُنَا بِكُرْبِنِي لَوْلَا دُعَاؤُكُمْ ۗ فَقَدْ
 كَذَّبْتُمْ فَسَوْفَ يَكُونُ لِزَامًا ﴿٧٧﴾

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا
 ءآخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ أَنفُسَ الَّتِي حَرَّمَ
 اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُونَ ۗ وَمَنْ
 يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا ﴿٦٨﴾ يُضْعَفُ
 لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَيَخْلُدُ فِيهِ
 مُهَانًا ﴿٦٩﴾ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ
 وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَئِكَ
 يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ ۗ وَكَانَ
 اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٧٠﴾ وَمَنْ تَابَ
 وَعَمِلَ صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللَّهِ
 مَتَابًا ﴿٧١﴾

68. "Na wale wasiomuomba Mungu mwengine pamoja na Allah, wala hawazini na atakayefanya hayo atapata madhara.

69. Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na

atadumu humo kwa kufedheheka.

70. Isipokuwa atakayetubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Allah Atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Allah ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

71. Na aliyetubu na akafanya mema, basi hakika huyo ametubu kweli kweli kwa Allah".

Miongoni mwa Sifa za Waja wa *Ar-Rahmaan* ni Kujiepusha na Ushirikina, Mauaji na Uzinzi

Amepokea Imamu Ahmad kuwa 'Abdullah ibn Mas'uud رضي الله عنه amesema: "Aliulizwa Mtume ﷺ ni dhambi gani ambayo ni kubwa?" Akasema:

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً وَهُوَ خَلَقَكَ»

"Ni kumfanyia Allah wapinzani (miungu mingine) ilhali Yeye Ndiye Aliyekuumba".

Akaulizwa: "Kisha ni ipi?" Akasema:

«أَنْ تَقْتُلَ وَلَدَكَ خَشِيَةً أَنْ يَطْعَمَ مَعَكَ»

"Ni kumuua mtoto wako kwa kuogopea kuwa atakula na wewe."

Akaulizwa: "Kisha na ipi?" Akasema:

«أَنْ تُزَانِيَ حَلِيلَةَ جَارِكَ»

"Ni kufanya zinaa na mke wa jirani yako."

Akasema 'Abdullah: "Allah تعالى Akateremsha kusadikisha hayo:

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ

"Na wale wasiomuomba mungu mwengine pamoja na Allah."¹

Na hivi ndivyo alivyonukuu An-Nasaa'iy,² na pia imepokewa na Al-Bukhaariy na Muslim.³

Imepokewa kutoka Said ibn Jubayr kuwa alimsikia Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما akihadithia kuhusu baadhi ya watu miongoni mwa washirikina ambao waliuma sana na kuzini kupita kiasi. Kisha walikuja kwa Mtume Muhammad ﷺ na kusema: "Yale unayozungumza na unayowaitia watu kwayo ni mazuri, lau utatuambia kuwa ipo njia ya kuyafuta yale tuliyoyafanya". Hapo Aya hii ikateremka:

¹ Ahmad 1:380.

² An-Nasaa'iy katika *Al-Kubraa* 6:420.

³ Fat-hul - Al-Bari 12:116 na Muslim 1:90-91.

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ

“Na wale wasiomuomba mungu mwengine pamoja na Allah.”

Na pia:

﴿ قُلْ يَاعِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ

“Sema: Enyi waja Wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tama na Rehema ya Allah.” (39:53).¹

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

﴿ وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ يَلْقَ أَثَامًا

“Na atakayefanya hayo atapata Atha-ma.”

Imepokewa kwa Abdullah ibn Amri amesema: “Athaama ni bonde katika Jahanamu.”²

Na amesema Ikrimah: “Atha-ma ni mabonde katika Jahanamu ambamo wazinifu wanaadhibiwa.” Hiyo pia imepokewa kutoka kwa Sa’id ibn Jubayr na Mujahid³. Na amesema As-Suddiy: “Atha-ma ni ile jaza ya adhabu, na hii iko karibu na dhahiri ya maana ya Aya.” Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Ameifafanua baada yake, nayo ni Kauli ya Aliyetukuka:

﴿ يُضَعَّفَ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama.”

Hii ina maana kuwa itaongezwa na kuzidishwa. Hivyo,

﴿ وَيَخَذُّ فِيهِ مَهَاتًا

“Na atadumu humo kwa kufedheheka.”

Maana yake: Kubezwa na kudhalilishwa.

¹ At-Twabari 9:414.

² Atw-Twabariy 19:308.

³ Atw-Twabariy 19: 308.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا

“Isipokuwa atakayetubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema.”

Hii ina maana kuwa jaza'a yake kwa haya aliyoyafanya katika zile sifa mbaya ataadhibiwa kwa njia iliyotajwa. Lakini,

إِلَّا مَنْ تَابَ

“Isipokuwa atakayetubu.”

Hapa duniani kwa kurudi kwa Allah تعالیٰ kwa madhambi yote hayo, hapo Allah تعالیٰ Atakubali toba yao. Na hii ni dalili ya kuwa toba ya muuaji inakubaliwa, na haina ukinzani baina yake na ile Aya katika Suratun Annisaa':

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِّدًا

“Mwenye kumuua Muumini kwa kukusudia.” (4:93).

Hakika hii Aya japokuwa iliteremshwa Madinah lakini maana yake ni ya kijumla, na inaweza kufasiriwa kumhusisha mtu asiyetubu, kwa sababu Aya hii inatufahamisha kuwa toba ni kwa wale wanaotubu. Kisha hakika Amesema Aliyetukuka:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

“Hakika Allah Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo duni ya hilo kwa Amtakaye.” (4:48).

Na imethibiti katika Sunna iliyo Sahihi kutoka kwa Mtume ﷺ kusihi toba ya muuaji, kama ilivyoelezwa katika kisa cha mtu aliyeya watu mia moja na kisha akatubia, na Allah تعالیٰ Alikubali toba yake, na Hadithi nyenginezo.¹

Na Kauli ya Aliyetukuka:

¹ Al-Bukhaariy 3470 na Muslim 7008.

فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٦٧﴾

“Basi hao Allah Atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Allah ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.

Imepokewa kutoka kwa Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنِّي لَأَعْرِفُ أَجْرَ أَهْلِ النَّارِ خُرُوجًا مِنَ النَّارِ، وَأَجْرَ أَهْلِ الْجَنَّةِ دُخُولًا إِلَى الْجَنَّةِ، يُؤْتَى بِرَجُلٍ فَيَقُولُ: نَحُوا عَنْهُ كِبَارَ ذُنُوبِهِ وَسَلُّوهُ عَنْ صِغَارِهَا، قَالَ: فَيَقَالُ لَهُ: عَمِلْتَ يَوْمَ كَذَا، وَكَذَا، وَعَمِلْتَ يَوْمَ كَذَا، وَكَذَا، وَكَذَا، فَيَقُولُ: نَعَمْ لَا يَسْتَطِيعُ أَنْ يُنْكِرَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا، فَيَقَالُ: فَإِنَّ لَكَ بِكُلِّ سَيِّئَةٍ حَسَنَةً، فَيَقُولُ: يَا رَبِّ عَمِلْتُ أَشْيَاءَ لَا أَرَاهَا هُنَا»

“Hakika mimi najua mtu wa mwisho kutoka motoni, na wa mwisho wa watu wa peponi kuingia peponi. Ataletwa mtu, na ataambiwa: “Muondoleeni madhambi yake makubwa na muulizeni kuhusu madhambi yake madogo.” Akasema: Ataambiwa: “Ulifanya kadha wa kadha siku kadha na kadha, na ulifanya siku kadha, kadhaa na kadhaa”. Atasema: “Ndio”. Hataweza kukanusha chochote katika hayo. Ataambiwa: “Kwa kila dhambi ulilotenda, utakuwa na thawabu moja sasa.” Atasema: “Ewe Mola wangu Mlezi! Nimefanya vitu ambavyo sivioni hapa.”

Akasema (Abu Dharr رضي الله عنه): “Hapo Mtume ﷺ akatabasamu mpaka magego yake yakaonekana.”¹ Muslim pia ameipokea Hadithi hiyo.²

Amepokea Ibn Abi Jaabir رحمه الله تعالى kuwa amemsikia Mak-huuli akihadithia, akisema: “Alikuwa Mzee mkongwe, nyusi zake zikiwa zimeanguka kwenye macho yake, akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Mtu amewahini wenziwe na amefanya uasherati, na hakuna jambo lolote baya isipokuwa amelifanya. Lau madhambi yake yatagawanywa kwa wote wa ardhini, wataangamia. Je, kuna toba yoyote kwake?” Mtume ﷺ akamwambia:

¹ Ahmad 5:170.

² Muslim 1:177.

«أَأَسْنَمْتُمْ؟»

“Je, umesilimu?”

Akasema : “Ama mimi nashuhudia kuwa hapana muabudiwa isipokuwa Allah Peke Yake na hana mshirika Naye, na kuwa Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.” Akasema Mtume ﷺ :

«إِنَّا لِلَّهِ غَافِرٌ لَكَ مَا كُنْتَ كَذَلِكَ، وَمُبَدَّلُ سَبَاتِكَ حَسَنَاتٍ»

“Hakika Allah Amekusamehe kwa yote uliyoyafanya mfano wa hayo, na Amekubadilishia maovu yako kuwa mema kwako.”

Akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Na hata hiyana yangu na uzinzi wangu?” Akasema:

«وَعَذْرَاتُكَ وَفَجْرَاتُكَ»

“Na hiyana yako na uzinzi wako uliofanya”.

Mtu huyo akaondoka huku analeta *Tahliil (Laa ilaha illa Llahu) na Takbir*¹

Kisha Akasema Aliyetukuka Kutupa habari ya ujumla wa Rehema Yake kwa waja Wake, na kuwa yeyote atakayeleta toba Kwake Atamsamehe kwa dhambi yoyote, kubwa au ndogo. Akasema Aliyetukuka:

«وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللَّهِ مَتَابًا»

“Na aliyetubu na akafanya mema, basi hakika huyo ametubu kweli kweli kwa Allah”.

Hii ina maana kuwa Allah تعالى Anakubali toba yake. Kama Alivyosema:

«وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَحِيمًا»

“Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghufira kwa Allah, atamkuta Allah ni Mwingi wa Maghufira, Mwenye Kurehemu.” (4:110).

¹Addurul-Manthuru 6:281, Ahmad 4:385, Majmau - Azawaid 1:32.

Na Akasema Aliyetukuka:

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ

“Je, Hawajui ya kwamba Allah Anapokea toba ya waja Wake.” (9: 104).

Na Amesema Aliyetukuka:

﴿ قُلْ يَنْعِبَادِي الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ﴾

“Sema: Enyi waja Wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na Rehema ya Allah.” (39:53).

Kwa yule mwenye kurudi na kutubu Kwake.

وَالَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٧٢﴾ وَالَّذِينَ إِذَا
ذُكِّرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ لَمْ يُخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا ﴿٧٣﴾ وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ
لَنَا مِن أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا ﴿٧٤﴾

72. “Na wale ambao hawatoi ushahidi wa uongo, na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa hishima yao.

73. Na wale ambao wanapokumbushwa Ishara za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu.

74. Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wanetu yaburudishayo macho, na Utujaalie tuwe waongozi kwa wachamungu”.

Baadhi ya Sifa za Waja wa Ar-Rahmaan (Sifa za Ziada)

Na hizi pia ni baadhi ya sifa za waja wa Ar-Rahmaan ni kuwa wao hawatoi ushahidi wa uongo, nao ni uongo wenyewe, ufasiki, kufuru, upuuzi na batili.

Na amesema ‘Amr ibn Qays: “Hivyo ni vikao viovu na vya uasherati.” Na panasemwa kuwa muradi wa Kauli Yake Aliyetukuka:

لَا يَشْهَدُونَ بِالزُّورِ

“Ambao hawatoi ushahidi wa uongo.”

Ushahidi wa uongo, nao ni kusema uongo makusudi kwa mtu mwengine. Hii imepokewa katika Sahihi mbili kutoka kwa Abi Bakrah kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَلَا أُتْبِتُكُمْ بِأَكْثَرِ الْكِبَارِ؟»

“Je, niwajulishe madhambi makubwa kuliko yote?”

Aliuliza suali hili mara tatu. Wakamjibu: “Kwanini tusitake, ewe Mtume wa Allah.” Akasema:

«الشُّرْكَ بِاللهِ وَعُقُوقُ الْوَالِدَيْنِ»

“Kumshirikisha Allah na kuwaasi wazazi wawili.”

Akaka baada ya kuwa ameegemea, akasema:

«أَلَا وَتَوَلَّى الزُّورِ، أَلَا وَشَهَادَةُ الزُّورِ»

“Jiepusheni na kauli ya uongo na ushahidi wa uongo.”

Aliendelea kuirudia kauli hiyo mpaka tukasema afadhali angalinyamaza.¹ Na dhahiri katika muktadha inaonekana kuwa kinachomaanishwa kwa wale wasiotoa ushahidi wa uongo, yaani ni wale wasiohudhuria au hawapo kinapotendeka. Na hivyo Amesema Aliyetukuka:

وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٦٧﴾

“Na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa hishima yao.”

Maana yake: Hawahudhuria pale unapokuwepo uongo, na wanapoafiki kupita sehemu yenye upuuzi wanapita na hawaachi iwachafue kabisa. Na hivyo Akasema:

مَرُّوا كِرَامًا ﴿٦٧﴾

“Hupita kwa hishima yao.”

¹ Fat'h al-Baariy 5:309 na Muslim 1:91.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِذَا ذُكِرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا ﴿٦٨﴾

“Na wale ambao wanapokumbushwa Ishara za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu.”

Na hii pia ni miongoni mwa sifa za Waumini:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٦٩﴾

“Hakika Waumini ni wale ambao kwamba Anapotajwa Allah nyoyo zao hujaa hofu, na wanaposomewa Ayah Zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi.” (8:2).

Kinyume na makafiri, ambao wanaposikia Maneno ya Allah تعالى hawaathiriki wala hawabadiliki kwa yale waliokuwa nayo. Wanaendelea na ukafiri wao, na utaghuti (ushetani) wao, ujinga na upotevu wao.

Hayo ni kama Allah تعالى Alivyosema:

وَإِذَا مَا أَنْزَلْنَا سُورَةً فَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هُدًىٰ ۖ إِيْمَانًا ۖ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٧٠﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ فزَادَتْهُمْ رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ

“Na ilipoteremshwa Surah wapo miongoni mwao wanasema: “Ni nani miongoni mwenu Surah hii imemzidishia Imani? Ama wale walioamini inawazidishia Imani, nao wanafurahi. Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, basi inawazidishia uovu juu ya uovu wao.” (9:124-125).

Hivyo Kauli Yake:

لَمْ يَخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا ﴿٧١﴾

“Hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu”.

Sifa hii ni kinyume na ile ya kafiri ambaye anaposikia Aya na ishara za Allah تعالی basi haathiriki bali anaendelea katika ile hali aliyokuwa nayo kama kwamba hakusikia, kiziwi na kipofu.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ

“Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wanetu yaburudishayo macho”.

Hii ina maana kuwa, wale wanaomuomba Allah تعالی Awape kutoka katika viuno vyao kizazi cha wenye kumtii na kumuabudu Yeye Peke Yake bila kumshirikisha na chochote. Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Hii inamaanisha, kizazi ambacho kitatia juhudi katika kumtii Allah تعالی na hivyo kuwaletea wao furaha na kuwaburudisha hapa duniani na kesho Akhera.”¹

Na imepokewa na Imamu Ahmad kutoka kwa Jubayrb ibn Nufayr aliyesema: Tulikuwa tumekaa na Al-Miqdaad ibn Al-Aswad siku moja, na akapita hapo mtu mmoja ambaye alisema: “Yamebarikiwa vipi haya macho mawili ambayo yamemuona Mtume wa Allah! Kama na sisi tungekuwa tumeona uliyoona na kushuhudia uliyoshuhudia.” Al-Miqdaad alikasirika sana, nami nikashangaa mno, kwani mtu yule hakusema ila kheri. Kisha alimkabili mtu yule na kumwambia: “Ni kitu gani kinachomfanya mtu awepo wakati ambapo Allah تعالی Amemfanya asiwepo, naye hajui angekuwaje lau angekuwepo? Naapa kwa Allah تعالی, wapo watu ambao walimuona Mtume wa Allah, na Allah تعالی Atawatupa wao kwa nyuso zao katika Moto, kwa sababu hawakumkubali wala kumuamini. Je. Wewe humshukuru Allah تعالی Ambaye Amewatoa katika tumbo za mama zenu mkiwa munamuamini Mola wenu Mlezi na yale aliyokuja nayo Mtume, na kuwa mitihani iliwapata watu wengine na sio nyinyi? Allah تعالی Alimtuma Mtume wake katika wakati mgumu sana kuliko Mitume wengine wote baada ya kipindi kirefu cha Ujahiliya, wakati ambao watu hawakuona dini bora na nzuri kama kuabudu masanamu. Naye alikuja na *Furqaan* (kipambanuzi) cha kutofautisha haki kutokana na batili na pia kumtenganisha baba na mtoto. Mtu alikuwa anatambua kuwa babake, mtoto wake au ndugu

¹Atw-Twabariy 19: 318.

yake ni kafiri, na kwa kuwa Allah تعالی Amefungua moyo wake kwa Imani, alijua kuwa lau jamaa yake ataaga dunia atakwenda Motoni, hivyo hakuwa ni mwenye kupumzika huku akijua kuwa kipenzi chake atakuwa Motoni.”

Hii ndiyo maana Anayomaanisha Allah تعالی katika Kauli hii:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ

“Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wanetu yaburudishayo macho.”

Na Isnadi yake ni Sahihi, japokuwa haikunukuliwa¹

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا

“Na Utujaalie tuwe waongozi kwa wachamungu”.

Amesema Ibn ‘Abbaas, na pia Al-Hasan, As-Suddiy, Qataadah na Ar-Rabii’ ibn Anas رضي الله عنهم: “Viongozi watakaokuwa ni vielelezo katika kheri.”² Na wamesema wengineo: “Waelekezaji ambao wanawaita watu wengine katika kheri.” Hawa wanataka ‘Ibadah zao ziunganishwe na ‘Ibada za watoto wao na vizazi vyao, na uongofu wao uende zaidi na kuwanufaisha wengine. Na huko ni kuongezwa thawabu na marejeo mazuri.” Kama ilivyonukuliwa katika Sahih Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا مَاتَ ابْنُ آدَمَ انْقَطَعَ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ ثَلَاثٍ: وَلَدٍ صَالِحٍ يَدْعُو لَهُ، أَوْ عِلْمٍ يُسْتَفَعُ بِهِ مِنْ بَعْدِهِ، أَوْ صَدَقَةٍ جَارِيَةٍ»

“Anapokufa mwanadamu amali zake zote hukatika isipokuwa kwa mambo matatu: Mtoto mwema anayemuomba, au elimu yenye manufaa kwa wengine baada yake au sadaka ya kuendelea.”³

¹ Ahmad 6:2.

² Atw-Twabariy 19:319.

³ Muslim 3:1255.

أُولَئِكَ مُجْرَوْنَ بِالْغُرْفَةِ بِمَا صَبَرُوا وَيُلْقَوْنَ فِيهَا نَجِيَّةً وَسَلَامًا ﴿٧٦﴾ خَلِيدِينَ
 فِيهَا حَسَنَةٌ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٧٧﴾ قُلْ مَا يَعْبَأُ بِكُمْ رَبِّي لَوْلَا دُعَاؤُكُمْ فَقَدْ كَذَّبْتُمْ
 فَسَوْفَ يَكُونُ لِزَامًا ﴿٧٨﴾

75. "Hao ndio watakaolipwa makao ya juu kwa kuwa walisubiri, na watakuta humo maamkio na salamu.

76. Wadumu humo – kituo na makao mazuri kabisa.

77. Sema: Mola wangu Mlezi Asingekujalini lau kuwa si kuomba kwenu. Lakini nyinyi mmemkadhibisha. Basi adhabu lazima iwe".

Jazaa kwa Waja wa Ar-Rahmaan na Onyo kwa Watu wa Makkah

Pale Alipotaja Aliyetukuka sifa za waja Wake Waumini, utajo katika sifa nzuri na njema, kauli zao na vitendo vitukufu. Alisema baada ya hayo yote:

أُولَئِكَ

"Hao."

Maaana yake: Waliosifika na sifa hizo,

مُجْرَوْنَ

"Ndio watakaolipwa."

Siku ya Kiyama. Watalipwa:

الْغُرْفَةَ

"Makao ya juu."

Nayo ni Pepo. Amesema Abu Ja'far Al-Baaqir, na Said ibn Jubayr, Adh-Dhahhaak na As-Suddiy: "Imeitwa hivyo kwa sababu ya kunyanyuka kwake." Haya wanalipwa kwa sababu ya,

بِمَا صَبَرُوا

"Kwa kuwa walisubiri."

Maana yake: Kuvumilia kwa kufanya yale waliyofanya.

وَيُلَقَّوْنَ فِيهَا

“Na watakuta humo.”

Maana yake: Peponi na,

نَحِيَّةً وَسَلَامًا

“Maamkio na salamu.”

Hii ina maana kuwa watatolewa salamu mwanzo kwa maneno ya kuwakaribisha na ya heshima. Amani itakuwa ndio yao na watatakiwa amani. Na Malaika wataingia katika sehemu zao katika kila mlango, wakisema: “Amani iwe juu yenu kwa yale mliyovumilia kwa kusubiri! Neema iliyoje kwa makazi ya Mwisho.”

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

خَالِدِينَ فِيهَا

“Wadumu humo.”

Maana yake: Watakaa humo na hawatatoka humo kabisa au kuondoka au kufa, hawatatoka kabisa wala kutaka au kutamani kuondoka kuelekea sehemu nyingine. Hii ni kama ile Kauli ya Aliyetukuka:

﴿ وَأَمَّا الَّذِينَ سُعِدُوا فَفِي الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ ﴾

“Na ama wale waliobahatika, wao watakuwamo Peponi wakidumu humo kwa muda wa kudumu kwa mbingu na ardhi.” (11:108).

Akasema Aliyetukuka:

حَسُنْتَ مُسْتَقْرًا وَمَقَامًا

“Kituo na makao mazuri kabisa.”

Mandhari yake ni mazuri na ni mahali pazuri kwa mapumziko na makao. Kisha Akasema Aliyetukuka:

قُلْ مَا يَعْبُؤُنَا بِكُرْبِي

“Sema: Mola wangu Mlezi Asingekujalini.”

Hii ina maana kuwa Asingeliwajali kwa Kuwatunza ikiwa hamungemuabudu Yeye, kwani Allah تعالى Ameumba wanadamu wamuabudu Yeye Peke Yake na wamtakase na Kumtukuza asubuhi na jioni. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَقَدْ كَذَّبْتُمْ

“Lakini nyinyi mmemkadhibisha.”

Enyi makafiri. Hivyo, na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَسَوْفَ يَكُونُ لِزَامًا ﴿٦٨﴾

“Basi adhabu lazima iwe.”

Maana yake: Kukadhibisha kwenu kutabaki nanyi daima, nanyi itawapelekeeni katika adhabu na maangamivu na kuharibikiwa duniani na kesho Akhera. Na inaingia hapo ile Siku ya Badr, kama alivyofasiri hivyo ‘Abdullah ibn Mas’ud, Ubayy ibn Ka’b, Muhammad ibn Ka’b Al-Quradhiy, Mujahid, Adh-Dhahhaak, Qataadah, As-Suddiy na wengineo¹.

فَسَوْفَ يَكُونُ لِزَامًا ﴿٦٨﴾

“Basi adhabu lazima iwe.”

Na amesema Al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى: Yaani, Siku ya Kiyama.² Wala hakuna ukinzani baina ya tafsiri mbili hizo.

Hapo ndio tumetamatisha Tafsir ya Suratu Al-Furqaan, na Sifa zote njema pamoja na Shukrani Anastahiki Allah تعالى Peke Yake.

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:324 na ‘Abdur-Razzaaq 3:72.

² Ad-Durr Al-Manthuur 6: 287.

Tafsiri ya Suratu Shu` araa

Sura ya 26

Iliteremshwa Makkah

(Na katika Tafsiri iliyopokelewa kutoka kwa Maalik, alisema kuwa hii Surah pia inaitwa *Suratul Jaami'ah*).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الشُّعَرَاءِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

طسّم ﴿١﴾ نِلَكَ ءَايَتُ الْكِتَابِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢﴾ لَعَلَّكَ بِنَجْعِ
نَفْسِكَ أَلَّا يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٣﴾ إِنْ كُنَّا نُنزِّلُ عَلَيْهِمْ مِنْ
السَّمَاءِ ءَايَةً فَظَلَّتْ أَعْيُنُهُمْ هَا خَضِيعِينَ ﴿٤﴾ وَمَا يَأْتِيهِمْ
مِنْ ذِكْرٍ مِنَ الرَّحْمَنِ مُحَدَّثٍ إِلَّا كَانُوا عَنْهُ مُعْرِضِينَ ﴿٥﴾
فَقَدْ كَذَّبُوا فَسَيَأْتِيهِمْ أَنْبِتُوا مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٦﴾
أَوْلَمْ يَرَوْا إِلَى الْأَرْضِ كَمْ أَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿٧﴾
إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ
لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٩﴾

طسّم ﴿١﴾ نِلَكَ ءَايَتُ الْكِتَابِ
الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢﴾ لَعَلَّكَ بِنَجْعِ
نَفْسِكَ أَلَّا يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٣﴾
إِنْ كُنَّا نُنزِّلُ عَلَيْهِمْ مِنْ
السَّمَاءِ ءَايَةً فَظَلَّتْ
أَعْيُنُهُمْ هَا خَضِيعِينَ ﴿٤﴾ وَمَا
يَأْتِيهِمْ مِنْ ذِكْرٍ مِنَ الرَّحْمَنِ مُحَدَّثٍ إِلَّا
كَانُوا عَنْهُ مُعْرِضِينَ ﴿٥﴾ فَقَدْ كَذَّبُوا
فَسَيَأْتِيهِمْ أَنْبِتُوا مَا كَانُوا بِهِ
يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٦﴾ أَوْلَمْ يَرَوْا إِلَى
الْأَرْضِ كَمْ أَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿٧﴾
إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ
مُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ
الرَّحِيمُ ﴿٩﴾

1. "Twaai Siin Miim.

2. Hizi ni Ayah za Kitabu kinachobainisha.

3. **Huenda labda ukajikera nafsi yako kwa kuwa hawawi Waumini.**
4. **Tungependa Tungeliwateremshia kutoka mbinguni Ishara zika nyenyekea shingo zao.**
5. **Wala hauwafikii ukumbusho mpya kutoka kwa Ar-Rahmaan ila wao hujitenga nao.**
6. **Kwa yakini wamekanusha; kwa hivyo zitakuja wafikia khabari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.**
7. **Je! Hawakuiona ardhi, mimea mingapi Tumeiotesha humo, ya kila namna nzuri?**
8. **Hakika katika haya zipo Ishara. Lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini.**
9. **Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.**

Makafiri Kuichukia kwao Qur'an, Lau Allah تعالیٰ Angelitaka Angeliwa - lazimisha Kuiamini

Ama kauli na maelezo kuhusu Herufi *Al-Muqatwtwa'ah* katika mwanzo wa Surah, hakika tumezizungumzia katika mwanzo wa Tafsir ya *Suratul Baqara*. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿١٠﴾

“Hizi ni Ayah za Kitabu kinachobainisha.”

Hizi ni Aya za Qur'ani zinazobainisha kwa uwazi. Yaani, Kitabu kilicho wazi na kisichokuwa na utata, ambacho kinapambanua baina ya haki na batili, na upotevu na uongofu. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لَعَلَّكَ بِنِعْمِ رَبِّكَ تَفْسَاكُ

“Huenda labda ukajikera nafsi yako.”

Maana yake: Ukaangamiza, “nafsi yako”, kwa sababu una hamu kubwa kuwaona wao wakiongoka na kuwahuzunikia sana.

أَلَا يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿١٠٩﴾

“Kwa kuwa hawawi Waumini”.

Hapa Allah Aliyetakasika Anamliwaza Mtume Wake kwa kukosa Imani miongoni mwa wale makafiri wasiomuamini. Hii ni kama Alivyosema:

فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَاتٍ

“Basi roho yako isitoke kwa majonzi juu yao.” (35:8).

Na kama Kauli Yake: *“Huenda ukaihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kuwasikitikia kwa kuwa hawayaamini.”* Mujaahid na ‘Ikrimah, na Qataadah, na ‘Atwiyah, na Adh-Dhahhaak, Al-Hasan na wengineo wanasema:

لَعَلَّكَ بِنِعْمِ نَفْسِكَ

“Huenda labda ukajikera nafsi yako.”

Maana yake: Ukajiu mwenyewe.¹ Kisha Akasema Aliyetukuka:

إِنْ كُنَّا نُنَزِّلُ عَلَيْهِمْ مِنَ السَّمَاءِ آيَةً فَظَلَّتْ أَعْيُنُهُمْ هَا خَاضِعِينَ ﴿١١٠﴾

“Tungependa Tungeliwateremshia kutoka mbinguni Ishara zikanyenyekea shingo zao”.

Lau Tungependa basi Tungeteremsha Ishara zetu ambazo zingewalazimisha wao kuamini kwa nguvu, lakini Sisi hatufanyi hivyo kwa sababu hatutaki kutoka kwa yeyote isipokuwa aamini kwa kupenda kwake. Na Akasema Aliyetukuka:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلَّهُمْ جَمِيعًا ۖ أَفَأَنْتَ تُكْرَهُ النَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا

مُؤْمِنِينَ ﴿١١١﴾

“Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?” (10:99).

¹ Atw-Twabariy 19:330 na Ad-Durr Al-Manthuur 6:360

Akasema Aliyetukuka:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً

“Na Mola Wako Mlezi Angelipenda Angewafanya watu wote wakawa Ummah mmoja.” (11:118).

Lakini Qadari Yake ndiyo yenye kutendwa, na Hukumu Yake ndio iliyopita, na Hoja Zake ndizo zilizofikishwa kwa wanadamu kwa kuwatumia Mitume na kuwateremshia Vitabu. Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَمَا يَأْتِيهِمْ مِّنْ ذِكْرٍ مِّنَ الرَّحْمَنِ مُحَدَّثًا إِلَّا كَانُوا عَنْهُ مُعْرِضِينَ ﴿٥﴾

“Wala haufikii ukumbusho mpya kutoka kwa Ar-Rahmaan ila wao hujitenga nao”. (26:5)

Kila wakati Kitabu kinapoteremshwa kutoka mbinguni, watu wengi walikuwa wakijitenga nacho na kukengeuka. Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi?” (12:103).

Na Amesema tena Aliyetukuka:

يَنْحَسِرُونَ عَلَىٰ آلْعِبَادِ ۗ مَا يَأْتِيهِمْ مِّنْ رَسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٣٠﴾

“Inafaa kusikitikiwa hawa waja: hakuwajia Mtume yeyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha (na wanakataa kumfuata).” (36:30).

Na Amesema tena Aliyetukuka:

ثُمَّ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا تَتْرًا ۗ كُلًّا مَّا جَاءَ أُمَّةً رُّسُولُهَا كَذَّبُوهُ

“Kisha Tukawatuma Mitume wetu, mmoja baada ya mwengine. Kila Ummah alipowafikia Mtume wao walikanusha.” (23: 44).

Na kwa hayo Anasema hapa Aliyetukuka:

﴿فَقَدْ كَذَّبُوا فَسَيَاتِهِمْ أَنْبَتُوا مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ﴾

“Kwa yakini wamekanusha; kwa hivyo zitakuja wafikia khabari za yale waliyokuwa wakiyafanyaia mzaha.” (26:6)

Hakika ni kuwa walikanusha haki na ukweli uliowajia wao, hivyo watakuja kujua habari za matokeo ya ukanushaji wao baada ya muda:

﴿وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ﴾

“...Na wanaodhulumu watakuja jua mgeuko gani watakaogeuka.” (26:227).

Kisha Allah تَعَالَى Anatupatia habari juu ya Ukuu wa Ufalme Wake na Utukufu wa Uwezo Wake kwa wale walio na ujasiri wa kumpinga Mtume Wake na kukanusha Kitabu Chake. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Aliye Mkuu, Muweza wa Kufanya kila kitu, Ambaye Ameumba ardhi na Akaotesha ndani yake kila mmea na matunda mazuri pamoja na kuweka hayawani. Amepokea Sufyaan Ath-Thawriy رَحْمَةً اللهُ تَعَالَى kutoka kwa mtu mmoja naye kutoka kwa Ash-Sha'biy kuwa watu wametokana na ardhi. Hivyo, yeyote anayeingia Peponi ni mzuri na mtukufu, na yeyote anayeingia Motoni ni muovu na mwenye kuchukiza.¹

﴿إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً﴾

“Hakika katika haya zipo Ishara”.

Maana yake: Dalili kwa Uweza wa Muumbaji wa vitu vyote, Ambaye kwamba Ameitandaza ardhi na Kuzinyanyua mbingu. Pamoja na haya yote watu wengi hawakumuamini, bali walimkadhibisha pamoja na kuwakanusha Mitume Wake na Vitabu Vyake. Hivyo hivyo wakaenda kinyume na Amri Zake na wakawa ni wenye kutenda Alivyokataza. Na Kauli Yake:

﴿وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ﴾

“Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Yeye Mwenye nguvu”.

¹ Ad-Durr Al-Manthuur 6:289.

Maana yake: Aliye na nguvu kwa kila kitu na Kuvishinda pamoja na Kuidhibiti. Naye pia ni.

الرَّحِيمُ

“Mwenye Kurehemu”.

Maana yake: Kwa viumbe Vyake, kwani Yeye Hafanyi haraka Kumuadhibu aliyeasi, bali Anampatia muda ili atubu, na ikiwa hatafanya hivyo basi Anamshika kwa kumpatia adhabu kali mno. Abul Aliyah, Qataadah, Rabii’ ibn Anas na Ibn Is-haaq wamesema: “Yeye ni Mwenye Nguvu katika Kutoa adhabu na Kushinda juu ya wale waliokengeuka maagizo Yake na kuabudu asiyekuwa Yeye.”¹ Na amesema Said Ibn Jubayr: “Mwenye Kurehemu kwa mwenye kutubia na kurudi Kwake.”

* * *

¹ Atw-Twabariy 23:304 na 3:260 na 5:511.

وَإِذْ نَادَى رَبُّكَ مُوسَىٰ أَنِ اتَّبِعْ أَقْوَامَ الطَّالِمِينَ ﴿١٠﴾ قَوْمَ فِرْعَوْنَ ۖ أَلَا يَتَّقُونَ ﴿١١﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ ﴿١٢﴾ وَيَضِيقُ صَدْرِي وَلَا يَنْطَلِقُ لِسَانِي فَأَرْسِلْ إِلَىٰ هَارُونَ ﴿١٣﴾ وَهُمْ عَلَىٰ ذَنْبٍ فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿١٤﴾ قَالَ كَلَّا ۗ فَاذْهَبَا بِبَايِعَتِنَا ۗ إِنَّا مَعَكُمْ مُسْتَمِعُونَ ﴿١٥﴾ فَايْتِمَا فِرْعَوْنَ فَقُولَا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾ أَنْ أَرْسِلَ مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٧﴾ قَالَ أَلَمْ نُرَبِّكَ فِيْنَا وَلِيدًا وَلِئِذَا مِتْنَا مِنَ عَمْرِكَ سَيِّئِينَ ﴿١٨﴾ وَقَعَلْتَ فَعَلْتِكَ الَّتِي فَعَلْتَ وَأَنْتَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿١٩﴾ قَالَ فَعَلَيْهَا إِذَا وَأَنَا مِنَ الضَّالِّينَ ﴿٢٠﴾ فَفَرَرْتُ مِنْكُمْ لَمَّا خِفْتُمْكُمْ فَوَهَبَ لِي رَبِّي حُكْمًا وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢١﴾ وَتِلْكَ نِعْمَةٌ تَمُنَّهَا عَلَيَّ أَنْ عَبَّدتَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٢٢﴾ قَالَ فِرْعَوْنُ وَمَا رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٣﴾ قَالَ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ إِنْ كُنْتُمْ مُوقِنِينَ ﴿٢٤﴾ قَالَ لِمَنْ حَوْلَهُ ۗ أَلَا تَسْتَعْبِقُونَ ﴿٢٥﴾ قَالَ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ﴿٢٦﴾ قَالَ إِنَّ رَسُولَكُمْ الَّذِي أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ ﴿٢٧﴾ قَالَ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ إِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾

وَإِذْ نَادَى رَبُّكَ مُوسَىٰ أَنِ اتَّبِعْ أَقْوَامَ الطَّالِمِينَ ﴿١٠﴾ قَوْمَ فِرْعَوْنَ ۖ أَلَا يَتَّقُونَ ﴿١١﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ ﴿١٢﴾ وَيَضِيقُ صَدْرِي وَلَا يَنْطَلِقُ لِسَانِي فَأَرْسِلْ إِلَىٰ هَارُونَ ﴿١٣﴾ وَهُمْ عَلَىٰ ذَنْبٍ فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿١٤﴾ قَالَ كَلَّا ۗ فَاذْهَبَا بِبَايِعَتِنَا ۗ إِنَّا مَعَكُمْ مُسْتَمِعُونَ ﴿١٥﴾ فَايْتِمَا فِرْعَوْنَ فَقُولَا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾ أَنْ أَرْسِلَ مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٧﴾ قَالَ أَلَمْ نُرَبِّكَ فِيْنَا وَلِيدًا وَلِئِذَا مِتْنَا مِنَ عَمْرِكَ سَيِّئِينَ ﴿١٨﴾ وَقَعَلْتَ فَعَلْتِكَ الَّتِي فَعَلْتَ وَأَنْتَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿١٩﴾ قَالَ فَعَلَيْهَا إِذَا وَأَنَا مِنَ الضَّالِّينَ ﴿٢٠﴾ فَفَرَرْتُ مِنْكُمْ لَمَّا خِفْتُمْكُمْ فَوَهَبَ لِي رَبِّي حُكْمًا وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢١﴾ وَتِلْكَ نِعْمَةٌ تَمُنَّهَا عَلَيَّ أَنْ عَبَّدتَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٢٢﴾

10. "Na Mola wako Mlezi, Alipomuita Musa, Akamwambia: Fika kwa watu madhalimu.

11. Watu wa Firauni. Hawaogopi?

12. Akasema: Hakika mimi nachelea wasinikanushe.
13. Na kifua changu kina dhiki, na ulimi wangu haukunjuki vyema. Basi mtumie ujumbe Haarun.
14. Na wao wana kisasi juu yangu, kwa hivyo naogopa wasije kuniua.
15. Akasema: Siyo hivyo kabisa! Nendeni na miujiza Yetu. Hakika Sisi tu pamoja nanyi, Tunasikiliza.
16. Basi mfikieni Firauni na mwambieni Hakika sisi ni Mitume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.
17. Waachilie wana wa Israili waende nasi.
18. (Firauni) akasema: Sisi hatukukulea wewe utotoni, na ukakaa kwetu katika umri wako miaka mingi?
19. Na ukatenda kitendo chako ulichotenda, nawe ukawa miongoni mwa wasio na shukrani?
20. (Musa) akasema: Nilitenda hayo hapo nilipokuwa miongoni mwa wale waliopotea.
21. Basi nikakukimbieni nilipokuogopeni, tena Mola wangu Mlezi Akanitunukia hukumu, na Akanijaalia niwe miongoni mwa Mitume.
22. Na hiyo ndiyo neema ya kunisumbulia, na wewe umewatia utumwani wana wa Israili?"

Baina ya Musa عليه السلام na Firauni

Anatupa habari Aliyetukuka pale Alipomuamuru mja na Mtume Wake, Musa ibn 'Imraan عليه السلام aliyezungumza naye, Alipomuita upande wa kuume wa Mlima Tur. Hapo Alizungumza naye, Akamtuma, Akamteua na Kumuamuru aende kwa Firauni na watu wake. Kwa hilo Akasema Aliyetukuka:

أَنْ أَنْتِ الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠﴾ قَوْمَ فِرْعَوْنَ ۗ أَلَا يَتَّقُونَ ﴿١١﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَخَافُ أَنْ
يُكَذِّبُونِ ﴿١٢﴾ وَيَضِيقُ صَدْرِي وَلَا يَنْطَلِقُ لِسَانِي فَأَرْسِلْ إِلَىٰ هَارُونَ ﴿١٣﴾ وَهُمْ عَلَىٰ ذَنْبٍ
فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿١٤﴾

“...Fika kwa watu madhalimu. Watu wa Firauni. Hawaogopi? Akasema: Hakika mimi nachelea watanikanusha. Na kifua changu kina dhiki, na ulimi wangu haukunjuki vyema. Basi mtumie ujumbe Haarun. Na wao wana kisasi juu yangu, kwa hivyo naogopa wasije kuniua.”

Hivyo, Musa عليه السلام alimuomba Allah تعالى Amuondolee shida, kama Alivyosema katika Suratua Twaaha:

قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ﴿٢٥﴾ وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي ﴿٢٦﴾

“Musa akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu, na Unifanyie nyepesi kazi yangu.” (20:25-26).

قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَىٰ ﴿٢٦﴾

“Hakika umepewa maombi yako, ewe Musa!” (20:36).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَهُمْ عَلَىٰ ذَنْبٍ فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿٢٧﴾

“Na wao wana kisasi juu yangu, kwa hivyo naogopa wasije kuniua”.

Kwa ajili ya kumuua yule Mkibiti, ambayo ndiyo iliyokuwa sababu ya yeye kuondoka Misri. Akasema Allah تعالى:

قَالَ كَلَّا

“Siyo hivyo kabisa!”

Allah تعالى Alimwambia: “Usiwe na hofu kabisa kuhusu hilo”. Hii ni kama Kauli Yake:

قَالَ سَتَشُدُّ عَضُدَكَ بِأَخِيكَ وَجَجَعُ لَكُمْ سُلْطٰنًا

“Tutautia nguvu mkono wako kwa ndugu yako, na Tutakupeni ushindi.” (28:35).

Kwa uthibitisho wa wazi hivyo:

فَلَا يَصِلُونَ إِلَيْكُمَا بِغَايَتِنَا أَنْتُمَا وَمَنْ اتَّبَعَكُمَا الْغَالِبُونَ ﴿٣٥﴾

“Hawatakufikieni kwa sababu ya ishara Zetu nyinyi na watakaokufuateni watashinda.” (28:35).

Kwa hiyo:

فَأَذْهَبَا بِغَايَتِنَا إِنَّا مَعَكُمْ مُسْتَمِعُونَ ﴿٣٦﴾

“Nendeni na miujiza Yetu. Hakika Sisi tu pamoja nanyi, Tunasikiliza.”

Hii ni kama Kauli Yake:

إِنِّي مَعَكُمْ أَسْمَعُ وَأَرَى ﴿٣٧﴾

“Hakika Mimi ni pamoja nanyi, Nasikia na Ninaona.” (20:46)

Hakika Mimi Niko pamoja nanyi kwa Kuwahifadhi, Kuwatunza, Kuwanusuru na Kuwasaidia. Hapo wakaelekezwa:

فَأْتِيَا فِرْعَوْنَ فَقُولَا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٨﴾

“Basi mfikieni Firauni na mwambieni Hakika sisi ni Mitume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Hii ni kama Kauli Yake katika Aya nyingine:

إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ

“Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi.” (20:47)

Hii ina maana kuwa sote tumetumwa kwako. Ujumbe wetu ni:

فَأَرْسَلْنَا مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ

“Waachilie wana wa Israili waende nasi.” (20:17)

Hii inamaanisha, waache waende zao, waache huru kutoka katika utumwa wako na mateso, kwani wao ni waja wa Allah تعالى Waumini na miongoni mwa kikundi Chake cha walio na ikhlasi na kwako wako katika adhabu ya kutweza. Aliposema hayo Musa عليه السلام, Firauni aligeuza uso wake na kumpuuza kabisa, na kisha kumtazama kwa jicho la dharau na kumdhaliisha. Akasema (Firauni):

قَالَ أَلَمْ نُرَبِّكَ فِينَا وَلِيدًا

‘Sisi hatukukulea wewe utotoni?’

Maana yake: Hakika yako wewe ni kuwa tulikulea ukiwa mtoto katika nyumba yetu na kitanda chetu. Pia tukakulisha na kukufadhili kwa miaka mingi, na baada ya yote hayo ndio unalipa ihsan yetu kwa njia hii: Uliua mmoja wa watu wetu na ukakanusha neema tulizokupa. Na hapa akasema:

وَأَنْتَ مِنَ الْكَافِرِينَ ﴿١٠﴾

“Nawe ukawa miongoni mwa wasio na shukrani?”

Kumaanisha, miongoni mwa wale waliokanusha neema na fadhila. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Ibn ‘Abbaas, ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, na akaichagua Ibn Jariir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى ¹ (Musa عليه السلام) akasema:

قَالَ فَعَلْتَهَا إِذَا

“Nilitenda hayo hapo”. Yaani, katika hali hiyo,

وَأَنَا مِنَ الضَّالِّينَ ﴿١١﴾

“Nilipokuwa miongoni mwa wale waliopotea.”

Akimaanisha, kabla sijapewa Wahyi na kunineemesha mimi Allah تَعَالَى kwa Kunipa risala na Unabii.

فَفَرَرْتُ مِنْكُمْ لَمَّا خِفْتُمْ فَوَهَبَ لِي رَبِّي حُكْمًا وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٢﴾

“Basi nikakukimbieni nilipokuogopeni, tena Mola wangu Mlezi Akanitunukia hukumu, na Akanijaalia niwe miongoni mwa Mitume.”

Maana yake: Hali hiyo ya kwanza imeisha na nyingine imechukua mahali pake (yaliyopita yamepita). Hakika Allah تَعَالَى Amenituma kwako, na ukimtii Yeye utasalimika na ukimuasi, utaangamia. Kisha akasema Musa عليه السلام:

وَتِلْكَ نِعْمَةٌ تَمُنُّهَا عَلَيَّ أَنْ عَبَّدتَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٣﴾

“Na hiyo ndiyo neema ya kunisembulia, na wewe umewatia utumwani wana wa Israili?”

Hii ina maana kuwa zile fadhila ulizonifanyia mimi katika kunilea hazifikii yale maovu ya kuwafanya watumwa Wana wa Israeli na kuwatumikisha kwa

¹ Atw-Twabariy 19:340.

kazi ngumu. Je, upo ulinganishi wowote baina ya fadhila zako kwa mtu mmoja na maovu uliyowafanyia kundi zima? Hayo uliyoyataja si chochote si lolote ukilinganisha na uliyowafanyia Wana wa Israeli.

قَالَ فِرْعَوْنُ وَمَا رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٣﴾ قَالَ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا إِنَّ كُنْتُمْ
 مُوقِنِينَ ﴿٢٤﴾ قَالَ لِمَنْ حَوْلَهُ أَلَا تَسْتَبْعُونَ ﴿٢٥﴾ قَالَ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٦﴾
 قَالَ إِنَّ رَسُولَكُمْ الَّذِي أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ ﴿٢٧﴾ قَالَ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا
 بَيْنَهُمَا إِنَّ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾

23. "Firauni akasema: Na nani huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote?"

24. Akasema: Ndiye Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na vilivyomo baina yao, ikiwa nyinyi ni wenye yakini.

25. (Firauni) akawaambia waliomzunguka: Hamsikilizi?

26. (Musa) akasema: Ndiye Mola wenu Mlezi, na Mola Mlezi wa baba zenu wa kwanza.

27. (Firauni) akasema: Hakika huyu Mtume wenu aliyetumwa kwenu ni mwendawazimu."

28. (Musa) akasema: Ndiye Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na vilivyomo baina yao, ikiwa nyinyi mnatia akilini."

Anasema Aliyetukuka Akitueleza kufuru ya Firauni, kukengeuka kwake, udhalimu wake na kukanusha kwake katika kauli yake (Firauni):

﴿٢٨﴾ وَمَا رَبُّ الْعَالَمِينَ

"Na nani huyo Mola Mlezi wa walimwengu wote?"

Na hiyo ni kuwa yeye alikuwa akiwaambia kaumu yake:

مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِّنْ إِلَٰهِ غَيْرِي

"Simjui kwa ajili yenu mungu asiyekuwa mimi." (28:38)

فَأَسْتَخَفَّ قَوْمَهُ فَاَطَاعُوهُ

“Na akawachezea watu wake, nao wakamtii.” (43:54).

Wao walikuwa wakimkanusha Muumbaji Aliyetukuka na wakiitakidi kuwa hapana Mola isipokuwa Firauni. Hivyo Musa عليه السلام alipomuambia, **“Hakika mimi ni Mtume kutoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote”**. Firauni alimuuliza: “Ni nani huyu unayedai kuwa ni Mola Mlezi wa walimwengu wote asiyekuwa mimi?” Hivi ndivyo walivyofasiri wanazuoni wema wa tangu (*Salaaf*) na Maimamu wa baadaye. As-Suddiy akasema: “Aya hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

قَالَ فَمَنْ رَبُّكُمَا يَا مُوسَى ﴿٤٩﴾ قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ حَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى ﴿٥٠﴾

“Firauni akasema: Basi Mola wenu Mlezi ni nani, ewe Musa? Akasema: Mola wetu Mlezi ni Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoa.” (20:49-50)

Wale miongoni mwa wanafalsafa na wengineo ambao wanadai ya kwamba hili lilikuwa ni suali kuhusu maumbile ya Allah تعالى wamekosea. Firauni hakuamini kuwa yupo Muumbaji kabisa, hivyo hakuwa katika nafasi ya kuweza kuuliza kuhusu maumbile ya Muumbaji; alikanusha kabisa kuwepo kwa Muumbaji, kama ilivyo dhahiri katika maana, japokuwa alipelekewa dalili na uthibitisho dhidi yake. Pale Firauni alipomuuliza kuhusu Mola Mlezi wa walimwengu wote, Musa عليه السلام alisema:

قَالَ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا

“Ndiye Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na vilivyomo baina yao.”

Hii ina maana kuwa Yeye ni Muumbaji wa vyote hivyo, Mwenye Kuvimiliki na Kuvidhibiti. Pia ndiye Muabudiwa wao asiyekuwa na mshirika. Yeye Ndiye Aliyeumba vitu vyote, naye ni Mjuzi wa ulimwengu wa juu pamoja na nyota zake, zile ambazo hazitembei na zinazotembea na kung’aa. Na pia anajua vilivyo ulimwengu wa chini na vilivyomo ndani yake; bahari, mabara, majabali, miti, hayawani, mimea na matunda. Na anajua vilivyomo baina ya sehemu mbili hizo, pepo, ndege na kila kilichoko katika hewa. Vyote hivyo ni viumbe vyake vinamnyenyekea na kujidhalilisha Kwake.

إِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٦﴾

“Ikiwa nyinyi mnatia akilini.”

Maana yake: Ikiwa muna mioyo ya kuamini na uoni. Kwa maneno hayo, Firauni aligeuka kuwatizama wakuu na viongozi wa dola yake waliomzunguka na kuwaambia kwa stihzai na kuonesha kwake kumkadhibisha Musa عليه السلام:

أَلَا تَسْتَعِينُونَ ﴿٢٧﴾

“Hamsikilizi?”

Kwa hili suali alikuwa akimaanisha, kwani nyinyi hamuoni ajabu kwa madai ya huyu kuwa nyinyi munaye mungu mwengine asiyekuwa mimi? Musa عليه السلام akawaambia:

رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ﴿٢٨﴾

“Ndiye Mola wenu Mlezi, na Mola Mlezi wa baba zenu wa kwanza.”

Maana yake: Aliyewaumbeni nyinyi na wazazi wenu, wale waliokuja kabla ya Firauni na zama zake. Hapo

قَالَ

“...akasema...”

Firauni kwa kaumu yake:

إِنَّ رَسُولَكُمْ الَّذِي أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ ﴿٢٩﴾

“Hakika Mtume wenu huyu aliyetumwa kwenu ni mwenda-wazimu.”

Mtu Huyu wenu hana akili katika mwito wake kuwa yupo Mungu mwengine asiyekuwa mimi. Hapo akasema Musa عليه السلام kwa wale watu ambao kwamba wametiwa shaka nyoyoni mwao na Firauni. Musa عليه السلام akamjibu kwa kusema:

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ إِنَّ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٣٠﴾

“Ndiye Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na vilivyomo baina yao, ikiwa nyinyi mnatia akilini.”

Hii ina maana, Allah تعالى Ndiye Aliyeifanya Mashariki kuwa sehemu ya kuchomoza sayari, na Akaifanya Magharibi kuwa ni sehemu ya kuzama kwao. Huu ni mfumo ambao kwayo Ametiisha sayari zote, zile zilizotulia tuli na zinazotembea. Ikiwa anayosema Firauni kweli kuwa yeye ni mungu wenu basi mwache azifanye sayari zibadilike kutoka katika mfumo wake wa sasa, hivyo azifanye sayari hizo zizame Mashariki na kuchomoza Magharibi. Hii ni kama ile Aya:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ حَاجَّ إِبرَاهِيمَ فِي رَبِّهٖ أَنْ ءَاتَهُ اللهُ الْمُلْكَ إِذْ قَالَ إِبرَاهِيمُ رَبِّيَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ قَالَ أَنَا أُحْيِي وَأُمِيتُ ۗ قَالَ إِبرَاهِيمُ فَإِنَّ اللهَ يَأْتِي بِالشَّمْسِ مِنَ الْمَشْرِقِ فَأْتِ بِهَا مِنَ الْمَغْرِبِ

“Humuona Yule aliyohojiana na Ibraahim juu ya Mola Wake Mlezi kwa sababu Allah Alimpa ufalme? Ibraahim aliposema: Mola wangu ni Yule Ambaye Huhuisha na Kufisha. Yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha. Ibraahim akasema: Allah Hulichomoza jua Mashariki, basi wewe lichomoze Magharibi.” (2:258).

Na kwa kuzingatia hilo, Firauni alipoona kuwa ameshindwa na kuvunjwa vunjwa hoja zake. Aligeukia katika matumizi ya cheo chake, madaraka yake na nguvu yake ya Dola. Na akaamini kuwa hilo pekee ndio litakalomsaidia kwa Musa عليه السلام na kumfanya atii. Firauni akasema kwa mujibu wa Allah تعالى Alivyoeleza kuhusu yeye:

* * *

قَالَ لَيْنٍ أَخَذْتَ إِلَهَهَا غَيْرِي لِأَجْعَلَنَّكَ مِنْ
 الْمَسْجُورِينَ ﴿٢٩﴾ قَالَ أَوْلَوْ جِئْتِكَ بِشَيْءٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾
 قَالَ فَأَتِ بِمِةٍ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٣١﴾ فَأَلْقَى
 عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿٣٢﴾ وَنَزَعَ يَدَهُ فَإِذَا هِيَ
 بَيْضَاءٌ لِلنَّظِيرِينَ ﴿٣٣﴾ قَالَ لِلْمَلَأِ حَوْلَهُ إِنَّ هَذَا لَسِحْرٌ
 عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾ يُرِيدُ أَنْ يُخْرِجَكُمْ مِنْ أَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِ
 فَمَاذَا تَأْمُرُونَ ﴿٣٥﴾ قَالُوا أَرْجِهْ وَأَخَاهُ وَأَبْعَثْ فِي
 الْمَدَائِينَ حَاشِرِينَ ﴿٣٦﴾ يَا تَوَكُّ بِكُلِّ سَحَابٍ عَلِيمٍ ﴿٣٧﴾
 فَجُمِعَ السَّحَرَةُ لِمِيقَاتِ يَوْمٍ مَعْلُومٍ ﴿٣٨﴾ وَقِيلَ لِلنَّاسِ
 هَلْ أَنْتُمْ مُجْتَمِعُونَ ﴿٣٩﴾ لَعَلَّنَا نَتَّبِعُ السَّحَرَةَ إِنْ كَانُوا هُمْ
 الْغَالِبِينَ ﴿٤٠﴾ فَلَمَّا جَاءَ السَّحَرَةُ قَالُوا لِفِرْعَوْنَ إِنَّ لَنَا
 لَأَجْرًا إِنْ كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ ﴿٤١﴾ قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ إِذَا لَمِنَ
 الْمُقْرَبِينَ ﴿٤٢﴾ قَالَ هُمْ مُوسَى الْقَوَا مَا أَنْتُمْ مُلْقُونَ ﴿٤٣﴾
 فَأَلْقَوْا حِبَاهُمْ وَعَصِيَّهُمْ وَقَالُوا بِعِزَّةِ فِرْعَوْنَ إِنَّا لَنَحْنُ
 الْغَالِبُونَ ﴿٤٤﴾ فَأَلْقَى مُوسَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا
 يَأْفِكُونَ ﴿٤٥﴾ فَأَلْقَى السَّحَرَةُ سَجِدِينَ ﴿٤٦﴾ قَالُوا ءَأَمْنَا
 بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾ رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ ﴿٤٨﴾

قَالَ لَيْنٍ أَخَذْتَ إِلَهَهَا غَيْرِي
 لِأَجْعَلَنَّكَ مِنَ الْمَسْجُورِينَ ﴿٢٩﴾
 قَالَ أَوْلَوْ جِئْتِكَ بِشَيْءٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾
 قَالَ فَأَتِ بِمِةٍ إِنْ كُنْتَ مِنَ
 الصَّادِقِينَ ﴿٣١﴾ فَأَلْقَى عَصَاهُ فَإِذَا
 هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿٣٢﴾ وَنَزَعَ يَدَهُ
 فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءٌ لِلنَّظِيرِينَ ﴿٣٣﴾ قَالَ
 لِلْمَلَأِ حَوْلَهُ إِنَّ هَذَا لَسِحْرٌ عَلِيمٌ
 ﴿٣٤﴾ يُرِيدُ أَنْ يُخْرِجَكُمْ مِنْ
 أَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ
 ﴿٣٥﴾ قَالُوا أَرْجِهْ وَأَخَاهُ وَأَبْعَثْ فِي
 الْمَدَائِينَ حَاشِرِينَ ﴿٣٦﴾ يَا تَوَكُّ
 بِكُلِّ سَحَابٍ عَلِيمٍ ﴿٣٧﴾

29. "(Firauni) akasema: Ukimfuata Mungu mwingine asiyekuwa mimi, basi bila ya shaka nitakufunga gerezani.

30. Akasema: Je! Ijapo kuwa nitakuletea kitu cha kubainisha wazi?

31. Akasema: Kilete basi, kama wewe ni kama wasemao kweli.

32. Basi akaitupa fimbo yake, mara ikawa nyoka wa kuonekana dhahiri.

33. Na akautoa mkono wake, na mara ukawa mweupe kwa watazamao.

34. (Firauni) akawaambia waheshimiwa waliomzunguka: Hakika huyu ni mchawi mtaalamu.

35. Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake. Basi mna shauri gani?

36. Wakasema: Mpe muda yeye na nduguye na uwatume mijini wapigao mbiu ya mgambo.

37. Wakuletee kila mchawi bingwa mtaalamu.”

Iliposimama Hoja, Firauni Alitumia Nguvu

Iliposimama hoja juu ya Firauni iliyo wazi na ya kimantiki, alitumia nguvu dhidi ya Musa kwa mkono na ufalme wake, akidhania ya kwamba hakutakuwa na mjadala wowote baada ya hayo. Hivyo akasema:

قَالَ لَئِنِ اتَّخَذَتِ إِلَهًا غَيْرِي لَأَجْعَلَنَّكَ مِنَ الْمَسْجُورِينَ ﴿٢٩﴾

“Ukimfuata Mungu mwengine asiyekuwa mimi, basi bila ya shaka nitakufunga gerezani.”

Kwa kauli hiyo, Musa عليه السلام alimjibu:

أُولَئِكَ جِئْتُكَ بِشَيْءٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾

“Ijapokuwa nitakuletea kitu cha kubainisha wazi?”

Maana yake: Na hoja za wazi, zenye kukata shauri.

قَالَ فَأْتِ بِدَلِيلٍ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٣١﴾ فَأَلْقَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿٣٢﴾

“Akasema: Kilete basi, kama wewe ni kama wasemao kweli. Basi akaitupa fimbo yake, mara ikawa nyoka wa kuonekana dhahiri.”

Muujiza huu ulikuwa wa dhahiri na wa wazi kabisa, ulikuwa na kiwiliwili kikubwa, mdomo mpana na umbo lenye kutisha na kubainisha. Hapo,

وَتَرَعَّ يَدُهُ

“Na akautoa mkono wake.”

Maana yake: Kutoka katika mfuko wake.

فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّظِيرِينَ ﴿٣١﴾

“Na mara ukawa mweupe kwa watazamao.”

Ulikuwa uking'aa kama kipande cha mwezi. Kwa kuwa Firauni alikuwa tayari ameangamia, alifanya haraka kukadhibisha kwa inadi. Hivyo, akasema kwa watu waheshimiwa waliomzunguka:

إِنَّ هَذَا لَسِحْرٌ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾

“Hakika huyu ni mchawi mtaalamu.”

Anayejua uchawi sana. Hivyo, Firauni akawa anajaribu kuwashawishi kuwa huo ulikuwa uchawi na wala si muujiza. Kisha aliwachochea watu dhidi ya Musa عليه السلام kujaribu kuwafanya wampinge na kumkanusha. Akasema:

يُرِيدُ أَنْ يُخْرِجَكُمْ مِنْ أَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِ

“Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake.”

Hakika yeye anataka kuvutia nyoyo za watu kwake kwa sababu ya hili, hivyo kuongezeka wanaomuunga mkono, wasaidizi na wafuasi wake. Hilo litamfanya awashinde na achukue dola yenu kutoka kwenu, basi hebu nipatieni ushauri kwa ninalotakiwa kufanya. Je, nifanye nini? Majibu yao yalikuwa ni ya pamoja, kwani Anatueleza Aliyetukuka:

قَالُوا أَرْجَاهُ وَأَبْعَثْ فِي الْمَدَائِنِ حَاشِرِينَ ﴿٣٣﴾ يَا تُؤْتِك بِكُلِّ سَحَابٍ عَلِيمٍ ﴿٣٤﴾

“Wakasema: Mpe muda yeye na nduguye na uwatume mijini wapigao mbiu ya mgambo. Wakulettee kila mchawi bingwa mtaalamu.”

Shauri lililotolewa ni kuwa msubirisheni yeye (Musa عليه السلام) na nduguye hadi wakusanyike pamoja wachawi kutoka kila mji na eneo ya dola yako ili waweze

kupambana nao na kufanya mazingaombwe kama walivyofanya, na hapo utamshinda. Naye firauni alitekeleza kama alivyoshauriwa. Hilo likawa ni katika usahilisho Aliouleta Allah تعالى katika suala hilo, wajumuike watu katika bonde moja. Hapo Miujiza na Ishara ya Allah تعالى, pamoja na Dalili Zake na Uthibitisho Wake upate kuonekana waziwazi kwa mchana mmoja

فَجُمِعَ السَّحَرَةُ لِمِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٢٩﴾ وَقِيلَ لِلنَّاسِ هَلْ أَنْتُمْ مُجْتَمِعُونَ ﴿٣٠﴾ لَعَلْنَا
 نَتَّبِعَ السَّحَرَةَ إِنْ كَانُوا هُمُ الْغَالِبِينَ ﴿٣١﴾ فَلَمَّا جَاءَ السَّحَرَةُ قَالُوا لِفِرْعَوْنَ أَإِنَّا لَنَا أَجْرًا
 إِنْ كُنَّا خُنُّنَ الْغَالِبِينَ ﴿٣٢﴾ قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ إِذَا لَمِنَ الْمُفْرَبِينَ ﴿٣٣﴾ قَالَ هُمْ مُوسَى
 أَلْقُوا مَا أَنْتُمْ مُلْقُونَ ﴿٣٤﴾ فَأَلْقَوْا حِبَاهُمْ وَعَصِيَّهُمْ وَقَالُوا بِعِزَّةِ فِرْعَوْنَ إِنَّا لَنَحْنُ
 الْغَالِبُونَ ﴿٣٥﴾ فَأَلْقَى مُوسَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ ﴿٣٦﴾ فَأَلْقَى السَّحَرَةُ
 سَعِيدِينَ ﴿٣٧﴾ قَالُوا ءَأَمَّنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٨﴾ رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ ﴿٣٩﴾

38. "Basi wakakusanywa wachawi wakati na siku maalumu.

39. Na watu wakaambiwa: Je! Mtakusanyika?

40. Huenda tutawafuata wachawi wakiwa wao ndio watakaoshinda.

41. Basi walipokuja wachawi wakamwambia Firauni: Je! Tutapata ujira tukiwa sisi ndio tulioshinda?

42. Naam! Na hakika mtakuwa katika watu wa mbele.

43. Musa akawaambia: Tupeni mnavyotaka kutupa.

44. Basi wakatupa kamba zao na fimbo zao, na wakasema: Kwa nguvu za firauni hakika sisi hapana shaka ni wenye kushinda.

45. Musa tena akatupa fimbo yake, nayo mara ikavimeza walivyovizua.

46. Wakasema: Tunamuamini Mola Mlezi wa walimwengu wote.

47. Mola Mlezi wa Musa na Harun.

Baina ya Musa عليه السلام na Wachawi

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu pambano lenyewe baina ya Musa عليه السلام na Wakibti (Wamisri) katika Suratul A'Raaf na katika Surat Twaha na pia katika Surah hii. Wakibti walikuwa wanataka kuizima nuru ya Allah تعالى kwa vinywa vyao, Allah تعالى Anakataa ila aitimize nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia. Haya ndio masuala ya ukafiri na Imani; hayapambani isipokuwa Imani huibuka mshindi. Allah تعالى Anasema:

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ وَلَكُمُ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ ﴿٢١﴾

“Bali Tunaitupa kweli juu ya uwongo ikauvunja na mara ukatoweka. Na ole wenu kwa mnayoyazua.” (21:18).

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ

“Na sema: Kweli imefika, na uongo umetoweka.” (17:81).

Na kwa kuzingatia hilo, wakati wachawi walipokuja, wakiwa wamekusanyika kutoka maeneo mbalimbali ya mji wa Misri. Na wakati huo Wachawi wa Misri walikuwa wajuzi na stadi katika fani hii ya mazingaombwe, na kundi kubwa lilipokuja na kukusanyika siku hiyo kutoka pembe zote za dola (Misri). Idadi yao inajulikana na Allah تعالى Peke Yake. Watu nao walifanya juhudi na bidii ili kujumuika katika siku hiyo. Na hapo mmoja wao akasema:

لَعَلَّآ تَتَّبِعُ السَّحْرَةَ إِن كَانُوا هُمُ الْغَالِبِينَ ﴿٢٢﴾

“Huenda tutawafuata wachawi wakiwa wao ndio watakaoshinda.”

Na hawakusema kuwa watafuata haki na ukweli, sawa ikiwa unatoka kwa wachawi au Musa عليه السلام. Hakika ni kuwa watu walikuwa ni wafuasi wa dini ya mfalme. Anaendelea تعالى Kutueleza:

فَلَمَّا جَاءَ السَّحْرَةُ

“Basi walipokuja wachawi.”

Maana yake: Walipofika katika mahakama ya Firauni, ambaye alikuwa amejengewa kilili. Hapo aliwakusanya watumishi, wafuasi, wasimamizi,

viongozi wa mikoa, na wanajeshi wa ufalme wake. Wachawi walinyanyuka mbele ya Firauni, wakitaka na kuomba ihsani kutoka kwake na kuwaleta wao karibu yake ikiwa watashinda katika mapambano hayo ambaye yeye ndiye aliyewaleta pamoja. Wakasema:

لَيْنَّا لَأَجْرًا إِن كُنَّا خُنُّوا الْعَلْبِيِّنَ ﴿٢٩﴾ قَالَ نَعَمْ وَإِن كُمْ إِذَا لَمِنَ الْمُقْرَبِينَ ﴿٣٠﴾

“Je! Tutapata ujira tukiwa sisi ndio tutakaoshinda? Naam! Na hakika mtakuwa katika watu wa mbele.”

Firauni aliwajibu hayo maneno. Yenye maana kuwa, nyinyi mutapata zaidi ya munayotaka; nitawafanya nyinyi miongoni mwa watu walio karibu sana na mimi. Hivyo walirudi katika sehemu zao za mapambano. Wakauliza (wachawi):

قَالُوا يَمْؤَسَىٰ إِمَّا أَنْ تُلْقَىٰ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوْلَىٰ مِنَ الْقَىٰ ﴿٣١﴾ قَالَ بَلْ أَلْقُوا

“Wakasema: Ewe Musa! Je, utatupa wewe, au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa? Akasema: Bali tupeni nyinyi.” (20:65-66).

Hapa tukio hilo limeelezwa kwa kifupi. Musa عليه السلام aliwaambia:

أَلْقُوا مَا أَنْتُمْ مُلْقُونَ ﴿٣٢﴾ فَأَلْقَوْا حِبَاهُمْ وَعِصِيَّهُمْ وَقَالُوا بِعِزَّةِ رَبِّنَا إِنَّا لَنَجُنُّ الْعَلْبِيُونَ ﴿٣٣﴾

“Tupeni mnavyotaka kutupa. Basi wakatupa kamba zao na fimbo zao, na wakasema: Kwa nguvu za Firauni hakika sisi hapana shaka ni wenye kushinda.”

Na hii ni kama walivyosema wajinga miongoni mwa watu wa kawaida wanapofanya kitu: “Hii ni kwa ajili ya fadhila ya fulani na fulani.” Na hakika Ametaja Allah تعالى katika Suratul A'raaf kuwa wao:

سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ وَأَسْرَبُوهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرِ عَزِيمٍ ﴿١١٦﴾

“Waliyazuga macho ya watu na wakawatia hofu, na wakaleta uchawi mkubwa.” (7:116).

Na Akasema katika Surah Twaha:

فَإِذَا جِبَاهُهُمْ وَعَصِيْبُهُمْ مُخَيَّلُ إِلَيْهِ مِن سِحْرِهِمْ أَنهَاتَسْعَى ﴿٦٦﴾

“Tahamaki kamba na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio.”

Hadi Kauli Yake:

وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى ﴿٦٧﴾

“Na mchawi hafanikiwi popote afikapo.” (20: 66-69).

Na Akasema hapa:

فَأَلْقَى مُوسَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ ﴿٦٨﴾

“Musa tena akatupa fimbo yake, nayo mara ikavimeza walivyovizua”.

Kwa kuvikamata na kuvishika kutoka kila pembe na kuvimeza na haikuacha chochote kati ya hizo isipokuwa ilivigusa. Anasema Allah تعالى:

فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٩﴾

“Kweli ikathibiti na yakabatilika waliyokuwa wakiyatenda.”

Hadi Kauli Yake Aliyetukuka:

رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ ﴿٧٠﴾

“Mola Mlezi wa Musa na Haarun.” (7:118-122).

Na hili lilikuwa somo kubwa sana, na uthibitisho na hoja ya nguvu isiyoacha udhuru wa yoyote ule. Hivyo ni kuwa wale waliokuja kumnusuru na wakawa na matumaini ya kushinda, walishindwa na hivyo kuwafanya wao kunyenyekea. Hapo katika wakati huo mgumu, walimuamini na wakamsujudia Allah تعالى Mola Mlezi wa walimwengu wote, ambaye Amewatuma Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام kwa ukweli na haki na Miujiza ya wazi kabisa. Huko kulikuwa ni kushindwa kukubwa kwa Firauni iwe juu yake laana ya Allah pamoja na Malaika na watu wote, kwa njia ambayo ulimwengu haujawahi kuona. Lakini mbali na hilo Firauni alibaki na kiburi na inadi yake na akaendelea kuita watu katika batili. Hapo alianza kuwatisha na kuwaonya waliokuwa wachawi:

إِنَّهُ لَكَبِيرٌ كُمْ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّعْرَ

*“Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliyekufundisheni uchawi.”
(20:71).*

Na akasema:

إِنَّ هَذَا لَمَكْرٌ مَكْرَتُمْوهُ فِي الْمَدِينَةِ

“Hizi ni njama mlizopanga mjini.” (7:123).

* * *

قَالَ ءَامَنْتُمْ لَهُ قَبْلَ أَنْ ءَاذَنَ لَكُمْ ^ط
 إِنَّهُ لَكَبِيرِكُمْ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ
 فَلَسَوْفَ تَعْمُونَ ^ع لَأَقْطَعَنَّ أَيْدِيَكُمْ
 وَأَرْجُلَكُمْ مِنْ خِلْفٍ وَلَأَصْلَبَنَكُمْ
 ضَمِيرٌ ^ط إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ ﴿٤٩﴾
 إِنَّا نَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لَنَا
 رَبُّنَا خَطِيئَتَنَا أَنْ كُنَّا أَوَّلَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٠﴾ * وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ
 مُوسَىٰ أَنْ أَسْرِ بِعِبَادِي إِنَّكَ مُتَّبَعُونَ ﴿٥١﴾ فَأَرْسَلْنَا فِرْعَوْنَ
 فِي الْمَدَائِنِ حَاشِرِينَ ﴿٥٢﴾ إِنَّ هَذِهِ لَشِرْذِمَةٌ قَلِيلُونَ ﴿٥٣﴾
 وَإِنَّهُمْ لَنَا لَغَائِظُونَ ﴿٥٤﴾ وَإِنَّا لَجَمِيعٌ حَادِرُونَ ﴿٥٥﴾
 فَأَخْرَجْنَاهُمْ مِنْ جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٥٦﴾ وَكُنُوزٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ
 ﴿٥٧﴾ كَذَٰلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٨﴾ فَاتَّبَعُوهُمْ
 مُشْرِقِينَ ﴿٥٩﴾ فَلَمَّا تَرَاءَا الْجَمْعَانِ قَالَ أَصْحَابُ
 مُوسَىٰ إِنَّا لَمُدْرِكُوكُمْ ﴿٦٠﴾ قَالَ كَلَّا إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهْدِينِ
 ﴿٦١﴾ فَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَضْرِبْ بِعَصَاكَ الْبَحْرَ ^ط
 فَانْفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَالطَّوْدِ الْعَظِيمِ ﴿٦٢﴾ وَأَزْلَفْنَا ثَمَّ
 الْأَخْرِينَ ﴿٦٣﴾ وَأَحْبَبْنَا مُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ أَجْمَعِينَ ﴿٦٤﴾ ثُمَّ
 أَعْرَفْنَا الْأَخْرِينَ ﴿٦٥﴾ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً ^ط وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ
 مُؤْمِنِينَ ﴿٦٦﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْرِضُ الرَّحِيمُ ﴿٦٧﴾

قَالَ ءَامَنْتُمْ لَهُ قَبْلَ أَنْ ءَاذَنَ لَكُمْ ^ط
 إِنَّهُ لَكَبِيرِكُمْ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ
 فَلَسَوْفَ تَعْمُونَ ^ع لَأَقْطَعَنَّ أَيْدِيَكُمْ
 وَأَرْجُلَكُمْ مِنْ خِلْفٍ وَلَأَصْلَبَنَكُمْ
 ضَمِيرٌ ^ط إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ ﴿٤٩﴾
 إِنَّا نَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لَنَا
 رَبُّنَا خَطِيئَتَنَا أَنْ كُنَّا
 أَوَّلَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٠﴾

49. "(Firauni) akasema: Je!
 Mmemuamini kabla sijaku-
 rurusuni? Bila ya Shaka
 yeye basi ndiye mkubwa
 wenu aliyekufunzeni
 uchawi. Basi mtakuja jua!
 Nitakata mikono yenu na
 miguu yenu kwa kutafa-
 utisha. Na nitakubandikeni
 misalabani nyote.

50. Wakasema: Haidhuru,
 kwani sisi ni wenye kurejea
 kwa Mola wetu Mlezi.

51. Hakika sisi tunatumai
 Mola wetu Mlezi Atatu-

samehe makosa yetu, kwa kuwa ndio wa kwanza wa kuamini."

Baina ya Firauni na Wachawi

Kuwatisha hakukufalia kitu na kuwaonya hakukuwazidishia ila imani na kujisalimisha, hii ni kwa sababu ya kunyanyuliwa kizuizi cha ukafiri kutoka katika nyoyo zao. Hapo ilidhihiri kwao haki kwa ajili ya wasichojua kaumu yao. Kuwa alichokuja nacho Musa عليه السلام hakiwezi kufanywa na mwanadamu yeyote yule isipokuwa kwa usaidizi wa Allah تعالى. Hivyo, kuijaalia kuwa ni hoja na dalili ya ukweli kwa alichokuja nacho kutoka kwa Mola Mlezi. Kwa hiyo alipowaambia Firauni:

ءَامَنْتُمْ لَهُ قَبْلَ أَنْ ءَاذَنَ لَكُمْ

“Je! Mmeuamini kabla sijakuruhusuni?”

Ilikuwa ni lazima kwenu kuniomba mimi ruhusa kwa muliyoyafanya. Nanyi hamkunitaka ushauri kwa hilo. Lau ningewapatia ruhusa basi mngefanya, na kama sikuwapatia idhini, mngeliacha. Kwani mimi ndiye mfalme ninayefaa kutiwa.

إِنَّهُ لَكَبِيرٌ لَّكَمُ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ

“Bila ya Shaka yeye basi ndiye mkubwa wenu aliyekufunzeni uchawi.”

Haya ni mazungumzo ya ukaidi na kila mmoja anajua kuwa ni upuuzi mtupu, kwani hawakuwa wamewahi kukutana na Musa عليه السلام kabla ya siku hiyo.

Vipi atakuwa mkubwa wao aliyewafunza wao uchawi? Haya hayasemi mwenye akili.

Kisha akawaonya wao Firauni kuwa atawakata mikono na miguu na kuwasulubu, lakini wakasema:

لَا ضَيْرَ

“Haidhuru.”

Hilo halitutishi wala hakuna tatizo lolote wala halitudhuru wala hatujali. Sababu ni kuwa:

إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ ﴿٢٦﴾

“Kwani sisi ni wenye kurejea kwa Mola Wetu Mlezi”.

Maana yake: Sisi tutarudi siku moja kwa Allah Aliyetukuka, Naye Kwake Hauptotei ujira wa mwenye kufanya amali njema. Unayotufanyia sisi hayafichiki Kwake, na Atatujazi kwa hilo jaza kamilifu. Hivyo wakasema:

إِنَّا نَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لَنَا رَبُّنَا

“Hakika sisi tunatumai Mola Wetu Mlezi Atatusamehe makosa yetu.”

Maana yake: Kwa madhambi yote tuliyoifanya na kwa uchawi uliotulazimisha kufanya.

أَنْ كُنَّا أَوَّلَ الْمُؤْمِنِينَ

“Kwa kuwa ndio wa kwanza wa kuamini.”

Maana yake: Kwa sababu sisi ni wa kwanza miongoni mwa watu wetu, Wakibiti, kuamini. Hivyo, akawaua wote.

* وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَسْرِ بِعِبَادِيٰ إِنَّكَ مُتَّبَعُونَ ﴿٥٢﴾ فَأَرْسَلْنَا فِرْعَوْنَ فِي الْمَدَائِنِ حَاشِرِينَ ﴿٥٣﴾ إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَشِرْذِمَةٌ قَلِيلُونَ ﴿٥٤﴾ وَإِنَّهُمْ لَنَا لَغَائِظُونَ ﴿٥٥﴾ وَإِنَّا لَجَمِيعٌ حَادِرُونَ ﴿٥٦﴾ فَأَخْرَجْنَاهُمْ مِّنْ جَنَّتِ وَعُيُونٍ ﴿٥٧﴾ وَكُنُوزٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ﴿٥٨﴾ كَذَٰلِكَ وَأَوْزَنْنَاهَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٩﴾

52. “Na Tulimuamrisha Musa kwa wahyi: Nenda na waja Wangu wakati wa usiku. Kwa hakika mtafuatwa.

53. Basi Firauni akawatuma mijini wapiga mbiu za mgambo;

54. (Wakieneza): Hakika hawa ni kikundi kidogo.

55. Nao wanatuudhi.

56. Na sisi ni wengi, wenye kuchukua hadhari.

57. Basi Tukawatoa katika bustani na chemchem,

58. Na makhazina, na vyeo vya hishima,

59. Kadhalika; na Tukawarithisha wana wa Israili.”

Kutoka kwa Wana wa Israili Misri

Baada ya Musa عليه السلام kukaa Misri kwa muda mrefu, na Firauni pamoja na waheshimiwa wake wametolewa hoja na uthibitisho kutoka kwa Allah تعالى, lakini pamoja na hayo wakaendelea kuwa na kiburi na inadi, hivyo hakukubaki juu yao isipokuwa adhabu ya kupigiwa mfano, mazingatio na onyo kwao. Hivyo, Allah تعالى Akaamuru Musa عليه السلام atoke na Wana wa Israili usiku mmoja kutoka Misri na aende sehemu atakayoamuriwa. Musa عليه السلام akafanya aliyoamriwa na Mola wake Mlezi Aliyetukuka. Alitoka nao baada ya kuazima mapambo mengi ya vito kwa watu wa Firauni. Wanazuoni wengi wa Tafsir wamesema kuwa walitoka baada ya kuchomoza kwa mwezi. Ametaja Mujaahid, Allah تعالى Amrehemu, kuwa mwezi ulipatwa usiku huo.¹ Allah تعالى Anajua zaidi. Musa عليه السلام aliuliza kuhusu kaburi la Nabii Yusuf عليه السلام na akaoneshwa yeye na mwanamke ajuza miongoni mwa Wana wa Israili. Naye akachukua sanduku lake la agano pamoja nao, na pamesemwa kuwa Nabii Yusuf عليه السلام aliusia kuwa pindi Wana wa Israili watakapotoka Misri, wachukue sanduku lake la agano yake pamoja nao.²

Kulipopambazuka, kukawa hakuna yeyote aliyeonekana katika makazi ya Wana wa Israili, Firauni alijawa na hasira na ghadhabu yake ikazidi kwani Allah تعالى Alikuwa tayari Amepitisha kuwa ataangamia. Naye akatuma haraka haraka wapiga mbiu ya mgambo katika kila mji, yaani kuhamasisha na kukusanya jeshi lake na kulileta pamoja. Naye aliwaita:

إِنَّ هَٰؤُلَاءِ

“Hakika hawa.”

Akimaanisha Wana wa Israili ni,

لَشِرْذِمَةٌ قَلِيلُونَ

“Kikundi kidogo.”

Maana yake: Ni kipote kidogo sana (hakiwezi kuwasumbua nyinyi mlio wengi). Akaendelea kusema:

¹ Atw-Twabariy 19: 354.

² Atw-Twabariy 19: 354.

وَأَيْتُمْ لَنَا لَغَائِظُونَ ﴿٢٦﴾

“Nao wanatuudhi.”

Maana yake: Kila wakati tunaposikia kuwahusu wao, inatufadhahisha na kututia hasira.

وَأِنَّا لَجَمِيعٌ حَادِرُونَ ﴿٢٧﴾

“Na sisi ni wengi, wenye kuchukua hadhari.”

Maana yake: Sisi kila wakati tunachukua tahadhari kwa hiyana zao. Baadhi ya wa tangu wema wanaisoma: *“Na sisi tuko tayari kwa silaha (na tunakuwa na tahadhari) kila wakati.”* Nami nataka kuwaangamiza wote mpaka mtu wao wa mwisho kabisa, na kuharibu ardhi zao zote na mali zao. Hivyo, yeye na jeshi lake wakaadhibiwa kwa vitu vile vile alivyotaka kuwaumiza navyo Wana wa Israili.

Allah تعالیٰ Anasema:

فَأَخْرَجْنَاهُمْ مِّنْ جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٢٨﴾ وَكُنُوزٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ﴿٢٩﴾

“Basi Tukawatoa katika bustani na chemchem, na makhazina, na vyeo vya hishima.”

Hapo wakatoka katika neema hizi kuelekea kwenye Jahanamu, hivyo kuacha hizo nyumba za juu za heshima (makasri), bustani, mito, mali, riziki, cheo, ufalme na nguvu katika huu ulimwengu. Kisha Allah تعالیٰ Anasema:

كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٣٠﴾

“Kadhalika; na Tukawarithisha wana wa Israili.”

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضَعُونَ مَشْرِقَ الْأَرْضِ وَمَغْرِبَهَا الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا

“Na Tukawarithisha watu waliokuwa wanadharauliwa mashariki na magharibi ya ardhi Tuliyoibariki.” (7:137)

Na Amesema Aliyetukuka:

وَتُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَئِمَّةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ ﴿٥٦﴾

“Na Tukataka kuwafanyia ihsani wale walioodhoofishwa katika ardhi hiyo na kuwafanya viongozi, na kuwafanya warithi wa neema hizo.” (28:5-6).

فَاتَّبِعُوهُمْ مُشْرِقِينَ ﴿٥٧﴾ فَلَمَّا تَرَاءَا الْجَمْعَانَ قَالَ أَصْحَابُ مُوسَى إِنَّا لَمُدْرِكُونَ ﴿٥٨﴾ قَالَ كَلَّا إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهْدِينِ ﴿٥٩﴾ فَأَوْحَيْنَا إِلَى مُوسَى أَنْ أَضْرِبْ بِعَصَاكَ الْبَحْرَ فَانفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَالطَّوْدِ الْعَظِيمِ ﴿٦٠﴾ وَأَزْلَفْنَا نَمَّ الْأَخْرِينَ ﴿٦١﴾ وَأُنْحَيْنَا مُوسَى وَمَنْ مَعَهُ أَجْمَعِينَ ﴿٦٢﴾ ثُمَّ أَعْرَفْنَا الْأَخْرِينَ ﴿٦٣﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ط وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٦٤﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٦٥﴾

60. *“Basi wakawafuata lilipocho moza juu.*

61. *Na yalipoonana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana!*

62. *(Musa) akasema: Hasha! Hakika Yu pamoja nami Mola Wangu Mlezi. Yeye Ataniongoa!*

63. *Tulimletea wahyi Musa Tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa.*

64. *Na Tukawajongeza hapo wale wengine.*

65. *Tukawaokoa Musa na waliokuwa pamoja naye wote.*

66. *Kisha Tukawazamisha hao wengine.*

67. *Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara; lakini wengi wao si katika wenye kuamini.*

68. *Na kwa hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu.”*

Firauni Kuwaandama Wana wa Israili na Kuangamia yeye na Watu Wake

Wanazuoni wengi wa Tafsiri wametaja kuwa Firauni alitoka na kundi kubwa mno, likijumlisha viongozi na serikali yote ya Misri katika zama zake.

Miongoni mwao walikuwa ni wale wenye kutoa uamuzi na waheshimiwa katika dola, wakiwemo maamiri na watoto wa kifalme, mawaziri, watu wakubwa, viongozi na wanajeshi.

Allah تعالی Anasema:

فَاتَّبَعُوهُمْ مُشْرِقِينَ ﴿٦٠﴾

“Basi wakawafuata lilipo chomoza jua.”

Hii ina maana kuwa waliwafikia Wana wa Israili wakati wa kuchomoza jua. Allah تعالی Anaendelea:

فَلَمَّا تَرَاءَا الْجَمْعَانِ

“Na yalipoonana majeshi mawili haya.”

Maana yake: Kila kundi liliona jengine, ana kwa ana. Hapo:

قَالَ أَصْحَابُ مُوسَىٰ إِنَّا لَمُدْرِكُونَ ﴿٦١﴾

“Watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana!”

Hii ni kuwa Firauni na watu wake waliwapata Wana wa Israili katika ufuko wa Bahari Nyekundu (Red Sea).

Hiyo ni kuwa Bahari ilikuwa mbele yao na Firauni na jeshi wakawa wapo nyuma yao. Hivyo wakasema (Wana wa Israili):

إِنَّا لَمُدْرِكُونَ ﴿٦١﴾ قَالَ كَلَّا إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهْدِينِ ﴿٦٢﴾

“Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana! (Musa) akasema: Hasha! Hakika Yu pamoja nami Mola Wangu Mlezi. Yeye Ataniongoa!”

Hakuna chochote munachohofia kitakachowapata nyinyi, kwani Allah تعالی Ndiye Aliyeniagiza mimi kuwaleta hapa, hakika Yeye Havunji Ahadi Yake.

Haarun عليه السلام alikuwa mbele pamoja na Yuusha' ibn Nuun na Muumini miongoni mwa familia ya Firauni na Musa عليه السلام alikuwa nyuma ya msafara huo.

Wamesema wengi miongoni mwa wanazuoni wa Tafsiri kuwa walisimama hapo bila kujua cha kufanya, hapo Yuusha' ibn Nuun au Muumini katika familia ya Firauni akamuuliza Musa عليه السلام: "Ewe Nabii wa Allah! Je, ni hapa ndipo alipokuamuru Mola wako Mlezi utulete?" Akasema: "Ndio."

Firauni na jeshi lake wakawa wanaokuja na kufika karibu sana nao. Hapo ndipo Allah تعالى Alimuamuru Musa عليه السلام apige bahari kwa fimbo yake, naye akaipiga na huku anasema: "Tengana kwa Idhini ya Allah تعالى."

Allah تعالى Anasema:

فَأَنفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَالطَّوْدِ الْعَظِيمِ ﴿٦٧﴾

"Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa."

Maana yake: Ikawa kama majabali makubwa. Amesema hayo Ibn Mas'ud na Ibn 'Abbaas na pia Muhammad ibn Ka'b, Adh-Dhahhaak, Qataadah na wengineo¹ رضي الله عنهم.

Akasema 'Atwaa' Al-Khurasaniy: "Hiyo ni njia baina ya majabali mawili." Naye Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما akasema: "Bahari iligawanyika zikatokea njia kumi na mbili, njia moja kwa kila kabila."²

Akaongeza As-Suddiy: "Na ndani yake kukawa na madirisha ambayo walikuwa wanaweza kuonana, na maji yalisimama wima kama ukuta."³

Hapo Allah تعالى Alituma upepo chini ya bahari ukainyausha, kwa hiyo ikawa ngumu kama uso wa ardhi. Anasema Allah تعالى:

فَأَضْرَبَ لَهِمْ طَرِيقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا لَا تَخَفُ دَرَكًا وَلَا تَخْشَى ﴿٦٨﴾

"Na uwapigie njia kavu baharini. Usikhofu kukamatwa wala usiogope." (20:77).

¹ Atw-Twabariy 19:358.

² Ad-Durr al-Manthuur 6:299.

³ Atw-Twabariy 19:357.

Na Akasema katika kisa hiki:

وَأَزَلَفْنَا ثُمَّ الْآخِرِينَ ﴿٦٠﴾

“Na Tukawajongeza hapo wale wengine”.

Maana yake: Huko. Amesema Ibn ‘Abbaas, ‘Atwaa’ Al-Khurasaniy, Qataadah na As-Suddiy:

وَأَزَلَفْنَا

“Na Tukawajongeza”.

Maana yake: Tulimleta Firauni na jeshi lake karibu na bahari.¹ Hapo basi ndio hatima ya kila mmoja ikafika:

وَأَجْبَيْنَا مُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ أَجْمَعِينَ ﴿٦١﴾ ثُمَّ أَعْرَفْنَا الْآخِرِينَ ﴿٦٢﴾

“Tukawaokoa Musa na waliokuwa pamoja naye wote. Kisha Tukawazamisha hao wengine”.

Hii ina maanisha kuwa, Tulimuokoa Musa عليه السلام, Wana wa Israili na wale waliofuata katika Dini yao. Hakuangamizwa hata mmoja miongoni mwao, lakini Firauni na jeshi lake lote waligharikishwa na hakuna hata mmoja aliyepona (wote waliangamia). Kisha Akasema Aliyetukuka:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لآيَةً

“Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara”.

Maana yake: Katika kisa hiki na yale yaliyomo ndani katika maajabu, ushindi na usaidizi kwa waja wa Allah تعالى, Waumini, ipo dalili na hoja za wazi na dhahiri na upepo wa Hekima ya Allah تعالى. Na Allah تعالى Anasema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٦٣﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٦٤﴾

“Lakini wengi wao si katika wenye kuamini. Na kwa hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu.”

Tafsiri na maelezo ya Aya hii tayari imetangulia.¹

¹ Atw-Twabariy 19:359.

² Tazama Aya ya 9 ya Surah hii hii.

وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٩﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٧٠﴾ قَالُوا نَعْبُدُ أَصْنَامًا فَنَنْظِلُهَا عَنْكَهِنَّ ﴿٧١﴾ قَالَ هَلْ يَسْمَعُونَكُمْ إِذْ تَدْعُونَ ﴿٧٢﴾ أَوْ يَنْفَعُونَكُمْ أَوْ يَضُرُّونَ ﴿٧٣﴾ قَالُوا بَلْ وَجَدْنَا آبَاءَنَا كَذَلِكَ يَفْعَلُونَ ﴿٧٤﴾ قَالَ أَفَرَأَيْتُمْ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٧٥﴾ أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ الْأَقْدَمُونَ ﴿٧٦﴾ فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِي إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾ الَّذِي خَلَقَنِي فَهُوَ يَهْدِينِ ﴿٧٨﴾ وَالَّذِي هُوَ يُطْعِمُنِي وَيَسْقِينِ ﴿٧٩﴾ وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ ﴿٨٠﴾ وَالَّذِي يُعِيتُنِي ثُمَّ يُجْحِبُنِي ﴿٨١﴾ وَالَّذِي أَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ الدِّينِ ﴿٨٢﴾ رَبِّ هَبْ لِي حُكْمًا ﴿٨٣﴾ وَالْحَقْفِي بِالصَّلَاحِيبِ ﴿٨٤﴾ وَأَجْعَلْ لِي لِسَانَ صِدْقٍ فِي الْآخِرِينَ ﴿٨٥﴾ وَأَجْعَلْنِي مِنْ وَرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيمِ ﴿٨٦﴾ وَأَغْفِرْ لَأَيِّئِ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الضَّالِّينَ ﴿٨٧﴾ وَلَا تُخْزِنِي يَوْمَ يُبْعَثُونَ ﴿٨٨﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ ﴿٨٩﴾ إِلَّا مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٩٠﴾

وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٩﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٧٠﴾ قَالُوا نَعْبُدُ أَصْنَامًا فَنَنْظِلُهَا عَنْكَهِنَّ ﴿٧١﴾ قَالَ هَلْ يَسْمَعُونَكُمْ إِذْ تَدْعُونَ ﴿٧٢﴾ أَوْ يَنْفَعُونَكُمْ أَوْ يَضُرُّونَ ﴿٧٣﴾ قَالُوا بَلْ وَجَدْنَا آبَاءَنَا كَذَلِكَ يَفْعَلُونَ ﴿٧٤﴾ قَالَ أَفَرَأَيْتُمْ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٧٥﴾ أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ الْأَقْدَمُونَ ﴿٧٦﴾ فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِي إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾

69. "Na wasomee khabari za Ibraahim.

70. Alipomwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini?

71. Wakasema: Tunaabudu masanamu, daima tunayanyenyekea.

72. Akasema: Je! Yanakusikieni mnapoyaita?

73. Au yanakufaeni, au yanakudhuruni?

74. Wakasema: Bali tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo hivyo.

75. Je! Mmewaona hawa mnaowaabudu.

76. Nyinyi na baba zenu wa zamani?

77. Kwani hakika hao ni adui zangu, isipokuwa Mola Mlezi wa walimwengu wote”.

Waadhi wa Kipenzi cha Allah, Ibraahim عليه السلام Katika Kupinga Ushirikina

Hii ni habari kutoka kwa Allah تعالى kuhusu mja, Mtume na Kipenzi Chake, Ibraahim عليه السلام Imamu wa *Hunafaa'* (wanaompwekesha Allah). Allah تعالى Alimuamuru Mtume Wake, Muhammad ﷺ awesomee Ummah wake kisa hiki ili nao waweze kufuata kielelezo chake katika Ikhlasu na kutegemea na kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila kumshirikisha na kujitenga na ushirikina na Washirikina. Hakika Allah تعالى Alimpa Ibrahim عليه السلام uwongofu kutoka Kwake kabla, yaani katika umri mdogo mpaka ukubwani mwake, aliwakataza kaumu yake kuabudu masanamu pamoja na Allah تعالى. Allah تعالى Anasema:

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٧٧﴾

“Alipomwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini?”

Yaani, Ni kwanini haya masanamu nyinyi munayanyenyekea?, Nao hawakusita.

قَالُوا نَعْبُدُ أَصْنَامًا مَّا فَنَنْظِلُ هَا عَنْكُمِينَ ﴿٧٨﴾

“Wakasema: Tunaabudu masanamu, daima tunayanyenyekea.”

Hii ni kumaanisha tutadumu katika kuyaabudu na kuyaomba. Nabii Ibraahim عليه السلام akawahoji zaidi:

قَالَ هَلْ يَسْمَعُونَكُمْ إِذْ تَدْعُونَ ﴿٧٩﴾ أَوْ يَنْفَعُونَكُمْ أَوْ يَضُرُّونَ ﴿٨٠﴾ قَالُوا بَلْ وَجَدْنَا

ءَابَاءَنَا كَذَلِكَ يَفْعَلُونَ ﴿٨١﴾

“Akasema: Je! Yanakusikieni mnapoyaita? Au yanakufaeni, au yanakudhuruni? Wakasema: Bali tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo hivyo.”

Hii ina maana kuwa walitambua kuwa masanamu yao hayawezi kufanya lolote wala chochote katika hayo. Na hakika wao wamewaona tu wazazi wao wakifanya hivyo, nao wakafanya haraka kufuata nyayo zao. Hapo Ibraahim akawaambia:

قَالَ أَفَرَأَيْتُمْ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٧٦﴾ أَتُنْتُمُ وَاَبَاؤُكُمْ الْأَقْدَمُونَ ﴿٧٧﴾ فَلَيْسَ بَعْدُ لِلَّهِ إِلَهٌ إِلَّا رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٨﴾

“Je! Mmewaona hawa mnaowaabudu. Nyinyi na baba zenu wa zamani? Kwani hakika hao ni adui zangu, isipokuwa Mola Mlezi wa walimwengu wote”.

Maana yake: Ni ikiwa masanamu haya yana maana yoyote na yanaweza kushawishi na kuvutia, basi yaache yanidhuru kwa njia yoyote ile, kwani mimi ni adui yao mkubwa na siyajali kabisa wala kuyafikiria.

Na mfano huu ni kama Alivyosema Allah عليه السلام kuhusu Nuuh:

فَأَجْمِعُوا أَمْرَكُمْ وَشُرَكَاءَكُمْ

“Nanyi tengezeni mambo yenu na washirika wenu.” (10:71).

Na akasema Huud عليه السلام:

إِنِّي أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾ مِنْ دُونِهِ ط فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونَ ﴿٥٥﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ ؕ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا ؕ إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

“Hakika mimi namshuhudia Allah, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnaowafanya washirika, mkamwacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula! Hakika mimi nimemtegemea Allah, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye Anamwendesha Atakavyo. Hakika Mola Wangu Mlezi yuko juu ya njia iliyonyooka.” (11:54-56).

Hivyo hivyo, Ibraahim عليه السلام alijitenga na kuwakana miungu yao, pale aliposema:

وَكَيْفَ أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُمْ بِاللَّهِ

“Na vipi nivikhofu hivyo mnavyovishirikisha, hali nyinyi hamkhofu kuwa nyinyi mnamshirikisha Allah.” (6:81).

Na Akasema Aliyetukuka:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ

“Hakika nyinyi muna mfano mzuri kwa Ibraahim.”

Hadi kauli Yake:

حَتَّىٰ تَوَدُّونَا بِاللَّهِ وَحْدَهُ

“Mpaka mtakapomuamini Allah Peke Yake.” (60:4).

Na Amesema Aliyetukuka:

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٦٩﴾ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ
﴿٧٠﴾ وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٧١﴾

**“Na wakumbushe Ibraahim alipomwambia babake na watu wake:
“Bila shaka mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu.
Isipokuwa Yule Aliyeniumba; kwa yakini Yeye Ataniongoa. Na
akalifanya neno hili ni neno lenye kubaki katika kizazi chake ili
warejee.” (43:26-28).**

Hii ina maana ya kurudi katika *Laa ilaaha illa Llahu* (Hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allah تعالی Peke Yake).

الَّذِي خَلَقَنِي فَهُوَ يَهْدِينِ ﴿٧٢﴾ وَالَّذِي هُوَ يُطْعِمُنِي وَيَسْقِينِ ﴿٧٣﴾ وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ ﴿٧٤﴾ وَالَّذِي يُمِيتُنِي ثُمَّ يُحْيِينِ ﴿٧٥﴾ وَالَّذِي أَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ
الَّذِينَ ﴿٧٦﴾

78. “Ambaye Ndiye Aliyeniumba, na Yeye Ndiye Ananiongoa.

79. Na Ambaye Ndiye Ananilisha na Kuninywasha.

80. Na ninapougua ni Yeye Ndiye Anayeniponesha.

81. Na Ambaye Atanifisha, na kisha Atanihuisha.

**82. Na Ambaye Ndiye ninayemtumai kunisamehe makosa yangu
Siku ya Malipo.”**

Ibraahim عليه السلام Anataja Ukairimu wa Allah تعالى Kwake

Ibraahim عليه السلام alisema kuwa hatamuabudu yeyote isipokuwa yule anayemfanyia vitu hivi:

الَّذِي خَلَقَنِي فَهُوَ يَهْدِينِ ﴿٦٩﴾

“Ambaye Ndiye Aliyeniumba, na Yeye Ndiye Ananiongoa.”

Hakika ni kuwa Yeye Ndiye Muumbaji Ambaye Amevikuduria vitu kwa uweza Wake na Kuwaongoa viumbe Vyake. Hivyo, kila mmoja anafuata njia aliyoandikiwa. Naye Peke Yake Ndiye Mwenye Kumuongoa Amtakaye na Kumpoteza Amtakaye.

وَالَّذِي هُوَ يُطْعِمُنِي وَيَسْقِينِ ﴿٧٠﴾

“Na Ambaye Ndiye Ananilisha na Kuninyweshwa.”

Yeye Ndiye Aliyeniumba, Mwenye Kuniruzuku kwa kile Alichonipangia na Kufanya sahali sababu za mbinguni na ardhini. Anayapeleka mawingu na Kuteremsha mvua na hivyo Kuhuisha ardhi na Kuotesha kila aina ya mimea na matunda ambayo ni riziki kwa waja. Na Anateremsha maji safi na tamu ambayo Alivyoviumba vinakunywa, wanyama hoa na wanadamu wengi. Na Kauli Yake:

وَإِذَا مَرَضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ ﴿٧١﴾

“Na ninapougua ni Yeye Ndiye Anayeniponesha.”

Hapa ananasibisha maradhi kwa nafsi yake, japokuwa Yeye Allah تعالى Ndiye Kakuduria, hii ni kuonesha heshima na adabu yake kwa Allah تعالى. Kama Alivyosema Aliyetukuka Kuwaamuru wenye kuswali waseme:

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٧٢﴾

“Tuongoe njia iliyonyooka.” (1:6).

Mpaka Mwisho wa Surah. Hivyo, neema na uongofu ukanasibishwa na Allah تعالى, lakini katika kitendo cha ghadhabu, mwenye kukifanya ameondoshwa. Hakutajwa, hii ni kuonesha adabu. Na upotevu umenasibishwa na watu. Hii ni kama walivyosema majini:

وَأَنَا لَا تَدْرِي أَشَرُّ أَرِيدَ بِمَنْ فِي الْأَرْضِ أَمْ أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ﴿٦٩﴾

“Na hatujui kama wanatakiwa shari wale wanaokaa katika ardhi au Mola wao Mlezi Anawatakia uongofu.” (72:10).

Na hivyo ndiyo alivyosema Ibraahim عليه السلام:

وَإِذَا مَرَضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ ﴿٧٠﴾

“Na ninapougua ni Yeye Ndiye Anayeniponesha.”

Yaani, ninapokuwa mgonjwa, hakuna hata mmoja anayeweza kuniponya isipokuwa Yeye. Naye Ananiponya kwa njia ambayo itanifanya nipone kabisa.

وَالَّذِي يُمِيتُنِي ثُمَّ يُحْيِينِ ﴿٧١﴾

“Na Ambaye Atanifisha, na kisha Atanihuisha.”

Yeye Ndiye Mwenye Kuhuisha na Kufisha, hakuna anayeweza shughuli hiyo ila Yeye, kwani Yeye Ndiye Mwenye Kuuanzisha uhai na Kuurudisha tena.

وَالَّذِي أَطْمَعُ أَنْ يَغْفِرَ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ الدِّينِ ﴿٧٢﴾

“Na Ambaye Ndiye ninayemtumai Kunisamehe makosa yangu Siku ya Malipo.”

Hakuna mwenye uwezo wa kusamehe dhambi hapa duniani na Akhera isipokuwa Yeye. Na ni nani anayesamehe madhambi ila Allah تعالى, Naye ni Mwenye Kufanya Atakalo.

رَبِّ هَبْ لِي حُكْمًا وَالْحَقْنَ بِالصَّالِحِينَ ﴿٧٣﴾ وَأَجْعَلْ لِي لِسَانَ صِدْقٍ فِي

الْآخِرِينَ ﴿٧٤﴾ وَأَجْعَلْ لِي مِنْ وَرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيمِ ﴿٧٥﴾ وَأَغْفِرْ لِأَيِّبَاتِي إِنَّهُمْ كَانُوا مِنَ الضَّالِّينَ

﴿٧٦﴾ وَلَا تُخْزِنِي يَوْمَ يُبْعَثُونَ ﴿٧٧﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ ﴿٧٨﴾ إِلَّا مَنْ أتَى اللَّهَ

بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٧٩﴾

83. “Mola wangu Mlezi! Nitunukie hukumu na Uniunganishe na watendao mema.

84. Na Unijaalie nitajwe kwa wema na watu watakaokuja baadaye.

85. Na Unijaalie katika warithi wa Bustani za neema.

86. Na Umsamehe baba yangu, kwani hakika alikuwa miongoni mwa wapotovu.

87. Wala Usinihizi Siku watapofufuliwa.

88. Siku ambayo kwamba mali hayatofaa kitu wala wana.

89. Isipokuwa mwenye kumjia Allah na moyo safi.”

Dua ya Nabii Ibraahim عليه السلام Kwake Yeye Mwenyewe na kwa Baba Yake

Na hili ni ombi lake Ibraahim عليه السلام kwa Mola wake Mlezi ampatie *Hukm.* Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Nayo ni elimu.”¹ Na Kauli Yake:

وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ

“Uniunganishe na watendao mema”.

Nijaalie mimi pamoja na wema hapa duniani na kesho Akhera. Hii ni kama alivyosema Mtume ﷺ wakati anakata roho:

اللَّهُمَّ! فِي الرَّفِيقِ الْأَعْلَى

“Ewe Allah, niweke pamoja na walio daraja ya juu (katika Pepo).”
Alisema maneno hayo mara tatu.²

Na Kauli Yake:

وَأَجْعَلْ لِي لِسَانَ صِدْقٍ فِي الْآخِرِينَ

“Na Unijaalie nitajwe kwa wema na watu watakaokuja baadaye”.

Nifanye mimi ni mwenye kukumbukwa kwa njia nzuri baada ya kufa kwangu, nitajwe kwa wema na nichukuliwe kama ruwaza njema na kielelezo chema. Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى:

¹ Al-Baghawiy 3:390.

² Fat-h al-Baariy 7:743.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٠٨﴾ سَلَّمَ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿١٠٩﴾ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١١٠﴾

“Na Tukamuachia (sifa nzuri) kwa watu wote waliokuja baadaye. Amani kwa Ibraahim. Hivyo ndivyo Tunawalipa watendao wema.” (37:108-110).

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَجْعَلِي مِن وَّرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيمِ ﴿١١٠﴾

“Na Unijaalie katika warithi wa Bustani za neema.”

Yaani, nineemeshe hapa duniani kwa kutajwa kwa wema baada ya kuondoka kwangu, na Unijaalie ni mwenye kurithi bustani za neema kesho Akhera.

Na Kauli Yake:

وَأَغْفِرْ لِأَبِي

“Na Umsamehe baba yangu”

Hii ni kama Kauli Yake:

رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ

“Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu.” (14:41).

Lakini hili ni jambo ambalo Nabii Ibraahim عليه السلام aliliacha baadaye, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَمَا كَانَ أَسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَن مَّوْعِدَةٍ وَعَدَّهَا إِتْيَاهُ

“Wala haikuwa Ibraahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye.” Hadi:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ ﴿١١١﴾

“Hakika Ibraahim alikuwa Mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu.” (9:114).

Allah تعالى Alimkataza Ibraahim عليه السلام kumuomba babake msamaha, kama Alivyosema:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ

“Hakika nyinyi muna mfano mzuri kwa Ibraahim na wale waliokuwa pamoja naye.”

Mpaka Kauli Yake:

وَمَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ

“Wala sina uwezo wa chochote kwa ajili yako mbele ya Allah.”
(60:4)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَا تُخْزِي يَوْمَ يُبْعَثُونَ ﴿٤٧﴾

“Wala usinihizi Siku watapofufuliwa.”

Hii inamaanisha Nihifadhi na Unilinde mimi na aibu Siku watakayofufuliwa viumbe vyote, wa mwanzo na wa Mwisho. Al-Bukhaariy amepokea kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuhusu Aya hii kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ إِبْرَاهِيمَ رَأَىٰ أَبَاهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَيْهِ الْعَبْرَةُ وَالْقَرَّةُ»

“Hakika Ibraahim atamuona baba yake Siku ya Kiyama akiwa amefunikwa na vumbi na giza.”¹

Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kwamba Mtume ﷺ: amesema,

«يَلْقَىٰ إِبْرَاهِيمُ أَبَاهُ فَيَقُولُ: يَا رَبِّ إِنَّكَ وَعَدْتَنِي أَنَّكَ لَا تُخْزِي يَوْمَ يُبْعَثُونَ، فَيَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: إِنِّي حَرَمْتُ الْجَنَّةَ عَلَى الْكَافِرِينَ»

“Ibraahim atakutana na baba yake, na atasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika Uliniahidi kuwa Hutanihizi Siku ya ufufuo (wa watu). Atasema Allah: Hakika Mimi Nimeharamisha Pepo kwa makafiri.”²

¹ Fat-h al-Baariy 8:357.

² Fath al-Baariy 8:357.

Hivi ndivyo ilivyopokewa kuhusu Aya hii. Katika Hadithi Zilizonukuliwa kuhusu Manabii kwa lafudhi hii ifuatayo:

اِيْلَقَىٰ اِبْرٰهِيْمُ اَبَاهُ اَزَرَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَعَلَىٰ وَجْهِ اَزَرَ قَرَّةٌ وَغَيْرَةٌ، فَيَقُوْلُ لَهُ اِبْرٰهِيْمُ:
 لَمْ اَقُلْ لَكَ لَا تَعْصِيْنِي، فَيَقُوْلُ اَبُوهُ: فَالْتِيْمَ لَا اَعْصِيْكَ، فَيَقُوْلُ اِبْرٰهِيْمُ: يَا رَبِّ
 نَكَ وَعَدْتَنِي اَنْ لَا تُخْرِجَنِي يَوْمَ يُبْعَثُوْنَ، فَاَيُّ خِزْيٍ اَخْزَىٰ مِنْ اَبِي الْاَبْعَدِ فَيَقُوْلُ اللهُ
 تَعَالَىٰ: اِنِّي حَرَّمْتُ الْجَنَّةَ عَلٰى الْكٰفِرِيْنَ، ثُمَّ يُقَالُ: يَا اِبْرٰهِيْمُ! اِنظُرْ تَحْتَ
 جِلْبِكَ، فَيَنْظُرُ، فَاِذَا هُوَ بِدِيْعٍ مُّتَلَطِّعٍ، فَيُؤْخَذُ بِقَوَانِمِهِ فَيُلْقَىٰ فِي النَّارِ،

*"Ibraahim atakutana na baba yake, Aazar Siku ya Kiyama, na uso wake utakuwa na giza na vumbi. Ibraahim atamuuliza: "Je, Si nilikuambia usiniasi". Hapo baba yake atasema: "Leo sitakuasi". Ibrahim atasema: "Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika Umeniahidi kuwa Hutanihizi Siku ya kufufuliwa (watu). Kuna hizaya gani kuliko ya kumuona baba yako akiwa katika hali hii?" Allah Mtukufu Atasema: "Hakika Mimi Nimeharamisha Pepo kwa makafiri". Kisha ataambiwa: "Ewe Ibraahim! Tazama chini ya mguu wako". Naye atatazama, hapo atamuona baba yake akiwa amebadilishwa kuwa fisi dume akiwa amefunikwa na kinyesi, naye atashikwa kwenye miguu na kuingizwa Motoni."*¹

Na imepokewa na Abu 'Abdur-Rahmaan An-Nasaa'iy رحمه الله تعالى katika Tafsiri ya *Sunan al-Kubraa* yake².

Na Kauli Yake:

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ ﴿٦٩﴾

"Siku ambayo kwamba mali hayatofaa kitu wala wana."

Maana yake: Mali ya mtu hayatamuokoa yeye na adhabu ya Allah تعالى, hata ikiwa ni kulipa kama fidia dhahabu sawa na ardhi.

¹ *Fat-h al-Baariy* 6:445.

² An-Nasaa'iy katika *al-Kubraa* 6:422.

وَلَا بُنُونَ

“Wala wana.”

Maana yake: Hata ikiwa utatoa fidia kwa watu wote wa ulimwengu huu. Siku hiyo hakuna kitu chochote kitakachomsaidia mtu isipokuwa Imani yake kwa Allah تعالی, kumtakasia Dini Yake na kujitenga na ushirikina wa watu wake. Kwa hiyo Akasema:

إِلَّا مَنْ آتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

“Isipokuwa mwenye kumjia Allah na moyo safi”.

Maana yake: Moyo umesalimika na uchafu wa ushirikina. Amesema Ibn Siriin رحمه الله تعالی: “Moyo msafi unajua Allah تعالی ni Haki, Kiyama kitakuja pasi na shaka yoyote na kuwa Allah تعالی Atawafufua walio katika makaburi yao.”¹ Amesema Said ibn Al-Musayyib: “Moyo msafi ni ule moyo ulio sahihi na sawa.”² Huu ni moyo wa Muumini, kwani moyo wa kafiri na mnafikiki una maradhi. Allah تعالی Amesema:

فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ

“Nyoyoni mwao muna maradhi.” (2:10).

Amesema Abu ‘Uthmaan Al-Naysaaburiy رحمه الله تعالی: “Huo ni moyo ulio mbali na kusalimika na uzushi (Bid’ah), moyo uliotulia katika Sunnah.”

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:366.

² Al-Baghawiy 3:390.

وَأُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٩٠﴾ وَبُرِزَتِ الْجَحِيمُ لِلْغَاوِينَ ﴿٩١﴾
 وَقِيلَ لَهُمْ آئِنَ مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٩٢﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ هَلْ
 يَنْصُرُونَكُمْ أَوْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٩٣﴾ فَكَبَّكُوا فِيهَا هُمْ وَالْغَاوُونَ
 ﴿٩٤﴾ وَجُنُودٌ إِبْلِيسَ أَجْمَعُونَ ﴿٩٥﴾ قَالُوا وَهُمْ فِيهَا
 يَخْتَصِمُونَ ﴿٩٦﴾ تَاللَّهِ إِنْ كُنَّا لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٩٧﴾ إِذْ
 نُسَوِّكُمْ بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٩٨﴾ وَمَا أَضَلَّنَا إِلَّا الْمُجْرِمُونَ
 ﴿٩٩﴾ فَمَا لَنَا مِنْ شَافِعِينَ ﴿١٠٠﴾ وَلَا صَدِيقٍ حَمِيمٍ ﴿١٠١﴾
 فَلَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةٌ فَنَتُخَدَّ مِنْ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٢﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ
 الرَّحِيمُ ﴿١٠٤﴾ كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوحٍ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٠٥﴾ إِذْ قَالَ
 لَهُمْ أَخُوهُمْ نُوحٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٠٦﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ
 ﴿١٠٧﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرًا ﴿١٠٨﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ
 أَجْرٍ ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠٩﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ
 وَأَطِيعُوا أَمْرًا ﴿١١٠﴾ * قَالُوا أَنْتُمْ مِنْ لَدُنْكُمْ أَنْتُمْ كَذِبُونَ ﴿١١١﴾
 قَالِ وَمَا عَلَّمِي مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٢﴾ إِنْ حِسَابُهُمْ
 إِلَّا عَلَى رَبِّي لَوْ تَشْعُرُونَ ﴿١١٣﴾ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الْمُؤْمِنِينَ
 ﴿١١٤﴾ إِنْ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُبِينٌ ﴿١١٥﴾

وَأُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٩٠﴾ وَبُرِزَتِ
 الْجَحِيمُ لِلْغَاوِينَ ﴿٩١﴾ وَقِيلَ لَهُمْ آئِنَ
 مَا كُنْتُمْ تَعْبُدُونَ ﴿٩٢﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ
 هَلْ يَنْصُرُونَكُمْ أَوْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٩٣﴾
 فَكَبَّكُوا فِيهَا هُمْ وَالْغَاوُونَ ﴿٩٤﴾
 وَجُنُودٌ إِبْلِيسَ أَجْمَعُونَ ﴿٩٥﴾ قَالُوا
 وَهُمْ فِيهَا يَخْتَصِمُونَ ﴿٩٦﴾ تَاللَّهِ إِنْ
 كُنَّا لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٩٧﴾ إِذْ
 نُسَوِّكُمْ بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٩٨﴾ وَمَا
 أَضَلَّنَا إِلَّا الْمُجْرِمُونَ ﴿٩٩﴾ فَمَا لَنَا
 مِنْ شَافِعِينَ ﴿١٠٠﴾ وَلَا صَدِيقٍ حَمِيمٍ
 ﴿١٠١﴾ فَلَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةٌ فَنَتُخَدَّ مِنْ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٢﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۖ
 وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾
 وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٠٤﴾

90. "Na Pepo itasogezwa kwa wachamungu.

91. Na Jahanamu itadhihirishwa kwa wapotovu.

92. Na wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu.

93. Badala ya Allah? Je! Wanakusaidieni, au wanajisaidia wenyewe?

94. *Basi watavurumizwa humo wao na hao wakosefu.*
95. *Na majeshi ya Ibilisi yote.*
96. *Watasema, na hali ya kuwa wanazozana humo:*
97. *Wallahi: Kwa yakini tulikuwa katika upotovu uliodhaahiri,*
98. *Tulipokufanyeni ni sawa na Mola Mlezi wa ulimwengu wote.*
99. *Na hawakutupoteza ila wale wakosefu.*
100. *Basi hatuna waombezi.*
101. *Wala rafiki wa dhati.*
102. *Laiti tungelipata kurejea tena tungelikuwa katika Waumini.*
103. *Hakika katika haya ipo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini.*
104. *Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.*

Wachamungu na Wapotovu Siku ya Kiyama na Mjadala wa Wapotovu na Kuhiliki Kwao

Allah تعالیٰ Anasema:

وَأَزَلَفْتِ الْجَنَّةَ

“Na Pepo itasogezwa”.

Hii ina maana kuwa italetwa karibu kwa watu wake, ikiwa imepambwa na kurembeshwa kwa wenye kutazama. Watu wake watakuwa ni wale wachamungu ambao walitia hima kwa kuacha vyote vya dunia na kutenda kwa ajili ya akhera hapa duniani.

Allah تعالیٰ Anaendelea Kusema:

وَبُرَزَّتِ الْجَحِيمُ لِلْغَاوِينَ

“Na Jahanamu itadhihirishwa kwa wapotovu”.

Maana yake: Wataoneshwa wao, na hapo shingo zitadhihiri huku ikipiga kite na kushusha pumzi (kwa majonzi), na mioyo yao itafika kooni. Wataambiwa watu wake kwa njia ya kusuta, kukemea na kukaripia:

﴿١٧﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ هَلْ يَنْصُرُونَكُمْ أَوْ يَنْتَصِرُونَ ﴿١٨﴾

“Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu. Badala ya Allah? Je! Wanakusaidieni, au wanajisaidia wenyewe?”

Maana yake: ile miungu na masanamu mliyokuwa mukiyaabudu badala ya Allah تعالى, haitaweza kuwasaidia nyinyi leo, na hata haiwezi kuwasaidia wala kuwatetea. Hakika siku ya leo, nyinyi na wao mutakuwa kuni na mafuta ya Moto, ambao bila shaka mtaungua. Na Kauli Yake:

﴿١٩﴾ فَكَيْبُوا فِيهَا هُمْ وَالْغَاوُونَ ﴿٢٠﴾

“Basi watavurumizwa humo wao na hao wakosefu.”

Amesema Mujaahid: “Hii inamaanisha watavurumishwa ndani yake.”¹ Wakasema wengineo: “Watavurumishwa ndani yake kwa nyuso zao.” Na Kaaf ni ya kurudia na kukariri, kusudio la Aya ni kwamba makundi kwa makundi miongoni mwa makafiri na viongozi wao ambao waliwaita na kuwalingania katika ushirikina.

﴿٢١﴾ وَجُنُودَ إبْلِيسَ أَجْمَعُونَ ﴿٢٢﴾

“Na majeshi ya Ibilisi yote.”

Wote watarushwa ndani ya Moto huo mpaka yule wa mwisho wao. Na Akaendelea:

﴿٢٣﴾ قَالُوا وَهُمْ فِيهَا يَخْتَصِمُونَ ﴿٢٤﴾ تَاللَّهِ إِنْ كُنَّا لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٥﴾ إِذْ نَسَوْنَكَ بَرِّتِ

﴿٢٦﴾ الْعَالَمِينَ ﴿٢٧﴾

“Watasema, na hali ya kuwa wanazozana humo: Wallahi: Kwa yakini tulikuwa katika upotovu uliodhaahiri. Tulipokufanyeni ni sawa na Mola Mlezi wa ulimwengu wote”.

¹ Atw-Twabariy 19:367.

Watasema wale wanyonge kati yao kuwaambia viongozi wao waliotakabari: “Hakika tulikuwa tunawafuata nyinyi; je, nyinyi mtasaidia kwa lolote kutoka kwenye Moto?” Watasema baada ya kutambua kuwa wao ndio wa kulaumiwa:

تَاللّٰهِ اِنْ كُنَّا لَفِي ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٧٧﴾ اِذْ نُسَوِّكُمْ بِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٧٨﴾

“Wallahi: Kwa yakini tulikuwa katika upotovu ulio dhahiri. Tulipokufanyeni ni sawa na Mola Mlezi wa ulimwengu wote.”

Tulikuwa tunatii amri zenu kama zinazotiiwa Amri za Mola Mlezi wa walimwengu wote, na tuliwaabudu nyinyi pamoja na Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

وَمَا اَضَلَّنَا اِلَّا الْجٰهِنُمُوْنَ ﴿٧٩﴾

“Na hawakutupoteza ila wale wakosefu”.

Hakika hawakutuita katika hilo isipokuwa wahalifu wenye kufanya madhambi. Hivyo:

فَمَا لَنَا مِنْ شٰفِعِيْنَ ﴿٨٠﴾

“Basi hatuna mwombezi”.

Kama watakavyosema:

فَهَلْ لَنَا مِنْ شٰفِعَآءَ فَيَشْفَعُوْا لَنَا اَوْ نُرَدُّ فَنَعْمَلْ غَيْرَ الَّذِيْ كُنَّا نَعْمَلُ

“Je, tunao waombezi ili watuombee? Au turudishwe tufanye yasiyokuwa yale tuliyokuwa tukifanya?” (7:53).

Hivyo ndivyo walivyosema:

فَمَا لَنَا مِنْ شٰفِعِيْنَ ﴿٨١﴾ وَلَا صٰدِقِيْنَ حَمِيْمٍ ﴿٨٢﴾

“Basi hatuna waombezi. Wala rafiki wa dhati.”

Maana yake: Wa karibu.

Na Kauli Yake:

فَلَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٧﴾

“Laiti tungelipata kurejea tena tungelikuwa katika Waumini.”

Hiyo ni kuwa wao watatamani kurudi tena katika hii dunia ili wafanye amali kwa kumtii Mola wao Mlezi kama wanavyodai. Hakika ni kuwa Allah تعالى Anajua ya kwamba lau watarudishwa tena hapa duniani watarudia yale waliyokatazwa, na hakika wao ni waongo. Allah تعالى Ametueleza katika Sura Swaad kuhusu vipi watu wa Motoni watajadiliana wao kwa wao:

إِنَّ ذَلِكَ لَحَقٌّ تَخَاصُمُ أَهْلِ النَّارِ ﴿٣٨﴾

“Bila shaka haya ya kuhasimiana watu wa Motoni – ni kweli.”
(38: 64).

Kisha Akasema Aliyetukuka:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٣٩﴾

“Hakika katika haya ipo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini.”

Hakika katika mzosano baina ya Ibraahim عليه السلام na watu wake, na kuwatolea hoja ya Tawhiid ni Ishara. Yaani dalili ya wazi kuwa hapana anayepaswa kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالى.

وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٤٠﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْرِضُ الرَّحِيمِ ﴿٤١﴾

“Lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini. Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu.”

كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوحٍ الْمُرْسَلِينَ ﴿٤٢﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ نُوحٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿٤٣﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ

أَمِينٌ ﴿٤٤﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرَهُ ﴿٤٥﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى رَبِّ

الْعَالَمِينَ ﴿٤٦﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرَهُ ﴿٤٧﴾

105. “Kaumu ya Nuuh waliwakadhibisha Mitume.

106. Alipowaambia ndugu yao, Nuuh: Je! Hamchimungu?

107. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.

108. Basi Mcheni Allah, na nitiini mimi.

109. Na sikutakini juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

110. Basi Mcheni Allah, na nitiini mimi”.

Waadhi wa Nuuh عليه السلام kwa Watu Wake na Majibu Yao

Hii ni habari kutoka kwa Allah تعالى kuhusu mja na Mtume Wake, Nuuh عليه السلام, naye ni Mtume wa kwanza aliyetumwa na Allah تعالى kwa watu wa ardhi baada ya kuwa watu wameanza kuabudu masanamu na miungu mingine. Allah تعالى Alimtuma kuja kukataza hilo na kuwaonya watu kwa adhabu mbaya yenye kuumiza kutoka Kwake. Lakini walimkadhibisha watu wake na wakaendelea katika yale waliokuwa nayo miongoni mwa vitendo viovu, kwa kuabudu masanamu pamoja na Allah تعالى. Allah تعالى Aliteremsha kuwa kumkadhibisha kwao (yaani Nabii Nuuh عليه السلام) ni sawa na kuwakadhibisha Mitume wote. Kwa hiyo Akasema:

كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوحٍ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٠٧﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ نُوحٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٠٨﴾

“Kaumu ya Nuuh waliwakadhibisha Mitume. Alipowaambia ndugu yao, Nuuh: Je! Hamchimungu?”

Hili ni suala lenye maana, je hamumuogopi Allah تعالى kwa kuabudu kwenu asiye kuwa Yeye?

إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٠٩﴾

“Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.” Hakika mimi ni Mtume kwenu kutoka kwa Allah تعالى; nami ni mwaminifu katika kutekeleza Aliyonituma Allah تعالى kwayo. Hakika mimi nafikisha ujumbe kutoka kwa Mola wangu Mlezi, nami sizidishi ndani yake wala kupunguza chochote.

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرًا ﴿١١٠﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ

“Basi Mcheni Allah, na nitiini mimi. Na sikutakini juu yake ujira.” Sitaki kwenu malipo wala jaza kwa kukunasihini nyinyi, bali ninaziacha thawabu zangu kuwa akiba yangu mbele ya Allah تعالى. Hivyo, fanyeni hivi:

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا

“Basi Mcheni Allah, na nitiini mimi”.

Bila shaka iko wazi kwenu kuwa ninasema ukweli na ninatekeleza nasiha zangu na amana niliyopewa pale nilipotumwa na Allah تعالى kwenu.

* قَالُوا أَنْتُمْ لَكُمْ وَأَتَّبَعَكَ الْأَرْذَالُونَ ﴿١١١﴾ قَالَ وَمَا عَلِمِي بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٢﴾
 إِنَّ حِسَابَهُمْ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّي لَوْ كَشَعُرُونَ ﴿١١٣﴾ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٤﴾ إِنَّ أَنَا إِلَّا
 نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿١١٥﴾

111. “Wakasema: Je! Tukuamini wewe, hali wanaokufuata ni watu wa chini?”

112. Akasema: Nayajuaje waliyokuwa wakiyafanya?”

113. Hisabu yao haiko ila kwa Mola wao Mlezi, laiti mngelitambua!

114. Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini.

115. Mimi si chochote ila ni Mwonyaji wa dhahiri shahiri”.

Matakwa ya Watu wa Nuhu عليه السلام na Majibu Yake

Wakasema: “Hatutakuamini wala kukufuata na kuwa sawa na hawa madhalili miongoni mwa watu, ambao kwamba wamekufuata na kukuamini, nao ni wa chini kabisa miongoni mwetu.” Kwa hiyo:

* قَالُوا أَنْتُمْ لَكُمْ وَأَتَّبَعَكَ الْأَرْذَالُونَ ﴿١١١﴾ قَالَ وَمَا عَلِمِي بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٢﴾

“Wakasema: Je! Tukuamini wewe, hali wanaokufuata ni watu wa chini? Akasema: Nayajuaje waliyokuwa wakiyafanya?”

Hii ina maana kuwa; ni kitu gani kinachonilazimisha mimi ikiwa watanifuata? Hata ikiwa walikuwa wakifanya mambo kabla, hainilazimu mimi kuwaangalia, kuwachunguza na kuhakiki asili zao. Hakika ninayotakiwa mimi ni kuwakubalia

ikiwa wataniamini; yale yaliyomo ndani ya nyoyo zao namuachia Allah تعالى. Hakika ni kuwa:

﴿٢٦﴾ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٧﴾ إِنَّ حِسَابَهُمْ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّي لَو تَشْعُرُونَ ﴿٢٨﴾

***“Hisabu yao haiko ila kwa Mola wao Mlezi, laiti mngelitambua!
Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini”.***

Inaonekana kama kwamba walimtaka awafukuze watu hao, kisha ndio watamfuata, lakini yeye alikataa hilo katakata. Na akasema:

﴿٢٩﴾ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٠﴾ إِنَّ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٣١﴾

***“Wala mimi si wa kuwafukuza Waumini. Mimi si chochote ila ni
Mwonyaji wa dhahiri shahiri.”***

Hakika ni kuwa mimi ni mwonyaji, hivyo atakayenitii, na kunifuata na kunisadiki kwa kuniamini, atakuwa pamoja nami, na mimi nitakuwa pamoja naye, sawa akiwa mtukufu au mtu wa kawaida, wa tabaka la juu au tabaka duni.

* * *

قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ يَنْتُوحَ لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمَرْجُومِينَ ﴿١١٦﴾
 قَالَ رَبِّ إِنِّ قَوْمِي كَذَّبُونِ ﴿١١٧﴾ فَأَفْتَحَ بَيْنِي وَبَيْنَهُمْ فَتَحًا
 وَبَجَّيْتُ وَمَنْ مَعِيَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَمَنْ
 مَعَهُ فِي الْفَلَكَ الْمَشْحُونِ ﴿١١٩﴾ ثُمَّ أَعْرَفْنَا بَعْدَ الْبَاقِينَ
 ﴿١٢٠﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۗ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ
 ﴿١٢١﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٢﴾ كَذَّبَتْ عَادُ
 الْمُرْسَلِينَ ﴿١٢٣﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ هُودٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٢٤﴾
 إِنِّي لَكُرْسُولُ آمِينٌ ﴿١٢٥﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ﴿١٢٦﴾ وَمَا
 أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۗ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّ الْعَالَمِينَ
 ﴿١٢٧﴾ أَتَبْنُونَ بِكُلِّ رِيعٍ ءَايَةً تَعْبَثُونَ ﴿١٢٨﴾ وَتَتَّخِذُونَ
 مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ﴿١٢٩﴾ وَإِذَا بَطَشْتُمْ بَطَشْتُمْ
 جَبَّارِينَ ﴿١٣٠﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ﴿١٣١﴾ وَاتَّقُوا الَّذِي
 أَمَدَّكُمْ بِمَا تَعْلَمُونَ ﴿١٣٢﴾ أَمَدَّكُمْ بِأَنْعَمٍ وَبَنِينَ ﴿١٣٣﴾
 وَجَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿١٣٤﴾ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ
 عَظِيمٍ ﴿١٣٥﴾ قَالُوا سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَوَعَظْتَ أَمْ لَمْ تَكُنْ مِنَ
 الْوَاعِظِينَ ﴿١٣٦﴾ إِنَّ هَذَا إِلَّا خُلُقُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٣٧﴾ وَمَا
 نَحْنُ بِمُعَدِّينَ ﴿١٣٨﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَهْلَكْنَاهُمْ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَةً ۗ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٣٩﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ
 الرَّحِيمُ ﴿١٤٠﴾

قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ يَنْتُوحَ لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمَرْجُومِينَ ﴿١١٦﴾
 قَالَ رَبِّ إِنِّ قَوْمِي كَذَّبُونِ ﴿١١٧﴾ فَأَفْتَحَ بَيْنِي
 وَبَيْنَهُمْ فَتَحًا وَبَجَّيْتُ وَمَنْ مَعِيَ مِنَ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَمَنْ مَعَهُ
 فِي الْفَلَكَ الْمَشْحُونِ ﴿١١٩﴾ ثُمَّ
 أَعْرَفْنَا بَعْدَ الْبَاقِينَ ﴿١٢٠﴾ إِنَّ فِي
 ذَلِكَ لَآيَةً ۗ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ
 مُؤْمِنِينَ ﴿١٢١﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ
 الرَّحِيمُ ﴿١٢٢﴾

116. "Wakasema: Ikiwa huachi, ewe Nuuu, bila ya shaka utapigwa mawe.

117. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha.

118. Basi hukumu baina yangu na wao kwa hukumu yako, au uniokoe mimi na walio pamoja nami, Wau-mini.

119. Kwa hivyo Tuka muokoa yeye na walio-kuwa pamoja naye katika marikebu iliyosheheni.

120. Kisha Tukawazamisha baadaye waliobakia.

121. Hakika katika haya ipo Ishara, lakini si wengi wao waliokuwa Waumini.

122. Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Yeye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.

Vitisho vya Kaumu Yake, Dua ya Nuuh عليه السلام Dhidi Yao na Kuangamizwa Kwao

Nabii wa Allah تعالى alikaa baina ya watu wake kwa kipindi kirefu akiwaita katika njia ya Allah تعالى usiku na mchana, kwa siri na kwa dhahiri. Kila alipokuwa akikariri mwito wake huo, ndivyo walivyozidi kujikita katika ukafiri uliopindukia na kuupinga mwito wake kwa ukali. Mwisho kabisa wakasema:

قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ يَنْوُحْ لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمَرْجُومِينَ ﴿١١٦﴾

“Ikiwa huachi, ewe Nuuh, bila ya shaka utapigwa mawe.”

Hii ina maana kuwa lau hutaacha ulinganizi wako huo wa kutuita sisi katika Dini yako, basi:

لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمَرْجُومِينَ ﴿١١٧﴾

“Bila ya shaka utapigwa mawe.”

Maana yake: Tutakupiga mawe. Hapo Nabii Nuuh عليه السلام aliomba dua dhidi yao, dua iliyojibiwa moja kwa moja na Allah تعالى. Akasema:

قَالَ رَبِّ إِنَّ قَوْمِي كَذَّبُونِ ﴿١١٨﴾ فَأَفْتَحَ بَيْنِي وَبَيْنَهُمْ فَتَحًا

“Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha. Basi hukumu baina yangu na wao kwa Hukumu Yako.”

Kama Alivyosema katika Aya nyingine:

فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَأَنْتَصِرْ ﴿١١٩﴾

“Ndipo akamuomba Mola wake Mlezi (akasema): “Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru.” (54:: 10).

Hadi Mwisho wa Aya. Na hapa Anasema Aliyetukuka:

فَأَنْجَيْنَاهُ وَمَنْ مَعَهُ فِي الْفَلَكَ الْمَشْحُونِ ﴿١١٦﴾ ثُمَّ أَغْرَقْنَا بَعْدَ الْبَاقِينَ ﴿١١٧﴾

“Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye katika marikebu iliyosheheni. Kisha Tukawazamisha baadaye waliobakia.”

Na *“Mash-huun – Marikebu iliyosheheni”* Ni ile iliyojaa pomoni kwa mizigo na jozi ya kila aina ya viumbe, dume na jike, waliobebwa ndani yake. Hii ina maana, Tulimuokoa Nuuh عليه السلام pamoja na wote waliomfuata, na Tukawazamisha waliomkanusha na kwenda kinyume na amri zake, wote kwa pamoja bila ya kubaki yeyote miongoni mwao. Allah تعالى Anasema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١١٩﴾

“Hakika katika haya ipo Ishara, lakini si wengi wao waliokuwa Waumini. Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Yeye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.

كَذَّبَتْ عَادَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٢٠﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ هُودٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٢١﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٢٢﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرًا ﴿١٢٣﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٢٤﴾ أَتَبْنُونَ بِكُلِّ رِيعٍ آيَةً تَعْبَثُونَ ﴿١٢٥﴾ وَتَتَّخِذُونَ مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ﴿١٢٦﴾ وَإِذَا بَطَشْتُمْ بَطَشْتُمْ جَبَّارِينَ ﴿١٢٧﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرًا ﴿١٢٨﴾ وَاتَّقُوا الَّذِي أَلْذِي أَمَدُّكُمْ ﴿١٢٩﴾ بِمَا تَعْلَمُونَ ﴿١٣٠﴾ أَمَدُّكُمْ بِأَنْعَمِ وَبَيْنَ ﴿١٣١﴾ وَجَنَّتٍ وَعُيُونٍ ﴿١٣٢﴾ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٣٣﴾

123. *“Kina ‘Aad waliwakanusha Mitume.*

124. *Alipowaambia ndugu yao, Huud: Je! Hamchimungu?*

125. *Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.*

126. *Basi Mcheni Allah, na nitiini mimi.*

127. *Na sikutakeni juu yake ujira, kwani ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.*

128. Je! Mnajenga juu ya kila mnyanyuko kumbusho la kufanyia upuuzi?

129. Na mnajenga majengo ya fakhari kama kwamba mtaishi milele!

130. Na mnapotumia nguvu, mnatumia nguvu kwa ujabari.

131. Basi mcheni Allah na nitiini mimi.

132. Na mcheni Aliyekupeni haya mnayoyajua.

133. Amekupeni wanyama wa kufuga na wana.

134. Na bustani na chemchem.

135. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Kubwa.”

Ulinganiaji wa Huud kwa Kaumu Yake

Hii ni habari kutoka kwa Allah ﷻ kuhusu mja na Mtume Wake, Huud عليه السلام, kuwa yeye aliilingania kaumu yake ya ‘Aad’ Kaumu yake hiyo ilikuwa ikiishi katika sehemu ya *Ahqaaf*, ambayo ilikuwa ni milima ya mchanga iliyochongwa karibu na Hadhramawt, iliyopakana na nchi ya Yemen. Wao waliishi baada ya zama za Nuuh عليه السلام, kama Allah ﷻ Alivyosema katika Suratul *A'raaf*:

وَأَذْكُرُوا إِذْ جَعَلْنَاكُمْ خُلَفَاءَ مِنْ بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادَكُمْ فِي الْخَلْقِ بَضْطَةً

“Na kumbukeni Alivyokufanyeni mshike pahala pa kaumu ya Nuuh, na Akakuzidishieni katika umbo.” (7:69).

Hivyo ni kuwa walikuwa ni watu wenye nguvu, waliojazia miili, washari na wakali, warefu sana; na walikuwa wameneemeshwa na riziki, mali, bustani, mito, wana, kilimo cha mimea na matunda. Pamoja na hayo yote walikuwa wakiabudu asiyekuwa Allah ﷻ. Hivyo, Allah ﷻ Alimtuma kwao Huud عليه السلام, mmoja wao, kama Mtume ﷺ anayeleta bishara njema na kuwaonya. Aliwalingania wao wamuabudu Allah ﷻ Peke Yake na kuwatahadharisha na Adhabu na Ghadhabu Yake ikiwa watamhalifu yeye na kumtolea ukali. Akawaambia kama alivyosema Nuuh عليه السلام kwa kaumu yake:

أَتَبْتُونُ بِكُلِّ رِيْعٍ ءَايَةً تَعْبَثُونَ ﴿١١٦﴾

“Je! Mnajenga juu ya kila mnyanyuko kumbusho la kufanyia upuuzi?”

Wametofautiana wanazuoni wa Tafsiri kuhusu maana ya neno *Rii'* lakini kwa muhtasari wamesema kuwa hiyo ni sehemu ya mnyanyuko katika njia panda maarufu, ambapo wanajenga huko majumba makubwa makubwa, yanayopendeza na imara. Na kwa hiyo akasema:

أَتَبْتُونُ بِكُلِّ رِيْعٍ ءَايَةً

“Je! Mnajenga juu ya kila mnyanyuko kumbusho?”

Maana yake: Kama majengo mashuhuri yanayojulikana.

تَعْبَثُونَ ﴿١١٧﴾

“La kufanyia upuuzi tu?”

Hii ina maana kuwa hakika nyinyi mnafanya hayo kwa mchezo na upuuzi wala sio kuwa mnayahitaji, bali ni kwa mchezo, upuuzi na kuonesha nguvu zenu. Hivyo basi Mtume wao aliwakataza kufanya hilo, kwani huko ni kupoteza wakati na kuchosha miili bila ya kupata faida yoyote. Hilo linawashughulisha wao kwa jambo ambalo halitawasaidia hapa duniani wala kesho Akhera. Kwa hiyo akasema:

وَتَتَّخِذُونَ مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ﴿١١٨﴾

“Na mnajenga majengo ya fakhari kama kwamba mtaishi milele!”

Amesema Mujaahid: “*Na Maswaani*” Ina maana ya ngome imara, zenye nguvu na ndefu ambazo zinajengwa ili zidumu.” Na maana ya Kauli Yake:

لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ﴿١١٩﴾

“... kama kwamba mtaishi milele!”

Maana yake: Muweze kuishi ndani yake milele na jambo hilo haliwezekani bali zitawa waondokea kutoka kwenu, kama zilivyotoweka kwa wale waliokuwa kabla yenu.

Na Kauli Yake:

وَإِذَا بَطَشْتُمْ بَطَشْتُمْ جَبَّارِينَ ﴿١١٦﴾

“Na mnapotumia nguvu, mnatumia nguvu kwa ujabari”.

Hapa wanasifiwa kwa kuwa na nguvu, ukali, ukatili na ujabari. Hivyo wanaambiwa:

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ﴿١١٧﴾

“Basi mcheni Allah na nitiini”

Maana yake: Muabuduni Mola wenu Mlezi na mtiini Mtume wenu. Kisha akaanza kuwakumbusha neema ambazo Allah تعالی Amewaneemesha nazo, akasema:

وَاتَّقُوا الَّذِي أَمَدَّكُمْ بِمَا تَعْلَمُونَ ﴿١١٧﴾ أَمَدَّكُمْ بِأَنْعَامٍ وَبَيْنَ ﴿١١٨﴾ وَجَنَّتِ وَعْيُونَ ﴿١١٩﴾
إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٢٠﴾

“Na mcheni Aliyekupeni haya mnayoyajua. Amekupeni wanyama wa kufuga na wana. Na bustani na chemchem. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Kubwa.” (26:132-135)

Hii inamaanisha ikiwa mtamkanusha na kumpinga (Mtume wenu). Akawalingania warudi kwa Allah تعالی kwa kuwahimiza na kuwahofisha, lakini hayakufalia kitu.

قَالُوا سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَوَعَظْتَ أَمْ لَمْ تَكُنْ مِنَ الْوَاعِظِينَ ﴿١٣٦﴾ إِنَّ هَذَا إِلَّا خُلُقُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٣٧﴾
﴿١٣٨﴾ وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ ﴿١٣٩﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَهْلَكْنَاهُمْ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ
﴿١٤٠﴾ مُؤْمِنِينَ ﴿١٤١﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٤٢﴾

136. “Wakasema: Ni mamoya kwetu, ukitupa mawaidha au hukuwa miongoni mwa watoao mawaidha.

137. Haya si chochote ila ni mtindo wa watu wa tokea zamani.

138. Wala sisi hatutaadhibiwa.

139. Wakamkanusha; Nasi Tukawaangamiza. Hakika bila ya shaka katika haya ipo Ishara. Lakini hawakuwa wengi wao wenye kuamini.

140. Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.

Jawabu ya Kaumu ya Huud عليه السلام na Adhabu Yao

Anatupasha habari Allah تعالى kwa jawabu lililotolewa na kaumu ya Huud baada ya kuwatahadharisha na kuwaonya, kuwahimiza na kuwahofisha, na kuwabainishia haki kwa uwazi kabisa.

قَالُوا سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَوَعَضْتَ أَمْ لَمْ تَكُنْ مِنَ الْوَاعِظِينَ ﴿١٣٩﴾

“Wakasema: Ni mamoja kwetu, ukitupa mawaidha au hukuwa miongoni mwa watoao mawaidha.”

Maana yake: Sisi hatuwezi kujirudi kwa yale tulio nayo. Allah تعالى Anatueleza katika Aya nyingine:

وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِي آلِهَتِنَا عَنْ قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٤٠﴾

“Wala sisi hatuiachi miungu yetu kwa kufuata kauli yako. Na wala sisi hatukuamini wewe.” (11:53).

Hivi ndivyo ilivyokuwa, hakika Allah تعالى Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢﴾

“Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawaamini.” (2:6).

Na Akasema:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٩٦﴾

“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini.” (10:96).

Wakasema:

﴿١٧﴾ إِنَّ هَذَا إِلَّا خُلُقُ الْأَوَّلِينَ

“Haya si chochote ila ni mtindo wa watu wa tokea zamani.”

Baadhi ya wanazuoni wanaoisoma Aya hii: *Khalq* (baada ya *Khuluqu*) kwa *Kha* ambayo imetiwa *Fat-hah* na *Saknah* katika *Laam*. Kulingana na maoni ya Ibn Mas’uud, Ibn ‘Abbaas, Al-‘Awfiy, ‘Alqamah na Mujaahid, wanamaanisha: “Uliyokuja nayo kwetu sisi si chochote si lolote, isipokuwa ni ngano (*Akhlaq*) za watu wa kale.”¹ Maneno haya ni sawa na yale waliyosema Washirikina wa Ki-Quraysh:

﴿١٨﴾ وَقَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا

“Na wakasema: “Ni visa vya watu wa zamani alivyoviandikisha (Muhammad), anavyosomewa asubuhi na jioni.” (25:5).

Na Akasema:

﴿١٩﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ هَذَا إِلَّا إِفْكُ افْتَرَاهُ وَأَعَانَهُ عَلَيْهِ قَوْمٌ ءَاخَرُونَ ۗ فَقَدْ جَاءُوا ظُلْمًا وَزُورًا ﴿٢٠﴾ وَقَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ

“Na wakasema wale waliokufuru: “Hayakuwa haya (aliyokuja nayo Muhammad) ila ni uzushi aliozua na wanamsaidia juu yake watu wengine.” Basi wameleta dhulma na uongo. Na wakasema: “Ni visa vya watu wa zamani.” (25:4-5).

Na Akasema tena:

﴿٢١﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ مَآذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ قَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٢﴾

“Na wanapoambiwa: Kateremsha nini Mola wenu Mlezi? Husema: Hadithi za kubuni za watu wa kale.” (16:24).

Na wanazuoni wengine wamesoma Neno “*Khuluq* kwa *Kha* na *Laam*” zikiwa na Dhummah, ambayo inamaanisha Dini yao. Hivyo, yale wanayoyafanya ni

¹ Atw-Twabariy 19:378.

katika dini ya mababa na mababu zao wa mwanzo, kama kwamba wanasema: "Sisi tunawafuata wao, tutaishi kama walivyoishi na kufa kama walivyokufa, na hakutakuwa na ufufuo, wala hukumu na wala malipo." Kwa hiyo wakasema:

وَمَا نَحْنُ بِمُعَذِّبِينَ ﴿١١٦﴾

"Wala sisi hatutaadhibiwa."

Na Kauli Yake Mtukufu:

فَكَذَّبُوهُ فَأَهْلَكْنَاهُمْ

"Wakamkanusha; Nasi Tukawaangamiza."

Maana yake: Waliendelea kumkadhibisha Nabii wa Allah, Huud عليه السلام, kwenda kinyume naye na kumfanyia inadi. Hapo Allah تعالى Aliwahiliki. Hakika imebainishwa sababu ya wao kuangamizwa katika sehemu kadhaa ndani ya Qur'ani: Allah تعالى Aliwapelekea upepo mkali usiozuilika. Yaani, upepo unaovuma kwa nguvu mno na wenye baridi kali. Hivyo, sababu ya kuhilikishwa ilifaa kwa maumbile yao, kwani wao walikuwa ni wenye nguvu na majabari miongoni mwa watu, kwa hiyo Allah تعالى Naye Akawashinda kwa Kutumia kilicho na nguvu na ukali zaidi kuliko wao. Kama Alivyosema Allah تعالى:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦٧﴾ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٦٨﴾

"Je! Hukuona jinsi Mola wako Mlezi Alivyowafanya 'Aad (Iraam). Iram waliokuwa wana majumba marefu marefu." (89:6-7).

Nao ni 'Aad wa mwanzo. Hiyo ni kama Alivyosema:

وَأَنْتُمْ أَهْلَكَ عَادًا الْأُولَىٰ ﴿٥٠﴾

"Na kwamba Yeye Ndiye Aliyewaangamiza 'Aad wa kwanza." (53: 50).

Nao walitokana na kizazi cha Iram ibn Saam ibn Nuuh عليه السلام.

إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧٠﴾

"Waliokuwa wana majumba marefu marefu." (89:7).

Ambao kwamba walikuwa wakikaa kwenye nguzo. Wale wanaodai kuwa Iram ulikuwa ni Mji, hakika wao wamechukua katika riwaya za *Israa'iliyyaat* (za wana wa Israili) kutokana na maneno ya Ka'b na Wahb, wala hakuna msingi wa kweli kwa hilo. Akasema Aliyetukuka:

الَّتِي لَمْ تُخْلَقْ مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ ﴿٨٩﴾

“Ambao hawakuumba mfano wao katika miji (mingine).” (89:8).

Hii ina maana kuwa hakujaumbwa mfano wa kabila hilo kwa nguvu walizokuwa nazo, ukali, ukatili wao, lau lengo lingekuwa ni mji, pangesemwa: “Ambao haujajengwa mfano wake katika ardhi.” Na Akasema Aliyetukuka:

فَأَمَّا عَادٌ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ
الَّذِي خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَكَانُوا بِقَائِلَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٩٠﴾

“Basi ‘Aad walitakabari katika ardhi bila ya haki na hawakuona ya kwamba Allah Aliyewaumba wao ni Mwenye Nguvu zaidi kuliko wao? Wakawa wanazikanusha Ishara Zetu.” (41:15).

Akasema Aliyetukuka:

وَأَمَّا عَادٌ فَأَهْلِكُوا بِرِيحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ﴿٩١﴾

“Na ama ‘Aad waliangamizwa kwa upepo mkali usiozuilika.”

Mpaka katika Kauli Yake:

حُسُومًا

“Moja kwa moja bila kusita.” (69:6-7).

Maana yake: Mfululizo kwa ukamilifu (siku saba na mchana minane). Hapo,

فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعِجَازٌ نَحْلٍ حَاقِيَةٍ ﴿٩٢﴾

“Utaona watu wameanguka kifudifudi kama kwamba ni magogo ya mitende, mabupu (yawazi ndani).” (69:7).

Waliachwa miili bila vichwa, kwa sababu upepo ulikuwa unakuja na kumbeba mmoja wao, baadaye kumwangusha kifudifudi, kwa njia ambayo mabongo yalikuwa yanatoka nje, kichwa kuvunjwa na kutupwa kando, kama kwamba ni mitende iliyong'olewa. Walikuwa wanajenga ngome zao katika majabali na mapango, na kuchimba mahandaki nusu ya kimo cha mtu, lakini hayo yote hayakuwasaidia kabisa dhidi ya Amri kutoka kwa Allah تعالى.

Allah تعالى Anasema:

إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ

“Hakika ijapo ajali itokayo kwa Allah haizuiliki. Laiti mngejua.”
(71:4).

Kwa hiyo akasema hapa Aliyetukuka:

فَكَذَّبُوهُ فَأَهْلَكْنَاهُمْ

“Wakamkanusha; Nasi Tukawaangamiza.”

* * *

كَذَّبَتْ ثَمُودُ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٤١﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ صَالِحٌ
 أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٤٢﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٤٣﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ
 وَأَطِيعُوا أَمْرَهُ ﴿١٤٤﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۗ إِنِ اجْتَبَيْتُمُوهُ
 فَلِيَ جُنَّةٌ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٤٥﴾ أَتَتَزَكُّونَ فِي مَا هَتَمْنَا بَيْنِينَ
 فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿١٤٦﴾ وَزُرُوعٍ وَخَلَائِصٍ فَطَعْمًا هَٰضِمًا
 وَتَنْجِيثًا مِنَ الْجِبَالِ بِيوتًا فَدَرِينًا ﴿١٤٧﴾ فَاتَّقُوا
 اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرَهُ ﴿١٤٨﴾ وَلَا تُطِيعُوا أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٤٩﴾ الَّذِينَ
 يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٠﴾ قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ
 مِنَ الْمُسْحَرِينَ ﴿١٥١﴾ مَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا فَأْتِ بَيِّنَاتٍ
 إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٥٢﴾ قَالَ هَذِهِ نَاقَةُ هَٰذَا ۖ شَرِبْ
 وَلَكُمْ شَرِبَ يَوْمٍ مَعْلُومٍ ﴿١٥٣﴾ وَلَا تَمْسُوهَا بِسُوءٍ
 فَيَأْخُذْكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٥٤﴾ فَعَقَرُوهَا فَاصْبَحُوا
 سَدِيدِينَ ﴿١٥٥﴾ فَأَخَذَهُمُ الْعَذَابُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً ۗ وَمَا
 كَانَ أَكْثَرَهُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿١٥٦﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ
 الرَّحِيمُ ﴿١٥٧﴾ كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوطٍ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٥٨﴾ إِذْ قَالَ
 لَهُمْ أَخُوهُمْ لُوطٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٥٩﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ
 ﴿١٦٠﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرَهُ ﴿١٦١﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ
 أَجْرٍ ۗ إِنِ اجْتَبَيْتُمُوهُ فَلِيَ جُنَّةٌ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾

كَذَّبَتْ ثَمُودُ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٤١﴾ إِذْ قَالَ
 لَهُمْ أَخُوهُمْ صَالِحٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٤٢﴾
 إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٤٣﴾ فَاتَّقُوا
 اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرَهُ ﴿١٤٤﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ
 عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۗ إِنِ اجْتَبَيْتُمُوهُ
 فَلِيَ جُنَّةٌ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٤٥﴾

141. "Kina Thamud waliwakanusha Mitume.

142. Alipowaambia ndugu yao Swaalih: Je! Hamumchimungu?

143. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.

144. Mcheni Allah, na nitiini.

145. Na sikutakini juu yake ujira, kwani Ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote".

Nabii Swaleh عليه السلام na Kaumu ya Thamud

Hii ni habari kutoka kwa Allah تعالى kuhusu mja na Mtume Wake, Swaleh

ambaye alipelekwa kwa kaumu yake Thamud. Kaumu yake walikuwa ni Waarabu waliokuwa wakiishi katika mji wa Hijr – ambao uko baina ya Waadi

Al-Quraa na Bilaad Ash-Shaam (Shamu kubwa). Na maskani na makazi yao ni maarufu na mashuhuri sana. Tayari tumetanguliza kutaja Hadithi zinazoelezea kupita kwa Mtume ﷺ pale alipotaka kuivamia Syria katika Suratul A'raaf. Aliwasili Tabuk, kisha akarudi Madina kujitayarisha kwa mapambano.¹ Kaumu hii ilikuja baada ya Aad, na kabla ya kuja kipenzi cha Allah تعالى, Ibrahim عليه السلام. Mtume wao, Swaleh عليه السلام aliwalingania katika njia ya Allah تعالى ili wamuabudu Yeye Peke Yake wala wasimshirikishe na chochote, na wamtii Yeye kwa kila amri iliyofikishwa kwao, lakini walikataa, wakamkadhibisha na kumpinga. Aliwaambia kuwa kwa ulinganizi wake huo hataki ujira kutoka kwao, hakika ni kuwa yeye anataka thawabu kutoka kwa Allah تعالى. Kisha akawakumbusha neema za Allah تعالى juu yao, akasema:

أَتْرَكُونَ فِي مَا هَبْنَاهَا آمِينَ ﴿١٤٦﴾ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿١٤٧﴾ وَزُرُوعٍ وَخَلِّ طَلْعُهَا هَضِيمٌ ﴿١٤٨﴾
 وَتَنْجُوتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بَيْوتًا فَرِهِينَ ﴿١٤٩﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ﴿١٥٠﴾ وَلَا تُطِيعُوا
 أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٥١﴾ الَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٢﴾

146. "Je! Mtaachwa salama salimini katika haya yaliyopo hapa?"

147. Katika bustani, na chemchem?

148. Na konde na mitende yenye makole yaliyowiva.

149. Na mnachonga milimani majumba kwa ustadi.

150. Basi mcheni Allah na nitiini mimi.

151. Wala msitii amri za waliopindukia mipaka.

152. Ambao wanafanya uufisadi katika nchi, wala hawatengenezi".

Kuwakumbusha Hali zao na Neema Walizopata

Mtume Swaleh عليه السلام anawalingania na kuwaonya jamaa zake kuhusu adhabu ya Allah تعالى ambayo inaweza kuwashukia na kuwakumbusha kuhusu neema kutoka kwa Allah تعالى Alizowapa. Hakika Amewapa riziki nyingi na Kuwajaalia amani na usalama kutokana na hatari yoyote ile. Akawapa bustani, chemchem zinazobubujika na Kuwatolea mimea na matunda. Kwa hiyo Akasema:

¹ Fat-hul Al-Bari 7:737

وَتَخَلَّى طَلْعَهَا هَضِيمٌ ﴿١٤١﴾

“Na mitende yenye makole yaliyowiva.”

Amepokea Al-'Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: “Iliyoiva na kukomaa, ndio **Hadhiim.**”¹ Amepokea 'Aliy ibn Abi Twalha kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

وَتَخَلَّى طَلْعَهَا هَضِيمٌ ﴿١٤٢﴾

“Na mitende yenye makole yaliyowiva.”

Inamaanisha kuota na kustawi sana. Amepokea Isma'il ibn Abi Khalid kutoka kwa 'Amr ibn Abi Amr ambaye amewahi kuwadiriki Maswahaba kuwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

وَتَخَلَّى طَلْعَهَا هَضِيمٌ ﴿١٤٣﴾

“Na mitende yenye makole yaliyowiva.”

Kuwa inamaanisha inapowiva na kuwa laini. Imepokewa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى, kisha akasema kuwa pia imepokewa na Abu Swaleh رحمه الله تعالى mfano wake. Na Kauli Yake:

وَتَتَّحِثُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا فَرِهِينَ ﴿١٤٤﴾

“Na mnachonga milimani majumba kwa ustadi.”

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما na wanazuoni wengine: “Kwa ujuzi na ustadi mkubwa.”¹ Kulingana na ripoti nyingine kutoka kwake amesema: “Walikuwa ni wenye tamaa na wabadhirifu.” Hii ndio rai ya Mujaahid na kundi jengine.³

Hakuna ukinzani baina ya rai mbili hizo, hakika ni kuwa wao walikuwa wakijenga nyumba zao kwa kuchonga katika milima kama aina ya michezo ya ubadhirifu, kujiona na upuuzi bila ya kuwa na haja yoyote ile kuwa hayo yawe ni makazi yao. Walikuwa stadi katika sanaa ya uwashi na kuchonga nakishi mawe, kama inavyojulikana vyema kwa yeyote aliyeona majumba yao. Kwa hiyo Akasema:

¹ At-Twabari 19:380.

² At-Twabari 19:382.

³ At-Twabari 19:383.

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۝

“Basi mcheni Allah na nitiini mimi.”

Kubalini kwa yatakayowafaidisha nyinyi hapa duniani na kesho Akhera; kwa kumuabudu Mola wenu Mlezi Aliyewaumbeni nyinyi, Aliyekuruzukuni ili mpate kumuabudu Yeye Peke Yake na mumtakase asubuhi na jioni.

وَلَا تُطِيعُوا أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ ۝ الَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ۝

“Wala msitii amri za waliopindukia mipaka. Ambao wanafanya ufisadi katika nchi, wala hawatengenezi.”

Maana yake: Viongozi wao na wakubwa wao, kuwaita wao katika Ushirikina na Ukafiri na kuipinga haki.

قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ مِنَ الْمُسَحَّرِينَ ۝ مَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا فَأْتِ بِآيَةٍ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ۝ قَالَ هَذِهِ نَاقَةٌ هَا شَرِبَتْ وَلَكُمْ شِرْبٌ يَوْمَ مَعْلُومٍ ۝ وَلَا تَمْسُوهَا بِسُوءٍ فَيَأْخُذَكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ۝ فَعَقَرُوهَا فَاصْبَحُوا تَنَدِيمِينَ ۝ فَأَخَذَهُمُ الْعَذَابُ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ۝ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ۝

153. **“Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa.**

154. **Wewe si chochote ila ni mtu kama sisi. Basi lete Ishara ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.**

155. **Akasema: Ngamia huyu jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalumu.**

156. **Wala msimguse kwa uovu, isije ikakushikeni adhabu ya Siku Kubwa.**

157. **Lakini wakamuua, na wakawa wenye kujuta.**

158. **Basi ikawapata adhabu. Hakika katika hayo ipo Ishara. Lakini hawakuwa wengi wenye kuamini.**

159. **Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.**

Jawabu la Thamud, Kutaka kwao Ishara na Kuwajia wao Adhabu

Anatupa habari hizi Aliyetukuka kuhusu Thamud kwa jawabu walizompa Nabii wao, Swaleh عليه السلام pale alipowaita wamuabudu Mola wao Mlezi Aliyetukuka. Wao:

قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ مِنَ الْمَسْحُورِينَ ﴿١٤١﴾

“Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa.”

Mujaahid na Qataadah wamesema: “Wanamaanisha kuwa ameathiriwa na uchawi.”¹ Kisha wakasema:

مَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا

“Wewe si chochote ila ni mtu kama sisi”.

Vipi wewe utaletewa Wahyi, ambapo sisi hatupati? Hii ni kama ile Aya ambayo inawaelezea wakisema:

أَفَلَيْ الذِّكْرِ عَلَيْهِ مِنْ بَيْنِنَا بَلْ هُوَ كَذَّابٌ أَشِرُّ ﴿١٤٢﴾ سَيَعْمُونَ غَدًا مِنَ الْكَذَّابِ الْأَشِرِّ ﴿١٤٣﴾

“Oh! Ameteremshiwa yeye tu ukumbusho baina yetu sote? Bali yeye ni muongo, na mwenye kujiona. Watajua kesho ni nani muongo anayejiona.” (54:25-26).

Kisha walitaka aje na Ishara ili wapate kujua kuwa aliyokuja nayo kutoka kwa Mola wao Mlezi ni kweli. Kilikusanyika kikundi na kutaka awatolee saa hiyo hiyo kutoka katika jabali ngamia jike ambaye ana mimba ya miezi kumi, na hapo wakaashiria jabali lililokuwa kati yao. Hapo Nabii wa Allah - Swaleh عليه السلام aliwafanya waahidi kuwa akitekeleza ombi lao, watamuamini na kumfuata, nao walikubali kwa hilo. Nabii wa Allah, Swaleh عليه السلام alisimama kuswali, na kumuomba Allah تعالى Awajibu ombi lao. Kisha lile jabali waliloashiria likapasuka kama walivyotaka. Hivyo, baadhi yao waliamini, lakini wengi miongoni mwao walikufuru.

قَالَ هَذِهِ نَاقَةٌ هَآءَا شَرِبْتَ وَلَكَرَّ شَرِبْتَ يَوْمَ مَعْلُومٍ ﴿١٤٤﴾

“Akasema: Ngamia huyu jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalumu.”

¹ Atw-Twabariy 19:184-185.

Hii inamaanisha ngamia huyo atakunywa kutoka kwenye vyanzo vyenu vya maji siku moja, na siku ya pili mutakunywa nyinyi.

وَلَا تَمْسُوْهَا بِسُوءٍ فَيَأْخُذْكُمْ عَذَابٌ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿١٤١﴾

“Wala msimguse kwa uovu, isije ikakushikeni adhabu ya Siku Kubwa”.

Akawatahadharisha adhabu ya kutoka kwa Allah تعالى ikiwa watamdhuru kwa njia yoyote. Ngamia huyo alikaa miongoni mwao kwa muda, akinywa maji, akila majani na kulisha, nao walifaidika na maziwa yake ambayo alichukua kwa kiasi kikubwa kwa kila mmoja kunywa mpaka akatosheka. Baada ya mambo haya kuendelea kwa muda, na wakati wa kuangamizwa kwao kukaribia, waliunda njama kumuua (Ngamia huyo), nao wakamuua:

فَعَقَرُوْهَا فَاصْبَحُوْا نَدِيْمِيْنَ ﴿١٤٢﴾ فَاَخَذَهُمُ الْعَذَابُ ۗ

“Lakini wakamuua, na wakawa wenye kujuta. Basi ikawapata adhabu”.

Hivyo ardhi yao iliteremshiwa zilzala ya nguvu, na ukaja kwao ukulele mkubwa ambao ulichukua mioyo yao kutoka sehemu zake. Wakapata matukio ambayo hawakuwa wenye kuyatarajia, na kulipokucha wakawa majumbani mwao kifudufudi, wamekufa.

إِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَايَةً ۗ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٤٣﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿١٤٤﴾

“Hakika katika hayo ipo Ishara. Lakini hawakuwa wengi wenye kuamini. Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.

كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوطٍ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٤٥﴾ اِذْ قَالَ لَهُمْ اٰخُوهُمْ لُوطُ اَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿١٤٦﴾ اِنِّيْ لَكُمْ

رَسُوْلٌ اٰمِيْنٌ ﴿١٤٧﴾ فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيعُوْنَ ﴿١٤٨﴾ وَمَا اَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ اَجْرٍ ۗ اِنِّ اَجْرِيْ اِلَّا

عَلَيَّ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٤٩﴾

160. "Watu wa Luutw waliwakanusha Mitume.

161. Alipowaambia ndugu yao Swaleh: Je! Hamumchimungu?

162. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.

163. Mcheni Allah, na nitiini.

164. Na sikutakini juu yake ujira, kwani Ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote".

Luutw عليه السلام na Wito Da'wah Yake

Allah تعالى Anatupa habari ya mja na Mtume Wake, Luutw عليه السلام. Jina lake kamili ni Luutw ibn Haaraan ibn Azaar, naye ni mtoto wa kaka yake Ibrahim *Khalil* عليه السلام. Allah تعالى Alimtuma kwa taifa kubwa katika uhai wa Nabii Ibrahim عليه السلام. Kaumu hiyo, ilikuwa ikiishi Saduum (Sodom) na vitongoji vyake, ambavyo Allah تعالى Aliangamiza na Kuibadilisha sehemu hiyo kuwa ni ziwa linalonuka sana, nayo ni mashuhuri katika ardhi ya Al-Ghur (Bonde la Jordan), inayopakana na milima ya Al-Quds (Jerusalem), baina ya milima na ardhi ya Al-Karak na Ash-Shawbak. Luutw عليه السلام aliwalingania katika njia ya Allah تعالى ili wamuabudu Yeye Peke Yake bila kumshirikisha, wamtii Mtume wao ambaye ametumwa na Allah تعالى kwao wao. Aliwakataza kabisa kumuasi Allah تعالى na kufanya madhambi waliyoyazua na kuyaanzisha ambayo hayakujulikana na kiumbe yeyote katika ardhi kabla ya wakati wao huo; kwa kuwalawiti wanaume.

Kwa hivyo Allah تعالى Alisema:



أَتَأْتُونَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعَلَمِينَ ﴿١٦٥﴾ وَتَذَرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ
 رَبُّكُمْ مِنْ أَرْوَاحِكُمْ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ عَادُونَ ﴿١٦٦﴾ قَالُوا
 لَيْن لَمْ تَنْتَه يَلُوطُ لَتَكُونَ مِنَ الْمُخْرَجِينَ ﴿١٦٧﴾ قَالَ إِنِّي
 لِعَمَلِكُمْ مِنَ الْقَالِينَ ﴿١٦٨﴾ رَبِّ نَجِّنِي وَأَهْلِي مِمَّا يَعْمَلُونَ
 ﴿١٦٩﴾ فَتَجَبَّيْنَهُ وَأَهْلَهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٧٠﴾ إِلَّا عَجُوزًا فِي الْغَيْرِينَ
 ﴿١٧١﴾ ثُمَّ دَمَرْنَا الْأَخْرِينَ ﴿١٧٢﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا
 فَسَاءَ ۗ مَطَرُ الْمُنذَرِينَ ﴿١٧٣﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۗ وَمَا كَانَ
 أَكْثَرَهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٧٤﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٧٥﴾
 كَذَّبَ أَصْحَابُ لَيْكَةِ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧٦﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ شُعَيْبٌ
 أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٧٨﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ
 وَأَطِيعُوا أَوْطِيعُونَ ﴿١٧٩﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۗ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا
 عَلَىٰ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٨٠﴾ * أَوْفُوا الْكَيْلَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ
 الْمُخْسِرِينَ ﴿١٨١﴾ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ﴿١٨٢﴾ وَلَا
 تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْنُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿١٨٣﴾
 وَاتَّقُوا الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالْجِبِلَّ الْأُولَىٰ ﴿١٨٤﴾

أَتَأْتُونَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعَلَمِينَ ﴿١٦٥﴾
 وَتَذَرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ رَبُّكُمْ مِنْ
 أَرْوَاحِكُمْ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ عَادُونَ
 ﴿١٦٦﴾ قَالُوا لَيْن لَمْ تَنْتَه يَلُوطُ
 لَتَكُونَ مِنَ الْمُخْرَجِينَ ﴿١٦٧﴾ قَالَ
 إِنِّي لِعَمَلِكُمْ مِنَ الْقَالِينَ ﴿١٦٨﴾ رَبِّ
 نَجِّنِي وَأَهْلِي مِمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٦٩﴾
 فَتَجَبَّيْنَهُ وَأَهْلَهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٧٠﴾
 إِلَّا عَجُوزًا فِي الْغَيْرِينَ ﴿١٧١﴾ ثُمَّ
 دَمَرْنَا الْأَخْرِينَ ﴿١٧٢﴾ وَأَمْطَرْنَا
 عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَسَاءَ ۗ مَطَرُ الْمُنذَرِينَ
 ﴿١٧٣﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۗ وَمَا كَانَ
 أَكْثَرَهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٧٤﴾ وَإِنَّ
 رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٧٥﴾

165. "Je! Katika viumbe vyote mawaingilia wanaume?"

166. Na mnaacha alichokuumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Ama kweli nyinyi ni watu mnaoruka mipaka!

167. Wakasema: Ewe Luutw! Usipoacha, hapana shaka utakuwa miongoni mwa wanaotolewa mji!

168. Akasema: Hakika mimi ni katika wanaokichukia hichi kitendo chenu.

169. *Mola wangu Mlezi! Niokoe mimi na ahali zangu na haya wayatendayo.*

170. *Basi Tukamwoko ya yeye na ahali zake wote.*

171. *Isipokuwa kikongwe katika waliokaa nyuma.*

172. *Kisha Tukawaangamiza wale wengine.*

173. *Na Tukawanyeshea mvua, basi ni ovu mno mvua ya waliyoonywa.*

174. *Hakika katika hayo ipo Ishara. Na hawakuwa wengi wao wenye kuamini.*

175. *Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu”.*

Katazo la Luutw kwa Matendo ya Kaumu yake, Jawabu Lao na Adhabu Waliopatiwa

Alipowakataza Nabii wa Allah wasifanye uasherati na liwati na kuwaongoza wao kuwajamii wake zao ambao Allah تعالی Amewaumbia. Jawabu yao kwake ilikuwa:

لَئِن لَّمْ تَنْتَهَ يَنْلُوطُ

“*Ewe Luutw! Usipoacha*”, Maana yake: Ikiwa hutaacha hayo uliyokuja nayo. Wakamwambia

لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمُخْرَجِينَ ﴿٢٧﴾

“*Hapana shaka utakuwa miongoni mwa wanaotolewa mji!*”

Maana yake: Tutakufukuza kabisa kukaa pamoja nasi. Hii ni kama Allah تعالی Alivyosema:

* فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوْنَا أَلْ لُوطِ مِنْ قَرْيَتِكُمْ إِنَّهُمْ أَنَاسٌ

يَتَطَهَّرُونَ ﴿٢٨﴾

“*Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila kusema: Wafukuzeni wafuasi wa Luutw katika mji wenu, hao ni watu wanaojitakasa.*”
(27: 56).

Alipoona ya kwamba hawaachi njia zao mbaya, na walikaidi katika kuendelea na upotevu na alijitenga nao na kujiondoa hatiani. Hapo akasema:

قَالَ إِنِّي لِعَمَلِكُمْ مِنَ الْقَالِينَ ﴿١٦٥﴾

“Hakika mimi ni katika wanaokichukia hichi kitendo chenu”.

Maana yake: Miongoni mwa waliofedheheshwa sana, sipendi wala siridhii hilo, nami niko mbali nanyi kwa kufanya kitendo hicho kiovu. Kisha alimuomba Allah تعالی dhidi ya watu wake kwa kusema:

رَبِّ يَحْنِي وَأَهْلِي مِمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٦٦﴾

“Mola wangu Mlezi! Niokoe mimi na ahali zangu na haya wayatendayo”.

Allah تعالی Akasema:

فَنَجِيئُهُ وَأَهْلَهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٦٧﴾

“Basi Tukamuokoa yeye na ahali zake wote”.

Maana yake: Wote kwa jumla. Lakini,

إِلَّا عَجُوزًا فِي الْغَابِرِينَ ﴿١٦٨﴾

“Isipokuwa kikongwe katika waliokaa nyuma”.

Huyo alikuwa ni mkewe, ambaye alikuwa ni mwanamke ajuza mbaya. Alibaki nyuma na hivyo kuangamizwa pamoja na wale wote waliobaki. Hiyo ni sawa na Alivyosema Allah تعالی kuhusu wao katika Suraul A'raaf (Surah ya 7), Huud (11) na pia katika Al-Hijr (15)¹, pale alipoagizwa na Allah تعالی kuichukua familia yake usiku, isipokuwa mkewe, na wasiwe ni wenye kugeuka nyuma pale watakapousikia ukulele utakapoteremka kwa watu wake. Hivyo, kwa subira walitii Amri ya Allah تعالی, na Allah تعالی Alituma Adhabu kwa kaumu hiyo ambayo ili wajumlisha wote kwa pamoja. Walinyeshewa mvua ya mawe ya udongo wa kuchomwa, uliorundikana. Kwa hiyo, Allah تعالی Akasema:

¹Tazama 7:80, 11:77, 15:58-76.

ثُمَّ دَمَرْنَا الْأَخْرِينَ ﴿١٧٧﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا

“Kisha Tukawaangamiza wale wengine. Na Tukawanyeshea mvua.”

Hadi Kauli Yake:

وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٧٨﴾

“Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu.”

كَذَّبَ أَصْحَابُ لَيْكَةِ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧٩﴾ إِذْ قَالَ لَهُمْ شُعَيْبٌ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٨٠﴾ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٨١﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرًا ﴿١٨٢﴾ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٨٣﴾

176. Watu wa Machakani waliwakanusha Mitume.

177. Shu’ayb alipowaambia: Je! Hamfanyi mkamcha Mungu?

178. Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu.

179. Mcheni Allah, na nitiini.

180. Na sikutakini juu yake ujira, kwani Ujira wangu hauko ila kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote”.

Mawaidha ya Shu’ayb عليه السلام kwa Watu wa Aykah

Hawa - yaani watu wa Aykah – ndio watu wa Madyan kwa rai iliyo sahihi. Nabii Shu’ayb عليه السلام alikuwa miongoni mwao, hakika Aya haikusema, ndugu yao Shu’ayb عليه السلام, kwa sababu walijinasibisha na ‘Ibaadah ya Aykah kwa maana ya Mti. Inasemwa kuwa ni kundi la miti mingi iliyosongamana sana katika kichaka, waliokuwa wakiabudu. Kwa hiyo, pale Allah تعالى Alipotaja watu wa Aykah waliwakadhibisha Mitume, hakutaja neno ndugu yao Shu’ayb عليه السلام. Hakika Yeye Alisema:

إِذْ قَالَ لَهُمْ شُعَيْبٌ

“Shu’ayb alipowaambia”.

Ikakatika nasaba ya undugu baina yao kwa sababu ya ile maana waliyo-jinasibisha nayo, japokuwa alikuwa ni ndugu kinasaba. Baadhi ya watu hawakuweza kuitambua nukta hii, hivyo wakadhania kuwa watu wa *Ay kah* ni mbali na watu wa Madyan, hivyo kudai kuwa Shu'ayb عليه السلام alitumwa na Allah تعالى kwa Ummah mbili; na wapo wanaosema: Ummah tatu.

Na Kauli Yake:

﴿أَصْنَبْ نَيْكَوْهُ﴾

“Na watu wa *Ay kah*.”

Ni kaumu ya Shu'ayb عليه السلام. Hii ilikuwa ni rai ya Ishaq ibn Bishr.¹ Mtu mwengine asiyekuwa Juwaybir amesema: “Watu wa *Ay kah* na Madyan ni wamoja (hawana tofauti yoyote).”²

Na Allah تعالى Anajua zaidi. Iliyo sahihi ni kuwa ni Ummah mmoja waliokuwa wakielezewa tofauti katika sehemu tofauti. Nabii Shu'ayb عليه السلام aliwalingania na kuwaamuru wao kuwa waadilifu katika vipimo, kama ilivyoelezwa katika kisa cha Madyan. Hiyo ni dalili ya kutosha kuwa wao walikuwa ni Ummah mmoja.

* أَوْفُوا الْكَيْلَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُخْسِرِينَ ﴿١٦٥﴾ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ﴿١٦٦﴾ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْنُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿١٦٧﴾ وَأَتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالْجِبِلَّ الْأُولِينَ ﴿١٦٨﴾

181. Timizeni kipimo sawa sawa, wala msiwe katika wanaopunja.

182. Na pimeni kwa haki iliyonyooka.

183. Wala msiwapunje watu vitu vyao, wala msifanye jeuri na ufisadi katika ardhi.

184. Na mcheni Aliye kuumbeni nyinyi na vizazi vilivyotangulia.”

¹Ad-Durr al-Manthuur 6:318.

²Atw-Twabariy 19:390.

Amri ya Kukamilisha Kipimo na Mizani

Allah تعالی Amewaamuru wakamilishe kipimo na mizani, na Aliwakataza kupunja. Akasema:

﴿ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُخْسِرِينَ ﴾

“Kamilisheni kipimo sawa sawa, wala msiwe katika wanaopunja.”

Maana yake: Mnapowapimia watu, wapimieni kamili wala msiwapunje katika kupima, hivyo kuwapatia pungufu. Na kuchukua kutoka kwao, timilifu na kamili ikiwa mnajipimia wenyewe. Inavyofaa na kutakiwa ni kuwa chukueni kama mnavyotoa, na toeni kama mnavyochukua.

﴿ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ﴾

“Na pimeni kwa haki iliyonyooka.”

Al-Qistwaas ni mizani. Na Kauli Yake:

﴿ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ ﴾

“Wala msiwapunje watu vitu vyao.”

Maana yake: Msiwapunguzie katika mali zao.

﴿ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴾

“Wala msifanye jeuri na ufisadi katika ardhi.”

Maana yake: Ujambazi wa njiani (mkata njia). Hii ni kama Alivyosema Allah تعالی katika Aya nyingine:

﴿ وَلَا تَفْعُدُوا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوعِدُونَ ﴾

“Wala msikae katika kila njia mkitisha watu.” (7:86).

Na Kauli Yake:

﴿ وَأَتَقُوا الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالْجِيلَ الْأَوَّلِينَ ﴾

“Na mcheni Aliyekuumbeni nyinyi na vizazi vilivyotangulia.”

Hapa anawatisha na adhabu ya Allah تعالى ambaye Amewaumba wao na Kuwaumba mababa zao wa awali. Hii ni kama alivyosema Musa عليه السلام:

قَالَ رَبُّكُمْ رَبُّ آبَائِكُمُ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٦﴾

“Ndiye Mola wenu Mlezi, na Mola Mlezi wa baba zenu wa kwanza.” (26: 26).

Amesema Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, As-Suddiy, Sufyaan ibn ‘Uyaynah na ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam:

وَالْجِبِلَّةَ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٦﴾

“Na vizazi vilivyotangulia.”

Inamaanisha, Yeye Ndiye Aliyeumba vizazi vya mwanzo. Ibn Zayd alisoma:

وَلَقَدْ أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا

“Na bila shaka yeye (Shetani) aliwapoteza viumbe wengi miongoni mwenu.” (36:62)¹

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:392.

قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ مِنَ الْمُسْحَرِينَ ﴿١٨٥﴾ وَمَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ
 مِثْلُنَا وَإِن نَّظُنُّكَ لَمِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿١٨٦﴾ فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا
 كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ إِن كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٨٧﴾ قَالَ رَبِّي
 أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨٨﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُم عَذَابُ يَوْمِ
 الظُّلَّةِ ۗ إِنَّهُ كَانَ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٨٩﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُم مُّؤْمِنِينَ ﴿١٩٠﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ
 الرَّحِيمُ ﴿١٩١﴾ وَإِنَّهُ لَتَنزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٩٢﴾ نَزَلَ بِهِ
 الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٩٣﴾ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٩٤﴾
 بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُّبِينٍ ﴿١٩٥﴾ وَإِنَّهُ لَفِي زُبُرِ الْأَوَّلِينَ ﴿١٩٦﴾ أَوْلَمْ
 يَكُنْ هُمْ ءَايَةً أَنْ يَعْلَمَهُ عُلَمَتُنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٩٧﴾ وَلَوْ
 نَزَّلْنَاهُ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَعْجَمِينَ ﴿١٩٨﴾ فَقَرَأَهُ عَلَيْهِمْ مَا
 كَانُوا بِهِ مُؤْمِنِينَ ﴿١٩٩﴾ كَذَلِكَ سَلَكْنَاهُ فِي قُلُوبِ
 الْمُجْرِمِينَ ﴿٢٠٠﴾ لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ
 الْأَلِيمَ ﴿٢٠١﴾ فَيَأْتِيهِمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٠٢﴾
 فَيَقُولُوا هَلْ نَحْنُ مُنظَرُونَ ﴿٢٠٣﴾ أَفِعَذَابِنَا يَسْتَعْجِلُونَ
 ﴿٢٠٤﴾ أَفَرَأَيْتَ إِن مَّتَّعْنَاهُمْ سِنِينَ ﴿٢٠٥﴾ ثُمَّ جَاءَهُمْ مَا
 كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٢٠٦﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا
 يُمْتَعُونَ ﴿٢٠٧﴾ وَمَا أَهْلَكْنَا مِن قَرِيْبَةٍ إِلَّا مَا مُنذِرُونَ
 ﴿٢٠٨﴾ ذِكْرَىٰ وَمَا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٢٠٩﴾

قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ مِنَ الْمُسْحَرِينَ ﴿١٨٥﴾ وَمَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا وَإِن نَّظُنُّكَ لَمِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿١٨٦﴾ فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ إِن كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٨٧﴾ قَالَ رَبِّي أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨٨﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُم عَذَابُ يَوْمِ الظُّلَّةِ ۗ إِنَّهُ كَانَ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٨٩﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُم مُّؤْمِنِينَ ﴿١٩٠﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٩١﴾

185. "Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa.

186. Na wewe si chochote ila ni mtu kama sisi. Na kwa yakini tunakuona wewe ni katika waongo.

187. Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao ukweli.

188. Akasema: Mola wangu Mlezi Anajua zaidi mnayo-yatenda.

189. Basi walimkanusha, na ikawashika adhabu ya siku ya kivuli. Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya Siku Kubwa.

190. Hakika katika hayo ipo Ishara, lakini hawakuwa wengi wenye kuamini.

191. Na hakika Mola wako Mlezi ndiye bila ya shaka ndiye Yeye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu”.

Jawabu ya Kaumu ya Shu’ayb عليه السلام, Kumkanusha Yeye na Ujio wa Adhabu juu yao

Allah تعالى Anatueleza jawabu ya kaumu yake, iliyokuwa sawa na ile ya Thamud waliyomjibu Mtume wao – mioyo na akili zao zilifanana – pale waliposema.

إِنَّمَا أَنْتَ مِنَ الْمُسَحَّرِينَ ﴿١٨٩﴾

“Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa.”

Wakimaanisha kuwa wewe umeathiriwa na uchawi, kama tulivyotangulia kueleza. Pia:

وَمَا أَنْتَ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا وَإِنْ نَظُنُّكَ لَمِنَ الْكٰذِبِينَ ﴿١٩١﴾

“Na wewe si chochote ila ni mtu kama sisi. Na kwa yakini tunakuona wewe ni katika waongo.”

Hii ina maana sisi tunadhania kuwa wewe unasema uwongo kwa makusudi, na hakika Allah تعالى Hakukutuma kwetu sisi. Kama ni kweli, basi:

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ

“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni.”

Amesema Adh-Dhahhaak: “Pembeni mwa mbingu.”¹ Na amesema Qataadah: “Kipande cha mbingu.”² Na akasema As-Suddiy: “Adhabu kutoka mbinguni.”

Haya yanashabihiana na yale waliyosema Ma-Quraysh kama anavyotuelezea Allah تعالى kwa Kauli Yake:

¹ Atw-Twabariy 19:393.

² Atw-Twabariy 22:485.

وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنْبُوعًا ﴿١٨٥﴾

“Na walisema: Hutakuamini mpaka ututimbulie chemchem katika ardhi hii”.

Mpaka Kauli Yake Allah تعالى،

أَوْ تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمَتَ عَلَيْنَا كَيْسًا أَوْ تَأْتِيَنَا بِاللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا ﴿١٩٢﴾

“Au utuangushie mbingu vipande vipande kama unavyodai; au utuletee Allah na Malaika uso kwa uso.” (17:90-92)

Na Kauli Yake:

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِن كَانَتْ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ

“Na waliposema: Ee Allah ikiwa haya ni ukweli utokao Kwako basi tunyeshie mawe kutoka mbinguni.” (8:32)

Hivyo ndivyo walivyosema makafiri hawa wajinga:

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كَيْسًا مِنَ السَّمَاءِ

“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni.”

Akawajibu:

قَالَ رَبِّيَ أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨٦﴾

“Akasema: Mola wangu Mlezi Anajua zaidi mnayoyatenda”.

Akasema: Allah تعالى Anawajua zaidi, ikiwa mnastahiki hilo, Atawajazi kwayo, naye si dhalimu hata kidogo kwenu nyinyi. Hivyo ndivyo ilivyotokea kwao - kama walivyotaka – malipo yao sawa na amali zao.

Hivyo Akasema Allah تعالى:

فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُمْ عَذَابٌ يَوْمِ الظُّلَّةِ إِنَّهُ كَانَ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٨٧﴾

“Basi walimkanusha, na ikawashika adhabu ya siku ya kivuli. Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya Siku Kubwa.”

Hili ndilo walilotaka, pale walipotaka kipande cha mbingu kiwaangukie wao. Hakika Allah تعالى Alijaalia adhabu yao kuwa ni joto kali sana kwa muda wa siku saba, hakuna kilichowahifadhi wao. Kisha walijiwa na kiwingu kilichowafunika, nao walikikimbilia ili kufunikwa na kivuli chake kutokana na jua kali. Pindi wote walipokusanyika chini yake, Allah تعالى Alituma cheche za moto, miale na moto mkali sana juu yao, Akaifanya ardhi kutikisika chini yao, na Akatuma dhidi yao ukelele mkubwa ambao uliharibu nyoyo zao.

Kwa hiyo Akasema Allah تعالى:

إِنَّهُمْ كَانُوا عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٨٦﴾

“Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya Siku Kubwa”.

Hakika Allah تعالى Anataja jinsi walivyoangamizwa katika sehemu tatu, kila sehemu ikilingana na muktadha wake. Katika Suratul A'raaf inataja kuwa walikumbwa na tetemeko wakaamkia majumbani mwao wamejifudikiza. Hiyo ni kuwa wao walisema:

لُنْخْرِجَنَّكَ بِدُشْعَيْبٍ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا أَوْ لَتَعُوذُنَّ فِي مِلَّتِنَا

“Ewe Shu'ayb! Tutakutoa wewe pamoja na wale waliokuamini katika mji wetu, au mrejee katika mila yetu.” (7:88).

Walitaka kumuogofya Nabii wa Allah na wafuasi wake, hivyo wakanyakuliwa na tetemeko la ardhi¹. Na katika Surah Huud, Allah تعالى Amesema:

وَأَخَذَتِ الَّذِينَ ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ

“Na ukelele uliwanyakua waliodhulumu.” (11:94).

Hiyo ni kwa sababu walimfanyia istihzai (kumcheza shere) Nabii wa Allah kwa kauli yao:

يَدُشْعَيْبٍ أَصْلُوتُكَ تَأْمُرُكَ أَنْ نَتْرَكَ مَا يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا أَوْ أَنْ نَفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا دَشَتُوا

إِنَّكَ لَأَنْتَ الْحَلِيمُ الرَّشِيدُ ﴿١٨٧﴾

¹ Tazama 7:91.

“Ewe Shu’ayb! Ni Swala zako ndizo zinazokuamrisha tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Ama hakika wewe ni mstahamilivu kweli na mwongofu!” (11:87).

Walisema hayo kwa istihzai na kejeli, hivyo ikawa sawa kwa ukelele uwajie ili uwanyamazishe wao, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَأَخَذَتِ الَّذِينَ ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ

“Na ukele uliwanyakua waliodhulumu.” (11:94).

Na hapa walisema:

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ

“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni”.

Kwa njia ya ukaidi na inadi. Hivyo, ikawa sawa kabisa kwao kupatikana na jambo ambalo hawakutarajia kabisa kuwafikia,

فَأَخَذَهُمُ عَذَابٌ يَوْمِ الظُّلَّةِ إِنَّهُ كَانَ عَذَابٌ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٠١﴾

“Na ikawashika adhabu ya siku ya kivuli. Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya Siku Kubwa.”

Imepokewa na Muhammad ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Yazid Al-Baahiliy kwamba alimuuliza Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Aya hii:

فَأَخَذَهُمُ عَذَابٌ يَوْمِ الظُّلَّةِ

“Na ikawashika adhabu ya siku ya kivuli”.

Akasema: “Allah تعالى Aliwatumia radi na moto mkali sana, ambazo ziliwatisha (hivyo waliingia ndani ya nyumba zao nazo ziliwafuata mpaka ndani kabisa na kuwashitusha zaidi), wakatoka katika nyumba zao na kukimbia katika viwanja. Hapo Allah تعالى Aliwatumia mawingu ambayo yaliwafunika (kuwa kivuli kwao) kutoka na joto la jua, na wakapata ubaridi na ladha. Wakati huo waliitana mmoja mmoja mpaka wote wakakusanyika chini ya kiwingu,

baadaye Allah تعالى Alituma moto kwao". Alisema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Hiyo ilikuwa ni adhabu ya siku ya kivuli, nayo ilikuwa ni adhabu ya siku kubwa."¹

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٨٥﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿١٨٦﴾

"Hakika katika hayo ipo Ishara, lakini hawakuwa wengi wenye kuamini. Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka Ndiye Yeye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu." (26:8-9).

Hii inamaanisha kuwa Allah تعالى ni Mwenye Nguvu katika Kutoa adhabu kwa makafiri, na ni Mwenye Kuwarehemu waja wake Waumini.

وَإِنَّهُ لَتَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٨٧﴾ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٨٨﴾ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٨٩﴾ بِلسانٍ عَرَبِيٍّ مُبِينٍ ﴿١٩٠﴾

192. "Na bila ya shaka huu ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

193. Ameuteremsha Roho muaminifu,

194. Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji,

195. Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi".

Qur'ani Imeteremshwa na Allah تعالى

Allah تعالى Anasema Kutupasha habari kuhusu Kitabu Alichokiteremsha kwa mja na Mtume Wake, Muhammad ﷺ:

وَإِنَّهُ

"Na hakika hii". Maana yake: Qur'ani iliyotangulia kutajwa mwanzo wa Surah katika Kauli Yake:

وَمَا يَأْتِيهِمْ مِنْ ذِكْرٍ مِنَ الرَّحْمَنِ مُحَدَّثٍ

"Wala hauwafikii ukumbusho mpya kutoka kwa Ar-Rahmaan." (26:5).

Na hii Qur'ani:

¹ Atw-Twabariy 19:394.

لَتَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٨٦﴾

“Ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Allah تعالیٰ Ameuteremsha kwako na Kukuletea Wahyi wewe. Kisha,

نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٨٧﴾

“Ameuteremsha Roho muaminifu.”

Naye ni Jibril عليه السلام. Rai hii imetolewa na wanazuoni wengi miongoni mwa *Salaf* (watangulizi wema) kama Ibn ‘Abbaas, Muhammad ibn Ka’b, Qataadah, ‘Atwiyah, Al-‘Awfiy, As-Sudiy, Adh-Dhahaak, Az-Zuhriy na Ibn Jurayj¹. Hii ni rai ambayo haina mzosano ndani yake. Amesema Az-Zuhriy: “Hii ni kama Kauli Yake:

قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“Sema: Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliyeiteremsha Qur’ani moyoni mwako kwa Idhini ya Allah, inayothibitisha yaliyokuwa kabla yake.” (2:97).

عَلَى قَلْبِكَ

“Moyoni mwako.”

“Ewe Muhammad, bila kuwa na doa, nyongeza au kasoro.”

لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٨٨﴾

“Ili uwe katika Waonyaji.”

Ili uwaonye watu kwayo kwa Adhabu ya Allah تعالیٰ kwa wale wenye kwenda kinyume nayo na kuikanusha na kuwapatia bishara njema Waumini wenye kuifuata. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُبِينٍ ﴿١٨٩﴾

“Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi.”

¹ Atw-Twabariy 19:396.

Maana yake: Qur'ani hii Tuliyoiteremsha kwako, hakika Tumeiteremsha kwa lugha yako ya Kiarabu fasaha na iliyokamilika, ili iwe bayana, wazi na dhahiri kabisa, wala isiache nafasi ya udhuru, na iwe ni yenye kusimamisha hoja, inayoonesha njia iliyonyooka.

وَإِنَّهُ لَفِي زُبُرِ الْأَوَّلِينَ ﴿١٨٦﴾ أَوْلَمْ يَكُنْ هُمْ آيَةً أَنْ يَعْلَمَهُ عُلَمَتُونَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٨٧﴾ وَلَوْ
نَزَّلْنَاهُ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَعْجَمِينَ ﴿١٨٨﴾ فَقَرَأَهُ عَلَيْهِمْ مَا كَانُوا بِهِ مُؤْمِنِينَ ﴿١٨٩﴾

196. "Na hakika haya yamo katika Vitabu vya kale.

197. Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili?

198. Na lau kuwa Tungeliiteremsha juu ya mmoja wa wasio kuwa Waarabu,

199. Na akawasomea, wasingelikuwa wenye kuamini".

Qur'ani Imetajwa katika Vitabu vya Kale

Allah تعالى Anasema: Qur'ani hii imetajwa katika Vitabu vya kale viliivyoachwa na Manabii wao walitoa bishara enzi za kale na pia sasa.

Kama Allah تعالى alivyochukua kwao ahadi kuwa wataifuata mpaka akasimama wa Mwisho katika Mitume wa Wana wa Israil wao na kuhutubia watu wake kwa bishara njema ya kuja kwa Ahmad ﷺ:

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَبْنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ
التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدُ

"Na wakumbushe aliposema Nabii 'Isaa ibn Maryam: Enyi wana wa Israili! Mimi ni Mtume wa Allah kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na kutoa habari njema ya Mtume atakayekuja baada yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad." (61:6).

Zubur hapa inamaanisha Vitabu, nayo ni wingi wa *Zabuur*. Hivyo hivyo *Zabuur* ni Kitabu alichoteremshiwa Nabii Daawuud عليه السلام. Allah تعالى Akasema:

وَكُلُّ شَيْءٍ فَعَلُوهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٢﴾

“Na kila jambo walilofanya limo katika vitabu.” (54:52).

Hii inamaanisha, imeandikwa juu yao katika vitabu vya Malaika. Kisha Aliyetukuka Akasema:

أَوَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ آيَةٌ أَنْ يَعْلَمَهُرُ غُلَمَانُؤا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٣﴾

“Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili?.”

Hii ina maana je, haitoshi kuwa wanazuoni wao, wana wa Israili waliokuwa mashahidi wa ukweli huu kwao kuwa Qur’ani hii imetajwa katika Vitabu vyao wanavyovisoma?, Muradi ni kuwa waadilifu miongoni mwao wanatambua yaliyo mikononi mwao katika sifa za Mtume Muhammad ﷺ, risala yake na Ummah wake. Hakika hizi zimetajwa katika Vitabu vyao, kama walivyo sema wale waliosilimu kati yao, mfano wa ‘Abdullah ibn Salaam na Salmaan al-Faarsiy na wengineo رضي الله عنهم waliokutana na Mtume ﷺ. Allah تعالى Amesema:

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ

“Ambao kwamba wanamfuata Mtume, Nabii asiyesoma wala kuandika.” (7:157).

Ukanushaji Mkali wa Maquraysh

Kisha Allah تعالى Anatuelezea ukali wa ukanushaji na inadi ya Maquraysh kwa Qur’ani hii. Lau kuwa ufasaha wa Qur’ani hii ungeteremshwa kwa asiyekuwa Muarabu (Muajemi) ambaye haelewi hata neno moja la Kiarabu basi pia hawangemuamini kabisa. Kwa hiyo Akasema:

وَلَوْ نَزَّلْنَاهُ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَعْجَمِينَ ﴿٥٤﴾ فَقَرَأَهُ عَلَيْهِمْ مَا كَانُوا بِمِءِ مُؤْمِنِينَ ﴿٥٥﴾

“Na lau kuwa Tungeliiteremsha juu ya mmoja wa wasiokuwa Waarabu, na akawasomea, wasingelikuwa wenye kuamini.”

Allah تعالى Ametuelezea kuhusu wao katika Aya nyingine:

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ﴿١٨٥﴾ لَقَالُوا إِنَّمَا سُكَّرَتْ أَبْصَارُنَا

“Na lau Tungewafungulia mlango wa mbingu, wakawa wanapanda basi wangelisema: Macho yetu yamelevywa.” (15:14-15).

Akasema Aliyetukuka:

﴿١٨٦﴾ وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْتَوْنِ

“Na lau Tungeliwateremshia Malaika, na maiti wangezungumza nao.” (6:111).

Na Akasema Aliyetukuka:

﴿١٨٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٧﴾

“Hakika wale ambao Neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini.” (10:96).

﴿١٨٨﴾ كَذَلِكَ سَلَكَنتَهُ فِي قُلُوبِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٨٨﴾ لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ

﴿١٨٩﴾ فَيَأْتِيهِمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٨٩﴾ فَيَقُولُوا هَلْ نَحْنُ مُنظَرُونَ ﴿١٩٠﴾ أَفَبِعَذَابِنَا

﴿١٩١﴾ يَسْتَعْجِلُونَ ﴿١٩١﴾ أَفَرَأَيْتَ إِن مَّتَّعْنَاهُمْ سِنِينَ ﴿١٩٢﴾ ثُمَّ جَاءَهُمْ مَا كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٩٢﴾

﴿١٩٣﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يُمْتَعُونَ ﴿١٩٣﴾ وَمَا أَهْلَكْنَا مِن قَرْيَةٍ إِلَّا هَا مُنذِرُونَ ﴿١٩٤﴾

﴿١٩٥﴾ ذِكْرَىٰ وَمَا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٩٥﴾

200. **“Namna hivi Tunaingiza katika nyoyo za wakosefu.**

201. **Hawataiamini mpaka waione adhabu chungu.**

202. **Basi itawafikia kwa ghafla, na hali hawana khabari.**

203. **Na watasema: Je, tutapewa muhula?**

204. **Basi, je, wanaihimiza adhabu yetu?**

205. **Waonaje kama Tukiwastarehesha kwa miaka,**

206. *Kisha yakawafikia waliyokuwa wakiahidiwa,*
 207. *Yatawafaa nini yale waliyostareheshewa?*
 208. *Wala hatukuangamiza mji wowote ila ulikuwa na waonyaji.*
 209. *Kuwa ni ukumbusho. Wala Sisi hatukuwa wenye kudhulumu."*

Wanaokadhibisha Hawataamini Mpaka Waione Adhabu

Allah تعالى Anasema: Hivyo ndivyo Tunavyoingiza kwa wanaokadhibisha, wanaokufuru, wanaokataa na wenye inadi, yaani Tumeingiza katika nyoyo za wahalifu. Wao wana sifa hii bainifu:

لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ

"Hawataamini."

Maana yake: Haki, hadi:

حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٢٠٦﴾

"Mpaka waione adhabu chungu."

Na wakati huo udhuru wa madhalimu hautawafaa chochote, watakuwa na laana, na makazi yao yatakuwa ni maovu kabisa. Hapo:

فَيَأْتِيهِمْ بَغْتَةً

"Basi itawafikia kwa ghafla."

Maana yake: Adhabu kutoka kwa Allah تعالى itakuja kwao kwa ghafla. Wao watakuwa:

وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٠٧﴾ فَيَقُولُوا هَلْ نَحْنُ مُنظَرُونَ ﴿٢٠٨﴾

"Na hali hawana khabari. Na watasema: Je, tutapewa muhula?"

Wakati huo watakapoiona adhabu hiyo watatamani kupata nafasi ya muda kidogo ili waweze kufanya amali kwa madai yao katika kumtii Allah تعالى, kama Allah تعالى Alivyosema:

وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ

"Na waonye watu siku itakapowajia adhabu."

Hadi Kauli Yake:

مَا لَكُمْ مِّنْ زَوَالٍ ﴿٤٤﴾

“Kwamba hamtaondokewa.” (14:44).

Kila dhalimu na muovu pindi atakaposhuhudia adhabu yake, atahisi majuto makubwa. Huyu hapa Firauni alipoombewa na Musa عليه السلام kwa Kauli yake:

رَبَّنَا إِنَّكَ آتَيْتَ فِرْعَوْنَ وَمَلَأَهُ زِينَةً وَأَمْوَالًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe Umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali katika maisha ya dunia.”

Hadi Kauli Yake:

قَالَ قَدْ أُجِيبَتِ دَعْوَتُكُمَا

“Allah Akasema: “Maombi yenu yamekubaliwa.” (10:88-89).

Dua hii ikawa ina athari kwa Firauni, hakuamini mpaka alipoiona adhabu chungu. Allah تعالى Anasema:

حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْعَرَقُ قَالَ ءَأَمِنْتُ أَنَّهُ لَآ إِلَهَ إِلَّا الَّذِي ءَأَمَنْتَ بِهِ ءَبْنَوْا إِسْرَءِيلَ

“Hata Firauni alipokuwa anataka kuzama akasema: Naamini kuwa hapana Mungu ila Yule waliyemuamini wana wa Israili.”

Hadi katika Kauli Yake:

وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾

“Na ukawa miongoni mwa mafisadi.” (10:90-91).

Na Akasema Aliyetukuka:

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَأَمِنَّا بِاللَّهِ وَحَدُّهُ

“Walipoiona Adhabu Yetu walisema: Tunamuamini sasa Allah Peke Yake.” (40:84).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَفِعْدَابِنَا يَسْتَعْجِلُونَ ﴿٢٩﴾

“Basi, je, wanaihimiza adhabu yetu?”

Huku ni kukataa na onyo kwao kwa sababu walikuwa wakimwambia Mtume kwa njia ya kukadhibisha na kuiona na kufikiria ipo mbali sana. Wakisema:

أَتُنْتَابِعْدَابِ اللَّهِ

“Tuletee adhabu ya Allah.” (29:29).

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ

“Na wanakuomba adhabu ifike upesi.” (29:53-54).

Kisha Akasema:

أَفَرَأَيْتَ إِنْ مَتَّعْنَاهُمْ سِنِينَ ﴿٢٩﴾ ثُمَّ جَاءَهُمْ مَا كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ
مَا كَانُوا يُمْتَعُونَ ﴿٣١﴾

“Waonaje kama Tukiwastarehesha kwa miaka, kisha yakawafikia waliyokuwa wakiahidiwa, yatawafaa nini yale waliyostarehesha?”

Hii inamaanisha, hata Tukilichelewesha jambo hilo ili kuwapa muda mdogo au Mwingi, na kisha adhabu ya Allah تعالى ikawateremkia, maisha yao ya starehe yatawafaidisha nini wakati huo?

Allah تعالى Anasema:

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحًى ﴿٧٩﴾

“Ni kama kwamba wao siku watapoiona (hiyo Saa) hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake.” (79:46).

Amesema tena Allah تعالى:

يُودُّ أَحَدُهُمْ لَوْ يُعَمَّرُ أَلْفَ سَنَةٍ وَمَا هُوَ بِمُزَحَّزِحٍ مِنْهُ مِنَ الْعَذَابِ أَنْ يُعَمَّرَ

“Kila mmoja wao anatamani lau angelipewa umri wa miaka elfu. Wala hayo ya kuzidishiwa umri hayamuondoshei adhabu.” (2:96).

Aidha Allah تعالى Amesema:

وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ﴿٩٢﴾

“Na mali yake yatamfaa nini atapokuwa anadidimia?” (92:11).

Na hapa Allah تعالى Anasema:

مَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يُمْتَعُونَ

“Yatawafaa nini yale waliyostareheshewa?”

Kwa mujibu wa Hadithi Sahihi, Mtume ﷺ anasema:

«يُؤْتَى بِالْكَافِرِ فَيُغْمَسُ فِي النَّارِ غَمْسَةً ثُمَّ يُقَالُ لَهُ: هَلْ رَأَيْتَ خَيْرًا قَطُّ؟ هَلْ رَأَيْتَ نَعِيمًا قَطُّ؟ فَيَقُولُ: لَا وَاللَّهِ يَا رَبِّ، وَيُؤْتَى بِأَشَدِّ النَّاسِ بُؤْسًا كَانَ فِي الدُّنْيَا، فَيُضْبَعُ فِي الْجَنَّةِ صَبْعَةً، ثُمَّ يُقَالُ لَهُ: هَلْ رَأَيْتَ بُؤْسًا قَطُّ؟ فَيَقُولُ: لَا وَاللَّهِ يَا رَبِّ»

“Ataletwa kafiri na kuvurumishwa Motoni mara moja. Kisha ataambiwa: “Je, umeona kheri yoyote? Je, umeona neema yoyote ulipokuwa duniani?” Atasema: “Wallahi, sijaona kabisa ewe Mola wangu Mlezi”. Na ataletwa mtu aliyekuwa hohehahe na shida nyingi duniani, na ataingizwa katika Pepo kwa muda mchache, kisha ataambiwa: “Je, uliona shida ya aina yoyote ulipokuwa duniani?” Atasema: “Wallahi, sijaona ewe Mola wangu Mlezi”. Kumaanisha kama hakuna chochote kilichotokea¹.

Kisha Allah تعالى Anatueleza kuhusu Uadilifu Wake kwa viumbe Vyake, kuwa Haangamizi taifa lolote mpaka mwanzo awe hajawaachia udhuru wowote,

¹ Ahmad 3:203. Muslim pia amenukuu riwaya kama hii, Na. 2807.

kwa Kuwaonya, Kuwatumia Mitume na Manabii na Kuwasimamishia hoja.
Anasema Aliyetukuka:

﴿٢٦﴾ وَمَا أَهْلَكْنَا مِنْ قَرِيْبٍ إِلَّا لَهَا مُنْذِرُونَ ﴿٢٧﴾ ذِكْرَىٰ وَمَا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٢٨﴾

“Wala hatukuangamiza mji wowote ila ulikuwa na waonyaji. Kuwa ni ukumbusho, Wala Sisi hatukuwa wenye kudhulumu.”

Hii ni kama ile Aya inayosema:

﴿٢٩﴾ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿٣٠﴾

“Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume.” (17:15).

Anasema tena:

﴿٣١﴾ وَأَهْلُهَا ظَالِمُونَ ﴿٣٢﴾

“Mpaka watu wake wawe madhalimu.” (28:59).

* * *

وَمَا تَنْزَلَتْ بِهِ الشَّيْطَانُ ﴿٢١٠﴾ وَمَا يُنْبِئِي هُمْ وَمَا
يَسْتَطِيعُونَ ﴿٢١١﴾ إِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ لَمَعْزُولُونَ ﴿٢١٢﴾
فَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا ءَاخَرَ فَتَكُونَ مِنَ الْمُعَذِّبِينَ ﴿٢١٣﴾
وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٢١٤﴾ وَأَخْفِضْ جَنَاحَكَ
لِمَنْ أَتَيْتَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢١٥﴾ فَإِنْ عَصَوْكَ فَقُلْ إِنِّي
بَرِيءٌ مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢١٦﴾ وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٢١٧﴾
الَّذِي يَرِنُكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٨﴾ وَتَقَلُّبِكَ فِي السِّنِّجِينِ ﴿٢١٩﴾
إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٢٢٠﴾ هَلْ أَنْتُمْ عَلَىٰ مَنْ تَنْزَلُ
الشَّيْطَانُ ﴿٢٢١﴾ تَنْزَلُ عَلَىٰ كُلِّ آفَاكٍ أَثِيمٍ ﴿٢٢٢﴾ يُلْقُونَ
السَّمْعَ وَأَكْثُرُهُمْ كَذِبُونَ ﴿٢٢٣﴾ وَالشُّعْرَاءُ يَتَّبِعُهُمُ
الْغَاوُونَ ﴿٢٢٤﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّهُمْ فِي كُلِّ وَادٍ يَهِيمُونَ ﴿٢٢٥﴾
وَأَنَّهُمْ يَقُولُونَ مَا لَا يَفْعَلُونَ ﴿٢٢٦﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا
وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَذَكَرُوا اللَّهَ كَثِيرًا وَانْتَصَرُوا مِنْ بَعْدِ مَا
ظَلَمُوا وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٢٢٧﴾

وَمَا تَنْزَلَتْ بِهِ الشَّيْطَانُ ﴿٢١٠﴾ وَمَا
يُنْبِئِي هُمْ وَمَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٢١١﴾
إِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ لَمَعْزُولُونَ ﴿٢١٢﴾

210. "Wala Mashetani hawakuteremka nayo,

211. Wala haitakiwi kwao, na wala hawawezi.

212. Hakika hao wame-tengwa na kusikia".

Qur'ani lliteremshwa na Jibril عليه السلام wala sio Shetani

Allah تعالى Anatueleza kuhusu Kitabu Chake, ambacho hakifikiwi na upotovu mbele yake wala nyuma yake, kwani kimetere-mshwa na Mwenye Hekima, Msifiwa. Allah تعالى Anasema Qur'an imetere-mshwa na Roho muaminifu

Ruh (yaani Jibril عليه السلام) aliyewezeshwa na Allah تعالى. Allah تعالى Anasema:

وَمَا تَنْزَلَتْ بِهِ الشَّيْطَانُ ﴿٢١٠﴾

"Wala Mashetani hawakuteremka nayo."

Kisha Anatueleza kuwa haiwezekani Qur'an kuteremshwa na Mashetani kwa sababu tatu za msingi. Ya kwanza ni kuwa hawataki, kwa sababu maumbile yao ni kuharibu na kuwapotosha watu. Na Qur'an ina maneno yenye kuamrisha mema na kukataza maovu, na yenye kuleta mwangaza, uwongofu na dalili

kubwa. Ipo tofauti kubwa baina ya Qur'an na Shetani, kwani Allah تعالى Anasema:

وَمَا يَنْبَغِي لَهُمْ

“Wala haitakiwi kwao.”

وَمَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٢١٠﴾

“...na wala hawawezi.”

Hii ni kumaanisha hata wakitaka hawataweza kutekeleza hilo. Allah تعالى Anasema:

لَوْ أَنْزَلْنَا هَذَا الْقُرْآنَ عَلَىٰ جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُ خَاشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللَّهِ

“Lau kuwa Tumeteremsha hii Qur'ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeluona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Allah.” (59:21).

Baadaye Allah تعالى Anatueleza kuwa hata wakitaka na wakawa na uwezo wa kuichukukua na kuifikisha, pia hawataweza kutekeleza hilo, kwa kuwa wamezuiliwa kuisikia Qur'ani pale inapoteremshwa chini, kwani mbingu zimejaa walinzi na vimondo vinvavyowapiga kwa wakati ambao Qur'ani ilikuwa ikiteremshwa kwa Mtume Muhammad ﷺ. Hivyo, hakuna hata Shetani mmoja ambaye angeweza kusikia hata herufi moja ya Qur'ani, ili kusiwe na utata katika jambo hilo. Hii ni katika Rehema ya Allah تعالى kwa waja Wake, Kuilinda Shari'ah Yake, Kukipa nguvu Kitabu Chake na Mtume Wake.

Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Anasema:

إِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ لَمَعْزُولُونَ ﴿٢١١﴾

“Hakika hao wametengwa na kusikia.”

Kama Allah تعالى Alivyosema;

وَأَنَّا لَمَسْنَا السَّمَاءَ فَوَجَدْنَا فِيهَا رَبًّا لَّدُنَّهَا مُلَمَّتًا حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهَبًا ﴿٢١٢﴾ وَأَنَّا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا

مَقْعِدًا لِلسَّمْعِ ۗ فَمَنْ يَسْتَمِعِ الْآنَ يَجِدْ لَهُ شُهَابًا رَّصَدًا ﴿٢١٣﴾

“Nasi tulizigusa mbingu, na tukazona zimejaa walinzi wenye nguvu na vimondo. Na hakika tulikuwa tukikaa humo katika baadhi ya makao ili kusikiliza; lakini sasa anayesikiliza atakuta kimondo kinamvizia!”

Hadi Kauli Yake Allah:

أَمْ أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشْدًا ﴿٢١٠﴾

“Au Mola wao Mlezi anawatakia uwongofu.” (72:8-10).

فَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ فَتَكُونُ مِنَ الْمَعْدِيَةِ ﴿٢١١﴾ وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٢١٢﴾
 وَأَخْفِضْ جَنَاحَكَ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢١٣﴾ فَإِنْ عَصَوْكَ فَقُلْ إِنَّي بِرَبِّي
 مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢١٤﴾ وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٢١٥﴾ الَّذِي يَرِنُكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٦﴾
 وَتَقَلُّبُكَ فِي السُّجُودِ ﴿٢١٧﴾ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٢١٨﴾

213. “Basi usimuombe mungu mwingine pamoja na Allah ukawa miongoni mwa watakaoadhibiwa.

214. Na uwaonye jamaa zako waliokaribu nawe.

215. Na watwae kwa upole wanaokufuata miongoni mwa Waumini.

216. Na ikiwa watakuasi basi sema: Mimi najitenga mbali na hayo mnayoyatenda.

217. Na umtegemee Mtukufu Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu.

218. Ambaye Anakuona unaposimama,

219. Na mageuko yako kati ya wanaosujudu.

220. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

Amri ya Kuwaonya Jamaa wa Karibu

Hapa Allah تعالى Anamuamuru (Mtume Wake) Amuabudu Yeye Peke Yake, wala asimshirikishe na chochote, na Anamwambia kuwa yeyote atakaye mshirikisha basi Atamuadhibu. Kisha Anasema Aliyetukuka Kumuamuru Mtume Wake awaonye jamaa zake wa karibu, yaani wale wanaohusiana naye kwa karibu zaidi, na awaambie kuwa hakuna kitakachomuokoa yeyote miongoni mwao isipokuwa Imani yao kwa Mola wao Mlezi Aliyetukuka. Pia Akamuamuru awe mpole na laini kwa waliomfuata miongoni mwa waja wa Allah تعالى walioamini, na kuwakataa wale waliomuasi, bila kujali ni akina nani. Na kwa hiyo Akasema:

فَإِنْ عَصَوْكَ فَقُلْ إِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٣٦﴾

“Na ikiwa watakuasi basi sema: Mimi najitenga mbali na hayo mnayoyatenda.”

Hili ni onyo hasa ambalo halipingani na lile onyo la kijumla; bali hili ni katika sehemu yake, kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya hizi:

لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أُنذِرَ ءَابَاؤُهُمْ فَهُمْ غَافِلُونَ ﴿٣٦﴾

“Ili uwaonye watu ambao baba zao hawakuonywa, basi wao wamekuwa wenye kughafilika.” (36:6).

لِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا

“Ili uwaonye watu wa Makkah na walio pembeni mwake.” (42:7).

وَأُنذِرَ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْ يُخَشِّرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ

“Na waonye kwayo wanaoogopa kuwa watakusanywa kwa Mola wao Mlezi.” (6:51).

Amesema tena Aliyetukuka:

لِتُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ ۚ وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُدًّا ﴿٣٧﴾

“Ili uwabashirie kwayo wachamungu, na uwaonye kwayo watu wabishi.” (19:97).

Aidha Allah تعالى Amesema,

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“Ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia.” (6:19).

Kama pia Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَآلِنَارُ مَوْعِدُهُ

“Na anayemkataa katika makundi, basi moto ndio pahala pa miadi yao.” (11:17).

Kulingana na Hadithi katika Sahihi Muslim, Mtume ﷺ amesema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَا يَسْمَعُ بِي أَحَدٌ مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ يَهُودِيٍّ وَلَا نَصْرَانِيٍّ، ثُمَّ لَا يُؤْمِنُ بِي إِلَّا دَخَلَ النَّارَ»

“Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo Mikononi Mwake! Hakuna yeyote miongoni mwa mataifa haya – Mayahudi na Manaswara – atakayesikia kuhusu mimi kisha asiniamini isipokuwa ataingia Motoni.”¹

Zipo Hadithi nyingi sana zilizopokelewa kuhusiana na kuteremshwa kwa Aya hizi tukufu, hapa tutanukuu tu baadhi yake:

Imepokewa kwa Imamu Ahmad, Allah تعالى Amrehemu, kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Pindi Allah تعالى Alipoteremsha Aya hii:

وَأُنذِرَ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٢١٤﴾

“Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe.” (26:214).

Mtume ﷺ alikwenda Asw-Swafaa, akapanda juu yake kisha akanadi,

«يَا صَبَاحَاهُ»

“Enyi watu”.

¹ Muslim 1:134.

Watu wakajumuika karibu yake, baadhi yao wakija kwa hiyari yao na wengine wakituma wawakilishi wao. Mtume ﷺ akasema:

«يَا بَنِي عَبْدِ الْمُطَلِّبِ، يَا بَنِي فِهْرٍ، يَا بَنِي لُؤَيٍّ، أَرَأَيْتُمْ لَوْ أَخْبَرْتُمْ أَنَّ خَيْلًا بَسَّحَ
هَذَا الْجَبَلَ تُرِيدُ أَنْ تُغَيِّرَ عَلَيْكُمْ صَدَقْتُمْوَنِي؟»

“Enyi Bani ‘Abdul Mutwtwalib, enyi Bani Fihir, enyi Bani Lu’ayy! Munafikiria nini nikiwajulisha kuwa kipo kikosi cha farasi chini ya mlima huu wakiwa tayari kuwashambulia – je, mutaniamini?”

Wakasema: “Ndio”. Akasema:

«فَإِنِّي نَذِيرٌ لَكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ»

“Hakika mimi ni muonyaji kwenu kwa adhabu kubwa iliyo karibu.”

Hapo Abu Lahab akasema: “Mwana kuangamia kwa siku yote iliyobakia! Hukutuita isipokuwa kwa hili.” Allah تعالى Akateremsha:

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ۝

“Pana kuangamia mikono ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia.”¹

Imepokewa pia na Al-Bukhaariy, Muslim, At-Tirmidhiy na An-Nasaa’iy². Imepokewa na Imamu Ahmad kuwa Aishah رضي الله عنها amesema: “Ilipoteremka Aya hii:

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ۝

“Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe.”

Mtume ﷺ alisimama na kusema:

«يَا فَاطِمَةُ ابْنَةُ مُحَمَّدٍ، يَا صَفِيَّةُ ابْنَةُ عَبْدِ الْمُطَلِّبِ، يَا بَنِي عَبْدِ الْمُطَلِّبِ، لَا أَمْلِكُ
لَكُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا سَلُونِي مِنْ مَالِي مَا شِئْتُمْ»

¹ Ahmad 1:307.

² Fat-h al-Baari 8:206, Muslim 1:193, Tuhfatul al-Ahwadhi 9:296 na An-Nass’iy katika Al-Kubraa 6:526.

“Ewe Faatwimah bint Muhammad, ewe Swafiyah bint ‘Abdul Mutwtwalib, enyi Bani ‘Abdul-Mutwtwalib, siwezi kuwasaidia mbele ya Allah na chochote. Niombeni chochote katika mali yangu.”¹ Hii imepokewa na Muslim.²

Imepokewa na Imamu Ahmad kuwa Qabiiswah ibn Mukhaariq na Zuhayr ibn Amri walisema wakati iliposhuka Aya:

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٢١٠﴾

“Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe.”

Mtume ﷺ alipanda juu ya jabali pembeni mwa mlima na akaanza kuita:

«يَا بَنِي عَبْدِ مَنَاةٍ، إِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ، وَإِنَّمَا مَثَلِي وَمَثَلُكُمْ كَرَجُلٍ رَأَى الْعَدُوَّ فَذَهَبَ
يَرْبُأُ أَهْلَهُ يَخْشَى أَنْ يَسْبِقُوهُ، فَجَعَلَ يُنَادِي وَيُخَيِّفُ: يَا صَبَاحَاهُ»

“Enyi Bani ‘Abdi Manaf, hakika mimi ni muonyaji, na mfano wangu na wenu ni wa mtu anayemuona adui hivyo anakwenda kuwaokoa familia yake, akihofia kuwa huenda adui yule akawafikia kabla yake.” Akaanza kuita kwa nguvu, *“Enyi watu”³*. Pia ilinukuliwa na Muslim na An-Nasaa’iy⁴.

Na Kauli Yake:

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٢١١﴾

“Na umtegemee Mtukufu Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu.”

Katika mambo yenu yote, kwani Yeye Ndiye Msaidizi wako, Mwenye Kukuhifadhi, Mwenye Kukunusuru na Ndiye Mwenye Kulinyanyua neno lako. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

الَّذِي يَرَبُّكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٢﴾

“Ambaye Anakuona unaposimama.”

¹ Ahmad 6:187.

² Muslim 1:192.

³ Ahmad 5:60.

⁴ Muslim 1:193 na An-Nasaa’iy katika ***Al-Kubraa*** 6:423.

Yeye Ndiye Mwenye Kukutazama kwa kila kitu, kama Allah تعالى Alivyosema:

وَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا

“Na ingoje hukumu ya Mola wako Mlezi, kwani wewe uko mbele ya Macho Yetu.” (52:48).

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما:

الَّذِي يَرَبُّكَ حِينَ تَقُومُ

“Ambaye Anakuona unaposimama.”

Maana yake: Akiwa katika Swala.¹ Amesema ‘Ikrimah: Anamuona akiwa amesimama, amerukuu na akisujudu.² Na amesema Al-Hasan kuhusu Aya hii:

الَّذِي يَرَبُّكَ حِينَ تَقُومُ

“Ambaye Anakuona unaposimama.”

Maana yake: Ikiwa utaswali peke yako. Na amesema Adh-Dhahhaak:

الَّذِي يَرَبُّكَ حِينَ تَقُومُ

“Ambaye Anakuona unaposimama.”

Maana yake: Unapolala kitandani au unapokaa.³ Na akasema Qataadah:

الَّذِي يَرَبُّكَ

“Ambaye Anakuona.”

Ukiwa umesimama, umeketi na katika hali zote.⁴ Na Kauli Yake:

وَتَقَلُّبُكَ فِي السُّجُودِ

“Na mageuko yako kati ya wanaosujudu.”

¹ Al-Qurtwubiy 13:144.

² Atw-Twabariy 19:412.

³ Ad-Durr al-Manthuur 6: 330.

⁴ Abdur-Razzaq 3:77.

Amesema Qataadah:

الَّذِي يَرِنَاكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٨﴾ وَتَقْلُبُكَ فِي السَّجْدِ ۖ ﴿٢١٩﴾

“Ambaye Anakuona unaposimama. Na mageuko yako kati ya wanaosujudu”.

Akasema: “Katika Swala – Anakuona ukiswali peke yako na unaposwali katika jamaa.”¹ Na hii ni kauli na rai ya ‘Ikrimah, ‘Atwaa’ Al-Khuraasaniy na Hasan Al-Baswriy.² Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٢٢٠﴾

“Hakika Yeye Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

Maana yake: Mwenye Kusikia kauli za waja Wake, Mwenye Kujua harakati zao zote na utulivu wao. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا
إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ ۗ

“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo.” (10:61).

هَلْ أُنَبِّئُكُمْ عَلَىٰ مَن تَنَزَّلُ الشَّيْطَانُ ﴿٢١٨﴾ تَنَزَّلُ عَلَىٰ كُلِّ أَفَّاكٍ أَثِيمٍ ﴿٢١٩﴾ يُلْقُونَ السَّمْعَ
وَأَكْثُرُهُمْ كَذِبُونَ ﴿٢٢٠﴾ وَالشُّعْرَاءُ يَتَّبِعُهُمُ الْغَاوُونَ ﴿٢٢١﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّهُمْ فِي كُلِّ وَادٍ
يَهِيمُونَ ﴿٢٢٢﴾ وَأَنَّهُمْ يَقُولُونَ مَا لَا يَفْعَلُونَ ﴿٢٢٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
الصَّالِحَاتِ وَذَكَرُوا اللَّهَ كَثِيرًا وَانْتَصَرُوا مِنْ بَعْدِ مَا ظَلَمُوا ۗ وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ
مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٢٢٤﴾

¹ Ad-Durr Al-Manthuur 6:331.

² Atw-Twabariy 19:413.

221. "Je! Nikwambieni nani wanawashukia Mashetani?"

222. Wanamshukia kila mzushi mkubwa mwingi wa dhambi.

223. Wanawapelekea yale wanayoyasikia; na wengi wao ni waongo.

224. Na watungaji mashairi ni wapotofu ndio wanawafuata.

225. Je! Huwaoni kwamba wao wanatangatanga katika kila bonde?

226. Na kwamba wao husema wasiyoyatenda?

227. Isipokuwa wale walioamini, na wakatenda mema, na wakamkumbuka Allah kwa wingi, na wakajitetea wanapodhulumiwa. Na wanaodhulumu watakuja jua mgeuko gani watakaogeuka."

Kukanusha Uwongo wa Washirikina

Allah تعالیٰ Anasema kuwambia washirikina waliodai kuwa aliyokuja nayo Mtume si haki wala ukweli, na kuwa ni kitu alichozua yeye mwenyewe katika nafsi yake au kuwa ni kitu kutoka katika ndoto na kutoka kwa Majini. Allah تعالیٰ Anasema kuwa Mtume Wake yuko juu ya kauli zao na madai yao hayo ya uwongo. Na Qur'an ni uteremsho Wake na Wahyi kutoka Kwake, ulioteremshwa na Malaika mtukufu, muaminifu na mwenye nguvu. Wahyi huo haukutoka kwa mashetani, kwani wao hawana utashi wowote kwa jambo kama hili la Qur'ani tukufu, hakika ni si vingine wao huteremka kwa walio kama wao miongoni mwa wapiga bao na ramli walio waongo. Kwa kuzingatia hilo Allah تعالیٰ Amesema:

هَلْ أَنْتُمْ كُمْ

"Je! Nikwambieni?"

Maana yake: Niwapashe habari nyinyi. Kisha akasema:

عَلَىٰ مَنْ تَنْزَلُ الشَّيَاطِينُ ﴿٢٢٦﴾ تَنْزَلُ عَلَىٰ كُلِّ آفَّاكٍ أَثِيمٍ ﴿٢٢٧﴾

"Nani wanawashukia Mashetani? Wanamshukia kila mzushi mkubwa mwingi wa dhambi."

Hii ina maana muongo katika kauli, yake na mzushi aliyebobea.



“Mwingi wa dhambi.”

Ina maana mpotovu katika matendo na mkosefu wa maadili mazuri. Huyu ndiye mtu anayeteremkiwa na Shetani miongoni mwa wapiga bao na waongo wengine wenye kufanya madhambi. Kwani Mashetani pia ni waongo mafasiki.

يُلْقُونَ السَّمْعَ

“Wanawapelekea yale wanayoyasikia.”

Yaani, wanajaribu kusikiliza yanayosemwa mbinguni, na kujaribu kusikiliza ya ghaibu na kisha kuongeza juu yake uwongo mara mia moja na kuwaambia marafiki zao wa kibinadamu, ambao nao huwaambia wengine. Kisha watu huamini wanayosema kwa sababu ya ukweli wa jambo moja peke yake ambalo lilisikika kutoka mbinguni. Habari hii imesihi katika Hadithi iliyonukuliwa na Al-Bukhaariy kutoka kwa Aishah رضي الله عنها alisema: “Watu walimuuliza Mtume ﷺ kuhusu Makuhani (wapiga ramli), akasema:

«إِنَّهُمْ لَيُسَوِّئُونَ»

“Hakika wao hawana chochote”.

Wakasema: “Ewe Mtume wa Allah! Hakika wao wanasema mambo yanayotokea kweli.” Mtume ﷺ akasema :

«تِلْكَ الْكَلِمَةُ مِنَ الْحَقِّ يَخْطِفُهَا الْجِنِّي فَيَقْرُؤُهَا فِي أُذُنِ وَلِيِّهِ كَقَرْفَرَةِ الدَّجَاجِ،
فَيَخْلِطُونَ مَعَهَا أَكْثَرَ مِنْ مِائَةِ كَذْبَةٍ»

“Hilo ni neno ambalo Jini analichukua, kisha analirongonya katika sikio la rafiki yake kama mlio wa kuku, lakini anachanganya pamoja nalo uwongo mia moja.”¹

Imepokewa tena na Al-Bukhaariy kutoka Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kwamba Mtume ﷺ amesema:

¹ Fat-h al-Baariy 13:545.

«إِذَا قَضَىٰ اللَّهُ الْأَمْرَ فِي السَّمَاءِ ضَرَبَتْ الْمَلَائِكَةُ بِأَجْنِحَتِهَا خُضْعَانًا لِقَوْلِهِ، كَأَنَّهُا سِلْسَلَةٌ عَلَىٰ صَفْوَانٍ، فَإِذَا فُرِعَ عَنْ قُلُوبِهِمْ قَالُوا: مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ؟ قَالُوا [اللَّيْلِ قَالَ]: الْحَقُّ، وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ، فَسَمِعَهَا مُسْتَرْفِعُوا السَّمْعَ، وَمُسْتَرْفِعُوا السَّمْعَ هَكَذَا بَعْضُهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ - وَصَفَ سُفْيَانُ بِيَدِهِ، فَحَرَفَهَا وَبَدَّدَ بَيْنَ أَصَابِعِهِ - فَسَمِعُ الْكَلِمَةَ فَيُلْقِيهَا إِلَىٰ مَنْ تَحْتَهُ، ثُمَّ يُلْقِيهَا الْآخَرَ إِلَىٰ مَنْ تَحْتَهُ، حَتَّىٰ يُلْقِيهَا عَلَىٰ لِسَانِ السَّاجِرِ أَوْ الْكَاهِنِ، فَرُبَّمَا أَدْرَكَهُ الشَّهَابُ قَبْلَ أَنْ يُلْقِيَهَا، وَرُبَّمَا أَلْقَاهَا قَبْلَ أَنْ يَدْرِكَهُ، فَيَكْذِبُ مَعَهَا مِائَةً كَذِبِيَّةً، فَيَقَالُ: أَلَيْسَ قَدْ قَالَ لَنَا يَوْمَ كَذَا وَكَذَا: كَذَا وَكَذَا؟ فَيُصَدِّقُ بِتِلْكَ الْكَلِمَةِ الَّتِي سَمِعْتَ مِنَ السَّمَاءِ»

“Anapohukumu Allah jambo mbinguni, Malaika hupiga mbawa zao kwa kunyenyekea kwa kauli Yake hiyo kama kwamba ni nyororo zinazopigwa juu ya jabali. Pindi khofu inapopungua katika nyoyo zao, wanasema: “Amesema nini Mola wenu Mlezi?” Wanasema: “Ukweli. Naye Ndiye Aliye juu na Mkuu.” Wanalisikia wadokozi wa usikivu (yaani Majini), na wasikilizaji hawa na huwadokeza wengine hali inakuwa hivi baadhi yao juu ya wengine – hapo Sufyaan alionesha kwa kuushikilia mkono wake na kuvipambanua vidole vyake – wanaposikia hayo, wanalitupa (neni) hilo chini mmoja kwa mwengine, mpaka kufika kwa mchawi au mpiga bao. Wakati mwengine huenda wakapigwa na vimondo kabla ya kulitupa (au kulifikisha), au analipitisha kabla ya kupigwa, naye huongeza uwongo ndani yake mia moja. Hivyo husemwa: “Je, hakutuambia siku kadhaa na kadhaa? Akasadikiwa kwa neno hilo ambalo lilisikiwa kutoka mbinguni.”¹

Al-Bukhaariy Amepokea kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الْمَلَائِكَةَ تَحَدَّثُ فِي الْعَتَانِ - وَالْعَتَانُ: الْعَمَامُ - بِالْأَمْرِ [يَكُونُ] فِي الْأَرْضِ، فَتَسْمَعُ الشَّيَاطِينُ الْكَلِمَةَ، فَتَقْرَأُهَا فِي أُذُنِ الْكَاهِنِ كَمَا تَقْرَأُ الْقَارُورَةَ، فَتَرِيدُونَ مَعَهَا مِائَةً كَذِبِيَّةً،

“Hakika Malaika wanazungumza kwenye mawingu kuhusu jambo fulani katika ardhi, na wanasikia Mashetani neno kutoka kwao. Nao

¹ Fat-h ul-Baariy 8:398.

hurongonya katika sikio la mpiga ramli kama maji yanavyomiminwa kutoka chupa ya glasi, lakini yeye huongeza uwongo mia moja.”¹

Kukanusha Dai kuwa Mtume ﷺ Alikuwa Mshairi

Kwa Kauli Yake Aliyetukuka:

وَالشُّعْرَاءُ يَتَّبِعُهُمُ الْغَاوُونَ ﴿٢١٠﴾

“Na watungaji mashairi ni wapotofu ndio wanawafuata”.

Imepokewa na ‘Aliy ibn Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Makafiri wanawafuata wapotovu miongoni mwa wanadamu na Majini.”² Na hiyo ndiyo ilikuwa rai ya Mujaahid, ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam na wengineo.³ Amesema ‘Ikrimah: “Washairi wawili walikuwa wakibezana na kufanyiana dhihaka, hivyo kundi moja la watu likawa linamuunga mkono mmoja wao na kundi jengine likimuunga mpinzani wake. Hapo Allah تعالى Aliteremsha Aya hii:

وَالشُّعْرَاءُ يَتَّبِعُهُمُ الْغَاوُونَ ﴿٢١٠﴾

“Na watungaji mashairi ni wapotofu ndio wanawafuata.”⁴

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَلَمْ تَرَ أَنَّهُمْ فِي كُلِّ وَادٍ يَهِيمُونَ ﴿٢١١﴾

“Je! Huwaouni kwamba wao wanatangatanga katika kila bonde?”

‘Aliy ibn Abi Twalhah amepokea kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Wao hushiriki katika kila aina ya upuuzi.”⁵ Na amepokea Adh-Dhahhaak kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Wao wanajiingiza katika kila fani ya maneno na mazungumzo.”⁶ Na hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid na wengineo.⁷ Na Kauli Yake Aliyetukuka:

¹ Al-Bukhaariy 3288.

² Atw-Twabariy 19:416.

³ Atw-Twabariy 19:415,416.

⁴ Ad-Durr al-Manthuur 6:323.

⁵ Atw-Twabariy 19:417.

⁶ Ad-Durr al-Manthuur 6:334.

⁷ Atw-Twabariy 19:417.

وَأَنْتُمْ يَقُولُونَ مَا لَا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦٦﴾

“Na kwamba wao husema wasiyoyatenda?”

Amepokea Al-Awfiy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema kuwa wakati wa Mtume ﷺ, watu wawili, mmoja kutoka katika Answaar na mwengine kutoka kabila jengine, walikuwa wakibezana na kufanyiana dhahaka. Kila mmoja alikuwa akishangiliwa na kundi la watu wake, ambao walikuwa ni wajinga miongoni mwao. Hapo Allah تعالى Alisema:

وَالشُّعْرَاءُ يَتَّبِعُهُمُ الْغَاوُونَ ﴿٣٦٧﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّهُمْ فِي كُلِّ وَادٍ يَهِيمُونَ ﴿٣٦٨﴾ وَأَنْتُمْ يَقُولُونَ مَا لَا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦٩﴾

“Na watungaji mashairi ni wapotofu ndio wanawafuata. Je! Huwaoni kwamba wao wanatangatanga katika kila bonde? Na kwamba wao husema wasiyoyatenda?”

Na muradi wa haya ni kuwa Mtume ﷺ aliyeteremshiwa Qur’ani hii si mpiga bao wala mshairi, kwa sababu hali yake ilikuwa tofauti kabisa na hali yao. Kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya hizi:

وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشِّعْرَ وَمَا يَنْبَغِي لَهُ ۚ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْآنٌ مُّبِينٌ ﴿٣٧٠﴾

“Wala Hatukumfundisha mashairi, wala haiwi kwake (kuwa mtunga mashairi). Haikuwa Qur’ani ila ukumbusho na Kitabu kibainishacho.” (36:69)

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٣٧١﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا تُوْمِنُونَ ﴿٣٧٢﴾ وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٣٧٣﴾ تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٧٤﴾

“Kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe wa Allah mwenye hishima kubwa. Wala si kauli ya mtunga mashairi. Ni machache sana mnayoyaamini. Wala si kauli ya mchawi kama mnavyodai. Ni kidogo sana kuwaidhika kwenu. Ni uteremsho utokao kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.” (69:40-43).

¹ Atw-Twabariy 19:416.

Washairi wa Kiislamu hawahusiki na maovu hayo:

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Isipokuwa wale walioamini, na wakatenda mema.”

Amepokea Muhammad ibn Ishaq رحمه الله تعالى kutoka kwa Yazid ibn ‘Abdallah ibn Qusaytw kuwa Abil Hasan Saalim Al-Barrad, mwachwa huru wa Tamiim Ad-Daariy amesema ilipoteremka Aya hii:

وَالشُّعْرَاءُ يَتَّبِعُهُمُ الْغَاوُونَ ﴿٢٢٤﴾

“Na watungaji mashairi ni wapotofu ndio wanawafuata.” (26:224).

Hapo Hasaan ibn Thaabit, ‘Abdullah ibn Rawaahah na Ka’b ibn Maalik رضي الله عنهم walikwenda kwa Mtume ﷺ wakiwa wanalia. Wakasema: “Hakika Allah تعالى Alijua Alipoteremsha Aya hii kuwa sisi ni watungaji mashairi.” Hapo Mtume ﷺ akawasomea:

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Isipokuwa wale walioamini, na wakatenda mema.”

Kisha Mtume ﷺ akasema:

وَأَنَّهُمْ

‘(Hii inamaanisha) nyinyi.’

Pia:

وَذَكَّرُوا اللَّهَ كَثِيرًا

“Na wakamkumbuka Allah kwa wingi.”

Mtume ﷺ Akasema:

وَأَنَّهُمْ

‘(Hii inamaanisha) nyinyi.’

Mtume ﷺ akasema,

وَأَنتَصَرُوا مِن بَعْدِ مَا ظَلَمُوا

“Na wakajitetea wanapodhulumiwa.”

Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى na Ibn Jariir رحمه الله تعالى wamenukuu katika riwaya ya Ibn Ishaq.¹ Lakini Surah hii imeteremka Makkah, itakuwaje sababu ya kuteremshwa kwake ni washairi wa Ki-Answaar? Jambo hilo ni lazima liangaliwe, kwani Hadithi zinazotajwa ni *Mursal*,² hivyo haziwezi kutegemewa. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Lakini kutojumlishwa huku. Pia kunawahusu washairi wa Ki-answaar na wengineo hadi washairi wa Kijahiliya waliojiingiza katika kuushutumu Uislamu na wafuasi wake, baadaye wakatubia na kurudi kwa Allah تعالى kwa wingi sana, ili kufuta yale mabaya waliyofanya hapo awali. Hakika walianza kuusifu Uislamu na wafuasi wake ili kufuta yale matusi waliyoyasema, kama mshairi Abdullah Ibn Azziba'ra alitoa shairi lifuatalo baada ya kusilimu:

Ewe Mtume wa Allah, hakika ulimi wangu
utajaribu kufuta maovu niliyofanya,
wakati nilipomfuata Shetani katika miaka ya upotovu.
Na yeyote anayefuata nyayo zake basi hakika amelaaniwa.

Hivyo hivyo, abu Sufyaan ibn Al-Haarith ibn 'Abdul-Mutwtwalib alikuwa ni miongoni mwa watu waliokuwa na uadui mkubwa sana na Mtume ﷺ japokuwa alikuwa ni binamu yake na alikuwa akimdhihaki kupita wote. Lakini aliposilimu, hakuna aliyekuwa akipendwa na yeye zaidi kuliko Mtume ﷺ. Alianza kumsifu Mtume ﷺ baada ya kumtukana huku nyuma. Na kumfanya rafiki baada ya huku nyuma alikuwa adui yake. Allah تعالى Anasema:

وَأَتَتْصَرُّوا مِنْ بَعْدِ مَا ظَلَمُوا

“Na wakajitetea wanapodhulumiwa.”

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: “Waliwajibu makafiri ambao walikuwa wakiwadhihaki Waumini kwa mashairi.”¹

Na hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya Mujahid, Qatadah na wengineo². Pia imenukuliwa katika Hadithi Sahihi kuwa Mtume ﷺ alimwambia Hassan:

¹ Atw-Twabariy 19:420.

² Hadithi *Mursal* ni ile ambayo *Tabii* anaiunganisha moja kwa moja na Mtume ﷺ, bila ya kutamja Swahaba katikati yake (mfasiri).

³ Atw-Twabariy 19:420.

⁴ Atw-Twabariy 19:419-420.

«أَهْجُهُمْ»

“Wadhihaki wao katika mashahiri.”

Au pia alisema:

«هَاجِهِمْ وَجِبْرِيلُ مَعَكَ»

“Wadhihaki wao na Jibril yu pamoja nawe.”¹

Imamu Ahmad amemnukuu Ka'b ibn Maalik رضي الله عنه akimuuliza Mtume ﷺ: “Allah تعالى Ameteremsha Aliyoteremsha kuhusu washairi.” Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الْمُؤْمِنَ يُجَاهِدُ بِنَفْسِهِ وَلِسَانِهِ، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَكَأَنَّ مَا تَرْمُونَهُمْ بِهِ نَضْحُ
النَّبْلِ»

“Hakika Muumini anapigana Jihadi kwa upanga na ulimi wake. Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Ni kama kwamba mnayoyatupa ni mishale.”²

Anamalizia Aliyetukuka kwa Kusema:

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٢٧﴾

“Na wanaodhulumu watakuja jua mgeuko gani watakaogeuka”.

Hii inafanana na ile Aya inayosema:

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ

“Siku ambayo hautawafaa madhalimu udhuru wao.” (40:52).

Kulingana na Hadithi Sahihi, Mtume ﷺ amesema:

«إِيَّائِكُمْ وَالظُّلْمَ، فَإِنَّ الظُّلْمَ ظُلُمَاتٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Tahadharini na dhulma, kwani dhulma itakuwa ni viza Siku ya Kiyama.”³

¹ Fathul- Bari 6:351.

² Ahmad 2:106. Pia Muslim 2578 kutoka kwa Jaabir. Tazama *Riyaadh Swalihin* Hadithi na 203.

³ Atw-Twabariy 19:428.

Qataadah ibn Di'aamah amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ ﴿٢١٧﴾

“Na wanaodhulumu watakujajua mgeuko gani watakaogeuka.”

Hii inahusu washairi na wengineo.

Huu ndio Mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Ash-Shu'araa'*. Sifa Njema zote ni za Allah تعالى, Mola Mlezi wa viumbe vyote.

* * *

Tafsiri ya Suratu An-Naml

Sura ya 27

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Kurehemu

سُورَةُ النَّامِلِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

طس ٤ تِلْكَ آيَاتُ الْقُرْآنِ وَكِتَابٍ مُّبِينٍ ٥ هُدًى وَبُشْرَى لِلْمُؤْمِنِينَ ٦ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ٧ إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ زَيْنًا هُمْ أَعْمَلُهُمْ فَهُمْ يَعْمَهُونَ ٨ أُولَئِكَ الَّذِينَ هُمْ سُوءُ الْعَذَابِ وَهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمْ الْأَخْسَرُونَ ٩ وَإِنَّكَ لَتَلْقَى الْقُرْآنَ مِنْ لَدُنِّ حَكِيمٍ عَلِيمٍ ١٠

طس ٤ تِلْكَ آيَاتُ الْقُرْآنِ وَكِتَابٍ مُّبِينٍ ٥ هُدًى وَبُشْرَى لِلْمُؤْمِنِينَ ٦ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ٧ إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ زَيْنًا هُمْ أَعْمَلُهُمْ فَهُمْ يَعْمَهُونَ ٨ أُولَئِكَ الَّذِينَ هُمْ سُوءُ الْعَذَابِ وَهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمْ الْأَخْسَرُونَ ٩ وَإِنَّكَ لَتَلْقَى الْقُرْآنَ مِنْ لَدُنِّ حَكِيمٍ عَلِيمٍ ١٠

1. Twa Siin. Hizi ni Ayah za Qur'ani na Kitabu kinachobainisha;
2. Uwongofu na bishara kwa Waumini,
3. Ambao wanashika Sala, na wanatoa Zaka, na akhera wana yakini nayo.
4. Kwa hakika wale wasioamini Akhera Tumewapambia vitendo vyao, kwa hivyo wanatangatanga ovyo.

5. Hao ndio watapata adhabu mbaya kabisa, na hao katika Akhera ndio watapata khasara zaidi.

6. Na hakika wewe unafundishwa Qur’ani inayotoka Kwake Mwenye Hikima, Mwenye Kujua.”

Qur’ani ni Uwongofu na Bishara Njema kwa Waumini, ni Onyo kwa Makafiri
Yametangulia maelezo katika mwanzo wa *Suratul Baqarah* kuhusu herufi za kukata. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

تِلْكَ آيَاتُ الْقُرْآنِ وَكِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿١﴾

“Hizi ni Ayah za Qur’ani na Kitabu kinachobainisha.”

Maana yake: Hizo ni Aya nyingi zenye kubainisha na zilizo wazi kabisa hazina utata wa aina yoyote.

هُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٢﴾

“Uwongofu na bishara kwa Waumini.”

Maana yake: Hakika wanaopata uwongofu na bishara kutoka kwa Qur’ani ni wale wenye kuamini, kuifuata na kuisadiki na kutekeleza yaliyo ndani yake, hivyo, akasimamisha Swala za Faradhi, akatoa Zaka, akawa na yakini kwa makazi ya Akhera, ufufuo baada ya mauti na jaza kwa amali alizotekeleza mja, kheri na shari yake na Pepo na Moto. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءً وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقْرٌ

“Sema: Qur’ani hii ni uwongofu na poza; kwa wale wasioamini umo uzito katika masikio yao.” (41:44).

Amesema tena Aliyetukuka:

لِتُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُدًّا ﴿٣٧﴾

“Ili uwabashirie kwayo wachamungu, na uwaonye kwayo watu wabishi.” (19:97).

Kwa hiyo Akasema hapa:

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ

“Kwa hakika wale wasioamini Akhera.”

Maana yake: Wanaikadhibisha na wanaiona iko mbali kufika kwake. Allah تعالى Anaendelea Kusema:

زَيْنًا هُمْ أَعْمَلَهُمْ فَهُمْ يَعْمَهُونَ ﴿٦﴾

“Tumewapambia vitendo vyao, kwa hivyo wanatangatanga ovyo.”

Hakika ni kuwa wanayaona ni mema yale wanayoyatenda na Tukawakunjulia katika madhambi yao na vishawishi vyao wakiwa wanatangatanga katika upotovu wao. Hii ilikuwa ni jaza kwa waliyokadhibisha katika ile nyumba ya akhera. Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوْلَ مَرَّةٍ

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza.” (6:110).

Anasema Aliyetukuka:

أُولَئِكَ الَّذِينَ هُمْ سُوءُ الْعَذَابِ

“Hao ndio watapata adhabu mbaya kabisa.”

Maana yake: Hapa duniani na kesho Akhera. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمُ الْآخْسَرُونَ ﴿٧﴾

“Na hao katika Akhera ndio watapata hasara zaidi.”

Maana yake: Hakuna mwengine yeyote mbali na wao miongoni mwa watu watakaokusanywa, watapoteza nafsi zao na mali yao.

Na Kauli Yake تعالى:

وَإِنَّكَ لَتَلْقَى الْقُرْآنَ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ عَلِيمٍ ﴿٨﴾

“Na hakika wewe unafundishwa Qur’ani inayotoka Kwake Mwenye Hikima, Mwenye Kujua.”

Hii ina maana,

وَإِنَّكَ

“Na hakika wewe.”

Ewe Muhammad. Amesema Qataadah:

لَتُؤَلِّقِي

“Unafundishwa.”

Maana yake: Unachukua:

الْقُرْآنَ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ عَلِيمٍ ﴿٦﴾

“Qur’ani inayotoka Kwake Mwenye Hikima, Mwenye Kujua.”

Maana yake: Kutoka kwa Mwenye Hikima, Mjuzi. Hii maana yake, Yeye ni Mwenye Hikima katika Amri Zake na Makatazo Yake, Mwenye Kujua kila jambo kubwa au dogo. Asemayo ni kweli timilifu. Hukumu Yake ni ya uadilifu uliotimia. Kama Alivyosema:

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

“Na yametimia Maneno ya Mola wako Mlezi kwa kweli na uadilifu.”

(6:115).

* * *

إِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِأَهْلِيهِ إِنِّي آنستُ نَارًا سَقَاتِيكُمْ مِّنْهَا بِخَبْرٍ
 أَوْ آتِيكُمْ بِشِهَابٍ قَبَسٍ لَّعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٧﴾ فَلَمَّا
 جَاءَهَا نُودِيَ أَنْ بُورِكَ مَن فِي النَّارِ وَمَنْ حَوْلَهَا
 وَسُبْحٰنَ اللَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٨﴾ يَمْوَسَىٰ إِنَّهُ أَنَا اللَّهُ
 الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٩﴾ وَأَلْقَىٰ عَصَاكَ ﴿١٠﴾ فَلَمَّا رَأَاهَا تَهْتَزُّ كَأَنَّهَا
 جَانٌّ وَلَّىٰ مُدْبِرًا وَلَمْ يُعَقِّبْ يَمْوَسَىٰ لَا تَخَفْ إِنِّي لَا
 أَخَافُ لَدَىٰ الْمُرْسَلُونَ ﴿١١﴾ إِلَّا مَن ظَلَمَ ثُمَّ بَدَّلَ حُسْنًا
 بَعْدَ سُوءٍ فَإِنِّي غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾ وَأَدْخَلَ يَدَكَ فِي جَيْبِكَ
 تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِن غَيْرِ سُوءٍ ۗ فِي تِسْعِ آيَاتٍ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ
 وَقَوْمِهِ ۗ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَسِقِينَ ﴿١٣﴾ فَلَمَّا جَاءَهُمْ
 آيَاتُنَا مُبْصِرَةً قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿١٤﴾ وَجَحَدُوا
 بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا ۗ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ
 عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٥﴾

إِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِأَهْلِيهِ إِنِّي آنستُ نَارًا سَقَاتِيكُمْ مِّنْهَا بِخَبْرٍ
 أَوْ آتِيكُمْ بِشِهَابٍ قَبَسٍ لَّعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٧﴾ فَلَمَّا
 جَاءَهَا نُودِيَ أَنْ بُورِكَ مَن فِي النَّارِ وَمَنْ حَوْلَهَا
 وَسُبْحٰنَ اللَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٨﴾ يَمْوَسَىٰ إِنَّهُ أَنَا اللَّهُ
 الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٩﴾ وَأَلْقَىٰ عَصَاكَ ﴿١٠﴾ فَلَمَّا رَأَاهَا تَهْتَزُّ كَأَنَّهَا
 جَانٌّ وَلَّىٰ مُدْبِرًا وَلَمْ يُعَقِّبْ يَمْوَسَىٰ لَا تَخَفْ إِنِّي لَا
 أَخَافُ لَدَىٰ الْمُرْسَلُونَ ﴿١١﴾ إِلَّا مَن ظَلَمَ ثُمَّ بَدَّلَ حُسْنًا
 بَعْدَ سُوءٍ فَإِنِّي غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾ وَأَدْخَلَ يَدَكَ فِي
 جَيْبِكَ تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِن غَيْرِ سُوءٍ ۗ فِي تِسْعِ آيَاتٍ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَقَوْمِهِ ۗ

إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَسِقِينَ ﴿١٣﴾ فَلَمَّا جَاءَهُمْ آيَاتُنَا مُبْصِرَةً قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿١٤﴾ وَجَحَدُوا بِهَا
 وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا ۗ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٥﴾

7. (Kumbuka) Musa alipowaambia ahali zake: Hakika nimeona moto, nitakwenda nikuleteeni khabari, au nitakuleteeni kijinga kinachowaka ili mpate kuota moto.

8. Basi alipofika ilinadiwa: Amebarikiwa aliomo katika moto huu na walioko pembezoni mwake. Na Ametakasika Allah, Mola Mlezi wa walimengu wote.

9. Ewe Musa! Hakika Mimi Ndiye Allah, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

10. Na itupe fimbo yako! Alipoiona ikitikisika kama nyoka, aligeuka nyuma wala hakungoja. Ewe Musa! Usikhofu! Hakika hawakhofu mbele Yangu Mitume.

11. Lakini aliyedhulumu, kisha akabadilisha wema baada ya ubaya, basi Mimi ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

12. Na ingiza mkono wako katika mfuko wako, utatoka weupe bila ya maradhi. Na katika Ishara tisa za kumpelekea Firauni na kaumu yake. Hakika hao walikuwa watu waovu.

13. Basi zilipowafikia Ishara Zetu hizo zenye kuonyesha, wakasema: Huu ni uchawi dhahiri.

14. Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo. Basi angalia ulikuwaje Mwisho wa mafisadi."

Kisa cha Musa عليه السلام na Mwisho wa Firauni

Hapa Allah تعالى Anamwambia Mtume Wake Muhammad ﷺ kuhusu yaliyomfikia Musa عليه السلام, jinsi Allah تعالى Alivyomchagua, Akazungumza naye, Akamuokoa na Akampatia miujiza mikubwa ya ajabu na dalili za nguvu. Alimtuma kwa Firauni na watu wake, lakini walikanusha dalili, wakakufuru na kwa kiburi walikataa kumfuata. Akasema Aliyetukuka:

إِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِأَهْلِيهِ

“(Kumbuka) Musa alipowaambia ahali zake.”

Kumbuka pale Musa عليه السلام alipokuwa anasafiri na familia yake na akapotea njia. Wakati huo ulikuwa ni usiku, katika kiza. Musa عليه السلام akaona pembezoni mwa mlima moto, maana akauona moto unawaka kwa kung'aa, hapo akasema kuwaambia ahli zake:

إِنِّي ءَأَنْتُمْ نَارًا سَعَاتِكُمْ مِّنْهَا يُخْرِجُ

“Hakika nimeona moto, nitakwenda nikuleteeni khabari.”

Kuhusu njia tutakayochukua.

أَوَّاتِيكُمْ بِشِهَابٍ قَبَسٍ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٧﴾

“Au nitakuleteeni kijinga kinachowaka ili mpate kuota moto.”

Kumaanisha kuwa kitawapa joto. Hiyo ikawa ni kama alivyosema kwani alikuja na habari kubwa na akapata ndani yake nuru kubwa. Kwa hiyo Akasema تعالى:

فَلَمَّا جَاءَهَا نُودِيَ أَنْ بُورِكَ مَنْ فِي النَّارِ وَمَنْ حَوْلَهَا

“Basi alipofika ilinadiwa: Amebarikiwa aliomo katika moto huu na walioko pembezoni mwake.”

Hii inamaanisha alipokuja karibu, akaona mandhari adhimu yenye kutisha, kwani moto ulikuwa unawaka kwenye kichaka cha chanikiwiti. Moto huo ulikuwa unazidi kung’aa na kichaka kilizidi kuwa kijani na kizuri. Hapo alinyanyua kichwa chake, na kuona kuwa mwangaza wake umeunganishwa na mawingu ya mbinguni. Ibn ‘Abbaas na wengine رضي الله عنهم wanasema: “Huo haukuwa moto, bali nuru yenye kung’ara”. Kulingana na riwaya nyingine ya Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما anasema kuwa hiyo ilikuwa ni Nuru ya Mola Mlezi wa viumbe vyote.¹ Nabii Musa عليه السلام alisimama kwa kustaajabu kwa alivyokuwa akiona, na hapo:

نُودِيَ أَنْ بُورِكَ مَنْ فِي النَّارِ وَمَنْ حَوْلَهَا

“Aliitwa: Amebarikiwa aliomo katika moto huu.”

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما anasema: “Ametakasika.”²

وَمَنْ حَوْلَهَا

“Na walioko pembezeni mwake.”

Maana yake: Malaika. Amesema hivyo Ibn ‘Abbaas, ‘Ikrimah, Said ibn Jubayr, al-Hasan na Qataadah رضي الله عنهم.³

¹ Atw-Twabariy 19:428

² Atw-Twabariy 19:428.

³ Atw-Twabariy 19:429, Al-Muharrar Al-Wajiz 4:250, Ad-Durr Al-Manthuur 6:341

Na Kauli Yake:

وَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧﴾

“Na Ametakasika Allah, Mola Mlezi wa walimWengu wote.”

Allah تعالى Ambaye kwamba Anafanya Anavyotaka na hakuna chochote kinachofanana Naye katika viumbe Vyake. Hakuna Alichokiumba kinachoweza kumdiriki, Naye Ndiye Aliye juu, Mtukufu na Aliye Mkuu, Ambaye Hafanani kabisa na Alivyoviumba. Mbingu na ardhi haviwezi kumdhibiti Yeye, bali Yeye ni Mmoja tu, Anayestahiki Kukusudiwa, Anayejitosheleza, ambaye hawezi kulinganishwa na viumbe Vyake. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

يَمْوَسَىٰ إِنَّهُ أَنَا اللَّهُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٨﴾

“Ewe Musa! Hakika Mimi ndiye Allah, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Anamweleza kuwa Yule anayezungumza Naye ni Mola Wake Mlezi, Allah تعالى, Mwenye Nguvu, Ambaye Ametiisha kila kitu na Kuvishinda, Mwenye Hekima katika Kauli na Vitendo Vyake. Baada ya hayo, Alimuamuru atupe fimbo yake iliyokuwa mikononi mwake, ili Amuoneshe dalili za wazi kabisa kuwa Yeye Ndiye Mwenye Uweza wa Kufanya kila kitu, Atakavyo. Pindi Musa عليه السلام alipotupa fimbo yake, iligeuka na kuwa joka kubwa linalotisha, ambalo lilikuwa linakwenda kasi sana pamoja na ukubwa wake. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

فَلَمَّا رَأَاهَا تَهْتَزُّ كَأَنَّهَا جَانٌّ

“Alipoiona ikitikisika kama nyoka.”

Jaan ni aina ya nyoka anayekwenda kwa kasi mno na mwepesi sana. Musa عليه السلام alipoona hayo kwa macho yake:

وَلَّىٰ مُدَبِّرًا لَّمَّا يُعَقِّبْ

“Aligeuka nyuma wala hakungoja.”

Maana: Hakutazama nyuma, kwani aliogopa. Hapo aliambiwa:

يَمْوَسَىٰ لَا تَخَفْ إِنِّي لَا يَخَافُ لَدَى الْمُرْسَلُونَ ﴿٩﴾

“Ewe Musa! Usikhofu! Hakika hawakhofu mbele Yangu Mitume.”

Hii ina maana ya, usihofu kwa unayoyaona, kwani Mimi Nimekuchagua wewe kuwa Mtume ﷺ na nitakufanya wewe kuwa Nabii mkubwa. Na Kauli Yake:

إِلَّا مَنْ ظَلَمَ ثُمَّ بَدَّلَ حُسْنًا بَعْدَ سُوءٍ فَإِنِّي غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٤﴾

“Lakini aliyedhulumu, kisha akabadilisha wema baada ya ubaya, basi Mimi ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.

Huku ni kuwavua na kuwatoa aina ya watu waliojitenga. Hii ni bishara njema kwa wanadamu wote kuwa yeyote yule aliyefanya dhambi kisha akaliacha, akatubia na kurudi kwa Allah تعالى, hakika Allah تعالى Atakubali toba yake, kama Alivyosema:

وَإِنِّي لَغَفَّارٌ لِّمَنْ تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ثُمَّ اهْتَدَىٰ ﴿٨٢﴾

“Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anayetubia, na akaamini na akatenda mema, tena akaongoka.” (20:82).

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ

“Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake,...” (4:110).

Na Aya katika masiala haya ni nyingi sana. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَدْخَلَ يَدَكَ فِي جَيْبِكَ تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ

“Na ingiza mkono wako katika mfuko wako, utatoka weupe bila ya maradhi.”

Hii ni ishara nyingine na dalili adhimu kwa Uweza wa Allah تعالى Kufanya Atakavyo. Huu pia ni uthibitisho wa ukweli wa aliyepewa muujiza huo. Allah تعالى Alimuamuru atie mkono wake kwenye upenyo wa nguo yake, naye alipoutia mkono wake na kuutoa tena, ulitoka ukiwa mweupe wenye kung'aa kama kwamba ulikuwa ni kipande cha mwezi au mwako unaong'ara wa radi. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فِي تِسْعِ آيَاتٍ

“Ni katika ishara tisa”.

Maana yake: Ishara hizi mbili kati ya miujiza tisa ambazo kwazo Nitakusaidia nazo na Nitazijaalia kuwa ni dalili kwako. Akaendelea:

إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَقَوْمِهِ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٢٧﴾

“Za kumpelekea Firauni na kaumu yake. Hakika hao walikuwa watu waovu.”

Hizi ndizo zilikuwa ishara tisa ambazo kwazo Allah تعالى Amesema:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ تِسْعَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ

“Na kwa hakika Tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi.” (17:101).

Kama tulivyotangulia kuelezea hapo nyuma.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَلَمَّا جَاءَهُمْ آيَاتُنَا مُبْصِرَةً

“Basi zilipowafikia Ishara Zetu hizo zenye kuonesha.”

Maana yake: Bayana, wazi na dhahiri kabisa,

قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٢٨﴾

“ Wakasema: Huu ni uchawi dhahiri.”

Hivyo nao wakataka kuupinga kwa uchawi wao, lakini wakashindwa na wakarudi wakiwa wametahayari.

وَجَحَدُوا بِهَا

“Na wakazikataa.”

Maana yake: Kwa kutamka.

وَأَسْتَقْبَلَتْهَا أَنْفُسُهُمْ

“Na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo.”

Maana yake: Walitambua ndani ya nafsi zao kuwa huo ni ukweli kutoka kwa Allah تعالى, lakini waliukataa, wakakaidi na wakajivuna,

ظُلْمًا وَعُلُوًّا

“Kwa dhulma na kujivuna.”

Hii inamaanisha walijidhulumu nafsi zao kwa sababu hii ndiyo ilikuwa tabia yao mbaya walioizoea. Na wakajivuna, yaani walijawa na kiburi katika kuifuata haki. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

فَأَنْظِرْ كَيْفَ كَانَ عَنقَبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤﴾

“Basi angalia ulikuwaje Mwisho wa mafisadi.”

Tazama ewe Muhammad jinsi ulivyokuwa mwisho wa mambo yao kwa kuangamizwa na Allah تعالى na kugharikishwa kila mmoja wao kwa asubuhi moja pekee. Nukta muhimu ya kisa hiki ni: Tahadharini enyi mnaomkadhibisha Muhammad ﷺ na kukanusha yale aliyokuja nayo kutoka kwa Mola wake Mlezi, msije mkapatikanwa na yaliyowakumba wao kwa njia moja au nyingine. Hakika ni kuwa Muhammad ﷺ ni mtukufu na mkubwa kuliko Musa عليه السلام, na dalili zake zina nguvu na uzito mkubwa kuliko dalili alizopatiwa Musa عليه السلام, kwani dalili alizopewa yeye na Allah تعالى zimechanganywa kwa kuwepo kwake na maadili yake makuu kabisa. Kungezeza hayo ni kuwa Mitume waliotangulia walitoa bishara ya kuja kwake na kuchukua ahadi kutoka kwa watu wao kuwa wakikutana naye watamfuata. Iwe juu yake bora ya Baraka na amani kutoka kwa Mola wake Mlezi.

* * *

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ عِلْمًا ۗ وَقَالَ أَحْمَدُ لِلَّهِ الَّذِي
فَضَّلَنَا عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾ وَوَرِثَ سُلَيْمَانُ
دَاوُدَ ۗ وَقَالَ يَتَاءَتِيهَا النَّاسُ غُلْمًا مِّنْطِقِ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا مِنْ
كُلِّ شَيْءٍ ۗ إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَضْلُ الْأَمِينُ ﴿١٦﴾ وَحِشْرَ
لِسُلَيْمَانَ جُنُودَهُ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ وَالطَّيْرِ فَهُمْ يُوزَعُونَ
﴿١٧﴾ حَتَّىٰ إِذَا أَتَوْا عَلَىٰ وَادِ النَّمْلِ قَالَتْ نَمْلَةٌ يَتَاءَتِيهَا
النَّمْلُ آذْخُلُوا مَسَكِنَكُمْ لَا تَحْطِمَنَّكُمْ سُلَيْمَانُ
وَجُنُودُهُ وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٨﴾ فَتَبَسَّ سَاحِجًا مِّنْ
قَوْلِهَا وَقَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ
عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَدْخِلْنِي
بِرَحْمَتِكَ فِي عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ ﴿١٩﴾ وَتَفَقَّدَ الطَّيْرَ
فَقَالَ مَا لِيَ لَأَ أَرَى الْهَدْيَ أَمْ كَانَ مِنَ الْغَائِبِينَ ﴿٢٠﴾
لَأُعَذِّبَنَّهُ عَذَابًا شَدِيدًا أَوْ لَأَذْخَنَّهُ أَوْ لَيَأْتِيَنِي
بِسُلْطَنٍ مُّبِينٍ ﴿٢١﴾

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ عِلْمًا ۗ
وَقَالَ أَحْمَدُ لِلَّهِ الَّذِي فَضَّلَنَا عَلَىٰ
كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾
وَوَرِثَ سُلَيْمَانُ دَاوُدَ ۗ وَقَالَ يَتَاءَتِيهَا
النَّاسُ غُلْمًا مِّنْطِقِ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا
مِنْ كُلِّ شَيْءٍ ۗ إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَضْلُ
الْأَمِينُ ﴿١٦﴾ وَحِشْرَ لِسُلَيْمَانَ
جُنُودَهُ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ وَالطَّيْرِ
فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿١٧﴾ حَتَّىٰ إِذَا أَتَوْا
عَلَىٰ وَادِ النَّمْلِ قَالَتْ نَمْلَةٌ يَتَاءَتِيهَا
النَّمْلُ آذْخُلُوا مَسَكِنَكُمْ لَا
تَحْطِمَنَّكُمْ سُلَيْمَانُ وَجُنُودُهُ وَهُمْ لَا
يَشْعُرُونَ ﴿١٨﴾ فَتَبَسَّ سَاحِجًا مِّنْ
قَوْلِهَا وَقَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ

نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَدْخِلْنِي بِرَحْمَتِكَ فِي عِبَادِكَ
الصَّالِحِينَ ﴿٢١﴾

15. "Na hakika Tuliwapa Daawuud na Sulaymaan ilimu, na wakasema: Alhamdu Lillahi, Kuhimidiwa kote ni kwa Allah Aliyetufadhilisha kuliko wengi katika waja Wake Waumini.

16. Na Sulaymaan alimrithi Daawuud, na akasema: Enyi watu! Tumefunzwa usemi wa ndege, na tumepewa kila kitu. Hakika hii ni Fadhila iliyo dhahiri.

17. Na alikusanyiwa Sulaymaan majeshi yake ya majini, na watu, na ndege, nayo yakapangwa kwa nidhamu.

18. Mpaka walipofika kwenye bonde la wadudu chungu! Alisema mdudu chungu mmoja: Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu, asikupondenii Sulaymaan na majeshi yake bila ya wao kutambua.

19. Basi (Sulaymaan) akatabasamu akacheka kwa neno hili, na akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Nizindue niishukuru Neema Yako Uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kutenda mema Uyapendayo, na Uniingize kwa Rehema Yako katika waja Wako wema”.

Kutajwa Dawud عليه السلام na Sulaymaan عليه السلام, Nidhamu ya Jeshi Lake na Kisa cha Kupita katika Bonde la Chungu.

Hapa Allah تعالى Anatufahamisha Neema Alizowapa waja Wake wawili na Manabii, Dawud عليه السلام na mwanae, Sulaymaan عليه السلام kwa Neema Nyingi, Fadhila tukufu na Sifa kemkem na nzuri. Akawajumlishia wao kupata ufanisi hapa duniani na kesho Akhera. Wakapewa mamlaka na nguvu kamili hapa duniani na Unabii na Utume.

Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ عِلْمًا ۗ وَقَالَ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي فَضَّلَنَا عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ

الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥٠﴾

“Na hakika Tuliwapa Daawuud na Sulaymaan ilimu, na wakasema: Alhamdu Lillahi, Kuhimidiwa kote ni kwa Allah Aliyetufadhilisha kuliko wengi katika waja Wake Waumini.”

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَوَرِثَ سُلَيْمَانُ دَاوُدَ

“Na Sulaymaan alimrithi Daawuud.”

Maana yake: Katika ufalme na Unabii, na muradi wa kauli hiyo hapa si mali. Lau ingekuwa hivyo basi hangehusishwa Sulaymaan عليه السلام peke yake kati ya watoto wengine wa Daawuud عليه السلام, kwani Nabii Daawuud عليه السلام alikuwa na wake mia moja. Lakini maana hapa ni kurithiwa Ufalme na Unabii, kwani Manabii hawarithiwi mali kama alivyotukhabarisha hilo Mtume ﷺ katika Kauli Yake:

«نَحْنُ مَعَاشِرَ الْأَنْبِيَاءِ لَا نُورَثُ، مَا تَرَكَنَاهُ فَهُوَ صَدَقَةٌ»

“Sisi kongamano la Manabii haturithiwi, tunachokiacha ni sadaka.”¹

Na Akasema Aliyetukuka:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ عَلِمْنَا مَنْطِقَ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا مِنْ كُلِّ شَيْءٍ

“Enyi watu! Tumefunzwa usemi wa ndege, na tumepewa kila kitu”.

Hii inamaanisha kuwa Sulaymaan عليه السلام alikuwa akizungumzia neema alizopewa na Allah تعالى, kwa Kumpa mamlaka na nguvu za kuweza kuwadhibiti wanadamu, majini na ndege. Pia alikuwa anajua lugha za ndege na wanyama, jambo ambalo hakupewa mwanadamu mwengine yeyote – kwa kiasi tunachojua kutokana na waliyotuongua Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ. Allah تعالى Alimuwezesha Sulaymaan عليه السلام kuweza kuelewa mazungumzo baina ya ndege angani na kufahamu mazungumzo ya hayawani tofauti. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

عَلِمْنَا مَنْطِقَ الطَّيْرِ وَأُوتِينَا مِنْ كُلِّ شَيْءٍ

“Tumefunzwa usemi wa ndege, na tumepewa kila kitu.”

Maana yake: Vitu vyote anavyohitaji Mfalme.

إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَضْلُ الْمُبِينُ ﴿٢١﴾

“Hakika hii ni Fadhila iliyo dhahiri”.

Bila shaka hii ni fadhila iliyo wazi kwetu kutoka kwa Allah تعالى. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

¹ Tuhfatul Ahwadhi 5:234.

وَحُثِرَ لِسُلَيْمَانَ جُنُودُهُ مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ وَالطَّيْرِ فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿٢٧﴾

“Na alikusanyiwa Sulaymaan majeshi yake ya majini, na watu, na ndege, nayo yakapangwa kwa nidhamu.”

Nabii Sulaymaan عليه السلام alikusanyiwa majeshi yake yote miongoni mwa Majini, wanadamu na ndege, naye akapanda pamoja nao kuonesha nguvu na utukufu mkubwa, wanadamu wakiwa nyuma yake. Majini waliwafuata wanadamu na walikuwa nyuma kwa daraja na cheo, na ndege walikuwa wanaruka juu ya kichwa chake. Wakati joto la jua linapozidi, ndege walikuwa wakimfunika kwa mbawa zao. Na Kauli Yake:

فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿٢٧﴾

“Nayo yakapangwa kwa nidhamu.”

Maana yake: Wa mwanzo na Mwisho waliletwa pamoja, ili asitangulie yeyote katika daraja na sehemu yake ambayo ndiyo nafasi na hadhi yake. Amesema Mujaahid: “Kwa kila kikundi alichagua msimamizi rasmi wa kuhakikisha nidhamu imetunzwa, na kuwaweka wa kwanza na wa Mwisho pamoja ili asitoke yeyote kati yao nje ya msitari – kama wanavyofanya wafalme leo.”¹

Na Kauli Yake:

حَتَّىٰ إِذَا أَتَوْا عَلَىٰ وَادِ النَّمْلِ

“Mpaka walipofika kwenye bonde la wadudu chungu.”

Maana yake: Pale Sulaymaan عليه السلام na aliokuwa nao miongoni mwa wanajeshi na askari walipopita katika bonde la wadudu chungu. Hapo:

قَالَتْ نَمَلَةٌ يَتَأْتِيهَا النَّمْلُ أَدْخُلُوا مَسْكِنَكُمْ لَا تَحْطَمَنَّكُمْ سُلَيْمَانُ وَجُنُودُهُ وَهُمْ لَا

يَشْعُرُونَ ﴿٢٨﴾

“Alisema mdudu chungu mmoja: Enyi wadudu chungu! Ingieni majumbani mwenu, asikupondeni Sulaymaan na majeshi yake bila ya wao kutambua.”

¹ At-Tabari 19:500-501.

Mara moja Sulaymaan عليه السلام alifahamu hilo kutoka kwake. Hivyo:

فَتَبَسَّ صَاحِبًا مِّنْ قَوْلِهَا وَقَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ
وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ

“Basi (Sulaymaan) akatabasamu akacheka kwa neno hili, na akasema: Ee Mola wangu Mlezi! Nizindue niishukuru Neema Yako Uliyoinineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kutenda mema uyapendayo.”

Hii ni kumaanisha kuwa Allah تعالى Amenipa ilhamu kumshukuru kwa Neema Alizonipa kwa kunifundisha mimi kuweza kuelewa usemi wa ndege na hayawani. Na pia Fadhila na Neema za kuwafanya wazazi wangu kuwa Waislamu na kukuamini Wewe Peke Yako.

وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ

“Na nipate kutenda mema uyapendayo.”

Maana yake: Amali (matendo) uzipendazo na zenye kukuridhisha Wewe tu. Na pia:

وَأَدْخِلْنِي بِرَحْمَتِكَ فِي عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ ﴿٢٠﴾

“Na Uniingize kwa Rehema Yako katika waja Wako wema.”

Na wakati Unanifisha, niweke pamoja na watu wema miongoni mwa waja Wako na Rafiki wa juu kabisa miongoni mwa mawalii Wako (rafiki Zako wa karibu).

وَتَفَقَّدَ الطَّيْرَ فَقَالَ مَا لِيَ لَا أَرَى الْهَدْيَ أَمْ كَانَ مِنَ الْغَائِبِينَ ﴿٢١﴾ لَأَعَذِّبَهُ

عَذَابًا شَدِيدًا أَوْ لَأَذْهَبَهُ أَوْ لِيَأْتِنِي بِسُلْطَنٍ مُّبِينٍ ﴿٢٢﴾

20. “Na akawakagua ndege, na akasema: Imekuwaje, mbona simuoni Hud-hud, au amekuwa miongoni mwa walioghibu?”

21. Kwa yakini nitamuadhibu kwa adhabu kali, au nitamchinja, au aniletee hoja ya kutosha”.

Kutoonekana kwa Hud-hud

Mujaahid, Said ibn Jubayr na wengineo wamepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما na wengineo wamesema: "Hud-hud alikuwa mtaalamu aliyekuwa akimuonesha Sulaymaan عليه السلام sehemu ya maji wakiwa jangwani wakati anahitaji maji. Hud-hud alikuwa akimtafutia maji katika tabaka tofauti za ardhi kama vile mtu anavyoona kitu kilicho wazi juu ya ardhi. Alikuwa anajua kwa yakini masafa yaliyopo chini ya ardhi kuyafikia maji hayo. Hud-hud anapoonisha yaliyopo maji, Sulaymaan عليه السلام alikuwa akiwaamuru Majini wachimbe sehemu hiyo mpaka wanatoa maji kutoka chini ya ardhi hiyo. Siku moja Sulaymaan عليه السلام alikuwa katika jangwa kati ya ardhi na akawakagua ndege wake, lakini asimuone Hud-hud. Hapo:

فَقَالَ مَا لِي لَأَرَى الْهَدُّهُ أَمْ كَانَ مِنَ الْغَائِبِينَ ﴿٢١﴾

"Na akasema: Imekuwaje, mbona simuoni Hud-hud, au amekuwa miongoni mwa walioghibu?"

Alihadithia siku moja 'Abdullah ibn 'Abbaas رضي الله عنهما Hadithi kama hii, na katika hadhira hiyo kulikuwa na mtu katika Khawaarij akiitwa Naafi' ibn Al-Azraq, alikuwa akimpinga Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما. Alimuambia: "Simama, ewe Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما, leo utashindwa kwa hoja." Akasema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Kwa nini?" Akasema: "Hakika wewe unatuambia kuwa Hud-hud anaweza kuona chini ya ardhi, lakini mtoto yeyote anaweza kutia mbegu kwenye mtego na kuufunika mtego huo na mchanga. Hud-hud atakuja na kuichukua mbegu hiyo, na mtoto huyo atamshika katika mtego huo. Akasema Ibn Abbaas رضي الله عنهما "Lau si kujua mtu huyu atakwenda kusema kuwa amemshinda Ibn Abbaas رضي الله عنهما kwa hoja, nisingekuwa na haja ya kumjibu kabisa". Kisha akamuambia Naafi': "Ole wako! Qadari inapomshukia mtu, macho yake yanapofuka, hivyo kukosa tahadhari yote." Naafi' akasema: "Wallahi sitajadiliana na wewe mara nyingine kitu chochote kuhusu Qur'ani."¹ Na Kauli Yake:

لَأُعَذِّبَنَّكَ عَذَابًا شَدِيدًا

"Kwa yakini nitamuadhibu kwa adhabu kali".

¹ Al-Qurtwubiy 13:177-178.

Amepokea Al-A'mash kutoka kwa Al-Minhaal ibn 'amr naye kutoka kwa Said ambaye amemsikia Ibn Abbaas رضي الله عنهما akisema: "Alimaanisha, kumnyonyoa (manyoya yake)"¹. Akasema 'Abdullah ibn Shaddaad: "Kwa kumnyonyoa manyoya na kumuanika juani"². Na hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya wengi miongoni mwa watangu wema (*As-Salaf Asw-Swaalih*): Kumnyonyoa na kumuacha aliwe na wadudu chungu. Na Kauli Yake:

أَوْ لَأَذْحَنَّهُ

"Au nitamchinja."

Maana yake: Kumuuua.

أَوْ لِيَأْتِيَنِي بِسُلْطَنٍ مُّبِينٍ ﴿١٦﴾

"Au aniletee hoja ya kutosha."

Maana: Udhuru wa wazi unaokubalika. Amesema Sufyaan ibn 'Uyaynah na 'Abdullah ibn Shaddad: Aliporudi Hud-hud aliambiwa na ndege wenziwe: "Ni kipi kilichokuweka (ukachelewa kurudi)? Hakika ameapa Sulaymaan عليه السلام kumwaga damu yako". Akasema: 'Je, ameweka fursa ya kutoa udhuru?' Wakasema: "Ndio". Amesema,

لَأُعَذِّبَنَّهُ عَذَابًا شَدِيدًا أَوْ لَأَذْحَنَّهُ أَوْ لِيَأْتِيَنِي بِسُلْطَنٍ مُّبِينٍ ﴿١٧﴾

"Kwa yakini nitamuadhibu kwa adhabu kali. Au aniletee hoja ya kutosha".

Akasema: "Basi nimepona."

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:443.

² Atw-Twabariy 19:443.

فَمَكَتْ غَيْرَ بَعِيدٍ فَقَالَ أَحَطْتُ بِمَا لَمْ نَحِطْ بِهِ
 وَجِئْتُكَ مِنْ سَبَإٍ بِنَبَإٍ يَقِينٍ ﴿٢٢﴾ إِنِّي وَجَدْتُ امْرَأَةً
 تَمْلِكُهُمْ وَأُوتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ وَهَا عَرْشٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾
 وَجَدْتُهَا وَقَوْمَهَا يَسْجُدُونَ لِلشَّمْسِ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَزَيْنُ
 لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيلِ فَهُمْ لَا
 يَهْتَدُونَ ﴿٢٤﴾ أَلَا يَسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي يُخْرِجُ الْخَبْءَ فِي
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ﴿٢٥﴾
 اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٢٦﴾ * قَالَ
 سَنَنْظُرُ أَصَدَقْتَ أَمْ كُنتَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٢٧﴾ أَذْهَبَ
 بِكَتَبِي هَذَا فَأَلْفِقْهُ إِجِيمٌ ثُمَّ تَوَلَّ عَنْهُمْ فَانظُرْ مَاذَا
 يَرْجِعُونَ ﴿٢٨﴾ قَالَتْ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوْا إِنِّي أَتَىٰ إِلِيَّ كِتَابٌ كَرِيمٌ
 ﴿٢٩﴾ إِنَّهُ مِنْ سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
 ﴿٣٠﴾ أَلَّا تَعْلَمُوا عَلَيَّ وَأُتُونِي مُسْلِمِينَ ﴿٣١﴾ قَالَتْ يَا أَيُّهَا
 الْمَلَأُوْا أَفْتُونِي فِي أَمْرِي مَا كُنتُ قَاطِعَةً أَمْرًا حَتَّىٰ
 دَشَّدُونَ ﴿٣٢﴾ قَالُوا نَحْنُ أَوْلُو قُوَّةٍ وَأُولُو بَأْسٍ شَدِيدٍ
 وَالْأَمْرُ إِلَيْكِ فَانظُرِي مَاذَا تَأْمُرِينَ ﴿٣٣﴾ قَالَتْ إِنَّ الْمُلُوكَ
 إِذَا دَخَلُوا قَرْيَةً أَفْسَدُوهَا وَجَعَلُوا أَعْرَبَهَا أَهْلَهَا أَذِلَّةً ۗ
 وَكَذَٰلِكَ يَفْعَلُونَ ﴿٣٤﴾ وَإِنِّي مُرْسَلَةٌ إِلَيْهِمْ بِهَدِيَّةٍ فَنَاظِرَةٌ
 بِمَ يَرْجِعُ الْمُرْسَلُونَ ﴿٣٥﴾

فَمَكَتْ غَيْرَ بَعِيدٍ فَقَالَ أَحَطْتُ بِمَا
 لَمْ نَحِطْ بِهِ وَجِئْتُكَ مِنْ سَبَإٍ بِنَبَإٍ
 يَقِينٍ ﴿٢٢﴾ إِنِّي وَجَدْتُ امْرَأَةً
 تَمْلِكُهُمْ وَأُوتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ
 وَهَا عَرْشٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾ وَجَدْتُهَا
 وَقَوْمَهَا يَسْجُدُونَ لِلشَّمْسِ مِنْ دُونِ
 اللَّهِ وَزَيْنُ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ
 فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيلِ فَهُمْ لَا
 يَهْتَدُونَ ﴿٢٤﴾ أَلَا يَسْجُدُوا لِلَّهِ
 الَّذِي يُخْرِجُ الْخَبْءَ فِي السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا
 تُعْلِنُونَ ﴿٢٥﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ
 الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٢٦﴾

22. "Basi (Hud-hud) akakaa si mbali na akasema: Nimegundua usilogundua wewe, na ninakujia hivi kutoka nchi ya Sabai, na ninakuletea khabari za yakini.

23. Hakika mimi nime-mkuta mwanamke anawatawala, naye amepewa kila kitu, na anacho kiti cha enzi kikubwa.

24. Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Allah; na Shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia Njia. Kwa hivyo hawakuongoka.

25. Na hawamsujudii Allah Ambaye Huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi, na Anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza.

26. Allah - hapana muabudiwa ila Yeye, Mola Mlezi wa Arshi tukufu.”

Hud-hud Kaja Mbele ya Sulayman عليه السلام Kumpasha Habari ya Sabai

Anasema Aliyetukuka:

فَمَكَتْ غَيْرَ بَعِيدٍ

“Basi akakaa si mbali.”

Hud-hud alighibu kwa muda mfupi sana. Kisha alikuja na kumwambia Sulayman

عليه السلام:

أَحَطْتُ بِمَا لَمْ تُحِطْ بِهِ

“Nimegundua usilogundua wewe.”

Maana yake: Nimejua jambo ambalo wewe na jeshi lako hamjui.

وَجِئْتُكَ مِنْ سَبَأٍ بِنْتًا يَقِينٍ ﴿٣٥﴾

“Na ninakujia hivi kutoka nchi ya Sabai, na ninakuletea khabari za yakini.”

Kumaanisha na habari za kweli na hakika. Sabai ni Himyar, nao ni falme za Yemen. Kisha akasema Hud-hud:

إِنِّي وَجَدْتُ أَمْرًا تَمَلِكُهُمْ

“Hakika mimi nimemkuta mwanamke anawatawala.”

Al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى amesema: “Naye alikuwa ni Bilqis bint Sharahil, Malkia wa Sabai.”¹ Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Ad-Durr Al-Manthuur 6:351.

وَأُوتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ

“Naye amepewa kila kitu.”

Katika mapambo ya ulimwengu, naye amepewa kila kitu ambacho ufalme wenye nguvu unatakiwa kuwa navyo.

وَهَا عَرْشٌ عَظِيمٌ

“Na anacho kiti cha enzi kikubwa.”

Maana yake: Kiti kikubwa ambacho kimepambwa na dhahabu, aina tofauti za vito na lulu. Wanasema wanazuoni wa Historia: “Kiti hicho kikubwa cha enzi kilikuwa katika kasri kubwa, lililokuwa imara na kuta ndefu. Kasri hilo lilikuwa na madirisha mia tatu na sitini katika upande wake wa mashariki, na idadi kama hiyo upande wake wa magharibi. Lilijengwa kwa njia ambayo kila siku jua lilikuwa likichomoza linang’aa kupitia dirisha moja wapo, na linapozama linaangaza kwenye dirisha lililolelekeana na lile jengine. Watu walikuwa wakilisujudia jua hilo asubuhi na jioni. Kwa hiyo akasema Hud-hud:

وَجَدْتُهُمْ وَقَوْمَهَا يَسْجُدُونَ لِلشَّمْسِ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَزَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ فَصَدَّهُمْ

عَنِ السَّبِيلِ

“Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Allah; na Shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia Njia”.

Maana: Njia ya haki.

فَهُمْ لَا يَهْتَدُونَ

“Kwa hiyo hawakuongoka.”

Na Kauli Yake Allah تعالى Maana yake ni kuwa:

وَزَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيلِ فَهُمْ لَا يَهْتَدُونَ ﴿٢٧﴾ أَلَّا يَسْجُدُوا لِلَّهِ

“Na Shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia Njia. Kwa hivyo hawakuongoka. Na hawamsujudii Allah”.

Hawaijui njia ya haki ambayo ni kumtakasia sijda Allah تعالى Peke Yake, sio kusujudia vile Alivyoviumba, kama nyota au vitu vingine vyovyote.

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ
الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾

“Na katika alama Zake ni kupatikana usiku na mchana na jua na mwezi; basi msilisujudie jua wala mwezi; basi msujudieni Allah Aliyeviumba; ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye.” (41:37).

Na Kauli Yake:

الَّذِي يُخْرِجُ الْخَبَاءَ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ambaye huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi”.

Amepokea ‘Aliy ibn Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Anajua kila kitu kilichofichikana mbinguni na ardhini.”¹

Na hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya Ikrimah, Mujaahid, Said ibn Jubayr, Qataadah na wengineo². Na Kauli Yake:

وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ﴿٣٨﴾

“Na anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza.”

Yeye, Anajua yale yanayofichwa na waja na wanayoyatangaza katika kauli na vitendo. Na hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

سَوَاءٌ مِّنْكُمْ مَّنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿٣٩﴾

“Ni sawa anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhihirisha, na anayejibanza usiku na anayetembea jahara mchana.” (13:10).

¹ Addur Al-Manthur 6:352

² Atw-Twabariy 19:445, ‘Abdur-Razzaaq 3:81 na Ad-Durr al-Manthuur 6:352.

Na kauli Yake:

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٢٧﴾

“Allah - hapana mola ila Yeye, Mola Mlezi wa Arshi tukufu”.

Yeye Ndiye Mwenye Kuombwa, Allah تعالى, Naye Ndiye Ambaye hakuna muabudiwa isipokuwa Yeye, Mola Mlezi wa Arshi tukufu, na hakuna aliye mkubwa kuliko Yeye katika viumbe vyote. Alipokuwa Hud-hud anaita katika kheri, na kumuabudu Allah تعالى Peke Yake na kumsujudia Yeye tu, ikawa ni haramu kumuua. Kuhusu hilo imepokewa Hadithi na Imamu Ahmad, Abu Dawwuud na Ibn Maajah kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ amekataza kuwaua aina nne za wanyama: Wadudu chungu, nyuki, Hud-hud na shorewanda (kipwe)”. Na Isnadi yake ni Sahihi¹.

* قَالَ سَنَنْظُرُ أَصَدَقْتَ أَمْ كُنْتَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٢٧﴾ أَذْهَبَ بِكِتَابِي هَذَا فَأَلْقَاهُ إِلَيْهِمْ ثُمَّ تَوَلَّى عَنْهُمْ فَانظُرْ مَاذَا يَرْجِعُونَ ﴿٢٨﴾ قَالَتْ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوْا إِنَّيَأُلْقِي إِلَيْكَ كِتَابًا كَرِيمًا ﴿٢٩﴾ إِنَّهُ مِن سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٣٠﴾ أَلَّا تَعْلَمُونَ عَلَيَّ وَأَتُونِي مُسْلِمِينَ ﴿٣١﴾

27. “Akasema (Sulaymaan): Tutatazama umesema kweli au wewe ni miongoni mwa waongo.

28. Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha waache na utazame watarejesha nini.

29. (Malkia) akasema: Enyi wahishiwiwa! Hakika nimeletewa barua tukufu.

30. Imetoka kwa Sulaymaan nayo ni: Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

31. Msinifanyie jeuri, na fikenki kwangu nanyi mmekwisha kuwa wenye kusalimu amri.”

¹ Ahmad 1:332, Abu Dawwuud 5:418 na Ibn Maajah 2:1074, pia kutoka kwa Ibn ‘Abbaas.

Barua ya Sulaymaan عليه السلام kwa Balqis

Allah تعالى Anatuelezea vile Sulayman عليه السلام alivyomuambia Hud-hud pale alipomhadithia kuhusu watu wa Sabai na malkia wao.

﴿ قَالَ سَنَنْظُرُ أَصَدَقْتَ أَمْ كُنتَ مِنَ الْكٰذِبِينَ ﴾

“Akasema (Sulaymaan): Tutatazama umesema kweli au wewe ni miongoni mwa waongo”.

Je, wewe ni mkweli katika habari zako hizo?

﴿ أَمْ كُنتَ مِنَ الْكٰذِبِينَ ﴾

“Au wewe ni miongoni mwa waongo”.

Katika maneno yako ili ujiepushe na ile adhabu kali niliyoahidi dhidi yako? Hivyo akaambiwa:

﴿ اذْهَبْ بِكِتٰبِيْ هٰذَا فَاَلْقِهْ عَلَيْهِمْ ثُمَّ تَوَلَّ عَنَّهُمْ فَاَنْظُرْ مَاذَا يَرْجِعُوْنَ ﴾

“Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha waache na utazame watarejesha nini.”

Hiyo ni kuwa Sulaymaan عليه السلام aliandika barua kwa Balqis na watu wake na akampa Hud-hud aipeleke. Panasemwa kuwa aliichukua katika mbawa zake, kama ilivyokuwa ada na desturi ya ndege au aliichukua kwenye mdomo wake. Alikwenda katika nchi yao na akafika katika kasri ya Balqis, hapo akaingia katika vyumba vya faragha na kuitupa barua kupitia kwenye kidirisha. Baada ya kufanya hivyo alikaa kando sehemu moja kwa heshima na adabu njema. Balqis alistaajabu na kubabaika alipoliona hilo, kisha akaifungua na kuisoma.

﴿ اِنَّهُ مِنْ سُلَيْمٰنَ وَاِنَّهُ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ﴾ ﴿ اَلَّا تَعْلُوْا عَلٰى وَاَنْتُمْ مُسْلِمِيْنَ ﴾

“Imetoka kwa Sulaymaan nayo ni: Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Msinifanyie jeuri, na fikenki kwangu nanyi mmekwisha kuwa wenye kusalimu amri.”

Balqisi baada ya hapo aliwakusanya pamoja viongozi wake wakuu wakiwemo mawaziri na wakuu wengine waandamizi wa himaya yake. Kisha akawaambia,

قَالَتْ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوٓأَيُّ إِنِّي أَخْتَبِكُمْ ۝

“(Malkia) akasema: Enyi wahishimiwa! Hakika nimeletewa barua tukufu.” (27:29)

Akimaanisha utukufu wa barua aliyoletewa akistaajabu barua hiyo kuletewa na ndege, na kisha ndege huyo kuondoka kwa adabu. Jambo hili hakuna yeyote katika wafalme anayeweza kulifanya. Na wala hawana ubunifu wa hilo. Balqisi akawasomea barua hiyo.

إِنَّهُ مِنْ سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۝

“Imetoka kwa Sulaymaan nayo ni: Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.” (27:30)

Hivyo walijua kuwa barua hiyo inatoka kwa Nabii wa Allah, Sulaymaan عليه السلام na kuwa hawawezi kupambana naye. Barua hiyo ilionesha balagha ya juu na ufasaha kwani amefikisha ujumbe kwa kutumia ibara nyepesi na nzuri. Na Kauli Yake:

أَلَّا تَعْلَمُونَ ۝

“Msinfanyie jeuri.”

Amesema Qataadah, ‘Msinioneshe Kiburi.’

وَأَتُونِي مُسْلِمِينَ ۝

“Na fikenii kwangu nanyi mmekwisha silimu.”¹

Amesema ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam: “Msikatae wala msifanye kiburi kuja kwangu.”

وَأَتُونِي مُسْلِمِينَ ۝

“Na fikenii kwangu nanyi mmekwisha silimu.”²

¹ Ad-Durr Al-Manthuur 6:354.

² Atw-Twabariy 19:453.

قَالَتْ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوْا أَفْتُونِ فِي أَمْرِي مَا كُنْتُ قَاطِعَةً أَمْرًا حَتَّى تَشْهَدُوْنَ ﴿٢٢﴾ قَالُوْا نَحْنُ
 أَوْلُوْا قُوَّةً وَأَوْلُوْا بِأَسْسِدِيْدٍ وَالْأَمْرُ إِلَيْكَ فَانظُرِي مَاذَا تَأْمُرِيْنَ ﴿٢٣﴾ قَالَتْ إِنَّ الْمُلُوْكَ
 إِذَا دَخَلُوْا قَرْيَةً أَفْسَدُوْهَا وَجَعَلُوْا أَعْرَاجَ أَهْلِهَا أِدْلَةً ۖ وَكَذَٰلِكَ يَفْعَلُوْنَ ﴿٢٤﴾ وَإِنِّي مُرْسَلَةٌ
 إِلَيْهِمْ بِهَدِيَّةٍ فَنَظِرَةٌ بِمَ يَرْجِعُ الْمُرْسَلُوْنَ ﴿٢٥﴾

32. "Akasema: Enyi wahishimiwa! Nipeni shauri katika jambo hili, kwani sikati shauri yoyote mpaka mhudhurie.

33. Wakasema: Sisi ni wenye nguvu na wakali kwa vita; na amri iko kwako, basi tazama ni nini unaamrisha.

34. Akasema: Hakika wafalme wanapouingia mji wanauharibu, na wanawafanya wale watukufu wake kuwa wanyonge. Na hivyo ndivyo watendavyo.

35. Lakini mimi nitawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayorudi nayo wajumbe".

Balqis Ashauriana na Viongozi Wake Wakuu

Alipowasomea barua ya Sulaymaan عليه السلام, aliwataka ushauri katika jambo lake hilo na yaliyowafikia. Kwa hiyo akasema:

يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوْا أَفْتُونِ فِي أَمْرِي مَا كُنْتُ قَاطِعَةً أَمْرًا حَتَّى تَشْهَدُوْنَ ﴿٢٢﴾

"Enyi wahishimiwa! Nipeni shauri katika jambo hili, kwani sikati shauri yoyote mpaka mhudhurie".

Maana yake: Mpaka muwepo na mnishauri. Hapo wahishimiwa walianza kutoa shauri:

قَالُوْا نَحْنُ أَوْلُوْا قُوَّةً وَأَوْلُوْا بِأَسْسِدِيْدٍ

"Wakasema: Sisi ni wenye nguvu na wakali kwa vita".

Walimkumbusha yeye kuhusu idadi yao kubwa, matayarisho yao kabambe na nguvu zao, kisha wakalirudisha kwake jambo hilo kwa uamuzi wa mwisho pale waliposema:

وَالْأَمْرُ إِلَيْكِ فَانظُرِي مَاذَا تَأْمُرِينَ ﴿٢٢﴾

“Na amri iko kwako, basi tazama ni nini unaamrisha”.

Hii inamaanisha kuwa sisi hatuna pingamizi, vikwazo wala tatizo lolote ikiwa unataka twende na kupigana naye. Lakini baada ya yote haya amri iko kwako na wewe ndiye mwenye uamuzi, hivyo tuamuru nasi tuko tayari kutekeleza. Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما Balqis alisema:

إِنَّ الْمُلُوكَ إِذَا دَخَلُوا قَرْيَةً أَفْسَدُوهَا وَجَعَلُوا أَعْرَةَ أَهْلِهَا أَذِلَّةً

“Hakika wafalme wanapouingia mji wanauharibu, na wanawafanya wale watukufu wake kuwa wanyonge”.

Mola Mlezi Aliyetukuka Akasema:

وَكَذَلِكَ يَفْعَلُونَ ﴿٢٣﴾

“...Na hivyo ndivyo watendavyo.”

Kisha Balqis kafuata njia ya amani na maslahi, mapatano, ya usalama na suluhu, hadaa na kumtuliza Sulaymaan عليه السلام. Akasema:

وَإِنِّي مُرْسِلَةٌ إِلَيْهِمْ بِهَدِيَّةٍ فَنَاظِرَةٌ بِمِ يَرْجِعُ الْمُرْسَلُونَ ﴿٢٤﴾

“Lakini mimi nitawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayorudi nayo wajumbe”.

Hii inamaanisha kuwa nitampelekea hadiya zinazolingana na hadhi na cheo chake, na tutangojea jawabu kutoka kwake. Huenda akakubali zawadi hizo na hivyo kutuacha sisi au atatutoza ushuru ambao tunaweza kulipa kila mwaka, ili asipigane nasi wala kuandaa vita dhidi yetu. Amesema Qataadah: “Allah Amrehemu na Amridhie – jinsi gani alivyokuwa na akili katika Uislamu wake na kabla ya hapo alipokuwa mshirikina. Alitambua kuwa hadiya ina athari kubwa kwa watu”. Amesema Ibn ‘Abbaas na wengineo رضي الله عنهم: “Aliwaambia watu wake, Nabii, hivyo mfuateni.”

¹ Atw-Twabariy 19:455.

فَلَمَّا جَاءَ سُلَيْمَنَ قَالَ أُوذِيْتُمْ بِمَالٍ فَمَا ءَاتَيْنِيَ اللَّهُ
 خَيْرٌ مِّمَّا ءَاتَيْتُكُمْ بَلْ أَنْتُمْ بِهَدْيِكُمْ تَفْرَحُونَ ﴿٣٦﴾ أَرْجِعْ
 إِلَيْهِمْ فَلَنَأْتِيَنَّهُمْ بِجُنُودٍ لَا قِبَلَ لَهُمْ بِهَا وَلَنُخْرِجَنَّهُمْ مِنْهَا أَذَلَّةً
 وَهُمْ صَاغِرُونَ ﴿٣٧﴾ قَالَ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوْا أَيُّكُمْ يَأْتِينِي بِعَرْشِهَا
 قَبْلَ أَنْ يَأْتُونِي مُسْلِمِينَ ﴿٣٨﴾ قَالَ عَفْرَيْتُ مِنَ الْجِنِّ
 أَنَا ءَاتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَنْ تَقُومَ مِنْ مَقَامِكَ وَإِنِّي عَلَيْهِ لَقَوِيٌّ
 أَمِينٌ ﴿٣٩﴾ قَالَ الَّذِي عِنْدَهُ عِلْمٌ مِّنَ الْكِتَابِ أَنَا ءَاتِيكَ
 بِهِ قَبْلَ أَنْ يَرْتَدَّ إِلَيْكَ طَرْفُكَ فَلَمَّا رَآهُ مُسْتَقِرًّا عِنْدَهُ
 قَالَ هَذَا مِنْ فَضْلِ رَبِّي لِيَتْلُوَنِي ءَأَشْكُرُ أَمْ أَكْفُرُ وَمَنْ
 شَكَرَ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ رَبِّي غَنِيٌّ كَرِيمٌ
 ﴿٤٠﴾ قَالَ نَكَرُوا لَهَا عَرْشَهَا نَنْظُرْنَ أَتَنَدِي أَمْ تَكُونُ مِنَ
 الَّذِينَ لَا يَهْتَدُونَ ﴿٤١﴾ فَلَمَّا جَاءَتْ قِيلَ أَهَكَذَا عَرْشُكَ
 قَالَتْ كَأَنَّهُ هُوَ وَأُوَيْدِنَا آلْعَلَمَ مِنْ قَبْلِهَا وَكُنَّا مُسْلِمِينَ ﴿٤٢﴾
 وَصَدَّهَا مَا كَانَتْ تَعْبُدُ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنَّهَا كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ
 كَافِرِينَ ﴿٤٣﴾ قِيلَ لَهَا ادْخُلِي الصَّرْحَ فَلَمَّا رَأَتْهُ حَسِبَتْهُ
 لُجَّةً وَكَشَفَتْ عَن سَاقِيهَا ءَقَالَ إِنَّهُ صَرْحٌ مُّمَرَّدٌ مِّنَ
 قَوَارِيرَ ءَقَالَتْ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي وَأَسْلَمْتُ مَعَ
 سُلَيْمَانَ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٤﴾

فَلَمَّا جَاءَ سُلَيْمَنَ قَالَ أُوذِيْتُمْ بِمَالٍ فَمَا ءَاتَيْنِيَ اللَّهُ خَيْرٌ مِّمَّا
 ءَاتَيْتُكُمْ بَلْ أَنْتُمْ بِهَدْيِكُمْ تَفْرَحُونَ ﴿٣٦﴾ أَرْجِعْ إِلَيْهِمْ فَلَنَأْتِيَنَّهُمْ بِجُنُودٍ
 لَا قِبَلَ لَهُمْ بِهَا وَلَنُخْرِجَنَّهُمْ مِنْهَا أَذَلَّةً
 وَهُمْ صَاغِرُونَ ﴿٣٧﴾

36. "Basi alipofika (Mjumbe) kwa Sulaymaan, alisema (Sulaymaan): Hivyo ndio nyinyi mnanisaidia kwa mali? Aliyonipa Allah ni bora zaidi kuliko Aliyokupeni nyinyi. Lakini nyinyi mnafurahia zawadi hii yenu.

37. Rejea kwao! Kwa yakini sisi tutawajia kwa majeshi wasiyoweza kuyakabili. Na hakika tutawatoa humo na hali wao wamekuwa madhalili na wanyonge".

Hadiya na Jawabu ya Sulaymaan عليه السلام.

Wanazuoni wengi wa Tafsiri miongoni mwa Salaf na wengineo wamesema kuwa Balqis alimpelekea zawadi

kubwa ya dhahabu, vito vya thamani, lulu na vitu vingine. Ni wazi kuwa Nabii Sulaymaan عليه السلام hata hakuviangalia vitu hivyo vilivyoletwa hata kidogo wala hakuvitilia maanani, bali aligeuka na kuwakemea:

أَتُمِدُّونَ بِمَالٍ

“Hivyo ndio nyinyi mnanisaidia kwa mali?”.

Kumaanisha kuwa je, munataka kunibembeleza kwa mali ili niwaache nyinyi na ushirikina na ufalme wenu? Hakika ni kuwa:

فَمَا آتَيْنَا آلَ اللَّهِ خَيْرٌ مِّمَّا آتَيْنَاكُمْ

“Aliyonipa Allah ni bora zaidi kuliko Aliyokupeni nyinyi”.

Hii ina maana kuwa aliyonipa mimi Allah تعالى katika ufalme, nguvu, mali na majeshi ni bora zaidi kuliko muliyonayo.

بَلْ أَنْتُمْ بِهِ بَيِّنَةٌ تَفَرَّحُونَ ﴿٣٦﴾

“Lakini nyinyi mnafurahia hii zawadi yenu”.

Hii inamaanisha nyinyi ndio mnashawishiwa na hadiya pamoja na zawadi, nasi hatutakubali kutoka kwenu isipokuwa Uislamu au upanga (vita baina yetu na nyinyi). Hapo akasema:

أَرْجِعْ إِلَيْهِمْ

“Rejea kwao!”

Maana yake: Pamoja na hadiya zenu, kwani:

فَلَنَأْتِيَنَّهُمُ الْجُنُودُ لَا قِبَلَ لَهُمْ بِهَا

“Kwa yakini sisi tutawajia kwa majeshi msiyoweza kuyakabili.”

Hawana uwezo wa kuweza kupambana nayo au kuyazuia.

وَلَنُخْرِجَنَّهُمْ مِنْهَا أَذِلَّةً

“Na hakika tutawatoa humo na hali wao wamekuwa madhalili.”

Tutawatoa nje ya ardhi yao wakiwa madhalili. Pia:

وَهُمْ صَبِرُونَ ﴿٣٧﴾

“Na wakiwa wanyonge.”

Pindi wajumbe wake waliporudi kwake na zawadi na wakamwambia aliyosema Sulaymaan عليه السلام, yeye na watu wake waliyapa uzito maneno ya Sulayman عليه السلام na kumtii. Alikwenda (yaani Bilqis) kwa (Sulaymaan عليه السلام) pamoja na jeshi lake kwa unyenyekevu na kusalimu amri, kwa kumheshimu Sulaymaan عليه السلام na akatia nia ya kumfuata Sulaymaan عليه السلام katika Uislamu.

Pale Nabii Sulaymaan عليه السلام alipopata habari ya kuwa wanakuja kwake alifurahika mno.

قَالَ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُوا أَيُّكُمْ يَا تَبْنِي بِعَرَشِهَا قَبْلَ أَنْ يَأْتُونِي مُسْلِمِينَ ﴿٣٨﴾ قَالَ عِفْرِيْتُ مَنِ
 الْجِنِّ أَنَا ءَاتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَنْ تَقُومَ مِنْ مَقَامِكَ ط وَإِنِّي عَلَيْهِ لَقَوِيٌّ أَمِينٌ ﴿٣٩﴾ قَالَ الَّذِي
 عِنْدَهُ عِلْمٌ مِنَ الْكِتَابِ أَنَا ءَاتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَنْ يَرْتَدَّ إِلَيْكَ طَرْفُكَ فَلَمَّا رَءَاهُ مُسْتَقِرًّا
 عِنْدَهُ قَالَ هَذَا مِنْ فَضْلِ رَبِّي لِيَتْلُوَنَ ءَأَشْكُرُ أَمْ أَكْفُرُ ط وَمَنْ شَكَرَ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ط
 وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ رَبِّي غَنِيٌّ كَرِيمٌ ﴿٤٠﴾

38. "Akasema: Enyi wahishimiwa! Ni nani kati yenu atakayeniletea kiti chake cha enzi kabla hawajanijia nao wamekwisha salimu amri.

39. Akasema: Afriti, katika majini: Mimi nitakuletea kabla hujainuka pahala pako hapo. Na mimi kwa hakika nina nguvu na Muaminifu.

40. Akasema mwenye ilimu ya Kitabu: Mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako. Basi alipokiona kimewekwa mbele yake, akasema: Haya ni katika Fadhila Zake Mola wangu Mlezi, ili Anijaribu nitashukuru au nitakufuru. Na mwenye kushukuru anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake; na anayekufuru, kwa hakika Mola wangu Mlezi ni Mkwasi na Mkarimu".

Kuletwa Kiti cha Bilqis kwa Haraka

Amepokea Muhammad ibn Is'haaq رَحْمَهُ اللهُ تَعَالَى kuwa Yazid ibn Ruuman amesema: “Pindi wajumbe waliporudi na ujumbe wao kutoka kwa Sulaymaan عليه السلام, Bilqis alisema: “Wallahi, nilijua kuwa yeye alikuwa zaidi ya mfalme, na hakika sisi hatuna uwezo wala nguvu za kupambana naye, na hatutafaidi kwa chochote kwa kuwa wakaidi dhidi yake. Hivyo, alituma salamu kwa Sulaymaan عليه السلام kwa kumwambia: Ninakuja kwako pamoja na viongozi wa watu wangu ili kutazama maelekezo yako kwetu na wito wako katika kuifuata Dini yako”. Kisha akaamrisha kiti chake cha enzi alichokuwa akikalia kilichotengenezwa kwa dhahabu kilichopambwa na yakuti, zumaridi (Kito cha thamani chenye rangi ya kijani iliyopauka) na lulu, kiingizwe chumba cha ndani kabisa katika vyumba saba, kimoja ndani ya chengine, na milango yote ifungwe. Kisha alimwambia naibu wake aliyemuacha nyuma kuendesha mambo ya ufalme wake: “Hifadhi vyema watu wangu na kiti changu, na usimuache yeyote kuja karibu nacho miongoni mwa waja wa Allah تَعَالَى au kukiona mpaka nitakaporudi”. Kisha aliondoka kwenda kukutana na Sulaymaan عليه السلام akiwa na majemadari elfu kumi na mbili miongoni mwa viongozi wa Yemen, chini ya kila kiongozi mmoja maelfu ya watu wengi. Nabii Sulaymaan عليه السلام alimtuma Jini kumletea habari ya maendeleo na masafa yake kila asubuhi na jioni, hata alipofika karibu, aliwakusanya majini na wanadamu waliokuwa chini yake, akawaambia:

يَأْتِيهَا الْمَلَأُوا أَيْكُم يَأْتِينِي بِعَرْشِهَا قَبْلَ أَنْ يَأْتُونِي مُسْلِمِينَ ﴿٣٦﴾

“Enyi wahishimiwa! Ni nani kati yenu atakayeniletea kiti chake cha enzi kabla hawajanijia nao wamekwisha salimu amri.”¹

قَالَ عِفْرِيتٌ مِّنَ الْجِنَّ

“Akasema: Afriti, katika majini.”

Amesema Mujaahid: “Maana yake: Jini Mkubwa”. Abu Swaalih amesema: “Alikuwa ni kama kwamba ni jabali.”²

¹ Atw-Twabariy 19:520.

² Ad-Durr Al-Manthuur 6:359.

أَنَا آتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَنْ تَقُومَ مِنْ مَقَامِكَ

“Mimi nitakuletea kabla hujainuka pahala pako hapo.”

Amesema Ibn Abbaas رضي الله عنهما: “Hii ina maana kuwa kabla hujainuka katika sehemu uliyokaa”¹. Amesema As-Suddiy na wengineo: “Alikuwa akikaa kutoa hukumu na uamuzi juu ya watu na kula, kuanzia mwanzo wa asubuhi mpaka katikati ya mchana”.

وَإِنِّي عَلَيْهِ لَقَوِيٌّ أَمِينٌ ﴿٣٦﴾

“Na mimi kwa hakika nina nguvu na Muaminifu.”

Amesema Ibn Abbaas رضي الله عنهما: “Maana yake: Ana nguvu ya kuibeba na muaminifu kwa vito ilivyokuwa navyo.” Akasema Sulaymaan عليه السلام: “Nakitaka kwa haraka zaidi kuliko hivyo”².

Kutokana na maelezo hayo inaonesha kuwa Sulaymaan عليه السلام alitaka kukileta kiti hicho kuonesha ukubwa wa nguvu zake na mamlaka ambayo Allah تعالى Amemtunukia na majeshi ambayo amedhalilishiwa na Allah تعالى. Nguvu ambazo hajapewa yeyote kabla yake wala hatakuwa nayo yeyote baada yake, ili hii iwe dalili ya Unabii wake mbele ya Bilqis na watu wake, kwani jambo hili litakuwa ni kubwa na la ajabu kama ataleta kiti chake kama kwamba yeye (Sulaymaan عليه السلام) yuko katika nchi ya Bilqis hata kabla ya kufika kwao, isitoshe kiti chenye kilikuwa kimefichwa na kulindwa na milango mingi iliyofungwa. Sulaymaan عليه السلام aliposema: “Nakitaka kwa haraka zaidi”. Hapo:

قَالَ الَّذِي عِنْدَهُ عِلْمٌ مِنَ الْكِتَابِ

“Akasema mwenye ilimu ya Kitabu.”

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنها amesema : “Huyo alikuwa Asaf, mwandishi wa Sulaymaan عليه السلام”. Hivyo ndivyo ilivyopokewa na Muhammad ibn Ishaq kutoka kwa Yazid ibn Ruuman kuwa, “alikuwa ni Asaf ibn Barkhiyaa”. Naye alikuwa ni Muumini wa kweli aliyekuwa akijua Jina kubwa la Allah تعالى¹.

¹ Al-Baghawiy 3:420.

² Al-Baghawiy 3:420.

Amesema Oataadah: “alikuwa Muumini miongoni mwa wanadamu, na jina lake lilikuwa Asaf.” Na Kauli Yake:

أَنَا آتِيكَ بِهِ قَبْلَ أَنْ يَرْتَدَّ إِلَيْكَ طَرْفُكَ

“Mimi nitakuletea kabla ya kupepesa jicho lako.”

Maana: Nyanyua macho yako na utazame upeo wa kuona kwako, na kabla hujachoka na kupepesa, utakiona mbele yako. Kisha aliinuka na kushika udhu, na akamuomba Allah تعالى. Amesema Mujaahid: “Alisema: *Yaadhal Jalaal wal Ikraam* (Ewe Mwenye Utukufu na Heshima).”² Pindi Sulaymaan عليه السلام na wahishimiwa wake walipokiona mbele yao,

قَالَ هَذَا مِنْ فَضْلِ رَبِّي

“Akasema: Haya ni katika Fadhila Zake Mola wangu Mlezi.”

Maana yake: Ni katika Neema ya Allah تعالى kwangu mimi. Haya yote ni,

لِيَتْلُوَنِي ۖ أَشْكُرُ أَمْ أَكْفُرُ ۗ وَمَنْ شَكَرَ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ

“Ili anijaribu (kwa kunipa mtihani) nitashukuru au nitakufuru. Na mwenye kushukuru, kwa hakika, ananishukuru kwa manufaa ya nafsi yake.”

Maana yake: Ili apate kunijaribu. Hii ni kama Kauli Yake:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا

“Anayefanya mema anajifanyia nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu ya nafsi yake vile vile.” (41:46).

وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِأَنْفُسِهِمْ يَمْهَدُونَ ﴿٤٤﴾

“Na anaye tenda mema, basi wanazitengezea nafsi zao.” (30:44).

¹ Al-Baghawiy 3:420.

² Al-Tabari 19:466.

Na kama Kauli Yake Allah تعالى, Hakika Yeye ni Mkwasi, hivyo Hawahitaji waja Wake na 'Ibaadah zao. Na pia:



“Karimu”.

Maana yake: Yeye ni Karimu katika Nafsi Yake hata kama hataabudiwa na yeyote. Hakika Ukubwa Wake haumtegemei yeyote. Maneno haya ni kama alivyosema Musa عليه السلام:

إِنْ تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأِنَّ اللَّهَ لَعَنِيَّ حَمِيدٌ ﴿١٤﴾

“Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Allah ni Mkwasi, Anajitosha, Msifiwa” (14:8).

Na katika Hadithi iliyonukuliwa katika Sahihi Muslim:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَجْرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجَنَّتُمْ كَانُوا عَلَى اتَّقَى قَلْبِ رَجُلٍ مِنْكُمْ مَا زَادَ ذَلِكَ فِي مُلْكِي شَيْئًا. يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَجْرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجَنَّتُمْ كَانُوا عَلَى أَفْجَرِ قَلْبِ رَجُلٍ مِنْكُمْ مَا نَقَصَ ذَلِكَ مِنْ مُلْكِي شَيْئًا. يَا عِبَادِي إِنَّمَا هِيَ أَعْمَالُكُمْ أَحْصِيهَا لَكُمْ نُمْ أَوْفِيكُمْ إِيَّاهَا فَمَنْ وَجَدَ خَيْرًا فَلْيَحْمِدِ اللَّهَ، وَمَنْ وَجَدَ غَيْرَ ذَلِكَ فَلَا يَلُومَنَّ إِلَّا نَفْسَهُ»

“Anasema Allah Aliyetukuka: Enyi waja Wangu, lau kama wa mwanzo wenu na wa Mwisho wenu, na binadamu wenu na Majini yenu watakuwa wote juu ya moyo wa mchamungu zaidi miongoni mwenu, hilo lisingezidisha chochote katika Ufalme Wangu. Enyi waja Wangu, lau kana wa mwanzo wenu na wa Mwisho wenu, na binadamu wenu na Majini yenu watakuwa wote juu ya moyo wa muovu zaidi miongoni mwenu, hilo Halingenipunguzia chochote katika Ufalme Wangu. Enyi waja Wangu, hakika hizo ni amali zenu Nawadhibitia, kisha Niwalipe wenyewe; kwa hivyo, mwenye kukuta ya kheri na amshukuru Allah, na mwenye kukuta yasiokuwa hivyo na asilaumu ila nafsi yake”¹.

¹ Muslim 4:1994. Pia tazama Al-Arba 'iina An-Nawawiiyyah, Hadithi nambari 24.

قَالَ تَكْرُؤًا لَهَا عَرْشَهَا نَنْظُرُ أَتَهْتَدِي أَمْ تَكُونُ مِنَ الَّذِينَ لَا يَهْتَدُونَ ﴿٣٦﴾ فَلَمَّا جَاءَتْ قِيلَ أَهَكَذَا عَرْشُكَ ۗ قَالَتْ كَأَنَّهُ هُوَ ۗ وَأُوَيْبِنَا أَلْغَمَ مِنْ قَبْلِهَا وَكُنَّا مُسْلِمِينَ ﴿٣٧﴾ وَصَدَّهَا مَا كَانَتْ تَعْبُدُ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ إِنَّهَا كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ كَافِرِينَ ﴿٣٨﴾ قِيلَ لَهَا ادْخُلِي الصَّرْحَ ۗ فَلَمَّا رَأَتْهُ حَسِبَتْهُ لُجَّةً وَكَشَفَتْ عَنْ سَاقِهَا ۗ قَالَ إِنَّهُ صَرْحٌ مُّمَرَّدٌ مِنْ قَوَارِيرَ ۗ قَالَتْ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي وَأَسْلَمْتُ مَعَ سُلَيْمَانَ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٩﴾

41. Akasema: Mgeuzieni kiti chake cha enzi hiki, tuone ataongoka, au atakuwa miongoni mwa wasioongoka.

42. Basi (Malkia) alipofika akaambiwa: Je! Kiti chako cha enzi ni kama hiki? Akasema: Kama kwamba ndicho hichi. (Sulaymaan na watu wake wakasema): Na sisi tumepewa ilimu kabla yake (Malkia), na tukawa Waislamu.

43. Na yale aliyokuwa akiyaabudu badala ya Allah yalimzuilia. Hakika yeye (Malkia) alikuwa katika kaumu ya makafiri.

44. Akaambiwa: Liingie behewa la hili jumba. Alipoliona alidhani ni maji, na akapandisha nguo mpaka kwenye miundi yake. (Sulaymaan) akasema: Hakika hilo ni behewa liliosakafiwa kwa vioo! Akasema (Malkia): Mola wangu Mlezi! Mimi nimejidhulumu nafsi yangu, na sasa nimesilimu pamoja na Sulaymaan kwa Allah, Mola Mlezi wa walimwengu wote”.

Mtihani wa Bilqis

Sulayman عليه السلام alipoletewa Kitii cha Bilqis kabla ya yeye na watu wake kufika, aliamuru kuwa baadhi ya sifa zake zibadilishwe, ili apate kumjaribu na kuona kama ataweza kukitambua na utulivu atakaokuwa nao baada ya kukiona. Je atafanya haraka kusema kuwa hiko ni kiti chake au si chake? Kwa hiyo akasema (Sulayman عليه السلام):

تَكْرُؤًا لَهَا عَرْشَهَا نَنْظُرُ أَتَهْتَدِي أَمْ تَكُونُ مِنَ الَّذِينَ لَا يَهْتَدُونَ ﴿٣٦﴾

“Mgeuzieni kiti chake cha enzi hiki, tuone ataongoka, au atakuwa miongoni mwa wasioongoka.”

Amesema Ibn Abbaas رضي الله عنهما “kiliondoshwa baadhi ya mapambo yake na sehemu zake”¹. Amesema Mujaahid: “Aliamuru kuwa kigeuzwe na kubadilishwa, amri hiyo ikatekelezwa. Hivyo kila kilichokuwa chekundu kilifanywa manjano na kinyume chake, na kila kilichokuwa kijani kilifanywa chekundu. Kila kitu kiligeuzwa kutoka katika ile hali yake ya awali”. Amesema ‘Ikrimah: “Walizidisha na kupunguza ndani yake”. Na amesema Qataadah: “Vile vya chini viliwekwa juu, na vya mwanzo vikawekwa mwisho, wakaongeza na kupunguza vitu vyengine”².

فَلَمَّا جَاءَتْ قَيْلٌ أَهْكَدًا عَرُّشِكِ

“Akaambiwa: Je! Kiti chako cha enzi ni kama hiki?”

Hii inamaanisha alioneshwa kiti chake cha enzi ambacho kilikuwa tayari kimegeuzwa na kubadilishwa, kimeongezwa na kupunguzwa. Alikuwa imara, mwenye akili, mwenye busara na mwanamke makini. Hakufanya haraka kusema kuwa ndicho kiti chake, kwani kilikuwa mbali naye. Pia hakufanya haraka kusema kuwa hakikuwa kiti chake, alipoona athari na sifa zake japokuwa baadhi ya vitu vilikuwa vimegeuzwa na kubadilishwa. Akasema:

كَأَنَّهُ هُوَ

“Kama kwamba ndicho hichi.” Maana yake: Kinafanana na kukaribiana. Na huu ni upeo wa akili na azima thabiti. Na Kauli Yake:

وَأَوْتَيْنَا آلَ عَادَ مِنَ قَبْلِهَا وَكُنَّا مُسْلِمِينَ ﴿١٧﴾

“Na sisi tumepewa ilimu kabla yake (Malkia), na tukawa Waislamu.”

Mujaahid amesema: “Haya yalisemwa na Sulaymaan عليه السلام.” Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَصَدَّهَا مَا كَانَتْ تَعْبُدُ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنَّهَا كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ كَافِرِينَ ﴿١٨﴾

“Na yale aliyokuwa akiyaabudu badala ya Allah yalimzuilia. Hakika yeye (Malkia) alikuwa katika kaumu ya makafiri.”

¹ Atw-Twabariy 19:469.

² Atw-Twabariy 19:469.

Haya ni maneno ya Nabii Sulayman عليه السلام aliyoundelea kuyasema, kulingana na kauli ya Mujaahid na Said ibn Jubayr, maana Sulayman عليه السلام alisema:

﴿١٧﴾ وَأَوْتَيْنَا آلْعَلَمَ مِنْ قَبْلِهَا وَكُنَّا مُسْلِمِينَ

“Na sisi tumepewa ilimu kabla yake (Malkia), na tukawa Waislamu.”

Naye alikuwa amezuiliwa. Yaani, Alizuiliwa kumuabudu Allah تعالى Peke Yake,

﴿١٨﴾ مَا كَانَتْ تُعْبُدُ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنَّهَا كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ كَافِرِينَ

“Na yale aliyokuwa akiyaabudu badala ya Allah, Hakika yeye (Malkia) alikuwa katika kaumu ya makafiri.”

Na haya aliyoyasema Mujaahid na Said ibn Jubayr ni mazuri. Amesema hayo pia Ibn Jariir رحمه الله تعالى². Kisha akasema Ibn Jariir رحمه الله تعالى: “Huenda ikawa lengo la kitendo:

وَصَدَّهَا

“Yalimzuilia.” Kiwakilishi hapa katika kitendo hicho inarudi kwa Sulaymaan عليه السلام au Allah تعالى, kumuezesha na kumkataza, hivyo ibara hiyo itakuwa ina maana:

مَا كَانَتْ تُعْبُدُ مِنْ دُونِ اللَّهِ

“Hakuwa ni mwenye kuabudu asiyekuwa Allah.”

Maana yake: Alimzuilia kuabudu asiyekuwa Allah تعالى.

﴿١٩﴾ إِنَّهَا كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ كَافِرِينَ

“Hakika yeye (Malkia) alikuwa katika kaumu ya makafiri.”

Nikasema: “Inaungwa mkono kauli ya Mujaahid kuwa yeye alidhihirisha Uislamu baada ya kuingia kwenye ukumbi kama itakavyokuja baadaye”. Na Kauli Yake:

قِيلَ لَهَا ادْخُلِي الصَّرْحَ فَلَمَّا رَأَتْهُ حَسِبَتْهُ لُجَّةً وَكَشَفَتْ عَنْ سَاقَيْهَا

“Akaambiwa: Liingie behewa la jumba hili. Alipoliona alidhani ni maji, na akapandisha nguo mpaka kwenye miundi yake.”

¹ Atw-Twabariy 19: 471.

² Atw-Twabariy 19: 472.

Hiyo ni kuwa Sulaymaan عليه السلام aliwaamrisha Mashetani kumjengea malkia kasri kubwa la kioo lipitalo maji chini yake. Yeyote asiyejua maumbile ya jengo hilo atadhani ya kuwa ni maji, lakini hakika ni kuwa kulikuwa na kioo baina ya mtu anayetembea na maji hayo.

Jumba Kubwa la Vioo la Sulayman (*Swarh Mumarrad*)

Asili ya *Swarh* katika lugha ya Kiarabu ni kasri na kila jengo kubwa lililonyanyuka. Amesema Allah تعالى kutupasha habari kuhusu Firauni, laana ya Allah تعالى iwe juu yake, hakika yeye alimuambia waziri wake Haamaan:

أَبْنِ لِي صَرْحًا لَعَلِّي أَبْلُغُ الْأَسْبَابَ ﴿٣٦﴾

“Nijengee mnara ila nipate kuzifikia njia.” (40:36).

Swarh ni kasri lililo juu katika ujenzi huko Yemen. *Mumarrad* inamaanisha jengo lenye nguvu, imara lililosakafiwa sawasawa na mororo. Ujenzi huo umetengenezwa:

مِنْ قَوَارِيرَ

“Lililosakafiwa kwa Vioo.”

Maana: Vioo. Kumaanisha iliyosakafiwa kwa umororo. *Marid* ni ngome iliyoko *Dawmat Al-Jandal*. Lengo kubwa la Sulaymaan عليه السلام kumtengenezea malkia kasri kubwa lililojengwa kwa vioo, ni kumuonesha ukubwa wa ufalme wake na nguvu alizonazo. Alipoona kwa macho yake aliyopewa na Allah تعالى na utukufu alionao (Sulayman عليه السلام), alinyenyekea kwa Amri ya Allah تعالى na akakiri kuwe yeye (Sulaymaan عليه السلام) ni Nabii Mtukufu, hivyo akasilimu kwa Allah تعالى na akasema:

رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي

“Mola wangu Mlezi! Mimi nimejidhulumu nafsi yangu.”

Kwa aliyotanguliza kwa kufuru na ushirikina aliokuwa akiufanya kuabudu yeye pamoja na kaumu yake jua badala ya Allah تعالى, hivyo akabadilika:

وَأَسْلَمْتُ مَعَ سُلَيْمَانَ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٧﴾

“Na sasa nimesilimu pamoja na Sulaymaan kwa Allah, Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Akawa ni mwenye kufuata Dini ya Sulaymaan عليه السلام katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya kumshirikisha, ambaye Ameumba kila kitu na kupima vyote hivyo kwa kipimo Chake cha sawa.



وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ فَإِذَا هُمْ فَرِيقَانِ يَخْتَصِمُونَ ﴿٤٥﴾ قَالَ يَبْقَوْمِ لِمَ تَسْتَعْجِلُونَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ لَوْلَا تَسْتَغْفِرُونَ اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٤٦﴾ قَالُوا أَطِیرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَعَكَ قَالَ طَیْرُكُمْ عِنْدَ اللَّهِ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ تُفْتَنُونَ ﴿٤٧﴾ وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ بَسْعَةٌ رَهَطٌ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿٤٨﴾ قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ ثُمَّ لَنَقُولَنَّ لِوَلِيِّهِ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ أَهْلِهِ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٤٩﴾ وَمَكَرُوا مَكْرًا وَمَكَرْنَا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٠﴾ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكْرِهِمْ إِنَّا دَمَرْنَاهُمْ وَقَوْمَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥١﴾ فَيَلَاكُ بِيُونُثِهِمْ حَاقِبَةٌ بِمَا ظَلَمُوا ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٥٢﴾ وَأَنْجَيْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٥٣﴾ وَلَوْطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَتَأْتُونَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُونِ النِّسَاءِ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّجْهَلُونَ ﴿٥٤﴾ * فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوا ءَالَ لُوطٍ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۗ إِنَّهُمْ أَنَاسٌ يَّتَطَهَّرُونَ ﴿٥٥﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا أَمْرَأَتَهُ قَدَّرْنَاهَا مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٥٦﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا ۗ فَسَاءَ مَطَرُ الْمُنذَرِينَ ﴿٥٧﴾

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ فَإِذَا هُمْ فَرِيقَانِ يَخْتَصِمُونَ ﴿٤٥﴾ قَالَ يَبْقَوْمِ لِمَ تَسْتَعْجِلُونَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ ۗ لَوْلَا تَسْتَغْفِرُونَ اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٤٦﴾ قَالُوا أَطِیرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَعَكَ قَالَ طَیْرُكُمْ عِنْدَ اللَّهِ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ تُفْتَنُونَ ﴿٤٧﴾

45. "Na kwa kina Thamud Tulimtuma ndugu yao Swaleh kuwaambia: Muabuduni Allah. Basi wakawa makundi mawili yanayogombana.

46. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa nini mnauhimiza uovu kabla ya wema? Kwa nini hamuombi msamaha kwa Allah ili mrehemewe?

47. Wakasema: Tuna kisirani nawe na wale walio pamoja nawe. Yeye akasema: Uaguzi wa ukorofi wenu uko kwa Allah; lakini nyinyi ni watu mnaojaribiwa."

Swaleh عليه السلام na Thamuud

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu Thamuud na walivyokuwa pamoja na Mtume wao Swaleh عليه السلام pale alipotumwa na Allah تعالى kwao, naye akawaita katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya kumshirikisha na yeyote.

﴿٤٥﴾ فَإِذَا هُمْ فَرِيقَانِ يَخْتَصِمُونَ

“Basi wakawa makundi mawili yanayogombana”.

Amesema Mujaahid: “Waumini na makafiri”¹. Hii ni kama Kauli Yake:

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لِلَّذِينَ اسْتُضْعِفُوا لِمَنْ ءَامَنَ مِنْهُمْ

أَتَعْلَمُونَ أَنَّ صَالِحًا مُرْسَلٌ مِنْ رَبِّهِ ؕ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلَ بِهِ مُؤْمِنُونَ ﴿٤٦﴾

﴿٤٦﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا بِالَّذِي ءَامَنْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ ﴿٤٧﴾

“Waheshimiwa wa kaumu yake wanaojivuna waliwaambia wanaoonewa wenye kuamini miongoni mwao: Je mtakaidi ya kwamba Swaleh ametumwa na Mola wake Mlezi? Wakasema: Hakika sisi tunayaamini yale aliyetumwa nayo. Wakasema wale wanaojivuna: Sisi tunyakataa hayo mnayoyaamini.” (7:75-76).

قَالَ يَفْقَوْمٍ لِمَ تَسْتَعْجِلُونَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ

“Akasema: Enyi watu wangu! Kwa nini mnauhimiza uovu kabla ya wema?”

Kumaanisha kwamba kwa nini munaomba adhabu iwajilie, wala hamuombi kutoka kwa Allah تعالى Rehema. Hivyo Akasema:

لَوْلَا تَسْتَغْفِرُونَ اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٤٨﴾ قَالُوا أَطِيرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَعَكَ

“Kwa nini hamuombi msamaha kwa Allah ili mrehemewe. Wakasema: Tuna kisirani nawe na wale walio pamoja nawe.”

Hii inamaanisha, hakika sisi hatuoni zuri lolote usoni mwako na nyusoni mwa wenye kukufuata. Hiyo ni kwa sababu ya uovu wao, alikuwa mmoja wao hapatwi

¹ Atw-Twabariy 19:475.

na jambo baya isipokuwa alisema: “Hii inatokana na Swaleh عليه السلام na wafuasi wake”. Amesema Mujaahid: “Walikuwa wakiwachukulia wenye kisirani.”¹ Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى kutoa habari kuhusu kaumu ya Firauni:

فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحَسَنَةُ قَالُوا لَنَا هَذِهِ وَإِنْ تُصِيبِهِمْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ

“Likiwafikia jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafikia ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi” (7:131).

Akasema Aliyetukuka:

وَإِنْ تُصِيبُهُمْ حَسَنَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَإِنْ تُصِيبُهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ قُلْ كُلٌّ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ

“Na likiwafikia jema wakisema: Hili limetoka kwa Allah. Na likiwafikia ovu husema: Hili limetoka kwako wewe. Sema: Yote yanatokana na Allah.” (4:78).

Maana yake: Kwa Hukumu na Amri Yake. Anaeleza Aliyetukuka kuhusu watu wa vitongoji, pale wajumbe walipokwenda kwao:

قَالُوا إِنَّا نَطَّيَّرْنَا بِكُمْ لَئِن لَّمْ تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُم مِّنَّا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨﴾ قَالُوا طَّيَّرْنَاكُمْ مَعَكُمْ

“Wakasema: Hakika sisi tumekorofika kwa ajili yenu: kama hamtaacha (hayo mnayoyasema) tutakupigeni mawe, na itakufikieni kutoka kwetu adhabu iumizayo. Wakasema: Ukorofi wenu mnao wenyewe.” (36:18-19).

Na hawa watu wa Thamuud walisema:

أَطَّيَّرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَّعَكَ قَالَ طَّيَّرْتُمْ عِنْدَ اللَّهِ

“Tuna kisirani nawe na wale walio pamoja nawe. Yeye akasema: Uaguzi wa ukorofi wenu uko kwa Allah.”

Maana yake: Allah تعالى Atawaadhibu kwa hilo. Anamalizia:

¹ Ad-Duur Al-Manthuur 6:369.

بَلْ أَنتُمْ قَوْمٌ تُفْتَنُونَ ﴿٤٧﴾

“Lakini nyinyi ni watu mnaojaribiwa”.

Amesema Qataadah: “Mnajaribiwa ili muonekane kama mtatii au mtaasi”¹.
Na dhahiri ya muradi wa Kauli Yake:

تُفْتَنُونَ ﴿٤٨﴾

“Mnaojaribiwa”. Kumaanisha mtaachiliwa katika hali ya upotovu mulionao.

وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ تِسْعَةُ رَهْطٍ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿٤٩﴾ قَالُوا
تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ ثُمَّ لَنَقُولَنَّ لِوَلِيِّهِ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ أَهْلِهِ وَإِنَّا
لَصَادِقُونَ ﴿٥٠﴾ وَمَكْرُؤًا مَكَرًا وَمَكْرَتًا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥١﴾ فَانظُرْ كَيْفَ
كَانَ عِقَابُهُمْ أَنَا دَمَرْنَاهُمْ وَقَوْمَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٢﴾ فَتِلْكَ بَيِّنَاتٌ لِمَا
ظَلَمُوا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٥٣﴾ وَأَحْبَبْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا
يَتَّقُونَ ﴿٥٤﴾

48. “Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya ufisadi katika nchi wala hawafanyi la maslaaha.

49. Wakasema: Apishaneni kwa Allah tutamshambulia usiku yeye na ahli zake; kisha tutamwambia mrithi wake: Sisi hatukuona maangamizo ya watu wake, na sisi bila ya shaka tunasema kweli.

50. Basi wakapanga mipango yao, na Sisi tukapanga mipango Yetu, na wao hawatambui.

51. Basi angalia ulivyokuwa mwisho wa mipango yao, ya kwamba Tuliwaangamiza wao pamoja na watu wao wote.

52. Basi hizo nyumba zao ni tupu kwa sababu ya walivyodhulumu. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo ishara kwa watu wanaojua.

53. Na Tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa wana mchamungu”.

¹ Ad-durr Al-Manthuur 6:369.

Vitimbi vya Kikundi cha Mafisadi na Khatima ya Kaumu ya Thamud

Allah تعالی Anatuelezea kuhusu waovu katika Thamud na viongozi wao ambao walikuwa ni walinganiaji wa kaumu yao katika upotovu, ukafiri na kumkadhibisha Swaleh عليه السلام. Hatimaye walimua Ngamia na walikuwa karibu kumuua Swaleh عليه السلام. Walipanga kumuacha akiwa amelala na familia yake usiku, ili wapate kumuua kwa kificho na kisha kuwaambia jamaa zake kuwa wao hawajui chochote kuhusu kilichotokea kwake. Katika hayo yote, wao wanasema ukweli kwa sababu hakuna aliyeona lolote. Akasema Aliyetukuka:

وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ

“Na walikuwamo mjini”. Maana yake: Katika mji wa Thamud,

تِسْعَةَ رَهْطٍ

“Rahtw tisa”. Maana yake: Watu tisa. Sifa yao:

يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ

“Wakifanya ufisadi katika nchi wala hawafanyi la maslaha”.

Hawa walilazimisha rai zao kwa kaumu ya Thamud, kwa kuwa wao ndio walikuwa ni wakubwa, viongozi na wajumbe wao. Amepokea Al-Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hawa ndio wale waliomuua Ngamia jike”¹.

Hii ina maana kuwa hilo lilitokea baada ya wao kutoa rai na maelekezo yao, Allah تعالی Awalaani. Amesema Allah تعالی:

فَتَادُوا صَاحِبِهِمْ فَتَعَاوَى فَعَقَرَهُ

“Basi mwisho wake wakamwita rafiki yao; naye akashika upanga akamtumbua ngamia, wakamua.” (54:29).

Amesema tena Aliyetukuka:

إِذْ أَنْبَعَتْ أَشَقْنَهَا

“Aliposimama muovu wao mkubwa (ili kumchinja Ngamia huyu wa miujiza).” (91:12).

¹ Atw-Twabariy 19:477.

Amesema 'Abdur-Razzaq kuwa Yahya ibn Rabi'ah Asw-swan'aaniy aliwaambia: "Nimemsikia 'Atwaa', naye ni Ibn Abi Rabaah – anasema:

وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ تِسْعَةُ رَهْطٍ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿٤٥﴾

"Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya ufisadi katika nchi wala hawafanyi la maslaha".

Akasema: "Walikuwa wakikopesha Dirham (sarafu za fedha)"¹. Wao walikuwa wakichukua kwayo, na ilikuwa ni kama kwamba wakifanya biashara nazo kulingana na idadi (wala sio kwa uzito) kama walivyokuwa wakifanya biashara kama hiyo Waarabu. Imenukuliwa na Imamu Malik kutoka kwa Yahyaa ibn Said ambaye amepokea kuwa Said ibn Al-Musayyib amesema: "Kupunja dhahabu na fedha (sarafu) ni aina ya kueneza ufisadi katika ardhi". Lengo kubwa la watu hawa makafiri waovu na mafasiki, lilikuwa miongoni mwa sifa zao ni kueneza ufisadi katika ardhi kwa kila njia wanayoweza. Katika njia hizo ni hii iliyotajwa na hawa Maimamu na nyenginezo. Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ

"Wakasema: Apishaneni kwa Allah tutamshambulia usiku yeye na ahli zake".

Maana yake: Walikula kiapo cha kumuua Nabii wa Allah Swaleh عليه السلام kwa kila waliyekutana naye usiku kwa kificho. Allah تعالیٰ, kitimbi na mbinu yao Akaipindua ikawa dhidi yao. Mujahidi amesema: waliapizana na kula kiapo juu ya kummaliza Nabii Swaleh عليه السلام. Hawakudiriki kumfikia hadi wote wao na jamaa zao wakahiliki.²

Amesema 'Abdur-Rahmaan ibn Abi Haatim³, "Walipomuua Ngamia, Swaleh عليه السلام aliwaambia:

تَمَتُّعُوا فِي دَارِكُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ ذَٰلِكَ وَعَدُّ غَيْرُ مَكْدُوبٍ ﴿٤٦﴾

"Stareheni katika mji wenu muda wa siku tatu. Hiyo ni Ahadi isiyokuwa ya uwongo." (11:65).

¹ 'Abdur-Razzaq 3:83.

² At-Twabarī 19:478

³ Huyu ni 'Abdur-Rahmaan ibn Zayd. Maelezo haya yamenukuliwa na Ibn Abi Hatim nambari 16485 na Atw-Twabarī nambari 27054.

Walisema: “Swaleh عليه السلام anadai kuwa atamalizana na sisi kwa muda wa siku tatu, lakini sisi tutammaliza yeye na familia yake kabla ya siku tatu kumalizika”. Swaleh عليه السلام alikuwa na Msikiti katika bonde majabalini sehemu ambayo alikuwa akifanya ‘Ibaadah zake.

Hivyo walitoka kuelekea kwenye pango hilo usiku mmoja, wakasema: “Akija kwa ajili ya Swala tutamuua, kisha sisi tutarudi. Tutakapomaliza tutakwenda kwa familia yake kuwamaliza pia”.

Allah تعالى Aliwatumia jiwe juu yao kutoka mlimani, wao wakahofia kuwa litawasaga, hivyo walikimbia kwenye pango, nalo jiwe likaufunga na kuuziba mdomo wa hilo pango wakiwa ndani.

Watu wao hawakujua walipo na kilichowasibu. Kwa hiyo Allah تعالى Aliwaadhibu watu hawa hapo hapo na wengine mahala pengine, na Allah تعالى Akamuokoa Swaleh عليه السلام na wale waliokuwa pamoja naye.

Kisha akasoma:

وَمَكْرُوا مَكْرًا وَمَكْرَتَا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٥﴾ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
مَكْرِهِمْ أَنَا دَمَرْنَاهُمْ وَقَوْمَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٦﴾ فَتِلْكَ بُيُوتُهُمْ خَاوِيَةٌ

“Basi wakapanga mipango yao, na Sisi Tukapanga Mipango Yetu, na wao hawatambui. Basi angalia ulivyokuwa mwisho wa mipango yao, ya kwamba Tuliwaangamiza wao pamoja na watu wao wote. Basi hizo nyumba zao ni tupu.”

Maana yake: Zipo tupu kabisa kwani hazina mtu yeyote ndani yake (zimehamwa). Kiini cha hayo yote kuwafikia ni:

بِمَا ظَلَمُوا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٤٧﴾ وَأُنْحَيْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَقَانُوا
يَتَّقُونَ ﴿٤٨﴾

“Kwa sababu ya walivyodhulumu. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo ishara kwa watu wanaojua. Na Tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa wanamchamungu.”

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ وَأَنْتُمْ تُبْصِرُونَ ﴿٤٥﴾ أَيُّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ
 شَهْوَةً مِّنْ دُونِ النِّسَاءِ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّجْهَلُونَ ﴿٤٦﴾ * فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا
 أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوا آلَ لُوطٍ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۖ إِنَّهُمْ أَنَاسٌ يَّتَطَهَّرُونَ ﴿٤٧﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا
 أُمَّرَأَتَهُ ۖ فَدَرَّزْنَاهَا مِنَ الْغَيْرِيبِ ﴿٤٨﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا فَسَاءَ ۖ مَطَرُ الْمُنْذَرِينَ ﴿٤٩﴾

54. *“Na Lutw alipowaambia watu wake: Je! Mnafanya uchafu nanyi mnaona?”*

55. *Hivyo nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio badala ya wanawake? Hakika nyinyi ni watu mnaofanya ujinga kabisa!*

56. *Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila ni kusema: Wafukuzeni wafuasi wa Lutw katika mji wenu. Hao ni watu wanaojitia usafi.*

57. *Basi Tukamuokoa yeye na ahali zake, isipokuwa mkewe; Tukamkadiria katika walio baki nyuma.*

58. *Na Tukawanyeshea mvua. Ni uovu kweli hiyo mvua ya waliokwisha onywa.”*

Lutw عليه السلام na Kaumu Yake

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu mja na Mtume Wake, Lut عليه السلام, na jinsi alivyoionya kaumu yake kwa adhabu ya Allah تعالى kwa sababu ya wao kufanya uasherati na uchafu ambao haukufanywa na yeyote katika wanadamu – kufanya jimai na wanaume wenziwao badala ya wanawake. Na hii ni dhambi kubwa mno, wanaume kukidhi matamanio yao kwa kustarehe na wanaume wenzao, na wanawake kwa wanawake wenzao (Maana: Ubaradhuli, ushoga na usagaji). Lut عليه السلام akawaambia:

أَتَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ وَأَنْتُمْ تُبْصِرُونَ ﴿٤٥﴾

“Je! Mnafanya uchafu nanyi mnaona?”

Maana yake: Ilhali mnaonana na munatekeleza kila aina ya uovu katika mikutano yenu.

أَيُّكُمْ لَتَأْتُونَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُونِ النِّسَاءِ ۚ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿٤٥﴾

“Hivyo nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio badala ya wanawake? Hakika nyinyi ni watu mnaofanya ujinga kabisa!”

Hii ina maana kuwa hamujui chochote cha maumbile au sheria iliyoletwa na Allah تعالى kwenu nyinyi. Hii ni kama ile Aya nyengine:

أَتَأْتُونَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿٤٦﴾ وَتَذَرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ ۚ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ

عَادُونَ ﴿٤٧﴾

“Je, munawaingilia wanaume katika viumbe! Na mnawacha alichokuumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Kweli nyinyi ni watu mnaoruka mipaka.” (26:165-166).

﴿٤٨﴾ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَخْرِجُوا آلَ لُوطٍ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۚ إِنَّهُمْ أَنَاسٌ

يَتَطَهَّرُونَ ﴿٤٩﴾

“Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila ni kusema: Wafukuzeni wafuasi wa Lutw katika mji wenu. Hao ni watu wanaojitia usafi.”

Hii inamaanisha wanapata shida na kuona aibu kwa sababu ya vitendo vyenu mnavyofanya, na kukubali kwenu mnayofanya, hivyo wafukuzeni na muwatoe kukaa kwao nanyi, kwani hawastahiki kuishi pamoja nanyi katika mji wenu. Kwa hiyo, wakaweka azimio la kutekeleza hilo, na hapo Allah تعالى Aliwaangamiza, na mwisho wa mfano huo unawasubiri makafiri. Anasema Allah تعالى:

فَأَنْجَبْنَاهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا امْرَأَتَهُ قَدَرْنَاهَا مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٥٠﴾

“Basi Tukamwokoja yeye na ahali zake, isipokuwa mkewe; Tukamkadiria katika waliobaki nyuma.”

Hii inamaanisha mkewe alikuwa ni miongoni mwa wale walioangamizwa pamoja na kaumu yake, kwani alikuwa anawasaidia katika dini yao na njia zao, kwa kuridhia matendo yao maovu waliokuwa wakiyafanya. Yeye ndiye

aliyewaambia kuhusu wageni wawili wa Lutw عليه السلام ili wapate kuja kwao. Hakufanya uchafu yeye mwenyewe, ili kutunza heshima ya Lutw عليه السلام wala si kwa sababu ya heshima na hadithi aliyokuwa nayo yeye mwenyewe. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَطَرًا

“Na Tukawanyeshea mvua.”

Maana: Changarawe za udongo mgumu wa kuchomwa motoni uliokamatana, zilizotiwa alama kwa Mola wako Mlezi; na hayo hayako mbali na wenye kudhulumu wengineo. Na hapa Akasema:

فَسَاءَ مَطَرُ الْمُنْذَرِينَ

“Ni uovu kweli mvua hiyo ya waliokwishaonywa.”

Kwa wale ambao walisimamishia hoja na dalili na wakafikiwa na onyo pamoja na tahadhari, lakini wao wakakengeuka na kwenda kinyume na Mtume na kumkadhibisha, na wakaazimia kumtoa miongoni mwao.

* * *

قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ وَسَلَامٌ عَلَىٰ عِبَادِهِ الَّذِينَ اصْطَفَىٰ ۗ اللَّهُ
 خَيْرٌ أَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٥٩﴾ أَمَّنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنْبَتْنَا بِهِ حَدَائِقَ
 ذَاتِ بَهْجَةٍ مَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُنبِتُوا شَجَرَهَا ۗ أُولَٰئِكَ
 مَعَ اللَّهِ ۗ بَلْ هُمْ قَوْمٌ يَعْدِلُونَ ﴿٦٠﴾ أَمَّنْ جَعَلَ الْأَرْضَ
 قَرَارًا وَجَعَلَ خِلَالَهَا أَنْهَادًا وَجَعَلَ لَهَا رَوَاسِيَ وَجَعَلَ
 بَيْنَ الْبَحْرَيْنِ حَاجِزًا ۗ أُولَٰئِكَ مَعَ اللَّهِ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا
 يَعْلَمُونَ ﴿٦١﴾ أَمَّنْ يُجِيبُ الْمُضْطَّرِّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ
 السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ ۗ أُولَٰئِكَ مَعَ اللَّهِ ۗ قَلِيلًا مَّا
 تَذَكَّرُونَ ﴿٦٢﴾ أَمَّنْ يَهْدِيكُمْ فِي ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ
 وَالْبَحْرِ وَمَنْ يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۗ
 أُولَٰئِكَ مَعَ اللَّهِ ۗ تَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٣﴾ أَمَّنْ
 يَبْدُوا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَمَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ
 أُولَٰئِكَ مَعَ اللَّهِ ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ
 ﴿٦٤﴾ قُلْ لَا يَعْلَمُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا
 اللَّهُ ۗ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٦٥﴾ بَلِ أَدْرَاكَ عِلْمَهُمْ
 فِي الْآخِرَةِ ۗ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِّنْهَا ۗ بَلْ هُمْ مِّنْهَا عَمُونَ ﴿٦٦﴾

قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ وَسَلَامٌ عَلَىٰ عِبَادِهِ
 الَّذِينَ اصْطَفَىٰ ۗ اللَّهُ خَيْرٌ أَمَّا
 يُشْرِكُونَ ﴿٥٩﴾ أَمَّنْ خَلَقَ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَنْزَلَ لَكُمْ
 مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنْبَتْنَا بِهِ
 حَدَائِقَ ذَاتِ بَهْجَةٍ مَا كَانَ
 لَكُمْ أَنْ تُنبِتُوا شَجَرَهَا ۗ أُولَٰئِكَ
 مَعَ اللَّهِ ۗ بَلْ هُمْ قَوْمٌ يَعْدِلُونَ ﴿٦٠﴾

**59. "Sema: Alhamdu Lillahi!
 Kuhimidiwa ni kwa Allah!
 Na Amani ishuke juu ya
 waja wake Aliowateua. Je!
 Allah ni bora, au wale
 wanaowashirikisha Naye?"**

**60. Au nani yule Aliye-
 ziumba mbingu na ardhi, na
 Akakuteremshieni maji
 kutoka mbinguni, na kwa
 hayo Tutazitesha bustani
 zenye kupendeza? Nyinyi
 hamna uwezo wa kuiotesha
 miti yake. Je! Yupo mungu
 pamoja na Allah? Bali hao
 ni watu waliopotoka".**

Amri ya Kumhimidi Allah تعالى na Kuwatakia Amani Mitume Yake

Allah تعالى Anamuamuru Mtume Wake aseme:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ

“Kuhimidiwa ni kwa Allah!”

Hii ina maana kwa Neema Zake nyingi kwa waja Wake na kwa Sifa Zake Tukufu na Majina Yake mazuri. Pia Aliamuru watakiwe Amani waja wa Allah تعالى Aliowachagua na Kuwateua, yaani Mitume Yake watukufu, Amani na Baraka za Allah تعالى ziwe juu yao wote.

Hii ndio iliyokuwa rai ya Abdurrahman bin Zaid bin Aslam na wengineo. Hakika makusudio ya Aliowachagua ni Manabii. Amesema: Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى:

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٣٧﴾ وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٨﴾ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ

رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٩﴾

“Ametakasika Mola Mlezi Mwenye Enzi na yale wanayomzulia. Na salamu juu ya Mitume. Na Sifa Njema zote ni za Allah Mola Mlezi wa walimwengu wote”. (37:180-182)

Ath-Thawriy na As-Suddiy wamesema: “Hii inawahusisha Maswahaba wa Mtume Muhammad ﷺ, Allah تعالى Awe radhi nao wote”.

Rai kama hii ilinukuliwa kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما, na hakuna ukinzani wowote baina ya rai mbili hizi, kwa sababu wao pia walikuwa ni miongoni mwa waja wa Allah تعالى Aliowachagua, japokuwa maelezo hayo yanawafaa na kuwastahili zaidi Manabii.

Anasema Aliyetukuka:

ءَاللهُ خَيْرٌ أَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣٩﴾

“Je! Allah ni bora, au wale wanaowashirikisha naye?”

Hili ni swali ambalo lina lengo la kuwasuta wapagani kwa kuabudu kwao miungu mingine badala ya Allah تعالى.

Dalili Kadhaa za Tawhidi (Kumpwekesha Allah تعالیٰ)

Kisha Alianza Aliyetukuka Kubainisha kuwa Yeye Peke Yake Ndiye Muumbaji, Mwenye Kuruzuku na Mwenye Kuratibu mambo. Akasema Aliyetukuka:

أَمَّنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

“Au nani yule aliyeziumba mbingu na ardhi”.

Maana yake: Aliumba mbingu ambazo ziko juu sana na safi kabisa, na Akajaalia ndani yake nyota zinazong’aa na sayari zinazozunguka. Na Akaiumba ardhi, na urefu na uzito unaotofautiana, na Akaumba kila kitu ndani yake, majabali, milima, mabonde, mandhari yenye miinuko na miporomoko, misitu, mimea, miti, matunda, bahari na hayawani wa aina tofauti, rangi, umbile na kadhalika. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً

“Na Akakuteremshieni maji kutoka mbinguni”.

Akaijaalia ni riziki kwa waja Wake.

فَأَنْبَتْنَا بِهِ حَدَابٍ ذَاتَ بَهْجَةٍ

“Na kwa hayo Tutazioletesha bustani zenye kupendeza?”

Maana yake: Yenye kuvutia na mandhari nzuri kwa mwenye kutazama.

مَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُنْبِتُوا شَجَرَهَا

“Nyinyi hamna uwezo wa kuiotesha miti yake”.

Nyinyi hamna uwezo kabisa wa kuiotesha miti yake. Yule aliye na uwezo wa kutekeleza hayo ni Muumbaji na Mwenye Kuruzuku, Ambaye Anafanya yote haya Peke Yake bila ya usaidizi wa aina yoyote kutoka kwa yeyote hata kwa sanamu na wapinzani wengine. Washirikina wenyewe walikubali hilo, kama Alivyosema Allah تعالیٰ katika Aya nyengine:

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

“Na kama ukiwauliza: “Ni nani aliyewaumba”. Kwa yakini watasema: “Ni Allah.” (43:87)

Aidha amesema:

وَلِإِن سَأَلْتَهُمْ مَنْ نَزَّلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِهَا لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

“Na ukiwauliza, “Ni nani ateremshaye maji mawinguni na kuihuisha ardhi baada ya kufa kwake? Bila shaka watasema: “Allah” (29: 63).

Wao wanakiri kuwa mwenye kufanya yote hayo ni Allah تعالى Peke Yake asiye kuwa na mshirika, kisha wao wanaabudu pamoja naye mwengine kwa wanaemtambua kuwa hawezi kuumba wala kuruzuku. Hakika ni kuwa Yule anayestahiki kuabudiwa Peke Yake katika ‘Ibaadah ni yule ambaye Ndiye Peke Yake Muumbaji na Mwenye Kuruzuku. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

أَأَلَّهُ مَعَ اللَّهِ

“ Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah? ”.

Kumaanisha kuwa je yupo mungu yoyote ambaye anaweza kuabudiwa pamoja na Allah تعالى, ilhali iko wazi kabisa kwa yeyote mwenye akili kuwa Yeye Ndiye Muumbaji na Mwenye Kuruzuku, kama mnavyokubali nyinyi? Kisha Akasema:

بَلْ هُمْ قَوْمٌ يَعِدُونَ ﴿٦٠﴾

“Bali hao ni watu waliopotoka”.

Maana yake: Wanawalinganisha wengine na kuwafananisha na Allah تعالى.

أَمْ نَجْعَلُ الْأَرْضَ قَرَارًا وَنَجْعَلُ خِلَالَهَا أَنْهَارًا وَنَجْعَلُ لَهَا رُوسِيَّ وَنَجْعَلُ بَيْنَ الْبَحْرَيْنِ

حَاجِرًا أَلَّهُ مَعَ اللَّهِ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦١﴾

61. “Au nani yule Aliyefanya ardhi mahali pa kutua, na Akajaalia ndani yake mito, na Akaweka milima? Na Akaweka baina ya bahari mbili kiziwizi? Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah? Bali wengi wao hawajui”.

Allah تعالیٰ Amesema:

أَمَّنْ جَعَلَ الْأَرْضَ قَرَارًا

“Au nani yule Aliyefanya ardhi mahali pa kutua”.

Maana yake: Bara imara lililotulia thabiti, halitembei wala kutikisika. Lau lingekuwa kinyume na hivyo haingekuwa dunia pahali pazuri kwa watu kuishi ndani yake. Lakini Alijaalia kwa Fadhila na Rehema Zake kuwa kama tandiko na busati imetulia tuli wala haitingishiki, kama Alivyosema Aliyetukuka katika Aya nyengine:

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً

“Allah ni Yule Aliyekufanyieni ardhi kuwa mahali penu pa kukaa, na mbingu kuwa dari.” (40:64).

وَجَعَلَ خِلَالَهَا أَتْهَرًا

“Na Akajaalia ndani yake mito.”

Ameweka mito yenye maji tamu, inayopita ardhini, na Akaifanya kuwa aina tofauti, mito mikubwa na mingine baina yake. Akaifanya itembee pande zote, mashariki, magharibi, kusini na kaskazini, kulingana na mahitaji ya binadamu katika maeneo, nchi na mabara tofauti, kwa namna Aliyowaumba wao katika pande mbalimbali za ardhi na Akawatamia riziki zao kulingana na mahitaji.

وَجَعَلَ لَهَا رَوَابِي

“Na Akaweka milima?”

Maana yake: Milima na majabali makubwa ambayo yanaituliza ardhi, kuifanya iwe imara ili isitingishike.

وَجَعَلَ بَيْنَ الْبَحْرَيْنِ حَاجِزًا

“Na Akaweka baina ya bahari mbili kiziwizi?”

Maana yake: Akaweka kizuizi baina ya maji tamu na yale ya chumvi, kuyazuia yasichanganyikane ili yasiharibu yale mengine. Hekima ya Allah تعالیٰ Imehukumu kuwa kila mmoja inafaa ibakie katika sifa iliyokusudiwa. Maji

matamu ni yale ya mito yanayomiminika miongoni mwa watu, na lengo la kuwepo kwake ni kuwa yawe tamu ili yatumiwe na wanyama kwa ajili ya kunywa, na kumwagilia mimea na miti ya matunda. Na bahari ya maji chumvi ni yale yanayozunguka mabara katika pembe zake zote. Maji yake yamekusudiwa yawe ni ya chumvi yasiyonyweka ili hewa isije ikaharibiwa kama Alivyosema Aliyetukuka:

* وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا
وَحِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٥٩﴾

“Naye Ndiye Anayeziunganisha bahari mbili; hii ni tamu, inayoondosha kiu, na hii ni yenye chumvi, kali; na akaweka kinga yao na kizuizi kizuiacho.” (25:53).

Kwa hilo Akasema Aliyetukuka:

أَلَيْسَ مَعَ اللَّهِ

“Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah?”.

Maana yake: Mungu yeyote anayeweza kufanya hivyo, au anayestahili kuabudiwa? Kwa kauli ya kwanza na ya pili, na kwa muktadha wa zote mbili ni sahihi. Anamalizia Allah تعالى Aya hiyo kwa Kusema:

بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٠﴾

“Bali wengi wao hawajui”.

Kwa kuabudu mwengine asiyekuwa Allah تعالى,

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ ۗ أَلَيْسَ مَعَ اللَّهِ
قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٦١﴾

62. “Au nani yule Anayemjibu mwenye shida pale Anapomuomba, na Akaiondoa dhiki, na Akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah? Ni machache mnayoyazingatia.”

Anatunabahisha Allah تعالى kuwa Yeye Ndiye Mwenye Kuombwa wakati wa shida na Kwake ndio wanaelekea pindi matatizo yanapowagonga au kuwafikia, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَاهُ

“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu.” (17:67).

Na Amesema تعالى:

ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْرُونَ ﴿٥٩﴾

“Kisha yakikuguseni madhara mnamnyanyatikia Yeye.” (16:53).

Kama hivyo Anasema hapa:

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ

“Au nani yule Anayemjibu mwenye shida pale Anapomuomba.”

Maana: Ni nani Aliye Peke Yake ambaye mtu mwenye shida anarudi Kwake, na wa Pekee Ambaye Anaondosha madhara pindi yanapomfikia? Imenukuliwa na Imamu Ahmad kuwa mtu mmoja kutoka Balhujaim alisema: “Ewe Mtume wa Allah, unawaita watu katika nini?” Akasema:

«أَدْعُو إِلَى اللَّهِ وَخَدُّهُ الَّذِي إِنْ مَسَّكَ ضُرٌّ فَدَعْوَتُهُ كَشَفَ عَنكَ، وَالَّذِي إِنْ أَضَلَّتْ بِأَرْضٍ قَفِرٍ فَدَعْوَتُهُ رَدَّ عَلَيْكَ، وَالَّذِي إِنْ أَصَابَتْكَ سَنَةٌ فَدَعْوَتُهُ أَنْتَبَتْ لَكَ»

“Ninaita kwa Allah Peke Yake, Ambaye likikupata dhara ukamuomba, Hukuondolea; na Ambaye ukipotea jangwani, ukamuomba, Atakurudisha (salama salimini); na Ambaye ukame ukikupata ukamuomba, Atakuoteshea mazao yako”. Akasema: “Niusie”. Akasema:

«لَا تَسْبِقْ أَحَدًا وَلَا تَزْهَدَنَّ فِي الْمَعْرُوفِ، وَلَوْ أَنْ تَلْقَى أَخَاكَ وَأَنْتَ مُبْسِطٌ إِلَيْهِ وَجْهَكَ، وَلَوْ أَنْ تُفْرَغَ مِنْ دَلْوِكَ فِي إِنَاءِ الْمُسْتَقِيِّ، وَأَتْرَزُ إِلَى نِصْفِ السَّاقِ فَإِنَّ أَيْتَ فَإِلَى الْكَعْبَتَيْنِ، وَإِيَّاكَ وَإِسْبَالَ الْإِزَارِ فَإِنَّ إِسْبَالَ الْإِزَارِ مِنَ الْمَخِيلَةِ وَإِنَّ اللَّهَ لَا يُجِبُ الْمَخِيلَةَ»

“Usimtusi yeyote na wala usichukie mazuri, japo ni kukutana na nduguyo kwa uso wa tabasamu, japo kumimina ndoo yako katika chombo cha anayetaka maji. Na vaa shuka mpaka nusu muundi, usipotaka kufanya hivyo basi mpaka kwenye kongo mbili, na tahadhari kuburuza shuka¹, kwani kuburuza shuka ni katika kiburi, na hakika Allah Hapendi kiburi”².

Kisa cha Mujaahid Aliyepigana Katika Njia ya Allah تعالى

Ametaja Al-Haafidh ibn ‘Asaakir رحمته الله تعالى katika historia yake ya Fatmah bint Al-Hasan Umm Ahmad Al-Ijliya kwamba alisema: “Wakati mmoja makafiri waliwashinda Waislamu katika vita. Alikuwapo farasi mzuri aliyemilikiwa na mtu tajiri ambaye pia alikuwa Mwema. Farasi huyo alisimama tu, hivyo mwenyewe akasema: “Una nini wewe? Ole wako! Mimi nilikuwa nakutayarisha tu kwa siku kama ya leo”. Farasi alimuambia: “Vipi mimi nisifanye vibaya, ikiwa uangalizi wangu umewaachia wasimamizi ambao hunidhulumu kwa kunipa chakula kichache?” Akasema: “Ninakuahidi mbele ya Allah تعالى kuwa kuanzia leo, mimi ndiye nitakayekulisha katika mapaja yangu”. Hivyo, farasi akaanza kukimbia, na mwenyewe akawa ni mwenye kuokolewa na baada ya hapo akawa anamlisha yeye mwenyewe katika mapaja yake. Jambo lake hilo likaenea kwa watu, nao walianza kuja kwake ili kusikia kutoka kwake mwenyewe. Habari hii ilimfikia Mfalme wa Roma, ambaye alisema: “Mji ambao uliona mtu huyu hautadhuriwa”. Alitaka kumleta mtu huyu katika mji wake, hivyo alimtuma murtadi (mtu aliyeacha Uislamu) aliyekuwa akiishi katika mji wake ili aende kwake, na alipomfikia alidai kuwa nia yake kwa Uislamu ni nzuri kabisa na wafuasi wake ni wazuri. Hivyo, mpiganaji yule alimuamini. Siku moja walikwenda kutembea kwenye ufuko wa bahari, lakini murtadi aliahidiana na mtu mwingine, mfuasi wa mfalme wa Roma, ili aje kumsaidia kumchukua mateka mpiganaji Jihadi. Walipotaka kutekeleza hilo, alinyanyua macho yake mbinguni na kusema: “Ewe Allah! Hakika amenidanganya kwa kuapa kwa Jina Lako, hivyo niokoe nao jinsi Unavyotaka”. Akasema:

¹ Ikawa inaburuza katika ardhi.

² Ahmad 5:64. Hadithi hii si Sahihi. Lakini sehemu zake nyingi za matini yake zinapatikana katika Hadithi ambazo ni Sahihi.

“Wakatokeza wanyama wawili wa pori na kuwachukua, na Mpiganaji Jihadi akarudi akiwa salama salimini.”¹

Warithi wa Dunia

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ

“Na Akakufanyeni warithi wa ardhi?”

Maana yake: Kila kizazi kinarithi kutoka kwa kizazi kilichotangulia, moja baada ya kingine, kama Alivyosema Allah تعالى:

إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَسْتَخْلِفْ مِنْ بَعْدِكُمْ مَا يَشَاءُ كَمَا أَنْشَأَكُمْ مِنْ ذُرِّيَةِ قَوْمٍ

ءَاخَرِينَ ﴿١٣٣﴾

“Akipenda Atakuondoeni na Awaweke wengine Awapendao badala yenu, kama vile Alivyokutoeni kutokana na uzazi wa watu wengine.” (6:133).

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلَائِفَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ

“Naye Ndiye Aliyekufanyeni makhalifa wa duniani, na Amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa.” (6:165).

Amesema Aliyetukuka:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً

“Na pale Mola wako Mlezi alipowaambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa.” (2:30).

Kumaanisha kaumu itakayokuja moja baada ya nyengine kama tulivyotangulia kueleza. Na hivyo ndivyo ilivyo Aya hiyo:

¹ Taarikh Dimashq 19:489.

وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ

“Na Akakufanyeni warithi wa ardhi?”

Maana yake: Ummah baada ya Ummah, kizazi baada ya kizazi na kaumu baada ya kaumu. Lau Angetaka, Angeweza Kuwaumba wote kwa wakati mmoja, na hangewafanya baadhi yao kuwa ni vizazi vya wengine. Lau Angependa, Angewaumba wote pamoja, kama Alivyomuumba adamu kutokana na udongo. Lau Angependa, Angewafanya baadhi yenu kuwa ni dhuria ya wengine, lakini hangemfanya yeyote miongoni mwao kufa mpaka wote wafe kwa wakati mmoja; kwa njia hiyo ardhi ingewadhiki na ingekuwa vigumu sana maisha yao na kuchuma kwao na wangukuwa ni wenye kudhuriana baadhi yao kwa wengine. Lakini Hekima Yake na Amri Yake imehukumu kuwa waumbwe wao kutokana na nafsi moja kisha waongezeke mara dufu, hivyo Akawaumba wao katika hii dunia, kizazi baada ya kizazi, na Ummah baada ya Ummah mpaka wakati wao ufike kikomo. Na hakutakuwa na yeyote atakayebaki katika ulimwengu huu kama alivyokadiria hayo Allah Aliyetukuka na kuhesabu idadi yao yote kwa ukamilifu wake. Kisha kitasimama Kiyama na kila mtendaji atapatiwa hesabu ya amali yake aliyoifanya, kwa kupatiwa ujira au adhabu kutegemea na matendo yake. Hivyo, Akasema Aliyetukuka:

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ ۗ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ

“Au nani yule Anayemjibu mwenye shida pale Anapomwomba, na Akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah?”

Maana yake: Mwenye Uweza wa kufanya hilo au muabudiwa pamoja na Allah تعالی baada ya yote haya awe ni mwenye kuabudiwa, baada ya kufahamu kuwa Allah تعالی ni wa Pekee Ambaye Anaweza kufanya hayo, Asiyekuwa na mshirika?”

قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٦٦﴾

“Ni machache mnayoyazingatia.”

Maana yake: Jinsi gani wanavyokuwa na fikra finyu kuhusu yale ambayo yanaweza kuwaongoa wao katika ukweli na kuwaonesha wao njia nyoofu.

أَمَّنْ يَهْدِيكُمْ فِي ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ وَالْبَحْرِ وَمَنْ يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ
 أَلَيْسَ اللَّهُ مَعَ اللَّهِ تَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٣﴾

63. "Au nani yule anayekuongoeni katika giza la bara na bahari, na akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehema zake? Je! Yupo mungu pamoja na Allah? Ametukuka Allah juu ya wanaowashirikisha Naye."

Anasema Aliyetukuka:

أَمَّنْ يَهْدِيكُمْ فِي ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ وَالْبَحْرِ

"Au nani yule anaye kuongoeni katika giza la bara na bahari?"

Kwa Alivyoumba miongoni mwa alama Zake zilizoko mbinguni na katika ardhi, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَعَلَّمَتِ وَيَا لَنَجْمٍ هُمْ يَتَّبِعُونَ ﴿٦٤﴾

"Na alama nyengine. Na kwa nyota wao wanajiongoza." (16:16).

Amesema tena Aliyetukuka:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ النُّجُومَ لِتَهْتَدُوا بِهَا فِي ظُلُمَاتِ اللَّيْلِ وَالْبَحْرِ

"Na Yeye Ndiye Aliyekuwekeeni nyota ili muongoke kwazo katika kiza cha bara na bahari." (6:97).

Na Anasema:

وَمَنْ يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ

"Na Akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehema zake?"

Maana yake: Mbele ya mawingu ambayo yana mvua ndani yake, kwayo Allah Huwaonesha Rehema waja Wake wanaokumbwa na ukame na waliokata tamaa. Basi:

أَلَيْسَ اللَّهُ مَعَ اللَّهِ تَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٥﴾

"Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah? Ametukuka Allah juu ya wanaowashirikisha naye."

أَمَّنْ يَبْدُوا أَلْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَمَنْ يَرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَلَيْسَ اللَّهُ بِذِي هَاتُوَا
بُرْهَانِكُمْ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٦٤﴾

64. “Au nani anayeuanzisha uumbaji, kisha akaurejesha? Na nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah? Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli”.

Yeye Ndiye Mwenye Uweza na Nguvu, hivyo Anayeumba viumbe na Hurejea Kuviumba.

Kama Alivyosema Aliyetukuka katika Aya nyengine:

﴿٦٥﴾ إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿٦٦﴾ إِنَّهُ هُوَ يُبْدِي وَيُعِيدُ ﴿٦٧﴾

“Hakika kutesa kwa Mola wako Mlezi ni kukali sana. Yeye Ndiye Aliyeanzisha na Ndiye Atakayewarejeza” (85:12-13).

Amesema tena Aliyetukuka:

﴿٦٨﴾ وَهُوَ الَّذِي يَبْدُوا أَلْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ﴿٦٩﴾ وَلَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ

“Na Yeye Ndiye Aliyeanzisha viumbe na Ndiye Atakayevirudisha mara nyengine, na jambo hili ni rahisi zaidi Kwake.” (30:27)

Anaendelea Aliyetukuka:

﴿٧٠﴾ وَمَنْ يَرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Na nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi?”

Kwa mvua Anayoiteremsha kutoka mbinguni na kuchepuza Baraka ya ardhi, kama Alivyosema kwengineko:

﴿٧١﴾ وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ﴿٧٢﴾ وَالْأَرْضِ ذَاتِ الصَّدْعِ ﴿٧٣﴾

“Naapa kwa mawingu yanayoleta mvua. Na kwa ardhi inayopasuka na kutoa mimea.” (86:11-12).

Na Amesema Aliyetukuka:

يَعْلَمُ مَا يَلْجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا

“Anajua yaingiayo katika ardhi na yatokayo humo na yateremkayo mbinguni na yapandayo humo.” (34:2).

Yeye ni Aliyetukuka, Anateremsha maji yenye Baraka kutoka mbinguni, ambayo yanapenya katika ardhi, kisha yanatiririka kama chemchem. Kisha kwa kupitia maji hayo anatoa kila aina ya mazao, matunda na maua na vyenginevyo, vikiwa na rangi tofauti. Hivyo:

كُلُوا وَارْزُقُوا أَتَعْمَكُمُ إِنِّي فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأُلْبَانِ

“Kuleni, na mchunge wanyama wenu. Hakika katika hayo zipo ishara kwa wenye akili.” (20:54).

Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

أَأَلَيْتُمْ مَعَ اللَّهِ

“Je! Yupo muabudiwa pamoja na Allah?”

Kumaanisha ni nani aliyefanya haya? Au kulingana na tafsiri nyengine: Baada ya haya yote (nani anayestahili kuabudiwa)? Basi:

قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.”

Toeni dalili kuonesha usahihi wa mnavyoviabudu miongoni mwa 'Ibaadah ya miungu wengine. Katika hilo naye anajua kuwa hawana hoja wala ushahidi, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ

الْكَافِرُونَ

“Na anayemuomba pamoja na Allah, muabudiwa mwengine hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hisabu yake iko kwa Mola Wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.” (23:117).

قُلْ لَا يَعْلَمُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٦٥﴾
 بَلِ أَدْرَاكَ عِلْمُهُمْ فِي الْآخِرَةِ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِنْهَا بَلْ هُمْ مِّنْهَا عَمُونَ ﴿٦٦﴾

65. "Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipokuwa Allah. Wala wao hawajui lini watafufuliwa.

66. Kwani huo ujuzi wao umefikilia kuijua Akhera? Bali wao wamo katika shaka nayo tu, bali wao ni vipofu nayo".

Mwenye Elimu ya Ghaibu ni Allah تعالی

Allah تعالی Anamuamuru Mtume Wake Kuwajulisha viumbe vyote kwamba hakuna miongoni mwa wakaazi wa mbinguni na ardhini anayejua ghaibu, ila Allah تعالی. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِلَّا اللَّهُ

"Isipokuwa Allah."

Hii ni ibara ya kipekee kabisa, inamaanisha hakuna anayejua ghaibu mbali na Allah تعالی, Yuko Peke Yake katika hili, akiwa hana mshirika katika Elimu hiyo. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

* وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ

"Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu." (6:59).

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنزِلُ الْغَيْثَ

"Kwa hakika ujuzi wa Kiyama uko kwa Allah tu; naye Huteremsha mvua (Atakapo)."

Mpaka mwisho wa Surah (31:34). Na Aya katika masiala haya ni nyingi sana:

﴿٦٦﴾ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٦٧﴾

"Wala wao hawajui lini watafufuliwa".

Hiyo ni kuwa viumbe vinavyoishi mbinguni na katika ardhi havijui Kiyama kitakuwa lini, kama Alivyosema Aliyetukuka:

ثُقُلْتِ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا تَأْتِيكُمُ إِلَّا بَعْتَةٌ

“Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haikujiini ila kwa ghafla tu.”
(7:187).

Aya inamaanisha, Elimu ya jambo kubwa na zito kwa viumbe vya mbinguni na ardhini.

بَلِ أَدْرَاكَ عِلْمُهُمْ فِي الْآخِرَةِ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِّنْهَا

“Kwani huo ujuzi wao umefikilia kujua Akhera? Bali wao wamo katika shaka nayo tu.”

Maana yake: Ujuzi wao na kustaajabu kwao kunamalizika bila ya kujua wakati wake hasa. Na wanasema wanazuoni wengineo. Hii ina maana wote wanakuwa sawa katika kulijua hilo, kama ilivyonyukuliwa Hadithi katika Sahih Muslim kuwa Mtume ﷺ alimuambia Jibril عليه السلام pale alipomuuliza kuhusu wakati wa Kiyama, alisema:

«مَا الْمَسْئُولُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ»

“Mwenye kuulizwa si mjuzi zaidi kuliko mwenye kuuliza.”¹

Kwa maana nyingine, wote wako sawa kwa ile hakika kuwa ujuzi wao hauendi mbali. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِّنْهَا

“Bali wao wamo katika shaka nayo tu.”

Ibara hii inarudi kwa wanadamu, muradi ikiwa ni makafiri, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَعَرِّضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًا لَّقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ بَلْ زَعَمْتُمْ أَلَّنْ نَجْعَلَ لَكُمْ

مَّوْعِدًا

¹Muslim 1:36

“Na wakahudhurishwa mbele ya Mola wako Mlezi kwa safu (wakaambiwa): Mmetujia kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza! Bali mlidai kwamba Hatutakuwekeeni miadi.” (18:48).

Maana yake: Makafiri miongoni mwenu. Na hivyo hivyo, ndivyo ilivyosemwa hapa:

بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِنْهَا

“Bali wao wamo katika shaka nayo tu.”

Wao wana shaka ya kuwepo na kutokea kwake.

بَلْ هُمْ مِنْهَا عُمُونَ ﴿٥٩﴾

“Bali wao ni vipofu nayo.”

Hakika ni kuwa wapo katika upofu na ujinga mkubwa kuhusu jambo hilo.

* * *

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَيُّذَا كُنَّا تُرَابًا
 وَءَابَاؤُنَا أَيُّذَا لَمُخْرَجُونَ ﴿٦٧﴾
 لَقَدْ وَعِدْنَا هَذَا لَحْنُ وَءَابَاؤُنَا مِنْ
 قَبْلُ إِنْ هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأُولِينَ ﴿٦٨﴾
 قُلْ سِيرُوا فِي
 الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٦٩﴾ وَلَا
 تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُنْ فِي ضَيْقٍ مِمَّا يَمْكُرُونَ ﴿٧٠﴾
 وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧١﴾ قُلْ
 عَسَى أَنْ يَكُونَ رَدِفَ لَكُمْ بَعْضُ الَّذِي تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٧٢﴾
 وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَئِنْ أَسْأَلْتَهُمْ لَا
 يَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَيَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا
 يُعْلِنُونَ ﴿٧٤﴾ وَمَا مِنْ غَائِبَةٍ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِلَّا فِي
 كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٧٥﴾ إِنَّ هَذَا الْقُرْآنَ يَفُصِّلُ عَلَى بَيْتِي
 إِسْرَائِيلَ أَكْثَرَ الَّذِي هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٧٦﴾ وَإِنَّهُ
 هُدًى وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٧﴾ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ
 بِحُكْمِهِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ ﴿٧٨﴾ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّكَ
 عَلَى الْحَقِّ الْمُبِينِ ﴿٧٩﴾ إِنَّكَ لَا تَسْمَعُ الْمَوْتَى وَلَا تَسْمَعُ
 الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلُوا مَدِيرِينَ ﴿٨٠﴾ وَمَا أَنْتَ بِهَادِي
 الْعُمَى عَنْ ضَلَالَتِهِمْ ۗ إِنْ تَسْمَعُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ
 مُسْلِمُونَ ﴿٨١﴾ * وَإِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ أَخْرَجْنَا هُمْ
 دَابَّةً مِّنَ الْأَرْضِ نَكَلِمُهُمْ أَنَّ النَّاسَ كَانُوا بِآيَاتِنَا لَا
 يُوقِنُونَ ﴿٨٢﴾

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَيُّذَا كُنَّا تُرَابًا
 وَءَابَاؤُنَا أَيُّذَا لَمُخْرَجُونَ ﴿٦٧﴾
 لَقَدْ وَعِدْنَا هَذَا لَحْنُ وَءَابَاؤُنَا مِنْ
 قَبْلُ إِنْ هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأُولِينَ
 ﴿٦٨﴾ قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا
 كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٦٩﴾
 وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُنْ فِي ضَيْقٍ
 مِمَّا يَمْكُرُونَ ﴿٧٠﴾

67. "Na wakasema walio-
 kufuru: Tutapokuwa
 mchanga, sisi na baba zetu,
 hivyo kweli tutakujatolewa?"

68. Haya haya tuliahidiwa
 sisi na baba zetu zamani.
 Hayakuwa haya ila ni
 hadithi za uwongo za watu
 wa kale.

69. Sema: Nendeni katika
 ardhi, na tazameni uliku-
 waje mwisho wa wakosefu.

70. Wala usiwahuzunike
 wala usiwe katika dhiki
 kwa sababu ya hila zao
 wanazozifanya."

Kuwa na Shaka na Kubainisha Hoja Hiyo

Allah تعالى, Anasema kwa Kutuelezea kuhusu washirikina wenye kukanusha ufufuo kuwa wao wameona haiwezekani kufufuliwa baada ya kuwa maiti, mifupa, na mchanga. Kisha Akasema:

لَقَدْ وَعِدْنَا هَذَا لَحْنُ وَاَبَاؤُنَا مِنْ قَبْلُ

“Haya haya tuliahidiwa sisi na baba zetu zamani.”

Bado tunaendelea kusikia maneno hayo sisi pamoja na baba zetu wala hatuoni uhakika wake wala kutokea jambo hilo. Na Kauli yao:

إِنَّ هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٦٧﴾

“Hayakuwa haya ila ni hadithi za uwongo za watu wa kale.”

Hapa wanamaanisha kuwa ahadi hiyo kuwa miili itarudishwa (kama ilivyokuwa),

إِلَّا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٦٨﴾

“Ila ni hadithi za uwongo za watu wa kale.”

Hii inamaanisha kuwa hekaya hizo zimechukuliwa kutoka kwa watu waliokuja kabla (wa zamani) kutoka katika vitabu vilivyopatikana kutoka kwa baadhi yetu kwa wengine, lakini hazina uhakika wowote. Allah Aliyetukuka Amesema Kuwajibu kwa yale waliyoyadhania ya ukafiri na ile nadharia yao kuwa hakutakuwa na ufufuo.

قُلْ

“Sema”Ewe Muhammad,

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَنقَبَةُ الْمُجْرِمِينَ ﴿٦٩﴾

“Nendeni katika ardhi, na tazameni ulikuwaje mwisho wa wakosefu.”

Maana yake: Wale wenye kukadhibisha Mitume na kwa yale waliokuja nayo katika masiala ya kufufuliwa na mengineyo, jinsi gani walivyokumbwa na Ghadhabu ya Allah تعالى, Adhabu Yake na onyo kali kutoka Kwake. Katika hao,

Allah تعالی Aliwaokoa Mitume Wake Watukufu na wafuasi wao Waumini. Hivyo ilikuwa ni dalili ya ukweli wa risala iliyoletwa na Mitume. Kisha Akasema Aliyetukuka Kumliwaza Mtume Wake:

وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ

“Wala usiwahuzunikia”. Wale wanaokadhibisha uliokuja nayo. Usiwe ni mwenye kuwahuzunikia kwa kutaka kujiua kwa majuto kwa ajili yao. Pia:

وَلَا تَكُنْ فِي ضَيْقٍ مِّمَّا يَمْكُرُونَ ﴿٧١﴾

“Wala usiwe katika dhiki kwa sababu ya hila zao wanazozifanya”.

Kwa sababu ya vitimbi vyao na kuyakataa uliyokuja nayo, kwani Allah تعالی Atakusaidia na Kukuunga mkono, na Ataidhirisha Dini yako juu ya wale wenye Kukupinga na Kukufanyia inadi, walio mashariki na magharibi.

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧١﴾ قُلْ عَسَى أَنْ يَكُونَ رَدِفَ لَكُمْ

بَعْضُ الَّذِي تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٧٢﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا

يَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ لَيَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٤﴾ وَمَا مِنْ غَائِبَةٍ فِي

السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٧٥﴾

71. “Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa mnasema kweli?”

72. Sema: Asaa ni karibu kukufikieni sehemu ya yale mnayoyahimiza.

73. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Fadhila kwa watu, lakini wengi wao hawashukuru.

74. Na hakika Mola wako Mlezi Anayajua yanayoficha vifua vyao na wanayoyatangaza.

75. Na hakuna siri katika mbingu na ardhi ila imo katika Kitabu kinachobainisha.”

Allah تعالی Anatueleza jinsi washirikina walivyouliza kuhusu Siku ya Kiyama, lakini wakadhania kuwa haitokuja kutokea:

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧٦﴾

“Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa mnasema kweli?”

Allah تعالی Akawajibu kwa kusema:

قُلْ

“Sema”Ewe Muhammad.

عَسَىٰ أَنْ يَكُونَ رَدِفَ لَكُمْ بَعْضُ الَّذِي تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٧٧﴾

“Asaa ni karibu kukufikieni sehemu ya yale mnayoyahimiza”.

Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Kile ambacho mnataka kifike haraka kimekuja karibu nanyi, au baadhi yake imekuja karibu”¹. Hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya Mujaahid, Adh-Dhahhaak, ‘Atwaa’, Al-Khuraasaaniy, Qataadah na As-Suddiy². Na hii ndiyo muradi (lengo) wa Kauli Yake Aliyetukuka:

وَيَقُولُونَ مَتَى هُوَ قُلْ عَسَىٰ أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا ﴿٧٨﴾

“Na watasema: Lini hayo? Sema: Asaa yakawa karibu.” (17:51).

Amesema tena Aliyetukuka:

يَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٧٩﴾

“Wanakupimiza adhabu (ije upesi upesi). Na hali ya kuwa Jahanamu itawazunguka makafiri.” (29:54).

Na hakika imeungishwa *Laam* katika Kauli Yake;

عَسَىٰ أَنْ يَكُونَ رَدِفَ لَكُمْ

“Asaa ni karibu kukufikieni”. Yenye maana ya kuharakishwa (kuletwa haraka) kwenu, kama alivyosema Mujaahid katika riwaya yake³. Kisha Akasema Allah تعالی:

¹ At-Tabari 19:492.

² At-Tabari 19:492 na Ad-Durr Al-Manthuur 6:375.

³ At-Tabari 19:492.

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ

“Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Fadhila kwa watu.”

Hakika ni kuwa Allah تعالى Anawapa Neema na Fadhila Zake kwa wingi japokuwa wanazidhulumu nafsi zao, pamoja na hayo yote hawamshukuru Allah تعالى ila wachache miongoni mwao.

وَإِنَّ رَبَّكَ لَيَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٦﴾

“Na hakika Mola wako Mlezi Anayajua yanayoficha vifua vyao na wanayoyatangaza.”

Maana yake: Yeye anajua dhamiri zao zilizofichwa katika vifua vyao na siri kama vile Anavyojua Dhahiri. Anasema Aliyetukuka katika Aya nyengine.

سَوَاءٌ مِنْكُمْ مَنْ أَسْرَأَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ

“Ni sawa anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhihirisha.”
(13:10). Aidha:

يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿٧٧﴾

“Yeye Anajua siri na duni kuliko siri.” (20:7).

Anasema tena:

أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ

“Jueni kuwa wanapojigubika nguo zao Yeye Anajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza.” (11:5).

Kisha Anatupasha habari Aliyetukuka kuwa Yeye ndio Mjuzi wa ghaibu iliyopo mbinguni na ardhini, na hakika Yeye ni Mjuzi wa ghaibu na yanayoonekana, nayo ni yale yasiyoonekana na waja na yale wanayoyaona. Hivyo, Akasema:

وَمَا مِنْ غَائِبَةٍ

“Na hakuna siri.” Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema : “Hiyo inamaanisha, hakuna chochote.”¹

¹ At-Tabari 19:494.

فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٧٦﴾

“Katika mbingu na ardhi ila imo katika Kitabu kinachobainisha.”

Hii ni kama Kauli Yake:

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِنَّ ذَلِكَ فِي كِتَابٍ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ

يَسِيرٌ ﴿٧٧﴾

“Je! Hujui kwamba Allah Anayajua yaliyomo mbinguni na katika ardhi? Hakika hayo yamo Kitabuni. Hakika hayo kwa Allah ni mepesi.” (22:70).

إِنَّ هَذَا الْقُرْآنَ يَقُصُّ عَلَى بَنِي إِسْرَائِيلَ أَكْثَرَ الَّذِي هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٧٨﴾ وَإِنَّهُ

هُدًى وَرَحْمَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٩﴾ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ بِحُكْمِهِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ ﴿٨٠﴾

فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۚ إِنَّكَ عَلَى الْحَقِّ الْمُبِينِ ﴿٨١﴾ إِنَّكَ لَا تَسْمَعُ الْمَوْتَى وَلَا تَسْمَعُ الصُّمَّ

الدُّعَاءَ إِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِينَ ﴿٨٢﴾ وَمَا أَنْتَ بِهَادِي الْعُجْبَىٰ عَن ضَلَالَتِهِمْ ۗ إِنَّ تَسْمَعُ إِلَّا مَن

يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٣﴾

76. “Hakika Qur’ani hii inawasimulia wana wa Israili mengi wanayo khitilafiana nayo.

77. Nayo hakika ni Uongofu na Rehema kwa Waumini.

78. Hakika Mola wako Mlezi Atawahukumu kwa Hukumu Yake, Naye ni Mwenye Nguvu, Mjuzi.

79. Basi Mtegemea Allah; hakika wewe uko juu ya Haki iliyo wazi.

80. Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya maiti wasikie, wala kuwafanya viziwi wasikie wito, wanapokwishageuka kwenda zao.

81. Wala huwezi kuwaongoa vipofu waache upotovu wao. Huwezi kuwafanya wasikie isipokuwa wenye kuziamini Ishara Zetu; na hao ndio watiifu.”

Qur'ani Inahadithia Tofauti baina ya Wana wa Israili na Allah تعالى Anahukumu baina Yao

Allah تعالى Anasema Kutupasha habari kuhusu Kitabu Chake Kitukufu ambacho ndani yake muna uwongofu, hoja, ushahidi na kipambanuzi baina ya haki na batili. Hakika Yeye Anatusimulia kuhusu Wana wa Israili, ambao walikabidhiwa Taurati na Injili:

أَكْثَرَ الَّذِي هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٦٧﴾

“Mengi wanayokhitilafiana nayo”.

Mfano ni kama hitilafu zao kuhusu Isa عليه السلام Mayahudi waliongopa kuhusu yeye ilhali Wakristo walivuka mipaka katika kumsifu na kumtukuzi. Hivyo Qur'ani ikaja na kauli ya kati na kati iliyo ya kweli, haki na ya uadilifu. Ikaeleza kuwa yeye alikuwa ni mja kati ya waja wa Allah تعالى, Nabii Wake na mmoja wa Mitume Wake, juu yake ziwe Rehema na Amani. Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ ۗ قَوْلَ الْحَقِّ الَّذِي فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٣٤﴾

“Huyo ndiye 'Isaa mwana wa Maryam. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka” (19:34).

Na Kauli Yake:

وَإِنَّهُ هُدًى وَرَحْمَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٠﴾

“Nayo hakika ni Uongofu na Rehema kwa Waumini.”

Huo ni uongofu kwa nyoyo za wenye kuiamini na ni rehema kwao katika amali zao. Kisha Anasema Aliyetukuka:

إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ

“Hakika Mola wako Mlezi Atawahukumu baina yao.”

Maana yake: Siku ya Kiyama.

بِحُكْمِهِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ

“Kwa Hukumu Yake, Naye ni Mwenye Nguvu”.

Katika Kulipiza kisasi. Naye pia ni,

الْعَلِيمُ ﴿٧٨﴾

"Mjuzi".

Kwa matendo yote na kauli zote anazotenda na kunena mja Wake.

Amri ya Kumtegemea Allah تعالى katika Kufikisha Ujumbe

Anasema Aliyetukuka:

فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ

"Basi Mtegemee Allah."

Katika mambo yako yote na katika kufikisha ujumbe kutoka kwa Mola wako Mlezi.

إِنَّكَ عَلَى الْحَقِّ الْمُبِينِ ﴿٧٩﴾

"Hakika wewe uko juu ya Haki iliyo wazi."

Jua ya kwamba wewe uko katika haki iliyo wazi kabisa japokuwa watakupinga wanaokupinga kwa sababu wao watakuwa ni wenye kuangamia. Neno la Mola wako Mlezi limethibitishwa kuwa wao hawataamini hata ikiwa wataletewa ishara zote. Kwa hilo Akasema Aliyetukuka:

إِنَّكَ لَا تَسْمَعُ أَمْوَاتٍ

"Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya maiti wasikie."

Maana yake: Hutawasikilizisha kitu chochote ambacho kitawanufaisha. Hivyo hivyo kwa wale wenye kifuniko katika mioyo yao na juu ya masikio yao uziwi wa ukafiri. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَلَا تَسْمَعُ الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِينَ ﴿٨٠﴾ وَمَا أَنْتَ بِهَدَى الْعَمَىٰ عَنِ ضَلَالَتِهِمْ ۗ إِنَّ

تَسْمَعُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ بِغَايَتِنَا فَهُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨١﴾

"Wala huwezi kuwafanya viziwi wasikie wito, wanapokwisha geuka kwenda zao. Wala huwezi kuwaongoa vipofu waache upotovu wao. Huwezi kuwafanya wasikie isipokuwa wenye kuziamini Ishara Zetu; na hao ndio watiifu."

Hakika anayekuitikia wito wako ni yule anayesikia na kuona, wale wenye masikizi na uoni wenye faida na manufaa, wenye moyo mwelekevu, na wenye kunyenyekea kwa Allah تعالى na ujumbe uliokuja kwao kupitia katika ndimi za Mitume, Amani iwe juu yao.

❖ وَإِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَابَّةً مِّنَ الْأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ النَّاسَ كَانُوا بِآيَاتِنَا

لَا يُوقِنُونَ ﴿٨٢﴾

82. "Na itapowaangukia kauli juu yao, Tutawatolea mnyama katika ardhi atakayewasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana yakini na Ishara Zetu."

Kutoka Mnyama katika Ardhi

Mnyama huyu atatoka zama za mwisho, wakati watu watakapoharibikiwa na kuacha Amri za Allah تعالى na kuibadili Dini ya kweli na ya haki. Allah تعالى katika wakati huo Atawatolea mnyama kutoka katika ardhi. Panasemwa ya kuwa atatoka Makkah, au kutoka sehemu nyingine kama yataavyokuja maelezo hayo kwa kina, Allah تعالى Akipenda. Mnyama huyo atazungumza na watu kuhusu hilo. Amesema Ibn 'abbaas, Al - Hasan na Qataadah رضي الله عنهم, na imepokelewa kutoka kwa 'Aliy رضي الله عنه: "Atazungumza maneno, kumaanisha atawasemesha"¹.

Hakika Hadithi na *Aathaar* nyingi zimejaa habazi za mnyama huyo, na hapa tutazitaja zile atakazotuwezesha Allah تعالى, kwani ni Kwake ndio tunataka usaidizi. Imenukuliwa na Imamu Ahmad رحمه الله تعالى kuwa Hudhayfa ibn Asid Al-Ghifaari رضي الله عنه amesema: "Mtume ﷺ alitoka katika chumba chake tukiwa tunazungumza kuhusu Kiyama. Akasema:

لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى تَرَوْا عَشْرَ آيَاتٍ: طُلُوعُ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا، وَالذُّخَانُ
وَالدَّابَّةُ وَخُرُوجُ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ، وَخُرُوجُ عِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ،
وَالدَّجَالُ، وَثَلَاثَةُ حُسُوفٍ: حَسْفٌ بِالْمَغْرِبِ، وَحَسْفٌ بِالْمَشْرِقِ، وَحَسْفٌ بِحَزِيرَةَ
الْعَرَبِ، وَنَارٌ تَخْرُجُ مِنْ قَعْرِ عَدْنٍ تَسُوقُ أَوْ تَحْسُرُ النَّاسَ، تَبَيَّتْ مَعَهُمْ حَيْثُ بَاتُوا
وَتَقِيلُ مَعَهُمْ حَيْثُ قَالُوا

¹ Atw-Twabariy 19:500.

“Kiyama hakitosimama mpaka mtakapoona alama kumi: Kuchomoza jua upande wa magharibi, moshi, mnyama, kuja kwa Ya’juuj na Ma’juuj, kuja kwa ‘Isaa ibn Maryam, Dajjaal, kudidimia kwa ardhi tatu, moja upande wa magharibi, moja mashariki na moja katika Bara Arabu, moto ambao utatoka katikati ya Yemen, utakaowapeleka au kuwakusanya watu, kusimama nao watakaposimama kwa usiku au kupumzika pamoja nao pale wanapopumzika wakati wa mchana”¹.

Hivi ndivyo alivyopokea Muslim na wanazuoni wa Sunan kutoka kwa Hudhayfah رضي الله عنه, Katika hadithi *mawquf*² At-Tirmidhi amesema, ni hadithi sahihi yenye daraja hasan³. Pia imepokewa na Imam Muslim kutoka kwa Hudhayfa رضي الله عنه katika hadith ambayo ni *marfuu’an*⁴. Allah تعالى Anajua zaidi.

Hadithi Nyengine

Imepokewa na Muslim ibn al-Hajjaj رحمه الله تعالى kuwa ‘Abdullah ibn ‘Amr رضي الله عنه amesema: “Nimehifadhi kutoka kwa Mtume ﷺ Hadithi ambayo bado sijaisahau. Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِنَّ أَوَّلَ الْآيَاتِ خُرُوجًا طُلُوعَ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا، وَخُرُوجُ الدَّابَّةِ عَلَى النَّاسِ ضُحَى، وَأَيُّهُمَا مَا كَانَتْ قَبْلَ صَاحِبَتِهَا فَالْأُخْرَى عَلَى إِثْرِهَا قَرِيًّا»

“Hakika alama ya kwanza kutokea ni kuchomoza jua kutoka magharibi, kutokeza mnyama kwa watu wakati wa Duhaa. Yoyote kati ya hizo mbili itakayotokeza mwanzo, basi ya pili itafuata kwa karibu nyuma yake.”⁵

Hadithi Nyengine

Imepokewa na Muslim رحمه الله تعالى katika Sahih yake kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

¹ Ahmad 4:6.

² Ni hadith ambayo imefika kwa sahaba tu.

³ Muslim 4:2225, Abu Daawuud 4:491, Tuhfat al-Ahwadhiy 6:413, An-Nasaa’iy katika al-Kubraa 6:456 na Ibn Maajah 2:1341.

⁴ Muslim 4:2226. Ni Hadithi ambayo inaonesha kuwa imefika kwa Mtume ama kwa vitendo, maneno kwa kuwa imeunganika moja kwa moja.

⁵ Muslim 4:2260.

«بَادِرُوا بِالْأَعْمَالِ سَيِّئًا، طُلُوعِ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا، وَالذُّخَانَ، وَالذَّجَالَ، وَالذَّابَّةَ،
وَخَاصَّةً أَحَدِكُمْ، وَأَمْرَ الْعَامَّةِ»

"Fanyeni haraka kufanya amali nzuri kabla ya mambo sita kutokeza kwenu: Kuchomoza jua kutoka magharibi, moshi, Dajjaal, mnyama, kifo cha mmoja wa vipenzi vyako, na mateso ya kijumla". Hii ilinukuliwa na Muslim peke yake.¹

Hadithi Nyengine

Ibn Majah رضي الله عنه amenukuu kutaka kwa Anas bin Malik رضي الله تعالى عنه kuwa amesema:

«بَادِرُوا بِالْأَعْمَالِ سَيِّئًا: الذُّجَالَ، وَالذُّخَانَ، وَذَابَّةَ الْأَرْضِ، وَطُلُوعِ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا، وَأَمْرَ الْعَامَّةِ، وَخَوِيصَّةً أَحَدِكُمْ»

"Fanyeni haraka kufanya amali nzuri kabla ya mambo sita kutokeza kwenu, Dajjal, Moshi, mnyama, Jua kuchomoza magharibi, mateso ya kijumla, na kifo cha mmoja wa vipenzi vyako." Hii ilinukuliwa na Muslim peke yake.²

Hadithi Nyengine

Imepokewa na Abu Daawud At-Tayalisi رضي الله تعالى عنه kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«تَخْرُجُ ذَابَّةُ الْأَرْضِ وَمَعَهَا عَصَا مُوسَى وَخَاتَمُ سُلَيْمَانَ عَلَيْهِمَا السَّلَامُ، فَتَخْطُمُ أَنْفَ الْكَافِرِ بِالْعَصَا، وَتُجَلِّي وَجْهَ الْمُؤْمِنِ بِالْخَاتَمِ، حَتَّى يَجْتَمِعَ النَّاسُ عَلَى الْخِوَانِ يُعْرِفُ الْمُؤْمِنُ مِنَ الْكَافِرِ»

"Atatoka mnyama kutoka katika ardhi akiwa na fimbo ya Musa na pete ya Sulaymaan. Ataigonga pua ya kafiri kwa fimbo, na ataufanya uso wa Muumini kung'aa kwa pete, mpaka watakapojumuika watu kwa ajili ya chakula, atampambanua Muumini kutokana na kafiri"³.

Pia hii imepokelewa na Imam Ahmad رضي الله تعالى عنه kwa maneno yafuatayo:

¹ Muslim 4:2267.

² Ibn Majah 2:1348.

³ At-Tayalisi 334.

«فَتَخَطِيمُ أَنْفِ الْكَافِرِ بِالْخَاتِمِ، وَتَجَلُّو وَجْهَ الْمُؤْمِنِ بِالْعَصَا، حَتَّىٰ إِنَّ أَهْلَ الْجِبَانِ
الْوَّاحِدِ لَيَجْتَمِعُونَ فَيَقُولُ هَذَا: يَا مُؤْمِنُ، وَيَقُولُ هَذَا: يَا كَافِرُ»

“Ataigonga pua ya kafiri kwa pete na ataufanya uso wa Muumini kung’aa kwa fimbo, mpaka watakapojumuika watu kwa ajili ya chakula, atampambanua Muumini kutokana na kafiri.”¹ Pia hii imepokelewa na Ibn Majah.²

Imepokewa na Ibn Jurayj kuwa Ibn Zubayr رضي الله عنه alimuelezea mnyama huyo kwa kusema: “Kichwa chake ni cha fahali (ng’ombe dume), macho yake ni kama ya nguruwe, masikio yake ni kama ya ndovu, pembe zake ni kama za paa dume, shingo yake ni kama mbuni, kifua chake ni kama cha simba, rangi yake ni kama ya chui, tako lakini kama la paka, mkia wake ni kama wa kondoo dume, na miguu yake ni kama ya ngamia. Baina ya viungo viwili ni masafa ya dhiraa kumi na mbili. Atakuja pamoja nayo fimbo ya Musa عليه السلام na pete ya Sulaymaan عليه السلام. Hakuna hata Muumini atakayebakia bila ya yeye kumweka pako jeupe kwenye uso wake, ambalo litapanuka mpaka uso wake utakuwa unang’aa. Hakuna kafiri atakayebakia bila yeye kumtia doa jeusi usoni mwake, ambalo litaenea mpaka uso wote kuwa mweusi. Mpaka watu watakapokuwa wanafanya biashara (kuuziana) masokoni, watakuwa wanasema: “Hii ni bei gani, ewe Muumini? Hii ni bei gani, ewe kafiri?” Hata watu wa nyumba moja watakuwa wanaketi kwenye meza kwa ajili ya kula, watamtambua Muumini kutokana na kafiri. Kisha atawaambia wao mnyama huyo: “Ewe fulani, pata bishara njema kwani wewe ni miongoni mwa watu wa Peponi. Na wewe fulani, hakika wewe ni mtu wa Motoni.” Hiyo ni Kauli ya Allah تعالى.

* وَإِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَابَّةً مِّنَ الْأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ النَّاسَ كَانُوا بِآيَاتِنَا

لَا يُوقِنُونَ ﴿٤٦﴾

“Na itapowaangukia kauli juu yao, Tutawatolea mnyama katika ardhi atakayewasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana yakini na Ishara Zetu.”³

* * *

¹ Ahmad 2:295.

² Ibn Majah 2:1351.

³ Al-Baghwi 3:429.

وَيَوْمَ نَخْشُرُ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ فَوْجًا مِمَّنْ
 يُكَذِّبُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿٨٣﴾
 حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُمْ قَالَ أَكَذَّبْتُمْ
 بِآيَاتِي وَلَمْ تُحِطُوا بِهَا عَلِمًا أَمَّا
 أَنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٨٤﴾ وَوَقَعَ
 الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ بِمَا ظَلَمُوا فَهُمْ لَا
 يَنْطِقُونَ ﴿٨٥﴾ أَلَمْ يَرَوْا أَنَّا
 جَعَلْنَا اللَّيْلَ لَيْسَكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ
 مُبْصِرًا ۗ إِنِّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٨٦﴾ وَيَوْمَ
 يُنْفَخُ فِي الصُّورِ فَنُزِعَ
 مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ
 إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ ۗ وَكُلُّ
 أُنثَىٰ دَٰخِرِينَ ﴿٨٧﴾ وَتَرَىٰ الْجِبَالَ
 تَحْسِبُهَا جَامِدًا وَهِيَ تَمُرُّ
 مَرَّ السَّحَابِ ۗ صَنَعَ اللَّهُ الَّذِي
 أَنْتَقَنَ كُلَّ شَيْءٍ ۗ إِنَّهُ خَبِيرٌ
 بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨٨﴾ مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ
 فَلَهُ خَيْرٌ مِّمَّا وَهُمْ مِنْ فِرْعَ
 يَوْمِئِذٍ ءَامِنُونَ ﴿٨٩﴾ وَمَنْ جَاءَ
 بِالسَّيِّئَةِ فَكُبَّتْ وُجُوهُهُمْ فِي
 النَّارِ هَلْ تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ
 تَعْمَلُونَ ﴿٩٠﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ أَنْ
 أَعْبُدَ رَبَّ هٰذِهِ الْبَلَدَةِ
 الَّذِي حَرَّمَهَا وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ ۗ
 وَأَمْرُهُ أَنْ أَكُونَ مِنَ
 الْمُسْلِمِينَ ﴿٩١﴾ وَأَنْ أَتْلُوَ الْقُرْآنَ
 ۗ فَمَنْ أَهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي
 لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّ فَقُلْ إِنَّمَا أَنَا
 مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿٩٢﴾ وَقُلِ الْحَمْدُ
 لِلَّهِ سَيُرِيكُمْ ءَايَاتِهِ فَتَعْرِفُونَهَا
 وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

وَيَوْمَ نَخْشُرُ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ فَوْجًا مِمَّنْ
 يُكَذِّبُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿٨٣﴾
 حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُمْ قَالَ أَكَذَّبْتُمْ
 بِآيَاتِي وَلَمْ تُحِطُوا بِهَا عَلِمًا أَمَّا
 أَنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٨٤﴾ وَوَقَعَ
 الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ بِمَا ظَلَمُوا فَهُمْ لَا
 يَنْطِقُونَ ﴿٨٥﴾ أَلَمْ يَرَوْا أَنَّا
 جَعَلْنَا اللَّيْلَ لَيْسَكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ
 مُبْصِرًا ۗ إِنِّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٨٦﴾

83. "Na siku Tutakapokusanya kutoka kila Ummah kundi katika wanaokadhibisha Ishara Zetu, nao watagawanywa mafungu mafungu.

84. Hata watakapofika, Atasema (Allah): Je! Nyinyisi mlizikanusha Ishara Zangu pasipo kuzijua vyema? Au mlikuwa mkifanywa nini?

85. Na kauli itawaangukia juu yao kwa vile walivyo-dhulumu. Basi hao hawatasema lolote.

86. Je! Hawaoni kwamba Sisi Tumeufanya usiku ili watulie, mchana wa kuangaza. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaoamini."

Kukusanywa Madhalimu Siku ya Kiyama

Allah تعالى Anasema kwa Kutupasha habari kuhusu Siku ya Kiyama na kukusanywa madhalimu mbele Yake miongoni mwa waliokadhibisha Ishara za Allah تعالى na Mitume Yake ili Kuwauliza kwa waliyofanya katika hii nyumba ya dunia, kwa Kuwakemea, Kuwakaripia, Kuwashutumu, Kuwadunisha na Kuwadhalilisha. Akasema:

وَيَوْمَ نَحْشُرُ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ فَوْجًا

“Na siku Tutakapokusanya kutoka kila Ummah kundi.”

Kutoka katika kila kaumu na kizazi kundi, maana *jamaa’ah*.

مِمَّنْ يُكَذِّبُ بِآيَاتِنَا

“Katika wanaokadhibisha Ishara Zetu.”

Kama Alivyosema:

أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

“Wakusanyeni wale waliodhulumu nafsi zao pamoja na wenzi wao.” (37:22).

Amesema tena:

وَإِذَا النُّفُوسُ رُوِّجَتْ

“Na roho zitakapounganishwa na viwiliwili vyake.” (81:7).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَهُمْ يُوزَعُونَ

“Nao watagawanywa mafungu mafungu.”

Amesema Ibn Abbaas رضي الله عنهما: “Watasukumwa”¹. ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd Aslam amesema: “Watapelekwa”². Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 19:501

² At-Tabari 19: 438.

حَتَّىٰ إِذَا جَاءُو

“Hata watakapofika.”

Na kusimama mbele ya Allah تعالى katika mahali pa hesabu.

قَالَ أَكْذَبْتُمْ بِآيَاتِي وَلَمْ تُحِيطُوا بِهَا عِلْمًا أَمَّا إِذَا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣١﴾

“Atasema (Allah): Je! Nyinyi si mlizikanusha Ishara Zangu pasipo kuzijua vyema? Au mlikuwa mkifanywa nini?.”

Wataulizwa kuhusu itikadi na amali zao, kwani wao ni miongoni mwa walioangamia, sio waliofuzu, kama Alivyosema Allah تعالى Kuhusu wao:

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٣٢﴾ وَلَٰكِن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿٣١﴾

“Hakusadiki wala hakuswali. Bali alikadhibisha na akarudi nyuma.”
(75:31-32).

Hapo hoja itathibitishwa dhidi yao na hivyo hawatakuwa na udhuru wowote, kama Alivyosema Allah تعالى:

هَذَا يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٥﴾ وَلَا يُؤَدِّنُ هُمْ فَيَعْتَدِرُونَ ﴿٣٦﴾

“Hii ni siku ambayo hawatasema kitu. Wala hawatapewa ruhusa kutoa udhuru, wakapata kutoa.” (77:35-36).

Na hapa ndivyo Alivyosema:

وَوَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ بِمَا ظَلَمُوا فَهُمْ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٧﴾

“Na kauli itawaangukia juu yao kwa vile walivyodhulumu. Basi hao hawatasema lolote.”

Watafedheheka, na kukosa jawabu, kwani hapa duniani walidhulumu nafsi zao, na sasa wamerudi kwa Mjuzi wa ghaibu na ya dhahiri, Ambaye Hakifichiki Kwake chochote. Kisha Allah تعالى Anatanabahisha Uweza Wake Timilifu, na Mamlaka Yake Makubwa, inayopasisha Yeye Kutiiwa, Kufuatwa Amri Zake na Kusadikisha risala ya ukweli waliokuja nayo Manabii Wake. Allah تعالى Amesema:

أَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا اللَّيْلَ لَيْسَكُنُوا فِيهِ

“Je! Hawaoni kwamba Sisi Tumeufanya usiku ili watulie?.”

Maana yake: Kwa giza la usiku wanasitisha shughuli zao kwa sababu Yake na kutuliza nafsi zao na kupumzika kwa harakati za kuchosha za mchana.

وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا

“Na mchana wa kuangaza.”

Maana yake: Uliojaa mwangaza, na kwa sababu ya hilo wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya masilahi na pato, kusafiri na kufanya biashara na mengineyo katika mambo yao ambayo wanahitaji kwayo. Allah تعالى Anamalizia Aya hiyo kwa Kusema:

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٨٣﴾

“Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaoamini”.

وَيَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ فَفَزِعَ مَنْ فِي السَّمَنَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ وَكُلُّ أَتَوُهُ
 دَاخِرِينَ ﴿٨٤﴾ وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسَبُهَا جَامِدَةً وَهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ صُنِعَ اللَّهُ الَّذِي أَتَقَنَ
 كُلَّ شَيْءٍ إِنَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَفْعَلُونَ ﴿٨٥﴾ مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ خَيْرٌ مِّمَّا وَهُمْ مِنْ فَزَعِ
 يَوْمِئِذٍ ءَامِنُونَ ﴿٨٦﴾ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَكُبَّتْ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ هَلْ تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا
 كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٨٧﴾

87. “Na siku litapopulizwa baragumu, watahangaika waliomo mbinguni na katika ardhi, ila Amtakaye Allah. Na wote watamfikia nao ni wanyonge.

88. Na unaiona milima unaidhania imetulia; nayo inakwenda kama mwendo wa mawingu. Huo ndio Ufundi wa Allah Aliyetengeneza vilivyo kila kitu. Hakika Yeye Anazo khabari za yote myatendayo.

89. Watakaokuja na mema, watapata bora kuliko hayo. Nao watasalimika na mahangaiko ya Siku hiyo.

90. Na watakaokuja na uovu, basi zitasunukishwa nyuso zao Motoni. Je! Kwani mnalipwa isipokuwa mliyokuwa mkiyatenda?"

Vitisho vya Siku ya Kiyama, Jazaa kwa Mema na Maovu Katika Siku Hiyo

Allah تعالی Anatueleza kuhusu hofu ya Siku ya kupulizwa *Swuur* (parapanda na baragumu). Nayo ni kama ilivyoelezwa katika Hadithi:

«قَرْنٌ يُنْفَخُ فِيهِ»

“Pembe inayopulizwa”.

Kulingana na Hadithi kuhusu baragumu *Swuur*: Hakika Israafiil ndiye atakayepuliza kwa Amri ya kutoka kwa Allah تعالی. Atapuliza kwa mara ya kwanza, kwa muda mrefu. Hii itakuwa ni ishara ya kumalizika kwa maisha ya hapa duniani, na Kiyama kitakuja juu ya watu wabaya kabisa miongoni mwa walioishi katika ulimwengu huu. Kila aliye mbinguni na katika ardhi ataogopa na kuhangaika,

إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ

“Ila Amtakaye Allah.”

Hawa watakuwa ni mashahidi, kwani wao wako hai mbele ya Mola wao Mlezi wanaruzukiwa¹. Imepokewa na Imamu Muslim ibn Al-Hajjaaj رحمه الله تعالی kutoka kwa Abdullah Ibn Amr رضي الله عنه amesema alikuja mtu kwake na kumwambia: “Ni Hadithi gani hii ambayo unahadithia watu kuwa Kiyama kitasimama kwa watu wa kadha na kadha?” Akasema: “*Subhaana Llahu* (Ametakasika Allah تعالی Ambaye Ameenpukana na kila aina ya upungufu) au *Laa ilaaha illa Llahu* (Hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالی) au maneno mfano wake. Hakika niliazimia kutohadithia chochote kwa yeyote daima. Hakika mtaona baada ya muda kidogo, tukio na jambo kubwa ambalo litaharibu Nyumba (Al-Ka’bah) na kutatokea kadha na kadha”. Kisha akasema, Mtume ﷺ amesema:

«يَخْرُجُ الدَّجَالُ فِي أُمَّتِي فَيَمُكُّتُ أَرْبَعِينَ - لَا أُدْرِي أَرْبَعِينَ يَوْمًا أَوْ أَرْبَعِينَ شَهْرًا
أَوْ أَرْبَعِينَ عَامًا - فَيَبْعَثُ اللَّهُ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ كَأَنَّهُ عُرْوَةٌ بَيْنَ مَسْعُودٍ قَيْطَلْبَةَ فَيَهْلِكُهُ،

¹ Atw-Twabraniiy katika Atw-Twiwaal 36.

ثُمَّ يَمْكُثُ النَّاسُ سَبْعَ سِنِينَ لَيْسَ بَيْنَ اثْنَيْنِ عَدَاوَةٌ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ رِيحًا بَارِدَةً مِنْ قِبَلِ الشَّامِ، فَلَا يَبْقَى عَلَى وَجْهِ الْأَرْضِ أَحَدٌ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ مِنْ خَيْرٍ أَوْ إِيمَانٍ إِلَّا قَبِضَتْهُ، حَتَّى لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ دَخَلَ فِي كَبِدِ جَبَلٍ لَدَخَلْتَهُ عَلَيْهِ حَتَّى تَفِيضَهُ،

“Dajjaal atatokea kwa Ummah wangu na ataishi kwa arobaini (sina hakika ni siku arobaini au miezi arobaini au miaka arobaini). Kisha Allah Aliyetukuka Atamtuma ‘Isa mwana wa Maryam ambaye ni kana kwamba ni Urwah bin Mas`uud, atamwinda na kumuuu. Kisha watu wataishi kwa miaka saba hapana uadui baina ya watu wawili. Kisha Allah Aliyetukuka Atatuma upepo baridi kutoka Shaam, hivyo hatobaki juu ya uso wa ardhi yeyote mwenye chembe ya kheri au Imani moyoni mwake isipokuwa roho yake itachukuliwa, hata lau mmoja wenu ataingia katika pango la jabali, upepo huo utamwingilia mpaka uitoe roho yake.”

Kisha akasema: Nimesikia hayo kutoka kwa Mtume ﷺ amesema,

اقْتَبَيْتُمُ شِرَارَ النَّاسِ فِي حِفَّةِ الطَّيْرِ وَأَحْلَامِ السَّبَاعِ لَا يَعْرِفُونَ مَعْرُوفًا، وَلَا يُنْكِرُونَ نُكْرًا، فَيَمْتَلُ لَهُمُ الشَّيْطَانُ فَيَقُولُ: أَلَا تَسْتَجِيبُونَ؟ فَيَقُولُونَ: فَمَا تَأْمُرُنَا؟ فَيَأْمُرُهُمْ بِعِبَادَةِ الْأَوْثَانِ، وَهُمْ فِي ذَلِكَ دَارٌ رِزْقُهُمْ حَسَنٌ عَيْشُهُمْ، ثُمَّ يَنْفُخُ فِي الصُّورِ فَلَا يَسْمَعُهُ أَحَدٌ إِلَّا أَصْعَى لَيْتًا وَرَفَعَ لَيْتًا - قَالَ - وَأَوَّلُ مَنْ يَسْمَعُهُ رَجُلٌ يَلُوطُ حَوْصَ إِبِلِهِ، قَالَ: قَبِضَتْهُ وَيَضَعُ النَّاسُ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ - أَوْ قَالَ يُنْزِلُ اللَّهُ - مَطَرًا كَأَنَّهُ لَطْلٌ - أَوْ قَالَ: اللَّطْلُ - نُعْمَانُ الشَّاكُ - فَتَبَّتْ مِنْهُ أَجْسَادُ النَّاسِ، ثُمَّ يَنْفُخُ فِيهِ أُخْرَى فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ، ثُمَّ يَقَالُ: يَا أَيُّهَا النَّاسُ هَلُمُّوا إِلَيَّ رَبِّكُمْ وَقَفُّوهُمْ بِهَمِّ مَنْسُؤِلُونَ، ثُمَّ يَقَالُ: أَخْرِجُوا بَعَثَ النَّارِ، فَيَقَالُ: مِنْ كَمِّ؟ فَيَقَالُ: مِنْ كُلِّ لَفٍ تِسْعِمَائَةِ وَتِسْعَةَ وَتِسْعِينَ، قَالَ: فَذَلِكَ يَوْمٌ يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا، وَذَلِكَ يَوْمٌ يَخْشَفُ عَنْ سَاقٍ

“Hapo watabaki walio waovu pekee miongoni mwa watu ambao watafanya uasherati kama ndege na watakuwa na tabia za Wanyama mwitu. Hawatajua mema wala hawatakataza maovu. Shetani atakuja kwao kwa mfano wa mwanadamu na kuwauliza: “Je, hamuniitikii wito wangu?” Watasema: “Kwani unatuamuru

nini?" Atawaamuru waabudu masanamu na wao katika kufanya hivyo watapata riziki zao na maisha yao yatakuwa mazuri. Kisha parapanda itapulizwa, hakuna atakayeisikia isipokuwa atageuza shingo upande wake (wa hiyo sauti). Wa kwanza kuisikia atakuwa ni mtu anayeshughulika katika kutengeneza birika ya maji kwa ajili ya ngamia wake. Atakapoisikia sauti hiyo atazimia na watu wengine nao watazimia. Kisha Allah Atatuma au Alisema: "Allah Atateremsha" - mvua kana kwamba ni matone ya umande au kivuli. Hii itafanya miili ya watu ichipuke, kisha parapanda itapulizwa mara nyengine na hapo watasimama watu na huku wanaona. Kisha kutasemwa: "Enyi watu! Njoooni mbele ya Mola wenu Mlezi na wasimamisheni kwani wao Wataulizwa". Kisha itatolewa Amri: "Watoeni wale ambao ni wa motoni". Kutaulizwa: "Wangapi?" Wataambiwa: "Katika kila elfu watoeni mia tisa na tisini na tisa (999)". Hiyo ndiyo siku ambayo itawafanya watoto wadogo waote mvi na hiyo ni siku ambayo Muundi utawachwa wazi"¹

Na Kauli Yake Mtume 齋:

ثُمَّ يَنْفُخُ فِي الصُّورِ فَلَا يَسْمَعُهُ أَحَدٌ إِلَّا أَصْنَىٰ لِنَا وَرَفَعَ لِنَا

"Kisha litapulizwa baragumu, hakuna atakayesikia ila atainamisha shingo yake na kukinyanyua ili kuisikiliza sauti hiyo".

Al-Layt ni kuinamisha shingo, yaani ili wapate kusikia vyema sauti inayotoka mbinguni. Huo ni mpulizo wa fazaa, kisha baada ya hiyo itapulizwa tena baragumu itakayomfanya kila mmoja afe, kisha kupulizwa mara nyengine ambayo itawafanya wafufuke ili wakutane na Mola wao Mlezi wa walimwengu wote – huku ni kukusanywa viumbe vyote kutoka katika makaburi yao. Kwa hiyo Anasema Aliyetukuka:

وَكُلُّ أُمَّةٍ دَاخِرِينَ

"Na wote watamfikia nao ni wanyonge."

¹ Muslim 4:2258.

Inasomwa kwa *madd* na bila ya *madd* kwa kitendo, na yote yana maana moja. na, kutii na kunyenyekea, hakuna atakayehalifu Amri Yake, kama Anavyosema Aliyetukuka:

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ

“Siku Atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitika kwa kumshukuru.”
(17:52).

Amesema tena Aliyetukuka:

ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِّنَ الْأَرْضِ إِذَا أَنتُمْ تَخْرُجُونَ ﴿٣٠﴾

“Kisha Atakapokuiteni wito mmoja tu, nyote mtatoka ardhini.”
(30:25).

Kulingana na Hadithi ya baragumu *Swuur*,¹ litakapopulizwa mara ya tatu, Allah تعالی Ataziamuru roho zingizwe katika tundu ya baragumu *Swuur*. Kisha Israafiil atalipuliza baada ya miili kumea katika makaburi yao na sehemu za mapumziko, na pindi atakapopuliza baragumu, roho zitaruka, roho za Waumini ziking'aa kwa nuru na roho za makafiri zitakuwa na kiza. Atasema Allah تعالی: *“Kwa Nguvu, Uwezo na Utukufu Wangu, kila roho itarudi katika mwili wake”*. Na roho zitarudi katika miili yake na zitaingia kama sumu inavyoingia pale mtu anapoumwa na kiumbe chenye sumu. Kisha watasimama wakikung'uta mchanga katika makaburi yao. Amesema Aliyetukuka:

يَوْمَ تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَأَنَّهُمْ إِلَى نُصُبٍ يُوفِضُونَ ﴿٧٠﴾

“Siku watakapotoka makaburini kwa upesi kama kwamba wanakimbia mfunda (mfundo wao, wanaposhindania).”(70:43)

Na Kauli Yake Allah تعالی,

وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسِبُهَا جَمَادًا وَهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ

“Na unaiona milima unaidhania imetulia; nayo inakwenda kama mwendo wa mawingu.”

¹ Atw-Twabraaniy katika Atw-Twiwaal 36.

Maana yake: Utaiona kama imetulia na kwamba itabaki kama ilivyokuwa, lakini itakuwa inapita kwa kasi kama inavyopita mawingu, yaani itaondoka kutoka katika sehemu zao. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

يَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا ﴿٩٣﴾ وَتَسِيرُ الْجِبَالُ سَيْرًا ﴿٩٤﴾

“Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikiso mkubwa kabisa. Na yang’oe majabali, yawe yanakwenda angani kwa mwendo wa kasi kabisa.” (52:9-10).

Anasema Aliyetukuka:

وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا ﴿١٠٦﴾ فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا ﴿١٠٧﴾ لَا تَرَى فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا ﴿١٠٨﴾

“Na wanakuuliza habari za milima. Waambie: Mola wangu Mlezi Ataivuruga vuruga. Na Ataiacha tambarare, uwanda. Hutaona humo mdidimo wala muinuko.” (20:105-107).

Amesema tena Aliyetukuka:

وَيَوْمَ نُسِirُ الْجِبَالِ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً

“Na siku Tutapoiondoa milima na ukaiona ardhi iwazi.” (18:47).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

صُنِعَ اللَّهُ الَّذِي أَنْتَقَنَ كُلَّ شَيْءٍ

“Huo ndio Ufundi wa Allah Aliyetengeneza vilivyo kila kitu.”

Hakika Anafanya hayo kwa Uweza na Nguvu Zake kubwa.

الَّذِي أَنْتَقَنَ كُلَّ شَيْءٍ

“Aliyetengeneza vilivyo kila kitu.”

Maana yake: Ametengeneza vilivyo kila Alichoumba na Akakiunda kulingana na Hekima Yake. Kwani Yeye,

إِنَّهُ خَيْرٌ بِمَا تَفْعَلُونَ ﴿٨٨﴾

“Hakika Yeye Anazo khabari za yote myatendayo.”

Maana yake: Yeye ni Mjuzi kwa wanayofanya waja Wake katika mambo ya kheri na mema, na shari na maovu, na Atawalipa kwayo kwa ukamilifu, thawabu au adhabu. Kisha Ameabainisha Aliyetukuka hali za watu wema na waovu siku hiyo kwa Kusema:

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ خَيْرٌ مِّمَّا

“Watakaokuja na mema, watapata bora kuliko hayo.”

Amesema Qataadah: “Kwa kumtakasa Allah تعالى Peke Yake”¹. Allah تعالى Ameelezea sehemu nyingine katika Qur’ani kuwa Atalipa mara kumi zaidi mfano wake. Allah تعالى Anasema:

وَهُمْ مِّنْ فِرْعَ يَوْمَئِذٍ ءَامِنُونَ ﴿٩١﴾

“Nao watasalimika na mahangaiko ya Siku hiyo.”

Hii ni kama Aya ifuatayo:

لَا تَحْزُنُهُمُ الْفِرْعُ الْأَكْبَرُ

“Hicho Kitisho Kikubwa hakitowahuzunisha.” (21:103).

Amesema tena Aliyetukuka:

أَفَمَنْ يُلْفَىٰ فِي النَّارِ خَيْرٌ أَمْ مَن يَأْتِي ءَامِنًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Je! Atakayetupwa Motoni ni bora au atakayekuja kwa amani Siku ya Kiyama?.” (41:40).

Na Amesema tena:

وَهُمْ فِي الْغُرُفَاتِ ءَامِنُونَ ﴿٣٧﴾

“Nao watakuwa salama katika maghorofa.” (34:37).

¹Atw-Twabarani 19:503.

Allah تعالی Anaendelea:

وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَكُبَّتْ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ

“Na watakaokuja na uovu, basi zitasunukishwa nyuso zao Motoni”.

Hii inamaanisha kuwa yeyote atakayekuja mbele ya Allah تعالی na madhambi na hana kabisa thawabu katika mizani yake, au madhambi yake ni mengi zaidi kuliko thawabu na amali zake njema.

Anasema Aliyetukuka:

هَلْ نَجْزُونَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾

“Je! Kwani mnalipwa isipokuwa mliyokuwa mkiyatenda?”

إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ رَبَّ هَذِهِ الْبَلَدَةِ الَّذِي حَرَّمَهَا وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ
مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٢٧﴾ وَأَنْ أَتْلُوا الْقُرْآنَ فَمَنْ أَهْتَدَىٰ فَأِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ وَمَنْ ضَلَّ
فَقُلْ إِنَّمَا أَنَا مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿٢٨﴾ وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ سَمِيحًا رَحِيمًا فَتَعَرَّفُونَهَا وَمَا رَبُّكَ
بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢٩﴾

91. “Ama mimi nimeamrisha nimuabudu Mola Mlezi wa mji huu Aliyeufanya ni Mtakatifu; na ni Vyake Yeye tu vitu vyote. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu, wenye kunyenyekea.

92. Na niisome Qur’ani. Na mwenye kuongoka, basi ameongoka kwa faida ya nafsi yake; na aliyepotea – basi sema: Hakika mimi ni miongoni mwa waonyaji.

93. Na sema: Alhamdu Lillahi, Sifa njema zote ni za Allah. Yeye Atakuonesheni Ishara Zake, na mtazijua. Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kughafilika na myatendayo”

Amri ya Kumuabudu Allah تعالى tu na Kuwaita Watu kwa Kutumia Qur'ani

Allah تعالى Anamuamuru Mtume Wake ﷻ asema:

إِنَّمَا أَمْرٌ أَنْ أَعْبُدَ رَبَّ هَذِهِ الْبَلَدَةِ الَّذِي حَرَّمَهَا وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ

“Ama mimi nimeamrisha nimuabudu Mola Mlezi wa mji huu Aliyeufanya ni Mtakatifu; na ni Vyake Yeye tu vitu vyote.”

Hii ni kama ile Aya:

قُلْ يَتَّيِبُوا النَّاسُ إِنْ كُنْتُمْ فِي شَكٍّ مِنْ دِينِي فَلَا أَعْبُدُ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ
أَعْبُدُ اللَّهَ الَّذِي يَتَوَفَّكُمُ ط

“Sema: “Enyi watu! Ikiwa nyinyi mnayo shaka katika Dini yangu, basi mimi siwaabudu mnaowaabudu nyinyi badala ya Allah. Lakini mimi namuabudu Allah Anayekufisheni.” (10:104).

Hakika ya kuwa neno *Rabb* (Mola Mlezi) limeunganishwa na neno la *Al-Baldah* (mji), katika ibara, ‘*Mola Mlezi wa mji huu*’ ni ishara ya hadhi, utukufu na uangalizi wa Allah تعالى kwa mji huo.

Hii ni kama Aya ifuatayo:

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ۖ الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِنْ جُوعٍ وَآمَنَهُمْ مِنْ خَوْفٍ ۖ

“Basi na wamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii (Al-Ka’bah). Ambaye Anawalisha wasipate njaa na Anawalinda na khofu.” (106:3-4).

Na Kauli Yake تعالى:

الَّذِي حَرَّمَهَا

“Aliyeufanya ni mtakatifu”.

Maana yake: Yule Aliyeufanya mji huu kwa Sheria, Hukumu na Amri Yake, Kuufanya Mtakatifu. Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Ibn ‘Abbaas رضی الله عنهما amesema:

«إِنَّ هَذَا الْبَلَدَ حَرَّمَ اللَّهُ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، لَا يُعْصَدُ شَوْكُهُ، وَلَا يُتَّقَرُ صَبْدُهُ وَلَا يَنْتَبِطُ لِقَطْعَتِهِ إِلَّا مَنْ عَرَفَهَا وَلَا يُحْتَلَى خَلَاهَا»

“Hakika mji huu umefanywa Mtukufu na Allah siku Alipoumba mbingu na ardhi. Kwa hiyo, ni Mtukufu kwa Kutakaswa na Allah mpaka Siku ya Kiyama. Misitu yake na michongoma haifai kukatwa, wala wanyama waliomo ndani hawafukuzwi (kwa kuwaondoa), wala hakiokotwi kilichopotea isipokuwa kwa yule atakayekitangaza hadharani, wala vichaka vyake kung’olewa.”

Hadithi kwa ukamilifu wake¹. Hakika hadithi hii imethibiti na kunukuliwa katika Sahihi, *Hasan* na *Musnad* kwa njia tofauti na kundi kubwa hivyo kuondoa shaka², kama ilivyobainishwa katika sehemu yake maalumu katika kitabu *al-Ahkaam*, Allah تعالى Ndiye Mwenye Kusifiwa na Kushukuriwa. Na Kauli Yake تعالى:

وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ

“Na ni Vyake yeye tu vitu vyote”.

Wataalamu wa sarufi ya kiarabu na kanuni zake, wanasema kuwa hapa kumetumika kanuni ya kuunganisha maelezo ya jumla kutoka katika maelezo mahususi, yaani Yeye ni Mola Mlezi wa mji huu na Mola Mlezi Mwenye Kumiliki kila kitu, hapana muabudiwa ila Yeye.

وَأْمُرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٦٦﴾

“Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu, wenye kunyenyekea.”

Maana yake: Kumpwekesha, kumtakasa na kuwa na Ikhlas Kwake na kwa utiifu wanafuata maagizo Yake. Na Kauli Yake:

وَأَنْ أَتْلُوا الْقُرْآنَ

“Na niisome Qur’an.”

¹ Fat’h al-Baariy 4: 56.

² Muslim 2: 986, abu Dawud 2:518, An-Nasa’iy 5: 203, Ibn Maajah 2:1083 na Ahmad 1:253.

Maana yake: Niwasomee watu, ili kuwafikishia ujumbe wake. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

ذَٰلِكَ نَتْلُوهُ عَلَيْكَ مِنَ الْآيَاتِ وَالذِّكْرِ الْحَكِيمِ ﴿٥٨﴾

“Haya Tunayokusomea ni katika Ayah na ukumbusho wenye hikima.” (3:58)

Na kama Kauli Yake Aliyetukuka:

نَتْلُوا عَلَيْكَ مِنْ نَبِيِّ مُوسَىٰ وَمِنْ مَوْسَىٰ وَفِرْعَوْنَ بِالْحَقِّ

“Tunakusomea habari za Musa na Firauni kwa haki.” (28:3)

Hii inamaanisha kuwa mimi ni mwenye kubalighisha na muonyaji. Na Kauli Yake:

فَمَنْ أَهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّ فَقُلْ إِنَّمَا أَنَا مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿٧٣﴾

“Na mwenye kuongoka, basi ameongoka kwa faida ya nafsi yake; na aliyepotea – basi sema: Hakika mimi ni miongoni mwa waonyaji”.

Hakika mimi nina kielekezo kutoka kwa Mitume ambao kwamba waliwaonya kaumu zao, wakafanya walivyoamriwa kutekeleza katika kufikisha ujumbe kwao na wakitekeleza ahadi walizoweka. Hesabu ya Ummah zao iko kwa Allah تعالیٰ, kama ilivyo katika Kauli Yake:

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٤٠﴾

“Juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hesabu.” (13:40)

Akasema tena:

إِنَّمَا أَنْتَ نَذِيرٌ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٢﴾

“Wewe ni mwonyaji tu, na Allah Ndiye Mlinzi wa kila kitu.” (11:12)

Na Kauli Yake:

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ سُبْحَانَ رَبِّهِمْ ۗ فَتَعْرِفُونَهَا ۚ

“Na sema: Alhamdu Lillahi, Sifa Njema zote ni za Allah. Yeye Atakuonesheni Ishara Zake.”

Maana yake: Allah تعالى Ndiye Mwenye Kustahiki Sifa zote njema, Ambaye Hamuadhibu yeyote ila baada ya kufikiwa na hoja juu yake na kuonywa (hivyo kumuacha bila ya udhuru wowote). Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

سُرِّيْكُمْ ءَايَاتِهِ فَتَعْرِفُونَا

“Yeye Atakuonesheni Ishara Zake, na mtazijua”.

Kama Alivyosema تعالى:

سُرِّيْهِمْ ءَايَاتِنَا فِي الْاَفَاقِ وَفِيْ اَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ اَنَّهُ الْحَقُّ

“Tutawaonesha ukweli wa Maneno Yetu haya katika nchi za mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli.” (41:53).

Na Kauli Yake تعالى:

وَمَا رُبُّكَ بِغَفْلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٥٣﴾

“Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kughafilika na myatendayo”.

Bali Yeye ni Shahidi na Anaona kila kitu. Imenukuliwa kuwa Imamu Ahmad alikuwa akiimba beti hizi mbili, kwa ajili yake au kwa mtu mwengine:

“Unapokuwa peke yako siku moja usiseme hilo,

Niko peke yangu lakini yuko mwenye kunitizama.

Usidhani ya kwamba Allah Ataghafilika hata kidogo,

Wala hakuna lenye kujificha Kwake.”

Huu ni mwisho wa Tafsir ya *Suratu an - Naml*, na Allah تعالى Ndiye Mwenye Kusifiwa na Mwenye Kushukuriwa.

* * *

Tafsiri ya Suratul Qasas

Sura ya 28

Iliteremshwa Makkah

Imepokewa na Imamu Ahmad ibn Hambal رحمه الله تعالى kuwa Ma'di Yakriba amesema: "Tulikuja kwa 'Abdullah na tukamtaka atusomee,



"Twa Siin Miim"

Ya mia mbili. Alisema: 'Haipo kwangu hiyo (yaani sijui); lakini nendeni kwa yule aliyejifunza kutoka kwa Mtume ﷺ naye ni Khabbaab ibn al-Aratt رضي الله عنه. Akasema: 'Hivyo tulikwenda kwa Khabbaab ibn al-Aratt رضي الله عنه, naye akatusomea.¹"



¹ Ahmad 1:419. Ipo kasoro katika Isnadi. Pia inaonekana kuwa inahusu Suratush Shu'aaraa'(26) ambayo ina Ayah mia na ishirini na saba (127). Hata hivyo, Ibn Kathir ametaja mapokezi ya kisomo cha Ibn Mas'uud ya Ayah ya ishirini ya *Ash- Shu'aaraa'*, kuonesha kuwa hakujua Surah hiyo, japokuwa mapokezi hayo, yaliyonukuliwa na *Atw-Twabariy* na wengineo ni, kama haya, si Sahihi. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْقَصَصِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

طسّم ﴿١﴾ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٢﴾ نَتْلُوا عَلَيْكَ مِنْ نَبَأِ مُوسَىٰ وَفِرْعَوْنَ بِالْحَقِّ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٣﴾ إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضِعُّ طَائِفَةً مِّنْهُمْ يُدَبِّحُ أَبْنَاءَهُمْ وَيَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾ وَنُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَيْمَةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ ﴿٥﴾ وَنَمَكِّنَ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَنُرِيَ فِرْعَوْنَ وَهَمَانَ وَجُنُودَهُمَا مِنْهُمْ مَا كَانُوا يَحْذَرُونَ ﴿٦﴾ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ ۖ فَإِذَا خِفْتِ عَلَيْهِ فَأَلْقِيهِ فِي الْيَمِّ وَلَا تَخَافِي وَلَا تَحْزَنِي ۗ إِنَّا رَادُّوهُ إِلَيْكِ وَجَاعِلُوهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٧﴾ فَالْتَقَطَهُ ءَالُ فِرْعَوْنَ لِيَكُونَ لَهُمْ عَدُوًّا وَحَزَنًا ۗ إِنَّ فِرْعَوْنَ وَهَمَانَ وَجُنُودَهُمَا كَانُوا خَاطِلِينَ ﴿٨﴾ وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرْتُ عَيْنِي لِي وَلَكَ لَا تَقْتُلُوهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

طسّم ﴿١﴾ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٢﴾ نَتْلُوا عَلَيْكَ مِنْ نَبَأِ مُوسَىٰ وَفِرْعَوْنَ بِالْحَقِّ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٣﴾ إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضِعُّ طَائِفَةً مِّنْهُمْ يُدَبِّحُ أَبْنَاءَهُمْ وَيَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾ وَنُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا فِي الْأَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ أَيْمَةً وَنَجْعَلَهُمُ الْوَارِثِينَ ﴿٥﴾ وَنَمَكِّنَ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَنُرِيَ فِرْعَوْنَ وَهَمَانَ وَجُنُودَهُمَا مِنْهُمْ مَا كَانُوا يَحْذَرُونَ ﴿٦﴾ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ ۖ فَإِذَا خِفْتِ عَلَيْهِ فَأَلْقِيهِ فِي الْيَمِّ وَلَا تَخَافِي وَلَا تَحْزَنِي ۗ إِنَّا رَادُّوهُ إِلَيْكِ وَجَاعِلُوهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٧﴾ فَالْتَقَطَهُ ءَالُ فِرْعَوْنَ لِيَكُونَ لَهُمْ عَدُوًّا وَحَزَنًا ۗ إِنَّ فِرْعَوْنَ وَهَمَانَ وَجُنُودَهُمَا كَانُوا خَاطِلِينَ ﴿٨﴾ وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرْتُ عَيْنِي لِي وَلَكَ لَا تَقْتُلُوهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

1. Twaa Siin Miim, (Tw.S.M.).
2. Hizi ni Aya za Kitabu kinachobainisha.
3. Tunakusomea khabari za Musa na Firauni kwa Haki kwa ajili ya watu wanao-amini.

4. Hakika Firauni alitakabari katika nchi, na akawagawa wananchi makundi mbali mbali. Akalidhoofisha taifa moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na akiwaacha watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa katika mafisadi.

5. Na Tukataka Kuwafadhili waliodhoofishwa katika nchi hiyo na Kuwafanya wawe viongozi na Kuwafanya ni warithi.

6. Na Kuwapa nguvu katika nchi, na kutokana na wao kuwaonesha kina Firauni na Hamana na majeshi yao mambo yale waliyokuwa wakiyaogopa”.

Habari za Musa عليه السلام na Firauni, na Alichotaka Allah تعالى kwa Watu Wao

Yametangulia mazungumzo kuhusu herufi za mkato (*al-Muqatwtwa'ah*). Na Kauli Yake:

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٢٨﴾

“Hizi ni Ayah za Kitabu kinachobainisha”.

Aya hizi zipo katika Kitabu kilicho wazi na kubainisha hakika ya mambo bila kuficha chochote, na kinatueleza kwa yaliyotokea na yatakayotokea katika siku za usoni. Na Kauli Yake:

تَتْلُوا عَلَيْكَ مِنْ نَبِيِّ مُوسَىٰ وَمِنْ عَذْرَٰتِ الْبِطْحَانِ

“Tunakusomea khabari za Musa na Firauni kwa Haki.”

Ayah hii ni kama ile Aliposema Aliyetukuka:

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ أَحْسَنَ الْقَصَصِ

“Sisi Tunasimulia simulizi nzuri.” (12:3)

Hii ina maana kuwa Tunakueleza mambo kama yalivyokuwa kama kwamba unayashuhudia na upo pale umehudhuria na unayaona kwa macho yako. Kisha Akasema Aliyetukuka:

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ

“Hakika Firauni alitakabari katika nchi.”

Maana yake: Ametakabari, akawatenza watu nguvu na kuwa mkatili.

وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا

“Akawagawa wananchi makundi mbali mbali.”

Maana yake: Akawafanya matabaka tofauti, kila moja akiliamuru kufanya anavyotaka yeye bila kikwazo chochote kile katika mambo ya dola yake.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

يَسْتَضْعِفُ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ

“Akalidhoofisha taifa moja miongoni mwao.”

Hawa walikuwa ni wana wa Israili (Bani Israa’iil), ambao wakati huo walikuwa kaumu bora wa zama hizo, japokuwa walishindwa nguvu na mfalme huyo aliyekuwa mkatili, ambaye aliwatumia kumfanyia kazi mbovu zaidi na kuwalazimisha kumfanyia yeye na watu wake kazi ngumu mchana na usiku.

Pamoja na hayo alikuwa akiwaua watoto wao wa kiume na kuwaacha watoto wa kike kuishi ili kuwadhalilisha. Kwa sababu ya chuki yake kwao pamoja na hofu kuwa huenda akatokea kijana miongoni mwao ambaye atasababisha kuvunjika na kuanguka kwa dola yake.

Hivyo, Firauni alichukua tahadhari dhidi ya hilo kutokea kwa kuamrisha kuwa vijana wa kiume wote wanaozaliwa na wana wa Israili wauliwe, lakini tahadhari hii haikumuokoa yeye na Amri ya kutoka kwa Allah تعالی.

Hiyo ni kuwa wakati wa Allah تعالی unapofika hauwezi kucheleweshwa, na kila jambo tayari limeandikwa katika Kitabu. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَتُرِيدُ أَنْ نَمُنَّ عَلَى الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا فِي الْأَرْضِ

“Na Tukataka Kuwafadhili waliodhoofishwa katika nchi hiyo.”

Hadi Kauli Yake:

تَحَذَّرُونَ ﴿١٠﴾

“Wakiyaogopa.”

Hakika Allah تعالی Aliwafanyia wao hilo, kama Alivyosema Allah تعالی:

وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضَعُونَ

“Na Tukawarithisha watu waliokuwa wanadharauliwa.”

Mpaka kwa Kauli Yake:

يَعْرُشُونَ ﴿١٣٧﴾

“Wakiyajenga.” (7:137).

Amesema tena:

كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٩﴾

**“Ndivyo hivyo Tulivyofanya kwa kuwarithisha wana wa Israili.”
(26: 59).**

Firauni alitaraji kuwa kwa ule uwezo na nguvu zake ataokoka kutoka kwa Musa عليه السلام, lakini hilo halikumsaidia yeye na chochote pamoja na uwezo wake wa ufalme mkubwa. Lakini hayo hayakumuokoa yeye na amri ya kutoka kwa Allah تعالى, ambayo haishindikizi. Kinyume na hayo yote, Hukumu ya Allah تعالى ilitekelezwa, kwani ilikuwa tayari ishaandikwa kuanzia mwanzo kuwa kuangamia kwake Firauni kutatokana na Mikono ya Nabii Musa عليه السلام.

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ ۖ فَإِذَا حِفَّتِ عَلَيْهِ فَأَلْقِيهِ فِي الْيَمِّ وَلَا تَخَافِي وَلَا تَحْزَنِي ۗ إِنَّا رَادُّوهُ إِلَيْكَ وَجَاعِلُوهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٧٧﴾ فَأَلْتَقَطَهُ آلُ فِرْعَوْنَ لِيَكُونَ لَهُمْ عَدُوًّا وَحَزَنًا ۗ إِنَّ فِرْعَوْنَ وَهَمَانَ وَجُنُودَهُمَا كَانُوا خَاطِئِينَ ﴿٧٨﴾ وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرْتُ عَيْنِي لِي وَلَكَ ۗ لَا تَقْتُلُوهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٧٩﴾

7. “Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapomkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi Tutamrudisha kwako na Tutamfanya miongoni mwa Mitume.

8. Basi wakamwokota watu wa Firauni, aje kuwa adui kwao na

huzuni. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa.

9. Na mkewe Firauni alisema: Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako. Msimuue! Huenda akatufaa, au tumpange kuwa mwenetu. Wala wao hawakutambua.”

Ufunuo kwa Mamake Musa عليه السلام Kuoneshwa mikakati

Imetajwa kuwa pale Firauni alipowaua vijana wengi sana wa wana wa Israili, Maqibti walihofia kuwa huenda wakamalizika wana wa Israili, hivyo watalazimika kufanya kazi hizo ngumu ambazo zilikuwa zikifanywa na wana wa Israili. Hapo walimwambia Firauni: “Hili likiendelea, na wazee wao wakawa wanakufa na vijana wanauliwa, wanawake wao hawataweza kufanya kazi iliyokuwa ikifanywa na wanaume. Hivyo, itabidi tufanye shughuli hizo sisi wenyewe.” Kwa ajili hiyo Firauni alitoa maagizo kuwa vijana wa wana wa Israili wauliwe mwaka mmoja na mwaka mwengine waachiliwe bila kuuliwa. Nabii Haaruun عليه السلام alizaliwa katika mwaka walioachwa vijana na Nabii Musa عليه السلام akazaliwa katika mwaka wa kuuliwa vijana. Firauni alikuwa na watu waliowakilishwa kufanya kazi hiyo, na wakunga waliokuwa wakiwapitia wanawake wa wana wa Israili na kuwatazama kama wana mimba. Wakimpata mmoja wao ana mimba, walikuwa wakiliandika jina lake. Wakati wa kuzaa unapofika, hakuna aliyeruhusiwa kuwashughulikia isipokuwa wanawake wa Kiqibti. Anapozaa mzazi mtoto wa kike walikuwa wakimuacha na kwenda zao, lakini akizaa kijana wa kiume, wauaji walikuwa wakiitwa kutekeleza kazi yao ya kuwaua kwa kutumia visu vyao vikali. Baada ya kufanya shughuli yao hiyo walikuwa wakienda zao, Allah تعالی Awalaani kwa kitendo chao hicho. Wakati mamake Musa عليه السلام aliposhika mimba ya Musa عليه السلام, mimba hiyo haikudhihiri wala haikuonesha ishara kama inavyokuwa kwa wanawake wengine, na hapana miongoni mwa wakunga aliyeweza kuhisi lolote. Lakini alipozaa mtoto wa kiume aliona dhiki kubwa na hakujua la kufanya. Alikuwa na hofu kubwa juu yake kwa kuwa alimpenda sana. Musa عليه السلام alipendwa na kila aliyemuona.

Hakika waliobarikiwa ni wale waliompenda kwa hisia za kimaumbile na kwa kuwa yeye ni Mtume ﷺ. Amesema Allah تعالی:

وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِّنِّي

“Na Nimekutilia mapenzi yanayotoka Kwangu.” (20:39).

Musa عليه السلام katika Nyumba ya Firauni

Pale mamake Musa عليه السلام alipokuwa anahangaika naye na hajui afanye nini, alipatiwa ufunuo moyoni mwake na akili yake kwa anachofaa kufanya, kama Anavyosema Allah تعالى:

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ ۖ فَإِذَا خِفْتِ عَلَيْهِ فَأَلْقِيهِ فِي الْيَمِّ وَلَا تَخَافِي وَلَا تَحْزَنِي ۗ إِنَّا رَأَدُّوهُ إِلَيْكَ وَجَاعِلُوهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٧﴾

“Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapomkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi Tutamrudisha kwako na Tutamfanya miongoni mwa Mitume.”

Nyumba ya mamake Musa عليه السلام ilikuwa karibu na ukingo wa mto Naili, hivyo alichukua sanduku na kilili cha mtoto, naye akaanza kumlea mtoto wake. Alipokuwa anakuja mtu yeyote kwake ambaye alihofia, alikuwa akienda na kumtia mtoto wake katika sanduku na kulitia katika mto baada ya kulifunga na kamba. Siku moja alikuja mtu ambaye alikuwa na wasiwasi naye katika nyumba yake, hivyo alifanya haraka kumtia mtoto wake katika sanduku hilo na kulitia katika mto lakini akasahau kulifunga.

Maji yalilichukua sanduku hilo mpaka kupita mbele ya nyumba ya Firauni, ambapo vijakazi walilichukua na kulipeleka kwa mke wa Firauni. Hawakujua kuna nini ndani yake na wala hawakutaka kulifungua ili wasije wakaingia matatani kwa kufanya hivyo bila ya yeye (mkewe Firauni) kuwepo. Sanduku lilipofunguliwa, walimpata mtoto aliyekuwa mwenye umbile zuri na bora kabisa kuliko wengine wote. Hapo Allah تعالى Aliujaza moyo wa mkewe Firauni kwa mahaba na upendo kwake pindi alipomuona; hii ni kwa kuwa alibarikiwa na kwa sababu Allah تعالى Alitaka Kumtukuzi na hivyo hivyo kuleta maangamivu ya mumewe. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

فَالْتَقَطَهُ ءَالُ فِرْعَوْنَ لِيَكُونَ لَهُمْ عَدُوًّا وَحَزَنًا^ط

“Basi wakamwokota watu wa Firauni, aje kuwa adui kwao na huzuni”.

Amesema Muhammad ibn Is’haaq رحمه الله تعالى na wengineo: “Laam iliyotumika hapa ni ya matokeo ya mwisho wala sio Laam ya kuthibitisha, kwani hawakumuokota kwa ajili hiyo. Hapana shaka kuwa dhahiri ya lafdhi inakwenda sambamba na waliyosema, lakini ukitazama maana ya sentensi inabaki kuwa Laam ni ya kuthibitisha. Maana yake ni kuwa Allah تعالى Aliwataka wamuokote ili Amfanye kuwa adui kwao na huzuni juu yao. Hiyo inakuwa ni kutaarifu kwa kufuta hadhari yake aliyochukua.” Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

إِنَّ فِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَجُنُودَهُمَا كَانُوا خٰطِئِينَ ﴿٢٨﴾

“Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa”.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرْتُ عَيْنِي لِي وَلَكَ^ط

“Na mkewe Firauni alisema: Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako”.

Hii inamaanisha kuwa pindi Firauni alipomuona mtoto huyo alitaka kumuua akihofu huenda akawa ni mtoto wa wana wa Israili. Lakini mkewe Asiyah bin Muzaahim alimtetea mtoto huyo na kujaribu kumleta karibu pamoja na kumpendezesha kwa Firauni, akasema:

قُرْتُ عَيْنِي لِي وَلَكَ^ط

“Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako”.

Hapo akasema Firauni: “Ama kwako ndio, lakini kwangu hapana”, Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Allah تعالى Alimuongoa huyo mke wa Firauni kwa sababu yake (Musa عليه السلام) na Kumuangamiza yeye (Firauni) mikononi mwake. Na Kauli Yake:

عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا

“Huenda akatufaa.”

Hili ndilo lililotokea katika kadhia yake (Asiyah), Allah تعالی Alimuongoa kupitia kwake na kumfanya aishi katika bustani za Peponi. Na Kauli Yake:

أَوْ نَتَّخِذْهُ وَلَدًا

“Au tumpange kuwa mwenetu.”

Alikuwa anataka kumchukua na kumpanga kama mtoto wake, kwani hakuwa na mtoto pamoja na mumewe. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٠﴾

“Wala wao hawakutambua.”

Hii inamaanisha kuwa wao hawakujua wala kutambua Aliyopanga Allah تعالی kwa Hekima Zake kubwa na dalili za uhakika kabisa kwao pale walipomuokota.

* * *

وَأَصْبَحَ فُؤَادُ أَمْرِ مُوسَىٰ فَرِغًا ۗ إِن كَادَتْ لَتُبْدَىٰ
 بِهِ لَوْلَا أَن رَّبَطْنَا عَلَىٰ قَلْبِهَا لِتَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ
 ﴿١٠﴾ وَقَالَتْ لِأُخْتَيْهِ فَصِيحَةٌ فَصِرَتْ بِهِ عَن جُنُبٍ وَهُمْ
 لَا يَشْعُرُونَ ﴿١١﴾ * وَحَرَمْنَا عَلَيْهِ الْمَرَاضِعَ مِن قَبْلُ
 فَقَالَتْ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُ لَكُمْ وَهُمْ
 لَهُ نَصِيبٌ ﴿١٢﴾ فَرَدَدْنَاهُ إِلَىٰ أُمِّهِ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا
 تَحْزَنَ ۗ وَلِتَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ
 لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾ وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَاسْتَوَىٰ ءَاتَيْنَاهُ
 حُكْمًا وَعِلْمًا ۗ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٤﴾ وَدَخَلَ
 الْمَدِينَةَ عَلَىٰ حِينِ غَفْلَةٍ مِّنْ أَهْلِهَا فَوَجَدَ فِيهَا رَجُلَيْنِ
 يَقْتَتِلَانِ هَذَا مِنْ شِيعَتَيْهِ وَهَذَا مِنْ عَدُوِّهِ فَاسْتَفْتَاهُ
 الَّذِي مِنْ شِيعَتَيْهِ عَلَىٰ الَّذِي مِنْ عَدُوِّهِ فَوَكَرَهُ مُوسَىٰ
 فَقَضَىٰ عَلَيْهِ ۗ قَالَ هَذَا مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّهُ عَدُوٌّ
 مُّضِلٌ مُّبِينٌ ﴿١٥﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ لِي
 فَغَفَرَ لَهُ ۗ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٦﴾ قَالَ رَبِّ بِمَا
 أَنْعَمْتَ عَلَيَّ فَلَنْ أَكُونَ ظَهِيرًا لِّلْمُجْرِمِينَ ﴿١٧﴾

وَأَصْبَحَ فُؤَادُ أَمْرِ مُوسَىٰ فَرِغًا ۗ إِن
 كَادَتْ لَتُبْدَىٰ بِهِ لَوْلَا أَن
 رَّبَطْنَا عَلَىٰ قَلْبِهَا لِتَكُونَ مِنَ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠﴾ وَقَالَتْ لِأُخْتَيْهِ
 فَصِيحَةٌ فَصِرَتْ بِهِ عَن جُنُبٍ وَهُمْ
 لَا يَشْعُرُونَ ﴿١١﴾ * وَحَرَمْنَا عَلَيْهِ
 الْمَرَاضِعَ مِن قَبْلُ فَقَالَتْ هَلْ أَدُلُّكُمْ
 عَلَىٰ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُ لَكُمْ وَهُمْ
 لَهُ نَصِيبٌ ﴿١٢﴾ فَرَدَدْنَاهُ إِلَىٰ
 أُمِّهِ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ
 ۗ وَلِتَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ
 وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

10. Na moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu. Alikuwa karibu kumdhihirisha, ingelikuwa Hatukumtia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa Waumini.

11. Naye akamwambia dada yake Musa: Mfuatie. Basi naye akawa anamuangalia kwa mbali bila ya wao kujua.

12. Na Tukamjaalia awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo, mpaka dada yake akasema: Je! Nikuonesheni watu wa nyumba watakaomlea kwa ajili yenu, nao pia watakuwa wema kwake?

13. Basi Tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ajue ya kwamba Ahadi ya Allah ni ya kweli, lakini wengi wao hawajui”.

Huzuni kubwa Ilimpata Mamake Musa عليه السلام na Kkurejeshewa kwa Mwanawe.

Allah تعالى Anatupasha habari kuwa moyo wa mamake Musa عليه السلام ulikuwa na huzuni pindi mtoto wake alipopotea katika mto, yaani hakuweza kufikiria chochote katika hii dunia isipokuwa Musa عليه السلام. Hii ilikuwa ni rai ya Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, ‘Ikrimah, Sa’iid ibn Jubayr, Abu ‘Ubaydah, adh-Dhahhaak, al-Hasan al-Baswriy, Qataadah na wengineo رضي الله عنهم¹.

إِنْ كَادَتْ لَتُبْدِي بِهِ

“Alikuwa karibu kumdhihirisha.”

Maana yake: Alikaribia kutoa habari kwa watu kuwa amepoteza mtoto wake kwa ile shida ya huzuni yake. Pia kutoa habari kwa hali aliyokuwa nayo lau si Allah تعالى Kumthibitisha na Kumpa subira. Amesema Allah تعالى:

لَوْلَا أَنْ رَّبَّنَا عَلَيَّ قَلْبَهَا لَتَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠﴾ وَقَالَتْ لِأُخْتِهِ قُصِّيه

“Ingelikuwa Hatukumtia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa Waumini. Naye akamwambia dada yake Musa: Mfuatie.”

Alimuamuru binti yake ambaye alikuwa mkubwa mwenye kufahamu anayo mwambia. Akamwambia binti yake huyo:

قُصِّيه

“Mfuatie.”

Maana yake: Fuata athari na utafute habari na dalili zake, jaribu kutafuta habari zake pembezoni mwa mji. Hivyo, alitoka kutekeleza hilo. Allah تعالى Anasema:

فَبَصُرَتْ بِهِ عَنْ جُنُبٍ

“Basi naye akawa anamuangalia kwa mbali.”

¹ At-Twabari 19:529.

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: Akitafakari neno "Kando kando"¹. Amesema Mujaahid: "Kumuangalia kwa mbali." Na Amesema Qataadah: "Akawa akimuangalia kana kwamba hakuwa na haja naye."²

Hiyo ni kuwa baada ya Musa عليه السلام kutulia katika nyumba ya Firauni, baada ya kupendwa na mke wa Firauni na kumtaka mumewe asimuue, walimletea wanyonyeshaji waliokuwa ndani ya nyumba, lakini hakumkubali yeyote miongoni mwao, na akakataa kuchukua titi la yeyote. Kwa ajili hiyo walimchukua sokoni huenda wakapata mwenye kumnyonyesha. Dada yake alipomuona mikononi mwao alimtambua, lakini hakuonesha ishara yoyote wala wao hawakuhisi chochote. Amesema Allah تعالى:

وَحَرَّمْنَا عَلَيْهِ الْمَرَاضِعَ مِنْ قَبْلُ

"Na Tukamjaalia awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo."

Hii inamaanisha kukatazwa kuliko kadiriwa na Allah تعالى, kwa sababu ya hadhi ya utukufu wake mbele ya Allah تعالى. Ilikuwa ni Amri kutoka Kwake kuwa asinyonye zaidi ya titi la mamake, na Allah تعالى Aliijaalia hii kuwa sababu ya yeye kurudi kwa mamake ili amnyonyeshe, hivyo kupata usalama na utulivu baada ya kuwa na hofu kubwa. Pale (dada yake) alipowaona wamechanganyikiwa kuhusu mwanamke atakaye mnyonyesha:

فَقَالَتْ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُ لَكُمْ وَهُمْ لَهُ نَصِيبٌ مِّنْهُ

"Akawaambia: Je! Nikuonesheni watu wa nyumba watakaomlea kwa ajili yenu, nao pia watakuwa wema kwake?"

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Aliposema hayo, walianza kumshuku, hivyo walimchukua na kumuuliza: 'Unajuaje kuwa hao watu watakuwa na nia nzuri kwake na kumtunza vyema?' Aliwaambia: "Hakika watakuwa na ikhlasi kwake na watamtunza vizuri ni kwa hamu yao ya kutaka kumfurahisha mfalme na pia kutarajia manufaa kwake." Walimuachilia baada ya yale aliyosema, akiwa amesalimika na madhara yao, walikwenda naye katika nyumba yao na kumleta

¹ Atw-Twabariy 19:532.

² Atw-Twabariy 19:532.

mtoto kwa mama yake. Alimpatia titi lake, naye akalikubali bila matatizo yoyote, na hapo walifurahi na kupeleka bishara kwa mke wa Firauni. Mke wa Firauni alimuita mamake Musa عليه السلام, akamfanyia wema na kumpa tunu kwa ukarimu. Yeye hakutambua kuwa huyo ni mamake hasa, lakini aliona kuwa mtoto amelikubali titi lake. Asiyah alimtaka akae naye ili amnyonyeshe na kumtunza mtoto, lakini alikataa, huku akisema: “Hakika mimi nina mume na watoto, hivyo siwezi kukaa nawe, lakini ukitaka nimnyonyeshe katika nyumba yangu, nitafanya hivyo.” Mke wa Firauni alikubali kwa hilo, na akawa anamlipa mshahara na zawadi za ziada, nguo na kumfanyia hisani. Mamake Musa عليه السلام alirudi na mtoto wake akiwa ameridhika, mwenye furaha kuwa baada ya kipindi cha hofu Allah تعالى Amemtunukia usalama, amani, utukufu, hadhi, jaha na riziki yenye kuendelea. Kulikuwa na muda mfupi baina ya shida na faraja, siku na usiku wake au mfano wake tu. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Ametakasika Ambaye Mikononi Mwake ipo Kwake Amri yote, Anachotaka kinakuwa na Asichotaka basi hakiwi. Yeye Anawajalia wale wenye kumcha baada ya kila hofu na huzuni faraja na baada ya kila dhiki, upenyo wa kutoka kwayo. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى amesema:

فَرَدَدْتَهُ إِلَىٰ أُمِّهِ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا

“Basi Tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike.”

Maana yake: Yeye mtoto.

وَلَا تَحْزَبْ

“Wala asihuzunike.” juu yake.

وَلِتَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ

“Na ajue ya kwamba ahadi ya Allah ni ya kweli.”

Hii inamaanisha kuwa Tulimuahidi kumrudishia mtoto wake na kumchagua kuwa miongoni mwa Mitume. Aliporudishwa kwake, alitambua kuwa mtoto wake ni mmoja kati ya Mitume, hivyo akatekeleza katika malezi yake kwake yale yanayopaswa kufanywa kimaumbile na kisheria. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

“Lakini wengi wao hawajui.”

Maana yake: Wao hawajui Hekima ya Allah تعالى katika Matendo Yake na Matokeo Yake mazuri ambayo kwayo Anasifiwa hapa duniani na Kesho Akhera. Huenda likatokea jambo ambalo watu hawalipendi, lakini matokeo yake ni mazuri katika jambo hilo, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۗ وَعَسَىٰ أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ۗ

“Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu.” (2:216).

Amesema tena Aliyetukuka:

وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَجَعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا ۖ

“Basi huenda mkakichukia kitu, na Allah Ametia kheri nyingi ndani yake.” (4:19)

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَاسْتَوَىٰ ؕ آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا ۗ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩﴾
 وَدَخَلَ الْمَدِينَةَ عَلَىٰ حِينِ غَفْلَةٍ مِّنْ أَهْلِهَا فَوَجَدَ فِيهَا رَجُلَيْنِ يَقْتَتِلَانِ هَٰذَا مِنْ شِيعَتِهِ
 وَهَٰذَا مِنْ عَدُوِّهِ ۗ فَاسْتَغْنَاهُ الَّذِي مِنْ شِيعَتِهِ عَلَىٰ الَّذِي مِنْ عَدُوِّهِ فَوَكَرَهُ مُوسَىٰ
 فَقَضَىٰ عَلَيْهِ ۗ قَالَ هَٰذَا مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّهُ عَدُوٌّ مُّضِلٌّ مُّبِينٌ ﴿٢٠﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي
 ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ لِي فَغَفَرَ لَهُ ۗ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٢١﴾ قَالَ رَبِّ بِمَا أَنْعَمْتَ
 عَلَيَّ فَلَنْ أَكُونَ ظَهِيرًا لِّلْمُجْرِمِينَ ﴿٢٢﴾

14. Na Musa alipofika utu-uzima barabara, Tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa walio wema.

15. Na akaingia mjini hali wameghafilika wenyeji wake, na akakuta humo watu wawili wanapigana - mmoja ni katika wenzake, na mwengine katika maadui zake. Yule mwenzake alimtaka msaada kumpiga adui yake. Musa akampiga ngumi, akamuua. Akasema: Hiki ni kitendo cha Shetani; hakika yeye ni adui, mpotezaji dhahiri.

16. Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe. Akamsamehe; hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.

17. Akasema: Mola wangu Mlezi! Kwa ulivyonineemesha, basi mimi sitakuwa kabisa msaidizi wa wakosefu.

Musa عليه السلام Kumuuu Mkihti

Alipoelezea mwanzo wa jambo la Musa عليه السلام, Allah تعالى Anaeleza kuwa pindi alipofikia utu uzima wake na kukomaa Allah تعالى Alimpatia hekima na elimu. Amesema Mujaahid: "Hii inakusudia Utume."¹

وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٠﴾

"Na hivi ndivyo Tunavyowalipa walio wema."

Kisha Allah تعالى Anatueleza namna Musa عليه السلام Alivyofikia hadhi aliyokadiriwa na Allah تعالى, hadhi ya Utume na kuzungumza na Allah تعالى, katika kadhia yake ya kumuua mkihti, ambayo ndiyo iliyokuwa sababu ya yeye kuondoka Misri kuelekea Madyan. Akasema Aliyetukuka:

وَدَخَلَ الْمَدِينَةَ عَلَىٰ حِينٍ غَفْلَةٍ مِّنْ أَهْلِهَا

"Na akaingia mjini hali ya kughafilika wenyeji wake."

Ibn Jurayj amepokea kutoka kwa 'Atwaa' al-Khurraasaanii kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Huo ulikuwa ni wakati baina ya Magharibi na Isha."² Ibn al-Munkadir amepokea kutoka kwa 'Atwaa' ibn Yasaar kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Huo ulikuwa ni wakati wa katikati ya mchana."³ Hivi ndiyo alivyosema Sa'iid ibn Jubayr, 'Ikrimah, as-Suddiy na Qataadah.

فَوَجَدَ فِيهَا رَجُلَيْنِ يُقْتَتِلَانِ

"Na akakuta humo watu wawili wanapigana."

¹ Ad-Durr al-Manthuur 5:531.

² Atw-Twabariy 19:538.

³ Atw-Twabariy 19:538.

Maana yake: Wanapigana na kushindana.

هَذَا مِنْ شِيعَتِهِ

“Mmoja ni katika wenzake.”

Maana yake: Muisraili.

وَهَذَا مِنْ عَدُوِّهِ

“Na mwengine katika maadui zake.”

Maana yake: Mkibti¹. Ndivyo alivyosema Ibn ‘Abbaas, Qataadah, as-Suddiy na Muhammad ibn Ishaq² رضي الله عنهم. Yule Muisraili aliomba msaada kwa Musa عليه السلام, na Musa عليه السلام naye aliitumia fursa hiyo ya kughafilika. Kwa hiyo akamuendea yule Mkibti:

فَوَكَرَهُ مُوسَى فَقَضَى عَلَيْهِ

“Musa akampiga ngumi, akamuua.”

Amesema Mujaahid: “Akampiga’, yaani alimpiga kwa ngumi yake.”³ “Akamuua”, yaani huo ndio uliokuwa umauti wake, naye akafa. Hapo, “Akasema”, Musa عليه السلام:

قَالَ

“Akasema”

هَذَا مِنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ إِنَّهُ عَدُوٌّ مُضِلٌّ مُبِينٌ ﴿٥٠﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ

لِي فَغَفَرَ لَهُ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥١﴾ قَالَ رَبِّ بِمَا أَنْعَمْتَ عَلَيَّ

“Hiki ni kitendo cha Shetani; hakika yeye ni adui, mpotezaji dhahiri.” Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe. Akamsamehe; hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu. Akasema: Mola wangu Mlezi! Kwa Ulivyonineemesha.”

¹ At-Tabari 19:539.

² At-Tabari 19:539, 540.

³ At-Tabari 19:540.

Hii inamaanisha kwa ulichonijaalia mimi kwa jaha, utukufu, nguvu, neema pamoja na baraka.

فَلَنْ أَكُونَ ظَهِيرًا لِلْمُجْرِمِينَ ﴿١٧﴾

“Basi mimi sitakuwa kabisa msaidizi kwa Wakosefu.”

Hii inamaanisha wale wanaokukufuru na wenye kwenda kinyume na kuhalifu Amri Zako.

* * *

فَأَصْبَحَ فِي الْمَدِينَةِ خَائِفًا يَتَرَقَّبُ
 فَإِذَا الَّذِي آسْتَنْصَرُهُ بِالْأَمْسِ
 يَسْتَصْرِخُهُ^ع قَالَ لَهُ مُوسَى إِنَّكَ لَغَوِيٌّ مُبِينٌ
 ﴿١٨﴾ فَلَمَّا أَنْ أَرَادَ أَنْ يَبْطِشَ بِالَّذِي هُوَ عَدُوٌّ لَهُمَا قَالَ
 يَمْوَسَىٰ أَتُرِيدُ أَنْ تَقْتُلَنِي كَمَا قَتَلْتَ نَفْسًا بِالْأَمْسِ^ط إِنْ
 تُرِيدُ إِلَّا أَنْ تَكُونَ جَبَّارًا فِي الْأَرْضِ وَمَا تُرِيدُ أَنْ تَكُونَ
 مِنَ الْمُصْلِحِينَ ﴿١٩﴾ وَجَاءَ رَجُلٌ مِّنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ
 يَسْعَىٰ قَالَ يَمْوَسَىٰ إِنَّ الْآمِلَاءَ يَأْتِمِرُونَ بِكَ لِيَقْتُلُوكَ
 فَاخْرُجْ إِنِّي لَكَ مِنَ النَّاصِحِينَ ﴿٢٠﴾ فَخَرَجَ مِنْهَا خَائِفًا
 يَتَرَقَّبُ^ط قَالَ رَبِّ نَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢١﴾ وَلَمَّا
 تَوَجَّهَ تَلْقَاءَ مَدْيَنَ قَالَ عَسَىٰ رَبِّي أَنْ يَهْدِيَنِي سَوَاءَ
 السَّبِيلِ ﴿٢٢﴾ وَلَمَّا وَزَدَ مَاءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةً
 مِّنَ النَّاسِ يَسْقُونَ وَوَجَدَ مِنْ دُونِهِمُ امْرَأَتَيْنِ
 تَذُودَانِ^ط قَالَ مَا خَطْبُكُمَا^ط قَالَتَا لَا نَسْقِي حَتَّىٰ يُصَدِرَ
 الرِّعَاءُ^ط وَأَبُونَا شَيْخٌ كَبِيرٌ ﴿٢٣﴾ فَسَقَى لَهُمَا ثُمَّ تَوَلَّىٰ
 إِلَى الظِّلِّ فَقَالَ رَبِّ إِنِّي لِمَا أَنْزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ﴿٢٤﴾

فَأَصْبَحَ فِي الْمَدِينَةِ خَائِفًا يَتَرَقَّبُ
 فَإِذَا الَّذِي آسْتَنْصَرُهُ بِالْأَمْسِ
 يَسْتَصْرِخُهُ^ع قَالَ لَهُ مُوسَى إِنَّكَ
 لَغَوِيٌّ مُبِينٌ ﴿١٨﴾ فَلَمَّا أَنْ أَرَادَ أَنْ
 يَبْطِشَ بِالَّذِي هُوَ عَدُوٌّ لَهُمَا قَالَ
 يَمْوَسَىٰ أَتُرِيدُ أَنْ تَقْتُلَنِي كَمَا قَتَلْتَ
 نَفْسًا بِالْأَمْسِ^ط إِنْ تُرِيدُ إِلَّا أَنْ
 تَكُونَ جَبَّارًا فِي الْأَرْضِ وَمَا تُرِيدُ أَنْ
 تَكُونَ مِنَ الْمُصْلِحِينَ ﴿١٩﴾

18. "Akapambazukiwa mjini asubuhi naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Mara yule yule aliyemtaka msaada jana akawa anampigia kelele amsaidie. Musa akamwambia: Hakika wewe ni mgomvi kweli kweli.

19. Basi alipotaka kumshika kwa nguvu yule aliye adui

wao wote wawili, akasema: Ewe Musa! Unataka kuniua kama ulivyomuua mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi, wala hutaki kuwa miongoni mwa watu wazuri."

Kufichuka Siri ya Musa عليه السلام kuua

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu Musa عليه السلام pale alipomuua yule Mkibti, akapambazukiwa:

فِي الْمَدِينَةِ خَائِفًا

“Mjini asubuhi naye anakhofu.”

Maana yake: Kwa fedheha ya alichofanya. Naye akawa:

يَتَرَقَّبُ

“Akiangalia huku na huku.”

Maana yake: Alikuwa akizunguka na kutazama kwa uangalifu huku akingojea matokeo yatakayomkumba kwa kitendo chake. Akapita katika baadhi ya njia, na hapo akamuona mtu yule aliyetaka usaidizi jana akipigana na Mkibti mwengine. Pindi tu Musa عليه السلام alipopita karibu yake, aliomba msaada mara nyengine tena dhidi ya mwingine. Musa عليه السلام akamwambia:

إِنَّكَ لَعَوَى مُبِينٌ ﴿١٨﴾

“Hakika wewe ni mgomvi kweli kweli.”

Maana yake: Ugomvi wa wazi mwingi wa shari. Kisha Musa عليه السلام aliazimia kumvamia Mkibti yule, lakini Muisraili, kwa sababu ya uoga wake na udhaifu, alidhania kuwa Musa عليه السلام amekusudia kumpiga yeye sababu ya yale aliyoyasema, akasema kwa kujitetea nafsi yake:

يَمْوَسَىٰ أَتُرِيدُ أَنْ نَمُوتَ لَكَ كَمَا مَاتَ نَفْسًا بِالْأَمْسِ

“Ewe Musa! Unataka kuniua kama ulivyomuua mtu jana?.”

Hakuna aliyejua jambo hilo isipokuwa yeye na Musa عليه السلام, lakini yule Mkibti aliposikia alichukua habari hiyo kwa milango ya Firauni na kumwambia hayo. Hivyo, Firauni alikuja kujua hilo, naye alikasirika sana na akaamua kumuua Musa عليه السلام. Firauni alituma watu ili wamlete mbele yake.

وَجَاءَ رَجُلٌ مِّنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ يَسْعَىٰ قَالَ يَمْوَسَىٰ إِنَّ أَمَلًا يَأْتِمُرُونَ بِكَ لِيَقْتُلُوكَ

فَأَخْرَجَ إِلَىٰ لَكَ مِنَ النَّاصِحِينَ ﴿٢٠﴾

20. "Na akaja mtu kutoka mwisho wa mji akipiga mbio, akasema: Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuua. Basi toka! Hakika mimi ni katika wanaokupa nasaha".

Akasema Aliyetukuka:

وَجَاءَ رَجُلٌ

"Na akaja mtu."

Amesifiwa kuwa ni mwanamme kwa sababu ya ujasiri wake wa kupita njia nyengine, njia fupi kuliko ile waliochukua wale waliotumwa kumshika Musa عليه السلام. Hivyo, aliwatangulia kwa Musa عليه السلام kumwambia: "Ewe Musa!

إِنَّ أَمَلًا يَأْتَمُرُونَ بِكَ

"Hakika wakubwa wana shauriana dhidi yako."

Hii inamaanisha wana shauriana kuhusu wewe:

لِيَقْتُلُوكَ فَآخْرُجْ

"Kukuua. Basi toka!"

Maana yake: Toka katika mji huu:

إِنِّي لَكَ مِنَ النَّاصِحِينَ ﴿٢٠﴾

"Hakika mimi ni katika wanaokupa nasaha."

فَخَرَجَ مِنْهَا خَائِفًا يَتَرَقَّبُ ۗ قَالَ رَبِّ زَيِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢١﴾ وَلَمَّا تَوَجَّهَ تَلْقَاءَ

مَدْيَنَ قَالَ عَسَىٰ رَبِّي أَن يَهْدِيَنِي سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿٢٢﴾ وَلَمَّا وَرَدَ مَاءَ مَدْيَنَ وَجَدَ

عَلَيْهِ أُمَّةً مِّنَ النَّاسِ يَسْقُونَ وَوَجَدَ مِنْ دُونِهِمُ امْرَأَتَيْنِ تَذُودَانِ ۗ قَالَ مَا خَطْبُكُمَا ۗ

قَالَتَا لَا نَسْقِي حَتَّىٰ يُصَدِرَ الرِّعَاءَ ۗ وَأَبُونَا شَيْخٌ كَبِيرٌ ﴿٢٣﴾ فَسَقَىٰ لَهُمَا ثُمَّ تَوَلَّىٰ إِلَى

الظِّلِّ فَقَالَ رَبِّ إِنِّي لِمَا أَنْزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ﴿٢٤﴾

21. Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhalimu.

22. Na alipoelekea upande wa Madyan alisema: Asaa (huenda) Mola wangu Mlezi Akaniongoa njia iliyo sawa.

23. Na alipoyafikia maji ya Madyan alikuta umati wa watu wananywesha (wanyama wao), na akakuta karibu yao wanawake wawili wanawazuia wanyama wao. Akasema: Mna nini? Wakasema: Hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao wachunga. Na baba yetu ni mzee sana.

24. Basi Musa akawanyweshea; kisha akarudi kivulini, na akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayoni-teremshia”.

Musa عليه السلام Akiwa Madyan na Kuwanyweshea wanyama wa Wanawake Wawili

Pindi yule mtu alipompa Musa عليه السلام habari kuhusu njama ya Firauni na dola yake dhidi yake, alitoka Misri peke yake. Hakuzoea kuwa peke yake, kwa sababu kabla ya hapo alikuwa akiishi maisha ya kifakhari na neema na uongozi.

فَخَرَجَ مِنْهَا خَائِفًا يَتَرَقَّبُ

“Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku.”

Maana yake: Alikuwa akigeuka na kutazama. Akasema:

قَالَ رَبِّ إِنِّي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٤﴾

“Akasema Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhalimu.”

Maana yake: Firauni na machifu wake. Imetajwa kuwa Allah تعالى Alimpelekea Malaika akiwa amepanda farasi, aliyekuwa akimuonesha njia. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Anasema Aliyetukuka:

وَلَمَّا تَوَجَّهَ تَلَقَّاءَ مَدْيَنَ

“Na alipoelekea upande wa Madyan.”

Maana yake: Alichukua njia yenye kupitika na rahisi, naye akafurahia hilo.

قَالَ عَسَىٰ رَبِّي أَن يَهْدِيَنِي سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿٢٨﴾

“Alisema: Asaa (huenda) Mola wangu Mlezi Akaniongoa njia iliyosawa.”

Hii inamaanisha njia iliyo nyoofu zaidi. Allah تعالى Akamfanyia hilo, kwani Alimuongoza katika njia iliyonyooka hapa duniani na Akhera, na Akamfanya muongofu mwenye kuongoza.

وَلَمَّا تَوَجَّهَ تَلْقَاءَ مَدْيَنَ

“Na alipoyafikia maji ya Madyan.”

Maana yake: Alipofika Madyan akaenda kunywa maji yake, kwani kulikuwa na kisima ambacho wachungaji walikuwa wakiwanyweshwa maji wanyama wao.

وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةٌ مِّنَ النَّاسِ يَسْقُونَ وَوَجَدَ مِنْ دُونِهِمْ امْرَأَتَيْنِ تَذُودَانِ

“Alikuta umati wa watu wananyweshwa (wanyama wao), na akakuta karibu yao wanawake wawili wanawazuia wanyama wao.”

Maana yake: Kundi likinyweshwa. Na mbali na hao: “akakuta wanawake wawili wanawazuia wanyama wao.”

Hawa wanawake walikuwa wakiwazuia wanyama wao wasinywe pamoja na wanyama wengine wa wachungaji, ili wasije wakadhuriwa. Pindi Musa عليه السلام alipowaona, aliwasikitikia na kuwaonea huruma. Hivyo,

قَالَ مَا خَطْبُكُمْ

“Akasema: Mna nini?”

Vipi ninyi mbona hamuwanyweshi wanyama wenu pamoja na hawa watu?

قَالَتَا لَا نَسْقِي حَتَّىٰ يُصَدِرَ الرِّعَاءَ

“Wakasema: Hatunyweshi sisi mpaka wamalize hao wachunga.”

Maana yake: Hatuwezi kunyweshwa mpaka hawa wamalize. Pia,

وَأَبُونَا شَيْخٌ كَبِيرٌ ﴿٢٨﴾

“Na baba yetu ni mzee sana.”

Hali hii ndiyo iliyotufanya sisi kuwa katika unayoyaona.

Amesema Allah تعالى Aliyetukuka:

فَسَقَى لَهُمَا

“Basi Musa akawanyweshea.”

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

ثُمَّ تَوَلَّى إِلَى الظِّلِّ فَقَالَ رَبِّ إِنِّي لِمَا أَنْزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ﴿٢٩﴾

“Kisha akarudi kivulini, na akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayoniteremshia.”

Na Kauli Yake:

إِلَى الظِّلِّ

“Akarudi kivulini”.

Amesema Ibn ‘Abbaas, Ibn Mas’uud na as-Suddiy: “Alikaa chini ya mti.”¹

Amesema ‘Atwaa’ ibn as-Saa’ib, pale Musa عليه السلام aliposema:

فَقَالَ رَبِّ إِنِّي لِمَا أَنْزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ﴿٣٠﴾

“Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri Utakayoniteremshia.”

Wanawake walimsikia².

* * *

¹ Atw-Twabariy 19:556.

² Atw-Twabariy 19:557.

فَجَاءَتْهُ إِحْدَاهُمَا تَمْشِي عَلَى اسْتِحْيَاءٍ قَالَتْ إِنَّ أَبِي يَدْعُوكَ لِيَجْزِيَكَ أَجْرَ مَا سَقَيْتَ لَنَا فَلَمَّا جَاءَهُ وَقَصَّ عَلَيْهِ الْقَصَصَ قَالَ لَا تَخَفْ نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾ قَالَتْ إِحْدَاهُمَا يَتَّابِتُ اسْتَجْرَهُ إِنَّ خَيْرَ مَنْ اسْتَجَرْتَ الْقَوِيُّ الْأَمِينُ ﴿٢٦﴾ قَالَ إِنِّي أُرِيدُ أَنْ أُنكِحَكَ إِحْدَى ابْنَتَيَّ هَاتَيْنِ عَلَى أَنْ تَأْجُرَنِي ثَمَنِي حِجَجٍ ۖ فَإِنْ أَتَمَمْتَ عَشْرًا فَمِنْ عِنْدِكَ ۖ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أَشُقَّ عَلَيْكَ ۖ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٢٧﴾ قَالَ ذَلِكَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ ۖ أَيَّمَا الْأَجَلَيْنِ قَضَيْتُ فَلَا عُدْوَانَ عَلَيَّ وَاللَّهُ عَلَىٰ مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٢٨﴾ * فَلَمَّا قَضَىٰ مُوسَىٰ الْأَجَلَ وَسَارَ بِأَهْلِهِ آنَسَ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ نَارًا قَالَ لِأَهْلِهِ امْكُثُوا إِنِّي آنَسْتُ نَارًا لَعَلِّي آتِيكُم مِّنْهَا بِخَبَرٍ أَوْ جَذْوَةٍ مِنَ النَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٢٩﴾ فَلَمَّا أَتَاهَا نُودِيَ مِنْ شَاطِئِ الْوَادِ الْأَيْمَنِ فِي الْبُقْعَةِ الْمُبْنَكَةِ مِنَ الشَّجَرَةِ أَنْ يَمْوَسَىٰ إِنِّي أَنَا اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٠﴾ وَأَنْ أَلْقِ عَصَاكَ ۖ فَلَمَّا رَآهَا تَهْتَزُّ كَأَنَّهَا جَانٌّ وَلَّىٰ مُدْبِرًا وَلَمْ يُعَقِّبْ ۚ يَمْوَسَىٰ أَقْبِلْ وَلَا تَخَفْ ۗ إِنَّكَ مِنَ الْآمِنِينَ ﴿٣١﴾ أَسْلَكَ يَدَكَ فِي جَيْبِكَ تَخَرُّجَ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ وَأَضْمَمَ إِلَيْكَ جَنَاحَكَ مِنَ الرَّهْبِ ۗ فَذَانِكَ بُرْهَنَانِ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَسِيقِينَ ﴿٣٢﴾

فَجَاءَتْهُ إِحْدَاهُمَا تَمْشِي عَلَى اسْتِحْيَاءٍ قَالَتْ إِنَّ أَبِي يَدْعُوكَ لِيَجْزِيَكَ أَجْرَ مَا سَقَيْتَ لَنَا فَلَمَّا جَاءَهُ وَقَصَّ عَلَيْهِ الْقَصَصَ قَالَ لَا تَخَفْ نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾ قَالَتْ إِحْدَاهُمَا يَتَّابِتُ اسْتَجْرَهُ إِنَّ خَيْرَ مَنْ اسْتَجَرْتَ الْقَوِيُّ الْأَمِينُ ﴿٢٦﴾ قَالَ إِنِّي أُرِيدُ أَنْ أُنكِحَكَ إِحْدَى ابْنَتَيَّ هَاتَيْنِ عَلَى أَنْ تَأْجُرَنِي ثَمَنِي حِجَجٍ ۖ فَإِنْ أَتَمَمْتَ عَشْرًا فَمِنْ عِنْدِكَ ۖ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أَشُقَّ عَلَيْكَ ۖ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٢٧﴾ قَالَ ذَلِكَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ ۖ أَيَّمَا الْأَجَلَيْنِ قَضَيْتُ فَلَا عُدْوَانَ عَلَيَّ وَاللَّهُ عَلَىٰ مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٢٨﴾

25. Basi mmoja katika wale wanawake wawili akamjia, naye anaona haya. Akasema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea. Basi alipomjia na akamsimulia visa vyake, alisema: Usiogope;

umekwishaokoka dhidi watu madhalimu.

26. Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yangu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.

27. Akasema: Mimi nataka kukuoza mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane. Ukitimiza kumi, khiari yako; lakini mimi sitaki kukutaabisha. Insha'Allah utanikuta miongoni mwa watu wema.

28. Musa akasema: Hayo yamekwishakuwa baina yangu na wewe. Muda mmojapo nikiumaliza sitiwi ubayani. Na Allah ni Mlinzi juu ya haya tunayoyasema”.

Musa عليه السلام Akakutana na Mzazi wa Wanawake Wawili, na Ndoa Yake kwa Mmoja wapo kwa Ujira wa Kuchunga Mbuzi

Pindi wale wanawake wawili waliporudi haraka nyumbani baba yao alistaajabu. Aliwauliza yaliyojiri, wakamueleza aliyofanya Musa عليه السلام. Hapo baba akamtuma mmoja wao aende akamuite aje kwa baba yake.

Amesema Allah تعالى:

فَجَاءَتْهُ إِحْدَاهُمَا تَمْشِي عَلَىٰ اسْتِخْيَاءٍ

“Basi mmoja katika wale wanawake wawili akamjia, naye anaona haya”.

Akitembea kama mwanamke huru, kama ilivyopokewa kutoka kwa Amiri wa Waumini, ‘Umar رضي الله عنه: “Alikuwa amejisitiri kwa kujifunika nguo yake”¹. Amepokea Ibn Abi Haatim kutoka kwa ‘Amr ibn Maymun kuwa ‘Umar رضي الله عنه amesema: “Alikuwa mwanamke akitembea kwa kuona haya, huku ameiweka nguo yake juu ya uso wake. Hakuwa miongoni mwa wale wanawake waliovuuliwa haya wenye ujasiri ambao ni viruka njia.”² Isnadi ya mapokezi haya ni Sahihi.

¹ At-Tabari 19:558.

² At-Tabari 19:559.

قَالَتْ إِنَّ أَبِي يَدْعُوكَ لِيَجْزِيَكَ أَجْرَ مَا سَقَيْتَ لَنَا

“Akasema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea”.

Huu ni upeo wa adabu katika ibara na mazungumzo, hakumualika moja kwa moja ili asianze kumdhania yeye dhana mbaya. Bali alisema: Baba yangu anakwita akulipe ujira wa kutunyweshea, yaani kukulipa malipo kwa wema wako wa kutunyweshea wanyama wetu.

فَلَمَّا جَاءَهُ وَقَصَّ عَلَيْهِ الْقِصَصَ

“Basi alipomjia na akamsimulia visa vyake”.

Alimuelezea kisa chake na yaliyotokea mpaka akalazimika kutoka katika nchi yake.

قَالَ لَا تَخَفْ نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾

“Alisema: Usiogope; umekwishaokoka dhidi ya watu madhalimu.”

Itulize nafsi yako na jicho lako, kwani ushatoka katika dola yao, nao hawana hukumu wala utawala wowote katika nchi yetu. Kwa hiyo akasema:

نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾

“Umekwishaokoka dhidi ya watu madhalimu.”

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

قَالَتْ إِحْدَاهُمَا يَأْتِيكِ آسْتَجِرُهُ إِنَّ خَيْرَ مَنْ آسْتَجَرْتَ الْقَوِيُّ الْأَمِينُ ﴿٢٦﴾

“Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yangu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.”

Binti mmoja kati ya wale wawili alisema maneno haya. Panasemwa kuwa ni yule binti aliyetembea nyuma ya Musa عليه السلام. Alimwambia baba yake:

يَأْتِيكِ آسْتَجِرُهُ

“Ewe baba yangu! Muajiri huyu.”

Kwa ajili ya uchungaji wa mbuzi hizi. Amesema 'Umar, Ibn 'Abbaas, Shurayh al-Qaadhi, Abu Maalik, Qataadah, Muhammad ibn Ishaah na wengineo رضي الله عنهم: "Pale aliposema:

إِنَّ خَيْرَ مَنْ أَسْتَعَجَزْتَ أَلْفَوْهُ الْأَمِينُ ﴿٢٥﴾

"Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu."

Babake alimuuliza: "Unajuaje hilo?" Alimwambia: "Yeye alinyanyua jabali ambao linaweza kunyanyuliwa na watu kumi, na tulipokuwa tunarudi pamoja, nilitembea mbele yake, akaniambia, tembea nyuma yangu. Nikikosea njia rusha kijiwe ili nipate kujua njia gani ya kuelekea."¹ Amesema 'Abdullah ibn Mas'uud رضي الله عنه: "Watu watambuzi bora ni watatu: Abubakr رضي الله عنه kumwelewa Umar رضي الله عنه; sahibu wa Yusuf عليه السلام pale aliposema:

أَكْرِمِي مَنُونَهُ

"Mtengenezee makazi yake." (12: 21)

Na sahibu wa kike wa Musa عليه السلام pale aliposema:

يَتَأْتِبِ أَسْتَعَجَزَهُ إِنَّ خَيْرَ مَنْ أَسْتَعَجَزْتَ أَلْفَوْهُ الْأَمِينُ ﴿٢٦﴾

'Ewe baba yangu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.'²

إِنِّي أُرِيدُ أَنْ أُنْكِحَكَ إِحْدَى أَبْتَنَيَّ هُنْتَيْنِ

"Mimi nataka kukuozza mmojawapo katika binti zangu hawa wawili".

Alitaka mzee huyu mkongwe kumuozesha mmoja kati ya binti zake wawili kwa mapatano ya kumchungia wanyama wake. Na Kauli Yake:

عَلَى أَنْ تَأْجُرَنِي ثَمَنِي حِجَجٍ فَإِنْ أَتَمَمْتَ عَشْرًا فَمِنْ عِنْدِكَ

"Kwa kunitumikia miaka minane. Ukitimiza kumi, khiari yako."

¹ Atw-Twabariy 19:562-564.

² Ibn Abi Shaybah 14:574.

Hii ilikuwa ni kumtumikia kwa kuchunga wanyama wake kwa miaka minane, lakini ukitaka kuzidisha miaka miwili, itakuwa juu yako, na kama sivyo miaka minane itatosha.

وَمَا أَرِيدُ أَنْ أُشُقُّ عَلَيْكَ ۚ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٢٧﴾

“Lakini mimi sitaki kukutaabisha. Insha’Allah utanikuta miongoni mwa watu wema.”

Maana yake: Sitaki kukutia katika mashaka wala kukutaabisha wala kujadiliana na wewe.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى Amepokea kuwa Ali bin Abi Rabah Al-Lakhami amesema, “Nimemsikia ‘Utbah bin An-Nadar As-Sulami رضي الله عنه, Sahaba wa Mtume akihadithia kwamba Allah تعالى Amesema:

«إِنَّ مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ آجَرَ نَفْسَهُ بِعَقْمَةِ فَرْجِهِ وَطَعْمَةِ بَطْنِيهِ»

“Mussa alijijiri mwenyewe kwa sababu ya kujiweka na kujizua na uchafu wa nafsi na kujitimizia mahitaji kwa kufanya kazi.”

Na Kauli Yake Allah عليه السلام kutupasha habari ya Musa:

قَالَ ذَٰلِكَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ أَيَّمَا الْأَجْلَيْنِ فَضَيْتُ فَلَا عُدْوَانَ عَلَيَّ وَاللَّهُ عَلَيَّ مَا تَقُولُ

وَكَيْلٌ ﴿٢٨﴾

“Musa akasema: Hayo yamekwisha kuwa baina yangu na wewe. Muda mmojawapo nikiumaliza sitiwi ubayani. Na Allah ni Mlinzi juu ya haya tunayo yasema.”

Musa عليه السلام alimwambia baba mkwe: “Suala hilo ni kama ulivyosema kuwa umeniajiri kwa miaka minane, na nikitimiza kumi hiyo ni juu yangu. Hata hivyo nikifanya uchache wake nitakuwa nimetimiza ahadi na kukamilisha masharti.”

Kwa hiyo akasema:

أَيَّمَا الْأَجْلَيْنِ فَضَيْتُ فَلَا عُدْوَانَ عَلَيَّ

“Muda mmojawapo nikiumaliza sitiwi ubayani.”

¹ Al-Bazzaar 1495.

Kumaanisha hakuna lawama juu yangu. Pamoja kuwa kukamilisha inaruhusiwa, lakini ni bora katika upande mwingine”.

Hii Aya ni kama ile Kauli ya Aliyetukuka:

فَمَنْ تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَنْ تَأَخَّرَ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ

“Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akarejea) si dhambi juu yake; na mwenye kukawia si dhambi juu yake.”(2:203)

Mtume ﷺ alimwambia Hamzah ibn ‘Amr al - Aslamiy رضي الله عنه aliyekuwa akifunga sana alipomuuliza kuhusu Saumu katika safari:

«إِنْ شِئْتَ فَصُمْ، وَإِنْ شِئْتَ فَأَنْطِرْ»

“Ukitaka fungua, na ukitaka fungua (kula).”¹

Japokuwa kufunga ni bora zaidi kulingana na dalili nyengine. Na zipo dalili kuonesha kuwa Musa عليه السلام alikamilisha muda mrefu zaidi kati ya hiyo mida miwili. Imepokewa na al-Bukhaariy kuwa Sa’iid ibn Jubayr alisema Myahudi kutoka hira aliniuliza mimi: “Musa alitekeleza muda upi wa kazi kati ya hiyo mida miwili?” Nikamjibu: “Mimi sijui mpaka niende nikaulize kwa wanazuoni Waarabu”. Nilikwenda kumuuliza Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما akaniambia: “Alitimize ule muda mrefu zaidi na bora kati yao, kwani pindi Mtume ﷺ anaposema atafanya kitu, basi alikuwa anatekeleza.”

Hivi ndivyo ilivyonukuliwa na al-Bukhaariy.²

* فَلَمَّا قَضَىٰ مُوسَى الْأَجَلَ وَسَارَ بِأَهْلِهِ آنَسَ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ نَارًا قَالَ لِأَهْلِهِ
 امْكُثُوا إِنِّي آنَسْتُ نَارًا لَعَلِّي آتِيكُمْ مِنْهَا بِخَبَرٍ أَوْ جَذْوَةٍ مِنَ النَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ
 ﴿٢٠٣﴾ فَلَمَّا أَتَاهَا نُودِيَ مِنْ شَطِئِ الْوَادِ الْأَيْمَنِ فِي الْبُقْعَةِ الْمُبْرَكَةِ مِنَ الشَّجَرَةِ أَنْ
 يَمْسِرَ إِلَىٰ - أَنَا اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٠٤﴾ وَأَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَلَمَّا رَءَاهَا هَتَّتْ لَهَا

¹ Al-Bukhary 1943.

² Angalia mjeledi wa sita Tafsir Surat Taha 20:11-16)

جَانٌّ وَّلِيٌّ مُدَبِّرًا وَلَمْ يُعَقِّبْ ۚ يَمْوَسَىٰ أَقْبَلَ وَلَا تَخَفْ ۗ إِنَّكَ مِنَ الْآمِنِينَ ﴿٢٩﴾ أَسَلُكَ
 يَدَكَ فِي جَيْبِكَ تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ وَأَضْمَمَ إِلَيْكَ جَنَاحَكَ مِنَ الرَّهْبِ ۗ
 فَذَلِكَ بُرْهَانَانِ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا فٰسِقِينَ ﴿٣٠﴾

29. Basi Musa alipotimiza muda wake na akasafiri na ahali wake, aliona moto upande wa Mlima Turi. Akawaambia ahali zake: Ngojeni! Mimi nimeona moto, labda nitakuleteeni kutoka huko khabari au kijinga cha moto ili mpate kuota moto.

30. Basi alipoufikia aliitwa kutoka ng'ambo ya bonde la kuliani katika eneo liliobarikiwa kutoka kwenye mti: Ewe Musa Hakika Mimi ni Allah, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

31. Na tupa chini fimbo yako. Basi alipoiona ikitikisika kama nyoka, akarudi nyuma wala hakutazama. (Akaambiwa): Ewe Musa! Njoo mbele wala usiogope. Hakika wewe ni miongoni mwa waliosalimika.

32. Ingiza mkono wako kwenye mfuko wako, utatoka mweupe pasipo na ubaya. Na jiambatishe mkono wako ukihisi khofu. Basi hizi ni dalili mbili zitokazo kwa Mola wako Mlezi kumpelekea Firauni na wakuu wa ummah wake. Hakika hao walikuwa watu mafasiki".

Musa عليه السلام Anarudi Misri na Kukirimiwa Utume na Miujiwa Njiani

Yametangulia maelezo katika tafsiri ya Aya kabla ya hii kuwa Musa عليه السلام alitimiza muda mrefu zaidi, mkamilifu zaidi, mwema zaidi, na msafi zaidi. Hii inaweza kueleweka pia katika Aya tukufu pale aliposema Aliyetukuka:

فَلَمَّا قَضَىٰ مُوسَىٰ الْأَجَلَ

"Basi Musa alipotimiza muda wake".

Maana yake: Ukamilifu zaidi ya mida hiyo miwili, na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

وَسَارَ بِأَهْلِيهِ

“Na akasafiri na ahali wake”.

Wanasema: “Musa عليه السلام alikuwa na hamu ya nchi yake na jamaa zake. Kwa hivyo aliazimia kuwazuru kwa siri, bila ya Firauni na kaumu yake kujua. Aliikusanya familia yake na wanyama (kondoo na mbuzi) wake aliopewa na baba mkwe, na kuanza safari usiku wa baridi, giza na mvua. Walipiga kambi na kila alipojaribu kuwasha moto hakufanikiwa. Alistaajabu kwa hilo, na alipokuwa katika hali hiyo,

ءَأَنْسَ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ نَارًا

“Aliona moto upande wa Mlima Turi.”

Aliona moto ukiwaka kwa mbali.

قَالَ لِأَهْلِهِ امْكُثُوا إِنِّي آنَسْتُ نَارًا

“Akawaambia ahali wake: Ngojeni! Mimi nimeona moto.”

Maana yake: Ningojeeni hapa wakati ninapokwenda huko.

لَعَلِّي آتَيْتُكُمْ مِنْهَا بِخَبَرٍ

‘Labda nitakuleteeni kutoka huko khabari.’

Hiyo ni kwa kuwa walikuwa wamepotea njia.

أَوْ جَذْوَةٍ مِنَ النَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٢٨﴾

“Au kijinga cha moto’, ‘Ili mpate kuota moto’, kwa ajili ya kupata uharara na kutoa ubaridi.”

Maana yake: Kipande cha moto. Amesema Allah تعالى:

فَلَمَّا أَتَتْهَا نُودِيَ مِنْ شَاطِئِ الْوَادِ الْأَيْمَنِ

“Basi alipoufikia aliitwa kutoka ng’ambo ya bonde la kuliani”.

Maana yake: Upande wa bonde ulioshikana na mlima kuliani kwake, upande wa magharibi, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْغَرْبِيِّ إِذْ قَضَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ الْأَمْرَ

**“Wala wewe hukuwa upande wa magharibi Tulipompa Musa Amri.”
(28:44).**

Hii inaonesha kuwa Musa عليه السلام aliukusudia moto uliokuwa upande wa Qibla na mlima wa upande wa magharibi ukiwa kuliani mwake. Alikuta moto huo ukiwaka kwenye mti wa kijani upande wa mlima karibu na bonde. Alisimama hapo kwa mshangao kwa aliyoyaona. Hapo Mola Wake Mlezi Akamuita:

مِن شَطِئِ الْأَوَادِ الْأَيْمَنِ فِي الْبُقْعَةِ الْمُبْرَكَةِ مِنَ الشَّجَرَةِ

“Kutoka ng'ambo ya bonde la kuliani katika eneo liliobarikiwa kutoka kwenye mti.”

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَنْ يَمْوَسَىٰ إِنَّي - أَنَا اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٥﴾

“Ewe Musa! Hakika Mimi ni Allah, Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Maana yake: Mwenye Kukuhutubia na Kuzungumza nawe ni Mola Mlezi wa walimwengu, Mwenye Kufanya Anavyotaka, hapana Muabudiwa ila Yeye wala Mola kama Yeye, Mtukufu Aliyetakasika, Ambaye hakuna wa kulingana katika Dhati Yake, Sifa Zake, Kauli na Vitendo Vyake. Na Kauli Yake:

وَأَنْ أَلْقِي عَصَاكَ ﴿٢٦﴾

“Na tupa chini fimbo yako”.

Ambayo iko mkononi mwako kama Alivyothibitisha hilo katika Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا تِلْكَ بِيَمِينِكَ يَمْوَسَىٰ ﴿٢٧﴾ قَالَ هِيَ عَصَايَ أَتَوَكَّؤُا عَلَيْهَا وَأَهشُّ بِهَا عَلَىٰ غَنَمِي

وَلِيَٰ فِيهَا مَنَارِبٌ أُخْرَىٰ ﴿٢٨﴾

“Na nini hicho kilichomo mkono wako wa kulia, ewe Musa?”

Akasema: Hii ni fimbo yangu; naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu. Tena inanifaa kwa matumizi mengine.” (20:17-18).

Na maana ni kuwa fimbo hii, ambayo unajua vizuri.

أَلْقَهَا يَمُوسَىٰ ﴿٢٠﴾ فَأَلْقَاهَا فَإِذَا هِيَ حَيَّةٌ تَسْعَىٰ ﴿٢١﴾

“Itupe, ewe Musa! Akaitupa, mara ikawa nyoka anayekwenda mbio.” (20:19-20).

Akajua ya kwamba Yule anayezungumza Naye na Kumhutubia ni Yule Ambaye Anakiamuru kitu chochote, “kuwa”, kikawa kama tulivyoeleza katika Tafsiri ya *Surat Twaaha*. Na Akasema hapa:

فَلَمَّا رَأَاهَا تَهْتَزُّ كَأَنَّهَا جَانٌّ وَلَّىٰ مُدَبِّرًا

“Basi alipoiona ikitikisika kama nyoka, akarudi nyuma.”

Nyoka huyo alikuwa anatembea haraka sana, mbali na ukubwa wake pamoja na upana wa mdomo wake na taya zake kung’atana. Lilimeza kila jiwe lililokutana naye, na kila jiwe lililoanguka kwenye mdomo wake lilianguka kwa sauti kama vile jabali kuanguka katika bonde. Alipoona hayo:

وَلَّىٰ مُدَبِّرًا وَلَمْ يَعْقِبْ

“Akarudi nyuma wala hakutazama.”

Wala hakuwa ni mwenye kutazama tazama kwani maumbile na tabia ya mwanadamu inakimbia hilo.

Pale Allah تعالى Alipomuambia:

يَمُوسَىٰ أَقْبِلْ وَلَا تَخَفْ

“Ewe Musa! Njoo mbele wala usiogope.”

Alirudi hapo hapo na kusimama katika mahali alipokuwa mwanzo.

Kisha Allah تعالى Akasema:

أَسَلِّكَ بِدَاكِ فِي جَيْبِكَ تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ

“Ingiza mkono wako kwenye mfuko wako, utatoka mweupe pasipo na ubaya.”

Utakapoungiza mkono wako katika nguo yako na kuutoa, utakuwa unang’aa kwa weupe kama kipande cha mwezi au mwanga wa radi. Kwa hiyo Akasema:

مِنْ غَيْرِ سُوءٍ

“Pasipo na ubaya.”

Bila ya ukoma (ugonjwa wa kuwa na weupe wa ngozi).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَضْمَمَ إِلَيْكَ جَنَاحَكَ مِنَ الرَّهْبِ

“Na jiambatisha mkono wako ukihisi khofu.”

Amesema Mujahid: “Kutokuwa na khofu”. Amesema Qataadah: “Bila kutishika”¹. Musa عليه السلام aliamrisha kuwa pindi anapohisi hofu ya kitu chochote aambatishe mkono wake ubavuni mwake ili atokwe na khofu. Akifanya hivyo, khofu yote aliyokuwa nayo itaondoka. Huenda pia mtu anapofanya hivyo, kufuata mfano wa Musa عليه السلام, na kuuambatisha mkono wake kwenye kifua chake (kwenye moyo), khofu yake itaondoka au kupunguzwa, Akipenda Allah تعالى; na Kwake ndio tunaweka mategemeo yetu. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَدَايِلِكَ بُرْهَنَانِ مِنْ رَبِّكَ

“Basi hizi ni dalili mbili zitokazo kwa Mola wako Mlezi.”

Maana yake: Kutupa fimbo, ambayo inabadilika kuwa nyoka anayetembea na kuutia mkono wake kwenye nguo yake ambao unatoka ukiwa mweupe bila ubaya wowote.

Hizi ni dalili mbili za uhakika na wazi kwa nguvu za Yule ambaye Anafanya Anavyotaka na ukweli wa Unabii wa yule aliyefanya miujiza hiyo.

¹ Atw-Twabariy 19:575.

Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَأَيْنَاهُ

“Kumpelekea Firauni na wakuu wa ummah wake.”

Maana yake: Kaumu yake miongoni mwa viongozi, wakuu na wafuasi wake.

إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٢٧﴾

“Hakika hao walikuwa watu mafasiki.”

Maana yake: Waliotoka katika kumtii Allah تعالیٰ, wenye kuhalifu Amri Zake na Dini Yake.

* * *

قَالَ رَبِّ إِنِّي قَتَلْتُ مِنْهُمْ نَفْسًا فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿٣٣﴾
 وَأَخِي هَارُونَ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَانًا فَأَرْسَلْهُ مَعِيَ رِدْءًا
 يُصَدِّقُنِي ۗ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ ﴿٣٤﴾ قَالَ سَنَسُدُّ
 عَضُدَكَ بِأَخِيكَ وَنَجْعُلُ لَكُمَا سُلْطَنًا فَلَا يَصِلُونَ إِلَيْكُمَا
 ۚ بِمَا يَتَيَّنَّ أَنْتُمَا وَمَنْ اتَّبَعَكُمَا الْفَاطِلِينَ ﴿٣٥﴾ فَلَمَّا جَاءَهُمْ
 مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا بَيِّنَاتٍ قَالُوا مَا هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّفْتَرَىٰ وَمَا
 سَمِعْنَا بِهَذَا فِي ءِآبَائِنَا الْأُولَىٰ ﴿٣٦﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ رَبِّي
 أَعْلَمُ بِمَنْ جَاءَ بِالْهُدَىٰ مِنْ عِنْدِهِ وَمَنْ تَكُونُ لَهُ عَاقِبَةُ
 الدَّارِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٣٧﴾ وَقَالَ فِرْعَوْنُ
 يَتَأَيُّهَا آتَمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهِ غَيْرِي فَأَوْقِدْ لِي
 يَنْهَمِنَنَّ عَلَى الظَّالِمِينَ فَأَجْعَلْ لِي صَرْحًا لَعَلِّي أَطَّلِعُ إِلَىٰ إِلَهِ
 مُوسَىٰ وَإِنِّي لأُظَنُّهُ مِنَ الكَذِبِينَ ﴿٣٨﴾ وَأَسْتَكْبِرُ هُوَ
 وَجُنُودُهُ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ إِلَيْنَا لَا
 يُرْجَعُونَ ﴿٣٩﴾ فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ ۗ
 فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾ وَجَعَلْنَاهُمْ
 أَيْمَةً يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يُنصَرُونَ ﴿٤١﴾
 وَأَتَّبَعْنَاهُمْ فِي هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ هُمْ
 مِنَ الْمَقْبُوحِينَ ﴿٤٢﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ مِنْ
 بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَ الْأُولَىٰ بَصَائِرَ لِلنَّاسِ وَهُدًى
 وَرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٤٣﴾

قَالَ رَبِّ إِنِّي قَتَلْتُ مِنْهُمْ نَفْسًا
 فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿٣٣﴾ وَأَخِي
 هَارُونَ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَانًا
 فَأَرْسَلْهُ مَعِيَ رِدْءًا يُصَدِّقُنِي ۗ إِنِّي أَخَافُ
 أَنْ يُكَذِّبُونِ ﴿٣٤﴾ قَالَ سَنَسُدُّ
 عَضُدَكَ بِأَخِيكَ وَنَجْعُلُ لَكُمَا سُلْطَنًا
 فَلَا يَصِلُونَ إِلَيْكُمَا ۚ بِمَا يَتَيَّنَّ أَنْتُمَا
 وَمَنْ اتَّبَعَكُمَا الْفَاطِلُونَ ﴿٣٥﴾

33. Akasema: Mola wangu
 Mlezi! Hakika mimi nili-
 muua mtu katika wao, kwa
 hivyo naogopa wataniua.

34. Na ndugu yangu
 Haaruun ni fasihi zaidi ulimi
 wake kuliko mimi. Basi
 mtume ende nami kuni-
 saidia, ili anisadikishe.
 Hakika mimi ninakhofu
 watanikadhibisha.

35. (Mwenyezi Mungu)
 Akasema: Tutautia nguvu
 mkono wako kwa nduguyo,
 na Tutakupeni madaraka,
 hata wasikufikilieni. Kwa
 sababu ya Ishara Zetu
 nyinyi na watakaoku-
 fuateni mtashinda".

Musa عليه السلام anaomba Usaidizi wa Nduguye Haaruun عليه السلام na Allah تعالى Kumkubalia Ombi Lake Hilo.

Allah تعالى Alipomuamuru kurudi kwa Firauni, ambaye ni sababu ya yeye kutoka Misri akimkimbia yeye na kuwa na khofu na mlipiza kisasi:

قَالَ رَبِّ إِنِّي قَتَلْتُ مِنْهُمْ نَفْسًا

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nilimuua mtu katika wao.”

Maana yake: Yule Mkibiti.

فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿٣٣﴾

“Kwa hivyo naogopa wataniua.”

Pindi watakaponiona. Kisha anapendekeza:

وَأَخِي هَارُونُ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَانًا

“Na ndugu yangu Haaruun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi.”

Hiyo ni kuwa Musa عليه السلام alikuwa na kithembe (kigugumizi), kwa sababu ya kuwa yeye alikula kaa la moto pale alipochaguzwa baina yake na tende au lulu. Musa عليه السلام alichukua kaa la moto akaliweka kwenye ulimi wake, hivyo akawa na shida katika mazungumzo. Kwa hiyo akasema:

وَأَحْلَلْتُ عُقْدَةً مِّن لِّسَانِي ﴿٣٤﴾ يَفْقَهُوا قَوْلِي ﴿٣٥﴾ وَأَجْعَل لِّي وَزِيرًا مِّنْ أَهْلِي ﴿٣٦﴾

هَارُونَ أَخِي ﴿٣٧﴾ أَشَدُّ بِمَآزِرِي ﴿٣٨﴾ وَأَشْرِكُهُ فِي أَمْرِي ﴿٣٩﴾

“Na ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu maneno yangu. Na nipe waziri katika watu wangu, Haaruun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu. Na umshirikishe katika kazi yangu.” (20:27-32).

¹ Haya yamo kwenye mapokezi kutoka kwa Said bin Jubayr yaliopokewa na At-Tabary katika Tafsir ya Surat Taha 20:27

Hii inamaanisha kuwa anisaidie katika Uliyoni amuru kwa kazi hii kubwa, nayo ni kufikisha ujumbe kwa mfalme huyu mwenye kiburi, jabari na mwenye inadi. Kwa hiyo akasema:

وَأَخِي هَارُونَ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَانًا فَأَرْسَلْهُ مَعِيَ رِدْءًا

“Na ndugu yangu Haaruun ni fasihi zaidi ulimi wake kuliko mimi. Basi mtume ende nami kunisaidia.”

Maana yake: Waziri, msaidizi na mwenye kutia nguvu jambo langu hilo (*la Da'wah*), anisadikishe kwa ninayoyasema na kumpa habari kuhusu Allah تعالى, kwani neno la watu wawili lina uzito zaidi katika akili za watu kuliko neno la mtu mmoja. Hivyo akasema:

إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَذِّبُونِ ﴿٣٦﴾

“Hakika mimi nina khofu watanikadhibisha.”

Muhammad ibn Ishaq رحمه الله تعالى amesema: (katika kutafsiri Neno Lake Allah تعالى)

رِدْءًا يُصَدِّقُنِي

“Ili anisadikishe.”

Maana yake: “kuwaelezea ninayo yasema, kwani yeye anaweza kunielewa kwa wasiyofahamu.” Alipoomba hilo Musa عليه السلام, Allah تعالى Alimwambia:

سَتَشُدُّ عَضُدَكَ بِأَخِيكَ

“Tutautia nguvu mkono wako kwa nduguyo.”

Tutautia nguvu utume wako na kukupa msaada kupitia kwa nduguyo, Haaruun عليه السلام, ambaye umeomba awe Nabii pamoja nawe, kama Alivyosema katika Aya nyengine:

قَدْ أَوْتَيْتَ سُؤْلَكَ يَمُوسَىٰ ﴿٣٧﴾

“Hakika umepewa maombi yako, ewe Musa!” (20:36).

وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيًّا ﴿٣٨﴾

“Nasi kwa Rehema Zetu Tukampa nduguye, Haaruun, awe Nabii.” (19:53).

Kwa hilo akasema mmoja kati ya *Salaf* (watangu wema): “Hakuna hata mmoja aliyefanya hisani kubwa kwa nduguye kama Musa عليه السلام alivyofanya kwa Haaruun عليه السلام, kwani alimwomba mpaka Allah تعالى Akamfanya kuwa Nabii na Mtume pamoja naye ili waende pamoja kwa Firauni na wakuu wake.” Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka kuhusu Musa عليه السلام:

وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ وَجِيهًا ﴿٣٦﴾

“Naye alikuwa mwenye hisima mbele ya Allah.” (33:69).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَنَجْعَلُ لَكُمْ سُلْطٰنًا

“Na Tutakupeni madaraka.”

Maana yake: Hoja yenye nguvu.

فَلَا يَصِلُونَ إِلَيْكُمْ

“Hata wasikufikilieni.”

Nao hawatakuwa na njia wala kufikia kuwaudhi nyinyi kwa sababu mnafikisha ishara za Allah تعالى, kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿٣٧﴾ يَتَأْتِيهَا الرُّسُولُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi.”

Mpaka kufikia Kauli Yake:

وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ

“Na Allah Atakulinda na watu.” (5:67).

الَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَالَاتِ اللَّهِ

“Wale waliokuwa wakifikisha ujumbe wa Allah.”

Mpaka Kauli Yake:

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ حَسِيبًا ﴿٣٩﴾

“Na Allah Ndiye Atoshaye Kuhesabu.” (33: 39).

Maana yake: Allah تعالى Anatosha kuwa Msaidizi na Mwenye Kukutia nguvu. Hivyo, Allah تعالى Aliwaeleza kuwa mwisho wao na wafuasi wao utakuwa mwema hapa duniani na kesho Akhera. Akasema Aliyetukuka:

أَنْتُمْ وَمَنْ أَتَّبَعَكُمْ أَغْلِبُونَ ﴿٤٠﴾

“Nyinyi na watakaokufuateni mtashinda.”

Hii ni kama ile Ayah Aliyosema Aliyetukuka:

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۚ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤١﴾

“Allah Amekwishaandika: ‘Bila shaka Nitashinda mimi na mitume Yangu!’ Hakika Allah ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.” (58: 21).

Amesema tena Aliyetukuka:

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi.” (40:51)

فَلَمَّا جَاءَهُمْ مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا بَيِّنَاتٍ قَالُوا مَا هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّفْتَرَىٰ وَمَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي

ءَابَائِنَا الْأُولَىٰ ﴿٥٢﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ رَبِّي أَعْلَمُ بِمَنْ جَاءَ بِالْهُدَىٰ مِنْ عِنْدِهِ وَمَنْ تَكُونُ

لَهُ عَاقِبَةُ الدَّارِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٥٣﴾

36. Basi alipowafikia Musa na Ishara Zetu, walisema: Haya si chochote ila ni uchawi uliozuliwa. Na hatukuyasikia haya kwa baba zetu wa zamani.

37. Na Musa akasema: Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kujua kabisa

nani anayekuja na uwongofu unaotoka Kwake, na nani atakayekuwa na mwisho mwema wa makazi. Hakika wenye kudhulumu hawatafanikiwa.”

Musa عليه السلام Mbele ya Firauni na Kaumu Zake

Allah تعالى Anatueleza kuja kwa Musa na nduguye kwa Firauni na wakuu wake, na kumuonesha yeye ile miujiza ya uhakika waliyopewa na Allah تعالى pamoja na dalili za nguvu kusadikisha wanayosema katika kumpwekesha na kufuata Amri Zake. Waliona hayo kwa macho yao Firauni na wakuu wake na kuyakinisha kuwa yanatoka kwa Allah تعالى, lakini kwa sababu ya ukafiri wao na uovu wao walifuata hoja za uwongo. Hii ni kuwa walikuwa wabaya sana na wenye kiburi katika kufuata haki. Hapo wakasema:

مَا هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّفْتَرٍ

“Haya si chochote ila ni uchawi uliozuliwa.”

Maana yake: Uliotungwa na kubuniwa. Wao walitaka tu kumpinga kwa hila, jaha lakini hilo halikuwa pamoja nao:

وَمَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي آبَائِنَا الْأُولِينَ

“Na hatukuyasikia haya kwa baba zetu wa zamani.”

Wakimaanisha kule kuabudu Mwenyezi Mungu Mmoja Peke Yake asiyekuwa na mshirika.

Wakasema: “Hatukuona yeyote miongoni mwa mababu zetu aliyefuata dini hiyo (yako); tuliwaona tu watu wakimshirikisha Allah تعالى na miungu mingine”. Musa عليه السلام aliwajibu kwa kusema:

رَبِّيَ أَعْلَمُ بِمَنْ جَاءَ بِالْهَدْيِ مِنْ عِنْدِهِ

“Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kujua kabisa nani anayekuja na uwongofu unaotoka Kwake”.

Maana yake: Kutoka kwangu na kwenu, na Ataamua baina yangu na yenu. Kwa hiyo akasema:

وَمَنْ تَكُونُ لَهُ عَنقَبَةُ الدَّارِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٣٧﴾

“...Ni nani atakayekuwa na mwisho mwema wa makazi.”

Maana yake: Atakayenusuriwa, kusaidiwa na kushinda. Kwani:

إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿٣٧﴾

“Hakika wenye kudhulumu hawatafanikiwa.”

Maana yake: Wanaomshirikisha Allah تعالى.

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يَتَأَيَّبَهَا الْمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهِ غَيْرِي فَأَوْقَدَ لِي يَهْمَنُ عَلَى
الطِّينِ فَاجْعَلْ لِي صَرْحًا لَعَلِّي أَطَّلِعُ إِلَى إِلَهِ مُوسَى وَإِنِّي لأظنُّهُ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٣٨﴾
وَأَسْتَكْبِرُ هُوَ وَجُنُودُهُ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ إِلَيْنَا لَا يُرْجَعُونَ ﴿٣٩﴾
فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ فَأَنظَرَ كَيْفَ كَانَتْ عَنقَبَةُ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾
وَجَعَلْنَاهُمْ أُيْمَةً يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يُنصَرُونَ ﴿٤١﴾ وَأَتَّبَعْنَاهُمْ فِي
هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ هُمْ مِنَ الْمَقْبُوحِينَ ﴿٤٢﴾

38. Na Firauni akasema: Enyi waheshimiwa! Sijui kama mnaye mungu asiye kuwa mimi. Ewe Haamaan! Niwashie moto unichomee udongo, unijengee mnara nipate kumchungulia mungu wa Musa. Na hakika mimi namwona yeye ni katika waongo.

39. Na alipanda kiburi yeye na majeshi yake katika nchi bila ya haki, na wakadhandia kuwa hawatarudishwa Kwetu.

40. Basi Tukamshika yeye na majeshi yake, na Tukawatupa baharini. Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa wenye kudhulumu?

41. Na Tuliwafanya ni waongozi waitao kwenye Moto. Na Siku ya Kiyama hawatanusuriwa.

42. Na Tukawafuatishia laana katika dunia hii, na Siku ya Kiyama watakuwa miongoni mwa wanaochusha.”

Matokeo ya Kiburi cha Firauni

Allah تعالى Anatupa habari kuhusu kufuru ya Firauni na uovu wake na jinsi alivyodai kwa uwongo uungu kwa nafsi yake ovu, Allah تعالى Amlaani, kama Alivyosema Allah تعالى:

فَأَسْتَحَفَّ قَوْمَهُ فَأَطَاعُوهُ

“Na akawachezea watu wake, nao wakamtii” (43:54).

Hilo ni kwa sababu aliwaita watu wake wautambue uungu wake, nao wakaitikia kwa sababu ya akili zao ndogo na ufinyu wa mawazo yao. Kwa hiyo akasema:

يَتَّبِعُهَا أَمْلًا مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِّنْ إِلَهٍ غَيْرِي

“Enyi waheshimiwa! Sijui kama mnaye mungu asiyekuwa mimi.”

Allah تعالى Amesema tena kutupasha habari yake (Firauni):

فَحَشَرَ فَنَادَى ﴿٢٣﴾ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَى ﴿٢٤﴾ فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْآخِرَةِ وَالْأُولَى ﴿٢٥﴾

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن يَتَّخِذُ آ

“Basi aliwakusanya watu akanadi. Akasema mimi ndiye Mola wenu mkuu’. Hapo Allah Akamtia Mkononi kwa kulipa tamko lake hili la mwisho na kwa lile tamko lake la mwanzo. Hakika katika haya limo onyo kubwa kwa wale wanaogopa.” (79: 23– 26).

Maana yake: Ni kuwa aliwakusanya watu wake na kuwaita wao kwa sauti yake kubwa sana akiwaeleza hilo waziwazi nao wakamuitikia kwa kusikia na kutii. Hivyo, Allah تعالى Alilipiza kisasi, na Kuwafanya kuwa ni mazingatio kwa wengine hapa duniani na Akhera. Hata alimkabili Musa عليه السلام kwa hilo na kumwambia:

لِّئِن آتَّخَذْتَ إِلَهًا غَيْرِي لِأَجْعَلَكَ مِنَ الْمَسْجُورِينَ ﴿٢٦﴾

“Kama ukishikilia kuwa kuna mungu mwengine badala yangu kwa yakini nitakufanya miongoni mwa wenye kufungwa gerezani.” (26: 29).

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَأَوْقَدَ لِي يَبْهَمُنُّ عَلَى الطِّينِ فَأَجْعَلْ لِي صَرْحًا لَعَلِّي أَطَّلِعُ إِلَى إِلَهِ مُوسَى

“Ewe Haamaan! Niwashie moto unichomee udongo, unijengee mnara nipate kumchungulia mungu wa Musa.”

Alimuamuru waziri na mshauri wake Hamana achome matofali ya udongo amwajiri mtu ili ajenge mnara mrefu sana, na hilo ni jumba kubwa lililo inuka juu kama alivyosema katika aya nyingine:

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يَبْهَمُنُّ ابْنِ لِي صَرْحًا لَعَلِّي أَبْلُغُ الْأَسْبَابَ ﴿٣٦﴾ أَسْبَابَ السَّمَوَاتِ فَأَطَّلِعَ إِلَى إِلَهِ مُوسَى وَإِنِّي لأَظُنُّهُ كَذِبًا ۗ وَكَذَلِكَ زُينَ لِفِرْعَوْنَ سُوءَ عَمَلِهِ وَصُدَّ عَنِ السَّبِيلِ ۗ وَمَا كَيْدُ فِرْعَوْنَ إِلَّا فِي تَبَابٍ ﴿٣٧﴾

“Na Firauni akasema: ‘Ewe Haamaan! Nijengee mnara ili nipate kuzifikia njia. Njia za mbinguni ili nikamuone Mungu wa Musa; na kwa yakini ninamjua kuwa ni muongo tu.’ Na hivi ndivyo Firauni alivyopambiwa ubaya wa vitendo vyake na akazuiliwa njia ya haki; lakini vitimbi vya Firauni havikuwa ila katika kuangamia tu.” (40: 36-37).

Hiyo ni kuwa Firauni alijenga mnara ambao haujawahi kuonekana katika dunia, kwa sababu alikuwa anataka kuwaonesha raia zake kuwa Musa عليه السلام anadanganya alipodai kuwa yupo Mungu mbali na yeye. Firauni kwa ajili hii alisema:

وَإِنِّي لأَظُنُّهُ مِنَ الْكَاذِبِينَ

“Na hakika mimi namwona yeye ni katika waongo.”

Pale aliposema kuwa yuko Mungu asiyekuwa mimi. Sio kuwa Firaun anapinga kuwa Allah تعالى Amemtuma Musa عليه السلام, kwa sababu yeye (Firauni) hakukubali wala kuamini kuwa yupo Muumbaji kabisa (imani yake ni kuwa hakuna Muumbaji kabisa). Hakika yeye alisema:

وَمَا رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٣﴾

“Na nani huyu Mola wa walimwengu.” (26:23).

Na kasema tena:

لِيُنْزِلَ عَلَيْكَ رَبُّكَ آيَاتِهِ لِيُخَوِّفَ بِنُورِهِ الَّذِينَ كَفَرُوا وَلْيَذْهَبَ اللَّهُ غَلْبًا لِلْإِيمَانِ ﴿٣٣﴾

“Kama ukishikilia kuwa kuna Mungu mwengine badala yangu kwa yakini nitakufanya miongoni mwa wenye kufungwa gerezani.” (26: 29),

Akasema tena:

يَتَأْتِيهَا الْمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهِ غَيْرِي ﴿٣٤﴾

“Enyi waheshimiwa! Sijui kama mnaye mungu asiyekuwa mimi.”

Hii ni kauli ya Ibn Jariir رحمه الله تعالى.¹ Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَسْتَكْبِرُ هُوَ وَجُنُودُهُ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ إِلَيْنَا لَا يُرْجَعُونَ ﴿٣٥﴾

“Na alipanda kiburi yeye na majeshi yake katika nchi bila ya haki, na wakadhania kuwa hawatarudishwa Kwetu.”

Nao walizidi jeuri na wakafanya ubabe na ufidadi katika ardhi kwa kuitakidi kuwa hakuna Kiyama wala ufufuo. Anasema Aliyetukuka:

فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿٣٦﴾ إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ﴿٣٧﴾

“Kwa hivyo Mola wako Aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu. Hakika Mola wako yuko katika malindizo.” (89:13-14).

Kwa hiyo akasema Aliyetukuka hapa:

فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ ﴿٣٨﴾

“Basi Tukamshika yeye na majeshi yake, na Tukawatupa baharini.”

Tuliwazamisha na kuwaangamiza katika bahari kwa asubuhi moja tu, na hakuna hata mmoja kati yao aliyebaki.

Allah تعالى Anaendelea:

¹ Atw-Twabariy 19:580.

فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّالِمِينَ ﴿٣٣﴾ وَجَعَلْنَاهُمْ آيَةً يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ

**“...Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa wenye kudhulumu?”
Na Tuliwafanya ni waongozi waitao kwenye moto.”**

Kwa wale waliowafuata na kuchukua njia hiyo hiyo kama walivyofanya wao, kuwakadhibisha Mitume na kukataa kuwepo kwa Muumbaji. Pia,

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يُنصَرُونَ ﴿٣٤﴾

“Na Siku ya Kiyama hawatanusuriwa.”

Hivyo kutwezwa kwao hapa duniani pamoja na udhalili kesho Akhera, kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَهْلَكْنَاهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ ﴿٣٥﴾

“Tuliwaangamiza wala hawakuwa na msaidizi.” (47:13).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَاتَّبَعْنَاهُمْ فِي هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً

“Na Tukawafuatishia laana katika dunia hii.”

Hii ina maana kuwa Allah تعالی Ameagiza kulaaniwa wao na mfalme wao, Firauni kwa ndimi za Waumini miongoni mwa waja Wake waliokuwa wakifuata Mitume, kama vile walivyolaaniwa hapa ulimwenguni na Manabii pamoja na wafuasi wao.

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ هُمْ مِنَ الْمَقْبُوحِينَ ﴿٣٦﴾

“Na Siku ya Kiyama watakuwa miongoni mwa wanaochusha.”

Amesema Qataadah: “Aya hii ni kama ile Kauli ya Aliyetukuka:

وَأَتَّبِعُوا فِي هَذِهِ لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ بِئْسَ الرِّفْدُ الْمَرْفُودُ ﴿٣٧﴾

‘Nao wamefuatishiwa laana hapa duniani na Siku ya Kiyama. Ni mabaya yalioje watakayopewa.’ (11:99)¹

¹ Atw-Twabariy 19:583.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَِ الْأُولَىٰ بِصَآئِرٍ لِلنَّاسِ وَهُدًى
 وَرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٣٩﴾

43. Na hakika bila ya shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kwishaziangamiza kaumu za mwanzo, ili kiwafumbue macho watu, na kiwe uwongofu, na rehema, ili wapate kukumbuka."

Kubainisha Neema za Allah عليه السلام kwa Musa

Allah تعالى Anatueleza kuhusu Neema Alizomtunukia mja na Mtume Wake, Musa عليه السلام. Alimteremshia Taurati baada ya kumuangamiza Firauni na wakubwa wake. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

مِنْ بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَِ الْأُولَىٰ

"Baada ya kuziangamiza kaumu za mwanzo."

Inamaanisha kuwa baada ya kuteremshwa kwa Taurati, hakuna taifa litakalo adhibiwa kwa ujumla wao, bali waliamrisha Waumini wapigane na maadui wa Allah تعالى miongoni mwa washirikina, kama Alivyosema:

وَجَاءَ فِرْعَوْنُ وَمَنْ قَبْلَهُ وَالْمُؤْتَفِكَةُ بِالْخَاطِئَةِ ﴿٤٠﴾ فَعَصَا رَسُولَ رَبِّهِمْ فَأَخَذَهُمْ أَخَذَةً
 رَابِيَةً ﴿٤١﴾

"Na Firauni na waliomtangulia na watu wa miji iliyopinduliwa, nao walikosa. Wakawaasi Mitume wa Mola wao; ndipo Akawakamata kwa Mkamato wenye nguvu sana" (69:9-10).

بِصَآئِرٍ لِلنَّاسِ وَهُدًى وَرَحْمَةً

"Ili kiwafumbue macho watu, na uongofu na rehema...." Maana yake: Kutokana na upofu na makosa. Na uongofu kwenye haki na rehema, yaani kumuonesha amali njema.

لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾

"Ili wapate kukumbuka". Maana yake: Watu huenda wakakumbuka kwayo na kuongozwa nayo.

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْعَرَبِيِّ إِذْ قَضَيْنَا إِلَىٰ مُوسَى الْأَمْرَ وَمَا
 كُنْتَ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٤٤﴾ وَلَكِنَّا أَنْشَأْنَا قُرُونًا فَتَطَاوَلَ
 عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ ۗ وَمَا كُنْتَ ثَاوِيًّا فِي أَهْلِ مَدْيَنَ تَتْلُوا
 عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا وَلَكِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ ﴿٤٥﴾ وَمَا كُنْتَ
 بِجَانِبِ الطُّورِ إِذْ نَادَيْنَا وَلَكِنْ رَحْمَةً مِن رَّبِّكَ لِتُنذِرَ
 قَوْمًا مَّا أَتَتْهُم مِّن نَّذِيرٍ مِّن قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ
 ﴿٤٦﴾ وَلَوْلَا أَن تُصِيبَهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ
 فَيَقُولُوا رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبِعَ آيَاتِكَ
 وَتَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾ فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِن
 عِنْدِنَا قَالُوا لَوْلَا أُوتِيَ مِثْلَ مَا أُوتِيَ مُوسَىٰ ؑ أَوْلَمْ
 يَكْفُرُوا بِمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ مِن قَبْلُ ۗ قَالُوا سِحْرَانِ تَظَاهَرَا
 وَقَالُوا إِنَّا بِكُلِّ كَافِرُونَ ﴿٤٨﴾ قُلْ فَأَنَّىٰ يَكْتُبُ مِن عِنْدِ
 اللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنهُمَا أَتَّبِعُهُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٩﴾
 فَإِن لَّمْ يَسْتَجِيبُوا لَكَ فَاعْلَمْ أَنَّمَا يَتَّبِعُونَ أَهْوَاءَهُمْ ؑ
 وَمَن أَضَلُّ مِمَّنِ اتَّبَعَ هَوَاهُ بِغَيْرِ هُدًى مِّنَ اللَّهِ إِنَّ
 اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٥٠﴾ * وَلَقَدْ وَصَّلْنَا لَهُمُ
 الْقَوْلَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٥١﴾

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْعَرَبِيِّ إِذْ قَضَيْنَا
 إِلَىٰ مُوسَى الْأَمْرَ وَمَا كُنْتَ مِنَ
 الشَّاهِدِينَ ﴿٤٤﴾ وَلَكِنَّا أَنْشَأْنَا
 قُرُونًا فَتَطَاوَلَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ ۗ وَمَا
 كُنْتَ ثَاوِيًّا فِي أَهْلِ مَدْيَنَ
 تَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا وَلَكِنَّا كُنَّا
 مُرْسِلِينَ ﴿٤٥﴾ وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ
 الطُّورِ إِذْ نَادَيْنَا وَلَكِنْ رَحْمَةً مِن
 رَّبِّكَ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَتْهُم مِّن
 نَّذِيرٍ مِّن قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ
 ﴿٤٦﴾ وَلَوْلَا أَن تُصِيبَهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا
 قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ فَيَقُولُوا رَبَّنَا لَوْلَا
 أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبِعَ آيَاتِكَ
 وَتَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾

44. Wala wewe hukuwa upande wa magharibi Tulipompa Musa Amri, wala hukuwa katika waliohudhuria.

45. Lakini Sisi Tuliziumba kaumu, na ukawa mrefu umri juu yao. Wala hukuwa mkaazi wa watu wa Madyan ukiwasomea Ayah Zetu. Lakini ni Sisi Tulikuwa Tukiwatuma Mitume.

46. Wala hukuwa kando ya mlima Tuliponadi. Lakini ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi ili uwaonye watu wasiopata kufikiwa na mwonyaji kabla yako, huenda wakakumbuka.

47. Na usije kuwasibu msiba kwa iliyoyatanguliza mikono yao, wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Mbona hukututumia Mtume nasi, tukafuata Ishara Zako, na tukawa miongoni mwa Waumini?"

Tanbihi ya Ushahidi wa Unabii wa Muhammad ﷺ

Allah تعالى anatoa angalizo juu ya ushahidi wa unabii wa Muhammad ﷺ, ambaye aliwaambia wengine mambo ya kale, na kuwazungumzia kana kwamba alikuwa anawasikia na kuwaona yeye mwenyewe. Naye alikuwa ni mtu asiyeweza kusoma wala kuandika kikasomwa "Ummiy", na alikulia pamoja na kaumu yake waliokuwa hawajui chochote katika hayo. Hivyo hivyo, Allah تعالى Alimueleza kuhusu Maryam na kisa chake.

Amesema Aliyetukuka:

وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَقُولُونَ أَقْلَمَهُمْ أَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٤٤﴾

"Nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao nani kati yao atamlea Maryam, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana." (3:44).

Wewe hukuwepo wakati huo, lakini Allah تعالى Ndiye Aliyekufunulia haya. Hivyo hivyo, Alipompa habari kuhusu Nuuh عليه السلام na kaumu yake, na jinsi Alivyomuokoa Nuuh عليه السلام na Kuwagharikisha watu wake, kisha Akasema Aliyetukuka:

تِلْكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهَا إِلَيْكَ مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَا أَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ مِنْ قَبْلِ هَذَا

فَأَصْبِرْ إِنَّ الْعَقِيبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٩﴾

"Hizi ni katika habari za ghaibu Tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii. Basi subiri! Hakika mwisho ni wa wacha Mungu." (11:49)

Akasema mwisho wa Surah:

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْفَرَى نَقُصُّهُ عَلَيْكَ

“Hizi ni katika khabari za miji ambazo Tunakusimulia.” (11:100).

Hapa Akasema baada ya kuelezea kisa cha Nabii Musa عليه السلام kuanzia mwanzo mpaka mwisho na jinsi Allah تعالى Alivyomteremshia Wahyi na kuzungumza naye, Anasema Aliyetukuka:

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْغَرْبِيِّ إِذْ قَضَيْنَا إِلَىٰ مُوسَى الْأَمْرَ

“Wala wewe hukuwa upande wa magharibi Tulipompa Musa Amri.” (28:44)

Hii inamaanisha kuwa ewe Muhammad ﷺ, wewe hukuwa upande wa magharibi wa mlima ambapo Allah تعالى Alisema na Musa عليه السلام kwenye mti uliokuwa upande wa mashariki ya bonde. Allah تعالى Anaendela:

وَمَا كُنْتَ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٤٤﴾

“Wala hukuwa katika waliohudhuria.”

Wakati wa tukio hilo, lakini Allah تعالى Alikufunulia hayo ili yawe ni dalili na hoja kwa matukio yaliyotokea karne nyingi zilizopita, hivyo watu kusahau hoja za Allah تعالى kwao na Aliyoyateremsha kwa Manabii Wake wa mwanzo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا كُنْتَ ثَاوِيًّا فِي أَهْلِ مَدْيَنَ تَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا

“Wala hukuwa mkaazi wa watu wa Madyan ukiwasomea Ayah Zetu.”

Nawe hukuwa ni mwenye kuishi miongoni mwa watu wa Madyan ukisoma Aya na Ishara Zetu, pale ulipoanza kueleza juu ya Mtume Wetu, Shu'ayb عليه السلام na yale aliyoyasema kwa watu wake na jinsi walivyomjibu.

وَلَكِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ ﴿٤٥﴾

“Lakini ni Sisi Tulikuwa Tukiwatuma Mitume.” Lakini Sisi ndio Tuliokufunulia hayo na Tukakutuma kwa watu kuwa ni Mtume.

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الطُّورِ إِذْ نَادَيْنَا

“Wala hukuwa kando ya mlima Tuliponadi.”

Qataadah amesema:

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الطُّورِ إِذْ نَادَيْنَا

“Wala hukuwa kando ya mlima Tuliponadi.”

Inamaanisha Musa عليه السلام na Allah تعالى Anajua zaidi hilo, nayo inafanana na Kauli ya Aliyetukuka:

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْغَرْبِيِّ إِذْ قَضَيْنَا إِلَىٰ مُوسَى الْأَمْرَ

“Wala wewe hukuwa upande wa magharibi Tulipompa Musa Amri.”

Kisha Anatueleza hapa kwa njia nyingine mahususi kuliko hiyo nayo ni mwito, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَإِذْ نَادَىٰ رَبُّكَ مُوسَىٰ

“Na Mola wako Alipomuita Musa.” (26:10).

Akasema tena Aliyetukuka:

إِذْ نَادَاهُ رَبُّهُ بِاللَّوَادِ الْأَقْدَاسِ طُوى ﴿١٦﴾

**“Mola Wake Alipomwita katika bonde takatifu la Twuwaa.”
(79: 16)**

Akasema tena:

وَنَدَيْنَاهُ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ الْأَيْمَنِ وَقَرَّبْنَاهُ نَجِيًّا ﴿٥٢﴾

**“Na Tulimwita upande wa kulia wa mlima na Tukamsogeza
kunong’ona naye.” (19: 52).**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَكِن رَّحْمَةً مِّن رَّبِّكَ

“Lakini ni Rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi.”

Maana yake: Wewe hukuwepo wala hukushuhudia chochote katika hayo, lakini Allah تعالى Ndiye Aliyekufunulia na Kukueleza kuhusu wao kama Rehema kutoka Kwake, kwako wewe na waja Wake, kwa kukutuma wewe kwao.

لَتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَتْهُم مِّن نَّذِيرٍ مِّن قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٤٤﴾

“Ili uwaonye watu wasiopata kufikiwa na mwonyaji kabla yako, huenda wakakumbuka.”

Hii inamaanisha kuwa huenda wao wakaongoka kwa uliyokuja nayo kutoka kwa Allah تعالى.

وَلَوْلَا أَن تُصِيبَهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ فَيَقُولُوا رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا

“Na usije kuwasibu msiba kwa iliyoyatanguliza mikono yao, wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Mbona nasi hukututumia Mtume.”

Hakika Sisi Tumekutuma kwao ili wasimamishiwe hoja dhidi yao, na hivyo kuondoka udhuru pale adhabu ya Allah تعالى itakapoteremka kwa sababu ya kufuru zao. Ili wakati huo wasiwe na hoja kuwa hatukuletewa Mtume wala mwonyaji, kama alivyosema Aliyetukuka baada ya Kuteremsha Kitabu Chake Kitukufu, Qur’ani:

أَن تَقُولُوا إِنَّمَا أُنزِلَ الْكِتَابُ عَلَي طَائِفَتَيْنِ مِن قَبْلِنَا وَإِن كُنَّا عَن دِرَاسَتِهِمْ لَغَنِيْلِينَ ﴿٤٥﴾
أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْكِتَابُ لَكُنَّا أَهْدَىٰ مِنْهُمْ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ

“Msije mkasema: ‘Hakika mataifa mawili kabla yetu yameteremshiwa Kitabu; na sisi tulikuwa hatuna khabari ya waliyokuwa wakiyasoma’. Au mkasema: ‘Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na Uwongofu na Rehema.”
(6:156-157).

Na Allah تعالى Amesema,

رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لَعَلَّ يُكُونُ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ

“Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Allah baada ya kuletwa Mitume.” (4:165).

يَتَأْهَلُ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ عَلَىٰ فِتْرَةٍ مِّنَ الرُّسُلِ أَنْ تَقُولُوا مَا جَاءَنَا مِن بَشِيرٍ وَلَا نَذِيرٍ ۗ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَشِيرٌ وَنَذِيرٌ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٩﴾

“Enyi watu wa Kitabu! Bila ya shaka amekujilieni Mtume Wetu akikubainishieni katika wakati usiokuwa na Mitume, msije mkasema: ‘Hakufika kwetu mbashiri wala mwonyaji. Na Mwenyezi Mungu anao uweza wa kila kitu.’ (5:19).

Na Aya katika jambo hili ni nyingi sana.

فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا لَوْلَا أُوتِيَٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَٰ مُوسَىٰ ۗ أَوَلَمْ يَكْفُرُوا بِمَا أُوتِيَٰ مُوسَىٰ مِنْ قَبْلُ ۗ قَالُوا سِحْرَانِ تَظَاهَرَا وَقَالُوا إِنَّا بِكُلِّ كَافِرُونَ ﴿٢٠﴾ قُلْ فَأْتُوا بِكِتَابٍ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنْهُمَا أَتَّبِعُهُ ۖ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢١﴾ فَإِنْ لَّمْ يَسْتَجِيبُوا لَكَ فَاعْلَمْ أَنَّمَا يَتَّبِعُونَ أَهْوَاءَهُمْ ۗ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنِ اتَّبَعَ هَوَاهُ بِغَيْرِ هُدًى مِّنَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٢﴾ * وَلَقَدْ وَصَّلْنَا لَهُمُ الْقَوْلَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٣﴾

48. Ilipowajia haki kutoka Kwetu walisema: Mbona hakupewa kama aliyopewa Musa? Je! Kwani wao hawakuyakataa aliyopewa Musa zamani? Walisema: Ni wachawi wawili wanasaidiana. Na wakasema: Hakika sisi tunawakataa wote.

49. Sema: Basi leteni Kitabu kinachotoka kwa Allah chenye kuongoka zaidi kuliko hivi viwili tukifuata, kama nyinyi mnasema kweli.

50. Na ikiwa hawakuitikii, basi jua kuwa wanafuata pumbao lao tu. Na nani aliyepotea zaidi kumshinda anayefuata pumbao lake bila ya uwongofu utokao kwa Allah. Hakika Allah Hawaongoi watu wenye kudhulumu.

51. Na sasa kwa yakini Tumewafikishia Neno ili wapate kukumbuka.

Ukaidi wa Makafiri na Kujibiwa Kwao

Allah تعالى Anatueleza kuwa lau wataadhibiwa watu kabla ya kuletewa hoja dhidi yao, watatumia udhuru kuwa hakuna Mtume aliyewajia, lakini ukweli ulipokuja kwao kupitia kwa Mtume Muhammad ﷺ kwa ukaidi wao, inadi, kufuru, ujinga wao walisema:

لَوْلَا أُوتِيَ مِثْلَ مَا أُوتِيَ مُوسَىٰ

“Mbona hakupewa kama aliyopewa Musa?”

Wakimaanisha – na Allah تعالى Anajua zaidi – miujiza mingi kama fimbo, mkono, tufani, nzige, chawa, vyura, damu, upungufu wa mazao na matunda – hivyo kuwaletea dhiki maadui wa Allah تعالى. Pia kupasuliwa bahari, kuletewa kivuli na mawingu (mawingu yaliokuwa yakiwafuata wana wa Israili katika jangwa), kuteremshwa kwa manna na salwa, na Ishara nyingine za wazi na dalili za uhakika. Miujiza ambayo Allah تعالى Aliipitisha Mikononi mwa Musa عليه السلام kama dalili na hoja kwa Firauni na wakubwa wake na wana wa Israili.

Hayo yote hayakuwa na athari yoyote kwa Firauni na wakubwa wake; bali walimkufuru Musa عليه السلام na nduguye Haaruun عليه السلام, kama Alivyowaambia:

أَجَعَلْنَا لَتَلْفَتْنَا عَمَّا وَجَدْنَا عَلَيْهِ ءَابَاءَنَا وَتَكُونَ لَكُمْ ءَالِكِبْرِيَاءُ فِي الْأَرْضِ وَمَا حُنُّ لَكُمْ

بِمُؤْمِنِينَ ﴿٧٨﴾

“Je, umekuja ili utuachishe tuliyouwakuta nayo baba zetu, na mpate nyinyi wawili ukubwa katika nchi? Wala sisi hatukuaminini nyinyi” (10:78).

Amesema tena تعالى:

فَكَذَّبُوهُمَا فَكَانُوا مِنَ الْمُهْلَكِينَ ﴿٤٨﴾

“Basi wakawakanusha, na wakawa miongoni mwa walioa-ngamizwa” (23: 48).

Wakaidi hawaamini Miujiza

Kwa hiyo akasema Allah تعالى:

أَوَلَمْ يَكْفُرُوا بِمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ مِنْ قَبْلُ

“Je! Kwani wao hawakuyakataa aliyopewa Musa zamani?”

Je, wanaadamu hawakukanusha aliyokuja nayo Musa عليه السلام pamoja na hizo ishara kubwa?

قَالُوا سِحْرَانِ تَظَاهَرَا

“Walisema: Ni wachawi wawili wanasaidiana.”

Yaani: Wanashirikiana.

وَقَالُوا إِنَّا بِكُلِّ كَافِرُونَ ﴿٤٩﴾

“Na wakasema: Hakika sisi tunawakataa wote.”

Kumaanisha tumemkanusha kila mmoja wao, kwa sababu ya usuhuba na uhusiano wa karibu baina ya Musa na Haaruun, kutajwa kwa mmoja wao kunamchanganya mwenziwe.

Kuwazulia Uwongo kuwa Musa عليه السلام na Haaruun عليه السلام ni Wachawi

Amesema Mujaahid ibn Jabr: “Mayahudi waliwaambia Maquraysh waseme haya kwa Muhammad ﷺ. Allah تعالى Akasema: ‘Je! Kwani wao hawakuyakataa aliyopewa Musa zamani?’ Wakasema:

تَظَاهَرَا

“...wanasaidiana...”

Akasema: ‘Hii inamaanisha Musa na Haaruun, wanasaidiana’, yaani wanashirikiana, mmoja kumuunga mwenziwe.”¹ Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Sa’iid

¹ Atw-Twabariy 19:588.

ibn Jubayr na Abu Raazin kuwa ibara: “Wachawi wawili”, wakimaanisha Musa عليه السلام na Haaruun عليه السلام¹. Na hii ni kauli nzuri yenye nguvu. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Jawabu dhidi ya uzushi

Ama kwa anayesoma:

تَظَاهَرَا

“Wanasaidiana.”

Imepokewa kwa ‘Aliy ibn Abi Twalhah na al-‘Awfiy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hii inamaanisha Tawrati na Qur’ani”². Hii ni kuwa amesema baada yake:

قُلْ فَأَتُوا بِكِتَابٍ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنْهُمَا أَتَّبِعُهُ

“Sema: Basi leteni Kitabu kinachotoka kwa Allah chenye kuongoka zaidi kuliko hivi viwili tukifuate.”

Mara nyingi Allah تعالى Anavitaja vitabu hivi viwili, Tawrati na Qur’ani pamoja, kama katika Kauli Yake Aliyetukuka:

قُلْ مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَىٰ نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ ﴿٥١﴾

“Sema: Nani aliyeteremsha Kitabu alichokuja nacho Musa, chenye nuru na uwongofu kwa watu.” Mpaka Aliposema:

وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مَبَارَكٌ

“Na hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa.” (6:91-92).

Akasema mwisho wa Surah hiyo:

نُورًا آتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتَابَ تَمَامًا عَلَىٰ الَّذِي أَحْسَنَ

“Kisha Tulimpa Musa Kitabu kwa kumtimizia Neema aliyefanya wema.” (6:154).

¹ At-Tabari 19:598.

² At-Tabari 19:589.

Akasema tena:

وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مَبْرُورًا فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٥٤﴾

“Na hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa. Basi kifuateni, na mcheni mungu ili mrehemewe.” (6:155).

Majini walisema:

إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أَنْزَلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَىٰ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“Hakika tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake.” (46:30).

Amesema Waraqah ibn Nawfal: “Huyu ni an-Namus¹, ambaye alikuja kwa Musa عليه السلام. Wale wenye ujuzi wanajua hata bila ya kufikiria kuwa miongoni mwa Vitabu vingi ambavyo Allah تعالى Ameviteremsha kwa Mitume Yake, hakuna Kitabu kilichokamilika, fasaha zaidi, kitukufu na adhimu kuliko kile Kitabu alichoteremshiwa Muhammad ﷺ, nayo ni Qur’ani. Na baada yake kwa utukufu, hadhi na ukubwa ni kile Kitabu alichoteremshiwa Musa ibn ‘Imraan عليه السلام, nacho ni Kitabu ambacho Allah تعالى Amesema:

إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ تَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا
وَالرَّبَّانِيُّونَ وَالْأَحْبَارُ بِمَا اسْتُحْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ

“Hakika Sisi Tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii walionyenyeka Kiislamu, na wachamungu, na wanazuoni waliwahukumu Mayahudi; kwani walikabidhiwa kukihifadhi Kitabu cha Allah. Nao wakawa ni mashahidi juu yake.” (5:44).

Injili iliteremshwa kutimiza Taurati, na kuhalalisha baadhi ya vitu ambavyo vilikuwa vimeharamishwa kwa wana wa Israili.

¹ Maana yake: Jibrili.

Kwa hivyo Akasema Aliyetukuka:

قُلْ فَأَتُوا بِكِتَابٍ مِّنْ عِندِ اللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنْهُمَا أَتَّبَعُهُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٨﴾

“Sema: Basi leteni Kitabu kinachotoka kwa Allah chenye kuongoka zaidi tukifuate, kama nyinyi mnasema kweli.”

Maana yake: katika juhudi zenu za kukanusha haki kwa hoja za batili.

Upotevu wa Wenye Kufuata Matamaniao

Allah تعالى Amesema:

فَإِنْ لَّمْ يَسْتَجِيبُوا لَكَ

“Na ikiwa hawakuitikii.”

Ikiwa hawatakujibu uliyowaambia, na hawafuati haki.

فَاعَلِمْنَا أَنَّهُمْ شَاكِرُونَ ﴿٢٩﴾

“Basi jua kuwa wanafuata pumbao lao tu.”

Bila ya dalili wala hoja yoyote. Anasema Aliyetukuka:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنِ اتَّبَعَ هَوَاهُ بَعْدَ إِسْرَائِيلَ ۗ فَكُلَّمَا نَزَّلْنَا آيَةً مِّنْ آيَاتِنَا إِذْ هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٣٠﴾

“Na nani aliyepotea zaidi kumshinda anayefuata pumbao lake bila ya uwongofu utokao kwa Allah.”

Maana yake: Bila ya hoja iliyochukuliwa kutoka kwenye Kitabu cha Allah تعالى.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٣١﴾

“Hakika Allah Hawaongoi watu wenye kudhulumu.”

وَلَقَدْ وَصَّلْنَا لَهُمُ الْقَوْلَ

“Na sasa kwa yakini Tumewafikishia Neno.”

Amesema Mujaahid: "Tumewaelezea hili Neno kwao"¹. Amesema as- Suddiy: "Wamebainishiwa wao neno."² Amesema Qataadah: "Amesema Aliyetukuka: 'Amewaambia waliyofanyiwa waliopita na Atakachofanya katika siku za mbele."

لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٨﴾

*"ili wapate kukumbuka."*³

Mujaahid na wengineo wamesema:

وَلَقَدْ وَصَّلْنَا

"Tumewafikishia."

Maana yake: Maquraysh."⁴

* * *

¹ At-Tabari 19:593.

² Ibn Abi Haatim 9:2987.

³ At-Tabari 19:593.

⁴ At-Tabari 19:594.

الَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾
 وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَامَنَّا بِهِ إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا
 مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿٥٣﴾ أُولَٰئِكَ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ بِمَا
 صَبَرُوا وَيَدْرُءُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ
 يُنفِقُونَ ﴿٥٤﴾ وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ وَقَالُوا
 لَنَّا أَعْمَلُنَا وَلَكُنَّا أَعْمَلُكُمْ سَلَمٌ عَلَيْكُمْ لَا نَبْتَغِي الْجَاهِلِينَ
 ﴿٥٥﴾ إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ
 يَشَاءُ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٥٦﴾ وَقَالُوا إِن نَّبْتَغِ
 أَهْدَىٰ مَعَكَ نُتَخَطَّفَ مِنْ أَرْضِنَا ۗ أَوَلَمْ نُمَكِّنْ لَهُمْ حَرَمًا
 ءَامِنًا يُحْيِي إِلَيْهِ نَمَرَاتٍ كُلِّ شَيْءٍ رِزْقًا مِنْ لَدُنَّا وَلَكِنَّ
 أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾ وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَرِيْبِهِ
 بَطَرْتَ مَعِيشتَهَا ۗ فَتِلْكَ مَسْكِنُهُمْ لَمَّا نُسَّكُن مِنْ بَعْدِهِمْ
 إِلَّا قَلِيلًا ۗ وَكُنَّا نَحْنُ الْوَارِثِينَ ﴿٥٨﴾ وَمَا كَانَ رَبُّكَ
 مُهْلِكَ الْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِي أُمَمَةٍ رَسُولًا يَتْلُوا عَلَيْهِمْ
 ءَايَاتِنَا ۗ وَمَا كُنَّا مُهْلِكِي الْقُرَىٰ ۗ إِلَّا وَأَهْلُهَا ظَالِمُونَ ﴿٥٩﴾
 وَمَا أَوْثَيْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّعَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا وَزَيَّنَّهَا ۗ
 وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٠﴾ أَفَمَنْ وَعَدْنَاهُ
 وَعَدًّا حَسَنًا فَهُوَ لَنَقِيْهِ كَمَنْ مَتَّعْنَاهُ مَتَّعَةً مِّنَعِ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا
 ثُمَّ هُوَ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ مِنَ الْمُحْضَرِينَ ﴿٦١﴾

الَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِ
 هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾ وَإِذَا يُتْلَىٰ
 عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَامَنَّا بِهِ إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
 رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿٥٣﴾
 أُولَٰئِكَ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ بِمَا
 صَبَرُوا وَيَدْرُءُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ
 وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٥٤﴾ وَإِذَا
 سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ وَقَالُوا لَنَّا
 أَعْمَلُنَا وَلَكُنَّا أَعْمَلُكُمْ سَلَمٌ عَلَيْكُمْ لَا
 نَبْتَغِي الْجَاهِلِينَ ﴿٥٥﴾

52. Wale Tuliowapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki.

53. Na wanaposomewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyekela.

54. Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyovumilia, na waka-ondoa ubaya kwa wema, na wakatoa katika Tuliyo-waruzuku.

55. Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao na husema: Sisi tuna vitendo vyetu, na nyinyi mna vitendo vyenu. Salamun Alaikum, Amani juu yenu! Sisi hatutaki kujibizana na wajinga.”

Waumini Miongoni mwa Watu wa Kitabu

Allah تعالى Anatueleza kuwa wanazuoni wema miongoni mwa Watu wa Kitabu wanaamini Qur’ani, kama Alivyosema Aliyetukuka:

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِمْ أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ

“Wale Tuliowapa Kitabu, wakakisoma¹ kama ipasavyo kusomwa, hao ndio kweli wanakiamini.” (2:121).

Na Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَشَعِينَ لِلَّهِ

“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanaomuamini Allah na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, wakimnyenyekea Allah.” (3:199).

Na Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِمْ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٧﴾ وَيَقُولُونَ

سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنْ كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٨﴾

“Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa hii, huanguka kifudufudi wanasujudu. Na wanasema: Subhaana Rabbinaa, Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika ahadi ya Mola wetu mlezi ni lazima itimizwe!.” (17:107-108).

Na Allah تعالى Amesema,

¹ Angalia mjeledi wa kwanza wa tafsir *Surat Al-Baqarah* (2:121) katika maelezo ya aya hii.

وَلْتَجِدْنَ أَقْرَبَهُمْ مَوَدَّةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصْرِي

“Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanaosema: Sisi ni Manaswara.”

Mpaka Kauli Yake:

فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٥٨﴾

“Basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia.” (5:82-83).

Amesema Sa'iid ibn Jubayr: “Hii iliteremshwa kwa makasisi sabini waliotumwa na mfalme Najaashi (mfalme wa Ethiopia). Walipokuja kwa Mtume ﷺ aliwasomea:

يَسَّ ۝ وَالْقُرْءَانَ الْحَكِيمِ ﴿٣٦﴾

‘Yaa Siin. Naapa kwa hii Qur’ani yenye kutengenezwa vizuri.’ (36:1-2)

Mpaka alipoimaliza kuisoma Surah yote. Makasisi walianza kulia, na wote walisilimu. Aya hizi nyingine ziliteremshwa kwao.”¹

الَّذِينَ ءَانَيْنَهُمُ اَلْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٧﴾ وَاِذَا يُتْلٰٓى عَلَيْهِمْ قَالُوْا ءَاْمَنَّا بِهٖ

۝ اِنَّهٗ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّنَا اِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِيْنَ ﴿٥٨﴾

“Wale Tuliowapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki. Na wanaposomewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyekoa.”

Hii inamaanisha kuwa kabla ya Qur’ani hii sisi tayari tulikuwa Waislamu, yaani tulimuamini Mwenyezi Mungu Mmoja Peke Yake, tukimtakasia Dini Yake na kufuata Amri Zake. Amesema Allah تعالی:

اُولٰٓئِكَ يُؤْتَوْنَ اَجْرَهُمْ مَّرَّتَيْنِ بِمَا صَبَرُوْا

“Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyovumilia.”

¹ Ibn Abi Haatim 9:2988.

Wale wenye sifa hizi, ambao waliamini Kitabu cha mbeleni (awali), kisha hiki cha pili (watapewa ujira wao mara mbili kwa kumuamini Mtume wa kwanza, kisha na wa pili). Kwa hiyo Akasema:

بِمَا صَبَرُوا

“Kwa walivyovumilia.”

katika kufuata haki, kwani kuchukua kitu mfano huu si rahisi katika nafsi. Imenukuliwa katika Hadithi Sahihi ya ‘Aamir ash-Sha’biy toka kwa Abu Burdah kuwa Abu Musa Al-Ash’ariy رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«ثَلَاثَةٌ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ: رَجُلٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ آمَنَ بِنَبِيِّهِ ثُمَّ آمَنَ بِي، وَعَبْدٌ مَمْلُوكٌ أَدَّى حَقَّ اللَّهِ وَحَقَّ مَوْلَاهُ، وَرَجُلٌ كَانَتْ لَهُ أُمَةٌ، فَأَدَّبَهَا فَأَحْسَنَ تَأْدِيبَهَا، ثُمَّ أَعْتَقَهَا فَتَرَوَّجَهَا»

“Watu wa tatu watapewa ujira wao mara mbili: Mtu miongoni mwa Watu wa Kitabu aliyemuamini Nabii wake na kisha akaniamini mimi, mtumwa anayetetekeleza haki za Allah na haki za bwana wake, na mtu aliyekuwa na kijakazi, akampatia adabu nzuri, kisha akamuacha huru na kumuoa.”¹

Amepokea Imamu Ahmad kuwa Abu Umaamah رضي الله عنه amesema: Nilikuwa natembea pamoja na Mtume ﷺ akiwa amepanda siku ya kukombolewa Makkah, akasema maneno mazuri. Na miongoni mwayo akasema:

«مَنْ أَسْلَمَ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِينَ فَلَهُ أَجْرُهُ مَرَّتَيْنِ وَلَهُ مَا لَنَا وَعَلَيْهِ مَا عَلَيْنَا وَمَنْ أَسْلَمَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ فَلَهُ أَجْرُهُ وَلَهُ مَا لَنَا وَعَلَيْهِ مَا عَلَيْنَا»

“Yeyote anayesilimu miongoni mwa watu wa Vitabu viwili, atapata ujira mara mbili, na ana haki na majukumu sawa kama sisi. Yeyote anayesilimu miongoni mwa washirikina atakuwa na ujira mmoja tu, naye ana haki na majukumu sawa na yetu.”²

¹ Fat’h al-Baariy 1:229.

² Ahmad 5:259.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَيَذَرُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ

“Na wakaondoa ubaya kwa wema.”

Wao hawalipizi baya kwa baya mfano wake, bali husamehe na kuachilia mbali (kupuuza yaliyopita). Anamalizia Aya hii Aliyetukuka:

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٥٢﴾

“Na wakatoa katika Tuliowaruzuku.”

Maana yake: Kwa yale Tuliowaruzuku ya halali wanatoa kutekeleza wajibu kwa kuwapa viumbe wa Allah تعالى kwa familia zao na jamaa wa karibu. Pia wanatoa Zakah ya Faradhi na ile yenye kupendeza kwa mambo ya ziada na sadaka na yenye kumkaribisha kwa Allah تعالى . Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ

“Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao.”

Wao hawatangamani na watu hao wenye mazungumzo hayo ya upuuzi, bali wao huwa kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٥٣﴾

“Na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa hishima yao.” (25:72)

Pia amesema:

وَقَالُوا لَنَا أَعْمَلْنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ سَلَمٌ عَلَيْكُمْ لَا نَبْتَغِي الْجَاهِلِينَ ﴿٥٤﴾

“Na husema: Sisi tuna vitendo vyetu, na nyinyi mna vitendo vyenu. Salamun Alaikum, Amani juu yenu! Sisi hatutaki kujibizana na wajinga.”

Mjinga anapomsemesha ujinga wake na kumwambia lisilostahiki kujibiwa, wao hupa nyongo wala hawajibu maneno machafu mfano wao. Hawasemi chochote ila maneno mema na mazuri. Kwa hiyo Allah تعالى Anasema kuhusu wao:

لَنَا أَعْمَلْنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ لَا تَبْتَغِي الْجَاهِلِينَ ﴿٥٦﴾

“Sisi tuna vitendo vyetu, na nyinyi mna vitendo vyenu. Salamun Alaikum, Amani juu yenu! Sisi hatutaki kujibizana na wajinga.”

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَئِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٥٧﴾
 وَقَالُوا إِن نَّتَّبِعِ أَهْدَىٰ مَعَكَ تُنْخَطِفُ مِنَ الْأَرْضِ نَفَاثَةً أُولَٰئِكَ لَئِمَّةٌ كَارِهِمُ الْكَارِهُنَّ أَتَمَنَّا بِمُنَاجَاةِ إِلَٰهِهِ
 ثُمَّ تَرْتِكُ كُلَّ شَيْءٍ رِّزْقًا مِّن لَّدُنَّا وَلَئِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٨﴾

56. Kwa hakika wewe humwongoi umpendaye, lakini Allah Humwongoa Amtakaye. Na Yeye Ndiye Anawajua zaidi waongokao.

57. Na wakasema: Tukiufuata uwongofu huu pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu. Je! Kwani Sisi Hatukuwaweka imara katika pahala patakatifu, penye amani, ambapo huletewa matunda ya kila aina kuwa ni riziki itokayo Kwetu? Lakini wengi wao hawajui”.

Allah تعالیٰ Humuongoa Amtakaye

Allah تعالیٰ Anamwambia Mtume Wake:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

“Kwa hakika wewe, ewe Muhammad, “Humuongoi umpendaye.”

Maana yake: Huna uwezo wa hilo, kwani ni juu yako kufikisha ujumbe na Allah تعالیٰ Ndiye Mwenye Kumuongoa Amtakaye.

Naye Ana Hekima ya juu na Kamili na Hoja za uhakika, kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿ لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ﴾

“Si juu yako kuwaongoa; lakini Allah Humwongoa Amtakaye...” (2:272).

Amesema tena Aliyetukuka:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

“Na wengi katika watu hawatakuwa wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.” (12:103).

Aya hii ni mahsusi zaidi kuliko hizo tulizozitaja zote. Hakika Amesema Aliyetukuka:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٠٤﴾

“Kwa hakika wewe humwongoi umpendaye, lakini Allah Humwongoa Amtakaye. Na Yeye Ndiye Anawajua zaidi waongokao”.

Yeye, Allah تعالى Ndiye Mwenye Kujua anayestahiki uwongofu na anayestahiki kupotea. Hakika imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Aya hii imeteremshwa kwa Abu Twaalib, ami yake Mtume ﷺ ambaye alikuwa akimsaidia, akimlinda na kumuhifadhi. Alikuwa anampenda Mtume sana, lakini haya yalikuwa ni mahaba ya kimaumbile, wala sio ya kisheria (kuwa Muhammad ni Mtume ﷺ). Alipofikiwa na mauti na wakati wake ukafika, Mtume ﷺ alimlingania katika Imani na aingie katika Uislamu, lakini Qadari ilimpita, hivyo kubaki katika aliyokuwa nayo, mfuasi wa ukafiri, na Allah تعالى Ndiye Mwenye Hekima iliyotimia. Amesema az-Zuhriy: Amenihadithia Sa'iid ibn al-Musayyib kuwa baba yake, al-Musayyib ibn Hazan al-Makhzuumiy alisema: “Alipojiwa Abu Twaalib na mauti, Mtume ﷺ alikuja kwake na kumkuta Abu Jahl ibn Hisham na ‘Abdullah ibn Abi Umayyah ibn al- Mughhiarah pamoja naye. Akasema Mtume ﷺ:

«يَا عَمَّ قُلْ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، كَلِمَةً أَحَاجُّ لَكَ بِهَا عِنْدَ اللَّهِ»

“Ewe ami yangu! Sema Laa ilaaha illa Llahu, neno ambalo naweza kukutetea nalo mbele ya Allah.”

Hapo akasema Abu Jahl na ‘Abdullah ibn Abi Umayyah: “Ewe Abu Twaalib! Je, utaacha na kukengeuka mila ya ‘Abdul-Mutwtwalib?” Mtume ﷺ alimkazania na kumhimiza aseme *Laa ilaaha illa Llahu*, nao waliendelea kumwambia: “Je, utaacha na kukengeuka mila ya ‘Abdul-Mutwtwalib?” Mpaka mwisho kabisa alisema kwa wazi kabisa kuwa yeye yuko katika mila ya ‘Abdul-Mutwtwalib

na akakataa katakata kusema *Laa ilaaha illa Llahu*. Hapo akasema Mtume ﷺ:

«وَاللّٰهُ لَا يَسْتَغْفِرُ لَكَ مَا لَمْ أَنَّهُ عَنكَ»

“Wallahi, nitaendelea kukuombea msamaha maadamu sijakatazwa kuhusu wewe (kukufanyia hivyo).”

Kisha Allah Akateremsha:

مَا كَانَتْ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولَىٰ قُرْبَىٰ

“Haimpasii Mtume na wale walioamini kuwatakia msamaha washirikina ijapokuwa ni jamaa zao.” (9:113).

Ikateremshwa kuhusiana na Abu Twaalib:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

“Kwa hakika wewe humwongoi umpendaye, lakini Allah Humwongoa Amtakaye.”

Imepokewa na (al-Bukhaariy na Muslim) kutoka kwa Hadithi ya az-Zuhriy.¹

Udhuru wa Watu wa Makkah Kutoamini na Kujibiwa Kwao

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقَالُوا إِن نَّتَّبِعِ الْهُدَىٰ مَعَكَ تَتَخَطَّفَ مِنَّا أَرْضُنَا

“Na wakasema: Tukiufuata uwongofu huu pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu.”

Allah تعالى Anasema kuhusu nyudhuru za baadhi ya makafiri kwa kutofuata uwongofu. Walimwambia Mtume ﷺ:

إِن نَّتَّبِعِ الْهُدَىٰ مَعَكَ تَتَخَطَّفَ مِنَّا أَرْضُنَا

“Tukiufuata uwongofu huu pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu.”

¹ Fat'h al-Baariy 8:365 na Muslim 1:54.

Tunahofia kuwa lau tutakufuata wewe kwa uliyokuja nayo katika uwongofu na tukaenda kinyume na makabila ya Waarabu washirikina waliotuzunguka, watajaribu kutudhuru na kupigana nasi (dhidi yetu) na kutunyakua popote tutakapokuwa. Allah تعالى Anasema Kuwajibu:

أَوْلَمْ نُمَكِّنْ لَهُمْ حَرَمًا آمِنًا

“Je! Kwani Sisi Hatukuwaweka imara katika pahala patakatifu.”

Udhuru huu waliotoa ni uwongo na batili, kwani Allah تعالى Amewajaalia kuwa katika mji wa amani na usalama na ni mahali adhimu patakatifu, ambapo pamekuwa na amani kuanzia ilipojengwa Al-kaaba. Vipi mahali hapo panaweza kuwa na amani na usalama wakati wa ukafiri wao na ushirikina wao, na hapatakuwa na amani hiyo wanapasilimu na kufuata haki?

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

يُجِيبُ إِلَيْهِ تَمَرَاتُ كُلِّ شَيْءٍ

“Wao huletewa matunda ya kila aina.”

Maana yake: Aina zote za matunda kutoka maeneo ya karibu, Taif na sehemu nyinginezo. Hivyo hivyo, watu wa Makkah walikuwa wanafanya biashara na bidhaa nyingine zilikuwa zikija katika mji wao.

رِزْقًا مِّنْ لَّدُنَّا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Kuwa ni riziki itokayo Kwetu? Lakini wengi wao hawajui?”

Hii ndio sababu wakasema waliyosema.

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِن قَرْيَةٍ بَطَرَتْ مَعِيشَتَهَا فَتِلْكَ مَسْجِدُهُمْ لَمَّا تَشْكَنُ مِنْ بَعْدِهِمْ إِلَّا قَلِيلًا ۗ وَكُنَّا نَحْنُ الْوَارِثِينَ ﴿٥٨﴾ وَمَا كَانَ رُبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِي أُمِّهَا رَسُولًا يَتْلُوا عَلَيْهِمْ ؕ أَيْنِمَّا ؕ وَمَا كُنَّا مُهْلِكِي الْقُرَىٰ إِلَّا وَأَهْلُهَا ظَالِمُونَ ﴿٥٩﴾

58. “Na miji mingapi iliyojifakharisha Tumeiangamiza! Na hayo maskani yao hayakukaliwa tena baada yao, ila kwa uchache tu. Na Sisi ndio Tumekuwa warithi wao.”

59. Na Mola wako Mlezi Haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika miji yake mikuu awesomee Ishara Zetu. Wala Hatuiangamizi miji mpaka watu wake wawe madhalimu.

Kuangamizwa Miji Baada ya Kusimamishiwa Hoja

Aliyetukuka Amesema kuhusu watu wa Makkah katika Kauli Yake:

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَرْيَةٍ بَطَرَتْ مَعِيشَتَهَا

“Na miji mingapi iliyojifakharisha Tumeiangamiza!”

Hakika ni kuwa walivuka mipaka na kiburi, wakakanusha Neema ya Allah تعالى kwa neema nyingi Alizowaneemesha miongoni mwa hizo ni riziki. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ ءَامِنَةً مُطْمَئِنَّةً يَأْتِيهَا رِزْقُهَا رَغَدًا مِنْ كُلِّ مَكَانٍ

“Na Allah Anakupigieni mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiujia kwa wingi kutoka kila mahali” – mpaka:

فَأَخَذَهُمُ الْعَذَابُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١١٣﴾

“Basi adhabu iliwafikia, hali ya kuwa wenyewe wamejidhulumu.” (16:112-113).

Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

فَتِلْكَ مَسْجِدُهُمْ لَمَّا تَشْكَنُ مِنْ بَعْدِهِمْ إِلَّا قَلِيلًا ۗ

“Na hayo maskani yao hayakukaliwa tena baada yao, ila kwa uchache tu.”

Nyumba zao zilibaki tupu (baada ya kuangamizwa) na huoni chochote isipokuwa makazi yao. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَكُنَّا هُنَّ أَوْلَٰرِثِينَ ﴿١١٤﴾

“Na Sisi ndio Tumekuwa warithi wao.”

Miji yao hiyo ikawa magofu isiyokuwa na mtu yeyote. Kisha Alisema Aliyetukuka Akieleza Uadilifu Wake, na kwamba Yeye Hamuangamizi yeyote kwa kumdhulumu; hakika ni kuwa Yeye Huwaangamiza wale Anaowaangamiza baada ya Kuwasimamishia hoja dhidi yao. Hivyo Anasema:

وَمَا كَانَ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِي أُمِّهَا

“Na Mola wako Mlezi Haangamizi miji mpaka ampeleke katika miji yake mikuu”.

Nao ni mji wa Makkah.

رَسُولًا يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا

“Mtume awesomee Ishara Zetu.”

Hii ni dalili kuwa Nabii asiyeweza kusoma wala kuandika kikasomwa “Ummiy”, Muhammad ﷺ alitumwa kutoka kwa Mama wa miji kama Mtume kwa miji yote, kwa Waarabu na Waajemi (wasiokuwa Waarabu), kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا

“Na ili uwaonye watu wa Mama wa miji na watu walio pembezoni mwake.” (6:92)

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyinyi nyote.” (7:158).

Amesema tena:

لِأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“Ili kwa hiyo nikuonyeni na kila imfikiayo.” (6:19).

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَأَلْنَا زُ مَوْعِدُهُ

“Na atakayemkataa katika makundi, basi Moto ndio mahali pa miadi yao.” (11:17).

Na ushahidi timilifu ni Kauli Yake Aliyetukuka,

وَإِنَّ مِنْ قَرِيْبَةٍ إِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوْهَا قَبْلَ يَوْمِ أَلْقِيْمَةِ أَوْ مُعَذِّبُوْهَا عَذَابًا شَدِيْدًا ۗ

“Na hakutakuwa mji wowote ila Sisi Tutauhilikisha kabla ya Siku ya Kiyama au Tutauadhibu adhabu kali.” (17:58)

Allah تعالیٰ Anatueleza kuwa Atuangamiza kila mji kabla Siku ya Kiyama. Hakika Amesema Aliyetukuka:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِيْنَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُوْلًا ﴿٥٨﴾

“Na Sisi si wenye Kuadhibu mpaka Tupeleke Mtume.” (17:15).

Allah تعالیٰ Akafanya utume wa Nabii Mtume asiyeweza kusoma wala kuandika kikasomwa “Ummiy” kwa miji yote, kwa sababu yeye ametumwa kwa Mama wa miji, asili yao ambayo wote wanarudi kwayo. Imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

بُعِثْتُ إِلَى الْأَحْمَرِ وَالْأَسْوَدِ

“Hakika nimetumwa kwa wekundu na weusi.”¹

Kwa ajili hii Amehitimisha kwake unabii, hakuna Nabii baada yake, bali sheria yake itabaki muda wa kubaki usiku na mchana mpaka Siku ya Kiyama.

وَمَا أَوْتِيْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّعُ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا وَرَبِّتْنٰهَا ۗ وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ۗ أَفَلَا

تَعْقِلُوْنَ ﴿٦٠﴾ أَفَمَنْ وَعَدْنَاهُ وَعَدًا حَسَنًا فَهُوَ لَاقِيْهِ كَمَنْ مَّتَّعْنَاهُ مَتَّعْنَاهُ مَتَّعَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ثُمَّ

هُوَ يَوْمَ أَلْقِيْمَةِ مِنَ الْمُحْضَرِيْنَ ﴿٦١﴾

60. “Na chochote mlishopewa ni matumizi ya maisha ya dunia na pambo lake. Na yaliyoko kwa Allah ndio bora na yatakayobaki zaidi. Basi je, hamfahamu?”

61. Je! Yule Tuliye muahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama Tuliye mstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, na kisha Siku ya Kiyama akawa miongoni mwa wanaohudhurishwa?”

Dunia Haidumu na Wenye Kuishughulikia Hawawi Sawa na wale Wenye Kuitafuta Akhera

Allah تعالی Anatueleza kuhusu uduni wa dunia na mapambo yake na starehe zake hazidumu ukilinganisha na ambayo Allah تعالی Ameyaandaa kwa ajili ya waja wema katika nyumba ya Akhera katika neema kubwa zenye kudumu. Amesema Aliyetukuka:

مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ

“Mlivyonavyo vitakwisha na vilivyoko kwa Allah ndivyo vitakavyobakia.” (16:96).

Na Amesema:

وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ لِلْأَبْرَارِ

“Na vilioko kwa Allah ni bora kabisa kwa watu wema.” (3:198).

Na Amesema:

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَعٌ

“Na uhai wa dunia kwa mkabala wa Akhera si kitu ila ni starehe ndogo tu.” (13:26).

Na Amesema Aliyetukuka:

بَلْ تُؤْتُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾ وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَتَقَى ﴿١٧﴾

“Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia. Hali ya kuwa ya Akhera ni bora zaidi na yenye kudumu.” (87:16-17).

Mtume ﷺ amesema:

«وَاللَّهِ مَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا كَمَا يَغْمِسُ أَحَدُكُمْ إِبْصَعَهُ فِي الْمِمْ، فَلْيَنْظُرْ مَاذَا يَرْجِعُ إِلَيْهِ»

¹ Muslim 1:370.

“Wallahi, maisha ya hapa dunia yakilinganishwa na ya Akhera ni kama mtu kuingiza kidole chake baharini. Atazame kinachorudi kwake”¹.

أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥٢﴾

“Basi je, hamfahamu?”

Hii inamaanisha kuwa je, hawana akili wale wenye kuitanguliza dunia kuliko Akhera?

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَفَمَنْ وَعَدْنَاهُ وَعْدًا حَسَنًا فَهُوَ لَئِيْقِيْهِ كَمَنْ مَّتَّعْنَاهُ مَتَّعْنَاهُ مَتَّعَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ثُمَّ هُوَ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ مِنَ الْمُحْضَرِيْنَ ﴿٥٣﴾

“Je! Yule Tuliyemuahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama Tuliyemstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, na kisha Siku ya Kiyama akawa miongoni mwa wanaohudhurishwa?”

Je, yule Muumini anayesadiki aliyoahidiwa na Allah تعالى kwa amali zake njema thawabu ambazo atazipata bila ya matatizo yoyote ni sawa na yule Kafiri anayekanusha kukutana na Allah تعالى na kwa Ahadi Yake na Adhabu? Hakika yeye anastarehe siku chache katika maisha haya.

ثُمَّ هُوَ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ مِنَ الْمُحْضَرِيْنَ ﴿٥٤﴾

“Kisha Siku ya Kiyama ni miongoni mwa wanaohudhurishwa?”

Mujaahid na Qataadah wamesema: “Atakuwa ni miongoni mwa wenye kuadhibiwa”. Kisha palisemwa: “Hakika Aya hii iliteremshwa kuhusu Mtume ﷺ na Abu Jahl.” Kadhalika Panasemwa: “Kuhusu Hamzah رضي الله عنه, ‘Aliy رضي الله عنه na Abu Jahl”². Rai zote mbili zilinukuliwa kutoka kwa Mujaahid³.

¹ Ahmad 4:230.

² Atw-Twabariy 19:604-605.

³ Atw-Twabariy 19:604-605.

Aya Hii kwa dhahiri, ina maana ya kijumla zaidi. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka pale Anapomuelezea Muumini aliye katika daraja za juu Peponi akimwangualia sahibu yake aliye katika tabaka ya chini Motoni, na kumwambia:

وَلَوْلَا نِعْمَةُ رَبِّي لَكُنْتُ مِنَ الْمُحْضَرِينَ ﴿٥٧﴾

“Na lau si Neema ya Mola wangu Mlezi, bila shaka ningalikuwa miongoni mwa waliohudhurishwa.” (37: 57)

Amesema tena Aliyetukuka:

وَلَقَدْ عَلِمْتِ الْإِنْتِ إِهْمَ لَمْحَضْرُونَ ﴿١٥٨﴾

“Na Majini wamekwishajua hakika wao bila shaka watahudhrishwa.” (37:158)

* * *

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ
 تَزْعُمُونَ ﴿٦٢﴾ قَالَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ رَبَّنَا
 هَؤُلَاءِ الَّذِينَ أَغْوَيْنَا أَغْوَيْنَاهُمْ كَمَا غَوَيْنَا تَبَرَّأْنَا إِلَيْكَ
 مَا كَانُوا إِيَّانَا يَعْبُدُونَ ﴿٦٣﴾ وَقِيلَ ادْعُوا شُرَكَاءَكُمْ
 فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَرَأَوُا الْعَذَابَ لَوْ أَنَّهُمْ كَانُوا
 يَهْتَدُونَ ﴿٦٤﴾ وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ
 ﴿٦٥﴾ فَعَمِيَّتْ عَلَيْهِمُ الْأَنْبَاءُ يَوْمَئِذٍ فَهُمْ لَا يَتَسَاءَلُونَ
 ﴿٦٦﴾ فَأَمَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَعَسَىٰ أَنْ
 يَكُونَ مِنَ الْمُفْلِحِينَ ﴿٦٧﴾ وَرَبُّكَ خَلَقَ مَا يَشَاءُ
 وَيَخْتَارُ ۗ مَا كَانَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ ۗ سُبْحَانَ اللَّهِ وَتَعَالَىٰ عَمَّا
 يُشْرِكُونَ ﴿٦٨﴾ وَرَبُّكَ يَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا
 يُعْلِنُونَ ﴿٦٩﴾ وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ لَهُ الْخِمْدُ فِي
 الْأُولَىٰ وَالْآخِرَةِ ۗ وَالَهُ الْخِمْدُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٧٠﴾ قُلْ
 أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ اللَّيْلَ سَرْمَدًا إِلَىٰ يَوْمِ
 الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِضِيَاءٍ ۗ أَفَلَا
 تَسْمَعُونَ ﴿٧١﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ
 النَّهَارَ سَرْمَدًا إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ
 بِاللَّيْلِ تَسْكُوتٍ فِيهِ ۗ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٧٢﴾ وَمِنْ
 رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا
 مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ
 الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٦٢﴾ قَالَ
 الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ رَبَّنَا هَؤُلَاءِ
 الَّذِينَ أَغْوَيْنَا أَغْوَيْنَاهُمْ كَمَا غَوَيْنَا
 تَبَرَّأْنَا إِلَيْكَ ۗ مَا كَانُوا إِيَّانَا
 يَعْبُدُونَ ﴿٦٣﴾ وَقِيلَ ادْعُوا
 شُرَكَاءَكُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا
 لَهُمْ وَرَأَوُا الْعَذَابَ ۗ لَوْ أَنَّهُمْ كَانُوا
 يَهْتَدُونَ ﴿٦٤﴾ وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ
 مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ ﴿٦٥﴾ فَعَمِيَّتْ
 عَلَيْهِمُ الْأَنْبَاءُ يَوْمَئِذٍ فَهُمْ لَا
 يَتَسَاءَلُونَ ﴿٦٦﴾

62. Na siku Atakapowaita na akasema: Wako wapi mliokuwa mkidai kuwa ni washirika wangu?

63. Watasema wale iliyo-thibiti juu yao kauli: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio tuliwapoteza. Tuliwapoteza kama tulivyopotea sisi. Tunajitenga nao mbele Yako. Hawakuwa wakituabudu sisi.

64. Na itasemwa: Waiteni

hao miungu wa kishirikina wenu! Basi watawaita, lakini hawatawaitikia, na wataiona adhabu; laiti wangelikuwa wameongoka!

65. Na siku Atapowaita na akasema: Mliwajibu nini Mitume?

66. Basi khabari zitawapotea siku hiyo, nao hawataulizana.

67. Ama mwenye kutubu na akaamini na akatenda mema, huyo atakuwa miongoni mwa wenye kufanikiwa."

Kujitenga Washirikina na Washirika Wao Siku ya Akhera

Allah تعالی Anatueleza jinsi Atakavyowakaripia wapagani washirikina Siku ya Kiyama pale Atakapowaita na Kuwaambia:

أَيْنَ شُرَكَاءِى الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٦٩﴾

"Wako wapi mliokuwa mkidai kuwa ni washirika wangu?"

Wako wapi miungu ambao mlikuwa mkiwaabudu duniani miongoni mwa masanamu na washirika? Wanaweza kuwasaidia au kuwakinga nyinyi?

Haya yanasemwa kwa njia ya kuwashutumumu na kuwatisha, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فُرَادَى كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَتَرَكْتُمْ مَا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ وَمَا نَرَى مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَؤُا لَقَدْ تَقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنْكُمْ

مَا كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٦٩﴾

"Na bila shaka nyinyi mmetujia mmoja mmoja kama Tulivyo-kuumbeni mara ya kwanza, na mmeyaacha nyuma yenu Tuli yokupeni, na hatuwaoni waombezi wenu pamoja nanyi ambao mlidai kuwa ni washirika wa Allah kwenu. Yamekatika mahusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyokuwa mkidai." (6:94)

Na Kauli Yake:

قَالَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ

“Watasema wale iliyothibiti juu yao kauli.”

Maana yake: Mashetani wakaidi na wale waliokuwa wakiita kwenye ukafiri. Hawa watasema:

رَبَّنَا هَتُّوْنَا أَعْوَيْنَا أَعْوَيْنَهُمْ كَمَا عَوَيْنَا تَبَرَّأْنَا إِلَيْكَ مَا كَانُوا إِبْنَانَا

يَعْبُدُونَ ﴿٢٧﴾

“Mola wetu Mlezi! Hawa ndio tuliwapoteza. Tuliwapoteza kama tulivyopotea sisi. Tunajitenga nao mbele Yako. Hawakuwa wakituabudu sisi.”

Watashuhudia dhidi yao kuwa wao ndio wamewapoteza, hivyo kuwafuata kisha wakajitenga katika kuwaabudu, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَأَتَّخِذُوا مِن دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لِّيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٢٨﴾ كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُونُونَ

عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٢٩﴾

“Na walifanya waungu wengine badala ya Allah ili wawe wenye kuwatia nguvu. Wapi! Watakanusha lbadah yao na watakuwa mahasimu zao.” (19:81-82).

Amesema tena Aliyetukuka:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِن دُونِ اللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَن

دُعَائِهِمْ غٰفِلُونَ ﴿٣٠﴾ وَإِذَا حُيِّرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كٰفِرِينَ ﴿٣١﴾

“Na wapotofu wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiye kuwa Allah ambao hawatawajibu mpaka Siku ya Kiyama, na hawatambui dua zao. Na ambao watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa lbadah yao.” (46:5-6).

Na alisema Kipenzi cha Allah, Ibraahim عليه السلام kwa kaumu yake:

إِنَّمَا أَخَذْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ
بَعْضُكُم بِبَعْضٍ وَيَلْعَنُ بَعْضُكُم بَعْضًا

“Hakika nyinyi mumefanya masanamu miungu badala ya Allah. Na mnapendana baina yenu katika maisha ya dunia, lakini Siku ya Kiyama mtakataana wenyewe kwa wenyewe.” (29: 25).

Amesema tena Aliyetukuka:

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوْا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿٣٠﴾

“Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwisha kuiona adhabu, na yatakatika mafungamano yao”

Mpaka Kauli Yake:

وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ ﴿٣١﴾

“Wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.” (2:166-167).

Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَقِيلَ ادْعُوا شُرَكَاءَكُمْ

“Na itasemwa: Waiteni hao miungu wa kishirikina wenu!”

Kumaanisha wawaokoe kwa yale mliyo ndani yake, kama mulivyotaka kutoka kwao duniani.

فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَرَأُوا الْعَذَابَ

“Basi watawaita, lakini hawatawaitikia, na wataiona adhabu.”

Watayakinisha kuwa wao bila shaka wanakwenda Motoni. Na Kauli Yake:

لَوْ أَنَّهُمْ كَانُوا يَهْتَدُونَ ﴿٣٢﴾

“Laiti wangelikuwa wameongoka!”

Watakapoiona adhabu na macho yao, watatamani kuwa walikuwa miongoni mwa walioongoka katika hii dunia. Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

وَيَوْمَ يَقُولُ نَادُوا شُرَكَاءِيَ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ
مُؤَبِقًا ﴿٥٢﴾ وَرِءَا أَلْمُجْرِمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُوَاقِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿٥٣﴾

“Na siku atakayosema Allah: ‘Waiteni washirika wangu ambao mlidai’. Basi watawaita, lakini hawatawaitikia; na Tutatia kizuwizi baina yao. Na wabaya watauona moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuepuka.” (18: 52-53).

Msimamo wao kwa Mtume Siku ya Kiyama

Na Kauli Yake:

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ مَاذَا أَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِينَ ﴿٥٤﴾

“Na siku Atapowaita na akasema: Mliwajibu nini Mitume?”

Mwito wa kwanza utakuwa ni kuulizwa kuhusu Tawhidi, na hiyo ni kuthibitisha Unabii – “Mliwaitikia vipi Mitume waliotumwa kwenu? Mliwashuhudiaje?” Ni kama yale atayoulizwa mja kaburini: Mola wako Mlezi ni nani? Mtume wako ni yupi? Na Dini yako ni ipi? Ama Muumini atashuhudia kuwa Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالى na kuwa Muhammad ﷺ ni Mja na Mtume Wake, ama kafiri atasema: “Ee, ee, sijui”. Hivyo, hatakuwa na jibu Siku ya Kiyama isipokuwa kunyamaza, kwa sababu yeyote anayekuwa kipofu hapa duniani, atakuwa kipofu Akhera na atapotea njia kabisa. Kwa hiyo Allah تعالى Akasema:

فَعَمِيَتْ عَلَيْهِمُ الْأَنْبَاءُ يَوْمَئِذٍ فَهُمْ لَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿٥٥﴾

“Basi zitawapotea khabari siku hiyo, nao hawataulizana”.

Amesema Mujaahid: “Hoja itafunikwa kwao (hawatakuwa na hoja yoyote).”¹ Hivyo, hawatakuwa ni wenye kuulizana kuhusu nasaba na ukuruba wao. Na Kauli Yake:

¹ Atw-Twabariy 1: 607.

فَأَمَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا

“Ama mwenye kutubu na akaamini na akatenda mema.”

Maana yake: Duniani.

فَعَسَىٰ أَنْ يَكُونَ مِنَ الْمُفْلِحِينَ ﴿٦٧﴾

“Huyo atakuwa miongoni mwa wenye kufanikiwa.”

Hiyo itakuwa ni Siku ya Kiyama. Na neno huenda linapotumika kwa Allah تعالى humanisha kutokea kwa jambo, na hili bila ya shaka litatokea kwa Fadhila na Rehema ya Allah تعالى.

وَرَبُّكَ خَلَقَ مَا يَشَاءُ وَيَخْتَارُ ۗ مَا كَانَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ ۗ سُبْحَانَ اللَّهِ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٨﴾ وَرَبُّكَ يَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُورُهُمْ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٦٩﴾ وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُولَىٰ وَالْآخِرَةِ ۗ وَهُوَ الْحَكِيمُ ۗ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٧٠﴾

68. “Na Mola wako Mlezi Huumba na Huteua Atakavyo. Viumbe hawana khiari. Allah Ametukuka na Ametakasika na hao wanao mshirikisha Naye.

69. Na Mola wako Mlezi Anayajua yaliyoficha vifua vyao, na wanayoyatangaza.

70. Naye ni Allah Ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye. Sifa zote Njema ni Zake Yeye, mwanzo na mwisho. Na Hukumu ni Yake Yeye. Na Kwake Yeye mtarejeshwa”.

Allah Peke Yake Ndiye Muumbaji, Mwenye Elimu na Uchaguzi

Allah تعالى Anatueleza kuwa Yeye Peke Yake Ndiye Muumbaji na wa Kutoa Uamuzi, na hakuna yeyote anayeweza kumpinga au kugeuza Hukumu Yake. Allah تعالى Amesema:

وَرَبُّكَ خَلَقَ مَا يَشَاءُ وَيَخْتَارُ ۗ

“Na Mola wako Mlezi Huumba na Huteua Atakavyo”.

Atakavyo, na lolote Analotaka huwa na Asilotaka Haliwi kabisa. Mambo yote ya kheri na shari yako Mikononi Mwake na yatarudi Kwake. Na Kauli Yake:

مَا كَانَ لَهُمُ الْخَيْرَةُ

“Viumbe hawana khiari.”

Hii ni kukanusha kwa kauli iliyo sahihi zaidi kwa rai mbili zilizopo. Hii ni kama Kauli Yake:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخَيْرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ

“Haiwi kwa Muumini mwanamume wala kwa Muumini mwanamke, Allah na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao.” (33:36).

Kisha Akasema:

وَرَبُّكَ يَعْلَمُ مَا تَكْنُ صُدُورُهُمْ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٦٦﴾

“Na Mola wako Mlezi Anayajua yaliyoficha vifua vyao, na wanayo yatangaza”.

Anajua vilivyofichwa na dhamira na yaliyobebwa na siri kama Anavyojua yanayodhihirishwa na yaliyo wazi kwa viumbe vyote.

سَوَاءٌ مِّنْكُمْ مَنْ أَسْرَأَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿٦٧﴾

“Ni sawa Kwake Allah, anayeficha kauli yake miongoni mwenu na anayeidhihirisha; na pia ajifichaye usiku na aendaye mchana” (13:10)

Na Kauli Yake:

وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Naye ni Allah Ambaye Hapana mungu isipokuwa Yeye.”

Kwani Yeye ni Peke Yake katika Uungu Wake na Mola, na hapana apasaye kuabudiwa asiyekuwa Yeye, na hakuna Mola Mlezi awezaye kuumba anachotaka na anayechagua atakacho mbali ya Yeye.

لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُولَىٰ وَالْآخِرَةِ

“Sifa zote Njema ni Zake Yeye, mwanzo na mwisho.”

Yote Afanyayo, Yeye ni Mwenye Kusifiwa kwa Uadilifu na Hekima Yake.

وَلَهُ الْحُكْمُ

“Na Hukumu ni Yake Yeye.”

Hakuna anayeweza kushindana Naye, kwa sababu ya Uweza Wake, Nguvu Zake, Hekima na Rehema Yake.

وَالِيهِ تَرْجِعُونَ ﴿٧٠﴾

“...Na Kwake Yeye mtarejeshwa.”

Maana yake: Nyote Siku ya Kiyama, na kila mmoja atalipwa kwa amali yake ya kheri au shari, na hapana amali yao yoyote itakayofichwa:

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ اللَّيْلَ سَرْمَدًا إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِضِيَاءٍ ۗ أَفَلَا تَسْمَعُونَ ﴿٧١﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ النَّهَارَ سَرْمَدًا إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِاللَّيْلِ تَسْكُونُونَ فِيهِ ۗ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٧٢﴾ وَمِنْ رَحْمَتِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

71. “Sema: Mwaonaje, Allah Angeliufanya usiku umekukalieni daima mpaka Siku ya Kiyama, mungu gani asiyekuwa Allah Atakayekuleteeni mwangaza? Basi je, hamsikii?”

72. Sema: Mwaonaje, Allah Angeliufanya mchana umekukalieni moja kwa moja mpaka Siku ya Kiyama, mungu gani asiyekuwa Allah Atakayekuleteeni usiku mkapumzika humo? Basi je, hamwoni?”

73. Na ni katika Rehema Zake Amekufanyieni usiku na mchana mpate kupumzika humo na mtafute Fadhila Zake, na ili mpate kushukuru”.

Usiku na Mchana ni katika Neema za Allah تعالى na Dalili ya Kuwa Yeye ni wa Pekee (Tawhiidi)

Allah تعالى Anawakumbusha waja Wake Neema Zake kwao kwa kutiisha usiku na mchana, bila ya vitu viwili hivyo wanadamu hawangeweza kuishi. Akabainisha kuwa lau Angeufanya usiku kudumu mpaka Siku ya Kiyama, hilo lingewadhuru kuwachosha na kuwatia msongo. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِضِيَاءٍ

“Mungu gani asiyekuwa Allah Atakayekuleteeni mwangaza?”

Maana yake: Kwa huo mnaona na kuliwazika kwa sababu yake.

أَفَلَا تَسْمَعُونَ ﴿٧١﴾

“Basi je, hamsikii?.”

Kisha Anaeleza Allah تعالى kuwa lau Angejaalia mchana wenye kutukalia, yaani kuwa daima dawamu nasi mpaka Siku ya Kiyama, hilo lingewadhuru wao, na kutaabisha miili kwa kutembea sana na kuwa na harakati na shughuli nyingi. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِلَيْلٍ تَشْكُونَ فِيهِ

“Mungu gani asiyekuwa Allah Atayekuleteeni usiku mkapumzika humo?.”

Ambamo munapumzika kutokana na harakati zenu na mashughuli yenu,

أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٧٢﴾ وَمِنْ رَحْمَتِهِ

“Basi je, hamwoni?. Na ni katika Rehema Zake.”

Kwenu kuwa,

جَعَلَ لَكُمْ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ

“Amekufanyieni usiku na mchana.”

Kwa Kuumba huu na huu (Maana yake: Usiku na mchana). Natija yake ni:

لِتَسْكُنُوا فِيهِ

“Ili mpate kupumzika humo.”

Maana yake: Usiku na pia:

وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

“Na mtafute Fadhila Zake.”

Maana yake: Mchana kwa kusafiri, kutembea na kufanya kazi. Na Kauli Yake:

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٦٢﴾

“Na ili mpate kushukuru.”

Kumshukuru Allah تعالى kwa kutekeleza aina tofauti za ‘Ibadah wakati wa usiku na pia mchana. Na yeyote anayekosa kutekeleza usiku basi anawahi mchana au kinyume chake, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ خِلْفَةً لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يَذَّكَّرَ أَوْ أَرَادَ شُكُورًا ﴿٦٢﴾

“Naye Ndiye Aliyefanya usiku na mchana ufuatane; kwa yule anayetaka kukumbuka au anayetaka kushukuru.” (25: 62).

Na zipo Ayah nyingi katika masuala haya.

* * *

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ
 تَزْعُمُونَ ﴿٧٤﴾ وَنَزَعْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا فَقُلْنَا
 هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ فَعَلِمُوا أَنَّ الْحَقَّ لِلَّهِ وَصَلَّ عَنْهُمْ مَا
 كَانُوا يَفْتُرُونَ ﴿٧٥﴾ * إِنَّ قُرُونًا كَانَتْ مِنْ قَوْمِ
 مُوسَى فَبَغَى عَلَيْهِمْ ۗ وَآتَيْنَاهُ مِنَ الْكُنُوزِ مَا إِنَّ مَفَاتِحَهُ
 لَتَتَوَّأُّ بِالْعُصْبَةِ أُولَى الْقُوَّةِ إِذْ قَالَ لَهُ قَوْمُهُ لَا تَفْرَحْ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ﴿٧٦﴾ وَأَتَّبِعْ فِيمَا ءَاتَاكَ اللَّهُ الْآدَارَ
 الْآخِرَةَ ۗ وَلَا تَسْ نَصِيْبَكَ مِنَ الدُّنْيَا ۗ وَأَحْسِن
 كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ ۗ وَلَا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ ﴿٧٧﴾ قَالَ إِنَّمَا أُوتِيْتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ
 عِنْدِي ۗ أَوْلَمْ يَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ قَدْ أَهْلَكَ مِنْ قَبْلِهِ مِنَ
 الْقُرُونِ مَنْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَأَكْثَرُ جَمْعًا ۗ وَلَا يُسْئَلُ عَن
 ذُنُوبِهِمُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٧٨﴾ فَخَرَجَ عَلَىٰ قَوْمِهِ فِي زِينَتِهِ
 ۗ قَالَ الَّذِينَ يُرِيدُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا يَلِيتَ لَنَا مِثْلَ
 مَا أُوتِيَ قُرُونُ إِنَّهُمْ لَذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٧٩﴾ وَقَالَ
 الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَيَلَكُمْ تَوَابُ اللَّهِ خَيْرٌ لِمَنْ ءَامَنَ
 وَعَمِلَ صَالِحًا وَلَا يُفْلِحُهَا إِلَّا الصَّابِرُونَ ﴿٨٠﴾

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ فَيَقُولُ أَيْنَ
 شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ
 تَزْعُمُونَ ﴿٧٤﴾ وَنَزَعْنَا مِنْ كُلِّ
 أُمَّةٍ شَهِيدًا فَقُلْنَا هَاتُوا
 بُرْهَانَكُمْ فَعَلِمُوا أَنَّ الْحَقَّ لِلَّهِ وَصَلَّ عَنْهُمْ مَا
 كَانُوا يَفْتُرُونَ ﴿٧٥﴾

74. Na siku Atakapowaita na Akasema: Wako wapi hao mliokuwa mkidai kuwa ni washirika Wangu?

75. Na Tutatoa shahidi katika kila ummah, na Tutasema: Leteni hoja zenu! Hapo watajua kwamba hakika kweli ni ya Allah, na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazua.

Kuwakemea Washirikina

Na huu ni wito mwingine kwa njia ya Kuwakemea wale wanaoabudu asiye-kuwa Allah تعالیٰ. Mola Mlezi Aliyetukuka Atawaita mbele

ya mashahidi kwa Kusema:

أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٧٤﴾

“Wako wapi hao mliokuwa mkidai kuwa ni washirika Wangu?”

Maana yake: Duniani. Anaendelea Aliyetukuka:

وَنَزَعْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا

“Na Tutatoa shahidi katika kila ummah.”

Amesema Mujaahid: “Hii inamaanisha Mtume”¹. Na hapo:

فَقُلْنَا هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ

“Tutasema: Leteni hoja zenu!”

Wa ukweli wa madai yenu kuwa Allah تعالى Ana washirika.

فَعَلِمُوا أَنَّ الْحَقَّ لِلَّهِ

“Hapo watajua kwamba hakika kweli ni ya Allah.”

Hivyo hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye Peke Yake. Hapo hawatazungumza na hawatakuwa na jawabu lolote kwa hilo.

وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٧٦﴾

“Na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazua.”

Maana yake: Yatatoweka wala hayatawafaa wao kabisa.

* إِنَّ قُرُونًا كَانَتْ مِنْ قَوْمِ مُوسَىٰ فَبَغَىٰ عَلَيْهِمْ ۗ وَآتَيْنَاهُ مِنَ الْكُنُوزِ مَا إِنَّ مَفَاتِحَهُ
لَتَتَوَّأُّ بِالْعُصْبَةِ أُولَى الْقُوَّةِ إِذْ قَالَ لَهُ قَوْمُهُ لَا تَفْرَحْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ﴿٧٦﴾
وَأَتَّبَعِ فِي مَا ءَاتَاكَ اللَّهُ الْآخِرَةَ ۗ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا ۗ وَأَحْسِنَ
كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ ۗ وَلَا تَتَّبِعِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ ﴿٧٧﴾

76. Hakika Qaaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na Tulimpa khazina ambazo funguo zake

¹ Atw-Twabariy 19:614

zinawatopeza watu wenye nguvu kuzichukua. Walipomwambia watu wake: Usijigambe! Hakika Allah Hawapendi wanaojigamba.

77. Na utafute, kwa Aliyokupa Allah, makazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Allah Alivyokufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Allah Hawapendi mafisadi.”

Kisa cha Qaaruni na Kupatiwa Waadhi na Kaumu Yake

Imepokewa kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

﴿ إِنَّ قُرُونًا كَانَتْ مِنْ قَوْمِ مُوسَى ﴾

“Hakika Qaaruni alikuwa katika watu wa Musa.”

Maana yake: “Alikuwa ni mtoto wa ami yake.”¹

Na hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya Ibraahim an-Nakha’iy, ‘Abdullah ibn al- Haarith ibn Nawfal, Sammaak ibn Harb, Qataadah, Maalik ibn Dinaar, Ibn Jurayj na wengineo kuwa yeye alikuwa ni binamu yake Musa عليه السلام.² Amesema Ibn Jurayj: “Yeye alikuwa ni Qaaruni ibn Yaswhar ibn Qaahith, na Musa alikuwa ni mtoto wa ‘Imraan ibn Qaahith.”³

﴿ وَأَتَيْنَهُ مِنَ الْكَؤُوبِ ﴾

“Na Tulimpa khazina.”

Maana yake: Mali. Anatueleza Aliyetukuka kuhusu mali hiyo:

﴿ مَا إِنَّ مَفَاتِحَهُ لَتَنُوتُنَّ بِالْعُصْبَةِ أُولَى الْقُوَّةِ ﴾

“Ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu kuzichukua.”

Hii inamaanisha kuwa kikundi cha watu wenye nguvu walikuwa wanashindwa kuzibeba kwa sababu ya wingi wake. Amepokea al-A’mash kutoka kwa

¹ Ibn Abi Haatim 9:3005.

² Atw-Twabariy 19:616.

³ Atw-Twabariy 19:615.

Khaythamah: “Funguo za khazina ya Qaaruni zilikuwa zimetengenezwa na ngozi, kila ufunguo ulikuwa sawa na kidole, na kila ufunguo ulikuwa wa chumba chake hasa. Alipokuwa anakwenda sehemu yoyote, funguo hizo zilikuwa zinabebwa na nyumbu sitini waliokuwa na alama nyeupe utosini na miguuni mwao.”¹ Rai nyengine pia zilitolewa, na Allah تعالى Anajua zaidi.

قَالَ لَهُ قَوْمُهُ لَا تَفْرَحْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ﴿٧٤﴾

“Walipomwambia watu wake: Usijigambe! Hakika Allah Hawapendi wanaojigamba.”

Maana yake: Watu wema katika watu wake walimnasihi kwa nasaha na uongofu, wakasema: “Usifurahi kwa uliyo nayo.” Yaani, usijigambe wala usiwe na kiburi kwa sababu ya mali uliyonayo. Jua kwamba:

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ﴿٧٥﴾

“Hakika Allah Hawapendi wanaojigamba.”

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Kuwa hii ina maana mwenye kufurahi”². Amesema Mujaahid: “Hii inamaanisha wale mafidhuli na wasojali, ambao hawamshukuru Allah تعالى kwa Alichowapa.”³

وَأَتَّبِعْ فِيمَا ءَاتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا

“Na utafute, kwa Aliyokupa Allah, makazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia.”

Hii inamaanisha kuwa tumia mali zako nyingi na neema kubwa ulizopewa na Allah تعالى kwa kumuabudu Mola wako Mlezi, ili upate kuwa karibu Naye kwa kufanya aina tofauti za amali njema ambazo zitakupatia thawabu hapa duniani na kesho Akhera.

¹ Atw-Twabariy 19:617.

² Atw-Twabariy 19:622.

³ Atw-Twabariy 19:623.

وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا

“Wala usisahau fungu lako la dunia.”

Katika yale Aliyoruhusu Allah تعالى kama vile vyakula, vinywaji, mavazi, makazi na wanawake. Hakika ni kuwa Mola wako Mlezi Ana haki juu yako, na nafsi yako ina haki juu yako, familia yako pia ina haki juu yako, na mke wako ana haki juu yako. Hivyo kila mmoja mpe haki yake.

وَأَحْسِنَ كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ

“Nawe fanya wema kama Allah Alivyokufanyia wema wewe.”

Maana yake: Kufanya wema kwa viumbe Vyake, kama Alivyokufanyia wema wewe.

وَلَا تَتَّبِعِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ

“Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi.”

Kwa hiyo, isiwe hima na malengo yako ni kueneza ufisadi na uharibifu katika ardhi na kuwadhuru viumbe vya Allah تعالى. Anamalizia Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ ﴿٧٨﴾

“Hakika Allah Hawapendi mafisadi.”

قَالَ إِنَّمَا أُوتِيتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ عِنْدِي ۗ أَوَلَمْ يَعْلَمَ أَنَّ اللَّهَ قَدْ أَهْلَكَ مِن قَبْلِهِ مِن

الْقُرُونِ مَن هُوَ أَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَأَكْثَرُ جَمْعًا ۗ وَلَا يُسْأَلُ عَن ذُنُوبِهِمُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٧٩﴾

78. Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyonayo. Je! Hakujuu kwamba Allah keshawaangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye, na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake. Na wakosefu hawataulizwa khabari ya dhambi zao.”

Allah تعالى Anatueleza Qaaruni alivyojibu mawaidha kutoka kwa watu wake walipomnasih:

قَالَ إِنَّمَا أُوتِيْتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ عِنْدِي

“Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo.”

Kumaanisha kuwa mimi sihitaji nasaha zenu; hakika ni kuwa Allah تعالى Amenipatia mali hii kwa sababu Anajua kuwa ninastahiki na Yeye Ananipenda. Kwa makadirio: “Amenipatia kwa sababu Anajua ninastahili hilo.”

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَانَا ثُمَّ إِذَا خَوَّلْتَهُ نِعْمَةً مِنَّا قَالَ إِنَّمَا أُوتِيْتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ

“Na madhara yanapomgusa mtu hutuomba. Kisha tunapompa Neema zitokazo Kwetu, husema: Nimepewa haya kwa ilimu.” (39: 49).

Tafsiri nyingine ya Aya hii inasema kuwa maana yake ni: “Kwa sababu tu ya yale Anayoyajua Allah تعالى kuhusu mimi ndio nikapata fadhila na neema hii.”

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَيْنَٰ أَذِقْنَهُ رَحْمَةً مِنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَّآءٍ مَّسَّتْهُ لِيَقُولَنَّ هَذَا إِلَىٰ

“Na pindi Tukimwonjisha Rehema itokayo Kwetu baada ya kumgusa kwa madhara, bila ya shaka husema: Haya nayastahiki mimi.” (41:50)

Hii inamaanisha kuwa mimi nastahiki hili. Imamu ‘Abdur-Rahmaan ibn Zayd ibn Aslam ameieleza Aya hii kwa vizuri zaidi katika tafsiri yake:

قَالَ إِنَّمَا أُوتِيْتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ عِنْدِي

“Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyonayo.”

Amesema: “Lau hakika haingekuwa Allah تعالى Hakuniridhia na wala hajui fadhila na wema wangu, Asingenipa mali.” Na Akasema Aliyetukuka:

أَوَلَمْ يَعْلَم أَنَّ اللَّهَ قَدْ أَهْلَكَ مِنْ قَبْلِهِ مِنْ الْقُرُونِ مَنْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَأَكْثَرُ جَمْعًا ۗ

“Je! Hakujua kwamba Allah keshwa waangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye, na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake.”¹

Haya ni yale yanayosemwa na watu wasiokuwa na elimu pindi wanapomuona mtu aliyekunjuliwa riziki na Allah تعالى. Wanasema kuwa ikiwa hakustahili, basi Allah تعالى Asingempa.

فَخَرَجَ عَلَى قَوْمِهِ فِي زِينَتِهِ ۗ قَالَ الَّذِينَ يُرِيدُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا يَا لَيْتَ لَنَا مِثْلَ مَا أُوتِيَ قُرُونُ إِنَّهُمْ لَذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٧٩﴾ وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَيَلَكُمْ ثَوَابُ اللَّهِ خَيْرٌ لِمَنْ ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا وَلَا يُلْقَاهَا إِلَّا الصَّابِرُونَ ﴿٨٠﴾

79. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale waliokuwa wanataka maisha ya duniani: Laiti tungelikuwa tunayo kama aliyopewa Qaaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa.

80. Na wakasema wale waliopewa ilimu: Ole wenu! Malipo ya Allah ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema. Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye subira”.

Qaaruni alivyotoka na mapambo yake, na Maoni ya Kaumu Yake Kuhusu Yeye

Allah تعالى Anatueleza namna Qaaruni alivyotoka siku moja mbele ya watu wake akiwa na mapambo yake ya kifalme; akiwa amevaa nguo nzuri pamoja na farasi wake wazuri, wafanya kazi wake na msafara wa watu wengi. Pindi tu wale waliokuwa na mwelekeo wa hii dunia walipomuona na mapambo hayo ya kifahari, walitamani kupata kama alivyopewa wakasema:

¹ Atw-Twabariy 19:626.

يَلَيْتَ لَنَا مِثْلَ مَا أُوتِيَ قُرُونُ إِنَّهُ لَذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٧٤﴾

“Laiti tungelikuwa tunayo kama aliyopewa Qaaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa”.

Maana: Ana bahati sana na anayo sehemu kubwa hapa duniani. Waliposikia kauli zao hizo wale watu waliopewa elimu yenye manufaa, waliwaambia:

وَيَلِّكُم مِّنْ ثَوَابِ اللَّهِ خَيْرٌ لِّمَنِ ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ﴿٧٥﴾

“Ole wenu! Malipo ya Allah ni bora kwa mwenye kuamini na akatenda mema.”

Malipo ya Allah تعالى na thawabu Anazowapatia waja Wake Waumini wema Kesho Akhera ni bora kuliko munayoona, kama ilivyokuja katika Hadithi sahihi:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: أَعَدَدْتُ لِعِبَادِي الصَّالِحِينَ مَا لَا عَيْنٌ رَأَتْ وَلَا أُذُنٌ سَمِعَتْ وَلَا خَطَرَ عَلَى قَلْبِ بَشَرٍ وَاقْرَأُوا إِن شِئْتُمْ: ﴿فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾»

Anasema Allah تعالى: **“Nimewaandalia waja Wangu wema kile kisichoonekana na jicho, wala kusikika na masikio, wala hakijapitia katika moyo wa mwanadamu. Soma ukipenda: Nafsi yoyote haijui yaliyofichwa katika hayo yanayofurahisha macho ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.” (32:17)¹**

وَلَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الصَّابِرُونَ ﴿٧٦﴾

“Wala hawatapewa hayo isipokuwa wenye subira”.

Amesema as-Suddiy: “Hakuna atakayepata Pepo isipokuwa wale wenye kusubiri, yeye ameifanya ibara hii kana kwamba ndiyo iliyokamilisha kauli ya wale waliopewa elimu”². Amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالى: “Hii haifikiwi isipokuwa na wale wanaosubiri dhidi ya kupenda hii dunia, wanaotaka nyumba ya Akhera. Yeye ameifanya hii ni sehemu ya Kauli ya Maneno ya Allah تعالى, Kuelezea hakika hii”³.

¹ Fat’hu Al-Baari 8:375.

² Ibn Abi Haatim 9:3016.

³ Fat’hu Al-Baari 10:269.

فَحَسَفْنَا بِهٖ وَبِدَارِهِ الْأَرْضَ فَمَا كَانَ لَهُ مِنْ فِئَةٍ
 يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُنْتَصِرِينَ ﴿٨١﴾
 وَأَصْبَحَ الَّذِينَ تَمَنَّوْا مَكَانَهُ بِالْأَمْسِ يَقُولُونَ وَيَكَافُ
 اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَوْلَا
 أَنْ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْنَا لَخَسَفَ بِنَا ۗ وَيَكَانَهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ
 ﴿٨٢﴾ تِلْكَ الْأْدَارُ الْأَخْرُءُ لِنَجْعَلَهَا لِلَّذِينَ لَا يُرِيدُونَ عُلُوًّا فِي
 الْأَرْضِ وَلَا فِسَادًا ۗ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٨٣﴾ مَنْ جَاءَ
 بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ خَيْرٌ مِمَّا ۗ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَى
 الَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٤﴾ إِنْ
 الَّذِي فَرَضَ عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لَرَأْدُكَ إِلَىٰ مَعَادٍ ۗ قُلْ
 رَبِّي أَعْلَمُ مَنْ جَاءَ بِالْهُدَىٰ وَمَنْ هُوَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٨٥﴾
 وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَنْ يُلْقَىٰ إِلَيْكَ الْكِتَابُ إِلَّا رَحْمَةً مِنْ
 رَبِّكَ ۗ فَلَا تَكُونَنَّ ظَهِيرًا لِّلْكَافِرِينَ ﴿٨٦﴾ وَلَا يَصُدُّكَ
 عَنْ آيَاتِ اللَّهِ بَعْدَ إِذْ أَنْزَلَتْ إِلَيْكَ ۗ وَأَدْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ ۗ
 وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٨٧﴾ وَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا
 آخَرَ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ ۗ لَهُ
 الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٨﴾

فَحَسَفْنَا بِهٖ وَبِدَارِهِ الْأَرْضَ فَمَا
 كَانَ لَهُ مِنْ فِئَةٍ يَنْصُرُونَهُ مِنْ
 دُونِ اللَّهِ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُنْتَصِرِينَ
 ﴿٨١﴾ وَأَصْبَحَ الَّذِينَ تَمَنَّوْا
 مَكَانَهُ بِالْأَمْسِ يَقُولُونَ وَيَكَافُ
 اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ
 عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَوْلَا أَنْ مَنَّ اللَّهُ
 عَلَيْنَا لَخَسَفَ بِنَا ۗ وَيَكَانَهُ لَا يُفْلِحُ
 الْكَافِرُونَ ﴿٨٢﴾

81. Basi Tukamdidimiza yeye na nyumba yake katika ardhi; wala halikuwepo kundi lolote la kumnusuru kwa Allah, wala hakuwa miongoni mwa wanaojitetea.

82. Na wale waliotamani kuwa pahala pake jana, wakawa wanasema: Kumbe Allah Humkunjulia Riziki Amtakaye katika waja Wake, na Humdhikisha

Amtakaye. Ingelikuwa Allah Hakutufanyia hisani Angelitudidimiza. Kumbe makafiri hawafanikiwi!"

Kudidimizwa Qaaruni na Nyumba Yake ardhini

Baada ya Allah تعالی Hutuelezea kuhusu majivuno na kiburi cha Qaaruni katika mapambo ya kifahari, na jinsi alivyojigamba mbele ya watu wake na kuwakandamiza, kisha Allah تعالی Anatueleza jinsi yeye na nyumba yake walivyodidimizwa na kumezwa na ardhi. Hakika jambo hilo limethibiti katika Sahihi ya al-Bukhaariy kutoka kwa Saalim kuwa baba yake alimuhadithia kuwa Mtume ﷺ amesema:

«بَيْنَمَا رَجُلٌ يَجْرُ إِزَارَهُ إِذْ خَسِيفَ بِهِ، فَهُوَ يَتَجَلَجَلُ فِي الْأَرْضِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Pale mtu mmoja alipoburuza izari yake, hapo hapo alimezwa na kudidimizwa na ataendelea kuzama chini ya ardhi mpaka Siku ya Kiyama.”

Kisha ilipokewa kwa Saalim kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه mfano wa Hadithi hiyo hapo juu¹. Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Sa’iid رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«بَيْنَمَا رَجُلٌ فِيمَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ خَرَجَ فِي بُرْدَيْنِ أَخْضَرَيْنِ يَخْتَالُ فِيهِمَا، أَمَرَ اللَّهُ الْأَرْضَ فَأَخَذَتْهُ، فَإِنَّهُ لَيَتَجَلَجَلُ فِيهَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Wakati mtu mmoja miongoni mwa wale waliokuwa kabla yenu alipotoka anatembea kwa majivuno na kiburi, huku amevaa nguo mbili za kijani. Hapo Allah Aliiamuru ardhi kummeza na ataendelea kuzama chini yake mpaka Siku ya Kiyama.”²

Hii imenukuliwa na Ahmad peke yake, na Isnadi yake ni Hasan. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَمَا كَانَ لَهُ مِنْ فِتْنَةٍ يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُنتَصِرِينَ ﴿٨٨﴾

“Wala halikuwepo kundi lolote la kumnusuru kwa Allah, wala hakuwa miongoni mwa wanaojitetea.”

¹ Atw-Twabariy 19:629.

² Ahmad 3:137.

Hii inamaana anakuwa mali yake haikumfaa kitu wala kundi lake wala wafanya kazi wake wala msafara uliokuwa ukiandamana naye. Wala hawakuweza kumuepusha na Ghadhabu ya Allah تعالى, Adhabu na Mateso Yake, wala hakuweza kujinusuru mwenyewe. Hakuweza kujinusuru wala kunusuriwa na wengine.

Watu Kuwaidhika kwa Kudididmizwa Kwake

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَصْبَحَ الَّذِينَ تَمَنَّوْا مَكَانَهُ بِالْأَمْسِ

“Na wale waliotamani kuwa pahala pake jana.”

Wale waliomuona na mapambo yake ya kifahari, walisema:

قَالَ الَّذِينَ يُرِيدُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا يَلِيتَ لَنَا مِثْلَ مَا أُوتِيَ قُرُونُ إِنَّهُ لَذُو

حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٨٦﴾

“Wakasema ambao wanataka maisha ya dunia; Laiti tungelikuwa tunayo kama aliyopewa Qaaruni! Hakika yeye ni mwenye bahati kubwa.”

Lakini pindi alipodidimizwa wakawa wanasema:

وَيَكُنَّ اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ

“Kumbe Allah Humkunjulia riziki Amtakaye katika waja Wake, na Humdhikisha Amtakaye”.

Kwa maana kwamba mali si mbadala wa Radhi za Allah تعالى. Hakika Allah تعالى hutoa na Kunyima, Humdhiki mtu na Kumkunjulia, na Hudunisha na Kunyanyua, Naye Ana Hekima Timilifu na hoja za juu na kubwa. Na hii ni kama Hadithi *Marfuu* kwa Ibn Mas'uud رضي الله عنه:

«إِنَّ اللَّهَ فَسَمَ بَيْنَكُمْ أَخْلَاقَكُمْ كَمَا فَسَمَ أَرْزَاقَكُمْ، وَإِنَّ اللَّهَ يُعْطِي الْمَالَ مَنْ يُحِبُّ
وَمَنْ لَا يُحِبُّ، وَلَا يُعْطِي الْإِيمَانَ إِلَّا مَنْ يُحِبُّ»

“Hakika Allah Amegawa baina yenu tabia zenu kama Alivyogawa riziki zenu. Na hakika Allah Anatoa mali kwa Ampendaye na Asiyempenda, wala Hampi Imani isipokuwa Anayempenda.”¹

Ni Hadithi ambayo inaonesha kuwa imefika kwa Mtume ﷺ ama kwa vitendo, maneno kwa kuwa imeunganika moja kwa moja. Anaendelea Aliyetukuka:

لَوْلَا أَن مِّنَ اللَّهِ عَلَيْنَا لَخَسَفَ بِنَا

“Ingelikuwa Allah Hakutufanyia hisani Angelitudidimiza”.

Lau si Upole Wake kwetu sisi na Hisani Yake Angetudidimiza kama Alivyomdidimiza, kwani tulitamani na kutaka kuwa kama yeye.

لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ ﴿٨٣﴾

“Kumbe makafiri hawafanikiwi!”

Wanamaanisha kuwa yeye alikuwa kafiri wala hawafaulu makafiri mbele ya Allah تعالى, si hapa duniani wala Kesho Akhera.

تِلْكَ الدَّارُ الْآخِرَةُ نَجْعَلُهَا لِلَّذِينَ لَا يُرِيدُونَ عُلُوًّا فِي الْأَرْضِ وَلَا فَسَادًا وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٨٤﴾
 مَن جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ خَيْرٌ مِّنْهَا ۖ وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَى الَّذِينَ عَمِلُوا
 السَّيِّئَاتِ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾

83. Hayo ndiyo makazi ya Akhera, Tumewafanyia wale wasiotaka kujitukuza duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wachamungu.

84. Atakayetenda wema atapata malipo bora kuliko huo wema alioutenda. Na atakayetenda uovu, hawalipwi watendao uovu ila waliyokuwa wakiyatenda”.

¹ Ahmad; 1:387 Isnadi yake ni dhaifu. Udhaifu wake ni kutokana mpokezi Assabah Muhammadi Al-Bajali. Al-Hafidh bin Hajar amesema: Ni mtu dhaifu.Taz (Takribu).

Neema za Akhera ni za Waumini Wanyenyekevu

Allah Aliyetukuka Anatueleza kuwa nyumba ya Akhera na neema zake za milele zizizokwisha wala kubadilika, ni kwa wale waja Wake Waumini wanyenyekevu wasiopenda kujitukuza katika ardhi, kwa kujinyanyua na kujitukuza juu ya viumbe vya Allah تعالى, kuwanyanyasa kwa kiburi na kueneza ufisadi baina yao. Amesema 'Ikrimah: "Al-'Uluwni majivuno na kiburi."¹ Amesema Ibn Jurayj:

لَا يُرِيدُونَ غُلُوقًا فِي الْأَرْضِ

"Wale wasiotaka kujitukuza duniani." Kujitukuza, kiburi na udhalimu, 'Wala ufisadi', kufanya maasiya na madhambi.² Ibn Jariir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa 'Aliy رضي الله عنه amesema: "Hakika mtu huwa anataka kanda za viatu vyake ziwe bora kuliko kanda za sahibu yake, hivyo anaingia katika Kauli ya Aliyetukuka:

تِلْكَ أَلْدَاوُ الْأَخِرَةُ جَعَلَهَا لِلَّذِينَ لَا يُرِيدُونَ غُلُوقًا فِي الْأَرْضِ وَلَا فُسَادًا³ وَالْعَقِيبَةُ

لِلْمُتَّقِينَ

"Hayo ndiyo makazi ya Akhera, Tumewafanyia wale wasiotaka kujitukuza duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wachamngu."³

Hii inafahamika kumaanisha kuwa ikiwa nia yake ni kujionesha na kuonekana vizuri kuliko wengine, basi hilo limeshutumiwa vikali. Imethibitika katika Hadithi Sahihi kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّهُ أَوْجِي إِلَيَّ أَنْ تَرَاضَعُوا حَتَّى لَا يَفْخَرَ أَحَدٌ عَلَى أَحَدٍ وَلَا يَتَّبِعِي أَحَدٌ عَلَى أَحَدٍ»

"Hakika nimefunuliwa kuwa mnyenyekee kwa kiasi ambacho hakuna yeyote ambaye atajivuna kwa wengine wala mmoja wenu asimdhulumu mwengine."⁴

¹ Atw-Twabariy 19: 637.

² Atw-Twabariy 19: 637.

³ Atw-Twabariy 19: 638. Isnadi yake ni dhaifu kuna Ash'at bin Said Al-Basri ni dhaifu. Na Abuu Salman Al-Araj kutoka kwa Ali ni *Mursal*.

⁴ Muslim 4/2199.

Ama mtu akipenda hilo kwa kuonekana mzuri na wa kupendeza, kufanya hivyo hakutakuwa na tatizo lolote. Imethibiti kuwa mtu mmoja alisema: “Ewe Mtume wa Allah! Hakika mimi napenda nguo yangu iwe nzuri, na viatu vyangu viwe vizuri – je, hiyo ni aina ya kiburi?” Akasema:

«لَا، إِنَّ اللَّهَ جَمِيلٌ يُحِبُّ الْجَمَالَ»

“Hapana! Hakika Allah ni Mzuri na Anapenda uzuri”¹

Na Amesema Aliyetukuka:

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ

“...Atakayetenda wema,”

Maana yake: Siku ya Kiyama,

فَلَهُ خَيْرٌ مِّمَّا

“Atapata malipo bora kuliko huo wema alioutenda.”

Hii inamaanisha thawabu kutoka kwa Allah تعالى ni bora kuliko amali njema ya mja Wake, na kwa nini isiwe hivyo, kwani Allah تعالى Huongeza maradufu juu yake? Hii ni ile nafasi ya Ukarimu na Fadhila kutoka kwa Allah تعالى.

Kisha Anasema:

وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُحْزَى الَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٤﴾

“Na atakayetenda uovu, hawalipwi watendao uovu ila waliyokuwa wakiyatenda.”

وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَكُبَّتْ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ هَلْ تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٥﴾

“Na watakoleta ubaya, basi zitasinukishwa nyuso zao Motoni waambiwe: ‘Kwani mnalipwa isipokuwa yale mliyokuwa mkiyatenda?’ (27:90).”

Hii ni nafasi ya fadhila na uadilifu

¹ Muslim 1:93.

إِنَّ الَّذِي فَرَضَ عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لَرَأْدُكَ إِلَى مَعَادٍ قُل رَّبِّي أَعْلَمُ مَنْ جَاءَ بِأَهْدَى
 وَمَنْ هُوَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٨٥﴾ وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَنْ يُلْقَى إِلَيْكَ الْكِتَابُ إِلَّا رَحْمَةً مِنْ
 رَبِّكَ ۗ فَلَا تَكُونَنَّ ظَهِيرًا لِلْكَافِرِينَ ﴿٨٦﴾ وَلَا يَصُدُّكَ عَنْ آيَاتِ اللَّهِ بَعْدَ إِذْ أَنْزَلَتْ
 إِلَيْكَ ۗ وَادْعُ إِلَى رَبِّكَ ۗ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٨٧﴾ وَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ
 لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ ۗ لَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٨﴾

85. Hakika Aliyekulazimisha kuifuata Qur'ani hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo. Sema: Mola wangu Mlezi Ndiye Anayemjua zaidi mwenye kuja na uwongofu, na nani aliyomo katika upotofu ulio dhahiri.

86. Nawe hukuwa unataraji kuletewa Kitabu; lakini ni rehema tu ya Mola wako Mlezi. Basi usiwe msaidizi wa makafiri.

87. Wala wasikuzuie kuzifuata Ayah za Allah baada ya kuteremshiwa wewe. Na lingania kwa Mola wako Mlezi, wala usiwe miongoni mwa washirikina.

88. Wala usimwombe pamoja na Allah mungu mwinginewe. Hapana mungu ila Yeye. Kila kitu kitaangamia isipokuwa Dhati Yake. Hukumu iko Kwake, na Kwake mtarejezwa”.

Amri ya Kufikisha Ujumbe wa Tawhiidi

Allah تعالیٰ Anamuamuru Mtume Wake kufikisha ujumbe na kuwasomea watu Qur'ani. Anaambiwa kuwa atarudishwa tena pahala pa marejeo, nayo ni Siku ya Kiyama, ambapo ataulizwa kuhusu aliyopaswa kuyachunga katika majukumu ya utume:

إِنَّ الَّذِي فَرَضَ عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لَرَأْدُكَ إِلَى مَعَادٍ

“Hakika Aliyekulazimisha kuifuata Qur'ani hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo”.

Maana yake: Amekufaradhia kuitekeleza kwa watu,

لَرَأْدُكَ إِلَى مَعَادٍ

“Hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo”.

Siku ya Kiyama Atamuuliza kuhusu hilo, kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَلَنَسْأَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْأَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ ﴿٦٩﴾

“Na kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekwa Mitume, na pia Tutawauliza (Mitume) waliopelekwa.” (7:6).

Amesema tena Aliyetukuka:

* يَوْمَ تَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ^ط

“Siku ambayo Allah Atawakunsanya Mitume Awaambie: ‘Mlijibiwa nini?’” (5:109).

Amesema tena Aliyetukuka:

وَجَاءَءَ بِالنَّبِيِّنَ وَالشَّهَادَاتِ

“Na wataletwa Manabii na mashahidi”. (39:69)

Bukhaariy amemnukuu Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما katika Sahihi yake akisema kuhusu Tafsiri ya Aya hii:

لَرَأْدُكَ إِلَى مَعَادٍ

“Hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo”.

Imamu Bukhari katika sahihi yake amenukuu maelezo ya Aya kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنهما; Akasema: “Kurudi Makkah”¹. Na hivyo ndivyo alivyopokea an-Nasaa’iy katika Tafsiri ya Sunan yake², na Ibn Jariir رحمه الله تعالى³. Al-‘Awfiy naye amepokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما mfano wa hivyo katika ibara ya Aya hii:

¹Fat’h al-Baariy 8:369.

²An-Nasaa’iy katika al-Kubraa 6:425.

³At-Tabari 19:641.

لَرَأْدُكَ إِلَىٰ مَعَادٍ

“Hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo.”

Maana yake: Atakurudisha Makkah kama Alivyokutoa humo.¹ Amepokea Muhammad ibn Ishaq رحمه الله تعالى kuwa Mujaahid amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake:

لَرَأْدُكَ إِلَىٰ مَعَادٍ

“Hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo’.

“Atakurudisha ulipozaliwa, Makkah.”² Na amefasiri Ibn ‘Abbaas رضي الله عنه mara nyingine, kwa Kauli Yake Aliyetukuka: “Hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo”, yaani mauti. Pia ameifasiri mara nyingine kwa Siku ya Kiyama ambayo inakuja baada ya mauti, na mara nyingine kuwa ni Pepo ambayo itakuwa ni malipo na mashukio yake kwa kutekeleza ujumbe wa Allah تعالى na kuufikisha kwa viumbe aina mbili, Majini na binadamu. Hii ni kwa sababu yeye ni mkamilifu zaidi wa waja wa Allah تعالى, fasaha, na ni mtukufu zaidi wa viumbe vyote vya Allah تعالى. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

قُلْ رَبِّيَ أَعْلَمُ مَنْ جَاءَ بِأَهْدَىٰ وَمَنْ هُوَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٨﴾

“Sema: Mola wangu Mlezi Ndiye Anayemjua zaidi mwenye kuja na uwongofu, na nani aliyomo katika upotofu uliodhahiri.”

Inamaanisha kuwa ewe Muhammad waambie wapinzani wako na waliokukadhibisha katika watu wako washirikina na wanaowafuata katika kufuru. “Mola wangu Mlezi Anawajua walioongoka kati yenu na mimi, hakika mtakuja jua nani kati yetu atakayekuwa na mwisho (Akhera) mwema wa furaha. Pia nani kati yetu atakuwa na mwisho mzuri na ushindi hapa duniani na Kesho akhera.” Kisha Alisema Aliyetukuka kumkumbusha Nabii Wake, Neema Zake nyingi Alizompa yeye pamoja na waja Wake pale Alipompeleka kwao:

وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَنْ يُلْقَىٰ إِلَيْكَ الْكِتَابُ

“Nawe hukuwa unataraji kuletewa Kitabu”.

¹ Atw-Twabariy 19:641.

² Atw-Twabariy 19:641.

Maana yake: Hukudhania kabla kuteremshiwa Wahyi kuwa ufunuo (Wahyi) huo utateremshwa kwako.

إِلَّا رَحْمَةً مِنْ رَبِّكَ

“Lakini, “Ni rehema tu ya Mola wako Mlezi.”

Hii ina maana kuwa hakika Allah تعالى Alikuteremshia Wahyi kwa Rehema Yake kwako na kwa waja kwa sababu yako. Kwa vile Allah تعالى Amekupatia Neema hii kubwa:

فَلَا تَكُونَنَّ ظَهِيرًا

“Basi usiwe msaidizi”.

Maana yake: Mwenye kuwasaidia, kuwapa nguvu na kuwasitiri.

لِلْكَافِرِينَ

“Wa Makafiri”.

Lakini tengana nao, pambana na upingane nao.

وَلَا يَصُدُّنَكَ عَنْ آيَاتِ اللَّهِ بَعْدَ إِذْ أَنْزَلْتُ إِلَيْكَ

“Wala wasikuzuie kuzifuata Ayah za Allah baada ya kuteremshiwa wewe.”

Hii inamaanisha kuwa usiathirike kwa kukhitilafiana na wewe na kuwazuia kwao watu katika kufuata njia yako; usitie wasiwasi kwa hilo wala usijali. Hakika Allah تعالى Atalifanya neno lako liwe juu, Ataiunga Mkono Dini yako na Ataudhirisha ujumbe Aliokutuma kuwa juu ya dini zote.

وَأَدْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ

“Na lingania kwa Mola wako Mlezi.”

Katika kuabudiwa Mola wako Mlezi Peke Yake, asiye na mshirika kabisa,

وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

“Wala usiwe miongoni mwa washirikina.”

وَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Wala usimwombe pamoja na Allah mungu mwenginewe. Hapana mungu ila Yeye.”

Hii ina maana kuwa haifai kuabudu chochote au yeyote ila Yeye, wala Uungu haumfai yeyote isipokuwa Utukufu Wake. Na Kauli Yake:

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ

“Kila kitu kitaangamia isipokuwa Dhati Yake.”

Hapa Allah تعالى Anatueleza na Kutufahamisha kuwa Yeye Atabaki daima dawamu, Mwenye Kubaki, na Mwenye Uhai wa milele na Mwendeshaji wa mambo yote (na Msimamia wa kila jambo), japokuwa viumbe Vyake vyote vitakufa lakini Yeye Hafi kabisa, kama Alivyosema Aliyetukuka:

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٦٧﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٦٨﴾

“Kila kilichoko juu yake (ardhi na mbingu) kitatoweka. Inabaki Dhati ya Mola wako Mlezi Mwenye Utukufu na Heshima.” (55:26- 27).

Allah تعالى Ametumia neno ‘**Wajhuhu**’ “**Uso Wake**” kumaanisha Dhati Yake (Maana yake: Yeye Mwenyewe), kama ilivyo Kauli Yake hapa:

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ

“Kila kitu kitaangamia isipokuwa Dhati Yake.”

Yaani: Isipokuwa Yeye. Imenukuliwa katika Hadithi Sahihi kwa njia ya Abu Salamah رضي الله عنه kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, amesema Mtume ﷺ:

«أَصْدَقَ كَلِمَةٍ قَالَهَا الشَّاعِرُ لَيْدٌ - أَلَا كُلُّ شَيْءٍ مَا خَلَا اللَّهَ بَاطِلٌ -»

“Neno la ukweli kabisa ni lile alilosema mshairi Labiid: ‘Tambua kuwa kila kitu mbali na Allah ni batili (uwongo).’¹

¹ Fat’h al-Baariy 7:183.

لَهُ الْحُكْمُ

“Hukumu iko Kwake.”

Maana yake: Ufalme na Udhibiti, na hakuna anayeweza kuipindua Hukumu au Uamuzi Wake. Pia,

وَالِيهِ تُرْجَعُونَ

“Na Kwake mtarejzwa.”

Maana yake: Siku ya marejeo yenu, na Atakulipeni kwa amali zenu mlizofanya: ikiwa ni amali nzuri basi mtalipwa mema na ikiwa ni amali mbaya basi itakuwa ni shari juu yao (hivyo kuadhibiwa).

Huu ndio mwisho wa Tafsiri ya *Suratul Qasas*, na Allah تعالی Ndiye Mwenye Kusifiwa na Kushukuriwa.

* * *

Tafsiri ya Suratul 'Ankabut

Sura ya 29

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْعَنْكَبُوتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْم ۝ أَحْسِبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ۝ وَلَقَدْ فَتَنَّا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۖ فَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْكٰذِبِينَ ۝ أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ أَنْ يَسْفُقُونَا ۖ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ۝ مَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ اللَّهِ فَإِنْ أَجَلَ اللَّهُ لَاتِ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۝ وَمَنْ جَاهَدَ فَإِنَّمَا يُجَاهِدُ لِنَفْسِهِ ۖ إِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ عَنِ الْعٰلَمِينَ ۝ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحٰتِ لَنُكَفِّرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَحْسَنَ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ۝ وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ حُسْنًا ۖ وَإِنْ جَاهَدَاكَ لِتُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۖ إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ فَأُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ۝ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحٰتِ لَنُدْخِلَنَّهُمْ فِي الصَّٰلِحِينَ ۝

الْم ۝ أَحْسِبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ۝ وَلَقَدْ فَتَنَّا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۖ فَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْكٰذِبِينَ ۝ أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ أَنْ يَسْفُقُونَا ۖ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ۝

1. "Alif Lam Mim (A.L.M.)"

2. "Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe?"

3. "Hakika Tuliwajaribu waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu Atawatambulisha walio wa kweli na Atawatambulisha walio waongo."

**4. “Au wanadhani wanaotenda maovu kwamba watatushinda?
Hukumu mbaya hiyo wanayohukumu.”**

Waumini Hujaribiwa Mpaka Ajulikane Mkweli na Mwongo

Maelezo juu ya herufi za mkato yameshatangulia mwanzoni mwa baadhi ya Sura. Kauli ya Allah تعالى،

أَحْسِبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكُوا أَنْ يَقُولُوا ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿١٤٤﴾

**“Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema:
Tumeamini. Nao wasijaribiwe?”**

Hili ni kanusho kwa njia ya swali, na maana yake ni kwamba, bila shaka, Allah تعالى Atawajaribu waja Wake Waumini kulingana na kiasi cha Imani waliyo nayo. Ni kama ilivyokuja katika Hadithi *Sahih*:

«أَشَدُّ النَّاسِ بَلَاءَ الْأَنْبِيَاءِ، ثُمَّ الصَّالِحُونَ، ثُمَّ الْأَمْثَلُ فَأَلْأَمْثَلُ، يَنْتَلِي الرَّجُلُ عَلَى حَسَبِ دِينِهِ، فَإِنْ كَانَ فِي دِينِهِ صَلَابَةٌ زِيدَ لَهُ فِي الْبَلَاءِ»

“Watu waliopewa mitihani mikali sana ni Mitume, kisha waja wema, kisha waliofuatia kwa ubora, kisha waliofuatia. Mtu hufanyiwa mitihani kulingana na utekelezaji wake wa kidini, kadiri utekelezaji wake wa Dini unavyokuwa mkubwa ndivyo mitihani nayo inavyokuwa mikubwa zaidi.”¹

Aya hiyo ni sawa na Kauli nyingine ya Allah،

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُدْخَلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٥﴾

**“Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu
Hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na
Hajawapambanua waliosubiri?” (3:142)**

Na mithili yake katika Surat Al-Baraa. Pia Allah تعالى Amesema katika Al-Baqarah،

¹ Tirmidh: (3298) Ahmad: 1/172.

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ^ط مَسَّيْتُمْ الْبَاسَاءَ
وَالضَّرَّاءَ وَزُلْزِلُوا حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصُرُ اللَّهُ^ط أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ

قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

“Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyowajia wale waliopita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Lini Nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa Nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu.” (2:214)

Kwa minajili hii, Allah تعالى Amesema hapa,

وَلَقَدْ فَتَنَّا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ^ط فَلْيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ صَدَقُوا وَلْيَعْلَمَنَّ الْكٰذِبِينَ ﴿٢١٤﴾

“Hakika Tuliwajaribu waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu Atawatambulisha walio wa kweli na Atawatambulisha walio waongo.”

Maana yake: Waliousadikisha wito wa Uislamu dhidi ya wenye kukadhibisha kauli na ulingano Wake. Juu ya yote, Allah تعالى Anayajua yaliyotukia na yanayojiri na namna ambavyo yangelikuwa yale ambayo hayakutendeka, iwapo yangelifanyika. Haya yanakubalika kwa maimamu wote wa *Sunnah wal-Jamaah*. Hii ndio rai ya Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na wengine, kuhusu Kauli ya Allah تعالى kama vile,

إِلَّا لِنَعْلَمَ

“...ila Tupate kumjua...” (2:143)¹

Isipokuwa ili Tuone, na hilo ni kwa sababu kuona kunaambatana na vilivyopo, na kujua ni kupana zaidi kuliko kuona, kwani inajumuisha chenye kukosekana na kupatikana.

¹ Aya hizi mara nyinyi hutafsiriwa kwa maana ya “mitihani” badala ya “atajua.” Zitambulike kwa maana zake kwa ujumla, pia na maelezo ya hapo juu.

Waovu Hawataweza Kumtoroka Allah تعالى.

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ أَنْ يَسْبِقُونَا ۗ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿١٠﴾

**“Au wanadhani wanao tenda maovu kwamba watatushinda?
Hukumu mbaya hiyo wanayo hukumu.”**

Maana yake: Wale ambao hawajaingia katika Imani, wasidhani kwamba watanusurika katika *Fitnah* na mtihani huu, kwani nyuma yao kuna adhabu nzito na kali zaidi kuliko mtihani huu. Kwa ajili hii Amesema,

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ أَنْ يَسْبِقُونَا

“Au wanadhani wanaotenda maovu kwamba watatushinda?”

Maana yake: Kututoroka,

سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿١١﴾

“Hukumu mbaya hiyo wanayo hukumu.”

Maana yake: Ni vibaya wanavyodhanika.

مَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ اللَّهِ فَإِنَّ أَجَلَ اللَّهِ لَآتٍ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢﴾ وَمَنْ جَاهَدَ فَإِنَّمَا يُجَاهِدُ لِنَفْسِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿١٣﴾ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُكَفِّرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَحْسَنَ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

5. “Mwenye kutaraji kukutana na Mwenyezi Mungu, basi hakika miadi ya Mwenyezi Mungu itafika bila ya shaka. Naye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

6. “Na anayefanya juhudi basi bila ya shaka anafanya juhudi kwa ajili ya nafsi yake. Hakika Mwenyezi Mungu si mhitaji wa walimwengu.”

7. “Na walioamini na wakatenda mema, kwa yakini Tutawafutia makosa yao, na Tutawalipa bora ya waliyokuwa wakiyatenda.”

Allah تعالی Atayatimiza Matarajio ya Waja Wema

Allah تعالی Anasema,

مَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ اللَّهِ

“Mwenye kutaraji kukutana na Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Katika Akhera na akatenda amali njema na kutarajia kupata malipo makubwa kutoka kwa Allah تعالی, basi Allah تعالی Atamtimizia matumaini yake na Atamlipa amali zake kwa ukamilifu na kwa wingi. Hilo, bila shaka, litajiri, kwani Yeye ni Mwenye Kusikia dua, ni Mwenye Kuyaona mahitaji ya kila jambo. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

مَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ اللَّهِ فَإِنَّ أَجَلَ اللَّهِ لَآتٍ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٤٦﴾

“Mwenye kutaraji kukutana na Mwenyezi Mungu, basi hakika Miadi ya Mwenyezi Mungu itafika bila ya shaka. Naye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.”

وَمَنْ جَاهَدَ فَإِنَّمَا يُجَاهِدُ لِنَفْسِهِ

“Na anayefanya juhudi basi bila ya shaka anafanya juhudi kwa ajili ya nafsi yake...”

Na Kauli nyingine:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ

“Anayetenda mema basi anajitendea mwenyewe nafsi yake...”
(41:46)

Maana yake: Katika amali njema, kwamba manufaa ya amali yake yanarejea kwake mwenyewe, kwani Allah تعالی si Mwenye haja ya matendo ya waja, na lau wote wangelikuwa na uchamungu sawa na wa moyo wa mtu mchamungu wao zaidi, basi hilo lisingezidisha chochote katika Ufalme Wake.

وَمَنْ جَاهَدَ فَإِنَّمَا يُجَاهِدُ لِنَفْسِهِ إِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾

“Na anayefanya juhudi basi bila ya shaka anafanya juhudi kwa ajili ya nafsi yake. Hakika Mwenyezi Mungu si mhitaji wa walimwengu.”

Kisha, Allah تعالی Ameeleza kwamba, pamoja na Kujitosheleza Kwake kwa viumbe wote, pamoja na Ukarimu na Hisani Yake kwao, Huwalipa Waumini jaza njema kabisa, na kwamba Atawasamehe makosa waliyoyatenda na Kuwapa malipo kwa mema waliyoyafanya. Atalipokea hata jambo dogo jema na Kulilipa kila moja mara kumi ya mfano wake, mpaka mara mia saba. Pia, Hulipa ovu kwa ovu mfano wake au Husamehe na Kulifuta, Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِن لَّدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye Hulizidisha na Hutoa kutoka Kwake malipo makubwa.” (4:40)

Kwa hivyo, Allah تعالی Amesema hapa,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُكَفِّرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَحْسَنَ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾

“Na walioamini na wakatenda mema, kwa yakini Tutawafutia makosa yao, na Tutawalipa bora ya waliyokuwa wakiyatenda.”

وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ حُسْنًا ۖ وَإِن جَاهَدَاكَ لِتُشْرَكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۖ إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ فَأُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣١﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُدْخِلَنَّهُمْ فِي الصَّالِحِينَ ﴿٣٢﴾

8. “Na Tumemuusia mwanaadamu kuwafanyia wema wazazi wake. Na ikiwa watakushikilia unishirikishe Mimi na usiyokuwa na ujuzi nayo, basi usiwatii.

9. Na walioamini na wakatenda mema, bila ya shaka Tutawatia miongoni mwa watu wema.

Amri ya Kuwafanyia Ihsani Wazazi

Allah تعالى Anawaamuru waja wake wawafanyie ihsani wazazi wao, baada ya Kuwahimiza juu ya kushikamana na kumpwekesha, kwani wazazi wawili ndio sababu ya kupatikana kwa mtu, kwa hivyo, anatakiwa awafanyie upeo wa ihsani, baba, kwa minajili ya kumkimu na mama yake kwa kumfanyia huruma. kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema,

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَيَالِ الَّذِينَ إِحْسَنًا ۖ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ وَلَا تَنْهَرَهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَأَخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذَّلِيلِ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾ ﴾

“Na Mola wako Mlezi Aameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemu wa hishima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyonilea utotoni.” (17:23-24)

Pamoja na wasia huu kuhusu huruma na ihsani kwao kama malipo na ihsani yao (Kwake), Allah تعالى Amesema,

﴿ وَإِنْ جَاهِدَاكَ لِتُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۗ

“Na ikiwa watakushikilia unishirikishe Mimi na usiyokuwa na ujuzi nayo, basi usiwatii.”

Maana yake: Ikiwa watakusisitiza kwamba uwafuate katika dini yao, kama ni washirikina basi jihadhari nao, usiwatii katika hilo, kwani marejeo yenu ni Kwangu, katika Siku ya Kiyama. Nam Nitakulipa kwa ihsani yako kwao na subira yako katika Dini yako, na Nitakujumuisha pamoja na waja wema, si katika kundi la wazazi wako, japokuwa ulikuwa mtu wao wa karibu sana duniani, kwani mtu atafufuliwa katika Siku ya Kiyama pamoja na awapendao, yaani mapenzi ya kidini. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُدْخِلَنَّهُمْ فِي الصَّالِحِينَ ﴿١٠﴾

“Na walioamini na wakatenda mema, bila ya shaka Tutawatia miongoni mwa watu wema.”

Katika kuitafsiri Aya hii, At-Tirmidhi alisimulia kutoka kwa Sa'd رضي الله عنه, amesema: “Aya nne ziliteremshwa kunihusu mimi. Akakitaja kisa, akasema: Mama Sa'd amesema: “Je, Allah تعالى Hakukuamrisha kufanya wema? Wallah! Sili wala sinywi mpaka nifariki dunia, vinginevyo kufuru.” Ameendelea kusema: Ikawa walipotaka kumlisha walimamanua kinywa chake kifunguke. Ikashuka Aya:

وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ حُسْنًا ۖ وَإِنْ جَاهَدَاكَ لِتُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا

“Na Tumemuusia mwanaadamu kuwafanyia wema wazazi wake. Na ikiwa watakushikilia unishirikishe Mimi na usiyokuwa na ujuzi nayo, basi usiwatii.”¹

Hadithi hii ilinukuliwa pia na Imamu Ahmad, Muslim, Abu Dawud na An-Nasai.² At-Tirmidhi amesema, *“Hasan Sahih.”*

* * *

¹ Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:48.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ فَإِذَا أُوذِيَ فِي اللَّهِ جَعَلَ
 فِتْنَةَ النَّاسِ كَعَذَابِ اللَّهِ وَلَئِن جَاءَ نَصْرٌ مِّن رَّبِّكَ لَيَقُولُنَّ
 إِنَّا كُنَّا مَعَكُمْ ؕ أَوَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِمَا فِي صُدُورِ
 الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾ وَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَيَعْلَمَنَّ
 الْمُنْفِقِينَ ﴿١١﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا
 اتَّبِعُوا سَبِيلَنَا وَلْنَحْمِلْ خَطِيئَتَكُمْ وَمَا هُمْ بِحَامِلِينَ مِنْ
 خَطِيئَتِهِمْ مِن شَيْءٍ ؕ إِنَّهُمْ لَكَذِبُونَ ﴿١٢﴾ وَلَيَحْمِلُنَّ
 أَثْقَاهُمْ وَأَثْقَالًا مَّعَ أَثْقَالِهِمْ ؕ وَلَيَسْئَلُنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَمَّا
 كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٣﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ
 فَلَبِثَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ عَامًا فَأَخَذَهُمُ
 الطُّوفَانُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٤﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَصْحَبَ
 السَّفِينَةَ وَجَعَلْنَاهَا ءَايَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٥﴾ وَإِبْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ
 لِقَوْمِهِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ
 تَعْلَمُونَ ﴿١٦﴾ إِنَّمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا
 وَتَخْلُقُونَ إِفْكًا ؕ إِنَّ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ لَا
 يَمْلِكُونَ لَكُمْ رِزْقًا فَابْتَغُوا عِنْدَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ
 وَأَشْكُرُوا لَهُ ؕ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿١٧﴾ وَإِن تَكْذِبُوا فَقَدْ
 كَذَّبَ أُمَمٌ مِّن قَبْلِكُمْ ؕ وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلْغُ
 الْمُبِينُ ﴿١٨﴾

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ
 فَإِذَا أُوذِيَ فِي اللَّهِ جَعَلَ فِتْنَةَ النَّاسِ
 كَعَذَابِ اللَّهِ وَلَئِن جَاءَ نَصْرٌ مِّن
 رَّبِّكَ لَيَقُولُنَّ إِنَّا كُنَّا مَعَكُمْ ؕ
 أَوَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِمَا فِي صُدُورِ
 الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾ وَلَيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَلَيَعْلَمَنَّ الْمُنْفِقِينَ ﴿١١﴾

10. "Na katika watu wapo wanaosema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu. Lakini wanapopewa maudhi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wanayafanya mateso ya watu kama ni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na inapokuja nusura kutoka kwa Mola wako Mlezi husema: Hakika sisi tulikuwa pamoja nanyi. Kwani Mwenyezi Mungu Hayajui yaliomo vifuani mwa walimwengu?"

11. "Na hapana shaka Mwenyezi Mungu Atawatambulisha walioamini, na Atawatambulisha wana-fiki."

Tabia za Wanafiki na Mwenendo wa Allah تعالی katika Kuwajaribu Watu

Allah تعالی Anaeleza sifa za kaumu ya wakadhibishaji ambao wanatamka imani kwa ndimi zao, ilhali imani haijaimarika katika nyoyo zao, kwamba watakapojiwa na mtihani au jaribio likiwajia duniani, basi hudhani kwamba hii ni nakama ya Allah تعالی kwao, nao huritadi. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ فَإِذَا أُوذِيَ فِي اللَّهِ جَعَلَ فِتْنَةَ النَّاسِ كَعَذَابِ اللَّهِ

“Na katika watu wapo wanaosema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu. Lakini wanapopewa maudhi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wanayafanya mateso ya watu kama ni Adhabu ya Mwenyezi Mungu.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: “Maana yake, mtihani ni kuritadi dini yake ikiwa atasumbuliwa kwa ajili ya Allah تعالی.”² Hii pia ilikuwa rai ya *Salaf* wengine. Aya hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ فَإِنْ أَصَابَهُ خَيْرٌ اطْمَأَنَّ بِهِ ۗ وَإِنْ أَصَابَتْهُ فِتْنَةٌ انْقَلَبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ

“Na katika watu wapo wanaomuabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni. Ikimfikia kheri hutulia kwayo, na ukimfikia msukosuko hugeza uso wake.”

Mpaka katika Kauli Yake,

ذَٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿١١﴾

“Huko ndiko kupotolea mbali!” (22:11-12),

Kisha, Allah تعالی Amesema:

وَلَيْنَ جَاءَ نَصْرٌ مِّن رَّبِّكَ لَيَقُولَنَّ إِنَّا كُنَّا مَعَكُمْ

“Na inapokuja nusura kutoka kwa Mola wako Mlezi husema: Hakika sisi tulikuwa pamoja nanyi.”

¹ Ahmad 1:181, Muslim 4:1877, Abu Dawud 3:177, An-Nasi katika Al-Kubra 6:348.

² Atw-Twabarīy 20: 13

Maana yake: Hata ikija nusura ya karibu kutoka kwa Mola wako, ewe Muhammad ﷺ, ushindi na ghanima nyingi, watakuambieni: "Sisi tulikuwa pamoja nanyi, yaani ndugu zenu katika dini." Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ بِكُمُ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ فَتْحٌ مِّنَ اللَّهِ قَالُوا أَلَمْ نَكُن مَّعَكُمْ وَإِنْ كَانَ لِلْكَافِرِينَ
نَصِيبٌ قَالُوا أَلَمْ نَسْتَحْوِذْ عَلَيْكُمْ وَنَمْنَعُكُم مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ

"Wale ambao wanakungojeeni, mkipata ushindi unaotoka kwa Mwenyezi Mungu wao husema: Si tulikuwa pamoja nanyi vile? Na ikiwa ni sehemu ya makafiri kushinda wao huwaambia: Hatukuwa ni waweza wa kukushideni, nasi tukakulingeni na hawa Waumini?." (4:141)

Allah تعالى Amesema;

فَعَسَى اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِنْدِهِ فَيُضْبِحُوا عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي أَنْفُسِهِمْ
تَنْدِيمٍ

"Huenda Mwenyezi Mungu Akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake wakawa wenye kujuta kwa waliyoyaficha katika nafsi zao." (5:52)

Allah تعالى Anapasha khabari kuwahu wao,

وَلِئِنْ جَاءَ نَصْرٌ مِّنَ رَبِّكَ لَيَقُولُنَّ إِنَّا كُنَّا مَعَكُمْ

"Na inapokuja nusura kutoka kwa Mola wako Mlezi husema: Hakika sisi tulikuwa pamoja nanyi.""

Kisha, Allah تعالى Akasema:

أَوَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِمَا فِي صُدُورِ الْعَالَمِينَ

"Kwani Mwenyezi Mungu Hayajui yaliomo vifuani mwa walimwengu?"

Maana yake: Kwani Allah تعالى Hayajui yaliyo nyoyoni mwao na kilichohifadhiwa na dhamira zao, japokuwa watadhihirisha kuwafikiana nanyi. Kauli ya Allah تعالى,

وَلْيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلْيَعْلَمَنَّ الْمُنْفِقِينَ ﴿١٠﴾

“Na hapana shaka Mwenyezi Mungu Atawatambulisha walioamini, na Atawatambulisha wanafiki.”

Maana yake: Hakika Allah تعالى Atawatahini watu kwa taabu na faraja, ili Apambanue baina ya hawa na hawa, baina ya wenye kumtii Allah تعالى kipindi cha taabu na cha faraja dhidi ya wanaomtii kulingana na utashi wao.

Na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجْتَهِدِينَ مِنكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَنَبْلُوَنَّكُمْ أَخْبَارَكُمْ ﴿٣١﴾

“Na bila ya shaka Tutakujaribuni mpaka Tuwadhihirishe wapiganao Jihadi katika nyinyi na wanaosubiri. Nasi Tutazifanyia mtihani khabari zenu.” (47:31)

Allah تعالى Amesema tena baada ya tukio la Uhud ambalo liliambatana na majaribio na mitihani:

مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ

“Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyonyo mpaka Apambanue wabaya na wema.” (3:179)

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّبِعُوا سَبِيلَنَا وَلْنَحْمِلْ خَطِيئَتَكُمْ وَمَا هُمْ بِحَامِلِينَ ﴿٣١﴾ مِنْ خَطِيئَتِهِمْ مِنْ شَيْءٍ إِنَّهُمْ لَكَذِبُونَ ﴿٣٢﴾ وَلَيَحْمِلُنَّ أَثْقَاهُمْ وَأَثْقَالًا مَّعَ أَثْقَالِهِمْ ۗ وَلَيَسْئَلَنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٣٣﴾

12. “Na waliokufuru waliwaambia walioamini: Fuateni njia yetu, nasi tutayabeba makosa yenu. Wala wao hawatabeba katika makosa yao chochote kile. Hakika hao ni waongo.”

13. “Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao. Na kwa yakini wataulizwa Siku ya Kiyama juu ya waliyokuwa wakiyazua.”

Ujasiri wa Makafiri kwamba Watabeba Madhambi ya Wengine Ikiwa Wataritadi

Allah تعالى Anaeleza kuhusu makafiri wa Kikuraishi kwamba waliwaambia wale walioamini miongoni mwao na wakafuata hidaya: “Tokeni katika dini yenu na mrejee katika dini yetu, na muifuate njia yetu.”

وَلَنَحْمِلَ خَطِيئَتَكُمْ

“...nasi tutayabeba makosa yenu.”

Maana yake: Madhambi yenu, ikiwa mnayo kwa kufanya hivyo, yawe juu yetu, na yatakuwa ni jukumu letu sisi.

Allah تعالى Aliwakadhibisha hao kwa Kusema:

وَمَا هُمْ بِحَامِلِينَ مِنْ خَطِيئَتِهِمْ مِنْ شَيْءٍ إِنَّهُمْ لَكَذِبُونَ ﴿١٧﴾

“Wala wao hawatabeba katika makosa yao chochote kile. Hakika hao ni waongo.”

Maana yake: Kuhusu waliyoyasema kwamba watayabeba madhambi yao, kwani hapana wa kubeba mizigo ya mwingine.

Allah تعالى Amesema:

وَأَنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمَلِهَا لَا تُحْمَلُ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ

“Na aliyetopewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe hauta-chukuliwa hata kidogo, na hata angemuomba jamaa yake.” (35:18)

وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿١٠﴾ يُبْصِرُونَ ﴿١١﴾

“Wala jamaa hatamuuliza jamaa yake. Ijapokuwa wataoneshwa waonane.” (70:10-11).

وَلَيَحْمِلُنَّ أَثْقَالَهُمْ وَأَنْفَالَهُمْ مَعَ أَثْقَالِهِمْ

“Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao.”

Ni kutoa khabari kuhusu wanaolingania kwenye ukafiri na upotevu, kwamba katika Siku ya Kiyama watabeba mizigo yao na mizigo mingine kwa sababu ya kuwapoteza watu, bila ya kupunguza chochote katika mizigo yao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ

“Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kujua.” (16:25)

Katika Sahihi kuna Hadithi:

«مَنْ دَعَا إِلَى هُدًى كَانَ لَهُ مِنَ الْأَجْرِ مِثْلُ أُجُورِ مَنْ اتَّبَعَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مِنْ غَيْرِ أَنْ يُنْقِصَ مِنْ أُجُورِهِمْ شَيْئًا، وَمَنْ دَعَا إِلَى ضَلَالَةٍ كَانَ عَلَيْهِ مِنَ الْإِثْمِ مِثْلُ آثَامِ مَنْ اتَّبَعَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مِنْ غَيْرِ أَنْ يُنْقِصَ مِنْ آثَامِهِمْ شَيْئًا»

“Anayelingania kwenye uongofu, atapewa malipo mfano wa wenye kumfuata, mpaka Siku ya Kiyama bila ya kupungua chochote katika malipo yao. Mwenye kuita katika upotevu atakuwa na madhambi mithili ya wale waliomfuata, mpaka Siku ya Kiyama, pasi na kupunguka chochote katika madhambi yao.”¹

Pia katika Sahih ipo Hadithi,

«مَا قُتِلَتْ نَفْسٌ ظُلْمًا إِلَّا كَانَ عَلَى ابْنِ آدَمَ الْأَوَّلِ كِفْلٌ مِنْ دَيْهَا، لِأَنَّهُ أَوَّلُ مَنْ سَنَّ الْقَتْلَ»

“Hapana nafsi inayouawa kwa dhuluma, bali sehemu ya dhambi hiyo itakwenda kwa mwana wa kwanza wa Adam. Ni kwa sababu yeye ndiye mtu wa kwanza kuanzisha kuua.”²

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَيَسْئَلُنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُوا يَفْعُرُونَ ﴿٢٠﴾

“Na kwa yakini wataulizwa Siku ya Kiyama juu ya waliyokuwa wakiyazua.”

¹ Muslim 4:2060.

² Fat'h Al-Bari 6:419.

Maana yake: Wanakadhibisha na kuzua uongo. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia Hadithi kutoka kwa Abu Umamah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ aliyafikisha aliyotumwa. Kisha amesema:

«إِيَّاكُمْ وَالظُّلْمَ، فَإِنَّ اللَّهَ يُعْزِمُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ قَيْلُوقُ: وَعِزَّتِي وَجَلَالِي لَا يَجُوزُنِي الْيَوْمَ ظُلْمٌ، ثُمَّ يَأْتِي مُنَادٍ يَقُولُ: أَيْنَ فُلَانُ بْنُ فُلَانٍ؟ فَيَأْتِي بِتَبَعُهُ مِنَ الْحَسَنَاتِ أَمْثَالَ الْجِبَالِ، فَيُشَخِّصُ النَّاسَ إِلَيْهَا أَبْصَارَهُمْ، حَتَّى يَقُومَ بَيْنَ يَدَيْ الرَّحْمَنِ عَزَّ وَجَلَّ، ثُمَّ يَأْمُرُ الْمُنَادِي فَيُنَادِي: مَنْ كَانَتْ لَهُ تِبَاعَةٌ أَوْ ظَلَامَةٌ عِنْدَ فُلَانِ بْنِ فُلَانٍ فَهَلُمَّ، فَيَقْبُلُونَ حَتَّى يَجْتَمِعُوا قِيَامًا بَيْنَ يَدَيْ الرَّحْمَنِ، فَيَقُولُ الرَّحْمَنُ: اأَفْضُوا عَنْ عِبْدِي، فَيَقُولُونَ: كَيْفَ نَقْضِي عَنْهُ؟ فَيَقُولُ: خُذُوا لَهُمْ مِنْ حَسَنَاتِهِ، فَلَا يَزَالُونَ يَأْخُذُونَ مِنْهَا حَتَّى لَا يَبْقَى مِنْهَا حَسَنَةٌ، وَقَدْ بَقِيَ مِنْ أَصْحَابِ الظَّلَامَاتِ، فَيَقُولُ: اأَفْضُوا عَنْ عِبْدِي، فَيَقُولُونَ: لَمْ يَبْقَ لَهُ حَسَنَةٌ، فَيَقُولُ: خُذُوا مِنْ سَيِّئَاتِهِمْ فَأَحْمِلُوهَا عَلَيْهِ»

“Tahadharini na dhuluma, kwani Allah Ataapa Siku ya Kiyama na Atasema: ‘Naapa kwa Nguvu Zangu na Utukufu Wangu! Leo, dhulma haitapita.’ Kisha mtangazaji atanadi: ‘Yuko wapi fulani bin fulani?’ Atakuja akifuatwa na mema mithili ya milima, watu wakiyakodolea macho kwa mshangao, mpaka asimame mbele ya Ar-Rahman.” Kisha, Allah Atamwamuru mtangazaji atanadi: ‘Wale ambao walimkopesha au walidhulumiwa na fulani bin fulani, njooni.’ Watakuja mpaka watakusanyika mbele ya Ar-Rahman.’ Ar-Rahman Atasema: ‘Mhukumuni mja wangu.’ Watasema: ‘vipi tuhukumu dhidi yake.’ Atasema: ‘mchukulieni mema yake.’ hawataacha kuyachukua, mpaka kusibakie jema lolote. Na waliodhulumiwa wamebakia, atasema: ‘Mhukumuni mja wangu.’ Watasema: ‘Hana jema lililosalia.’ Atasema: ‘Chukueni maovu yao mbebesheni yeye.”

Kisha Mtume ﷺ aliinukuu Aya hii:

وَلْيَحْمِلْ أُنْفُسَهُمْ وَأَنْفَالًا مَّعَ أَنْفُسِهِمْ ۗ وَلَيَسْئَلَنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُوا

يَفْتَرُونَ ﴿٢٩﴾

“Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao. Na kwa yakini wataulizwa Siku ya Kiyama juu ya waliyokuwa wakiyazua.”¹

Hadithi hii inathibitishwa katika *Sahih* kwa namna tofauti na hii:

«إِنَّ الرَّجُلَ لَبَأْتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِحَسَنَاتٍ أَمْثَالِ الْجِبَالِ وَقَدْ ظَلَمَ هَذَا، وَأَخَذَ مَالَ هَذَا، وَأَخَذَ مِنْ عِرْصِي هَذَا، فَيَأْخُذُ هَذَا مِنْ حَسَنَاتِي، وَهَذَا مِنْ حَسَنَاتِي، فَإِذَا لَمْ يَبْقَ لَهُ حَسَنَةٌ، أُخِذَ مِنْ سَيِّئَاتِهِمْ فَطُرِحَ عَلَيْهِ»

“Mtu atakuja Siku ya Kiyama akiwa na mema mithili ya milima, huku akiwa amemdhulumu huyu, kachukua mali ya huyu, amechafua hadhi ya huyu. Basi kila mmoja atachukua kutoka katika mema yake, na mwingine naye hivyo hivyo. Ikiwa hakuna jema lake litakalosalia, basi maovu yao yatachukuliwa na kuwekewa yeye.”²

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَلَبِثَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ عَامًا فَأَخَذَهُمُ
الطُّوفَانُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٠٦﴾ فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَصْحَابَ السَّفِينَةِ وَجَعَلْنَاهَا آيَةً
لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٧﴾

14. “Na hakika Tulimtuma Nuhu kwa watu wake, na akakaa nao miaka elfu kasoro miaka khamsini. Basi tufani liliwachukua, nao ni madhalimu.”

15. “Nasi Tukamuokoa yeye na wenziwe wa katika safina, na Tukaifanya kuwa ni Ishara kwa walimwengu wote.”

¹ Ad-Durr Al-Manthur 5:272.

² Fat’hul bari 6:419.

Nuh عليه السلام na Kaumu Yake

Hili ni liwazo kutoka kwa Allah تعالى kwa mja na Mtume Wake ﷺ Akimpasha khabari kuhusu Nuh عليه السلام kwamba alikaa na kaumu yake kwa muda huu, akiwalingania usiku na mchana, kwa siri na dhahiri. Pamoja na haya, hakuna kilichozi kwa isipokuwa kuikimbia haki na kuikataa na kumkadhibisha. Hawakumwamini ila watu wachache. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

فَلَيْتَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ عَامًا فَأَخَذَهُمُ الطُّوفَانُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٠﴾

“Na akakaa nao miaka elfu kasoro miaka khamsini. Basi tufani liliwachukua, nao ni madhalimu.”

Maana yake: Baada ya muda huu mrefu, hakukuwanufaisha kufikishwa ujumbe wa maonyo. Basi, ewe Muhammad! Usivunjike moyo juu ya waliokufuru katika kaumu yako, wala usihuzunike juu yao, kwani Allah تعالى Humhidi Amtakaye na Kumpoteza Amtakaye; na Huanzisha jambo na mambo yote hurejewa Kwake.

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ

“Hakika wale ambao Neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa itawajia kila Ishara...”
(10:96-97)

Na ujue, kuwa Allah تعالى Atakupa ushindi, Atakunusuru na Kukusaidia. Atadhalilisha adui zako, Atawashinda na Kuwafanya chini zaidi ya wote. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: “Nuh عليه السلام alipewa utume akiwa na miaka arubaini, na aliishi na kaumu yake miaka elfu moja kasoro khamsini, baada ya gharika aliishi kwa muda wa miaka sitini, mpaka watu wakaongezeka na wakaenea.”¹

فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَصْحَابَ السَّفِينَةِ

“Nasi Tukamuokoa yeye na wenziwe wa katika safina...”

¹ Muslim 4:1997.

Maana yake: Waliomwamini Nuh عليه السلام. Maelezo kwa ufafanuzi juu ya hayo yamekwishatangulia katika *Surat Hud*.¹ Tafsiri iliyotangulia inatosheleza kiasi cha kutokuwepo haja ya kuirejea. Kauli ya Allah تعالى:

وَجَعَلْنَاهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

“...na Tukaifanya kuwa ni Ishara kwa walimwengu wote.”

Maana yake: Tukaijaalia safina hiyo ni yenye kubakia. Ama ni yenyewe, kama alivyosema Qatadah: “Ilibakia mpaka mwanzoni mwa Uislamu katika mlima wa Judi, au namna yake ambayo Allah تعالى Aliijaalia iwe ukumbusho kwa watu kuhusu Neema Zake kwa viumbe kuonesha namna Alivyowaokoa dhidi ya gharika.² Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَأَيُّهُمُ أَنَا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ فِي الْفُلِكِ الْمَشْحُونِ ﴿١١﴾ وَخَلَقْنَا لَهُم مِّن مِّثْلِهِ مَا

يَرْكَبُونَ ﴿١٢﴾

“Na ni Ishara kwao kwamba Sisi Tuliwapakia dhuriya wao katika jahazi lililosheheni. Na Tukawaumbia kutoka mfano wake wanavyo vipanda.” Mpaka,

وَمَتَّعْنَا إِلَىٰ حِينٍ ﴿١٤﴾

“...na starehe kwa muda.” (36:41-44).

Na Allah تعالى Amesema:

إِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكُم فِي الْجَارِيَةِ ﴿١٥﴾ لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَتَعِيهَا أذُنٌ وَعَيْةٌ ﴿١٦﴾

“Maji yalipofurika Sisi Tulikupandisheni katika safina. Ili Tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalosikia liyahifadhi.” (69:11-12),

Allah تعالى Amesema hapa,

فَأَنْجَيْنَاهُ وَأَصْحَابَ السَّفِينَةِ وَجَعَلْنَاهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ ﴿١٧﴾

“Nasi Tukamuokoa yeye na wenziwe wa katika safina, na Tukaifanya kuwa ni Ishara kwa walimwengu wote.”

¹ Angalia Mjledi wa 5 Tafsiri ya Surat Hud (10:25).

² Ad-duru Al-Manthuru 5/273.

Hii ni njia ya kuhama kutoka kwa kitu maalumu na kwenda katika jinsi ya vitu hivyo kwa ujumla. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحَ وَجَعَلْنَهَا رُجُومًا لِلشَّيَاطِينِ

“Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa, na Tumeyafanya ili kuwapigia mashetani...” (67:5)

Maana yake: Na Tukajaalia sampuli ya mataa hayo kuwapigia, kwani kinachotumika kuwapigia si pambo la mbingu. Pia, Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ طِينٍ ﴿١٢﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَكِينٍ ﴿١٣﴾

“Na kwa yakini Tumemuumba mtu kutokana na asili ya udongo. Kisha Tukamjaalia awe tone¹ mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti.” (23:12-13)

Hili lina mifano mingi.

وَابْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٢٨﴾ إِنَّمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا وَتَخْلُقُونَ إِفْكًا إِنَّ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ لَكُمْ رِزْقًا فَابْتَغُوا عِنْدَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ وَأَشْكُرُوا لَهُ ۗ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿١٢٩﴾ وَإِنْ تَكْذِبُوا فَقَدْ كَذَّبْتُمْ مِنْ قَبْلِكُمْ وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا أَنْ يَبْلُغَ الْمُبِينُ ﴿١٣٠﴾

16. “Na Ibrahim pale alipowaambia watu wake: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na mcheni Yeye. Hiyo ndiyo kheri yenu, ikiwa nyinyi mnajua.”

17. “Hakika nyinyi mnaabudu masanamu badala ya Mwenyezi Mungu, na mnazua uzushi. Hakika hao mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu Hawakumilikiini riziki yoyote. Takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu, na mumuabudu Yeye, na mumshukuru Yeye. Kwake Yeye ndio mtarudishwa.”

¹ Angalia katika Tafsiri ya Surat Al-Hajj (22:5) na Surat Al-Mu-uminun (23:13)

18. "Na mkikadhibisha, basi kaumu kadhaa wa kadhaa za kabla yenu zilikwisha kadhibisha. Na si juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe waziwazi."

Ibrahim عليه السلام Awahutubia Watu Wake

Allah تعالى Anaeleza kuhusu mja, Mtume na kipenzi chake, Ibrahim عليه السلام, kiongozi wa *Al-Hunafa*, kwamba aliwalingania kaumu yake katika kumwabudu Allah تعالى Peke Yake, asiye na mshirika; na kumfanyia ikhilasi katika kumcha na kutaka riziki kutoka Kwake Peke Yake, asiye na mshirika; na kumpwekesha na kumshukuru, kwani Yeye ni wa kushukuriwa kwa neema nyingi, hapana mwingine wa kustahiki haya. Allah تعالى Aliwaambia kaumu yake:

أَعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ

"Muabuduni Mwenyezi Mungu, na mcheni Yeye."

Maana yake: Mtakasieni ibada na khofu,

ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ

"Hiyo ndiyo kheri yenu, ikiwa nyinyi mnajua."

Maana yake: Mtakapofanya hayo, mtapata kheri duniani na Akhera, na shari itaondolewa kwenu duniani na Akhera. Kisha, Allah تعالى Alipasha khabari kwamba masanamu waliyokuwa wakiyaabudu, hayadhuru wala kunufaisha, na Akawaambia, "Bali (masanamu hayo) mmeyapangia majina na kuwaita miungu, kwa hakika hayo ni viumbe kama nyinyi. Na hivi ndivyo alivyosimulia Al-'Awfi kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما.¹ Na ndivyo alivyosema Mujahid, As-Suddi. Pia Al-Waali alisimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa, "Na mnazua uzushi, yaani, mnachonga masanamu," ilhali hayamiliki riziki yenu.² Hii inasisitiza zaidi kumuomba Allah تعالى Peke Yake, kama vile Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

"Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada." (1:5)

¹ At-Tabari 20:18.

² At-Tabari 20:19.

رَبِّ آبِنِ لِي عِنْدَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ

“Mola wangu Mlezi! Nijengee kwako nyumba Peponi...” (66:11)

Kwa ajili hii, Amesema:

فَأَبْتَغُوا

“Takeni...”

Maana yake: Tafuteni.

عِنْدَ اللَّهِ الرَّزْقَ

“...riziki kwa Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Si kwa asiyekuwa yeye, kwani asiyekuwa Yeye hamiliki chochote,

وَأَعْبُدُوهُ وَأَشْكُرُوا لَهُ

“...na mumuabudu Yeye, na mumshukuru Yeye.”

Maana yake: Kuleni katika Riziki Zake na mumwabudu Yeye Peke Yake na mumshukuru juu ya Neema Zake juu yenu,

إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿١٧﴾

“Kwake Yeye ndio mtarudishwa.”

Maana yake: Katika Siku ya Kiyama na Kumlipa kila mwenye amali kwa amali yake. Kauli ya Allah تعالى:

وَإِنْ تَكْذِبُوا فَقَدْ كَذَّبَ أُمَمٌ مِّن قَبْلِكُمْ

“Na mkikadhibisha, basi kaumu kadhaa wa kadhaa za kabla yenu zilikwishakadhibisha.”

Maana yake: Amekufikishieni yaliyowapata miongoni mwa adhabu na matokeo ya kuwapinga Mitume.

وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلْغُ الْمُبِينُ ﴿٢٠﴾

“Na si juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe waziwazi.”

Maana yake: Jukumu la Mtume ni kukufikishieni Ujumbe alioamrisha na Allah تعالی, na Allah تعالی Humuacha apotee Amtakaye na Humuongoa Amtakaye. Basi, fanyeni bidii ili muwe katika wenye furaha. Qatadah aliizungumzia Kauli ya Allah تعالی:

وَإِنْ تَكْذِبُوا فَقَدْ كَذَّبْتُمْ مِنْ قَبْلِكُمْ

“Na mkikadhibisha, basi kaumu kadhaa wa kadhaa za kabla yenu zilikwishakadhibisha...”

Allah تعالی Anamliwaza Nabii Wake ﷺ. Rai hii ya Qatadah inamaanisha kwamba maelezo ya awali ya Allah تعالی (kuhusu Ibrahim عليه السلام), yamekatika, halafu yanaendelea tena kuanzia katika Kauli ya Allah تعالی, ***“.....Basi haikuwa jawabu ya watu wake....”*** Ibn Jarir رحمه الله تعالی kwa upande wake naye amesema kama hivyo. Dhahiri ya mtiririko wa maneno unaonesha kuwa haya yote ni maneno ya Ibrahim عليه السلام Mwandani wa Allah تعالی. Huwatolea hoja wao kwa kuthibitisha uwepo wa siku ya Kiama. Kwa Maneno Yake baada ya yote haya Akasema:

فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ

“.....Basi haikuwa jawabu ya watu wake.....”

Allah تعالی Ndiye Mjuzi zaidi.



أَوْلَمْ يَرَوْا كَيْفَ يُبْدِئُ اللَّهُ الْخَلْقَ
 ثُمَّ يُعِيدُهُ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿١٩﴾
 قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ
 فَانظُرُوا كَيْفَ بَدَأَ الْخَلْقَ ۚ ثُمَّ اللَّهُ يُنشِئُ النَّشْأَةَ الْآخِرَةَ
 إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٠﴾ يُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ
 وَيَرْحَمُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَإِلَيْهِ تُقْلَبُونَ ﴿٢١﴾ وَمَا أَنْتُمْ
 بِمُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ۗ وَمَا لَكُمْ مِنْ
 دُونِ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٢٢﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا
 بِآيَاتِ اللَّهِ وَلِقَائِهِ أُولَٰئِكَ يَئِسُوا مِنْ رَحْمَتِي وَأُولَٰئِكَ
 هُمُ عَذَابِ أَلِيمٌ ﴿٢٣﴾ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا
 أَنْ قَالُوا اقْتُلُوهُ أَوْ حَرِّقُوهُ فَأَنْجَاهُ اللَّهُ مِنَ النَّارِ ۗ إِنَّ فِي
 ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٤﴾ وَقَالَ إِنَّمَا اتَّخَذْتُمْ مِنْ
 دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَانَا مَوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ ثُمَّ يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ وَيَلْعَنُ بَعْضُكُم
 بَعْضًا وَمَأْوَاكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿٢٥﴾ *
 فَمَا مِنْ لَهُ لَوْطٌ وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّي ۗ إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ
 الْحَكِيمُ ﴿٢٦﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَجَعَلْنَا فِي
 ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ ۚ وَءَاتَيْنَاهُ أُجْرَهُ فِي الدُّنْيَا ۗ وَإِنَّهُ فِي
 الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٢٧﴾

أَوْلَمْ يَرَوْا كَيْفَ يُبْدِئُ اللَّهُ الْخَلْقَ
 ثُمَّ يُعِيدُهُ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ
 ﴿١٩﴾ قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ
 فَانظُرُوا كَيْفَ بَدَأَ الْخَلْقَ ۚ ثُمَّ اللَّهُ
 يُنشِئُ النَّشْأَةَ الْآخِرَةَ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٠﴾ يُعَذِّبُ مَنْ
 يَشَاءُ وَيَرْحَمُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَإِلَيْهِ
 تُقْلَبُونَ ﴿٢١﴾ وَمَا أَنْتُمْ
 بِمُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي
 السَّمَاءِ ۗ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ
 مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٢٢﴾ وَالَّذِينَ
 كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَلِقَائِهِ
 أُولَٰئِكَ يَئِسُوا مِنْ رَحْمَتِي
 وَأُولَٰئِكَ هُمُ عَذَابِ أَلِيمٌ ﴿٢٣﴾

19. "Je! Wao hawaoni jinsi Mwenyezi Mungu Anavyoanzisha Uumbaji, na kisha Akarudisha tena. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi."

20. "Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi

Alivyoanzisha Uumbaji; kisha Mwenyezi Mungu Ndiye Anayeumba umbo la baadaye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.”

21. “Humuadhibu Amtakaye, na Humrehemu Amtakaye. Na Kwake Yeye mtapelekwa.”

22. “Na nyinyi si wenye kushinda katika ardhi wala katika mbingu. Wala nyinyi hamna mlinzi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu.”

23. “Na waliozikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na kukutana Naye, hao ndio wenye kukata tamaa na Rehema Yangu, na hao ndio wenye kupata adhabu chungu.”

Ushahidi wa Kuwepo Maisha Mengine Baada ya Kifo

Allah تعالی Anaeleza kuhusu Al-Khalil Ibrahim عليه السلام kwamba aliwaonesha uthibitisho wa marejeo waliyokuwa wakiyakanusha kutokana na wanayoyashuhudia. Kabla Allah تعالی Hajawaumba hawakuwa kitu chochote wala kutajika. Kisha wakafanywa wawepo na wakawa watu wenye kusikia na kuona. Mwenye kuyaanzisha haya, ni Muweza wa kuyarejesha, hili ni sahali na jepesi mno Kwake. Halafu Akawaongoza katika kuzingatia alama zenye kuonekana angani miongoni mwa vitu mbalimbali alivyoviumba Allah تعالی: Mbingu na vilivyomo humo, kama vile nyota zenye kutoa nuru, zilizotulia na zinazokwenda; ardhini na vilivyomo, kama vile nyanda, milima, mabonde, majangwa na ardhi kame, miti, mito, matunda, bahari. Yote haya ni mambo yanayofahamisha kuwa kuzuka kwake ni kutokana Kuwepo Mwenye Kuyatengeneza Mwenye Kutenda Mwenyewe, Mfanyaji Mwenye khiyari Yake, Ambaye Huliambia jambo liwe, nalo huwa.

Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

أَوَلَمْ يَرَوْا كَيْفَ يُبْدِئُ اللَّهُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٧﴾

“Je! Wao hawaoni jinsi Mwenyezi Mungu Anavyoanzisha Uumbaji, na kisha Akarudisha tena. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.”

Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

“Na Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.” (30:27)

Kisha, Allah تعالى Amesema:

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ بَدَأَ الْخَلْقَ ثُمَّ اللَّهُ يُنشِئُ النَّشْأَةَ الْآخِرَةَ

“Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi Alivyoanzisha Uumbaji; kisha Mwenyezi Mungu Ndiye Anayeumba umbo la baadaye.”

Maana yake: Siku ya Kiyama,

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.”

Maana yake: Yeye ni Hakimu Mwenye Udhibiti, Ambaye Hufanya Ayatakayo, na Huhukumu Atakavyo, hakuna wa kuipinga Hukumu Yake, wala Haulizwi juu ya Anachokifanya, ilhali wao ni wenye kuulizwa. Kuumba na Kutoa Amri ni Kwake, chochote Akifanyacho ni kwa Uadilifu, kwa sababu Yeye ni Mfalme Ambaye Hadhulumu, japo uzito wa mdudu chungu. Ni kama ilivyokuja katika Hadithi ambayo watu wa Sunnah waliinukuu:

«إِنَّ اللَّهَ لَوِ عَذَّبَ أَهْلَ سَمَاوَاتِهِ وَأَهْلَ أَرْضِهِ لَعَذَّبَهُمْ وَهُوَ غَيْرُ ظَالِمٍ لَّهُمْ»

“Lau Allah Angeliwaadhibu wakazi wa mbingu Zake na wa ardhi Yake, Angelifanya hivyo bila ya kuwa Mwenye Kuwadhulumu.”¹

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

يُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَيَرْحَمُ مَنْ يَشَاءُ

“Humuadhibu Amtakaye, na Humrehemu Amtakaye.”

¹ Abu Dawud 5:75, Ibn Majah 1:30.

Maana yake: Mtarejea katika Siku ya Kiyama.

وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ

“Na nyinyi si wenye kushinda katika ardhi wala katika mbingu.”

Maana yake: Hamshindi Yeye, mkazi yeyote wa mbingu wala wa ardhi Yake, bali Yeye ni Mwenye Kuwahibiti waja Wake. Kila kitu kinamkhofu Yeye na kinahitaji Kwake, na Yeye si mhitaji wa yeyote.

وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٢٤﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِعَاثِتِ اللَّهِ وَلِقَائِهِ

“Wala nyinyi hamna mlinzi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na waliozikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu na kukutana Naye...”

Maana yake: Walimpinga na wakakanusha jambo la kurejea,

أُولَئِكَ يَسُؤُونَ مِنْ رَحْمَتِي

“...hao ndio wenye kukata tamaa na Rehema Yangu...”

Maana yake: Hawana fungu lao katika hiyo Rehema,

وَأُولَئِكَ هُمْ عَذَابُ أَلِيمٍ ﴿٢٥﴾

“...na hao ndio wenye kupata adhabu chungu.”

Maana yake: Maumivu makali duniani na Akhera.

فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا اقْتُلُوهُ أَوْ حَرِّقُوهُ فَأَنْجَاهُ اللَّهُ مِنَ النَّارِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٦﴾ وَقَالَ إِنَّمَا اتَّخَذْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُمْ بِبَعْضٍ وَيَلْعَنُ بَعْضُكُمْ بَعْضًا وَمَأْوَأَتُهُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِّنْ نَّصِيرِينَ ﴿٢٧﴾

24. “Basi haikuwa jawabu ya watu wake ila ni kusema: Muuweni au mchomeni moto! Mwenyezi Mungu Akamuokoa na moto. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaoamini.”

25. "Na amesema: Hakika nyinyi mmeyashika masanamu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani. Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makazi yenu ni Motoni. Wala hamtapata wa kuwanusuru."

Majibuu ya Watu wa Ibrahim na Namna Allah تعالی Alivyoudhibiti Moto

Allah تعالی Anatoa khabari kuhusu watu wa Ibrahim عليه السلام kuhusu kufuru, ukaidi na kiburi chao na walivyoikataa haki na kuchagua batili, kwamba hawakuwa na jawabu baada ya kauli hii ya Ibrahim عليه السلام iliyokusanya hidaya na ubainifu.

إِلَّا أَنْ قَالُوا اقْتُلُوهُ أَوْ حَرِّقُوهُ

"...ila ni kusema: Muueni au mchomeni moto!"

Hayo ni kwa sababu hoja ilisimama dhidi yao na hoja ikawashinda, wakaamua kutumia mamlaka na nguvu za dola yao,

قَالُوا أَتَبْنُوا لَهُ بُيُوتًا فَأَلْقَوْهُ فِي الْجَحِيمِ ﴿٣٧﴾ فَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَسْفَلِينَ ﴿٣٨﴾

"Wakasema: Mjengeeni jengo, na kisha mtupeni motoni humo! Basi walitaka kumfanyia vitimbi, lakini Tukawafanya wao ndio wa chini." (37:97-98)

Na hili ni kuwa wao walitumia muda mrefu kukusanya kuni nyingi na wakazizungushia ukuta, kisha wakauwasha moto. Mwale wa moto wake ukapanda mpaka kufikia angani, wala haujawahi kuwashwa moto mkubwa kama huo. Wakamkusudia Ibrahim عليه السلام, wakamkamata kisha wakamtupia ndani ya moto.

Allah تعالی Akaujaalia kuwa baridi na salama kwa Ibrahim عليه السلام. Akatoka akiwa salama baada ya kukaa kwa siku kadhaa humo. Kwa ajili hii na mithili yake, Allah تعالی Alimfanya awe kiongozi kwa watu, kwani alijitolea nafsi yake kwa ajili ya Ar-Rahman, na mwili wake kwa ajili ya moto na mwanaye kwa ajili ya kujisogeza karibu ya Allah تعالی, akaifanya mali yake kwa ajili ya wageni. Mintarafu ya hii, watu wa dini zote wamekuwa ni wenye mahaba naye.

Kauli ya Allah تعالى:

فَأَخْرَجَهُ اللَّهُ مِنَ النَّارِ

“Mwenyezi Mungu Akamuokoa na moto.”

Maana yake: Alimpa salama kwa kuufanya uwe baridi na salama,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾

“Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaoamini.”

Waadhi wa Ibrahim عليه السلام kwa Watu Wake.

وَقَالَ إِنَّمَا اتَّخَذْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Na amesema: Hakika nyinyi mmeyashika masanamu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani.”

Anaiambia kaumu yake, kwa kuikemea juu ya maovu wayafanyayo kwa kuyaabudu masanamu: “Kwa hakika! Mmeyachukua haya ili mpate urafiki na mapenzi duniani kutokana na kuyaabudu katika maisha haya.

ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Kisha Siku ya Kiyama...”

Hali hii itakuwa kinyume chake, kiasi kwamba urafiki na mapenzi haya yanageuka kuwa chuki na uadui, kisha,

يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ

“...mtakataana nyinyi kwa nyinyi...”

Maana yake: Mtayakana mliyokuwa nayo,

وَيَلْعَنُ بَعْضُكُم بَعْضًا

“...na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi.”

Maana yake: Wafuasi watawalaani viongozi wao, na wao watawalaani wafuasi.

كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعَنَتْ أُخْتَهَا

“Kila utakapoingia umma utawalaani wenzake.” (7:38)

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

الْأَخْلَاءُ يَوْمَئِذٍ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ إِلَّا الْمُتَّقِينَ ﴿٦٧﴾

“Siku hiyo marafiki watakuwa ni maadui, wao kwa wao, isipokuwa wachamungu.” (43:67)

Allah تعالى Amesema hapa:

ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ وَّيَلْعَنُ بَعْضُكُم بَعْضًا وَمَأْوَاكُمُ النَّارُ

“Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makazi yenu ni Motoni.”

Maana yake: Mwisho wenu na marejeo yenu baada ya matukio ya Kiyama ni Motoni, wala hamtakuwa na msaidizi wa kukunusuruni, wala wa kukuokoeni dhidi ya adhabu ya Allah تعالى. Na hii ni hali ya makafiri. Ama Waumini ni kinyume chake.

﴿ فَقَامَنَ لَهُ لُوطٌ وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّي إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٨﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ

إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ وَءَاتَيْنَاهُ أُجْرَهُ فِي الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي

الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦٩﴾

26. “Lut’i akamuamini, na akasema: Mimi nahamia kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

27. “Na Tulimtukia (Ibrahim) Is-haq na Yaa’qub. Na Tukajaalia katika dhuriya wake Unabii na Kitabu, na Tukampa ujira wake katika dunia; naye hakika katika Akhera bila ya shaka ni katika watu wema.”

Imani ya Lut عليه السلام na Kuhama Kwake Pamoja na Ibrahim عليه السلام.

Allah تعالى Anaeleza khabari kumhusu Ibrahim عليه السلام kwamba Lut عليه السلام alimwamini. Yeye ni mtoto wa nduguye. Wanasema kuwa jina lake ni Lut عليه السلام bin Haaran bin Azar. yaani hakuamini yeyote katika kaumu yake, isipokuwa Lut عليه السلام na Sarah, mke wa Ibrahim *Al-Khalil* عليه السلام. Hata hivyo, husemwa, ni namna gani inavyokusanywa Aya hii na Hadithi iliyoandikwa katika *Sahih* kwamba pindi Ibrahim عليه السلام alipopita kwa fidhuli yule na akauliza kuhusu Sarah ni nani kwake. Amkajibu: "Ni dada yangu." Kisha akamjia mkewe na kumwambia: "Mimi nilimwambia kwamba wewe ni dada yangu, lakini usinikadhibishe, kwani katika uso wa dunia, hakuna muumini ghairi yangu mimi na wewe, basi wewe ni dada yangu katika Dini." Kana kwamba inasadifiana na maana hii – Allah تعالى Ndiye Mjuzi – kwamba katika uso wa ardhi, hakuna wanandoa wawili walio katika Uislamu isipokuwa mimi na wewe, kwani Lut عليه السلام ni mmojawapo wa watu wa kaumu yake ambaye alimwamini. Alihamia nchi ya Shamu (Syria) pamoja naye. Kisha akapelekwa kuwa Mtume kwa watu wa Sadum (Sodoma) na eneo lake.¹ Naye Ndiye Aliyewaamuru mengi ambayo tayari tumeyaeleza na mengine yatafuata. Kauli ya Allah تعالى:

وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّي

“Na akasema: Mimi nahamia kwa Mola wangu Mlezi.”

Kiwakilishi hapa katika Kitenzi kinaashiria anayezungumza hapa ni Nabii Lut عليه السلام, kwa kuwa yeye ndiye wa karibu zaidi kutajwa kabla ya maneno haya. pia upo uwezekano kwamba kinarejea kwa Ibrahim عليه السلام. Ibn ‘Abbas na Adh-Dhahhak wamesema hivyo, kuwa Ibrahim عليه السلام ndiye anayetajwa kwa njia ya kiwakilishi hapa katika Kauli ya Allah تعالى:

﴿ فَتَأْمَنَ لَهُ لُوطٌ ﴾

“Lut akamuamini...”

Maana yake: Katika kaumu yake. Halafu, Allah تعالى Anaeleza kwamba aliamua kuhama kutoka kwao kwa ajili ya kutaka kuitangaza Dini waziwazi na kujizatiti katika hilo. Kwa ajili hii, Amesema:

¹ Fat’h Al-Bari 6:447.

إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٩﴾

“Hakika Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Maana yake: Nguvu ni Zake na kwa Mtume Wake na kwa Waumini. Ni Mwenye Hikima katika Kauli na Vitendo Vyake na Hukumu Zake za masuala ya Kudura na Sharia. Oatadah amesema: “Wote kwa pamoja, walihama kutoka Kutha, mojawapo ya viunga vya Kufa, na wakaenda Shamu (Syria).”¹

Imetajwa kwetu kwamba Mtume ﷺ amesema: “Hakika kutakuwa na Hijra (kuhama) kwa mara ya pili, ambapo watu wa ardhi watahamia ardhi aliyohamia Nabii Ibrahim عليه السلام (Shaam) alipotoka Iraq. Itawaacha watu waovu kuhamia Ardhi hiyo, aliyohamia Ibrahim عليه السلام (Shaam). Hivyo Ardhi itawatupa wao, na *Arrahmaan* Atawachukia watu hao. Moto utawakusanya wao pamoja na Nyani na Nguruwe. Popote watakapokuwa usiku au mchana Moto huo watakuwa nao. Utamla moto huo hata yule aliyejitenga nao.” Na katika riwaya nyingine Mtume ﷺ anasema, ‘Kutakuwa na uhamiaji mwengine (Hijra) baada ya Hijra ya Madina. Watu bora katika ardhi watalazimiana sehemu aliyohamia Ibrahim عليه السلام.” Imamu katika Musnadi wake ameileta Hadithi hii kwa urefu kupitia upokezi wa Abdillahi bin Amri bin Al-Asi رضي الله عنه.

Allah تعالى Ampatia Ibrahim عليه السلام Watoto, Is-haq عليه السلام na Ya'qub عليه السلام na Akaandika Utume Utokane na Dhuriya Wake.

Kauli ya Allah تعالى:

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ

“Na Tulimtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaa'qub.”

Ni kama Kauli ya Allah تعالى:

فَلَمَّا أَعْتَرَهُمْ وَمَا يَعْْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ وَكُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿١٩﴾

“Basi alipojitenga nao na yale waliyokuwa wakiyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu, Tulimpa Is-haq na Yaaqub, na kila mmoja Tukamfanya Nabii.” (19:49)

¹ At-Tabari 20:26.

Kwamba, pindi alipoiacha kaumu yake, Allah تعالی Alilituliza jicho lake (alimfurahisha) kwa kupata mtoto mwema, Nabii katika zama za uhai wa babu yake.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً

“Naye Tukampa Is-haq, na Yaaqub kuwa ni ziada.” (21:72)

Maana yake: Nyongeza,

فَبَشَّرْنَاهَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ ﴿٧٢﴾

“Basi Tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq Yaaqub.” (11:71)

Maana yake: Baada ya mtoto huyu, na yeye atapata mtoto katika uhai wenu ambaye ni kitulizo cha macho yenu (furaha kwenu).

وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ

“Na Tukajaalia katika dhuriya wake Unabii na Kitabu...”

Hii ni baraka kubwa, pamoja na Allah تعالی Kumfanya kuwa Al-Khalil Wake. Alimfanya kuwa kiongozi wa watu, kwani Alijaalia Utume na Kitabu katika dhuriya wake. Basi, hakupatikana Nabii yeyote baada ya Ibrahim عليه السلام, isipokuwa kutoka katika uzao wake. Manabii wote wa Wana wa Israil wanatokana na uzao wa Ya'qub bin Is-haq bin Ibrahim عليه السلام, mpaka mwisho wao akawa 'Isa bin Maryam عليه السلام. Akasimama katikati ya watu wake akiwapa bishara kuhusu Nabii Mwarabu Mkuraishi, kutoka ukoo wa Banu Hashim, ambaye ni Mtume wa mwisho kabisa, kiongozi wa wanaadamu duniani na Akhera. Ndiye ambaye Allah تعالی Alimteua kutoka taifa la Waarabu, ni kutoka katika uzao wa Ismail bin Ibrahim عليه السلام, wala hakuwahi kupatikana nabii kupitia katika uzao huo wa Ismail عليه السلام, isipokuwa yeye ﷺ.

وَأَتَيْنَاهُ أَجْرَهُ فِي الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٣﴾

“...na Tukampa ujira wake katika dunia; naye hakika katika Akhera bila ya shaka ni katika watu wema.”

Allah تعالی Alimkusanyia pamoja furaha ya duniani na ya Akhera. Duniani akawa na riziki kunjufu na ya faraja, makazi mazuri, maji yenye ladha njema, mke wa kupendeza na mwema, sifa njema, kutajwa kuzuri na kila mmoja anampenda na anamfanya rafiki. Sawa na alivyosema Ibn 'Abbas, Mujahid, Qatadah na wengine رضي الله عنهم: "Ni pamoja na kumtii Allah تعالی katika kila hali."¹

Ni kama Alivyosema Allah تعالی:

وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى ﴿٣٧﴾

"Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi?" (53:37)

Maana yake: Aliyatimiza yote aliyoamrisha na pia akamtii Mola wake kwa ukamilifu. Kwa minajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَأَتَيْنَاهُ أَجْرَهُ فِي الدُّنْيَا وَإِنَّا لَهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٣٧﴾

"...na Tukampa ujira wake katika dunia; naye hakika katika Akhera bila ya shaka ni katika watu wema."

Pia ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٣٧﴾

"Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, Hanif,² wala hakuwa miongoni mwa washirikina."

Mpaka,

وَإِنَّا لَهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٣٧﴾

**"...na hakika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema."
(16:120-122)**

* * *

¹ At-Tabari 20:27 28.

² Angalia Tafsiri ya Surat Al-Isra (16-120).

وَلَوْطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ إِنَّكُمْ لَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا
 سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ أَحَدٍ مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿٢٨﴾ أَهْيَأْكُمْ
 لَأْتُونَ الرِّجَالَ وَتَقَاطِعُونَ السَّبِيلَ وَتَأْتُونَ فِي نَادِيَكُمُ
 الْمُنْكَرَ ۗ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَتَيْنَا
 بِعَذَابِ اللَّهِ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٩﴾ قَالَ رَبِّ
 أَنْصُرْنِي عَلَى الْقَوْمِ الْمُفْسِدِينَ ﴿٣٠﴾ وَلَمَّا جَاءَتْ
 رُسُلُنَا لُوطًا بِالْبَشَرِ قَالُوا إِنَّا مَهْلِكُوا أَهْلَ هَذِهِ
 الْقَرْيَةِ ۗ إِنَّ أَهْلَهَا كَانُوا ظَالِمِينَ ﴿٣١﴾ قَالَ إِنَّ
 فِيهَا لُوطًا قَالُوا نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَنْ فِيهَا لَنَنْجِيَنَّكَ وَأَهْلَكَ
 إِلَّا أُمَّرَاتَهُ كَانَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٣٢﴾ وَلَمَّا أَنْ جَاءَتْ
 رُسُلُنَا لُوطًا سِئَاءَ يَوْمٍ وَّضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا وَقَالُوا لَا
 تَخَفْ وَلَا تَحْزَنْ ۗ إِنَّا مُنْجِيكَ وَأَهْلَكَ إِلَّا أُمَّرَاتَكَ كَانَتْ
 مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٣٣﴾ إِنَّا مُنْزِلُونَ عَلَى أَهْلِ هَذِهِ
 الْقَرْيَةِ رِجْزًا مِنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٣٤﴾
 وَلَقَدْ تَرَكْنَا مِنْهَا آيَةً بَيِّنَةً لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٣٥﴾ وَإِلَى
 مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا فَقَالَ يَنْقُورِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَارْجُوا
 الْيَوْمَ الْآخِرَ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٣٦﴾
 فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ
 جِثِيمِينَ ﴿٣٧﴾

وَلَوْطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ إِنَّكُمْ
 لَأْتُونَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا
 مِنْ أَحَدٍ مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿٢٨﴾
 أَهْيَأْكُمْ لَأْتُونَ الرِّجَالَ وَتَقَاطِعُونَ
 السَّبِيلَ وَتَأْتُونَ فِي نَادِيَكُمُ
 الْمُنْكَرَ ۗ فَمَا كَانَ جَوَابَ
 قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَتَيْنَا
 بِعَذَابِ اللَّهِ إِنْ كُنْتَ مِنَ
 الصَّادِقِينَ ﴿٢٩﴾ قَالَ رَبِّ
 أَنْصُرْنِي عَلَى الْقَوْمِ
 الْمُفْسِدِينَ ﴿٣٠﴾

28. "Na pale Lut'i alipo-
 waambia watu wake:
 Hakika nyinyi mnafanya
 uchafu, ambao hapana
 mmoja katika walimwengu
 aliyekutangulieni kwa
 hayo."

29. "Je! Nyinyi mnawa-
 ingilia wanaume, na
 mnaikata njia? Na katika
 mikutano yenu mnafanya
 maovu? Basi haikuwa
 jawabu ya watu wake
 isipokuwa kusema: Tuletee
 hiyo adhabu ya Mwenyezi

Mungu ikiwa wewe ni katika wasemao kweli."

30. "Akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ninusuru na watu mafisadi hawa!"

Khutuba za Lut عليه السلام na Kilichotokea Baina Yake na Watu Wake

Allah تعالى Anaeleza khabari za Nabii Wake, Lut عليه السلام kwamba alilikataza kaumu yake maovu yao pamoja na amali zao chafu za kuwaendea wanaume. Na kuwa kwa kitendo chao hiki, hakijawahi kufanywa na yeyote katika wanaadamu. Pamoja na haya, walikuwa wakimkufuru Allah تعالى na kumkadhibisha Mtume Wake. Pia wakifanya ukhalifu na wakikata njia, yaani, wakisimama njiani na kua watu na kuwaporu mali zao.

وَتَأْتُونَ فِي نَادِيكُمْ الْمُنْكَرَ

"Na katika mikutano yenu mnafanya maovu?"

Maana yake: Wanafanya yasiyolaikiana na kauli na matendo katika majilisi zao ambazo walikuwa wakijumuika. Hawakuwa wakikatazana chochote katika hayo. Wapo waliosema: "Walikuwa wakiendeano wao kwa wao katika hadhara." Mujahid aliyasema haya.¹

Kuna kauli kwamba walikuwa wakishindana kufusa huku wakiwa wanacheka. Haya aliyasema 'Aishah رضي الله عنها na Al-Qasim.²

Wengine wamesema kuwa walikuwa wakiwashindanisha makondoo dume au kufanya mapigano ya majogoo. Yote hayo walikuwa wakiyafanya, na walikuwa waovu zaidi na hivyo. Kauli ya Allah تعالى:

فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَأَتَيْنَا بَعْدَ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٣٠﴾

"Basi haikuwa jawabu ya watu wake isipokuwa kusema: Tuletee hiyo adhabu ya Mwenyezi Mungu ikiwa wewe ni katika wasemao kweli."

Haya ni kwa mintarafu ya kufuru, stihzai na ufidhuli wao. Kwa hivyo, Mtume ﷺ aliomba nusura dhidi yao, akasema:

¹ At-Tabari 20:29, Al-Baghawi 3:466.

² At-Tabari 20:30.

قَالَ رَبِّ أَنْصُرْنِي عَلَى الْقَوْمِ الْمُفْسِدِينَ ﴿٣١﴾

"Ewe Mola wangu Mlezi! Ninusuru na watu mafisadi."

وَلَمَّا جَاءَتْ رُسُلُنَا إِبْرَاهِيمَ بِالْبُشْرَى قَالُوا إِنَّا مُهْلِكُوا أَهْلَ هَذِهِ الْقَرْيَةِ إِنِ أَهْلُهَا كَانُوا ظَالِمِينَ ﴿٣٢﴾ قَالَ إِنِّ فِيهَا لُوطٌ قَالَوَا نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَنْ فِيهَا لَنَنْجِيَنَّهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا أُمَّرَأَتَهُ كَانَتْ مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٣٣﴾ وَلَمَّا أَنْ جَاءَتْ رُسُلُنَا لُوطًا سِيءَ بِهِمْ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا وَقَالُوا لَا تَخَفْ وَلَا تَحْزَنْ إِنَّا مُنْجِيُونَ ﴿٣٤﴾ قَالَ إِنَّا مُنْجِيُونَ عَلَى أَهْلِ هَذِهِ الْقَرْيَةِ رِجْزًا مِّنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿٣٥﴾ وَلَقَدْ تَرَكْنَا مِنْهَا آيَةً بَيِّنَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٣٦﴾

31. *"Na wajumbe wetu walipomjia Ibrahim na bishara, wamesema: Hakika sisi hapana shaka tutawahiliki watu wa mji huu, kwani watu wake hakika wamekuwa madhalimu."*

32. *"Akasema: Hakika humo yumo Lut'i. Wao wakasema: Sisi tunajua zaidi nani yumo humo. Hapana shaka tutamuokoa yeye na ahali wake, isipokuwa mkewe aliye miongoni mwa wataokaa nyuma."*

33. *"Na wajumbe Wetu walipomfikia Lut'i, alihuzunika kwa ajili yao, na moyo uliona dhiki kwa ajili yao. Wakasema: Usiogope, wala usihzunike. Hakika sisi tutakuokoa wewe na ahali wako, ila mkeo aliye miongoni mwa wataokaa nyuma."*

34. *"Kwa yakini Sisi Tutawateremshia watu wa mji huu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya uchafu wanaoufanya."*

35. *"Na Tumeacha katika mji huo Ishara ilio wazi kwa watu wanaotumia akili zao."*

Lut عليه السلام Aomba Nusura kwa Mola Wake na Ujio wa Malaika kwa Ibrahim عليه السلام, Kisha kwa Lut عليه السلام.

Baada ya Lut عليه السلام kumwomba Allah تعالى Alete nusura dhidi ya kaumu yake, Allah تعالى Aliwapeleka Malaika Wake kwenda kumnusuru, wakapita kwanza kwa Ibrahim عليه السلام kwa namna ya wageni. Akawapokea kwa namna inayotakiwa mgeni kufanyiwa. Ibrahim عليه السلام alipoona hawakuwa na hamu ya chakula, akakosa imani kwao na akaingiwa na khofu kutokana nao. Wakaanza kumtuliza na kumpa bishara ya kupata mtoto mwema kupitia kwa mkewe, Sarah, ambaye alikuwepo hapo.

Akastaajabishwa na hayo, kama ilivyokwishatangulia kuelezwa katika *Surat Hud* na *Hijr*. Baada ya kumletea Ibrahim عليه السلام bishara na kumpasha khabari kwamba wametumwa kwenda kuwaangamiza kaumu ya Lut عليه السلام, Ibrahim عليه السلام alianza kuwatetea ili kwamba huenda wakapewa muda na asaa Allah تعالى Akawaongoa. Baada ya kusema: Sisi ni wa kuwaangamiza wakazi wa mji huu:

قَالَ إِنَّ فِيهَا لُوطًا قَالُوا نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَنْ فِيهَا لَنَنْجِيَنَّهٗ وَأَهْلَهُ إِلَّا امْرَأَتَهُ كَانَتْ

مِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٦٧﴾

“Akasema: Hakika humo yumo Lut’i. Wao wakasema: Sisi tunajua zaidi nani yumo humo. Hapana shaka Tutamuokoa yeye na ahali wake, isipokuwa mkewe aliye miongoni mwa wataokaa nyuma.”

Maana yake: Katika wenye kuangamizwa, kwa sababu alikuwa akiwasaidia katika kufuru, uovu na liwati yao. Wakaondoka kwa Ibrahim عليه السلام wakaenda kwa Lut عليه السلام na kuingia wakiwa katika sura za mashababi wazuri. Alipowaona wakiwa hivyo,

يَوْمَ يَمُوتُ يَمٌّ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا

“...alihuzunika kwa ajili yao, na moyo uliona dhiki kwa ajili yao.”

Maana yake: Alishikwa na khofu kwa jambo lao kwamba, ikiwa atawapokea kama wageni wake, aliichelea kaumu yake, na kama hakuwakaribisha kuwa wageni wake, basi aliwakhofia kitakachowakumba. Kwa wakati huo hakuwajua kwamba walikuwa akina nani.

وَقَالُوا لَا تَخَفْ وَلَا تَحْزَنْ إِنَّا مُنْجُونَ وَأَهْلَكَ إِلَّا أَمْرَاتِكَ كَانَتْ مِنَ الْغَيْبِ
 إِنَّا مُنْزِلُونَ عَلَىٰ أَهْلِ هَذِهِ الْقَرْيَةِ رِجْزًا مِّنَ السَّمَاءِ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ

“Wakasema: Usiogope, wala usihuzunike. Hakika sisi tutakuokoa wewe na ahali wako, ila mkeo aliye miongoni mwa wataokaa nyuma. Kwa yakini sisi tutawateremshia watu wa mji huu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya uchafu wanaoufanya.”¹

Hapo ni kwamba, Jibril عليه السلام aliung’oa mji wao kutoka katika misingi ya ardhi na kuunyanyua angani, akaupindua juu chini na kuutupa juu yao. Allah تعالی Akapeleka kwa wao changarawe za udongo mgumu uliokamatana, yaliyotiwa alama kwa Mola wako, wala haya hayako mbali na madhalimu. Allah تعالی Akajaalia mahali pao kuwa ziwa lililovunda, lenye kunuka.

Pia aliwajaalia kuwa mazingatio kwa wanaadamu mpaka siku ya Ufufuo, na wao ni katika watu watakaopewa adhabu kali zaidi katika siku ya marejeo.

Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَلَقَدْ تَرَكْنَا مِثَاقَ بَيْتِهَا

“Na Tumeacha katika mji huo Ishara ilio wazi...”

Maana yake: Dhahiri,

لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ

“...kwa watu wanaotumia akili zao.”

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَأَنكُمْ لَتَمُرُّونَ عَلَيْهِمْ مُّصْبِحِينَ ﴿١٣٧﴾ وَيَالَيْلِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٣٨﴾

“Na hakika nyinyi mnawapitia wakati wa asubuhi. Na usiku. Basi je! Hamyatii akilini?” (37:137-138)

¹ Angalia mjeledi wa 5, Tafsiri ya surat Hud (11:82).

وَالِى مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا فَقَالَ يَنْقَوْمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَرْجُوا الْآخِرَ وَلَا تَعْتَوْا فِي
 الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٣٦﴾ فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ
 جِثْمِينَ ﴿٣٧﴾

36. "Na kwa Madyana Tulimtuma ndugu yao Shuaibu, naye akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu na iogopeni Siku ya Akhera, wala msende katika ardhi mkifisidi."

37. "Lakini walimkanusha basi ukawatwaa mtikiso wa ardhi, wakapambazukiwa ndani ya nyumba zao nao wamefudikia."

Kiasi cha Shu'ayb عليه السلام na Kaumu Yake

Allah تعالى Akaeleza kumhusu mja na Mtume wake Shu'ayb عليه السلام kwamba aliionya kaumu yake, watu wa Madyan. Aliwaamuru wamwabudu Allah تعالى Peke Yake, Asiyeye na mshirika, na waikhofu adhabu na nakama ya Allah تعالى katika Siku ya Kiyama. Amesema:

يَنْقَوْمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَرْجُوا الْآخِرَ

"Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu na iogopeni Siku ya Akhera..."

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: "Baadhi yao wamesema kwamba inamaanisha: iogopeni Siku ya Mwisho."¹

Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لِمَنْ كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ

**"...kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho."
 (33:21)**

وَلَا تَعْتَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٣٦﴾

"...wala msende katika ardhi mkifisidi."

¹ At-Tabari 20:34.

Aliwakataza wasiende ardhini wakifanya ufisadi, ambako ni kwenda huku na huko na kuwafanyia watu mabaya. Maovu hayo ni kwamba, walikuwa wakipunguza vipimo na mizani na wakiwazuia watu njiani.

Haya yakiwa ni pamoja na kumkufuru kwao Allah **تعالى** na Mtume Wake. Allah **تعالى** Akawahiliki kwa zilizala kubwa ilioitetemesha nchi yao, na *Sayhah* (ukelele mkali) uliozitoa nyoyo kutoka katika miili yao, na adhabu katika Siku ya Kivuli ambapo roho zilitolewa kutoka katika matulizano yake.

Hiyo ilikuwa adhabu ya siku kuu. Kisa chao kimeshatangulia kuelezwa kwa urefu katika *Surat Al-A'raaf*, *Hud* na *Ash-Shu'araa*.¹

Kauli ya Allah **تعالى**:

فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَنِينًا

“...wakapambazukiwa ndani ya nyumba zao nao wamefudikia.”

Qatadah amesema, “Wakiwa maiti.”² Wengine wamesema kuwa walirundikwa pamoja.³

* * *

¹ At-Tabari 20:34.

² Tafsiri ya Surat Al-A'raaf (7:85), Surat Hud (11:84) na Surat Ash-Shu'araa (29:36).

³ At-Tabari 20:34.

وَعَادًا وَثَمُودًا وَقَدْ تَبَيَّنَ لَكُمْ^ط
 مِنْ مَّسْكِينِهِمْ^ط وَزَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ
 أَعْمَلَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيلِ
 وَكَانُوا مُسْتَبْصِرِينَ ﴿٣٨﴾ وَقُرُورَ
 وَفِرْعَوْنَ وَهَمَانَ^ط وَلَقَدْ جَاءَهُمْ
 مُوسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ فَاسْتَكْبَرُوا فِي
 الْأَرْضِ وَمَا كَانُوا سَابِقِينَ ﴿٣٩﴾
 فَكُلًّا أَخَذْنَا بِذَنبِهِ^ط فَمِنْهُمْ
 مَنْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِ حَاصِبًا وَمِنْهُمْ
 مَنْ أَخَذَتْهُ الصَّيْحَةُ وَمِنْهُمْ
 مَنْ خَسَفْنَا بِهِ الْأَرْضَ وَمِنْهُمْ
 مَنْ أَغْرَقْنَا وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ
 وَلَكِنْ كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٠﴾
 مِثْلُ الَّذِينَ أَخَذُوا مِنَ دُونِ اللَّهِ
 أَوْلِيَاءَ كَمَثَلِ الْعَنكَبُوتِ اتَّخَذَتْ
 بَيْتًا وَإِنَّ أَوْهَرَ^ط الْبُيُوتِ لَبَيْتُ
 الْعَنكَبُوتِ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾
 إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يَدْعُونَ مِنْ
 دُونِهِ مِنْ شَيْءٍ وَهُوَ الْعَزِيزُ
 الْحَكِيمُ ﴿٤٢﴾ وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ
 نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا
 إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٤٣﴾ خَلَقَ اللَّهُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ إِنَّ فِي
 ذَلِكَ لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٤﴾
 أَتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ
 وَأَقِرِ الصَّلَاةَ^ط إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى
 عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ^ط وَلَذِكْرُ اللَّهِ
 أَكْبَرُ^ط وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾
 * وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ
 إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا
 مِنْهُمْ وَقُولُوا ءَامَنَّا بِالَّذِي
 أُنزِلَ إِلَيْنَا وَأُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَإِلَيْنَا
 وَإِلَهُكُمْ وَاحِدٌ وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿٤٦﴾

وَعَادًا وَثَمُودًا وَقَدْ تَبَيَّنَ لَكُمْ
 مِنْ مَّسْكِينِهِمْ^ط وَزَيْنَ لَهُمُ
 الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ
 السَّبِيلِ وَكَانُوا مُسْتَبْصِرِينَ ﴿٣٨﴾
 وَقُرُورَ وَفِرْعَوْنَ وَهَمَانَ^ط
 وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مُوسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ
 فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانُوا
 سَابِقِينَ ﴿٣٩﴾ فَكُلًّا أَخَذْنَا
 بِذَنبِهِ^ط فَمِنْهُمْ مَنْ أَرْسَلْنَا
 عَلَيْهِ حَاصِبًا وَمِنْهُمْ مَنْ أَخَذَتْهُ
 الصَّيْحَةُ وَمِنْهُمْ مَنْ خَسَفْنَا بِهِ
 الْأَرْضَ وَمِنْهُمْ مَنْ أَغْرَقْنَا
 وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلَكِنْ
 كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٠﴾

38. "Na pia kina A'di na Thamud. Nanyi yamekwisha kubainikieni kutokana na maskani zao. Na Shetani aliwapambia vitendo vyao, na akawazuilia Njia, na hali walikuwa wenye kuona."

39. "Na pia Qaruni na Firauni na Hamana! Na

Musa aliwajja kwa Ishara waziwazi, lakini walijivuna katika nchi, wala hawakuweza kushinda."

40. "Basi kila mmoja Tulimtesa kwa mujibu wa makosa yake. Kati yao wapo Tuliowapelekea kimbunga cha changarawe; na kati yao wapo walionyakuliwa na ukelele; na kati yao wapo ambao Tuliowadidimiza katika ardhi; na kati yao wapo Tuliowazamisha. Wala Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuwadhulumu, lakini walikuwa wenyewe wakijidhulumu nafsi zao."

Kutajwa Kuangamizwa Umma Uliowakataa Mitume Wao

Allah تعالیٰ Anaeleza juu kuhusu umma uliokadhibisha Mitume Alivyo waadhibu adhabu mbalimbali na Kuwalipiza kisasi. 'Ad, kaumu ya Hud عليه السلام, waliokuwa wakiishi *Al-Ahqaaf* (milima ya mchanga ya tao), karibu na Hadhramawt, katika Yemen. Thamud, kaumu ya Swaleh عليه السلام, waliishi *Al-Hijr*, karibu na *Wadi Al-Qura*. Waarabu walikuwa wakijua makazi yao vyema na mara nyingi hupita hapo. Qarun, mmiliki wa mali nyingi na funguo za hazina nzito. Firaun, Mfalme wa Misr katika zama za Musa عليه السلام; na waziri wake, Haman, ni Waqibti wawili waliomkufuru Allah تعالیٰ na Mtume Wake.

فَكُلًّا أَخَذْنَا بِذُنُوبِهِمْ

"Basi kila mmoja Tulimtesa kwa mujibu wa makosa yake."

Maana yake: Adhabu Yake inanasibiana na makosa yao,

فَمِنْهُمْ مَّنْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِ حَاصِبًا

"Kati yao wapo Tuliowapelekea kimbunga cha changarawe..."

Na wao ni 'Ad kwamba wamesema: "Ni nani wenye nguvu kutushinda sisi?" Ukawajia upepo wenye kelele, wenye baridi kali sana, wenye kuvuma kwa nguvu, ukiwa unasomba changarawe za ardhini na kuwatupia, pia unawabeba kutoka ardhini, ikawa unamnyanyua mmoja wao toka ardhini mpaka juu angani, kisha unamgeuza kichwa chini na kumvurumisha. Kisha kiwiliwili kinabakia bila kichwa, kama vile magogo ya mitende yaliyong'olewa,

وَمِنْهُمْ مَّنْ أَخَذَتْهُ الصَّيْحَةُ

“...na kati yao wapo walionyakuliwa na ukelele...”

Hao ni Thamud ambao walikwishaupatiwa ushahidi na dalili ikadhihiri kupitia kwa ngamia jike ambaye jiwe lilipasuka na kumtoa ngamia sawa kabisa na walivyooomba. Pamoja na hayo hawakuamini, bali waliendelea na uasi na kufuru yao, wakawatishia Nabii Swaleh عليه السلام na Waumini walio pamoja naye. Wakapanga kumfukuza na kumpiga mawe. Ikawajia *Sayhah* (ukelele) iliyowaondolea sauti na kutembea.

وَمِنْهُمْ مَّنْ حَسَفْنَا بِهِ الْأَرْضَ

“...na kati yao wapo ambao Tuliowadidimiza katika ardhi...”

Huyo ni Qarun ambaye aliruka mipaka, akafanya maovu, kiburi, akamwasi Allah تعالى, akatembea ardhini kwa maringo, akafurahi, akafanya kiburi, akajiona bora kuliko wengine na akatembea kwa majivuno. Allah تعالى Akaifanya ardhi immeze yeye na nyumba yake. Ataendelea kuzama ndani yake, mpaka Siku ya Kiyama.

وَمِنْهُمْ مَّنْ أَعْرَفْنَا

“...na kati yao wapo Tuliowazamisha.”

Huyo ni Firauni na waziri wake, Haman, pamoja na majeshi yao wote waligharikishwa katika asubuhi moja tu, wala hakusalia hata mmoja wa kusimulia yaliyowakumba wenzake.

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُظْلِمَهُمْ

“Wala Mwenyezi Mungu hakuwa mwenye kuwadhulumu...”

Maana yake: Katika Aliyowafanyia.

وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٦﴾

“...lakini walikuwa wenyewe wakijidhulumu nafsi zao.”

Maana yake: Bali Aliwafanyia hayo, jaza yenye kuwafikiana na yaliyochumwa na mikono yao.

مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ كَمَثَلِ الْعَنْكَبُوتِ اتَّخَذَتْ بَيْتًا ۗ وَإِنَّ أَوْهَنَ الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوتِ ۗ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا
يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مِنْ شَيْءٍ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤٢﴾ وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضَّرِبُهَا
لِلنَّاسِ ۗ وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٤٣﴾

41. "Mfano wa waliowafanya walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, ni mfano wa buibui alivyojitandia nyumba. Na hakika nyumba dhaifu mno kuliko zote ni jumba la buibui, laiti kuwa wanajua."

42. "Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anajua kila kitu wanachokiomba badala Yake Yeye. Na Yeye Ndiye Mtukufu Mwenye Nguvu Mwenye Hikima."

43. "Na hiyo ni mifano Tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu."

Kumithilishwa kwa Miungu ya Washirikina na Nyumba ya Buibui

Huu ni mfano ambao Allah تعالی Aliupiga kwa washirikina kwa kuifanya miungu vitu ambavyo ni ghairi ya Allah تعالی huku wakitaraji kunusuriwa na kuruzukiwa nao, na wakiwang'angania wakati wa shida.

Basi, wao katika hayo, ni kama nyumba ya buibui kutokana na udhaifu na uduni wake. Hawapati chochote kutoka kwa miungu yao hiyo, bali ni kama anayeng'angana na nyumba ya buibui, kwani hanufaiki nayo chochote. Lau wangeliyajua haya, wasingelimfanya asiyekuwa Allah تعالی kuwa mlinzi.

Hii ni kinyume na Muislamu anayeamini moyoni, pamoja na haya anafanya amali njema katika kuifuata shariah, kwani yeye ni mwenye kushikamana na kishikio madhubuti kisichovunjika, kwa sababu ya nguvu na umadhubuti wake.

Kisha, Allah تعالی Aliwaonya wanaomwabudu asiyekuwa Yeye na kumshirikisha. Allah تعالی Anazijua amali zao na Anavijua wanavyomshirikisha navyo katika washindani, na Atawajazia kulingana na wasifu wao. Kwa hakika Yeye ni Mwenye Hikima, Mjuzi. Kisha, Allah تعالی Amesema:

وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٣٨﴾

“Na hiyo ni mifano Tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu.”

Maana yake: Wala hawayafahamu haya na kuyazingatia, isipokuwa waliozama katika elimu. Ibn Abu Hatim alinukuu kutoka kwa ‘Amri bin Murrah kwamba: “Sijaipita Aya yoyote katika Kitabu cha Allah تعالى ambayo siujui, bali lilinihuzunisha hilo. Kwa sababu, nilisikia kwamba Allah تعالى Amesema:

وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٣٨﴾

“Na hiyo ni mifano Tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu.”¹

خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٩﴾ أَتَلُمَا
أَوْحَىٰ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ وَأَقْرَبَ الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ
وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٠﴾

44. Mwenyezi Mungu Ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Kwa hakika katika hayo ipo Ishara kwa Waumini.

45. Soma uliyofunuliwa katika Kitabu, na ushike Swala. Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumtaja Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu Anayajua mnayoyatenda.

Allah تعالى Anaeleza Kudura Yake kubwa kwamba Yeye Aliumba mbingu na ardhi kwa haki, yaani, si katika njia ya kufanya upuuzi au mchezo,

لِتُجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا تَسْعَىٰ ﴿٤١﴾

“...ili kila nafsi ilipwe kwa iliyoyafanya.” (20:15)

¹ Ibn Abi Hatim na. 17344, Ad-Dur Al-Manthur 6:464.

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَفْتُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحَسَنَى ﴿٣١﴾

“...ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema Awalipe mema.” (53:31)

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٢﴾

“Kwa hakika katika hayo ipo Ishara kwa Waumini.”

Maana yake: Kwa dalili wazi wazi kwamba Allah تعالى ni Mpweke katika Kuumba na Kuyapanga mambo na Uungu.

Amri ya Kufikisha Ujumbe, Kusoma Qur’an na Kuswali

Kisha Allah تعالى Alimwamuru Mtume Wake na Waumini kusoma Qur’an, yaani kuisoma na kuifikisha kwa watu.

وَأَقِمِ الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ

“...na ushike Swala. Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumtaja Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa.”

Maana yake: Kwamba Swala inajumuisha mambo mawili: kuacha machafu na maovu, yaani, kuidumisha kwake huchukulika katika kuyaacha hayo.

Imamu Ahmad alinukuu kwamba Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Mtu mmoja alimjia Mtume ﷺ akasema: “Fulani huwa anasali usiku, kukicha huiba.” Akasema:

«إِنَّهُ سَيَنْهَاهُ مَا تَقُولُ»

“Swala hiyo itamkataza hayo unayoyasema.”¹

Halikadhalika, Swala hujumuisha kumtaja Allah تعالى, na hilo ndilo lengo kuu. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

¹ Ahmad 2:447.

وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ

“Na kwa yakini kumtaja Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa.”

Maana yake: Ni kubwa kuliko la awali,

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anayajua mnayoyatenda.”

Maana yake: Anazijua amali na kauli zenu zote. Abu Al-‘Aliyah aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ۗ

“Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu.”

Amesema: “Hakika, Swala ina mambo matatu. Hivyo basi Swala yoyote isio na mambo haya matatu sio swala: Ikhilasi, kuwa na khofu kwa Allah تعالى na kumtaja Allah تعالى. Ikhilasi humuamuru mambo mema, kuwa na khofu kwa Allah تعالى, humzuia dhidi ya maovu, na kumtaja Allah تعالى ni Qur’an, ambayo ina maamrishi na makatazo. Ibn ‘Awn Al-Answari amesema: “Ukiwa katika Swala, uko katika jambo jema, na inakuepusha dhidi ya machafu na maovu, na unalolifanya ni katika kumtaja Allah تعالى, ambalo ndilo kubwa.”

* وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ وَقُولُوا ءَامَنَّا

بِالَّذِي أُنزِلَ إِلَيْنَا وَأُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَإِلَيْنَا وَإِلَيْكُمْ وَإِلَيْنَا وَإِلَيْكُمْ وَخُنْ لَهُدْ مُسْلِمُونَ ﴿٤٦﴾

46. “Wala msjadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tumeyaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu. Na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja. Na sisi ni wenye kusilimu kwake.”

Kujadiliana na Watu wa Kitabu

Kinachomaanishwa hapa ni kwamba, yeyote anayetaka kuuliza juu ya dini kutoka kwao, basi ajadiliane kwa yaliyo mema, kwani hilo litakuwa ni lenye manufaa zaidi. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ

“Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema...” (16:125)

Allah تعالى Aliwaambia Musa عليه السلام na Harun عليه السلام pindi Alipowatuma kwa Firaun

فَقُولَا لَهُ قَوْلًا لَّيِّنًا لِّعَلَّهُ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَخْشَى ﴿٤٤﴾

“Muambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa.” (20:44).

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ

“...isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao.”

Maana yake: Wanaoupa mgongo ukweli, wakazifumbia macho hoja za wazi wazi, wakakaidi na wakafanya kiburi. Basi, wakati huo atabadilika kutoka katika majadiliano na kuingia katika mapambano na kupigana nao kwa yale wanayowazuilia na kuwarudisha. Allah تعالى Amesema:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيُقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ط

وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنْفَعٌ لِلنَّاسِ

“Kwa hakika Tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na Tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na Tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu.”

Mpaka, Kauli Yake,

﴿٢٥﴾ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ

**“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu Mwenye Kushinda.”
(57:25)**

Jabir amesema: “Hapa Allah تعالى Ametuamuru kwamba, mwenye kukikhalifu kitabu cha Allah تعالى tumpige upanga.” Na Kauli Yake Allah تعالى

وَقُولُوا ءَامَنَّا بِالَّذِي ءُنزِلَ ءِإَيْنَا وَأُنزِلَ إِلَيْكُمْ

“Na semeni: Tumeyaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu.”

Maana yake: Ikiwa watatoa khabari kwa ambayo hatuujui ukweli wala uongo wake, basi sisi, hatutangulizi kuzikanusha, kwani yawezekana kuwa ni kweli, wala hatuharakishi kuzisadiki, kwani yawezekana kuwa za uongo. Lakini, tunaamini kwa ujumla chini ya sharti kwamba isiwe imebadilishwa au imetafsiriwa vingine. Bukhari رحمه الله تعالى amesema kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Watu wa Kitabu walikuwa wakiisoma Taurat kwa lugha ya Kiebrania na wanaitafsiri kwa Kiarabu kwa ajili ya waislamu. Mtume ﷺ amesema:

﴿٢٥﴾ لَا تُصَدِّقُوا أَهْلَ الْكِتَابِ وَلَا تَكْتُمُوهُمْ، وَقُولُوا: ءَمَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ، وَإِلَيْنَا وَإِلَيْكُمْ رَاجِدٌ، وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ

“Msiwasadiki wala kuwakadhibisha Watu wa Kitabu. Semeni: Tumemwamini Allah na yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoshushwa kwenu. Mola wetu na wenu ni mmoja, nasi ni wanyenyekevu Kwake.”

Hadithi hii ilisimuliwa na Bukhari peke yake. Bukhari alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kwamba amesema: “Vipi mnawauliza Watu wa Kitabu ilhali Kitabu chenu alichoteremshiwa Mtume ﷺ ndicho cha hivi karibuni kabisa, mnakisoma kikiwa halisi, hakikuchafuliwa, kimekwisha kukuelezeni kwamba Watu wa Kitabu walibadilisha kitabu cha Allah تعالى wakakigeuza na kukiandika kwa mikono yao na wakasema: Kinatoka kwa Allah تعالى, ili wanunue kutokana

nacho, thamani ndogo? Ilimu iliyokujieni haikuwakatazeni juu ya kuwauliza? Hapana, Wallah! Hatujawahi kumwona mtu yeyote miongoni mwao akiwauliza kuhusu mliyoteremshiwa.”¹ Bukhari, pia alinukuu kutoka kwa Humayd bin ‘Abdur-Rahman kwamba alimsikia Mu‘awiyah رضي الله عنه akizungumza na kikundi cha Makuraishi huko Madinah. Akamtaja Ka‘b Al-Ahbaar, akasema: “Alikuwa mmojawapo wa wakweli zaidi katika hao wanaozungumzia juu ya Watu wa Kitabu. Pamoja na hayo, bado huwa tunakuta kuna uongo ndani yake.”²

(Mimi nasema), maana yake, kunaweza kuwepo uongo kilugha pasi na makusudio, kwa sababu alikuwa akisimulia kutoka maandiko yanayodhaniwa vyema, ilhali kuna mambo yaliyowekwa na ya uongo. Hayo ni kwa sababu, katika desturi yao hawakuwepo mahodari wa kuyahifadhi moyoni, kama ilivyo kwa umma huu. Pamoja na haya, zimekuwepo Hadithi nyingi katika umma huu ambazo hapana azijuaye, isipokuwa Allah تعالى na wale ambao, Allah تعالى. Amewapa ujuzi wa hadithi hizo kwa kiasi chake. Hamdi na Shukurani ni za Allah تعالى.



¹ Fath Al-Bari 8:20.

² Bukhari na. 7363.

وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ ۚ
 فَالَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ
 يُؤْمِنُونَ بِهِ ۖ وَمِنْ هَؤُلَاءِ مَنْ يُؤْمِنُ بِهِ ۚ
 وَمَا تَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا الْكَافِرُونَ ﴿٤٧﴾ وَمَا كُنْتَ تَتْلُوا
 مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُ بِيَمِينِكَ ۖ إِذَا لَأَزْتَابُ
 الْمُبْطِلُونَ ﴿٤٨﴾ بَلْ هُوَ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ فِي صُدُورِ
 الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ ۚ وَمَا تَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا
 الظَّالِمُونَ ﴿٤٩﴾ وَقَالُوا لَوْلَا أَنْزَلَ عَلَيْنَا آيَاتٌ مِّنْ
 رَبِّهِ ۗ قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ
 ﴿٥٠﴾ أَوَلَمْ يَكْفِهِمْ أَنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ يُتْلَى
 عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَرَحْمَةً وَذِكْرَى لِقَوْمٍ
 يُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾ قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ بِنبِيِّ وَيَتَّكُمُ شَهِيدًا ۖ
 يَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا
 بِالْبَيْطِلِ وَكَفَرُوا بِاللَّهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٥٢﴾
 وَتَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ ۚ وَلَوْلَا أَجَلٌ مُّسَيَّءٌ لِّجَآءِهِمْ
 الْعَذَابُ وَلَيَأْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٣﴾
 يَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ
 ﴿٥٤﴾ يَوْمَ يَغْشَاهُمْ الْعَذَابُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ
 أَرْجُلِهِمْ وَيَقُولُ دُوُقُوءًا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٥﴾

وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ ۚ
 فَالَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ
 يُؤْمِنُونَ بِهِ ۖ وَمِنْ هَؤُلَاءِ مَنْ يُؤْمِنُ بِهِ ۚ
 وَمَا تَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا
 الْكَافِرُونَ ﴿٤٧﴾ وَمَا كُنْتَ تَتْلُوا
 مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُ
 بِيَمِينِكَ ۖ إِذَا لَأَزْتَابُ الْمُبْطِلُونَ
 ﴿٤٨﴾ بَلْ هُوَ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ فِي
 صُدُورِ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ ۚ وَمَا
 تَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا الظَّالِمُونَ ﴿٤٩﴾

47. "Na namna hivi Tumeku-
 teremshia Kitabu (cha
 Qur'ani). Basi wale
 Tuliowapa Kitabu (cha
 Biblia) wataiamini
 (Qur'ani), na miongoni
 mwa hawa (washirikina)
 wapo watakaoiamini. Na
 hawazikatai Ishara Zetu
 isipokuwa makafiri."

48. "Na wewe hukuwa
 kabla yake unasoma kitabu
 chochote, wala hukuki-
 andika kwa mkono wako
 wa kulia. Ingelikuwa hivyo

wangelifanya shaka wavunjifu."

49. "Bali hii (Qur'ani) ni Ishara zilizo wazi katika vifua vya waliopewa ilimu. Na hawazikatai Ishara Zetu isipokuwa wenye kudhulumu."

Ushahidi kwamba Qur'an lilitemshwa Kutoka kwa Allah تعالی.

Ibn Jarir رحمه الله تعالی amesema: "Allah تعالی Amesema, 'Kama ambavyo Tuliteremsha Kitabu kwa Mitume wa kabla yako, ewe Muhammad! Pia Tulikiteremsha Kitabu hiki kwako.'"¹

Na haya aliyoyasema ni ya sawa na yananasibiana nayo na uhusiano wake pia ni wa kweli. Kauli ya Allah تعالی:

فَالَّذِينَ ءَاتَيْنَهُمُ الْكِتَابَ يُؤْمِنُونَ بِهِ

"Basi wale Tuliowapa Kitabu (cha Biblia) wataiamini (Qur'ani)..."

Maana yake: Wanachuoni wao watambuzi walioichukua na kuisoma itakikanavyo, kama vile 'Abdullah bin Salaam, Salman Al-Farisi na mfano wao,

وَمِنْ هَؤُلَاءِ مَنْ يُؤْمِنُ بِهِ

"...na miongoni mwa hawa (washirikina) wapo watakaoiamini."

Maana yake: Waarabu wa Kuraishi na wengine.

وَمَا نَجِدُ بِغَايِبَتِنَا إِلَّا الْكٰفِرُونَ ﴿٤٧﴾

"Na hawazikatai Ishara Zetu isipokuwa makafiri."

Maana yake: Hawaikadhibishi na kupinga ukweli wake isipokuwa anayeficha haki ndani ya batili, na anayeufunika mwangaza wa jua kwa kufumba macho, lakini wapi!

وَمَا كُنْتُمْ تَتْلُوا مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُمْ بِيَمِينِكُمْ

"Na wewe hukuwa kabla yake unasoma kitabu chochote, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kulia."

¹ At-Tabari 20:50.

Maana yake: Ewe Muhammad umekaa na kaumu yako kwa muda mrefu, kabla ya kukujia hii Qur'an, na katika kipindi hicho hukuwahi kusoma kitabu chochote wala kuweza kuandika, bali kila mmoja katika kaumu yako na wengine anajua kwamba wewe ni **ummiy**, (husomi kilichoandikwa wala kuandika chochote kikasomwa). Huu ni wasifu wake katika Vitabu vilivyopita. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الَّذِي الَّذِي تَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ
وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُمْ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ

“Ambao wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anayewaamrisha mema na anawakanya maovu...” (7:157)

Na hivi ndivyo ilivyokuwa siku zote kwa Mtume ﷺ mpaka Siku ya Kiyama. Hakuweza kuandika wala kupiga mstari, japo herufi moja kwa mkono wake, bali alikuwa na waandishi wake walikuwa wakiandika mbele yake wahyi na barua mbalimbali kwenda maeneo kadha wa kadha.

إِذَا لَازَتْكَ الْمُتَبَلِّغُونَ ﴿٥٠﴾

“Ingelikuwa hivyo wangelifanya shaka wavunjifu.”

Maana yake: Lau ungelikuwa unaweza kuandika, baadhi ya watu majahili wangelitia shaka na kusema: Haya umejifunza kutoka katika Vitabu vilivyorithiwa kutoka kwa Mitume wa hapo kabla. Pamoja na haya, walijasema hayo licha ya kujua kwao kwamba yeye ni *Ummiy*, hawezi kuandika.

وَقَالُوا أَسْطِطِرُّ الْآلُوفِينَ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٥١﴾

“Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni.” (25:5)

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Sema: Ameyateremsha haya Ajuaye siri za katika mbingu na ardhi.” (25:6)

Katika Aya hii, Allah تعالى Anasema:

بَلْ هُوَ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ فِي صُدُورِ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ

“Bali hii (Qur’ani) ni Ishara zilizo wazi katika vifua vya waliopewa ilimu.”

Maana yake: Qur’an hii ni *ishara* wazi wazi katika kuujuu ukweli, amri, makatazo na khabari. Maulamaa huihifadhi moyoni, na Allah تعالى Amewarahisishia kuihifadhi huko, kuisoma na kuitafsiri.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدَكِّرٍ ﴿١٧﴾

“Na bila ya shaka Sisi Tumeifanya Qur’ani iwe nyepesi kufahamika. Lakini yupo anayekumbuka?” (54:17)

Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا وَقَدْ أُعْطِيَ مَا آمَنَ عَلَىٰ مِنْهُ الْبَشَرُ، وَإِنَّمَا كَانَ الَّذِي أُوتِيَهُ وَحْيًا أَوْحَاهُ اللَّهُ إِلَيْ، فَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَكْثَرَهُمْ تَابِعًا»

“Hapana Nabii yeyote, bali alipatiwa kitu cha kuwafanya watu wamuamini, na mimi nimepatiwa Wahyi alionifunulia Allah, basi natarajia kuwa na wafuasi wengi zaidi kuliko wao.”¹

Na katika Hadithi ya ‘Iyadhw bin Himar رضي الله عنه katika *Sahih Muslim*, Anasema:

«إِنِّي مُبْتَلِيكَ وَمُبْتَلِي بِكَ، وَمُنَزَّلُ عَلَيْكَ كِتَابًا لَا يَغْسِلُهُ الْمَاءُ، تَقْرُؤُهُ تَابِعًا وَمِطْطَانًا»

“Mimi Nakujaribu wewe na Ninawajaribu wengine kupitia kwako. Pia Ninakuteremshia kitabu ambacho hakitaoshwa na maji, utakisoma ukiwa umelala na ukiwa macho.”²

¹Fat’h Al-Bari 8:619.

²Muslim 4:219.

Maana yake: Lau maji yatapaosha mahali palipoandikwa maandiko hayo, basi mahali hapo pasingelihitajiwa tena, kwa sababu, Hadithi nyengine imebainisha kuwa: "Lau Qur'an ingelikuwa katika Ngozi isingeunguzwa na moto."³ kwa sababu imehifadhiwa vifuani na imerahisishwa katika ulimi na udhibiti nyoyoni kwa lafudhi na maana. Kwa ajili hii, ilikuja katika Vitabu vilivyotangulia kwamba umma huu ni wenye kukibeba Kitabu nyoyoni mwao.

وَمَا تَجِدُ بِغَايَتِنَا إِلَّا الظَّالِمُونَ ﴿٥١﴾

"Na hawazikatai Ishara Zetu isipokuwa wenye kudhulumu."

Maana yake: Huukadhibisha, kuubeza ukweli wake na kuukataa isipokuwa madhalimu, yaani warukaji mipaka wenye kiburi ambao wanaujua ukweli, lakini wanaupinga. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٥٢﴾

"Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini. Ijapo kuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu." (10:96-97)

وَقَالُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَاتٌ مِّن رَّبِّهِ قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِندَ اللَّهِ وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥٢﴾ أُولَئِكَ يَكْفِهِمْ أَنَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَرَحْمَةً وَذِكْرَىٰ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٣﴾ قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ شَهِيدًا ۗ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْبَطِلِ وَكَفَرُوا بِاللَّهِ أُوتِيَكَ هُمُ الْخَسِرُونَ ﴿٥٤﴾

50. "Na wamesema: Mbona hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Ishara ziko kwake Mwenyezi Mungu; ama mimi kwa hakika ni mwonyaji mwenye kubainisha tu."

¹Ahmad 4:155. Hadithi hii ni dhaifu kuna mpokezi Hajaj bin Muhammad Al-Masisi Al-Awari.

51. “Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa? Hakika katika hayo zipo rehema na mawaidha kwa watu wanaoamini.”

52. “Sema: Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Shahidi baina yangu na nyinyi. Anayajua yaliomo katika mbingu na ardhi. Na wale wanaoamini upotovu na wakamkataa Mwenyezi Mungu, hao ndio waliokhasiri.”

Washirikina Wanataka Ishara, na jawabu kwao

Allah تعالیٰ Anaelezea ufidhuli wa washirikina kutaka ishara zinazoonesha kuwa Muhammad ﷺ ni Mtume, kama vile Swaleh عليه السلام alivyomtoa ngamia jike. Allah تعالیٰ Amesema:

قُلْ

“Sema...” (Muhammad!).

إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ

“Ishara ziko Kwake Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Kwa hakika jambo hilo lipo kwa Allah تعالیٰ, kwa sababu, kama Anajua kwamba mtaongoka kwa kujibiwa kwenu ombi lenu, kwani hilo ni sahali na jepesi mno Kwake. Lakini, Yeye Anajua kwamba nyinyi mmekusudia kuwa wakaidi na kunipa mtihani, basi hakujibuni kwa hilo. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ:

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوَّلُونَ ۗ وَءَاتَيْنَا ثُمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوا بِهَا ۗ

“Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na Tuliwapa Wathamudi ngamia jike kuwa ni Ishara iliyodhaahiri, lakini walidhulumu kwayo.” (17:59)

وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥٩﴾

“...ama mimi kwa hakika ni mwonyaji mwenye kubainisha tu.”

Maana yake: Kwa hakika, nimetumwa kwenu kama mwonyaji, na nimekwisha yabainisha maonyo. Jukumu langu ni kukufikishieni Ujumbe wa Allah تعالى.

مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ وَمَنْ يُضِلِّ فَلَنْ تَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُرْشِدًا ﴿١٧﴾

“Ambaye Mwenyezi Mungu Anamwongoa basi huyo ni mwenye kuongoka. Na anayemuacha kupotea basi hutampatia mlinzi wala mwongozi.” (18:17)

﴿ لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهُ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ﴾

“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye.” (2:272)

Kisha, Allah تعالى Alibainisha kukithiri kwa ujahili wao na upumbavu wao pindi walipotaka ishara za kuwajulisha juu ya ukweli wa aliyowaletea Muhammad ﷺ, bila shaka, alikwishawajia na Kitabu kitukufu ambacho hakikutwi na ubatilifu kabla au baada. Kitabu ambacho ni kikubwa kuliko muujiza wowote, kwani wambuji na wataalamu wa lugha walishindwa kuleta mfano wake, bali hata sura kumi, bali hata sura moja pia. Allah تعالى Amesema:

أَوَلَمْ يَكْفِهِمْ أَنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ

“Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa?”

Kwamba, kwani haikuwatosha ishara kwamba Sisi Tumekuteremshia Kitabu kikuu ambacho ndani yake kuna khabari za kabla yao, maelezo ya mambo ya baada yao, na yaliyo miongoni mwao. Wakati huo huo, wewe ni “Ummiy”, Hajui kusoma wala kuandika kikasomwa, wala hukuwahi kuchanganyika na Watu wa Kitabu, lakini umewaletea khabari za yaliyo katika Maandiko yaliyotangulia kwa ubainifu ulio sawa sawa katika waliyokhitilafiana ndani yake na kwa ukweli dhahiri kabisa. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

﴿ أَوَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ آيَةٌ أَنْ يَعْلَمَهُرُ عَلَمُهُمْ قَوْمًا بِتِي إِسْرَائِيلَ ﴾

“Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili?” (26:197)

وَقَالُوا لَوْلَا يَأْتِينَا بِآيَاتٍ مِّن رَّبِّنَا أَوْلَمَ تَأْتِيهِم بَيِّنَةٌ مَّا فِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٣٣﴾

“Na wamesema: Kwa nini hakutuletea muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Je! Haikuwafikilia dalili wazi ya yaliyomo katika Vitabu vya kale?” (20:133)

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنَ الْأَنْبِيَاءِ مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا قَدْ أُعْطِيَ مِنَ الْآيَاتِ مَا مِثْلُهُ آمَنَ عَلَيْهِ النَّبَرُ، وَإِنَّمَا كَانَ الَّذِي أُوتِيَهُ وَخِيَا أَوْحَاهُ اللَّهُ إِلَيْهِ، فَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَكْثَرَهُمْ تَابِعًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Hapakuwa na Nabii yeyote katika Manabii, isipokuwa alipewa miujiza ya kuwafanya watu wamwamini. Muujiza niliopatiwa mimi ni Wahyi alionifunulia Allah, basi natarajia kwamba mimi nitakuwa na wafuasi wengi zaidi yao katika Siku ya Kiyama.”¹

Pia imenukuliwa na Bukhari na Muslim.² Allah تعالى Amesema:

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَرَحْمَةً وَذِكْرَىٰ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١٣٤﴾

“Hakika katika hayo zipo rehema na mawaidha kwa watu wanaoamini.”

Maana yake: Hakika katika Qur’an kuna rehema, maana yake, ubainifu wa ukweli na uondoshaji wa upotovu na ukumbusho kwa Waumini juu ya kuteremshwa kwa mateso na adhabu kwa wakadhibishaji na waasi. Kisha, Allah تعالى Amesema:

قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ بَيِّنًا وَبَيْنَكُمْ شَهِيدًا

“Sema: Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Shahidi baina yangu na nyinyi.”

¹ Ahmad 2:341.

² Fat’h Al-Bari 8:619, Muslim 1:134.

Maana yake: Yeye ni Mjuzi zaidi kuhusu maneno ya ukadhibishaji mnayotoa, na Anayajua ninayokuambieni pale ninapokupeni khabari kwamba Yeye Kanituma mimi. Kama ningelikuwa naongopa juu Yake, basi Angelilipiza kisasi kwangu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤٤﴾ لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ
الْوَتِينَ ﴿٤٦﴾ فَمَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٤٧﴾

“Na lau kama angelituzulia baadhi ya maneno tu, Bila ya shaka Tungelimshika kwa Mkono wa Kulia, kisha kwa hakika Tungelimkata mshipa mkubwa wa moyo! Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza kutuzuia.” (69:44-47)

Kwa hakika, mimi ni mkweli katika niliyokupeni khabari. Kwa ajili hii, Alinisaidia kwa miujiza dhahiri na dalili zenye kukata (ubishi).

يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Anayajua yaliomo katika mbingu na ardhi.”

Maana yake: Hapana cha kufichikana dhidi Yake,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْبَاطِلِ وَكَفَرُوا بِاللَّهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٥٠﴾

“Na wale wanaoamini upotovu na wakamkataa Mwenyezi Mungu, hao ndio waliokhasiri.”

Maana yake: Siku ya Kiyama, Atawalipa kwa waliyoyafanya na Atawakabili kwa waliyoyafanya, katika kukadhibisha kwao ukweli na kufuata upotovu.

Waliwakadhibisha Mitume wa Allah تعالى, pamoja na kusimamisha dalili juu ya ukweli wao. Wakaamini mataghuti na masanamu bila ushahidi.

Basi, Atawalipa kwa hayo, kwani Yeye ni Mwingi wa Hekima, Mjuzi.

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ ۗ وَلَوْلَا أَجَلٌ مُّسَمًّى لَجَاءَهُمُ الْعَذَابُ وَلَيَأْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٧﴾ يَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٤٨﴾ يَوْمَ يَغْشَاهُمْ الْعَذَابُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ وَيَقُولُ ذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٩﴾

53. *“Na wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka. Na lau kuwa hapana wakati maalumu uliowekwa, basi adhabu ingeliwajia, na ingeliwatokea kwa ghafla, na hali wao hawana khabari.”*

54. *“Wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka, na hali Jahannamu kwa hakika imewazunguka makafiri!”*

55. *“Siku itapowafunika adhabu hiyo kutoka juu yao na chini ya miguu yao, na atasema: Onjeni hayo mliyokuwa mkiyatenda!”*

Washirikina Waomba Waharakishiwe Adhabu

Allah تعالی Anaeleza kuhusu washirikina kutaka adhabu yao kutoka kwa Allah تعالی iharakishwe.

Ni kama aya:

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِنَّكَ كَاتِبُ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ
أَوْ آتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٨٣﴾

“Na waliposema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyochungu.” (8:32)

Katika Aya hii Allah تعالی Anasema,

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ ۗ وَلَوْلَا أَجَلٌ مُّسَمًّى لَجَاءَهُمُ الْعَذَابُ

“Na wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka. Na lau kuwa hapana wakati maalumu uliowekwa, basi adhabu ingeliwajia...”

Lau kama Allah تعالى Hakupitisha hukumu kuwa iakhirishwe mpaka Siku ya Kiyama, basi adhabu ingeliwajia katika muda wa karibu na kwa wepesi kama wanavyotaka iharakishwe. Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَلَيَأْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٣﴾ يَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ
بِالْكَافِرِينَ ﴿٥٤﴾

**“...na ingeliwatokea kwa ghafla, na hali wao hawana khabari.
“Wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka, na hali Jahannamu
kwa hakika imewazunguka makafiri!..” (29:53-54)**

Maana yake: wanaomba waharakishiwe adhabu japo itawatokea tu, hakuna mashaka. Halafu, Allah تعالى Amesema:

يَوْمَ يَغْشَاهُمْ الْعَذَابُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ

**“Siku itapowafunika adhabu hiyo kutoka juu yao na chini ya miguu
yao...”**

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

هُم مِّنْ جَهَنَّمَ مَهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ

**“Jahannamu itakuwa kitanda chao na juu yao nguo za moto za
kujifunika.” (7:41).**

Na Allah تعالى Amesema;

هُم مِّنْ فَوْقِهِمْ ظُلَلٌ مِّنَ النَّارِ وَمِنْ تَحْتِهِمْ ظُلَلٌ

**“Yatawekwa juu yao matabaka ya moto, na chini yao matabaka.”
(39:16).**

Na Allah تعالى Amesema,

لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا يَكْفُرُونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ

**“Lau wangelijua wale waliokufuru wakati ambao hawatazuia
Moto kwenye nyuso zao wala migongo yao.” (21:39)**

Kwa hivyo, moto utawafunika pande zao zote. Na hii ni adhabu kali zaidi ya kimaumbile.

Kauli ya Allah تعالى:

وَيَقُولُ ذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٧﴾

“...na atasema: Onjeni hayo mliyokuwa mkiyatenda!”

Ni kitisho na karipio kali. Hii ni adhabu ya kisaikolojia.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٤٨﴾ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾

“Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu! Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo.” (54:48-49)

Na Allah تعالى Amesema:

يَوْمَ يُدْعُونَ إِلَىٰ نَارِ جَهَنَّمَ دَعَاً ﴿٥٢﴾ هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٥٣﴾ أَفَسِحْرٌ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿٥٤﴾ أَصَلَوْهَا فَأَصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٥﴾

“Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu, (Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha!Je! Huu ni uchawi, au hamwoni tu? Uingieni, mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu. Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda.” (52:13-16).

* * *

يَعْبَادِي الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ أَرْضِي وَاسِعَةٌ فَإِنِّي فَاعْبُدُونِ
 ۞ كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ۗ ثُمَّ إِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ۞
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُبَوِّئَنَّهُمْ مِّنَ الْجَنَّةِ
 غُرَفًا تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ نِعْمَ أَجْرُ
 الْعَمِلِينَ ۞ الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ۞
 وَكَأَيِّن مِّن دَآئِبَةٍ لَا تَحْمِلُ رِزْقَهَا اللَّهُ يَرْزُقُهَا وَإِيَّاكُمْ ۗ وَهُوَ
 السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۞ وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّن خَلَقَ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۗ فَأَنَّى
 يُؤْفَكُونَ ۞ اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ مِن عِبَادِهِ
 وَيَقْدِرُ لَهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ۞ وَلَئِن سَأَلْتَهُم
 مِّن نَّزْلِ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْبَبَا بِهِ الْأَرْضَ مِن بَعْدِ
 مَوْتِهَا لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۗ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا
 يَعْقِلُونَ ۞

يَعْبَادِي الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ أَرْضِي
 وَاسِعَةٌ فَإِنِّي فَاعْبُدُونِ ۞ كُلُّ
 نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ۗ ثُمَّ إِلَيْنَا
 تُرْجَعُونَ ۞ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُبَوِّئَنَّهُمْ مِّنَ
 الْجَنَّةِ غُرَفًا تَجْرِي مِن تَحْتِهَا
 الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ نِعْمَ أَجْرُ
 الْعَمِلِينَ ۞ الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ
 يَتَوَكَّلُونَ ۞ وَكَأَيِّن مِّن دَآئِبَةٍ لَا
 تَحْمِلُ رِزْقَهَا اللَّهُ يَرْزُقُهَا وَإِيَّاكُمْ ۗ وَهُوَ
 السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۞

56. "Enyi waja wangu mliloamini! Kwa hakika ardhi yangu ina wasaa. Basi niabuduni Mimi Peko Yangu."

57. "Kila nafsi itaonja mauti. Kisha mtarudishwa Kwetu."

58. "Na ambao wameamini na wakatenda mema, bila ya shaka Tutawaweka katika maghorofa ya Peponi yenye kupitiwa chini yake mito, wakidumu humo. Ni mwema ulioje huo ujira wa watendao."

59. "Ambao walisubiri, na wakamtegemea Mola wao Mlezi."

60. "Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu Anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kujua."

Amri ya Kuhama na Ahadi ya Kuruzukiwa na Kulipwa Malipo Mema

Hii ni Amri ya Allah ﷻ kwa waja wake Waumini kuhama kutoka katika mji ambao hawawezi kusimamisha Dini ndani yake na kwenda katika ardhi kunjufu ambapo panayumkinika kusimamishwa Dini kwa maana ya kumpwekesha Allah ﷻ na wamwabudu kama Alivyowaamuru.

Kwa minajili hii, Allah ﷻ Amesema:

يَعْبَادِي الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ أَرْضِي وَاسِعَةٌ فَإِنِّي فَاعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

“Enyi waja wangu mlioamini! Kwa hakika ardhi Yangu ina wasaa. Basi niabuduni Mimi Peke Yangu.”

Kwa hivyo, pindi walipodhikika kuishi, wenye kunyongeshwa huko Makkah, walitoka na kwenda katika nchi ya Uhabeshi (Ethiopia) ili wapate salama katika dini yao huko. Wakawakuta watu wazuri kwa kupokea wageni, As-hamah An-Najjashi, mfalme wa Uhabeshi (Allah ﷻ Amrehemu). Akawapa makazi na akawasaidia na kuwaunga mkono, akawapa heshima nchini mwake. Baada ya hapo, Mtume ﷺ alihama na masahaba waliosalia kwenda *Madinah An-Nabawi, Yathrib Al-Mutwahharah*.

Kisha, Allah ﷻ Amesema:

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةٌ لِّلْمَوْتِ ثُمَّ إِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٥٧﴾

“Kila nafsi itaonja mauti. Kisha mtarudishwa Kwetu.”

Maana yake: Mauti yatawakuta popote mlipo, basi muwe katika kumtii Allah ﷻ na jinsi Alivyowaamuru. Kufanya hivyo ni kheri kwenu, kwani mauti hayana budi wala hakuna pa kuyakwepea. Halafu marejeo ni kwa Allah ﷻ. Basi, mwenye kumtii, Atamlipa malipo bora na Atamlipa thawabu timilifu. Kwa ajili hii, Allah ﷻ Amesema:

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُؤْتِيَنَّهُمْ مِّنَ الْجَنَّةِ غُرَفًا تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Na ambao wameamini na wakatenda mema, bila ya shaka Tutawaweka katika maghorofa ya Peponi yenye kupitiwa chini yake mito...”

Maana yake: Nitawapa makazi ya mahali pa juu katika Janna ambazo mito inapita chini yake ikiwa katika namna tofauti tofauti, tokea maji, mvinyo, asali na maziwa. Watatumia na kuyatiririsha namna watakavyopenda.

خَلِيدِينَ فِيهَا

“...wakidumu humo.”

Maana yake: Watakaa humo milele, bila ya kutaka kuondoka kutoka humo,

نِعْمَ أَجْرُ الْعَمَلِينَ ﴿٥٦﴾

“Ni mwema ulioje huo ujira wa watendao.”

Neema za maghorofa haya ni malipo juu ya amali za Waumini.

الَّذِينَ صَبَرُوا

“Ambao walisubiri...”

Maana yake: Katika Dini yao, wakahama kwenda kwa Allah تعالى, wakapigana na adui, wakatengana na ahli na ndugu kwa ajili ya kutafuta Radhi za Allah رحمة الله تعالى na kutumaini yaliyo Kwake na kusadiki miadi Yake. Ibn Abu Hatim alimnukuu Abu Mu’aniq Al-Ash’ari kwamba Malik bin Al-Ash’ari alimsimulia kwamba Mtume ﷺ alimweleza, kwamba,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ غُرَفًا يُرَى ظَاهِرُهَا مِنْ بَاطِنِهَا، وَبَاطِنُهَا مِنْ ظَاهِرِهَا، أَعَدَّهَا اللَّهُ تَعَالَى لِمَنْ أَطْعَمَ الطَّعَامَ، وَأَطَابَ الْكَلَامَ، وَتَابَعَ الصَّلَاةَ وَالصِّيَامَ، وَقَامَ بِاللَّيْلِ وَالنَّاسُ يَنَامُونَ»

“Peponi kuna vyumba nje yake huonekana kutoka ndani yake, na ndani yake huonekana kutoka nje. Allah Amewaandalia watakaolisha chakula, wenye maneno mazuri, anayesali na kufunga kwa mfuatano na anayesimama kwa Swala usiku huku watu wakiwa wamelala.”¹

¹ At-Tabari 17:372.

وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٥٦﴾

“...na wakamtegemea Mola wao Mlezi.”

Katika hali zao zote. Katika dini na dunia yao. Kisha, Allah تعالى Aliwaambia kwamba riziki haifungamani na sehemu moja tu, bali ni yenye kuwaenea viumbe Wake popote walipo. Kadhalika, riziki za Muhajirina zipo huko wanakohamia zikiwa nyingi, kunjufu zaidi na nzuri, kwani wao kwa muda mchache, wamekuwa wakuu wa miji, maeneo yote. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَكَايِنٍ مِّن دَابَّةٍ لَّا تَحْمِلُ رِزْقَهَا

“Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao!”

Maana yake: Wanyama hawawezi kuikusanya na kuihifadhi kwa ajili ya kesho,

اللَّهُ يَرْزُقُهَا وَإِيَّاكُمْ

“Mwenyezi Mungu Anawaruzuku hao na nyinyi pia.”

Maana yake: Allah تعالى Anawapa riziki yao, ingawa ni wadhaifu na Anawarahisishia. Yeye Humpelekea kila kiumbe, riziki inayomfaa, hata mdudu chungu ndani ya ardhi. Ndege angani na samaki katika maji.

Allah تعالى Amesema:

* وَمَا مِن دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَىٰ اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۗ كُلٌّ فِي

كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٥٧﴾

“Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:6)

وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٥٨﴾

“Na Yeye Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.”

Maana yake: Mwenye kusikia kauli za waja Wake, Mjuzi wa harakati na maskani yao.

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ فَأَنَّى يُؤْفَكُونَ ﴿٥٦﴾
 اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ ۖ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٥٧﴾
 وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ نَزَّلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِهَا لَيَقُولُنَّ اللَّهُ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٥٨﴾

61. “Na ukiwauliza; Nani aliyumba mbingu na ardhi na akafanya jua na mwezi kutii Amri Yake? Bila ya shaka, watasema: Mwenyezi Mungu. Wapi basi wanakogeuzwa?”

62. Mwenyezi Mungu Humkunjulia, na Humdhikishia, riziki amtakaye katika waja wake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

63. “Na ukiwauliza: Ni nani anayeteremsha maji kutoka mbinguni, na akahuisha ardhi baada ya kufa kwake? Bila ya shaka watasema: Ni Mwenyezi Mungu. Sema: Alhamdu Lillahi, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Bali wengi katika wao hawafahamu.”

Ushahidi wa Tawhiid

Allah تعالى Anasema kwa Kuthibitisha kwamba hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, kwa sababu washirikina wanamwabudu asiyekuwa Yeye, bado walitambua kwamba Yeye Ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi, jua na mwezi, Kuutiisha usiku na mchana. Na kwamba Yeye Ndiye Muumbaji, Mwenye kuwaruzuku wao, Kukadiria muda wa uhai wao, Kukhitilafiana kwao na Kutofautiana kwa riziki zao, kiasi kwamba ikawepo hitilafu baina yao. Wakawepo matajiri na mafakiri, na Yeye Anayajua yanayomfaa kila mmoja miongoni mwao. Pia kuhusu wanaostahiki utajiri dhidi ya wanaostahiki ufakiri. Akataja kwamba Yeye Peke Yake Ndiye Aliyekiumba kila kitu, Ndiye Anayewadhibiti. Ikiwa ni hivyo, basi, ni kwa nini aabudiwe asiyekuwa Yeye? Kwanini ategemewe asiyekuwa Yeye? (Kama ambavyo Yeye ni Mmoja katika Ufalme Wake, basi inatakiwa Awe Mmoja katika kuabudiwa Kwake.) Mara nyingi, Allah تعالى Huthibitisha nafasi ya Uungu kwa kutambua kwao Tawhiid

kwamba Mola ni Mmoja tu. Washirikina walikuwa wanalitambua hilo, kama ambavyo walikuwa wakisema katika *Talbiyah* zao (wakati wa Hijja na Umra): “Nimekuitika, huna mshirika, isipokuwa mshirika Uliye Naye, Unammiliki yeye pamoja na anachokimiliki.”



وَمَا هَذِهِ الْحَيَوةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَهُوٌ وَلَعِبٌ ۗ وَإِنَّ الدَّارَ
 الْآخِرَةَ لَهِيَ الْحَيَوةُ ۗ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٦٤﴾ فَإِذَا
 رَكَبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَاؤُ اللَّهِ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّهْتُمْ
 إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ ﴿٦٥﴾ لِيَكْفُرُوا بِمَا ءَاتَيْنَاهُمْ
 وَلِيَتَمَتَّعُوا ۗ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٦٦﴾ أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا
 حَرَمًا ءَامِنًا وَيُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ ؕ أَفَبِالْبِطْلِ
 يُؤْمِنُونَ وَبِعِمَّةٍ اللَّهِ يَكْفُرُونَ ﴿٦٧﴾ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى
 عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُ ؕ أَلَيْسَ فِي
 جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ﴿٦٨﴾ وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا
 لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٦٩﴾

وَمَا هَذِهِ الْحَيَوةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَهُوٌ
 وَلَعِبٌ ۗ وَإِنَّ الدَّارَ الْآخِرَةَ لَهِيَ
 الْحَيَوةُ ۗ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٦٤﴾
 فَإِذَا رَكَبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَاؤُ اللَّهِ
 مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّهْتُمْ
 إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ ﴿٦٥﴾
 لِيَكْفُرُوا بِمَا ءَاتَيْنَاهُمْ
 وَلِيَتَمَتَّعُوا ۗ فَسَوْفَ
 يَعْلَمُونَ ﴿٦٦﴾

64. "Na haya maisha ya dunia si chochote ila ni pumbao na mchezo. Na nyumba ya Akhera ndiyo maisha khasa; laiti

wangelikuwa wanajua!"

65. "Na wanapopanda katika marikebu, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia utiifu. Lakini anapowavusha wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha."

66. "Wapate kuyakanya tuliyowapa, na wajistareheshe. Lakini watakuja jua!"

Allah تعالى Anaeleza kuhusu uduni wa dunia, kuondoka kwake na kumalizika kwake, na kwamba haiwezi kudumu na upeo wa yaliyomo humo ni upuuzi na mchezo:

وَإِنَّ الدَّارَ الْآخِرَةَ لَهِيَ الْحَيَوةُ

"Na nyumba ya Akhera ndiyo maisha khasa..."

Maana yake: Maisha ya daima, ya kweli ni yale ambayo hayataondoka wala kumalizika, bali ni yenye kuendelea daima milele.

Kauli ya Allah تعالى:

لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٦٤﴾

“...laiti wangelikuwa wanajua!”

Maana yake, wangetanguliza yenye kuendelea, badala ya yenye kumalizika. Kisha Allah تعالى Alieleza kuhusu washirikina wakati wa janga humwomba Yeye Peke Yake, Asiye na mshirika, basi, kwa nini wasiwe hivyo daima?

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلِكِ دَعَوْا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

“Na wanapopanda katika marikebu, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia utiifu.”

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَهُهُ فَلَمَّا جَنَّكُمُ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ

“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu. Na anapowavusha mkafika nchi kavu, mnageuka.” (17:67)

Allah تعالى Amesema katika Aya hii:

فَلَمَّا جَنَّهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ ﴿٦٥﴾

“Lakini anapowavusha wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha.”

Hapa Ibn Kathir رحمه الله تعالى ameeleza kisa cha kusilimu Ikrimah bin Abi Jahl رضي الله عنه ambacho tayari tumeshelekieleza,

لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَاهُمْ وَلِيَتَمَتَّعُوا

“Wapate kuyakana Tuliowapa, na wajistareheshe.”

Wanachuoni wengi wa lugha ya Kiarabu, wafasiri na kanuni zake wanasema kuwa herufi *lamu* iliyo katika neno *liyakfuruu* (wapate kuyakana) ni *Lamul-‘Aaqibah* (lamu ya athari, matokeo au hali ya mwisho wa jambo). Ni kwa sababu wao hawakusudii hayo, na hapana shaka ni kwa sababu inanasibiana nao.

Ama kwa kuichukulia kwamba ni Kudura ya Allah تعالى kwao na kuhukumu hivyo kwao kwa ajili ya hilo, basi hiyo itakuwa ni *Lamut-Ta'ail* (sababu). Na tumeshabainisha hilo. Kauli Yake:

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا ءَامِنًا وَيُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ ؕ أَفَبِالْبِطْلِ يُؤْمِنُونَ
وَبِعِصْمَةِ اللَّهِ يُكْفَرُونَ ﴿٦٧﴾ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِالْحَقِّ لَمَّا
جَاءَهُ ؕ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ﴿٦٨﴾ وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَهُمْ صُبُلَنَا وَإِنَّ
اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٦٩﴾

67.“Je! Hawaoni ya kwamba Tumeifanya nchi takatifu ina amani, na hali watu wengine wananyakuliwa kote kwa majirani zao? Je! Wanaamini upotovu, na Neema za Mwenyezi Mungu wanazikataa?”

68.“Na nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu au anayekanusha Haki inapomjia? Je! Si katika Jahannamu ndio yatakuwa makazi ya makafiri?”

69.“Na wanaofanya juhudi kwa ajili Yetu, Sisi Tutawaongoa kwenye Njia Zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na watu wema.”

Ukafiri wa Makuraishi Pamoja na Neema Waliopewa ya Utukufu wa Mji wa Makka.

Allah تعالى Anasema Akiwakumbusha Makuraishi washukuru kuhusu mahali Pake patukufu alipopajaalia kwa ajili ya watu, mkazi na mgeni. Mwenye kuingia atakuwa amesalimika, basi wao wako katika amani kubwa, kwani Waarabu wanaolizingira eneo lao huvamiana na kuuana wao kwa wao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَا يَلْفِ قُرَيْشٍ ﴿٦٩﴾ إِلَيْهِمْ رِحْلَةَ الْشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ﴿٧٠﴾ فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ﴿٧١﴾
الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِّنْ جُوعٍ وَءَامَنَهُمْ مِّنْ خَوْفٍ ﴿٧٢﴾

“Kwa walivyozea Maqureshi, Kuzoea kwao safari za siku za baridi na siku za joto. Basi nawamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii,

Ambaye Anawalisha wasipate njaa, na Anawalinda na khofu.”
(106:1-4)

أَفِإلْبَطِلِ يُؤْمِنُونَ وَبِنِعْمَةِ اللَّهِ يَكْفُرُونَ ﴿٧﴾

“Je! Wanaamini upotovu, na Neema za Mwenyezi Mungu wanazikataa?”

Maana yake: hivi shukurani yao kwa neema hii kubwa imekuwa kumshirikisha na kumwabudu asiyekuwa Yeye, miongoni mwa masanamu na washindani.

بَدَلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْآبْوَارِ ﴿٢٨﴾

“Waliobadilisha Neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo?”
(14:28)

Wakamkufuru Nabii, mja na Mtume ﷺ. Lililokuwa la sawa kwao ni kuzitakasa ibada kwa ajili ya Allah تعالى, na kwamba wasimshirikishe. Na wamsadikishe Mtume ﷺ kumtukua na kumheshimu. Lakini walimkadhibisha, wakampiga vita na wakamtoa katika maeneo yao. Basi, Allah تعالى Alizinyakua Neema Alizowapa na Akawaua baadhi yao katika vita vya badr. Kisha ushindi ukawa wa Allah تعالى, Mtume Wake na Waumini. Allah تعالى Akampa Mtume Wake ushindi wa Makkah, Akawafedhehesha na Kuwadhalilisha makafiri. Kisha Allah تعالى Akasema:

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُ ﴿٢٨﴾

“Na nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu au anayakanusha Haki inapomjia?”

Maana: Hapana mwenye adhabu kubwa zaidi ya aliyemkadhibisha Allah تعالى na akasema: “Allah تعالى Hakumpa wahyi, wala hakufunuliwa chochote.” Pia aliyesema: “Nitateremsha mithili ya alichokiteremsha Allah,” na mfano wa haya. Hapana mwenye mateso makali zaidi ya aliyeikadhibisha haki baada ya kumfikia. Mtu wa kwanza katika hawa ni mzushi, na wa pili ni mkadhibishaji. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ﴿٢٩﴾

“Je! Si katika Jahannamu ndio yatakuwa makazi ya makafiri?”

Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِيْنَا

“Na wanaofanya juhudi kwa ajili Yetu...”

Maana yake: Mitume, Masahaba wake na wafuasi mpaka Siku ya Kiyama.

لَنَهْدِيَهُمْ سُبُلَنَا

“...Sisi Tutawaongoa kwenye njia Zetu.”

Maana yake: Tutawaonesha njia Zetu duniani na Akhera. Ibn Abu Hatim alimnukuu ‘Abbas Al-Hamdani Abu Ahmad, mmojawapo wa watu wa ‘Akkaa (Palestina) akiizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِيْنَا لَنَهْدِيَهُمْ سُبُلَنَا وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٦٩﴾

“Na wanaofanya juhudi kwa ajili Yetu, Sisi Tutawaongoa kwenye njia Zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na watu wema.”

Akasema: “Ni ambao wanatenda kulingana na wanavyojua. Allah تعالى Akawaongoza kwenye wasiyoyajua.” Ahmad bin Al-Hawari amesema: “Nikamweleza hayo Abu Sulayman Ad-Daraniy, likamfurahisha akasema, Mwenye kupata ilhamu ya jambo la kheri hatakiwi kulifanya jambo hilo mpaka alisikie katika mapokezi, akilisikia alifanyie kazi na kumshukuru Allah تعالى kwa sababu ya kuafikiana na haki kilichomo nafsi mwake.”¹

وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٦٩﴾

“Na hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na watu wema.”

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alimnukuu Ash-Sha’bi kwamba amesema: ‘Isa bin Maryam عليه السلام amesema, “Mfanyie Ihsani aliyekufanyia ubaya, si kwa aliyekufanyia wema.”

Huu ndio mwisho wa Tafsiri ya Surat Al-`ankaboot. Sifa zote njema na Shukrani zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

¹Ibn Abu Hatim (17451) 9/3084. Mtiririko wake umekatika.

Tafsiri ya Suratu Ar-Rum

Sura ya 30

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الرَّحْمٰنِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْم ﴿١﴾ غَلَبَتِ الرَّوْمُ ﴿٢﴾ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ
بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٣﴾ فِي بَضْعِ سِنِينَ ۗ ﴿٤﴾
لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ بَعْدُ ۗ وَيَوْمَئِذٍ
يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٥﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ ۗ
يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ
الرَّحِيمُ ﴿٦﴾ وَعَدَّ اللَّهُ لَا تُخْلِفُ اللَّهُ
وَعْدَهُ ۗ وَلَيَكُنْ أَكْثَرُ النَّاسِ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿٧﴾ يَعْلَمُونَ ظَهْرًا مِنَ
الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ عَنِ الْآخِرَةِ هُمْ
غَافِلُونَ ﴿٨﴾

الْم ﴿١﴾ غَلَبَتِ الرَّوْمُ ﴿٢﴾ فِي أَدْنَى
الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ
سَيَغْلِبُونَ ﴿٣﴾ فِي بَضْعِ سِنِينَ ۗ ﴿٤﴾
لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ بَعْدُ ۗ وَيَوْمَئِذٍ
يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٥﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ ۗ
يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ
الرَّحِيمُ ﴿٦﴾ وَعَدَّ اللَّهُ لَا تُخْلِفُ اللَّهُ
وَعْدَهُ ۗ وَلَيَكُنْ أَكْثَرُ النَّاسِ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿٧﴾ يَعْلَمُونَ ظَهْرًا مِنَ
الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ عَنِ الْآخِرَةِ هُمْ
غَافِلُونَ ﴿٨﴾

1. "Alif Lam Mim (A.L.M.)"

2. "Warumi wameshindwa."

3. "Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda,"

4. "Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi."

5. ***“Kwa Nusura ya Mwenyezi Mungu Humnusuru Amtakaye. Naye Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu.”***

6. ***“Ni Ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Havunji Ahadi Yake. Lakini watu wengi hawajui.”***

7. ***“Wanajua hali ya dhahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.”***

Kuubashiri Ushindi wa Warumi

Aya hizi zilishuka wakati ushindi wa mfalme Sabur (wa Uajemi) dhidi ya Ash-Sham (Syria) na nchi zinazoizunguka za Al-Hijaz pamoja na nchi za mbali za Warumi. Hiraql (Heraclius), mfalme wa warumi alilazimika kukimbilia Constantinople na wakamzingira huko kwa kipindi kirefu. Baadaye, dola ilirejea kwa Heraclius kama itakavyoelezwa. Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuhusu kauli ya Allah تعالى:

الْمَرُّ غَلَبَتِ الرُّومُ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ

“Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa. Katika nchi iliyo karibu.”

Kwamba amesema: “Walishindwa halafu wakashinda.” Amesema: “Washirikina walikuwa wakipenda Uajemi iishinde Roma, kwa sababu wao ni watu wa kuabudu masanamu, ilhali, Waislamu walikuwa wakipenda kwamba Roma iishinde Uajemi, kwa sababu wao ni Watu wa Kitabu. Hilo likatajwa kwa Abubakr رضي الله عنه. Abubakr رضي الله عنه naye akamtajia Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akasema:

«أَمَّا إِنَّهُمْ سَيُنَلِّبُونَ»

“Kwa hakika watashinda.”

Abubakr رضي الله عنه akawaambia. Wakasema: “Hebu weka muda baina yetu na wewe. Ikiwa sisi tutashinda, basi tupate kitu kadha na kadha. Na kama mtashinda nyinyi, basi mtapata kitu kadha wa kadha.” Akaweka muda wa miaka mitano. Warumi hawakushinda. Abubakr رضي الله عنه akamtajia Mtume ﷺ kuhusu jambo hilo, akasema:

«أَلَا جَعَلْنَاهَا إِلَىٰ دُونَ - أَرَاهُ قَالَ: الْعَشْر -»

“Kwa nini hukufanya pungufu zaidi.” – nadhani amesema, Idadi yoyote iliyopo “Chini ya kumi.”

Amesema Sa'id bin Jubayr, “Maana ya *Al-Bidh'* ni idadi yoyote iliyopo chini ya kumi. Baadaye, Warumi walishinda, na akasema, ushindi huo ndio ule ambao Allah تعالى Amesema:

الْم ﴿١﴾ غَلَبَتِ الرُّومُ ﴿٢﴾ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٣﴾
 فِي بَضْعِ سِنِينَ ۗ لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ بَعْدُ ۗ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٤﴾ بِنَصْرِ
 اللَّهِ ۗ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٥﴾

“Alif Lam Mim (A.L.M) Warumi wameshindwa. Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda. Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa Nusura ya Mwenyezi Mungu Humnusuru Amtakaye. Naye Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu.”

Hivi ndivyo alivyonukuu At-Tirmidhi na An-Nasai pia. At-Tirmidhi amesema: “Ni Hasan Gharib.”²

Hadithi Nyingine

Abu 'Isa At-Tirmidhi alimnukuu Niyar bin Mukram Al-Aslami kuwa amesema: Pindi iliposhuka,

الْم ﴿١﴾ غَلَبَتِ الرُّومُ ﴿٢﴾ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٣﴾
 فِي بَضْعِ سِنِينَ ۗ

“Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa. Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda. Katika miaka michache.”

¹ Ahmad 1:276.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 9:51, An-Nasai katika Al-Kubra 6:426.

Wakati Aya hii ilipotremka, Waajemi walikuwa wamewashinda Warumi. Waislamu walikuwa wakipenda Warumi wawashinde Waajemi, kwa sababu wao (Warumi) na wao wenyewe (Waislamu) ni Watu wa Kitabu. Allah تعالى Amesema kuhusu jambo hili:

وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٢﴾

“Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa Nusura ya Mwenyezi Mungu Humnusuru Amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.”

Makuraishi walikuwa wakipenda ushindi wa Waajemi kwa sababu wao na hao si Watu wa Kitabu, wala hawana imani juu ya kufufuliwa. Allah تعالى Alipotremsha Aya hii, Abubakr رضي الله عنه alitoka akitangaza katika pande mbali mbali za Makkah:

الْم ﴿١﴾ غُلِبَتِ الرُّومُ ﴿٢﴾ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٣﴾

فِي بَضْعِ سِنِينَ ۗ

“Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa. Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda. Katika miaka michache.”

Baadhi ya Makuraishi wakamwambia Abubakr رضي الله عنه: “Hii ni bahati nasibu baina yetu na nyinyi. Sahibu yenu amedai kwamba Warumi watawashinda Waajemi katika miaka michache, basi kwa nini tusiwekeane dau baina yetu na wewe?” Akasema: “Naam.” Hiyo ilikuwa kabla ya kuharamishwa kwa bahati nasibu. Abubakr رضي الله عنه akawekeana dau na washirikina. Baada ya kuwekeana walimwambia Abubakr رضي الله عنه, “Muda mchache huo tufanye kwamba ni miaka mingapi? Ni mitatu mpaka tisa?, basi tukubaliane baina yetu na wewe kwamba ni kati kati yake. Basi wakakubaliana miaka sita. Basi, ikapita miaka sita kabla hawajashinda, basi washirikina wakachukua lile dau la Abubakr رضي الله عنه. Ulipoingia mwaka wa saba, Warumi waliwashinda waajemi. Waislamu wakamlaumu Abubakr رضي الله عنه kwa kukubaliana miaka sita. Akasema Abubakar رضي الله عنه ni kwa sababu, Allah تعالى Amesema, “Katika miaka michache.” Watu wengi wakashilimu kwa tukio hilo. Hivi ndivyo ilivyosimuliwa na At-Tirmidhi, halafu akasema: “Ni *Hadith Hasan*.”¹

¹ Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:52.

Warumi ni Akina Nani

Hebu sasa, tuzungumzie maneno yaliyoko katika Aya hizi tukufu:

الْمَرْغُلَيْتِ الرُّومِ

“Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa.”

Maelezo kuhusu herufi moja moja mwanzoni mwa sura mbalimbali yalikuwisha tangulia katika *Surat Al-Baqarah*. Ama Warumi, wanatokana na uzao wa Al-Isi bin Is-haq bin Ibrahim, na wao ni wana wa ami wa Wana wa Israil. Pia huitwa Wana wa Al-Asfar, na walikuwa katika dini ya Wayunani (Wagiriki) ambao walitokana na uzao wa Yafith bin Nuh, wana wa ami wa Waturuki. Waliokuwa wakiabudu sayari saba, ambazo pia ziliitwa *Al-Mutahayyirah*, walikuwa wakisali kwa kuelekea upande wa kaskazini, na ndio waliouanzisha mji wa Damascus, wakajenga hekalu yake, ambalo ndani yake kuna mihrabu zilizoelekezwa kaskazini. Warumi waliifuata dini yao mpaka baada ya kutumwa Al-Masih, kwa kiasi cha miaka mia tatu. Aliyeitawala Sham (Syria) pamoja na Al-Jazirah (ardhi yenye rutuba kutoka jangwa la Syria mpaka Ghuba ya Uajemi) aliitwa Kaisari. Mtu wa kwanza kuingia katika dini ya Manasara katika wafalme alikuwa Constantine bin Costas na mama yake, Maryam Al-Haylaaniyyah (Ash-Shadqaniyyah) kutoka ardhi ya Harran, ambaye aliingia katika unasara kabla yake. Akamwita mwanaye katika dini yake, ambaye kabla ya hapo alikuwa mwanafalsafa. Kisha akamfuata. Inasemekana, hiyo ilikuwa imani kwa nje tu (*taqiyyah*). Manasara wakajumuika kwake na katika zama zake waliendesha midahalo na ‘Abdullah bin Ariyus, kukatokea baina yao khitilafu nyingi ambazo hazikuweza kupatiwa ufumbuzi, isipokuwa aliafikiana na mkusanyiko wao wa maaskofu mia tatu kumi na wanane na wakaweka imani yao kwa Constantine. Hiyo ndiyo ambayo wao huiita Amana kuu, lakini kwa hakika, ni Usaliti wa Kufedhehesha. Wakamwekea kanuni, wakimaanisha vitabu vya hukumu kuhusu mambo ya haramu na ya halali, na mengine waliyokuwa wakiyahitaji. Wakaibadili dini ya Masihi عليه السلام, wakupunguza na kuongeza baadhi ya mambo. Wakasali kwa kuelekea upande wa mashariki na wakabadili kaida ya siku ya Jumamosi na kuwa Jumapili, wakaabudu msalaba na wakahalalisha nguruwe. Wakazusha sikukuu kama vile siku ya msalaba, misa, ubatizo, Jumapili ya Matawi na kadhalika. Wakabuni cheo cha Papa, naye ndiye mkubwa wao, kisha maaskofu wakuu, kisha maaskofu, halafu makasisi na mashemasi.

Pia walianzisha maisha ya utawa. Mfalme aliwajengea makanisa na maeneo ya ibada, akaasisi mji ulioitwa kwa jina lake, Constantinople. Inasemekana kwamba katika enzi zake alijenga makanisa elfu kumi na mbili, maeneo matatu ya ibada katika *Bayt Lahm* (Bethlehem) na kwamba mama yake alijenga Kanisa mahali walipodai kuwa amesulubiwa Yesu. Hawa ndio walioifuata dini ya wafalme. Baada yao, wakazuka wafuasi wa Ya'qub Al-Askaf, kisha Nestorians, wafuasi wa Nestorius, wapo katika makundi na madhehebu mengi. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ:

«إِنَّهُمْ افْتَرَقُوا عَلَى اثْنَتَيْنِ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً»

“Waligawanyika katika makundi sabini na mbili.”

Iliyoyo ni kwamba wao waliendelea katika Ukristo. Kila alipofariki Kaisari mmojawapo, mwingine aliendeleza mahali pake baada yake, mpaka mwishowe akawa Heraclius. Alikuwa mtu mwenye busara, mwerevu na mwenye akili zaidi na uoni wa mbali. Akawa kiongozi mwenye kushika hatamu na mwenye kuheshimiwa sana. Akapingwa na Kisra (Chosroes), mfalme wa Uajemi na nchi maeneo kama vile Iraq, Khuraasan, Ar-Riy na ardhi yote ya Waajemi. Huyoyo ni Sabur Dhul-Aktaaf (Shapur). Ilikuwa dola yake pana zaidi kuliko ya Kaisari. Aliyeshika uongozi wa Waajemi na wapumbavu wa Wafursi, na walikuwa, Wamajusi wakiabudu moto.

Namna Kaisari Alivyomshinda Kisra

Yalikwishatangulia maelezo kutoka kwa 'Ikrimah kuwa amesema: “Kisra alimpeleka naibu wake pamoja na jeshi kwa Kaisar na wakapigana naye. Kauli iliyo mashuhuri ni kwamba Kisra alipigana vita dhidi ya Kaisar mwenyewe katika miji yake. Akamshinda na kumzidi mpaka akawa hakusaliwa na mji zaidi ya Constantinople. Wakamweka kizuizini hapo kwa muda mrefu mpaka akapata dhiki kubwa humo. Manasara walikuwa wakimtukuza kuzidi kiasi, kiasi kwamba Kisra hakuweza kuuvamia mji, kwa sababu ya ngome yake, huku nusu yake ikiwa upande wa nchi kavu na nyingine upande wa majini, ambapo waliweza kufikiwa na msaada kupitia huko. Baada ya haya kuchukua muda mrefu Kaisari alibuni mbinu. Katika nafsi yake, alifikiria kufanya hadaa. Akamtaka Kisra aondoke kutoka katika ardhi yake kwa kupatiwa mali ya kufanyia suluhu na ampe masharti aliyoyataka. Akamkubalia hayo, na akataka mali nyingi kutoka kwake, ambayo mfalme yeyote wa duniani hakuwa na uwezo

wa kuimudu, miongoni mwa dhahabu, vito vya thamani, nguo, watumishi wa kike na wa kiume na namna nyingi. Kaisari aliridhia na akampa hima kwamba alikuwa navyo vyote alivyovitaka, ingawa alimchukulia kwamba alikuwa punguani baada ya kuyataka aliyoyataka, kwa sababu hata kama wangaliunganika pamoja naye na kukusanya walivyo navyo, basi visingelifikia sehemu moja ya kumi ya mahitaji yake. Akamwomba Kisra ampe fursa ya kwenda katika ardhi ya Ash-Sham na majimbo ya mamlaka yake ili aweze kuvikusanya vitu hivyo kutoka katika khazina zake na maeneo ambapo mali zake zilipozika. Kisra akamwachilia. Kaisari alipotaka kutoka katika mji wa Constantinople, aliwakusanya watu wa dini yake na akasema: 'Mimi natoka kwa ajili ya jambo ambalo nimeamua kulifanya pamoja na askari niliowateua kutoka katika jeshi langu. Nikirejea kwenu kabla ya mwaka mmoja, basi mimi nitaendelea kuwa mfalme wenu, na kama sitarejea kwenu kabla ya mwaka, basi nyinyi mtakuwa na khiyari: mkitaka mtaendelea kuniunga mkono, na mkitaka mtamteua mwingine ghairi yangu.' Wakamjibu: 'Wewe ni mfalme wetu kadiri utakavyoendelea kuwa hai hata kama utaondoka kwa muda wa miaka kumi.'" Kaisari alipoondoka katika mji wa Constantinople na kikosi maalumu cha askari wa farasi, Kisra alipiga kambi nje ya Constantinople akisubiri kurejea kwake. Kaisari akapanda upesi na akaondoka kwa kasi, mpaka akafika katika ardhi ya Uajemi na akaanza kuwaua watu wake na wote walio katika umri wa kupigana, mmoja baada ya mmoja. Hakuacha kuwaua mpaka akafika Al-Madaain, ambao uliokuwa ndio ngome ya mamlaka ya mfalme Kisra. Akaua waliokuwa humo na akachukua mali na khazina zake zote. Akawateka wake na wanawake wa Kisra. Akamnyoa mwanaye na akampandisha juu ya punda wake. Akampelekea yeye pamoja na viongozi wa watu wake katika ufedheheshaji na udhalilishaji wa hali ya juu. Akamwandikia Kisra kwamba: 'haya ndiyo uliyoyataka, basi yachukue.' Baada ya kumfikia Kisra, alishikwa na huzuni kubwa ambayo hapana aijuaye isipokuwa Allah تعالی. Hasira yake ikawa kali sana juu ya mji wa Constantinople. Akafanya juhudi ya kuuzingira kadiri ilivyoyumkinika, lakini hakuweza. Baada ya kushindwa alipanda ili adhibiti kivuko cha mto Jayhun ambayo ndio iliyokuwa njia pekee ingeweza kumfikisha kwa Kaisari katika mji wa Constantinople. Kaisari alipolijua hilo alifanya mbinu ambayo haikuwahi kufanywa kabla yake. Ni kwamba, aliwaacha askari pamoja na vitu alivyokuwa navyo katika kivuko cha mto. Akapanda na baadhi ya wanajeshi, akaamuru wabebe pumba na kinyesi cha wanyama na kusafiri navyo kwa masafa ya kiasi cha siku moja kwa kuelekea mto unakotokea. Halafu akaamuru mizigo ile itupwe katika maji. Kisra alipopita na askari wake,

walidhani kwamba Warumi wametumbukia humo ili wapite. Wakapanda kuwafuata na kivuko kikawa hakiko chini ya Waajemi. Kaisari akawaambia watu wake wainuke na kuruka mtoni. Wakatumbukia na kuondoka kwa kasi. Wakawapita Kisra na askari wake na wakaingia Constantinople. Hiyo ni siku kubwa kwa Manasara. Kisra na majeshi yake wakabaki wakiwa wamechanganyikiwa, hawajui cha kufanya. Hawakuweza kufika katika mji wa Kaisari huku ardhi yao imeharibiwa na Warumi na wakachukua mali zao na kuwateka wanawake na watoto wao. Huu ukawa ushindi wa Warumi dhidi ya Wafursi (Waajemi). Ushindi huo ulikuwa miaka tisa tangu Wafursi wawashinde Warumi. Mgogoro huu baina ya Wafursi na Warumi, ulitokea pale Warumi waliposhindwa baina ya Adhru'aat (Ash-Sham) na Busra, kwa mujibu wa aliyoyasema Ibn 'Abbas, 'Ikrimah na wengine. Hiyo ni sehemu ukingoni mwa Ash-Sham katika mpaka wake na Al- Hijaz. Mujahid amesema: "Hiyo ilikuwa ni sehemu ya Al-Jazirah (Rasi ya Arabuni), ambayo iko karibu na ardhi ya Warumi kuliko Uajemi." Allah تعالى Ndiye Mjuzi.

Kauli ya Allah تعالى:

لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ بَعْدُ

"Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake."

Maana yake: Kabla ya hayo na baada yake,

وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ

"Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa Nusura ya Mwenyezi Mungu..."

Maana: Kwa Warumi, watu wa Kaisari, Mfalme wa Ash-Sham, dhidi ya Waajemi, watu wa Kisra, Mfalme wa Wamajusi. Ushindi wa Warumi dhidi ya Waajemi ulitokea katika siku sawa na siku ya Badr, kwa mujibu wa Maulamaa wengi, kama vile Ibn 'Abbas, Ath-Thawri, As-Suddi na wengine رضي الله عنهم. Ilisimuliwa katika Hadithi aliyoinukuu At-Tirmidhi, Ibn Jarir, Ibn Abu Hatim na Al-Bazzar kutoka kwa Abu Sa'id, amesema: "Ilipofika siku ya Badr, Warumi waliwashinda Wafursi. Hilo likawapendeza Waumini na wakalifurahia. Allah تعالى Alishateremsha Aya:

وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ بِنَصْرِ اللَّهِ ۗ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ

الرَّحِيمُ ﴿٧﴾

“Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa Nusura ya Mwenyezi Mungu Humnusuru Amtakaye. Naye Ndiye Mwenye nguvu Mwenye Kurehemu.”¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Az-Zubayr Al-Kilabi kuwa amesema: “Niliuona ushindi wa Waajemi kwa Warumi, kisha nikaona ushindi wa Warumi kwa Waajemi, halafu nikaona ushindi wa Waislamu dhidi ya Waajemi na Warumi. Yote hayo katika kipindi cha miaka kumi na mitano.” Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الْعَزِيزُ

“Naye Ndiye Mwenye nguvu...”

Maana yake: Katika Kuwashinda na Kuwalipizia maadui Zake kisasi,

الرَّحِيمُ

“Mwenye Kurehemu.”

Waja wake Waumini. Kauli ya Allah تعالى:

وَعَدَ اللَّهُ لَا تُخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ

“Ni Ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Havunji Ahadi Yake.”

Maana yake: Khabari hii tuliyokusimulia, ewe Muhammad! Kwamba Sisi Tutawapa ushindi Warumi. Ni ahadi ya kweli toka kwa Allah تعالى. Pia ni khabari sahihi kabisa ambayo haibadiliki na hapana shaka kutokea kwake, kwa sababu Allah تعالى Ameshapitisha Sunna yake kulinusuru taifa moja kati ya mawili yanayopigana ambalo liko karibu zaidi na ukweli lishinde na mwisho mwema kuwa upande wao,

وَلَيْكِنْ أَكْثَرُ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

“Lakini watu wengi hawajui.”

Maana yake: Kuhusu Hukumu ya Allah تعالى juu ya Uumbaji, na Matendo Yake ni ya hikima yenye kupita katika uadilifu. Kauli ya Allah تعالى:

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:50, At-Tabari 20:73.

يَعْلَمُونَ ظَهْرًا مِّنَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ عَنِ الْآخِرَةِ هُمْ غٰفِلُونَ ﴿٦﴾

“Wanajua hali ya dhahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.”

Maana yake: watu wengi hawana elimu, isipokuwa ya dunia, uchumi wake na masuala yake mbalimbali, pamoja na vilivyomo. Basi wao, ni mahodari katika kuyapata mahitaji yao na kujipatia kipato, ilhali wameghafilika sana na mambo ya kidini na yenye kuwanufaisha Akhera. Wameghafilika nayo, wala hawana fikra nayo. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى amesema: “Wallah! Mmoja wao hufikia katika kuipenda dunia hali ambayo mmoja wao anaweza kuigeuza *Dirham* katika kiganja chake na kukujulisha uzani wake, lakini hajui namna ya kusali vyema.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

يَعْلَمُونَ ظَهْرًا مِّنَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ عَنِ الْآخِرَةِ هُمْ غٰفِلُونَ ﴿٧﴾

“Wanajua hali ya dhahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.”

Maana yake: “Makafiri wanajua namna ya kupata maendeleo duniani, lakini ni majahili wa masuala ya kidini.”¹

* * *

¹At-Tabari 20:76.

أَوْلَمْ يَتَفَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِمْ ۗ مَا خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ
 وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ
 بِلِقَائِي رَبِّهِمْ لَكَافِرُونَ ﴿٨﴾ أَوْلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ
 فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۗ كَانُوا أَشَدَّ
 مِنْهُمْ قُوَّةً وَأَنَارُوا الْأَرْضَ وَعَمَرُوهَا أَكْثَرَ مِمَّا عَمَرُوهَا
 وَجَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ ۗ فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ
 وَلَٰكِن كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٩﴾ ثُمَّ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ
 اسْتَفْتُوا السُّوَائِيَ أَن كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَكَانُوا بِهَا
 يَسْتَهْزِءُونَ ﴿١٠﴾ اللَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ثُمَّ إِلَيْهِ
 تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُبْلِسُ الْمُجْرِمُونَ ﴿١٢﴾
 وَلَمْ يَكُن لَّهُمْ مِّنْ شُرَكَائِهِمْ شُفَعَاءُ وَكَانُوا
 بِشُرَكَائِهِمْ كَافِرِينَ ﴿١٣﴾ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُومِنُونَ
 بِتَفَرُّقُونَ ﴿١٤﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ فَهُمْ فِي رَوْضَةٍ يُحْبَرُونَ ﴿١٥﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ
 كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقَائِ الْآخِرَةِ فَأُولَٰئِكَ فِي
 الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ﴿١٦﴾ فَسُبْحٰنَ اللَّهِ حِينَ تُمْسُونَ
 وَحِينَ تُصْبِحُونَ ﴿١٧﴾ وَلَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ وَعَشِيًّا وَحِينَ تُظْهِرُونَ ﴿١٨﴾ تُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ
 الْمَمَاتِ وَتُخْرِجُ الْمَمَاتِ مِنَ الْحَيِّ وَتُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا
 وَكَذَٰلِكَ تُخْرَجُونَ ﴿١٩﴾

أَوْلَمْ يَتَفَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِمْ ۗ مَا خَلَقَ
 اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا
 إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا
 مِّنَ النَّاسِ بِلِقَائِي رَبِّهِمْ لَكَافِرُونَ
 ﴿٨﴾ أَوْلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ
 فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن
 قَبْلِهِمْ ۗ كَانُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً
 وَأَنَارُوا الْأَرْضَ وَعَمَرُوهَا أَكْثَرَ مِمَّا
 عَمَرُوهَا وَجَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ ۗ
 فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلَٰكِن
 كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٩﴾ ثُمَّ كَانَ
 عَاقِبَةُ الَّذِينَ اسْتَفْتُوا السُّوَائِيَ أَن
 كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَكَانُوا بِهَا
 يَسْتَهْزِءُونَ ﴿١٠﴾

8. "Je! Hawajifikirii nafsi zao? Mwenyezi Mungu Hakuumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake ila kwa Haki na kwa muda maalumu. Na hakika watu wengi bila ya shaka ni wenye kukataa kuwa watakutana na Mola wao Mlezi."

9. “Je! Hawatembei katika ardhi wakaona ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Nao walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao, na wakitimbua ardhi na wakaistawisha zaidi kuliko walivyoistawisha wao. Na Mitume wao wakawajia na dalili zilizowazi. Basi hakuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wakijidhulumu nafsi zao.”

10. “Kisha ulikuwa mwisho wa waliofanya ubaya ni kuzikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakawa wanazifanyia maskhara.”

Alama za Upekee wa Allah تعالی (Tauhidi)

Allah تعالی Anatanabahisha juu ya tafakuri kuhusu viumbe wake kunajulisha Kuwepo Kwake na Upweke Wake katika Kuviumba, na kwamba Yeye ni Mola ambaye hapana wa kuabudiwa kwa haki ila Yeye, wala hapana Mola isipokuwa Yeye. Amesema:

أَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِمْ

“Je! Hawajifikirii nafsi zao?”

Maana yake: Katika kutazama, kuzingatia na taamuli namna Allah تعالی Alivyounda vitu mbali mbali, toka ulimwengu wa juu na wa chini na baina yake, kama vile viumbe wa namna kwa namna na jinsi kadha wa kadha. Kisha wajue kwamba havikuumbwa kwa mzaha au bure tu bali kwa ukweli, na kwamba vimewekewa muda uliopangwa, ambayo ni Siku ya Kiyama.

Kwa minajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ بِلِقَائِ رَبِّهِمْ لَكٰفِرُونَ ﴿٣٠﴾

“Na hakika watu wengi bila ya shaka ni wenye kukataa kuwa watakutana na Mola wao Mlezi.”

Kisha Akawaeleza kuhusu ukweli wa Mitume Wake katika waliyokuja nayo, ambao Aliwatia nguvu kwa Kuwapa miujiza na dalili zilizo dhahiri katika kuwaangamiza waliowakufuru na Kuwaokoa waliowasadiki. Allah تعالی Amesema:

أَوْلَمَرَيسِرُوا فِي الْأَرْضِ

“Je! Hawatembei katika ardhi...”

Maana yake: kwa fahamu na akili zao, kuangalia kwao na kusikia khabari za waliopita. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَنِيبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ كَانُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ

“...wakaona ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Nao walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao...”

Maana yake: Umma na vizazi vilivyopita vilikuwa na nguvu zaidi kuliko nyinyi, ambao mmeletewa Muhammad ﷺ, tena walikuwa na mali nyingi na watoto wengi. Wala nyinyi hamkupewa japo sehemu moja ya kumi katika walivyopewa wao. Walimakinishwa ardhini kumakinika ambako nyinyi hamjakufikia. Walijenga humo duniani majengo marefu ambayo waliyajenga mengi zaidi kuliko ninyi, na waliyatumia zaidi kuliko mnavyoyatumia nyinyi. Pamoja na haya, Mitume walipowajia na dalili bayana, huku wakiwa wanayafurahia yale waliyopewa, Allah تعالى Aliwaadhibu kwa sababu ya madhambi yao, wala hawakuwa na wa kuwakinga dhidi ya Allah تعالى. Si mali zao wala watoto wao waliowazuia dhidi ya Ghadhabu za Allah تعالى, wala hawakuwaondolea japo uzito wa mdudu chungu, wala Allah تعالى si Mwenye Kuwadhulumu kuhusu adhabu Alizowapelekea,

وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٩﴾

“...lakini walikuwa wakijidhulumu nafsi zao.”

Maana yake: Kwa hakika walipatiwa kulingana na walivyozikadhibisha Aya za Allah تعالى na wakazifanyia stihizai. Hayakuwa hayo, isipokuwa kwa sababu ya madhambi yao yaliyopita na ukadhibishaji wao uliotangulia. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

ثُمَّ كَانَ عَنِيبَةَ الَّذِينَ أَصْنَعُوا أَلْسُوأَىٰ أَنْ كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَكَانُوا بِهَا يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٢٠﴾

“Kisha ulikuwa mwisho wa waliofanya ubaya ni kuzikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakawa wanazifanyia maskhara.”

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَدْرُؤُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza, Tunawaacha katika maasi yao wakitangatanga.” (6:110)

فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ ۗ

“Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Alizipotoa nyoyo zao.” (61:5)

فَإِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمُوا أَنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَن يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوبِهِمْ ۗ

“Na wakigeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu Anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao.” (5:49)

Pia ilisemwa kuwa maana ya hayo ni,

ثُمَّ كَانَ عِقَابَ الَّذِينَ اسْتَوُوا أَلْسُوَآءَ

“Kisha ulikuwa mwisho wa waliofanya ubaya...” (30:10)

Maana yake: Mwisho wao ulikuwa ni mbaya, kwa sababu walizikadhibisha Aya za Allah تعالى na wakawa wanazifanyia mzaha. Hii ni rai ya Ibn Jarir رضي الله عنهما¹ na aliyankuu haya kutoka kwa Ibn ‘Abbas na Qatadah رحمه الله تعالى.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwao wote wawili na kutoka kwa Adh-Dhahhak bin Muzahim. Hilo liko dhahiri - Allah Ndiye Mjuzi - kwa Kauli Yake,

وَكَانُوا بِهَا يَسْتَهْزِءُونَ ﴿١١٠﴾

“...na wakawa wanazifanyia maskhara.”

¹ At-Tabari 20:79.

اللَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨﴾ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُبْلِسُ
 الْمُجْرِمُونَ ﴿٩﴾ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ مِّنْ شُرَكَائِهِمْ شُفَعَاتٌ وَأَكَانُوا بِشُرَكَائِهِمْ كَافِرِينَ ﴿١٠﴾
 وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ فَهُمْ فِي رَوْضَةٍ يُحْبَرُونَ ﴿١٢﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقَاءِ
 الْآخِرَةِ فَأُولَٰئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ﴿١٣﴾

11. "Mwenyezi Mungu Huanzisha uumbaji, kisha Akaurudisha mara ya pili, na kisha mtarejeshwa Kwake."

12 "Na itaposimama Saa wakosefu watakata tamaa."

13. "Wala hawatakuwa na waombezi miongoni mwa waliokuwa wakiwashirikisha na Mungu; na wao wenyewe watawakataa hao washirikishwa wao."

14. "Na siku itaposimama Saa, siku hiyo watagawanyika."

15. "Ama walioamini na wakatenda mema watafurahishwa katika Bustani."

16. "Na ama waliokufuru na wakazikanusha Ishara Zetu na mkutano wa Akhera, hao basi watahudhurishwa katika adhabu."

Allah تعالى Anasema:

اللَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ

"Mwenyezi Mungu Huanzisha Uumbaji, tena Akaurudisha mara ya pili..."

Kama ambavyo Yeye ni Mweza wa Kuuanzisha, basi pia ni Mweza wa Kuurudisha mara nyingine,

ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿١٣﴾

"...na kisha mtarejeshwa Kwake." Maana yake: Katika Siku ya Kiyama Atamlipa kila mtenda amali kwa amali yake. Kisha Amesema:

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُبْلِسُ الْمُجْرِمُونَ ﴿١٣﴾

"Na itaposimama Saa wakosefu watakata tamaa."

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما: "Waovu watakata tamaa." Mujahid amesema: "Waovu watafedheheka." Na katika masimulizi mengine, "Wenye dhambi watajuta."¹

وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ مِّنْ شُرَكَائِهِمْ شُفَعَاءُ

"Wala hawatakuwa na waombezi miongoni mwa waliokuwa wakiwashirikisha na Mungu..."

Maana yake: Miungu waliyokuwa wakiiabudu badala ya Allah تعالى Haitawaomba, na itawakataa na kuwasaliti katika kipindi ambacho wanahitaji mno msaada wao kuliko wakati wowote ule. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُومِئذٍ يَنفِرُ قَوْمٌ

"Na siku itaposimama Saa, siku hiyo watagawanyika."

Qatadah amesema: "Wallah! huu ni utengano ambao hakuna tena kukutana baada yake."² Maana yake ni kwamba atakapomwingiza huyu peponi na kumtupa huyu motoni, huo ndio mwisho wa kukutana kati yao.

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَهُمْ فِي رَوْضَةٍ يُحْبَرُونَ

"Ama walioamini na wakatenda mema watafurahishwa katika Bustani."

Mujahid na Qatadah wamesema: "Hii inamaanisha kwamba watafurahia maisha ya starehe."³

فَسُبْحَانَ اللَّهِ حِينَ تُمْسُونَ وَحِينَ تُصْبِحُونَ ﴿١٧﴾ وَ لَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

وَعَشِيًّا وَحِينَ تُظْهِرُونَ ﴿١٨﴾ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيتِ وَيُخْرِجُ الْمَمِيتَ مِنَ الْحَيِّ وَيُحْيِي

الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ وَكَذَلِكَ تُخْرَجُونَ ﴿١٩﴾

17. "Basi Subhanallah! Mtakaseni Mwenyezi Mungu jioni na asubuhi,"

¹At-Tabari 20:80.

²At-Tabari 20:81.

³At-Tabari 20:82.

18. “Na Sifa zote Njema ni Zake katika mbingu na ardhi, na usiku na mchana.”

19. “Hukitoa kilicho hai kutokana na kilicho kufa, na Hukitoa kilicho kufa kutokana na kilicho hai. Na Huihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Na kama hivyo ndivyo mtavyofufuliwa.”

Amri ya Swala Tano

Hapa, Allah تعالى Anaitukuza Nafsi Yake Tukufu na Anawaamuru waja Wake wamtukuze, wamhimidi katika nyakati hizi ambazo huja kwa kufuatana, ambazo hujulisha ukamilifu wa Kudura Yake na Nguvu Zake. Haya ni pindi usiku unapoingia pamoja na giza lake na wakati wa asubuhi inapoingia na mapambazuko yake kwa kutoa mwangaza. Halafu akaeleza juu ya Kumhimidi, kunakonasibiana na Kumtakasa. Allah تعالى Amesema:

وَلَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Na Sifa zote Njema ni Zake katika mbingu na ardhi...”

Maana yake: Yeye ni wa Kusifiwa kwa ajili ya Alivyoviumba mbinguni na ardhini, Kisha Amesema:

وَعَشِيًّا وَحِينَ تُظْهِرُونَ ﴿١٥﴾

“...na usiku na mchana”

Al-’Ishaa ni pindi giza linapokuwa nene na Idh-har ni muda ambapo mwangaza unakuwa mkali zaidi. Ametakasika Aliyeumba vyote hivyo viwili, Mwenye Kuipasua asubuhi na Mwenye Kuujalia usiku kuwa muda wa kupumzika. Allah تعالى Anasema:

وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ﴿١٦﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١٧﴾

“Na kwa mchana unapolidhihirisha! Na kwa usiku unapolifunika!”
(91:3-4)

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١٧﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ﴿١٦﴾

“Naapa kwa usiku unapofunika! Na mchana unapodhihiri!..” (92:1-2)

وَاللُّصْحَىٰ ﴿٣٠﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٣١﴾

“Naapa kwa mchana! Na kwa usiku unapotanda!” (93:1-2)

Kuna Aya nyingi kuhusu mada hii. Kauli ya Allah تعالى:

تُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيتِ وَتُخْرِجُ الْمَمِيتَ مِنَ الْحَيِّ

“Hukitoa kilicho hai kutokana na kilicho kufa, na hukitoa kilicho kufa kutokana na kilicho hai.”

Hicho ni kile ambacho kimetuzingira katika Uweza wake wa Kuumba vitu na kinyume chake. Aya hizi tukufu zenye kufuatana, zote ni za namna hii. Zinataja Kuumbwa kwa vitu na kinyume cha vitu hivyo, ili Awajulishe viumbe Wake juu ya Kudura Yake. Miongoni mwake ni Kutoa mbegu kutoka katika mimea na Kutoa mimea kutoka katika mbegu; kuku kutokana na yai na yai kutokana na kuku; mwanaadamu kutokana na manii na manii kutokana na mwanaadamu; na muumini kutokana na kafiri na kinyume chake. Kauli Yake.

وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٣١﴾ وَاللُّصْحَىٰ ﴿٣٠﴾

“Na Huihuisha ardhi baada ya kufa kwake.”

Ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَيُّهُ هُمْ الْأَرْضُ الْمَمِيتَةَ أَحْيَيْنَاهَا وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ ﴿٣٢﴾

“Na Ishara hiyo kwao - ardhi iliyokufa, nasi Tukaifufua, na Tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila!”

Mpaka,

وَفَجَّرْنَا فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ ﴿٣٣﴾

“...na Tukatimbia chemchem ndani yake.” (36:33-34)

وَتَرَى الْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ وَأُنْبِتَتْ مِنْ كُلِّ زَوْجٍ

بِهَيْجٍ ﴿٣٤﴾

“Na unaiona ardhi imetulia kimya, lakini Tunapoyateremsha maji juu yake husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.”

Mpaka,

فِيهَا وَأَنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُورِ ﴿٧﴾

“...na kwamba hakika Mwenyezi Mungu Atawafufua walio makaburini.” (22:5-7)

Na kauli yake Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۖ حَتَّىٰ إِذَا أَقْلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا

“Na Yeye Ndiye Anayepeleka pepo kuwa ni bishara kabla ya kufika Rehema Yake. Hata hizo pepo zinapobeba mawingu mazito...”

Mpaka Kauli Yake,

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾

“...ili mpate kukumbuka.” (7:57)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Anasema katika Aya hii:

وَكَذَٰلِكَ تُخْرَجُونَ ﴿٥٨﴾

“Na kama hivyo ndivyo mtavyofufuliwa.”

* * *

وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنْتُمْ بَشَرٌ
 تَنْتَشِرُونَ ﴿٢٠﴾ وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ
 أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ
 فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ وَمِنْ ءَايَاتِهِ خَلْقُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافُ اللَّسَانَاتِ وَاللَّوْنِكُمْ إِنَّ
 فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْعٰلَمِينَ ﴿٢٢﴾ وَمِنْ ءَايَاتِهِ مَتَابِعُهُمْ
 بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَآبِغَاؤُهُمْ مِنْ فَضْلِهِ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٢٣﴾ وَمِنْ ءَايَاتِهِ يُرِيكُمُ
 الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَيُخْرِجُ بِهِ
 الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ
 يَعْقِلُونَ ﴿٢٤﴾ وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ
 بِأَمْرِهِ ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِنَ الْأَرْضِ إِذَا أَنْتُمْ
 تَخْرَجُونَ ﴿٢٥﴾ وَ لَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلِّ
 لَّهُ قَنِينٌ ﴿٢٦﴾ وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ
 وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ﴿٢٧﴾ وَ لَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ فِي السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٨﴾

وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ
 ثُمَّ إِذَا أَنْتُمْ بَشَرٌ تَنْتَشِرُونَ ﴿٢٠﴾
 وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ
 أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا
 وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ
 فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾

20. "Na katika Ishara Zake ni kuwa kakuumbeni kwa udongo. Kisha mmekuwa watu mliotawanyika kote kote."

21. "Na katika Ishara zake ni kuwa Amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri."

Miongoni mwa Ishara za Allah تعالى.

Allah تعالى Anasema,

وَمِنْ ءَايَاتِهِ

"Na katika Ishara Zake..."

Zenye kuonesha Utukufu Wake na Ukamilifu wa Kudura Zake, ni kwamba Alimuumba baba yenu, Adam kutokana na udongo,

ثُمَّ إِذَا أَنتُم بِبَشَرٍ تَنْتَشِرُونَ ﴿٢٠﴾

“Kisha mmekuwa watu mliotawanyika kote kote.”

Asili yenu kwa hiyo ni udongo, kisha kutokana na maji yenye kudharaulika. Kisha likabadilika na kuwa pande la damu, halafu pande la nyama, kisha likawa mfupa ulio katika umbo la mwanaadamu. Halafu Allah تعالی Akaivisha nyama mifupa hiyo. Halafu Allah تعالی Akapulizia roho ndani yao, na Kumuezesha kusikia na kuona. Baadaye, akatoka kutoka tumbo la mama yake akiwa mdogo, dhaifu, hana nguvu za kwenda. Kisha, kadiri umri wake unavyozidi kuwa mrefu, nguvu zake na mwendo wake utakuwa unazidi kukamilika, mpaka anafikia umri ambapo anajenga miji na ngome, anasafiri kwenda maeneo mbalimbali ya majimbo, anapanda juu ya bahari, kuzunguka sehemu mbalimbali za ardhi. Anachuma na kukusanya mali, huku akiwa na fikra, akili, ustadi, mbinu, rai na ujuzi wa kujichumia mambo ya duniani na akhera kila mmoja kwa jinsi yake mwenyewe. Ni Mtukufu Aliyewawezesha na Kuwarahisishia na Kuwatiisha na Akawafundisha fani mbalimbali za kimaisha na uchumi na Akawafanya watofautiane katika elimu na uwezo wa kifikra, uzuri na ubaya, wema na uovu, furaha na taabu. Kwa ajili hii Allah تعالی Amesema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنتُم بِبَشَرٍ تَنْتَشِرُونَ ﴿٢١﴾

“Na katika Ishara Zake ni kuwa Kakuumbeni kwa udongo. Kisha mmekuwa watu mliotawanyika kote kote.”

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alimnukuu Abu Musa رضي الله عنه akisema: Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ خَلَقَ آدَمَ مِنْ قَبْضَةٍ قَبْضَهَا مِنْ جَمِيعِ الْأَرْضِ، فَجَاءَ بَنُو آدَمَ عَلَى قَدْرِ الْأَرْضِ، جَاءَ مِنْهُمْ الْأَبْيَضُ وَالْأَحْمَرُ وَالْأَسْوَدُ وَبَيْنَ ذَلِكَ، وَالْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ، وَالسَّهْلُ وَالْحَزَنُ وَبَيْنَ ذَلِكَ»

“Allah Alimuumba Adam kutokana na kofi la mchanga Alilolichota katika ardhi yote. Wakaja wanaadamu kwa kiasi cha ardhi. Miongoni mwao, wapo waliokuja kwa weupe, wekundu, weusi na baina ya rangi hizo, wabaya na wazuri, laini na wagumu na baina ya hayo.”¹

¹ Ahmad 401-406.

Hadithi hii ilinukuliwa pia na Abu Dawud na At-Tirmidhi, ambaye amesema: "Hadithi hii ni *Hasan Sahih*."¹ Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا

"Na katika Ishara Zake ni kuwa Amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu..."

Maana yake: Amekuumbieni wanawake katika jinsi yenu wawe wake zenu,

لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا

"...ili mpate utulivu kwao."

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

* هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا

"Yeye Ndiye Aliyekuumbeni katika nafsi moja; na katika hiyo hiyo Akamfanya mwenzi wake, ili akae naye kwa utulivu." (7:189)

Kwa kauli hiyo, anamaanisha Hawwa. Allah تعالى Alimuumba kutokana na Adam kutoka katika ubavu wake mfupi wa upande wake wa kushoto. Lau kama Allah تعالى Angeliwajaalia wanaadamu wote kuwa wanaume na wanawake wao Akawajaalia watokane na jinsi nyingine, ima majini au hayawani, basi usingelikuwapo utangamano baina ya wanandoa. Bali kungelikuwa na utengano iwapo wangelitoka katika jinsi tofauti. Allah تعالى Alijaalia yawepo mapenzi na rehema baina ya waume na wake. Mwanamume hushikamana na mkewe, ama kwa mahaba au kwa huruma kwake, ikiwa wana mtoto au kumhitaji kwa ajili ya masuala ya kukimu ama kwa mazoea baina yao na mengine,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٣٠﴾

"Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri."

¹ Abu Dawud 5:67, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:290.

وَمِنْ آيَاتِهِمْ خَلْقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافُ أَلْسِنَتِكُمْ وَأَلْوَانِكُمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِلْعَالَمِينَ ﴿٢٠﴾ وَمِنْ آيَاتِهِمْ مَتَابِعُ مَا يُكْمَرُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَآبِغَاؤُكُمْ مِنْ فَضْلِهِ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُسْمَعُونَ ﴿٢١﴾

22. "Na katika Ishara Zake ni Kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika haya zipo Ishara kwa wajuji."

23. "Na katika Ishara Zake ni kulala kwenu usiku na mchana, na kutafuta kwenu Fadhila Zake. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaosikia."

Allah تعالیٰ Anasema:

وَمِنْ آيَاتِهِمْ

"Na katika Ishara Zake..."

Zenye kujulisha juu ya Kudura Yake kubwa,

خَلْقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

"...ni Kuumba mbingu na ardhi..."

Maana yake: Kuumbwa mbingu kwa marefu na mapana yake, namna ilivyo angavu, ung'avu wa sayari na nyota zake zilizotulia na zenye kwenda; na Kuumbwa kwa ardhi pamoja na kuwekwa kwake chini na ujazo wake, kadhalika na milima, mabonde na bahari zake, majangwa, wanyama na miti. Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَأَخْتِلَافُ أَلْسِنَتِكُمْ

"...na kutafautiana ndimi zenu..."

Maana yake: Lugha mbalimbali. Bado, wapo wanaotumia lugha ya Kiarabu na wapo Watatar ambao wana lugha nyingine. Pia wapo Wakaraj (Wajojia), Warumi, Wafaransa, Waberberi, Watukluri (wa Sudan), Wahabeshi (Waethiopia), Wahindi, Waajemi, Waswaqaalbah (Waslav), Wakhazar, Waarmenia, Wakurudi na wengine. Allah تعالیٰ Ndiye Azijuaye lugha nyingi tofauti tofauti za wanaadamu, na kukhitilafiana kwa rangi zao ambazo ndio

pambo lao. Watu wote wa ardhini, bali wa dunia nzima, tangu Allah تعالى Amuumbe Adam عليه السلام mpaka siku ya kiyama, kila mmoja akiwa na macho mawili, nyusi sehemu mbili, pua moja, paji moja la uso, mdomo mmoja na mashavu mawili. Hapana hata mmoja katika wao aliyeshabihiana na mwingine, bali ni lazima atofautiane naye kwa jambo kama vile mkaao, mwonekano au mazungumzo, iwe kwa dhahiri au kwa siri inayodhihiri kwa uchunguzi makini. Kila uso mmojawapo una staili yake katika dhati yake na mwonekano wake usiofanana na mwingine. Lau kutakuwa na kikundi cha watu ambao wanaonekana kufanana katika uzuri au ubaya, hapana budi kuwepo tofauti baina ya mtu mmoja wao na mwingine.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْعَالِمِينَ ﴿٢٠﴾

“Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi.”

Maana yake: Wanaotambua.

وَمِنَ آيَاتِهِ مَتَابُكُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَآبِغَاؤِكُمْ مِّنْ فَضْلِهِ

“Na katika Ishara Zake ni kulala kwenu usiku na mchana, na kutafuta kwenu Fadhila Zake.”

Maana yake: Miongoni mwa alama za Allah تعالى, ni kwamba Amejaalia usingizi usiku na mchana. Ndani yake yanapatikana mapumziko, utulivu wa harakati na kuondoka kwa taabu na uchovu. Amekujaalieni kusambaa na kwenda katika kutafuta maisha na safari wakati wa mchana, hiki ni kinyume cha kulala.

وَمِنَ آيَاتِهِ يُرِيكُمُ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَيُخْرِجُ بِهِ الْأَرْضَ

بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢١﴾ وَمِنَ آيَاتِهِ أَنْ تَقُومَ

السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ ۗ ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِّنَ الْأَرْضِ إِذَا أَنتُمْ تَخْرُجُونَ ﴿٢٢﴾

24. “Na katika Ishara Zake hukuonesheni umeme kwa kukutieni khofu na tamaa. Na hukuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaozingatia.”

25. “Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa Amri Yake. Kisha Atakapokuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi.”

Allah تعالیٰ Amesema:

وَمِنْ آيَاتِهِ

“Na katika Ishara Zake...”

Zenye kujulisha Utukufu Wake, kwamba Yeye,

يُرِيكُمْ أَلْبَرَقَ خَوْفًا وَطَمَعًا

“...hukuonesheni umeme kwa kukutieni khofu na tamaa.”

Maana yake: Wakati mwingine mnakhofia litakalotokea baadaye, kama vile mvua nyingi na radi ya kuangamiza inayoifuatia. Wakati mwingine mnakuwa na matumaini kwa kuona radi ikimulika ambayo yaweza kufuatiwa na mvua yenye kuhitajika. Kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Amesema:

وَيُنَزِّلُ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَيُخْرِجُ بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا

“Na hukuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo huifufua ardhi baada ya kufa kwake.”

Maana yake: Baada ya kuwa kame, ikiwa haina mimea wala chochote. Yanapoifikia maji, basi,

أَهْرُتْ وَرَبَّتْ وَأُنْبِتُ مِنْ كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ﴿٥﴾

“...husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.” (22:5)

Katika hayo, kuna mazingatio na ushahidi dhahiri juu ya Marejeo na kusimama kwa Kiyama. Kwa minajili hii, Allah تعالیٰ Amesema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٥﴾

“Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaozingatia.”

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَمِنْ آيَاتِهِمْ أَنْ تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ

“Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa Amri Yake.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَيُؤَمِّسُكَ السَّمَاءُ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ

“...na Amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa Idhini Yake.” (22:65)

✦ إِنَّ اللَّهَ يُمَسِّكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا

“Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezuilia mbingu na ardhi zisiondoke.” (35:41)

Pindi ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alipokuwa akiapa kwa mkazo, amesema: “Hapana. Naapa kwa Ambaye mbingu na ardhi zimesimama kwa Amri Yake. Yaani, zinasimama madhubuti kwa Amri Yake kwazo na Kuzitiisha Kwake. Halafu, ikishakuwa Siku ya Kiyama mbingu na ardhi zitabadilishwa na maiti watatoka makaburini mwao wakiwa hai kwa Amri ya Allah تعالى na Kuwaita Kwake. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِّنَ الْأَرْضِ إِذَا أَنتُمْ تَخْرُجُونَ ﴿٥٥﴾

“Kisha Atakapokuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi.”

Maana yake: Kutoka ardhini. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٦﴾

“Siku atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.” (17:52)

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿٣٦﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿٣٧﴾

“Kwa hakika hayo ni Zajrah (ukelele mmoja tu).¹ Mara watakuwa kwenye uwanda wa mkutano!” (79:13-14)

إِن كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٣٨﴾

“Haitakuwa ila Swayhah (ukelele mmoja tu),² mara wote watahudhurishwa mbele yetu.” (36:53)

وَلَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلٌّ لَهُ قَنِينٌ ﴿٣٩﴾ وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ؕ وَلَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ؕ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤٠﴾

26. “Na Vyake Yeye vilivyo mbinguni na katika ardhi. Vyote vinamt’ii Yeye.”

27. “Na Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake. Naye ndiye Mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Allah تعالى Anasema:

وَلَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Na Vyake Yeye vilivyo mbinguni na katika ardhi.”

Maana yake: Ni miliki Yake na ni waja Wake,

كُلٌّ لَهُ قَنِينٌ ﴿٣٩﴾

“Vyote vinamtii Yeye.”

Maana yake: Wanyenyekvu na kujisalimisha Kwake iwe kwa kutii au kwa kulazimishwa.

¹ Angalia Tafsiri ya Surat As-Saaffaat (37:19).

² Angalia Tafsiri ya Surat Hud (11)94).

Kurudia Kuumba ni rahisi Mno

Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

“Na Yeye Ndiye Anayezisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.”

Ibn Abu Twalhah amesema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: “Maana yake, ni rahisi mno Kwake”¹ Mujahid amesema: “Kukirejesha ni rahisi zaidi Kwake kuliko Kukiumba kwa mara ya kwanza, na Kukiumba, pia ni rahisi sana Kwake.”² Hii ilikuwa ndiyo rai ya Ikrimah na wengine pia.³ Na Bukhari amenukuu kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ amesema,

«قَالَ اللهُ: كَذَّبَنِي ابْنُ آدَمَ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ ذَلِكَ، وَشَتَمَنِي وَلَمْ يَكُنْ لَهُ ذَلِكَ، فَأَمَّا تَكْذِيبُهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ: لَنْ يُعِيدَنِي كَمَا بَدَأَنِي وَلَيْسَ أَوَّلُ الْخَلْقِ بِأَهْوَنَ عَلَيَّ مِنْ إِعَادَتِهِ، وَأَمَّا شَتْمُهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ: اتَّخَذَ اللهُ وَلَدًا، وَأَنَا الْأَحَدُ الصَّمَدُ الَّذِي لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفْوًا أَحَدًا»

“Allah Amesema: ‘Mwanaadamu amenikadhibisha, wala hana haki ya hilo. Amenibeza, wala hana haki ya hilo. Ama kunikadhibisha kwake ni kauli yake: ‘Hatanirudisha kama Alivyonzisha, wala Kuumba kwa mara ya kwanza si kwepesi zaidi Kwangu kuliko Kukirejesha. Ama Kunishutumu kwake ni kauli yake: ‘Allah kajifanyia mwana,’ ilhali, Mimi ni Mmoja, Mwenye Kucusudiwa, Ambaye Sikuzaa wala Kuzaliwa wala hakuna wa kufanana na Mimi.”

Hadithi hii ilinukuliwa na Bukhari peke yake.⁴ Kauli ya Allah تعالى:

وَلَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Naye Ndiye Mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi.”

¹ At-Tabari 20:92.

² At-Tabari 20:92.

³ At-Tabari 20:92.

⁴ Fath Al-Bari 8:611-612.

'Ali bin Abu Twalhah kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما: Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

"Hapana kitu kama mfano wake." (42:11)

Qatadah amesema: Maelezo yake ni kwamba, hapana wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye.

* * *

ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِّنْ أَنْفُسِكُمْ ۗ هَلْ لَكُمْ مِّنْ مَا مَلَكَتْ
 أَيْمَانُكُمْ مِّنْ شُرَكَاءَ فِي مَا رَزَقْنَاكُمْ فَأَنْتُمْ فِيهِ سَوَاءٌ
 تَخَافُونَهُمْ كَخِيفَتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ ۗ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ
 لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾ بَلِ اتَّبَعَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَهْوَاءَهُمْ
 بِغَيْرِ عِلْمٍ ۖ فَمَنْ يَهْدِي مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ ۗ وَمَا هُمْ مِنْ نَّاصِرِينَ
 ﴿٢٩﴾ فَأَقْرِبْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۗ فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ
 النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ
 وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾ * مُبَيِّنِينَ إِلَيْهِ
 وَأَتَّقُوهُ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُشْرِكِينَ
 ﴿٣١﴾ مِنَ الَّذِينَ فَرَقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيعًا ۗ كُلُّ
 حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٣٢﴾ وَإِذَا مَسَّ النَّاسَ ضُرٌّ
 دَعَوْا رَبَّهُمْ مُبِيِّنِينَ إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا أَذَقَهُمْ مِنْهُ رَحْمَةً إِذَا فَرِيقٌ
 مِنْهُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾ لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَاهُمْ ۖ فَتَمَتَّعُوا
 فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٣٤﴾ أَمْ أَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا فَهُوَ
 يَتَكَلَّمُ بِمَا كَانُوا بِهِ يُشْرِكُونَ ﴿٣٥﴾ وَإِذَا أَدَقْنَا النَّاسَ
 رَحْمَةً فَرِحُوا بِهَا ۗ وَإِن تُصِيبَهُمْ سَيِّئَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ إِذَا
 هُمْ يَقْتَبُونَ ﴿٣٦﴾ أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ
 يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٣٧﴾

ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِّنْ أَنْفُسِكُمْ ۗ هَلْ
 لَكُمْ مِّنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّنْ
 شُرَكَاءَ فِي مَا رَزَقْنَاكُمْ فَأَنْتُمْ فِيهِ
 سَوَاءٌ تَخَافُونَهُمْ كَخِيفَتِكُمْ
 أَنْفُسَكُمْ ۗ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ
 لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾ بَلِ اتَّبَعَ
 الَّذِينَ ظَلَمُوا أَهْوَاءَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۖ
 فَمَنْ يَهْدِي مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ ۗ وَمَا هُمْ
 مِنْ نَّاصِرِينَ ﴿٢٩﴾

28. "Amekupigieni mfano kutokana na nafsi zenu. Je! Katika hao iliyowamiliki mikono yenu ya kulia mnao washirika katika hivyo Tulivyokuruzukuni, mkawa nyinyi katika hivyo ni sawasawa, mnawaogopa kama mnavyoogopana wenyewe kwa wenyewe? Namna hivi Tunazipambanua Aya Zetu kwa watu wenye akili."

29. "Bali waliodhulumu wamefuata mapendo ya nafsi zao pasi na kujua. Basi

nani atamwongoa ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha apotee? Wala hao hawatakuwa na wa kuwanusuru."

Mfano Unaojulisha Upekee wa Allah تعالی (Tauhidi)

Huu ni mfano Alioupiga Allah تعالی kwa wanaomshirikisha, ambao humwabudu Yeye pamoja na vitu vingine, pia humfanyia washirika licha ya kwamba wanakiri kuwa washirika wanaompachikia ambayo ni masanamu na washindani ni waja Wake, wanamilikiwa Naye. Ni sawa na wanavyokuwa katika *Talbiyah* zao wakisema: “Tumekuitika, huna mshirika, isipokuwa mshirika wako, Unammiliki yeye pamoja na anavyovimiliki.” Allah تعالی Amesema:

ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِّنْ أَنْفُسِكُمْ

“Amekupigieni mfano kutokana na nafsi zenu.”

Mnayoishuhudia na kuifahamu katika nafsi zenu.

هَلْ لَّكُمْ مِّنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّنْ شُرَكَاءَ فِي مَا رَزَقْنَاكُمْ فَأَنْتُمْ فِيهِ سَوَاءٌ

“Je! Katika hao iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia mnao washirika katika hivyo tulivyo kuruzukuni, mkawa nyinyi katika hivyo ni sawasawa...”

Maana yake: Yeyote katika nyinyi haridhii kwamba mtumwa wake awe mshirika wake katika mali zake, basi Allah تعالی Naye Haridhii hali hiyo Kwake,

تَخَافُونَهُمْ كَخِيفَتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ

“...mnawaogopa kama mnavyoogopana wenyewe kwa wenyewe?”

“Mnachelea kwamba watakuwa na fungu katika mali zenu pamoja nanyi.” Abu Mijlaz amesema, “Hamukhofii kwamba mtumishi wenu atakuwa na mgao wake katika mali zenu, kwa sababu hana haki hiyo? Halikadhalika, Allah تعالی hana mshirika.”¹ Maana yake ni kwamba, kwa kuwa kila mmoja wenu haipendi hali hiyo, basi vipi mnamwekea Allah تعالی washindani. At-Tabarani alinukuu kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema, “Washirikina walikuwa wakisoma *Talbiyah* kwa kusema, ‘Tumekuitika, huna mshirika, isipokuwa mshirika wako, Unammiliki yeye pamoja na anavyovimiliki.’ Allah تعالی Akateremsha Aya:

¹ At-Tabari 20:96.

هَلْ لَكُمْ مِّنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّنْ شُرَكَاءَ فِي مَا رَزَقْنَاكُمْ فَأَنْتُمْ فِيهِ سَوَاءٌ تَخَافُونَهُمْ
كَخِيفَتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ

“Je! Katika hao iliyowamiliki mikono yenu ya kulia mnao washirika katika hivyo tulivyokuruzukuni, mkawa nyinyi katika hivyo ni sawasawa, mnawaogopa kama mnavyooogopana wenyewe kwa wenyewe?”¹

Kama unavyofahamisha mfano huu juu ya kuwa mbali na hilo na kutakasika Kwake Allah تعالى kwa namna iliyo bora zaidi. Allah تعالى Amesema:

كَذَلِكَ نَفْصِلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾

“Namna hivi Tunazipambanua Aya Zetu kwa watu wenye akili.”

Kisha, Allah Aliwabainishia washirikina kuhusu hilo kwamba walimwabudu asiye kuwa Yeye kwa upumbavu na ujinga wao.

بَلِ اتَّبَعَ الَّذِينَ ظَلَمُوا

“Bali waliodhulumu wamefuata...”

Maana yake: Washirikina,

أَهْوَاءَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ

“...mapendo ya nafsi zao...”

Maana yake: Katika ibada yao kwa waungu waongo pasi na elimu,

فَمَنْ يَهْدِي مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ

“Basi nani atamwongoa ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha apotee?”

Maana yake: Hakuna wa kuwaongoza pindi Allah تعالى Akishawaandikia kupotea kwao.

¹ At-Tabarani 12:20, kwa isnadi dhaifu.

وَمَا هُمْ مِّنْ نَّصِيرِينَ ﴿٣٠﴾

“Wala hao hawatakuwa na wa kuwanusuru.”

Maana yake: Hakuna wa kuwaokoa dhidi ya Kudura ya Allah تعالى au kuwapa kimbilio, kwa sababu akitakacho huwa na asichokitaka hakiwi.

فَأَقْزَمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۗ فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ۗ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ۗ
ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣١﴾ * مُبِينًا إِلَيْهِ وَاتَّقُوهُ
وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٣٢﴾ مِنَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا
شِيْعًا ۗ كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٣٣﴾

30. “Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyonyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.”

31. “Muwe wenye kutubia Kwake, na mcheni Yeye, na shikeni Swala, na wala msiwe katika washirikina.”

32. “Katika wale ambao kwamba wameigawanya dini yao, na wakawa makundi makundi, kila kikundi kinafurahia kilicho nacho.”

Amri ya Kushikamana na Itikadi ya Upekee wa Allah تعالى (Tauhidi)

Allah تعالى Anasema, ‘Basi, uelekeze uso wako na uendeleo katika dini ambayo Allah تعالى Alikuwekea, ya kumwabudu Allah تعالى Peke Yake, dini ya Ibrahim عليه السلام, ambayo Allah تعالى Alikuongoza kuifuata na Akakukamilishia neema kamilifu. Pia utashikamana na *Fitrah* yako iliyosalimika ambayo Allah تعالى Ameumba viumbe wake katika umbile linalowafanya kumfahamu na kumpwekesha, na kujua kuwa hapana Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, kama yalivyotangulia maelezo hayo katika tafsiri ya Neno Lake Allah تعالى:

¹ Muslim 4:2197.

وَأَشْهَدُهُمْ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَىٰ

“...na Akawashuhudisha juu ya nafsi zao, Akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwa nini, ndio Wewe Mola wetu Mlezi!” (7:172)

Pia katika Hadithi:

«إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حُتَفَاءً، فَاجْتَالَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ عَن دِينِهِمْ»

“Nimewaumba waja wangu Hunafa (wasiokuwa wapotevu), shetani akawapoteza kutoka katika dini yao.”¹

Tena, tutataja Hadithi zinazoeleza kuwa Allah تعالى Ameumba viumbe vyake katika umbile la Uislamu kisha baadhi yao wakazukiwa na dini nyingine kama vile Uyahudi, Ukristo na Umajusi:

لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ

“Hapana mabadiliko katika Uumbaji wa Mwenyezi Mungu.”

Baadhi ya maulamaa wamesema: Maana yake, msilibadili umbo Aliloliumba Allah تعالى, mkawabadilisha watu kutoka katika *Fitra* ya Allah تعالى ambalo Allah تعالى Aliwaumba juu yake. Haya ni maelezo yenye maana ya amri ndani yake. Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

وَمَن دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا

“...na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani.”

Hii ni maana nzuri tena sahihi. Maana yake ni kwamba, Allah تعالى Aliweka usawa wa viumbe vyote katika *Fitra* na kwa asili iliyonyooka. Hazaliwi yeyote, isipokuwa juu ya asili hiyo, wala watu hawajatofautiana katika hilo. Kwa minajili hii, Ibn ‘Abbas, Ibrahim An-Nakha’i, Sa’id bin Jubayr, Mujahid, ‘Ikrimah, Qatadah, Adh-Dhahhak na Ibn Zayd رضي الله عنهم wamesema juu ya Kauli ya Allah تعالى:

¹ Tabari 20:99.

لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ

“Hapana mabadiliko katika Uumbaji wa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Katika Dini ya Allah.¹ Bukhari naye amesema: Kauli ya Allah تعالى،

لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ

“Hapana mabadiliko katika Uumbaji wa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Katika Dini ya Allah تعالى، umbo la wale wa awali ni dini yao, yaani, dini na *Fitra* ni Uislamu. Kisha, Alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ مَزْلُودٍ يُوَلَّدُ إِلَّا عَلَى الْفِطْرَةِ فَأَبَوَاهُ يُهَوِّدَانِهِ أَوْ يُنَصْرَانِهِ أَوْ يُمَجْسَانِهِ، كَمَا تُنْتَجِجُ الْبَيْهَمَةُ بِبَيْهَمَةٍ جَمْعَاءَ، هَلْ تُحْسِنُونَ فِيهَا مِنْ جَدْعَاءَ؟»

“Hapana mtoto azaliwaye isipokuwa huwa katika Fitrah, basi wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi, au Mkiristo au Mmajusi, kama vile mnyama anavyozaa mnyama kama yeye, je, mnamwona yeyote miongoni mwao aliyezaliwa akiwa mlemavu.”

Halafu (Abu Hurayrah رضي الله عنه) amesema،

فَطَرَتِ اللَّهُ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ

“Ndilo umbile la Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika Uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyonyooka sawa.”

Hii ilinukuliwa na Muslim pia.¹ Kauli ya Allah تعالى:

ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ

“Hiyo ndiyo Dini iliyonyooka sawa.”

Maana yake: Kushikamana na sharia na *Fitrah* iliyosalimika ndiyo Dini iliyonyooka،

¹Fat’h Al-Bari 8:372; 11:512, Muslim 4:2047, 2048.

وَلَيْكِبْ أَكْثَرُ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

“Lakini watu wengi hawajui.”

Maana yake: Watu wengi hawalijui hili na wanapotoka mbali na njia. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.”
(12:103)

وَأَنْ تَطِيعَ أَكْثَرَ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

“Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na Njia ya Mwenyezi Mungu.” (6:116)

Kauli ya Allah تعالى:

﴿ مُنِيبِينَ إِلَيْهِ ﴾

“Muwe wenye kutubia kwake...”

Ibn Zayd na Ibn Jurayj wamesema: “Inamaanisha wenye kurejea Kwake.”¹

وَأَتَّقُوهُ

“...na mcheni Yeye...”

Maana yake: Mwogopeni na kwamba Yeye Anakuchungeni,

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ

“...na shikeni Swala...”

Na ndio utii mkubwa,

﴿ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴾

“...na wala msiwe katika washirikina.”

¹ At-Tabari 20:100.

Maana yake: Bali kuweni wenye kumpwekesha Yeye na kumtakasia Ibada, wala si mwingine. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Yazid bin Abu Maryam kuwa amesema: “Umar رضي الله عنه alipita kwa Mu’adh bin Jabal رضي الله عنه na kusema, ‘Ni nini msingi wa umma huu?’ Mu’adh رضي الله عنه akasema: ‘Ni mambo matatu, na hayo ndio yataleta uokovu, Ikhlas, ambayo ndiyo *Fitrah*, Swala ambayo ni kipambanuzi, na Utii ambao ni kinga.’ Umar رضي الله عنه akasema: ‘Umesema kweli.’”¹

Kugawanyika Katika Madhehebu²

Akasema:

مِنَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيعًا كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٣٠﴾

“Katika wale ambao kwamba wameigawanya dini yao, na wakawa makundi makundi, kila kikundi kinafurahia kilicho nacho.”

Maana yake: Msiwe kama washirikina, ambao waliigawanya dini yao, yaani waliibadilisha na wakaamini baadhi yake na kuyakataa baadhi. Baadhi ya wanazuoni, husoma *faaraqaw Diynahum*, maana yake waliacha nyuma ya migongo yao. Hao ni kama vile Wayahudi, Wakristo, Majusi, Wanaoabudu Masanamu na watu wa dini nyingine potovu, tofauti na wafuasi wa Uislamu. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيعًا لَسْتَ فِي شَيْءٍ إِنَّمَا أَمْرُهُمْ إِلَى اللَّهِ

“Hakika walioigawa Dini yao na wakawa makundi makundi, huna uhusiano nao wowote. Bila ya shaka shauri yao iko kwa Mwenyezi Mungu...” (6:159)

Wafuasi wa dini za kabla yetu walikhitilafiana juu ya yaliyokuwa baina yao kutokana na maoni na madhehebu yaliyopotoka, huku kila kundi katika wao likidai kwamba ndilo linalofuata ukweli. Umma huu kadhalika, umegawanyika katika yaliyo baina yao, na yote hayako katika Hidaya, isipokuwa kundi moja

¹ At-Tabari 20:98: Isnadi yake ni dhaifu mno

² Kichwa hiki cha habari kimeongezwa katika chapa ya kiingereza.

tu ambalo ni la *Ahlu-Sunnat Wal-Jama'ah*, wanaoshikamana na Kitabu cha Allah تعالى na Sunna ya Mtume ﷺ na yale waliyoyafuata kizazi cha kwanza, miongoni mwa Masahaba na wafuasi wao na maimamu wa Waislamu, wa mwanzoni na wa baada yao. Ni sawa na alivyonukuu Al-Hakim katika *Al-Mustadrak* yake kwamba Mtume ﷺ amesema kundi lililonusurika kuwa ni:

«مَا أَنَا عَلَيْهِ وَأَصْحَابِي»

*"Lile ambalo mimi na masahaba wangu niko juu yake."*¹

وَإِذَا مَسَّ النَّاسَ ضُرٌّ دَعَوْا رَبَّهُمْ مُنِيبِينَ إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا أَذَاقَهُمْ مِنْهُ رَحْمَةً إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾ لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَاهُمْ فَتَمَتَّعُوا فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٣٤﴾ أَمْ أَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا فَهُوَ يَتَكَلَّمُ بِمَا كَانُوا بِهِ يُشْرِكُونَ ﴿٣٥﴾ وَإِذَا أَذَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً فَرِحُوا بِهَا وَإِنْ تُصِيبُهُمْ سَيِّئَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ إِذَا هُمْ يَقْتَبُونَ ﴿٣٦﴾ أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٣٧﴾

33. *"Yakiwapata watu madhara humwomba Mola wao Mlezi nao wametubu Kwake. Kisha akiwaonjesha rehema itokayo Kwake, mara kikundi miongoni mwao humshirikisha Mola wao Mlezi,"*

34. *"Kwa kuyakataa Tuliowapa. Basi stareheni. Mtakuja jua!"*

35. *"Au Tumewateremshia hoja ambayo kwayo ndio wanafanya ushirikina?"*

36. *"Na watu Tunapowaonjesha rehema huifurahia, na ukiwasibu uovu kwa iliyoyatanguliza mikono yao wenyewe, mara wanakata tamaa."*

37. *"Kwani hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu Humkunjulia riziki Amtakaye na Humdhikisha Amtakaye? Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaoamini."*

¹ Al-Haakim 1:129.

Kayumba kwa Mwanadamu baina ya Kumpwekesha Allah تعالى (Tawhiid) na Ushirikina na Baina ya Faraja na Kukata Tamaa.

Allah تعالى Anakhabarisha kwamba watu wanapokuwa katika hali ya shida humwomba Allah تعالى Pekee, asiye na mshirika, na kwamba Akishawapatia neema juu yao, mara kundi mojawapo katika wao kwa hiyari yao, wanamshirikisha Allah تعالى na kumwabudu pamoja na Yeye na vitu vingine. Kauli ya Allah تعالى:

لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَاهُمْ

“Kwa kuyakataa Tuliowapa.”

Kwa baadhi ya maulamaa, herufi lamu iliyo katika neno *Liyakfuru* ni ya kuonesha matokeo (*Al-'Aaqibah*) ya jambo. Na wengine wamesema ni ya uthibitisho (*At-Ta'lii*) lakini ni uthibitisho wa Kudura ya Allah تعالى juu yao. Kisha, Allah تعالى Akawaonya,

فَسَوْفَ نَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾

“Mtakuja jua!”

Mmoja wao amesema: Wallah! Lau Mlinzi anayesimamia lindo angelinionya ningelikhofu, seuze mwenye kuonya hapa Ambaye Ndiye Hukiambia kitu 'Kuwa,' nacho kikawa? Kisha, Allah تعالى Akawakanusha washirikina waliyokhitilafiana, kama vile kumwabudu mwingine pasi na hoja wala ushahidi.

أَمْ أَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا

“Au Tumewateremshia hoja...”

Maana yake: Ushahidi,

فَهُوَ يَتَكَلَّمُ

“... ambayo kwayo ndio wanatamka...”

Maana yake: Wanatamka,

بِمَا كَانُوا بِهِ يُشْرِكُونَ ﴿٢٩﴾

“... Ambayo kwayo ndio wanafanya ushirikina?”

Swali hili ni fasaha, yaani hawana lolote katika haya. Halafu, Allah تعالى Amesema:

وَإِذَا أَدْقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً فَرِحُوا بِهَا ۗ وَإِن تُصِيبَهُمْ سَيِّئَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ إِذَا هُمْ
يَقْتُلُونَ ﴿٣٠﴾

“Na watu Tunapowaonjesha rehema huifurahia, na ukiwasibu uovu kwa iliyoyatanguliza mikono yao wenyewe, mara wanakata tamaa.”

Hili ni kanusho kwa mwanaadamu kwa namna alivyo, isipokuwa wale ambao Allah تعالى Anawakinga na Kuwasaidia, kwani mwanaadamu anapopatwa na neema hujivuna. Allah تعالى Amesema tena:

ذَهَبَ السَّيِّئَاتُ عَنِّي ۖ إِنَّهُ لَفَرِحَ فَخُورٌ ﴿٣١﴾

“...Taabu zimekwishaniondokea. Hakika yeye hujitapa na kujifakharisha.” (11:10)

Maana yake: Anafurahi katika nafsi yake na anajivuna kwa mwingine, na akipatwa na shida hukosa matumaini na kukata tamaa ya kupata kheri yoyote baada ya hayo. Allah تعالى Amesema,

إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Ila wale waliosubiri wakatenda mema.” (11:11)

Maana yake: Waliosubiri katika nyakati za taabu na wakatenda mema katika vipindi vya faraja. Ni kama ilivyothibiti katika *Sahih* Mbili,

«عَجَبًا لِلْمُؤْمِنِ لَا يَقْضِي اللَّهُ لَهُ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، إِنْ أَصَابَتْهُ سَرَاءٌ شَكَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ صَبَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ»

“Ajabu kwa Muumini, Allah Hapitishi jambo kwake, bali huwa ni kheri kwake. Ilikimpata la furaha, hushukuru. Hiyo inakuwa kheri kwake. Ikimsibu shari husubiri na hiyo nayo inakuwa kheri kwake.”¹

¹ Muslim 4:2295.

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ

“Kwani hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu Humkunjulia riziki Amtakaye na Humdhikisha Amtakaye?”

Inamaanisha kuwa Yeye Ndiye Mdhibiti Ambaye Huyafanya hayo kwa Hikima Zake na Uadilifu Wake, Huikunjulia kaumu mojawapo na Kuwadhikisha wengine,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٣٧﴾

“Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanaoamini.”

* * *

فَقَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ
 لِلَّذِينَ يُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ ۗ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٣٨﴾
 وَمَا آتَيْتُم مِّن رِّبَا يَرْبُوا فِي أَمْوَالِ النَّاسِ فَلَا يَرْبُوا عِنْدَ
 اللَّهِ ۗ وَمَا آتَيْتُم مِّن زَكَاةٍ تُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ
 هُمُ الْمُضْعِفُونَ ﴿٣٩﴾ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ ثُمَّ رَزَقَكُمْ ثُمَّ
 يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ۗ هَلْ مِن شُرَكَائِكُمْ مَّن يَفْعَلُ مِن
 ذَٰلِكُمْ مِثْلَ شَيْءٍ ۗ سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٠﴾ ظَهَرَ
 الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ
 بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٤١﴾ قُلْ سِيرُوا فِي
 الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلُ ۗ كَانَ
 أَكْثَرُهُم مُّشْرِكِينَ ﴿٤٢﴾ فَأَقْرِبْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ الْقَدِيمِ مِن
 قَبْلِ أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ ۗ يَوْمَئِذٍ يَصْدَعُونَ ﴿٤٣﴾
 مَن كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۗ وَمَن عَمِلَ صَالِحًا فَلِأَنفُسِهِمْ
 يَمْهَدُونَ ﴿٤٤﴾ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
 مِن فَضْلِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ ﴿٤٥﴾

فَقَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ
 وَابْنَ السَّبِيلِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ لِلَّذِينَ
 يُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ ۗ وَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْمُفْلِحُونَ ﴿٣٨﴾ وَمَا آتَيْتُم مِّن رِّبَا
 يَرْبُوا فِي أَمْوَالِ النَّاسِ فَلَا يَرْبُوا
 عِنْدَ اللَّهِ ۗ وَمَا آتَيْتُم مِّن زَكَاةٍ
 تُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْمُضْعِفُونَ ﴿٣٩﴾ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ
 ثُمَّ رَزَقَكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ
 ۗ هَلْ مِن شُرَكَائِكُمْ مَّن يَفْعَلُ مِن
 ذَٰلِكُمْ مِثْلَ شَيْءٍ ۗ سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَىٰ
 عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٠﴾

38. "Basi mpe jamaa haki yake, na masikini, na msafiri. Hayo ni kheri kwa watakao radhi ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufanikiwa."

39. "Na mnachokitoa kwa riba ili kiongezoke katika mali ya watu, basi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini mnachokitoa kwa Zaka kwa kutaka Radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio wataozidishiwa."

40. "Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni, kisha Akakuruzukuni, kisha Anakufisheni, na kisha Anakufufueni. Je! Yupo yeyote katika hao mnaowashirikisha na Mwenyezi Mungu afanyae lolote katika hayo? Yeye Ametakasika, na Ametukuka na hayo mnayomshirikisha Naye."

Amri ya Kushikamana na Udugu na Kuharamishwa kwa Riba

Allah تعالیٰ Anaamrisha Kumpa,

ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ

“... jamaa haki yake...”

Maana yake: Ihsani na kushikamana na undugu,

وَالْمَسْكِينِ

“...na masikini...”

Huyo ni iambaye hana kitu cha kujikimu nacho au ana kitu lakini hakimtoshelezi,

وَابْنِ السَّبِيلِ

“...na msafiri.”

Ni msafiri mwenye haja ya mali na shida nyingine katika safari yake,

ذَٰلِكَ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ يُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ

“Hayo ni kheri kwa watakapo radhi ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani: kumtazama Allah تعالیٰ katika Siku ya Kiyama, ambalo ndilo lengo la juu zaidi,

وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٣٨﴾

“Na hao ndio wenye kufanikiwa.” Yaani, duniani na Akhera. Halafu amesema:

وَمَا آتَيْتُم مِّن رَّبًّا لَّيْرُبُوا فِي أَمْوَالِ النَّاسِ فَلَا يَرْتَبُوا عِنْدَ اللَّهِ

“Na mnachokitua kwa riba ili kiongezeke katika mali za watu, basi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Mwenye kutoa zawadi ili watu wampatie nyingi kuliko aliyoitua yeye, atakuwa hana thawabu kwa Allah تعالیٰ. Hivi ndivyo Aya hii alivyotafsiri Ibn ‘Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, ‘Ikrimah, Muhammad bin Ka’b na Ash-`Aha’bi رضي الله عنهم.¹

¹ At-Tabari 20:104,105.

Kauli ya Allah تعالى:

﴿ وَمَا آتَيْتُم مِّن زَكَاةٍ تُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُضْعِفُونَ ﴾

“Lakini mnachokitoa kwa Zaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio wataozidishiwa.”

Maana yake: Wale ambao Allah تعالى Atawazidishia thawabu na malipo. Ni kama ilivyokuja katika *Sahih*,

«وَمَا تَصَدَّقَ أَحَدٌ بِعَدْلِ تَمْرَةٍ مِنْ كَنْبِ طَلَبٍ إِلَّا أَخَذَهَا الرَّحْمَنُ بَيْنَ يَدَيْهِ فَيُرِيهَا لِصَاحِبِهَا، كَمَا يُرِي أَحَدُكُمْ فَلْوَهُ أَوْ فَصِيلَهُ حَتَّى تَصِيرَ التَّمْرَةُ أَغْظَمَ مِنْ أَحَدٍ»

“Hatoi Sadaka mtu yeyote sawa na tende kwenye chumo halali, bali, Mwingi wa Rehema Huichukua kwa Mkono wa Kuume na Humzidishia aliyeitoa, kama mmoja wenu anavyomchungu ndama wa farasi au ngamia aliyeachishwa ziwa na mpaka tende inakuwa kubwa kuliko mlima wa Uhud.”¹

Kuumba, Kuruzuku, Kufisha na Kuhuisha Vipo Mkononi mwa Allah تعالى.

Kauli ya Allah تعالى:

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ ثُمَّ رَزَقَكُمْ

“Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni, kisha Akakuruzukuni...”

Maana yake: Muumbaji na Mtoa riziki. Humtoa mwanadamu tumboni mwa mama yake hana mavazi, elimu, usikivu, uoni wala nguvu. Halafu Humruzuku hayo yote pamoja na samani, mavazi, mali, umiliki na chumo.

ثُمَّ يُمِيتُكُمْ

“...kisha Anakufisheni...”

Inamaanisha, baada ya maisha haya,

¹ Muslim 2:702.

تُمْتِحِيكُمْ

“...na kisha Anakufufueni.” Yaani, katika Siku ya Kiyama.

هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ

“Je! Yupo yeyote katika hao mnaowashirikisha na Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Mnaowaabudu kinyume na Allah تعالى،

مَنْ يَفْعَلُ مِنْ دَالِكُمْ مِنْ شَيْءٍ

“... afanyae lolote katika hayo?”

Maana yake: Yeyote kati yao, hawezi kufanya chochote kati ya hayo, bali Allah تعالى Ndiye Pekee katika Kuumba, Kuruzuku, Kuhuisha na Kufisha. Halafu Atafufua viumbe Siku ya Kiyama. Kwa ajili hii, baada ya yote haya Allah تعالى Amesema,

سُبْحٰنَهُۥ وَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٤١﴾

“Yeye Ametakasika, na Ametukuka na hayo mnayo mshirikisha Naye.”

Maana yake: Ana heshima ya juu Ametakasika, Ameepukana (na kila upungufu), ni Mkuu, ni Mshindi dhidi ya kuwa na mshirika, au kifani, au wa kulingana au mwana au mzazi, bali, Yeye ni Mmoja, Mpweke, wa Kutegemewa, Ambaye Hakuzaa wala Kuzaliwa, wala Hana yeyote aliyefanana Naye.

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٤٢﴾ قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلُ ۗ كَانُوا

أَكْثَرُهُمْ مُشْرِكِينَ ﴿٤٣﴾

41. “Ufisadi umedhiri bara na baharini kwa iliyoyafanya mikono ya watu, ili Mwenyezi Mungu Awaoneshe baadhi ya waliyoyatenda. Huenda wakarejea kwa kutubu.”

42. “Sema: Safirini duniani muangalie ulikuwaje mwisho wa waliotangulia. Wengi wao walikuwa washirikina.”

Madhara ya Madhambi Humu Duniani

Ibn 'Abbas, 'Ikrimah, Adh-Dhahhak, As-Suddi na wengine رضي الله عنهم wamesema: Maana ya *Al-Barr* ni ardhi tupu au mwitu, na maana ya *Al-Bahr* ni miji mikubwa na midogo.¹ Katika riwaya ya Ibn 'Abbas na 'Ikrimah رضي الله عنهما, *Al-Bahr* ni miji mikubwa na midogo katika kingo za mito.² Wengine wamesema: "Maana ya *Al-Barr* ni bara kama inavyojulikana, na *Al-Bahari* ni bahari kama inavyojulikana." Zayd bin Rafi' amesema,

ظَهَرَ الْفَسَادُ

"Ufisadi umedhihiri..."

Maana yake: Kukatika kwa mvua katika nchi kavu na kufuatiwa na baa la njaa, na imezuiliwa kunyesha baharini na kuwaathiri vibaya wanyama wa humo." Haya yamenukuliwa na Abu Hatim رحمه الله تعالى, na amesema: "Muhammad bin 'Abdullah bin Yazid Al-Muqri alitusimulia kutoka kwa Sufyan kutoka kwa Humayd bin Al-Qays Al-A'raj kutoka kwa Mujahid:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ

"Ufisadi umedhihiri bara na baharini..."

Akasema: "Ufisadi katika nchi kavu ni kuuawa kwa mwanaadamu na ufisadi wa baharini ni uharamia." Kwa mujibu wa rai ya awali, maana ya Kauli ya Allah تعالى:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ

"Ufisadi umedhihiri bara na baharini kwa iliyoyafanya mikono ya watu..."

Maana yake: Kwa kuwa na upungufu wa mazao na matunda ni kwa sababu ya maasi. Abu Al-'Aliyah amesema: "Mwenye kumuasi Allah تعالى ardhini atakuwa amefanya ufisadi ardhini, kwa sababu kutengemaa ardhi na mbingu hutokana na utii." Kwa ajili hii, imekuja Hadithi,

¹ At-Tabari 20:108.

² At-Tabari 20:108.

«لَحْدٌ يُقَامُ فِي الْأَرْضِ أَحَبُّ إِلَيَّ أَهْلِهَا مِنْ أَنْ يُمَطَّرُوا أَرْبَعِينَ صَبَاحًا»

“Adhabu inayosimamishwa ardhini ni bora kwa wakazi wake, kuliko wanyeshewe na mvua kwa siku arubaini.”¹

Sababu ya haya ni kwamba adhabu za Allah تعالى zilizowekwa zikisimamiwa kwa watu itazuia watu au wengi wao kukiuka yaliyoharamishwa. Maasi yakiachwa, itakuwa sababu ya kufika baraka kutoka mbinguni na ardhini. Kwa ajili hii, Nabii ‘Isa bin Maryam عليه السلام atakapoteremka kutoka mbinguni katika zama za mwishoni, atahukumu kwa sharia hii iliyotwaharika katika wakati huo, kama vile kuua nguruwe, kuvunja msalaba na kuondoa *Jizyah*. Hata kubali isipokuwa Uislamu au upanga. Allah تعالى Akishamuangamiza Dajjal na wafuasi wake pia na Ya’juj na Ma’juj katika zama zake, ardhi itaambiwa: “Toa baraka zako.” Kundi la watu watakula komamanga moja na kupata kivuli chini ya ganda lake, na maziwa ya ngamia mmoja mwenye mimba yatawatosha kundi kubwa la watu. Hayo si jingine, isipokuwa ni kutokana na baraka za kuitumia Sharia aliyopewa Mtume Muhammad ﷺ. Basi, kila unaposimamishwa uadilifu, baraka na kheri huongezeka katika jamii.

Kwa ajili hii, ilithibiti katika *Sahih* kwamba:

«إِنَّ الْفَاجِرَ إِذَا مَاتَ تَسْتَرِيحُ مِنْهُ الْعِبَادُ وَالْبِلَادُ وَالشَّجَرُ وَالِدَوَابُّ»

“Mwovu akifariki, waja, ardhi, miti na wanyama hupumzika.”²

Imamu Ahmad bin Hambal رحمه الله تعالى amenukuu kwamba Abu Qahdham amesema: Kuna mtu katika zama za Ziyad, alikuta kifurushi ambacho kilikuwa na nafaka, yaani, ngano kubwa mithili ya kokwa za tende zikiwa zimeandikwa, ‘Hizi ziliota katika kipindi ambacho uadilifu ulikuwa ukifanyika.’³ Kauli ya Allah تعالى:

¹ An-Nasai 8:75.

² Ibn Abu Hatim alitaja bila isnadi ya wasimulizi chini ya maelezo ya Aya hii. Bila ya nyongeza ya maneno, “Kisha akasoma...” mpaka mwisho wake, ilinukuliwa na At-Tirmidhi, na 2013 na wengine, na inachukuliwa kwamba ni *Hadith Hasan*.

³ Al-Bukhari: 6512.

لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا

“...ili Mwenyezi Mungu Awaoneshe baadhi ya waliyoyatenda.”

Maana yake: Anawajaribu kwa upungufu wa mali, watu na matunda ukiwa mtihani kwao na malipo kutokana na vitendo vyao.

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٣٨﴾

“Huenda wakarejea kwa kutubu.”

Maana yake: Dhidi ya maasi. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَبَلَّوْنَهُمْ بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٣٩﴾

“Na Tukawajaribu kwa mema na mabaya ili wapate kurejea.”

(7:168) Kisha Allah تعالى Akasema:

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلُ

“Sema: Safirini duniani muangalie ulikuwaje mwisho wa waliotangulia.”

Maana yake: Kabla yenu.

كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُشْرِكِينَ ﴿٤٠﴾

“Wengi wao walikuwa washirikina.” Maana yake: Angalieni kilichowakumba kutokana na kuwakadhibisha Mitume na kuzikufuru neema.

فَأَقْرَعْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ الْقَیْمِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنْ اللَّهِ يَوْمَئِذٍ يَصَّدَّعُونَ ﴿٤١﴾

مَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۖ وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلَا نُفْسِيهِمْ يَمْهَدُونَ ﴿٤٢﴾ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا

وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْ فَضْلِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٤٣﴾

43. “Basi uelekeze uso wako kwenye Dini Iliyonyooka kabla ya kufika Siku hiyo isiyozuilika, inayotoka kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo watu watatengana.”

44. “Anayekufuru basi ukafiri wake utakuwa juu yake mwenyewe, na anayetenda mema, basi wanazitengezea nafsi zao.”

45. “Ili Awalipe walioamini na wakatenda mema kutokana na Fadhila yake. Hakika Yeye Hawapendi makafiri.”

Amri ya Kuifuata Njia Iliyonyooka Kabla ya Siku ya Kiyama

Allah تعالى Anawaamuru waja wake kufanya hima katika kuwa na msimamo wa kumcha Yeye na kufanya upesi katika mambo ya kheri:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ الْغَيْرِ مِنَ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ

“Basi uelekeze uso wako kwenye Dini Iliyonyooka kabla ya kufika Siku hiyo isiyozuilika, inayotoka kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Siku ya Kiyama, pindi Atakapotaka, na hakuna wa kuizuia,

يَوْمَئِذٍ يَصَّدُّعُونَ ﴿٤٥﴾

“Siku hiyo watu watatengana.”

Maana yake: Watafarakana. Kundi moja litakuwa Peponi na jingine Motoni. Kwa ajili hii. Allah تعالى Amesema:

مَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۗ وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلَا نَفْسَ لَهُ يَمْهَدُونَ ﴿٤٦﴾ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْ فَضْلِهِ ۗ

“Anayekufuru basi ukafiri wake utakuwa juu yake mwenyewe, na anayetenda mema, basi wanazitengezea nafsi zao. Ili Awalipe walioamini na wakatenda mema kutokana na Fadhila Yake.”

Maana yake: Atawalipa kwa malipo bora, jema moja kwa kumi mfano wake mpaka mara mia saba, mpaka kiasi Akitakacho Allah تعالى,

إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ ﴿٤٧﴾

“Hakika Yeye Hawapendi makafiri.”

Pamoja na haya, Yeye ni Muadilifu kwao, wala Hadhulumu.

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ يُرْسِلَ الرِّيحَ مُبَشِّرَاتٍ لِيُذِيقَكُمْ مِنْ رَحْمَتِهِ وَلِتَجْرِيَ الْفُلُكُ بِأَمْرِهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٤٦﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ رُسُلًا إِلَى قَوْمِهِمْ فَجَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَأَنْتَقَمْنَا مِنَ الَّذِينَ أَجْرَمُوا ۗ وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾ اللَّهُ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَيَبْسُطُهُ فِي السَّمَاءِ كَيْفَ يَشَاءُ وَيَجْعَلُهُ كِسْفًا فَتَرَى الْوَدْقَ يَخْرُجُ مِنْ خِلَابِهِ ۗ فَإِذَا أَصَابَ بِهِ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٨﴾ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلِ أَنْ يُنْزَلَ عَلَيْهِمْ مِنَ قَبْلِهِ لُمْتُسِينَ ﴿٤٩﴾ فَانظُرْ إِلَى آثَارِ رَحْمَتِ اللَّهِ كَيْفَ نُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا إِنَّ ذَلِكَ لَمُعْجِزٌ لِمَنِ الْمَوْتُ ۗ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٠﴾ وَإِنِ أَرْسَلْنَا رِيحًا فَرَأَوْهُ مُصْفَرًّا لَظَلُّوا مِنْ بَعْدِهِ يَكْفُرُونَ ﴿٥١﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ يُرْسِلَ الرِّيحَ مُبَشِّرَاتٍ لِيُذِيقَكُمْ مِنْ رَحْمَتِهِ وَلِتَجْرِيَ الْفُلُكُ بِأَمْرِهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٤٦﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ رُسُلًا إِلَى قَوْمِهِمْ فَجَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَأَنْتَقَمْنَا مِنَ الَّذِينَ أَجْرَمُوا ۗ وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾

46. "Na katika Ishara Zake ni Kuzituma pepo ziletazo bishara njema, na ili Kukuonjesheni baadhi ya Rehema Zake, na ili majahazi yende kwa Amri Yake; na mtafute kutokana na Fadhila Yake, na ili mumshukuru."

47. "Na hakika Tulikwisha watuma Mitume kwa kaumu zao, na wakawajia kwa hoja zilizo wazi. Tukawaadhibu wale waliofanya ukosefu. Na ilikuwa ni haki juu Yetu kuwanusuru Waumini."

Miongoni mwa Ishara za Allah تعالیٰ ni Pepo Zinzovuma

Allah تعالیٰ Anataja Neema Zake juu ya viumbe wake katika Kupeleka pepo zenye bishara njema kutokana na Rehema Zake, kwa kunyesha mvua baada yake. Allah تعالیٰ Amesema,

وَلِيُذِيقَكُمْ مِنْ رَحْمَتِهِ

"...na ili Kukuonjesheni baadhi ya Rehema Zake..."

Maana yake: Mvua Anayoteremsha na Kuwahuisha watu na ardhi,

وَلْتَجْرِيَ الْفُلُكُ بِأَمْرِهِ

“...na ili majahazi yende kwa Amri Yake...”

Ikimaanisha baharini, kwani husukumwa na upepo,

وَلْتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

“...na mtafute kutokana na Fadhila Yake...”

Maana yake: Katika biashara, maisha na kusafiri kutoka jimbo hadi jimbo na nchi hadi nchi,

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“...na ili mumshukuru.”

Maana yake: Mumshukuru Allah تعالیٰ kwa Neema Zake juu yenu za dhahiri na zilizofichama, ambazo hazihesabiki. Kisha amesema: Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ رُسُلًا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ فَجَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَأَتَقَمْنَا مِنَ الَّذِينَ أَجْرَمُوا

“Na hakika Tulikwishawatuma Mitume kwa kaumu zao, na wakawajia kwa hoja zilizo wazi. Tukawaadhibu wale waliofanya ukosefu.”

Haya ni maneno ya kuliwaza kutoka kwa Allah تعالیٰ kwenda kwa mja na Mtume Wake Muhammad ﷺ, kwa sababu yeye, hata kama watamkadhibisha wengi katika kaumu yake miongoni mwa watu, basi Mitume waliokuwa kabla yake walikadhibishwa licha ya kuwaletea watu wao dalili wazi wazi kuhusu utume wao. Lakini Allah تعالیٰ Aliwaadhibu watu waliowakadhibisha na Kuwakhalifu Mitume, na Kuwanusuru waumini.

وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ

“Na ilikuwa ni haki juu Yetu Kuwanusuru Waumini.”

Maana yake: Ni haki Aliyojiwajibisha katika Nafsi Yake Tukufu, kwa namna ya Kuwakirimu na Kuwatendea wema. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ:

كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

“...Mola wenu Mlezi Amezilazimisha Rehema...” (6:54)

Ibn Abi Hatim رضي الله عنه amepokea kutoka kwa Abi Dardaa رحمه الله تعالى kuwa: Amemsikia Mtume ﷺ anasema:

«مَا مِنْ أَمْرٍ مُّسْلِمٍ يَرُدُّ عَنْ عِزِّهِ إِلَّا كَانَ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يَرُدَّهُ عَنْهُ نَارَ جَهَنَّمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Hakuna Muislamu yeyote anayerudisha heshima ya ndugu yake Muislamu, isipokuwa itakuwa haki juu ya Mwenyezi mungu kumrudisha kutokana na moto wa Jahannam siku ya kياما”.

Kisha akasoma Aya hii:

وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾

“Na ilikuwa ni haki juu Yetu Kuwanusuru Waumini.”¹

اللَّهُ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَيَبْسُطُهُ فِي السَّمَاءِ كَيْفَ يَشَاءُ وَيَجْعَلُهُ كِسْفًا فَتَرَى
الْوَدَّاقَ يَخْرُجُ مِنْ خِلَالِهِ ۖ فَإِذَا أَصَابَ بِهِ مِنْ يَسَاءٍ مِنْ عِبَادِهِ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٨﴾
وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلِ أَنْ يُنْزَلَ عَلَيْهِمْ مِنَ قَبْلِهِ لَمُبْتَلِينَ ﴿٤٩﴾ فَأَنْظِرْ إِلَىٰ آثَرِ رَحْمَتِ اللَّهِ
كَيْفَ تَنْحِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ لَمُحِي الْمَوْتِ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٠﴾
وَلَئِنْ أَرْسَلْنَا رِيحًا فَرَأَوْهُ مُصْفَرًّا لَظَلُّوا مِنْ بَعْدِهِ يَكْفُرُونَ ﴿٥١﴾

48. “Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezituma pepo zikayatimua mawingu, kisha Akayatandaza mbinguni kama Apendavyo. Na Akayafanya mapande mapande, basi ukaiona mvua inatoka ndani yake. Anapowafikishia Awatakao katika waja wake, mara hao huwa na furaha.”

¹ Mfano wake imepokewa na Al-Bukhari nambari 6512

49. “Na ingawa kabla ya kuteremshiwa walikuwa wenye kukata tamaa.”

50. “Basi ziangalie athari za Rehema ya Mwenyezi Mungu, jinsi Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Basi hakika Huyu Ndiye bila ya shaka Mwenye Kuhuisha wafu. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu.”

51. “Na Tungeutuma upepo na wakauona umekuwa rangi ya manjano, juu ya hayo wangeendelea kukufuru.”

Kuhuishwa kwa Ardhi ni Dalili ya Kufufuliwa

Allah تعالى Anabainisha namna Anavyoyaumba mawingu ambayo maji huteremka kutoka humo. Allah تعالى Amesema:

اللَّهُ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا

“Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezituma pepo zikayatimua mawingu...”

Ima kutoka baharini, kama walivyotaja hivyo wengi, ama namna atakavyo Allah تعالى,

فَيَسُطُّهُ فِي السَّمَاءِ كَيْفَ يَشَاءُ

“...kisha Akayatandaza mbinguni kama Apendavyo.”

Maana yake: Anayatawanya, Kuyazidisha, Kuyakuza, na Kujalia wingi kutoka katika uchache. Yeye Huanzisha mawingu ambayo huonekana kama ngao, kisha anayajaza katika upeo wote wa macho. Wakati mwingine huja mawingu kutoka upande wa baharini. Mazito, yaliyojazwa (maji). Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ ۗ حَتَّىٰ إِذَا أَقَلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنَهُ

لِبَلَدٍ مَّيْمَنٍ

“Na Yeye Ndiye Anayepeleka pepo (za kuvuma) kuwa ni bishara kabla ya kufika Rehema Yake. Hata hizo pepo zinapobeba mawingu mazito Tunayachunga mpaka kwenye nchi iliyokufa.”

كَذَٰلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾

**“Basi hali kadhalika Tunavyowafufua wafu, ili mpate kukumbuka.”
(7:157)**

Kadhalika, Allah تعالى Amesema katika Aya hii:

اللَّهُ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَيَبْسُطُهُ فِي السَّمَاءِ كَيْفَ يَشَاءُ وَيَجْعَلُهُ كِسْفًا

“Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezituma pepo zikayatimua mawingu, kisha Akayatandaza mbinguni kama Apendavyo. Na Akayafanya mapande mapande...”

Mujahid, Abu ‘Amr bin Al-‘Ala’, Matar Al-Warraaq na Qatadah wamesema: “Yaani vipande.”¹ Wengine wamesema, maana yake ni kuwa, (mawingu), “Yamelundikana,” ni sawa sawa na alivyosema Adh-Dhahhak. Wengine wamesema: “Meusi, kutokana na maji mengi, Utayaona yakiwa na giza, mazito yakiwa karibu na ardhi.”

Kauli ya Allah تعالى,

فَتَرَى الْوَدْقَ يَخْرُجُ مِنْ خَلِيلِهِ

“...basi ukaiona mvua inatoka ndani yake.”

Maana yake: Ukaiona mvua, nayo ni matone yanatoka baina ya mawingu hayo,

فَإِذَا أَصَابَ بِهِ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٥٨﴾

“Anapowafikishia Awatakao katika waja wake, mara hao huwa na furaha.”

Maana yake: Kutokana na kuihitaji, wanafurahi kuteremka na kuwafika kwake huko kwao.

¹ At-Tabarani 20:114

وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ أَنْ يُنَزَّلَ عَلَيْهِمْ مِنْ قَبْلِهِ لَمُبْلِسِينَ ﴿٤٦﴾

“Na ingawa kabla ya kuteremshiwa walikuwa wenye kukata tamaa.”

Maana ya maneno haya ni kwamba, hiyo kaumu ambayo imepatwa na mvua hii, walikuwa na hamu ya kuteremshiwa mvua kwa muda mrefu kabla ya hapo. Ilipowajia, ikawa imewajia katika kipindi cha haja kubwa. Kwa hivyo hilo likawa jambo kubwa mno kwao. Maana yake ni kwamba, walikuwa na haja sana ya kuteremka kwake, na kabla yake, pia, haikuwateremkia kwa muda mrefu, kwa hivyo wakawa wanaisubiri katika wakati wake wa ada, ikachelewa, halafu ukapita muda mrefu. Wakaingojea, ikachelewa. Halafu, ikawajia kwa ghafla, baada ya kukosa matumaini nayo na kuikatia tamaa, baada ya ardhi yao kuwa kame na isiyoyana na kitu. Ikatingishwa kuwa hai, ikarutubika na ikaotesha kila jozi njema. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

فَانظُرْ إِلَىٰ آثَارِ رَحْمَةِ اللَّهِ

“Basi ziangalie athari za Rehema ya Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Mvua,

كَيْفَ تُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا

“...jinsi Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake.”

Kisha Akatanabahisha juu ya kuvihuisha viwiliwili baada ya kufa kwake, kutengana na kuchanikachanika.

إِنَّ ذَٰلِكَ لَمَعِيَ الْبُحْرَىٰ

“Basi hakika Huyu Ndiye bila ya shaka Mwenye Kuhuisha wafu.”

Maana yake: Kwa hakika, Aliyeyafanya haya, ni Mweza wa Kuwahuisha maiti, pasi na shaka yoyote.

وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٧﴾

“Na Yeye ni Muweza wa kila kitu.”

وَلَيْنَ أَرْسَلْنَا رِيحًا فَرَأَوْهُ مُصْفَرًّا لَّظَلُّوا مِنْ بَعْدِهِ يَكْفُرُونَ ﴿٤٦﴾

“Na Tungeutuma upepo na wakauona umekuwa rangi ya manjano, juu ya hayo wangeendelea kukufuru.”

وَلَيْنَ أَرْسَلْنَا رِيحًا

“Na Tungeutuma upepo...”

Mkavu kwenda katika mimea walioipanda, ikaota, ikakomaa na kusimama juu ya mashina yake, wakauona umegeuka rangi ya manjano, yaani umekuwa wa manjano na kuoza, basi wangukuwa baada yake, yaani baada ya hali hii, wanakufuru, maana yake, wakizipinga neema zilizotangulia kwao.

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالی:

أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَحْرُثُونَ ﴿٤٧﴾

“Je! Mnaona makulima mnayoyapanda?”

Mpaka katika Kauli Yake:

بَلْ نَحْنُ مُحْرَمُونَ ﴿٤٨﴾

“Bali sisi Tumenyimwa.” (56:63-67)

* * *

فَإِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتَىٰ وَلَا تُسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلَّوْا
 مُدْبِرِينَ ﴿٥٢﴾ وَمَا أَنْتَ بِهَادٍ الْعُمَىٰ عَنِ ضَلَالَتِهِمْ ۗ إِنَّ
 تُسْمِعُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٥٣﴾ * اللَّهُ
 الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً
 ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۗ وَهُوَ
 الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴿٥٤﴾ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُقْسِمُ الْمُجْرِمُونَ
 مَا لَنَا بِالنَّارِ غَيْرَ سَاعَةٍ ۗ كَذَلِكَ كَانُوا يُؤْفَكُونَ ﴿٥٥﴾ وَقَالَ
 الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَالْإِيمَانَ لَقَدْ لَبِئْتُمْ فِي كِتَابِ اللَّهِ إِلَى
 يَوْمِ الْبَعْثِ ۗ فَهَذَا يَوْمَ الْبَعْثِ وَلَكِنَّكُمْ كُنْتُمْ لَا
 تَعْلَمُونَ ﴿٥٦﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَا يُنْفَعُ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَعذِرَتُهُمْ
 وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٥٧﴾ وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا
 الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ۗ وَلَئِنْ جِئْتَهُمْ بِآيَةٍ لَيَقُولَنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا مُبْتَطَلُونَ ﴿٥٨﴾ كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ
 عَلَىٰ قُلُوبِ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٩﴾ فَأَصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ
 اللَّهِ حَقٌّ ۗ وَلَا يَسْتَخْفَنَّكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٠﴾

فَإِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتَىٰ وَلَا تُسْمِعُ
 الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِينَ ﴿٥٢﴾
 وَمَا أَنْتَ بِهَادٍ الْعُمَىٰ عَنِ ضَلَالَتِهِمْ ۗ
 إِنَّ تُسْمِعُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا فَهُمْ
 مُسْلِمُونَ ﴿٥٣﴾

52. “Kwani wewe hakika huwafanyi maiti wakasikia, wala viziwi wakasikia wito wakishageuka kukupa mgongo.”

53. “Wala wewe huwangoi vipofu na upotovu wao. Huwasikilizishi ila wanaoziamini Aya Zetu. Hao ndio Waislamu, walio-nyenyekea.”

Makafiri ni Sawa na Maiti, Viziwi na Vipofu

Allah تعالیٰ Anasema: kama ambavyo huwezi kuwasikilizisha maiti makaburini

mwao, au maneno yako kuwafikia viziwi, ambao hawasikii na ambao wanakugeuzia mgongo, hivyo huwezi kuwaongoza vipofu kwenye haki na kuwatoa upotevuni.

Jambo hilo liko kwa Allah تعالیٰ, kwani Yeye, kwa Kudura Yake Huwasikilizisha wafu sauti za walio hai Akitaka. Humhidi Amtakaye na Kumuacha apotee Amtakaye. Hayo si kwa mwingine yeyote isipokuwa Yeye tu. Kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Amesema:

﴿إِنْ تَسْمَعُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ بِقَائِلَتِنَا فَهُمْ مُسْلِمُونَ﴾

“Huwasilizishi ila wanaoziamini Aya Zetu. Hao ndio Waislamu, walionyenyeka.”

Maana yake: Wanyenyeketu, waitikivu, watiifu. Hao ndio wanaousikia ukweli na wanaufuata. Hii ni hali ya Waumini. Ule wa kwanza ni mfano wa makafiri.

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

﴿إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ﴾

“Hakika wanaokubali ni wale wanaosikia. Na ama wafu Mwenyezi Mungu Atawafufua, na kisha Kwake Yeye ndio watarejeshwa.”
(6:36)

Ummul-Muuminun, ‘Aishah رضي الله عنها aliitumia Aya hii,

﴿فَإِنَّكَ لَا تَسْمَعُ الْمَوْتَىٰ﴾

“Kwani wewe hakika huwafanyi maiti wakasikia...”

Kama ushahidi dhidi ya ‘Abdullah bin ‘Umar رضي الله عنهما, katika masimulizi yake kwamba Mtume ﷺ aliwahutubia maiti waliotupwa ndani ya kisima cha Badr, siku tatu baada ya vita vya Badr, kwa kuwakaripia, mpaka ‘Umar رضي الله عنه akamuambia Mtume ﷺ, “Jamaa unaowasemesha wamekuwa mizoga.” Mtume ﷺ akasema,

﴿وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ مَا أَنْتُمْ بِأَسْمَعَ لِمَا أَقُولُ مِنْهُمْ، وَلَكِنْ لَا يُجِيبُونَ﴾

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Nyinyi si wenye kuyasikia vyema ninayosema kuliko wao, lakini hawawezi kujibu.”¹

Maana yake ni kwamba, ‘Aishah رضي الله عنها alilitafsiri tukio hili kwamba Mtume ﷺ amesema: “Kwa hakika, wao sasa, wanajua kwamba nilichokuwa nikiwaambia kilikuwa cha kweli.”²

¹Fath Al-Bari 7:351.

²Fath Al-Bari 7:351.

Qatadah amesema: "Allah تعالى Aliwarudishia uhai kwa ajili yake ili waweze kuyasikia alichokisema kwa njia ya makemeo na kuwakebehi."¹

﴿ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴾

54. "Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni kutokana na udhaifu kisha Akajaalia nguvu baada ya unyonge, kisha Akajaalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba Atakavyo. Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye Uweza."

Kutaja Hali Mbalimbali za Mwanaadamu

Allah تعالى Anajulisha kupita kwa mwanadamu katika hatua za kuumbwa, moja hadi nyingine. Asili yake ni udongo, kisha manii, kisha donge la damu, kisha pande la nyama, halafu anakuwa mifupa. Baadaye, mifupa inavishwa nyama na kupuliziwa roho ndani yake, kisha anatoka tumboni mwa mama yake akiwa dhaifu, mwembamba. Halafu anakuwa kidogo kidogo, halafu anakuwa mtoto mdogo, anafikia kubaleghe na kuwa kijana mwenye nguvu baada ya udhaifu. Halafu anaingia katika kupungua na kuzeeka, anakuwa mzee na kuwa kikongwe. Huo ni udhaifu baada ya kuwa na nguvu. Kwa hivyo anadhoofika katika akili, nguvu za kutembea na za kimwili. Nywele zake zinageuka mvi na sifa zake za nje na za ndani zinabadilika, Na kwa kuzingatia hayo. Allah تعالى Amesema:

﴿ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۗ ﴾

"...kisha Akajaalia baada ya nguvu unyonge na ukongwe. Anaumba Atakavyo."

Yaani: Anafanya Ayatakayo na Anawafanyia waja wake kwa namna Aitakayo,

﴿ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴾

"Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye Uweza."

¹Fath Al-Bari 7:351.

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُقْسِرُ الْمُجْرِمُونَ مَا لَبِثُوا غَيْرَ سَاعَةٍ كَذَلِكَ كَانُوا يُؤْفَكُونَ ﴿٥٥﴾
 وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَالْإِيمَانَ لَقَدْ لَبِثْنَا فِي كِتَابِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْبَعْثِ فَهَذَا يَوْمُ
 الْبَعْثِ وَلَكِنَّكُمْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٥٦﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَا يُنْفَعُ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَعذِرَتُهُمْ
 وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٥٧﴾

55. "Na siku itaposimama Saa wakosefu wataapa kwamba hawakukaa duniani ila saa moja tu. Hivyo ndivyo walivyokuwa wakipotozwa."

56. "Na waliopewa ilimu na Imani watasema: Hakika nyinyi mlikwishakaa katika Hukumu ya Mwenyezi Mungu mpaka Siku ya kufufuliwa. Basi hii ndiyo Siku ya kufufuliwa! Lakini nyinyi mlikuwa hamuijui."

57. "Basi Siku hiyo hautawafaa waliodhulumu udhuru wao, wala haitotakiwa toba yao."

Ujahili wa Makafiri Duniani na Akhera

Allah تعالی Anaeleza kuhusu ujahili wa makafiri duniani na Akhera. Duniani wamefanya waliyoyafanya yanayohusiana na kuabudu masanamu. Akhera watakuwa na ujinga mkubwa pia.

Katika hayo ni kumuapia Allah تعالی kuwa hawakukaa duniani isipokuwa saa moja tu. Wanakusudia kwa hilo kusimamisha hoja kuwa hawakupewa muda wa kutosha ili wakose udhuru.

Allah تعالی Amesema:

كَذَلِكَ كَانُوا يُؤْفَكُونَ ﴿٥٥﴾ وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَالْإِيمَانَ لَقَدْ لَبِثْنَا فِي كِتَابِ اللَّهِ
 إِلَى يَوْمِ الْبَعْثِ

"Hivyo ndivyo walivyokuwa wakipotozwa. Na waliopewa ilimu na Imani watasema: Hakika nyinyi mlikwishakaa katika Hukumu ya Mwenyezi Mungu mpaka Siku ya kufufuliwa."

Waumini wenye elimu ya Akhera watawajibu, sawa na walivyosimamisha hoja kuhusu Allah تعالى duniani, watawaambia pindi watakapoapa kwa Allah تعالى kwamba hawakukaa zaidi ya saa,

لَقَدْ لَبِثْتُمْ فِي كِتَابِ اللَّهِ

“Hakika nyinyi mlikwisha kaa katika Hukumu ya Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Ndani ya Kitabu cha amali,

إِلَى يَوْمِ الْبَعْثِ

“...mpaka Siku ya kufufuliwa.”

Maana yake: Tangu siku mlipoumbwa, mpaka Siku ya kufufuliwa kwenu.

وَلِكِنَّكُمْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٥١﴾

“Lakini nyinyi mlikuwa hamjui.”

Allah تعالى Amesema:

فَيَوْمَئِذٍ

“Basi Siku hiyo...”

Maana yake: Siku ya Kiyama,

لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَعذِرَتُهُمْ

“...hautawafaa waliodhulumu udhuru wao...”

Maana yake: Kudai kwao udhuru kwa waliyofanya,

وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٥٢﴾

“...wala haitotakiwa toba yao.”

Inamaanisha, wala hawatarejea duniani. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَإِنْ يَسْتَعْتَبُوا فَمَا هُمْ مِنَ الْمُعْتَبِينَ ﴿٥٣﴾

“Na wakiomba radhi hawakubaliwi.” (41:24)

وَلَقَدْ صَرَّتْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ۖ وَلَئِنْ جِئْتَهُمْ بِآيَةٍ لَيَقُولَنَّ الَّذِينَ
كَفَرُوا إِنَّ أَنْتُمْ إِلَّا مُبْطِلُونَ ﴿٥٨﴾ كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِ الَّذِينَ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿٥٩﴾ فَأَصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ ۗ وَلَا يَسْتَخْفَنَّكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٠﴾

58. "Na hakika Tulikwishawapigia watu kila mfano katika hii Qur'ani. Na ukiwaletea Ishara yoyote hapana shaka waliokufuru watasema: Nyinyi si chochote ila ni waongo."

59. "Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyopiga muhuri kwenye nyoyo za wasiojua."

60. "Basi subiri. Hakika Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki. Wala wasikupaparisha hao wasiokuwa na yakini."

Kufundisha kwa kutumia Mifano Ndani ya Qur'an, na Makafiri Kukosa Mazingatio.

Allah تعالیٰ Anasema:

وَلَقَدْ صَرَّتْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ

"Na hakika Tulikwishawapigia watu kila mfano katika hii Qur'ani."

Maana yake: Tumewabainishia ukweli na Kuwafafanulia na Tukawapigia mifano ndani yake ili waweze kupambanukiwa na ukweli na kuufuata,

وَلَئِنْ جِئْتَهُمْ بِآيَةٍ لَيَقُولَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ أَنْتُمْ إِلَّا مُبْطِلُونَ ﴿٥٨﴾

"Na ukiwaletea Ishara yoyote hapana shaka waliokufuru watasema: Nyinyi si chochote ila ni waongo."

Lau wangeliona ishara yoyote, iwe kwa mapendekezo yao au vinginevyo, hawaiamini, bali wanaitakidi kwamba ni uchawi na batili. Sawa na walivyosema katika kupasuka mwezi na mfano wake. Ni sawa na Alivyosema Allah تعالیٰ katika Aya nyingine,

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ
يَرَوْا آعَذَابَ الْأَلِيمِ ﴿٦٧﴾

“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwishathibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyochungu.” (10:96-97)

Kwa ajili hiyo, Amesema katika Aya hii:

كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾ فَأَصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ ۗ

“Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga muhuri kwenye nyoyo za wasiojua. Basi subiri. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki.”

Yaani, Uwe na subira juu ya kukhalifu kwao na ukaidi wao, kwani Allah تعالى Atayatimiza Aliyokuahidi kwa Kukupa ushindi juu yao na Akaujaalia mwisho mwema kuwa ni wako na kwa waliokufuata. Hayo ni kwa duniani na Akhera.

وَلَا يَسْتَخْفِنَكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٩﴾

“Wala wasikupaparishe hao wasiokuwa na yakini.”

Maana yake: Bali kuwa imara katika Aliyokutuma Allah تعالى, kwani huo ni ukweli, hauna shaka ndani yake. Usiupe mgongo, wala hakuna hidaya nyingine ya kuifuata isipokuwa, ukweli wote umekusanywa ndani yake.

Fadhila za Usomaji Sura Hii Wakati wa Swala ya Alfajiri

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى amemnukuu Sahaba wa Mtume ﷺ kwamba Mtume ﷺ aliswalisha Swala ya Asubuhi. Akasoma *Suratu Ar- Rum*, akatingwa. Akasema:

«إِنَّهُ يَلْبِسُ عَلَيْنَا الْقُرْآنَ، فَإِنَّ أَقْوَامًا مِنْكُمْ يُصَلُّونَ مَعَنَا لَا يُحْسِنُونَ الرُّضْوَةَ، فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمْ الصَّلَاةَ مَعَنَا فَلْيُحْسِنِ الرُّضْوَةَ»

“Tumetatizika na usomaji wetu wa Qur’an, kwani, kuna baadhi ya

watu miongoni mwenu ambao wanasali pamoja nasi, hawaufanyi vizuri udhu wao. Basi yeyote katika nyinyi mwenye kushiriki Swala pamoja nasi, aufanye vyema udhu wake.”¹

Ina isnadi na matini nzuri. Ndani yake kuna siri ya ajabu na khabari ngeni. Nayo ni kwamba, yeye Mtume ﷺ aliathirika na upungufu wa udhu wa baadhi ya aliowaongoza katika Swala. Hilo linajulisha kwamba Swala ya maamuma inafungamana na ya Imamu.

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Ar-Rum*. Himdi na Shukrani ni za Allah تعالیٰ.

* * *

¹ Ahmad 3:471.

Tafsiri ya Suratu Luqman

Sura ya 31

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ لُقْمَانَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْم ﴿١﴾ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ ﴿٢﴾ هُدًى وَرَحْمَةً
لِّلْمُحْسِنِينَ ﴿٣﴾ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ
وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾ أُولَئِكَ عَلَى هُدًى مِّن
رَّبِّهِمْ ۗ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَن
يَشْتَرِي لَهْوَ الْحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ
وَيَتَّخِذَهَا هُزُوًا ۚ أُولَئِكَ هُمُ عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٦﴾ وَإِذَا تُتْلَىٰ
عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا وَلَّىٰ مُسْتَكْبِرًا ۚ كَانَ لَمَّا يَسْمَعُهَا كَأَن فِي أُذُنَيْهِ
وَقْرًا ۖ فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا
وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ جَنَّاتُ النَّعِيمِ ﴿٨﴾ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ
وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا ۖ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٩﴾

الْم ﴿١﴾ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ

﴿٢﴾ هُدًى وَرَحْمَةً لِّلْمُحْسِنِينَ

﴿٣﴾ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ

الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤﴾

أُولَئِكَ عَلَى هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۗ

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥﴾

1. "Alif Lam Mim (A.L.M.)"

2. "Hizi ni Aya za Kitabu chenye hikima."

3. "Kuwa ni Uwongofu na Rehema kwa wafanyao wema."

4. "Wanaoshika Swala, na wanatoa Zaka, nao wana yakini na Akhera."

5. "Hao ndio walio na uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, hao ndio wenye kufanikiwa."

Tulikwishatangeliza maneno katika *Suratu Al-Baqarah*, yanayofungamana na mwanzoni mwa Sura hii, nayo ni kwamba, Allah تعالی Ameijalia Qur'an hii kuwa ni uongofu, ponyo na rehema kwa watu wema, hawa ni wale ambao wametenda amali njema, katika kuifuata Shariah. Wakasimamisha Swala za faradhi kwa mipaka yake, nyakati zake na sunna zinazofuatana nazo miongoni mwa Sunna za (*Rawaatib*) na nyinginezo. Wakatoa Zaka ya faradhi kwa wenye kustahiki; wakaunga ndugu na jamaa zao; wakawa na yakini juu ya malipo katika Akhera; wanatafuta thawabu za Allah تعالی, hawafanyi ria, wala kutaka ujira toka kwa watu wala shukurani. Kwa hiyo Mwenye kuyafanya hayo kwa namna inavyostahiki, bila shaka atakuwa miongoni mwa wale ambao Allah تعالی Amesema Kuwahusu,

أُولَئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۗ

“Hao ndio walio na uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi...”

Maana yake: Wako katika uoni, ubainifu, utaratibu ulio dhahiri,

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٦١﴾

“...na hao ndio wenye kufanikiwa.”

Maana yake: Duniani na Akhera.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْتَرِي لَهْوَ الْحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّخِذَهَا هُزُوًا ۗ
 وَأُولَئِكَ هُمُ عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٦٢﴾ وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ آيَاتُنَا وَوَلَّىٰ مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا
 كَأَنَّ فِي أُذُنَيْهِ وَقْرًا فَبَسَّرَهُ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٦٣﴾

6. “Na miongoni mwa watu wapo wanaonunua maneno ya upuuzi, ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu pasipo kujua, na wanaichukulia ni maskhara. Hao watapata adhabu ya kuwafedhehesha.”

7. “Na (mtu kama huyo) anaposomewa Aya Zetu huzipa mgongo kwa kujivuna, kama kwamba hakuzisikia, kama kwamba masikioni mwake mna uziwi. Basi mbashirie kuwa atapata adhabu chungu.”

Waovu hujishughulisha na Mazungumzo ya Kipuuzi na Kuichukia Qur'an

Baada ya Kutaja Hali za watu Wema, ambao ndio wanaongozwa na Kitabu cha Allah تعالى na wananufaika kwa kukisikiliza.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

اللَّهُ نَزَلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُتَشَابِهًا مَثَانِيَ تَقْشَعِرُّ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ

“Mwenyezi Mungu Ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.” (39:23)

Aliunganisha kutaja hali za waovu ambao wameyapa mgongo manufaa ya kusikiliza maneno ya Allah تعالى, wakaelekea katika kusikiliza zumari na nyimbo zenye kuambatana na vyombo vya muziki. Ni kama alivyosema Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْتَرِي لَهْوَ الْحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

“Na miongoni mwa watu wapo wanaonunua maneno ya upuuzi, ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu...”

Alisema, “Hayo – Wallah – ni nyimbo.”¹ Qatadah alisema, Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْتَرِي لَهْوَ الْحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ

“Na miongoni mwa watu wapo wanaonunua maneno ya upuuzi, ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu pasipo kujua...”

“Wallah! Anaweza asitumie mali yake katika hayo, lakini, kule kununua kwake kuna maana ya kwamba anapenda na inamtosha mtu kuwa ni mpotevu

¹ At-Tabari 20:127.

kuchagua maneno ya batili yenye madhara kwake akawacha ya haki na yenye manufaa.”¹ Ilisemwa kwamba makusudio ya Kauli ya Allah تعالى:

يَشْتَرِي لَهْوَ الْحَدِيثِ

“...wanaonunua maneno ya upuuzi...”

Ni ununuzi wa watumishi wa kike wenye kuimba. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa maana yake ni kila maneno yanayozuia ujumbe wa Allah تعالى na kuifuata njia Yake.² Kauli ya Allah تعالى:

لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

“...ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu...”

Yaani, kwa hakika, huyafanya haya kwa ajili ya kuupinga Uislamu na watu wake. Kauli ya Allah تعالى:

وَيَتَّخِذَهَا هُزُوًا

“...wanaichukulia ni maskhara.”

Mujahid alisema: “Maana yake ni kuidhihaki njia ya Allah تعالى na kuifanyia stihizai.”³ Kauli ya Allah تعالى:

أُولَئِكَ هُمُ عَذَابٌ مُّهِينٌ

“Hao watapata adhabu ya kuwafedhehesha.”

Yaani, kama ambavyo wamezipuuzwa Aya za Allah تعالى na njia Yake, basi watapuuzwa katika Siku ya Kiyama kwa kutiwa katika adhabu ya kudumu na kuendelea. Kisha, Allah تعالى Alisema:

وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِ آيَاتُنَا وَوَلَّى مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا كَأَنَّ فِي أُذُنَيْهِ وَقْرًا

“Na (mtu kama huyo) anaposomewa Aya Zetu huzipa mgongo kwa kujivuna, kama kwamba hakuzisikia, kama kwamba masikioni mwake mna uziwi.”

¹ At-Tabari 20:127.

² At-Tabari 20:130.

³ At-Tabari 20:131.

Yaani, huyu mpenda anasa, mchezo na muziki, pindi anaposomewa Aya za Qur'an hugeuka, akazikataa, kuzipa mgongo, na kujitia uziwi ilhali hana huo uziwi, kama vile hakuzisikia, kwa sababu anajisikia udhia kuzisikiliza kwani hanufaiki nazo, wala hana haja nazo,

فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٧﴾

“Basi mbashirie kuwa atapata adhabu chungu.”

Maana yake: katika Siku ya Kiyama, Allah تعالى Atamtia machungu kama vile alivyokuwa akijisikia uchungu kukisikiliza Kitabu cha Allah تعالى na Aya Zake.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ جَنَّاتُ النَّعِيمِ ﴿٨﴾ خَالِدِينَ فِيهَا وَعَدَّ اللَّهُ
حَقًّا وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٩﴾

8. “Hakika walioamini na wakatenda mema watakuwa nazo Bustani za neema.”

9. “Watadumu humo - ni ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kweli. Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Kutajwa Makazi Mema kwa Waumini

Hapa yanatajwa makazi ya watu wema, watakaokuwa wenye furaha huko Akhera, wale waliomwamini Allah تعالى na wakawasadiki Mitume, wakatenda amali njema zenye kufuata Shariah ya Allah تعالى,

هُمْ جَنَّاتُ النَّعِيمِ ﴿٨﴾

“...watakuwa nazo Bustani za neema.”

Yaani, wataneemeka humo kwa namna mbalimbali kwa mambo matamu na ya furaha, kama vyakula, vinywaji, mavazi, makazi, vipando, wanawake, mandhari, sauti, ambavyo havijawahi kupita katika akili ya mwanaadamu yeyote. Watakaa humo daima pasi na kuondoka wala kuwa na haja ya kubadilishwa. Kauli ya Allah تعالى,

وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا

“...ni ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kweli.”

Yaani, haya yatatukia tu, hayana shaka, kwa sababu ni katika ahadi ya Allah تعالیٰ, Yeye Hakhalifu miadi, kwa sababu Yeye ni Mkarimu sana, Mneemeshaji, Afanyaye Ayatakayo, Muweza wa kila kitu.

وَهُوَ الْعَزِيزُ

“Na Yeye Ndiye Mwenye Nguvu...”

Ambaye Amekishinda kila kitu na vitu vyote vinamnyenyekea Yeye,

الْحَكِيمُ

“...Mwenye Hikima.”

Katika Kauli na Matendo Yake, Ambaye Ameijaalia Qur’an kuwa mwongozo kwa waumini,

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءً وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى

“Sema: Qur’ani hii ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni.” (41:44)

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا

“Na Tunateremsha katika Qur’ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhalimu ila khasara.” (17:82)

* * *

خَلَقَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۗ وَأَلْقَىٰ فِي الْأَرْضِ رَوْسِي
 أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ ۗ وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ
 مَاءً فَأَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿١٠﴾ هَذَا خَلْقُ اللَّهِ
 فَأَرُونِي مَاذَا خَلَقَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ ۗ بَلِ الظَّالِمُونَ فِي
 ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿١١﴾ وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنْ اشْكُرْ لِلَّهِ
 ۗ وَمَنْ يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ
 غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿١٢﴾ وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لِابْنِهِ وَهُوَ يَعِظُهُ
 يَا بُنَيَّ لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ ۗ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٣﴾
 وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهْتًا عَلَىٰ وَهْنٍ
 وَفَصَّلَتْهُ فِي عَامَيْنِ أَنْ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَىٰ الْمَصِيرِ
 ﴿١٤﴾ وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ
 بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۗ وَصَاحِبَتُهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۗ
 وَاتَّبَعَ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ فَأُنْتَبِهُكُمْ
 بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾ يَا بُنَيَّ إِنِّي أُنْفِقُ الْوَيْسَاقَ حَبِيبًا
 خَزَائِلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمَوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ
 يَأْتِيهَا اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٦﴾ يَا بُنَيَّ أَقِمِ الصَّلَاةَ
 وَأْمُرْ بِالْمَعْرُوفِ وَانْهَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا أَصَابَكَ ۗ
 إِنَّ ذَلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٧﴾ وَلَا تَصْعَقْ خَدْلَكَ لِلنَّاسِ
 وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ
 فَخُورٍ ﴿١٨﴾ وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَأَعْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ ۗ
 إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿١٩﴾

خَلَقَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۗ
 وَأَلْقَىٰ فِي الْأَرْضِ رَوْسِي أَنْ تَمِيدَ
 بِكُمْ وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ ۗ وَأَنْزَلْنَا
 مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ
 كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿١٠﴾ هَذَا خَلْقُ
 اللَّهِ فَأَرُونِي مَاذَا خَلَقَ الَّذِينَ مِنْ
 دُونِهِ ۗ بَلِ الظَّالِمُونَ فِي ضَلَالٍ
 مُبِينٍ ﴿١١﴾

10. "Ameziumba mbingu bila ya nguzo mnazoziona; na Ameweka katika ardhi milima ili ardhi isikuyu-mbisheni; na Ametawanya humo kila namna ya viumbe; na Tumetemsha maji kutoka mbinguni, na Tukaotesha katika ardhi mimea mizuri ya kila namna."

11. "Huu ni Umbaji wa Mwenyezi Mungu. Basi Nionesheni wameumba nini hao wasio kuwa Yeye! Lakini madhalimu wamo katika upotovu uliyo dhahiri."

Ushahidi wa Upekee wa Allah تعالی (Tawhidi)

Allah تعالی Anabainisha Kudura Yake kubwa juu ya Kuumba mbingu na ardhi, na yaliyomo katika hivyo viwili na baina Yake.

خَلَقَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا

“Ameziumba mbingu bila ya nguzo mnazo ziona...”

Al-Hasan na Qatadah walisema: “Haina nguzo zenye kuonekana na zisizoonekana.”¹

وَأَلْقَى فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ

“...na Ameweka katika ardhi milima...”

Yaani, milima inayoiimarisha ardhi na kukandamiza uzito wake ili isitikisike pamoja na maji yake. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema,

أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ

“...ili ardhi isikuyumbisheni...”

ili isiwe inapepea pamoja nanyi,

وَبَنَى فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ

“...na Ametawanya humo kila namna ya viumbe...”

Yaani, Aliweka humo kila namna ya hayawani kwa namna ambayo hakuna ajuaye idadi ya jinsi na rangi zao isipokuwa Aliyewaumba.

Allah تعالی Aliposema kwamba Yeye ni Muumbaji, pia Alijulisha kwamba ni Mwenye Kuruzuku. Kwa Kauli Yake,

وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿٣١﴾

“...na Tumeteremsha maji kutoka mbinguni, na Tukaotesha katika ardhi mimea mizuri ya kila namna.”

¹ At-Tabari 20:132.

Yaani, kwa kila jozi ya mimea mizuri, yenye mandhari nzuri. Ash- Sha'abi amesema, "Watu nao pia, ni mazao ya ardhi, basi atakayeingia Janna ni mwema, na mwenye kuingia Jahanamu ni muovu."

هَذَا خَلْقُ اللَّهِ

"Huu ni Uumbaji wa Mwenyezi Mungu."

Haya Aliyoyataja Allah تعالى Kuanzia Kuumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao yote haya yamepatikana kwa kitendo cha Allah تعالى na Kuumba Kwake na Mipangilio Yake katika hayo. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema,

فَأَرْوِنَ مَاذَا خَلَقَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ

"Basi nionesheni wameumba nini hao wasiokuwa Yeye!"

Kwa maana, masanamu na washindani mnaowaabudu,

بَلِ الظَّالِمُونَ

"Lakini madhalimu..."

Kwa maana, wanaomshirikisha Allah تعالى ambao wanamwabudu pamoja na mwingine,

فِي ضَلَالٍ

"...wamo katika upotovu..."

Yaani, ujahili na upofu.

مُبِينٍ

"...uliyodhaahiri." Yaani, dhahiri shahiri, hauna kificho.

وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنْ اشْكُرْ لِلَّهِ وَمَنْ يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ وَمَنْ كَفَرَ

فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ

12. "Na Tulimpa Luqman hikima, Tukamwambia: Mshukuru Mwenyezi Mungu. Na mwenye kushukuru basi hakika anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake. Na aliyekufuru, basi Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Msifiwa."

Kutajwa kwa Luqman

Salaf walikhitilafiana kuhusu Luqman katika kauli mbili: Je alikuwa Nabii, au mja mwema bila kuwa Nabii? wengi walifuata kauli ya pili. Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى amesema kutoka kwa Ash-Sh'ath na 'Ikrimah kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema: *"Luqman alikuwa mtumwa wa kihabeshi (Ethiopia) ambaye alikuwa seremala."*¹

'Abdullah bin Az-Zubayr رضي الله عنه amesema: "Nilimwambia Jabir bin 'Abdullah, 'Mmewahi kusikia jambo gani kumhusu Luqman?" Akasema: 'Alikuwa mfupi, pua fupi na alitokea Nawbah (Nubia).'"² Yahya bin Sa'id Al-Answari amesema kuwa Sa'id bin Al-Musayyab amesema: *"Luqman alitokea Misr ya upande wa Sudan (Kusini mwa Misr), na alikuwa na midomo minene, Allah Alimpa hikima, lakini aliuzuia Utume dhidi yake."*³ Al-Awza'i رحمه الله تعالى amesema: 'Abdur-Rahman bin Harmalah alinisimulia, amesema: Mtu mmoja mweusi alikuja kwa Sa'd bin Al-Musayyab kumuuliza. Sa'id bin Al-Musayyab akamwambia: "Usihuzunike kwa ajili ya kuwa kwako mweusi. Miongoni mwa watu bora walikuwepo watatu ambao wallikuwa weusi, Bilal, Mihja', mtumwa aliyeachwa huru na 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه na Luqman mwenye hikima ambaye alikuwa Mnubi mweusi na midomo minene."⁴

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Khalid Ar-Rib'i kuwa amesema: "Luqman alikuwa mtumwa aliyekuwa seremala, bwana wake akamwambia, 'Mchinje kondoo huyu.' Akamchinja. Akasema, 'Lete vipande viwili vilivyo vizuri zaidi vitokanavyo naye.' Akatoa ulimi na moyo. Halafu akakaa kwa kipindi alichotaka Allah تعالى, kisha akamwambia tena, 'Mchinje kondoo huyu.' Akamchinja. Akasema, 'Lete vipande viwili vilivyo vibaya zaidi vitokanavyo naye.' Akatoa ulimi na moyo. Akasema bwana wake, 'Nimekuamuru utoe vipande viwili vilivyo vizuri zaidi, ukaleta hivyo. Nikakuamuru tena ulete vipande viwili vilivyo vibaya zaidi, umeleta vivyo hivyo?' Luqman akasema: 'Hakuna kilicho kizuri zaidi ya hivyo iwapo vitakuwa vyema na hakuna kibaya kama hivi ikiwa vitakuwa vibaya.'"⁵

¹ At-Tabari 20:135: Isnadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abu Hatim 9:3097 na Ad-Dur Al-Manthur 5:310.

³ At-Tabari 20:135.

⁴ At-Tabari 20:135.

⁵ At-Tabari 20:135.

Shu'bah amesema kutoka kwa Al-Hakim kutoka kwa Mujahid: "Luqman alikuwa mja mwema na hakuwa Mtume ﷺ."¹ Kauli ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ

"Na Tulimpa Luqman hikima..."

Yaani, fahamu, elimu na uzingativu,

أَنْ أَشْكُرَ لِلَّهِ

"...Tukamwambia: Mshukuru Mwenyezi Mungu."

Yaani, Tulimwamuru amshukuru Allah تعالى kwa Fadhila alizompatia yeye peke yake pasi na mwingine katika watu wa jinsi yake na wa zama zake.

Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ

"Na mwenye kushukuru basi hakika anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake."

Maana yake, manufaa na thawabu za hayo yanarejea kwa wenye kushukuru. Ni kwa ajili ya Kauli Yake,

وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِأَنْفُسِهِمْ يَمْهَدُونَ ﴿٤٤﴾

"...na anayetenda mema, basi wanazitengezea nafsi zao." (30:44)

وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٤٥﴾

"Na aliyekufuru, basi Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Msifiwa."

Yaani, si Mwenye haja kwa waja, Hadhuriki hata kama watakufuru wakazi wote wa ardhini, kwani Yeye si Mwenye haja kwa asiyekuwa Yeye. Hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, wala hatuabudu isipokuwa Yeye.

¹ At-Tabari 20:134.

وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لِابْنِهِ وَهُوَ يَعِظُهُ يَا بُنَيَّ لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٠﴾
 وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهَتَا عَلَىٰ وَهَنٍ وَفَصَّلَهُ فِي عَامَيْنِ أَنْ اشْكُرْ لِي
 وَلِوَالِدَيْكَ إِلَىٰ الْمَصِيرِ ﴿١١﴾ وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ
 فَلَا تُطِعْهُمَا ۗ وَصَاحِبِهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۗ وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ
 فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٢﴾

13. "Na Luqman alipomwambia mwanawe kwa kumpa mawaidha: Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu. Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa."

14. "Na Tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (Tumemuusia): Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni Kwangu Mimi ndiyo marudio."

15. "Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwatii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anayeelekea kwangu. Kisha marejeo yenu ni Kwangu Mimi, na Mimi Nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda."

Wasia wa Luqman kwa Mwanaye.

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu wasia wa Luqman kwa mwanaye. Yeye ni Luqman bin 'Anqaa bin Sadun na jina la mwanaye ni Thaarani. Kwa mujibu wa kauli ya As-Suhayli. Allah تعالیٰ Alimtaja vyema sana, na Alimpa hekima. Yeye alimuusia mwanaye ambaye, anamuhurumia na kumpenda zaidi ya watu wote, basi ana haki ya kupatiwa elimu bora zaidi.

Kwa ajili hii, kwanza alimuusia amwabudu Allah تعالیٰ, Mpweke, Asiye na mshirika. Kisha akamtahadharisha:

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٠﴾

"Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa."

Yaani, hiyo ni dhuluma kubwa zaidi. Bukhari¹ alimnukuu 'Abdullah kuwa amesema: Pindi ilipotemka Aya:

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ

“Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma...” (6:82)

Hilo lilikuwa zito kwa Masahaba wa Mtume ﷺ, wakasema: “Nani kati yetu hachanganyi imani yake na dhulma?” Mtume ﷺ akasema:

«إِنَّهُ لَيْسَ بِذَلِكَ، أَلَا تَسْمَعُ إِلَى قَوْلِ لُقْمَانَ: ﴿يَبْنَى لَا تُشْرِكْ بِاللهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ﴾»

“Hiyo si maana yake. Je, hukuisikia kauli ya Luqman: ‘Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu. Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa.’”

Na ilinukuliwa na Muslim.

Halafu akaunganisha na usia wake kwake kwamba amwabudu Allah تعالى Peke Yake na kuwafanyia wema wazazi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

﴿وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Mola wako Mlezi Ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema.” (17:23)

Mara nyingi Allah تعالى huyataja hayo kwa pamoja ndani ya Qur’an, katika Aya hii, Allah تعالى Anasema:

﴿وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهْتًا عَلَىٰ وَهْنٍ ﴿٥٠﴾

“Na Tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu.”

¹ Fat’h Al-Bari 8:372.

Mujahid amesema: “Ni taabu ya kulea mtoto.”¹ Qatadah alizema: “Ni uchovu juu ya uchovu.”² ‘Ata Al-Khuraasani amesema: “Udhaifu juu ya udhaifu.”

Kauli ya Allah تعالى:

وَفَصَّلُهُ فِي عَامَيْنِ

“...na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili.”

Maana yake: kulelewa na kunyonyeshwa kwake, baada ya kuzaliwa ni miaka miwili.

✽ وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُنْمِ الرِّضَاعَةَ

“Akinamama watawanyonyesha watoto wao kwa muda wa miaka miwili kwa wale wanaotaka kukamilisha muda wa kunyonyesha.” (2:233)

Kwa ajili hii, Ibn ‘Abbas na maimamu wengine رضي الله عنهم walitambua kwamba kipindi cha ujauzito, kwa ufupi zaidi ni miezi sita. Ni kwa sababu Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

وَحَمَلُهُ وَفَصَّلُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا

“Na kuchukua mimba kwake hata kumwachisha ziwa ni miezi thalathini.” (46:15)

Hapa anachokitaja Allah تعالى ni malezi ya mama wa mtoto, taabu na mashaka yake katika kukesha usiku na mchana, ili mtoto aikumbuke ihsani yake iliyotangulia kwa ajili yake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾

“Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyonilea utotoni.” (17:24).

Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema,

¹At-Tabari 20:137.

²At-Tabari 20:137.

أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلَوْلَا دَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ﴿١٠﴾

“(Tumemuusia): Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni Kwangu Mimi ndiyo marudio.”

Yaani, Mimi Nitakulipa malipo mengi kwa ajili ya hayo.

وَإِنْ جَاهِدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا

“Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwatii.”

Yaani, wakikuhimiza sana kwamba uwafuate katika dini yao, usiwakubalie hilo, wala hilo halikuzuii kushirikiana nao na kuishi nao duniani katika jambo jema, yaani kuwafanyia ihsani,

وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَيَّ

“...nawe ishike njia ya anayeelekea Kwangu.” Yaani, Waumini

ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١١﴾

“Kisha marejeo yenu ni Kwangu Mimi, na Mimi Nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.”

At-Tabarani alinukuu kutoka katika *Kitab Al-'Ish'rah* kwamba Sa'd bin Malik amesema: Aya hii iliteremshwa kunihusu mimi:

وَإِنْ جَاهِدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا

“Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwatii.”

Amesema: “Mimi nilikuwa ni mtu mwenye kumfanyia ihsani mama yangu. Niliposilimu, aliniambia: ‘Ewe Sa'd! Ni jambo gani hili ulilolizusha?’ Utaiacha dini hii uliyo nayo sasa, la sivyo sitakula wala kunywa mpaka nife, na kwa hivyo utafedheheka kwa sababu yangu. Watu nao watasema, ‘ewe mtu aliyemuua mama yake.’ Nikasema: ‘Usifanye hivyo ewe mama yangu! Kwani

mimi sitaiacha dini yangu hii, kwa ajili ya kitu kingine chochote.' Akapitisha mchana na usiku bila ya kula. Kukapambazuka huku akiwa na njaa kali. Akapitisha siku nyingine na usiku wake bila ya kula. Kulipokucha alikuwa na njaa kali zaidi. Akapitisha mchana na usiku mwingine bila kula, huku njaa ikiwa ni zaidi. Nilipoona hivyo, nikasema: "Wallah! Unajua kwamba, lau kama ungelikuwa una nafsi mia moja, kisha ikatoka moja baada ya nyingine, mimi sitaiacha dini yangu hii kwa ajili ya chochote. Ukitaka, kula na kama ukitaka usile.' Basi akala."¹

يَبْنِيْ لَهُمْ اِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبِيْبٍ مِّنْ حَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِيْ صَخْرَةٍ اَوْ فِي السَّمٰوٰتِ اَوْ فِي الْاَرْضِ
يٰٓاَيُّهَا اللّٰهُ اِنَّ اللّٰهَ لَطِيْفٌ حَبِيْرٌ ﴿١٠﴾ يَبْنِيْ اَقِمِ الصَّلٰوةَ وَاْمُرْ بِالْمَعْرُوْفِ وَاَنْهَ عَنِ
الْمُنْكَرِ وَاَصْبِرْ عَلٰى مَا اَصَابَكَ اِنَّ ذٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْاُمُوْرِ ﴿١١﴾ وَلَا تُصَوِّرْ خَدٰكَ
لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْاَرْضِ مَرْحًا اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُوْرٍ ﴿١٢﴾ وَاَقْصِدْ فِي
مَشِيْكَ وَاغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ اِنَّ اَنْكَرَ الْاَصْوٰتِ لَصَوْتُ الْحَمِيْرِ ﴿١٣﴾

16. "Ewe mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu Atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyofichika, Mwenye khabari za yote."

17. "Ewe mwanangu! Shika Swala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayokupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa."

18. "Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila anayejivuna na kujifakhirisha."

19. "Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda."

¹ Ilitajwa na Ibn Al-Athir katika *Usd Al-Ghabah* 2:216.

Huu ni wasia wa manufaa ambao Allah تعالى Ameuelezea kuhusu Luqman, mwenye hikima, ili watu waufuate na kuuiga. Amesema:

يَبُيِّئُ إِنَّهَا إِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ حَرْدَلٍ

“Ewe mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali...”

Yaani, lau kama dhulma au dhambi ina uzito wa mbegu ya khardali. Baadhi ya Maulamaa wamesema kwamba katika Kauli Yake, *Innaha* katika Aya inahusu jambo na kisa chenyewe. Pia wamesema kuwa maana yake ni juu ya uzito wa khardali. Mtazamo wa wanazuoni wa awali ni aula zaidi. Kauli ya Allah تعالى:

يَأْتِ بِهَا اللَّهُ

“...basi Mwenyezi Mungu Atakileta.”

Yaani, Allah تعالى Atakihudhurisha katika Siku ya Kiyama, pindi Atakapokiweka katika uzani wa mambo ya uadilifu. Ikiwa ni chema basi ni kheri na kama ni kiovu, basi ni shari.

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا

“Nasi Tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote.” (21:47)

Na Allah تعالى Amesema:

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧٧﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٧٨﴾

“Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!” (99:7-8)

Lau kama chembe hiyo imehifadhiwa na kufichwa ndani ya jabali gumu au inakwenda katika pande mbalimbali za mbinguni na ardhini, basi, Allah تعالى Ataitenda, kwani hakuna cha kufichika dhidi Yake. Wala hakipotei Kwake hata japo chembe ya kitu mbinguni na ardhini. Kwa ajili hii. Allah تعالى Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٠﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyofichika, Mwenye khabari za yote.”

Yaani, ni Mpole na Mwenye Elimu. Vitu havifichikani Kwake, hata kama vitakuwa vidogo sana, vyepesi na hafifu.

خَبِيرٌ ﴿١١﴾

“...Mwenye khabari za yote.”

Hata hatua za mwendo wa sisimizi katika usiku wa giza totoro. Halafu akasema:

يُنَبِّئُ أَقِمِ الصَّلَاةَ

“Ewe mwanangu! Shika Swala...”

Yaani, kwa kuchunga mipaka, faradhi na nyakati zake.

وَأْمُرْ بِالْمَعْرُوفِ وَأَنْهَ عَنِ الْمُنْكَرِ

“...na amrisha mema, na kataza maovu...”

Yaani, kwa kiasi cha uwezo na juhudi yako,

وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا أَصَابَكَ

“...na subiri kwa yanayokupata.”

Tambua kwamba jambo la kuamrisha mema na kukataza maovu halina budi kupata udhia kutoka kwa watu, basi akamwamuru awe mwenye subira. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ ذَٰلِكَ مِّنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٢﴾

“Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.”

Yaani, subira dhidi ya udhia wa watu ni miongoni mwa mambo ya kuazimiwa. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ

“Wala usiwabeuwe watu...”

Anasema kuwa: Usiugeuze uso wako upande tofauti na watu, pindi ukizungumza nao au wakikusemesha kutokana na kuwadharau kwako na kuwafanyia kiburi, bali uwe laini kwao na uwakunjulie uso wako. Ni sawa na ilivyokuja katika Hadithi:

«وَلَوْ أَنْ تَلْفَى أَخَاكَ وَوَجْهَكَ إِلَيْهِ مُتَبَسِّطًا، وَإِيَّاكَ وَإِسْبَالَ الْإِزَارِ فَإِنَّهَا مِنَ الْمَخْبِيلَةِ،
وَالْمَخْبِيلَةُ لَا يُجِبُّهَا اللَّهُ»

“Japo ukutane na nduguyo na uso wako uwe na bashasha. Na nakupa tahadhari dhidi ya kuburuza nguo yako, kwani hii ni katika majivuno. Allah Hayapendi majivuno.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا

“...wala usitembee katika nchi kwa maringo.”

Maana yake, majivuno, mwenye kiburi, jeuri na ukaidi. Usifanye hayo, Allah تعالى Atakukasirikia.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٣١﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila anayejiwuna na kujifakhirisha.”

Yaani, mwenye kujiona na kuipenda nafsi yake, mwenye kujifakhirisha mbele ya mwingine. Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾

“Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima.” (17:37)

Tumekwishalieleza hili katika mahali pake.

¹ Abu Dawud 4:345.

Amri ya Kutembea kwa Wastani

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ

“Na ushike mwendo wa katikati...”

Yaani, tembea kwa wastani, si mwendo wa taratibu sana na wa kivivu wala wa uliozidi kiasi. Bali wa kati kwa kati, baina ya hali mbili hizi,

وَأَغْضُضْ مِنْ صَوْتِكَ

“...na teremsha sauti yako.”

Usizidishe sana mazungumzo wala kupaza sauti bila ya kuwepo faida ndani yake.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿١٠﴾

“Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda.”

Mujahid na wengine walisema, “Sauti mbaya zaidi ni ya punda, yaani kadiri mtu anyanyuavyo sauti yake, basi, hushabihiana na ya punda katika kuwa kwake ya juu na kupanda. Pamoja na haya, ni yenye kumghadhabisha Allah تعالى. Kushabihishwa huku na punda ni dalili ya kwamba imeharamishwa na ya kukaripiwa upeo wa kukemewa.”

Ni kwa sababu Mtume ﷺ alisema:

«لَيْسَ لَنَا مَثَلُ السُّوءِ، الْعَائِدُ فِي هَيْبَةِ كَالْكَلْبِ يَتِيءُ ثُمَّ يُوَدُّ فِي فَنِيهِ»

“Mfano mbaya si wetu. Mtu anayeirudia (kuichukua) zawadi yake, ni kama mbwa anayetapika, halafu anayarudia matapishi yake.”¹

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 4:522.

Nasaha za Luqman

Huu ni wasia wenye manufaa sana, ni baadhi ya visa vilivyo katika Qur'an tukufu, kuhusu Luqman mwenye hekima. Ilisimuliwa kumhusu yeye, mambo mengi kuhusu hekima na mawaidha. Tutataja mifano na desturi za visa hivyo. Imamu Ahmad alimnukuu Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: Mtume ﷺ alitupasha khabari kwa kusema:

«إِنَّ لُقْمَانَ الْحَكِيمِ كَانَ يَقُولُ: إِنَّ اللَّهَ إِذَا اسْتَوْدَعَ شَيْئًا حَفِظَهُ»

*"Hakika, Luqman, mwenye Hekima, alikuwa akisema: 'Ikiwa kitu kitategemezwa kwa Allah, basi Atakihifadhi.'"*¹

Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema: "Luqman alimwambia mwanaye, akiwa katika kumuaidhi: 'Ewe mwanangu! Nakutahadharisha At-Taqannu' (ulaghai) kwani ni wenye kutia khofu usiku na lawama mchana."² Ilisimuliwa kwamba As-Thari bin Yahya alisema: "Luqman alimwambia mwanaye, 'Hikima imewaketisha masikini vikao vya wafalme."³ Pia alinukuu kutoka kwa 'Awn bin 'Abdullah kuwa alisema: 'Luqman alimwambia mwanaye, "Ewe Mwanangu! Utakapoendea mkusanyiko wa watu, watupie mshale wa Uislamu, yaani As-Salaam. Halafu ukae upande wao. Wala usitamke jambo, mpaka uwaone wametamka. Wakimtaja Allah تعالى, ungana nao, lakini wakiingia katika ghairi ya hayo, waache na uende katika kundi jingine'."⁴



¹ Ahmad 2:87.

² Al-Hakim 2:4.

³ Ad-Dur Al-Manthur 5:316.

⁴ Az-Zuhd ya Ibn Al-Mubarak uk 332.

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَسْبَغَ
 عَلَيْكُمْ نِعْمَهُ ظَهْرَةً وَبَاطِنَةً * وَمِنَ النَّاسِ
 مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّبِينٍ
 وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا بَلْ نَتَّبِعُ مَا
 وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا ؕ أُولَئِكَ كَانَ الشَّيْطَانُ يَدْعُوهُمْ إِلَى
 عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿٢٠﴾ * وَمَن يُسَلِّمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ
 مُحْسِنٌ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ ؕ وَإِلَى اللَّهِ عَاقِبَةُ
 الْأُمُورِ ﴿٢١﴾ وَمَن كَفَرَ فَلَا يَحْزُنكَ كُفْرُهُ ؕ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ
 فَنُنذِرُهُم بِمَا عَمِلُوا ؕ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٢٢﴾
 نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابِ غَلِيظٍ ﴿٢٣﴾
 وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّن خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ؕ
 قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ ؕ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٤﴾ لِلَّهِ مَا فِي
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ؕ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٢٥﴾ وَلَوْ
 أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِن شَجَرَةٍ أَقْلَمٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِن
 بَعْدِهِ سَبْعَةُ أَنْحَارٍ مَا نَفَذْتَ كَلِمَتُ اللَّهِ ؕ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ
 حَكِيمٌ ﴿٢٦﴾ مَا خَلَقَكُمْ وَلَا بَعَثَكُمْ إِلَّا كَتَفْسٍ وَاحِدَةً
 إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٢٧﴾

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَسْبَغَ
 عَلَيْكُمْ نِعْمَهُ ظَهْرَةً وَبَاطِنَةً * وَمِنَ
 النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ
 وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٢٠﴾ وَإِذَا
 قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا
 بَلْ نَتَّبِعُ مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا ؕ
 أُولَئِكَ كَانَ الشَّيْطَانُ يَدْعُوهُمْ إِلَى
 عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿٢١﴾

20. "Kwani hamuoni ya kwamba Mwenyezi Mungu Amevifanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Akakujaliziene Neema Zake, za dhahiri na za siri? Na miongoni mwa watu wapo wanaobishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru."

21. "Na wanapoambiwa: Fuateni Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, husema:

Bali tunafuata tuliyowakuta nayo baba zetu. Je! Ijapokuwa Shetani anawaita kwenye adhabu ya Moto uwakao?"

Kukumbushwa neema

Allah تعالی Anawajuzi waja Wake Neema Zake kwao, duniani na Akhera, kwa Kuwatiishia vilivyo mbinguni, kama nyota wanazonufaika kwa mwanga wake nyakati za usiku na mchana, na Anayoyaumba humo, kama vile mawingu, mvua, theluji na mvua ya mawe, na Alifanya mbingu iwe paa lililohifadhiwa. Pia, vile ambavyo Allah تعالی Aliwaambia ardhini kuwa sakafu, kuwe na mito, miti, mazao na matunda. Akakamilisha Neema Zake za dhahiri na za batini, kama Kutuma Mitume, Kuteremsha Vitabu, na Kuondoa mashaka na nyudhuru. Pamoja na haya yote, hawakuamini watu wote, wapo miongoni mwao wanaobisha tauhidi Yake Allah تعالی, Kutuma kwake Mitume. Wanabisha hayo kwa Allah تعالی bila elimu, wala kuegemea hoja madhubuti, wala Kitabu sahihi kilichorithiwa. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُنِيرٍ ﴿٣١﴾

“Na miongoni mwa watu wapo wanaobishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru.”

Yaani, chenye kubainisha, chenye mwangaza,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ

“Na wanapoambiwa...”

Maana yake, hao wanaobisha kuhusu Tauhidi ya Allah تعالی,

اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ

“Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu...”

Juu ya Mtume Wake, nazo ni sharia zilizotwahirika,

قَالُوا بَلْ نَتَّبِعُ مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا

“...husema: Bali tunafuata tuliyowakuta nayo baba zetu.”

Yaani, hawakuwa na hoja, ila kuwafuata mababa waliotangulia. Allah تعالی Amesema:

أُولُو كَابِءَابَاؤُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ ﴿١٧﴾

“Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawaelewi kitu, wala hawakuongoka?” (2:170)

Yaani, ni ipi fikra yenu nyie watoa hoja ya kufuata waliyofanya baba zenu, kuwa walikuwa wapotevu, nanyi mko nyuma yao katika waliyokuwa nayo. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema:

أُولُو كَانِ الشَّيْطَانُ يَدْعُوهُمْ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿١٨﴾

“Je! Ijapokuwa Shetani anawaita kwenye adhabu ya Moto uwakao?”

✽ وَمَنْ يُسَلِّمْ وَجْهَهُ إِلَىٰ اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ وَإِلَى اللَّهِ عَنَقَبَةُ

الْأُمُورِ ﴿١٩﴾ وَمَنْ كَفَرَ فَلَا تَحْزُنْكَ كُفْرُهُ ۗ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ فَنُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ

عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٢٠﴾ نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابِ غَلِيظٍ ﴿٢١﴾

22. “Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwishakamata fundo lilio madhubuti. Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu.”

23. “Na anayekufuru, isikuhuzunisha kufuru yake. Kwetu ndio marudio yao, na hapo Tutawaambia waliyoyatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.”

24. “Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.”

Allah تعالى Anaeleza juu ya mwenye kusalimisha uso wake kwa ajili ya Allah تعالى, yaani anafanya amali zake kwa kumtakasia Allah تعالى na kuzifuata Amri na Shariah Zake, Kwa ajili hii, Amesema:

وَهُوَ مُحْسِنٌ

“...naye akawa anafanya wema...”

Yaani, katika amali zake, kwa kuyafuata aliyooamrisha na kuyaacha aliyoyakataza,

فَقَدْ اسْتَمَسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ

“...basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti.”

Yaani, amepokea ahadi imara kutoka kwa Allah تعالی kwamba hawatamuadhibu.

وَأِلَى اللَّهِ عَنقَبَةُ الْأُمُورِ ﴿٢٠﴾ وَمَنْ كَفَرَ فَلَا مَحْزَنَ لَكَ كُفْرُهُ

“Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu. Na anayekufuru, isikuhuzunisha kufuru yake.”

Maana yake: ‘Usiwahuzunikia ewe Muhammad katika kumkufuru kwao Allah تعالی na yale uliyokuja nayo, kwani Kudura ya Allah تعالی ni yenye kuleta athari kwao, marejeo yao ni kwa Allah تعالی na Atawaambia waliyoyafanya, yaani Atawajazi,

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٢١﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.”

Hakifichiki cha kujificha. Halafu Allah تعالی Amesema:

نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا

“Tunawastarehesha kwa uchache...”

Yaani, duniani,

ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ

“...kisha Tutawasukuma...”

Maana yake, Tutawasababishia wawe,

إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٢٢﴾

“...kwenye adhabu ngumu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

إِنَّ الَّذِينَ يَفْتُرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾ مَتَّعَ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا
مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

“Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjeshwa adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.”
(10:69-70)

وَلَيْن سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿٦٩﴾ اللَّهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٧٠﴾

25. “Na ukiwauliza: Nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Wewe sema: Alhamdulillah! Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui.”

26. “Ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mkwasi, Mwenye Kusifiwa.”

Washirikina Wanakiri Kwamba Allah تعالی Ndiye Muumbaji

Allah تعالی Anatoa khabari ya hao wanaomshirikisha, kwamba wao wanajua kuwa Allah تعالی, Muumba mbingu na ardhi, Peke Yake, hana mshirika. Pamoja na haya wanamuabudu pamoja na washirika na wanakiri kuwa hao wameumbwa na wanamilikiwa na Allah تعالی. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَلَيْن سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ

“Na ukiwauliza: Nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Wewe sema: Alhamdulillah!”

Yaani, pindi hoja ikisimama kwenu, kwa kukubali kwao,

بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٩﴾

“Lakini wengi wao hawajui.”

Kisha, Allah تعالى Amesema:

لِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

“Ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na katika ardhi.”

Yaani, Yeye Ndiye Aliyeviumba na Ndiye Mmiliki wao,

اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيْدُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mkwasi, Mwenye Kusifiwa.”

Maana yake, si mhitaji wa asiyekuwa Yeye, na kila kitu kinahitajia Kwake, Mwenye Kuhimidiwa katika kila Alichokiumba, Mwenye Kushukuriwa mbinguni na ardhini, pia ni mwenye Kuhimidiwa katika mambo yote.

وَلَوْ اَنَّمَا فِي الْاَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ اَقْلَمٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ اُنْحُرٍ مَا نَفِدَتْ

كَلِمَتُ اللّٰهِ اِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٧٧﴾ مَا خَلَقَكُمْ وَلَا بَعَثَكُمْ اِلَّا كَنَفْسٍ وَّاحِدَةٍ اِنَّ اللّٰهَ

سَمِيْعٌ بَصِيْرٌ ﴿٧٨﴾

27. “Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, Maneno ya Mwenyezi Mungu yasingelikwisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

28. “Hakuwa Kuumbwa kwenu, wala kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye Kuona.”

Maneno ya Allah تعالى Hayawezi Kuhesabiwa au Kumalizwa

Allah تعالى Anaeleza juu ya Sifa Zake Tukufu kama Ukubwa, Kiburi, Utukufu, Majina Yake Mazuri na Kalima Zake Timilifu ambazo hakuna yeyote azijuaye. Hapana kiumbe ajuaye Dhati Yake au idadi yake.

Ni sawa na alivyosema Kiongozi wa viumbe na Mwisho wa Mitume ﷺ:

«لَا أُحْصِي ثَنَاءَ عَلَيْكَ أَنْتَ كَمَا أَثْنَيْتَ عَلَيَّ نَفْسِكَ»

“Nashindwa kukusifu Wewe vya kutosha; Wewe Uko sawa na Ulivyojisifu Mwenyewe.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَمٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ أُخْرٍ مَا نَفِدَتْ
كَلِمَتُ اللَّهِ

“Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, Maneno ya Mwenyezi Mungu yasingelikwisha.”

Yaani, hata kama miti yote ya ardhini itafanywa kuwa kalamu, na bahari ikafanywa wino na pamoja nayo zikaongezwa bahari saba, kisha zikatumika kuyaandika Maneno ya Allah تعالى yenye kuonesha Ukuu, Sifa na Utukufu Wake, basi kalamu zingelivunjika na maji yangekwisha, hata kama vitaongwezwata vifaa vingine mithili yake. Idadi ya saba imetajwa kuonesha kiasi kikubwa, wala haikukusudiwa kuchukuliwa kama ilivyo, wala haimaanishi kwamba bahari hizo ni kama hizi zilizopo, zinazoizunguka dunia, kama wasemavyo waliochukua kutoka katika *Israiliyyat*, ambazo haziaminiwi wala kukadhibishwa. Bali ni kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine.

قُلْ لَوْ كَانَ الْبَحْرُ مِدَادًا لَكَلِمَتِ رَبِّي لَنَفِدَ الْبَحْرُ قَبْلَ أَنْ تَنفَدَ كَلِمَتُ رَبِّي وَلَوْ جِئْنَا

بِمِثْلِهِ مَدَدًا ﴿١٥﴾

“Sema: kama bahari ingelikuwa wino kwa maneno ya Mola wangu, kwa hakika bahari zote zingalikwisha kabla ya maneno ya Mola wangu, hata Tungelileta nyengine mfano wake.” (18:109)

Basi si makusudio ya Kauli Yake,

¹ Muslim 1:352.

بِسْمِ اللَّهِ

“...mithili yake...”

Kwamba ni nyingine tu, bali na mithili yake tena na tena, na kuendelea hivyo hivyo, kwani hakuna ukomo wa Aya za Allah تعالى na Kalima Zake, Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٧﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Yaani, ni Mshindi, Ameshinda kila kitu, Amekitiisha kila kitu na Kukizidi, basi hapana wa kuzuia Atakayo wala wa kukhalifu wala wa kupinga Hukumu Yake. Yeye ni Mwenye Hikima katika Kuumba, Kuamuru, Kauli, Matendo, Shariah na Mambo Yake yote.

Kauli ya Allah تعالى,

مَا خَلَقْنَاكُمْ وَلَا نَبْعَثُكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ

“Hakukuwa kuumbwa kwenu wala kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu.”

Yaani, Kuumbwa watu wote na Kufufuliwa Siku ya Marejeo si kwa mnasaba mwingine, ila kwa Kudura Yake.

Ni kama Kuumbwa kwa nafsi moja. Yote ni mepesi mno Kwake,

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٢٨﴾

“Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.” (36:82)

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٢٩﴾

“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50)

Yaani, huli amuru jambo mara moja tu, jambo hilo linatokea, haihitajiki kukariri wala kusisitiza,

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿٧٩﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿٨٠﴾

“Kwa hakika hayo ni Zajrah (ukelele) mmoja tu. Mara watakuwa kwenye uwanda wa mkutano!” (79:13-14)

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٨١﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.”

Yaani, Kama Anavyosikia maneno yao yote, pia Anayaona matendo yao yote, kama Anavyoiona na Kuisikia nafsi moja. Kwa ajili hii.

Allah تعالى Amesema,

مَا خَلَقُكُمْ وَلَا بَعَثُكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ

“Hakukuwa Kuumbwa kwenu, wala Kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu.”

* * *

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُوَلِّجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوَلِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلًّا يَجْرِي إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَأَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٩﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الْبَطْلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٣٠﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ الْفُلْكَ تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِنِعْمَتِ اللَّهِ لِيُرِيكُمْ مِّنْ آيَاتِهِ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٣١﴾ وَإِذَا غَشِيَهُم مَّوْجٌ كَالظُّلَلِ دَعَوْا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ فَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ وَمَا يَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا كُلُّ خَتَّارٍ كَفُورٍ ﴿٣٢﴾ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ آتِفُوا رَبِّكُمْ وَأَخْشَوْا يَوْمًا لَا تَجْرِي وَالِدٌ عَن وَلَدِهِ وَلَا مَوْلُودٌ هُوَ جَازٍ عَن وَالِدِهِ شَيْئًا ۗ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِاللَّهِ الْغُرُورُ ﴿٣٣﴾ إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنزِلُ الْغَيْثَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ ۗ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا تَكْسِبُ غَدًا ۗ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿٣٤﴾

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُوَلِّجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوَلِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلًّا يَجْرِي إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَأَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٩﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الْبَطْلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٣٠﴾

29. "Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu Huuingiza usiku katika mchana, na Huuingiza mchana katika usiku, na Amedhalilisha jua na mwezi? Vyote hivyo vinakwenda mpaka wakati uliowekwa. Na Mwenyezi Mungu Anazokhabari za mnyoyatenda."

30. "Hivi ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu Ndiye wa kweli, na hakika wanachokiomba ni cha

uwongo. Na kwamba hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mtukufu na Ndiye Mkubwa."

Kutajwa Uweza wa Allah تعالى na Ukubwa Wake

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye,

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ

“Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu Huuingiza usiku katika mchana...”

Yaani, Anachukua kutoka katika usiku na kuongeza katika mchana, kwa hivyo, mchana unakuwa mrefu na usiku mfupi, na hilo linatokea kipindi cha majira ya joto. Mchana unaongezeka mpaka unafikia upeo wake. Halafu unaanza kupungua na baadaye usiku unakuwa mrefu na mchana unapungua. Hii hutokea katika zama za majira ya baridi.

وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلًّا يَجْرِي إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى

“...na Amedhalilisha jua na mwezi? Vyote hivyo vinakwenda mpaka wakati uliowekwa.”

Kwa maana, mpaka katika ukomo uliowekwa. Ilisemwa pia, mpaka Siku ya Kiyama. Maana zote mbili ni sahihi. Kauli ya kwanza inatiliwa nguvu na Hadithi ya Abu Dharr رضي الله عنه iliyo ndani ya Sahih Mbili, kwamba Mtume ﷺ amesema:

«يَا أَبَا ذَرٍّ! أَتَدْرِي أَيَّنَ تَذْهَبُ هَذِهِ الشَّمْسُ؟»

“Ewe Abu Dharr! Unakujua linakokwenda jua hili?”

Nikasema: “Allah na Mtume Wake ni wajuzi zaidi.”

«فَإِنَّهَا تَذْهَبُ فَتَسْجُدُ تَحْتَ الْعَرْشِ، ثُمَّ تَسْتَأْذِنُ رَبَّهَا فَيُوشِكُ أَنْ يُقَالَ لَهَا: ارْجِعِي مِنْ حَيْثُ جِئْتِ»

“Linakwenda na kusujudu chini ya Arshi, kisha linamwomba idhini Mola Wake, na karibuni litaambiwa, ‘Rejea huko huko ulikotoka.’”

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema: “Jua ni kama maji yatiririkayo, linapita njia yake angani, likitua, hupita katika njia yake chini ya dunia mpaka linachomoza upande wake wa kuchomozea. Kadhalika mwezi.” Isnadi yake ni sahihi.

¹Bukhari na. 4803, Muslim na, 159.

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنْتَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٣١﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Je! Hujui kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua yaliomo mbinguni na katika ardhi?” (22:70)

Yaani, Allah Ndiye Muumbaji na Mwenye Kujua vitu vyote. Sawa na Kauli Yake,

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ

“Mwenyezi Mungu ni Yule Ambaye Ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hizo.” (65:12)

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الْبَطْلُ

“Hivi ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu Ndiye wa kweli, na hakika wanachokiomba ni cha uwongo.”

Yaani, kwa hakika, Anazidhihirisha Aya Zake ili muweze Kujua kutokana nazo kuwa Yeye ni wa kweli, yaani ni yupo kweli tena ni Mola wa kweli. Na kwamba kila kilicho ghairi Yake ni batili, kwani Yeye Hahitaji mwingine na kwamba kila kitu kina haja Naye, kwa sababu kila kilichomo mbinguni na ardhini ni kiumbe Chake na mja Wake. yeyote kati yao, hawezi kukitikisa kitu cha uzito wa atomi, isipokuwa kwa Idhini Yake. Lau kama watakusanyika wakazi wa ardhini ili waumbe nzi, wangelishindwa. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الْبَطْلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٣١﴾

“Hivi ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu Ndiye wa kweli, na hakika wanachokiomba ni cha uwongo. Na kwamba hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mtukufu na Ndiye Mkubwa.”

Yaani, ni Mtukufu Ambaye hakuna zaidi yake, Mkubwa kuliko kila kitu, kila kinachonyenyekea ni dhalili Kwake Yeye.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ الْفُلُكَ تَجْرَى فِي الْبَحْرِ بِنِعْمَتِ اللَّهِ لِيُرِيكُمْ مِنْ آيَاتِهِ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
لِكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٣١﴾ وَإِذَا غَشِيَهُمْ مَوْجٌ كَالظُّلَلِ دَعَوْا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا
نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ فَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ وَمَا يَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا كُلُّ خَتَّارٍ كَفُورٍ ﴿٣٢﴾

31. "Kwani huoni kwamba marikebu hupita baharini zikichukua neema za Mwenyezi Mungu, ili Kukuonesheni baadhi ya Ishara Zake? Hakika katika haya zipo Ishara kwa kila mwenye kusubiri, mwenye kushukuru."

32. "Na wimbi linapowafunika kama wingu, wao humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia dini. Lakini Anapowaokoa wakafika nchi kavu, wapo baadhi yao huenda mwendo wa sawa. Wala hazikanushi Ishara Zetu ila aliyekhaini kafiri mkubwa."

Allah تعالی Anaeleza kwamba Yeye Ndiye Aliyeyitiisha bahari ili meli zipite humo kwa Idhini Yake. Yaani kwa Ulatifu na Nguvu Zake. Kwani lau kama Asingelijaalia ndani ya maji kuwe na nguvu za kubeba meli, basi zisingelipita. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

لِيُرِيكُمْ مِنْ آيَاتِهِ

"...ili kukuonesheni baadhi ya Ishara Zake?"

Yaani, miongoni mwa Kudura Zake,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٣١﴾

"Hakika katika haya zipo Ishara kwa kila mwenye kusubiri, mwenye kushukuru."

Yaani, mwenye subira wakati wa shida, mwenye kushukuru wakati wa faraja. Kisha, Allah تعالی Amesema:

وَإِذَا غَشِيَهُمْ مَوْجٌ كَالظُّلَلِ

"Na wimbi linapowafunika kama wingu..." Yaani, kama milima na mawingu,

دَعَوْا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

"...wao humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia Dini."

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَاهُ

“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu.” (17:67)

Na Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلِكِ

“Na wanapopanda katika marikebu...” (29:65)

Kisha, Allah تعالى Amesema:

فَلَمَّا نَجَّوهُمْ إِلَى الْبَرِّ فَمِنْهُمْ مُقْتَصِدٌ

“Lakini Anapowaokoa wakafika nchi kavu, wapo baadhi yao huenda mwendo wa sawa.”

Mujahid alisema: “Inarejea kwa makafiri – kama kwamba alilitafsiri neno *Muqtaswid* kwa maana ya mkanushaji¹ kama ilivyo katika Aya ifuatayo,

فَلَمَّا نَجَّوهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ ﴿٦٥﴾

“Lakini anapowavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha.” (29:65)

وَمَا يَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا كُلُّ خَتَّارٍ كَفُورٍ ﴿٦٦﴾

“Wala hazikanushi Ishara Zetu ila aliyekhaini kafiri mkubwa.”

Neno *Khattaar*, maana yake ni mtu khaini. Hii ilikuwa rai ya Mujahid, Al-Hasan, Qatadah na Malik, akisimulia kutoka kwa Zayd bin Aslam.² Naye kila anapoahidi, huivunja ahadi yake, na maana yake inarejea pia katika namna mbaya mno ya khiyana. Kauli ya Allah تعالى:

كُفُورٍ ﴿٦٦﴾

“...kafiri mkubwa.” Maana yake, mpingaji neema na kutokushukuru, bali anazisahau, wala hazikumbuki.

¹ At-Tabari 20:157.

² At-Tabari 20:157.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ وَأَحْشَوْا يَوْمًا لَا تَجْزِي وَالِدٌ عَنِ وَلَدِهِ وَلَا مَوْلُودٌ هُوَ جَارٍ
عَنِ وَالِدِهِ شَيْئًا إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِاللَّهِ
الْغُرُورُ ﴿٣٣﴾

33. "Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi, na iogopeni siku ambayo mzazi hatamfaa mwana, wala mwana hatamfaa mzazi kwa lolote. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala asikudanganyeni na Mwenyezi Mungu mdanganyifu."

Amri ya Kumcha Allah تعالى na Kuikumbuka Siku ya Kufufuliwa

Allah تعالى Anawaonya watu kuhusu Siku ya Marejeo na Anawaamuru kumcha na kumkhofu Yeye na kuogopa Siku ya Kiyama, pindi,

لَا تَجْزِي وَالِدٌ عَنِ وَلَدِهِ

"...mwana hatamfaa mzazi kwa lolote."

Yaani, lau kama mzazi atataka mwana amkomboe kwa nafsi yake kwa yaliyokuwa kabla yake, kadhalika mtoto akitaka mzazi awe fidia kwa nafsi yake, hatakubaliwa. Kisha, Allah تعالى Aliwarudia kuwapa mawaidha, kwa Kauli Yake,

فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا

"Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia..."

Yaani, yasiwadanganye mkasahau maisha bora ya Akhera,

وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِاللَّهِ الْغُرُورُ ﴿٣٤﴾

"...wala asikudanganyeni na Mwenyezi Mungu mdanganyifu."

Yani, *Shaytan*. Hili amelisema Ibn 'Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak na Qatadah¹ رضي الله عنهم. Kwani yeye humghuri mwanadamu, kumwongopea kwa ahadi na kudai kumfadhilisha, wala hakuna lolote katika hayo.

¹ At-Tabari 20:159.

Ni kama Allah تعالى Alivyosema,

يَعِدُّهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ^ط وَمَا يَعِدُّهُمْ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٤١﴾

“Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shet’ani hawaahidi ila udanganyifu.”(4:120)

Wahb bin Munabbih alisema: ‘Uzayr alisema, “Pindi nilipoona balaa kwa watu wangu, nilishikwa na huzuni kubwa, dhiki yangu ikazidi na usingizi ukanitoka. Nikamnyenyekea Mola wangu, nikasali na kufunga saumu. Katika unyenyekevu huo nilikuwa nalia. Akanijia Malaika, na nikamwambia, ‘Nijulishe, je roho za waja wema zitawashufaia madhalimu au mababa kwa watoto wao?’ Akasema: ‘Kiyama kitapambanua hukumu na Ufalme wa Allah تعالى Utadhihirika, wala hakutakuwa na udhuru. Hakuna atakayezungumza ila kwa Idhini ya Mola wake. Mzazi hatachukuliwa mahali pa mwanaye, wala kinyume chake; wala ndugu kwa nduguye; wala mja kwa bwana wake. Wala hapana atakaye mjali mwingine, wala hatasikitika atakapomwona mwenye huzuni, wala hapana wa kumwonea huruma, wala mwanadamu hatabebeshwa mzigo wa mtu mwingine. Kila mmoja atajali nafsi yake, ataililia nafsi yake, atabeba mzigo wake, wala hakutakuwa na wa kumbebea mzigo wake.” Aliyanukuu Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى.

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنزِلُ الْغَيْثَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ^ط وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا تَكْسِبُ غَدًا^ط وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ^ط إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿٤٢﴾

34. “Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anayeiteremsha mvua. Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na hajui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote hajui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujua, Mwenye Khabari.”

Allah تعالى Ndiye Ajuaye Ghaibu

Hizi ni funguo za ghaibu ambazo Allah تعالى Peke Yake Amejiwekea. Hapana aijuaye ghaibu isipokuwa hujulishwa na Allah تعالى. Kwa hivyo, ujuzi wa wakati wa kuwadia kwa Saa hakuna Nabii, Mtume Wake wala Malaika wa karibu na Allah تعالى Ajuuae,

لَا تُحِيطُ بِأَيِّ لَوْحَاتِهَا إِلَّا هُوَ

“Haidhirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye.” (7:187)

Kadhalika, kuteremka kwa mvua, hapana ajuaye isipokuwa Allah تعالى, lakini pindi Anapoiamuru huwajulisha hilo Malaika waliowakilishwa kazi hiyo, na wale Awatakao Allah تعالى katika viumbe wake. Kadhalika, hapana ajuaye vilivyo matumboni, katika ambavyo Allah تعالى Anataka Kuviumba, isipokuwa Yeye. Lakini Akishaamuru kwamba awe mwanamume au mwanamke, mwovu au mwema, Huwajulisha malaika waliowakilishwa kazi hiyo, na viumbe Wake Awatakao. Pia, nafsi haijui itakachokichuma kesho yake, duniani na Akhera.

وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ

“Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani.”

Katika mji wake au mwingine katika ardhi yoyote ya Allah تعالى. Hapana alijuaye hilo. Hii inashabihiana na Kauli ya Allah تعالى:

﴿ وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ﴾

“Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu.” (6:59)

Sunna imeyasimulia mambo hayo matano kwa kuyaita funguo za ghaibu. Imamu Ahmad amemnukuu Buraydah رضي الله عنه, kuwa amesema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«خَمْسٌ لَا يَعْلَمُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: ﴿١﴾ إِنْ أَرَادَ اللَّهُ عِنْدَهُ عِلْمَ السَّاعَةِ وَنَزَلَ الْعَيْنِ
وَبَدَأَ مَا فِي الْأَرْحَامِ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا تَكْسِبُ غَدًا وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ
إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿٢٤﴾»

“Mambo matano. Hapana ayajuaye isipokuwa Allah: ‘Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye

Anayeiteremsha mvua. Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujua, Mwenye Habari.’¹

Hadithi hii ina isnadi sahihi, lakini Bukhari na Muslim hawakuinukuu.

Hadithi ya Ibn ‘Umar رضي الله عنهما.

Imamu Ahmad alimnukuu Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: Mtume ﷺ alisema:

«مَفَانِيحُ الْغَيْبِ خُمْسٌ لَا يَعْلَمُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ: ﴿۱﴾ إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُرَكَّبُ الْقَبْرِ
وَيَسْمُرُ مَا فِي الْأَرْحَامِ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا تَكْسِبُ غَدًا وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ
إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿۲﴾»

“Funguo za ghaibu ni tano. Hapana azijuaye isipokuwa Allah: ‘Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anayeiteremsha mvua. Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na nafsi yoyote haijui itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujua, Mwenye Habari.’²

Hii ilinukuliwa na Bukhari peke yake, ambapo aliisimulia katika Kitabu cha Swala ya Mvua katika *Sahih* yake.³

Aliinukuu pia katika Tafsiri kwa namna nyingine, kwamba ‘Abdullah Ibn ‘Umar رضي الله عنهما alisema: Mtume ﷺ alisema:

«مَفَانِيحُ الْغَيْبِ خُمْسٌ»

“Funguo za ghaibu ni tano.”

Halafu akasoma,

¹ Ahmad 5:353.

² Ahmad 2:24

³ Fat’h Al-Bari 2:609.

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُبْرِكُ اللَّيْلُ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْآرْحَامِ

“Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anayeiteremsha mvua. Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi.”¹

Hiyo, kadhalika, aliinukuu Bukhari peke yake.

Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه.

Katika kuitafsiri Aya hii, Bukhari alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa alisema siku moja Mtume ﷺ alikuwa amesimama mbele ya watu, mtu mmoja akamjia kwa kutembea, akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Imani ni nini?” Akasema:

«الْإِيمَانُ أَنْ تُؤْمِنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ، وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَلِقَائِهِ، وَتُؤْمِنَ بِالْبَعْثِ الْآخِرِ»

“Imani ni kwamba, umuamini Allah na Malaika Wake, Vitabu, Vyake, Mitume Wake na kukutana Naye, na uamini kufufuliwa huko Akhera.”

Akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Uislamu ni nini?” Akasema:

«الْإِسْلَامُ أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ وَلَا تُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا، وَتُقِيمَ الصَّلَاةَ، وَتُؤْتِيَ الزَّكَاةَ الْمَفْرُوضَةَ، وَتَصُومَ رَمَضَانَ»

“Uislamu ni kwamba, umwamini Allah wala usimshirikishe na kitu, usimamisha Swala, utoe Zaka ya faradhi na ufunge Ramadhani.”

Akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Ihsani ni nini?” Akasema:

«الْإِحْسَانُ أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ»

“Ihsani ni kwamba, umuabudu Allah kama vile unamuona, na kama humuoni, basi Yeye Anakuona.”

Akasema: “Ewe Muhammad! Saa itatokea lini?” Akamjibu,

¹Fat’h Al-Bari 8:373.

«مَا الْمَسْئُولُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ، وَلَكِنْ سَأَحَدُّثُكَ عَنْ أَشْرَاطِهَا: إِذَا وَلَدَتْ
الْأُمَّةَ رَبَّتَهَا فَذَاكَ مِنْ أَشْرَاطِهَا، وَإِذَا كَانَ الْحَقَّاءُ الْعُرَاءُ رُؤُوسَ النَّاسِ فَذَاكَ مِنْ
أَشْرَاطِهَا فِي خَمْسٍ لَا يَعْلَمُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ: هَلْ إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنزِلُ الْعَقَبَتِ
وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ»

“Muulizwaji wa hiyo saa si mwenye kujua zaidi ya muulizaji, lakini nitakueleza baadhi ya alama zake: Ni pindi kijakazi atakapomzaa bi mkuu wake. Basi, hiyo ni miongoni mwa alama zake. Pindi wenye miguu mitupu, wasiovaa nguo watakapokuwa viongozi wa watu. Hiyo ni katika alama zake. Saa ni mojawapo ya mambo matano ambayo hapana ayajuaye isipokuwa Allah: ‘Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye Ndiye Anaye-iteremsha mvua. Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi.”

Kisha, yule mtu akaondoka. Akasema:

«رُدُّوهُ عَلَيَّ»

“Mrudisheni kwangu.”

Wakamfuata ili wamrudishe, lakini hawakuona kitu chochote. Mtume ﷺ akasema:

«هَذَا جِبْرِيلُ جَاءَ لِيُعَلِّمَ النَّاسَ دِينَهُمْ»

“Huyu ni Jibril, amekuja kuwafundisha watu Dini yao.”¹

Ilinukuliwa na Bukhari katika Kitabu cha Imani, kadhalika Muslim kutoka katika isnadi mbalimbali.² Tulikwishazungumzia haya katika utangulizi wa Bukhari na hapo tukataja kwa urefu Hadithi ya Amiri wa Waumini, ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه. Hizi zilinukuliwa na Muslim.

وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ

“Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani.”

¹ Fat’hu - Al-Bari 8:373.

² Fat’hu - Al-Bari 1:140, Muslim 1:139.

Qatadah amesema: Kuna vitu ambavyo Allah تعالى Amejihifadhia Nafsi Yake, na Hakumfahamisha Malaika wa karibu wala Nabii aliyetumwa.

إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ

“Hakika kujua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu.”

Basi, hakuna mtu yeyote ajuaye lini Saa itasimama, wala mwaka wake, au mwezi, au usiku au mchana,

وَيُنزِلُكَ الْغَيْثَ

“Na Anateremsha mvua.”

Hakuna ajuae lini mvua itanyesha. Mchana wala usiku,

وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ

“Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi.”

Hakuna ajuaye kilicho tumboni, ni kiume au kike, chekundu au cheusi, au ni nini hasa,

وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا تَكْسِبُ غَدًا

“Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho.”

Ni kheri ama shari? Wala wewe mwanaadamu hujui lini utakufa, ni leo ama kesho, huenda ni kesho utakufa au kupatwa na janga.

وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ

“Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani.”

Yaani, hakuna yeyote duniani ajuaye kwamba ataulaza wapi mwili wake. Ni baharini, au nchi kavu, ni katika uwanda au mlimani.¹ Imeelezwa katika Hadithi,

«إِذَا أَرَادَ اللَّهُ قَبْضَ عَبْدٍ بِأَرْضٍ جَعَلَ لَهُ إِلَيْهَا حَاجَةً»

“Allah Akitaka kuitoa roho ya mja katika ardhi fulani, basi humjaalia huko haja yake.”²

¹ At-Tabari 20:160.

² Al-Hakim 1:42.

Abu Al-Qasim At-Tabarani رحمه الله تعالى alinukuu katika kitabu chake *Al-Mu'jam Al-Kabir* kwa isnadi ya Usamah bin Zayd رضي الله عنه, alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا جَعَلَ اللَّهُ مِيتَةً عَبْدٍ بِأَرْضٍ إِلَّا جَعَلَ لَهُ فِيهَا حَاجَةً»

“Allah hajaalii kifo cha mja katika ardhi fulani, bali humfanya awe na haja humo.”²

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Surat Luqman*, Alhamdulillah, Mola wa viumbe wote. Allah تعالى Anatutosha na pia ni Mbora wa kumtawakali.

* * *

¹ At-Tabarani 1:178.

Tafsiri ya Suratu As-Sajda

Sura ya 32

Iliteremshwa Makkah

Katika kuonesha fadhila za sura hii Bukhari amemnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema kuwa: Mtume ﷺ alikuwa akiisoma katika Al-Fajiri ya siku ya Ijumaa,

الْم ﴿١﴾ تَنْزِيلُ

“Alif Lam Mim (A.L.M.) Huu ni mteremsho...”

Kisomo cha As-Sajdah na,

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ

“Hakika kilimpitia binaadamu...” (76:1)¹

Hii ilinukuliwa na Muslim pia.² Imamu Ahmad alimnukuu Jabir رضي الله عنه, kuwa amesema, Mtume ﷺ alikuwa halali, mpaka asome

الْم ﴿١﴾ تَنْزِيلُ

“Alif Lam Mim (A.L.M.) Huu ni mteremsho...” na

تَبْرَكَ الَّذِي يَمُدُّهُ الْمَلَكُ

“...Ametukuka Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wote.”³ (67:1)

Ahmad peke yake ndiye aliyenukuu.

* * *

¹ Fat'h Al-Bari 2:438.

² Muslim 2:599.

³ Ahmad 3:340.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ السَّجْدَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْم ﴿١﴾ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ
 ﴿٢﴾ أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ لِتُنذِرَ
 قَوْمًا مَّا أَتَتْهُمْ مِنْ نَذِيرٍ مِّنْ قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٣﴾
 اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ
 أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ ۗ مَا لَكُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ وَلِيٍّ
 وَلَا شَفِيعٍ ۗ أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٤﴾ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ مِنَ السَّمَاءِ
 إِلَى الْأَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ
 مِّمَّا تَعُدُّونَ ﴿٥﴾ ذَلِكَ عِلْمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيزِ
 الرَّحِيمِ ﴿٦﴾ الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ۗ وَبَدَأَ خَلْقَ
 الْإِنسَانِ مِنْ طِينٍ ﴿٧﴾ ثُمَّ جَعَلَ نَسْلَهُ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ مَّاءٍ
 مَّهِينٍ ﴿٨﴾ ثُمَّ سَوَّاهُ وَنَفَخَ فِيهِ مِنْ رُوحِهِ ۗ وَجَعَلَ لَكُمُ
 السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿٩﴾
 وَقَالُوا أَإِذَا ضَلَلْنَا فِي الْأَرْضِ أَإِنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ ۗ بَلْ
 هُمْ بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ كَافِرُونَ ﴿١٠﴾ * قُلْ يَتَوَفَّنَا مَلِكُ الْمَوْتِ
 الَّذِي وَكَّلَ بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾

الْم ﴿١﴾ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ
 فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ أَمْ
 يَقُولُونَ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ
 رَبِّكَ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَتْهُمْ مِنْ نَذِيرٍ
 مِّنْ قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٣﴾

1. "Alif Lam Mim (A.L.M.)"

2. "Huu ni mteremsho wa Kitabu kisichokuwa na shaka yoyote kinachotoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote."

3. "Au wanasema: Ame-kizua? Bali hichi ni Kweli iliyotoka kwa Mola wako Mlezi ili uwaonye watu wasiofikiwa na mwonyaji kabla yako; huenda waka-ongoka."

Qur'an ni Kitabu cha Allah
 Ambacho Hakina Shaka
 Ndani Yake

Maneno kuhusu herufi za
 mkato yamekwishatangulia
 mwanzoni mwa Surat Al-

Baqarah kwa kiasi kisicholeta haja ya kurudia hapa. Kauli ya Allah تعالى،

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ

“Huu ni mteremsho wa Kitabu kisichokuwa na shaka yoyote...”

Maana yake: Hamna shaka wala wasiwasi ndani yake.

مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٢﴾

“Kutoka kwa Mola wa walimwengu?”

Kisha Allah تعالى Alieleza madai ya washirikina wanaosema kwamba:

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ

“Au wanasema: Ameitunga mwenyewe (Qur’an)?”

Maana yake: Amezua mwenyewe،

بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أَتَتْهُمْ مِّنْ نَّذِيرٍ مِّن قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٣٣﴾

“Bali hichi ni Kweli iliyotoka kwa Mola wako Mlezi ili uwaonye watu wasiofikiwa na mwonyaji kabla yako; huenda wakaongoka.”

Maana yake: Wafuate ukweli.

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۗ مَا لَكُمْ مِّن دُونِهِ مِن وَلِيٍّ وَلَا شَفِيعٍ ۗ أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٣٤﴾ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ مِنَ السَّمَاءِ إِلَى الْأَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّونَ ﴿٣٥﴾ ذَلِكَ عَلِيمٌ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٣٦﴾

4. “Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi na viliomo baina yao kwa siku sita, na Akakaa kwenye Kiti cha Enzi. Nyinyi hamna mlinzi wala mwombezi isipokuwa Yeye tu. Basi, je, hamkumbuki?”

5. “Anapitisha mambo yote yalio baina ya mbingu na ardhi, kisha

yanapanda kwake kwa siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu kwa mnavyohisabu nyinyi.”

6. “Huyu Ndiye Mwenye Kuyajua yasiyoonekana na yanayoonekana. Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu.”

Allah تعالیٰ Ndiye Muumbaji na Mwenye Kuuendesha Ulimwengu

Allah تعالیٰ Anaeleza kwamba Yeye Ndiye Muumbaji wa vitu vyote. Aliumba mbingu na vilivyo baina ya hivyo kwa siku sita. Kisha Akalingana sawa katika Arshi. Maelezo juu ya hayo yamekwishapita tayari.

مَا لَكُمْ مِّنْ دُونِهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا شَفِيعٍ

“Nyinyi hamna mlinzi wala mwombezi isipokuwa Yeye tu.”

Maana yake: Bali Yeye ni Mfalme Ambaye ni Mdhibiti wa mambo yote, Muumbaji wa kila kitu, Anaendesha kila kitu, Muumbaji wa kila kitu. Hakuna Muumbaji mwingine zaidi Yake, wala hapana wa kuombea isipokuwa baada ya idhini Yake. Kauli ya Allah تعالیٰ,

أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ

“Basi, je, hamkumbuki?”

Maana yake: Enyi mnaoabudu miungu batili na kuwategemea. Yeye ni Mtukufu, Mtakatifu, na Ameepukana na kuwa na kifani au mshirika, au waziri au mshindani au mlinganifu. Hapana Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, wala hakuna Mola Mlezi ambaye si Yeye.

Kauli ya Allah تعالیٰ Kuwa,

يُذَبِّرُ الْأَمْرَ مِنَ السَّمَاءِ إِلَى الْأَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ إِلَيْهِ

“Anapitisha mambo yote yalio baina ya mbingu na ardhi, kisha yanapanda Kwake...”

Maana yake: Amri Yake inateremka kutoka juu ya mbingu mpaka katika mpaka wa mbali zaidi katika ardhi ya saba. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ,

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ الْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ

“Mwenyezi Mungu ni Yule ambaye Ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hizo. Amri Zake zinashuka baina yao...”(65:12)

Amali zinapanda mpaka katika mahali pa kunukuliwa, katika mbingu ya dunia. Masafa baina ya hivyo ni mwendo wa miaka mia tano, na unene wa mbingu ni mwendo wa miaka mia tano.

Mujahid, Qatadah na Adh-Dhahaak wamesema: Malaika huteremka na kupanda kutoka na kwenda masafa ya mwendo wa miaka mia tano, lakini Yeye Anaukata umbali huo katika muda wa kupepesa ukope wa jicho tu. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema,

فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّونَ ﴿٦٥﴾ ذَلِكَ عِلْمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ

“kwa siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu kwa mnavyohisabu nyinyi. Huyu Ndiye Mwenye Kuyajua yasiyoonekana na yanayoonekana.”

Maana yake: Mwenye Kuyaendesha mambo haya, Ambaye pia ni Shahidi wa amali za waja Wake. Hupanda Kwake iliyo tukufu na duni, kubwa na ndogo.

Yeye ni Mwenye Nguvu Ambaye Amekishinda kila kitu, Kukitiisha na wamemnyenyekea Yeye waja Wake. Ni Rahimu kwa waja Wake Waumini.

Yeye ni Mwenye Nguvu katika Rehema Zake na Rahimu katika Nguvu Zake.

Huu ndio ukamilifu, Nguvu kuwa pamoja na Rehema, na Rehema kuwa pamoja na Nguvu. Yeye ni Rahimu pasi na udhalili.

الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهُ ۗ وَبَدَأَ خَلْقَ الْإِنسَانِ مِن طِينٍ ﴿٦٦﴾ ثُمَّ جَعَلَ نَسْلَهُ مِن سُلَالَةٍ مِّن مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٦٧﴾ ثُمَّ سَوَّاهُ وَنَفَخَ فِيهِ مِن رُّوحِهِ ۗ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿٦٨﴾

7. “Ambaye Ametengeneza vizuri umbo la kila kitu; na Akaanzisha Kumuumba mtu kwa udongo.”

8. “Na kisha Akajaalia uzao wake utokane na kizazi cha maji madhaifu.”

9. “Kisha Akamtengeneza, na Akampulizia roho yake, na Akakujaalieni kusikia na kuona, na nyoyo za kufahamu. Ni uchache mnavyoshukuru.”

Uumbwaji wa Mwanaadamu Hatua kwa Hatua

Allah تعالى Anasema kwamba Yeye Ndiye Aliyeumba kila kitu vyema, Akakikamilisha na Kukiweka sawa. Malik amesema, Zayd bin Aslam aliizungumzia Aya,

الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهُ

“Ambaye Ametengeneza vizuri umbo la kila kitu...”

Kwa kusema: “Alikiumba kila kitu vyema, kama vile Kukijaalia kiwe katika vyenye kutangulizwa au vyenye kuakhirishwa. Baada ya Allah تعالى kutaja Kuumbwa kwa mbingu na ardhi, Aliingia katika Kutaja Kuumbwa kwa mwanaadamu. Allah تعالى Amesema,

وَبَدَأَ خَلْقَ الْإِنْسَانِ مِن طِينٍ

“...na Akaanzisha Kumuumba mtu kwa udongo.”

Maana yake: Alimuumba Adam عليه السلام, baba wa wanaadamu, kutokana na udongo.

ثُمَّ جَعَلْ نَسْلَهُ مِن سُؤْلِ مِّن مَّاءٍ مَّهِينٍ

“Na kisha Akajaalia uzao wake utokane na kizazi cha maji madhaifu.”

Maana yake: Kadhalika wazaane kutokana na rutubisho la mbegu inayotoka katika viuno vya wanaume na baina ya mbavu za mwanamke.

ثُمَّ سَوَّاهُ

“Kisha Akamtengeneza...”

Maana yake: Adam عليه السلام, baada ya Kumuumba kwa udongo, Alimuumba Akamsawazisha na Akamsimamisha wima.

فِيهِ مِنْ رُوحِهِ ۗ وَجَعَلَ لَكُمْ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ

“...na Akampulizia roho yake, na Akakujaalieni kusikia na kuona, na nyoyo za kufahamu.”

Yaani, akili,

قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿١٠﴾

“Ni uchache mnavyoshukuru.”

Maana yake: Kwa nguvu hizi Alizokuruzukuni Allah تعالى. Mtu mwema ni yule mwenye kuzitumia katika kumtii Mola Wake.

وَقَالُوا أَإِذَا ضَلَلْنَا فِي الْأَرْضِ أَإِنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ ۗ بَلْ هُمْ بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ كَافِرُونَ ﴿١١﴾
 قُلْ يَتَوَفَّيْكُمْ مَلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١٢﴾

10. “Nao husema: Tutapokwishapotea chini ya ardhi, ni kweli tutarudishwa katika umbo jipya? Bali wao wanakanusha kwamba watakutana na Mola wao Mlezi.”

11. “Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa juu yenu; kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu Mlezi.”

Jibu kwa Wale Wanaokanusha Kufufuliwa

Allah تعالى Anaeleza Kuhusu washirikina ambao walikanusha kufufuliwa, pindi waliposema:

أَإِذَا ضَلَلْنَا فِي الْأَرْضِ

“Tutapokwisha potea chini ya ardhi...”

Yaani, miili yetu imechanika na imegawanyika ardhini na kupotea,

أَإِنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ

“...ni kweli tutarudishwa katika umbo jipya?”

Yaani, “Kweli tutarejea kutoka katika hali hiyo?” Kuona kwao kuwa hili haliwezekani ni kwa mnasaba wa uwezo wao dhaifu, si kwa mnasaba wa

Aliyewaanzisha, Akawaumba kutoka katika kutokuwepo, Ambaye Akitaka jambo Huliambia “Kuwa,” nalo huwa. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema,

بَلْ هُمْ بِلِقَاءِ رَبِّهِمْ كَافِرُونَ ﴿٣١﴾

“Bali wao wanakanusha kwamba watakutana na Mola wao Mlezi.”

Kisha Allah تعالی Amesema,

﴿ قُلْ يَتَوَفَّنَا مَلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ بِكُمْ ﴾

“Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa juu yenu...”

Lililo dhahiri katika Aya hii, ni kwamba, Malaika wa Mauti ni nafsi makhususi iliyoteuliwa miongoni mwa Malaika. Ni kama ilivyo wazi pia katika Hadithi ya Al-Barau tuliyoinkuu katika Tafsiri ya *Surat Ibrahim*.¹ Qatadah na wengine walisema kwamba Malaika wa mauti ana wasaidizi.²

Hivi ndivyo ilivyonukuliwa katika Hadithi, kwamba wasaidizi wake hutoa roho kutoka sehemu mbali mbali za mwili, mpaka inapofika katika koromeo, basi Malaika wa Mauti huichukua. Mujahid alisema: “Dunia imekusanywa pamoja na kufanywa mithili ya beseni, na yeye huchukua kutoka humo, katika muda wowote autakao.”³ Kauli ya Allah تعالی,

﴿ ثُمَّ إِلَيَّ رَبُّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴾

“...kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu Mlezi.”

Yaani, Siku ya Marejeo yenu na kusimama kwenu kutoka makaburini kwenu, kwa ajili ya malipo yenu.

* * *

¹ Angalia Tafsiri ya Surat Ibrahim (14:27).

² At-Tabari 20:175.

³ At-Tabari 20:175.

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ
 رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا
 مُوقِنُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدًىٰ وَلٰكِنْ
 حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ
 أَجْمَعِينَ ﴿٦٧﴾ فَذُوقُوا بِمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا إِنَّا
 نَسِينَاكُمْ ۖ وَذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾
 إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا الَّذِينَ إِذَا ذُكِرُوا بِهَا حُزُوا سُجَّدًا
 وَسَبَّحُوا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٦٩﴾
 تَتَجَافَىٰ جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا
 وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٧٠﴾ فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا
 أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾
 أَفَمَن كَانَ مُؤْمِنًا كَمَن كَانَ فَاسِقًا ۗ لَا يَسْتَوُونَ ﴿٧٢﴾
 أَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ جَنَّاتُ الْمَأْوَىٰ
 نُزُلًا ۖ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧٣﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فَسَقُوا فَمَأْوَاهُمُ
 النَّارُ ۖ كُلَّمَا أَرَادُوا أَن يَخْرُجُوا مِنْهَا أُعِيدُوا فِيهَا وَقِيلَ لَهُمْ
 ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنْتُمْ بِهِ تَكَذِّبُونَ ﴿٧٤﴾
 وَلَتُدْفَعُنَّهُمْ مِنَ الْعَذَابِ الْأَلَدِيِّ دُونَ الْعَذَابِ الْأَكْبَرِ
 لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٧٥﴾ وَمَن أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ
 ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا ۗ إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ ﴿٧٦﴾

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا
 رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا
 وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا
 مُوقِنُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ
 نَفْسٍ هُدًىٰ وَلٰكِنْ حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي
 لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ
 أَجْمَعِينَ ﴿٦٧﴾ فَذُوقُوا بِمَا نَسِيتُمْ
 لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا إِنَّا نَسِينَاكُمْ ۖ
 وَذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ بِمَا كُنْتُمْ
 تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾

12. "Na ungeliliwaona wakosefu wanavyoinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao Mlezi, (wakisema): Mola wetu Mlezi! Tumeshana, na Tumeshasikia. Turejeshe tukatende mema, kwani hakika sisi tumekwishakuwa na yakini sasa."

13. "Na lau Tungelitaka Tungempa kila mtu uwongofu wake. Lakini imekwishakuwa kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahannamu

kwa wote hawa, majini na watu."

14. “Basi onjeni kwa vile mlivyousahau mkutano wa Siku yenu hii. Na Sisi hakika Tunakusahauni. Basi onjeni adhabu ya milele kwa yale mliyokuwa mkiyatenda.”

Hali ya washirikina Siku ya Kufufuliwa

Allah تعالى Anaeleza hali za washirikina zitakavyokuwa katika Siku ya Kiyama na watakachokisema pindi watakapoona kufufuliwa na kusimama mbele ya Allah تعالى wakiwa duni waliodhalilika huku vichwa vyao wameinamisha chini, yaani kutokana na aibu na fedheha, huku wakisema:

رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا

“...Mola wetu Mlezi! Tumshaona, na tumeshasikia.”

Yaani, “Sisi kwa sasa tunasikia kauli yako na tunatii Amri Yako,” Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

أَسْمِعْ بِهِمْ وَأَبْصِرْ يَوْمَ يَأْتُونَنَا

“Watasikia na wataona vizuri vilioje Siku watakayotujia!” (19:38)

Kadhalika, watajirudi nafsini mwao na kulaumiana, pindi watakapoingia Motoni. Watasema:

لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦٧﴾

“Lau kuwa tungelisikia, au tungelikuwa na akili, tusingelikuwa katika watu wa Motoni!” (67:10)

Kadhalika, watasema,

رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا

“...Mola wetu Mlezi! Tumshaona, na tumeshasikia. Turejeshe...”

Yaani, duniani,

نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿٦٨﴾

“...tukatende mema, kwani hakika sisi tumekwisha kuwa na yakini sasa.”

Maana yake: “Tumeshakuwa na yakini na uhakika kwamba Ahadi Yako ni ya kweli, na kwamba kukutana Nawe ni kweli. Mola wako تعالى Anajua zaidi kwamba lau kama Atawarudisha duniani watakuwa kama walivyokuwa hapo awali, makafiri, wakadhibishaji wa *dalili* za Allah تعالى na kuwakhaliifu Mitume Wake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَىٰ النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتَنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِبِعَابَتِ رَبِّنَا

“Na ungeona watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi...” (6:27)

Katika Aya hii alisema,

وَلَوْ شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدًى

“Na lau Tungelitaka Tungempa kila mtu uwongofu wake.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلَّهُمْ جَمِيعًا

“Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi.” (10:99)

وَلَيْكِنَ حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿٣٢﴾

“Lakini imekwishakuwa Kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahannamu kwa wote hawa, majini na watu.”

Yaani, kutoka kwa viumbe wa namna mbili, makazi yao ni Motoni, wala hawatakuwa na pa kutorokea wala njia ya kutokea. Tunajikinga kwa Allah تعالى na Maneno Yake Timilifu, dhidi ya hayo,

فَذُوقُوا بِمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا

“Basi onjeni kwa vile mlivyou sahau mkutano wa Siku yenu hii.”

Maana yake: Watu wa Motoni wataambiwa kwa namna ya kukaripiwa: “Onjeni

adhabu hii, kwa sababu ya kuikadhibisha kwenu na kunena kwenu kwamba haitakuwepo na kuisahau kwenu, kwani mliifanyia vitendo vya mtu mwenye kuisahau.”

إِنَّا نَسِينَكُم

“...Na Sisi hakika Tunakusahauni.”

Tutakufanyieni namna afanyavyo msahaulivu, hata hivyo Allah تعالی Hasahau kitu, wala hapotelewi nacho, bali hiyo ni namna ya kuwakabili.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

الْيَوْمَ نَنسَدُكُمْ كَمَا نَسَيْتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا

“Leo Tunakusahauni kama nyinyi mlivyosahau mkutano wa siku yenu hii...” (45:34)

Kauli ya Allah تعالی,

وَذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

“Basi onjeni adhabu ya milele kwa yale mliyokuwa mkiyatenda.”

Yaani, kwa sababu ya kufuru yenu na ukadhibishaji wenu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

لَا يَذُوقُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿١٥﴾ إِلَّا حَمِيمًا وَغَسَاقًا ﴿١٦﴾

“Hawataonja humo chochote kibaridi wala kinywaji, Ila maji ya moto sana na usaha.”

Mpaka Kauli Yake Allah تعالی,

فَلَنْ نَّزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿١٧﴾

“Nasi hatutakuzidishieni ila adhabu!” (78:30)

إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا الَّذِينَ إِذَا ذُكِرُوا بِهَا حُزُوا سُجَّدًا وَسَبَّحُوا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا
 يَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٢﴾ تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا
 رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٣﴾ فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

15. *"Hakika wanaoziamini Aya Zetu ni hao tu ambao wakikumbushwa hizo, basi wao huanguka kusujudu, na humsabihi Mola wao Mlezi kwa kumhimidi, nao hawajivuni."*

16. *"Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumuomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na Tulivyowaruzuku."*

17. *"Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho - ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda."*

Hali ya Watu wa Imani na Malipo yao

Allah تعالیٰ Anasema:

إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا

"Hakika wanaoziamini Aya Zetu..."

Yaani, kwa hakika huzisadiki,

الَّذِينَ إِذَا ذُكِرُوا بِهَا حُزُوا سُجَّدًا ﴿١٢﴾

"...ni hao tu ambao wakikumbushwa hizo, basi wao huanguka kusujudu..."

Yaani, huzisikiliza, wakazitii kwa kauli na matendo.

وَسَبَّحُوا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٣﴾

"...na humsabihi Mola wao Mlezi kwa kumhimidi, nao hawajivuni."

Yaani, kuacha kumfuata na kumnyenyekea namna wafanyavyo majahili. Amesema Allah تعالى،

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦٠﴾

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.” (40:60)

Kisha Allah تعالى Amesema،

تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ

“Mbavu zao zinaachana na vitanda...”

Hiyo inamaanisha kusimama usiku na kuacha kulala au kujilaza katika matandiko yenye kustarehesha. Mujahid na Al-Hasan waliizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ

“Mbavu zao zinaachana na vitanda...”

Hiyo inamaanisha *Qiyamul-Layl* (Sala ya usiku).¹ Adh-Dhahhak alisema: “Ni Swala ya Isha pamoja na jamaa, na Swala ya Alfajiri katika Swala ya jamaa.

يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا

“...kwa kumuomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini...”

Yaani, kwa kukhofia matata ya Adhabu Yake na kuwa na matumaini na Thawabu Zake nyingi.

وَمِمَّا زَرَعْتَهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٦١﴾

“...na hutoa kutokana na Tulivyowaruzuku.”

Hivyo wanafanya matendo ya Faradhi na Sunna. Kiongozi wao duniani na Akhera ni Mtume ﷺ. Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Mu’adh bin Jabal رضي الله عنه alisema: Siku moja asubuhi nilikuwa nasafiri pamoja na Mtume ﷺ nikiwa karibu naye huku sote tukiwa katika mwendo. Nikasema: “Ewe Mtume!

¹ At-Tabari 20:180.

Nifahamishe amali itakayoniingiza Peponi na kuniweka mbali na Moto.”
Alisema:

«لَقَدْ سَأَلْتُ عَنْ عَظِيمٍ وَإِنَّهُ لَيَسِيرٌ عَلَى مَنْ يَسَّرَهُ اللَّهُ عَلَيْهِ، تَعْبُدُ اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُ بِهِ
شَيْئًا، وَتُقِيمُ الصَّلَاةَ وَتُؤْتِي الزَّكَاةَ، وَتَصُومُ رَمَضَانَ، وَتَحُجُّ الْبَيْتَ»

“Umeuliza juu ya jambo kubwa, na ni jepesi kwa aliyerahisishiwa na Allah. Umwabudu Allah, wala usimshirikishe na kitu chochote, usimamishe Swala, utoa Zaka, ufunge katika mwezi wa Ramadhani na uhiji katika Nyumba tukufu.”

Kisha akasema:

«أَلَا أَدُلُّكَ عَلَىٰ أَبْوَابِ الْخَيْرِ؟ الصَّوْمُ جُنَّةٌ، وَالصَّدَقَةُ تُطْفِئُ الْخَطِيئَةَ، وَصَلَاةُ
الرَّجُلِ فِي جَوْفِ اللَّيْلِ»

“Nikujulishe juu ya milango ya kheri? Saumu ni ngao, Sadaka huyafuta madhambi na Swala ya mtu katika usiku wa manane.”

Halafu akasoma:

تَتَجَافَىٰ جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ

“Mbavu zao zinaachana na vitanda...” Mpaka akafikia,

جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٤٧﴾

“...ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda.”

Kisha akasema:

«أَلَا أَخْبِرُكَ بِرَأْسِ الْأَمْرِ وَعَمُودِهِ وَذِرْوَةِ سَنَامِهِ؟»

“Nikuambie kitu kikubwa kuliko yote, nguzo zake na kilele chake?”

Nikasema: “Ndiyo, ewe Mtume wa Allah.” Akasema:

«رَأْسُ الْأَمْرِ الْإِسْلَامُ، وَعَمُودُهُ الصَّلَاةُ، وَذِرْوَةُ سَنَامِهِ الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

“Msingi wa mambo yote ni Uislamu, moja ya nguzo zake ni Swala na Kilele chake ni Jihadi katika njia ya Allah.”

Kisha akasema:

«أَلَا أَخْبِرُكَ بِمَلَايِكَةِ ذَٰلِكَ كُتُبِهِ؟»

“Nikujulishe kinachoyamiliki yote hayo?”

Nikasema: “Ndiyo, ewe Mtume wa Allah.” Akashika ulimi wake, halafu akasema:

«كُفَّ عَلَيْكَ هَٰذَا»

“Jizuilie dhidi ya huu.”

Nikasema: “Ewe Mtume wa Allah! Tutawajibika kwa tuyasemayo?” Akasema:

«نَكَيْتَكَ أَتُكُّ يَا مُعَاذُ، وَهَلْ يَكُفُّ النَّاسَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ - أَوْ قَالَ: عَلَىٰ
مَنَاخِرِهِمْ - إِلَّا حَصَانِدُ أَلْسِنَتِهِمْ»

“Mama yako awe mkiwa dhidi yako Mu’adh! Je watu watatupwa Motoni juu ya nyuso zao au pua zao kwa lipi? Alisema – Isipokuwa ni kwa mavuno ya ndimi zao?”¹

Ameinukuu At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah, na At-Tirmidhi alisema: “Ni Hasan Sahih.”² Kauli ya Allah تعالى،

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ

“Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho...”

Hakuna anayeujua ukubwa ambao Allah تعالى Ameuficha katika Pepo, miongoni mwa neema nzuri za kudumu, ambazo hapana aliyewahi kuziona. Kutokana na watu kuzificha amali zao, basi Naye Allah تعالى Amezificha thawabu zao. Ni malipo yenye kuwafikiana kabisa, kwani malipo ni katika jinsi ya amali yenyewe. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema: “Watu wamezificha amali zao, basi Naye Allah تعالى Akaficha kwa ajili yao, mambo ambayo hapana jicho lilowahi kuyaona, wala haikupita fikra katika moyo wa mwanaadamu.”

¹ Ahmad 5:231.

² Tuhfatul Al-ahwadhi 7:362, An-Nasai katika Al-Kubra 6:428, Ibn Majah 2:1314.

Ameyanukuu haya Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى. Bukhari amesema, Kauli ya Allah تعالى،

فَلَا تَعَلَّمُ نَفْسٌ مَّا أَخْفَىٰ لَهُمْ مِّن قُرْءَانٍ مِّن قُرْءَانٍ

“Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho...”

Kisha alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«قَالَ اللَّهُ تَعَالَى: أَعَدَدْتُ لِعِبَادِي الصَّالِحِينَ مَا لَا عَيْنٌ رَأَتْ، وَلَا أُذُنٌ سَمِعَتْ، وَلَا خَطَرَ عَلَى قَلْبِ بَشَرٍ»

“Allah Amesema: ‘Nimewaandalia waja wangu wema ambayo hapana jicho lililoona, wala sikio kusikia, wala haikuingia katika fikra za mtu.”

Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: “Mkitaka, someni:

فَلَا تَعَلَّمُ نَفْسٌ مَّا أَخْفَىٰ لَهُمْ مِّن قُرْءَانٍ مِّن قُرْءَانٍ

“Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho.”¹

Ameinukuu Muslim na At-Tirmidhi. At-Tirmidhi amesema, *“Hasan Sahih.”²* Na katika nukuu ya Bukhari kuna Hadithi hii:

«وَلَا خَطَرَ عَلَى قَلْبِ بَشَرٍ، ذُخْرًا مِّن بَلَاءٍ مَّا أُطْلِعْتُمْ عَلَيْهِ»

“...Wala haijawahi kuingia katika moyo wa mtu. Kila mlichowahi kukiona si kitu ukilinganisha na mlichotunziwa.”³

Abu Hurayrah رضي الله عنه, tena, amesema, Mtume ﷺ amesema:

¹ Fat’hul Al-Bari 8:375.

² Muslim 4:2174, Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:56.

³ Fat’h ul Al-Bari 8:375.

«مَنْ يَدْخُلِ الْجَنَّةَ يَنْعَمَ لَا يَأْسَ، لَا تَبْلَى ثِيَابُهُ، وَلَا يَفْنَى شَبَابُهُ، فِي الْجَنَّةِ مَا لَا عَيْنٌ رَأَتْ، وَلَا أُذُنٌ سَمِعَتْ، وَلَا خَطَرَ عَلَى قَلْبِ بَشَرٍ»

“Atakayeingia Peponi atapata neema, wala hapunjiki, nguo zake hazitachakaa, wala ujana wake hautaisha. Peponi kuna ambayo hapana jicho lolote lililoyaona, wala sikio lililosikia, wala haikupita katika fikra za mwanaadamu.”¹

أَفَمَنْ كَانَ مُؤْمِنًا كَمَنْ كَانَ فَاسِقًا ۗ لَا يَسْتَوُونَ ﴿١٨﴾ أَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ جَنَّاتُ الْمَأْوَى نُزُلًا بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فَسَقُوا فَمَأْوَاهُمُ النَّارُ ۗ كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا أُعِيدُوا فِيهَا وَقِيلَ لَهُمْ ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنتُمْ بِهَا تَكْذِبُونَ ﴿٢٠﴾ وَلَنُذِيقَنَّهُمْ مِنَ الْعَذَابِ الْأَلَدِّ دُونَ الْعَذَابِ الْأَكْبَرِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢١﴾ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا ۗ إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ ﴿٢٢﴾

18. “Ati aliye Muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa.”

19. “Ama walioamini na wakatenda mema, watakuwa nazo Bustani za makaazi mazuri. Ndio pa kufikia kwa waliyokuwa wakiyatenda.”

20. “Na ama wale waliotenda uovu, basi makazi yao ni Motoni. Kila wakitaka kutoka humo watarudishwa humo humo. Na wataambiwa: Onjeni adhabu ya Moto ambayo mliyokuwa mkiikanusha.”

21. “Na Tutawaonjesha adhabu khafifu kabla ya adhabu kubwa, huenda labda watarejea.”

22. “Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa kwa Ishara za Mola wake Mlezi, kisha akazikataa? Hakika Sisi Tutajilipiza kwa wakosefu.”

¹ At-Tabari 20:186, Muslim 4:2181.

Muumini na Fasiki Hawako Sawa

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Uadilifu na Ukarimu Wake kwamba Hatawaweka sawa katika Hukumu Siku ya Kiyama, waliokuwa wakiziamini Aya Zake na wafuasi wa Rasuli Wake pamoja na waliokuwa mafasiki, yaani ambao walikuwa nje ya kumtii Mola wao, wakadhibishaji wa Mitume wa Allah تعالى waliotumwa kwao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ اجْتَرَحُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ نَجْعَلَهُمْ كَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَوَاءٌ
مَحْيَاهُمْ وَمَمَاتُهُمْ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٢١﴾

“Je! Wanadhani wanaotenda maovu kuwa Tutawafanya kama walioamini, na wakatenda mema, sawa sawa uhai wao na kufa kwao? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu!” (45:21).

أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ
كَالْفُجَّارِ ﴿٢٨﴾

“Je! Tuwafanye walioamini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au Tuwafanye wachamungu kama waovu?” (38:28)

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.” (59:20)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema,

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ

“Ati aliye muumini atakuwa sawa na aliye mpotovu? Hawawi sawa.”

Yaani, mbele ya Allah تعالى katika Siku ya Kiyama. ‘Ataa bin Yasaar, As-Suddi na wengine walisema kwamba Aya hiyo iliteremshwa kumhusu ‘Ali bin Abu

Twalib na 'Uqbah bin Abu Mu'aytaw رضي الله عنهما¹. Kwa hivyo, Allah تعالى Amehukumu baina yao, akasema:

أَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Ama walioamini na wakatenda mema.”

Yaani, nyoyo zao zimesadiki Aya za Allah تعالى, na wakatenda kulingana na hukumu ya Allah تعالى, yaani amali njema,

فَلَهُمْ جَنَّاتُ الْمَأْوَىٰ

“Watakuwa nazo Bustani za makazi mazuri.”

Maana yake: Ambazo zina makazi, majengo na maghorofa marefu,

رُؤًى

“Ndio pa kufikia...”

Yaani, kukaribishwa ugeni na kufanyiwa ukarimu,

بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٢﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فَسَقُوا

“...kwa waliyokuwa wakiyatenda. Na ama wale waliotenda uovu...”

Yaani, wametoka nje ya twaa, basi makazi yao ni Motoni. Kila wakitaka kutoka humo, hurudishwa humo humo.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ تَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا

“Kila wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo...” (22:22)

Al-Fadhili bin 'Iyaadh alisema: “Wallah! Mikono na miguu yao itafungwa, na kwamba moto wenye miale utawainua wao, na huku Malaika wakiwaswaga wao.”

¹ At-Tabari 20:188.

وَقِيلَ لَهُمْ ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنتُمْ بِهَا تُكذَّبُونَ ﴿١٢﴾

“Na wataambiwa: Onjeni adhabu ya Moto ambayo mlikuwa mkiikanusha.”

Yaani, hayo wataambiwa kwa kukaripiwa, Kauli ya Allah تعالى

وَلَنذِيقَنَّهُمْ مِنَ الْعَذَابِ الْأَلَدِّ نَ دُونَ الْعَذَابِ الْأَلَمِّ

“Na Tutawaonjisha adhabu khafifu kabla ya adhabu kubwa”.

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, maana ya adhabu ndogo ni misiba ya kidunia, maradhi na matatizo yake. pamoja na mambo yanayopita kwa wakazi wake ili watubie Kwake.¹ Imesimuliwa mithili ya hivyo, kutoka kwa Ubayy bin Ka'b, Abu Al-'Aliyah, Al-Hasan, Ibrahim An-Nakha'i, Adh-Dhahhak, 'Alqamah, 'Atiyah, Mujahid, Qatadah, 'Abdul-Karim Al-Jazari na Khuswayf² رضي الله عنهم. Kauli ya Allah تعالى

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِقَاتِلِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا

“Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa kwa Ishara za Mola wake Mlezi, kisha akazikataa?”

Yaani, hakuna dhalimu zaidi ya yule ambaye, Allah تعالى Amemkumbusha Aya Zake, Akambainishia na Kumdhirishia, kisha, baadaye anaziacha na kuzikana, anazipa mgongo na kuzisahau kama vile hazijui. Qatadah amesema: “Ole wenu mnaopuza kumkumbuka Allah تعالى kwani mwenye kuacha kumkumbuka Allah تعالى atakuwa amejipumbaza pumbaziko kubwa, amepata ufakiri mkubwa na amefanya dhambi iliyo kubwa mno. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alimkhofisha mwenye kuyafanya haya, kwa kusema,

إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ ﴿١٣﴾

“Hakika Sisi tutajilipiza kwa wakosefu.”

Yaani, “Tutalipiza kisasi kikali Sisi wenyewe dhidi ya wenye kuyafanya hayo”

* * *

¹ At-Tabari 20:189.

² At-Tabari 20:189, 190.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَلَا تَكُن فِي مِرْيَةٍ مِّن لِّقَائِهِ
 وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٣٢﴾ وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَيْمَةً
 يَهْتَدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا ۖ وَكَانُوا بِبَايِعَتِنَا يُوقِنُونَ
 ﴿٣٣﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا
 كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٣٤﴾ أَوْلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا
 مِن قَبْلِهِمْ مِّنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَةً ۖ أَفَلَا يَسْمَعُونَ ﴿٣٥﴾ أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَسُوقُ الْمَاءَ
 إِلَى الْأَرْضِ الْجُرُزِ فَنُخْرِجُ بِهِ زَرْعًا تَأْكُلُ مِنْهُ أَنْعَامُهُمْ
 وَأَنْفُسُهُمْ ۖ أَفَلَا يُبْصِرُونَ ﴿٣٦﴾ وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا
 الْفَتْحُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٧﴾ قُلْ يَوْمَ الْفَتْحِ لَا يَنْفَعُ
 الَّذِينَ كَفَرُوا إِيمَانُهُمْ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٣٨﴾ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ
 وَانْتَظِرْ إِنَّهُمْ مُنْتَضِرُونَ ﴿٣٩﴾

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَلَا
 تَكُن فِي مِرْيَةٍ مِّن لِّقَائِهِ ۖ وَجَعَلْنَاهُ
 هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ۖ وَجَعَلْنَا
 مِنْهُمْ أَيْمَةً يَهْتَدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا
 صَبَرُوا ۖ وَكَانُوا بِبَايِعَتِنَا يُوقِنُونَ
 ﴿٣٣﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ
 يَخْتَلِفُونَ ﴿٣٤﴾

23. "Hakika Sisi Tulikwi-shampa Musa Kitabu. Basi usiwe na shaka kuwa kakipokea. Na tukakifanya kuwa ni uwongofu kwa Wana wa Israili."

24. "Na Tukawafanya miongoni mwao waongozi wanaoongoa watu kwa Amri Yetu, waliposubiri na wakawa na yakini na Ishara Zetu."

25. "Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Atakayefafanua baina yao Siku ya Kiyama katika waliyokuwa wakikhitalifiana."

Kitabu cha Musa عليه السلام na Uongozi wa Wana wa Israil

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Mja na Mtume Wake Musa عليه السلام, kwamba Yeye Alimpa Kitabu, nacho ni Taurati. Kauli ya Allah تعالى,

فَلَا تَكُن فِي مِرْيَةٍ مِّن لِّقَائِهِ

"Basi usiwe na shaka kuwa kakipokea."

Qatadah alisema: "Inamaanisha usiku wa *Isra*."¹ Kisha alisimulia kwamba Abu 'Aliyah Ar-Riyaahi alisema: Alinisimulia mtoto wa ami ya Mtume wenu, yaani, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, amesema, Mtume ﷺ amesema:

«أَرَيْتُ لَيْلَةَ أُسْرِي بِي مُوسَىٰ بَنَ عِمْرَانَ رَجُلًا آدَمَ طَوَالًا جَعْدًا كَأَنَّهُ مِنْ رَجَالِ
شَنْوَةَ، وَرَأَيْتُ عَيْسَىٰ رَجُلًا مَرْبُوعَ الْخَلْقِ إِلَى الْحُمْرَةِ وَالْبَيَاضِ، سَبَطَ الرَّأْسِ،
وَرَأَيْتُ مَالِكًا خَازِنَ النَّارِ وَالِدَ الْجَالِ»

"Katika usiku niliopelekwa Israi, nilimwona Musa bin 'Imran akiwa ni mtu mrefu mwenye rangi ya kahawia na nywele za singa, akionekama kama mtu wa kutokea Shanu-ah. Nimemwona Isa, mtu wa umbo la wastani na rangi nyeupe yenye wekundu, akiwa na nywele zilizonyooka. Pia nilimwona Malik, mtunzaji wa Moto na Ad-Dajjal."

Miongoni mwa Aya ambazo Allah تعالى alimuonesha zilikuwa:

فَلَا تَكُنْ فِي مِرْيَةٍ مِّنْ لِّقَائِهِ

"Basi usiwe na shaka kuwa kakipokea."

Yaani, "alikwishamuona Musa عليه السلام na akakutana naye katika Usiku wa *Israi*."²

Kauli ya Allah تعالى،

وَجَعَلْنَاهُ

"Na Tukakifanya..."

Yaani, Kitabu Tulichompatia,

هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٢٦﴾

"...kuwa ni uwongofu kwa Wana wa Israili."

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى، katika *Surat Al-Isra*,

¹ At-Tabari 20:193.

² At-Tabari 20:194.

وَأَتَيْنَا مُوسَىٰ آلَ كِتَابٍ وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا تَتَّخِذُوا مِن دُونِي وَكَيْلًا ﴿٢٣﴾

“Na Tukampa Musa Kitabu, na Tukakifanya uwongofu kwa Wana wa Israili. (Tukawambia): Msiwe na mtegemewa ila Mimi!” (17:2)

وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَيْمَةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا وَكَانُوا بِآيَاتِنَا يُوقِنُونَ ﴿٢٤﴾

“Na Tukawafanya miongoni mwao waongozi wanaoongoa watu kwa Amri Yetu, waliposubiri na wakawa na yakini na Ishara Zetu.”

Kwa kuwa walikuwa na subira katika kushika Amri za Allah تعالى, kuacha makatazo Yake, kuwasadiki Mitume Wake na kuwafuata katika waliyokuja nayo, kulikuwa na viongozi miongoni mwao ambao waliwaongoza wengine kwenye ukweli, kwa Amri ya Allah تعالى; wanaamrisha mema na kukataza maovu. Kisha, baada ya wao kubadilisha na kugeuza (Maneno ya Allah تعالى) na kupindua, walinyang’anywa nafasi hiyo, na nyoyo zao zikawa ngumu, huku wakiyageuzageuza Maneno ya Allah تعالى kwa kuyatoa mahala pake, kwa hivyo hawakufanya amali njema wala itikadi sahihi. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema,

وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَيْمَةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا

“Na Tukawafanya miongoni mwao waongozi wanaoongoa watu kwa Amri Yetu, waliposubiri ...”

Qatadah na Sufyan wamesema: “Waliposubiri kwa kuipa mgongo dunia.” Al-Hasan bin Swalih amesema: Sufyan amesema: “Hivi ndivyo hao walivyokuwa. Wala haitakikani mtu kuwa kiongozi anayefuatwa, isipokuwa mpaka ayaache mambo ya kidunia.” Hivyo, Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ آتَيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ آلَ كِتَابٍ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى

الْعَالَمِينَ ﴿٢٥﴾ وَأَتَيْنَاهُم بَيِّنَاتٍ مِّنَ الْأَمْرِ

“Na hakika Tuliwapa Wana wa Israili Kitabu na hukumu na Unabii, na Tukawaruzuku vitu vizuri, na Tukawafadhilisha kuliko walimwengu. Na Tukawapa maelezo wazi ya Amri.” (45:16-17)

Ni kama Alivyosema katika Aya hii,

إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٢٦﴾

“Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Atakayefafanua baina yao Siku ya Kiyama katika waliyokuwa wakikhitalifiana.”

Yaani, kuhusu itikadi na amali mbalimbali.

أَوَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ أَفَلَا يَسْمَعُونَ ﴿٢٧﴾ أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَسُوقُ الْمَاءَ إِلَى الْأَرْضِ الْجُرُزِ فَنُخْرِجُ بِهِ زَرْعًا تَأْكُلُ مِنْهُ أَنْعَامُهُمْ وَأَنْفُسُهُمْ أَفَلَا يُبْصِرُونَ ﴿٢٨﴾

26. “Je! Haijawabainikia kwamba kaumu ngapi Tuliziangamiza kabla yao, nao wanapita katika maskani zao hizo? Hakika katika hayo zipo Ishara. Basi, je, hawasikii?”

27. “Je! Hawaoni ya kwamba Tunayapeleka maji kwenye ardhi kavu, kisha kwayo Tunaitoa mimea wanayokula wanyama wao na wao wenyewe? Je! Hawaoni?”

Jifunzeni Kutokana na Yaliyopita

Allah تعالى Anasema, Wakadhibishaji hawa nao hawaongoki kwa kutomfuata Mtume, kwani Allah تعالى Aliuangamiza umma wa watu walizokuwa kabla yao kutokana na kukadhibisha Mitume wao, na kukhalifu waliyokuja nayo katika njia iliyonyooka. Basi, hapana yeyote kati yao aliyesalia, wala dhati wala athari.

هَلْ نَحْسُ مِنْهُمْ مِّنْ أَحَدٍ أَوْ تَسْمَعُ لَهُمْ رِكْرًا ﴿٢٩﴾

“Je! Unawaona hata mmoja katika wao au unasikia hata mchakato wao?” (19:98)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ

“...wanapita katika maskani zao hizo?”

Yaani, wakadhibishaji hawa wanapita katika maskani ya wakadhibishaji hao walioangamizwa, lakini hawamwoni yeyote katika waliokuwa wakiishi humo na kupastawisha, wamefutika.

كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا

“Kama kwamba hawakuwako huko.” (11:95)

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَتِلْكَ بُيُوتُهُمْ خَاوِيَةٌ بِمَا ظَلَمُوا

“Basi hizo nyumba zao ni tupu kwa sababu ya walivyodhulumu.” (27:52)

Na Amesema,

فَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ فِيهَا خَاوِيَةٌ عَلَى عُرُوشِهَا وَيَبْرِ مَعْطَلَةٍ وَقَصْرِ مَشِيدٍ ﴿٥٤﴾ أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ

“Miji mingapi Tuliangamiza iliyokuwa ikidhulumu, ikawa imebaki magofu, na visima vilivyoachwa, na majumba yaliyokuwa madhubuti? Je! Hawatembei katika ardhi...” (22:45-46).

Hadi Kauli Yake;

وَلَكِن تَعْمَى الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ ﴿٥٥﴾

“...lakini zinazopofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.”

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema katika Aya hii,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً

“Hakika katika hayo zipo Ishara.”

Yaani, katika kuondoka kaumu hizo, kuangamizwa kwao na yaliyowakumba ni kwa sababu ya kukadhibisha Mitume wao. Kunusurika kwa waliowaamini ni ishara, mazingatio, mawaidha na dalili muhimu.

أَفَلَا يَسْمَعُونَ ﴿٥٦﴾

“Basi, je, hawasikii?”

Yaani, kuhusu khabari za waliotangulia kwamba jambo gani liliwatokea.

Kuhuishwa Ardhi kwa maji ni Ushahidi wa Kufufuliwa

Kauli ya Allah تعالى،

أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَسُوقُ الْمَاءَ إِلَى الْأَرْضِ الْجُرُزِ

“Je! Hawaoni ya kwamba Tunayapeleka maji kwenye ardhi kavu...”

Allah تعالى Anabainisha Upole Wake kwa viumbe Wake na Ihsani Yake kwao, kwa Kuwapelekea maji, ama kutoka angani au kutokana na maji yatiririkayo ardhini, yanayopita katika mito kutoka milimani mpaka katika ardhi inayoyahitaji katika wakati wake. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

إِلَى الْأَرْضِ الْجُرُزِ

“...kwenye ardhi kavu...”

Nayo, ni ambayo haina mimea. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَأِنَّا لَجَنَعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيدًا جُرُزًا ﴿٨﴾

“Na hakika Sisi Tutavifanya vyote vilio juu ya ardhi kuwa kama nchi iliopigwa na ukame.” (18:8)

Yaani kavu isiyo na mimea. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَسُوقُ الْمَاءَ إِلَى الْأَرْضِ الْجُرُزِ فَنُخْرِجُ بِهِ زَرْعًا تَأْكُلُ مِنْهُ أَنْعَامُهُمْ

وَأَنْفُسُهُمْ أَفَلَا يُبْصِرُونَ ﴿١٦﴾

“Je! Hawaoni ya kwamba Tunayapeleka maji kwenye ardhi kavu, kisha kwayo Tunaitoa mimea wanayokula wanyama wao na wao wenyewe? Je! Hawaoni?”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ إِلَى طَعَامِهِ ﴿٢٤﴾ أَنَا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ﴿٢٥﴾

“Hebu mtu na atazame chakula chake. Hakika Sisi Tumemimina maji kwa nguvu.” (80:24-25)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَفَلَا يُبْصِرُونَ ﴿٢٧﴾

“Je! Hawaoni?”

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْفَتْحُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٨﴾ قُلْ يَوْمَ الْفَتْحِ لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ

كَفَرُوا إِيمَانُهُمْ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٢٩﴾ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ وَانْتَظِرْ إِنَّهُمْ مُنْتَظَرُونَ ﴿٣٠﴾

28. “Wanasema: Ushindi huu ni lini, kama mnasema kweli?”

29. “Sema: Siku ya Ushindi, wale waliokufuru imani yao haitawafaa kitu, wala wao hawatapewa muhula.”

30. “Basi wapuuze, nawe ngoja; hakika wao wanangoja.”

Makafiri Walivyooomba Kuharakishiwa Adhabu na Kujibiwa Kwao

Allah تعالى Anaeleza juu ya makafiri kutaka kwao kuharakishiwa adhabu ya Allah تعالى na kuletwa kwa ghadhabu na mateso Yake, kwa kudhani kwamba haitawapata, na kwa sababu ya ukafiri na ukaidi wao.

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْفَتْحُ

“Na Wanasema: Ushindi huu ni lini.”

Yaani, ni lini utatushinda ewe Muhammad? Kama unavyodai kwamba kuna wakati ambapo utatuzidi nguvu na kulipiza kisasi juu yetu, basi yatakuwa lini haya? Sisi hatukuoni wewe na masahaba wako, isipokuwa mnajificha, mna khofu na mmedhalilika.

Kauli ya Allah تعالى,

قُلْ يَوْمَ الْفَتْحِ

“Sema: Siku ya Ushindi...”

Maana yake: Mtakapofikwa na adhabu na ghadhabu za Allah تعالى duniani na Akhera,

لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِيمَانُهُمْ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٣٠﴾

“...wale waliokufuru imani yao haitawafaa kitu, wala wao hawatapewa muhula.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَلَمَّا جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَرِحُوا بِمَا عِنْدَهُمْ مِنَ الْعِلْمِ

“Walipowajia Mitume wao kwa dalili zilizowazi walijitapa kwa ilimu waliyokuwa nayo.” (40:83)

Atakayesema kwamba kusudio la ushindi huu ni ushindi wa Makkah, atakuwa amekwenda mbali sana na amekosea vibaya, kwani, katika Siku ya Ushindi wa Makkah, Mtume ﷺ alikubali kusilimu kwa mateka walioachwa huru. Idadi yao ilikaribia elfu mbili. Kama maana ya Aya hii ilikuwa ni Ushindi wa Makkah, basi asingelikubali kusilimu kwao ni kwa sababu ya Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ يَوْمَ الْفَتْحِ لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِيمَانُهُمْ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٣٠﴾

“Sema: Siku ya Ushindi, wale waliokufuru imani yao haitawafaa kitu, wala wao hawatapewa muhula.”

Makusudio ya *Al-Fat'h* (ushindi) katika Aya hii ni hukumu na upambanuzi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَأَفْتَحُ بَيْنِي وَبَيْنَهُمْ فَتْحًا

“Basi Hukumu baina yangu na wao kwa hukumu Yako.” (26:118)

Pia ni sawa na Kauli nyingine za Allah تعالى:

قُلْ جَمَعُ بَيْنَنَا رُبَّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ ﴿٣٠﴾

“Sema: Mola wetu Mlezi Atatukusanya, kisha Atatuhukumu kwa haki.” (34:26).

Na Allah تعالى Amesema,

وَأَسْتَفْتِحُوا وَحَابَ كُلِّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ ﴿٢٣﴾

“Na wakaomba ushindi, na akashindwa kila jabari mkaidi.” (14:15).

وَكَانُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri.”
(2:89)**

إِنْ تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ

“Kama mnataka hukumu basi hukumu imekwisha kujieni.” (8:19).

فَاعْرِضْ عَنْهُمْ وَأَنْتَظِرُ إِنَّهُمْ مُنْتَظِرُونَ ﴿٢٤﴾

“Basi wapuuze, nawe ngoja; hakika wao wanangoja.”

Yaani, wapuuze hao washirikina na ufikishe uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

اتَّبِعْ مَا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Fuata uliyofunuliwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Hapana mungu ila Yeye.” (6:106)

Na usubiri, kwani Allah تعالى Atayatimiza Aliyokuahidi, na Atakunusuru dhidi ya waliokukhalifu. Hakika, Yeye Havunji miadi.

إِنَّهُمْ مُنْتَظِرُونَ ﴿٢٥﴾

“...hakika wao wanangoja.”

Yaani, wewe unangoja, na wao kadhalika wanapanga hila dhidi yenu,

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَتَرَبَّصُ بِهِ رَيْبَ الْمُنُونِ ﴿٢٦﴾

“Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi, tunamtarajia kupatilizwa na dahari.” (52:30)

'Wewe utayaona matokeo ya subira yako juu yao na juu ya kutekeleza Ujumbe wa Allah تعالی, na katika kunusuriwa kwako na kutiwa kwako nguvu watayaona yatakayofuata baada ya kukungoja wewe na Masahaba wako, watapatwa na mateso mabaya na adhabu ya Allah تعالی kwao.' Allah تعالی Anatutosha, Yeye ni Mbora kabisa wa kumtegemea.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu As-Sajdah*.



Tafsiri ya Suratul Ahzaab

Sura ya 33

Iliteremshwa Madinah

سُورَةُ الْاِحْزَابِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ اتَّقِ اللَّهَ وَلَا تُطِيعِ الْكٰفِرِينَ وَالْمُنٰفِقِينَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ۝ وَأَتَّبِعَ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ۝ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ۝ مَا جَعَلَ اللَّهُ لِرَجُلٍ مِّن قَلْبَيْنِ فِي جَوْفِهِ ۗ وَمَا جَعَلَ أَزْوَاجَكُمُ اللَّائِي تُظَاهَرُونَ مِنْهُنَّ أُمَّهَاتِكُمْ ۗ وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ ۗ ذٰلِكُمْ قَوْلِكُمْ بِأَفْوَاهِكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَقُولُ الْحَقَّ وَهُوَ يَهْدِي السَّبِيلَ ۝ اذْعُوهُمْ لِآبَائِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ ۗ فَإِن لَّمْ تَعْلَمُوا ءَابَاءَهُمْ فإِحْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ وَمَوَالِيكُمْ ۗ وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُمْ بِهِ ۚ وَلٰكِن مَّا تَعَمَّدَتْ قُلُوبُكُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ۝ النَّبِيُّ أَوْلَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنفُسِهِمْ ۗ وَأَزْوَاجُهُ أُمَّهَاتُهُمْ ۗ وَأُوَّلُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ ۗ إِلَّا أَن تَفْعَلُوا إِلَىٰ أَوْلِيَآئِكُمْ مَّعْرُوفًا ۗ كَانَ ذٰلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا ۝

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi
wa Rehema, Mwenye
Kurehemu.

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ اتَّقِ اللَّهَ وَلَا تُطِيعِ الْكٰفِرِينَ وَالْمُنٰفِقِينَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ۝ وَأَتَّبِعَ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ۝ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ۝

1. "Ewe Nabii! Mche Mwenyezi Mungu wala usiwatii makafiri na wanafiki. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima."

2. "Na fuata uliyofunuliwa kwa wahyi kutoka kwa Mola wako Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari ya mnayomatenda."

3. "Na mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni wa kutegemewa."

Amri ya Kutowatii Makafiri na Wanafiki, na Kufuata Wahyi Wake na Kumtegemea Yeye.

Utanabahishaji huu ni wa Mtume pamoja na walio chini yake, kwani Allah تعالی Anapomwamuru mja na Mtume Wake kufanya hivi, basi huwa wa chini yake wana wajibu zaidi kutekeleza hicho alichoamrisha Mtume ﷺ. Twaḥq bin Habib alisema: "Maana ya *Taqwa* ni kumtii Allah تعالی kutokana na Nuru itokayo kwa Allah تعالی na kutarajia malipo ya Allah na kuacha kumuasi Allah تعالی kwa Nuru toka kwa Allah تعالی kwa kukhofu adhabu ya Allah تعالی. Kauli ya Allah تعالی:

وَلَا تُطِيعِ الْكٰفِرِيْنَ وَالْمُنٰفِقِيْنَ

"...wala usiwatii makafiri na wanafiki..."

Yaani, msiwasikilize wala kuwashauri,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٦٠﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima.

Yaani, kwa hivyo, Yeye Ndiye Anayestahiki kufuatwa Amri Zake na Kumtii, kwani Yeye Ndiye Mwenye Kujua mwisho wa mambo yote, ni Mwingi wa Hikima katika Ayafanyayo na katika Kauli Zake. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَأَتَّبِعْ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ

"Na fuata uliyofunuliwa kwa wahyi kutoka kwa Mola wako Mlezi."

Yaani, kutoka katika Qur'an na Sunna,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿٦١﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari ya mnayoyatenda."

Maana yake, hapana chochote cha kufichama dhidi Yake, Yaani katika mambo na hali zako zote,

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni wa kutegemewa.”

Yaani, Allah تعالى Anatosha kuwa wa kumtegemea kwa mwenye kumtegemea na kurudi Kwake.

مَا جَعَلَ اللَّهُ لِرَجُلٍ مِّن قَلْبَيْنِ فِي جَوْفِهِ ۗ وَمَا جَعَلَ أَزْوَاجَكُمُ اللَّائِي تُظَاهِرُونَ مِنهِنَّ
 أُمَّهَاتِكُمْ ۗ وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ ۚ ذَٰلِكُمْ قَوْلِكُمْ بِأَفْوَاهِكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَقُولُ الْحَقَّ وَهُوَ
 يَهْدِي السَّبِيلَ ﴿٥﴾ أَدْعُوهُمْ لِأَبَائِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ ۚ فَإِن لَّمْ تَعْلَمُوا آبَاءَهُمْ
 فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ وَمَوَالِيكُمْ ۗ وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُم بِهِ وَلَٰكِن مَّا
 تَعَمَّدَتْ قُلُوبُكُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٦﴾

4. **“Mwenyezi Mungu Hakumwekea mtu yeyote kuwa ana nyoyo mbili ndani ya mwili wake. Wala Hakuwafanya wake zenu - ambao mnawalinganisha migongo yao na migongo ya mama zenu - kuwa ni mama zenu. Wala Hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa. Hayo ni maneno ya vinywa vyenu tu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Anayesema kweli, Naye Ndiye Anayeongoa Njia.”**

5. **“Waiteni kwa baba zao, maana huo ndio uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa hamuajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika Dini, na rafiki zenu. Wala si lawama juu yenu kwa mlivyokosea. Lakini ipo lawama katika yale ziliyofanya nyoyo zenu kwa makusudi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”**

Kubatilishwa Ubini wa Mtoto wa Hiari

Allah تعالى Anatoa mifano halisi, inayofahamika kiakili, kabla ya Kueleza makusudio. Nayo ni kwamba, kama ambavyo mtu mmoja hawezi kuwa na nyoyo mbili mwilini mwake, na mke wa mtu hawezi kuwa mama yake ikiwa atamtamkia neno la *Dhwihaar* (kuufananisha mgongo wa mkewe na wa mama yake) kwa kumwambia: “Wewe kwangu mimi ni sawa na mgongo wa mama yangu.” Yaani mama yake mume. Kadhalika, mtu akimchukua mtoto wa hiari, hawi ndiye mwanaye halisi.

Allah تعالى Amesema:

مَا جَعَلَ اللَّهُ لِرَجُلٍ مِّن قَلْبَيْنِ فِي جَوْفِهِ ۚ وَمَا جَعَلَ أَزْوَاجَكُمُ اللَّائِي تُظَاهِرُونَ مِنهُنَّ أُمَّهَاتِكُمْ

“Mwenyezi Mungu Hakumuekea mtu yeyote kuwa ana nyoyo mbili ndani ya mwili wake. Wala Hakuwafanya wake zenu - ambao mnawalinganisha migongo yao na migongo ya mama zenu - kuwa ni mama zenu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

مَا هُنَّ أُمَّهَاتُهُمْ ۖ إِنَّ أُمَّهَاتُهُمْ إِلَّا اللَّائِي وَلَدْنَهُمْ

“...hao si mama zao. Hawakuwa mama zao ila wale waliowazaa.”
(58:2)

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ

“Wala Hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa.”

Hii imekusudia kukanusha. Iliteremshwa katika suala la Zayd bin Harithah رضي الله عنه, aliyekuwa mwacha huru wa Mtume ﷺ, alimfanya mwanaye wa hiari kabla ya Utume, akawa anaitwa Zayd bin Muhammad. Allah تعالى Akataka Kuuondoa unasibishaji wa ubini huu, kwa Kauli Yake:

وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ

“Wala hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa.”

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katikati ya Sura hii,

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رُّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ

شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٤٠﴾

“Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.” (33:40)

Katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

ذٰلِكُمْ قَوْلُكُمْ بِأَفْوَاهِكُمْ

“Hayo ni maneno ya vinywa vyenu tu.”

Yaani, kupanga kwenu kuwa hao wanenu ni kauli ambayo si hukumu ya kumfanya awe mwenenu halisi, kwani yeye ameumbwa kutokana na migongo ya mtu mwingine. Hivyo, haiyumkiniki awe na baba wawili sawa na ambavyo haiwezekani mtu mmoja kuwa na nyoyo mbili,

وَاللَّهُ يَقُولُ الْحَقَّ وَهُوَ يَهْدِي السَّبِيلَ ﴿٤١﴾

“Na Allah Anasema kweli, Naye Ndiye Anayeongoa Njia.”

Sa'id bin Jubayr amesema,

يَقُولُ الْحَقَّ

“...Anasema kweli..”

Yaani, Uadilifu. Qatadah amesema:

وَهُوَ يَهْدِي السَّبِيلَ ﴿٤٢﴾

“...Naye Ndiye Anayeongoa Njia.” Yaani, njia iliyonyooka.

Imamu Ahmad alisema: Hasan alitusimulia hivi, Zuhayr alitueleza kutoka kwa Qaabus, yaani Ibn Abu Dhabyaan, amesema kwamba baba yake alimwambia kwa kusema: "Nilimwambia Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, 'Una rai gani juu ya Kauli ya Allah تعالى,

مَا جَعَلَ اللَّهُ لِرَجُلٍ مِّنْ قَلْبَيْنِ فِي جَوْفِهِ

"Mwenyezi Mungu Hakumuekea mtu yeyote kuwa ana nyoyo mbili ndani ya mwili wake".

Maana yake ni nini?' Akasema: "Mtume ﷺ alisimama siku moja kusali, akatetemeka." Wanafiki wakasema, 'Hamwoni kwamba ana nyoyo mbili? Moyo mmoja uko pamoja nanyi, na mwingine pamoja nao.' Allah تعالى Akateremsha Aya,

مَا جَعَلَ اللَّهُ لِرَجُلٍ مِّنْ قَلْبَيْنِ فِي جَوْفِهِ

"Mwenyezi Mungu Hakumuekea mtu yeyote kuwa ana nyoyo mbili ndani ya mwili wake."¹

Hii ilisimuliwa pia na At-Tirmidhi ambaye alisema: "Ni *Hadith Hasan*."² Pia ilisimuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى kutokana na Hadithi ya Zuhayr.³

Mtoto wa Hiari Aitwe kwa Jina la Baba Yake Halisi

Kauli ya Allah تعالى:

أَدْعُوهُمْ لِأَبَائِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ

"Waiteni kwa baba zao, maana huo ndio uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu."

Hii ni Amri inayofuta yaliyokuwepo mwanzoni mwa Uislamu, pindi ilipojuzishwa watoto wa kando, yaani wa kupanga kuitwa kwa nasaba ya mwenye kupanga kuwa mwanaye. Allah تعالى Aliamuru nasaba zao zirejeshwe kwa baba zao wa

¹ Ahmad 1:267

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:58

³ Ahmad na. 2410 na At-Tabari 20:204. maulamaa wengi wa Hadithi wanaichukulia isnadi ya Hadithi hii kuwa ni ina kasoro.

kweli, na kwamba, huu ndio uadilifu na wema. Bukhari amenukuu kuwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما amesema: "Sisi hatukuwa tukimwita Zaid bin Harithah رضي الله عنه, mtumwa aliyeachwa huru na Mtume ﷺ, isipokuwa kwa jina la Zayd bin Muhammad, mpaka ilipoteremka,

أَدْعُوهُمْ لِأَبَائِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ

"Waiteni kwa baba zao, maana huo ndio uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu."¹

Hii ilisimuliwa pia na Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai.²

Watu walikuwa wakiwafanyia muamala wa mtu na mwanaye katika kila nyanja, kama vile kukaa faragha na maharimu na mengineyo. Kwa ajili hii, Sahlah bint Suhayl رضي الله عنها, mke wa Abu Hudhaifah رضي الله عنه amesema, "Ewe Mtume wa Allah! sisi tulikuwa tukimwita Salim kwamba ni mwanetu, na Allah تعالى Ameiteremsha Aya aliyoiteremsha. Naye, Salim alikuwa akiingia nyumbani kwangu, lakini nilikuwa nikihisi kuwa Abu Hudhaifah alikuwa haipendi hali hiyo." Akasema Mtume ﷺ:

«أَرْضِعِيهِ تَحْرُمِي عَلَيْهِ»

"Mnyonyeshe, atakuwa maharimu wako."³

Kwa hivyo, baada ya hukumu hii kufutwa, Allah تعالى Alimruhusu mtu kumwoa mtalaka wa mtoto wa hiari (kupanga), na Mtume ﷺ alimwoa Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها, mtalaka wa Zayd bin Harithah رضي الله عنه. Allah تعالى Amesema:

لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا

"...ili isiwe taabu kwa Waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kupanga watapokuwa wamekwishatimiza nao shuruti za talaka."
(33:37)

¹ Fat'hul - Al Baari 8:377.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:72. Annasai 6:429. Muslim 4:8847.

³ Muslim 2:1076. Maana yake, kama alivyonukuu An-Nawawi kutoka kwa Qadhi Iyad, ni kwamba, ilikuwa angeliyakamua maziwa yake na ayanywe pasi na kumgusa.

Allah تعالى Amesema, katika Ayat At-Tahrim,

وَحَلَّتْ عَلَيْكُمُ آبَاءُكُمْ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ

“(Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu.” (4:23)

Mke wa mwana wa hiari hakujumuishwa kwa sababu mtoto huyo hakutokana na viuno vya mtu huyo. Ama mwana kwa njia ya kunyonya, kisheria anachukua nafasi sawa na ya mwana wa kutokana na viuno, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ iliyo katika *Sahih Mbili*:

«حُرِّمُوا مِنَ الرِّضَاعَةِ مَا يُحْرَمُ مِنَ النَّسَبِ»

“Yanayoharamisha kutokana na kunyonya, ni kama yanayosababisha kutokana na nasaba.”¹

Ama kumwita mwana wa mtu mwingine kwa namna ya ukarimu na mapenzi, si miongoni mwa yaliyokatazwa na Aya hii, kwa ushahidi wa aliyoyanukuu Ahmad na walioandika *Sunan* isipokuwa At-Tirmidhi, kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Sisi, vijana wa Banu ‘Abd Al-Muttwalib tulikuja kwa Mtume ﷺ katika *Jamaraat*. Akaanza kutupiga makofi mapaja yetu huku akisema:

«[أَبَيْتِي] لَا تَرْمُوا الْجَمْرَةَ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ»

“Enyi wanangu wadogo! msitupe mawe katika Jamarah, mpaka jua lichomoze.”²

Abu ‘Ubaydah na wengine wamesema: “Neno – *Ubayniyy* (Enyi Wanangu wadogo) – kisarufi ya lugha ya kiarabu ni udogeshi wa neno “*Ban yya*” ambalo lina dalili dhahiri, kwani tukio hili lilikuwa katika Hijja ya Kuaga, katika mwaka wa kumi.” Kauli ya Allah تعالى:

أَدْعُوهُمْ لِأَبَائِهِمْ

“Waiteni kwa baba zao...”

¹ *Al-Fath* 8:392, *Muslim* 2:1069.

² *Ahmad* 1:234, *Abu dawud* 2:480, *An-Nasai* 5:271, *Ibn Majah* 2:1007.

Suala la Zayd bin Harithah رضي الله عنه. Aliuawa mwaka wa nane, katika vita vya *Mu-utah*. Ndani ya *Sahih* Muslim kuna Hadithi ya Anas bin Malik رضي الله عنه kwamba amesema: Mtume ﷺ ameniambia,

«يَا بَنِي»

“Ewe Mwanangu!”¹

Pia iliandikwa na Abu Dawud na At-Tirmidhi.²

فَإِنْ لَّمْ تَعْلَمُوا آبَاءَهُمْ فَاِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ

“Na ikiwa hamwajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika Dini, na rafiki zenu.”

Allah تعالى Aliamrisha nasaba za watoto wa hiari irudishwe kwa baba zao ikiwa watajulikana, na wasipojulikana basi ni ndugu zao katika dini na rafiki zao kama mbadala wa kutokujulikana kwa baba zao halisi. Kwa ajili hii Mtume ﷺ alisema, siku alipotoka Makkah mwaka wa *‘Umrat Al-Qadhwa*, ambapo binti wa Hamzah alimfuata huku akimwita, “Ewe ami, ewe ami!” ‘Ali رضي الله عنه akamchukua akamwambia Fatmah رضي الله عنها, “Mchungu mtoto wa ami yako,” naye akamchukua. ‘Ali, Zayd na Ja’far رضي الله عنهم walikhasimiana juu ya nani wa kumlea, na kila mmoja alitoa hoja zake. ‘Ali رضي الله عنه akasema: “Mimi ninastahiki zaidi kwake, kwa sababu yeye ni binti wa ami yangu.” Zaidi رضي الله عنه akasema: “Ni biti wa kaka yangu.” Ja’far bin Abu Twalib رضي الله عنه akasema: “Ni binti wa ami yangu, pia nimemwoa *Khalah* wake (dada wa mama yake) – akimaanisha Asmaa bint ‘Umays رضي الله عنها.” Mtume ﷺ alikata shauri kwamba alelewe na *Khalah* wake, halafu akasema:

«الْخَالَةُ بِمَنْزِلَةِ الْأُمِّ»

“Dada wa mama ana daraja sawa na mama.”

Akamuambia ‘Ali رضي الله عنه:

«أَنْتَ مِثِّي وَأَنَا مِثْلُكَ»

“Wewe ni wangu, nami ni wako.”

¹ Muslim 3:1693.

² Abu Dawud 5:247, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:120.

Halafu akamwambia Ja'far رضي الله عنه:

«أَشْبَهْتَ خَلْقِي وَخُلُقِي»

"Unashabihiana nami kwa umbo na tabia."

Akamwambia Zayd رضي الله عنه:

«أَنْتَ أَخُونَا وَمَوْلَانَا»

"Wewe ni ndugu yetu na rafiki yetu."¹

Ndani ya Hadithi hii, kuna hukumu nyingi, mojawapo iliyo muhimu ni kwamba, Mtume ﷺ alihukumu kwa haki na akawaridhisha wote walioshindana, na akamwambia Zayd رضي الله عنه:

«أَنْتَ أَخُونَا وَمَوْلَانَا»

"Wewe ni ndugu yetu na rafiki yetu."

Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

فَأَخَوَانُكُمْ فِي الدِّينِ وَمَوْلَايَكُمْ

"...basi ni ndugu zenu katika Dini, na rafiki zenu."

Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُمْ بِهِ

"Wala si lawama juu yenu kwa mlivyokosea."

Yaani, iwapo baadhi yenu, kwa makosa mmejiita kwa nasaba isiyo ya baba zenu khalisi, baada ya kufanya juhudi na kuondoka kwa wasaa wa kuutafuta ukweli wake, basi Allah تعالى Alishaondoa dhambi katika kukosea na Alishaondoa dhambi ndani yake.

Ni sawa na katika Aya nyingine ambapo Allah تعالى Anawaelekeza na Kuwaamuru waja wake waseme:

¹ Fat'h Al-Bari 7:570.

رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ كُنَّا مُسِيئِينَ أَوْ نَحْنُ مَغْضُوبٌ عَلَيْهِمْ

“Mola wetu Mlezi! Usituchukulie tukisahau au tukikosea.” (2:286)

Na iliandikwa ndani ya *Sahih* Muslim kwamba Mtume ﷺ amesema:

«قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: قَدْ فَعَلْتُ»

“Allah Amesema: ‘Nimeshafanya (hivyo).’¹

Katika *Sahih* Bukhari kuna Hadithi ya ‘Umar bin Al-‘As رضى الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ alisema:

«إِذَا اجْتَهَدَ الْحَاكِمُ فَأَصَابَ فَلَهُ أَجْرَانِ، وَإِنْ اجْتَهَدَ فَأَخْطَأَ فَلَهُ أَجْرٌ»

“Hakimu akifanya Ijtihad na akapatia, basi ana malipo mawili, na akifanya Ijtihad na akakosea, basi ana ujira mmoja.”²

Katika Hadithi nyingine,

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى رَفَعَ عَنِ أُمَّتِي الْخَطَأَ وَالسَّيِّئَانَ وَمَا يُكْرَهُمْ عَلَيْهِ»

“Allah Ameusamehe umma wangu jambo la kukosea, kusahau na kulazimishwa.”³

Allah تعالى Amesema:

وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُمْ بِهِ، وَلَكِنْ مَا تَعَمَّدَتْ قُلُوبُكُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ

غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٢٨٦﴾

“Wala si lawama juu yenu kwa mlivyokosea. Lakini ipo lawama katika yale ziliyofanya nyoyo zenu kwa makusudi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

¹ Muslim 1:116.

² *Fat'h Al-Bari* 13:330, Ijtihad ina maana ya kufanya juhudi.

³ *Tuhfatul Al-Ahwadhi* 1:659.

Yaani, madhambi ni kwa mwenye kufanya jambo la batili kwa makusudi, kama Allah تعالى Alivyosema;

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ

“Mwenyezi Mungu Hakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi.” (5:89)

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akisema, ‘Umar رضي الله عنه alisema: “Allah تعالى Amemtuma Muhammad ﷺ kuufikisha ukweli, na Alimteremshia Kitabu. Miongoni mwa alivyoviteremsha kwake ni Aya ya kupiga mawe, Kwa hiyo Mtume ﷺ alipiga mawe (kuwaadhibu wazinifu), nasi pia tukapiga mawe baada ya kufariki kwake.” Kisha akasema: “Pia tulikuwa tukisoma, ‘Wala msijinasibishe kwa wasiokuwa baba zenu.’ Pia, Mtume ﷺ amesema:

«لَا تُطْرُونِي كَمَا أَطْرَبِي عَيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ، فَإِنَّمَا أَنَا عَبْدُ اللَّهِ، فَقُولُوا: عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ»

“Msizidisha sana kunisifu, kama alivyosifiwa Isa bin Maryam hakika! Mimi ni mja wa Allah, basi semeni: ‘Ni mja na Mtume Wake.’”

Au Ma’mar رضي الله عنه amesema huenda alisema:

«كَمَا أَطْرَبَتِ النَّصَارَى ابْنَ مَرْيَمَ»

“Kama Wakristo walivyomsifu sana mwana wa Maryam.”¹

Pia ilisimuliwa katika Hadithi nyingine,

«ثَلَاثٌ فِي النَّاسِ كُفْرٌ: الطَّعْنُ فِي النَّسَبِ، وَالْيَأْحَى عَلَى الْمَيِّتِ، وَالْإِسْتِغْنَاءُ بِالنُّجُومِ»

“Mambo matatu katika watu ni kufuru: Mtu kukashifu nasaba, kuomboleza maiti kwa makelele na kuomba mvua kwa nyota.”²

¹ Ahmad 1:47.

² Muslim na. 934, Ahmad 5:342.

الَّذِينَ أُولَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنۢ بَيْنِ أَهْلِهِمْ وَأُولُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ
بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ إِلَّا أَن تَفْعَلُوا إِلَىٰ أَوْلِيَائِكُم مَّعْرُوفًا
كَانَ ذَٰلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا ﴿٦﴾

6. *“Nabii ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao. Na wake zake ni mama zao. Na jamaa ni karibu wao kwa wao katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuliko Waumini wengine na Wahamiaji. Ila muwe mnawafanyia wema marafiki zenu. Haya yamekwisha andikwa Kitabuni.”*

Utiifu kwa Mtume ﷺ, na wakeze ni mama wa Waumini

Allah تعالیٰ Anajua huruma ya Mtume ﷺ kwa umma wake na nasaha zake kwao, basi Akamjalilia kuwa mbora wao zaidi kuliko wao kwa nafsi zao, na hukumu yake kwao ni kipaumbele zaidi kuliko khiyari yao wenyewe. Ni sawa na kauli ya Allah تعالیٰ katika Aya nyingine:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ
حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٥﴾

“La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayotoa, na wanyenyekee kabisa.” (4:65)

Na katika Sahih:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّىٰ أَكُونَ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ نَفْسِهِ وَمَالِهِ وَوَلَدِهِ
وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ»

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake. Yeyote katika nyinyi hawi muumini, mpaka mimi niwe wa kupendwa naye zaidi kuliko nafsi yake, mali yake, wanawe na watu wote.”¹

¹ Fat’hul Al-Bari 1:75.

Pia, katika *Sahih*, ni kuwa, 'Umar رضي الله عنه amesema: "Ewe Mtume wa Allah! Wallah! Wewe nakupenda sana kuliko kitu chochote, ila nafsi yangu." Akasema:

«لَا، يَا عُمَرُ! حَتَّى أَكُونَ أَحَبَّ إِلَيْكَ مِنْ نَفْسِكَ»

"Hapana, Ewe 'Umar! Mpaka nitakapokuwa wa kupendwa zaidi kwako kuliko nafsi yako."

Akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Wallahi! Wewe nakupenda sana kuliko kitu kingine chochote, hata nafsi yangu." Akasema Mtume ﷺ:

«الآنَ يَا عُمَرُ»

"Sasa, ewe 'Umar (umepatia)."

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema katika Aya hii:

أَلَنبِيُّ أَوْلَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنفُسِهِمْ

"Nabii ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao."

Bukhari رحمه الله تعالى alinukuu katika Aya hii tukufu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ مُؤْمِنٍ إِلَّا وَأَنَا أَوْلَى النَّاسِ بِهِ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، افْرُقُوا إِنْ شِئْتُمْ: ﴿أَلَنبِيُّ أَوْلَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنفُسِهِمْ﴾»

*"Hapana Muumini, isipokuwa mimi ni mbora zaidi kwake kuliko watu wote katika dunia na akhera. Mkipenda, someni: "**Nabii ni aula kwa waumini kuliko nafsi zao...**"*

فَأَيْنَمَا مُؤْمِنٍ تَرَكَ مَالًا فَلْيَرِثْهُ عَضْبَتُهُ مَنْ كَانُوا، وَإِنْ تَرَكَ دِينًا أَوْ ضِيَاعًا فَلْيَأْتِنِي فَأَنَا مَوْلَاهُ»

"Basi Muumini yeyote mwenye kuiacha mali yake nyuma, ni kwa

¹ Fat'hul Al-Bari 11:532.

ajili ya warithi wake, na akiacha deni au mayatima, basi wanijje kwani mimi ndio mlezi wao."

Hii ilinukuliwa na Bukhari رحمه الله تعالى peke yake, pia aliinukuu katika Kitabu cha Karadha.¹ Kauli ya Allah تعالى:

وَأَزْوَاجُهُمْ أُمَّهَاتُهُمْ

"Na wake zake ni mama zao."

Yaani, hao ni haramu kwao. Ama kwa upande wa heshima haijuzu kuka na faragha, wala uharamu hauenei mpaka kwa mabinti na madada zao kwa mujibu wa makubaliano ya pamoja ya wanazuoni (*Ijma*). Kauli ya Allah تعالى:

وَأُولُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ

"Na jamaa ni karibu wao kwa wao katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu..." (Yaani katika Hukumu ya Allah)."

Yaani, jamaa wa karibu ni bora wa kurithisha kuliko Muhajirina na Answar. Hii inafuta hukumu iliyokuwepo ya kuweza kurithi kwa njia ya kiapo cha udugu ulio baina yao. Kama kauli ya Ibn 'Abbas na wengine رضي الله عنهم: "Muhajirina walikuwa wakiwarithi Answar pasi na undugu na ujamaa, bali kwa undugu aliwawekea Mtume ﷺ baina yao."² Pia, hivi ndivyo alivyosema Sa'id bin Jubayr na wengine katika maulamaa wa *Salaf* na wa kizazi cha baadaye.

إِلَّا أَنْ تَفْعَلُوا إِلَيَّ أُولِيَاءِكُمْ مَعْرُوفًا

"Ila muwe mnawafanyia wema marafiki zenu."

Yaani, kurithiana kumeisha, kumbakia kusaidiana, kufanyiana wema, kuungana, ihsani na wasia. Kauli ya Allah تعالى:

كَانَ ذَلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا ﴿٦﴾

"Haya yamekwishaandikwa Kitabuni."

¹ *Fat'hul Al-Bari* 8:376, 5:75.

² Bukhari na. 2292, 4580, 6747.

Yaani, hukumu hii, nayo ni kwamba, jamaa wa damu ni bora baadhi yao kwa wenzao. Ni hukumu kutoka kwa Allah تعالی, ambayo ni Kudura, ilioandikwa katika Kitabu cha awali ambacho hakirekebishwi wala hakibadilishwi. Haya ni kwa mujibu wa Mujahid na wengine, kwamba, hata kama Allah تعالی Alishaweka sharia iliyo kinyume chake katika wakati fulani, na kuna hikima katika kufanya hivyo, na Yeye Alijua kuwa hii ingefuwa na Hukumu Yake ya asili iliyowekwa tangu zamani ingetawala, na hii ni Hukumu Yake ya kisharia iliyopitishwa.



suriana na kuafikiana. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ كِتَابٍ وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَضْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَىٰ ذَلِكُمْ إِصْرِي قَالُوا أَقْرَضْنَا قَالَ فَاشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٣١﴾

“Na pale Mwenyezi Mungu Alipochukua ahadi kwa Manabii: Nikishakupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyonyo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika Agizo Langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.” (3:81)

Ahadi na agano hili alichukua kutoka kwao baada ya kuwatuma. Kadhalika katika ahadi hii. Allah تعالى Amewataja Mitume watano kati yao, ambao walipata shida na taabu kubwa. Hii ni katika namna ya kueleza jambo kwa ujumla, halafu kwa makhususi. Wao wametajwa kwa majina katika Aya hii, na katika Kauli ya Allah تعالى:

﴿ شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّىٰ بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ ﴾

“Amekuamrisheni Dini ile ile aliyomuusia Nuhu na Tuli yokufunulia wewe, na Tuli yowausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo.” (42:13)

Hivyo, Allah تعالى katika Aya hii Ametaja pande mbili, yaani Mtume wa mwanzo na wa mwisho, kadhalika Ametaja Mitume waliokuja katikati ya wawili hao kwa mpangilio. Huu ndio wasia ambao aliuchukulia Agano toka kwao.

﴿ وَإِذْ أَخَذْنَا مِنَ النَّبِيِّينَ مِيثَاقَهُمْ وَمِنْكَ وَمِنْ نُوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ ابْنِ مَرْيَمَ ﴾

“Na Tulipochukua ahadi kwa Manabii na kwako wewe, na Nuhu na Ibrahim na Isa mwana wa Mariamu...”

Katika Aya hii, Allah تعالیٰ Alianza kwa Mtume wa Mwisho ﷺ, kwa sababu ya utukufu wake, kisha akawataja kwa mpangilio wa kuja kwao amani juu yao. Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa *Al-Mythaq Al-Ghalidh* (Agano) maana yake ni *Al-'Ahd* (Ahadi).¹

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

لَيْسَ لَكَ الصِّدْقَيْنِ عَنْ صِدْقِيَوْمٍ

“Ili (Mwenyezi Mungu) Awaulize wakweli juu ya ukweli wao.”

Mujahid amesema: *“Al-Muballighina ni wale wanaofikisha Ujumbe kutoka kwa Mitume.”*²

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

وَأَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ

“Na Amewaandalia makafiri...”

Yaani, katika umma wao,

عَذَابًا أَلِيمًا

“...Adhabu chungu.”

Yaani, ya kuumiza sana.

Sisi tunashuhudia kwamba Mitume walikwishafikisha Ujumbe wa Mola wao, wameupa umma nasaha, wamewapambanulia juu ya ukweli ulio bayana, ambao hauna utata, wala mashaka, wala kutanza. Ikiwa majahili, wakaidi, waasi na wenye nyoyo ngumu wakadhibishaji watakataa, lakini ujumbe waliokuja nao Mitume ndio wa kweli, na wanaowakhalifu ndio walio katika upotevu. Kama watu wa peponi watakavyosema:

لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ

“Hakika Mitume wa Mola Wetu Mlezi walileta Haki.” (7:43)

¹ At-Tabari 20:213.

² At-Tabari 20:214.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءَتْكُمْ جُنُودٌ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا
وَجُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا ؕ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ﴿٩﴾ إِذْ جَاءَكُمْ مِنْ فَوْقِكُمْ وَمِنْ
أَسْفَلَ مِنْكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونًا ﴿١٠﴾

9. "Enyi mliaoamini! Zikumbukeni Neema za Mwenyezi Mungu zililo juu yenu. Pale yalipokufikilieni majeshi, nasi Tukayapelekea upepo, na majeshi msiyoyaona. Na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda."

10. "Walipokujieni kutoka juu yenu, na kutoka chini yenu; na macho yalipokodoka, na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkamdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali."

Kusambaratishwa maadui katika vita vya Ahzab (Khandaq)

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu Neema, Fadhila na Ihsani Yake kwa waja Wake Waumini kwa Kuwaondosha maadui zao na Kuwawezesha kuwashinda katika mwaka walipokusanyika na wakapanga njama, huo ni mwaka wa *Al-Khandaq*, katika mwezi Shawwal (mfungo mosi), mwaka wa tano baada ya *Al-Hijrah* kwa mujibu wa rai sahihi iliyo mashuhuri. Musa ibn 'Uqbah na wengine wamesema, ulikuwa mwaka wa nne.¹ Sababu ya kuja kwa makundi ni kwamba, kikundi cha wakuu wa Kiyahudi wa Banu An-Nadhwir ambao Mtume ﷺ aliwafukuza kutoka Madinah kwenda Khaybar, akiwemo Sallam bin Abu Al-Huqayq, Sallam bin Mish'kam na Kinanah bin Ar-Rabi', walikwenda Makkah, wakajumuika na wakuu wa Kikuraishi na wakawashawishi kumpiga vita Nabii ﷺ wakawaahidi kuwasaidia na kuwaunga mkono. Wakawakubalia hilo. Wakaliendea kabila la Ghatafaan na kuwaita, na wao wakakubali pia. Makuraishi wakatoka pamoja na watu kutoka makabila mengine na wafuasi wao, chini ya uongozi wa Abu Sufyan Sakhr bin Harb. Kabila la Ghatwafaan liliongozwa na 'Uyaynah bin Hisn bin Badr. Idadi yao wote walikaribia kufikia elfu kumi. Mtume ﷺ aliposikia kuja kwao, akawaamuru Waislamu wachimbe

¹ *Fat'h Al-Bari* 7:453.

khandaki kuzunguka Madinah kutokea mashariki. Hayo ni kwa ushauri wa Salman Al-Faarīs رضي الله عنه. Waislamu wakalishughulikia hilo na wakafanya juhudi. Mtume ﷺ alibeba mchanga pamoja nao pamoja na kuchimba. Katika kuchimba kwake huko, kulikuwa na ishara bayana na dalili za wazi. Washirikina wakaja na wakapiga kambi upande wa mashariki mwa Madinah, karibu na Uhud. Kikundi kimoja kati yao kilipiga kambi katika sehemu ya juu zaidi katika ardhi ya Madinah. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِذْ جَاءُوكُم مِّن فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنكُمْ

“Walipokujieni kutoka juu yenu, na kutoka chini yenu...”

Akatoka Mtume ﷺ pamoja na baadhi ya Waislamu waliokuwa naye, ambao walifikia kiasi cha watu elfu tatu. Pia, ilisemekana kwamba walikuwa mia saba. Migongo yao waliielekeza upande wa (mlima) Sal' na nyuso zao mkabala na adui, na khandaki, ambalo ni shimo lisilo na maji ndani yake lilikuwa baina ya makundi mawili, ambalo huzuia askari wa farasi na wa miguu wasiwafikie Waislamu. Wanawake na watoto walikuwa katika ngome za Madinah. Banu Quraidhwah, ambao ni kabila mojawapo ya Kiyahudi, walikuwa na ngome upande wa Mashariki mwa Madinah. Walikuwa na mkataba na Mtume ﷺ, wao walikaribia kufikia wapiganaji mia nane. Huyay bin Akhtwab An-Nadahari, akawaenda hakuacha kuwashawishi, mpaka wakavunja mkataba na wakaungana na makundi dhidi ya Mtume ﷺ. Mgogoro ukawa mkubwa zaidi na jambo likawa gumu zaidi na hali ikadhikika sana. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

هُنَالِكَ آتَىٰ الْمُؤْمِنُونَ وَزُلْزِلُوا زِلْزَالًا شَدِيدًا

“Hapo ndipo Waumini walipojaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali.” (33:11)

Wakamzingira Mtume ﷺ na Masahaba wake kwa miezi mingi, isipokuwa hawakuwafikia na vita baina yao havikutokea, bali 'Amri bin 'Abd Wadd Al-'Amiri ambaye alikuwa miongoni mwa wapanda farasi shujaa na mashuhuri katika zama za Ujahili, alipanda farasi pamoja na wenzake kadhaa. Walilikeuka khandaki na wakapita kuelekea upande wa Waislamu. Mtume ﷺ akaita kikosi chake cha farasi kwa ajili ya kumkabili na ilisemekana kwamba hakuna

aliyejitokeza. Akamwamuru 'Ali رضي الله عنه, akamkabili na kupambana naye katika mpambano wa mtu mmoja mmoja kwa muda, kisha 'Ali رضي الله عنه akamuua, ikawa alama ya ushindi. Kisha, Allah تعالى Akawapelekea makundi upepo wenye kuvuma kwa nguvu, mpaka wakasalia bila ya hema wala kitu chochote, hawakuweza kuwasha moto wala kufanya jambo lolote, wakaondoka wakiwa hawakupata kitu, wamekhasirika. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءَتْكُمْ جُنُودٌ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا

“Enyi mlioamini! Zikumbukeni Neema za Mwenyezi Mungu zililo juu yenu. Pale yalipokufikilieni majeshi, nasi Tukayapelekea upepo...”

Mujahid amesema: “Ulikuwa upepo wa mashariki.” Rai hii inatiliwa nguvu na Hadithi,

«نُصِرْتُ بِالصَّبَا، وَأُهْلِكْتُ عَادًا بِالذَّبُورِ»

“Nimenusuriwa kwa pepo zivumazo toka mashariki na watu wa Ad waliangamizwa kwa pepo zivumazo toka magharibi..”¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَجُنُودًا لَّمْ تَرَوْهَا

“...na majeshi msiyoyaona...”

Hao ni Malaika ambao waliwatikisa na wakatia uoga na khofu nyoyoni mwao. Ikawa kila kiongozi wa kabila anasema: “Enyi Banu fulani na fulani njooni kwangu.” Wakamzingira, na akasema: “Tujiokoe, tujiokoe,” kutokana na khofu na uoga ambao Allah تعالى Aliutia nyoyoni mwao. Muslim aliandika ndani ya *Sahih* yake kuwa Ibrahim At-Taymi alisema kuwa baba yake alimwambia: “Tulikuwa kwa Hudhayfah bin Al-Yaman رضي الله عنه, mtu mmoja akasema, Lau ningelimiriki Mtume ﷺ, ningelishiriki pamoja naye vitani na ningepambana kwa juhudi zote.” Hudhaifah رضي الله عنه akamuuliza, ‘Kweli wewe ungelifanya hivyo?’ Nilikuwa pamoja na Mtume ﷺ katika usiku wa mapambano ya *Al-Ahzaab* ambapo kulikuwa na baridi na upepo mkali. Mtume ﷺ amesema:

¹ *Fat’hul - al-Bari* 2:604.

«أَلَا رَجُلٌ يَأْتِي بِخَبَرِ الْقَوْمِ يَكُونُ مَعِيَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Kuna mtu atakayeleta khabari za watu hao? Naye atakuwa pamoja nami katika Siku ya Kiyama.”

Hakuna aliyemjibu. Akarudia mara ya pili na ya tatu mithili yake. Halafu akasema:

«يَا حَذِيقَةُ! قُمْ فَأَتِنَا بِخَبَرِ مِنَ الْقَوْمِ»

“Ewe Hudhaifah! Simama na utuletee khabari za watu hao.”

Baada ya kunitaja jina langu, ikawa sina budi kusimama. Akaniambia:

«الَّتِي بِخَبَرِ الْقَوْمِ وَلَا تَدْعُرُهُمْ عَلَيَّ»

“Niletee khabari za hao watu, lakini usiwatie wasiwasi juu yangu.”

Basi nikaondoka kwa kutembea kama vile nilikuwa napita baina ya njiwa, mpaka nikawafikia. Nikamwona Abu Sufyan akiupasha joto mgongo wake kwa moto. Nikaupachika mshale katika upinde nikadhamiria kuurusha. Nikakumbuka kauli ya Mtume ﷺ,

«وَلَا تَدْعُرُهُمْ عَلَيَّ»

“Wala usiwatie wasiwasi juu yangu.”

Lau kama ningeliurusha ningempiga. Basi nikarejea kwa kutembea kama vile natembea baina ya njiwa. Nikamwendea Mtume ﷺ. Kisha nikaanza kujisikia baada ya kuwasili na kutulia. Nikampa khabari Mtume ﷺ, akanivalisha nguo yake ya ziada aliyokuwa akiitumia katika Sala. Nikalala mpaka asubuhi. Baada ya kupambazuka Mtume ﷺ akasema:

«قُمْ يَا نَوْمَانُ»

“Simama, ewe mlalaji.”¹

¹ Muslim 3:1414.

Kauli ya Allah تعالى:

إِذْ جَاءُوكُم مِّن فَوْقِكُمْ

“Walipokujieni kutoka juu yenu...”

Yaani, makundi,

وَمِن أَسْفَلَ مِنكُمْ

“...na kutoka chini yenu...”

Hudhaifa رضي الله عنه alitangulia kusema kuwa hao ni Banu Quraidhah,

وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ

“...na macho yalipokodoka, na nyoyo zikapanda kooni...”

Kwa sababu ya khofu na uoga mkubwa,

وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونَا

“...nanyi mkamdhanja Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: “Baadhi ya waliokuwa pamoja na Mtume ﷺ walidhani kwamba mwisho mbaya utakuwa kwa Waumini, na kwamba hayo atayafanya Allah تعالى.” Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى aliizungumzia kauli ya Allah تعالى:

وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونَا

“...na macho yalipokodoka, na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkamdhanja Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali.”

Kuwa: “Waislamu walikuwa na kila aina ya dhana na kukazuka unafiki, mpaka Mu’attib bin Qushayr, kaka wa Banu ‘Amr bin ‘Awf alisema: ‘Muhammad alikuwa akitupa ahadi kwamba tungeweza kupata khazina za Kisra, lakini hakuna yeyote katika sisi anayeweza kuthubutu japo kwenda na kujisaidia.’”¹ Al-Hasan aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

¹ Ibn Hisham 1:522.

وَتَطْمَئِنُّونَ بِاللَّهِ الظُّنُونًا ﴿١١﴾

“...nanyi mkamdhanja Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali.”

“Kulikuwa na dhana za namna kwa namna, wanafiki walidhani kwamba Muhammad ﷺ na Masahaba wake wataangamizwa. Waumini walikuwa na yakini kwamba Ahadi ya Allah تعالى na Mtume Wake ni kweli na kwamba Angeliifanya Dini Yake ishinde, hata kama washirikina waliichukia.”² Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abu Sa’id رضي الله عنه alisema: “Katika siku ya Khandaq tulisema: ‘Ewe Mtume wa Allah! Je kuna jambo tunalopaswa kulisema? Kwani nyoyo zetu zimefika kooni.’ Mtume ﷺ akasema:

«نَعَمْ، قُولُوا: اللَّهُمَّ اشْتُرْ عَوْرَاتِنَا وَأَمِنْ رُوَعَاتِنَا»

“Ndiyo, semeni: ‘Ewe Allah! Utusitiri udhaifu wetu na utuondolee uoga wetu.”

Akapiga nyuso za maadui wake kwa upepo, akawashinda kwa upepo. Kadhalika, Imamu Ahmad bin Hambali رحمه الله تعالى aliinukuu kutoka kwa Abu ‘Amir Al-‘Aqad رحمه الله تعالى.³

هَذَا لِكَ اَبْتَلِي اَلْمُؤْمِنُوْنَ وَزَلْزَلُوْا زَلْزَالًا شَدِيْدًا ﴿١٢﴾ وَاِذْ يَقُوْلُ اَلْمُنْفِقُوْنَ وَاَلَّذِيْنَ
فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ مَا وَعَدْنَا اَللّٰهَ وَرَسُوْلَهُٓ اِلَّا غُرُوْرًا ﴿١٣﴾ وَاِذْ قَالَتْ طَآئِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا هَلْ
يَنْتَبِرُ لَآ مَقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوْا وَاَسْتَعْزِنُ فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ اَلنَّبِيَّ يَقُوْلُوْنَ اِنَّ بُيُوْتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ
بِعَوْرَةٍ اِنْ يُّرِيْدُوْنَ اِلَّا فِرَارًا ﴿١٤﴾

11. “Hapo ndipo Waumini walipojaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali.”

12. “Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu.”

¹ At-Tabari 20:221.

² Ahmad 3:3.

13. "Na kundi moja katika miongoni mwao liliposema: Enyi watu wa Yathrib! Hapana kukaa nyinyi! Rudini. Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: Hakika nyumba zetu ni tupu. Wala hazikuwa tupu; hawakutaka ila kukimbia tu."

Kujaribiwa kwa Waumini, na Msimamo Wanafiki Katika Tukio la Al-Ahzaab

Allah تعالى Anaeleza hali hiyo pindi makundi yalipotemka kuizunguka Madinah na huku Waislamu wamezingirwa katika upeo wa tabu na dhiki kubwa, na Mtume ﷺ akiwa baina yao. Walifanyiwa mtihani, wakajaribiwa na kutetemeshwa mtetemesho mkubwa. Wakati huo wanafiki walidhihirika na walio na maradhi nyoyoni walitamka yaliyokuwa yamefichwa katika nafsi zao:

وَإِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ إِلَّا غُرُورًا ﴿١٣﴾

"Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Hawakutuahidi ila udanganyifu tu."

Ama kuhusu mnafiki, unafiki wake ulidhihiri, na mtu ambaye moyoni mwake kulikuwa na mashaka alidhoofika kutokana na wasiwasi mkubwa uliompata katika nafsi yake kwa sababu ya wasiwasi ulioletwa na udhaifu wa imani yake na hali yake ya dhiki aliyomo. Watu wengine walisema sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَإِذْ قَالَتْ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ

"Na kundi moja katika miongoni mwao liliposema: Enyi watu wa Yathrib!"

Yaani تعالى, Al-Madihan.

Sawa na ilivyoandikwa ndani ya *Sahih*:

«أَرَيْتُ فِي الْمَنَامِ دَارَ هِجْرَتِكُمْ، أَرْضُ بَيْنَ حَرَّتَيْنِ، قَدَّهَبَ وَهَلِي أَنَّهُمَا مَجْرُ فَإِذَا هِيَ يَثْرِبُ»

*"Nilioneshwa ndotoni, Mji wenu wa kuhamia, ni ardhi iliyo baina ya maeneo mawili ya lava. Mwanzoni nilidhani ni Hajar kumbe ni Yathrib."*¹

Katika tamko jingine,

«الْمَدِينَةُ»

"Madinah".

Ilisemwa kuwa asili ya jina la *Yathrib*, ni mtu mmoja aliyeishi hapo alietokea (kwa watu wa) Al-'Amaalyq aliyelitwa Yathrib bin 'Ubayd bin Mahlaayil bin 'Aws bin 'Amlaaq bin Laawudh bin Iram bin Sam bin Nuh. Hayo aliyasema As-Suhayli: "Ilisimuliwa na baadhi yao kuwa alisema: "Ina majina kumi na moja katika Taurat, Madina, Twaaba, Twiyba, Al-Maskina, Al-Jaabirah. Al-Muhibba, Al-Mahbuba, Al-Qasima, Al-Majbura, Al-'Adhraa na Al-Marhuma.'" Kauli ya Allah تعالى:

لَا مَقَامَ لَكُمْ

"Hapana kukaa nyinyi!"

Yaani, 'Hapana pamoja na Mtume ﷺ, hamwezi kufanya ulinzi,'

فَارْجِعُوا

"Rudini."

Yaani, majumbani mwenu na katika makazi yenu,

وَسْتَغْنَيْنَّ فَرِيقٌ مِّنْهُمْ النَّبِيَّ

"Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume..."

Al-'Awfi amesema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema: "Hao walikuwa Banu Harithah ambao walisema: 'Tunakhofia kuibiwa katika nyumba zetu."² Rai hii pia ilielezwa na wengine. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema kwamba 'Aws bin Qaydhiwi³ ndiye aliyesema hayo. Yaani, walitoa udhuru kurejea majumbani kwao kwa kuwa hazikuwa na mtu wa kulinda pasiibwe, hivyo wanazikhofia. Allah تعالى Amesema:

¹ Fat'hul Al-Bari 12:439.

² At-Tabari 20:226.

³ At-Tabari 2:255.

وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ

“Wala hazikuwa tupu...”

Yaani, si kama wanavyodai,

إِنْ يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا ﴿١٤﴾

“...hawakutaka ila kukimbia tu.”

وَلَوْ دُخِلَتْ عَلَيْهِمْ مِّنْ أَقْطَارِهَا ثُمَّ سُئِلُوا الْفِتْنَةَ لَأْتَوْهَا وَمَا تَلَبَّثُوا فِيهَا إِلَّا بَسِيرًا ﴿١٥﴾
 وَلَقَدْ كَانُوا عَاهِدُوا اللَّهَ مِنْ قَبْلُ لَا يُؤَلُّونَ الْأَدْبَرَ وَكَانَ عَهْدُ اللَّهِ مَسْئُولًا ﴿١٦﴾ قُلْ
 لَنْ يَنْفَعَكُمْ الْفِرَارُ إِنْ فَرَرْتُمْ مِنَ الْمَوْتِ أَوِ الْقَتْلِ وَإِذَا لَا تُمْتَعُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٧﴾ قُلْ
 مَنْ ذَا الَّذِي يَعْصِمُكُمْ مِنَ اللَّهِ إِنْ أَرَادَ بِكُمْ سُوءًا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِنْ
 دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٨﴾

14. *“Na lau kuwa wangelilingiliwa kwa pande zote, kisha wakatakiwa kufanya khiana, wangelifanya, na wasingelisita ila kidogo tu.”*

15. *“Na hakika walikwisha muahidi Mwenyezi Mungu kabla yake kwamba hawatageuza migongo yao. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yene kuulizwa.”*

16. *“Sema: Kukimbia hakukufaeni kitu ikiwa mnakimbia mauti au kuuwawa, na hata hivyo hamtastareheshwa ila kidogo tu.”*

17. *“Sema: Ni nani wa kukulindeni na Mwenyezi Mungu pindi Akikutakieni uovu, au Akikutakieni rehema? Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu.”*

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu hao,

يَقُولُونَ إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ إِنْ يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا ﴿١٩﴾

“...kwa kusema: Hakika nyumba zetu ni tupu. Wala hazikuwa tupu; hawakutaka ila kukimbia tu.” (33:13)

Kwamba, lau kama maadui wangeliingia kutokea kila upande wa Madinah, kisha wawaombe wawe makafiri, basi wangelikufuru haraka. Wao hawaichungi Imani wala hawashikamani nayo iwapo watakabiliwa na khofu kidogo tu. Hivi ndivyo ilivyotafsiriwa na Qatadah, 'Abdur-rahman bin Zayd na Ibn Jarir.¹ Huku ni kulaumiwa kwao katika upeo wa lawama. Kisha Allah تعالی Akawakumbusha juu ya waliyomwahidi kabla ya khofu hii, kwamba hawatageuza migongo, wala hawatakimbia vitani,

وَكَانَ عَهْدُ اللَّهِ مَسْئُولًا ﴿٥٦﴾

“Na Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa.” Yaani, Allah تعالی Atawauliza kuhusu ahadi hiyo, hayo hayana budi. Halafu Aliwajulisha kwamba kukimbia kwao huko hakutaakhirisha muda wao, wala hakutarefusha umri wao, bali huenda kufanya hivyo kukawa ndio sababu ya kuharakishwa kuchukuliwa kwao, tena kwa ghafla. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَإِذَا لَا تُمْتُّعُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٧﴾

“...na hata hivyo hamtastareheshwa ila kidogo tu.” Yaani, baada ya kukimbia na kutoroka kwao,

فَلَنْ مَتَّعَ الدُّنْيَا قَلِيلًا وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقَى

“Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kumchamungu.” (4:77)

Kisha, Allah تعالی Amesema:

قُلْ مَنْ ذَا الَّذِي يَعْصِمُكُمْ مِنَ اللَّهِ إِنْ أَرَادَ بِكُمْ سُوءًا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ

مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٥٨﴾

“Sema: Ni nani wa kukulindeneni na Mwenyezi Mungu pindi Akikutakieni uovu, au Akikutakieni rehema? Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, si wao wala wengine ambao wana uwezo wa kuwaondosha au kuwaokoa isipokuwa Allah تعالی.

¹ At-Tabari 20:227.

* قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الْمَعْوِفِينَ مِنْكُمْ وَالْقَائِلِينَ لِإِخْوَانِهِمْ هَلُمَّ إِلَيْنَا وَلَا يَأْتُونَ الْبَأْسَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٨﴾ أَشِحَّةً عَلَيْكُمْ ۖ فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَى عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۖ فَإِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوكُمْ بِالنِّسَةِ حِدَادٍ أَشِحَّةً عَلَى الْخَيْرِ ۗ أُولَئِكَ لَمْ يُؤْمِنُوا فَأَحْبَطَ اللَّهُ أَعْمَلَهُمْ ۗ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿١٩﴾ يَحْسَبُونَ الْأَحْزَابَ لَمْ يَذْهَبُوا ۖ وَإِنْ يَأْتِ الْأَحْزَابَ يَوَدُّوا لَوْ أَنَّهُمْ بَادُونَ فِي الْأَعْرَابِ يَسْتَغْلِبُونَ عَنْ أَنْبِيَائِهِمْ ۖ وَلَوْ كَانُوا فِيكُمْ مَا قَاتَلُوا إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢٠﴾ لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾ وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ ۗ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٢٢﴾ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ ۖ فَمِنْهُمْ مَن قَضَىٰ حَاجَهُ ۖ وَمِمَّن مَّن يَنْتَظِرُ ۗ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا ﴿٢٣﴾ لَيَجْرِيَ اللَّهُ الصِّدِّيقِينَ بَصِدْقِهِمْ ۖ وَيُعَذِّبُ الْمُنَافِقِينَ ۖ إِنَّ شَاءَ اللَّهُ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٢٤﴾ وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَأْتُوا خَيْرًا ۗ وَكَفَىٰ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ قَوِيًّا عَزِيمًا ﴿٢٥﴾

* قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الْمَعْوِفِينَ مِنْكُمْ وَالْقَائِلِينَ لِإِخْوَانِهِمْ هَلُمَّ إِلَيْنَا وَلَا يَأْتُونَ الْبَأْسَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٨﴾ أَشِحَّةً عَلَيْكُمْ ۖ فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَى عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۖ فَإِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوكُمْ بِالنِّسَةِ حِدَادٍ أَشِحَّةً عَلَى الْخَيْرِ ۗ أُولَئِكَ لَمْ يُؤْمِنُوا فَأَحْبَطَ اللَّهُ أَعْمَلَهُمْ ۗ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿١٩﴾

18. "Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anawajua hao wanaozulia, na wanao-waambia ndugu zao: Njoo ni kwetu! Wala hawaingii vitani ila kidogo tu."

19. "Wana choyo juu yenu. Ikifika khofu utawaona wanakutazama na macho yao yanazunguka, kama yule ambaye aliyezimia kwa kukaribia mauti. Na khofu ikiondoka wana-kuudhini kwa ndimi kali, nao ni mabakhili kwa kila la kheri. Hao hawakuamini,

basi Mwenyezi Mungu Amevibatilisha vitendo vyao. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.”

Allah تعالى Anaeleza juu ya Elimu Yake Kuwaenea wote waliotaka kuwazuia wengine kushiriki vitani na wale wanaowaambia ndugu zao, yaani, masahibu, marafiki na jamaa zao,

هَلُمَّ إِلَيْنَا

“Njooni kwetu!”

Yaani, katika ambayo sisi tumo katika kivuli na matunda. Na wao, licha ya hayo,

وَلَا يَأْتُونَ الْبَاسَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٣٥﴾ أَشِحَّةً عَلَيْكُمْ

“Wala hawaingii vitani ila kidogo tu. Wana choyo juu yenu.”

Yaani, mabakhili katika mapenzi na huruma kwenu. Suddi amesema:

أَشِحَّةً عَلَيْكُمْ

“Wana choyo juu yenu.”

Yaani, katika ghanima,

فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَىٰ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ

“Ikifika khofu utawaona wanakutazama na macho yao yanazunguka, kama yule ambaye aliyezimia kwa kukaribia mauti.”

Yaani, kutokana na kuzidi kwa woga na khofu yao. Na hivyo ndivyo waoga hawa walivyo na khofu ya kupigana,

فَإِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوكُمْ بِأَلْسِنَةٍ حِدَادٍ

“Na khofu ikiondoka wanakuudhini kwa ndimi kali...”

Yaani, kukishakuwa na amani, wao huzungumza kwa maneno fasaha na kudai kwamba wao ni mashujaa na waungwana sana, ilhali wanaongopa kwa hayo.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema:

سَلِّقُواكُمْ

“...wanakuudhini...”

Yaani, “Wataanza kukusemeni.”¹ Qatadah amesema: “Lakini inapokuja katika suala la ghanima, watu watakaokuwa waovu zaidi kupatiwa fungu la ngawira ni wale wanaosema, ‘Tupatie, sisi tulikuwa huko pamoja nawe,’ lakini wakati wa mapigano walikuwa waoga mno na wanaoelekea kushindwa kutetea ukweli.”² Pamoja na hayo, ni wachoyo katika kheri, yaani hakuna kheri katika wao. Wamejumuisha uoga, uongo na uchache wa kheri. Kauli ya Allah تعالى:

أُولَئِكَ لَمْ يُؤْمِنُوا فَأَحْبَطَ اللَّهُ أَعْمَلَهُمْ ۗ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٢٠﴾

“Hao hawakuamini, basi Mwenyezi Mungu Amevibatilisha vitendo vyao. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.”

Yaani, ni sahali na rahisi mno Kwake.

مَحْسَبُونَ الْأَحْزَابِ لَمْ يَذْهَبُوا ۗ وَإِن يَأْتِ الْأَحْزَابَ يَوَدُّوْا لَوْ أَنَّهُمْ بَادُونَ فِي الْأَعْرَابِ
يَسْتَلُوبُونَ ۗ عَنِ الْأَنْبِيَاءِ ۗ وَلَوْ كَانُوا فِيكُمْ مَا قَتَلُوا إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢٠﴾

20. “Wanafikiri yale makundi ya maadui hayajaondoka. Na yakija hayo makundi watatamani laiti wao wako majangwani pamoja na mabedui, wakiuliza khabari zenu. Na lau wakiwa pamoja nanyi hawapigani ila kidogo tu.”

Hii pia ni miongoni mwa sifa yao mbaya, uoga na khofu,

مَحْسَبُونَ الْأَحْزَابِ لَمْ يَذْهَبُوا

“Wanafikiri yale makundi ya maadui hayajaondoka.”

Bali wao bado wapo karibu yao, na watarejea kwa wao,

¹ At-Tabari 20:232.

² At-Tabari 20:232.

وَإِنْ يَأْتِ الْأَحْزَابُ يَوْدُوا لَوْ أَنَّهُمْ بَادُوا فِي الْأَعْرَابِ يَسْتَغْلِبُونَ عَنْ أَنْبَاءِكُمْ

“Na yakija hayo makundi watatamani laiti wao wako majangwani pamoja na mabedui, wakiuliza khabari zenu.”

Yaani, wanatamani kwamba ikiwa makundi yatakuja, basi wao hawatakuwa pamoja nanyi huko Madinah, bali watakuwa jangwani wakiulizia khabari zenu na yaliyotokea baina yenu na adui yenu,

وَلَوْ كَانُوا فِيكُمْ مَا قَتَلُوا إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٨﴾

“Na lau wakiwa pamoja nanyi hawapigani ila kidogo tu.”

Maana yake, lau kama wangelikuwa pamoja nanyi wasingelipigana pamoja nanyi isipokuwa kidogo tu kutokana na uoga na udhaifu wa imani yao.

Allah تعالی Ndiye Awajuaye zaidi.

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ

كَثِيرًا ﴿١٩﴾ وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ اللَّهُ

وَرَسُولُهُ ﴿٢٠﴾ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٢١﴾

21. “Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anayemtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.”

22. “Na Waumini walipoyaona makundi, walisema: Haya ndiyo Aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli. Na hayo haya-kuwazidisha ila Imani na Utiifu.”

Amri ya Kumfuata Mtume ﷺ.

Aya hii tukufu ni msingi mkubwa wa kumfuata Mtume ﷺ katika kauli, matendo na hali zake. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amewaamuru watu wamuige Mtume ﷺ katika siku ya *Al-Ahzaab* kuhusiana na subira, kulinda, juhudi na kungoja kwake faraja toka kwa Mola Wake, Rehema na Amani za Allah تعالى zimwendee yeye daima mpaka Siku ya Hukumu. Allah تعالى Anawaambia wale ambao walipatwa na wasiwasi, wakatikisika katika na kujisikia shida katika siku ya *Al-Ahzaab*:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ

"Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu..."

Yaani, juu ya kumuiga na kumfanya mwongozo. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

لِمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا

"...kwa anayemtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana."

Msimamo wa Waumini kwa Al-Ahzaab (Makundi)

Kisha Allah تعالى Alieleza kuhusu waja Wake Waumini waliosadikisha Ahadi ya Allah تعالى kwao na Kuufanya mwisho mwema uwepo kwao duniani na Akhera. Allah تعالى Amesema:

وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَصَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ

"Na Waumini walipoyaona makundi, walisema: Haya ndiyo Aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake."

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na Qatadah walisema: "Wanamaanisha Alichokisema Allah تعالى katika *Surat Al-Baqarah*."

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُدْخِلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ مَسْتَهْتِمُ الَّذِينَ سَاءُوا
وَالضَّالِّينَ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصُرَ اللَّهُ أَلاَّ إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ

“Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyowajia wale waliopita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Lini Nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja? Jueni kuwa Nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu.” (2:214)¹

Yaani, haya ndiyo Aliyotuahidi Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ kuhusu mitihani na majaribio ambayo itafuatiwa na nusura ya karibu kutoka kwa Allah تعالی. Kauli ya Allah تعالی:

وَصَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ^ع

“Na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wamesema kweli.”

Na Kauli Yake تعالی:

وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٣١﴾

“Na hayo hayakuwazidisha ila Imani na utiifu.”

Ni dalili ya kuongezeka kwa Imani na nguvu yake kwa mnasaba wa watu na hali zao. Ni kama walivyosema maimamu wengi: Imani yaweza kuongezeka au kupungua.

Hayo tulikwishayaeleza mwanzoni mwa maelezo yetu juu ya Bukhari, na Shukurani na Hamdi ni kwa Allah تعالی. Maana ya Kauli ya Allah تعالی:

وَمَا زَادَهُمْ

“Na hayo hayakuwazidisha...”

Yaani, hali hiyo, dhiki na shida,

إِلَّا إِيمَانًا

“...ila Imani”: kwa Allah تعالی,

وَتَسْلِيمًا ﴿٣١﴾

“...na utiifu.” Yaani, katika kufuata Amri Zake na kumtii Mtume Wake ﷺ.

¹ At-Tabari 20:236.

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُمْ مَّنْ يَنْتَظِرُ
 وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا ﴿١٨﴾ لَيَجْزَى اللَّهُ الصَّادِقِينَ بِصِدْقِهِمْ وَيُعَذِّبُ الْمُنَافِقِينَ إِن شَاءَ
 أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٩﴾

23. "Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwishakufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo."

24. "Ili Mwenyezi Mungu Awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao, na Awaadhibu wanaafiki pindi Akitaka, au Apokee toba yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."

Kusifiwa kwa Msimamo wa Waumini na Kukataliwa Jambo la Wanafiki

Baada ya Allah تعالیٰ Kueleza kwamba wanafiki walivunja ahadi waliyotoa kwa Allah تعالیٰ kwamba hawatageuza migongo yao, Ameeleza wasifu wa Waumini kwamba wao waliendelea kushikamana na Ahadi na Agano,

صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ

"Wapo waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa..."

Baadhi yao wamesema: "muda wake." Bukhari amesema: "Ahadi yake, na inarejea katika Aya ya kwanza."¹

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا ﴿١٩﴾

"... na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (Ahadi) hata kidogo."

Yaani, hawakuibadilisha ahadi ya Allah تعالیٰ nafsini mwao wala kutaraji kuivunja. Bukhari alimnukuu Zayd bin Thabit رضي الله عنه kuwa amesema:

¹ Fat'h Al-Bari 8:377.

“Tulipouandika Msahafu, Aya moja katika *Surat Al-Ahzaab* ilikosekana ambayo nilikuwa nikimsikia Mtume ﷺ akiisoma na sikuikuta na yeyote, isipokuwa Khuzaymah bin Thabit Al-Answaari رضي الله عنه ambaye ushahidi wake ulihesabiwa na Mtume ﷺ kuwa ni sawa na wa watu wawili.”

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ

“Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu.”¹

Aliipokea Bukhari peke yake, bila ya Muslim. Ahmad aliandika katika *Musnad* wake na Tirmidhi na Nasai katika *Sunan* zao. Tirmidhi alisema: “Ni *Hasan Sahih*.”² Bukhari amenukuu tena kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kwamba alisema: “Tunaiona Aya hii kuwa iliteremshwa kumhusu Anas bin An-Nadhr رضي الله عنه :

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ

“Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu.”³

Bukhari peke yake aliinukuu, na inatiliwa nguvu na isnadi nyinginezo pia. Imamu Ahmad alimnukuu Anas رضي الله عنه kuwa amesema: “Ami yangu, Anas bin An-Nadhr رضي الله عنه , ambaye mimi nimeitwa kufuata jina lake, hakushiriki pamoja na Mtume ﷺ katika vita vya Badr. Hili lilimsononesha sana, na akasema, “Vita vya kwanza alivyopigana Mtume ﷺ nimekosa kuwepo, ikiwa Allah تعالى Atanionesha vita vingine vya kupigana pamoja na Mtume ﷺ, basi Allah تعالى Ataona nitakachokifanya!” Hakutaka kusema vinginevyo. Akashiriki pamoja na Mtume ﷺ katika vita vya Uhud, ambapo alikutana na Sa’d bin Mu’adh رضي الله عنه. Anas رضي الله عنه akamwambia: ‘Ewe Abu ‘Amri, unakwenda wapi?’ Akasema: ‘Ninakwenda kwenye harufu ya peponi, mimi nitaipata katika Uhud.’ Akapigana nao mpaka akauawa. mwili wake ukakutwa na majeraha zaidi ya themanini iliyotokana na vipigo, michomo ya mikuki na mishale. Dada yake, yaani, shangazi yangu, Ar-Rubayah bint An-Nadhr رضي الله عنها alisema:

¹ *Fat’h Al-Bari* 8:377.

² Ahmad 5:188, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:520, An-Nasai katika Al-Kubra 6:430.

³ *Fat’h Al-Bari* 8:377.

‘Wala sikumtambua kaka yangu, isipokuwa kwa ncha za vidole vyake.’
Ikateremka Aya hii:

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُمْ مَّنْ يَنْتَظِرُ
وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا ﴿٣٣﴾

“Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwishakufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha hata kidogo.”

Walikuwa wakidhani kwamba iliteremshwa kumhusu yeye na masahaba wake, Allah تعالى Awe radhi nao.¹ Hii ilinukuliwa pia na Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai.² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Musa bin Twalhaf kuwa amesema: “Mu’awiyah bin Abu Sufyan رضي الله عنه alisimama halafu akasema, nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«طَلَحَهُ مِنْ قَضَىٰ نَحْبِهِ»

“Twalhaf ni miongoni mwa waliotekeleza ahadi yake.”³

Kwa ajili hii, Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ

“Baadhi yao wamekwisha kufa...”

Yaani, ahadi Yake.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَنْتَظِرُ

“...na baadhi wanangojea...”

Kuwa “Ni siku ya vita ili wafanye vyema.”⁴ Al-Hasan amesema:

فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ

“Baadhi yao wamekwishakufa...”

¹ Ahmad 3:194.

² Muslim 3:1512, Tuhfat Al-ahwadhi 9:60, An-Nasai katika Al-Kubra 6:430.

³ At-Tirmidhi na.3432, 3433.

⁴ At-Tabari 2:238.

Yaani, “Walikufa katika ukweli na uaminifu na wengine bado wanasubiri kufa katika namna hiyo hiyo na baadhi yao hawakubadilisha hata kidogo.”¹ Ni hivyo pia alivyosema Qatadah na Ibn Zayd. Baadhi yao walisema, maana ya *Nahba* yake ni nadhiri yake. Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا بَدَلُوا تَبْدِيلًا ﴿٣٣﴾

“...wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.”

Yaani, hawakuyabadilisha waliyoyaahidi wala kukosa uaminifu kwa kufanya usaliti, bali waliendelea na waliyoyaahidi wala hakuivunja kama wanafiki ambao amesema:

إِنَّ بُيُوتَنَا عَوْرَةٌ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ إِنْ يُرِيدُونَ إِلَّا فِرَارًا ﴿٣٤﴾

“Hakika nyumba zetu ni tupu. Wala hazikuwa tupu; hawakutaka ila kukimbia tu.” (33:13).

وَلَقَدْ كَانُوا عَاهِدُوا اللَّهَ مِنْ قَبْلُ لَا يُؤَلُّونَ الْأَدْبَرَ

“Na hakika walikwisha muahidi Mwenyezi Mungu kabla yake kwamba hawatageuza migongo yao.” (33:15)

Kauli ya Allah تعالى:

لَيَجْزِيَ اللَّهُ الصَّادِقِينَ بِصِدْقِهِمْ وَيُعَذِّبُ الْمُنَافِقِينَ إِنْ شَاءَ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ

“Ili Mwenyezi Mungu Awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao, na Awaadhibu wanafiki pindi Akitaka, au Apokee toba yao.”

Yaani, Allah تعالى Huwapa mtihani waja wake kwa kuwatia khofu na kitisho, ili Awapambanue wachafu dhidi ya wasafi na kudhihirika jambo la kila mmoja wao kwa vitendo, licha ya kwamba Allah تعالى Anajua kila kitu kabla ya kutokea kwake, lakini Hawaadhibu viumbe kwa Ilimu Yake tu, bali mpaka wayatende yale Ayajuayo. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

وَلَتَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ تَعْلَمَ الْمُجَاهِدِينَ مِنْكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَتَبْلُوَنَّكُمْ أَوْحَاءَكُمْ ﴿٣٥﴾

“Na bila ya shaka Tutakujaribuni mpaka Tuwadhihirishe wapiganao

¹ At-Tabari 2:239.

Jihadi katika nyinyi na wanaosubiri. Nasi Tutazifanyia mtihani khabari zenu.” (47:31)

Hii inamaanisha kukijua kitu baada ya kutukia kwake, ingawa Allah تعالى Anakijua kabla ya kufanyika. Kadhalika, Allah تعالى Amesema:

مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ ۗ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى الْغَيْبِ

“Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyonyo mpaka Apambanue wabaya na wema. Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kukujuulisheni mambo ya ghaibu.” (3:179)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

لِيَجْزِيَ اللَّهُ الصَّالِحِينَ بِصِدْقِهِمْ

“Ili Mwenyezi Mungu Awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao...”

Yaani, kwa sababu ya subira yao katika waliyomuahidi Allah تعالى na kuwa nayo imara katika kuyasimamia pamoja na kuyahifadhi,

وَيُعَذِّبُ الْمُنَافِقِينَ

“...na Awaadhibu wanafiki...” Hawa ni wavunjaji wa ahadi zao kwa Allah تعالى, wanaozikhalifu Amri Zake, kwa ajili hiyo wanastahiki mateso na adhabu Yake, lakini wako chini ya kutaka Kwake duniani. Akitaka Atawaacha waendeleo na wanayoyafanya mpaka watakapokutana Naye na Kuwaadhibu, na Akitaka Atawasamehe kwa Kuwaongoza watoke katika unafiki na kwenda katika imani, na amali njema baada ya ufasiki na uasi. Kwa kuwa Rehema na Ukirimu Wake kwa waja Wake ni wenye kushinda Ghadhabu Zake, Amesema:

إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَنَالُوا خَيْرًا ۗ وَكَفَىٰ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ

قَوِيًّا عَزِيمًا

25. “Na Mwenyezi Mungu Aliwarudisha nyuma makafiri juu ya ghadhabu yao; hawakupata kheri yoyote. Na Mwenyezi Mungu Amewatosheleza Waumini katika vita. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Uweza.”

Allah تعالی Alirudisha Nyuma Makundi ya Makafiri

Allah تعالی Anaeleza namna Alivyoyafukuza makundi ya makafiri kutoka Madinah kwa Kuwapelekea upepo na majeshi ya Malaika, lau kama Allah تعالی Asingemjaalia Mtume Wake kuwa rehema ya ulimwengu, basi, upepo huo ungelikuwa mkali zaidi kuliko upepo mkavu Alioupeleka kwa 'Ad. Hata hivyo, Allah تعالی Amesema:

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ

“Na Mwenyezi Mungu Hakuwa wa Kuwaadhibu nawe umo pamoja nao...” (8:33)

Kwamba Aliwapelekea upepo ambao uliwatawanya. Wao ni mchanganyiko wa makabila na makundi yenye maoni mbalimbali. Allah تعالی Alinasibisha na Kupeleka hewa ambayo iliuvunja mkusanyiko wao, na Akawarejesha wakiwa wameshindwa na kupata khasara kwa chuki na uadui, wala hawakupata kheri, si duniani, ambapo walikosa waliyoyatamani, kama vile ushindi na ghanima, wala si Akhera, kutokana na madhambi waliyoyafanya, kwa kumtangazia uadui Mtume ﷺ na dhamira yao ya kumuua na kuliharibu jeshi lake. Mwenye kutaka kufanya jambo na akadhamiria kwa dhati kabisa, kwa hakika ni sawa na aliyelifanya. Kauli ya Allah تعالی:

وَكَفَى اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ

“Na Mwenyezi Mungu Amewatosheleza Waumini katika vita.”

Yaani, hawakuwa na haja ya kuwapiga kwa ajili ya kuwaondosha katika ardhi yao, bali Allah تعالی Peke Yake Anatosha, na Alimsaidia mja wake na Akalipa ushindi jeshi lake. Kwa ajili hii, Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ، صَدَقَ وَعْدُهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ وَأَعَزَّ جُنْدَهُ، وَهَزَمَ الْأَحْزَابَ وَحْدَهُ، فَلَا شَيْءَ بَعْدَهُ»

“Hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah, Mpweke,

Alikuwa Mkweli katika Ahadi Yake, Alimnusuru mja Wake, Akalipa nguvu jeshi Lake, Aliyashinda makundi. Yeye Peke Yake na hakuna kitu baada Yake Yeye.”

Imepokewa kutokana na Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه¹ Katika *Sahih* Mbili, ‘Abdullah bin Abu Awfaa رضي الله عنه alisema: Mtume ﷺ aliomba dua ifuatayo dhidi ya Al-Ahzaab:

«اللَّهُمَّ مُنْزِلَ الْكِتَابِ سَرِيعَ الْحِسَابِ، اهْزِمِ الْأَخْرَابَ، اللَّهُمَّ اهْزِمْهُمْ وَزَلِّزْلُهُمْ»

“Ewe Allah! Uliyeteremsha Kitabu, Mwepesi wa hisabu, Yashinde makundi. Ewe Allah! Washinde na Uwatikise.”²

Na Kauli ya Allah تعالى:

وَكَفَى اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ

“Na Mwenyezi Mungu Amewatosheleza Waumini katika vita.”

Ni ishara ya kukoma vita baina yao na makuraishi. Hivyo ndivyo ilivyotokea baadaye, washirikina hawakuwashambulia Waislamu, bali Waislamu ndio waliowavamia katika ardhi zao. Ni sawa na alivyonukuu Imamu Ahmad kutoka kwa Sulayman bin Surad رضي الله عنه: Katika siku ya vita vya Al-Ahzaab Mtume ﷺ amesema,

«الآن نَغْزُوهُمْ وَلَا يَغْزُونَا»

“Sasa tutawashambulia, wala hawatatushambulia.”³

Hivi ndivyo alivyoandika Bukhari katika *Sahih* yake.⁴ Kauli ya Allah تعالى:

وَكَانَ اللَّهُ قَوِيًّا عَزِيزًا ﴿٣٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Uweza.”

Yaani, kwa Hila na Nguvu Zake, Aliwarejesha wakiwa mikono mitupu na hawakupata kheri yoyote, Allah تعالى Akaupa nguvu Uislamu na wafuasi wake, Akatimiza Ahadi Yake, Akamnusuru Mtume na mja Wake. Hivyo, Himdi na Shukurani ni Zake.

¹ *Fat'h Al-Bari* 7:469, *Muslim* 3:2089.

² *Fat'h Al-Bari* 7:469, *Muslim* 3:1363.

³ *Ahmad* 4:162.

⁴ *Fat'h Al-Bari* 7:467.

وَأَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ صَيَاصِبِهِمْ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا ﴿٢٦﴾ وَأَوْرَثْنَاكُمْ أَرْضَهُمْ وَدِيَارَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ وَأَرْضًا لَمْ تَطْفُوهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٢٧﴾ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لِأَزْوَاجِكَ إِن كُنْتُنَّ تُرِدْنَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا فَتَعَالَيْنَ أُمَتِّعْكُنَّ وَأُسَرِّحْكُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴿٢٨﴾ وَإِن كُنْتُنَّ تُرِدْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالْآخِرَةَ فَإِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْمُحْسِنَاتِ مِنْكُنَّ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾ يٰبِسَاءَ النَّبِيِّ مَن يَأْتِ مِنْكُنَّ بِفَاحِشَةٍ مُّبِينَةٍ يُضَعَّفْ لَهَا الْعَذَابَ ضِعْفَيْنِ ۗ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٣٠﴾ * وَمَن يَفْعَلْ مِنْكُنَّ لِلَّهِ وَرَسُولِهِ وِتْعَمَلْ صَالِحًا نُؤْتِهَا أَجْرَهَا مَرَّتَيْنِ وَأَعْتَدْنَا لَهَا رِزْقًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾ يٰبِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَأَحَدٍ مِنَ النِّسَاءِ ۗ إِنِ اتَّقَيْتُنَّ فَلَا تَحْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقَلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٣٢﴾ وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَىٰ ۗ وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۗ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾ وَأذْكُرْنَ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَالْحِكْمَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ﴿٣٤﴾

وَأَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ صَيَاصِبِهِمْ وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا ﴿٢٦﴾ وَأَوْرَثْنَاكُمْ أَرْضَهُمْ وَدِيَارَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ وَأَرْضًا لَمْ تَطْفُوهَا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٢٧﴾

26. "Na Akawateremsha wale waliowasaidia (maadui) katika Watu wa Kitabu kutoka katika ngome zao; na akatia khofu katika nyoyo zao. Baadhi yao mkawa mnawaua, na wengine mnawateka."

27. "Na Akakurithisheni ardhi zao na nyumba zao na mali zao, na ardhi msiyopata kuikanyaga. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu."

Kampani Dhidi ya Banu Quraydhwah

Zilitangulia taarifa kuwa Banu Quraydhwah, pindi yalipofika majeshi ya Al-Ahzaab na wakapiga kambi nje ya Madinah, wao walivunja mkataba na Mtume ﷺ. Hili lilifanywa na wakala Huyay bin Akhtab An-Nadhwari - Allah تعالى Amlaani – ambaye aliingia ndani ya ngome yao na akamshawishi kiongozi wa Banu Quraydha, Kaa'b bin Asad, mpaka akavunja mkataba. Miongoni mwa aliyomwambia ni haya: “Ole wako! Nimekuletea fursa ya ushindi. Nimekuletea makuraishi pamoja na makundi kutoka makabila kadha wa kadha, Ghatwafaan na wafuasi wao. Hawataondoka hapa, ila mpaka wamwangamize Muhammad na Masahaba wake.’ Kaa'b akamjibu: ‘Wallah umeniletea fursa ya udhalilishaji. Ole wako ewe Huyay, kwani wewe ni mwenye nuksi, basi utuache.’ Lakini, hakuacha kumshawishi mpaka akamkubalia. Huyay akaweka sharti kwamba, ikiwa makundi hayo yataondoka bila kufanya lolote, yeye (Huyay) ataungana nao katika hali zao katika ngome. Quraydhwah walipovunja mkataba, na khabari hiyo kumfikia Mtume ﷺ, ilimhuzunisha sana pamoja na Waumini. Baada ya Allah تعالى Kumpa ushindi na Kuwarudisha maadui wakiwa wamefeli na kukhasirika, Mtume ﷺ akarejea Madinah na watu wakaweka chini silaha. Mtume ﷺ akiwa anaoga kutokana na mavumbi ya vita hivyo katika nyumba ya Ummu Salamah رضي الله عنها, Jibril عليه السلام alimjia akiwa amevaa kilemba cha hariri iliyotariziwa akiwa juu ya nyumbu ambaye alitandikwa nguo ya hariri iliyotariziwa. Akasema: “Umeweka chini silaha ewe Mtume wa Allah?” Mtume ﷺ akasema: “Ndiyo.” Akasema: “Lakini, Malaika bado hawajaweka chini silaha zao. Hivi sasa ndio natokea katika kuwasaka watu hao.” Kisha akasema: “Allah تعالى Anakuamrisha uinuke kuwaendea Banu Quraydhwah.” Na katika riwaya alimuambia: “Wewe ni mpiganaji gani! Mmeshaweka chini silaha zenu?” Akajibu, “Ndiyo.” Akasema: “Sisi bado hatujaweka chini silaha zetu. Inuka uwaendee hao.” Mtume ﷺ akauliza: “Wapi?” Akajibu: “Banu Quraydhwah, Allah تعالى Ameniamuru niwatikise.” Mtume ﷺ akasimama upesi na kuwaamuru watu waende kwa Banu Quraydhwah, waliokuwa umbali wa maili kadhaa kutoka Madinah.¹ Hiyo ilikuwa baada ya Sala ya Adhuhuri. Mtume ﷺ akasema:

«لَا يُضَلِّينَ أَحَدًا مِنْكُمْ الْعَصْرَ إِلَّا فِي بَنِي قُرَيْظَةَ»

“Yeyote kati yenu asisali Alasiri, isipokuwa kwa Banu Quraydhwah.”²

¹ Angalia Bukhari na 4117, 4118, Ahmad 6:56, na Al-Majma' 6:140.

² Bukhari 4119, na Muslim 1770.

Watu wakaenda wakakutwa na wakati wa Swala wakiwa njiani. Baadhi yao wakasali njiani na wakasema: "Mtume ﷺ hakukusudia jingine ila tutembe haraka." Wengine wakasema: "Hatutaisali, mpaka tufike kwa Banu Quraydhwah." Hakuna yeyote katika makundi mawili hayo aliyemkemea mwenzake. Mtume ﷺ akaja nyuma baada yao, akiwa amemwacha Ibn Umm Maktum رضي الله عنه kusimamia huko Madinah na akampa 'Ali bin Abu Twalib رضي الله عنه kushika bendera. Mtume ﷺ akawazingira siku ishirini na tano. Jambo hili lilipowachukua muda mrefu, walifiki hukumu ya Sa'd bin Mu'adh رضي الله عنه, kiongozi wa Aws, kwa sababu washirika wao katika zama za ujahili na wakadhani kwamba atawafanyia wema katika jambo hilo, kama alivyofanya 'Abdullah bin Ubayy bin Salul kwa washirika wake, Banu Qaynuqa', alipomwomba Mtume ﷺ kuwaacha huru. Wakadhani Sa'd رضي الله عنه angelifanya kama Ibn Ubayy kwa hao. Hawakujua kuwa Sa'd رضي الله عنه alipigwa mshale katika mshipa mkuu wa kati wa mkononi, katika vita vya Khandaq. Mtume ﷺ akautia pisho na akamweka katika hema msikitini ili awe anamzuru kwa karibu. Miongoni mwa mambo ambayo Sa'd رضي الله عنه alioyaomba katika dua yake ni kwamba: "Ewe Allah! Ikiwa bado kuna kitu chochote kuhusu vita kilichobakia dhidi ya Makuraishi, basi nibakishe kwa ajili yake, na kama umeshaondosha vita baina yetu na wao, basi acha uvujaji damu uanze upya, wala usinifishe, mpaka niridhike juu ya Banu Quraydhwah." Allah تعالی Akamjibu dua yake, na wakaingia katika hukumu yake kwa khiyari yao kwa kupata yaliyo katika nafsi zao. Hapo, Mtume ﷺ alimwita kutoka Madinah ili apitishe hukumu yao. Alipowasili huku akiwa amepanda juu ya punda waliyemwandalia, baadhi ya Aws walianza kumsihi asiwe mkali kwao na kumwambia: "Ewe Sa'd! Wao ni washirika wako, basi wafanyie ihsani." Wakawa wanalia na kujaribu kuulainisha moyo wake juu yao, ilhali yeye akiwa kimya, bila ya kuwajibu. Walipozidi sana, aliwaambia, "Sasa umewadia wakati wa Sa'd kuhakikisha kwamba, hapana lawama yoyote ya mwenye kulaumu itakayomtoa katika njia ya Allah تعالی." Wakatambua kwamba hatawaacha hai. Alipofika karibu na hema ambamo alikuwemo Mtume ﷺ, Mtume ﷺ alisema:

«قُرُّمُوا إِلَىٰ سَيِّدِكُمْ»

"Simameni kwa ajili ya kiongozi wenu."

¹ Bukhari 4119, na Muslim 1770.

Waislamu wakasimama kwa ajili yake, na wakamkaribisha kwa heshima kulingana na hadhi yake ili hukumu yake iwe na athari kubwa kwao. Baada ya kukaa, Mtume ﷺ alimwambia,

«إِنَّ هَؤُلَاءِ - وَأَشَارَ إِلَيْهِمْ - قَدْ نَزَّلُوا عَلَيَّ حُكْمَكَ، فَأَحْكُمْ فِيهِمْ بِمَا شِئْتَ»

“Kwa hakika, hawa - Akafanya ishara ya kuwaonesha – wameafikiana kuikubali hukumu yako, basi wahukumu utakavyo.”

Sa'd رضي الله عنه akasema: “Hukumu yangu itafanyika juu yao.” Mtume ﷺ akasema: “Ndiyo.” Sa'd رضي الله عنه akasema: “Na walio ndani ya hema hili.” Akasema: “Ndiyo.” Akasema: “Na walio hapa.” Akaashiria upande aliokuwepo Mtume ﷺ, lakini hakumwangalia Mtume ﷺ usoni mwake, kwa kumheshimu, na kumtukuza. Mtume ﷺ akamwambia: “Ndiyo.” Sa'd رضي الله عنه akasema: “Mimi ninatoa hukumu kwamba wapiganaji wauawe na mali zao zichukuliwe.” Mtume ﷺ akasema:

«لَقَدْ حَكَمْتَ بِحُكْمِ اللَّهِ تَعَالَى مِنْ فَوْقِ سِنِّ أَرْقَمَةَ»

“Umehukumu kwa Hukumu ya Allah kutokea juu ya mbingu saba.”

Katika riwaya alisema:

«لَقَدْ حَكَمْتَ بِحُكْمِ الْمَلِكِ»

“Umehukumu kwa hukumu ya Mfalme.”¹

Mtume ﷺ akaamuru kuchimbwa makhandaki, yakachimbwa, na wao wakaletwa wakiwa wamefungwa mabegani mwao, na shingo zao zikakatwa. Walikuwa baina ya mia saba na mia nane. Watoto ambao walikuwa bado kubaleghe na wanawake walichukuliwa mateka na mali zao kuzuiliwa.¹ Yote haya yameelezwa kwa muhtasari na kwa kina pia, kwa dalili na Hadithi zake. Maelezo yake kwa urefu yamo ndani ya vitabu vya Sira ambavyo tumeviandika kwa ufupi na kwa urefu. Hamdi na Shukurani zinamstahiki Allah تعالى. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

¹ Kama hivyo ilinukuliwa na Al-Bukhari na. 4122, Muslim na. 1768 na 1769, na Ahmad 6:141, 142.

وَأَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ

“Na Akawateremsha wale waliowasaidia (maadui)...”

Yaani, waliowasaidia makundi kumpiga vita Mtume ﷺ:

مِنَ أَهْلِ الْكِتَابِ

“...katika Watu wa Kitabu...”

Yaani, Mayahudi wa Banu Quraidhwah, katika uzao wa Banu Israil. Wazazi wao wa zamani waliteremka Hijaz kwa hamu ya kumfuata Nabii ambaye hawezi kusoma wala kuandika kikasomwa “Ummi” ambaye wanamkuta ameandekiwa katika Taurati na Injili.

فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ

“...yalipowajia yale waliyokuwa wakiyajua waliyakanusha.” (2:89)

Laana ya Allah تعالی iwashukie.

مِن صَيِّصِيهِمْ

“...kutoka katika ngome zao...”

Kwa maana, himaya zao. Hivyo ndivyo alivyosema Mujahid, ‘Ikrimah, Qatadah, Suddi na wengine, katika *Salaf*.²

وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ

“...na Akatia khofu katika nyoyo zao.”

Nayo ni khofu, kwa sababu waliwasaidia washirikina kumpiga vita Mtume ﷺ. Lakini asiyejua si sawa na anayejua. Wao waliwakhofisha waislamu wakaazimia kuwaua ili wapate nguvu za kidunia. Hali ikawa kinyume chake kwao, wasaidizi wao wakageuka kukimbia na Waislamu wakashinda huku makafiri wakishindwa. Waliitafuta nguvu, wakadhalilika, walitaka kuwaangamiza Waislamu, wakaangamia wao. Pamoja na haya yote, wana hali mbaya zaidi Akhera, hivyo, kwa ujumla huku ni kukhasirika sana.

¹ At-Tabari 20:247. Pia angalia *Fat'h Al-Bari* 7:414.

² At-Tabari 20:249.

Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema:

فَرِيقًا تَقْتُلُونَ وَتَأْسِرُونَ فَرِيقًا ﴿٣٣﴾

“Baadhi yao mkawa mnawaua, na wengine mnawateka.”

Imamu Ahmad alinukuu kwamba ‘Atwiyyah Al-Quradhi amesema: “Nilitambulishwa kwa Mtume ﷺ katika siku ya Quraydhwah, kwa sababu hawakuwa na hakika nami. Mtume ﷺ aliwaambia wanitizame iwapo nilikuwa tayari nimeota nywele za mwilini. Walitazama na wakaona kwamba sikuwa nimeota nywele zozote za mwilini, kwa hivyo wakaniacha niondoke, na wakaniunganisha pamoja na mateka wengine.”¹ Hii ilinukuliwa pia na wakusanyaji wa *Sunan* na At-Tirmidhi alisema ni *Hasan Sahih*.² An-Nasai amenukuu masimulizi sawa na hayo kutoka kwa ‘Atwiyyah.³

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَوْرَثْنَاكُمْ أَرْضَهُمْ وَدِيَارَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ

“Na Akakurithisheni ardhi zao na nyumba zao na mali zao...”

Yaani, Alizijaalia ziwe zenu baada ya nyinyi kuwaua,

وَأَرْضًا لَّمْ تَطْعُوهَا

“...na ardhi msiyopata kuikanyaga.”

Ilisemwa: “Ni Khaybar.” Pia imesemwa kwamba ni: “Makkah.” Mtazamo huu ni wa Malik kutoka kwa Zayd bin Aslam. Pia ilisemwa: “Fursi na Rumi.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: Inawezekana kuwa inarejea katika yote hayo.

وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٣٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”⁴

¹ Ahmad 4:383.

² Abu Dawud 4:561, Tuhfatul Al-Ahwadhi 5:207, An-Nasai katika Al-Kubra 5:185, Ibn Majah 2:849.

³ An-Nasai katika Al-Kubra 5:185.

⁴ At-Tabari 20:250.

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلٌّ لِأَزْوَاجِكَ إِنْ كُنْتُنَّ تُرِدْنَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزَيَّنَّتْهَا فَتَعَالَيْنَّ أُمَتِّعَنَّ
 وَأُسَرِّحَنَّكَ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴿٢٦﴾ وَإِنْ كُنْتُنَّ تُرِدْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالْآخِرَةَ فَإِنَّ اللَّهَ
 أَعَدَّ لِلْمُحْسِنَاتِ مِنْكُنَّ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٧﴾

28. "Ewe Nabii! Waambie wake zako: Ikiwa mnataka maisha ya dunia na pambo lake, basi njooni, nitakupeni kitoka nyumba, na kukuacheni mwachano mzuri."

29. "Na ikiwa mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume wake na nyumba ya Akhera, basi Mwenyezi Mungu Amewaandalia wafanyao mema, miongoni mwenu, malipo makubwa."

Kuharishwa kwa Wake wa Mtume

Hii ni Amri ya Allah تعالى kwa Mtume Wake ﷺ kwamba awape khiyari wakeze, baina ya kuwaacha na waende kwa mwingine ambaye watapata kwake mahitaji ya maisha ya kidunia na mapambo yake, na baina ya kuwa na subira katika hali ya dhiki iliyoko kwa Mtume ﷺ, na kwamba wao kwa kufanya hivi watapata malipo makubwa. Wao wakachagua na kuridhia kubakia kwa Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na Akhera. Baada ya hayo, Allah تعالى Aliwapatia vyote, kheri za dunia na furaha ya Akhera. Bukhari amepokea kuwa 'Aishah رضي الله عنها, mke wa Mtume ﷺ alimjia yeye, pindi Allah تعالى Alipomwamuru kuwaachia wakeze wachague. Mtume ﷺ alianzia kwangu, akaniambia:

«إِنِّي ذَاكِرٌ لِّكَ أَمْرًا فَلَا عَلَيْكَ أَنْ تَسْتَعْجِلِي حَتَّى تَسْتَأْمِرِي أَبَوَيْكَ»

"Mimi nitakutajia jambo, lakini usiliharakishe, mpaka ukaombe ushauri wazazi wako."

Na alikuwa akijua kwamba wazazi wangu hawakuwa wakiniamuru kumwacha. Kisha akasema:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى قَالَ: ﴿يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلٌّ لِأَزْوَاجِكَ﴾»

"Allah Amesema: "Ewe Nabii! Waambie wake zako..."

Mpaka mwisho wa Aya mbili. Nikamwambia, “Nitawashauri wazazi wangu kitu gani ninachokihitaji?”¹ Yeye pia, aliisimulia isnadi ya wasimulizi, na aliongeza, “Akasema, kisha wake wote wa Mtume ﷺ walifanya kama mimi.”² Imamu Ahmad alimnukuu ‘Aisha رضي الله عنها akisema, “Mtume ﷺ alitupa khiyari, nasi tulimchagua yeye, kwa hivyo, kuchagua hakukuwa na maana yoyote ya talaka.”³ Ilinukuliwa (na Bukhari na Muslim) kutokana na Hadithi ya Al-A’mash.⁴ Imamu Ahmad alinukuu kuwa Jabir رضي الله عنه alisema: “Abubakr رضي الله عنه alikuja kubisha hodi kwa Mtume ﷺ huku kukiwa na watu walioketi mlangoni kwake, na Mtume ﷺ naye alikuwa amekaa, hakumruhusu. Akaja ‘Umar رضي الله عنه kupiga hodi, naye hakupewa idhini. Halafu, akawaruhusu Abubakr na ‘Umar رضي الله عنهما, wakaingia, na kumkuta Mtume ﷺ akiwa ameketi, na wakeze wamemzunguka. Mtume ﷺ alikuwa amenyamaza kimya. ‘Umar رضي الله عنه akasema: ‘Nitamwambia jambo Mtume ﷺ huenda akacheka.’ ‘Umar رضي الله عنه akasema: ‘Ewe Mtume wa Allah! Lau ungelimwona binti wa Zayd – mke wa ‘Umar – akiniomba nimpe matumizi, hivi punde tu, nikamsukuma huko! Mtume ﷺ akacheka mpaka magego yake yakadhihiri, halafu akasema:

«هُنَّ حَزَلِي بَسَأْتِي التَّقَّة»

“Hao wamenizunguka, wakiniomba matumizi.”

Abubakr رضي الله عنه akasimama kumuendea ‘Aishah رضي الله عنها ili ampige, na ‘Umar رضي الله عنه akamuendea Hafswah رضي الله عنها, huku wote wawili wakisema: ‘Mnamwomba Mtume ﷺ mambo ambayo hana!’ Mtume ﷺ akawakataza, na wakeze wakasema, ‘Wallah! Hatutamwomba Mtume ﷺ, baada ya kikao hiki, chochote asicho nacho.’ Basi Allah تعالى Akateremsha Aya ya kuwapa khiyari. Mtume ﷺ alianza kwa ‘Aishah رضي الله عنها, akamwambia:

«إِنِّي أَدْكُرُ لَكَ أَمْرًا مَا أَحِبُّ أَنْ تَعْجَلِي فِيهِ حَتَّى تَسْتَأْمِرِي أَبِيكَ»

“Mimi nitakutajia jambo, lakini sipendi uliharakisha, mpaka ukaombe ushauri wa wazazi wako.”

¹ Fat’hu Al-Baari 8:379.

² Fat’hu Al-Baari 8:380.

³ Ahmad 6:45.

⁴ Fathu Al-Baari 9:280, Muslim 2:1104.

'Aishah رضي الله عنها akauliza: 'Ni jambo gani hilo?' Mtume ﷺ akamsomea,

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلُوبًا لَّا تَزُوجُكَ

"Ewe Nabii! Waambie wake zako..."

'Aishah رضي الله عنها akasema: 'Niwatake ushauri wazazi wangu kuhusu wewe? Mimi namchagua Allah تعالى na Mtume Wake, na ninakuomba usimtajie mkeo yeyote juu ya nililochagua.' Mtume ﷺ akasema:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى لَمْ يَبْعَثْنِي مُعْتَمًا، وَلَكِنْ بَعَثَنِي مُعَلِّمًا مَّيْسَرًا، لَا تَسْأَلُنِي امْرَأَةً مِنْهُمْ عَمَّا اخْتَرْتُ إِلَّا أَخْبَرْتُهَا»

*"Allah Hakunituma niwe laghai, lakini Amenituma kufundisha kwa wepesi. Mwanamke yeyote katika wao hataniuliza jambo juu ya ulivyochagua, bali nitamwambia."*¹

Hii ilinukuliwa na Muslim peke yake, bila ya Bukhari; akaiandika yeye na An-Nasai.²

'Ikrimah amesema: "Na kwa wakati huo alikuwa na wake tisa, watano kutoka kabila la kikuraishi, ambao ni 'Aishah, Hafswah, Umm Habibah, Saudah na Umm Salamah رحمه الله تعالى. Pia alikuwa na mkewe Swafiyah bint Huyay An-Nadhwiyyah, Maymunah bint Al-Harith Al-Hilaliyah, Zaynab bint Jahsh Al-Asadiyyah na Juwayriyyah bint Al-Harith Al-Mustwalaqiyyah رحمه الله تعالى.

يَبْسَأُ النَّبِيُّ مَنْ يَأْتِ مِنْكُمْ بِفَحِشَةٍ مُّبِينَةٍ يُضَعَفُ لَهَا الْعَذَابُ ضِعْفَيْنِ ۗ وَكَانَ
ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٣٠﴾ * وَمَنْ يَقْنُتْ لِلَّهِ وَرَسُولِهِ وَتَعَمَلْ صَالِحًا نُؤْتِهَا
أَجْرَهَا مَرَّتَيْنِ وَأَعْتَدْنَا لَهَا رِزْقًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾

30. "Enyi wake wa Nabii! Atakayefanya uchafu dhahiri miongoni mwenu, Atazidishiwa adhabu mara mbili. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi."

¹ Ahmad 3:328.

² Muslim 2:1104, An-Nasai 5:383.

³ At-Tabari 20:252.

31. “Na miongoni mwenu atakeyemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akatenda mema, Tutampa malipo yake mara mbili, na Tutamwandalia riziki ya ukarimu.”

Wake wa Mtume ﷺ si kama Wanawake Wengine

Allah تعالى Anawapa mawaidha wake wa Mtume ﷺ ambao walimchagua Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na Akhera na wakaendelea kuwa ni wake wa Mtume ﷺ. Akanasibisha waelezwe hukumu yao na kuhusishwa kwao tu, na si kwa wanawake wengine. Kuwa yeyote miongoni mwao atakayefanya uchafu wa wazi. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: “Huo ni uasi na tabia mbaya.”¹ Vyovyote itakavyochukulika, hili ni sharti, ambalo maana yake jambo linalowekewa sharti si lazima liweze kutukia. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِن أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ

“Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu amali zako zitaanguka...” (39:65).

Na kama Kauli yake Allah تعالى:

وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٨﴾

“Na lau wangelimshirikisha yangeliwaharibikia waliyokuwa wakiyatenda.” (6:88)

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَبِيدِ ﴿٨١﴾

“Sema: Ingelikuwa Rahmani ana mwana, basi mimi ningelikuwa wa kwanza kumuabudu.” (43:81)

لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا لَأَصْطَفَىٰ مِمَّا خَلَقَ مَا يَشَاءُ ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٤﴾

“Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka kuwa na mwana, basi bila ya shaka Angeliteua Amtakaye katika Aliowaumba. Subhanahu, Ametakasika na hayo! Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda Atakalo.” (39:4)

¹ Al-Baghawi 3:527.

Kwa kuwa hadhi yao ni ya juu, inaweza kusemwa kwamba, lau kama wangelifanya dhambi yoyote, basi ingelikuwa ni nzito mno, hivyo ni kwa ajili ya kuhifadhi hadhi yao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

مَنْ يَأْتِ مِنْكُمْ بِفَحِشَةٍ مُّبِينَةٍ يُضَعَفْ لَهَا الْعَذَابُ ضِعْفَيْنِ

“Atakayefanya uchafu dhahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili.”

Malik alimnukuu Zayd bin Aslam katika Kauli kwamba,

يُضَعَفْ لَهَا الْعَذَابُ ضِعْفَيْنِ

“...atazidishiwa adhabu mara mbili.”

Amesema duniani na Akhera. Na kutoka kwa Ibn Abu Najih, kuwa Mujahid alitoa masimulizi mithili ya hayo.

وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٤٠﴾

“Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.”

Yaani, sahali na rahisi. Kisha Akataja Uadilifu na Fadhila Zake katika Kauli Yake,

* وَمَنْ يَقْنُتْ مِنْكُمْ لِلَّهِ وَرَسُولِهِ

“Na miongoni mwenu atakeyemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake...”

Yaani, atakayemtii Allah تعالى na Mtume wake ﷺ na akakubali,

نُؤْتِيهَا أَجْرَهَا مَرَّتَيْنِ وَأَعْتَدْنَا لَهَا رِزْقًا كَرِيمًا ﴿٤١﴾

“...Tutampa malipo yake mara mbili, na Tutamuandalia riziki ya ukarimu.”

Yaani, katika pepo, kwani watakuwa katika makazi ya Mtume ﷺ katika mahali pa juu zaidi pa ‘Illiyin, juu ya makazi ya viumbe wote, katika Wasilah ambayo ndiyo makazi ya Peponi yaliyokaribiana zaidi na Arshi.

يَنْسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَأَحَدٍ مِنَ النِّسَاءِ ۗ إِنَّ اتَّقِيْتَنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي
 فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٣٢﴾ وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ
 الْأُولَى ۗ وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۗ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ
 عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾ وَأَذْكُرَنَّ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ
 مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَالْحِكْمَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ﴿٣٤﴾

32. "Enyi wake wa Nabii! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine. Kama mnamcha Mungu basi msilegeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema."

33. "Na kaeni majumbani kwenu, wala msijishaue kwa majishauo ya kijahilia ya kizamani. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara."

34. "Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na Hikima. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye khabari."

Amri ya Kuwa na Adabu kwa Mama wa Waumini Ili wawe kigezo kwa wengine.

Hizi ni adabu ambazo Allah تعالی Aliwaamuru wake wa Mtume ﷺ wazitekeleze ili wanawake wa umma wawaige wao. Allah تعالی Aliwaambia wake wa Mtume ﷺ kwamba ikiwa watamcha Allah تعالی kama Alivyowaamuru, basi hakuna mwanamke yeyote wa kushabihiana nao wala wa kuwa sawa nao katika fadhila na hadhi. Kisha, Allah تعالی Amesema:

فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ

"...basi msilegeze sauti zenu..." Suddi na wengine walisema: "Kwa kauli hiyo Anamaanisha kauli laini wakati wanapozungumza na wanaume. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

فَيَطْمَعُ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ

“...akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake.”

Yaani, kitu kichafu.

وَقُلْنَا قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٣٣﴾

“Na semeni maneno mema.”

Ibn Zayd alisema: “Ni mazungumzo mema na mazuri yanayojulikana vyema kuwa ni ya kheri.”¹ Maana yake ni kwamba, wazungumze na watu wa kando katika namna ambayo hakuna ulainifu, yaani, mwanamke asizungumze na mtu wa kando sawa na anavyozungumza na mumewe. Kauli ya Allah تعالى:

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ

“Na kaeni majumbani kwenu...”

Yaani, bakieni majumbani mwenu, wala msitoke pasi na haja. Miongoni mwa haja za kisharia, ni Swala msikitini kwa kufuata masharti yake. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ:

«لَا تَمْنَعُوا إِمَاءَ اللَّهِ مَسَاجِدَ اللَّهِ وَلْيَخْرُجْنَ وَهُنَّ تَفَلَّاتٌ»

“Msiwazuie wajakazi wa Allah kwenda katika misikiti ya Allah, lakini watoke wakiwa hawajajitia manukato.”²

Na katika masimulizi mengine,

«وَبُيُوتُهُنَّ خَيْرٌ لَّهُنَّ»

“Nyumba zao ni bora kwao.”³

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَبْرَجْ. تَبْرَجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى

“...wala msijishaue kwa majishauo ya kijahilia ya kizamani.”

¹ At-Tabari 20:258.

² Ad-Dur Al-Manthur 6:602.

³ Abu Dawud 1:381.

Mujahid amesema, “Wanawake walikuwa wakitoka na kutembea mbele ya wanaume, na hii ilikuwa ndiyo *Tabarruj* ya *Jahiliyyah*.”¹ Qatadah alisema:

وَلَا تَبْرَجْ. تَبْرُجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى

“...wala msijishaue kwa majishauo ya kijahilia ya kizamani.”

“Amesema walipotoka majumbani mwao wakitembea kwa maringo na kujipitisha pitisha Allah تعالى Amewakataza hilo”² Muqatil bin Hayyan amesema:

وَلَا تَبْرَجْ. تَبْرُجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى

“...wala msijishaue kwa majishauo ya kijahilia ya kizamani.”

“*Tabarruj* ni pale mwanamke anapojitanda mtandio kichwani mwake, lakini haufungi vyema.”³ Kwa hiyo vinaonekana vidani vyake, herini na shingo. Vyote hivyo vinadhihirika. Hiyo ndiyo *Tabarruj*, na Allah تعالى Anawaenezea Amri Yake wanawake wote wa Waumini kuhusu suala la *Tabarruj*. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Na shikeni Sala, na toeni Zaka na mtiini Allah na Mtume Wake...”

Kwanza, Allah تعالى Amewakataza uovu, halafu Amewaamuru kheri kama vile kusimamisha Sala, ambayo ni kumwabudu Allah تعالى Peke Yake, asiye na mshirika; na kutoa zaka, ambayo ni kuwafanyia ihsani viumbe,

وَأَطِعْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“...na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake.”

Huu ni aina ya muundo katika maneno, huanza kwa kutaja mambo mahususi, kisha kuhitimisha na ya jumla.

¹ Abu Dawud 1:382.

² Ad-Dur Al-Manthur 6:602.

³ At-Tabari 20:259

Wake wa Mtume ﷺ ni katika Familia yake (Ahlul - Bayt)

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na Kukusafisheni baarabara.”

Kauli hii iko wazi kuwa familia ya Mtume ﷺ ni pamoja na wakeze na wao ndio sababu ya kuteremshwa Aya hii. Na wanachuoni wanakubaliana hili katika hali zote iwe ni sababu ya pekee au pamoja na sababu nyingine, na ndio rai sahihi. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu 'Ikrimah kwamba alikuwa akinadi sokoni,

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na Kukusafisheni baarabara.”

Kuwa, Aya hii iliteremshwa makhususi kwa wake wa Mtume ﷺ.¹ Hivi ndivyo alivyonukuu Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume...”

Kwamba iliteremshwa khususan kwa wake wa Mtume ﷺ. "Ikrimah alisema: "Yeyote asiyekubaliana nami kwamba iliteremshwa kwa ajili ya wakeze Mtume ﷺ, basi niko tayari kukutana naye na kuomba laana ya Allah تعالى iwashukie waongo."² Hiyo ndiyo sababu ya kuteremshwa. [lakini katika Aya hiyo wanaingia wanawake wengine katika njia ya ujumuishaji wa hukumu na uenezi.] Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Swafiyyah bint Shaybah رضي الله عنها alisema: 'Aishah رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ alitoka siku moja asubuhi akiwa amevaa Joho lililokuwa na milia ya nywele nyeusi za Ngamia. Akaja

¹ At-Tabari 20:267.

² Imenukuliwa na Ibn Abu Hatim na 'Asaakir. Ad-DurAl-Manthur 5:376.

Hasan رضي الله عنه, akamfunika na nguo aliyokuwa nayo. Kisha, akaja Husayn رضي الله عنه, akamjumuisha katika kumfunika, akaja Fatmah رضي الله عنها, akamjumuisha pamoja naye, akaja 'Ali رضي الله عنه akamjumuisha pia, halafu akasema:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume...”¹

Muslim aliandika katika *Sahih* yake kutoka kwa Yazid bi Hayyan alisema: “Nilikwenda mimi, Huswayn bin Sabrah na ‘Umar bin Muslim, kwa Zayd bin Arqam. tulipokaa kwake, Huswayn alimwambia: ‘Umepata kheri nyingi ewe Zayd. Wewe umemwona na umesikia mazungumzo ya Mtume ﷺ, umeshiriki pamoja naye vitani na umesali nyuma yake. Bila shaka, umepata kheri nyingi sana ewe Zayd! Tueleze ewe Zayd! Kitu gani ulichokisikia kwa Mtume ﷺ. Akasema: “Ewe binamu yangu! Wallah! Umri wangu umekuwa mkubwa sana, na ahadi yangu imeshafika, nimesahau baadhi ya niliyokuwa nikiyafahamu toka kwa Mtume ﷺ, basi nitakachokusimulieni, mkipokee, na msikhofoe chochote ambacho sitakuambieni.” Halafu akasema: “Mtume ﷺ alisimama baina yetu siku moja karibu na kisima kilichoitwa Khumma, baina ya Makkah na Madinah, akamhimidi na kumsifu Allah تعالى, akakhutubu, akatukumbusha, halafu akasema:

«أَمَا بَعْدُ، أَلَا أَيُّهَا النَّاسُ! فَإِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ يُوشِكُ أَنْ يَأْتِيَنِي رَسُولُ رَبِّي فَأَجِيبْ، وَأَنَا تَارِكٌ فِيكُمْ ثَقَلَيْنِ: أَوَّلُهُمَا كِتَابُ اللَّهِ تَعَالَى، فِيهِ الْهُدَىٰ وَالنُّورُ فَخُذُوا بِكِتَابِ اللَّهِ وَاسْتَمْسِكُوا بِهِ»

“Amaa ba’d: Kwa hivyo, Enyi watu! Mimi ni kiumbe, na hivi karibuni atakuja Mjumbe wa Mola wangu, nami nitamjibu. Ninakuachieni mambo mawili: cha kwanza ni Kitabu cha Allah, ndani yake kuna hidaya na nuru. Kichukueni Kitabu cha Allah na mshikamane nacho.”

Akahimiza juu ya kushikamana na Kitabu cha Allah تعالى, kisha akasema:

¹ At-Tabari 20:261, Muslim na. 2081.

«وَأَهْلُ بَيْتِي أَذْكُرُّكُمْ اللَّهُ فِي أَهْلِ بَيْتِي، أَذْكُرُّكُمْ اللَّهُ فِي أَهْلِ بَيْتِي»

“Na familia yangu (Ahl Al-Bayt). Mkumbukeni Allah kuhusu familia yangu, mkumbukeni Allah kuhusu familia yangu.”

Mara tatu.” Huswain akamwambia: “Ni watu gani wa familia yake (*Ahl Al-Bayt*), ewe Zayd? Wake zake si miongoni mwa familia yake?” Akasema: “Wake zake ni katika wanafamilia wake, lakini wanafamilia wake ni wale walioharamishiwa kupewa Sadaka.” Akauliza tena: “Hao ni akina nani?” Akasema: “Hao ni familia ya ‘Ali, Aqil, Ja’far na Abbas رضي الله عنهم”. Akauliza, “Je hao wote ni haramu kupatiwa Sadaka baada ya kufariki kwake.” Akasema: “Ndiyo.”¹ Maelezo haya ni kutoka kwa Zayd bin Arqam na si *Marfu*².

Amri ya Kufuata Qur’an na Sunna

Mtu ambaye hana mashaka katika kuizingatia Qur’an anatambua kwamba wake wa Mtume ﷺ wanaingia katika Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na Kukusafisheni baarabara.”

Kwa sababu mfuatano wa Kauli hizi unakwenda pamoja nao. Kwa hivyo, Allah عزوجل Amesema baada ya haya yote:

وَأَذْكُرَنَّ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَالْحِكْمَةِ

“Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na Hikima.”

Yaani, ‘Mtende kulingana na alichokiteremsha Allah تعالى kwa Mtume Wake majumbani mwenu, nayo ni Qur’an na Sunna, ambazo Allah تعالى Alimfunulia Mtume Wake ﷺ katika nyumba zenu.’ Hayo ni kwa mujibu wa Qatadah na

¹ Muslim 4:1873.

²Maana yake, yasichukilike kwamba yametoka kwa Mtume ﷺ.

³At-Tabari 20:268.

wengine.³ Pia mkumbuke juu ya neema hizi ambazo ni khususan kwenu, si kwa watu wengine, kwamba Wahyi unateremshwa majumbani kwenu, na si kwa watu wengine, na 'Aishah Siddiqah bint Siddiq رضي الله عنهما ndiye wa kwanza kabisa kwa neema hizi, na ndiye aliyefadhiliwa zaidi katika fungu hili, ndiye kahusika zaidi na rehema hizi nyingi, kwani Wahyi haukuteremshwa kwa Mtume ﷺ katika tandiko la mke yeyote wa Mtume ﷺ isipokuwa yeye tu, kama alivyolieleza hili Mtume ﷺ mwenyewe. Baadhi ya maulamaa, Allah تعالى Awarehemu, walisema: "Hii ni kwa sababu Mtume ﷺ hakumwoa bikira yeyote zaidi yake, wala hakuna mtu yeyote aliyewahi kulala naye isipokuwa Mtume ﷺ." Kwa hivyo, amenasibishwa kuhusika peke yake kwa fadhila hizi, na kuwa wa peke yake katika daraja hii ya juu. Lakini ikiwa wake zake ni katika familia yake basi udugu wake unastahiki zaidi kuitwa hivyo. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Abu jamilah alisema: "Hasan bin 'Ali رضي الله عنهما alichaguliwa kuwa Khalifah pindi alipouawa 'Ali رضي الله عنه." Alisema: Akiwa katika Swala, mtu mmoja alimrukia na kumchoma kwa jambia lake. Huswayn alidai kwamba alisikia kuwa mtu aliyemchoma alitokea kwa Banu Asad, na Hasan رضي الله عنه alikuwa wakati huo akisujudu. Akasema: "Wanadai kwamba alijeruhiwa katika nyonga yake. Akaugua kwa miezi kadha, halafu akapona. Akakaa katika mimbari na kusema: "Enyi watu wa Iraq! Mcheni Allah kuhusu sisi, kwani sisi ni viongozi na wageni wenu. Pia, sisi ni katika *Ahl Al-Bayt* ambao Allah تعالى Amesema:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na Kukusafisheni barabara."

Aliendelea kuyasema haya mpaka hakusalia yeyote msikitini isipokuwa kila mmoja alikuwa akigumia kwa kulia. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ﴿٣٤﴾

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye khabari."

Yaani, kwa Ulatifu Wake kwenu, mmeweza kufikia daraja hii, na kwa kujua Kwake khabari zenu na kwamba nyinyi mnafaa kupata hadhi hii, Amekupeni

hayo na kuyafanya kuwa maalumu kwenu. Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, alisema: “Na mkumbuke Neema za Allah تَعَالَى juu yenu, kwa Kukujaalieni kuwa katika nyumba ambamo husomwa Aya za Allah تَعَالَى na Hikima Zake. Hivyo, mshukuruni Allah تَعَالَى kwa hayo na mumhimidi.

إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ﴿٣٤﴾

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye khabari.”

Yaani, Mpole kwenu kwa sababu Amekufanyeni kuwa katika nyumba ambazo ndani yake husomwa Aya za Allah تَعَالَى. Na kwamba Yeye Anawajua vyema Akakuchagueni kuwa wake wa Mtume wake.¹ Qatadah alisema:

وَأَذْكُرْتَ مَا يُتْلَىٰ فِي بُيُوتِكُنَّ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَالْحِكْمَةِ

“Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na Hikima.”

Kuwa: “Anawakumbusha juu ya Neema Zake.” Hayo aliyankuu Ibn Jarir تَعَالَى: ² Atwiyah Al-’Awfi aliizungumzia Kauli ya Allah تَعَالَى:

إِنَّ اللَّهَ كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا ﴿٣٤﴾

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye khabari.”

“Yaani, ni Mjuzi wa mahali panapostahiki kuiweka hikima.” Aliinukuu Ibn Abu Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, kisha akasema: Kadhalika aliisimulia kutoka kwa Ar- Rabi’ bin Anas, kutoka kwa Qatadah.

* * *

¹ At-Tabari 20:268.

² At-Tabari 20:268.

إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ
 وَالْقَنَبِيِّنَ وَالْقَنَبِيَّاتِ وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ وَالصَّابِرِينَ
 وَالصَّابِرَاتِ وَالْخَشِيعِينَ وَالْخَشِيعَاتِ وَالْمُتَصَدِّقِينَ
 وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّيِّمِينَ وَالصَّيِّمَاتِ وَالْحَفِظِينَ
 فُرُوجَهُمْ وَالْحَفِظَاتِ وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا
 وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾ وَمَا
 كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ
 يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ
 ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا ﴿٣٦﴾ وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ
 وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ اللَّهَ وَتُخْفَى فِي
 نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ
 تَخْشَاهُ ۗ فَلَمَّا قَضَى زَيْدٌ مِنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ
 عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ
 وَطَرًا ۗ وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٣٧﴾ مَا كَانَ عَلَى النَّبِيِّ
 مِنْ حَرَجٍ فِيمَا فَرَضَ اللَّهُ لَهُ سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ
 قَبْلُ ۗ وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ قَدَرًا مَقْدُورًا ﴿٣٨﴾ الَّذِينَ يُبَلِّغُونَ
 رِسَالَاتِ اللَّهِ وَيَخْشَوْنَهُ وَلَا يَخْشَوْنَ أَحَدًا إِلَّا اللَّهَ ۗ وَكَفَى
 بِاللَّهِ حَسِيبًا ﴿٣٩﴾ مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ
 وَلَكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ

عَلِيمًا ﴿٤٠﴾

إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ
 وَالْقَنَبِيِّنَ وَالْقَنَبِيَّاتِ وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ
 وَالصَّابِرِينَ وَالصَّابِرَاتِ وَالْخَشِيعِينَ وَالْخَشِيعَاتِ
 وَالْمُتَصَدِّقِينَ وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّيِّمِينَ
 وَالصَّيِّمَاتِ وَالْحَفِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَالْحَفِظَاتِ
 وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ
 مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾

35. "Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake, na watiifu wanaume na watiifu wanawake, na wasemao kweli wanaume na wana-wake, na wanaosubiri wanaume na wanawake, na wanyenyekavu wana-ume na wanawake, na watoao sadaka wanaume na wanawake, na wanao-funga wanaume na wana-wake, na wanao jihifadhi tupu zao wanaume na

wanawake, na wanaomdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wanaume na wanawake, Mwenyezi Mungu Amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.”

Maelezo Kuhusu Sababu za Kuteremshwa

Imamu Ahmad alimnukuu Ummu Salamah رضي الله عنها, mke wa Mtume ﷺ, kuwa amesema. Nilimwambia Mtume ﷺ, “Kwa nini sisi hatutajwi katika Qur’an sawa na wanavyotajwa wanaume?” Hakunipuuza kwa hilo, kwani siku moja, alikuwa akihubiri katika mimbari, na wakati huo nilikuwa nikitana nywele zangu. Nikazibana kisha nikatoka kuelekea ndani ya chumba changu, nyumbani kwangu. Nikaweka sikio langu katika kuti la mtende, nikamsikia Mtume ﷺ akisema:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَقُولُ: ﴿إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ﴾﴾

“Enyi Watu! Allah Anasema: “Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake...” Mpaka mwisho wa Aya.”¹

Hii ilinukuliwa na Nasai na pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى.² Kauli ya Allah تعالى,

﴿إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ﴾

“Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake...”

Ni ushahidi kwamba Imani ni tofauti na Uislamu, nao ni makhsusi, kwa sababu ya Kauli ya Allah تعالى,

﴿قَالَتِ الْأَعْرَابُ قُلْ ءَامَنَّا لَمْ نُوْمِنُوا وَلَكِنْ قَوْلُوا أَسْلَمْنَا لَمَّا يَدْخُلِ الْإِيمَانُ فِي قُلُوبِكُمْ﴾

﴿قُلُوبِكُمْ﴾

“Mabedui wamesema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani Imani haijaingia katika nyoyo zenu.” (49:14)

¹ Ahmad 6:305.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:431.

Katika *Sahih* Mbili kuna Hadithi,

«لَا يَزِينِي الرَّأْيِي جِئِنَ يَزِينِي وَهُوَ مُؤْمِنٌ»

*"Hazini mzinifu na pindi anapozini akawa Muumini."*¹

Basi, Uzinifu unamvua Muislamu imani yake, wala hiyo haimaanishi kuwa yeye ni kafiri, kwa mujibu wa makubaliano ya Waislamu. Kwa hivyo imeonesha kwamba Imani ni makhususi kuliko Uislamu, kama tulivyoeleza mwanzoni mwa sherehe ya *Al-Bukhari*. Kauli ya Allah تعالى،

وَالْقَنِينِ وَالْقَنِينَتِ

"...na watiifu wanaume na watiifu wanawake..."

Kunuti ni utii katika utulivu,

أَمَّنْ هُوَ قَنِينٌ ءَأَنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا مَحْذَرُ الْأَخِرَةِ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِمْ

"Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola wake Mlezi..." (39:9)

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَلَّهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلٌّ لَهُ قَنِينٌ ﴿٣٠﴾

"Na Vyake Yeye vilivyo mbinguni na katika ardhi. Vyote vinamtii Yeye." (30:26)

يَذَرِيكُمْ أَقْنِي لِرَبِّكِ وَأَسْجُدِي وَأَرْكَبِي مَعَ الرَّاكِبِينَ ﴿٣٤﴾

"Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao." (3:43)

وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾

"...na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kuqunuti (kunyenyekaa)." (2:238)

¹ Fat'h Al-Bari 10:33, Muslim 177.

Kwa hivyo, baada ya Uislamu, kuna kiwango cha juu zaidi kinachotakikana kufikiwa, nayo ni *Iman*, kisha *Qunut* inasimama katika yote mawili,

وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ

“...na wasemao kweli wanaume na wanawake...”

Hii ni katika kauli zao, kwani ukweli, ni tabia ya kusifiwa. Kwa minajili hii, kuna baadhi ya Masahaba walikuwa hawakuwahi kuongopa, si katika ujahili wala ndani ya Uislamu. Nayo ni alama ya Imani, kama ambavyo uongo ni ishara ya unafiki, na atakayekuwa mkweli atapata nusura:

«عَلَيْكُمْ بِالصِّدْقِ فَإِنَّ الصِّدْقَ يَهْدِي إِلَى الْبِرِّ، وَإِنَّ الْبِرَّ يَهْدِي إِلَى الْجَنَّةِ، وَإِنَّاكُمْ
وَالكُذِبِ، فَإِنَّ الكُذِبَ يَهْدِي إِلَى الْفُجُورِ، وَإِنَّ الْفُجُورَ يَهْدِي إِلَى النَّارِ، وَلَا يَزَالُ
الرَّجُلُ يَصْدُقُ وَيَتَحَرَّى الصِّدْقَ حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ صَدِيقًا، وَلَا يَزَالُ الرَّجُلُ
يَكْذِبُ وَيَتَحَرَّى الكُذِبَ حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ كَذَابًا»

“Kuweni wakweli, kwani ukweli huongoza kwenye wema, na wema huongoza kwenda peponi. Nakutahadharisheni na uongo, kwani huo uongo huongoza kwenda katika uasi ambao huongoza kwenda Motoni. Wala mtu haachi kusema ukweli na kujihimu kuwa mkweli mpaka huthibitishwa mkweli kwa Allah. Na mtu haachi kuongopa na kujihimu kuwa mwongo mpaka huthibitishwa kwa Allah.”¹

Kuna Hadithi nyingi zimazohusiana na mada hii.

وَالصَّابِرِينَ وَالصَّابِرَاتِ

“...na wanaosubiri wanaume na wanawake...”

Hii ni sifa ya wavumilivu, nayo ni subira juu ya mambo yanayomsibu mtu, na kutambua kwamba lililo katika kudura ni lenye kutukia bila ya shaka. Wao hukabiliana na hayo kwa subira na uimara na kwa hakika subira ni katika pigo la kwanza, yaani, huwa ngumu zaidi mwanzoni mwa janga, kisha, baada yake ni sahali zaidi. Nayo ni sifa ya uvumilivu na uimara.

¹ Muslim 4:2013.

وَالْخَشِيعِينَ وَالْخَشِيعَاتِ

“...na wanyenyeketu wanaume na wanawake...”

Maana ya *Khushu'* ni ushwari, utulivu, uangalifu, umakini na unyenyekevu. Kinachompelekea mtu kuwa katika hali hii ni ni khofu yake kwa Allah تعالى na kutambua kwamba Yeye ni Mwenye Kuchunga. Ni sawa kama ilivyo katika Hadithi,

«اعْبُدُ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ»

“Muabudu Allah kama vile unamuona, na kama humuoni, basi Yeye Anakuona.”¹

وَالْمُتَّصِدِّينَ وَالْمُتَّصِدِّاتِ

“...na watoao sadaka wanaume na wanawake...”

Sadaka ni kuwafanyia ihsani watu wenye unyonge wenye haja, ambao hawana kipato wala cha kupatia kipato. Watoaji wanatoa kutoka katika mali ya ziada kwa ajili ya utiifu kwa Allah تعالى na ihsani kwa viumbe Wake. Imenukuliwa Hadithi katika *Sahih* Mbili,

«سَبْعَةٌ يُظِلُّهُمُ اللَّهُ فِي ظِلِّهِ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ - فَذَكَرَ مِنْهُمْ - وَرَجُلٌ تَصَدَّقَ بِصَدَقَةٍ فَأَخْفَاهَا حَتَّى لَا تَعْلَمَ شِمَالُهُ مَا تُنْفِقُ يَمِينُهُ»

“Watu saba Allah Atawafunika katika kivuli Chake katika siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa Chake tu. Miongoni mwa aliowataja ni – mtu aliyetoa Sadaka akaificha kiasi kwamba mkono wake wa kushoto haukujua kinachofanywa na wa kuumeni.”²

Hadithi nyingine,

«وَالصَّدَقَةُ تُطْفِئُ الْخَطِيئَةَ كَمَا يُطْفِئُ الْمَاءُ النَّارَ»

“Sadaka huyazima makosa kama vile maji yanavyozima moto.”³

¹ Fat'h Al-Bari 1:140,

² Fat'h Al-Bari 2:168, Muslim 2:715.

³ Tuhfatul Al-ahwadhi 3:237.

Hadithi za kuhimiza Sadaka ni nyingi sana na zenyewe zimeelezwa mahali zinapostahiki.

وَالصَّائِمِينَ وَالصَّائِمَاتِ

“...na wanaofunga wanaume na wanawake...”

Katika Hadithi aliyoinukuu Ibn Majah,

«وَالصَّوْمُ زَكَاةُ الْبَدَنِ»

“Saumu ni Zaka ya mwili.”¹

Yaani, inamtakasa, kumtwaharisha na kumsafisha uchafu kitabia na kisharia. Sawa na alivyosema Sa’d bin Jubayr ataingia katika Kauli ya Allah تعالى:

وَالصَّائِمِينَ وَالصَّائِمَاتِ

“...na wanaofunga wanaume na wanawake...”²

Saumu ni njia kubwa zaidi ya kuyakata matamanio. Sawa na alivyosema Mtume ﷺ:

«يَا مَعْشَرَ الشَّبَابِ! مَنْ اسْتَطَاعَ مِنْكُمُ الْبَاءَةَ فَلْيَتَزَوَّجْ، فَإِنَّهُ أَعْيَشُ لِنَفْسِهِ وَأَخْصَنُ لِلْفَرْجِ، وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَعَلَيْهِ بِالصَّوْمِ فَإِنَّهُ لَهُ وِجَاءٌ»

“Enyi kundi la vijana! Yeyote miongoni mwenu mwenye kuwa na uwezo wa kuoja basi, aoe. Kwani hilo ndilo hasa la kulifumba jicho na kuihifadhi tupu. Na asiyemudu, basi ni juu yake Saumu kwani hiyo inamlinda.”³

Alinasibisha na Kauli ya baada yake,

وَالْحَفِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَالْحَافِظَاتِ

“...na wanaojihifadhi tupu zao wanaume na wanawake...”

Yaani, dhidi ya mambo ya haramu na madhambi, isipokuwa kwa namna iliyoruhusiwa. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

¹ Ibn Majah 1:555.

² Sawa na hayo yalinukuliwa na Ibn Abu Hatim, *Ad-Dur Al-Manthur* 5:380.

³ *Fat’hul Al-Bari* 9:14.

وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٣٥﴾ إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ
مَلُومِينَ ﴿٣٦﴾ فَمَنْ أَبْتَغَىٰ وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٣٧﴾

“Na ambao wanahifadhi tupu zao. Isipokuwa kwa wake zao, au iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi - Lakini wanaotaka kinyume ya haya, basi hao ndio wanaoruka mipaka.”
(70:29-31)

Kauli ya Allah تعالى،

وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ

“...na wanaomdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wanaume na wanawake...”

Ibn Abu Hatim رضي الله عنه alimnukuu Abu Sa'id Al-Khudri رحمه الله تعالى kuwa amesema, Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا أَتَيْتَ الرَّجُلَ امْرَأَتَهُ مِنَ اللَّيْلِ فَصَلِّا رَكَعَتَيْنِ كُنِّيَا تِلْكَ اللَّيْلَةَ مِنَ الذَّاكِرِينَ اللَّهَ
كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ»

“Mtu akimwamsha mkewe usiku na wakasali raka mbili, basi wataandikwa katika usiku huo miongoni mwa wanaume na wanawake wanaomkumbuka sana Allah.”

Mithili ya Hadithi hii ilinukuliwa na Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah kutoka katika Hadithi ya Abu Said رضي الله عنه na Abu Hurayrah رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ.¹ Imamu Ahmad alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kwamba amesema, Mtume ﷺ alikuwa akipita katika njia mojawapo ya Makkah. Akafika katika Mlima wa Jumdan, akasema:

«هَذَا جُندَانٌ، سِيرُوا، فَقَدْ سَبَقَ الْمُفْرَدُونَ»

“Huu ni (mlima wa) Jumdan, nendeni, kwani Al-Mufarriduna wameshatangulia.”

¹ Abu Dawud 2:74, An-Nasai katika Al-Kubra 6:433, Ibn Majah 1:423.

Wakasema: "Al-Mufarriduna ni nini?" Mtume ﷺ akasema:

«الذَّاكِرُونَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ»

"Wanaume wanaomtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi na wanawake."

Kisha akasema:

«اللَّهُمَّ اغْنِرْ لِلْمُحَلِّقِينَ»

"Ewe Allah! Wasamehe walionyoa."

Wakasema: "Na wanaopunguza?"

«اللَّهُمَّ اغْنِرْ لِلْمُحَلِّقِينَ»

"Ewe Allah! Wasamehe walionyoa."

Wakasema: "Na wanaopunguza?"

«وَالْمُقْصِرِينَ»

"Na wale waliopunguza nywele."

Hii ilinukuliwa na Imamu Ahmad kwa isnadi hii.¹ Pia, ilinukuliwa na Muslim, isipokuwa sehemu yake ya mwishoni.² Kauli ya Allah تعالى,

أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾

"...Mwenyezi Mungu Amewaandalia msamaha na ujira mkubwa."

Ni habari ya hao wote wanaomkumbuka, maana yake, Allah تعالى Amewaandalia Maghufira Yake kwa madhambi yao na malipo makubwa, ambayo ni Pepo.

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ^٤

وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا ﴿٣٦﴾

¹ Ahmad 2:411.

² Muslim 2:946.

36. "Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi."

Sababu za Kuteremshwa

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Barzah Al-Aslami amesema: "Julaybib alikuwa mtu ambaye aliyezoea kupita kwa wanawake na kutaniana nao. Nikamwambia mke wangu, 'Msimwachilie Julaybib kuingia, ikiwa ataingia, nitakufanyieni kitu kadha na kadha.' Ilikuwa kwamba, ikiwa Answaar yeyote alikuwa na ndugu wa kike, hamwozeshi mpaka kwanza atambue Mtume ﷺ alikuwa na haja ya kumwoa ama la. Mtume ﷺ alimwambia mtu mmoja katika Answaar.

«رَوْجِي ابْنَتِكَ»

"Niozeshe binti yako."

Akasema: "Ndiyo, ewe Mtume wa Allah! Itakuwa heshima na neema kwangu." Mtume ﷺ akasema:

«إِنِّي لَنْتُ أُرِيدُهَا لِنَفْسِي»

"Mimi simhitaji kwa ajili yangu."

Akasema: "Ni kwa ajili ya nani, ewe Mtume wa Allah?" Mtume ﷺ akasema:

«لِجُلَيْبٍ»

"Ni kwa ajili ya Julaybib."

Akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Ngoja nimtake ushauri mama yake." Akaenda kwa mama wa binti na kumwambia: "Mtume ﷺ anamposa mwanao." Akasema: "Itakuwa neema." Akasema: "Hamchumbii kwa ajili yake, bali kwa ajili ya Julaybib." Akasema: "Julaybib yupi, Julaybib yupi? Wallah! Hapana, hatumwozeshi." Alipotaka kusimama ili amjulishe Mtume ﷺ juu ya aliyoyasema mama yake, binti aliuliza, "Ni nani anayeniposa kwenu?" Mama yake akampa khabari. Akasema: "Mnamkatalia Mtume ﷺ amri yake? Mwachilieni, kwani hatanipoteza." Baba yake akaenda kwa Mtume ﷺ na

kumwambia. Jambo lako kwa binti huyo limekubaliwa. Kwa hivyo, akamwozesha Julaybib. Mtume ﷺ akaenda vitani, na baada ya Allah تعالى Kumpa ushindi, aliwaambia Masahaba رضي الله عنهم:

«هَلْ تَفْقِدُونَ مِنْ أَحَدٍ»

“Je kuna yeyote msiyemwona?”

Wakasema: “Hatumwoni fulani na fulani.” Akasema Mtume ﷺ:

«انظروا هل تفقدون من أحدٍ»

“Angalieni, kuna msiyemwona?”

Wakasema: “Hapana.” Akasema:

«لَكِنِّي أَفْقِدُ جُيَيْبًا»

“Lakini mimi simwoni Julaybib.”

Akasema tena:

«فَاطِبْرُهُ فِي الْقَتْلِ»

“Mtafuteni katika waliouawa.”

Wakamtafuta na kumkuta pembeni mwa watu saba aliowaua, kisha akauawa. Wakasema: “Ewe Mtume wa Allah! Huyu hapa pembeni mwa watu saba aliowaua kabla hajauawa.” Mtume ﷺ akamjia, akasimama karibu yake na kusema mara mbili au tatu:

«قَتَلَ سَبْعَةً وَقَتَلَهُ، هَذَا مِنِّي وَأَنَا مِنْهُ»

“Aliua watu saba kabla hajauliwa yeye. Yeye ni wangu, nami ni wake.”

Halafu Mtume ﷺ alimweka juu mikono yake na kumshikilia mpaka kaburi lake likachimbwa, halafu akamweka kaburini mwake. Hapakutajwa kwamba alimwosha, Allah تعالى Awe radhi naye.” Thabit رضي الله عنه alisema: “Hakukuwa na mjane ambaye watu walitamani sana kumwoa isipokuwa yeye.” Is-haq bin

'Abdullah bin Abu Twalhah alimuuliza Thabit رضي الله عنه: "Je unajua dua aliyoomba Mtume ﷺ kwa ajili ya mwanamke huyo?" Akasema: 'Alisema':

«اللَّهُمَّ صُبَّ عَلَيْهَا الْخَيْرَ صَبًّا وَلَا تَجْعَلْ عَيْشَهَا كَدًّا»

"Ewe Allah! mmiminie kheri zako, wala usiyafanye maisha yake kuwa magumu."

"Naam, hivi ndivyo ilivyokuwa. Katika Ansvar, hakukuwa na mjane ambaye watu walitamani sana kumwoa isipokuwa yeye." Hivi ndivyo alivyoinukuu Imamu Ahmad kwa ukamilifu.¹ Muslim na An-Nasai walikinukuu kisa cha mauti yake, katika *Al-Fadhwaail*.² Al-Hafidh bin 'Umar bin 'Abdul-Barr رحمه الله تعالى alitaja hivyo katika *Al-Istiy'aab*, kwamba pindi mwanamke aliposema wakati wa upweke wake, "Je mnamkatalia Mtume ﷺ amri yake?" Aya hii iliteremshwa,

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ

"Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri katika jambo lao."³

Twawus amesema kwamba alimuuliza Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya rakaa mbili baada ya Alasiri, akazikataza, kisha Ibn 'Abbas رضي الله عنهما akasoma:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ

"Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri katika jambo lao."⁴

Aya hii inajumuisha mambo yote. Nayo ni kwamba, Akishahukumu Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ kuhusu jambo lolote, haitakiwi yeyote kwenda kinyume,

¹ Ahmad 4:422.

² Muslim 2482, An-Nasaai Al-Kubra 8246.

³ Al-Istiaab 1:259.

⁴ Abdur-Razzaak 2:430.

wala hapana khiyari hakuna mwenye khiyari, wala rai au kauli nyingine. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا
مِمَّا قَضَيْتَ وَوَسَلِمُوا تَسْلِيمًا ﴿٣٥﴾

“La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayotoa, na wanyenyekee kabisa.” (4:65)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Akazidisha kuonya dhidi ya kulikhalifu hilo, Alisema:

وَمَنْ يَعَصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

“Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi.”

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣٧﴾

“Basi nawatahadhari wanaokhalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu.” (24:63)

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ اللَّهَ وَتُخْفِي فِي
نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَاهُ فَلَمَّا قَضَىٰ زَيْدٌ مِنْهَا وَطَرًا
زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَنْوَابِ أَزْوَاجِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا
وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٣٨﴾

37. “Na ulipomwambia yule Mwenyezi Mungu Aliyemneemesha, nawe ukamneemesha: Shikamana na mkeo, na mche Mwenyezi Mungu. Na ukaficha nafsini mwako Aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyafichua, nawe ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu Ndiye

Mwenye haki zaidi kumchelea. Basi Zaid alipokwisha haja naye tulikuoza wewe, ili isiwe taabu kwa Waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kupanga watapokuwa wamekwishatimiza nao shuruti za talaka. Na Amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa.”

Allah تعالى Anamlaumu Mtume Wake Katika Kisa cha Zayd رضي الله عنه na Zaynab رضي الله عنها, na Kumuamuru Amuoze Zainabu رضي الله عنها Baada Talaka na Kwisha Eda.

Allah تعالى Anamjulisha Mtume Wake ﷺ, kuwa alimwambia mtumwa aliyemwacha huru, Zayd bin Harithah رضي الله عنه, ambaye Allah تعالى Alimneemesha kusilimu na kumfuata Mtume ﷺ,

وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ

“...nawe ukamneemesha...”

Yaani, kwa kumpa uhuru. Na yeye alikuwa kiongozi mkubwa, aliyepewa cheo cha juu, mpendwa sana kwa Mtume ﷺ aliyekuwa akiitwa, mpendwa, na mwanaye, Usama رضي الله عنه alikuwa akiitwa, mpendwa mwana wa mpendwa. ‘Aishah رضي الله عنها alisema, “Mtume ﷺ hakumtuma katika Sariyah [safari ya kijeshi ambayo Mtume ﷺ mwenyewe hakwenda] bali alimfanya kuwa kamanda wao. Na lau kama angeliishi baada yake, basi angelimchaguwa kuwa khalifa wao. Aliinukuu Imamu Ahmad.¹ Mtume ﷺ alimfungisha ndoa na binti wa shangazi yake, Zaynab bint Jahsh Al-Asadiyyah رضي الله عنها, ambaye mama yake alikuwa akiitwa Umaymah bint ‘Abdul-Muttwalib. Mahari yake aliyompatia ilikuwa dinari ishirini na dirhamu sitini, mtandio, ushungi na kanzu fupi, vibaba khamsini vya chakula na ishirini vya tende. Hayo aliyasema Muqatil bin Hayyan. Akaishi naye kwa kadiri ya mwaka au zaidi, halafu kukatokea kutokuelewana baina yao. Zayd رضي الله عنه akaja kwa Mtume ﷺ kumshitaki. Mtume ﷺ akawa anasema: “*Shikamana na mkeo na umche Allah.*” Allah تعالى Amesema:

وَتُخْفَى فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَاهُ

“Na ukaficha nafsini mwako Aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyafichua, nawe ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Haki zaidi kumchelea.”

¹ Ahmad 6:227, 281.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa 'Aishah رضي الله عنها alisema: "Lau kama Muhammad ﷺ angeliyaficha aliyofunuliwa na Allah تعالى katika Kitabu cha Allah تعالى, basi angeliificha Aya hii:

وَتُخْفَى فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْشَى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَاهُ^ط

"Na ukaficha nafsini mwako Aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyafichua, nawe ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Haki zaidi kumchelea."¹

Allah تعالى Amesema:

فَلَمَّا قَضَى زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا

"Basi Zaid alipokwisha haja naye tulikuoza wewe..."

Maana ya *Watwar* ni haja. Yaani, 'Baada ya nikahi yake kwa Zayd رضي الله عنه ilipoondoka na akaachana naye, Tulikuoza naye,' na walii wa Zaynab رضي الله عنها Alikuwa Allah تعالى, kwa maana ya kwamba, Allah تعالى Alimpa ufunuo Mtume ﷺ kwamba aingie kwake bila ya walii, wala akdi, wala mahari wala shahidi wa kibinaadamu. Imamu Ahmad alinukuu kuwa Thabit alieleza kuwa Anas رضي الله عنه alisema: "Ilipomalizika eda ya Zaynab رضي الله عنها, Mtume ﷺ alimwambia Zayd bin Harithah رضي الله عنه:

اِذْهَبْ فَاذْكُرْهَا عَلَيَّ¹

"Nenda kwake na umwambie juu yangu (kwamba nataka nimwoe)."

Alikwenda kwake na kumkuta akikanda kinyunya chake. Zayd alisema: "Basi nilipomwona tu, nilijisikia kumheshimu, kiasi kwamba sikumudu hata kumtazama na kumwambia alichokisema Mtume ﷺ." Nikageuka na kusogea pembeni. Nikasema: "Ewe Zaynab! Pokea bishara, Mtume ﷺ amenituma kuja kukuposa kwa niaba yake." Akasema: "Mimi sitafanya chochote, mpaka nimwombe Mola wangu, Allah تعالى." Akaenda mahali pake pa kusali. Qur'an ikateremshwa, na Mtume ﷺ akaja na akaingia kwake bila ya idhini. Tulikuwepo pindi alipoingia Mtume ﷺ, na akatulisha karamu ya nyama na mikate. Watu wakatoka na wakasalia watu wakizungumza hapo nyumbani baada ya kula

¹ At-Tabari 20:274

chakula. Mtume ﷺ akatoka, nami nikamfuata. Mtume ﷺ akawa anakwenda katika vyumba vya wakeze, kimoja baada ya kingine, akiwasalimia na wao wakimwambia: “Ewe Mtume wa Allah! Umemkutaje mkeo (mpya)? sikumbuki kama baadaye nilimwambia kuwa watu wamekwishaondoka au alipewa khabari na Mtu mwingine. Akaenda na akaingia katika nyumba, nami nikamfuata ili niingie pamoja naye. Akaweka pazia baina yangu na yeye. Ikateremshwa Aya juu ya Hijabu na akawahutubia watu kuwa Allah تعالى Ameamrisha:

﴿لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ﴾

“Msiingie nyumba za Nabii ila mpewe ruhusa...”

Aliinukuu Muslim na An-Nasai.¹ Bukhari, Allah Amrehemu, alinukuu Hadithi ya Anas رضي الله عنه: “Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها alikuwa akijifakharisha kwa wake wa Mtume ﷺ kwa kusema: ‘Familia zenu zimekuozesheni nyinyi, lakini Allah تعالى Aliniandalia nikaha yangu kutokea juu ya mbingu saba.’”² Katika Tafsiri tuliyoitanguliza, ya Surat An-Nur, tulitaja kuwa Muhammad bin ‘Abdullah binJahsh alisema: “Zaynab na ‘Aishah (Allah Awe radhi nao), walikuwa wakitambiana kila mmoja kwa mwenzake. Zaynab رضي الله عنها akasema: “Mimi ndiye ambaye ndoa yangu ilitokana na ufunuo kutoka mbinguni.” ‘Aishah رضي الله عنها akasema: “Mimi ndiye ambaye utetezi wangu ulitajwa katika ufunuo kutoka mbinguni.” Zaynab رضي الله عنها akaikubali hoja hiyo.³ Kauli ya Allah تعالى:

لَيْكِن لَّا يَكُونُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ أَدْعِيَائِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا

“...ili isiwe taabu kwa Waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kupanga watapokuwa wamekwishatimiza nao shuruti za talaka.”

Yaani, ‘Tulikuruhusu kumwoa, na tuliyafanya haya ili kusibakie uzito kwa Waumini kuwaoa watalaka wa watoto wao wa hiari. Hayo ni kwamba, kabla ya Utume, Mtume ﷺ alikuwa amempanga Zayd bin Harith رضي الله عنه kuwa mwanaye wa hiari, na akawa akiitwa Zayd bin Muhammad. Baadaye Allah تعالى Akaukata unasaba huu kwa kauli Yake,

¹ Ahmad 3:195, Muslim na.1428, An-Nasai 6:79

² Fat’h Al-Bari 13:415.

³ At-Tabari 19:118.

وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ

“Wala hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa.”

Hadi Kauli Yake Allah تعالى،

أَدْعُوهُمْ لِأَبَائِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ

“Waiteni kwa baba zao, maana huo ndio uadilifu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu.” (33:4-5)

Kisha, akaongeza hilo bayana na kusisitiza kwa jambo la Mtume ﷺ kumwoa Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها baada ya Zayd bin Harithah رضي الله عنه kumpa Talaka Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema katika Aya ya Kuliharamisha hilo,

وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ

“...Na (mmeharamishiwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu.” (4:23)

Yaani, ni haramu kuwaoa wake wa watoto wenu halisi, na wala si watoto wa hiari (wa kupanga). Jambo hili (la watoto wa kupanga) lilikithiri sana kwao.

وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٣٨﴾

“Na Amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa.”

Yaani, jambo ambalo lililotokea ni kwa Kudura ya Allah تعالى، pia ni lazima na halikuwa la kukwepeka. Katika Ilimu ya Allah تعالى، ilikuwa kwamba Zaynab رضي الله عنها Atakuwa mke wa Mtume ﷺ.

مَا كَانَ عَلَى النَّبِيِّ مِنْ حَرَجٍ فِيمَا فَرَضَ اللَّهُ لَهُ سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلُ وَكَانَ

أَمْرُ اللَّهِ قَدَرًا مَقْدُورًا ﴿٣٩﴾

38. “Hapana ubaya kwa Nabii kufanya aliyomhalalishia Mwenyezi Mungu. Huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa waliopita zamani. Na Amri ya Mwenyezi Mungu ni Kudura iliyokwisha kadiriwa.”

Kauli ya Allah تعالى:

مَا كَانَ عَلَى النَّبِيِّ مِنْ حَرَجٍ فِيمَا فَرَضَ اللَّهُ

“Hapana ubaya kwa Nabii kufanya Aliyomhalalishia Mwenyezi Mungu.”

Yaani, katika Aliyomhalalishia na Kumwamuru, katika kumwoa Zaynab رضي الله عنها, ambaye aliachwa na mwanaye wa kupanga, Zayd bin Harithah رضي الله عنه. Kauli ya Allah تعالى:

سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلُ

“Huo ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu kwa waliopita zamani.”

Yaani, hii ni Hukumu ya Allah تعالى kwa Manabii wa kabla yake, hakuwa ni Mwenye kuwaamuru jambo lenye ubaya kwao. Hili ni jibu la kuwakanushia wanafiki ambao walidai kuwa ni jambo la nuksani, kwa Mtume ﷺ kumwoa mke wa Zayd رضي الله عنه, mtumwa aliyempatia uungwana na pia mwanaye wa hiari (kupanga),

وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ قَدَرًا مَقْدُورًا

“Na Amri ya Mwenyezi Mungu ni Kudura iliyokwisha kadiriwa.”

Yaani, Amri Yake Anayoikadiria ilikuwa ni yenye kutukia, hapana cha kuizuia wala kupinga. Akitakacho Yeye huwa, na Asichokitaka hakiwi. Kauli ya Allah تعالى:

الَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَالَاتِ اللَّهِ وَيَخْشَوْنَهُ وَلَا يَخْشَوْنَ أَحَدًا إِلَّا اللَّهَ وَكَفَى بِاللَّهِ حَسِيبًا

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ

عَلِيمًا

39. “Waliokuwa wakifikisha risala za Mwenyezi Mungu na wanamwogopa Yeye, na wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Atoshaye Kuhisabu.”

40. “Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Kuwasifu wanaofikisha Ujumbe wa Allah تعالى.

Allah تعالى Anawasifu,

الَّذِينَ يُبَلِّغُونَ رِسَالَاتِ اللَّهِ

“(Hao wa zamani) waliokuwa wakifikisha risala za Mwenyezi Mungu...”

Yaani, kwa viumbe wake na wanatimiza amana zake,

وَيَخْشَوْنَ

“...na wanamwogopa Yeye...”

Yaani, wanamkhofu Yeye, wala hawamwogopi mwingine asiyekuwa Yeye, kwa hivyo hakuna kitisho cha yeyote chenye kuwazuia kuufikisha Ujumbe wa Allah تعالى,

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ حَسِيبًا

“...Na Mwenyezi Mungu Ndiye Atoshaye Kuhisabu.”

Maana yake ni kuwa, Allah تعالى Anatosha kuwa Mwenye Kususuru na Kusaidia. Kiongozi wa watu wote mahali hapa na katika kila eneo, ni Muhammad, Mtume ﷺ, kwa sababu Yeye alisimama kwa ajili ya kuutekeleza na kuufikisha Ujumbe kwa wakazi wa mashariki na magharibi na kwa wanaadamu wa namna zote. Kwa hivyo, Allah تعالى Amelifanya neno lake, Dini na Sheria yake kuzishinda dini na sheria zote. Manabii waliokuwa kabla yake walikuwa wakitumwa kwa kaumu makhususi, ama Mtume ﷺ ametumwa kwa viumbe wote, Waarabu na wasiokuwa hao.

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote...”
(7:158)

Kisha umma wake ukarithishwa nafasi ya ufikishaji, na Masahaba رضي الله عنهم ndio walifikia mahali pa juu sana katika jukumu hilo baada yake. Wao walifikisha Ujumbe sawa na alivyowaamuru katika kauli, matendo na hali zake zote, iwe kwa usiku na mchana wake, wakati wa ukaazi na safari zake, kwa siri na dhahiri zake, Allah Awe radhi nao. Baada yao, kila kizazi kilirithishwa

na kuendelea mpaka katika zama zetu hizi. Hivyo, kwa mwangaza wao, wafuasi hufuata na wanapita katika njia yao. Tunamwomba Allah, Mkarimu, Mwenye Kuneemesha Atujaalie kuwa miongoni mwa wenye kufuata njia yao.

Mtume ﷺ si Baba wa Yeyote

Kauli ya Allah تعالى:

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ

“Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu...”

Baada ya haya, hakukuwa na ruhusa ya kuitwa Zayd bin Muhammad رضي الله عنه, yaani hakuwa baba yake, japokuwa alimfanya mwanaye wa hiari. Hakuna mtoto wa kiume wa Mtume ﷺ ambaye aliishi mpaka kufikia umri wa kubaleghe. Khadijah رضي الله عنها alimzalia Mtume ﷺ watoto walioitwa, Qasim, At-Twayyib na Twaahir, na wote walifariki dunia wakiwa wadogo na mtoto wake mwingine Ibrahim mama yake alikuwa Mariam Al-Qibtiya. Pia alipata watoto wane wa kike kupitia kwa Khadija: Zaynab, Ruqayyah na Umm Kulthum, Allah Awe radhi nao wote. Watatu walifariki wakati wa uhai wake Mtume ﷺ, akabakia Fatmah رضي الله عنها, mpaka akafiwa na Mtume ﷺ, na yeye akafariki miezi sita baadaye.

Yeye ni Mtume wa Mwisho

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَنَكُنَّ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٦١﴾

“...bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ

“Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi Kuliko wote Kujua wapi Anaweka ujumbe Wake.” (6:124)

Aya hii inataja kwamba hapana Nabii baada yake. Ikiwa hakuna Nabii baada

yake, basi hakuna Mtume baada yake pia, kwa sababu hadhi ya Mtume ni ya juu kuliko ya Nabii, kwani kila Mtume ni Nabii na si kinyume chake. Hilo limesimuliwa katika *Hadith Mutawaatir* nyingi, kutoka kwa Mtume ﷺ, kupitia katika kundi la Masahaba, Allah تعالى Awe radhi nao. Imamu Ahmad alinukuu masimulizi kutoka kwa Ubayy bin Ka'b, kutoka kwa baba yake, kwamba Mtume ﷺ amesema:

«مَثَلِي فِي النَّبِيِّنَ كَمَثَلِ رَجُلٍ بَنَى دَارًا فَأَحْسَنَهَا وَأَكْمَلَهَا، وَتَرَكَ فِيهَا مَوْضِعَ لَبَنَةٍ لَمْ يَضَعُهَا، فَجَعَلَ النَّاسُ يَطُوفُونَ بِالْبُنْيَانِ وَيَعْجَبُونَ مِنْهُ وَيَقُولُونَ: لَوْ تَمَّ مَوْضِعُ هَذِهِ اللَّبَنَةِ، فَأَنَا فِي النَّبِيِّنَ مَوْضِعُ تِلْكَ اللَّبَنَةِ»

*"Mfano wangu mimi miongoni mwa mitume ni kama mtu aliyejenga nyumba, akaipendezesha na kuikamilisha. Akaacha sehemu ya tofali moja ambalo hakuliweka mahali pake. Watu wakaanza kutembea kulizunguka jengo, wakilistaajabia na kusema: 'Pangelitimia tu mahali pa tofali hili.' Basi nafasi yangu mimi kwa Manabii ni kama lile tofali. "*¹

Pia ilinukuliwa na Tirmidhi, ambaye alisema, *"Hasan Sahih."*²

Hadithi Nyingine

Imamu Ahmad alimnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الرِّسَالَةَ وَالنَّبُوَّةَ قَدْ انْقَطَعَتْ فَلَا رَسُولَ بَعْدِي وَلَا نَبِيٍّ»

"Utume na unabii umeshakatika, basi hapana Mtume wala Nabii baada yangu."

Hilo likawakhofisha watu, akasema:

«وَلَكِنَّ الْمُبَشِّرَاتِ»

"Lakini watakuwepo vibashirio."

Wakasema: "Ewe Mtume wa Allah! *Al-Mubash-Shirat* ni nini?" Akasema:

¹ Ahmad 5:136.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 10:81.

رُؤْيَا الرَّجُلِ الْمُسْلِمِ، وَهِيَ جُزْءٌ مِنْ أَجْزَاءِ الشُّبُورِ»

“Ndoto za Muislamu, nazo ni sehemu mojawapo miongoni mwa mafungu ya utume.”¹

Hii ilinukuliwa na At-Tirmidhi pia, amesema: *“Sahih Gharib.”²*

Hadithi Nyingine

Abu Dawud At-Twayalisi alimnukuu Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه, kwamba alisema, Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ لِي وَمَنْ لُ الْأَنْبِيَاءِ كَمَنْ لِي رَجُلٍ بَنَى دَارًا فَأَكْمَلَهَا وَأَحْسَنَهَا إِلَّا مَوْضِعَ لَبْتِهِ، فَكَانَ مَنْ دَخَلَهَا فَتَنَظَرَ إِلَيْهَا قَالَ: مَا أَحْسَنَهَا إِلَّا مَوْضِعَ هَذِهِ اللَّبْتِ، فَأَنَا مَوْضِعُ اللَّبْتِ خَيْمِ بِي الْأَنْبِيَاءِ عَلَيْهِمُ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ»

“Mfano wangu na Mitume wengine ni kama mtu aliyejenga nyumba, akaikamilisha na kuipendezesha, isipokuwa sehemu ya tofali moja tu. Ikawa mwenye kuingia na kutizama, husema: ‘Ni nzuri mno, kasoro mahali pa tofali hili moja. Basi, mimi ndio tofali lile moja. Manabii wamekhitimishiwa kwangu.”³

Ilinukuliwa na Bukhari pia, Muslim na At-Tirmidhi ambaye amesema, *“Ni Sahih Gharib pamoja na isnadi yake.”⁴*

Hadithi Nyingine

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Sa‘id Al-Khudri رضي الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ aseema:

«مَنْ لِي وَمَنْ لُ النَّبِيِّنَ كَمَنْ لِي رَجُلٍ بَنَى دَارًا فَأَتَمَّهَا إِلَّا لَبْتَهُ وَاحِدَةً، فَجِئْتُ أَنَا فَأَتَمَمْتُ تِلْكَ اللَّبْتَهُ»

¹ Ahmad 3:267. Ni kwamba, masalia pekee ya Utume yatakayoendelea kuwepo baada yake ﷺ ni ndoto za kweli za Waumini wa kweli, ambayo ilikuwa moja ya sifa kuu za Utume. Angalia *Fat’h Al-Bari* namba 6990.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:551.

³ Musnad At-Tayaalisi 247.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 6:645, Muslim 4:1791, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:158.

*"Mfano wangu na Mitume ni kama mtu aliyejenga nyumba na akaitimiza, kasoro tofali moja tu. Basi, mimi nimekuja na kulitimiza tofali lile."*¹ Ilinukuliwa na Muslim peke yake.²

Hadithi Nyingine

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa alisema, Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ مَثَلِي وَمَثَلَ الْأَنْبِيَاءِ مِنْ قَبْلِي كَمَثَلِ رَجُلٍ ابْتَنَى بُيُوتًا فَأَكْمَلَهَا وَأَحْسَنَهَا وَأَجْمَلَهَا إِلَّا مَوْضِعَ لَبَنَةٍ مِنْ زَاوِيَةٍ مِنْ زَوَائِيهَا، فَجَعَلَ النَّاسُ يَطُوفُونَ وَيُعْجِبُهُمُ الْبَيْتَانُ وَيَقُولُونَ: أَلَا وَضَعْتَ هَهُنَا لَبَنَةً قَتَيْمٌ بَيْتَانِكَ»

"Mithili yangu na Mitume waliokuja kabla yangu ni kama mtu aliyejenga nyumba kadhaa, akazikamilisha, akazifanya vyema na kuzipendezesha isipokuwa tofali moja katika moja ya kona zake. Watu wakaanza kuzunguka na kuyashangaa majengo huku wanasema: 'Ikiwa utaliweka tofali hapa, basi ujenzi wako utakuwa umetimia.'"

Mtume ﷺ amesema:

«فَكُنْتُ أَنَا اللَّبَنَةُ»

*"Mimi nimekuwa ndio tofali hilo."*³

Waliinukuu (Bukhari na Muslim).⁴

Hadithi Nyingine

Muslim alimnukuu Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«فُضِّلْتُ عَلَى الْأَنْبِيَاءِ بِسِتِّ : أُعْطِيتُ جَوَامِعَ الْكَلِمِ، وَنُصِرْتُ بِالرُّعْبِ وَأُجِلْتُ لِيِ الْغَنَائِمِ، وَجُعِلَتْ لِيِ الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا، وَأُرْسِلْتُ إِلَى الْخَلْقِ كَافَّةً، وَخُتِمَ بِيِ النَّبِيُّونَ»

¹ Ahmad 3:9.

² Muslim 4:1791.

³ Ahmad 2:312.

⁴ Bukhari na. 3535, Muslim 4:1790.

“Nimefadhilishwa juu ya Mitume kwa mambo sita. Nimepewa uwezo wa kuzungumza kwa mukhtasari, nimenusuriwa kwa njia ya khofu (katika nyoyo za maadui), nimehalalishiwa ghanima, ardhi imefanywa twahara kwangu na kuwa mahali pa kusali na kwamba nimetumwa kwa viumbe wote, na utume unakomea kwangu.”¹

Ilinukuliwa na Tirmidhi na Ibn Majah pia. At-Tirmidhi alisema, *“Ni Hasan Sahih.”²*

Hadithi Nyingine

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Sa'id Al-Khudri رضى الله عنه, kuwa alisema, Mtume ﷺ alisema:

«مَثَلِي وَمَثَلُ الْأَنْبِيَاءِ مِنْ قَبْلِي كَمَثَلِ رَجُلٍ بَنَى دَارًا فَأَتَمَّهَا إِلَّا مَوْضِعَ لَبْنٍ وَاحِدٍ، فَجِئْتُ أَنَا فَأَتَمَمْتُ تِلْكَ اللَّبْنَةَ»

“Mithili yangu na Manabii wa kabla yangu ni kama mtu aliyejenga nyumba na kuitimiza yote, isipokuwa mahali pa tofali moja. Nikaja mimi na kulitimiza tofali lile.”³

Pia ilinukuliwa na Muslim.⁴

Hadithi Nyingine

Jubayr bin Mut'im رضى الله عنه alisema, nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِنَّ لِي أَسْمَاءَ أَنَا مُحَمَّدٌ، وَأَنَا أَحْمَدُ، وَأَنَا الْمَاجِي الَّذِي يَمْحُو اللَّهُ تَعَالَى بِي الْكُفْرَ، وَأَنَا الْحَاشِرُ الَّذِي يُخَسِّرُ النَّاسَ عَلَى قَدَمَيَّ وَأَنَا الْعَاقِبُ الَّذِي لَيْسَ بَعْدَهُ نَبِيٌّ»

“Mimi nina majina kadha: Mimi ni Muhammad; mimi ni Ahmad; mimi ni Al-Mahi (mfutaji) ambaye Allah Atafuta kufuru kupitia

¹ Muslim 1:371.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 5:160, Ibn Majh 1:188.

³ Ahmad 3:9.

⁴ Muslim 4:1791.

kwangu; mimi ni Al-Hashir ambaye watu watakusanyika miguuni mwangu; mimi ni Al-'Aqib, wa mwisho ambaye hakuna tena Nabii baada yangu."¹

Ilinukuliwa katika *Sahih* Mbili.² Kuna Hadithi nyingi sana juu ya mada hii. Allah تعالی Alikwishaeleza ndani ya Kitabu Chake kitukufu, na Mtume Wake ﷺ katika Sunna *Mutawaatir* (zilizopokelewa na kundi kubwa) kwamba hakuna Nabii baada yake, ili watambue kwamba kila atakayedai nafasi hii baada yake, basi huyo atakuwa ni mwongo mkubwa na mzushi tu, mpotevu mwenye kupoteza.

Hata kama atabadili maana, akaleta madai ya uongo, akatumia uchawi, matalasimu na mazingaombwe, basi vyote hivyo si halali na ni upotevu kwa wenye kutumia akili. Ni sawa na Aliyoyasababisha Allah تعالی yatokee katika jambo la Al-Aswad Al-'Ansi huko Yemen na Mwongo mkubwa, Musaylamah Al-Kadhaabu wa Yamamah, miongoni mwa hali mbaya na kauli za kipuuzi zilimjulisha kila aliyekuwa mwenye akili na ufahamu kwamba hao walikuwa waongo wawili wapotoshaji, Allah تعالی Awalaani. Ni hivyo hivyo kwa kila mwenye kudai hivyo mpaka Siku ya Kiyama, mpaka wamalizikie kwa *Masih Dajjal*. Kila mmoja katika hawa waongo, Allah تعالی Anaumba pamoja nao mambo ambayo maulamaa na Waumini watayatumia kuthibitisha kuwa wao ni waongo. Huku ni katika kutimia kwa ulatifu wa Allah تعالی kwa viumbe wake. Waongo hawa hawaamrishi mema wala kukataza maovu, isipokuwa kwa njia ya itifaki fulani au kwa sababu ya dhamiri fulani iliyojificha, na inakuwa katika ghaya ya uongo na uovu katika kauli na vitendo vyao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

هَلْ أَنتُمْ عَلَىٰ مَن تَنزَلُ الشَّيْطِينُ ﴿٢٢٢﴾ تَنزَلُ عَلَىٰ كُلِّ آفَاكٍ أَثِيمٍ ﴿٢٢١﴾

“Je! Nikwambieni nani wanaowashukia Mashetani? Wanamshukia kila mzushi mkubwa mwingi wa dhambi.” (26:221-222)

Hali hii ni kinyume na ya Manabii, kwani wao walikuwa na upeo wa juu wa wema, ukweli, uongofu, uimara, uadilifu katika waliyoyasema na waliyoyafanya, wanaamrisha mema na kukataza maovu. Pamoja na haya, walisaidiwa na miujiza, dalili dhahiri, ushahidi waziwazi. Allah تعالی Awateremshie Rehema na Amani daima kadiri ya kuendelea kuwepo kwa ardhi na mbingu.

¹ Ahmad 4:80.

² *Fat'h Al-Bari* 8:509, Muslim 4:1828.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا اللَّهَ ذِكْرًا
 كَثِيرًا ۝ وَسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ۝
 هُوَ الَّذِي يُصَلِّي عَلَيْكُمْ وَمَلَائِكَتُهُ
 لِيُخْرِجَكُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۚ وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ
 رَحِيمًا ۝ فَحَيِّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُ سَلَامٌ ۚ وَأَعَدَّ لَهُمْ أَجْرًا
 كَرِيمًا ۝ يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِدًا وَمُبَشِّرًا
 وَنَذِيرًا ۝ وَدَاعِيًا إِلَى اللَّهِ بِإِذْنِهِ وَسِرَاجًا مُّبِينًا ۝
 وَبَشِيرَ الْمُؤْمِنِينَ بَأَنَّ لَهُم مِّنَ اللَّهِ فَضْلًا كَثِيرًا ۝ وَلَا
 تُطْعِ الْكَافِرِينَ وَالْمُنَافِقِينَ وَدَعِ أَذْنَهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ
 وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ۝ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَكَحْتُمُ
 الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ مِن قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ ۚ فَمَا
 لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِن عِدَّةٍ تَعْتَدُونَهَا ۚ فَمَتَّبِعُوهُنَّ وَسَرَّحُوهُنَّ
 سَرَاحًا جَمِيلًا ۝ يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَحْلَلْنَا لَكَ أَزْوَاجَكَ
 الَّتِي ءَاتَيْتَ أَجُورَهُنَّ ۚ وَمَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ مِمَّا أَفَاءَ اللَّهُ
 عَلَيْكَ وَبَنَاتِ عَمَّكَ وَبَنَاتِ عَمَّتِكَ وَبَنَاتِ خَالَكَ وَبَنَاتِ
 خَلَّتِكَ الَّتِي هَاجَرْنَ مَعَكَ وَأَمْرًا ۚ مُؤْمِنَةً ۚ إِن وَهَبْتَ
 نَفْسَهَا لِلنَّبِيِّ ۖ إِن أَرَادَ النَّبِيُّ أَنْ يَسْتَنْكِحَهَا خَالِصَةً لَّكَ مِن
 دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۚ قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا عَلَيْهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ
 وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ لِكَيْلَا يَكُونَ عَلَيْكَ حَرَجٌ ۚ
 وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ۝

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَذْكُرُوا اللَّهَ ذِكْرًا
 كَثِيرًا ۝ وَسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ۝
 هُوَ الَّذِي يُصَلِّي عَلَيْكُمْ
 وَمَلَائِكَتُهُ لِيُخْرِجَكُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ
 إِلَى النُّورِ ۚ وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ
 رَحِيمًا ۝ فَحَيِّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُ
 سَلَامٌ ۚ وَأَعَدَّ لَهُمْ أَجْرًا كَرِيمًا ۝

41. "Enyi mlioamini! Mdhukuruni Mwenyezi Mungu kwa wingi wa kumdhukuru."

42. "Na mtakaseni asubuhi na jioni."

43. "Yeye na Malaika Wake ndio wanakurehemuni ili kukutoeni gizani mwende kwenye nuru. Naye ni Mwenye Kuwarehemu Waumini."

44. "Maamkiano yao siku ya kukutana Naye yatakuwa: Salama! Na Amewandalia malipo ya ukarimu."

Fadhila za Kumkumbuka Sana Allah تعالى.

Allah تعالى Anawaamuru waja Wake Waumini wakithirishe kumtaja Mola wao Mwenye Kuwafadhili kwa aina za neema, kwani watalipwa malipo mengi kwa hayo na makazi mema.

Imamu Ahmad alimnukuu 'Abdullah bin Busr رضي الله عنه akisema: "Mabedui wawili walikuja kwa Mtume ﷺ, mmoja wao akasema, "Ewe Mtume wa Allah! Ni mtu gani aliye bora?" Mtume ﷺ akamjibu:

«مَنْ طَالَ عُمُرُهُ وَحَسَنَ عَمَلُهُ»

"Atakayekuwa na umri mrefu na amali zake kuwa njema."

Mwenzake akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Sharia za Kiislamu zimekuwa nyingi kwetu. Kwa hivyo, nifundishe jambo nitakaloshikamana nalo." Mtume ﷺ akamfundisha:

«لَا يَزَالُ لِسَانُكَ رَطْبًا بِذِكْرِ اللَّهِ تَعَالَى»

*"Ulimi wako usiache kuwa laini kwa kumtaja sana Mola wako."*¹

At-Tirmidhi na Ibn Majah waliinukuu sehemu ya pili ya nukuu hii. At-Tirmidhi alisema, "*Hadithi hii ni Hasan Gharib.*"² Imamu Ahmad aliandika kutokana na Hadithi ya 'Abdullah bin 'Amri رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ قَوْمٍ جَلَسُوا مَجْلِسًا لَمْ يَذْكُرُوا اللَّهَ تَعَالَى فِيهِ إِلَّا رَأَوْهُ حَسْرَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*"Hapana watu wanaoketi katika majlisi ambayo hakumkumbuka Allah ndani yake, isipokuwa katika Siku ya Kiyama watayaona ni ya kujutia."*³

'Ali bin Abu Twalhah amesema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

¹ Ahmad 4:190.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:621, Ibn Majah 1:1246.

³ Ahmad 2:224.

أَذْكُرُوا اللَّهَ ذِكْرًا كَثِيرًا ﴿٤١﴾

“Mdhukuruni Mwenyezi Mungu kwa wingi wa kumdhukuru.”

Kuwa, “Allah تعالی Hakuwafaradhishia waja wake jambo lolote, bali Aliliwekea mipaka maalumu, kisha anakubali udhuru wa walio na nyudhuru, lakini katika ibada ya Dhikri Allah تعالی Hakuijalia kuwa na mpaka wa kuishia, na hakumkubalia yeyote udhuru wa kuiacha ila mwenye kushurutishwa kuiacha.

Kwa hivyo, Allah تعالی Amesema:

فَأَذْكُرُوا اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ

“...basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu mkisimama, na mkikaa, na mnajinyoosha kwa kulala.” (4:103)

Usiku na mchana, bara na baharini, safarini na katika makazi, katika hali ya utajiri na ufakiri, katika uzima na kuugua, kwa usiri na uwazi, na katika kila hali. Kauli ya Allah تعالی:

وَسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٤٢﴾

“Na mtakaseni asubuhi na jioni.”

Ikiwa mtafanya hivi, “Yeye na Malaika Wake watakuleteeni Rehema.”¹

Kuna Hadithi na Aya nyingi sana zenye kuhimiza jambo la kumtaja Allah تعالی kwa wingi, na Aya hii tukufu inasisitiza juu ya kukithirisha dhikri. Waandishi wengi, kama vile Nasai na Ma’mar na wengine wameandika vitabu vingi kuhusu *Al-Adhkaar* katika nyakati mbalimbali za usiku na za mchana.

Kauli ya Allah تعالی:

وَسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٤٢﴾

“Na mtakaseni asubuhi na jioni.”

Yaani, wakati wa asubuhi na jioni. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

¹ At-Tabari 20:280.

فَسُبْحَانَ اللَّهِ حِينَ تُمْسُونَ وَحِينَ تُصْبِحُونَ ﴿٤١﴾ وَ لَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
وَعَشِيًّا وَحِينَ تُظْهِرُونَ ﴿٤٢﴾

“Basi Subhanallah! Mtakaseni Mwenyezi Mungu jioni na asubuhi. Na Sifa zote njema ni Zake katika mbingu na ardhi, na alasiri na adhuhuri.” (30:17-18)

Kauli ya Allah تعالى:

هُوَ الَّذِي يُصَلِّي عَلَيْكُمْ وَمَلَائِكَتُهُ

“Yeje na Malaika Wake ndio wanakurehemuni...”

Hii inatumaanisha juu ya dhikri, yaani, Allah تعالى Anakukumbukeni, kwa hivyo, na nyinyi mumkumbuke. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِّنكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ
وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿٤٣﴾ فَادْكُرُونِي أُدْكُرْكُمْ وَأَشْكُرُوا لِي وَلَا
تَكْفُرُونِ ﴿٤٤﴾

“Kama Tulivyomtuma Mtume kwenu anayetokana na nyinyi, anakusomeeni Aya Zetu na kukutakaseni na kukufundisheni Kitabu na hikima na kukufundisheni mliyokuwa hamyajui. Basi Nikumbukeni Nitakukumbukeni, na Nishukuruni wala msinikufuru.” (2:151-152)

Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: مَنْ دَكَرَنِي فِي نَفْسِهِ دَكَرْتُهُ فِي نَفْسِي، وَمَنْ دَكَرَنِي فِي مَلَأِ دَكَرْتُهُ فِي مَلَأِ خَيْرِ مِثْلِهِ»

“Allah Anasema: ‘Mwenye kunikumbuka katika nafsi yake, Mimi Nitamkumbuka katika Nafsi Yangu, na atakayenikumbuka katika mjumuiko, na Mimi Nitamkumbuka katika mkusanyiko bora kuliko huo.”

Ufafanuzi wa Rehema ya Allah تعالی "Swala" Katika Aya hii¹

Maana ya neno "Salaah" Rehema ya Allah تعالی kwa waja wake ni kwamba Yeye Humsifu mja wake mbele ya Malaika, kwa mujibu wa Bukhari alivyomnukuu Abu Al-'Aliyah.² Pia Abu Ja'far Ar-Razi رحمه الله تعالی aliinukuu kutoka kwa Ar-Rabi' bin Anas kutoka kwa Anas رضي الله عنه. Wengine walisema: "Salaah ya Allah تعالی maana yake Rehema." Inaweza kusemwa kwamba hakuna khitilafu baina ya rai hizi mbili. Allah Aalam. Ama Salaah ya Malaika ni kwa maana ya dua na kuwaombea watu maghufira. Ni sawa na katika Kauli nyingine ya Allah تعالی:

الَّذِينَ يَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ
 ءَامَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِهِمْ
 عَذَابَ الْجَحِيمِ ﴿٧﴾ رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتِ عَدْنِ الَّتِي وَعَدْتَهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ ءَابَائِهِمْ
 وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٨﴾ وَقِهِمُ السَّيِّئَاتِ

"Wale wanaobeba A'rshi, na wanaoizunguka, wanamsabihi na kumhimidi Mola wao Mlezi, na wanamuamini, na wanawaombea msamaha walioamini kwa kusema: Mola Wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa Rehema na Ujuzi. Basi wasamehe waliotubu na wakaifuata Njia yako, na waepushe na adhabu ya Jahannamu. Mola Wetu Mlezi! Na Waingize katika Bustani za Milele ulizo waahidi. Na uwape haya pia wale waliofanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na dhuriya wao. Hakika Wewe ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima. Na waepushe na maovu." (40:7-9)

Kauli ya Allah تعالی:

لِيُخْرِجَكُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

"...ili kukutoeni gizani mwende kwenye nuru."

¹ Hii ni moja ya vichwa vya habari vilivyoongezwa katika tafsiri ya kiingereza.

² Al-Bukhari Kitabu cha tafsiri Surat Al-Ahazab, Sura ya 10.

Yaani, kutokana na Rehema Zake kwenu na kumsifu kwenu na dua za Malaika kukuombeeni, Anakutoeni kutoka katika kiza cha ujahili na upotevu kwenda katika nuru ya hidaya na yakini.

وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا ﴿٤١﴾

“Naye ni Mwenye Kuwarehemu Waumini.”

Duniani na Akhera. Ama duniani, ni kwa Kuwaongoa katika ukweli ambao wengine hawakuutambua, na Akawaonesha njia ambayo wasiokuwa wao hawakuiona, kama wale wanaohubiri katika ukafiri au bidaa na wafuasi wao katika waovu. Ama Rehema Yake kwao huko Akhera, ni Kuwaweka salama dhidi ya khofu kubwa na Kuwaamuru Malaika Wake wawapokee kwa Kuwapa bishara ya kufuzu kuingia Peponi na kunusurika mbali na moto. Wala hayo si kwa jingine, isipokuwa ni Mahaba Yake na Ukarimu Wake kwao. Imamu Ahmad alinukuu kuwa Anas رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ na kikundi cha Masahaba wake walimkuta mtoto njiani. Mama yake alipowaona watu hao, alimkhofia mwanaye kukanyagwa, akamkimbilia huku akisema: ‘Mwanangu, mwanangu!, Alikimbia na akamchukua. Masahaba wakasema: ‘Ewe Mtume wa Allah! Mwanamke huyo hatomtupa mwanaye Motoni.’ Mtume ﷺ akasadikisha:

«لَا، وَاللَّهِ لَا يُلْقِي حَبِيْبُهُ فِي النَّارِ»

“Hapana, Wallah! Hatomtupa kipenzi chake Motoni.”¹

Isnadi yake ina ukamilifu wa kanuni za *Sahih* Mbili. Wala hakuandika yeyote katika wakusanyaji wa Vitabu Sita. Lakini katika *Sahih* ya Imamu Bukhari, imenukuliwa kutoka kwa Amiri wa Waumini, ‘Umar bin Al- Khattab رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alimwona mwanamke miongoni mwa mateka wa kivita, akiwa amembeba mwanaye, akamkumbatia kifua kwake na akamnyonyesha. Mtume ﷺ akauliza:

«أَتُرَوْنَ هَذِهِ تُلْقِي وَلَدَهَا فِي النَّارِ وَهِيَ تَقْدِرُ عَلَى ذَلِكَ؟»

“Mnadhani huyu atamtupa mwanaye katika moto ingawa ana nguvu za kuweza kufanya hivyo?”

¹ Ahmad 3:104.

Wakasema: "Hapana." Akasema Mtume ﷺ:

«قَوْلَاهُ! اللَّهُ أَرْحَمُ بِعِبَادِهِ مِنْ هَذِهِ بَوْلِدَاهَا»

"Wallah! Allah ni Mwenye Rehema kwa waja wake kuliko mwanamke huyu kwa mwanaye."¹

Kauli ya Allah تعالى:

تَحِيَّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُ سَلَامٌ

"Maamkiano yao siku ya kukutana naye yatakuwa: Salama!"

Maana yake iko dhahiri - Allah Aalam, **"Maamkiano yao..."** Yaani, kutoka kwa Allah تعالى, **"...siku ya kukutana Naye yatakuwa: Salama!"** Yaani, katika Siku ambayo Allah تعالى Atawasalimu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

سَلَامٌ قَوْلًا مِنْ رَبِّ رَحِيمٍ ﴿٥٨﴾

"Salama!" Hiyo ndiyo kauli itokayo kwa Mola Mlezi Mwenye Kurehemu." (36:58)

Qatadah alidai kwamba maana yake ilikuwa kwamba watasalimiana kwa *Salaam* katika Siku watakyokutana na Allah تعالى huko Akhera.²

Ni kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine,

دَعْوَتُهُمْ فِيهَا سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ۗ وَءَاخِرُ دَعْوَتُهُمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ

الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

"Wito wao humo utakuwa: "Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu!" Na maamkio yao humo ni "Salama". Na mwisho wa wito wao ni: "Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote." (10:10)

¹ Fat'h Al-Bari 10:440.

² At-Tabari 20:280.

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَعَدَّ لَهُمْ أَجْرًا كَرِيمًا ﴿٤١﴾

“Na Amewaandalia malipo ya ukarimu.”

Yaani, Peponi na kila kilichomo, kama vile vyakula, vinywaji, mavazi, maskani, ndoa, faraja na mandhari zilizomo, ambazo hapana jicho lililowahi kuona wala sikio lililosikia, wala kupita katika akili ya mwanaadamu.

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَهِيدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٤٢﴾ وَدَاعِيًا إِلَى اللَّهِ بِإِذْنِهِ وَسِرَاجًا مُنِيرًا ﴿٤٣﴾
 وَبَشِيرِ الْمُؤْمِنِينَ بِأَنَّ لَهُم مِّنَ اللَّهِ فَضْلًا كَبِيرًا ﴿٤٤﴾ وَلَا تَطْعِ الْكٰفِرِينَ وَالْمُنٰفِقِينَ
 وَدَعِ أَذْنَهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿٤٥﴾

45. “Ewe Nabii! Hakika Sisi Tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na mwonyaji.”

46. “Na mwitaji kumwendea Mwenyezi Mungu kwa Idhini Yake, na taa yenye kutoa nuru.”

47. “Na wabashirie Waumini ya kwamba wana fadhila kubwa inayotoka kwa Mwenyezi Mungu.”

48. “Wala usiwatii makafiri na wanafiki, na usijali udhia wao. Nawe mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mtegemewa.”

Sifa za Mtume ۞

Imamu Ahmad alimnukuu ‘Ataa bin Yasaar kuwa alisema: “Nilikutana na ‘Abdullah bin ‘Amri bin Al-‘As رضي الله عنه, nikamwambia, “Nijulishe sifa za Mtume ۞ zilizo katika Taurati.” Akasema: “Naam, Wallah! Yeye ni mwenye kusifiwa katika Taurati kama baadhi yake zilivyotajwa ndani ya Qur’an, “Ewe Mtume, Kwa hakika! Sisi Tumekupeleka uwe shahidi, mtoaji bishara na mwonyaji, mwokozi wa walio, wasiojua kusoma wala kuandika kikasomwa “Ummi”. Wewe ni mja na Mjumbe Wangu, nimekuita *Al-Mutawakkil* (Mwenye kutegemea). Wewe si mkali wala mgumu, wala mwenye makelele masokoni. Hulipizi ubaya kwa ubaya,, bali hufanyi kinyongo na unasamehe.

Allah تعالی Hataichukua roho yako, isipokuwa mpaka uwaweke paliponyooka wale waliokwenda upogo, na waseme *Laa ilaaha illallah*, maneno ambayo yatafungua macho ya kipofu, na sikio lililosikia, na nyoyo zilizoghafilika'.¹ Pia ilinukuliwa na Bukhari katika Kitabu cha Biashara na *Tafsir*.² Wahb bin Munabbih alisema: "Allah تعالی Alimpa Wahyi Nabii mmojawapo miongoni mwa Manabii wa Banu Israil aliyeitwa Shay'aa (Isaya): "Simama kwa kaumu yako, banu Israil, Mimi Nitautamkisha ulimi wako maneno ya ufunuo. Nitamtuma Mtume asiyejua kusoma wala kuandika kikasomwa "Ummi" kutoka kwa watu walio Ummi. Hatokuwa mkali wala mgumu wala mpiga kelele masokoni, lau kama atapita karibu na taa, hataizima, kwa sababu ya utulivu wake. Lau kama atapita katika mafunjo, hakuna sauti itakayosikika kutokea chini ya nyayo zake. Nitamtuma awe mtoaji bishara na mwonyaji, ambaye hatatoa maneno yaliyokosa maadili mema. Kupitia kwake, nitayafumbua macho ya kipofu, masikio yasiyosikia, na nyoyo zilizoghafilika. Nitamwongoza katika kila jambo jema na nitampa kila tabia njema. Nitajaalia utulivu kuwa ndilo vazi lake, wema ndio alama yake na Taqwa kuwa dhamiri yake, hekima kuwa matamshi yake, ukweli na uaminifu ndio kawaida yake, kustahamili na mambo mema ndio mazoea yake, ukweli kuwa ni njia yake, uadilifu ndio sira yake na uongofu ndio kiongozi wake na Uislamu ndio mila yake. Ahmad ndilo jina lake, na kupitia kwake Nitawaongoza watu baada ya upotevu. Nitawafundisha baada ya wao kuwa na ujahili, Nitawanyanyua baada ya kuwa duni, Nitawafanya wajulikane baada ya kutokujulikana, na kuwa wengi baada ya uchache, na kuwatajirisha baada ya kuwa katika ufakiri, kuwaunganisha pamoja baada ya kufarakana. Kupitia kwake, Nitawakutanisha mataifa yaliyotawanyika na nyoyo zilizokosana, na utashi uliotofautiana. Pia Nitawaokoa watu wengi dhidi ya kuhiliki kwao, na Nitaujaalia umma wake uwe mbora kuliko umma mwengine na katika wanaadamu, wataamrisha mema na kukatazana maovu, wenye kunipwekesha Mimi katika ibada, Waumini, wenye kujitakasa, wenye kuyasadiki waliyokuja nayo Mitume Wangu. Nitawafahamisha Tasbihi, Tahmidi, kunisifu, kunitukuza na Tauhidi, misikitini mwao, katika hali ya kuketi na kula kwao na kurejea majumbani mwao. Swala zao watazielekeza Kwangu kwa kusimama na kukaa, watapigana katika njia ya Allah تعالی wakiwa safu na

¹ Ahmad 2:174

² *Fat'hu Al-Bari* 4:402, 8:449

majeshi, na watatoka maelfu majumbani mwao kwa ajili ya kutafuta Radhi Zangu, wataosha nyuso na mikono yao na watazifunga nguo zao viunoni. Dhabihu yao itakuwa damu zao na Kitabu chao kitukufu kimo vifuani mwao. Watakuwa kama watawa usiku na kama simba wakati wa mchana. Nitajaalia miongoni mwa wanafamilia wake na kizazi chake kuwa ni wale walio mbele zaidi (kwa imani), wakweli, waliouawa shahidi na watu wema. Umma wake baada yake, watawaongoza watu katika ukweli na kuweka uadilifu. Nitawapa nguvu wenye kuwanusuru. Nitawasaidia watakaowaombea dua, na Nitafanya mwisho mbaya kwa wenye kuwakhaliu au kuruka mipaka dhidi yao au kutaka kupora kitu walicho nacho. Nitawafanya warithi wa Mtume wao, walinganiaji kwa Mola wao, kwa kuamrishana mema na kukatazana maovu, watasimamisha Sala, watatoa Zaka, watatekeleza ahadi zao. Nitaitimiza kheri kwao, ambayo Niliianza kwa mwanzo wao. Hizi ni Fadhila Zangu ambazo Namtunuku Nimtakaye, Nami ni Mwenye Fadhila Kubwa.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

شَهِيدًا

“...uwe shahidi...”

Yaani, juu ya Upweke wa Allah تعالى, na kwamba hapana zaidi Yake ambaye ni wa kuabudiwa kwa haki, na awe shahidi katika Siku ya Kiyama, kuhusu amali za watu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَجَعَلْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا ﴿٤١﴾

“...na Tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?” (4:41),

Kama Kauli Yake,

لَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا

“...ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu.” (2:143)

¹ Ibn Abu Hatim na. 17714.

Kauli ya Allah تعالى:

وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٤١﴾

“...mbashiri na mwonyaji.”

Yaani, kuwapa waumini khabari njema kwa kupata malipo mengi, na kuwaonya makafiri kuhusu adhabu mbaya.

Kauli ya Allah تعالى:

وَدَاعِيًا إِلَى اللَّهِ بِإِذْنِهِ

“Na mwitaji kumwendea Mwenyezi Mungu kwa Idhini Yake...”

Yaani, mlinganiaji viumbe kumwabudu Mola wao, ikiwa ni Amri Yake Allah تعالى yeye kufanya hivyo.

وَسِرَاجًا مُنِيرًا ﴿٤٢﴾

“...na taa yenye kutoa nuru.”

Yaani, jambo lako la ukweli ulilokuja nalo liko dhahiri kama jua linapochomoza na kuangaza kwake, halipingi isipokuwa mkaidi.

Maneno ya Allah تعالى:

وَلَا تُطِيعُ الْكُفْرِينَ وَالْمُنَافِقِينَ وَدَعَّ أَدْنَاهُمْ

“Wala usiwatii makafiri na wanafiki, na usijali udhia wao.”

Yaani, usimtii wala usimsikilize yeyote kati yao, katika wayasemayo,

وَدَعَّ أَدْنَاهُمْ

“...na usijali udhia wao.”

Yaani, acha na usiwajali, kwani kila jambo lao linaishia kwa Allah تعالى na Yeye Anawatosha.

Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema:

وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿٤٣﴾

“Nawe mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mtegemewa.”

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ بِمَا
 لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُونَهَا فَمَعِيَهُنَّ وَسَرَحُوهُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴿٤٩﴾

49.“Enyi mliaoamini! Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa talaka kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayoihisabu. Basi wapeni cha kuwaliwaza, na muwawache kwa kuwachana kwa wema.”

Kitoka Nyumba na Hukumu ya Eda ya Mwanamke Aliye Achwa Kabla ya Jimai

Ndani ya Aya hii tukufu kuna hukumu nyingi. Mojawapo ni matumizi ya neno *Nikah* kwa ajili ya mkataba wa ndoa tu. Wala ndani ya Qur’an hakuna Aya nyingine iliyo wazi zaidi katika hilo kuliko hii. Humo pia, kuna uhalali wa kumpa talaka mwanamke kabla ya kumuingilia. Kauli ya Allah تعالى:

الْمُؤْمِنَاتِ

“...wanawake Waumini...”

Hii inamaanisha kama ilivyo kawaida, ingawa hakuna tofauti ya hukumu baina ya mwanamke muumini (Muislamu) na mwanamke wa watu waliopewa Kitabu katika jambo hili, kwa mujibu wa muwafaka wa maulamaa. Ibn ‘Abbas, Sa’id bin Musayyab, Hasan Al-Basri, ‘Ali bin Husayn Zaynul-‘Abidin na kundi katika *Salaf* رضي الله عنهم waliitumia Aya hii kama ushahidi kwamba talaka huwa haiwezi kutukia, isipokuwa ikitanguliwa na ndoa. Ni kwa sababu Allah تعالى Amesema:

إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ

“Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa talaka...”

Hapa, Allah تعالى Ameanza kutaja Ndoa kwanza kisha ndio akataja Talaka, maana yake ni kwamba, talaka kabla yake haisihi wala haitatukia.¹ Abu Hatim alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema: “Ikiwa mtu atasema, ‘Kila

¹ At-Tabari 20:283.

mwanamke nitakayemuoa, atakuwa tayari nimemwacha kwa talaka.” Alisema: Hakuna chochote katika hilo kwani Allah تعالى Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ

“Enyi mlioamini! Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa talaka...”¹

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema tena: “Allah تعالى Amesema,

إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ

“...Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa talaka...”

Hamwoni kwamba talaka inakuja baada ya ndoa?” Ilisimuliwa Hadithi kuhusu hilo kutoka kwa ‘Amri bin Shu‘ayb, toka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, alisema: Mtume ﷺ amesema,

«لَا طَّلَاقَ لِابْنِ آدَمَ فِيمَا لَا يَمْلِكُ»

“Hapana talaka kwa mwanaadamu katika asivyo na mamlaka navyo.”

Ilinukuliwa na Ahmad, Abu Dawud Tirmidhi na Ibn Majah. Tirmidhi alisema: “Hadithi hii ni *Hasan*, na ndiyo iliyo bora zaidi katika yaliyosimuliwa kuhusu mlango huu.”² Sawa na hii alinukuu Ibn Majah kutoka kwa ‘Ali na Miswar bin Makhramah رضي الله عنهما, kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

«لَا طَّلَاقَ قَبْلَ نِكَاحٍ»

“Hapana talaka kabla ya nikaha.”³

Kauli ya Allah تعالى:

فَمَا لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُونَهَا

“...basi hamna eda juu yao mtakayoihisabu.”

¹ Imenukuliwa na Al-Mundhir na Ibn Hatim. Angalia Ad-Dur Al-Manthur 5:392.

² Ahmad 2:207, Tuhfatul Al-Ahwadhi 4:355, Ibn Majah 1:660.

³ Ibn Majah 1:660.

Hii ni Amri ambayo maulamaa wanaafikiana, kwamba mwanamke akipewa talaka kabla ya kujamiwa na mumewe, atakuwa hana eda, na anaweza kwenda kuolewa na yeyote amtakaye. Hukumu hii haitomuhusu mwanamke aliyefiwa isipokuwa mwenye mumewe, kwani yeye atakaa eda kutokana na hali hiyo kwa muda wa miezi mnne na siku kumi, hata kama hakutenda naye tendo la ndoa.

Kauli ya Allah تعالى:

﴿فَمَتَّعُوهُنَّ وَسَرَحُوهُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا﴾

“Basi wapeni cha kuwaliwaza, na muwawache kwa kuwachana kwa wema.”

Kitoka nyumba kilichokusudiwa hapa inamaanisha kitu cha ujumla zaidi ya kuwa nusu ya mahari iliyotajwa au kitoka nyumba maalumu, ikiwa mahari hakutajiwa au kubainishwa katika Ndoa. Allah تعالى Amesema:

﴿وَإِنْ طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَبِضْفٍ مَا فَرَضْتُمْ﴾

“Na mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari makhsusi, basi wapeni nusu ya mahari mlioagana...”
(2:237).

Na Allah تعالى Amesema:

﴿لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ طَلَقْتُمْ الْيَسَاءَ مَا لَمْ تَمْسُوهُنَّ أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً وَمَتَّعُوهُنَّ عَلَى

الْمُوسَعِ قَدْرُهُ وَعَلَى الْمُقْتَرِ قَدْرُهُ مَتَّعًا بِالْمَعْرُوفِ حَقًّا عَلَى الْحَسَنِينَ﴾

“Hapana ubaya kwenu mkiwapa talaka wanawake ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari yao. Lakini wapeni cha kuwaliwaza, mwenye wasaa kadiri awezavyo na mwenye dhiki kadiri awezavyo - maliwaza kwa mujibu wa dasturi kuwa ni haki juu ya watendao mema.” (2:236)

Katika *Sahih Bukhari* kuna Hadithi ya Sahli bin Sa'd na Abu Usayd رضي الله عنهما, walisema: “Mtume ﷺ alimwoa Umaymah bint Sharaahil na alipoingia kwake, alimsogezea mkono, ikawa kama vile hakupenda hilo, kwa hivyo alimwambia

Abu Usayd ampatie (Umaymah) nguo zake mbili.”¹ Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Ikiwa mahari ilikwishatajwa, atakuwa hana haki ya zaidi ya nusu, lakini kama haikutajwa, basi anatakiwa ampatie kitoka nyumba (kiliwazo) kulingana na wasaa, na huku ndiko kuachana kwema.”²

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَحْلَلْنَا لَكَ أَزْوَاجَكَ الَّتِي ءَاتَيْتَ أُجُورَهُنَّ وَمَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ مِمَّا أَفَاءَ
 اللَّهُ عَلَيْكَ وَبَنَاتِ عَمِّكَ وَبَنَاتِ عَمَّتِكَ وَبَنَاتِ خَالَكَ وَبَنَاتِ خَالَتِكَ الَّتِي هَاجَرْنَ
 مَعَكَ وَامْرَأَةً مُؤْمِنَةً إِنْ وَهَبْتَ نَفْسَهَا لِلنَّبِيِّ إِنْ أَرَادَ النَّبِيُّ أَنْ يَسْتَنْكِحَهَا خَالِصَةً لَكَ مِنْ
 دُونِ الْمُؤْمِنِينَ قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا عَلَيْهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ لِكَيْلَا
 يَكُونَ عَلَيْكَ حَرَجٌ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٥٠﴾

50. “Ewe Nabii! Tumekuhalalishia wake zako uliowapa mahari yao, na uliowamiliki kwa mkono wako wa kulia katika aliokupa Mwenyezi Mungu, na mabinti wa ami zako, na mabinti wa shangazi zako, na mabinti wa wajomba zako, na mabinti wa dada za mama yako waliohama pamoja nawe; na mwanamke Muumini akijitoa mwenyewe kwa Nabii, kama mwenyewe Nabii akitaka kumwoa. Ni halali kwako wewe tu, si kwa Waumini wengine. Sisi Tunajua Tuliowafaridhia wao katika wake zao na wanawake ilio wamiliki mikono yao ya kulia. Ili isiwe dhiki kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Wanawake Waliohalalishwa kwa Mtume ۞

Allah تعالى Anamwambia Nabii wake ۞ kwamba Amemhalalishia katika wanawake, wake zake aliowatolea mahari zao, na hapa imetajwa kwa jina la *Ujur*. Ni sawa na alivyosema Mujahid na wengine.³ Mahari yake kwa wake zake ilikuwa ni Wakia (*Uqiyyah*) kipimo cha dhahabu) kumi na mbili na Nusu

¹ Fat’h Al-Bari 9:269.

² At-Tabari 20:283.

³ At-Tabari 20:284.

(Nash). Kwa hivyo, wote walipokea Dirham mia tano, isipokuwa Ummu Habibah bint Abu Sufyan رضي الله عنها, kwani Najash, Allah Amrehemu, alitoa Dinar mia nne kwa niaba ya Mtume ﷺ. Pia Swafiyah bint Huyay ambaye Mtume ﷺ alimchagua kutokana na mateka katika vita vya Khaybar, halafu akamwacha huru na akakufanya kuwacha huru kuwa ndio mahari yake. Kadhalika Juwayriyah bint Al-Harith Al-Mustalqiyah رضي الله عنها, ambapo Mtume ﷺ alilipa mkataba wake wa kuununua uhuru wake kutoka kwa Thabit bin Qays bin Shammaas, halafu akamwoa. Allah تعالى Awe radhi nao wote. Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ مِمَّا أَفَاءَ اللَّهُ

“...na uliowamiliki kwa mkono wako wa kulia katika Aliokupa Mwenyezi Mungu...”

Yaani, amekuruhusu mateka wa kike mliowachukua kutoka katika ghanima. Aliwamiliki Swafiyah na Juwayriyah akawapa uhuru wao akawaoa. Alimiliki Rayhanah bint Sham'un Nadhriyah na Maariyah Qibtwiyyah, ambaye ni mama wa mwanaye, Ibrahim wote wawili walikuwa masuria, Allah تعالى Awe radhi nao. Kauli ya Allah تعالى:

وَبَنَاتِ عَمِّكَ وَبَنَاتِ عَمَّتِكَ وَبَنَاتِ خَالَكَ وَبَنَاتِ خَالَتِكَ

“...na mabinti wa ami zako, na mabinti wa shangazi zako, na mabinti wa wajomba zako na mabinti wa dada za mama yako...”

Huu ni uadilifu ambao upo kati na kati baina ya kuharamisha na kuhalalisha, kwani wakristo huwa hawamwoi mwanamke isipokuwa ikiwa baina yake na mwanamke kuna mababu kuanzia saba na kwenda juu. Mayahudi huoa binti wa kaka yake na wa dada yake. Ikaja sharia hii kamilifu na twahara kwa kuvunja kuharamisha kwa wakristo. Imeruhusu kumwoa binti wa ami na wa shangazi, na binti wa mjomba na wa dada wa mama. Pia kuyaharamisha ambayo mayahudi wameyaruhusu kwa kuhalalisha mtu kumwoa binti wa kaka au wa dada, na hili ni jambo la kuchukiza. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَمْرًا مُؤْمِنَةً إِنْ وَهَبَتْ نَفْسَهَا لِلنَّبِيِّ إِنْ أَرَادَ النَّبِيُّ أَنْ يَسْتَنْكِحَهَا خَالِصَةً لَّكَ

“...na mwanamke Muumini akijitoa mwenyewe kwa Nabii, kama mwenyewe Nabii akitaka kumwoa. Ni halali kwako wewe tu...”

Yaani, ni halali kwako, ewe Nabii, mwanamke Muumini, ikiwa atajitoa nafsi yake kwako kwamba umuoje pasi na mahari, ikiwa utapenda hivyo. Aya hii inaambatana na masharti mawili. Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Sahl bin Sa'd As-Sa'idi رضى الله عنه kwamba Mtume ﷺ alijiwa na mwanamke, na akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Mimi nimejitolea mwenyewe kwako." Mwanamke huyo akasimama kisimamo kirefu. Mtu mmoja akasimama na kusema: "Ewe Mtume wa Allah! Niozeshe mimi huyo mwanamke ikiwa wewe huna haja naye." Mtume ﷺ akasema:

«هَلْ عِنْدَكَ مِنْ شَيْءٍ تُضِدُّهَا بِهَا؟»

"Una kitu chochote utakachompatia kama mahari?"

Akasema: "Mimi sina kitu zaidi ya nguo yangu hii." Mtume ﷺ akasema:

«إِنْ أُعْطِيَتْهَا إِزَارَكَ جَلَسْتَ لَا إِزَارَ لَكَ، فَاتَّيَسَّرَ شَيْئًا»

"Ukimpatia nguo yako hiyo ya chini, utakaa ukiwa huna nguo, tafuta kitu (kingine)."

Akasema: "Sina kitu kingine."

«التَّيَسَّرَ وَلَوْ خَاتَمًا مِنْ حَدِيدٍ»

"Tafuta kitu, japo pete ya chuma."

Akatafuta, lakini hakupata kitu. Mtume ﷺ akasema:

«هَلْ مَعَكَ مِنَ الْقُرْآنِ شَيْءٌ؟»

"Je una (jua) chochote katika Qur'an."

Akasema: "Naam, Sura fulani na Sura fulani." Akazitaja. Mtume ﷺ akasema:

«زَوَّجْتُكَهَا بِمَا مَعَكَ مِنَ الْقُرْآنِ»

*"Nimemuozesha kwako kwa kiasi cha Qur'an unayojua."*¹

Pia, ilinukuliwa na Bukhari na Muslim, kutokana na Hadithi ya Malik.² Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu masimulizi kutoka kwa baba yake kuwa, 'Aishah

¹ Ahmad 5:336.

² Fat'h Al-Bari 9:97, Muslim 2:1040.

alisema: "Mwanamke aliyetoa nafsi yake kwa Mtume ﷺ alikuwa Khawlah bint Hakim رضي الله عنها."¹ Bukhari alimnukuu 'Aishah رضي الله عنها kuwa alisema: "Nilikuwa nikimwonea wivu mwanamke mwenye kujitoa nafsi yake kwa Mtume ﷺ na kusema: 'Mwanamke anajitoa nafsi yake?' Lakini Allah تعالى Alipotereemsha Aya:

* تُرْجَى مَن كَشَاءُ مِثْنُ وَتُتَوَى إِلَيْكَ مَن كَشَاءُ وَمَنْ أِبْتَغَيْتَ مِمَّنْ عَزَلْتَ فَلَا جُنَاحَ

عَلَيْكَ

***"Unaweza kuakhirisha zamu kwa umtakaye katika wao, na umsogeze umtakaye. Na kama ukimtaka yule uliyemtenga, basi si vibaya kwako."* (33:51)**

Nilisema, 'Simuoni Mola wako isipokuwa Anaharakisha katika matamanio yako.'² Ibn Abu Hatim رضي الله عنهما alinukuu kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "Mtume ﷺ hakuwa na mke yeyote ambaye alijitolea nafsi yake kwake." Haya yalinukuliwa na Ibn Jarir³ رضي الله تعالى عنه kutoka kwa Yunus bin Bukhair yaani, hakumkubalia yeyote aliyejitoea nafsi yake kwake, japokuwa hilo lilikuwa ruhusa na ni makhususi kwake, kwani jambo hilo limewekwa katika khiyari yake. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine:

إِنْ أَرَادَ النَّبِيُّ أَنْ يَسْتَنْكِحَهَا

"...kama mwenyewe Nabii akitaka kumwoa."

Yaani, akilichagua hilo. Kauli ya Allah تعالى:

خَالِصَةً لَّكَ مِنَ الدُّنْيَا الْمُؤْمِنِينَ

"Ni halali kwako wewe tu, si kwa Waumini wengine..."

'Ikrimah alisema: "Inamaanisha, si halali kwa mwingine yeyote kumuoa mwanamke aliyejitolea nafsi yake kwake. ikiwa mwanamke atajitolea nafsi yake kwa mwanamume si halali kwake (kumuoa), mpaka ampatie kitu."⁴

¹ Al-Bayhaqi 7:55.

² Fat'h Al-Bari 8:385.

³ At-Tabari 20:288.

⁴ Ad-Dur Al-manthur 6:63.

Haya yalikuwa ni maoni ya Mujahid pia, Ash-Sha'bi na wengine.¹ Yaani, ikiwa mwanamke atajitoea mwenyewe kwa mtu, na yeye akataka kufunga naye ndoa, basi atahitajika kumpa *Mahr Al-Mithl* (yaani, mahari mithili anayoweza kupatiwa mwanamke kama huyo). Ni sawa na alivyoamua Mtume ﷺ juu ya jambo hilo kumhusu Birwa bint Waashiq, pindi alipojitoea nafsi yake, Mtume ﷺ akatoa uamuzi kwamba itolewe *Mahr Al-Mithl* pindi mumewe alipofariki.

Suala la Mume kufariki pamoja na kujamiiana kwa wanandoa, yana hukumu sawa katika mahari isiyotajwa (*Al-Mithl*) katika hukumu ya mwanamke aliyojitoea nafsi yake kuolewa. Hukumu ni kwa watu wengine halimuhusu Mtume, kwa sababu Mtume ana haki ya kuoa pasi na kuwepo mahari wala walii, wala shahidi. Kwa mwanamke aliyejitolea nafsi yake kwake hata kama amemuungilia. Ni kama katika kisa cha Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها. Kwa ajili hii, Qatadah alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

خَالِصَةً لَّكَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ

“Ni halali kwako wewe tu, si kwa Waumini wengine...”

Kuwa Allah تعالى Anasema, ‘mwanamke hana haki ya kujitolea, nafsi yake kwa mtu yeyote bila *Walii* wala mahari, isipokuwa kwa Mtume ﷺ.”² Kauli ya Allah تعالى:

قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا عَلَيْهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ

“Sisi Tunajua Tuliowafaridhia wao katika wake zao na wanawake iliowamiliki mikono yao ya kulia.”

Ubayy bin Ka'b, Mujahid, Hasan, Qatadah, Ibn Jarir wamezumgumzia Aya hii:

قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا عَلَيْهِمْ فِي أَزْوَاجِهِمْ

“Sisi Tunajua Tuliowafaridhia wao katika wake zao...”

Yaani, kuhusu kuweka ukomo wa idadi yao kuwa wanawake wane huru,³ na wanaowataka katika wajakazi, na masharti ya walii, mahari na mashahidi wa

¹ At-Tabari 20:286,287.

² At-Tabari 20:286.

³ At-Tabari 20:286.

ndoa. Haya ni kwa ajili ya umma, lakini Tumekuruhusu wewe, wala hatukukuwajibishia chochote katika masharti hayo.'

لِكَيْلَا يَكُونَ عَلَيْكَ حَرَجٌ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٥٠﴾

"Ili isiwe dhiki kwako. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."

* * *